


# *Elimu ya Dini ya Kiislamu*

---

## **Shule za Sekondari Kitabu cha 4**

Toleo la Pili



**Elimu ya Dini ya Kiislamu Kitabu cha 4**

Toleo la Pili

---

Islamic Education Panel

# ***Elimu ya Dini ya Kiislamu***

## **Shule za Sekondari**

### **Kitabu cha 4**

**Toleo la Pili**

**Islamic Education Panel**

## **Elimu ya Dini ya Kiislamu**

### **Shule za Sekondari Kitabu cha Nne**

Toleo la Pili,

© Islamic Education Panel,

1 Ramadhan, 1437,(H.C)

6 Juni,2016 Miladia(A.D)

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kutoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya Islamic Education Panel.

ISBN 978-9987-743-01-8

Kimeandikwa na kusambazwa na  
Islamic Education Panel,  
S.L.P 55014,

Tovuti: [www.islamiceducationtz.com](http://www.islamiceducationtz.com)

E-mail:[info@Islamiceducationtz.com](mailto:info@Islamiceducationtz.com)

Dar es Salaam.

**TANZANIA.**

## NENO LA AWALI

Sifa zote njema zinamstahiki Allah(s.w), Bwana Mlezi wa walimwengu wote. Rehema na amani zimuendee Mtume Muhammad(s.a.w) na ahli zake, swahaba zake na wale wote wanaofuata mwenendo wake na kuliendea kwa hima lengo la kuletwa kwake la kuutawalisha Uislamu katika jamii.

Tunamshukuru Allah(s.w) kwa kutuwezesha kutoa toleo la pili la kitabu hiki cha **Nne** cha "**Elimu ya Dini ya Kiislamu Shule za Sekondari**". hiki ni kitabu cha kiada cha somo la Elimu ya Dini ya kiislamu kwa kidato cha Nne . Kama ilivyokuwa katika toleo la kwanza, mada za somo hili zimegawanywa katika fani tano na kila fani imefanywa sura ya kitabu hiki kama ifuatavyo:

- (i)Tawhiid
- (ii) Fiqh
- (iii) Qur'an
- (iv) Sunnah na Hadith
- (v)Tarekh(Historia)

Pamoja na kufanyiwa uhariri, toleo hili limeboreshwa zaidi kwa kuingizwa matin ya aya zilizorejewa katika kufafanua mada mbali mbali. Pia kila sura ya kitabu hiki imeambatanishwa na mazoezi ya kutosha yanayo mchochea mwanafunzi kusoma kwa mazingatio.

Nitumaini letu kuwa wanafunzi na waalimu wa somo hili watafaidika vyema na watajitahidi kwa kadiri ya uwezo wao kuingiza ujuzi uliopatikana kutokana na kitabu hiki katika maisha yao ya kila siku ya kibinafsi na kijamii. Uislamu unakemea vikali tabia ya kujua mambo kinadharia bila ya kuyaingiza katika utendaji.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿١٢٦﴾

كَبُرَ مَقْتًا عِنْدَ اللَّهِ أَنْ تَقُولُوا مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿١٢٧﴾

---

*“Enyi mliamini! Mbona mnasema msiyoyatenda? Ni chukizo kubwa mbele ya Allah kusema msiyoyatenda” (61:2-3)*

Tunatoa wito kwa wasomaji wote wa kitabu hiki kutoa maoni na mapendekezo yatakayo pelekea kuboresha somo hili na kuwawezesha wanafunzi kufikia lengo kuu kama lilivyo ainishwa katika muhtasari. Maoni na mapendekezo chanya yatazingatiwa katika chapisho linalofuata.

## **Wabillah Tawfiq**

## YALIYOMO

UK

<b>Neno la awali .....</b>	<b>(iii)</b>
<i>Sura ya Kwanza .....</i>	<b>1</b>
<b>TAWHIID .....</b>	<b>1</b>
<b>KUAMINI MITUME WA MWENYEZI MUNGU(S.W) .....</b>	<b>1</b>
Umuhimu wa Kuamini Mitume .....	1
Historia ya Maisha ya Mitume .....	2
Mwisho wa Utume .....	2
Maana ya Kuamini Mitume katika Maisha ya kila Siku .....	5
<b>KUAMINI SIKU YA MWISHO .....</b>	<b>9</b>
Umuhimu wa Kuamini Siku ya Mwisho.....	9
Ainisho la Siku ya Mwisho .....	9
Hoja za Wapinzani wa Siku ya Mwisho na Udhaifu Wake.....	10
Ulazima wa Kuwepo Siku ya Mwisho .....	14
Ushahidi wa Historia Juu ya Ufufuo .....	19
Ushahidi wa Ufufuo Utokanao na Maisha ya kila Siku.....	22
Mazingira ya Siku ya Mwisho kwa Mujibu wa Qur'an na Hadith .....	23
Mtazamo wa Uislamu juu ya Shufaa .....	40

Nini Shufaa .....	40
Nani Watakao Shufaia? .....	41
Nani Watakaostahiki Kushufaiwa? .....	41
Maana ya Kuamini Siku ya Mwisho katika Maisha ya Kila Siku .....	43
Toba ya Kweli .....	45
<b>KUAMINI QADAR YA MWENYEZI MUNGU(S.W) .....</b>	<b>48</b>
Maana ya Qadar .....	48
Mtazamo wa Uislamu juu ya Qadar .....	48
Tofauti ya Qadar na Qudra .....	50
Maana Pana ya Qadar .....	50
Maana ya Qudra ya Mwenyezi Mungu(s.w) .....	53
Kueleweka Vibaya kwa Qadar na Qudra ya Mwenyezi Mungu(s.w) .....	54
Suala la Uongofu .....	59
Mbona Kuna Uovu na Mateso Duniani? .....	60
Maana hasa ya Kuamini Qadar ya Mwenyezi Mungu katika Maisha ya kila Siku .....	62
<b>TOFAUTI KATI YA UISLAMU NA DINI NYINGINE .....</b>	<b>68</b>
Ukafiri na Madhara yake katika Jamii .....	69
Itikadi ya Ukafiri .....	69
Madhara ya Ukafiri katika Jamii .....	70
Ushirikina na Madhara yake katika Jamii .....	71

Itikadi ya Ushirikina .....	71
Utawa na Madhara yake katika Jamii .....	74
Itikadi ya Utawa .....	74
Madhara ya Utawa katika Jamii .....	75
Matunda ya Kusimama kwa Uislamu katika Jamii.....	76
Itikadi ya Uislamu .....	76
<i>Sura ya Pili</i> .....	78
<b>FIQH</b> .....	78
<b>NDOA YA KIISLAMU</b> .....	78
Maana ya Ndoa .....	78
Umuhimu wa Ndoa kwa Mtazamo wa Uislamu .....	78
Kumuendeleza Mwanadamu Kiuchumi .....	83
Kuchagua Mchumba.....	84
Ruhusa ya Kuwaoa Ahlal Kitaab(Mayahudi na Wakristo).....	85
Ruhusa ya Wachumba Kuonana Kabla ya Ndoa .....	86
Kizazi, Rika na Elimu .....	87
Umaharimu .....	87
Mahari .....	89
Kiasi Gani Kinachojuzu Kutolewa Mahari ? .....	90
Je, Mahari Inashusha Hadhi ya Mwanamke? .....	91



Khutuba ya Ndoa .....	92
Kufunga Ndoa Kiislamu .....	93
Ndoa ya Mke Mmoja Hadi Wanne.....	97
Hekima ya Ukewenza .....	99
<b>Zoezi la 2.1</b> .....	102
<b>TALAKA NA EDA</b> .....	103
Maana ya Talaka .....	103
Talaka katika Uislamu.....	103
Suluhu kati ya Mume na Mke .....	104
Haki ya Kutaliki .....	107
Aina za Talaka .....	108
Taratibu za Kutaliki Kiislamu.....	115
Talaka Kabla ya Jimai: .....	120
Talaka ya Aliyerukwa na Akili na Aliyetenywa Nguvu ....	121
Malezi ya Mtoto Mchanga baada ya Talaka .....	121
Eda ya Kufiwa.....	122
Kuingizwa au Kutolewa Eda .....	123
<b>Zoezi 2.2</b> .....	124
<b>MIRATHI YA KIISLAMU</b> .....	125
Maana ya Mirathi .....	125

Mwanamke ana Haki ya Kurithi .....	125
Mirathi katika Jamii za Kijahili .....	126
Mambo ya Kuzingatia Kabla ya Kugawanya Urithi .....	127
Qur'an inavyogawa Mirathi .....	128
Wanaume Wenye Kurithi ni Kumi na Tano (15).....	132
Wanawake Wenye Kurithi ni Kumi (10) .....	133
Kuzuiliana.....	133
Wenye Kupewa Mafungu .....	134
Asaba - Warithi Wasio na Mafungu Maalum.....	135
Musharakah - Kushirikiana Fungu:.....	136
Ugawaji wa Mirathi .....	136
Mifano ya Namna ya Kurithisha .....	137
Sehemu ya Masikini na Jamaa wa Karibu katika Mirathi: .....	141
<b>Zoezi 2:3</b> .....	141
<b>KUDHIBITI UZAZI</b> .....	142
Historia ya Kampeni ya Kudhibiti Uzazi.....	142
Kustawi kwa Kampeni ya Kudhibiti Uzazi .....	143
Hoja za Kudhibiti Uzazi Hivi Leo .....	144
Udhaifu wa Hoja za Kudhibiti Uzazi: .....	146
Hoja ya Uhaba wa Rasilimali za Kiuchumi .....	147
Tatizo la Vifo na Maradhi .....	148

Hoja ya Ugumu wa Malezi .....	150
Hoja ya Ubora na siyo Uwingi wa Watu.....	151
Hoja ya Nyongeza .....	152
Matokeo ya Kufuata Sera ya Kudhibiti Uzazi .....	152
Msimamo wa Uislamu Juu ya Kudhibiti Uzazi .....	158
Kupanga Uzazi katika Uislamu.....	163
Hitimisho Juu ya Kudhibiti Uzazi .....	163

<b>Zoezi 2:4 .....</b>	<b>164</b>
------------------------	------------

## **HADHI NA HAKI ZA MWANAMKE**

<b>KATIKA JAMII .....</b>	<b>165</b>
Utangulizi.....	165
Hadhi na Haki za Mwanamke katika Jamii za Kijahili ....	165
Jami za Magharibi .....	166
Jamii za Mashariki.....	173
Jamii za Kiafrika.....	175
Hadhi na Haki za Mwanamke katika Jamii ya Kiislamu..	176
Mtizamo wa Uislamu juu ya Usawa kati ya Mwanamume na Mwanamke. ....	177
Haki za Mwanamke katika Uislamu .....	186
Haki za Uchumi.....	187
Ni Uislamu pekee umemuinua mwanamke kiuchumi na maadili.....	187

Haki za Kijamii .....	189
Haki ya kushiriki katika siasa.....	192
Je, Wanawake Wanayo Haki ya Kupiga Kura? .....	194
Je, Wanawake wanayo haki ya kushiriki katika Bunge?.....	195
Je, Uislamu unawakataza wanawake kuwa viongozi? ...	197
Kwa nini Mwanamke Haruhusiwi Kuwa Mkuu wa Nchi? .....	198
Je, Wanawake Wanaweza kuwa Majaji? .....	199
Haki ya Elimu .....	200
Kujiepusha na Vishawishi vya Zinaa.....	203
Mavazi na Stara ya Kiislamu.....	206
Mipaka ya Stara (Awrah) ya Mwanamume.....	207
Mipaka ya Stara (Awrah) ya Mwanamke.....	208
Kwa nini Stara zaidi yatakikana kwa Mwanamke? .....	209
Kubisha Hodi. ....	211
Makatazo ya kuwashika wanawake na kukaa faragha nao.....	212
Adhabu ya Wazinifu .....	213
Adhabu kwa Wenye Kuwasingizia Wanawake Watahirifu kuwa Wamezini.....	215
<b>Zoezi 2:5</b> .....	216

<b>MISINGI YA MAADILI KATIKA UISLAMU .....</b>	<b>217</b>
Binadamu si Mnyama .....	217
Mtizamo wa Kikafiri juu ya Maadili .....	219
Lengo kuu la Maisha kwa Mtazamo wa Makafiri.....	220
Utambuzi wa Mema na Maovu kwa	
Mtizamo wa Makafiri .....	221
Msimamizi wa Maadili kwa Mtizamo wa Makafiri .....	222
Motisha wa Kufuata Maadili kwa Mtizamo	
wa Makafiri.....	222
Mtizamo wa Uislamu Juu ya Uadilifu .....	223
Majibu ya Maswali Manne Yanavyotolewa na Uislamu ..	226
Lengo Kuu la Maisha kwa Mtizamo wa Uislamu .....	226
Chem chem ya Ujuzi wa Wema na Uovu kwa	
Mtizamo wa Uislamu .....	227
Msimamizi wa Maadili kwa Mtizamo wa Uislamu .....	227
Motisha inayowapelekea Waislamu kusimamisha Uadilifu	
katika Jamii.....	228
 <b>Zoezi 2:6 .....</b>	 <b>228</b>
 <b>UTAMADUNI .....</b>	 <b>229</b>
Utamaduni wa Muislamu .....	229
Vipengele vya Utamaduni wa Kiislamu .....	232
Tabia njema .....	232

Vazi la Kiislamu.....	234
Miiko katika kula na kunywa .....	240
Vyakula Vilivyo Haramishwa.....	241
Vinywaji Vilivyoharamishwa .....	243
Vyakula na Vinywaji Halali .....	244
Adabu za Kula .....	245
Michezo na Burudani.....	251
Michezo Iliyuruhusiwa katika Uislamu .....	251
Michezo Iliyoharamishwa katika Uislamu.....	252
Sherehe na Burudani.....	255
Sherehe ya Kiislamu ni tofauti sana na hizi za Kitwaghuti.....	256
Nyimbo na mashairi .....	257
Misiba na Maombolezo .....	258
Maombi na Dua .....	260
<b>Zoezi la 2:7 .....</b>	<b>268</b>
<b>SHERIA KATIKA UISLAMU .....</b>	<b>269</b>
Maana ya Sheria .....	269
Kazi ya Sheria katika Jamii.....	269
Chimbuko la sheria za Kitwaghuti.....	270
Udhaifu wa Sheria Zilizotungwa na Binadamu .....	271
Udhaifu katika Usimamizi wa Sheria za Kitwaghuti.....	273

Chimbuko la Sheria ya Kiislamu.....	273
Vyanzo Vingine vya Sheria ya Kiislamu .....	274
Halali na Haramu Katika Sheria ya Kiislamu.....	278
Mahakama ya Kiislamu .....	279
Taratibu za Mashtaka katika Sheria ya Kiislamu .....	283
Haki za Mtuhumiwa wakati wa Kuhojiwa.....	285
Mgawanyo wa Makosa .....	288
Makosa ya Hudud .....	288
Makosa ya Qisas .....	292
Makosa ya Ta'azir.....	293
Haki za wasiokuwa Waislamu (Dhimmi) .....	293
<b>Zoezi 2:8</b> .....	295
<b>UCHUMI KATIKA UISLAMU</b> .....	295
Maana ya Uchumi .....	295
Nadharia ya Uchumi wa Kiislamu.....	296
Tofauti kati ya mfumo wa uchumi wa Kiislamu na ile ya Kitwaghuti .....	297
Milki ya Rasilimali.....	299
Wajibu wa Kufanyakazi.....	301
Uchaguzi wa kazi .....	302
Tofauti ya malipo .....	302

Hifadhi ya Wafanyakazi.....	303
Umuhimu wa uchumi katika Uislamu .....	303
Mazingatio muhimu katika uchumi wa Kiislamu .....	305
Sera ya uchumi katika Uislamu.....	307
Haki ya Serikali kuzuia Dhulma .....	307
Nafasi ya serikali katika ugawaji.....	308
Haki na Uhuru wa kuchuma katika Uislamu.....	309
Biashara.....	309
Biashara haramu.....	313
Haki ya Kumiliki Mali .....	318
Mipaka ya Umilikaji Mali .....	319
Ubadhilifu ni Kufanya Mojawapo ya Mambo Matatu .....	320
Mgawanyo wa mali katika Uislamu .....	320
Matukio Maalum ya Kutolewa kwa Sadaka .....	322
Sadaka Wakati wa Dharura .....	324
Njia za uchumi zilizoharamishwa .....	325
Suala la Omba-Omba .....	328
Mfumo wa benki .....	330
Mabenki ya Riba .....	330
Tatizo la Riba.....	331
Madhara ya Riba katika Jamii.....	331
Uharamu wa Riba katika Uislamu .....	333
Ufumbuzi wa Tatizo la Riba .....	333



Mali yenye Kuchangiwa Mtaji kwa Hisa .....	337
Faida Anazopata Atakayekuwa Mwenye Kumiliki Mali ...	337
Faida kwa Wenye Kununua Hisa.....	337
Benki za Kiislamu .....	338
Uzuri wa Benki za Kiislamu .....	349

<b>Zoezi 2:9</b> .....	340
------------------------	-----

## **SIASA NA UENDESHAJI WA DOLA KATIKA UISLAMU** .....

Maana ya siasa .....	341
Mifumo ya siasa ya Kitwaghuti .....	341
Mifumo ya siasa ya Kiislamu .....	344
Dhana ya Dola .....	344
Dola za Kitwaghuti .....	345
Vyombo vya Kijasusi.....	346
Vyombo vya Itikadi .....	347
Dosari za Dola za Kitwaghuti.....	348
Dhana ya Utawala katika Uislamu.....	349
Vyombo vya Dola ya Kiislamu.....	349
Kazi za Bunge la Kiislamu .....	349
Kazi za Warasimu (Ulul-Amri).....	351
Kazi za Mahakama .....	351

Uraia katika Dola ya Kiislamu .....	353
Msonge wa Uongozi katika Dola ya Kiislamu .....	353
Msonge wa Uongozi katika Uislamu .....	354
Kwa nini Utii Uelekezwe Kwanza kwa Allah (s.w.)? .....	354
Kwa nini Mtume(s.a.w) Achukue Nafasi ya Pili ya Utii? .....	356
Masharti ya Kuwatii Viongozi (Ulul-amri) .....	357
Sifa za Anayestahiki Kuwa Kiongozi .....	360
Wajibu wa Kiongozi katika Dola ya Kiislamu .....	365
Vyombo vya Dola katika Uislamu.....	369
Demokrasia katika Dola ya Kiislamu .....	369
Tafauti ya Serikali ya Kiislamu na ile ya kidemokrasia ...	370
Serikali ya Kiislamu ni ya Ki-khalifa .....	370
Usimamishaji Haki katika Dola ya Kiislamu .....	372
Haki Zinazomstahiki Kila Mwanaadamu .....	374
Haki za raia katika Dola ya Kiislamu.....	379
Haki za wasiokuwa waislamu katika Dola ya Kiislamu...	384
<b>Zoezi 2:10</b> .....	390
<i>Sura ya Tatu</i> .....	393
<b>QUR'AN</b> .....	393
<b>MADAI YA MAKAFIRI DHIDI YA QUR'AN NA UDHAIFU WA MADAI HAYO.</b> .....	393

Madai ya Makafiri dhidi ya Qur'an.....	393
Tofauti za Kimsingi kati ya Qur'an na Biblia .....	404
Qur'an ni Furqan (inasadikisha Ukweli).....	407
Muhammad Hakuwa Tajiri Baada ya Utume .....	411
Baadhi ya Mifano ya Hali yake Kiuchumi .....	412
<b>UTHIBITISHO KUWA QUR'AN NI NENO LA ALLAH(S.W)</b> .....	416
Kuhifadhiwa kwa Qur'an .....	435
Lugha ya Qur'an: .....	446
Je Qur'an Ilikusanywa na Kuandikwa katika Msahafu Wakati wa Uongozi wa Abu-Bakr(r.a) .....	438
Kwa nini Qur'an Imeshushwa kwa Lugha ya Kiarabu? .....	447
Ujumbe wa Qur'an Utawafikiaje Wale wasio Waarabu au Wale Wasiojua Kiarabu?.....	448
Haja ya Kujifunza Lugha ya Kiarabu kwa Waislamu.....	449
Namna ya Kuiendea Qur'an .....	449
 <b>Zoezi 3.1</b> .....	453
 <b>MAFUNZO YA SURA ZILIZOCHAGULIWA</b> .....	454
1. Suratul Al-A'ala.....	454

<b>Zoezi 3:2</b> .....	460
2. Suratu Dhuhaa (93) .....	461
3. Suratu - Alam - Nashrah (94) .....	465
<b>Zoezi 3:3</b> .....	469
4. Suratut - Tyn (95) .....	469
<b>Zoezi 3:4</b> .....	473
<i>Sura ya Nne</i> .....	475
<b>SUNNAH NA HADITH</b> .....	475
Hadith zilizochaguliwa .....	475
<b>KUMTANGULIZA MWENZIO NA KUFARIJIANA</b> .....	475
Hadith 1: .....	476
Hadith 2: .....	476
<b>UHARAMU WA KIBRI NA MAJIVUNO</b> .....	477
Hadith 3: .....	477
Hadith 4: .....	478
<b>TABIA NJEMA</b> .....	478

Hadith 5:.....	479
Hadith 6:.....	479
<b>UPOLE, UANGALIFU NA UTULIVU .....</b>	<b>480</b>
Hadith 7:.....	480
Hadith 8:.....	481
<b>KUTOA SALAMU.....</b>	<b>482</b>
Hadith 9:.....	482
Hadith 10:.....	483
<b>Zoezi 4 .....</b>	<b>483</b>
<i>Sura ya Tano .....</i>	<i>484</i>
<b>TAREKH.....</b>	<b>484</b>
<b>UONGOZI WA DOLA YA KIISLAMU WAKATI WA MAKHALIFA WA MTUME(S.A.W) .....</b>	<b>484</b>
Utangulizi.....	484
Uchaguzi wa Abubakar Kuwa Khalifa .....	484
Mawazo Tofauti Kuhusiana na Uchaguzi wa Abubakar ..	486
Uchaguzi wa `Umar bin Khattab kuwa Khalifa wa Pili....	487
Uchaguzi wa Uthman bin Affan Kuwa Khalifa wa Tatu ..	488
Uchaguzi wa Ali bin Abu Twalib kuwa Khalifa wa nne...	489
Kuzuka Imani ya Kishia .....	491
Uendeshaji wa Dola ya Kiislamu Wakati wa	

Makhalifa .....	492
Kazi na Wajibu wa Khalifa.....	492
Malipo ya Khalifa.....	493
Khalifa na Utungaji Sheria .....	493
Khalifa na Mahakama .....	494
Khalifa na Uendeshaji wa Dola kwa Ujumla.....	496
Haki za wasiokuwa Waislamu chini ya uongozi wa Khalifa.....	496
Kuanzishwa kwa Polisi. ....	497
Kuanzishwa kwa Magezea .....	498
Khalifa na Kamati za Utendaji .....	498
Uongozi wa Majimbo na Wilaya.....	499
Pato la Serikali.....	499
Ulinzi na Usalama .....	500
Usalama wa Taifa.....	501
Upinzani Dhidi ya Dola ya Kiislamu Wakati wa Makhalifa .....	502
Uasi wa Dola (Riddah).....	502
Sababu zilizopelekea Uasi .....	503
Kukomeshwa kwa Riddah na Chokocho Nyingine .....	504
Kuporomoka kwa Dola ya Kiislamu Aliyoicha Mtume(s.a.w) .....	506
Upinzani Kutoka Miongoni mwa Waislamu.....	506

Madai Dhidi ya Khalifa Uthman .....	506
Fitna za Abdullah bin Sabaa .....	510
Hatua ya Serikali Dhidi ya Waanzilishi wa Fitna na Farka .....	511
Kuwasilisha Malalamiko Kwenye Kikao cha Magavana ..	512
Khalifa Uthman Kufa Shahidi.....	513
Vita vya Wenyewe kwa Wenyewe.....	514
Vita Kati ya Bibi Aisha na Khalifa Ali.....	516
Vita Kati ya Khalifa Ali na Gavana Muawiya .....	516
Suluhu .....	519
Kuibuka kwa Khawarij .....	520
Tamko la Wapatanishi .....	520
Muawiyah Ateka Jimbo la Misri.....	521
Ghasia Sehemu Mbali Mbali za Dola ya Kiislamu .....	521
Kutekwa kwa Makka, Madina na Yemen.....	522
Kuuwawa kwa Ali(r.a).....	522
Kuanzishwa Ufalme.....	523
 <b>Zoezi la 5.1 .....</b>	 524
 <b>KUHUISHA UISLAMU WAKATI WA TABIINA .....</b>	 525
Utangulizi .....	525

Khalifa 'Umar bin Abdul Aziz .....	525
Maimamu Wanne wa Fiq-hi.....	528
Imam Abu Hanifah.....	529
Imam Malik bin Anas.....	530
Imam Muhammad Idris al-Shafii .....	530
Imam Ahmad bin Muhammad bin Hambal .....	531
<b>Zoezi la 5.2 .....</b>	<b>533</b>
<b>KUHUISHA UISLAMU KATIKA KARNE YA 20 A.D ....</b>	<b>534</b>
Utangulizi.....	534
Baadee – U-Zaman Said Nursi.....	534
Mwanzo wa Harakati Zake .....	534
Ikhwani Muslimiin wa Misr. ....	539
Muundo .....	542
Matatizo.....	542
Mafanikio .....	542
Ikhwani Muslimiin wa Sudan.....	543
Wanaharakati wa Sudan katika Uwanja wa Siasa.....	544
Matatizo .....	544
Mafanikio .....	544
Jama'atil Islamy ya Pakistan. ....	544



Muundo na kazi za Jama'atil-Islamy.....	547
Mafanikio .....	548
Matatizo:.....	548
<b>Zoezi la 5:3</b> .....	549
<b>HISTORIA YA KUHUISHA UISLAMU TANZANIA</b> .....	550
Historia ya Kuingia Uislamu Afrika ya Mashariki .....	551
Upinzani Dhidi ya Uislamu Afrika ya Mashariki .....	552
Mbinu za kuwaghilibu na kuwaritadisha waislamu Afrika Mashariki .....	553
Kupigwa Vita Uislamu Tanganyika .....	555
Hesabu ya Schools zote Tanganyika 1955 .....	557
Mchango wa Waislamu Katika Kuleta Uhuru Tanganyika .....	558
Mkutano wa Kwanza wa Waislamu, 1962. ....	561
Pingamizi katika kuleta mabadiliko ya kuwanufaisha Waislamu, 1963. ....	561
Mkutano wa Pili wa Waislamu, 1963 .....	564
Juhudi za Kuanzisha Chuo Kikuu cha Kiislamu Chini ya EAMWS, 1964 .....	567
"Mgogoro" wa EAMWS, 1968 .....	569
Mvutano wa Nyerere, Tewa na Bibi Titi kuhusu EAMWS, 1968. ....	575

Kuasisiwa BAKWATA, 1968.....	579
Athari ya BAKWATA kwa Waislamu na Uislamu .....	585
Kuibuka kwa Vikundi Mbalimbali Badala ya BAKWATA.....	587
Sheikh Malik na Warsha.....	588
Juhudi za Kuirekebisha BAKWATA, 1979 .....	590
Kuanzishwa Seminari ya Masjid Qubah,1983 .....	592
Kuibuka kwa Seminari Nyingi za Kiislamu.....	593
Kuanzishwa Vyuvo vya Ualimu na Chuo Kikuu cha Waislamu .....	594
Kuanzishwa BARAZA KUU ,1992.....	594
Kadhia ya Mabucha ya Nyama ya Nguruwe,1993.....	597
Mauaji ya Waislamu Mwembechai, 1998 .....	602
Kuanzishwa Kamati za Kuendeleza Uislamu, 2002.....	605
<b><i>Rejea za Sura ya Tano</i></b> .....	607

## Sura ya Kwanza

# TAWHIID

Katika kitabu hiki somo la Tawhiid linahusika na mada zifuatazo:

- Kuamini Mitume wa Mwenyezi Mungu(s.w).
- Kuamini siku ya Mwisho.
- Kuamini Qadar ya Mwenyezi Mungu(s.w).
- Tofauti ya Uislamu na Dini nyingine.

## KUAMINI MITUME WA MWENYEZI MUNGU(S.W)

### Umuhimu wa Kuamini Mitume

Kuamini Mitume wa Mwenyezi Mungu(s.w) ni nguzo ya nne ya Imani ya Kiislamu. Katika Qur'an tunafahamishwa kuwa waumini wa kweli pamoja na kuamini vipengele vingine vya nguzo za Imani wanaamini Mitume wote wa Mwenyezi Mungu(s.w).

قُولُوا ءَامِنًا بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْنَا وَمَا أُنزِلَ إِلَىٰ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ  
وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ وَالْأَسْبَاطِ وَمَا أُوتِيَ مُوسَىٰ وَعِيسَىٰ وَمَا أُوتِيَ  
التَّابُوتَ مِن رَّبِّهِمْ لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِّنْهُمْ وَنَحْنُ لَهُ مُسْلِمُونَ ﴿١٣٦﴾

*Semeni nyinyi (Waislamu kuwaambia Mayahudi na wakristo); Tumemwamini Mwenyezi Mungu na yale tuliyoteremshiwa, yale yaliyoteremshwa kwa Ibrahimu na Ismail na Is-haqa na Yaaqubu na kizazi (chake Yaaqubu); na waliyopewa Musa na Isa na pia yale waliyopewa Manabii (wengine) kutoka kwa Mola wao; hatutafautishi baina ya yoyote katika hao. (Wote tunawaamini); na sisi tumenyenyekea kwake” (2:136).*

ءَامِنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مِن رَّبِّهِ وَالْمُؤْمِنُونَ كُلٌّ ءَامِنٌ بِاللَّهِ  
وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِّن رُّسُلِهِ ؕ وَقَالُوا  
سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا غُفْرَانَكَ رَبَّنَا وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ ﴿٢٠٨﴾

*Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola wake na Waislamu, (pia wameamini hayo); wote wamemwamini Mwenyezi Mungu, na Malaika*

wake, na Vitabu vyake, na **Mitume yake**; (nao hao Waislamu na Mtume wao husema), Hatutafautishi baina ya yoyote katika Mitume yake (wote tunawaamini)”. Na husema: “Tumesikia na tumetii (tunakuomba) msamaha, Mola wetu! na marejeo ni kwako” (2:285).

Aya hizi zinasisitiza kuwa ili mtu awe muumini wa kweli hana budi kuwaamini Mitume wote wa Mwenyezi Mungu(s.w). Kuamini baadhi ya Mitume wa Mwenyezi Mungu(s.w) na kuwakanusha wengine kama walivyofanya Mayahudi na Wakristo ni ukafiri kama tunavyofahamishwa katika aya zifuatazo:

إِنَّ الَّذِينَ يَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيُرِيدُونَ أَنْ يُفَرِّقُوا بَيْنَ اللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيَقُولُونَ نُؤْمِنُ بِبَعْضٍ وَنَكْفُرُ بِبَعْضٍ وَيُرِيدُونَ أَنْ يَتَّخِذُوا بَيْنَ ذَلِكَ سَبِيلًا ﴿١٥٠﴾ أُولَٰئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ حَقًّا وَأَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ عَذَابًا مُّهِينًا ﴿١٥١﴾

“Hakika wale wanaomkanusha Mwenyezi Mungu na Mitume yake, na wanataka kutenga baina ya Mwenyezi Mungu na Mitume yake, kwa kusema: “Wengine tunawaamini na wengine tunawakataa” na wanataka kushika njia iliyo katikati ya haya (si ya Kiislamu khasa wala ya Kikafiri). Hao ndio makafiri kweli. Na tumewaandalia makafiri adhabu idhalilishayo. (4:150-151).

## Historia ya Maisha ya Mitume

Ukichunguza historia ya maisha ya Mitume na kaumu zao na hasa wale Mitume ambao habari zao zimesimuliwa kwa urefu katika Qur’an kama vile Nuhu, Ibrahim, Lut, Musa, Sulaiman, Isa na Muhammad (Rehema na Amani ziwe juu yao), utayakinisha kuwa ni lazima wawe ni wajumbe wa Mwenyezi Mungu(s.w). Katika historia ya maisha ya Mitume, yapo matukio mbali mbali yaliyo nje kabisa ya uwezo wa mwanaadamu ambayo iwapo yatazingatiwa ipasavyo, huwa ni ishara na hoja kubwa ya kuwepo Aliye mjuzi mwenye Hikima na uwezo wa hali ya juu aliyewatuma hapa ulimwenguni kama wajumbe wake.

## Mwisho wa Utume

Ili kulelewa vizuri suala hili la mwisho wa Utume yafaa kwanza tuzingatie haya yafuatayo. Kilicho muhimu na cha msingi kabisa kwa Mtume yeyote si kule kuwepo kwake kimwili bali ni kule kufikisha kwake kikamilifu ujumbe aliopewa na Mwenyezi Mungu kwa watu ili watu baada ya kujua ujumbe wa Mwenyezi Mungu wasiwe na hoja tena iwapo watachagua kupotea. Mitume wote waliomtangulia Muhammad(s.a.w), baadhi ya mafundisho yao yamepotea

kabisa na baadhi yamepotoshwa na kuchanganywa na hekaya za watu. Katika vitabu vilivyoitangulia Qur'an kwa mfano, Taurati, Zaburi na Injili hakuna hata kimoja ambacho kipo katika hali ya usahihi wake wa asili. Hata wanaodai kuvifuata vitabu hivyo wanakiri kuwa nakala walizonazo leo si zile walizopewa Mitume. Si hivyo tu bali hata historia ya maisha ya Mitume waliomtangulia Muhammad(s.a.w) zimechanganywa na simulizi za watu katika vitabu hivyo hata inakuwa vigumu kupambanua haki na batili. Hivyo, iliibidi aletwe Mtume baada ya Mtume aliyeeondoka iwapo:

**Kwanza**, Mafundisho ya Mtume aliyetangulia yamechanganywa na hekaya za uzushi, au yamesahauliwa au yamepotea. Katika hali kama hiyo Mtume anahitajika ili aje aifundishe Dini katika usahihi wa awali ili wale wanotaka kuongoka waongoke.

**Pili**, Mafundisho ya Mtume aliyeeondoka hayakukamilika kiasi cha kukidhi haja ya wakati uliopo.

**Tatu**, Mtume aliyetangulia alipelekwa kwa watu wa taifa fulani maalumu au nchi fulani na pakawepo haja ya kuletwa Mtume wa watu wa taifa au nchi nyingine iliyoibuka au pengine Mtume anaweza kuletwa amsaidie Mtume mwingine. Katika Qur'an ipo mifano miwili tu kama hiyo. Nabii Harun (a.s) alikuwa msaidizi wa Nabii Musa(a.s) na Nabii Lut(a.s), Nabii Ismail(a.s) na Nabii Is-haq(a.s) walikuwa wasaidizi wa Nabii Ibrahim(a.s).

Hayo matatu ndiyo mahitajio makuu ya kimsingi yanayopelekea kuletwa kwa Mtume mwingine baada ya kuondoka yule aliyetangulia. Kwa kuzingatia haya utaona wazi kuwa hapana haja ya kuja Mtume mwingine baada ya Muhammad(s.a.w) kwa sababu:

**Kwanza**, Mafundisho ya Mtume(s.a.w) yako hai na yamehifadhiwa kwa ahadi ya Allah(s.w):

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ ﴿١٠﴾

*Hakika sisi ndio tulioteremsha mawaidha (haya) (hii Qur'an); Na hakika sisi ndio tutakaoyalinda' (15:9).*

Pia Sunnah zake Mtume(s.a.w) zimehifadhiwa kikamilifu kiasi ambacho mtu anaweza kujua bila shaka yoyote ni yepi mafundisho ya Mtume juu ya jambo fulani na yepi ambayo Mtume(s.a.w) kazuliwa. Hivyo sharti la kwanza la kuja Mtume mwingine linaondoka.

**Pili**, Mwenyezi Mungu amekamilisha mwongozo wake kwa Nabii Muhammad(s.a.w) na hivyo Uislamu ni Dini (mfumo) wa maisha kamilifu kwa walimwengu wote. Mwenyezi Mungu(s.w) anahitabitisha hili katika Qur'an:

..... أَلْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتَمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ

لَكُمْ الْإِسْلَامَ دِينًا ..... ﴿٥:٣﴾

“..... Leo nimekukamilishieni dini yenu, na kukutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni Uislamu uwe dini yenu.....” (5:3).

Aya hii ilimshukia Mtume(s.a.w) katika Hija ya kuaga, 9 Dhul-Hijjah 10 A.H. Inasemekana hii ndiyo aya ya mwisho kushuka. Tukiutafiti Uislamu kwa makini kama mfumo kamili wa maisha tunaona unadhihiri ukweli wa aya hii ya Qur’an. Uislamu unatoa mwongozo kwa maisha haya na ya akhera na hakuna jambo lililo muhimu katika kumuongoza binaadamu lisilokuwemo katika mwongozo aliokuja nao Muhammad(s.a.w). Hivyo hoja ya kuhitajia Mtume ili aje kukamilisha dini pia inaondoka.

Hata hivyo kuna baadhi ya watu wanaosema kwamba kupita tu kwa muda mrefu peke yake ni sababu ya kuhitajia Mtume mwingine. Hii ni kwa sababu wanasema mwongozo ulioletwa karne 14 zilizopita ni wa kale mno kiasi ambacho hauwezi kukidhi mahitaji ya watu wa leo. Mawazo haya hayana msingi kabisa, kwa sababu ziufatazo:

(i) Mafundisho ya Uislamu ni ya milele kwa sababu ni ufunuo utokao kwa Mwenyezi Mungu mjuzi wa yote ya kale, ya sasa na yajayo, tena mwenye uhai wa milele. Elimu ya binadamu ndiyo yenye ukomo, na ni jicho la binadamu lisiloweza kuona hata kesho achilia mbali miaka milioni moja ijayo. Elimu na hikima ya Mwenyezi Mungu imesalimika na upungufu kama huo.

(ii) Uislamu umeegemeza mafundisho yake juu ya umbile la binaadamu. Na umbile la binaadamu limesalia vile vile katika zama zote. Watu wote wamejengwa kwa majengo yale yale yaliyowajenga watu wa kale kabisa na hivyo umbile lao kimsingi ni lile lile.

(iii) Katika maisha ya binaadamu kuna mizani maridadi kabisa baina ya mambo yanayodumu na mambo yanayobadilika. Misingi muhimu na maadili hayabadiliki kutokana na kupita kwa muda. Qur’an na Sunnah ya Muhammad(s.w) vinatoa kanuni na misingi ya milele ya Uislamu na kwa kutumia Ijtihad misingi hiyo inaweza kutekelezwa kadri hali itakavyobadilika. Uislamu ndiyo Dini pekee iliyoweka utaratibu madhubuti unaoweza kuoanisha maendeleo ya binadamu na misingi ya kitabu cha Mwenyezi Mungu (Qur’an) na Sunnah ya Mtume Muhammad(s.a.w).

**Tatu**, tukirudi katika hitajio letu la tatu la kuhitajia kuletwa Mtume mwingine, tunaona kuwa Muhammad(s.a.w) hakuletwa kwa taifa au watu maalum bali kwa walimwengu wote. Qur’an yasema:

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا..... ﴿١٥٨﴾

*Sema (Ewe Nabii Muhammad): “Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu nyinyi nyote” (7:158).*

Kutokana na hoja zote hizi itaonekana wazi kwa nini hapana haja ya kuja Mtume mwingine baada ya Muhammad(s.a.w). Na kuwa yeye ni “Khataman-Nabiyyina” yaani mwisho wa (msururu) wa Mitume wa kweli.

مَا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِّن رِّجَالِكُمْ وَلَكِن رَّسُولَ اللَّهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ  
وَكَانَ اللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا ﴿٣٣﴾

*Muhammad si baba wa yoyote katika wanaume wenu, bali yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na mwisho wa Mitume, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu” (33:40).*

Na Mtume Muhammad(s.a.w) mwenyewe pia anasema:

*Palikuwa na Mitume waliowaongoza Bani Israil katika njia sahihi. Kila Mtume alipokufa alifuatiwa na Mtume mwingine. Lakini hapana Mtume atakayekuja baada yangu. Kazi hii (ya kuufundisha Uislamu na kuusimamisha) inaweza kufanywa na Makhalfi (viongozi wa Kiislamu) (Bukhari).*

## Maana ya Kuamini Mitume katika Maisha ya kila Siku

Hatua ya **kwanza** katika kuamini Mitume wa Mwenyezi Mungu ni kuyakinisha kuwa Mwenyezi Mungu(s.w) amewateua wajumbe miongoni mwa wanadamu wanaume kufikisha ujumbe wake kwa wanaadamu wa enzi zote za historia. Uyakini juu ya wajumbe hawa tunaupata kutokana na dalili mbalimbali zilizodhihiri kutokana na historia ya maisha yao na mafundisho yao.

Hatua ya **pili** katika kuamini Mitume wa Mwenyezi Mungu ni kuwatii Mitume, kufuata mafundisho yao na kuigiza tabia na mwenendo wao katika kuuendesha maisha kila siku. Hii ndio hatua inayotoa maana halisi ya kuamini Mitume wa Mwenyezi Mungu katika maisha ya kila siku.

Hebu sasa tuangalie nini maana ya kumuamini Mtume Muhammad(s.a.w) katika maisha ya kila siku. Maana halisi ya kumuamini Mtume(s.a.w) kama ilivyobainishwa katika Qur’an na Sunnah ni kutenda haya yafuatayo:

### (i) Kumtii Mtume(s.a.w)

Kwa kufuata kwa ukamilifu na kwa unyenyekevu yale yote aliyoyaamrisha Mtume(s.a.w) na kuyaacha na kujiepusha mbali kwa moyo mkunjufu yale yote aliyoyakemea na kuyakataza. Mwenyezi Mungu(s.w) anatufahamisha katika

Qur'an kuwa njia pekee ya kupata mafanikio kutoka kwake katika maisha ya dunia na akhera ni kumtii Mwenyezi Mungu na kumtii Mtume wake. Ukirejea aya nyingi za Qur'an utakuta amri ya **kumtii Mwenyezi Mungu** imeambatanishwa na amri ya **kumtii Mtume(s.a.w)**.

قُلْ أَطِيعُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ ط فَإِنْ تَوَلَّوْا فَإِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْكٰفِرِينَ ﴿٣١﴾

*Sema: "Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume (wake). Na kama mkikengeuka, (Mwenyezi Mungu atakutieni adabu) kwake Mwenyezi Mungu hawapendi makafiri" (3:32).*

Pia rejea aya zifuatazo: (4:59), (59:7) na (3:31).

### **(ii) Kuiga tabia na mwenendo wa Mtume Muhammad(s.a.w)**

Kumuamini Mtume hakuishii kwenye kufuata mafundisho yake tu bali na kuiga tabia yake kwa kadri iwezekanavyo na kuiga mwenendo wa maisha yake yote kwa ujumla. Mtume(s.a.w) hakutenda jambo lolote katika maisha yake lililo kinyume na ridhaa ya Mwenyezi Mungu. Pale alipoteleza kidogo kutokana na ubinadamu kinyume na ridhaa ya Mwenyezi Mungu(s.w), Mola wake alimkosoa pale pale na kumsamehe kwa kosa lile.

Kwa hiyo tabia ya Mtume(s.a.w) na mwenendo wa maisha yake umeridhiwa na Mwenyezi Mungu(s.w). Hivyo kila mwenye kumuigiza Mtume kitabia na mwenendo moja kwa moja atakuwa na uhakika wa kupata upendo na radhi ya Mwenyezi Mungu(s.w) Qur'an inatuthibitishia;

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ  
الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا ﴿٢١﴾

*"Bila shaka mnao mfano mwema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwa mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na kumtaja (kumkumbuka) Mwenyezi Mungu sana" (33:21).*

### **(iii) Kumpenda Mtume(s.a.w)**

Ni katika umbile la mwanaadamu kuwa hakithamini kitu asichokipenda na hawezi kumheshimu na kumtii mtu asiyempenda. Heshima na utii bila ya upendo ni unafiki. Hali kadhalika iwapo mja hatakuwa na upendo na Mwenyezi Mungu na Mtume wake zaidi kuliko chochote kile, ni vigumu kuwa na heshima na utii halisi kwa Mwenyezi Mungu(s.w) na Mtume wake. Kinyume chake atakuwa anavitii na kuviheshimu vile anavyovipenda zaidi. Msisitizo wakumpenda Mwenyezi Mungu, Mtume wake na Dini yake tunaupata katika aya ifuatayo:



قُلْ إِنْ كَانَ آبَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ وَإِخْوَانُكُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ وَعَشِيرَتُكُمْ  
 وَأَمْوَالٌ اقْتَرَفْتُمُوهَا وَتِجَارَةٌ تَخْشَوْنَ كَسَادَهَا وَمَسَاكِينُ تَرْضَوْنَهَا أَحَبَّ  
 إِلَيْكُمْ مِنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَجِهَادٍ فِي سَبِيلِهِ فَتَرَبَّصُوا حَتَّى يَأْتِيَ  
 اللَّهُ بِأَمْرِهِ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ ﴿٩٤﴾

*Sema: “Kama baba zenu na wana wenu na ndugu zenu na wake zenu na jamaa zenu na mali mlizochuma na biashara mnazoogopa kuharibikiwa, na majumba mnayoyapenda; (ikiwa vitu hivi) ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kupigania Dini yake basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake; na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu maasi (njia iliyonyooka)” (9:24).*

Kumpenda Mwenyezi Mungu(s.w) na kumpenda Mtume(s.a.w) si jambo lingine zaidi ya kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa unyenyekevu na upendo. Kwa maana nyingine muumini wa kweli hatatii matashi ya nafsi yake au amri ya yeyote kinyume na Qur’an na Sunnah ya Mtume(s.a.w). Ni katika maana hii Mtume(s.a.w) anasema:

*“Hatakuwa mmoja wenu ni muumini wa kweli mpaka anipende zaidi kuliko chochote kile ikiwa ni pamoja na familia yake, mali yake na watu wote” (Muslimu).*

*“Yeyote yule anayependa Sunnah yangu ananipenda, na yeyote yule anayenipenda atajikuta yuko ubavuni mwangu huko peponi” (Tirmidh).*

*“Yule aliyeridhika na kukinai kuwa Mwneyezi Mungu ni Bwana wake, kuwa Uislamu ndio mtindo wake pekee wa maisha, na kuwa Muhammad ni Mtume wake, hakika ameonja ladha tamu ya imani” (Muslim).*

Hadith hizi zinatufahamisha umuhimu na maana ya kumpenda Mtume. Upendo wa kweli kwa Mtume ni kutii ujumbe aliokuja nao na kufuata kwa ukamilifu Sunnah yake. Lakini utakuta kuwa baadhi ya watu wamefunga upendo wa Mtume katika nyimbo za kumsifu Mtume kwa sifa mbalimbali bila ya kufuata mafundisho yake na bila ya kumuigiza katika kusimamisha Dini ya Mwenyezi Mungu(s.w). Upendo wa namna hii, unaoishia kwenye kuwasifu Mitume kwa sifa kadhaa wa kadhaa, tunaona katika historia umewapelekea watu kuwashirikisha Mitume na Mwenyezi Mungu(s.w). Mtume(s.a.w) katika kutuongoza tusirudie kosa hili la historia la kuwasifu Mitume kupindukia mipaka anatuonya katika Hadith ifuatayo:

'Umar(r.a) amesema kuwa Mtume(s.a.w) amesema: "Msizidisha kwenye kunisifu kama walivyoizidisha Manasara (Wakristo) katika kumsifu Mwana wa Maryam. Mimi ni mja wa Mwenyezi Mungu tu, kwa hiyo niiteni: "Mja wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake" (Bukhari).

#### (iv) Kumfanya Mtume(s.a.w) Hakimu katika kila jambo

Imani ya kweli juu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ni pamoja na kuridhika kwa moyo mkunjufu na hukumu yake katika kuwaamua waliogombana au kuridhika kwa moyo mkunjufu na uamuzi wake juu ya jambo lolote lile. Katika Qur'an tunafahamishwa:

فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴿٦٥﴾

"Naapa kwa (haki ya) Mola wako. Wao hawawi wenye kuamini (kweli kweli) mpaka wakufanye (wewe ndiye) hakimu (mwamuzi) katika yale wanayokhitalifiana, kisha wasione uzito nyoyoni mwao juu ya hukumu uliopitisha na wanyenyekee kabisa" (4:65).

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا لِمُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَىٰ اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾

"Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake hakika amepotea upotofu (upotevu) ulio wazi (kabisa)" (33:36).

Katika aya hizi tunafahamishwa kuwa mtu hatakuwa muumini wa kweli mpaka hapo atakapomfanya Mwenyezi Mungu(s.w) na Mtume wake(s.a.w) ndio Mahakimu wake pekee kwa kuridhika na hukumu ya Qur'an na Sunnah.

..... سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٥١﴾ وَمَنْ يُطِعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَخَشِيَ اللَّهَ وَيَتَّقْهِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَائِزُونَ ﴿٥٢﴾

".....Tunasikia na tunakubali", na hao ndio watakaofuzu. Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kumuheshimu Mwenyezi Mungu na kumuogopa hao ndio wenye kufuzu, (kufaulu)" (24:51-52).

## KUAMINI SIKU YA MWISHO

### Umuhimu wa Kuamini Siku ya Mwisho

Kuamini siku ya mwisho ni nguzo ya tano ya Imani ya Kiislamu. Pamoja na nguzo hii kuwa ya tano katika orodha ya nguzo za Imani, ni nguzo ya msingi mno kwani ndio nguzo inayompa mja msukumo wa kutenda wema na kujiepusha na maovu katika maisha ya kila siku kwa matarajio ya kupata makazi mema ya peponi na kuepukana na adhabu kali ya motoni. Katika Qur'an, msisitizo wa kuamini Mwenyezi Mungu(s.w) mara nyingi umeambatanishwa na msisitizo wa kuamini siku ya mwisho. Kwa mfano katika Qur'an tunasoma:

﴿لَيْسَ الْبِرَّ أَنْ تُوَلُّوا وُجُوهَكُمْ قِبَلَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَلَكِنَّ الْبِرَّ مَنْ ءَامَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالْكِتَابِ وَالنَّبِيِّينَ.....﴾



*Sio wema (peke yake tu) kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi, bali wema hasa ni (wa wale) wanaomwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na Malaika na Vitabu na Manabii.....” (2:177).*

### Ainicho la Siku ya Mwisho

Kuamini siku ya mwisho ni miongoni mwa mambo ya ghaibu ambayo mwanaadamu hana uwezo wa kuyadiriki kwa milango ya fahamu bali huhitajia matumizi makubwa ya akili pamoja na elimu ya ufunuo (Wahyi) kutoka kwa Muumba mwenyewe kupitia kwa Mitume wake. Mitume walifahamishwa vyema mazingira halisi ya siku ya mwisho, ili waweze kuwaonya na kuwatahadharisha wanaadamu kwa maisha hayo kwa msisitizo wa uhakika. Ukirejea msisitizo wa maonyo ya Mitume kwa watu wao utakuwa na picha ya uhakika waliokuwa nao juu ya siku ya mwisho.

Kuamini siku ya mwisho ni kuamini kuwa kuna maisha ya milele baada ya maisha haya ya hapa duniani na kuwa maisha hayo yana hatua muhimu zifuatazo:

- (i) Kutokwa na roho
- (ii) Maisha ya Kaburini (Bar-zakh)
- (iii) Kufufuliwa na kuhudhurishwa katika Hisabu
- (iv) Kuhesabiwa au mwanaadamu kuhukumiwa kulingana na utendaji wake hapa duniani.
- (v) Kulipwa malipo mema ya kukaa peponi milele au kulipwa adhabu kwa kuingizwa motoni Jahannam, kulingana na namna mja alivyofikia au alivyo kwenda kinyume na lengo la maisha ya duniani.

Katika Qur'an siku ya mwisho imeitwa kwa majina mengi ili kutoa picha ya yatakayotokea huko. Imeitwa kwa majina kama: Siku ya Kiyama (siku ya kusimama mbele ya Mahakama ya Mwenyezi Mungu), Siku ya malipo, Siku ya hukumu, Siku ya hesabu, Siku ya huzuni, Siku ya kufichuliwa siri, Siku ya Mtingisho, Siku ya Ahadi, Siku yenye kushuhudiwa na kadhalika.

Siku ya mwisho si jambo linalokubalika kwa wanaadamu wote kama ilivyo katika kumuamini Mwenyezi Mungu(s.w). Imani juu ya siku ya mwisho nayo imewagawanya wanaadamu katika makundi makubwa mawili, kundi la **makafiri** wanaokataa kuwepo kwa siku ya mwisho na kundi la **waumini** wanaokiri kuwepo siku ya mwisho.

## Hoja za Wapinzani wa Siku ya Mwisho na Udhaifu Wake

Msingi wa hoja za wapinzani wa siku ya malipo ni kukana kuwepo kwa Mwenyezi Mungu(s.w) mwenye uwezo juu ya kila kitu na aliyumba ulimwengu na vyote vilivyomo kwa lengo maalum. Msingi wa kukana kuwepo Mwenyezi Mungu(s.w) ni kukwepa majukumu na kutafuta starehe ya dunia kwa uhuru bila ya kuchunga mipaka yoyote iliyowekwa na Mwenyezi Mungu(s.w). Kutokana na msingi huu mbaya wapinzani wa siku ya mwisho hutetea msimamo wao kwa hoja zifuatazo:

- (i) Mwanaadamu hana lengo la maisha, isipokuwa kustarehe tu.
- (ii) Hakuna uwezekano wa kupatikana uhai baada ya kuoza na kusagika sagika.
- (iii) Waliokufa hawajarudi wakatoa ushahidi.

Hebu tuone udhaifu wa hoja hizi:

### (i) Mwanaadamu hana lengo la maisha, isipokuwa kustarehe tu.

Msingi mkubwa wa hoja hii ni kupenda starehe za dunia kama anavyotufahamisha Mwenyezi Mungu(s.w) katika aya zifuatazo:

بَلْ تُوذِرُونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ﴿١٦﴾ وَالْآخِرَةَ خَيْرٌ وَأَبْقَى ﴿١٧﴾

“Lakini nyinyi mnapenda zaidi maisha ya dunia, hali ya kuwa ya akhera ni bora na yenye kudumu” (87:16-17).

Kwa ajili ya kupenda maisha ya dunia na starehe zake makafiri wamejitia uziwi na upofu na kukataa kutafakari juu ya hali halisi ya mazingira ya ulimwengu ambayo yanaonesha wazi kwa kila mwenye akili timamu, kuwa yanamuumba mweledi mwenye nguvu na hekima: Ulimwengu uliomzunguka mwanaadamu upo kwa manufaa ya mwanaadamu katika kurahisisha na kustawisha maisha yake. Bado makafiri wanadai kuwa ulimwengu huu haukukusudiwa kufikia

lengo lolote na wala mwanaadamu mwenyewe hana lengo lolote la maisha ila kuufaidi tu ulimwengu, Hivyo katika maisha haya mwanaadamu hawajibiki kwa yeyote na kufa ndiyo mwisho wa mchezo wa bahati nasibu ya maisha.

**Udhaifu** wa hoja hii uko wazi kwa kila mwenye akili timamu. Akili haikubali kuwa ulimwengu huu, namna ulivyoumbika na namna ulivyofungamana na taratibu na sheria madhubuti, uwe hauna muumbaji mwenye uwezo, ujuzi na hekima isiyo mipaka, aliyeuumba kwa lengo maalumu. Wala akili haikubali kuwa mwanadamu mwenye vipawa vya akili, ufahamu na utambuzi wa hali ya juu kuliko viumbe vyote lengo lake la maisha liishie kwenye kula, kunywa na kuishi kama wanyama. Akili inatulazimisha tutafute lengo halisi la kuumbwa ulimwengu na vyote vilivyomzunguka mwanaadamu na mwanaadamu ni lazima awe na lengo tofauti na lile la wanyama na viumbe wenigne. Mwenyezi Mungu(s.w) anatumia hili katika Qur'an:

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَاءَ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا بَطْلًا ۚ ذَٰلِكَ ظَنُّ الَّذِينَ كَفَرُوا  
فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ كَفَرُوا مِنَ النَّارِ ﴿٣٧﴾

*“Na Hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake bure. Hii ni dhana ya wale waliokufuru. Basi adhabu kali ya moto itawathibitikia wale waliokufuru” (38:27).*

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا لَعِينًا ﴿٣٨﴾

*“Na hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake kwa mchezo” (44:38).*

Hapa akili inatulazimisha tuone kuwa mwanaadamu ametunukiwa vipaji vyote alivyonavyo na neema zote zilizomzunguka kwa lengo maalum. Na lengo hili si jingine ila lile Mwenyezi Mungu(s.w) analotufahamisha katika Qur'an:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥١﴾

*“Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu” (51:56).*

Kumuabudu Mwenyezi Mungu(s.w) ni kumtii Mwenyezi Mungu(s.w) katika kila kipengele cha maisha kwa kutii kwa unyenyekevu amri zake zote na kuacha kwa moyo mkunjufu makatazo yake yote na kusimamisha ufalme wake, kwa kuamrisha mema na kukataza maovu. Je, kama mwanaadamu pamoja na kuruzukiwa neema zote alizonazo na zilizomzunguka ili afikie lengo hili la kumtumikia Mwenyezi Mungu(s.w), ataamua kumkana Mwenyezi Mungu(s.w) na kuitumikia nafsi yake au kuwatumikia viumbe wenzake kinyume na Mwenyezi Mungu(s.w) jambo ambalo ana uhuru nalo, Mwenyezi Mungu hatamuuliza juu ya jambo hili? Inayumkinika kweli mwisho wa yule aliyeishi kulingana na lengo awe sawa na yule aliyeishi kinyume na lengo? Kama kufa ndio mwisho wa

maisha ya mwanaadamu, tofauti za hawa wawili zitaonekana wapi? Hapana! Akili inatumuru tuone kuwa hapana budi kuwepo siku ya malipo au siku ya hukumu ili yule aliyemtunukia mwanaadamu neema zote alizonazo amuulize jinsi alivyozitumia neema hizo. Mwenyezi Mungu(s.w) anatumfahamisha:

ثُمَّ لَتَسْعَلَنَّ يَوْمَئِذٍ عَنِ النَّعِيمِ ﴿٨﴾

“Kisha kwa hakika siku hiyo mtaulizwa juu ya neema (mlizopewa mmezitumiaje)” (102:8).

Hivyo hoja ya kuwa mwanaadamu hana lengo hapa duniani ni dhana tu isiyo na uthibitisho wowote wa kiakili.

### (ii) Hapana uwezekano wa kupata uhai baada ya kufa

Wapinzani wa siku ya mwisho wamepinga kuwepo kwake si kwa kuwa na ushahidi unaowathibitishia kutokuwepo kwake, bali wameona tu kuwa mtu baada ya kufa na kuoza na kuwa udongo ni muhali kurudi tena kwenye umbo lake la awali. Hili ni jambo lililoingia akilini mwao. Wasi wasi au dhana yao hii ameithibitisha Mwenyezi Mungu katika Qur'an:

يَقُولُونَ أَءِنَّا لَمَرْدُودُونَ فِي الْحَافِرَةِ ﴿١٠﴾ أئِذَا كُنَّا عِظْمًا خِجْرَةً ﴿١١﴾  
قَالُوا تِلْكَ إِذًا كَرَّةٌ خَاسِرَةٌ ﴿١٢﴾

“(Makafiri) wanasema (kwa stihizai): Je! Tutarudishwa katika hali yetu ya kwanza (tutafufuliwa)? Hata tukiwa mifupa mibovu (iliyooza)? Wanasema kwa stihizai: Basi marejeo haya ni yenye hasara (kwetu)” (79:10-12).

Pia rejea Qur'an (56:47-48),

Allah(s.w) ameonyesha udhaifu wa hoja hii katika suratu Yaasyn aya ya 77 hadi 82 (36:77 - 82).

أَوَلَمْ يَرَ الْإِنْسَانُ أَنَّا خَلَقْنَاهُ مِنْ نُطْفَةٍ فَإِذَا هُوَ خَصِيمٌ مُبِينٌ ﴿٧٧﴾  
وَضَرَبَ لَنَا مَثَلًا وَنَسِيَ خَلْقَهُ قَالَ مَنْ يُحْيِي الْعِظْمَ وَهِيَ رَمِيمٌ ﴿٧٨﴾  
قُلْ يُحْيِيهَا الَّذِي أَنْشَأَهَا أَوَّلَ مَرَّةٍ وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ ﴿٧٩﴾ الَّذِي  
جَعَلَ لَكُم مِّنَ الشَّجَرِ الْأَخْضَرِ نَارًا فَإِذَا أَنْتُمْ مِّنْهُ تُوقَدُونَ ﴿٨٠﴾  
أَوَلَيْسَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِقَدِيرٍ عَلَىٰ أَن يَخْلُقَ مِثْلَهُمْ ۗ

بَلَىٰ وَهُوَ الْخَلْقُ الْعَلِيمُ ﴿٨١﴾ إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَنْ يَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٨٢﴾

*Je, mwanaadamu hatambui ya kwamba tumemuumba kwa tone la manii? Amekuwa hasimu yetu aliye dhahiri (Sasa)! Na akatupigia mfano, na akasahau kuumbwa kwake (kwa manii) - akasema: “Nani atakayeihisha mifupa na hali imesagika?” Sema: “Ataihuisha yule aliyeiumba mara ya kwanza, naye ni Mjuzi wa kila (namna ya) kuumba.” Ambaye amekufanyieni moto katika mti mbichi, mkawa nanyi kwa (mti) huo mnauwasha. Je, yule aliyeziumba mbingu na ardhi (mnaona) hana uweza wa kuumba (mara ya pili) mfano wao (wanaadamu)? Kwa nini? Naye ni Mwumbaji mkuu, Mjuzi (wa kila jambo). Hakika amri yake anapotaka chochote (kile kitokee) ni kukiambia: ‘Kuwa, basi mara huwa. (36:77- 82).*

Pia rejea Qur’an:(30:27),(50:15),(75:3 - 4),(88:17-20).

Katika kuonesha udhaifu wa hoja hii ya mkafiri, katika aya hizi Allah(s.w) anawauliza maswali ya msingi yafuatayo:

- (i) Aliyemuumba mwanaadamu mara ya kwanza atashindwa kumuumba mara ya pili ?
- (ii) Ni kipi chepesi kuumba mara ya kwanza au mara pili?
- (iii) Je, Allah(s.w) alipomuumba mwanaadamu mara ya kwanza alibahatisha kwa hiyo hawezi kumuumba tena mara ya pili ?
- (iv) Je, aliyeumba mbingu na ardhi na vyote vilivyomo atashindwa kumuumba mwanadamu mara pili?

Hivyo, ni udhaifu mkubwa sana mtu kudhania kuwa aliyemuumba mwanaadamu kutokana na udongo kisha mbegu za uzazi, hawezi kumrudisha tena kwenye umbo la awali baada ya kufa na kuwa udongo!.

**(iii) Waliokufa hawajarudi wakatoa ushahidi**

وَقَالُوا مَا هِيَ إِلَّا حَيَاتُنَا الدُّنْيَا نَمُوتُ وَنَحْيَا وَمَا يُهْلِكُنَا إِلَّا الدَّهْرُ وَمَا لَهُم بِذَلِكَ مِنْ عِلْمٍ إِنْ هُمْ إِلَّا يَظُنُّونَ ﴿٨٥﴾

*“Na wanaposomewa aya zetu zilizo wazi hawana hoja ila husema Waleteni baba zetu (wazee wetu waliokufa) ikiwa nyinyi ni wasemao kweli (kuwa watu watafufuliwa)” (45:25).*

Makafiri wanaona ni hoja ya kukana kuwepo maisha baada ya kufa kwa vile hawajawaona wale waliokufa wakifufuliwa na kuendelea kuishi tena pamoja nao. Hii si hoja kwa sababu Mwenyezi Mungu(s.w) amebainisha wazi kuwa kufufuliwa hakutatokea kwa mtu mmoja mmoja kwa wakati wake katika ulimwengu huu bali kutakuwa kwa watu wote, wa mwanzo na wa mwisho, kwa wakati mmoja katika ulimwengu mwingine wenye mazingira mengine tofauti na haya. Hivyo kutofufuka wazee wao au watu waliotangulia kwa wakati huu wanaodai wao, hakuondoi uwezekano wa kufufuka watu katika wakati alioupanga mwenyewe Mwenyezi Mungu(s.w). Mwenyezi Mungu anasisitiza:

قُلْ إِنَّ الْأَوَّلِينَ وَالْآخِرِينَ ﴿٤٩﴾ لَمَجْمُوعُونَ إِلَىٰ مِيقَاتِ يَوْمٍ مَّعْلُومٍ ﴿٥٠﴾

*Sema: “Bila shaka wa kwanza na wa mwisho” watakusanywa kwa wakati (uliowekwa) katika siku maalum” (56:49-50).*

Hivyo kutofahamika kwa mwanaadamu wakati wa Kiyama kitakapotokea sio sababu kabisa ya kukana kuwepo kwake kwani kuna mengi tusingiyadiriki kwa milango yetu ya fahamu lakini bado tunakiri kuwa yapo. Kutokana na dalili mbalimbali zinazoonyesha kuwepo kwa hayo. Umeme hatuuoni lakini tunakiri upo, kwa nini? Hivyo Mwenyezi Mungu(s.w) anawahakikishia Makafiri:

## Ulazima wa Kuwepo Siku ya Mwisho

Baada ya kuona hoja za wale wakanao kuwepo siku ya mwisho na udhaifu wa hoja hizo, hebu tuangalie hoja za waumini wa siku ya malipo. Kimantiki ni lazima iwepo siku ya mwisho ili:

- (i) Mwanadamu aulizwe juu ya vipaji na neema mbalimbali alizotunukiwa na mola wake alitumiaje.
- (ii) Mifumo au njia sahihi ya maisha ibainishwe.
- (iii) Ubainike ukweli kwa waliozuliwa uovu.
- (iv) Walipwe wale waliotenda wema bila ya ujira stahiki hapa ulimwenguni.
- (v) Waovu na wababe wapate adhabu stahiki ya makosa yao.
- (vi) Waliodhulumiwa walipwe haki zao mbele ya Hakimu muadilifu.

**(i) Mwanaadamu aulizwe juu ya vipaji na neema mbalimbali alizotonukiwa na Mola wake alitumiaje**

Pamoja na elimu yote aliyotunukiwa binaadamu bado amepewa uhuru wa kuamua juu ya kumuamini Mwenyezi Mungu na kumuabudu inavyostahili au kumkana Mwenyezi Mungu na kuwaabudu wengine badala yake. Kimantiki



ni lazima pawe na siku ya malipo, ili mwanaadamu aulizwe jinsi alivyozitumia neema za Mwenyezi Mungu(s.w) na vipaji alivyotunukiwa. Katika kuendea lengo la kuumbwa kwake. Lengo la kumbwa mwanadamu limebainishwa:

﴿٥١﴾ وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ

“Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu” (51:56).

Ili mwanaadamu afikiw lengo hili mwanaadamu ametunukiwa neema mbalimbali kama Mwenyezi Mungu(s.w) anavyobainisha:

﴿٥٢﴾ هُوَ الَّذِي خَلَقَ لَكُمْ مَّا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا.....

“Yeye(Allah) ndiye aliyekuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi.....)(2:29)

﴿٥٣﴾ \*وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ وَحَمَلْنَاهُمْ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَرَزَقْنَاهُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَى كَثِيرٍ مِّمَّنْ

﴿٥٤﴾ خَلَقْنَا تَفْضِيلًا

Na hakika tumewatukuza wanaadamu na tumewapa vya kupanda barani na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri, na tumewatukuza kuliko wengi katika wale tuliowaumba, kwa utukufu ulio mkubwa(kabisa)(17:70)

Hivyo, kimantiki ni lazima mwanaadamu aulizwe juu ya neema alizotunukiwa katika kuendea lengo. Mwenyezi Mungu(s.w) anasisitiza:

﴿١٠٢﴾ ثُمَّ لَتَسْأَلُنَّ يَوْمَئِذٍ عَنِ النَّعِيمِ

Kisha kwa hakika mtaulizwa (siku hiyo) juu ya neema (mlizitumiaje)(102;8)

### **(ii) Mfumo au njia sahihi ya maisha ibainishwe.**

Katika maisha ya dunia tunaona kuna njia za maisha au dini nyingi zinazofuatwa na watu na kila mfuasi wa dini hizo au njia hizo za maisha anadai kuwa njia yake ndiyo sahihi inayoweza kumnawirisha mwanaadamu na kumfanya aishi kwa usalama na amani. Lakini ukweli uko pale pale kwamba njia sahihi ya maisha itakayomnawirisha mwanaadamu na kumuwezesha kuishi kwa furaha na amani hapa ulimwenguni ni lazima iwe ni moja tu. Kimantiki hatuna budi kukubali kuwa njia ya maisha iliyo sahihi ni lazima iwe moja tu kwa sababu wanaadamu ni jamii moja yenye lengo moja la maisha na wenye usawa katika kuhitajia mahitaji muhimu yanayowafanya waishi kwa furaha na amani. Hivyo hapana budi utaratibu wa kuyaendea maisha uwe ni mmoja. Lakini ni njia ipi hiyo ya maisha itakayomuwezesha mwanaadamu kuishi kwa furaha na amani? Hapa ndipo wanaadamu walipotofautiana kwa kiasi kikubwa.

Kimantiki njia hii ni lazima ifundishwe au ielekezwe na Muumba wa wanaadamu. Hivi ndivyo hasa alivyofanya Muumba kwa kuleta Mitume na vitabu vya kuelekeza njia hiyo. Lakini pamoja na kuletewa mwongozo kwa njia ya Mitume na vitabu, bado wanaadamu wamepewa uhuru wa kufuata mwongozo huu wakiamua kufanya hivo au kuukanusha na kufuata miongozo mingine waliyoiunda wao wenyewe. Wale watakaoamua kufuata mwongozo wa Mwenyezi Mungu(s.w) watakuwa na kila haki ya kudai kuwa wao ndio wenye kufuata njia sahihi ya maisha. Lakini pia wale waliompinga Mwenyezi Mungu, Mitume wake na Vitabu vyake, wataona kuwa njia za maisha zilizoundwa kulingana na miongozo yao waliyoitoa wenyewe ndizo sahihi kuliko njia zote.

Hivyo ni lazima iwepo siku ya mwisho ili ibainike dini au njia sahihi ya maisha kama inayosisitiza katika Qur'an:

لِيَبَيِّنَ لَهُمُ الَّذِي حَتَّوْا فِيهِ وَيَعْلَمَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنَّهُمْ كَانُوا كَذِبِينَ ﴿١٦﴾

*(Atawafufua) ili kuwabainishia yale waliyokhitilafiana na ili wajue waliokufuru ya kwamba wao walikuwa ni waongo” (16:39).*

### ***(iii) Ubainike ukweli kwa waliozuliwa uovu***

Pamoja na ulazima wa kubainishwa tofauti kati ya njia za maisha, pia kuna ulaizima wa kuwa na siku ya kubainishwa haki kati ya watu binafsi au vikundi vya watu. Mtu binafsi au kikundi cha watu waweza kusingiziwa jambo na pakatolewa ushahidi wa uwongo kwa maslahi ya mtu au kikundi fulani mpaka ikawa vigumu kwa walimwengu kuona ukweli kinyume na shutuma. Inawezekana hao walisingiziwa jambo hilo wakaadhibiwa au wakaaibika na kufedheheka na wakawa hawana la kufanya bali wakabakia kusunoneka tu, kisha mwisho wa maisha ya watu hawa waliosingiziwa, iwe ni kuoza na kuwa vumbi? Hapana. Akili haikubali hivyo. Ni lazima pawe na siku ambayo ukweli utabainishwa na mjuzi wa mambo yote. Ndio maana tunaposingiziwa jambo tunamtupia Mwenyezi Mungu kwa viapo tukiwa na uhakika kabisa kuwa kuna siku tutakuwa mbele yake atatuamua kwa uadilifu.

### ***(iv) Walipwe mema wale waliotenda mema bila ya ujira stahiki hapa duniani***

Kutokana na maumbile ya mwanaadamu kila jambo jema alilolifanya hutaraji kupata malipo. Lakini pamoja na ukweli huu tunafahamu pia kuwa si kila wema tunaofanya unalipika. Kuna mengi mema tunayofanya lakini hatutarajii kupata malipo yoyote hapa duniani na tukilazimisha malipo ya wema huo tuliufanya tunapata malipo duni sana yasiyolingana kabisa na thamani ya wema tuliufanya. Mifano katika maisha ya kila siku iko mingi. Hebu kadiria, ni malipo gani anayostahiki kupata mama kutoka kwa manawe kwa kazi ya kumlea tokea kwenye tumbo la uzazi hadi kufikia kujitegemea. Nani atakaye mlipa yule

anayeokoa maisha ya watu kwa kuondoa kitu cha hatari kilichotegwa katika barabara mbugani pasipo na mtu yeyote? Atalipwa wapi yule aliyejitoa muhanga mali yake na nafsi yake kwa manufaa ya jamii? Atalipwa wapi yule aliyejitoa muhanga maisha yake kwa ajili ya kupigania haki za wengine? Kimantiki ni lazima pawe na siku ya malipo ili walipwe ujira wao wale wote waliofanya mema hapa duniani bila ya kupata malipo stahiki ya wema waliotenda. Allah(s.w) anasisitiza:

هَلْ جَزَاءُ الْإِحْسَنِ إِلَّا الْإِحْسَانُ ﴿٦٠﴾

*Hakuna malipo ya ihsani ila kulipa ihsani(vile vile).(55:60)*

Hapa ndipo hutofautiana matendo ya mwenye kuamini siku ya malipo na wenye kukanusha siku ya malipo. Wenye kukanusha siku ya malipo watataka wahakikishiwe kupata malipo kwa njia moja au nyigine kwa kila jema wanalolifanya hapa hapa duniani. Hawatoi msaada wowote au kutenda wema wowote mpaka kwanza wapige darubini na kuona ni jinsi gani watakvoweza kupata malipo yao kwa mali au hali. Kama hakuna uwezekano wowote wa kupata malipo hawawezi kutoa msaada huo. Kinyume chake watu wanaotaraji malipo katika maisha ya akhera, hufanya kila jambo kwa kutaraji malipo ambayo ni bora na ya kudumu ukilinganisha na malipo ya hapa duniani ambayo ni duni mno na yenye kuisha kwa muda mfupi. Kwa matarajio ya malipo ya akhera utawakuta waumini wanatenda wema kwa ajili ya wema tu bila ya kuchoka au kukata tamaa.

**(v) Waovu na wababe wapate adhabu stahiki ya makosa yao**

Katika kawaida ya maisha ya kila siku, kila anaye kosa hupewa adhabu moja au nyingine ili iwe fidia ya matendo yake maovu. Lakini pia inatokea katika maisha ya kila siku kuwa kuna wale wanaofanya maovu kwa siri bila kujulikana. Mara nyingi watu huiba au huzini bila kujulikana. Wezi na wazinzi hawa wanalionekana wanalipata adhabu kali hata ile ya kupoteza maisha yao au sehemu ya miili yao. Sasa watapata wapi adhabu hii waliyoikwepa hapa duniani kwa ujanja? Kimantiki siku ya hukumu ambapo waovu hawa watahukumiwa na kuadhibiwa inavyostahiki lazima iwepo.

Pia katika maisha ya kila siku tunaona watu wenye nguvu au madaraka wakitenda maovu wazi wazi bila ya kuwa na mtu wa kuwahukumu na kuwaadhibu. Mara nyingi hawa, hasa wafalme, huwa juu ya sheria na kila walifanyalo hata likiwa ovi kiasi gani hufanywa zuri na hushangiliwa na washabiki wao. Ni mara ngapi watawala huchukua mali ya umma na kufuja kwa kiasi wakitakacho katika kukidhi matashi ya nafsi zao na tamaa zao? Ni mara ngapi watu hawa huwachukua mabinti za watu na hata wake za watu na kuwafisidi bila ya kuulizwa na yeyote? Mtu wa kawaida akifanya haya huadhibiwa vikali. Ni mara

ngapi watawala huzusha hila na kusababisha vifo vya mamiloni ya watu kwa ajili ya ubinafsi wao. Je, wafalme au watawala hawa wanaofisidi katika ardhi kwa utashi wao watapata wapi adhabu stahiki? Hapana! Ni lazima pawe na maisha mengine baada ya maisha haya ya hapa duniani ili wale wote waliofisidi katika ardhi na kukwepa adhabu kwa ujanja wao au kwa madaraka yao au kwa utajiri wao wahukumiwe na Hakimu muadilifu, Mwenye nguvu juu ya kila kitu, Mwenye kujitosheleza kwa kila kitu na Mwenye ujuzi juu ya kitu na wapate adhabu inayolingana na makosa yao.

**(vi) Waliodhulumiwa walipwe haki zao mbele ya Hakimu muadilifu**

Hapana mwanaadamu mwenye akili timamu anayekubali au kuridhika adhulumiwe haki yake hata iwe ndogo kiasi gani. kila anapodhulumiwa hufanya juu chini kwa njia moja au nyingine aipate haki hiyo akipenda ndiyo aitoe au aisamehe. Lakini tunaona katika maisha ya kila siku watu wakidhulumiwa wazi wazi na wasiwe na popote pa kudai haki zao. Tunaona mifano mingi katika historia ya mwanaadamu ambapo mamlaka ya nchi bila ya haki yoyote hudhulumu jasho la baadhi ya wananchi wake kwa visingizio mbalimbali. Firaun na Ufalme wake alinyakua uhuru wa wana-Israil na kuwafanya watumwa wa kuwatumikia Wamisri. Baya zaidi ufalme huu ulilofanya katika kuwadhulumu baadhi ya wananchi wake hawa ni kule kuwaua watoto wao wa kiume na kuwaacha watoto wa kile tu kama Qur'an inavyotukumbusha:

وَإِذْ نَجَّيْنَاكُمْ مِّنْ آلِ فِرْعَوْنَ يَسُومُونَكُمْ سُوءَ الْعَذَابِ يُذَيِّبُونَ  
أَبْنَاءَكُمْ وَيَسْتَحْيُونَ نِسَاءَكُمْ ۗ وَفِي ذَٰلِكُمْ بَلَاءٌ مِّن رَّبِّكُمْ عَظِيمٌ ﴿٤٩﴾

“Na (kumbukeni) Tulipokuokoeni toka kwa watu wa Firauni waliokupeni adhabu mbaya; wakiwachinja watoto wenu wanaume na kuwawacha hai wanawake; na katika hayo (kuokolewa huko) ilipatikana neema kubwa iliyotoka kwa Mola wenu” (2:49).

Hawa watoto wachanga waliokosea nini ufalme wa Firaun hata ikabidi wasistahiki kukosa haki yao ya maisha? Waarabu walikuwa wakiwazika hai watoto wao wa kike kwa kisingizio eti wasije kuwaabisha na kuwavunja heshima. Ni lazima iwepo siku ya hukumu ili watoto hawa wapatiwe haki zao kama Qur'an inavyotukumbusha:

وَإِذَا الْمَوْءُدَةُ سُئِلَتْ ﴿٨١﴾ بِأَيِّ ذَنْبٍ قُتِلَتْ ﴿٨٢﴾

“Na Mtoto mwanamke aliyezikwa hali ya kuwa yu hai atakapoulizwa kwa kosa gani aliuawa” (81:8-9).

## Ushahidi wa Historia Juu ya Ufufuo

Pamoja na hoja hizo zilizotokana na akili zetu na uzoefu wetu wa maisha ya kila siku zilizotuhitishia kutoepukika kwa siku ya malipo, bado Mwenyezi Mungu(s.w) anatuhirishia uhakika na urahisi wa jambo hili kwa kutufahamisha matukio mbalimbali ya historia.

**Kwanza**, Mwenyezi Mungu(s.w) anatufahamisha tukio la kihistoria la mtu aliyefufuka baada ya kufa na kukaa kipindi cha miaka mia moja. Aya ifuatayo inatufahamisha kisa hiki:

أَوْ كَالَّذِي مَرَّ عَلَىٰ قَرْيَةٍ وَهِيَ خَاوِيَةٌ عَلَىٰ عُرُوشِهَا قَالَ أَنَّىٰ يُحْيِي هَٰذِهِ  
 اللَّهُ بَعْدَ مَوْتِهَا ۗ فَأَمَاتَهُ اللَّهُ مِائَةً عَامٍ ثُمَّ بَعَثَهُ ۗ قَالَ كَمْ لَبِثْتَ ۗ قَالَ  
 لَبِثْتُ يَوْمًا أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ ۗ قَالَ بَلْ لَبِثْتَ مِائَةً عَامٍ فَأَنْظِرْ إِلَىٰ طَعَامِكَ  
 وَشَرَابِكَ لَمْ يَتَسَنَّهْ ۗ وَأَنْظِرْ إِلَىٰ حِمَارِكَ وَلِنَجْعَلَكَ ءَايَةً لِلنَّاسِ ۗ  
 وَأَنْظِرْ إِلَىٰ الْعِظَامِ كَيْفَ نُنشِزُهَا ثُمَّ نَكْسُوهَا لَحْمًا ۗ فَلَمَّا تَبَيَّنَ  
 لَهُ قَالَ أَعْلَمُ أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٥١﴾

“Au kama yule aliyepita karibu na mji uliokuwa umekufa akasema: “Mwenyezi Mungu atauhuisha vipi (mji) huu (na watu wake) baada ya kufa kwake”? basi Mwenyezi Mungu alimfisha kwa miaka mia kisha akamfufua akamuuliza “umekaa muda gani”? Akasema: “Nimekaa muda wa siku moja au sehemu ya siku”. (Mwenyezi Mungu) akasema: Bali umekaa miaka mia; nawe tazama chakula chako na vinywaji vyako, havikuharibika. Na mtazame punda wako (amekuwa mifupa mitupu iliyolika lika) Na ili tukufanye uwe hoja kwa watu (ndio tumekufufua hivi). Na itazame mifupa ya punda wako jinsi tunavyoinyanyua, kisha tunaivisha nyama”. Basi yalipombainikia (haya yule aliyefufuliwa) alinena: “Na juwa kwamba Mwenyezi Mungu ni mwenye uwezo juu ya kila kitu” (2:259).

**Pili**, katika Qur’an tunapata tukio lingine la kihistoria linaloonesha jinsi ufufuo ulivyo jambo jepesi kwa Mwenyezi Mungu(s.w). Mfano huu ni ule wa kufufuliwa ndege wanne wa Nabii Ibrahim(a.s) kama tunavyofahamishwa katika aya ifuatayo:

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ أَرِنِي كَيْفَ تُحْيِي الْمَوْتَىٰ قَالَ أُولَٰئِم تُؤْمِن ۗ قَالَ  
 بَلَىٰ وَلَٰكِن لِّيَطْمَئِنَّ قَلْبِي ۗ قَالَ فَخُذْ أَرْبَعَةً مِّنَ الطَّيْرِ فَصُرْهُنَّ إِلَيْكَ ثُمَّ  
 أَجْعَلْ عَلَىٰ كُلِّ جَبَلٍ مِّنْهُنَّ جُزْءًا ثُمَّ ادْعُهُنَّ يَأْتِينَكَ سَعْيًا ۗ وَاعْلَمْ أَنَّ  
 اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٦٦﴾

“Na (kumbuka) Ibrahim aliposema: Mola wangu: Nionyeshe jinsi utakavyofufua watu” (Mwenyezi Mungu) akasema: “Huamini”? Akasema: “La (Naamini), lakini (nataka kuona hayo) ili moyo wangu utulie (zaidi)”. Akasema: “Basi chukua ndege wanne na uwaozeshe kwako kisha (wadhibiti vizuri sura zao hata wasikupotee popote unapowaona), kisha (wachinje) uweke juu ya kila jabali sehemu katika wao. Kisha wete, watakuja mbio. Na ujue ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, na mwenye hikima” (2:260).

**Tatu**, katika Qur’an pia tunafahamishwa kisa cha vijana wa pangoni ambao Mwenyezi Mungu(s.w) aliwalaza kwa kipindi cha miaka 309 ndipo akawaamsha ili wawe ni ushahidi wa kufufuliwa watu baada ya kufa:

إِذْ أَوْىءَ الْفِتْيَةُ إِلَى الْكَهْفِ فَقَالُوا رَبَّنَا آتِنَا مِن لَّدُنكَ رَحْمَةً وَهَيِّئْ لَنَا مِنْ  
 أَمْرِنَا رَشَدًا ﴿٦٧﴾ فَضَرَبْنَا عَلَىٰ آذَانِهِمْ فِي الْكَهْفِ سِنِينَ عَدَدًا ﴿٦٨﴾

“Vijana hao walipokimbilia katika pango na wakasema: “Mola wetu; tupe rehema zinazotoka Kwako na Tutengenezee uwongofu katika (kila) jambo letu”. “Tukaziba masikio yao (wakalala hawasikii habari yoyote) katika pango hiyo kwa idadi ya miaka mingi” (18:10-11).

وَلَبِثُوا فِي كَهْفِهِمْ ثَلَاثَ مِائَةٍ سِنِينَ ۖ وَازْدَادُوا تِسْعًا ﴿٦٩﴾

“Na walikaa katika Pango yao miaka mia tatu, nawakazidisha (miaka tisa)”. (18:25).

**Nne**, kufufuka watu wa Nabii Musa (a.s) baada ya kufishwa kwa muda walipodai kumuona Mwenyezi Mungu(s.w) ana kwa ana kama tunavyofahamishwa katika Qur’an:

وَإِذْ قُلْتُمْ يَا مُوسَىٰ لَنْ نُؤْمِنَ لَكَ حَتَّىٰ نَرَى اللَّهَ جَهْرَةً فَأَخَذَتْكُمُ الصَّاعِقَةُ  
 وَأَنْتُمْ تَنْظُرُونَ ﴿٧٠﴾ ثُمَّ بَعَثْنَاكَ مِنْ بَعْدِ مَوْتِكَ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٧١﴾

“Na (kumbukeni habari hii pia:) Mliposema: Ewe Musa! Hatutakuamini mpaka tumwone Mwenyezi Mungu wazi wazi” Yakakunyakueni mauti ya ghafla na hali mnaona. Kisha tukakufufueni baada ya kufa kwenu, ili mpate kushukuru (2:55-56).

**Tano**, kufufuka yule Myahudi aliyeliwa kwa dhulma na kumtaja muuaji wake kama inavyobainishwa katika Qur’an:

وَإِذْ قَتَلْتُمْ نَفْسًا فَادَّارَأْتُمْ فِيهَا ۗ وَاللَّهُ حَرِجٌ مَّا كُنْتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿٧٢﴾ فُكُلْنَا  
أَصْرِيئِهِ بِبَعْضِهَا ۗ كَذَلِكَ يُحْيِي اللَّهُ الْمَوْتَىٰ وَيُرِيكُمْ ءَايَاتِهِ لَعَلَّكُمْ  
تَعْقِلُونَ ﴿٧٣﴾

“Na (kumbukeni khabari hii inayotajwa sasa hivi) Mlipoiua nafsi, kisha mkakhitilafiana kwa hayo; (wengine wanasema kauawa na fulani na wengine wanasema fulani mwingine). Na Mwenyezi Mungu ni mtoaji wa hayo mliyokuwa mkiyaficha (Basi akayatoa akajulikana huyo aliyemwua)”.Tukasema: “Mpigeni kwa baadhi ya (sehemu) yake (huyo ng’ombe) Ndiyvo hivi Mwenyezi Mungu huwahuisha wafu, na anakuonyesheni dalili zake ili mpate kufahamu” (2:72-73).

**Sita**, Nabii Isa (a.s) kwa idhini ya Mwenyezi Mungu(s.w) aliweza kufufua wafu waliokufa miaka mingi iliyopita ikiwa ni miongoni mwa dalili za utume wake kama tunavyofjifunza katika Qur’an:

وَرَسُولًا إِلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ أَنِّي قَدْ جِئْتُكُمْ بِآيَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ ۗ أَنِّي أَخْلُقُ لَكُمْ  
مِّنَ الطَّيْرِ كَهَيْئَةِ الطَّيْرِ فَأَنْفُخُ فِيهِ فَيَكُونُ طَيْرًا بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ وَأُبْرِئُ الْأَكْمَهَ  
وَالْأَبْرَصَ ۗ وَأُحْيِي الْمَوْتَىٰ بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ وَأُنَبِّئُكُمْ بِمَا تَأْكُلُونَ وَمَا تَدَّخِرُونَ فِي  
بُيُوتِكُمْ ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَةً لِّكُمْ ۖ إِن كُنْتُمْ مُّؤْمِنِينَ ﴿٢١﴾

“Na (atamfanya) Mtume kwa wana wa Israili, (kuwaambia); “Nimekujieni na hoja kutoka kwa Mola wenu, ya kwamba nakuumbieni katika udongo kama sura ya ndege, kisha nampuliza, mara anakuwa ndege, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na ninawaponesha vipofu na wenye mabalanga, na ninawafufua (baadhi ya) waliokufa, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na nitakwambieni mtakavyovila na matakavyoweka akiba katika nyumba zenu. Bila shaka katika haya imo hoja kwenu ikiwa nyingi ni watu wa kuamini” (3:49).

## Ushahidi wa Ufufuo Utokanao na Maisha ya kila Siku

Pia Mwenyezi Mungu(s.w) anatupa mifano kadhaa inayotokana na maisha yetu ya kila siku inayotutanabaihisisha juu ya uhakika wa ufufuo. Hapa tutataja mifano **mitatu** ambayo ni dhahiri mno katika maisha yetu ya kila siku.

**Kwanza**, Mwenyezi Mungu(s.w) anatupigia mfano wa kufa kwa mimea katika ardhi wakati wa kiangazi na kufufuka kwake baada ya mvua kunyesha:

وَمِنْ آيَاتِهِمْ أَنْكَ تَرَى الْأَرْضَ خَاشِعَةً فَإِذَا أَنْزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَاءَ اهْتَزَّتْ

وَرَبَّتْ إِنَّ الَّذِي أَحْيَاهَا لَمُحْيٍ الْمَوْتَى إِنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٤١﴾

*Na katika ishara zake (kuwa yuko Mwenyezi Mungu) ni kwamba unaona ardhi imedhalilika (kwa kukosa mvua) lakini tunapoiteremshia maji mara unaiona inataharaki na kuumuka; bila shaka aliyeihuiisha ndiye atakayehuiisha waliokufa. Hakika yeye ndiye mwenye uweza juu ya kila kitu” (41:39).*

Mfano huu wa kuhuishwa kwa mimea katika maisha yetu ya kila siku unadhihirika wakati wa kiangazi ardhi inapokuwa katika hali ya vumbi vumbi na mimea iliyokauka na kukatika katika. Lakini mara tu baada ya mvua kunyesha mimea mizuri ya kijani kibichi huchipuka tena. Pia mara hiyo hiyo hutokea wadudu wengi ambao hawakuwepo wakati wa kiangazi. Je, huyu mwenye uwezo wa kufufua ardhi baada ya kufa kwake hana uwezo wa kumfufua mwanaadamu baada ya kufa kwake?

**Pili**, Mwenyezi Mungu(s.w) anatupa mfano mwingine wa usingizi. Mtu akiwa amelala hajitambui kabisa na hana habari na lolote linalotendeka. Mara nyingine katika hali hiyo ya kulala mtu husafiri masafa ya mbali na hushiriki katika matendo mbalimbali kwa njia ya ndoto. Katika hali ya usingizi moyo wa mtu unakuwa katika hali ya furaha iwapo ataota ndoto nzuri na iwapo ataota ndoto mbaya moyo wake huwa katika hali ya huzuni na khofu. Ni mara ngapi tumewasikia watu wakicheka huku wamo usingizini na mara ngapi pia tumewaona watu wakiamka ghafla kutoka usingizini huku wanatetemeka. Sote tunafahamu usingizi na tunafahamu ndoto.

Je, ukizingatia kulala usingizi na kuamka si mfano halisi wa kufa na kufufuliwa? Anaye kulaza usingizini na kukuotesha ndoto mbalimbali na hatimaye kukuamsha, si muweza wa kukufisha na kukufufua? Je, unayo chembe ya mamlaka juu ya usingizi wako?

وَجَعَلْنَا نَوْمَكُمْ سُبَاتًا ﴿٧٨﴾ وَجَعَلْنَا اللَّيْلَ لِبَاسًا ﴿٧٩﴾ وَجَعَلْنَا النَّهَارَ مَعَاشًا ﴿٨٠﴾

*Na tukaufanya usingizi wenu kama kufa. Na tukaufanya usiku kama nguo (mna lofunikwa) na tukaufanya mchana kama kufufuka (78:9-11).*



**Tatu**, kuzimia na kuzinduka ni ushahidi mwingine wa ufufuo. Mtu aliyezimia hana tofauti kubwa na mtu aliyekufa kwani haji tambui wala hajiwezi kwa lolote, na anapozindukana hajui lolote lililoendelea katika kipindi cha kuzimia kwake. Qur'an inatukumbusha juu ya kuzimia kwa Nabii Musa (a.s) pale alipotaka kumuona Mwenyezi Mungu(s.a.w).

وَلَمَّا جَاءَ مُوسَىٰ لِمِيقَاتِنَا وَكَلَّمَهُ رَبُّهُ قَالَ رَبِّ أَرِنِي إِلَيْكَ ۚ قَالَ  
لَنْ تَرِنِي وَلَكِنِ أَنْظِرْ إِلَى الْجَبَلِ فَإِنِ اسْتَقَرَّ مَكَانَهُ فَسَوْفَ تَرِنِي ۚ  
فَلَمَّا تَجَلَّىٰ رَبُّهُ لِلْجَبَلِ جَعَلَهُ دَكًّا وَخَرَّ مُوسَىٰ صَعِقًا ۚ فَلَمَّا أَفَاقَ  
قَالَ سُبْحٰنَكَ تُبْتُ إِلَيْكَ وَأَنَا أَوَّلُ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٤٣﴾

*Na alipofika Musa katika miadi yetu, na Mola wake akazungumza naye, (Musa) alisema: “Mola wangu nioneshe (nafsi yako) ili nikuone”. Akasema (Mwenyezi Mungu); “Hutaniona, lakini tazama jabali (lililo mbele yako) kama litakaa mahali pake (bila kupasuka na kutawanyika) utaweza kuniona. “Basi Mola wake alipojionesha katika jabali (alipoonyesha baadhi ya ishara zake) alilifanya ni lenye kuvunjika vunjika; na Musa akaanguka hali ya kuzimia. Alipozindukana alisema: “(Naitakidi kuwa) wewe ndiyo mtukufu, (haliyumkiniki hilo nililolitaka). Natubu kwako, na mimi ni wa kwanza wa wanaoamini (haya) (7:143).*

Mifano hii iliyotolewa katika Qur'an inatuondolea chembe ya shaka juu ya ufufuo. Kazi hiyo ya kufufua wafu ni nyepesi mno kwa Mwenyezi Mungu(s.w):

إِنَّمَا قَوْلُنَا لِشَيْءٍ إِذَا أَرَدْنَاهُ أَنْ نَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٤٤﴾

*Kauli Yetu kwa kitu tunachotaka (kiwe) ni kukiambia “kuwa”, basi kinakua tu (16:40).*

Ni wale tu wenye shaka juu ya kuwepo Mwenyezi Mungu(s.w) na sifa zake ndio watakao kuwa na shaka na ufufuo na maisha ya Akhera. Vinginevyo kila mwenye uhuru wa mawazo na fikra, atakiri kuwepo siku ya malipo na atajiandaa vyema kwa siku hiyo.

## **Mazingira ya Siku ya Mwisho kwa Mujibu wa Qur'an na Hadith**

Baada ya kupitia hoja madhubuti zinazoonesha ulazima au kutoepukika kuwepo siku ya malipo (maisha ya Akhera), la muhimu linalofuatia ni kujua sura halisi ya maisha hayo ili kumuwezesha kila muumini kupata hisia za hakika na picha kamili ya maisha ya Akhera. Kupata picha kamili ya maisha yajayo ni

silaha kubwa ya kumuhimiza mja kuishi kulingana na lengo la kuumbwa kwake. Kuishi kulingana na lengo la kuumbwa ndiyo njia pekee inayompelekea mja kupata radhi za Mwenyezi Mungu(s.w) na kupata maisha ya furaha ya milele huko akhera na ndiyo njia pekee ya kuepukana na ghadhabu za Mwenyezi Mungu(s.w) na adhabu kali isiyo na mfano huko akhera. Ili kupata picha kamili ya maisha ya akhera, katika kitabu hiki tumegawanya maisha ya kahera katika hatua sita zifuatazo:

- (i) Kufikwa na mauti
- (ii) Kipindi cha Barazakh (Kaburini)
- (iii) Kufufuka na kukusanyika kwenye uwanja wa Hisabu
- (iv) Siku ya Hukumu
- (v) Makazi ya Peponi
- (vi) Makazi ya Motoni

### **(i) Kufikwa na mauti**

Umauti ni hatua ya kutengana roho na mwili ambapo roho hubaki hai mpaka siku ya mwisho na mwili husambaratika kaburini au penginepo kulingana na aina ya kifo.

أَيَّمَا تَكُونُوا يُدْرِكُكُمُ الْمَوْتُ وَلَوْ كُنْتُمْ فِي بُرُوجٍ مُّشِيدَةٍ ..... ﴿٧٨﴾

“Popote mlipo mauti yatakufikeni, na hata mkiwa katika ngome madhubuti.....” (4:78).

Kifo ni kitendo kinachomhuzunisha kila mtu lakini hakuna yeyote anayeweza kuizuia roho isitengane na mwili wake wakati unapofika. Hebu turejee Qur’an inavyotutanabaisha:

فَلَوْلَا إِذَا بَلَغَتِ الْحُلُقُومَ ﴿٨٦﴾ وَأَنْتُمْ حِينِيذٍ تَنْظُرُونَ ﴿٨٧﴾ وَحَنْ أَقْرَبُ

إِلَيْهِ مِنْكُمْ وَلَيْكِن لَّا تُبْصِرُونَ ﴿٨٨﴾ فَلَوْلَا إِنْ كُنْتُمْ غَيْرَ مَدِينِينَ ﴿٨٩﴾

تَرْجِعُونَهَا إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٩٠﴾

“Basi mbona (Roho) ifikapo kooni na nyinyi wakati ule mwatazama nasi tunakaribiana naye zaidi (huyo anayetoka roho) kuliko nyinyi, wala nyinyi hamuoni. Kama nyinyi hammo katika mamlaka (yangu) kwa nini hamuirudishi (hiyo roho) ikiwa mnasema kweli” (56:83-87).

**Anahisi nini mwenye kufikwa na mauti**

Katika Qur'an tunafahamishwa kuwa muda mfupi kabla ya kutokwa na roho kuna hisia mbili tofauti, hisia za watu waovu na hisia za watu wema (waumini). Watu wema hupewa bishara njema na huliwazwa na Malaika. Hivyo hufurahia kufa ili wakapate malipo ya peponi kama tunavyojifunza katika Qur'an:

يَتَأْتِيهَا النَّفْسُ الْمَطْمَئِنَّةُ ﴿٧٧﴾ أَرْجِعِي إِلَىٰ رَبِّكِ رَاضِيَةً مَّرْضِيَةً ﴿٧٨﴾  
فَادْخُلِي فِي عِبَادِي ﴿٧٩﴾ وَاَدْخُلِي جَنَّتِي ﴿٨٠﴾

*Ewe nafsi yenye kutua! Rudi kwa Mola wako, hali ya kuwa utaridhika (kwa utakayoyapata) na Mwenyezi Mungu aridhike na wewe. Basi ingia katika (kundi la) waja wangu (wema). Uingie katika pepo yangu” (89:27-30).*

**Hawa roho zao hutolewa kwa upole.**

وَالنَّشِيطَاتِ نَشَاطًا ﴿٨١﴾

*“Na kwa wale(malaika) wanaotoa (roho za watu wema) kwa ulatifu (taratibu)” (79:2).*

Watu waovu kabla ya kutolewa roho huoneshwa yale maovu waliyojitangulizia na adhabu ya Mwenyezi Mungu inayowangojea. Kisha watakuja Malaika wa kuwasimanga na kuwatisha. Hivyo hawatapenda kufa bali watatamani kuongezwa muda kidogo ili wapate kufanya wema ili kusalimika na adhabu kali ya Mwenyezi Mungu(s.w) iliyo mbele yao kama tunavyokumbushwa katika Qur'an:

وَوُجُوهُ يَوْمَئِذٍ بِآسِرَةٍ ﴿٨٢﴾ تَنْظُرُونَ أَن يُفْعَلَٰ بِهَا فَاغْرَةٌ ﴿٨٣﴾ كَلَّا إِذَا بَلَغَتِ  
التَّرَاقِيَ ﴿٨٤﴾ وَقِيلَٰ لَهَا مِن رَّاٰقٍ ﴿٨٥﴾ وَظَنَّ أَنَّهُ الْفِرَاقُ ﴿٨٦﴾ وَالتَّتَفَتِ الْأَسَاقُ  
بِالْأَسَاقِ ﴿٨٧﴾ إِلَىٰ رَبِّكَ يَوْمَئِذٍ الْمَسَاقُ ﴿٨٨﴾ فَلَا صَدَقَ وَلَا صَلَّىٰ ﴿٨٩﴾  
وَلٰكِن كَذَّبَ وَتَوَلَّىٰ ﴿٩٠﴾ ثُمَّ ذَهَبَ إِلَىٰ أَهْلِهِ يَتَمَطَّىٰ ﴿٩١﴾ أَوْلَىٰ لَكَ فَأَوْلَىٰ  
﴿٩٢﴾ ثُمَّ أَوْلَىٰ لَكَ فَأَوْلَىٰ ﴿٩٣﴾

*Na nyuso (nyingine) siku hiyo zitakunjana. Zitajua ya kuwa zitafikiwa na msiba uvunjao uti wa mgongo. Sivyo (hivi mnavyofanya)! (Roho) itakafikiwa katika mitulinga (mifupa ya mabegani) Na kukasemwa: “Ni nani wa kumponesha mgonjwa huyu”? Na mwenyewe akajua kwa hakika kuwa hiyo ni (saa ya) kufariki (dunia). Na utakapoambatanishwa muundi kwa muundi Siku hiyo ni*

*kuchungwa(tu) kupelekwa kwa Mola wako. Hakusadiki wala hakusali. Bali alikadhibisha na akarudi nyuma. Kisha alikwenda kwa watu wake, na huku akiringa. (Ataambiwa): “Imekwisha kukufika (adhabu ya Mwenyezi Mungu) imekwisha kukufika” (75:24-35).*

Kwa kuwa watu waovu hawatapenda kufa, itabidi roho zao zitolewe kwa nguvu kama tunavyojifunza katika Qur'an:

وَالنَّزِعَاتِ غَرْقًا ﴿١١﴾

“Naapa kwa wale (malaika) wavutao kwa nguvu (roho za watu wabaya)” (79:1).

Hisia za wenye kufikwa na mauti pia zinabainishwa katika Hadith ifuatayo:

*Ubaidah bin Samit (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Yeyote yule anayetaka kukutana na Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu anapenda kukutana naye, na yeyote asiyetaka kukutana na Mwenyezi Mungu, pia Mwenyezi Mungu hana haja ya kukutana naye. Aysha au baadhi ya wake za Mtume walisema; “Hakika (ni kweli) hatupendi kifo”. Alijibu (Mtume): “Sio hivyo, bali wakati kifo kinapomjia muumini, anapewa habari njema juu ya Ridhaa ya Mwenyezi Mungu na neema zake”. Baada ya habari hii hatakuwa na kitu chochote atakachokipenda zaidi kuliko kifo (kinachomkaribia). Kwa hiyo anataka kukutana Mwenyezi Mungu(s.w) na Mwenyezi Mungu(s.w) Naye atataka kukutana naye. Na asiye muumini, kifo kinapomkaribia anapewa habari mbaya juu ya adhabu kali ya Mwenyezi Mungu(s.w). Na hapatakuwa na kitu kisichopendeza mbele yake kuliko hicho kifo kinacho mngoja mbele yake. Kwa hiyo hataki kukutana na Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu hapendi kukutana naye” (Bukhari na Muslim).*

## (ii) Maisha ya Kaburini (Barzakh)

Maisha ya kaburini ni kile kipindi anachokaa mtu baada ya kufa kwake mpaka kufufuliwa kwake. Kipindi kati ya parapanda la kwanza ambalo ni amri ya kufa viumbe vyote na parapanda la pili ambalo ni amri ya kufufuliwa viumbe vyote vitakavyotakiwa vifufuke, huitwa barzakh. Tunajulishwa juu ya Barzakh katika aya ifuatayo:

حَتَّىٰ إِذَا جَاءَ أَحَدَهُمُ الْمَوْتُ قَالَ رَبِّ ارْجِعُونِ ﴿٢٠﴾ لَعَلِّي أَعْمَلُ

صَلِحًا فِيمَا تَرَكْتُ كَلَّا إِنَّهَا كَلِمَةٌ هُوَ قَائِلُهَا وَمِن وَرَائِهِم بَرْزَخٌ إِلَىٰ

يَوْمٍ يُبْعَثُونَ ﴿٢١﴾

*Hata yanapomfikia mmoja wao mauti, husema: “Mola wangu! Nirudishe (ulimwenguni)” Ili nifanye mema sasa badala ya yale niliyoyaacha”. Hujibiwa na Malaika akaambiwa: “Hapana” Hakika hili ni neno tu analolisema yeye (aliye mwovu anapofikiwa na mauti); na mbele yao kuna maisha ya **Barzakh** (ya baada ya kufa) mpaka siku watakapofufuliwa” (23:99-100).*

Katika kipindi hiki cha maisha ya Barzakh ni mambo gani yanayoendelea katika nafsi ya mwenye kufa? Wengi kwa kujiliwaza katika wakati huo hufikiria kuwa watu wanakuwa mapumzikoni. Na watu wale wasioamini siku ya mwisho huamini kuwa kifo ndio mwisho wa maisha ya watu na iliyobakia ni kuoza na kuwa chumvi chumvi zitakazotumika ardhini.

Katika kipindi cha Barzakh roho za watu wema zitakaa mahali pazuri kungojea malipo yao ya peponi, na zile za watu waovu zitakuwa mahabusu, zikingojea siku ya hukumu yao. Hivi ndivyo tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Abu Hurairah(r.a) amesimulia kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ambaye alisema: “Hakika maiti hupelekwa kaburini na hukaa kaburini bila ya hofu wala fadhaa. Baada ya hapo ataambiwa:”Ulikuwa katika nini? Atajibu: “Nilikuwa katika Uislamu”. Kisha ataulizwa: “Huyu ni nani? Atajibu” “Muhammad, Mtume wa Mwenyezi Mungu. Alitujia na hoja zilizo wazi kutoka kwa Mwenyezi Mungu(s.w) na kwa hiyo tulimuamini. Ataulizwa tena: “Umemuona Mwenyezi Mungu? Atajibu: “Si katika uwezo wa yeyote kumuona Mwenyezi Mungu. Kisha patawekwa uwazi utakaomuwezesha kuona moto unaofoka. Ataambiwa Angalia kile ambacho Mwenyezi Mungu amekuokoa (amekukinga) nacho. Kisha patawekwa uwazi utakaomuwezesha kuona pepo na vile vile vilivyomo ndani yake. Ataambiwa: Hii ni sehemu yako kutokana na uthibiti wa imani uliyoishi nayo na ukafa nayo na ambayo utafufuliwa nayo, Insha Allah. Mtu muovu, atakaa katika kaburi lake kwa khofu na fadhaa. Ataulizwa: Ulikuwa katika nini? Atajibu: Sijui. Kisha ataulizwa tena: Ni nani huyu? Atajibu: Nilisikia watu wakisema kama ninavyosema. Kisha utawekwa uwazi kwa kumuwezesha kuona pepo ataangalia na kuona uzuri wake na vilivyomo ndani yake. Ataambiwa: Angalia kile ambacho Mwenyezi Mungu amekukosesha (kutokana na imani yako mbovu). Kisha utawekwa uwazi wa kumuwezesha kuona moto. Ataambiwa: Hii ndio sehemu yako ambayo uliendesha maisha yako kwa kuwa na mashaka nayo, na umekufa ukiwa na mashaka nayo na utafufuliwa katika hali hiyo hiyo, Insha Allah. (Ibn Majah).*

*Aysha(r.a) amesimulia kuwa mwanamke wa Kiyahudi alimuendea na kumsimulia adhabu ya kaburini. Akamwambia; Mwenyezi Mungu akukinge na adhabu ya kaburini. Mtume akajibu; “ndiyo”. Adhabu ya kaburini ni jambo la kweli. Aysha alisema: “Sikumuona Mtume baada ya hapo kuswali swala yoyote bila ya kumuomba Mwenyezi Mungu amkinge na adhabu ya kaburini. (Bukhari na Muslim).*

Bara'a bin 'Azib(r.a) amesimulia kutoka kwa Mtume(s.a.w) aliyesema: "Malaika wawili watamjia (maiti), watamkalisha na kumuuliza: Ni nani Bwana wako? Atajibu: Mwenyezi Mungu ndiye Bwana wangu? Kisha watamuuliza: Ni ipi Dini yako? Atajibu: Dini yangu ni Islam (Uislamu). Kisha watamuuliza: Ni nani huyo ambaye aliletwa kwenu? Atajibu: Alikuwa ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Watamuuliza: Amekuleteeni habari gani? Atajibu: nimesoma kitabu cha Mwenyezi Mungu nikaamini kutokana nacho na nikaithibitisha imani hiyo (katika matendo). Kwa hiyo kuna msemo wake huu: Mwenyezi Mungu huwathibitisha imani hiyo wale walioamini kwa kauli thabiti. (Qur'an 14:27). Mtume akasema: Mtangazaji (mwenye kunadi) atatangaza (atanadi) kutoka mbinguni: Hakika mja wangu amesema ukweli. Mteengeeni sehemu katika pepo na mvisheni mavazi ya peponi. Na mfungulieni mlango wa peponi. Kisha utafunguliwa. Akasema (Mtume): Kisha hewa yake (peponi) na harufu yake nzuri (ya manukato) itamjia na (pepo) itakurubishwa kwake kiasi cha upeo wa macho. Kwa kafiri (asiye amini) (Mtume) alitaja kifo chake na akasema: Roho yake itarudishwa katika kiwili wili chake na Malaika wawili watamjia, watamkalisha na kumuuliza: Ni nani Bwana (Mola) wako? Atajibu: Haa! Haa! Sijui! Watamuuliza tena: Ni nani huyo aliyeletwa kwenu? Atajibu: Haa! Haa! Sijui! Kisha mwenye kunadi atanadi kutoka mbinguni: Hakika amesema uwongo. Kwa hiyo mkunjulieni kitanda cha Motoni. Akasema (Mtume): Kisha joto lake na upepo wa moto utamjia na kaburi lake litakuwa jembamba sana kwake mpaka mbavu zake mbili zibadilishane. Kisha atakabidhiwa kwa Malaika kipofu na kiziwi mwenye pande (rungu) la chuma. Kama mlima ungalipigwa na chuma hicho ungelikuwa vumbi. Atampiga kwa chuma hicho kwa kipigo ambacho kitasikika kwa kila aliye katika mashariki na magharibi isipokuwa viumbe wa aina mbili (majini na watu) hawatasikia. Atakuwa vumbi na kisha roho itarudishwa tena kwake (Ahmad, Abuu Daud).

### (iii) Kufufuka na kukusanyika kwenye uwanja wa hesabu

Watu wote wa mwanzo na wa mwisho watafufuka baada ya kupigwa (baragumu) Parapanda la pili. Kisha watahudhurishwa mbele ya Mwenyezi Mungu(s.w) ili kila mmoja alipwe anachostahiki kwa uadilifu. Hii ndiyo siku ya Kiyama kama inavyobainishwa katika aya zifuatazo:

وَنُفِخَ فِي الصُّورِ فَصَعِقَ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ إِلَّا مَنْ شَاءَ

اللَّهُ ثُمَّ نُفِخَ فِيهِ أُخْرَىٰ فَإِذَا هُمْ قِيَامٌ يَنْظُرُونَ ﴿١٠١﴾

"Na litapigwa baragumu watoke roho watu waliomo mbinguni na waliomo ardhini ila yule amtakaye Mwenyezi Mungu. Tena litapigwa mara nyingine Hapo watafufuka (wote) wawe wanatazamana (nini litatokea)" (39:68).

Pia rejea Qur'an (36:51-54),(80:33-42),(99:1-8).

Aya hizi zinatufahamisha kuwa hali ya maisha hayo itakuwa ni tofauti kabisa na hali ya hapa ulimwenguni. Muelekeo wa watu wote baada ya kufufuliwa utakuwa kwa Mola wao katika uwanja wa Hisabu. Japo katika aya nyingi za Qur'an siku ya kufufuliwa imeunganishwa moja kwa moja na siku ya Hisabu, bado katika Hadith imebainishwa wazi kuwa patapita muda mrefu wa taabu na mashaka kabla ya kufika katika Hisabu. Patakuwa na jua kali na joto kali sana. Ardhi na mbingu vitakuwa shaba kama tunavyofahamishwa katika aya hii. **“Siku mbingu zitakapokuwa kama shaba iliyoyeyuka”** (70:8). Katika hali hii ya joto na jua kali watu watabubujikwa na jasho litakalofurika kama tunavyofahamishwa katika Hadith zifuatazo:

*Abu Hurairah(r.a) amesimulia kuwa Mtume(s.a.w) amesema: Siku ya Kufufuliwa (Siku ya Kiyama) watu watatokwa na jasho kwa kiasi ambacho jasho lao litafurika juu (litakuwa na kina) kiasi cha dhira sabini na litawazamisha watu mpaka kufikia masikioni (Bukhari na Muslim).*

Mbubujiko na mafuriko haya ya jasho yatategemeana na matendo waliyoyatanguliza waja, kama tunavyopata ufafanuzi katika Hadith ifuatayo:

*Miqdad(r.a) amesimulia: Nimesikia Mtume(s.a.w) akisema: Siku ya Kiyama jua litashushwa karibu na viumbe kiasi cha umbali wa maili moja. Watu watatokwa na jasho kulingana na matendo yao. Kwa watu wengine jasho litafurika kiasi cha kufikia fundo za miguu, wengine litafika mpaka magotini na katika watu kuna wale watakozamishwa mzamisho mkubwa mpaka (akiashiria mdomoni kwake kwa mkono wake) (Muslim).*

Kila mmoja siku hiyo atahakikisha kuwa siku aliyoahidi Mwenyezi Mungu na kukariri mara nyingi katika ujumbe wake, ndio hiyo iliyowadia na hapana popote pa kukimbilia isipokuwa kwa Mola wake. Kila mmoja ataona matendo yake yamehudhurishwa na katika hali hii Qur'an inauliza:

وَمَا أَدْرَاكَ مَا يَوْمَ الدِّينِ ﴿١٧﴾ ثُمَّ مَا أَدْرَاكَ مَا يَوْمَ الدِّينِ ﴿١٨﴾ يَوْمَ  
لَا تَمْلِكُ نَفْسٌ لِّنَفْسٍ شَيْئًا ۗ وَالْأَمْرُ يَوْمَئِذٍ لِلَّهِ ﴿١٩﴾

*“Ni nini kitakachokujulisha siku ya malipo ni siku gani hiyo? Tena nini kitakachojulisha siku ya malipo ni siku gani hiyo? Ni siku ambayo nafsi haitamiliki nafsi (nyingine) chochote, na amri siku hiyo itakuwa ya Mwenyezi Mungu tu” (82:17-19).*

Kwa ujumla kipindi kati ya kufufuliwa na kufikia hisabu, kitakuwa kigumu sana na kila mtu atahisi ugumu wake kwa kiasi ambacho hata Mitume wa Mwenyezi Mungu ambao ni vipenzi vyake wataihisi. Hapana nafsi itakayojiamini kama tunavyofahamishwa katika Hadith ifuatayo:

*Aysha(r.a) amesimulia kuwa alikumbuka moto na akaangua kilio. Mtume wa Mwenyezi Mungu akauliza: Ni kitu gani kinacho kuliza? Nikajibu: Nimekumbuka moto na nikaanza kulia. “Je, utawakumbuka wake zako siku ya Kiyama”? Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: “Sikiliza! Katika sehemu tatu (zifuatazo) hakuna atakayemkumbuka yeyote yule: karibu na mizani mpaka ajue kuwa mizani yake itakuwa nyepesi au nzito; na karibu na kupewa kitabu kilichorikodiwa matendo mpaka atakapoitwa: Njoo, soma kitabu chako na mpaka atakapopewa kitabu chake kwa mkono wa kulia au kushoto au nyuma ya mgongo wake; na karibu na njia nyembamba (Siratwa) itakayowekwa baina ya ncha mbili za moto wa Jahannam” (Abu Daud).*

Hata hivyo, tunafahamishwa katika Hadith kuwa katika hicho kipindi kigumu cha baina ya kufufuliwa na kuhukumiwa, waumini waliotenda mema watawekwa vivulini na kila Mtume atapewa kisima au haudhi ya maji ya kuwanyweshwa watu wa Umma wake walioamini pamoja naye, Mtume(s.a.w) ameahidiwa Kauthar katika Qur'an:

إِنَّا أَعْطَيْنَاكَ الْكَوْثَرَ ﴿١٠٨﴾

“Hakika tumekupa Kauthar (kheri nyingi)” (108:1)

#### (iv) Siku ya Hukumu

Siku ya hukumu ndio siku kuu ambapo ufalme wa Mwenyezi Mungu(s.w) utaonekana kwa kila mtu. Kila mtu atayakinisha kuwa ufalme ni wa Mwenyezi Mungu(s.w) peke yake hata wale waliokanusha hapo awali katika maisha ya dunia. Hata hivyo Mwenyezi Mungu(s.w) atauliza: **“Leo Ufalme ni wa nani?”** Wote watakuwa kimya, halafu atajibu Mwenyewe kama ilivyo katika aya ifuatayo:

يَوْمَ هُمْ بَارِزُونَ لَا يَخْفَىٰ عَلَى اللَّهِ مِنْهُمْ شَيْءٌ ۗ لِمَنِ الْمُلْكُ الْيَوْمَ لِلَّهِ

الْوَحْدِ الْقَهَّارِ ﴿١٠٩﴾

“Siku watakatodhihiri (mbele ya Mwenyezi Mungu), na haitafichikana habari yao yoyote kwa Mwenyezi Mungu. Leo Ufalme ni wa nani? Ni wa Mwenyezi Mungu mmoja, Mwenye Nguvu (za kufanya atakalo)” (40:16).

Hukumu itatolewa katika ardhi iliyotambarare kabisa ambapo viumbe vyote vitahudhurishwa. Malaika wote watasimama katika safu:

يَوْمَ يَقُومُ الرُّوحُ وَالْمَلَائِكَةُ صَفًّا ۗ لَا يَتَكَلَّمُونَ إِلَّا مَنْ أُذِنَ لَهُ

الرَّحْمَنُ وَقَالَ صَوَابًا ﴿١١٠﴾



“Siku ambayo zitasimama roho (za viumbe wote) na Malaika safu safu; hatasema siku hiyo ila yule ambaye (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa Rehema amempa idhini (ya kusema) na atasema yaliyo sawa” (78:38).

Kisha kiti cha Enzi cha Mwenyezi Mungu kitahudhurishwa pale na Nuru ya Mwenyezi Mungu itazagaa kila mahali na kila mmoja atakuwa na uhakika kuwa Mwenyezi Mungu yupo kwa kuchukua Hisabu. Qur'an tukufu inatupa picha ya Siku ya Kiyama kuwa:

وَأَشْرَقَتِ الْأَرْضُ بِنُورِ رَبِّهَا وَوُضِعَ الْكِتَابُ وَجِئَءَ بِالنَّبِيِّينَ وَالشُّهَدَاءِ

وَقُضِيَ بَيْنَهُم بِالْحَقِّ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿١١﴾

“Na ardhi (siku hiyo) itang'ara kwa nuru ya Mola wake, na madaftari (ya vitendo) yatawekwa na wataletwa Manabii na mashahidi na kutahukumiwa baina yao kwa haki wala hawadhulumiwa” (39:69).

Kila mmoja atapita katika hisabu, japo wengine hisabu zao zitakuwa ngumu sana na wengine nyepesi sana. Hebu tuzingatie Hadith ifuatayo:

*Aysha(r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Yeyote atakayehisabiwa (atakaye ulizwa) katika siku ya Hukumu, ataangamia. Nikauliza (Aysha): Je, Mwenyezi Mungu hakusema: “Basi yeye atahisabiwa hisabu nyepesi?” (84:8). Akajibu: Hayo kwa hakika ni maelezo ya ujumla lakini yule ambaye atakaye hesabiwa kila kitu kwa undani wake, ataangamia. (Bukhari na Muslim).*

Pia Hadith ifuatayo inasisitiza juu ya kila mtu kuulizwa na Mwenyezi Mungu.

*Ad bin Haatim(r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Hapana yeyote kati yenu ambaye hataongea na Mola wake. Hapatakuwa na mkalimani yeyote kati ya Mwenyezi Mungu na yeye na hapatakuwa na pazia ya kumzuia Mwenyezi Mungu asionekane. Mja ataangalia kuliani kwake, lakini hataona chochote isipokuwa matendo yake aliyoyatanguliza. Ataangalia mbele yake, lakini hatoona chochote isipokuwa moto unamjia usoni mwake. Kwa hiyo jikinge na moto (kwa kutoa sadaka) angalau (kwa kutoa) kipande cha tende (Bukhari na Muslim).*

Vile vile tunafahamishwa katika Hadith kuwa hapana yeyote atakayetoka kwenye uwanja wa Hisabu bila ya kuulizwa mambo yafuatayo:

1. Ujana wako umeutumiaje?
2. Umri wako umeutumiaje?
3. Mwili wako na vipaji vyako umevitumiaje?

4. Mali yako umeipataje na umeitumiaje?

5. Umeitumiaje elimu yako?

Kila mchungu (kila kiongozi katika ngazi yoyote ile) ataulizwa juu ya uchungaji wake. Mitume ndio watakaokuwa wa kwanza kuulizwa. Mwenyezi Mungu(s.w) atawauliza Mitume:

Ni lipi jibu lenu? Watajibu: Hatuna ujuzi. Hakika Wewe Ndiye mjuzi wa siri (ghaibu). Mitume watapumbaa kwa woga baada ya kuulizwa swali hili. Kisha Mtume Nuhu(a.s) ataitwa na kuulizwa kama tunavyofahamishwa katika Hadith ifuatayo:

*Abuu Sayyid(r:a) amesimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Nuhu (a.s) atahdhurishwa katika siku ya Hukumu, ataulizwa: “Je, umefikisha (ujumbe wangu)? “Ndiyo”atajibu. Kisha wafuasi wake wataulizwa”: Aliwafikishia (ujumbe wangu)? Watajibu: Hapana mwonyaji aliyetujia! Ataulizwa (Nuhu) ni nani mashahidi wako? Atajibu: Muhammad na Umma wake. Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Kisha mtaitwa (mtahudhurishwa) na mtatoa ushahidi kuwa kwa hakika alifikisha ujumbe (wa Mwenyezi Mungu kwa watu wake). Kisha Mtume akasoma (aya ifuatayo): Na vivyo hivyo tumekufanyeni umati bora ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume awe shahidi juu yenu. Na hakukifanya kibla ulichokuwa nacho (mara ya kwanza kuwa ndiyo kibla chako sasa na mpaka mwisho wa Ulimwengu) ila tupate kumjulisha anayegeuka akarejea nyuma. Na Mwenyezi Mungu kwa watu ni mpole sana (na) Mwenye Rehema (2:143) (Bukhari).*

Habari juu ya kuulizwa kwa Nabii Isa (a.s) inatolewa katika Qur'an:

وَإِذْ قَالَ اللَّهُ يَٰعِيسَىٰ ابْنَ مَرْيَمَ ۗ أَنْتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ اتَّخِذُونِي وَأُمِّيَ ٱلنَّهْيَيْنِ  
 مِن دُونِ اللَّهِ ۗ قَالَ سُبْحٰنَكَ مَا يَكُونُ لِي ۚ أَن أَقُولَ مَا لَيْسَ لِي بِحَقِّ ۚ إِن  
 كُنْتُ قُلْتُهُۥ فَقَدْ عَلِمْتَهُۥ ۚ تَعَلَّمُ مَا فِي نَفْسِي وَلَا أَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِكَ ۚ إِنَّكَ  
 أَنْتَ عَلَّمُ ٱلْغُيُوبِ ﴿١١٦﴾ مَا قُلْتُ لَهُمْ إِلَّا مَآ أَمَرْتَنِي بِهٖۤ ۚ أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ  
 رَبِّي وَرَبَّكُمْ ۚ وَكُنْتُ عَلَيْهِمْ شَهِيدًا مَّا دُمْتُ فِيهِمْ ۗ فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي كُنْتُ أَنْتَ  
 ٱلرَّقِيبَ عَلَيْهِمْ ۚ وَأَنْتَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿١١٧﴾ إِن تَعَدَّيْتُمْ فَلِإِيْهِمْ عِبَادَتُكُمْ  
 وَإِن تَغْفِرْ لَهُمْ فَلَإِنَّكَ أَنْتَ ٱلْعَزِيزُ ٱلْحَكِيمُ ﴿١١٨﴾ قَالَ اللَّهُ هٰذَا يَوْمٌ يَنْفَعُ

الصَّٰدِقِينَ صَدَقْتُمْ ۗ لَهُمْ جَنَّٰتٌ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا  
أَبَدًا ۗ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ ۗ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١١٩﴾

Na (Kumbukeni) Mwenyezi Mungu atakaposema: “Ewe Isa bin Maryam, Je, wewe uliwaambia watu “Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa Waungu badala ya Mwenyezi Mungu”? Aseme (Nabii Isa) “Wewe umetakasika na kuwa na mshirika. Hainijuzii mimi kusema ambayo si haki yangu kuyasema (kwa kuwa nia ya uwongo). Kama ningalisema bila shaka ungalijua; unayajua yaliyomo nafsini mwangu, lakini siyajui yaliyomo nafsini mwako; hakika wewe ndiye ujuaye mambo ya ghaibu Sikuwaambia lolote ila yale uliyoniamrisha: Ya kwamba! Mwabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu na Mola wenu! Na nilikuwa shahidi juu yao nilipokuwa nao; na uliponikamilishia muda wangu, wewe ukawa mchungaji juu yao, na wewe shahidi juu ya kila kitu ikiwa utawaadhibu, basi bila shaka hao ni waja wako; na ukivasamehe basi kwa hakika wewe ndiye mwenye nguvu na mwenye hikima (hutaambiwa kuwa wamekushinda kuwatia adabu). Mwenyezi Mungu atasema: “Hii ndiyo siku ambayo wakweli utawafaa ukweli wao. Wao watapata Bustani zipitazo mbele yake mito, Humo watakaa milele. Mwenyezi Mungu amewawia radhi; nao wawe radhi naye. Huku ndiko kufaulu kukubwa. (5:116-119).

Hivyo hivyo kila Mtume ataulizwa juu ya jukumu alilopewa. Mwenyezi Mungu atampa malaika Jibril amri: Ee! Jibril, niletee moto. Jibril atatii amri mara moja. Kisha Mwenyezi Mungu(s.w) atauliza moto: Ewe Moto! Sema ni nani Muumba wako? Hapo kila mmoja atakaribia kufa kwa woga na wote watapiga magoti mbele ya Mwenyezi Mungu. Ni katika hali hii Qur’an inatufahamisha:

وَتَرَىٰ كُلَّ أُمَّةٍ جَائِيَةً ۗ كُلُّ أُمَّةٍ تُدْعَىٰ إِلَىٰ كِتَابِهَا الْيَوْمَ تُجْزَوْنَ مَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٢٨﴾

Na utaona kila umma unapiga magoti (siku hiyo) na kila umma utaitwa kwenda (kusoma) kitabu chao (waambiwe): “Leo mtalipwa yale mliyokuwa mkiyatenda” (45:28).

Waovu na madhalimu watapiga kelele na kila mmoja katika waumini (wa kweli) atasema: “Nafsi yangu! Nafsi yangu! Nafsi yangu! Watakapokuwa katika hali hiyo moto utalisambaza tena joto lake kwa mara ya pili, na watarudi katika hali ya kuogopa na kutetemeka. Katika mara ya tatu, watu wataanguka kifufufudi na hapo baba atamkimbia mtoto, ndugu atamkimbia ndugu yake na mume atamkimbia mkewe.

وَلَا يَسْئَلُ حَمِيمٌ حَمِيمًا ﴿١٠﴾

“Wala jamaa hatamuuliza jamaa (yake)” (70:10).

Kisha watu watahudhurishwa mmoja mmoja mbele ya Mola wao kuulizwa. Hapana yeyote atakayeongea bila ya kuulizwa. Hapatakuwa na ndugu wala rafiki wa kumsaidia au kumuonea huruma mtu mwingine. Mahojiano na Mwenyezi Mungu itakuwa kama tunavyofahamishwa katika Hadith ifuatayo:

*Abu Hurairah(r.a) amehadithia: Waliuliza Masahaba: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Tutamuona Bwana wetu siku ya Kiyama? Akauliza (Mtume) Je, mnaona ugumu kuona mwanga wa jua katikati ya mchana wakati halikufunikwa na mawingu? Wakajibu: "Hapana". Akawauliza (tena): Mnaona vigumu kuona mwanga wa mwezi katika mbala mwezi kali wakati ambapo hamna mawingu? wakajibu: "hapana" Akasema: Naapa kwa yule ambaye maisha yangu yamo mikononi mwake, hamtapata shida katika kumuona Bwana wenu bali mtamuona kama msivyoona shida kuona jua katikati ya mchana na mwezi wakati wa mbalamwezi kali. Kisha (Mwenyezi Mungu) atakutana na mja na kumuuliza: Ewe fulani sikukukataza na nikakupa nguvu, na sikukupa uongozi na roho? Ulikifiki kuwa utakutana na mimi? 'Hapana' atajibu. Atasema Mwenyezi Mungu(s.w): Sasa nimekusahau kama ulivyonisahau. Qur'an: Na itasemwa: "Leo tunakusahauni kama nyinyi mlivyosahau siku yenu hii, na mahali penu ni motoni, wala hamna wa kukunusuruni" (45:34). Kisha Mwenyezi Mungu atakutana na mtu wa pili. (Mtume) akaeleza habari zake kama yule wa kwanza. Kisha Mwenyezi Mungu atakutana na mtu wa tatu na atamuuliza maswali yale yale: Mja huyo atajibu: Ee Bwana, nilikuamini na nikaamini kitabu chako, na Mitume wako, niliswali, nikafunga na kutoa zaka. Atataja matendo mema aliyoyafanya kwa kiasi atakachoweza. Mwenyezi Mungu tamwambia: Njoo hapa (kama hivyo unavyosema ndivyo) Sasa tutakuletea mashahidi. Atajiuliza ni nani atakayetoa ushahidi dhidi yangu? Kisha mdomo wake utafungwa na makalio yatapewa amri: yatasema Makalio yake, nyama yake na mifupa yake itaongea juu ya vitendo vyake na kwa hivyo ataomba msamaha na huyo atakuwa ni mnafikiri ambaye amekasirikwa na Mwenyezi Mungu(s.w) (Muslim).*

Kwa ujumla kabla ya kuulizwa na kisha kujitetea kiasi hicho, kila mja atapewa uwezo wa kuona matendo yake aliyoyatanguliza ambayo yamehifadhiwa katika kitabu maalum ambacho atapewa aambiwe akisome mwenyewe kama tunavyofahamishwa katika Qur'an:

وَكُلِّمْنَا إِنْسَانَ الْأَزْمَانِ طَيْرَهُ فِي عُنُقِهِ ۖ وَخَرَجَ لَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ كِتَابًا  
يَلْقَاهُ مَنْشُورًا ﴿١٧﴾ أَقْرَأَ كِتَابِكَ كَفَىٰ بِنَفْسِكَ الْيَوْمَ عَلَيْكَ حَسِيبًا ﴿١٨﴾

*Na kila mwanaadamu tumemfungiwa (jaza ya) ya vitendo vyake shingoni mwake; na tutamtotea siku ya Kiyama daftari (iliyoandikwa ndani yake kila alilolifanya) atakayoikuta imekunjuliwa (aambiwe) "Soma daftari yako. Nafsi yako inakutosha leo kukuhisabu" (17:13-14).*

Daftari hili ni daftari la ajabu, litakuwa limenukuu kila kitu mja alichokitenda katika maisha yake. Tunaweza kukiangalia kitabu hiki zaidi ya mfano wa televisheni ya matendo ya mtu ya kila siku kutokea kwenye baleghe yake mpaka kufariki kwake dunia. Televisheni hii itaonesha hata fikra zilizofichikana akilini na siri zilizohifadhiwa vifuani. Kila kitu kitaonekana kwa uwazi katika kitabu hicho. Kitabu hiki kinatolewa picha yake na Qur'an katika aya ifuatayo:

وَوُضِعَ الْكِتَابُ فترى الْمَجْرِمِينَ مُشْفِقِينَ مِمَّا فِيهِ وَيَقُولُونَ يَا وَيْلَتَنَا  
 مَالِ هَذَا الْكِتَابِ لَا يُغَادِرُ صَغِيرَةً وَلَا كَبِيرَةً إِلَّا أَحْصَاهَا وَوَجَدُوا  
 مَا عَمِلُوا حَاضِرًا وَلَا يَظْلُمُ رَبُّكَ أَحَدًا ﴿١١﴾

*Na madaftari yatawekwa (mbele yao). Utaona wabaya wanavyoogopa kwa sababu ya yale yaliyomo (madaftarini) na watasema: "Ole wetu" (Ee kuangamia kwetu leo)! Na watakuta yote yale waliyoyafanya yamehudhuria hapo; na Mola wako hamdhulumu yeyote" (18:49).*

Pia tumefahamishwa katika Qur'an:

فَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ ﴿٧٧﴾ وَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ﴿٧٨﴾

*Basi anayefanya wema (hata) wa kiasi cha uzito wa mdudu chungu ataona jaza yake. Na anayefanya uovu (hata) wa uzito wa mdudu chungu (atom's weight) ataona jaza yake" (99:7-8).*

### (v) **Makazi ya Peponi**

Kabla hatujaelezea maisha ya Peponi yatakavyokuwa hebu tuangalie maana ya neno Jannat (Pepo). Jannat ilivyoelezwa katika Qur'an na Hadith ni Bustani nzuri zilizo na matunda na miti mizuri ya kila aina, yenye kupitiwa na mito ya maji mazuri na matamu kuliko asali na meupe kuliko maziwa na yenye harufu nzuri kuliko miski. Pia ndani ya bustani hii nzuri isiyo na mfano wake patakuwa na majumba ya ghorofa mazuri yasiyo na mfano yenye fanicha nzuri zisiso hadithika. Maelzo ya Qur'an na Hadith katika kuelezea uzuri wa pepo ni kama mfano tu kwani vipaji hivi vya fahamu tulivyo navyo ni vya hapa hapa duniani tu na havina uwezo kabisa kuyaingiza katika picha sahihi matukio yote ya maisha ya Akhera. Katika maisha hayo ya Akhera watu watakuwa na maumbile na vipaji vinavyolingana na maisha hayo na kila mja ataona na kuhisi maisha ya huko kwa uhakika. Hivi ndivyo anavyotufahamisha Mtume Muhammad(s.a.w) katika Hadith ifuatayo:

*Abu Hurairah(r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kasema: Mwenyezi Mungu(s.w) kasema: Nimemwandalia mja wangu mema ambayo hapana jicho lililowahi kuona, na hapana sikio lililopata kusikia, na hapana moyo wa mtu uliopata kufahamu (kufikiri). Na soma kama unapenda. "Nafsi yoyote haijui iliyofichiwa katika hayo yanayofurahisha macho (huko Peponi) ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyafanya (32:17)" (Bukhari na Muslim).*

Kwa maana ya jumla, neno Jannat limetumiwa katika Uislamu kama kielelezo cha mazingira mazuri katika maisha ya Akhera ambapo watu wema walioishi hapa duniani kwa wema, kwa kufuata barabara kanuni za maisha ya kila siku kama zilivyowekwa na Mwenyezi Mungu(s.w), wataishi milele kwa furaha na amani. Hali ya mazingira ya maisha ya wakazi wa Peponi inafafanuliwa katika Hadith zifuatazo:

*Jabir(r.a) anasimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: hakika wakazi wa Peponi watakula na kunywa lakini hawatakuwa wanatema, wala hawendi haja ndogo au kubwa, wala kutokwa na uchafu puani. Waliuliza (Masahaba): Kitakuwaje chakula? Alijibu (Mtume) kitakuwa kitamu kama utamu wa miski na watakuwa wamejazwa na Tasbihi na Tahmid kama walivyojaaliwa kupumua (Muslim).*

*Abu Sayyid na Abu Hurairah wamesimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: "Mwenye kunadi atanadi: "Kwenu pana afya ya kudumu na daima hamtakuwa wagonjwa, na kwenu kuna maisha ya milele na hapana kufa, na kwenu kuna ujana unaoendelea daima hamtazeeka, na kwenu mna neema ziendeleazo na daima hamtapungukiwa na mahitaji". (Muslim).*

Pamoja na Hadith hizi, Qur'an inatuchorea picha ya maisha ya peponi pamoja na wakazi wake na sifa zitakazowawezesha kuingia humo. Hebu tuzingatie aya chache zifuatazo:

إِنَّ أَصْحَابَ الْجَنَّةِ الْيَوْمَ فِي شُغْلٍ فَاكِهِونَ ﴿٥٥﴾ هُمْ وَأَزْوَاجُهُمْ فِي ظِلَّلٍ  
عَلَى الْأَرَائِكِ مُتَّكِنُونَ ﴿٥٦﴾ هُمْ فِيهَا فَاكِهِةٌ وَهُمْ مَا يَدْعُونَ ﴿٥٧﴾

*"Kwa yakini watu wa peponi leo wamo katika shughuli (zao), wamefurahi. Wao na wake zao wamo katika vivuli, wameegemea juu ya viti vya fahari. Watapata humo (kila namna ya) matunda na watapata kila watakavyovitaka. Salama (tu juu yao), ndilo neno litokalo kwa Mola (wao) Mwenye Rehema" (36:55-58).*

﴿ قُلْ أُوْنِتِيكُمْ بِخَيْرٍ مِّنْ ذَٰلِكُمْ ۚ لِلَّذِينَ اتَّقَوْا عِنْدَ رَبِّهِمْ جَنَّاتٌ  
تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا وَأَزْوَاجٌ مُّطَهَّرَةٌ وَرِضْوَانٌ ۗ

مَنْ أَلَّهِ ۗ وَاللَّهُ بِصِيرٍ بِالْعِبَادِ ﴿١٥﴾ الَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا إِنَّا أَمْنَا  
فَاغْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ﴿١٦﴾ الصَّابِرِينَ وَالصَّادِقِينَ  
وَالْقَانِتِينَ وَالْمُنْفِقِينَ وَالْمُسْتَغْفِرِينَ بِالْأَسْحَارِ ﴿١٧﴾

*Sema: “Nikwambieni yaliyo bora kuliko hivyo? Kwa ajili ya wamchao Mwenyezi Mungu ziko bustani kwa Mola wao, zipitazo mito mbele yake. Watakaa humo milele na wake (zao) waliotakaswa (na kila uchafu na kila ubaya). Na wana radhi ya Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu anawaona (wote) waja (wake). Ambao ndio wanasema: Mola wetu! Hakika sisi tumeamini basi tughufirie madhambi yetu, na tuepushe na adhabu ya moto” Wafanyao subira, na wasemao kweli, na watiio, na watoao (sadaka) na waombao maghufira saa za karibu ya Alfajiri” (3:15-17).*

Pia rejea aya zifuatazo: (18:30-31), (22:23), (7:42-43), (39:20), (15:45-48), (35:33-35), (43:68-73), (47:15), (52:27-28), (38:49-54), (76:5-22) na (70:22-35).

### (vi) Makazi ya Motoni

Moto umetumiwa katika Qur’an na Hadith kuonesha mazingira mabaya watakayoshukia watu waovu, waliompinga Mwenyezi Mungu na kuendesha maisha yao ya hapa duniani kinyume na kanuni na taratibu alizoziweka Mwenyezi Mungu(s.w). Maisha ya motoni ni kinyume na maisha ya peponi ambayo picha yake tumeshaiona. Tunafahamishwa katika Qur’an kuwa motoni kuna daraja au milango saba na kwa kila mlango iko sehemu iliyogawanywa.

وَإِنَّ جَهَنَّمَ لَمَوْعِدُهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٤٣﴾ هَا سَبْعَةُ أَبْوَابٍ لِّكُلِّ بَابٍ مِّنْهُمْ  
جُزْءٌ مَّقْسُومٌ ﴿٤٤﴾

*“Na bila shaka Jahannam ndipo mahali pa walipoahidiwa. Ina milango saba; na kwa kila mlango iko sehemu yao iliyogawanywa” (15:43-44).*

Daraja hizi za moto zimepewa majina kama tusomavyo katika Qur’an:

- **Jahannam:** Katika aya nyingi jina hili limetumiwa kama jina la ujumla la maisha ya Motoni.
- **Lahab:** Moto wenye muwako mkubwa kabisa (111:3).
- **Hutwamah:** Moto wa kuvunja vunja – ambao uliowashwa kwa ukali (104:4).
- **Sai’ra:** Moto mkali wa kuunguza (4:55).

- **Saqara:** Moto Mkali (26:91 na 102:6).

- **Haawiya:** Moto uwakao kwa ukali (101:9).

Wakosaji wataingia katika aina hizi za moto kulingana na makosa yao. Kwa ujumla aina yoyote ya moto ulioandaliwa kwa ajili ya makafiri hata ukiwa wa daraja ya chini namna gani, utakuwa ni mkali usio na mfano na usiovumilika hata kwa muda mfupi sana kama Mwenyezi Mungu anavyotufahamisha:

﴿١١﴾ **إِنَّهَا سَاءَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا**

“Hakika hiyo (Jahannam) ni kituo kibaya na mahali (pabaya kabisa) pa kukaa (hata kwa muda mfupi)” (25:66).

Hebu tuone pia anavyotufahamisha Mtume(s.a.w) juu ya kiwango cha ukali wa adhabu ya motoni:

*Nuuman bin Bashir (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Hakika atakaye kuwa na adhabu nyepesi kabisa katika wakazi wa motoni ni yule atakayekuwa na viatu vya moto. Kwa moto huu, (wa miguu) utachemsha ubongo wake kama maji yachemkavyo kwenye birika. Haitaonekana kuna kiwango cha chini kabisa cha adhabu”. (Bukhari na Muslim).*

Kwa ujumla moto wa adhabu aliouandaa Mwenyezi Mungu kwa watu waovu ni mkali sana.

Humo ndani ya shimo la moto wa Jahannam patakuwa na mashimo (mabonde) na shimo baya kabisa kuliko yote ni “*Jabal-Huzn*”, ambapo Jahannam yenyewe inaomba kukingwa na moto huo wa “*Jabal-Huzn*” mara sabini kwa siku. Ndani ya mazingira ya motoni patakuwa na miti michungu na miti maarufu kwa uchungu wake ni “*Zaqquum*”. Tunapata maelezo kamili ya mti wa “*Zaqquum*” ambao umemea katikati ya Jahannam na watakaostahiki kuula katika aya ziufatazo:

﴿١٧﴾ **أَذَلِكْ خَيْرٌ نُّزُلًا أَمْ شَجَرَةُ الزَّقُّومِ** ﴿١٨﴾ **إِنَّا جَعَلْنَاهَا فِتْنَةً لِلظَّالِمِينَ**

﴿١٩﴾ **إِنَّهَا شَجَرَةٌ تَخْرُجُ فِي أَصْلِ الْجَحِيمِ** ﴿٢٠﴾ **طَلْعُهَا كَأَنَّهُ رُءُوسُ**

﴿٢١﴾ **الشَّيْطِينِ** ﴿٢٢﴾ **فَأَيُّهُمْ لَّا يَكُونُ مِنْهَا فَأَمَّا لَعْنُونَ مِنْهَا الْبُطُونَ** ﴿٢٣﴾ **ثُمَّ إِنَّ**

﴿٢٤﴾ **لَهُمْ عَلَيْهَا لَسْوَابًا مِّنْ حَمِيمٍ**

Je karibisho la namna hii silo bora au kupata mti wa “*Zaqquum*”? (Mti mchungu kabisa watakaolishwa watu wa motoni). Kwa yakini sisi tumeufanya



ni adhabu ya (hao) madhalimu (wa nafsi zao). Hakika huo ni mti unaotoka (unaoota) katikati ya Jahannam. Panda zamatunda yake (zinatisha) kama kwamba ni vichwa vya mashetani. Bila shaka wao watakula katika (mti) huo, na kwa huo wajaze matumbo (yao). Kisha bila shaka utawathubutikia uchungu wa mti huo, mchanganyiko wa maji ya moto” (37:62-67).

Pia katika mazingira ya motoni patakuwa na **nyoka** na **ng’e** wakubwa wenye sumu kali watakaowauma wakazi wa humo kama sehemu ya adhabu yao kama tunavyofahamishwa katika Hadith ifuatayo:

“Abdullah bin Harith bin Jazin(r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema; “Kuna nyoka huko motoni wakubwa kama ngamia. Mmoja wao akikuuma mara moja, uchungu wake hubakia kwa miaka arobaini. Kuna ng’e huko motoni wakubwa kama nyumbu. Mmoja wao akimuuma mtu uchungu wake utabakia kwa muda wa miaka arobaini” (Ahmad).

Kwa vyovyote itakavyokuwa maisha ya motoni yatakuwa magumu sana kwa wakazi wake. Chakula chao kitakuwa cha moto wa kuunguza kila kitu tuboni, mavazi yao yatakuwa ya moto, kinywaji chao cha moto kitakacho chemsha matumbo yao kama maji yachemkavyo kwenye sufuria ya shaba. Picha halisi ya manzigira ya motoni, maisha ya wakazi wake na sifa zitakazowafanya wastahiki kuingia humo, imetolewa na aya nyingi za Qur’an na hizi zifuatazo ni aya chache tu katika hizo:

إِنَّ جَهَنَّمَ كَانَتْ مِرْصَادًا ﴿١١﴾ لِلطَّغْيِينِ مَتَابًا ﴿١٢﴾ لِّلْبَشِيرِ فِيهَا أَحْقَابًا ﴿١٣﴾ لَا يَدْخُلُونَ فِيهَا بَرْدًا وَلَا شَرَابًا ﴿١٤﴾ إِلَّا حَمِيمًا وَعَسَاقًا ﴿١٥﴾ جَزَاءً وَفَاقًا ﴿١٦﴾ إِنَّهُمْ كَانُوا لَا يَرْجُونَ حِسَابًا ﴿١٧﴾ وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا كِذَابًا ﴿١٨﴾ وَكُلَّ شَيْءٍ أَحْصَيْنَاهُ كِتَابًا ﴿١٩﴾ فَذُوقُوا فَلَنْ نَزِيدَكُمْ إِلَّا عَذَابًا ﴿٢٠﴾

Kwa hakika Jahannam inawangoja wabaya. Ni makazi ya maasi. Wakae humo dahari nyingi (karne baada ya karne). Hawataonja humo baridi (wala usingizi) wala kinywaji. Ila maji yachemkayo sana na usaha (Wanalipwa) malipo yaliyo sawa (na amali zao). Hakika wao hawakuwa wakiogopa hisabu (ya Mwenyezi Mungu). Na wakikadhibisha Aya Zetu kukadhibisha (kukubwa kabisa). Na (hali ya kuwa) kila kitu Tumekidhibiti kwa kukiandika. Nasi Hatutakuzidishieni kitu ila adhabu. Basi onjeni (leo adhabu yangu). Juu ya adhabu. (78:21-30).

وَجَاءَ يَوْمَئِذٍ بُرْهَانَ رَبِّهِمْ ۗ  
 يَقُولُ يَلِيَّتَنِي قَدَمْتُ لِحَيَاتِي ﴿٢٤﴾ فَيَوْمَئِذٍ لَا يُعَذِّبُ عَذَابَهُ  
 أَحَدٌ أَحَدًا وَلَا يُوثِقُ وِثْقَهُ أَحَدٌ أَحَدًا ﴿٢٥﴾

*Basi Siku hiyo italetwa Jahannam. Siku hiyo mwanaadamu atakumbuka, lakini kukumbuka huko kutamfaa nini? Atasema: “Laiti ningelitanguliza (wema) kwa ajili ya uhai wangu (huu wa leo)” Basi siku hiyo hataadhibu yoyote namna ya kuadhibu Kwake (Mwenyezi Mungu). Wala hatafunga yoyote jinsi ya kufunga Kwake (Mwenyezi Mungu)” (89:23-26).*

Aya hizi chache zinatupa picha ya kutisha ya maisha ya Motoni ambapo wakazi wake hawatakuwa na hata chembe ya furaha na hawatakuwa japo watatamani sana kufa. Na hasara kubwa zaidi watakayoipata ni kutomuona Mwenyezi Mungu(s.w). Kwani kumuona Mwenyezi Mungu ni kilele cha furaha na ilihali watu wa motoni wameharamishwa hata chembe ya furaha. Kwa ujumla marejeo ya motoni ni marejeo mabaya kabisa na kila mja mwema hana budi kuomba mara kwa mara:

..... رَبَّنَا أَصْرِفْ عَنَّا عَذَابَ جَهَنَّمَ ۖ إِنَّ عَذَابَهَا كَانَ غَرَامًا ﴿٢٦﴾  
 إِنَّهَا سَاءَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا ﴿٢٧﴾

*“...Mola wetu! Tuondolee adhabu ya Jahannam, bila shaka adhabu yake ni yenye kuendelea. Hakika hiyo (Jahannam) ni kituo kibaya na mahali (pabaya kabisa) pa kukaa (kwa muda mfupi au mrefu)” (25:65-66).*

## Mtazamo wa Uislamu Juu ya Shufaa

### Nini Shufaa?

Kwa mujibu wa Qur'an na Hadith sahihi, Shufaa ni uombezi utakaotolewa na wale waliopewa idhini na Mwenyezi Mungu(s.w) kuwaomba watu mbali mbali ili:

- (i) Watolewe motoni na kupelekwa Peponi.
- (ii) Wafanyiwe hisabu nyepesi.
- (iii) Waingizwe peponi wale ambao mizani ya mema yao na maovu yao imekuwa sawa sawa.
- (iv) Wapandishwe daraja katika pepo, watolewe daraja ya chini na kupelekwa daraja ya juu.

## Nani Watakao Shufaia?

Watakao shufaia ni pamoja na Malaika, Mitume, Watu wema ikiwa ni pamoja na Watoto wachanga na amali njema kama swalaa, saumu, kusoma Qur'an na kadhalika.

## Nani Watakaostahiki Kushufaiwa?

Kwa mujibu wa Qur'an, Shufaa haitaombwa kwa misingi ya upendeleo wa udugu, urafiki, ukoo, utaifa au upendeleo mwingine wa aina yoyote. Bali Shufaa itajuzu tu kwa wale atakaowataka Mwenyezi Mungu(s.w) kuwa waombewe na atatoa idhini juu ya kuombewa kwao. Idhini ya Shufaa itategemeana na mwenendo aliokuwa nao anayeombewa. Mitume watawashufaia wafuasi wao waliowafuata kwa uadilifu. Watu wema watawashufaia jamaa zao, jirani zao, rafiki zao wanachi wenzao waliowatendea wema kwa ajili ya Mwenyezi Mungu(s.w). Watoto wadogo watawashufaia wazazi wao waliokuwa wema kwao. Shufaa hizi zitapata idhini ya Mwenyezi Mungu(s.w) na kukubaliwa iwapo tu wale waliombewa walikuwa waumini ambao kwa njia moja au nyingine waliteleza na kuchupa mipaka ya Mwenyezi Mungu(s.w) na wakastahiki kuwa katika hali hiyo ya dhiki. Kwa kafiri, mushriki na mnafiki, shufaa ya aina yoyote haitakubaliwa juu yao hata kama itaombwa na Mitume au vipenzi vya Mwenyezi Mungu(s.w) kwa mfano, maombezi ya Nabii Nuhu kwa ajili ya mwanawe kafiri yalikataliwa na akawa ni miongoni mwa waliogharikishwa kama tunavyojifunza katika Qur'an:

وَنَادَى نُوحٌ رَبَّهُ فَقَالَ رَبِّ إِنَّ أَبِي مِنْ أَهْلِي وَإِنَّ وَعْدَكَ الْحَقُّ وَأَنْتَ أَحْكَمُ  
 الْحَكَمِينَ ﴿١١٠﴾ قَالَ يَنْتُوخُ إِنَّهُ لَيْسَ مِنْ أَهْلِكَ إِنَّهُ عَمَلٌ غَيْرُ صَالِحٍ فَلَا  
 تَسْأَلِنَ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ إِنِّي أَعِظُكَ أَنْ تَكُونَ مِنَ الْجَاهِلِينَ ﴿١١١﴾

*Na Nuhu alimuomba Mola wake (alipomuona mwanawe anaangamia) akasema: "Ewe Mola wangu! Mwanangu ni katika watu wa nyumbani kwangu (mbona anaangamia)? Na hakika ahadi yako ni haki; nawe ni Mwenye haki kuliko mahakimu (wote)". Akasema (Mwenyezi Mungu): "Ewe Nuhu! Huyu si miongoni mwa watu wako. Yeye ni (mwenye) mwendo usiokuwa mzuri. Basi usiniombe ambayo huyajui. Mimi nakunasihi usiwe miongoni mwa wajinga" (11:45-46).*

Pia tunafahamishwa katika Hadith jinsi Nabii Ibrahim (a.s) atakavyo kataliwa maombi yake kwa Mwenyezi Mungu(s.w) katika kumuomba baba yake Azar aepushwe na adhabu kali walioandaliwa washirikina. Hebu tuiangalie Hadith ifuatayo:

*Abu Hurairah(r.a) amesimulia kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu aliyesema: Ibrahim atakutana na baba yake Azar katika siku ya Kiyama. Uso wa Azar utakuwa umefunikwa na lami na mavumbi. Ibrahim atamsemesha: "Sikukuambia kuwa usiache kunitii (usinikadhibishe)?" Baba yake atamjibu: "Leo sitaacha kukutii". Ibrahim ataomba: Ewe Mola! Hakika umeniahidi kuwa hutanjifedhehesha siku watakapofufuliwa watu. Sasa ni fedheha gani zaidi kuliko kuwekwa mbali na baba yangu?" Mwenyezi Mungu(s.w) atasema: Hakika Nimeiharamisha Pepo kwa Washirikina. Kisha itasemwa kwa Ibrahim: Angalia ni kitu gani kulichoko miguuni mwako. Ataangalia, Hamaki! Shingo kubwa itatokeza. Ataburuzwa (Azar) kwa miguu yake na kutupiwa motoni". (Bukhari).*

Vile vile tukirejea Qur'an tunaona tena jinsi Mtume Muhammad(s.a.w) alivyokataliwa maombi yake alipowaombea wanafiki kama tunavyofahamishwa katika aya zifuatazo:

أَسْتَغْفِرُ لَهُمْ أَوْ لَا تَسْتَغْفِرُ لَهُمْ إِنْ تَسْتَغْفِرْ لَهُمْ سَبْعِينَ مَرَّةً فَلَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَهُمْ  
ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ كَفَرُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ

*(Ewe Mtume)! Waombe msamaha (hao wanafiki) au usiwaombe, (yote sawa sawa). Hata ukiwaombea msamaha mara sabini, Mwenyezi Mungu Hatawasamehe. Hayo ni kwa sababu ya kuwa wao wamemkataa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, Na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu wavunjao amri (zake)" (9:80).*

Hivyo kutokana na maelezo yote haya, tumeona kuwa shufaa itakuwepo, lakini itawanufaisha tu walioamini na sio makafiri, washirikina na wanafiki. Jambo muhimu kwa Muislamu ni kujitakasa kwa kutenda mema na kuacha maovu na kuwa mwepesi wa kurejea kwa Mwenyezi Mungu(s.w) kwa toba ya kweli baada ya kumkosea au kuhisi kumkosea. Daima si vyema Muislamu kuzembea katika kufanya mema na kuendelea kufanya maovu kwa matarajio ya kupata shufaa ya Mtume au ya yeyote yule amtegemeaye kuwa atamshufai. Kuna mambo mawili ya kuzingatia kwa wale wanaoacha kujitahidi kutekeleza wajibu wao kama anavyoridhia Mwenyezi Mungu(s.w) na badala yake wakaishi watakavyo kwa tegemeo la kupata uokovu kutokana na shufaa:

**Kwanza**, kutegemea shufaa ni jambo la kubahatisha mno, kwani si jambo lililoko kwenye mamlaka ya yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu pekee. Ni mpaka kwanza Mwenyezi Mungu(s.w) amridhie muombaji na ampe idhini ya kuomba na kisha ni mpaka ayaridhie maombi hayo ndio Atoe shufaa.

**Pili**, shufaa nyingine itakuja baada ya mtu kuadhibiwa kwanza, adhabu ambayo ni kali mno, inayodhalilisha na kuhikilisha hata kama mja atakaa humo kwa muda mfupi sana, ni vyema tuzingatie sana aya ifuatayo:

فَيَوْمَئِذٍ لَا يُعَذِّبُ عَذَابُهُ أَحَدًا ﴿١٥﴾

“Basi Siku hiyo hataadhibu yeyote namna ya kuadhibu Kwake (Mwenyezi Mungu(s.w))” (89:25).

Pia tuzingatie Hadith ifuatayo:

Nuuman bin Bashir(r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Hakika atakayekuwa na adhabu nyepesi kabisa katika wakazi wa motoni atakuwa yule atakayekuwa na viatu vya moto. Kwa moto huu, (wa miguu) utachemsha ubongo wake kama maji yachemkavyo kwenye birika. Haitaonekana kuna mwenye adhabu kali kuliko hii, lakini hiki ndicho kiwango cha chini kabisa cha adhabu. (Bukhari na Muslim).

Hivyo jambo la busara kwa Muislamu ni kujitahidi kuepukana na adhabu kali ya Mwenyezi Mungu(s.w) aliyowaandalia watu maasi na badala yake ayaendee kwa juhudi kubwa inayoambatana na subira, yale yatakayompelekea kustahiki kuingizwa Peponi moja kwa moja. Kisha mara kwa mara tuombe:

..... رَبَّنَا أَصْرِفْ عَنَّا عَذَابَ جَهَنَّمَ إِنَّ عَذَابَهَا كَانَ غَرَامًا ﴿١٦﴾

إِنَّهَا سَاءَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا ﴿١٧﴾

“.....Mola wetu! tuondolee adhabu ya Jahannam, bila shaka adhabu yake ni yenye kuendelea. Hakika hiyo (Jahannam) ni kituo kibaya na mahali pa kukaa” (25:65-66)

## Maana ya Kuamini Siku ya Mwisho katika Maisha ya Kila Siku

Picha ya maisha ya Akhera tumeshaipata kutokana na maelezo ya Qur'an na Hadith. Lakini je, picha hii pekee yatosha kumfanya mja awe muumini wa kweli? Hebu tuyazingatie tena maneno ya Mwenyezi Mungu(s.w).

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَقُولُ ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَبِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَمَا هُم بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٨﴾

يَتَّخِذُونَ اللَّهَ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَمَا يَتَّخِذُونَ إِلَّا أَنفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿١٩﴾

Na hakika watu wako wasemao: “Tumemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho; na hali ya kuwa wao si wenye kuamini. Wanataka kumdanganya Mwenyezi Mungu na wale walioamini, lakini hawadanganyi ila nafsi zao; nao hawatambui” (2:8-9).

Mwenyezi Mungu(s.w) katika Suratul-Ma'uun ameanza na swali la mshangao: **“Je, umemuona yule anayekadhibisha siku ya malipo?”** Si kwa kutaraji jibu lolote kutoka kwetu bali ni ili tutanabahi juu ya matendo ambayo tukiyafanya hatutakuwa tu waumini wa siku ya mwisho, japo tumezoea kuyafanya na tunayaona ni ya kawaida na madogo. Matendo anayotutanabahisha kwayo katika sura hii ni kuwasukuma au kuwanyanyasa yatima, kutowalisha maskini, kutosimamisha sala, kufanya ria na kuwanyima wanaadamu wenziwe misaada wanayohitajia na ilihali wanauwezo wa kuwasaidia. Kinyume chake, muumini wa kweli wa Siku ya Malipo huwasaidia wanaadamu wenzake ili iwe sababu ya kusamehewa na Mola Wake na kuepushwa na adhabu ya Moto kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

وَيُطْعَمُونَ الطَّعَامَ عَلَىٰ حُبِّهِ مِسْكِينًا وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا ﴿٨﴾ إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ  
لِوَجْهِ اللَّهِ لَا نُرِيدُ مِنْكُمْ جَزَاءً وَلَا شُكْرًا ﴿٩﴾ إِنَّا نَخَافُ مِنْ رَبِّنَا يَوْمًا  
عَبُوسًا قَمَطِيرًا ﴿١٠﴾

“Na huwalisha chakula maskini na mayatima na wafungwa, na hali yakuwa wenyewe wanakipenda (chakula hicho). (Husema wenyewe katika nyoyo zao wanapowapa chakula hicho): “Tunakulisheni kwa ajili ya kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu (tu) hatutaki kwenu malipo wala shukrani. “Hakika sisi tunaogopa kwa Mola wetu hiyo siku yenye shida na taabu” (76:8-10).

Muumini wa Siku ya mwisho daima huiogopa adhabu ya Mwenyezi Mungu(s.w) itakayowafika wachupao mipaka yake. Pamoja na kujitahidi kujiepusha na maovu, huwa mwepesi wa kutubia kwa Mwenyezi Mungu(s.w) kwa kosa lolote atakalolifanya kwa kuteleza au kutojua. Mwenyewe Mwenyezi Mungu(s.w) anatumiza tuharakie kuleta toba kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

﴿ وَسَارِعُوا إِلَىٰ مَغْفِرَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ  
أُعِدَّتْ لِلْمُتَّقِينَ ﴿١٣٣﴾

“Na yaendeeni upesi upesi maghufira ya Mola wenu na Pepo (yake) ambayo upana wake (tu) ni (sawa na) mbingu na ardhi. (Pepo) iliyowekewa wamchao Mungu” (3:133).

إِنَّمَا التَّوْبَةُ عَلَى اللَّهِ لِلَّذِينَ يَعْمَلُونَ السُّوءَ بِجَهْلَةٍ ثُمَّ يُتُوبُونَ مِنْ قَرِيبٍ فَأُولَئِكَ يَتُوبُ اللَّهُ عَلَيْهِمْ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿١٧﴾

“Toba inayopokelewa na Mwenyezi Mungu ni ya wale wanaofanya uovu kwa ujinga, kisha wakatubia kwa upesi. Hao ndio Mwenyezi Mungu huipokea toba yao. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye hikima” (4:17).

Muumini wa siku ya mwisho, anajua kwa hakika kifo kinaweza kumfika wakati wowote na hatapewa mtu wasaa wa kuahirisha kifo chake hata sehemu ya elfu moja na moja ya sekunde. Pia muumini anafahamu vema kuwa toba itakayotolewa baada ya kuona dalili za wazi wazi za kifo haitakuwa ni yenye kukubaliwa mbele ya Mwenyezi Mungu(s.w) kama tunavyojifunza katika Qur’an:

وَلَيْسَتِ التَّوْبَةُ لِلَّذِينَ يَعْمَلُونَ السَّيِّئَاتِ حَتَّىٰ إِذَا حَضَرَ أَحَدَهُمُ الْمَوْتُ قَالَ إِنِّي تُبْتُ إِلَيْنَ وَلَا الَّذِينَ يَمُوتُونَ وَهُمْ كُفَّارٌ ﴿١٨﴾  
أُولَئِكَ أَعْتَدْنَا لَهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٨﴾

“Hawana toba wale ambao hufanya maovu mpaka mauti yamemhudhuria mmoja wao, (hapo) akasema: “Hakika mimi sasa natubu”. Wala (hawana toba) wale ambao wanakufa katika hali ya ukafiri. Hao tumewaandalia adhabu iumizayo” (4:18).

## Toba ya Kweli

Mwenyezi Mungu(s.w) anatuamrisha:

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا تُوبُوا إِلَى اللَّهِ تَوْبَةً نَّصُوحًا عَسَىٰ رَبُّكُمْ أَن يُكَفِّرَ عَنْكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ وَيُدْخِلَكُم جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ..... ﴿١٩﴾

Enyi mlioamini! Tubuni kwa Mwenyezi Mungu toba iliyo ya kweli, huenda Mola wenu atakufutieni maovu yenu na kuingizeni katika pepo zipitazo mito mbele yake.....” (66:8).

..... وَأَسْتَغْفِرُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٢٠﴾

“.....Na ombeni msamaha kwa Mwenyezi Mungu hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe, Mwingi wa kurehemu” (73:20).

Mwenyezi Mungu(s.w) ameahidi kuwasamehe wale watakao hudhurisha mbele yake toba ya kweli kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

إِلَّا مَنْ تَابَ وَءَامَنَ وَعَمِلَ عَمَلًا صَالِحًا فَأُولَئِكَ يُبَدِّلُ اللَّهُ  
سَيِّئَاتِهِمْ حَسَنَاتٍ ۗ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٧٦﴾ وَمَنْ تَابَ وَعَمِلَ  
صَالِحًا فَإِنَّهُ يَتُوبُ إِلَى اللَّهِ مَتَابًا ﴿٧٧﴾

“Ila yule atakayetubia na kuamini na kufanya vitendo vizuri, basi hao ndio Mwenyezi Mungu atawabadilishia maovu yao kuwa mema; na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu. Na aliyetubia na kufanya wema, basi kwa hakika yeye anatumu kweli kweli kwa Mwenyezi Mungu” (25:70-71).

ثُمَّ إِنَّ رَبَّكَ لِلَّذِينَ عَمِلُوا السُّوءَ بِجَهْلَةٍ ثُمَّ تَابُوا مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ  
وَأَصْلَحُوا إِنَّ رَبَّكَ مِنْ بَعْدِهَا لَغَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١١٩﴾

“Naye ndiye anayepokea toba za watu wake na anasamehe makosa, na anayajua yote mnayoyatenda. Kisha hakika Mola wako kwa wale waliofanya ubaya kwa ujinga, kisha wakatubia baada ya hayo na wakatenda mema; bila shaka Mola wako baada ya hayo ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu” (16:119).

وَإِذَا جَاءَكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِآيَاتِنَا فَقُلْ سَلَمٌ عَلَيْكُمْ ۖ كَتَبَ رَبُّكُمْ  
عَلَىٰ نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ ۖ أَنَّهُ مَنْ عَمِلَ مِنْكُمْ سُوءًا بِجَهْلَةٍ ثُمَّ تَابَ مِنْ  
بَعْدِهِ وَأَصْلَحَ فَأَنَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٥٤﴾

“Na (wewe Mtume) wanapofika wale (mafakiri) wanaoamini aya zetu (na hali wamekosa kidogo; wanakuja kutubia) waambie, “Amani iwe juu yenu, Mola wenu amejilazimisha rehema, kwamba atakayefanya miongoni mwenu uovu kwa ujinga, kisha akatumu baada yake na akafanya wema, kuwa Mwenyezi Mungu atamghufiria kwani yeye ni Mwingi wa msamaha (na Mwingi wa rehema)” (6:54).



﴿ قُلْ يَبْعَادَى الَّذِينَ اسْتَرْفُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِن رَّحْمَةِ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ جَمِيعًا إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴾

*Sema: “Enyi waja wangu mliojidhulumu nafsi zenu! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu; bila shaka Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote; hakika yeye ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu” (39:53).*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa toba ya kweli yenye kupokelewa na Mwenyezi Mungu(s.w) ni ile itakayoletwa kwa kuzingatia masharti yafuatayo:

**Kwanza**, mwenye kuleta toba awe amefanya kosa kwa ujinga au kwa kutelezeshwa na vishawishi mbali mbali vilivyo mzingira bila ya kudhamiria.

**Pili**, baada ya kutanabahi kuwa ametumbukia kwenye kumkosea Mola wake, muumini anajuta moyoni na kulaumu nafsi yake kama walivyojuta Baba yetu Adamu (a.s) na Mama yetu Hawwa walipomlilia Mwenyezi Mungu kwa kusema:

﴿ قَالَا رَبَّنَا ظَلَمْنَا أَنفُسَنَا وَإِن لَّمْ تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴾

*“Mola wetu! tumedhulumu nafsi zetu, na kama hutatusamehe na kuturehemu, bila shaka tutakuwa miongoni mwa wenye khasara” (7:23).*

Pia katika Hadith iliyosimuliwa na Abubakar Swidiq na kukubaliwa na Maimamu wote wa Hadith Mtume(s.a.w) ametufundisha kuleta majuto moyoni mwetu kwa kuomba:

*“Ee Mwenyezi Mungu! Hakika nimeidhulumu nafsi yangu dhulma kubwa Hapana yoyote mwenye kusamehe dhambi isipokuwa wewe tu. Basi nakuomba nipatie msamaha utokao kwako na unihurumie. Hakika wewe ni Msamehevu, Mreheimevu”.*

**Tatu**, kuazimia moyoni kuacha maovu na iwapo makosa yake yamehusiana na kudhulumu haki za watu itabidi muumini awatake radhi wale aliwakosea na kurejesha haki zao.

**Nne**, kumuamini Mwenyezi Mungu(s.w) ipasavyo, kwa kufuata maamrisha yake yote ili kupata radhi yake na kujiప్పusha na makatazo yake yote ili kuepukana na ghadhabu yake.

**Tano**, baada ya toba, kuzidisha amali njema kwa kuwahurumia wengine kwa kutoa Sadaqa ya hali na mali, kwa kuzidisha swala na fungu za Sunnah, na kufanya juhudi ya kusimamisha Uislamu kwa mali na Nafsi. Rejea Qur’an: (61:10-13).

## KUAMINI QADAR YA MWENYEZI MUNGU(S.W)

### Maana ya Qadar

Kilugha neno “**Al-Qadar**” limetumika katika Qur’an kwa maana ya “**kiasi**”, “**kipimo**”, **kukadiria kipimo maalumu**”. Hebu turejee aya zifuatazo ambamo neno Qadar limetumiwa:

إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ ﴿٥١﴾

“Kwa hakika Sisi tumekiumba kila kitu kwa kiasi (chake mahsusi)” (54:49).

..... وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ فَقَدَرَهُ تَقْدِيرًا ﴿٥٢﴾

“.....Na (Mwenyezi Mungu) Ameumba kila kitu na Akakikadiria kipimo (chake)” (25:2).

وَالْقَمَرَ قَدَرْنَاهُ مَنَازِلَ حَتَّىٰ عَادَ كَالْعُرْجُونِ الْقَدِيمِ ﴿٣٦﴾

“Na mwezi tunaukadiria vituo, mpaka unakuwa (mwembamba) kama chaparare la mtende kuu kuu” (36:39).

### Mtazamo wa Uislamu Juu ya Qadar

Kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu ni makosa makubwa kudhani kuwa mtu anaweza kufanya jambo lolote kinyume na uwezo na idhini ya Mwenyezi Mungu. Na ni makosa makubwa pia kudhani kuwa mtu anaweza kumlaumu Mwenyezi Mungu kwa maovu anayotenda. Utatanishi wote wanaoupata watu juu ya suala hili unaondoka kwa sababu Uislamu umeyagawanya maisha ya binadamu katika maeneo makuu mawili:

- (a) Eneo ambalo binaadamu hana hiari, na
- (b) eneo ambalo binaadamu anao uchaguzi.

#### (a) Eneo ambalo binaadamu hana hiari

Binaadamu hana hiari kabisa katika baadhi ya mambo katika maisha yake. Mambo hayo humtokea atake asitake. Yaani hana uwezo wa kuchagua wala kuyabadilisha. Kwa mfano mtu hana hiari ya kuwachagua wazazi wake. Hawezi kuchagua tarehe ya kuzaliwa wala nchi atakayozaliwa. Hawezi kuchagua rangi ya ngozi yake wala aina ya nywele, rangi ya macho, kimo au vipawa vingine.

Damu itazunguka mwilini bila kuipangia yeye safari hiyo, moyo wake utadunda bila yeye kuuamrisha, atapepesa macho kutwa nzima bila kupanga. Mwili mzima wa binadamu unafanya kazi bila yeye kuupigia kura. Kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu binadamu hataulizwa au kuhisabiwa juu ya jambo lolote ambalo yeye hakuwa na hiari nalo. Yaani hakuna mtu atakayeulizwa kwa nini wewe ulizaliwa siku ya Jumanne badala ya Jumatano? Au kwa nini ulifariki mwezi wa Shaaban badala ya kusubiri hadi mwezi wa Ramadhan? Au kwa nini ulikuwa mrefu namna hii badala ya kuwa na kimo cha wastani? Kwa hakika ni rehema kubwa ya Mwenyezi Mungu kwamba mambo hayo hatuyadhibiti sisi wenyewe.

Hebu fikiria kama moyo ungekuwa unapiga kwa amri yetu, tungeweza je kulihakikisha hilo tunapolala usingizi au tunaposahau? Matatizo yangekuwa hayo hayo lau myeyusho wa chakula (digestion) ungekuwa uko chini ya udhibiti wetu n.k.

**(b) Eneo ambalo binaadamu ana uchaguzi**

Hata hivyo lipo eneo ambalo binadamu anao uhuru wa kuchagua hili au lile. Mtu anaweza kwa mfano kuchukua bastola na kumuua mtu na kumpora mali yake au anaweza kuchukua chakula na kumpa mwenye njaa. Mtu anaweza kutumia pesa zake kwa kuwanunulia nguo wazazi wake na maskini au anaweza kwenda nazo kilabuni kunywa pombe. Mtu anaweza kumuamini Mwenyezi Mungu na kumtii au anaweza kukataa kumuamini na akaamua kumuasi. Mtu anaweza kusema kweli au akaamua kusema uwongo. Anaweza kumtendea mwenziwe haki au anaweza kumdhulumu. Katika eneo hili binadamu ni mas-uli, yaani atahisabiwa na Mwenyezi Mungu kwa yote aliyoyafanya. Kwani ni mambo ambayo binadamu amepewa uhuru wa kuchagua kutenda hili au lile. Kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

إِنَّا هَدَيْنَاهُ السَّبِيلَ إِمَّا شَاكِرًا وَإِمَّا كَفُورًا ﴿٣﴾

“Hakika Sisi Tumemuongoa, (tumembainishia) njia. Basi atakuwa mwenye shukrani au mwenye kukufuru” (76:3).

وَقُلِ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكُمْ ۗ فَمَنْ شَاءَ فَلْيُؤْمِنْ وَمَنْ شَاءَ فَلْيُكْفُرْ ..... ﴿٢٩﴾

“Na sema: Huu ni ukweli uliotoka kwa Mola wenu, basi anayetaka na aamini na anayetaka na akufuru.....” (18:29).

أَلَمْ نَجْعَلْ لَهُ عَيْنَيْنِ ﴿٨﴾ وَلِسَانًا وَشَفَتَيْنِ ﴿٩﴾ وَهَدَيْنَاهُ النَّجْدَيْنِ ﴿١٠﴾

Je, hatukumpa (binadamu) macho mawili? Na ulimi na midomo miwili? Na Tukambainishia zote njia mbili? (90:8 -10).

Hivyo ni dhahiri kuwa katika eneo hili binadamu hajapangiwa na Mwenyezi Mungu lipi aje kulifanya atake asitake. Mwenyezi Mungu amempa mwongozo wa kuufuata lakini kampa na hiari ya kuufuata au kuuacha. Na ndio maana ataulizwa. Na ukweli kuwa watu wanaweza kumuasi Mwenyezi Mungu ni ushahidi tosha kuwa watu wanao uhuru wa kuchagua kutenda mema au maovu, kwani lau si hivyo watu wote wangekuwa kama malaika.

Hata hivyo, kuna mambo mawili yakuzingatia:

**Kwanza** isidhaniwe kuwa maadam watu wanao uhuru wa kuchagua kutenda lolote basi Mwenyezi Mungu hajui mpaka jambo hilo litokee. Yeye anajua yote atakayofanya mja hadi hatima yake ya mwisho siku ya Kiyama hata kabla mtu huyo hajazaliwa. Allah(s.w) anayajua atakayochagua kuyafanya lakini hakumshurutisha kuyafanya.

**Pili**, isidhaniwe kuwa maadam mtu amechagua kumuasi Mwenyezi Mungu basi mtu huyo anapotenda uovu huo Mwenyezi Mungu huchukia lakini hana uwezo wa kumzuia. Mtu hawezi kufanya lolote ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Yaani mtu anaweza tu kutenda jema au ovu kwa sababu ya kutumia vizuri au vibaya neema alizopewa na Allah(s.w). Kwa mfano tuseme mtu amekusudia kwenda kuswali Ijumaa lakini kabla hajaondoka Mwenyezi Mungu akamnyang'anya mtu huyo neema ya akili au fahamu au akakosa nguvu hata za kukaa, ni dhahiri kuwa hataweza kuswali Ijumaa. Na hivyohivyo kwa mtu anayekusudia kwenda kuvunja duka na kupora mali, kabla ya kufanya hivyo akavunjika mgongo au akatiwa upofu machoni ni dhahiri kuwa hawezi kutenda lile alilolikusudia. Hivyo maovu hayatendeki kinyume na Qadar ya Allah(s.w).

## **Tofauti ya Qadar na Qudra**

Mara kwa mara neno “Qadar” hufananishwa katika matumizi na neno “Qudra”. Ambapo neno “Qudra” lina maana ya uwezo na neno “Qadar” lina maana pana zaidi. Lina maana ya mpango (plan) au utaratibu wa mfumo mzima pamoja na umilikaji wake. “Qudra ya Mwenyezi Mungu” (s.w) ni uwezo wa Mwenyezi Mungu(s.w) juu ya kila kitu. Mwenyezi Mungu(s.w) akitaka jambo lolote liwe huwa vile vile anavyotaka pasi na kipingamizi au kizuizi chochote. Ni kwa msingi huu unakuja msemu: “Jitihada za mja hazivunji Qudra ya Mwenyezi Mungu”.

## **Maana Pana ya Qadar**

Qadar ya Mwenyezi Mungu(s.w) ni mpango mzima unaomiliki kupatikana (kutokea), kuwepo na hatimaye kutoweka (kuondoka) viumbe vyote vilivyo hai na visivyo hai mbinguni na ardhini. Ni hakika kuwa Mwenyezi Mungu(s.w) hakuumba mbingu na ardhi na pepo na moto na vyote vilivyomo katika maisha

haya ya ulimwenguni na vyote vitakavyokuwepo katika maisha ya akhera kwa kubahatisha tu bali ni lazima awe ameumba kila kitu kwa lengo maalum na kuliwekea utaratibu (kanuni au sheria) maalum ili kuwezesha kufikia lengo hilo. Ukweli ni kwamba kila kilichomo mbinguni na ardhini na kila kitakachokuwemo huko akhera na kila kitendo na kila tukio linalotokea hapa ulimwenguni limo katika mpango madhubuti wa Mwenyezi Mungu(s.w) na hutokea kwa kufuata bila ya hiari kanuni (sheria) madhubuti alizoziweka Mwenyezi Mungu pamoja na kanuni (Sheria za maumbile) zinazomiliki utekelezaji wake. Hii ndio Qadar ya Mwenyezi Mungu(s.w).

Kwa mfano, ni kawaida kwamba Muhandisi yeyote aliyemjuzi na hodari kabla hajatengeneza chochote kile anachokusudia kutengeneza, ni lazima kwanza akilini mwake awe na picha kamili ya kile anachotaka kutengeneza ili kukidhi haja maalumu. Baada ya kuwa na picha kamili, ambayo mara nyingi atajitahidi kuiwakilisha katika karatasi kwa maandishi na michoro, ni lazima pia awe na picha kamili ya namna atakavyotengeneza kitu hicho, wakati wa kuanza na kumaliza kutengeneza, mahali pakutengenezea kitu hicho, ukubwa na thamani ya kitu hicho. Kama ni muhandisi mweledi zaidi atajaribu hata kukisia muda wa kutumika kitu hicho. Huu ndio utaratibu anaotarajiwa au fuata kila fundi mjuzi na hodari wa kutengeneza vitu, kabla hajaanza kutengeneza chochote anachokitengeneza. Atakapoanza kutengeneza atafuata mpango ule ule aliouchora kichwani mwake mara tu alipojiwa na fikra ya kutengeneza hicho anachokusudia kutengeneza. Tunajua, kwa kuwa mwanadamu ana udhaifu, mkubwa na ujuzi wake ni mdogo sana, mpango wake huu wa awali unaweza ukatofautiana na sura halisi ya kile kilichokusudiwa. Pamoja na hivyo, bado tunaweza kuutafakari mfano huu wa ufundi wa mwanadamu na bado ukaweza kutusaidia kujua na kuingiza akilini mwetu uwezo wa Mwenyezi Mungu katika uumbaji wake na katika kuviendesha viumbe vyake mpaka kufikia lengo la kuumbwa kwao.

Tunafahamu vyema kuwa Mwenyezi Mungu(s.w) ni mjuzi, Mwenye Hekima na Uwezo usio na kikomo. Pia tunafahamu vyema kuwa Yeye Mwenyezi Mungu(s.w) Ndiye Muumbaji wa vyote vilivyomo mbinguni na ardhini na vitakavyokuwemo katika maisha ya Akhera ambayo hatuna shaka nayo. Kwa hiyo, inakubalika akilini mwetu, na ndio hasa ukweli, kuwa Mwenyezi Mungu(s.w) aliye fundi wa mafundi wote, ni lazima uumbaji wake nao kabla ya kuanza uwe umetanguliwa na fikra au haja ya kuumba, kisha mpango wa maumbile yote na utaratibu utakaofuatwa na kila kiumbe ili kufikia lengo. Kwa maana nyingine, akili zetu zinatulazimisha tuone kuwa Mwenyezi Mungu(s.w) kabla ya kuanza kuumba alijua fika yafuatayo:

- Kwa nini aumbe – lengo la kuumba kila alichokiumba.
- Viumbe vyote atakavyoviumba – aina ya viumbe, na idadi ya kila aina ya kiumbe.

- Namna ya kuumbwa kila kiumbe ili kiwe na sifa zitakazo kiwezesha kufikia lengo.
- Mahali na wakati wa kutokea kila kiumbe, muda wa kuishi kwake na wakati wa mwisho wa kuwepo kwake.
- Kanuni na sharia zitakazo miliki kutokea, kuwepo na kutoweka kwa maumbile yote na sharia zitakazotawala matukio yote.

Aya zifuatazo zinatupa picha juu ya Qadar ya Mwenyezi Mungu(s.w):

وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ مِنْ نُطْفَةٍ ثُمَّ جَعَلَكُمْ أَزْوَاجًا وَمَا تَحْمِلُ مِنْ  
أُنْثَىٰ وَلَا تَضَعُ إِلَّا بِعِلْمِهِ وَمَا يُعَمَّرُ مِنْ مُعَمَّرٍ وَلَا يُنْقَصُ مِنْ عُمْرِهِ  
إِلَّا فِي كِتَابٍ إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿١١﴾

“Na Mwenyezi Mungu Amekuumbeni kwa udongo, kisha kwa tone la manii, kisha akakufanyeni wanaume na wanawake. Na mwanamke yeyote hachukui mimba wala hazai ila kwa ilimu yake (Mwenyezi Mungu). Na Mwenye kupewa umri hapewi umri (zaidi) wala hapunguziwi umri wake ila yako katika kitabu (cha Mwenyezi Mungu). Bila shaka haya ni sahali kwa Mwenyezi Mungu” (35:11).

﴿ وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ إِلَّا عَلَى اللَّهِ رِزْقُهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَقْرَهَا  
وَمُسْتَوْدَعَهَا كُلٌّ فِي كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٦﴾

“Na hakuna mnyama yeyote (yaani kiumbe chochote) katika ardhi ila riziki yake iko juu ya Mwenyezi Mungu. Na anajua makao yake ya milele na mahali pake pa kupita tu (napo ni hapa duniani). Yote yamo katika kitabu kinachodhihirisha (kila kitu)” (11:6).

مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي أَنْفُسِكُمْ إِلَّا فِي كِتَابٍ مِنْ  
قَبْلِ أَنْ نَبْرَأَهَا إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٢٢﴾

“Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafasi zenu ila umekwisha andikwa katika kitabu (cha Mwenyezi Mungu) kabla hatujaumba. Kwa yakini hilo ni sahali kwa Mwenyezi Mungu” (57:22).

إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ ﴿٥١﴾

“Kwa hakika tunakiumba kila kitu kwa kiasi” (54:49).

الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَلَمْ يَكُن لَّهُ

شَرِيكٌ فِي الْمَلِكِ وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ فَقَدَرَهُ تَقْدِيرًا ﴿٢٥﴾

“Mwenyezi Mungu ambaye ni wake (peke yake) Ufalme wa mbingu na ardhi wala hakuzaa mtoto wala hana mshirika katika ufalme (wake), na ameumba kila kitu na akakikadiria kipimo (chake)” (25:2).

Aya hizi zinaashiria kuwa mpango mzima wa Mwenyezi Mungu(s.w) umedhibitiwa katika kitabu chake maalumu.

Utekelezaji wa mpango Mkuu wa Mwenyezi Mungu(s.w), hauko mikononi mwa yeyote isipokuwa Yeye mwenyewe pekee. Anaweka sharia madhubuti zinazotawala kila kitu katika hatua ya uumbaji, uendelezaji wa viumbe, na katika yote yatakayotokea kulingana na lengo alilokusudia. Sheria zote za maumbile zinazofanya viumbe viendeleo kama vilivyo au yatokee matukio mbali mbali kama yanavyotokea ziko katika utaratibu wa utekelezaji na mpango mkuu wa Mwenyezi Mungu(s.w). Yale yote yanayomtokea mwanaadamu nje ya uwezo wake hutokea kulingana na Qadar ya Mwenyezi Mungu(s.w). Kwa mfano vipaji alivyonavyo mtu, bahati zinazompitia, fursa anazopata katika mambo mbalimbali, mazuri na mabaya yanayomsibu yote yako katika Qadar ya Mwenyezi Mungu(s.w).

## Maana ya Qudra ya Mwenyezi Mungu(s.w)

“Qudra” ni uwezo wa Mwenyezi Mungu(s.w) usio na mipaka. Mwenyezi Mungu(s.w) anauwezo wa kufanya chochote atakacho. Chochote kile anachotaka kitokee na kiwe, hukipa amri ya “kuwa” na kikawa pale pale na vile vile anavyotaka kama tunavyokumbushwa katika Qur’an:

إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَنْ يَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٣٦﴾

“Hakika amri yake anapotaka chochote (kile kitokee) ni kukiambia: “Kuwa basi mara huwa” (36:82).

وَمَا أَمْرُنَا إِلَّا وَاحِدَةٌ كَلَمْحٍ بِالْبَصَرِ ﴿٥٠﴾

“Na hakukuwa (kupitisha) amri yetu ila ni mara moja (tu hivi) kama kupepesa jicho” (54:50).

..... أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٥٤﴾

“.....Fahamuni kwamba (kwa Mwenyezi Mungu ni kutoa) amri (tu). Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu, Mola wa waliwengu wote” (7:54).

## Kueleweka Vibaya kwa Qadar na Qudra ya Mwenyezi Mungu(s.w)

Kuna baadhi ya Waislamu wanaopotosha maana ya Qadar na Qudra ili kiwe kisingizio cha kutowajibika ipasavyo. Mara nyingi watu hawa hupotosha maana ya Qadar na Qudra katika maeneo yafuatayo:

**Kwanza;** kuacha kutekeleza wajibu wao kwa Mwenyezi Mungu(s.w) kwa kisingizio: “Imeshaandikwa katika kitabu cha Mwenyezi Mungu kuwa hatutatekeleza wajibu huu, sisi tunahatia gani, ni Yeye Mwenyewe aliyetuandikia kutotekeleza wajibu wetu”.

**Pili;** baadhi ya watu wajiitao Waislamu huacha kutekeleza amri za Mwenyezi Mungu(s.w) kama vile kusimamisha swala, kufunga, na kadhalika na kuacha kuwafanyia wema wanaadamu wenzao kwa kisingizio kuwa hawajajaaliwa kufanya hivyo na kuahidi (kwa stihizai) kuwa watatenda wema na kutekeleza amri za Mwenyezi Mungu hapo watakapojaaliwa.

**Tatu;** baadhi ya watu miongoni mwa Waislamu hufanya maovu kwa shangwe wakidai kuwa hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu(s.w) alivyowakadiria tangu hapo awali na wasingeliweza kukiuka Qadar ya Mwenyezi Mungu(s.w).

Vibaya zaidi watu hawa wanaojitua Waislamu huyatolea madai yao haya ushahidi wa aya za Qur’an na Hadith za Mtume(s.a.w). Aya zifuatazo na nyingine za mfano wake zimetumika kupotosha maana ya kuamini Qadar ya Mwenyezi Mungu(s.w) katika maisha ya kila siku:

..... وَمَنْ يُضَلِّ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ هَادٍ ﴿٣٦﴾ وَمَنْ يَهْدِ اللَّهُ فَمَا لَهُ

مِنْ مُضِلٍّ ۗ ﴿٣٧﴾

“.....Na aliyehukumiwa na Mwenyezi Mungu kupotea, basi hana wa kumuongoa. Na ambaye Mwenyezi Mungu amemuongoa hakuna awezaye kumpoteza.....” (39:36-37).

اللَّهُ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ وَيَقْدِرُ لَهُ ۚ إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٢٩﴾

Mwenyezi Mungu Humkunjulia riziki Amtakaye katika waja wake na Humdhikishia Amtakaye. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa kila kitu” (29:62).



لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَإِنْ تُبَدُّوا مَا فِي أَنْفُسِكُمْ أَوْ  
تُخْفُوهُ يُحَاسِبِكُمْ بِهِ اللَّهُ فَيَغْفِرُ لِمَنْ يَشَاءُ وَيُعَذِّبُ مَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ عَلَىٰ

كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٨٤﴾

(*Yote*) vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini ni vya Mwenyezi Mungu. Na kama mkidhihirisha yaliyomo katika nyoyo zenu, au mkiyaficha, Mwenyezi Mungu atakutakeni hisabu ya (*yote*) hayo; kisha amsamehe amtakaye na amuadhibu amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu” (2:284).

Maana ya aya hizi ni kuwa katika yale mambo ambayo mwanaadamu ana hiari nayo, Allah(s.w) humuachia ayafanye kwa uhuru wake. Mwanaadamu akianza kufanya wema, Allah(s.w) humuwezesha kupitia kanuni na sharia za maumbe alizowiweka. Pia akiamua kufanya maovu, Allah(s.w) humuwezesha kufanya maovu hayo kupitia kanuni na sheria za maumbile alizoweka.

Kwa hiyo, kutokana na maelezo haya utaona wazi kuwa uhuru wa kudhamiria au kuamua kutenda mema au maovu uko mikononi mwa mwanaadamu mwenyewe. Pia amepewa mwongozo wa kuyabaini mema na kuacha maovu pindi akiamua kufanya hivyo, na pia amepewa vipaji na uwezo wa kuendea kufanya mabaya pindi ikiamua hivyo. Ni matumizi mazuri au mabaya ya uhuru wake wa kutenda apendavyo, yatakayosababisha ama matunda mazuri hapa duniani na jaza njema huko akhera au matunda maovu hapa duniani na adhabu kali huko akhera. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu(s.w) anavyotufahamisha katika aya nyingi za Qur’an. Hebu tuzingatie hizi zifuatazo:

وَمَا أَصْبَحُكُمْ مِّنْ مُّصِيبَةٍ فِيمَا كَسَبَتْ أَيْدِيكُمْ وَيَعْفُوا عَنْ كَثِيرٍ ﴿٢٨٥﴾

“Ambao malaika waliwafisha hali wamejidhulumu nafsi zao (kwa maasi yao). Basi watasalimu amri (kwa Mwenyezi Mungu waseme:) “Hatukuwa tukifanya uovu wowote”. (Ati wanamdanganya Mwenyezi Mungu. Malaika watawaambia): “Ndiyo, hapana shaka Mwenyezi Mungu anajua sana mliyokuwa mkitenda” (16:28).

مِنْ أَهْتَدَىٰ فَإِنَّمَا يَهْتَدِي لِنَفْسِهِ ۗ وَمَنْ ضَلَّ فَإِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا ۗ وَلَا

تَزُرُّ وَازْرَةً وَزَرَ أُخْرَىٰ ۗ وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ تَبْعَثَ رَسُولًا ﴿٢٨٦﴾

Anayeongoka, basi anaongoka kwa maslahi ya nafsi yake mwenyewe, na anayepotea, basi anapotea kwa khasara (ya nafsi) yake mwenyewe. Wala

*hatabeba mbebaji mzigo wa mwingine. Na sisi si wenye kuwaadhibisha (viumbe) mpaka tuwapelekee Mtume (awafahamishe yaliyo ya haki. Basi wakiyakataa ndipo wanapoangamizwa)” (17:15).*

Kwa ujumla aya hizi zinatufahamisha kuwa kila mja amepewa nafasi sawa ya kutenda wema au uovu yaani lolote atakaloamua kulifanya katika haya mawili litakuwa sahali kwake. Pia iko katika mpango wa Mwenyezi Mungu kuwa matunda ya kutenda mema ni wema hapa duniani na huko akhera, na matunda ya kutenda maovu ni uovu hapa duniani na akhera. Huu ndo utaratibu aliouweka Mwenyezi Mungu na kuubainisha kwa watu kupitia kwa mitume na vitabu vyake. Ameyadhihirisha mema na maovu na kumuacha huru kila mtu afanye ampendavyo.

Kwa hiyo akiamua mtu kuongoka ataongoka na kufaulu katika maisha hapa hapa duniani na akhera na akiamua mtu kupotea atapotea na kuhasirisha maisha yake ya hapa duniani na akhera. Huu ndio ukweli aliousisitiza Mwenyezi Mungu(s.w) katika Suratush-Shamsi:

وَالشَّمْسِ وَضُحَاهَا ﴿١﴾ وَالْقَمَرِ إِذَا تَلَّهَا ﴿٢﴾ وَالنَّهَارِ إِذَا جَلَّهَا ﴿٣﴾  
 وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَاهَا ﴿٤﴾ وَالسَّمَاءِ وَمَا بَنَاهَا ﴿٥﴾ وَالْأَرْضِ وَمَا طَحَاهَا ﴿٦﴾  
 وَنَفْسٍ وَمَا سَوَّاهَا ﴿٧﴾ فَأَلْهَمَهَا فُجُورَهَا وَتَقْوَاهَا ﴿٨﴾ قَدْ أَفْلَحَ ﴿٩﴾  
 مَنْ رَزَقْنَاهَا ﴿١٠﴾ وَقَدْ خَابَ مَنْ دَسَّاهَا ﴿١١﴾

*“Naapa kwa jua na kwa muangaza wake. Na kwa mwezi unapoliandama, na kwa usiku unapolifunika. Na kwa mbingu na kwa aliyezijenga. Na kwa ardhi na kwa Aliyeitandaza. Na kwa nafsi (roho) na Aliyeitengeneza. Kisha akafahamisha uovu wake na wema wake. Bila shaka amejahasirisha aliyeviza (nafsi yake)” (91:1-10).*

Baada ya maelezo haya inaeleweka sasa kuwa si katika Qadar ya; Mwenyezi Mungu(s.w) kuwatiisha waja wake kwa nguvu katika kutenda wema au maovu, bali wanauhuru kamili wa kutenda wapendavyo na Mwenyezi Mungu huwawezesha kufanya hivyo. Lakini bado kuna jambo moja linalotia wasiwasi baadhi ya watu juu ya nguzo hii ya Qadar, ambalo inabidi liwekwe wazi. Jambo hili ni kuhusu ujuzi wa Mwenyezi Mungu(s.w) juu ya kila jambo linalotokea na litakalotokea katika maisha ya dunia na akhera. Watu mara nyingi katika kujiliwaza na kujiridhisha kwa ouvu wanaoufanya husema: “Kabla Mwenyezi Mungu hajaniumba alijua kuwa nitamuasi kwa kufanya kitendo kiovu kadhaa, mahali kadhaa na siku kadhaa. Kama Mwenyezi Mungu alijua kuwa nitafanya kitendo hicho kiovu, bila shaka Yeye ndiye aliyenikadiria

nifanye hivyo. Sasa mimi ningeliwezaje kukiuka Utaratibu wake?” Kwa uoni huu huu wengine husema: “Mwenyezi Mungu anawajua fika watakaolingia Peponi na watakaolingia Motoni, kwa hiyo hata mtu akijitahidi namna gani kama yuko kwenye orodha ya watu wa motoni, yeye ni mtu wa motoni tu na kama mtu yuko kwenye orodha ya watu wa peponi, hata akiasi namna gani yeye atakuwa ni mtu wa peponi tu”. Kwa uoni huo mja hukata tamaa na kuridhika na hali ya kutenda maovu kwa kisingizio cha Qadar. Tatizo hili linakuwepo kutokana na kutozifahamu fika sifa za Mwenyezi Mungu(s.w), khususan sifa yake ya Ujuzi. Hatuna budi kufahamu kuwa Ujuzi wa Mwenyezi Mungu(s.w) hauna mipaka ya wakati au mahali. Yeye alikijua kila kitu kabla hajakiumba. Chochote kile kinachotendeka au kitakachotendeka katika wakati wowote ule katika kona yoyote ile ya dunia na akhera, Yeye ana ujuzi nacho. Hebu turejee Qur’an tuone inavyotukumbusha juu ya Upeo wa Ujuzi wa Mwenyezi Mungu(s.w):

﴿ وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ إِلَّا عَلَى اللَّهِ رِزْقُهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَقَرَّهَا

وَمُسْتَوْدَعَهَا كُلٌّ فِي كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٦﴾

“Na hakuna nyama yoyote (yaani kiumbe chochote) katika ardhi ila riziki yake iko juu ya Mwenyezi Mungu. Na anajua makao yake ya milele na mahali pake pa kupita tu. (Napo ni hapa duniani). Yote yamo katika Kitabu kinachodhihirisha (kila kitu)” (11:6).

﴿ وَعِنْدَهُ مَفَاتِحُ الْغَيْبِ لَا يَعْلَمُهَا إِلَّا هُوَ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ

﴿ وَمَا تَسْقُطُ مِنْ وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٌ فِي ظُلْمَتِ الْأَرْضِ وَلَا رَطْبٌ

وَلَا يَابِسُ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٥٩﴾

“Na ziko kwake (Mwenyezi Mungu tu) funguo za siri; hakuna azijuaye ila Yeye tu. Na anajua yaliyomo barani na baharini. Na halianguki jani ila analijua. Wala (haianguki) punje katika giza la ardhi ila anajua). Wala (hakianguki) kilichorutubika wala kilichoyabisika (ila anakijua) (hapana chochote), ila kimo katika Kitabu kidhihirishacho (kila kitu) jambo” (6:59).

﴿ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ وَمِنَ الْأَرْضِ مِثْلَهُنَّ يَتَنَزَّلُ الْأَمْرُ بَيْنَهُنَّ

﴿ لِيَتَعَمَّرُوا أَنْ اللَّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ وَأَنَّ اللَّهَ قَدْ أَحَاطَ بِكُلِّ شَيْءٍ عِلْمًا ﴿١٧﴾

“Mwenyezi Mungu ni yule ambaye ameziumba mbingu saba, na ardhi kuwa mfano wa hizo. Amri (zake) zinashuka baina yao, ili mujuwe kwamba Mwenyezi Mungu ni mwenye uwezo juu ya kila kitu, na kwamba Mwenyezi Mungu amekizunguka kila kitu kukijua (vilivyo kwa ilimu Yake)” (65:12)

Baada ya kuzingatia aya hizi hapana budi kuelewa mambo muhimu yafuatayo:

**Kwanza:** kama tulivyoona katika maelezo ya nyuma, ni katika Qadar ya Mwenyezi Mungu(s.w) kuwa kila mwanaadamu amepewa uhuru wa kuamua kufanya apendavyo wema au uovu. Hivyo, kila mja katika maisha yake amewekewa njia mbili: Njia ya kutenda wema na njia ya kufanya uovu. Akiamua kutenda wema atakuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Kwa msingi huu pia kila mtu amepangiwa sehemu mbili za kushukia huko akhera Peponi au Motoni. Akiamua kutenda wema katika maisha ya hapa duniani atapata jaza ya pepo huko akhera badala ya moto na akiamua kutenda maovu katika maisha ya hapa duniani atapata adhabu ya moto na ataikosa pepo huko akhera. Tumewekewa wazo hili au ukweli huu na Hadith zifuatazo:

*Abu Hurairah amesimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Hapana yeyote atakayeingia peponi, kwa mema yake ili azidi kushukuru na hapana yeyote atakayeingia motoni mpaka aoneshwe sehemu yake ya peponi kwa mema yake ili azidi kujuta (Bukhari).*

*Anas amesimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Hakika mja anapolazwa kaburuni na jamaa zake wakawa wamerejea nyumbani anasikia sauti ya miguu yao. Malaika wawili huingia na kumkalisha na kumuuliza: Ulikuwa ukisemaje juu ya huyu Muhammad? Kama ni muumini atajibu: "Ninashuhudia kuwa yeye ni Mtumwa wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake". Ataambiwa: Angalia sehemu yako motoni ambayo Mwenyezi Mungu amekubadilishia na sehemu katika pepo... (Bukhari na Muslim).*

**Pili:** lazima tufahamu kuwa Mwenyezi Mungu(s.w) ni mwenye Uoni, Usikivu na Ujuzi usio na mipaka. Hivyo, pamoja na utaratibu wake aliojiwekea kuwa Yeye hatamdhulumu yeyote katika viumbe vyake, hatuna budi kufahamu kuwa ni katika sifa zake kuwaona watu watakaokuwa katika orodha ya motoni na katika orodha ya peponi hata kabla ya kuzaliwa kwao. Ni kumuelewa Mwenyezi Mungu(s.w) kwa ufyny sana, kwa kudhania kuwa Yeye atakuwa katika hali ya kutojua, kama sisi tusivyojua mashukio au kituo cha mwisho cha safari ya maisha ya mja kitakuwa peponi au motoni, mpaka vitabu na mizani vitakapobainisha ni nani wa peponi na ni nani wa motoni. Mwenyezi Mungu(s.w) ametakasika na udhaifu huu. Yeye anajua kila kitu tangu kabla ya mwanzo wake mpaka baada ya mwisho wake. Ujuzi wake haupatikani kwa kusoma au kutafiti bali ni mojawapo ya sifa zake Takatifu za uungu zinazompwekesha na chochote kile. Ujuzi Wake unajitengemea ambapo wengine katika wanaadamu, majini na malaika ujuzi wao hutegemeana na kiasi kile alichowafunza Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, hatuna budi kuelewa kuwa kujua kwa Mwenyezi Mungu(s.w) kuwa mja fulani ataingia motoni, haina maana kuwa Mwenyezi Mungu ndiye aliyemfanya aingie motoni, bali amejiingiza mwenyewe motoni. Kila mmoja anao uhuru kamili wa kuingia peponi au motoni. Lakini ni katika sifa za Mwenyezi Mungu(s.w) kuwa ni

lazima awe mjuzi kamili juu ya wale watakaolingia Peponi na wale watakaolingia Motoni hata kballa ya wakati huo wa kuingia Peponi au Motoni kufika.

## Suala la Uongofu

Baadhi ya watu hujiuliza: Kama sote tuna fursa sawa ya kuchagua kutenda mema au maovu mbona Qur'an yasema Mwenyezi Mungu humuongoza amtakaye na kumuacha kupotea amtakaye?

Uongofu utokao kwa Mwenyezi Mungu uko wa namna mbili: Kwanza uongofu kwa maana ya kumfahamisha mtu njia sahihi ya kufuata. Na pili uongofu kwa maana ya msaada utokao kwa Mwenyezi Mungu.

Uongofu kwa maana ya kwanza, yaani kujulishwa njia ya heri na ya shari, na kujulishwa jambo lipi mtu atende na lipi aliwache, ni uongofu ambao kila mtu anaupata. Na uongofu huo ni wa namna tatu: Fitra yaani kupandikizwa uongofu katika nafsi yake mtu:

وَنَفْسٍ وَمَا سَوَّاهَا ﴿٧﴾ فَأَلْهَمَهَا فُجُورَهَا وَتَقْوَاهَا ﴿٨﴾

*“Na kwa nafsi na aliyeitengeneza. Kisha akaifahamisha uovu wake na wema”*  
(91:7-8).

Na uongofu wa namna ya pili ni kipawa cha akili, ambacho kinaweza kutumika kuisadikisha imani. Na njia ya tatu ni uongofu aliopewa binadamu kwa kupitia Mitume na Vitabu vya Mwenyezi Mungu. Hivyo kila mtu amepata uongofu kutoka kwa Mwenyezi Mungu angalau kwa njia mbili za mwanzo.

Uongofu, kwa maana ya msaada, wanaupata wale tu wanaoamua kuufuata kikweli kweli ule uongofu waliopewa. Tuseme mathalan mtu fulani amepotea njiani au hajui njia ya kwenda mahali fulani akaamua kumuuliza askari. Baada yakumuelekeza mtu yule aliyepotea aseme: Sikuamini, mwongo mkubwa wee! Askari atamwambia: Sawa fuata njia unayojua. Lakini iwapo mtu aliyepotea baada ya kuelekezwa atasema: Ahsante sana kwa kunielekeza nafikiri nitafika ninakokusudia, askari anaweza kumwambia: Subiri kidogo mimi nakwenda huko huko nitakupeleka hadi unapokwenda. Huu ni mfano tu, na Mwenyezi Mungu hawezi kufananishwa na askari au kiumbe yeyote. Kusudio hapa ni kuonesha kuwa watu wanaofuata muongozo wa Mwenyezi Mungu huzidishiwa uongofu:

وَالَّذِينَ أَهْتَدُوا زَادَهُمْ هُدًى وَآتَاهُمْ تَقْوَاهُمْ ﴿١٧﴾

*“Na wale wanaokubali kuongoka anawazidishia uongofu na anawapa (jaza) ya ucha Mungu wao”* (47:17).

ثُمَّ نَقُصُّ عَلَيْكَ نَبَأَهُم بِالْحَقِّ إِنَّهُمْ فِتْيَةٌ ءَامَنُوا بِرَبِّهِمْ وَزِدْنَاهُمْ هُدًى ﴿١٣﴾

“Sisi tunakusimulia habari zao kwa kweli. Hakika wao walikuwa ni vijana waliomuamini Mola wao Nasi tukawazidishia uongofu” (18:13).

Ili kuweka wazi zaidi uongofu wa aina hii wazi zaidi uongofu wa aina hii ya pili hebu tuizingatie kwa makini aya ifuatayo:

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ يَهْدِيهِمْ رَبُّهُم بِإِيمَانِهِمْ ۖ

تَجْرِي مِنْ تَحْتِهِمُ الْأَنْهَارُ فِي جَنَّاتِ النَّعِيمِ ﴿٩﴾

“Hakika wale walioamini na kufanya vitendo vizuri, Mola wao atawaongoza kwa sababu ya imani yao (wende katika Pepo). Itakuwa inapita mito mbele yao, katika Mabustani yenye neema” (10:9).

Kwa nini watapewa Mabustani yenye neema huko akhera? Hii itakuwa ni kwa sababu walifuata Njia Sahihi katika maisha yao katika ulimwengu huu kibinafsi na kijamii na wakaziepuka njia potofu.

Waliwezaje wao kupata katika kila hatua, kila kona na kila njia panda kipambanuzi sahihi cha kutenga jema na baya, kweli na uwongo, haki na batili? Na isitoshe walipata wapi wao nguvu na uwezo wa kudumu kijasiri katika njia Sahihi na kuepuka wakati wote njia potofu? Mola wao ndiye chanzo halisi cha yote hayo. Yeye ndiye aliyewapa uongofu na uwezo wa kudumu kutenda mema hata katika hali ngumu vipi.

Kwa nini Mola wao aliwapa uongofu huo na uwezo kama huo? Aliwapa hayo kwa sababu ya Imani yao.

Ni imani ya namna gani hiyo inayoleta matunda kama hayo? Imani inayoleta matunda kama hayo si ile ya kutamka tu bali imani inayomuongoza mtu katika tabia na mwenendo wake na yenye uwezo wa kujitafsiri kimatendo.

## **Mbona Kuna Uovu na Mateso Duniani?**

Kuna baadhi ya watu ambao huuliza hivi: Iwapo Mwenyezi Mungu anawapenda waja wake mbona anaacha maovu na mateso yaendeleo duniani? Kwa nini asiyaazuie?

**Kwanza:** ni makosa kumhukumu Mwenyezi Mungu ambaye ni Mjuzi wa kila kitu kwa vipimo vya kibinaadamu. Hii ni kwa sababu binadamu mara nyingi anaathiriwa na hisia zake binafsi na maslahi yake katika kufanya maamuzi yake. Kwa mfano tunaamua kuwa kitu fulani ni chema au kibaya? Tuchukue

mifano rahisi. Mvua ikinyesha mkulima aliyepanda anamshukuru Mwenyezi Mungu lakini mtu anayekwenda pikiniki au anayefanya sherehe ya arusi, mvua hasa ikinyesha kutwa nzima ni nuksi kubwa kwake! Au tuseme mtu amekodi teksi anawahi ndege uwanjani kwenda kumzika mama yake. Kwa sababu ya msongamano wa magari barabarani amechelewa kufika uwanjani na hivyo ndege imemwacha na safari kaikosa. Atalaani mtu huyo na kudai kuwa huo ni mkosi mkubwa. Baada ya nusu saa akisikia kuwa ndege ile imeanguka na watu wote wamekufa utamsikia anamshukuru Mungu kwa bahati njema aliyoiipata! Binaadamu hawana haki ya kumuuliza Mwenyezi Mungu kama tunavyofahamishwa katika Qur'an:

﴿ ۞ ﴾ لَا يُسْأَلُ عَمَّا يَفْعَلُ وَهُمْ يُسْأَلُونَ

*“Haulizwi (Mwenyezi Mungu) anayoyafanya lakini wao (viumbe) wataulizwa”  
(21:23).*

Hii haina maana kuwa binaadamu wanakatazwa kujaribu kutafuta hikima ya Mwenyezi Mungu katika kuamrisha au kukataza kwake mambo, La! Kinyume chake wanahimizwa kufanya hivyo. Wanachokatazwa ni kujaribu kumhukumu Mwenyezi Mungu au kuyakataa na kuyapinga yale ambayo hikima yake hawaijui. Hivyo katika hizi jitihada za kujaribu kubahatisha kuona hikima ya kuyaacha maovu na mateso yawepo baadhi ya watu wanasema kuwa lau si kuwepo kwa uovu watu wasingejua nini wema, bila kuwepo maradhi watu wasingejua thamani ya afya na bila ya mauti watu wasingeyathamini maisha. Wengine wanasema hata wadudu wabaya tunaodhani wanawabughudhi binadamu, tunadhani hivyo kwa sababu tu hatujajua thamani yao kwetu.

Jambo la kukumbuka ni kuwa kwa mujibu wa Qur'an binadaamu katika kipindi chote cha maisha yake hapa duniani yupo katika majaribio. Na majaribio hayo yatachukua sura mbali mbali za heri na shari. Na jingine ni kwamba ili mtihani huo uwe na maana yoyote watu lazima wawe na hiari ya uchaguzi. Hii ina maana kuwa watu wanaweza kuchagua uovu pia. Hivyo iwapo Mwenyezi Mungu atawapa watu hiari ya uchaguzi lakini atahakikisha hawachagui kufanya ufisadi na uovu nini maana ya kutoa mtihani? Hii haina maana kuwa baada ya kuumbwa ulimwengu Mwenyezi Mungu ameususa na kuuacha uende vyovyote utakavyokwenda, La! Bali kila kitu kipo katika Qadar yake.

## **Maana Hasa ya Kuamini Qadar ya Mwenyezi Mungu katika Maisha ya kila Siku**

Miongoni mwa Qadar ya Mwenyezi Mungu ni yale yote aliyonayo mwanaadamu ambayo hana mamlaka nayo kabisa, na miongoni mwa hayo ni kuwepo kwake hapa duniani, neema alizotunukiwa, vipaji, fursa na bahati alizonazo. Tunafahamu vyema kuwa mwanaadamu hana chembe ya mamlaka juu ya kuzaliwa kwake, kukua kwake na kufa kwake. Si katika uwezo wa mwanaadamu kuchagua wazazi wa kumzaa, kuchagua nyumba ya kuzaliwa ya kitajiri au ya kifalme, n.k. Wala si katika mamlaka yake kuchagua taifa au nchi atakayotokea. Bali kila mtu amejikuta amezaliwa na wazazi waliomzaa, amejikuta ametokea katika nyumba aliyotokea na amejikuta taifa lake ni hilo alilionalo. Yote haya pamoja na fursa na bahati ambazo humtokea mwanaadamu hana mamlaka nayo na ni katika Qadar ya Mwenyezi Mungu(s.w).

Mgawanyo kati ya wanaadamu wa vipaji na neema nyingine alizoruzukiwa mwanaadamu ni mfano mwingine mzuri wa kuonesha Qadar ya Mwenyezi Mungu(s.w). Vipaji vya mwanaadamu vimetofautiana sana. Wakati wengine wamezaliwa na nguvu na afya, wengine wamezaliwa dhaifu na hubakia na udhaifu huo katika maisha yao yote; ambapo wengine wamezaliwa katika nyumba ya utajiri na kuishi maisha ya kitajiri katika maisha yao yote, wengine wamezaliwa katika umasikini wakakua nao na kufa nao; wengine wamezaliwa na akili na uwezo wa hali ya juu wa kufikiri na kufahamu mambo; ambapo wenigne wamezaliwa hali ya ulemavu wa akili, na kahdalika. Tofauti hizi na nyingi nyinginezo zinanzopatikana kwa wanaadamu zimetokana na mgawanyo wa Mwenyezi Mungu ambao mwanaadamu hana chembe ya mchango. Kwa ujumla vipaji vyote alivyonavyo mwanaadamu vikubwa na vidogo, mgawanyo wake uko katika Qadar ya Mwenyezi Mungu(s.w). Hivyo:

**Kwanza** kuwa fursa, bahati, vipaji na neema zote tulizonazo hatukuzipata kwa uwezo wetu, hatuna budi kutumia vitu hivi kama dhamana kwetu. Kwa maana nyingine Muumini anatakiwa atumie vipaji vyake vyote na neema zote alizoruzukiwa na Mwenyezi Mungu(s.w) pamoja na bahati na fursa zote anazozipata, kwa uzuri ili kumuwezesha kufikia kwa ukamilifu lengo la maisha yake, kwa kufuata utaratibu aliouelekeza Mwenyezi Mungu kupitia kwa Mitume Wake na vitabu vyake. Ni muhimu kila Muumini ajue kuwa neema zote alizotunukiwa na Mwenyezi Mungu(s.w) ikiwa ni pamoja na vipaji, fursa na bahati, amepewa kama kujaribiwa kuwa atakuwa muadilifu na kuzitumia vilivyo iwe ndio shukrani yake kwa Mwenyezi Mungu au atazikhini na kuwa miongoni mwa waliokosa shukrani. Hebu tuzingatie aya zifuatazo:



هَلْ أَتَى عَلَى الْإِنْسَانِ حِينٌ مِّنَ الدَّهْرِ لَمْ يَكُن شَيْئًا مَّذْكُورًا ﴿١﴾  
 إِنَّا خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِن نُّطْفَةٍ أَمْشَاجٍ نَّبْتَلِيهِ فَجَعَلْنَاهُ سَمِيعًا بَصِيرًا ﴿٢﴾  
 إِنَّا هَدَيْنَاهُ السَّبِيلَ إِمَّا شَاكِرًا وَإِمَّا كَفُورًا ﴿٣﴾

*Hakika ulimpitia binaadamu wakati mrefu katika dahari, hakuwa kitu kinachotajwa. (Binaadamu ndiye kiumbe cha mwisho kuletwa ulimwenguni). Kwa hakika tumemuumba mtu kutokana na mbegu ya uhai iliyochanganyika: (ya mwanamume na mwanamke), ili tumfanyie mtihani (kwa amri zetu na makatazo yetu); kwa hivyo tukamfanya ni mwenye kusikia (na) mwenye kuona. Hakika Sisi Tumemuongoa, (Tumembainishia) njia (zote mbili hizi; kuwa hii ndiyo ya kheri na hii ndiyo ya shari). Basi (mwenyewe tena) atakuwa mwenye shukrani au awe mwenye kukufuru (kukanusha)'' (76:1-3).*

ثُمَّ لَتُسْأَلُنَّ يَوْمَئِذٍ عَنِ النَّعِيمِ ﴿٤﴾

*Kisha kwa hakika mtaulizwa siku hiyo juu ya neema (mlizopewa mlizitumiaje)'' (102:8).*

Hivyo, utaona kuwa Imani hii inamtaka mja atumie kwa juhudi kubwa vipaji vyote, fursa na bahati nzuri alizozipata, pamoja na neema zote kwa ujumla, si kama apendavyo yeye bali kwa kufuata barabara utaratibu aliouweka Mwenyezi Mungu(s.w) na wala si kwa faida yake tu binafsi bali pia kwa faida ya jamii nzima ya wanaadamu. Muumini wa kweli akiwa na vipaji na neema kubwa kuliko wengine hatajivuna, bali ataona kuwa amepewa jukumu kubwa zaidi kwa kuwa atatakiwa atende vizuri na kwa kiwango cha juu zaidi kuliko wale aliowazidi ili aoneshe shukrani zake kwa Mwenyezi Mungu(s.w). Katika Hadith iliyosimuliwa na Bibi Aysha(r.a), tunafahamishwa kwamba Mtume(s.a.w), kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa daraja na hadhi kubwa aliyopewa kuliko wanaadamu wote, alikuwa akisimama usiku katika swala mpaka miguu yake ilikuwa inavimba na alikuwa akitenda wema kuliko yeyote yule. Bibi Aysha alipomsihi kwa nini anasimama sana kwenye swala mpaka miguu ivimbe na huku ameshasamehewa dhambi zake zote za nyuma na za baadaye Mtume(s.a.w) alijibu:

*“Je, nisiwe mja mwenye kushukuru?”*

**Pili**, kwa upande mwingine, muumini wa kweli, atakapokuwa ametunukiwa vipaji vidogo, fursa finyu na chache, bahati mbaya na riziki haba, hatalalama na kukata tamaa bali ataridhika na alichopewa na pia atamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumpangia majukumu madogo anayoweza kuyabeba kwani

huenda angalipangiwa majukumu makubwa zaidi au angelikabidhiwa dhamana kubwa zaidi ya hizo alizonazo, angelishindwa na kufeli mtihani wake. Muumini huyu anafahamu fika kuwa kila alilolipanga Mwenyezi Mungu ndilo linalosadifu ukweli wa maumbile na ndio pekee linaloleta amani na ustawi katika jamii na katika mwenendo wa maumbile kwa ujumla. Hivyo, waumini wa kweli wa Qadar ya Mwenyezi Mungu hawatajivuna na kuwa na kiburi kutokana na vipaji vikubwa walivyonavyo na wala wale wenye vipaji vidogo hawatanyongeka na kushikwa na donge la chuki na husuda moyoni mwao. Kinyume chake, wale wasiomuamini Mwenyezi Mungu na Qadar yake, wakipewa vipaji vikubwa hutakabari na kuona wamevipata kwa ujanja wao na jitihada yao. Huwakandamiza wanyonge badala ya kuwahurumia na kuwasaidia. Wenye vipaji vidogo hujidhalilisha kwa wengine, nyoyo zao huwa na kutu ya chuki na husuda juu ya wale aliowaneemesha Mwenyezi Mungu na humuona Mwenyezi Mungu ni mwenye upendeleo na mwenye kuwasahau baadhi ya waja wake.

**Tatu**, muumini wa kweli ni yule ambaye atajitahidi kutumia vipaji vyake vyote, fursa na bahati zake zote kwa jitihada zote kwa kadri ya uwezo wake wote, kisha matunda ya jitihada hizo ayategemeze kwa Mwenyezi Mungu(s.w). Zikitoa matunda mazuri hatafurahi kupita kiasi, bali atakuwa na furaha ya kawaida ikiambatana na kumshukuru Mwenyezi Mungu sana kwa kusali sunna ya shukra, kutoa sadaqa na kuzidisha kufanya wema kwa wanaadamu wenziwe. Juhudi zake zikitoa matunda dhaifu yasiyotarajiwa, hatakata tamaa akawa ni mwenye kusononeka, mwenye kuchanganyikiwa na mwenye kushindwa katika maisha bali ataridhika na matunda hayo na ataona ndio haki aliyoikadiria Mwenyezi Mungu ambayo ndiyo yenye manufaa naye. Atasema; *“Al-hamdulillah ‘Alaa Kullihaali”*.

**Nne**, Pia, miongoni mwa Qadar ya Mwenyezi Mungu ni matukio yote yanayotokea nje ya uwezo wa mwanaadamu. Kama mwanaadamu asivyo na uhuru wa kuzaliwa kwake ndivyo asivyo na uhuru wa kufa kwake. Ajali zote zinazomtokea mwanaadamu hana mamlaka nazo. Japo mwanaadamu amepewa uwezo wa kusababisha ajali au maradhi kutokea, hana uwezo wa kuifanya ajali itokee nje ya utaratibu aliouweka Mwenyezi Mungu(s.w). Japo mwanaadamu amepewa uwezo wa kusababisha kifo cha mtu, mtu hawezi kufa mpaka wakati wake wa kufa uwe umefika. Tukikumbuka kisa cha Nabii Ibrahim; moto uliamrisha usimuunguze bali umwe baridi na salama kwake jambo ambalo si kawaida ya ufanyaji kazi wa moto. Hivyo, Nabii Ibrahim hakuungua kwa vile hivyo ilikuwa kinyume na mpango wa Mwenyezi Mungu(s.w). Pia Nabii Ibrahim alipotii amri ya kumchinja mwanawe, kisu kilichokuwa kikali sana hakikumchinja ambapo kisu hicho hicho kiiweza kumchinja kondoo. Hivyo Nabii Ismail(a.s) hakuchinjika kwa vile hiyo ilikuwa kinyume na Qadar ya Mwenyezi Mungu(s.w). Kwa ujumla yote yanayomtokea mwanaadamu, nje ya mamlaka yake, yawe ya kufurahisha au kuhuzunisha ni katika mpango madhubuti aliouweka Mwenyezi Mungu(s.w) kabla ya kuumba. Rejea Qur’an katika aya zifuatazo:

وَأَنَّهُ هُوَ أَضْحَكَ وَأَبْكَى ﴿٤٣﴾

“Na kwa Yeye ndiye anayeleta ya kufurahisha na ya kuliza” (53:43).

لَخُنٌ قَدَرْنَا بَيْنَكُمْ الْمَوْتَ وَمَا لَخُنٌ بِمَسْبُوقِينَ ﴿٤٤﴾

“Sisi Tumekuwekeeni mauti; basi hatutashindwa (kukufufueni wala)” (56:60).

يَغْفِرْ لَكُمْ مِّنْ ذُنُوبِكُمْ وَيُؤَخِّرْكُمْ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ۚ إِنَّ أَجَلَ اللَّهِ إِذَا جَاءَ

لَا يُؤَخَّرُ ۗ لَوْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٤٥﴾

“Atakusameheni madhambi yenu na atakuahirisheni (bila ya balaa) mpaka muda uliowekwa. Hakika ijapo ajali tokayo kwa Mwenyezi Mungu haizuiliki laiti mngejua” (71:4).

وَمَا أَصَابَكُمْ مِّنْ مُّصِيبَةٍ فِيمَا كَسَبَتْ أَيْدِيكُمْ وَيَعْفُوا عَنْ كَثِيرٍ ﴿٤٦﴾

“Na misiba inayokupateni ni kwa sababu ya vitendo vya mikono yenu, na (juu ya hivi Mwenyezi Mungu) anasamehe mengi” (42:30).

Kwa ujumla aya hizi zimetufahamisha kuwa ajali haina kinga, ikiwa itokee ni lazima itatokea kama alivyokadiria Mwenyezi Mungu(s.w). Kwa hiyo wajibu wa muumini wa kweli ni kujitahidi kufanya kila analoliweza kwa kufuata utaratibu anaoridhia Mwenyezi Mungu(s.w) na kuridhika na matokeo ya mwisho yatakayotokea. Kwa mfano, muumini atajitahidi kufanya kazi kwa upeo wa juhudi na maarifa yake na kisha mamtokeo ya matunda ya kazi yake amuachie Mwenyezi Mungu(s.w) na chochote atakachokipata, kikubwa au kidogo aone kuwa ndicho kiasi alichokadiriwa na Mwenyezi Mungu(s.w). Kwa upande mwingine muumini anatakiwa ajitahidi kujitahadhari na magonjwa,, ajali, na kadhalika. Baada ya jitihada hizi atakapotokewa na ajali au msiba wowote ni lazima aelewe kuwa umetokea kwa Qadar ya Mwenyezi Mungu na hapana yeyote wa kuweza kuzuia ajali hiyo kutokea isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake.

Imani hii humfanya muumini awe mvumilivu na mwenye subira juu ya matatizo yote yatakayomsibu akijua kuwa hapana lolote linaloweza kutokea nje ya mpango na utaratibu wa Mwenyezi Mungu(s.w). Bali Muumini atajitahidi mno asiwe ndiye sababu ya tukio hilo. Kwa mfano, japo njaa hutokea kama alivyopanga mwenyezi mungu, uvivu wako wa kutofanya kazi kwa juhudi na maarifa, utahesabiwa kwa hilo. Pia japo kila mtu amepangiwa ajali yake na hana uwezo wa kuiepa, mwenye kusababisha ajali hiyo kwa uzembe wake, atakuwa makosani. Ni vyema tusimalize kabla ya kuzingatia Hadithi zifuatazo:

*Abu Hurairah(r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Muumini mwenye nguvu mbele ya Mwenyezi Mungu(s.w) ni bora kuliko muumini dhaifu lakini wote ni wazuri. Kitumainie kile kitakacho kunufaisha na utake msaada wa Mwenyezi Mungu na usikate tamaa. Na ukifikwa na janga (bahati mbaya) lolote usiseme: Ningelifanya hili ingalikuwa hivi na hivi lakini sema: Hii ni Qadar ya Mwenyezi Mungu (Mwenyezi Mungu amekadiria iwe hivyo), amefanya kama atakavyo”, ili usije ukakaribisha vitendo vya shetani. (Muslim).*

*Suhaib(r.a), amesimulia kuwa Mtume(s.a.w) amesema; Kwa Muumini kila hali au kila jambo linalomtokea huwa ni zuri kwake jambo ambalo halipatikani kwa yeyote asiyekuwa Muumini. Akiwa katika wasaa humshukuru Mwenyezi Mungu na hilo ni jambo zuri kwake; na akiwa katika dhiki, husubiri na hilo ni zuri kwake. (Muslim).*

Funzo kubwa tunalolipata hapa ni kwamba kila jambo linalotokea nje ya uwezo na jitihada za binaadamu limetokea kwa Qadar ya Mwenyezi Mungu na Muumini wa kweli hulipokea kwa moyo mkunjufu lolote zuri au baya litakalomfika kwani yote ni kheri kwake. Akifikwa na zuri humshukuru Mwenyezi Mungu jambo ambalo humzidishia imani na ithibati katika kutenda wema. Mwenyezi Mungu(s.w) amesema:

وَإِذْ تَأَذَّنَ رَبُّكُمْ لَئِن شَكَرْتُمْ لَأَزِيدَنَّكُمْ ..... ﴿٧﴾

*Na (kumbukeni) alipotangaza Mola wenu (kuwa) “Kama mkishukuru, nitakuzidishieni...” (14:7).*

Pia akifikwa na baya husubiri. Kitendo cha kusubiri kina matokeo mazuri na kina ujira mkubwa mbele ya Mwenyezi Mungu(s.w).

..... إِنَّمَا يُوفَّى الصَّابِرُونَ أَجْرَهُمْ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿١٠﴾

*“...Na bila shaka wafanyao subira watapewa ujira wao pasina hisabu” (39:10).*

وَلَنَبْلُوَنَّكُمْ بِشَيْءٍ مِّنَ الْخَوْفِ وَالْجُوعِ وَنَقْصٍ مِّنَ الْأَمْوَالِ وَالْأَنْفُسِ

وَالثَّمَرَاتِ ۗ وَبَشِّرِ الصَّابِرِينَ ﴿١١﴾ الَّذِينَ إِذَا أَصَابَتْهُمُ مُصِيبَةٌ قَالُوا

إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ ﴿١٢﴾

*Na Tutakutieni katika misuko suko wa hofu, njaa, upungufu wa mali na wa watu na wa matunda. Na wapashe habari njema wale wanaosubiri. Ambao uwapatapo msiba husema: “Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake Yeye tutarejea” (2:155-156).*

Hivyo imani ya kweli juu ya Qadar ya Mwenyezi Mungu haina budi kumfikisha muumini katika hali ya kuwa na yakini kuwa heri na shari, zote ziko mikononi mwa Mwenyezi Mungu(s.w). Kwa hiyo kila wakati atajitahidi kutimiza wajibu wake na kumuachia Mwenyezi Mungu(s.w) matokeo. Na kutokana na imani hii hatavunjika moyo na kuanza kulalama ovyo akipata matokeo mabaya wala hatavimba kichwa na kujigamba matokeo yakiwa mazuri. Mwenyezi Mungu(s.w) anasema katika Qur'an:

مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي أَنْفُسِكُمْ إِلَّا فِي كِتَابٍ مِّنْ قَبْلِ أَنْ نَّبْرَأَهَا إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٢٢﴾ لِّكَيْلَا تَأْسَوْا عَلَىٰ مَا فَاتَكُمْ وَلَا تَفْرَحُوا بِمَا آتَاكُمْ ۗ وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ ﴿٢٣﴾

*“Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwisha andikwa katika Kitabu kabla hatujaumba. Kwa yakini hilo ni sahali kwa Mwenyezi Mungu; ili msihuzunike sana juu ya kitu kilichokupatani wala msifurahi sana kwa alichokupeni. Na Mwenyezi Mungu Hampendi kila akivunaye, ajifaharishaye” (57:22-23).*

Mtu anayeamini Qadar na Qudra ya Mwenyezi Mungu(s.w) pamoja na kujua kuwa heri na shari zinatoka kwa Mwenyezi Mungu(s.w), anajua pia kuwa vyote hivyo ni mtihani kwake kutoka kwa Mola wake. Hivyo linalomshughulisha ni kujitahidi awezavyo ili afuzu mtihani huo. Isitoshe kwa kuwa hana malengo ya kilimwengu, hayapimi mafanikio yake au kushindwa kwake kwa kupata au kukosa ushindi wa kilimwengu. Kinyume chake, lengo pekee lililo mbele yake ni kujitolea maisha yake na mali yake katika njia ya Mwenyezi Mungu na hupima mafanikio au kushindwa kwa juhudi zake kulingana na kiwango alichofikia katika kutekeleza wajibu wake. Anaamini amefuzu kwa Rehema ya Mwenyezi Mungu(s.w), hata kama hajapata chochote kulingana na kipimo cha mafanikio ya ulimwengu, kwani ana yakini kuwa Mola wake ambaye kwa ajili yake amejitolea maisha yake na mali yake hataacha kumlipa malipo mema kwa juhudi zake.

Mtu anayeamini Qadar ya Mwenyezi Mungu(s.w) siku zote huyaweka mategemeo yake yote kwa Mwenyezi Mungu(s.w), ambaye ndiye mhibiti wa rasilimali zote. Na hivyo huendelea kutimiza wajibu wake hata wakati anapokabiliwa na mazingira magumu kwa moyo ule ule wa ujasiri na subira. Hii ni kwa sababu anayakinisha maneno ya Mwenyezi Mungu aliposema katika Qur'an:

قُلْ لَنْ يُصِيبَنَا إِلَّا مَا كَتَبَ اللَّهُ لَنَا هُوَ مَوْلَانَا وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ

الْمُؤْمِنُونَ ﴿١٠٦﴾

*Sema: Halitatusibu ila Alilotuandikia Mwenyezi Mungu. Yeye ni Mola wetu. Basi Waislamu na wamtegemee Mwenyezi Mungu tu” (9:51).*

## TOFAUTI YA UISLAMU NA DINI NYINGINE

Katika masomo ya nyuma tumejifunza kuwa mwanaadamu hana hiari ya kuishi bila ya kufuata Dini moja au nyingine. Pia tumejifunza kuwa Dini zimegawanyika katika makundi makubwa mawili:

- (i) Dini ya Mwenyezi Mungu inayojulikana kwa jina la **Uislamu**, na
- (ii) Dini walizoziunda wanaadamu ambazo nazo zimegawanyika katika makundi makubwa matatu yafuatayo:
  - (a) Dini ya Ukafiri
  - (b) Dini ya Ushirikina na
  - (c) Dini ya Utawa

Pamoja na kuwepo kwa Dini nyingi Qur'an inabainisha wazi kuwa:

إِنَّ الدِّينَ عِنْدَ اللَّهِ الْإِسْلَامُ ..... ﴿١٠٧﴾

*“Bila shaka Dini (ya haki) mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu...” (3:19).*

وَمَنْ يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِينًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿١٠٨﴾

*“Na anayetaka Dini isiyokuwa na Kiislamu basi haitakubaliwa kwake. Naye akhera atakuwa katika wenye khasara (kubwa kabisa)” (3:85).*

Pia Mwenyezi Mungu anasisitiza kuwa ameleta Uislamu ili uwe juu ya dini nyingine zote katika kumboresha na kumnufaisha mwanaadamu kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِأَهْدَىٰ دِينٍ لِّحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ

وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿١٠٩﴾

*“Yeye (Mwenyezi Mungu) ndiye aliyemtuma Mtume wake kwa uongofu na kwa Dini ya haki ili kuifanya ishinde dini zote ijapokuwa makafiri watachukia” (61:9).*

Ili tuelewe vema ubora wa Uislamu juu ya dini nyingine kuu tatu tulizozitaja, katika somo hili tutafanya mawili yafuatayo:

- (i) Tutaichunguza itikadi ya kila dini na madhara yake katika maisha ya jamii.
- (ii) Tutaangalia ubora na matunda ya kusimama uislamu katika jamii.

## Ukafiri na Madhara yake katika Jamii

Kafiri ni jina linalo tokana na neno, “**Kufr**” lenye maana ya kukana au kufunika ukweli uliodhahiri. Kukana huku kunaweza kuwa kwa maneno, maandishi au vitendo. Kwa hiyo, dini ya ukafiri ni njia ya maisha iliyofumwa katika msingi wa kuukana ukweli wa kuwepo Mwenyezi Mungu Muumba pamoja na kuukana mwongozo wake aliomshushia mwanaadamu ili umuongoze katika njia iliyonyooka. Kwa hiyo, kwa mtazamo wa Uislamu hata kama kinadharia mtu atakubali kuwepo Mwenyezi Mungu Muumba, lakini katika utendaji wake akakataa kufuata mwongozo wa Mwenyezi Mungu bado atahesabiwa kuwa ni Kafiri kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

..... وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ ﴿٥٤﴾

“.....Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu basi hao ndio makafiri” (5:44).

## Itikadi ya Ukafiri

Makafiri wakanao kuwepo kwa Mwenyezi Mungu Muumba na Mmilik wa Ulimwengu na vyote vilivyomo wamejenga nadharia yao ya maisha juu ya itikadi yenye vipengele vifuatavyo:

- (i) Hakuna Muumba wa Ulimwengu na vyote vilivyomo. Bali ulimwengu pamoja na mwanaadamu vimeibuka vyenyewe kwa bahati (*chance creation*) nasibu.
- (ii) Kwa kuwa ulimwengu na vyote vilivyomo vimetokea kwa bahati tu hapa kusudio au lengo lolote la maumbile. Hali kadhalika mwanaadamu wenyewe hana lengo lolote analotakiwa alifikie ili kukidhi haja ya kuwepo kwake hapa duniani na hapana yeyote aliye juu yake atakayemuuliza namna alivyoendesha maisha yake hapa ulimwenguni. Kwa maana nyingine, lengo la maisha ya mwanaadamu ni kule kuishi kwenyewe. Kwa hiyo kupata mahitaji ya maisha na kuendeleza maisha ndio lengo.
- (iii) Kwa kuwa hakuna Muumba wa ulimwengu, mwanaadamu anajukumu la kuunda utaratibu wa maisha atakaoufuata ili kumuwezesha kuishi kwa furaha na amani. Utaratibu huu wa maisha kuunda kwa kutumia ujuzi alionao, mazingira yake, uzoefu alioupata kutokana na historia yake na kutokana na msukumo wa mahitaji ya kimwili na msukumo wa matashi ya nafsi yake.

(iv) Kwa kuwa mwanaadamu ametokea kwa bahati nasibu atatoweka hivyo hivyo na huo utakuwa ndio mwisho wake. Pia ulimwengu utakujatoweka hivyo hivyo na huo utakuwa ndio mwisho wa maumbile. Kwa maana nyingine makafiri wanaitakaidi kuwa hapana maisha mengine baada ya maisha haya ya hapa duniani.

Ni wazi kuwa itikadi ya ukafiri imejengwa juu ya misingi ya uwongo inayopingana na ukweli wa maumbile. Hivyo, Dini ya Ukafiri haiwezi kuwa dini sahihi yenye kutarajiwa kumnufaisha mwanaadamu.

## Madhara ya Ukafiri katika Jamii

Ukafiri hauna manufaa yoyote katika jamii ila hasara tupu. Mwenyezi Mungu anaupigia mfano ukafiri katika jamii katika aya ifuatayo:

وَمَثَلُ كَلِمَةٍ خَبِيثَةٍ كَشَجَرَةٍ خَبِيثَةٍ اجْتُثَّتْ مِنْ فَوْقِ الْأَرْضِ مَا لَهَا مِنْ قَرَارٍ ﴿٦٦﴾

*“Na mfano wa neno baya (itikadi ya uwongo) ni kama mti mbaya ambao umeng’olewa katika ardhi, hauna uimara” (14:26).*

Aya hii inatufahamisha kuwa pamoja na ukafiri kuwa dini dhaifu isiyoweza kuushinda Uislamu iwapo Waislamu watasimama kuusimamisha, bado ni mti mbaya unaotoa matunda mabaya (yenye sumu) yenye kuidhuru jamii. Madhara ya ukafiri katika jamii ni mengi sana, bali tuzingatie hali halisi tunayoiona katika jamii ya kikafiri hivi leo. Katika jamii ya kikafiri hakuna wema au huduma ya bure. Kila mtenda wema kwa wengine hutarajia kupata maliop ya wema huo kwa njia moja au nyingine hapa hapa duniani kwa vile hatarajii malipo ya akhera. Maskini na wanyonge hawapati misaada na huruma kutoka kwa matajiri kwa kuwa hawana cha kulipa. Kinyume chake katika jamii ya kikafiri masikini na wanyonge hukandamizwa na kudhulumiwa haki zao na matajiri na wenye hadhi.

Makafiri kwa kuwa wanaitakidi kuwa lengo la maisha yao ni kustarehe hapa duniani hutumia njia yoyote itakayowawezesha kufikia lengo hilo. Ukandamizaji na dhulma iliyotapakaa ulimwenguni kote ni matunda ya ukafiri, mauaji na vita vilivyotapakaa kote duniani na ushindani wa kutegeneza silaha hivi leo ni matunda mengine ya ukafiri. Hivi leo kila mwenye nguvu ndiye mwenye sauti katika jamii. Mataifa yenye nguvu huyanyonya na kuyapeleka puta mataifa madogo. Haya na Utu ni maadili yaliyotoweka kabisa katika jamii za kikafiri. Watu hutembea barabarani nusu uchi na huko ulaya na Marekani vimeundwa vilabu ambapo wanawake na wanaume hukaa pamoja wakiwa uchi wa mnyama (*Nudism*). Zimezushwa programu na kampeni za kuwashawishi wazazi wasizae watoto zaidi ya wanne kwa kuchelea ufukara na kushindwa kuihudumia familia kwa chakula, mavazi na elimu! Zinaa imefanywa ni jambo la kimaendeleo na kushinikizwa kwa vivutio mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuwafundisha watoto



mashuleni, kutumia mipira ya zinaa(kondom). Ulevi wa pombe na madawa ya kulevya umekuwa ndio mtindo wa maisha katika jamii za kikafiri. Kamari, riba na rushwa vimefanywa ndio vitega uchumi vikuu katika jamii. Suala la malezi hivi sasa halina umuhimu wowote kunaendeshwa kampeni za kuwafanya wazazi wasiwajibike kwa malezi ya watoto. Kampeni za *Child abuse* yaani mtoto asikanywe afanye analotaka bila ya kubughudhiwa hivi sasa zimetawala Marekani na Ulaya, matokeo yake watoto wanajiua na kuuana ovyo. Maovu yote haya katika jamii za kikafiri yamepewa majina mazuri ya: “Maendeleo”, “uhuru”, “Haki za binaadamu”, “Demokrasia”, na kadhalika.

Utawala wa kidhalimu kwa jina zuri la “Demokrasia” umekuwa ndio mtindo wa siasa za kikafiri. Sera za watawala katika jamii za kikafiri ni zile za mwanasiasa wa Kitaliano, Nicollo Machiavelli ya kumuondoa kwa kumuweka kuzuizini au kumuua yeyote yule atakayeonesha kutoridhika na utawala ulioshika hatamu hata kama wanakiuka haki za raia zao kiasi gani. Katika jamii za kikafiri wenye madaraka huwa watawala na mabwana wa raia badala ya kuwa viongozi na watumishi wa raia. Utaona katika jamii za kikafiri, raia wanyonge ambao ndio wengi hunyonywa na kukandamizwa kisiasa na kiuchumi na kikundi cha watu wachache – watawala na matajiri. Wanapotokea watu kudai haki na uhuru halisi wa raia ulioishia mikononi mwa wachache, hukamatwa na kuadhibiwa na kupachikwa majina mabaya mabaya kama vile wapinga maendeleo, vibaraka wa maadui, magaidi, wachochezi na kadhalika, ili raia wasiwasikilize na kuwasaidia katika kudai haki zao badala yake wawasuse na kuwatenga. Watawala hujipa haki ya kuwatungia wengine sharia na utaratibu wa maisha kwa jina la “Ubunge” kwa manufaa yao. Haya ni baadhi ya matunda machungu ya ukafiri.

## **Ushirikina na Madhara yake katika Jamii**

### ***Itikadi ya Ushirikina***

Ushirikina ni Dini iliyojengwa juu ya imani ya kuwepo miungu yenye kushirikishwa na Mwenyezi Mungu. Miungu hawa walioshirikishwa na Mwenyezi Mungu wamepachikwa uwezo wa kumiliki na kuyaendesha maisha ya mwanaadamu hapa ulimwenguni kwa ujumla. Ushirikina ni itikadi ya kihistoria iliyokongwe sawa na historia ya mwanaadamu. Miungu iliyoshirikishwa na Mwenyezi Mungu ni mingi ikiwa ni pamoja na viumbe visivyoonkana kama vile majini na malaika; viumbe hai kama vile wanyama miti mikubwa na viumbe visivyo hai kama vile jua, mwezi, nyota, milima, mito na maziwa, n.k.

Pia masanamu yaliyofinyangwa kutokana na udongo, chuma, shaba na mengine yalichongwa kutokana na miti au mawe na huabudiwa pamoja na Mwenyezi Mungu. Baada ya kupachikwa majina kama vile Uzza, Manat, Wadd, Suwa’a, Yaghutha, Yauka, Nasra, n.k. (Rejea Qur’an (53:19-23), (71:21-23).

Masanamu haya yanaitakidiwa kuwakilisha watu wacha Mungu katika vizazi vilivyotangulia na kwamba yanauwezo wa kuwakurubisha watu kwa Mwenyezi Mungu kama tunavyojifunza katika Qur'an:

أَلَا لِلَّهِ الدِّينُ الخَالِصُ ۗ وَالَّذِينَ اتَّخَذُوا مِن دُونِهِ أَوْلِيَاءَ مَا  
تَعْبُدُهُمْ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَا إِلَى اللَّهِ زُلْفَى ..... ﴿٣﴾

*Mola wa kuitakidiwa ni Mwenyezi Mungu tu, lakini wale wawafanyao wengine kuwa waungu badala yake (husema:) "Sisi hatuwaabudu hawa ila wapate kutufikisha karibu kabisa na Mwenyezi Mungu....." (39:3).*

Vile vile washirikina wanawafanya Miungu mitume wao na wacha Mungu (viongozi) wao kama tunavyofahamishwa katika Qur'an:

وَقَالَتِ الْيَهُودُ عِزَّىٰرُ بْنُ اللَّهِ ۖ وَقَالَتِ النَّصْرَى الْمَسِيحُ ابْنُ اللَّهِ ۗ  
ذَٰلِكَ قَوْلُهُمْ بِأَفْوَاهِهِمْ يُضَاهِئُونَ قَوْلَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِن قَبْلُ ۗ  
فَتَلَّهُمُ اللَّهُ ۗ أَنَّىٰ يُؤفَكُونَ ﴿٤﴾

*"Na Mayahudi husema: "Uzeiri ni mwana wa Mwenyezi Mungu", na Wakristo wanasema, "Masihi ni mwana wa Mwenyezi Mungu". Haya ndiyo wayasemayo kwa vinywa vyao. Wanayaiga maneno ya wale waliokufuru kabla yao... (ili) Mwenyezi Mungu awaangamize wanageuzwa namna gani hawa" (9:30).*

Pia tunafahamishwa kuwa Mayahudi na Wakristo wanawashirikisha viongozi wao na Mwenyezi Mungu katika aya ifuatayo:

اتَّخَذُوا أَحْبَابَهُمْ وَرُهْبَانَهُمْ أَرْبَابًا مِّن دُونِ اللَّهِ وَالْمَسِيحَ ابْنَ  
مَرْيَمَ وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا إِلَهًا وَاحِدًا ۗ لَّا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ سُبْحٰنَهُ عَمَّا  
يُشْرِكُونَ ﴿٥﴾

*"Wanawafanya wanavyuoni wao na watawa wao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu, na wamemfanya Masihi mwana wa Mariamu (pia Mungu) hali hawakuamrisha isipokuwa kumuabudu Mungu mmoja. Hakuna anayestahiki kuabudiwa ila yeye. Ametakasika na yake wanayomshirikisha nayo" (9:31).*

Hakuna tofauti ya msingi kati ya njia ya maisha iliyoundwa katika misingi ya ukafiri na ile iliyoundwa katika misingi ya ushirikina. Washirikina kinadharia

hukiri kuwepo kwa Mwenyezi Mungu lakini kiutendaji hawafuati mwongozo wake katika kuendesha maisha yao ya kila siku. Huunda miongozo yao ya maisha kwa misingi ya dhana wakiongozwa na matashi ya nafsi zao kama wafanyavyo makafiri.

Mwenyezi Mungu anatutahadharisha juu ya ubaya wa ushirikina kupitia kwa Luqman:

وَإِذْ قَالَ لُقْمَنُ لِأَبْنَيْهِ وَهُوَ يَعِظُهُ يَا بُنَيَّ لَا تُشْرِكْ بِاللَّهِ إِنَّ الشِّرْكَ

لُظْلُمٌ عَظِيمٌ ﴿١٣﴾

*“Na Luqman alipomwambia mwanawe na hali ya kuwa anampa nasaha. Ewe mwanangu! Usimshirikishe Mwenyezi Mungu, maana kushirikisha ndio dhulma kubwa” (31:13).*

Katika aya hii tunajifunza kuwa ushirikina umesababisha **dhulma** kubwa katika jamii. Tufahamu kuwa, anayedhulumiwa si Mwenyezi Mungu kwani yeye ni mtenza nguvu na muweza juu ya kila kitu. Wanaodhulumiwa kutokana na ushirikina ni watu katika jamii za kishirikina kwa namna mbalimbali.

**Kwanza:** Itikadi ya miungu wengi waliopachikwa uwezo wa kumdhuru au kumnufaisha mwanaadamu, imebuniwa na watu wachache katika jamii ili iwe chambo cha kuwanasa watu na kuwanyonya kwa kirahisi. Viongozi wa dini na watawala katika jamii za kishirikina kwa kutumia miungu wa kisanamu na miungu wengine walio shirikishwa na Mwenyezi Mungu, waliwapumbaza raia zao na kuwanyonya na kuwanyanyasa kiasi cha kukidhi matashi yao. Watawala katika jamii za kishirikina walipata chochote walichotaka kutoka kwa raia zao kwa hiari zao. Walipata na mabinti wazuri walipewa kwa hiari na kwa furaha na wenye mabinti. Walipotaka watu watolewe muhanga kwa ajili ya tambiko kwa miungu, watu walitoa watoto wao kwa ridhaa. Watawala katika jamii za kishirikina waliwatungia watu wao sharia kwa ajili tu ya kukidhi matashi yao na viongozi wa madhehebu walishirikiana na watawala kwa kuwahubiria raia kutii sharia za dola ili kupata baraka na fanaka kutoka kwa miungu.

**Pili:** Dhulma nyingine kubwa inayoendelezwa na ushirikina mpaka hivi leo ni kule kumfanya mwanaadamu aamini au afuate mambo kibubusa (kimkumbo-mkumbo) bila ya kudadisi. Wafuasi wa dini mbali mbali za kishirikina hawaruhusiwi kudadisi au kuuliza maswali juu ya mambo muhimu ya kiitikadi. Kwa mfano Wakristo hawaruhusiwi kuhoji juu ya utatu wa Mungu, kusulubiwa kwa Yesu, na uwana wa Mungu wa Yesu. Ushirikina humzuga mwanaadamu asitumie kipawa chake cha kufikiri na uhuru wake wa kuamua kufuata zuri au baya.

**Tatu:** Ushirikina huwafanya watu katika jamii waishi katika maovu na kuacha kutenda mema kwa tamaa ya kupata shufaa mbele ya Mwenyezi Mungu kupitia

kwa waungu wanao washirikisha naye. Kwa mfano, Wakristo wanaitakidi kuwa watapokelewa mbinguni (wataingia peponi) bila ya kusimamisha sharia ya Mwenyezi Mungu hapa Ulimwenguni maadamu wanamuamini Yesu kuwa ni mwana wa Mungu aliyemwaga damu yake msalabani kama kafara ya dhambi zao. Hivyo ushirikina huwapelekea wafuasi wake kudhulumu nafsi zao kiasi kikubwa, kwa kubobea katika maovu huku wakijitumainisha kupata pepo ya Mwenyezi Mungu katika maisha ya akhera.

## Utawa na Madhara yake katika Jamii

Utawa ni hali ya kujitenga na shughuli za dunia au kujiweka katika hali ya kujinyima raha za kimwili na kujiepusha na maudhi ya walimwengu ili kupata wasaa wa kumtumikia Mwenyezi Mungu na kupata radhi zake kwa urahisi.

### Itikadi ya Utawa

Watawa huitakidi kuwa:

- (i) Kuna Muumba mmoja wa Ulimwengu na vyote vilivyomo.
- (ii) Lengo la maisha ya mwanaadamu ni kumtumikia (kumuabudu) Mwenyezi Mungu ili kupata maisha ya furaha ya milele huko akhera.

(iii) Ili kuweza kumuabudu Mwenyezi Mungu katika maisha yote, mwanaadamu mcha-Mungu hanabudi kujitenga na maisha ya dunia kwani kuishi kwa raha hapa ulimwenguni ni ishara ya wazi ya kukosa maisha ya raha ya milele huko akhera. Kwa maana nyingine kila mtu atakavyojitesa kwa kujinyima chakula, kuvaa nguo mbaya na chafu, kutokunywa na kutokula vizuri, kuishi kwenye nyumba mbovu, kutoa au kuolewa, kuishi porini, kusafiri kwa miguu badala ya kutumia vipando vilivyopo, n.k. ndivyo atakavyopata radhi za Mwenyezi Mungu na ni ishara ya kufuzu katika maisha ya akhera.

Utawa ni itikadi kongwe iliyoibuka kila mwanaadamu alipoacha mafundisho sahihi ya mitume wa Mwenyezi Mungu na akaunda utaratibu wake mpya juu ya namna ya kumuabudu Mwenyezi Mungu katika maisha ya kila siku. Watawa, japo huonekana machoni mwa watu wasiojua kuwa ni wacha-Mungu, si wacha-Mungu bali wamemuasi Mwenyezi Mungu kwa kuacha kufuata njia sahihi ya maisha aliyowawekea na badala yake wakabuni njia yao. Katika Qur'an Allah(s.w)anatufahamisha juu ya utawa wa Wakristo kama ifuatavyo:

ثُمَّ قَفَّيْنَا عَلَىٰ آثَرِهِمْ بِرُسُلِنَا وَقَفَّيْنَا بِعِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ وَءَاتَيْنَاهُ  
الْإِنْجِيلَ وَجَعَلْنَا فِي قُلُوبِ الَّذِينَ اتَّبَعُوهُ رَأْفَةً وَرَحْمَةً وَرَهَابِيَّةً

أَبْتَدَعُوهَا مَا كَتَبْنَاهَا عَلَيْهِمْ إِلَّا ابْتِغَاءَ رِضْوَانِ اللَّهِ فَمَا رَعَوْهَا حَقَّ رِعَايَتِهَا فَفَاتِنَا الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنْهُمْ أَجْرَهُمْ وَكَثِيرٌ مِنْهُمْ فَاسِقُونَ ﴿٧٧﴾

*Kisha tukawafuatisha nyuma yao Mitume wetu(wengine) na tukamfuatisha Isa bin Mariamu, na tukampa Injili na Tukauweka upole na rehema katika nyoyo za wale waliomfuata. Na uruhubani(wanaume kutoaoa na wanaweake kutoolewa) wameubuni (wenyewe). Sisi hatukuwaandikia hayo(wenyewe walifanya haya) ili kuitaka radhi ya Mwenyezi Mungu. Lakini hawakuufuata huo uruhubani wao kama inavyotakiwa kuufuata. Basi tukawapa wale walioamini miongoni mwao ujira wao, na wengine wao ni waasi.” (57:27).*

Katika aya hii tunajifunza kuwa Uruhubani (Utawa) si utaratibu wa maisha alioufundisha Mwenyezi Mungu kupitia kwa Mitume wake na vitabu vyake, bali ni utaratibu uliobuniwa na watu wenyewe. Kwa kufuata utaratibu huu waliobuni wenyewe, watawa wamekosa radhi za Mwenyezi Mungu kinyume kabisa na mategemeo yao. Radhi za Mwenyezi Mungu ni kwa wale tu wanaofuata kwa ukamilifu mwongozo wa Mwenyezi Mungu katika maisha yao ya kila siku na wakautawalisha Uislamu katika jamii.

## Madhara ya Utawa katika Jamii

Watawa japo wanamuamini Mwenyezi Mungu hawajatofautiana na makafiri na washirikina katika kuidhulumu na kuidumaza jamii ya mwanaadamu. Watawa wanasaidiana na makafiri na washirikina katika kuidhulumu na kuidumaza jamii kama ifuatavyo:

**Kwanza**,Utawa huwafanya wale waliomuamini Allah(s.w) na siku ya mwisho, waache jukumu la kuamrisha mema na kukataza maovu katika jamii na kuwapa makafiri na washirikina kueneza fisaadi katika ardhi kwa wasaa.

**Pili**,itikadi ya kitawa inawafanya baadhi ya watu waliojitenga maporini, misikini,mahekaluni, na kadhalika. wapewe hadhi ya uungu na kuabudiwa wakiwa hai na baada ya kufa kwao kama Allah(s.w) anavyotutanabaisha:

اتَّخَذُوا أَحْبَابَهُمْ وَرُهْبَانَهُمْ أَرْبَابًا مِنْ دُونِ اللَّهِ وَالْمَسِيحَ ابْنَ مَرْيَمَ وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا إِلَهًا وَاحِدًا ۗ لَّا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۚ سُبْحٰنَهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٧٨﴾

*(Mayahudi na wakristo) wamewafanya wanavyuoni wao na watawa wao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu na (wamemfanya) masihi mwana wa Maryamu(pia mungu), hali hawakuamishwa isipokuwa kumuabdu Mungu mmoja, hakuna anayestakiki kuabudiwa kwa haki ila yeye. Ametakasika na yale wanayomshirikisha nayo. (9:31)*

Hivyo itikadi ya utaa huwatumbukiza waumini kwenye ushirikina.

## **Matunda ya Kusimama kwa Uislamu katika Jamii**

### ***Itikadi ya Uislamu***

Uislamu ni Dini ya Mwenyezi Mungu iliyojengwa juu ya Itikadi ifuatayo:

- (i) Muumba na Mmiliki wa Ulimwengu na vyote vilivyomo ni Mwenyezi Mungu, Mwenye Uwezo, Ujuzi na Hekima juu ya kila kitu.
- (ii) Mwenyezi Mungu amemuumba mwanaadamu ili amuabudu yeye pekee kwa kumtii na kumnyenyekea katika maisha yake yote.
- (iii) Viumbe vyote vilivyomzunguka mwanaadamu katika ulimwengu viko pale kwa ajili ya maisha yake.
- (iv) Mwanaadamu hapa Ulimwenguni ni khalifa wa Mwenyezi Mungu Mwenye dhima ya kusimamisha ufalme wake (Dola yake) kwa kufuata mwongozo wake aliowashushia wanaadamu kupitia kwa Mitume wake na Vitabu vyake. Lakini ni wale tu watakao muamini na kufuata mwongozo wake vilivyo katika maisha yao ya kila siku ndio watakaostahiki kuchukua cheo hiki cha ukhalifa. (Reja Qur'an: 24:55).
- (v) Pana maisha ya akhera ambapo wale watakaomuabudu Mwenyezi Mungu inavyostahiki na wakafanya juhudi katika kusimamisha ufalme wake kwa mali zao na nafsi zao, watazawadiwa maisha ya raha ya milele huko peponi. Na wale watakao takabari na kukataa kumuamini Mwenyezi Mungu na kukataa kumtii kwa kutofuata mwongozo wake na kutosimamisha ufalme wake katika maisha yao ya hapa duniani, watastahiki dhabu kali motoni katika maisha ya akhera.

Kuna manufaa mengine makubwa yanayopatikana katika kufuata Uislamu kama njia yao pekee ya maisha. Tukirejea kitbu cha tatu (3) cha Elimu ya Dini ya Kiislamu shule za Sekondari, utaona matunda ya kusimamisha Tawhiid katika jamii yameorodheshwa kwa urefu. Katika kitabu hiki tutakumbushia kwa muhtasari kuwa Uislamu ukisimama katika jamii:

- (i) Humkomboa mwanaadamu kutokana na utumwa wa aina zote.
- (ii) Humfanya mwanaadamu awe muadilifu katika utendaji wa maisha ya kila siku.

- (iii) Humfanya mwanaadamu awe mpole na mwenye huruma kwa mwanaadamu wenziwe na viumbe wengine.
- (iv) Humfanya mwanaadamu awe mvumilivu na mwenye subira.
- (v) Humfanya mwanaadamu awe jasiri katika kusimamisha Uadlifu katika jamii.
- (vi) Humuwezesha mwanaadamu kuwa na mtazamo mpana na sahihi juu ya maisha.

***Hitimisho:***

Baada ya kuzipitia dini zote kuu nne; Uislamu, Ukafiri, Ushirikina na Utawa, imetudhahirikia kuwa dini zote zilizoundwa na watu zina madhara makubwa yanayomhulikisha mwanaadamu katika maisha ya dunia na akhera. Ni Uislamu pekee ambao uko pale kwa ajili ya kumletea mwanaadamu furaha na amani ya kweli hapa duniani na huko akhera. Ni kwa msingi huu dini hii imeitwa kwa jina la “***Uislamu***” yaani “***Amani***”.



*Sura ya Pili***FIQH**

Katika kitabu hiki fiqh inazingatia mada kuu zifuatazo:

- Ndoa ya Kiislamu
- Talaka na Eda
- Mirathi ya Kiislamu
- Kudhibiti Uzazi
- Hadhi na Haki za Mwanamke katika Jamii
- Misingi ya maadili katika Uislamu
- Utamaduni
- Sharia katika Uislamu
- Uchumi katika Uislamu
- Siasa na uendeshaji wa dola katika Uislamu.

**NDOA YA KIISLAMU***Maana ya Ndoa*

Ndoa, kwa ujumla, ni mkataba wa kuishi pamoja kati ya mume na mke kwa kufuata utaratibu uliowekwa na jamii. Kwa mfano, hapa Tanzania mume na mke watatambulika kuwa wameoana kisheria, pale watakapokuwa wamefunga mkataba wa kuishi pamoja mbele ya Mkuu wa wilaya au mbele ya walii na mashahidi wawili (ndoa ya kiislamu) au mbele ya Padri (Kanisani).

Ndoa ya Kiislamu ni mkataba wa hiari kati ya mume na mke wa kuishi pamoja kwa kuzingatia masharti na taratibu zilizowekwa na sheria ya Kiislamu. Ndoa yoyote iliyofungwa kinyume na masharti na taratibu za Kiislamu, haikubaliki kwa Waislamu.

**Umuhimu wa Ndoa kwa Mtazamo wa Uislamu**

Katika Uislamu ndoa ni jambo lililokokotenzwa sana kama tunavyojifunza katika Hadithi zifuatazo:

Katika Hadithi iliyopokelewa na Imamu Bukhaary, Allah(s.w) amesisitiza kuwa ndoa ni katika sunnah yake na akaongeza kusema:



*“Yeyote anayekataa sunna yangu si pamoja nami” .Anas(r.a) amesema kuwa Mtume wa Allah amesema, “Mtu anapooa huwa amekamilisha nusu ya dini, kisha amche Allah ili akamilishe nusu iliyobakia.” (Bukhaary).*

Ndoa inasisitizwa kutokana na umuhimu wake katika kuijenga na kuiendeleza jamii kwa:

- (i) Kuihifadhi jamii na zinaa.
- (ii) Kuendeleza kizazi kwa utaratibu mzuri.
- (iii) Kujenga mapenzi na huruma katika familia.
- (iv) Kukuza uhusiano na Udugu katika jamii.
- (v) Kukilea kizazi katika maadili mema.
- (vi) Kuwafanya watu wawajibike ipasavyo.

### **(i) Kuhifadhi Jamii na Zinaa**

Matamano ya jimai ni katika maumbile na hayaepukiki. Wanyama pia wameumbwa na matamano haya lakini yanatofautiana sana na yale yaliyopandikizwa kwa mwanadamu. Matamano ya jimai kwa wanyama yanakuja juu wakati maalum, wakati ule tu wanapokuwa tayari kupandikiza mbegu ya uzazi. Matamano ya jimai kwa wanadamu wa kawaida yako pale siku zote, mradi tu vipatikane vishawishi.

Kwa hali hii, endapo mwanadamu ataachiwa huru atosheleze matamano yake ya jimai apendavyo pasina kuwekewa mipaka, kwa vyovyote patatokea madhara makubwa kwake binafsi na kwa jamii nzima. Hivyo Mwenyezi Mungu(s.w) aliyemuumba mwanadamu kwa lengo maalum na anayelifahamu vyema umbile la mwanadamu na matashi yake kuliko yoyote yule, amemuwekea utaratibu madhubuti wa kukidhi haja zake za kimaumbile pasina kuleta kero kwa yeyote katika jamii.

Mwenyezi Mungu(s.w) ameharamisha jimai nje ya ndoa ili kuikinga jamii na madhara makubwa ya zinaa ambayo huidunisha na kuivuruga kwa kiasi kikubwa. Mwenyezi Mungu(s.w) amehalalisha ndoa na kuitilia mkazo kwa wale wenye uwezo kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

..... وَأُحِلَّ لَكُمْ مَا وَرَاءَ ذَلِكَ أَنْ تَبْتَغُوا بِأَمْوَالِكُمْ مُحْصِنِينَ غَيْرَ

مُسْفِحِينَ .

*“..... Na mmehalalishiwa (kuoa wanawake) mighairi ya hawa. Muwatafute kwa mali zenu, kwa kuwaoa bila ya kufanya zinaa.....” (4:24).*

..... وَالْحَصْنَتُ مِنَ الْمُؤْمِنَاتِ وَالْحَصْنَتُ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ  
 مِنْ قَبْلِكُمْ إِذَا آتَيْتُمُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ مُحْصِنِينَ غَيْرَ مُسْفِحِينَ وَلَا  
 مُتَّخِذِي أَخْدَانٍ ..... ﴿٥﴾

“... Na (mmehalalishiwa kuwaoa) wanawake wema wa Kiislamu na wanawake wema katika wale waliopewa kitabu kabla yenu. (Ni halali kuwaoa) mtakapowapa mahari yao mkafanya nao ndoa bila ya kufanya uzinzi wala kuwaweka vimada....” (5:5)

Aya hizi zinatubainishia kuwa ndoa ni ngao ya kujikinga na kitendo kichafu cha zinaa.

Pia Mtume(s.a.w) amesisitiza ndoa kwa lengo hili hili la kujikinga na zinaa kama tunavyojifunza katika hadithi ifuatayo:

*Abdullah bin Mas'ud(r.a) ameeleza kuwa Mtume(s.a.w)amesema:*

“Enyi kongamano la vijana! Na aoe yule aliye na uwezo miongoni mwenu, hakika kuoa kunainamisha macho na asiyeweza kuoa na afunge; hakika funga hukata matamano” (Bukhaary na Muslim).

Pia Mtume(s.a.w) amesema:

*Mmoja wenu atakapomuona mwanamke kisha akamtamani, hana budi kumuendea mkewe kwani ana kile kile aliche nacho huyo mwanamke aliyemtamani. (At-Tirmidh).*

Hadithi hizi zimesisitiza ndoa na kuonesha umuhimu wake katika kuikinga jamii na zinaa. Uislamu kwa kusisitiza ndoa, umefunga njia zote zitakazo wapelekea wanaume na wanawake kutosheleza matamano ya jimai nje ya ndoa. Uislamu umekataza uzinifu wa kila aina na umesisitiza ndoa ili kuwawezesha wanaume na wanawake balebhe, kukidhi matashi ya kimaumbile na wakati huo huo wawe na upendo na ushirikiano wa kudumu ili waweze kuwalea watoto watakopatikana.

### **(ii) Kuendeleza Kizazi cha Mwanadamu kwa Utaratibu Mzuri**

Lengo la ndoa haliishii kwenye kufurahia jimai tu bali kitendo hicho kinakusudiwa kiwe ndio sababu ya kupatikana watoto watakao endeleva kizazi cha mwanadamu. Lengo hili la ndoa linabainishwa wazi katika aya ifuatayo:

فَاطِرُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ جَعَلَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا وَمِنَ الْأَنْعَامِ  
 أَزْوَاجًا يَذُرُّكُمْ فِيهِ لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۗ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ ﴿١١﴾

(Yeye ndiye) Muumba wa mbingu na ardhi. Amekuumbieni wake (zenu) katika jinsi yenu; na wanyama nao (Akawaumbia) wake (zao katika jinsi moja na wao); anakuzidisheni kwa namna hii (ya kuchanganyika dume na jike). Hakuna chochote mfano wake; naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona. (42:11).

Katika aya hii tunafahamishwa kuwa Mwenyezi Mungu(s.w) amewaumba wanadamu na wanyama katika dume na jike ili papatikane kizazi. Katika aya ifuatayo pia lengo hili linabainishwa:

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ أَنْتَقُوا رَبَّكُمْ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا  
 زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَاءً ..... ﴿١١﴾

Enyi watu! Mcheni Mola wenu ambaye amekuumbeni katika nafsi moja. Na akamuumba mkewe katika nafsi ile ile. Na akaeneza wanaume wengi na wanawake kutoka kwa wawili hao..... (4:1).

Wanadamu wamewekewa utaratibu wa ndoa ili wasije wakazaana kiholela bila ya kuchukua jukumu la malezi.

### (iii) Kujenga Mapenzi, Huruma na Ushirikiano katika Familia

Lengo jingine la ndoa ni kuleta utulivu wa moyo kati ya mume na mke na kupandikiza mapenzi, huruma na ushirikiano kati yao na kuendeleza maadili hayo kwa watoto wao.

Lengo hili limebainishwa katika Qur-an kama ifuatavyo:

وَمِنْ آيَاتِهِمْ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلَ  
 بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً وَرَحْمَةً ۗ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٢١﴾

Na katika ishara Zake ni kuwa amekuumbieni wake zenu katika jinsi yenu ili mpate utulivu kwao, naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Bila shaka katika hayo zimo ishara kwa watu wanaofikiri.” (30:21).

..... هُنَّ لِبَاسٍ لَّكُمْ وَأَنْتُمْ لِبَاسٌ لَّهُنَّ ..... ﴿١٧٧﴾

“..... Wao ni nguo kwenu na nyinyi ni nguo kwao...” (2:187).

Pamoja na lengo la kuzaa watoto, aya hizi zinatupa lengo la hali ya juu la ndoa ambalo halipatikani kwa wanyama. Lengo la jimai kwa wanyama ni kuzaana tu kwa kiasi kwamba, baada tu ya kitendo hicho uhusiano wa dume na jike hukatika. Kwa wanadamu, mahusiano ya mume na mke hayapaswi kuishia tu kwenye jimai bali yanatarajiwa yalete utulivu wa nyoyo na fikra kwa wawili hao na kuwa chimbuko la mapenzi, huruma na ushirikiano kati yao. Mume na mke waliofungamana katika misingi ya ndoa, wanatarajiwa kushirikiana kwa mapenzi kiasi cha kuchangia furaha zao na huzuni zao. Ushirikiano kati yao uliofungamana na huruma na mapenzi umepandikizwa ili waweze kulea kizazi kipya kwa maadili yanayotakikana ili kujenga jamii ya makhalifa wa Mwenyezi Mungu.

#### (iv) Kukuza Uhusiano na Udugu katika Jamii

Uhusiano na mshikamano wa kidamu wa familia moja hutanuka pale watoto wa familia moja watakapooana na watoto wa familia nyingine.

Hivyo, mapenzi, huruma na ushirikiano wa udugu hutanuka kutoka kwenye familia moja, kisha kwenye ukoo, kisha kwenye kabila hadi kufikia taifa na mataifa. Sisi sote tu familia ya Adamu na Hawa, hivyo tunapaswa tupendane, tushirikiane na tuhurumiane kama tunavyokumbushwa katika Qur-an:

وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ مِنَ الْمَاءِ بَشَرًا فَجَعَلَهُ نَسَبًا وَصِهْرًا ۗ وَكَانَ رَبُّكَ قَدِيرًا ﴿٥٤﴾

Naye ndiye aliyemuumba mwanadamu kwa maji kisha akamfanyia nasaba (ya damu) na ujamaa wa ndoa. Na Mola wako ni Mwenye uweza (juu ya kila jambo). (25:54)

يَتَّيِبُهَا لِلنَّاسِ ۖ إِنَّهَا خَلَقْنَاكُمْ مِنْ ذَكَرٍ وَأُنثَىٰ ۖ وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا وَقَبَائِلَ

لِتَعَارَفُوا ..... ﴿١٣﴾

Enyi watu! Kwa hakika tumekuumbeni (nyote) kutokana na mwanamume (Adam) na mwanamke (Hawwa) na tumekufanyeni mataifa na makabila (mbali mbali) ili mjuane..... (49:13)

Aya hizi zinatudhihirishia wazi kuwa mahusiano ya ndoa kati ya mume na mke ndio msingi wa jamii ya mwanadamu. Wanadamu wanalijenga familia zao kwa kufuata utaratibu aliouweka Mwenyezi Mungu(s.w) ulimwengu huu ungalikuwa

ni uwanja wa furaha na amani kwani watu wanalihurumiana na kushirikiana kwa mapenzi. Endapo wanaume na wanawake katika jamii hawatoishi maisha ya ndoa na kuamua kutosheleza matashi ya jimai nje ya ndoa, itakuwa ndio chanzo cha vurugu na kuparaganyika kwa jamii. Inatosha kusema kuwa miongoni mwa vurugu na mparaganyiko wa jamii hivi leo inatokana na uzinzi na kubeza maisha ya ndoa.

### **(v) Kukilea Kizazi katika Maadili Mema**

Upendo kwa watoto hauishii tu kwenye kuwapa watoto chakula balini lazima uambatane na malezi yao yote. Malezi ya watoto ni pamoja na kuwaelimisha katika nyanja mbali mbali zinazohusu maisha yao, kuwafunza tabia njema na utaratibu wa maisha anaouridhia Mwenyezi Mungu(s.w). Malezi ya watoto katika familia ni kazi tosha na ya kudumu na mama anatakiwa awe nyumbani kwa kazi hii. Hakuna mtu au taasisi yoyote inayoweza kuifanya kazi hii vizuri badala ya familia. Watoto waliokosa malezi ya kifamilia hata kama watapelekwa kwenye shule za malezi hawawezi kuwa sawa kitabia - upendo, huruma na mwenendo mwema na wale waliopata malezi ya familia.

## **Kumuendeleza Mwanadamu Kiuchumi**

Ndoa ni changamoto kwa waangalizi wa familia, hasa baba. Katika kuilea familia wazazi huwa macho sana katika kutekeleza majukumu yao ili kukidhi mahitaji muhimu ya familia. Mahitaji muhimu ya familia ni pamoja na chakula, mavazi, makazi na gharama za kuwaelimisha watoto.

Baba ambaye ndiye mkuu wa familia hulazimika kufanya kazi kwa juhudi kubwa na Maarifa. Pia wazazi, kwa kuzingatia jukumu la malezi linalo wakabili, huwa macho katika kutumia kile walicho kichuma kwa kuhakikisha kuwa wanatumia mali yao katika mambo ya lazima kwa familia. Ni kwa msingi huu Mwenyezi Mungu(s.w) anatufahamisha katika Qur-an kuwa watoto hawaleti ufakiri kwani kila mtoto amepangiwa riziki yake ambayo hupitia mikononi mwa wazazi kwa njia ya uchumi.

Tunajifunza hili katika aya ifuatayo:

..... وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ مِمَّنْ إِمْلَقِي نَحْنُ نَرْزُقُكُمْ ..... 

.....Wala msiwaue watoto wenu kwa kuhofia umasikini. Sisi tunakupeni riziki nyingi na wao pia.....” (6:151).

## Kuchagua Mchumba

Jambo la kwanza katika kuendea taratibu za kukamilisha ndoa ya Kiislamu ni kuchagua mchumba. Katika kuchagua mchumba, Mtume(s.a.w) anatusasihi katika hadithi ifuatayo:

*Abu Hurairah amesimulia kuwa: Mtume(s.a.w) amesema: “Mwanamke anaolewa kwa vitu vine: kwa utajiri wake, hadhi yake, uzuri wake wa sura na kwa dini yake (Uchaji-Mungu wake). Mchague yule mwenye msimamo mzuri wa dini.....” (Bukhaary na Muslimu)*

Hadithi hii inatufahamisha kuwa vitu vinavyoweza kuwa vichocheo vya mtu kumchagua mchumba ni hivyo vinne vilivyotajwa, lakini Mtume(s.a.w) anatusisitiza tukifanye kichocheo cha dini kiwe namba moja kasha ndio vifuatie hivyo vingine. Ukweli ni kwamba mke mcha-Mungu atatii amri za Allah(s.w) na Mtume wake ambazo zitampelekea kumtii na kumheshimu mumewe. Halikadhalika, mume mcha-Mungu, atamtii Allah(s.w) na huchunga mipaka aliyomuwekea, jambo litakalompelekea kumhurumia mkewe na kumtendea haki inavyostahiki. Hivyo, maisha ya wacha-Mungu hawa katika familia yatakuwa ni yale ya kuhurumiana, kusaidiana na kushirikiana katika kuilea na kuiendeleza familia katika misingi ya ucha-Mungu.

Pia katika suala la kuchagua mchumba Mtume(s.a.w) anazidi kutuasa katika hadithi ifuatayo:

*Abu Hurairah(r.a) amesimulia kuwa Mtume(s.a.w) amesema “Utakapochumbiwa na mwanamume unayempenda kwa dini (Ucha-Mungu wake) basi kubali uolewe naye. Kama hutafanya hivyo patakuwa na huzuni na vurugu katika ulimwengu.*

Msisitizo wa kuwaoa wanawake wacha-Mungu au kuolewa na wanaume wacha-Mungu uko bayana katika Qur-an kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

وَلَا تَنْكِحُوا الْمُشْرِكَةَ حَتَّىٰ تُؤْمِنَ ۚ وَلَا أُمَةٌ مُّؤْمِنَةٌ خَيْرٌ مِّنْ مُّشْرِكَةٍ وَلَا  
 أَعْجَبَتْكُمْ ۗ وَلَا تُنكِحُوا الْمُشْرِكِينَ حَتَّىٰ يُؤْمِنُوا ۚ وَلَعَبْدٌ مُّؤْمِنٌ خَيْرٌ مِّنْ  
 مُّشْرِكٍ وَلَا أَعْجَبَكُمْ ۗ أُولَٰئِكَ يَدْعُونَ إِلَى النَّارِ وَاللَّهُ يَدْعُوا إِلَى الْجَنَّةِ  
 وَالْمَغْفِرَةِ بِإِذْنِهِ ۗ وَيُبَيِّنُ ءَايَاتِهِ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٣٠﴾

Wala msiwaoe wanawake makafiri mpaka waamini. Na mjakazi mwenye kuamini ni bora kuliko muungwana kafiri, hata ingawa kakupendezeni. Wala msiwaoe wanaume makafiri (wanawake Waislamu) mpaka waamini. Na mtumwa mwenye kuamini ni bora kuliko muungwana kafiri, hata akikupendezeni. Hao

*makafiri wanaitia kwenye moto. Na Mwenyezi Mungu anaitia kwenye Pepo na Samahani, kwa amri yake. Naye hueleza aya zake kwa watu ili wapate kukumbuka.” (2:221)*

الْحَيْثُوتُ لِلْحَيْثِينَ وَالْحَيْثُونَ لِلْحَيْثِثِطِ وَالطَّيِّبَتُ لِلطَّيِّبِينَ  
وَالطَّيِّبُونَ لِلطَّيِّبَتِ ..... ﴿٢٢١﴾

*Wanawake wabaya ni wa wanaume wabaya; na wanaume wabaya ni wa wanawake wabaya; na wanawake wema ni wa wanaume wema; na wanaume wema ni wa wanawake wema, .....” (24:26)*

الزَّانِي لَا يَنْكِحُ إِلَّا زَانِيَةً أَوْ مُشْرِكَةً وَالزَّانِيَةُ لَا يَنْكِحُهَا إِلَّا زَانٍ أَوْ  
مُشْرِكٌ وَحَرِّمَ ذَلِكَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٤﴾

*Mwanamume mzinifu hafungamani ila na mwanamke mzinifu au mwanamke mshirikina; na mwanamke mzinifu hafungamani ila na mwanamume mzinifu au mwanamume mshirikina, na hayo yameharamishwa kwa waislamu.” (24:3)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa waislamu si tu wameharamishiwa kuwaoa au kuolewa na makafiri na washirikina bali pia wameharamishiwa kuwaoa au kuolewa na watu wazunifu na waliozama katika maasi mengineyo hata kama watadai kuwa ni waislamu. La muhimu tunalopata hapa ni kuwa waumini wanatakiwa wawe makini katika kuchagua wachumba. Wazingatie wema na ucha-Mungu wa hao wanaowatarajia wawe wake au waume zao.

## Ruhusa ya Kuwaoa Ahlal Kitaab(Mayahudi na Wakristo)

..... وَالْحَصْنَتُ مِنَ الْمُؤْمِنَاتِ وَالْحَصْنَتُ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ  
مَنْ قَبْلِكُمْ إِذَا آتَيْتُمُوهُنَّ أَجُورَهُنَّ مُحْصِنِينَ غَيْرَ مُسْفِحِينَ وَلَا  
مُتَّخِذِي أَخْدَانٍ ..... ﴿٥٠﴾

*“..... Na (mmehalalishiwa kuwaoa) wanawake wema wa Kiislamu na wanawake wema katika wale waliopewa kitabu kabla yenu, mtakapo wapa mahari yao na kufunga nao ndoa, bila ya kufanya uzunifu au kuwaweka vimada.....” (5:5)*

Katika aya hii inatolewa ruhusa kwa wanaume wa Kiislamu kuwaoa wanawake wema wa ah-lal-kitaab ambao ni wanawake wema wa Kiyahudi

na Kikristo kama inavyofafanuliwa katika Qur-an. Pamotokea kutofautiana miongoni mwa wanazuoni wa Kiislamu juu ya ruhusa hii ya kuoa Ahlal-kitaab.

Kulingana na Sheikh Abdallah Saleh Alfarsy katika sherehe ya aya hii (5:5) ameeleza kuwa Mkristo aliyeruhusiwa kuoelwa na Muislamu ni yule tu ambaye ukoo wake umeingia katika dini hiyo kabla ya Uislamu haujaja. Amezidi kusisitiza Sheikh “Ama hawa wanaoitwa Misheni wanaoingia katika Ukristo sasa si halali kuwaoa. ni haram wala ndoa haisihi”.

Kulingana na maoni ya Ibn Abbas(r.a), Muislamu anaweza kumuoa mwanamke wa Ahlal-Kitaabi aliye katika himaya ya Dola ya Kiislamu tu, na haruhusiwi kumuoa mwanamke wa Ahlal-Kitaabi ambaye yuko katika dola ambazo ni maadui wa Dola ya Kiislamu au yuko katika dola za Kikafiri. Tofauti na maoni haya ya Ibn Abbas, Said bin Masayyab na Hassan Basri wanasema kuwa ruhusa hii ya kuwaoa wanawake wema wa Ahlal-Kitabi imetolewa kwa ujumla.

Ileleweke kuwa kuwaoa Ahlal-Kitaabi si amri bali ni ruhusa kutoka kwa Mwenyezi Mungu(s.w) kama ruhusa nyingine zilizotolewa katika Qur-an. Kuitumia ruhusa hii pasina haja na pasina kuzingatia malezi ya watoto katika misingi ya Uislamu ni hatari kubwa. Ikitokea mtu anaishi katika nchi ya Ahlal-Kitabi na hana namna ya kumpata mwanamke mwema wa Kiislamu wa kumuoa, itakuwa kwake vyema kumuoa mwanamke mwema miongoni mwa hao Ahlal-Kitaabi badala ya kufanya uzinifu au kukaa na mwanamke bila ndoa. Ama pale ambapo kuna mabinti wema wa Kiislamu kuna haja gani ya kumuoa binti wa Kikristo?

Jambo la msingi la kusisitiza hapa ni kwamba, aliyetoa ruhusa hii ni Mwenyezi Mungu(s.w), Mjuzi mwenye Hekima. Hivyo, kwa vyovyote vile kuna hekima kubwa katika ruhusa hii.

Ni haramu kwa wanawake wa Kiislamu kuolewa na wanaume Wakristo au Mayahudi. Hivyo kwa mtazamo wa Kiislamu hapana ndoa kati ya mwanamume Mkristo au Myahudi na mwanamke Muislamu. Mtu atakayemwozesha binti yake kwa Mkristo, ajue wazi kuwa ameruhusu zinaa. Vile vile kwa waislamu ni haramu kushiriki katika sherehe za ndoa za namna hiyo kama ilivyo haramu kushiriki katika sherehe zote za kidini za Makafiri, Washirikina na Ahlal-Kitaabi. Kusherehekea pamoja nao, moja kwa moja, ni kuwaunga mkono katika hayo wanayosherehekea kinyume na Mwenyezi Mungu(s.w).

## **Ruhusa ya Wachumba Kuonana Kabla ya Ndoa**

Pamoja na sifa ya ucha-Mungu na wema, tunatakiwa tuwaoe wanawake tunaowapenda kwa sura na umbo; hivyo hivyo wanawake nao wachague wanaume wanaowapenda kwa sura na umbo ili kuzidisha mapenzi na upendo baina yao katika familia. Kwa mantiki hii Allah(s.w) ameruhusu wachumba kuonana kabla ya kufunga ndoa kama tunavyojifunza katika hadithi zifuatazo:



*Abu Hurairah(r.a) ameeleza kuwa mwanamume mmoja alikuja kwa Mtume(s.a.w) akasema: “Ninakusudia kumuoa mwanamke miongoni mwa answari.” Akasema Mtume(s.a.w), “Mwangelie kwanza kwa sababu kuna dosari katika macho ya Answari.” (Muslim).*

*Jabir(r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu(s.w) amesema: “Mmoja wenu atakapochumbia, na akawa na uwezo wa kumtazama yule anayemchumbia na afanye hivyo.” (Bukhaary na Muslim).*

Pamoja na ruhusa hii, bado waislamu wanalazimika kuendelea kuzingatia mipaka ya “Hijaab”, kwamba hawaruhusiwi kukaa faragha au kutembea faragha mwanamke na mwanamume wasio maharimu.

## **Kizazi, Rika na Elimu**

*Sifa nyingine za kuzingatia wakati wa kuchagua mchumba ni kizazi na rika. Kuhusu kizazi Mtume(s.a.w) anatanasihi: “Oeni wale wanawake wenye upendo na huruma, wenye kizazi na hakika watakuwa ni wenye manufaa katika kuongeza idadi yenu miongoni mwa mataifa.” (Abu Daud, Nasai)*

Kwa vijana ambao ndio mara yao ya kwanza kuingia katika maisha ya ndoa, pamoja na kuzingatia sifa za msingi zilizoelezwa, ni vema wakachaguana vijana kwa vijana kama alivyoshauri Mtume(s.a.w) katika hadithi ifuatayo:

*Jabir (r.a) ameeleza: “Tulikuwa na Mtume(s.a.w) katika vita. Tulipokaribia Madina wakati wa kurejea nilisema: “Ee Mtume wa Mwenyezi Mungu, hakika nimeoa hivi karibuni.” Akauliza, “Umeoa”? Nikajibu, “Ndio” Akauliza: “Bikra au mjane?” Nikajibu “Mjane” Akasema, “Kwa nini asiwe bikra ili uweze kucheza naye, naye aweze kucheza nawe.....” (Bukhaary na Muslim)*

Jambo lingine la kuzingatia wakati wa kuchagua mchumba ni Elimu. Kama mume na mke watakuwa na Elimu sahihi juu ya Uislamu na taaluma nyingine za mazingira yao watakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kuwalea watoto wao kimaadili na kitaaluma. Katika kuisitiza hili tuzingatie mchango wa bibi Khadija(r.a) alioutoa katika kuupeleka mbele Uislamu kutokana na utajiri wake na mchango wa bibi ‘Aisha(r.a) alioutoa katika kuufundisha Uislamu kutokana na Elimu yake ya Uislamu.

## **Umaharimu**

Maharimu ni wanawake na wanaume walioharamishwa kuoana kutokana na ukaribu wa nasaba kama ilivyobainishwa katika Qur-an na Sunnah. Wanaume wa Kiislamu wameharamishiwa kuwaoa wanawake wanaobainishwa katika aya zifuatazo:

وَلَا تَبْكُوا مَا نَكَحَ آبَاؤُكُمْ مِنَ النِّسَاءِ إِلَّا مَا قَدْ سَلَفَ إِنَّهُ  
 كَانَ فَحِشَةً وَمَقْتًا وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿٢٢﴾ حُرِّمَتْ عَلَيْكُمْ أُمَّهَاتُكُمْ  
 وَبَنَاتُكُمْ وَأَخَوَاتُكُمْ وَعَمَّاتُكُمْ وَخَالَاتُكُمْ وَبَنَاتُ  
 الْأَخِ وَبَنَاتُ الْأَخْتِ وَأُمَّهَاتُكُمْ وَالنِّسَاءُ اللَّاتِي أَرْضَعْنَكُمْ وَأَخَوَاتُكُمْ مِنَ الرِّضَاعَةِ  
 وَأُمَّهَاتُ نِسَائِكُمْ وَرَبَائِبُكُمُ اللَّاتِي فِي حُجُورِكُمْ مِّنْ نِّسَائِكُمُ اللَّاتِي  
 دَخَلْتُم بِهِنَّ فَإِن لَّمْ تَكُونُوا دَخَلْتُم بِهِنَّ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ  
 وَحَلَائِلُ أَبْنَائِكُمُ الَّذِينَ مِنْ أَصْلَابِكُمْ وَأَن تَجْمَعُوا بَيْنَ  
 الْأَخْتَيْنِ إِلَّا مَا قَدْ سَلَفَ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٢٣﴾

Wala msiwaoe wake waliowaoa baba zenu; isipokuwa yale yaliyokwishapita. Bila shaka jambo hili ni uovu na chukizo na ni njia mbaya (kabisa). Mmeharamishiwa (kuoa) mama zenu, watoto wenu, dada zenu, shangazi zenu, ndugu za mama zenu, watoto wa ndugu zenu, watoto wa dada zenu, na mama zenu waliowanyonyesheni, na dada zenu wa kunyonya, na mama wa wake zenu, na watoto wenu wa kambo walio katika ulinzi wenu, walio zaliwa na wake zenu mliowaingilia. Lakini kama nyinyi hamjawaingilia basi si vibaya kwenu (kuwaoa). Na mmeharamishiwa wake wa watoto wenu waliotoka katika migongo yenu. Na (mmeharamishiwa) kuwaoa madada wawili wakati mmoja, isipokuwa yale yaliyokwisha pita. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kurehemu na Mwenye kusamehe. (4:22-23).

﴿ وَالْمُحْصَنَاتُ مِنَ النِّسَاءِ إِلَّا مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ ۗ كَتَبَ اللَّهُ عَلَيْكُمْ  
 وَأُحِلَّ لَكُمْ مَّا وَرَاءَ ذَٰلِكُمْ ..... ﴾ ﴿٢٤﴾

“Na pia mmeharamishiwa wanawake wenye (waume zao) isipokuwa wale iliyowamiliki mikono yenu ya kuume. Ndiyo Sheria ya Mwenyezi Mungu juu yenu. Na mmehalalishiwa (kuoa wanawake) minghairi ya hawa.....” (4:-24)

Aya hizi zinabainisha wanawake walioharamishwa kuwaoa kuwa ni hawa wafuatao:

1. Mwanamke aliyepata kuolewa na baba yako, (babu yako, baba wa baba yako - wa kuumeni na kikeneni).
2. Mama aliyekuzaa (babu aliyezaa waliokuzaa, mama wa bibi aliyezaa aliokuzaa...).
3. Binti yako uliyemzaa (au binti aliyezaliwa na uliyemzaa...). Pia binti wa kunyonya na mwanao (na kikazi chake...).
4. Dada yako khalisa au wa kwa baba au wa kwa mama.
5. Shangazi yako- dada wa baba yako,(na dada wa babu yako...).
6. Mama mdogo; ndugu wa mama yako (au ndugu wa bibi yako...).
7. Binti wa ndugu yako mwanamume, khalisa au wa kwa baba au kwa mama (na kila aliyezaliwa naye).
8. Binti wa dada yako khalisa au wa kwa baba au kwa mama
9. Mama wa kukunyonyesha (na mama zake wa kumzaa au wa kumnyonyesha).
- 10.Dada yako wa kunyonya naye (aliyenonyeshwa na aliyekunyonyesha).
- 11.Mama yake mkeo wa kumzaa au wa kumnyonyesha (na bibi yake pia wa kumzaa mama yake au wa kumnyonyesha Ama ndugu yake mama yake mkeo yaani mama mdogo wake au shangazi yake wa kuzaliwa au kunyonya; unaweza kumuoa akifa mkeo au utakapomuacha na eda ikaisha.
- 12.Binti wa mkeo uliyemuingilia (na mjukuu wake.....).
- 13.Mke aliyeolewa na mwanao wa kumzaa au wa kunyonyeshwa na mkeo (na kizazi chake); si mke wa mtoto wa kupanga au mtoto wa kulea.
- 14.Mtu na ndugu yake pamoja (au mtu na shangazi yake au mtu na mama yake mdogo pamoja. Akifa mke au ukimuacha na eda ikaisha unaweza kumuoa dada yake, au shangazi yake, au mama yake mdogo.
- 15.Mke wa mtu, bado mwenyewe hajafa wala hajamuacha ni Haram kumuoa. Wanawake hao wameharamishwa kuolewa na wanaume wanaofanana na hawa kwa upande wa kiumeni.

## Mahari

Kabla ya mkataba wa ndoa kupitishwa jambo muhimu ni mwanamke kutaja kiasi cha mahari atakacho penda kupokea kama hidaya au zawadi anayopewa kwa amri ya Mwenyezi Mungu(s.w) kutoka kwa anayemuoa. Uhuru wa kutamka kiasi cha mahari uko kwa muolewaji na bila ya mahari hayo kutolewa taslimu au kwa ahadi ya kulipa baadaye, ndoa haiswihi.

Msisitizo wa mahari unapatikana katika aya zifuatazo:

وَأَتُوا النِّسَاءَ صَدُقَاتِهِنَّ نِحْلَةً فَإِنْ طِبَّنَ لَكُمْ عَنْ شَيْءٍ مِّنْهُ نَفْسًا فَكُلُوهُ

هَيْئًا مَّرِيئًا ﴿٤﴾

*Na wapeni wanawake mahari yao, hali ya kuwa ni hidaya (aliyowapa Mwenyezi Mungu). (Lakini hao wake zenu) wakikupeni kwa radhi ya nafsi zao kitu katika hayo (mahari)basi kuleni kwa furaha na kunufaika. (4:4).*

..... وَالْحَصْنَتُ مِنَ الْمُؤْمِنَاتِ وَالْحَصْنَتُ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا

الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكُمْ إِذَا آتَيْتُمُوهُنَّ أَجُورَهُنَّ مُحْصِنِينَ ..... ﴿٥﴾

*“...Na (mmehalalishiwa kuwaoa) wanawake wema wa Kiislamu na wanawake wema katika wale waliopewa Kitabu kabla yenu,mtakapowapa mahari yao, kafunga nao ndoa...” (5:5)*

Katika aya hizi tunajifunza kuwa kutoa mahari kuwapa wanawake tunaowaoa ni jambo la lazima aliloliamrisha Mwenyezi Mungu(s.w), lakini wenye kuolewa kwa hiari yao wenyewe, wakiamua kuyasamehe mahari hayo au kuyapunguza hata baada ya kutaja, hapana ubaya wowote bali ni jambo zuri pia lenye kuzidisha mapenzi baina ya mume na mke. Pia mume anaweza kukopesha mahari na mkewe akaja kumlipa baadaye.

Lakini kulingana na hadithi ya Mtume(s.a.w) mtu akimlaghai mwanamke kuwa atamlipa mahari hapo baadaye ili akubali wafunge naye ndoa na huku ana nia ya kutomlipa, basi hiyo ndoa haitosihika na huyo mwanamume atahesabiwa kuwa anakaa kimada na huyo mwanamke mbele ya Mwenyezi Mungu(s.w). Mahari ndiyo inayomuhlalishia mume tendo la ndoa kwa mkewe kama tunavyojifunza katika hadithi:

*Uqbah bin Amir(r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu(s.w) amesema: Jambo la msingi katika ndoa ni kwamba utimize kwanza kutoa kile kilichofanya sehemu za siri (za mwanamke) kuwa halali (kwako). (Bukhaary na Muslim).*

## Kiasi Gani Kinachojuzu Kutolewa Mahari?

Hapana kiwango maalum cha mahari kilichowekwa na Sheria ya Kiislamu. Mahari ni haki ya mwanamke mwenye kuolewa na ndiye pekee mwenye uhuru kamili wa kutaja kiasi cha mahari anachokitaka. Akipenda anaweza kudai mrundi wa dhahabu na fedha (Qur-an: 4:20), au akitaka anaweza kupokea kiasi kidogo sana cha mali kama vile shilingi 1/- au chini zaidi kuliko hivyo au akitaka anaweza akasamehe asitake kitu chochote ila kauli nzuri tu.

Lakini tunashauriwa katika Qur-an kuwa mtoaji mahari na mpokeaji mahari waangaliane hali. Kama hali ya mtoaji ni nzuri, ni vyema azidishe mahari kuliko kile kiasi kilichotajwa iwapo ana uwezo huo. Na mpokeaji wa mahari, endapo ataona hali ya mtoaji si nzuri kiuchumi, basi ampunguzie mahari na apokee kiasi kidogo zaidi ya kile alichokitaja mwanzoni. Huku kuangaliana hali kunazidisha mapenzi na huruma baina ya mume na mke.

Pamoja na kuwa mahari hayana kiwango maalum kilichowekwa, inashauriwa yasiwe ya juu sana kiasi cha kuifanya ndoa kuwa jambogumu na kurahisisha uzinifu katika jamii. Hebu tuusikilize ushauri wa Umar bin Khattab(r.a) (Khalifa wa Pili wa Mtume(s.a.w) ambaye amesema:

*‘‘Kuweni waangalifu msifanye mahari ghali. Ingelikuwa kufanya hivyo ni jambo zuri la kumpelekea mtu kwenye ucha-Mungu, Mtume(s.a.w) angelikuwa wa kwanza katika jambo hilo. Sikumbuki kumuona Mtume(s.a.w) katika kumuoa yeyote katika wake zake au katika kuwaoza yeyote katika binti zake kwa zaidi ya Wakia 12.5 (kumi na mbili na nusu) ambazo ni sawa na Dirham 500’’.*

Pia katika hadithi iliyosimuliwa na Jabir(r.a) Mtume(s.a.w) amesema:

*Atakayetoa viganja viwili vya tende au shairi kama mahari ya mkewe (naye akaridhia) atakuwa ameufanya uchi wa mkewe uwe halali kwake. (Abu Daud).*

## **Je, Mahari Inashusha Hadhi ya Mwanamke?**

Kama tulivyojifunza katika Qur-an (4:4), mahari ni hidaya kutoka kwa Mwenyezi Mungu(s.w). Kwa maana nyingine, mahari ni mali anayoitoa mwanamume kumpa mwanamke anayetaka kumuoa kwa ajili ya kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu(s.w) aliyemuamrisha kutoa mali hiyo ili kumhalalishia mwanamke anayemtaka awe mkewe wa ndoa. Na mwanamke anapokea mahari hayo ikiwa ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu(s.w).

Kwa mtazamo huu wa Uislamu mwanamume anapotoa mahari hatakuwa na hata chembe ya hisia kuwa ni bei ya mwanamke anayemuoa. Hali kadhalika, kwa mtazamo huu, mwanamke atakapopokea mahari yake hatakuwa na hata chembe ya hisia kuwa amejiuza kwa mume anayemuoa. Ilivyo, ni kwamba katika jamii nyingi zisizo za Kiislamu, mahari imefanywa kama bei ya kumnunulia mke inayotozwa na wazazi au walezi wa mwanamke anayeolewa. Ni katika mtazamo huu wa biashara unaowafanya wale wajiitao watetezi wa Haki na Hadhi ya Mwanamke, waishutumu mahari kuwa imetoa mchango mkubwa katika kumnyanyasa mwanamke katika jamii. Ni kweli kabisa kuwa mwanamke, kwa kisingizio cha mahari, amekandamizwa na kunyanyaswa kiasi kikubwa na wanaume katika jamii nyingi za Kikafiri. Lakini, ni kweli kuwa mahari waliyotoa wanaume katika jamii hizi ndio hasa sababu ya kuwashusha wanawake hadhi zao na kuwakandamiza? Je, mahari yakiondolewa kama watetezi wa haki za

wanawake wanavyodai, wanawake watapata haki zao na hadhi yao ikarudi mahali pake? Ukweli ni kwamba tatizo haliko kwenye mahari bali tatizo liko kwenye kukiuka maamrishi na makatazo ya Mwenyezi Mungu(s.w) katika utoaji wa hayo mahari na katika kuendesha maisha ya kila siku kwa ujumla.

## Khutuba ya Ndoa

Kabla ya kuozesha (kufungisha ndoa), ni Sunnah kwanza kuleta khutuba ya ndoa (mawaidha ya ndoa) kwa ufupi ili kuwakumbusha wanaoana na Waislamu wengine wachunge ahadi waliyoichukua mbele ya Mwenyezi Mungu(s.w) kuwa watakaa kwa wema katika maisha ya ndoa na ikibidi kuachana, wataachana kwa wema vile vile. Ni vyema katika mawaidha haya kuwafahamisha hawa wenye kuoana na kuwakumbusha Waislamu wote waliohudhuria kuwa maisha ya ndoa yatakuwa ya furaha na upendo endapo kila mmoja, mume na mke, atajua wajibu wake kwa mwenziwe na akawajibika kwake ipasavyo. Ndoa iliyofanikishwa kulingana na ahadi ya ndoa ni msingi wa furaha, ushirikiano, utulivu na amani katika familia na jamii kwa ujumla. Ndoa pia imekusudiwa iwaokoe wenye kuoana na adui Shetani na iwasalimishe kwa Mwenyezi Mungu(s.w). Kwa ujumla, katika khutuba hii, ni vyema umuhimu wa ndoa uelezwe kwa muhtasari.

Msisitizo wa Khutuba unaonekana katika hadithi zifuatazo:

*Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema; Ndoa yoyote ambayo ndani yake hamna Tashahhud (Maamkizi ya Mwenyezi Mungu(s.w) ni kama kata isiyo na mkono. (Tirmidh).*

*Abu Hurairah ameeleza kuwa Allah(s.w) amesema: Jambo lolote muhimu lililofanyika bila ya kumtukiza(Kumhimidi) Mwenyezi Mungu(s.w) kwa utukufu wake,limekosa baraka. (Ibn Majah).*

Kutokana na hadithi iliyosimuliwa na Abdullah bin Mas'ud(r.a), Mtume(s.a.w) amefundisha tashahud mbili, ya kwanza ni ile ya swala (Tahiyatu) na ya pili ni ile inayopatikana katika khutuba ya kukidhiwa haja, kama vile khutuba ya ndoa, ambayo inaanza na kuendelea kama ifuataavyo:

نَحْمَدُهُ وَنَسْتَعِينُهُ وَنَسْتَغْفِرُهُ وَنَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْ شُرُورِ أَنْفُسِنَا وَسَيِّئَاتِ  
أَعْمَالِنَا مَنْ يَهْدِ اللَّهُ فَلَا مُضِلُّ لَهُ وَمَنْ يَضِلَّ فَلَا هَادِيَ لَهُ  
وَأَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ سَيِّدَنَا  
مُحَمَّدًا عَبْدَهُ وَرَسُولَهُ.

*Sifa zote anastahiki Mwenyezi Mungu(s.w). tunamtukiza kwa Utukufu wake, Tunataka msaada wake, na msamaha Wake, na tunajikinga kwake na shari ya nafsi zenu na shari ya vitendo vyetu viovu. Ambaye Mwenyezi Mungu amemuongoa, hakuna awezaye kumpoteza, na ambaye amempoteza hatakuwa na wa kumwongoa. Na ninashuhudia kuwa hapana mola ila Mwenyezi Mungu(s.w),na ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mtumwa wake na Mjumbe Wake.*

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿١٧﴾

*Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha wala msife isipokuwa mmekwisha kuwa Waislamu kamili. (3:102).*

يَتَأَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَاءً ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي تَسَاءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ ۚ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيبًا ﴿١٨﴾

*Enyi Watu! Mcheni Mola wenu ambaye amekuumbeni katika nafsi (asili) moja. Na akamuumba mkewe katika nafsi ile ile. Na akaeneza wanaume wengi na wanawake kutoka wawili hao. Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye kwaye mnaombana. Na (muwatazame) jamaa. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mlinzi juu yenu. (4:1).*

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا ﴿١٩﴾ يُصَلِّحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ ۗ وَاللَّهُ وَرَسُولُهُ ۚ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا

عَظِيمًا ﴿٢٠﴾

*Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na semeni maneno ya haki. Atakutengenezeeni vizuri vitendo vyenu na atakusameheni madhambi yenu; Na anayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake bila shaka amefuzu kufuzu kukubwa.(33:70-71).*

## Kufunga Ndoa Kiislamu

Ili ndoa ifungike Kiislamu ni lazima yatekelezwe yafuatayo:

(i) Mume atekeleze masharti ya kuoa.

- (ii) Mke atekeleze masharti ya kuolewa.
- (iii) Pawe na Walii au Idhini yake.
- (iv) Pawe na mashahidi wawili au zaidi.
- (v) Pawe na idhini (ridhaa) ya mwenye kuolewa.
- (vi) Pawe na ljabu na Kabuli.

**(i) Masharti ya Kuo**

- (a) Mke anayemuoa awe Muislamu mwema au ahlul-kitaab mwema.
- (b) Awe anaoa kwa hiari yake (halazimishwi).
- (c) Asiwe maharimu wa mke anayemuoa.
- (d) Awe baleghe na mwenye akili timamu.
- (e) Asiwe katika Ihramu ya Hijja (asiwe amehirimia Hijja).
- (f) Asiwe na ndoa ya wake wane ambao anaishi nao katika ndoa.

**(ii) Masharti ya Kuolewa**

- (a) Mume anayemuoa awe muislamu mwema.
- (b) Asiwe katika ndoa ya mume mwingine.
- (c) Asiwe katika eda ya mume mwingine.
- (d) Awe mwema (Rejea Qur-an, 5:5).
- (e) Asiwe maharimu kwa mume anayemuoa.
- (f) Awe na akili timamu.
- (g) Asiwe katika Ihramu ya Hijja.
- (h) awe anaolewa kwa ridhaa yake, sio kwa kulazimishwa.

**(iii) Walii au Idhini yake**

Ndoa ya Kiislamu haikamiliki mpaka awepo walii wa binti anayeolewa ambaye ndiye muozeshaji au pawe na idhini yake kama tunavyojifunza katika hadithi zifuatazo:

*Abu Mussa(r.a) ameeleza kuwa Mtume(s.a.w) amesema: “Hakuna ndoa ila kwa kuozeshwa na walii”.(Ahmed, Tirmidh, Abu Daud na Ibn Majah).*

*Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Hapana mwanamke atakayemuozesha mwanamke mwingine, wala hapana mwanamke atakayejioza mwenyewe.Hakika mwanamke mzinifu ni yule anayejiozesha mwenyewe. (Ibn Majah)*



Kazi ya Walii ni kufungisha ndoa yeye mwenyewe. Lakini anaweza kuwakilishwa na mtu mwingine, mwanamume mjuzi, afungishe ndoa kwa niaba yake.

Katika sheria ya Kiislamu mawalii wanaoweza kuozaesha ni hawa wafuatao kwa mujibu wa daraja zao:

1. Baba Mzazi wa mwanamke anayeolewa.
2. Babu mzaa baba yake.
3. Ndugu yake wa kiume wa baba mmoja na mama mmoja.
4. Ndugu yake wa kiume wa baba mmoja.
5. Mtoto wa kiume wa ndugu yake wa kiume wa baba mmoja na mama mmoja (Mpwa wake).
6. Mtoto wa kiume wa ndugu yake wa kiume wa baba mmoja.
7. Baba yake mdogo (Ami) aliyezaliwa na baba yake kwa baba mmoja na mama mmoja..
8. Baba yake mdogo (Ami) aliyezaliwa na baba yake kwa baba tu.
9. Mtoto wa kiume wa baba yake mdogo wa kwa baba yake mdogo na mama.
10. Mtoto wa kiume wa baba yake mdogo kwa baba tu.
11. Serikali (Hakim au Kadhi) katika nchi za Kiislamu.

Walii wa daraja ya chini katika orodha hii hawezi kuozaesha mpaka iwe walii wa daraja ya juu yake hayupo. Kwa mfano, babu hawezi kuozaesha kama baba mzazi yupo, ndugu yake hawezi kuozaesha ikiwa babu yupo, na kadhalika. Ikiwa walii wa daraja ya chini ataozaesha na hali yakuwa walii wa daraja ya juu yupo, na hakuridhia, basi ndoa haitasihi.

Mtu ambaye hayumo katika orodha ya mawalii wala si mtoto wa kiume wa hao waliotajwa hapo juu hawezi kuozaesha. Endapo mawalii wote watakosekana, Kadhi au kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu atamuzaesha binti huyo.

Walii ili aweze kuozaesha ni lazima atimizwe masharti yafuatayo:

- (a) Awe Muislamu mwanamume.
- (b) Asiwe mtumwa (awe muungwana).
- (c) Awe mwenye akili timamu.
- (d) Awe anaanzaesha baada ya kupatikana idhini ya mwenye kuolewa.
- (e) Awe muadilifu.

**(iv)Pawe na Mashahidi wawili**

Ndoa haisihi bila ya kushuhudiwa na mashahidi wawili wenye sifa zifuatazo:

- (a)Wawe watu Wazima waliokwisha baleghe. Watoto hawawezi kuwa mashahidi.
- (b) Wawe na akili timamu.
- (c) Wawe Waislamu wanaume.
- (d) Wawe waadilifu.
- (e) Wawe waungwana (sio watumwa).

**(v)Ridhaa (Idhini) ya mwenye Kuolewa**

Ili ndoa ya Kiislamu ikamilike ni lazima idhini ya mwanamke anayeolewa ipatikane. Allah(s.w) ameliweka hili wazi kamatunavyojifunza katika hadithi zifuatazo:

*Abu Hurairah(r.a) ameeleza kuwa Mtume(s.a.w) amesema: Msichana baleghe atatakiwa idhini ya kuolewa kwake. Akinyamaza kimya, itachukuliwa kuwa amekubali, na akikataa hatalazimishwa kuolewa. (Tirmidh, Abu Daud, Nisai).*

*Abu Hurairah(r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Mwanamke aliyewahi kuolewa hataolewa mpaka akubali, wala mwanamke bikra hataozwa mpaka atakwe idhini. Waliuliza: Idhini yake itakuwa vipi? Akasema (Mtume): Kama atanyamaza kimya". (Bukhaary na Muslim).*

**(vi)Pawe na Ijabu na Kabuli**

**Ijabu:** ni yale maneno anayosema walii kumwambia mume anayeoa kama hivi:"Nimekuoza Aisha binti Salim" wala asiseme:

*"Ninakuoza....."*

**Kabuli** ni maneno ya mume ya kukubali kumuoza binti anayetaka kumuoza kwa kusema: "Nimekubali kumuoza Aisha bint Salim", wala asiseme: **"Ninakubali kumuoza..."**

Kwa hiyo Ijabu ni kauli rasmi anayotoa walii au muwakilishi wake mbele ya mashahidi wawili ya kumuoza mke kwa mume na Kabuli ni kauli rasmi anayoitoa mume ya kumkubali mke katika ndoa.

**Walii:** Shaaban bin Abdurahman.

**Shaaban:** Labbayka.

**Walii:** Umekubali kumuoza Aisha bint Salim?

**Shaaban:** Naam, Nimekubali kumuoa 'Aisha bint Salim.

**Walii** atamuuliza Shaaban kama hivyo mara mbili na mara ya tatu atamalizia kama ifuatavyo:

**Walii:** (Mara ya tatu): Ewe Shaaban bin Abdurahman, nakuoza kwa namna alivyoamrisha Mwenyezi Mungu, nayo ni kukaa naye kwa wema na kutokana naye kwa wema vile vile.

**Ijabu:** Nimekuoza Aisha binti Salim kwa ridhaa yake mwenyewe,

(Kutajwa mahari si lazima).

**Kabuli:** Nimekubali kumuoa Aisha bint Salim

**Muhimu:** Kilicho lazima katika kufungisha ndoa ni kupatikana kwa Ijabu na Kabuli. Kwa mfano, Walii badala ya kumuuliza Shaaban mara mbili: "Umekubali kumuoa...", anaweza kumuoza Shaban moja kwa moja kwa kauli ya Ijabu: Shaaban bin Abdurahman Nimekuoza...".

Baada ya ndoa kufungwa ni sunnah kumshika mkono mwenye kuoza na kumuomba dua kama alivyofanya Mtume(s.a.w) kwa Abdul-Rahman bin Awf (r.a) kwa kusema:

*"Baarakallahu laka". "Mwenyezi Mungu akubariki" (Bukhaary na Muslim)*

## **Ndoa ya Mke Mmoja Hadi Wanne**

Suala la ndoa ya mke zaidi ya mmoja ni suala linalopingwa na baadhi ya watu hasa wale wanaodai kuwa ni watetezi wa haki za wanawake. Mwanaume kuoza mke zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja imeonekana kwa wapinzani wa ukewenza kuwa ni jambo lililopitwa na wakati na linalomdunisha mwanamke na kumnyima haki zake. Dai hili linatokana na hali halisi iliyodhihiri katika jamii mbali mbali za kikafiri za kale na za sasa ambapo mwanamke ananyanyaswa na kudhalilishwa kweli kweli. Ni katika hali hii ya kudhalilishwa mwanamke, ndipo wakatokea wanaojiita watetezi wa haki za wanawake na wakawashawishi wanawake wajiunge pamoja na kudai kupata haki zao sawa na wanaume.

Mpaka sasa mafanikio yaliyopatikana katika harakati hizi za "kumkomboa" mwanamke ni wanawake kufanya kila kazi zinazofanywa na wanaume, kuvaa sawa na wanaume, kuwa huru kuchanganyika na wanaume, kushindana na wanaume katika nyanja za siasa na uchumi, mume mmoja mke mmoja na kadhalika.

Watetezi wa Haki za wanawake wa mtazamo huu, wanapoukuta Uislamu umeruhusu kuoza wake wengi, mmoja hadi wane, hurejea historia na hujisaili, "Tumejifunza vya kutosha katika historia kuwa wanaume wamewafanya

wanawake mashine zao za kuwafanyia kazi na kuwazalia watoto na kila mwanamume alipooa wake wengi na kuwaweka chini ya himaya yake, ndivyo mwanamke alivyozidi kumnyimwa haki zake na kudhalilishwa, iweje tena leo turuhusu jambo hili liendeleo? Hili linapingana kabisa na juhudi zetu katika kumkomboa mwanamke!” Fikra hizi zina ukweli mkubwa ndani yake, lakini kasoro yake kubwa ni kule kuulinganisha Uislamu na jamii nyingine. Jamii ya Kiislamu ni jamii iliyoundwa kwa misingi iliyowekwa na Mwenyezi Mungu ambaye ni Muumba, Mjuzi mwenye Hekima aliye Muumba mwanadamu kwa lengo na kumuwekea utaratibu madhubuti wa maisha utakao muwezesha kufikia lengo na kuishi hapa ulimwenguni kwa furaha na amani. Uislamu kupitia kwa Mitume na vitabu vya Allah(s.w)umekusudiwa usimamisha uadilifu katika ardhi:

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيَقُومَ  
الْأَنَاسُ بِالْقِسْطِ ..... ﴿٥٧﴾

“Kwa hakika tuliwapeleka Mitume wetu na dalili wazi wazi na Tukaviteremsha vitabu na uadilifu pamoja nao, ili watu wasimamie uadilifu.....” (57:25)

Katika sheria ya Kiislamu kuoa wake zaidi ya mmoja hadi wane ni jambo lililoruhusiwa na Allah(s.w). Aya ya Qur-an iliyo ruhusu kuoa mke zaidi ya mmoja hadi wane ilishuka mara tu baada ya vita vya uhudi – vita vya pili vya Jihadi kwa umma huu wa Mtume(s.a.w) - ambapo Waislamu wengi wapatao sabini walikufa shahidi na kuacha wake wengi wajane na watoto yatima kama tunavyojifunza katika aya:

وَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا تُقْسِطُوا فِي آلَيْتِمَىٰ فَانكِحُوا مَا طَابَ لَكُمْ مِنَ النِّسَاءِ  
مَتَىٰ وَتَلَسَّ وَرُبَعٌ فَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا تَعْدِلُوا فَوَاحِدَةٌ أَوْ مَا مَلَكَتْ  
أَيْمَانُكُمْ ۚ ذَٰلِكَ أَدْنَىٰ أَلَّا تَعُولُوا ﴿٥٨﴾

Na kama mkiogopa kutowafanyia uadilifu mayatima, basi oeni mnaowapenda katika wanawake wawili, au watatu au wanne. Na mkiogopa kuwa hamuwezi kufanya uadilifu, basi oeni mmoja tu, au (wawekeni masuria) wale ambao mikono yenu ya kuume imewamiliki. Kufanya hivyo ndiko kutakupelekeni kutofanya jeuri. (4:3).

Aya hii inatupa mafundisho yafuatayo:

**Kwanza**, ukewenza ni ruhusa kutoka kwa Allah(s.w) hivyo wanaume wema na wanawake wema wa Kiislamu hawanabudi kuipokea ruhusa hii kwa lengo la kumcha Allah(s.w).

**Pili**, ruhusa hii haikutolewa kwa ajili tu ya kukidhi matamaniao ya kimwili bali ruhusa hii imeshuka ili kuwaruhusu wanaume wema wa Kiislamu wawaoe wajane au wanawake wema wanaohitajia nusura na kuepusha wanawake wema kuolewa na wanaume waovu au kukaa bila ya kuolewa jambo ambalo ni mtihani kwa jamii.

**Tatu**, pamoja na kuoa kwa nia hiyo njema ya kuwapatia hifadhi wajane, mayatima na wanawake wema wenye kuhitajia hifadhi ya waume wema wachache waliopo ruhusa hii haikuachwa wazi kwa kuruhusu wanaume kuoa wake wengi wapendavyo kama ilivyokuwa wakati wa Ujahili, bali imetoa ruhusa ya wanawake wane tu.

**Nne**, endapo mwanaume hatakuwa na uwezo wa kukidhi matamaniao ya jimai kwa wake zake wote au hatakuwa muadilifu kwa wake zake wote, basi sheria hii inamnyima ruhusa hii ya kuoa mke zaidi ya mmoja.

**Tano**, Aya inaagiza: “**Fankihu**” yaani “**Oeni**” wala sio “**Chukueni**”

Hivyo, katika kutumia ruhusa hii ya kuoa mke wa pili hadi wanne, ni lazima kuoa kwa kufuata utaratibu na kuchunga masharti yote ya ndoa ya Kiislamu. Kwa mfano hatalazimishwa mwanamume kuoa mke wa pili na wala hatalazimishwa mwanamke kuolewa na mume aliyekwisha oa.

Mume anayekusudia kuoa mke wa pili au zaidi, kiuadilifu na kiucha-Mungu hanabudi kumtaarifu au kuwataarifu wake zake wa kwanza.

Mkewe au wakeze, kwa upande wao, hawanabudi kumridhia aoe huku wakimshauri na kumuusia kuwa azingatie sharti la uadilifu lililolekwa katika kutolewa kwa ruhusa hii.

Ni muhimu kuzingatia kuwa ruhusa ya ukewenza imetolewa na mwenyewe Allah(s.w) ambaye ni Mjuzi mwenye Hikima, hivyo hapana nafasi ya mjadala kuwa inafaa au haifai. Hata hivyo kwa kuzingatia hali halisi ya jamii, bado hekima ya ruhusa hii iko bayana.

## **Hekima ya Ukewenza**

Kuna sababu nyingi za kibinafsi, kimaadili, kiuchumi na kijamii zinazoonesha kuwa wakati mwingine, kuoa mke zaidi ya mmoja ni jambo lisilobudi. Hebu turejee mifano ya hali kadhaa zifuatazo:

**(a) Kama Mke ni Tasa**

Mfikirie mwanamume ambaye amehakikisha kuwa mkewe ni tasa na bado anahamu ya kupata mtoto atakayekuwa mrithi wake. Katika hali hii mwanamume huyu atafanya mojawapo katika haya yafuatayo:

- (i) Atakaa na kusononeka kwa kukosa mtoto katika maisha yake yote au
- (ii) Atamuacha huyu mke asiye zaa ili aoe mwingine anayezaa au
- (iii) Atatembea na wanawake wengine nje ya ndoa ili wampatie watoto, japo kisheria si watoto wake au
- (iv) Ataendelea kukaa na mkewe kwa mapenzi na furaha, kisha aoe mke mwingine atakayemzalia watoto ambao watakuwa wake kisheria.

Utakuta, uchaguzi (iv) wa kuoa mke wa pili, ndio ulio bora kabisa.

Wengi katika jamii ya Kiislamu, wameoa mke wa pili kwa sababu hii:

**(b) Kama Mke ana maradhi ya kudumu**

Mfikirie tena mwanamume ambaye mkewe ana ugonjwa wa kudumu kwa kiasi kwamba hana uwezo wa kutekeleza majukumu yake kama mke. Bila shaka mwanamume huyu atafanya mojawapo katika haya yafuatayo:

- (i) Atajizuia na matamano yake ya kimwili kwa muda wote wa maisha yake uliobakia.
- (ii) Anaweza kumtaliki mkewe mgonjwa wakati ambapo anahitajia uangalizi, huruma na mapenzi ya hali ya juu kutoka kwake, ili aoe mke mwingine atakaye tosheleza mahitaji yake, au.
- (iii) Anaweza kubakia na mkewe mgonjwa na kufanya uzinifu kwa siri na wanawake wengi nje ya ndoa, au.
- (iv) Ataoa mke wa pili atakayemsaidia kumuhudumia mkewe mgonjwa.

Hebu tuzijadili hizi hatua tatu za mwanzo kwa mtazamo wa mafundisho ya Uislamu.

Hatua ya **kwana** inakwenda kinyume na umbile la mwanadamu. Mwenyezi Mungu(s.w) analifahamu fika umbile la mwanadamu na haja yake ya kutosheleza matamano ya jimai na ameweka utaratibu mzuri wa sheria ya ndoa wa kutosheleza mahitajio haya ya kimaumbile.

Hatua ya **pili** ni kinyume kabisa ha ubinadamu. Kumwacha mke kwa sababu amekuwa mgonjwa, badala ya kumuhudumia kwa upendo na huruma, ni kinyume kabisa na utu.

Hatua ya **tatu** ni haramu na ni uchafu katika Uislamu.

Utaona kuwa hatua ambayo itamuwezesha mume huyu aendelee kumtunza mkewe kwa huruma na wakati huo huo aweze kutosheleza mahitajio yake ya kimaumbile kwa utaratibu mzuri wa heshima na ucha-Mungu ni kuoa mke wa pili.

***(c) Wanawake Wajane:***

Wajane ni wanawake waliofiwa na waume zao au waliotalakiwa.

Hakuna jamii isiyo na wajane, na idadi yao huongezeka zaidi nyakati za vita ambapo wanaume wengi huuliwa vitani. Je, wanawake hawa warudishwe kwa wazazi au walezi wao na kukaa hivyo hivyo bila ya kukidhi matashi yao ya kimaumbile mpaka wazeeke? Au waachwe wawe Malaya na kuitokomezwa jamii kutokana na matatizo mbali mbali yanayosababishwa na zinaa? Kwa vyovyote vile utaona kuwa njia pekee ya kuwahifadhi wanawake wajane na watoto wao ni hii ruhusa ya kuoa mke zaidi ya mmoja hadi wane - kwa kufuata masharti yaliyowekwa.

***(d) Wanawake wakiwa wengi katika Jamii:***

Inatokea katika jamii nyingi wanawake kuwa wengi zaidi kuliko wanaume. Katika jamii hizi, kama tutaweka sheria ya mume mmoja – mke mmoja, kama wanavyodai watetezi wa usawa wa mwanamke, wanawake watakao kosa wanaume wa kuwaoa watakwenda wapi? Watafanyaje ili kukidhi matashi yao ya kimaumbile? Je, kama watajizuilia mpaka wazeeke huoni hii itawaathiri kimwili, na kisaikologia na kuwafanya wasiwe watu wenye manufaa katika jamii? Nani atakayetoa hifadhi kwa wanawake hawa kiuchumi na kimaadili? Ilivyo katika maumbile ya mwanadamu, kila mwanamke wa kawaida anahitajia kuwa na mwanamume anayempenda na kumhurumia. Hivyo, wanawake hawa watakapowakosa wanaume wa ndoa, watafanya kila hila ya kuwashawishi wanaume kwa kuwawekea mitego mbali mbali kama vile kujipitisha mbele yao wakiwa wamejipodoa na kujiremba, kutembea mbele yao uchi, kuzurura kwenye majumba ya sinema, n.k., ambayo itawanasa na kuwatumbukiza katika zinaa.

Mfikirie mwanamke anayeishi kwa kuvizia wanaume. Je, atakuwa na utulivu na usalama katika maisha yake? Je, jamii yenye wanawake wa namna hii wa kuwavizia na kuwateka kwa tashiwishi waume za watu, inaweza kuwa jamii yenye amani na furaha? Wanawake wa namna hii mara nyingi wamekuwa ndio chanzo cha vurugu katika unyumba wa watu, kuwafitinisha watu na kusababisha vifo. Ikitokea mwanamke wa namna hii kupata mimba, jukumu la kumlea mtoto ni lake mwenyewe.

Hivyo, watoto wanaozaliwa nje ya ndoa mara nyingi hukosa malezi mazuri na wengi wao huishia kuwa wezi wavuta bangi, na wahuni wa kupindukia katika jamii.

Kwa vyovyote vile iko haja kwa kila mwanamke kupata mume wa kukidhi haja zake na kuhifadhi maisha yake na utu wake. Uislamu umetoa ruhusa ya kuoa wake zaidi ya mmoja hadi wanne ili kumfanya kila mwanamke anayetaka kuolewa, aolewe na kupata hifadhi na haki zake zote zinazomstahiki.

Kwa nini mwanamke asiruhusiwe kuolewa na Mume zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja?

Wapinzani wa ukewenza, wanadai kuwa ili pawe na usawa, wanawake waruhusiwe kuolewa na mume zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja endapo wanaume wataruhusiwa kuoa mke zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja.

Kimaumbile na kisaikolojia, mwanamke ni wa mwanamume mmoja.

Iliyoyoy, takriban katika jamii zote za ulimwenguni, mwanamume ndiye kiongozi wa familia. Fikiria ingalikuwaje kama familia moja ingalikuwa na viongozi wawili au zaidi!

## Zoezi la 2.1

1. Ni hali ya kawaida katika jamii yetu kupita mwaka au miaka miwili pasina kusikia au kushuhudia ndoa ikifungwa, hali ya kuwa kuna mabinti na mabarobaro wengi waliofikia umri wa kuoa na kuolewa. Bainisha:
  - (a) Sababu zilizoasisi na kustawisha hali hiyo.
  - (b) Manufaa yanayokosekana katika jamii hiyo.
  - (c) Madhara yanayopatikana kutokana na hali hiyo.
  - (d) Mapendekezo ya kurekebisha hali hiyo.
2. *“basi oeni mnaowapenda katika wanawake wawili, au watatu au wanne.....(4:3)”*.
  - (a) Ni sifa zipi zinazopaswa kuzingatiwa kwa muislamu anayetafuta mchumba?
  - (b) Muislamu mwanamke au mwanaume, hatakiwi kisheria kuolewa (na) au kumuoa nani?
3. Allah(s.w) anaonya katika Qur'an kuwa: wala usiikaribie zinaa, kwa hakika huo (uzinifu) ni uchafu na ni njia mbaya kabisa (17:32).

Kwa kuzingatia mmomonyoko wa maadili uliopo ambapo habari, makala na picha zinazochoea uzinifu, zimefurika katika magazeti, majarida, televisheni na kwenye tovuti; Pendekeza hatua muafakaa ambazo Waislamu wanastahiki kuzichukua ili kizazi chao kisipite njia hii mbaya na kutumbukia kwenye shimo la uchafu.



4. Soma kwa mazingatio aya ya 3 iliyo kwenye sura ya 4, kisha:

- (a) Taja sababu moja kubwa inayomruhusu Muislamu kuwa na, ndoa ya mke na mume mmoja.
- (b) Ni sababu zipi za kimazingira zinazoonesha hekma ya mwanaume kuoja wake wawili, watatu hadi wanne.

5. Ni neno la kuaminiwa; mtu akitaka kazi ya askofu...

Basi imempasa askofu awe asiyelaumika, mume wa mke mmoja,... (1Timotheo 3:1-2). Lakini kwasababu ya zinaa kila mwanamume na awe na mke wake mwenyewe...(1Wakorintho 7:2).

Jadili kwa kubainisha tafauti zilizopo baina ya maagizo haya ya biblia na yale ya Qur'an 4:3.

## TALAKA NA EDA

### *Maana ya Talaka*

Talaka ni utaratibu wa kuvunja mkataba wa ndoa waliofunga mume na mke wakati wa kufunga ndoa mbele ya mashahidi wawili. Baada ya kuvunja mkataba huu kwa kufuata sharia ya Kiislamu, mwanamke aliyetalakiwa huwa huru kuolewa na mume mwingine.


### **Talaka katika Uislamu**

Talaka katika Uislamu si jambo la kupendeza. Kwa hiyo mume na mke wanatakiwa wajitahidi kusuluhishana na kuvumiliana ili hatua ya kupeana talaka isifikwiwe.

Talaka ni jambo la halali lililo ruhusiwa inapokuwa hapana budi na wala si jambo la kulifanyia mas-khara kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Ibn Umar amesimulia kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: "Katika halali inayochukiza mbele ya Mwenyezi Mungu(s.w) ni talaka". (Abu Daud).*

Kwa upande mwingine, kama Mwenyezi Mungu(s.w) angaliharamisha talaka, hali ya maisha ingalikuwaje katika familia zile ambazo mume na mke wamekosana kiasi cha kila mmoja kutotaka kumuona mwenziwe! Kwa hiyo, mume au mke atakapofanya kosa au makosa makubwa yasiyovumilika kwa mwenziwe, Mwenyezi Mungu(s.w) ametoa ruhusa wapeane talaka na kuachana kwa wema na mapenzi kama inavyosisitizwa katika Qur-an:

.....  

 .....  
 الطَّلُقُ مَرَّتَانٍ فَاِمْسَاكٌ بِمَعْرُوفٍ اَوْ تَسْرِيحٌ بِاِحْسَنٍ

*Talaka (za kuweza kurejeana) ni mara mbili. Kisha ni kumuweka kwa wema au kumwacha kwa ihsani...". (2:229).*

وَإِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَاءَ فَبَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَأَمْسِكُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ أَوْ سَرَحُوهُنَّ

بِمَعْرُوفٍ ۚ..... ﴿١٣﴾

*Na mtakapowapa wanawake talaka nao wakafikia kumaliza eda yao, basi warejeeni kwa wema au tokaneni nao kwa wema... (2:231).*

فَإِذَا بَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَأَمْسِكُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ أَوْ فَارِقُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ ۚ..... ﴿١٤﴾

*Basi wanapofikia muda wao, ima warejeeni kwa wema, au farikianeni nao kwa wema..... (65:2).*

Kwakuwa ndoa ni mkataba waliowekeana mume na mke wa kuishi kwa wema na kuachana kwa wema ikibidi kuachana, hapana sababu kabisa ya kujenga chuki na uhasama kati ya wawili hawa kwa sababu tu eti wanashindwa kuuendeleza mkataba wao. Katika aya hizi tunaamrisha kuvunja mkataba huu kwa wema kwa kufuata utaratibu aliouweka Mwenyezi Mungu(s.w) na baada ya hapo kila mmoja kuwa huru.

## Suluhu kati ya Mume na Mke

Wanadamu wanapoishi pamoja, kutokana na udhaifu wa kibinadamu kukwaana na kugombana ni jambo la kawaida. Hivyo mume na mke ambao wako karibu sana, hawana budi kuvumiliana kwa kiasi kikubwa. Mmoja akimwona mwenzie amekasirika hana budi kutulizana na kujifanya kama mjinga. Kila mmoja hana budi kujitahidi kwa jitihada zake zote kumtendea wema mwenzake na kumpa haki zake. Vile vile kila mmoja hana budi kuwa tayari kusamehe haki ndogo ndogo alizonyimwa na mwenziwe. Mwenendo huu wa kuvumiliana na kusameheana hudumisha amani na upendo katika nyumba. Hatuna budi kukumbuka kuwa kuvumiliana na kusameheana, hakuleti tu furaha na amani katika nyumba na katika jamii kwa ujumla bali pia ni matendo ya kiucha-Mungu yenye malipo makubwa mbele ya Mwenyezi Mungu(s.w) kama tunavyojifunza katika Qur-an:

..... وَيَعْفُوا وَيَصْفَحُوا ۗ أَلَا تُحِبُّونَ أَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ

غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١١﴾

*"... Na wasamehe na waachilie mbali (yaliyopita). Je, nyinyi hampendi Mwenyezi Mungu akusameheni? Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa msamaha, Mwingi wa rehema (basi nanyi sijfiken na sifa hizi)". (24:22).*

وَجَزَاءُ سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِّثْلُهَا ۗ فَمَنْ عَفَا وَأَصْلَحَ فَأَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ ۗ إِنَّهُ لَا

تُحِبُّ الظَّالِمِينَ ﴿٤٢﴾

*Na malipo ya ubaya ni ubaya ulio sawa na ubaya huo; lakini anayesamehe na kusuluhisha ugomvi, ujira wake uko kwa Mwenyezi Mungu; bila shaka yeye hawapendi madhalimu. (42:40).*

Aya hizi zinatufahamisha kuwa kusamehe ni sababu ya mtu kusamehewa makosa yake na Mola wake na pia ni sababu ya kupatamalipo makubwa mbele ya Mwenyezi Mungu(s.w). Hivyo ikitokea mume na mke wakahitilafiana na kugombana, hawana budi kujisuluhisha wenyewe kwa njia hii ya kusubiri na kusameheana kama Mwenyezi Mungu(s.w) anavyotushauri katika Qur-an:

وَإِنْ أَمْرًا خَافَتْ مِنْ بَعْلِهَا نُشُوزًا أَوْ إِعْرَاضًا فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا أَنْ

يُصْلِحَا بَيْنَهُمَا صُلْحًا وَالصُّلْحُ خَيْرٌ وَأُحْضِرَتِ الْأَنْفُسُ الشُّحَّ ۗ

وَإِنْ تَحْسَبُوا فَتَرًا فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ﴿١٢٨﴾

*Na kama mke akiona kwa mume wake kugombana gombana na kutengana tengana, basi si vibaya kwao wakitengeneza baina yao suluhu (njema wakastahimiliana bila kuachana) maana sulhu ni kitu bora. Na nafsi zimewekewa ubakhili mbele (hakuna mtu anayetaka kumuachia mwingine haki yake). Na kama mkifanya mema (kuwafanyia wake zenu) na mkimcha Mwenyezi Mungu (msiwapunguzie haki zao, bila shaka Mwenyezi Mungu atakulipeni) kwani Mwenyezi Mungu anazo habari za yote mnayoyatenda. (4:128).*

Kitokea mume na mke wenyewe wameshindwa kujisuluhisha mpaka ugomvi ukajitokeza nje, Waislamu walio karibu nao kwa urafiki, ujirani, udugu, n.k. waingilie kati na kuwapatanisha ndugu zao kabla sumu ya shetani haijaenea katika nyumba. Msuluhishaji atumie busara kubwa na ajitahidi kwa kadiri ya uwezo wake katika kufanya kazi hiyo akijua kuwa hiyo ni kazi nyeti na yenye malipo makubwa sana mbele ya Mwenyezi Mungu(s.w) kama tunavyosoma katika Qur-an:

\* لَا خَيْرَ فِي كَثِيرٍ مِّن نَّجْوَاهُمْ إِلَّا مَنْ أَمَرَ بِصَدَقَةٍ أَوْ مَعْرُوفٍ أَوْ  
 إِصْلَاحٍ بَيْنَ النَّاسِ وَمَن يَفْعَلْ ذَلِكَ ابْتِغَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ فَسَوْفَ  
 نُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿١١٤﴾

*Hakuna kheri katika mengi wanayoshauriana kwa siri. Isipokuwa (mashauri ya)wale wanaoamrisha kutoa sadaqa au kufanya mema au kupatanisha baina ya watu. Na Atakayefanya hivi kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu, basi tutampa ujira mkubwa.(4:114).*

Msuluhishi huyu akishindwa, kabla mume hajakimbilia kutoa talaka au mke hajakimbilia kudai talaka, ni vyema Waislamu hawa wakashitakie ugomvi wao kwa kadhi. Kadhi atajitahidi kuwapa mawaidha mazuri na kumkumbusha kila mmoja haki zake na wajibu wake kwa mwingine, kisha baada ya kumsikiliza kila mmoja wao kuhusiana na ugomvi wao, hatatoa uamuzi pale pale bali ataomba muda wa kupekua zaidi kesi hiyo. Kadhi atachagua ndugu waadilifu kutoka kila upande watakaomsaidia kupeleleza kiini cha ugomvi na ni nani aliye mkosea mwenziwe.

Kisha Kadhi atamuita mume na mke na kuwapatanisha akisaidiana na jamaa wa kwa mume na mke. Kadhi atamsihi mkosa asirejee tena makosa yake na amtake mwenziwe msamaha na vile vile aombe msamaha kwa Mwenyezi Mungu(s.w). Pia aliyekosewa ataombwa amsamehe mwenzake ili na Mwenyezi Mungu amsamehe makosa yake na kupata ujira mkubwa kutoka kwake. Wawili hawa wakiwa na nia ya kupatana, baada ya hatua hizi, Mwenyezi Mungu(s.w) ameahidi kuwapatanisha kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

وَإِن خِفْتُمْ شِقَاقَ بَيْنِهِمَا فَابْتَغُوا حَكْمًا مِّنْ أَهْلِهِ وَحَكْمًا مِّنْ أَهْلِهَا  
 إِن يُرِيدَا إِصْلَاحًا يُوَفِّقِ اللَّهُ بَيْنَهُمَا ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا خَبِيرًا ﴿٦٥﴾

*Na kama mkijua kuwa kuna ugomvi baina ya mke na mume basi pelekani mwamuzi mmoja katika jamaa za mwanamume na mmoja katika jamaa za mwanamke. Kama wakitaka mapatano Mwenyezi Mungu atawapatanisha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa habari za siri na habari za dhahiri. (4:35).*

Ni nani mbora wa kutekeleza ahadi yake kuliko Mwenyezi Mungu? Hivyo, mume na mke wasikimbilie talaka bali wajitahidi kutafuta suluhu baina yao kwa nia njema na kwa jitihada zao zote. Ndipo waachane endapo suluhu itashindikana kabisa. Na kutokana na ahadi hii, haitashindikana endapo watakuwa wacha Mungu.

Pia kabla ya kufikia hatua ya talaka, mume na mke wanaruhusiwa kutengana kwa muda wa miezi mine. Suluhu ikishindikana katika muda huo itabidi waachane kama tunavyojifunza katika Qur-an:

لِّلَّذِينَ يُؤَلُّونَ مِن نِّسَابِهِمْ تَرَبُّصُ أَرْبَعَةِ أَشْهُرٍ ۖ فَإِن فَاءُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ  
رَّحِيمٌ ۖ وَإِن عَزَمُوا الطَّلَاقَ فَإِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٢٧﴾

*Kwa wale wanaoapa kwamba watajitenga na wake zao, (muda wao) ni kungojewa miezi mine. Na kama wakirejea, basi Mwenyezi Mungu ni mwingi wa kusamehe, mwingi wa kurehemu. Na wakiazimia kuacha (basi) Mwenyezi Mungu ni mwenye kusikia, mwenye kujua. (2:226-227)*

## Haki ya Kutaliki

Katika jamii nyingi za kijahili haki ya kutoa talaka iko kwa mwanamume tu na mwanamke hana haki yoyote ya kumtaliki mumewe. Katika sheria ya Kiislamu haki ya kutoa talaka iko kwa wote, mume na mke.

### (a) Haki ya Mume kutoa talaka

Ilivyo katika kawaida ya maumbile mwanamume ndiye anayeanza kutoa posa au pendekezo la kuoana. Katika sheria ya Kiislamu, mwanamume pia ndiye anayepaswa kutoa mahari kumpa anayemtaka waoane, ndiye mwenye jukumu la kumlisha mkewe na kukidhi haja zake zote, na ndiye kiongozi wa familia. Kwa kuzingatia ukweli huu. Uislamu umempa haki ya kutoa talaka lakini iwe inapokuwa hapana budi na iwe ni kwa wema na kwa kutekeleza masharti yaliyowekwa na sheria.

### (b) Haki ya mke kumwacha mumewe

Ndoa katika Qur-an imeelezwa kuwa lengo lake ni kuleta upendo na huruma kati ya mume na mke - (Rejea Qur-an, 30:21). Endapo mwanamke ataona sababu za msingi ambazo, zinaifanya ndoa yao isifikie lengo hili, mwanamke anapewa uhuru wa kudai talaka kwa mumewe. Mumewe akimkatalia, anaruhusiwa mwanamke kwenda mbele ya vyombo vya Sheria ya Kiislamu na kudai talaka. Itabidi mume alazimishwe kutoa talaka iwapo vyombo hivi vya sheria vitashindwa kuwasuluhisha. Wakati mwingine, mwanamke anaweza kumtaliki mumewe bila hata ya kukubaliana naye au kupitia mahakamani.

Inawezekana hivi kwa namna mbili:

- (i) Kama tangu mwanzo, katika kufunga mkataba wa ndoa mume alikubaliana na mkewe kuwa atakuwa na uhuru wa kuvunja ndoa, endapo mume

atamfanyia au atafanya jambo fulani asilolipenda; basi atakapovunja ahadi hiyo, mkewe atakuwa na uhuru wa kumwacha bila ya kudai talaka kwake au mahakamani. Kwa maana nyingine mwanamume tangu mwanzo katika mkataba wao wa ndoa, amempa mkewe haki ya kumtalakisha, endapo atafanya au atamfanyia jambo fulani asilolipenda.

Talaka ya aina hii huitwa “**Khul**”.

- (ii) Kama katika mkataba wa ndoa, mwanamume alitoa haki yake ya “kutamka” talaka na kumpa mkewe ili kumpa uhuru na uwezo zaidi wa kuvunja mkataba wa ndoa endapo ataona haifikii lengo lake.

***(c)Kuvunja ndoa kwa makubaliano ya mume na mke:***

Wakati mwingine, mume na mke wote baada ya kuona kuwa hawaishi kwa maelewano kama ilivyotarajiwa, wana uhuru wa kukubaliana kuachana kwa wema. Mahakama ya Kiislamu haitaingilia kati, labda itokee kuvunjwa kwa sheria nyingine kutokana na kuachana kwao huko. Aina hii ya Talaka huitwa “Mubarat”.

***(d)Haki ya Mahakama ya Kiislamu katika kuvunja Ndoa***

Wakati mwingine, hata bila ya makubaliano ya mume na mke, mahakama ya Kiislamu ina uwezo wa kuvunja ndoa. Kwa mfano talaka ya aina ya “Li’aan” husimamiwa na serikali.

## **Aina za Talaka**

Kuna aina nyingi za talaka ambazo ni vyema kila Muislamu akazifahamu. Kutojua talaka inavyopatikana, mtu anaweza kukaa na mke aliyekwisha achika kitambo. Kuna aina nyingi za talaka lakini tunaweza kuzigawanya kwenye makundi makuu mawili:

(1)Talaka rejea.

(2)Talaka isiyorejewa.

### ***1. Talaka Rejea***

Talaka rejea ni aina yoyote ya talaka ambayo inampa mtu fursa ya kumrejea mkewe baada ya kumpa talaka na baada ya kuona kuwa kuna haja ya kusuluhishana na kurejeana. Kuna aina kubwa mbili za talaka rejea.

(a)Talaka moja. (Talaki-Ahsan).

(b)Talaka mbili (Talaki-Hasan).

**(a) Talaka moja:**

Talaka moja hupatikana baada ya mume mwenye akili timamu kumtamkia mkewe akiwa katika twahara maneno ya kudhihirisha dhamira ya kumwacha kama vile: “Nimekuacha”, baada ya eda kwisha mkewe huyo atakuwa ameachika kwa talaka moja.

**(b) Talaka mbili:**

Katika aina hii ya talaka, mume baada ya kushindwa kufikia suluhu na mkewe, huamua kumuacha kwa talaka mbili kwa kumuandikia au kumtamkia kuwa amemuacha katika twahara ya kwanza (kama tulivyoona katika talaka moja), kisha kumtamkia tena kuwa amemuacha talaka ya pili katika twahara ya pili au ya tatu. Pia inahesabiwa talaka mbili kama baada ya kutoa talaka moja, wawili walipatana na kurejeana kabla ya kipindi cha eda kwisha, kisha wakakosana wakati mwingine kiasi cha kufikia hatua ya mume kutoa talaka nyingine. Vile vile kama wawili baada ya kuachana kwa talaka moja, watafikia maafikiano ya kuoana tena kisha wakagombana tena kiasi cha kupeana talaka, zitaahesabika talaka mbili.

Utaratibu mwingine wa kuacha kwa talaka mbili ni sawa tu na ule wa kuacha kwa talaka moja tuliouona. Hii nayo ni talaka rejea, kwa maana ya kwamba mtu anaweza kumrejea mkewe kabla ya kipindi cha eda kwisha.

Pia baada ya kuachana mwanamume anaruhusiwa kufunga tena ndoa na mke aliyemuacha endapo wataelewana na akiwa bado hajaolewa na mume mwingine. Mke aliyeachwa kwa talaka zaidi ya mbili harejewa tena kama inavyositizwa katika Qur-an:

الطَّلُقُ مَرَّتَانٍ ۖ فَإِمْسَاكَ بِمَعْرُوفٍ أَوْ تَسْرِيحٍ بِإِحْسَانٍ..... ﴿٢٢٩﴾

*Talaka (unazoweza kumrejea mwanamke) ni (zile zilizotolewa) mara mbili. Kisha kumuweka kwa wema au kumwacha kwa ihsani... (2:229).*

Aina nyingine za talaka rejea ni hizi zifuatazo

**(c) Talaka ya ‘Ilaa**

Aina hii ya talaka inapatikana kwa mtu kuamua kujitenga na mkewe zaidi ya miezi mine. Katika jamii za kijahilia palikuwa na tabia ya wanaume, kwa sababu mbali mbali, kuapa kutofanya tendo la ndoa na wake zao kwa kipindi kisichojulikana. Uislamu unamruhusu mtu kutengana na mkewe kwa kipindi kisichozidi miezi mine.

لِلَّذِينَ يُؤْلُونَ مِنْ نِسَائِهِمْ تَرَبُّصُ أَرْبَعَةِ أَشْهُرٍ ۖ فَإِنْ فَاءُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ

رَحِيمٌ ﴿٣٣﴾

*Kwa wale wanaoapa kwamba watajitenga na wake zao (muda wao) ni kungojewa miezi mine. Na kama wakirejea (wakatangamana na wake zao) basi Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) mwingi wa kurehemu. (2:226)*

Baada ya miezi mine kupita bila ya mume kumrejea mkewe, ndoa itavunjika, bila hata ya kutamka kuwa amemuacha. Kama atataka kumrejea tena mkewe itambidi afunge ndoa upya. Ni kwa mtazamo huu vile vile, mwanamke ana haki ya kudai talaka mbele ya kadhi endapo mumewe atakuwa amemsusa (amemuacha bila ya maagano yoyote) zaidi ya miezi mine. Mwanamke huyu atakuwa ameachika Kiislamu na atakuwa huru kuolewa na mume mwingine. Hekima ya hukumu hii ni kuwapa wanawake haki zao na uhuru wao wanaostahiki.

#### (d) Talaka ya Zihhaar

Katika jamii ya Waarabu wakati wa ujahili, palikuwa na aina nyingine ya kumsusa mke kwa kumwambia: “Ninakuona kama mgongo wa mama yangu”. Baada ya mume kutamka maneno haya hakuwa tena anamuingilia mkewe na kumtekelezea vilivyo haki zake nyingine na wala hakuwa anamwacha ili apate kuolewa na mume mwingine. Uislamu umekataza desturi hii na kuwaadhibu vikali wale wanaofanya hivyo kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

قَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّتِي تُجَدِّلُكَ فِي زَوْجِهَا وَتَشْتَكِي إِلَى اللَّهِ وَاللَّهُ  
يَسْمَعُ تَحَاوُرَكُمَا ۚ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ﴿٤١﴾ الَّذِينَ يُظَاهِرُونَ مِنْكُمْ مِمَّنْ  
نَسَاءِهِمْ مَا هُنَّ أُمَّهَاتُهُمْ ۖ إِنَّ أُمَّهَاتُهُمْ إِلَّا الَّتِي وَلَدْتَهُمْ ۚ وَإِنَّهُمْ  
لَيَقُولُونَ مُنْكَرًا مِنَ الْقَوْلِ وَزُورًا وَإِنَّ اللَّهَ لَعَفُوفٌ غَفُورٌ ﴿٤٢﴾

*Mwenyezi Mungu amekwisha sikia usemi wa mwanamke yule anayejadiliana nawe sababu ya mumewe, na anashtaki mbele ya Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu anayasikia majibizano yenu; hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kusikia, mwenye kuona. Wale miongoni mwenu wawaambiao wake zao kuwa wanawaona kama mama zao (kwa hivyo wakajiepusha nao wasiwaingilie, wala wasiwape ruhusa ya kuolewa na waume wengine); hao si mama zao. Hawakuwa mama zao ila wale walio wazaa wanasema neno baya na la uwongo. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye msamaha, mwenye maghfirah. (58:1-2)*



وَالَّذِينَ يُظَاهِرُونَ مِن نِّسَائِهِمْ ثُمَّ يَعُودُونَ لِمَا قَالُوا فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مِّن قَبْلِ أَن يَتَمَاسَا ۚ ذَٰلِكُمْ تُوَعُّظُونَ بِهِ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٥٨﴾  
 فَمَن لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامُ شَهْرَيْنِ مُتَتَابِعَيْنِ مِن قَبْلِ أَن يَتَمَاسَا ۗ فَمَن لَّمْ يَسْتَطِعْ فإِطْعَامُ سِتِّينَ مِسْكِينًا ۗ ذَٰلِكَ لِتُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ۗ وَتِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ وَلِلْكَافِرِينَ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٥٩﴾

*Na wale wawaitao wake zao mama zao, kisha wakarudia katika yale waliyoyasema (wakataka kuwarejea wake zao wakae kama mke na mume), basi wampe mtumwa uhuru kabla ya kugusana. Mnapewa maonyo kwa haya. Na Mwenyezi Mjangu anajua mnayoyatenda Na asiyepata (mtumwa) basi afunge saumu ya miezi miwili mfululizo kabla ya kugusana; na asiyeweza basi awalishe masikini sitini (kila masikini kibaba kimoja). (Mmeamrisha) haya ili mumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu; na kwa makafiri iko adhabu iumizayo. (58:3-4)*

Tunajifunza katika aya hizi kuwa, mtu akimsusia mkewe kwa kumwambia kuwa anamuona kama mama yake anaharamishiwa mkewe na hawezi tena kumrejea kama mkewe mpaka atoe kafara kwa:

- (a) Kumwacha mtumwa huru.
- (b) Kama hana mtumwa, kufunga miezi miwili mfululizo (bila ya kupumzika katikati).
- (c) Kama hana uwezo wa kufunga kwa sababu za kisheria zinazomruhusu mtu kutofunga Ramadhani, atalisha masikini sitini.

Kama mtu hatatekeleza adhabu hii kwa hiari yake, mahakama ya Kiislamu itaingilia kati na kumlazimisha kufanya hivyo, ili mkewe awe halali kwake. Muda wa miezi mine ukipita kabla hajatekeleza adhabu hii, mkewe atakuwa ameachika kama ilivyo katika talaka ya 'Illa. Mkewe atakuwa huru kuolewa na mume yeyote aliye halali kwake. Pia mume anaweza kumrejea mkewe kwa ndoa mpya, endapo atamuwahi kabla hajaolewa na mwingine lakini pia kwa kutekeleza adhabu iliyotolewa, Qur'an 58:3-4).

### (e) Talaka ya Khul

Hii ni aina ya talaka ambayo inapatikana kwa mwanamke kudai aachwe. Kama mwanamke atakuwa hapati furaha na amani katika ndoa ya mume aliye

naye, kwa sababu zake mwenyewe ana haki ya kudai talaka kwa mumewe na itabidi mumewe ampe talaka kwa kufuata utaratibu wa kawaida wa kutoa talaka, na baada ya kipindi cha eda, mwanamke atakuwa ameachika. Kama mke amedai apewe talaka kwa sababu zake mwenyewe bila ya mumewe kumnyima haki yake yeyote, atalazimika kumrudishia mumewe mahari, ili iwe kikomboleo kwake. Hata hivyo, wanaume wanaweza kusamehe mahari hayo. Iliyoye kawaida mwanamume haruhusiwi kudai mahari kama ndiye aliyetoa talaka, kama inavyobainishwa katika Qur-an:

..... وَلَا تَحِلُّ لَكُمْ أَنْ تَأْخُذُوا مِمَّا آتَيْتُمُوهُنَّ شَيْئًا إِلَّا أَنْ يَخَافَا

أَلَّا يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ ۗ فَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ فَلَا جُنَاحَ

عَلَيْهِمَا فِيمَا آفَتَدْت بِهِ ۗ تِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ فَلَا تَعْتَدُوهَا ۗ وَمَنْ يَتَعَدَّ

حُدُودَ اللَّهِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٢٩﴾

.....Wala si halali kwenu kuchukua chochote mlichowapa (wake zenu), isipokuwa (wote wawili) wakiogopa ya kwamba hawataweza kusimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu (yaani hawataweza kuishi kwa wema). Basi mkiogopa kwamba hawataweza kusimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu, hapo itakuwa hapana dhambi kwao (mwanamume wala mwanamke katika) kupokea (au kutoa) ajikomboleacho mwanamke. Hii ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu; basi msiruke. Na watakaoiruka mipaka ya Mwenyezi Mungu, hao ndio madhalimu. (2:229).

Iliyoye katika sheria ni kwamba kabla mwanamke hajafikia kuomba talaka, atamshitaki mumewe katika mahakama ya Kiislamu au kwa Kadhi, endapo atakuwa anamtesa au kumdhulumu haki zake. Mwanamume atashauriwa kutekeleza wajibu wake kwa mkewe. Mwanamume akizidi kukengeuka, itabidi mke adai talaka mbele ya mahakama, kama mume amekataa kutoa talaka kwa hiari yake. Kwa hali hii, kwa kuwa mwanamke ndiye aliyekosewa, hatalazimika kurudisha mahari au chochote alichopewa na mumewe. Na mwanamume naye hatalazimika kumpa kitoka nyumba.

Wanawake wanaodai talaka kwa sababu zao binafsi zisizo za msingi, kwa sababu tu eti wanataka kubadilisha mazingira, wajue kuwa mchezo huo ni mbaya sana mbele ya Mwenyezi Mungu(s.w) kama tunavyojifunza katika Hadith:

*Shaaban(r.a)ameeleza kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Mwanamke yeyote atakaye dai talaka kwa mumewe bila kosa, hata harufu ya Pepo imeharamishwa kwake. (Ahmad, Tirmidh).*

**(f) Talaka ya Mubarat**

Talaka hii inapatikana kwa makubaliano ya mume na mke kuachana kwa wema baada ya kuona kuwa hakuna maelewano katika ndoa.

**2. Talaka Isiyorejewa**

Talaka isiyorejewa ni ile ambayo mtu hawezi tena kumreja mkewe hata kama watasuluhishana kabla ya eda au baada ya eda. Kuna aina kuu mbili za talaka zisizorejewa:

(a) Talaka Tatu.

(b) Talaka ya Li'aan.

**(a) Talaka tatu**

Talaka tatu zinapatikana kwa kutamka dhamira ya kumuacha mke mara tatu katika kila twahara ndani ya twahara tatu za eda. Vile vile zitahesabika talaka tatu kama mume katika muda wa ndoa yao amewahi kutoa talaka rejea mbili kwa kipindi kimoja cha eda au vipindi tofauti ambapo walipatana na kurejeana. Pia kama mtu na mkewe waliwahi kuvunja ndoa mara moja kwa talaka mbili kisha mara zote hizo mbili walipatana kufunga ndoa tena watakapopeana talaka katika ndoa yao hii ya mwisho, talaka hiyo itahesabika kuwa ni talaka ya tatu.

Ni kinyume kabisa na sheria ya Kiislamu kutoa talaka tatu mfululizo katika kikao kimoja au katika twahara moja kwa matamshi. Wanachuoni wengi wamekubaliana kuwa talaka ya namna hiyo itahesabiwa kuwa ni talaka moja. Waislamu wanaofanya hivyo, wajue kuwa huko ni kuzifanyia mzaha aya za Mwenyezi Mungu na kuvuka mipaka ya Mwenyezi Mungu.

..... وَمَنْ يَتَعَدَّ حُدُودَ اللَّهِ فَقَدْ ظَلَمَ نَفْسَهُ ۗ

“.....Na anayeruka mipaka ya Mwenyezi Mungu basi amejidhulumu nafsi yake.....” (65:1).

Uislamu umekataza vikali mchezo wa kutoa talaka tatu kwa mpigo kama tunavyojifunza katika hadithi:

*Mahmuud bin Labiid(r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu alielezwa juu ya mtu aliyetoa talaka tatu mfululizo kwa mkewe. Kisha Mtume alisimama akiwa amechukizwa sana na akasema: “Unacheza na Kitabu cha Mwenyezi Mungu(s.w) nikiwa bado tupo pamoja (nikiwa bado sijafa)?” (Mtume alikasirika) kwa kiasi ambacho mtu mmoja alisimama akauliza: Je, siwezi kumuua? (Nisai)*

Hukumu ya talaka tatu ni kwamba baada ya mume kutamka talaka ya tatu hawezi tena kumreja mkewe katika kipindi cha eda hata kama watapatana vipi. Baada ya kipindi cha eda kwisha, mkewe atakuwa ameachika kwa talaka tatu na atakuwa huru kuolewa na mume mwingine yeyote aliyehalalishwa kwake katika sheria ya Kiislamu. Lakini ni haramu mwanamke huyo kuolewa na mumewe wa kwanza mpaka aolewe na mume mwingine. Kisha akiachika kwa mume wa pili kwa sababu za msingi au akiachwa mjane, ndipo itakuwa halali kwake kuolewa na mume wake wa kwanza. Ndoa ya namna hii inajulikana kwa jina la “Tahlil”.

Qur-an inabainisha hukumu hii katika aya ifuatayo:

فَإِنْ طَلَّقَهَا فَلَا تَحِلُّ لَهُ مِنْ بَعْدُ حَتَّى تَنْكِحَ زَوْجًا غَيْرَهُ ۗ فَإِنْ طَلَّقَهَا  
فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا أَنْ يَتَرَاجَعَا إِنْ ظَنَّا أَنْ يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ ۗ وَتِلْكَ  
حُدُودُ اللَّهِ يُبَيِّنُهَا لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٢٣٠﴾

*Na kama amempa talaka (ya tatu) basi (mwanamume huyo) si halali kwake baada ya hapo mpaka aolewe na mume mwingine. Na (mwanamume huyo mwingine) akimwacha, basi hapana dhambi kwao kurejeana (kwa kuoana tena) wakiona kuwa watasimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na hii ni mipaka ya Mwenyezi Mungu anayoibainisha kwa watu wajua. (2:230)*

Hukumu hii kali imetolewa ili Waislamu wasifanye mas-khara na talaka. Kuna baadhi ya Waislamu, wakikwaruzana tu kidogo na wake zao hutishia talaka au anatoa talaka kabisa. Mtu akiendelea na mchezo huu atajistikia ameshamuacha mkewe kwa talaka tatu na hana namna tena ya kumreja. Ni katika mchezo huu wa kutoa talaka tatu bila kufikiri na kumuogopa Mwenyezi Mungu, baadhi ya Waislamu wameishia katika majuto.

Baadhi ya Waislamu wanadiriki kumdanganya Mwenyezi Mungu kwa mtu kumuhonga mume mwingine amuo mtalaka wake kwa lengo la kumuacha baada ya muda mfupi (na ikiwezekana asimguse) ili awe halali kuolewa na mume wake wa mwanzo. Huku ni kuzifanyia mzaha sheria za Mwenyezi Mungu na ni Haramu ya uwazi. Ndoa za namna hiyo hazisihi mbele ya Mwenyezi Mungu(s.w).

### **(b) Talaka ya Li'aan**

Talaka hii hupatikana kwa viapo viwili cha mume na mke. Ikitokea kwamba mume au mke amemkamata mwenzie ugoni lakini hapana mashahidi wanne walioshuhudia kitendo hicho ila yeye mwenyewe itabidi, kama mume ndiye aliyemkamata mkewe ugoni, aape kwa kurudia mara nne kuwa anashuhudia

kuwa mkewe mzinifu, kisha mara ya tano aape kwamba laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake ikiwa yeye ni miongoni mwa waongo. Mke naye ataapa mara nne kujitetea kuwa yeye hakufanya kitendo hicho kisha mara ya tano aape kuwa laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake kama mumewe ni miongoni mwa wasemao kweli. Viapo hivi vinabainishwa katika aya zifuatazo:

وَالَّذِينَ يَرْمُونَ أَزْوَاجَهُمْ وَلَمْ يَكُنْ لَهُمْ شُهَدَاءُ إِلَّا أَنْفُسُهُمْ فَشَهَدَةُ  
 أَحَدِهِمْ أَرْبَعُ شَهَدَاتٍ بِاللَّهِ إِنَّهُ لَمِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٦﴾ وَالْخَمْسَةَ  
 أَنْ لَعْنَتَ اللَّهِ عَلَيْهِ إِنْ كَانَ مِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿٧﴾ وَيَدْرُؤُاَ عَنْهَا الْعَذَابَ أَنْ  
 تَشْهَدَ أَرْبَعَ شَهَدَاتٍ بِاللَّهِ إِنَّهُ لَمِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿٨﴾ وَالْخَمْسَةَ أَنْ  
 غَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهَا إِنْ كَانَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٩﴾

*Na wale wanaowasingizia wake zao (kuwa wamezini) na hawana mashahidi ila nafsi zao, basi ushahidi wa mmoja wao utakuwa kushuhudilia mara nne kwa kiapo cha Mwenyezi Mungu ya kwamba: bila shaka yeye ni mmoja wa wanaosema kweli. Na mara ya tano (aape) kwamba laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake ikiwa ni miongoni mwa waongo. Na (mke) itamuondokea adhabu kwa kutoa shahada mara nne kwa kiapo cha Mwenyezi Mungu ya kwamba (mume) ni miongoni mwa waongo. Na mara ya tano (aape) ya kwamba hasira ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake kama (mumewe) yu miongoni mwa wanaosema kweli, (na yeye mke ndiye mwongo). (24:6-9)*

Baada ya kuapizana hivi, hapo hapo ndoa itakuwa imevunjika moja kwa moja kwani wawili hawa hawategemewi tena kurejeana na kukaa kwa furaha na amani.

## Taratibu za Kutaliki Kiislamu

Kama palivyo na taratibu za kuoa Kiislamu ndivyo hivyo pia ilivyokatika kuvunja ndoa.

Itakapofikia hatua kuwa mume na mke hawanabudi kuachana, itabidi ufuatwe utaratibu wa kuachana kama ulivyobainishwa katika shariaya Allah(s.w):

يَأْتِيهَا النَّبِيُّ إِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَاءَ فَطَلَّقُوهُنَّ لِعَدَّتِهِنَّ وَأَحْصُوا الْعِدَّةَ<sup>ط</sup>  
وَاتَّقُوا اللَّهَ رَبَّكُمْ لَا تُخْرِجُوهُنَّ مِنْ بُيُوتِهِنَّ وَلَا تَخْرُجْنَ إِلَّا أَنْ  
يَأْتِيَنَّ بِفَحِشَةٍ مُبَيَّنَةٍ<sup>ع</sup> وَتِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ<sup>ع</sup> وَمَنْ يَتَعَدَّ حُدُودَ اللَّهِ فَقَدْ  
ظَلَمَ نَفْسَهُ لَا تَدْرِي لَعَلَّ اللَّهَ يُحْدِثُ بَعْدَ ذَلِكَ أَمْرًا ﴿١﴾

*Ewe Mtume mtakapotoa talaka kwa wanawake, toeni talaka katika wakati wa eda zao. (Yaani waacheni wakati wa twahara zao ambazo katika twahara hizo hamkuwahi bado kuwaingilia.) Na fanyeni hisabu ya (siku za) eda. Na mcheni Allah, Mola wenu. Msiwatoe katika nyumba zao wala msitoke wenyewe. Ila wakifanya jambo la ufasiki ulio wazi. Na hii ni mipaka ya Allah. Na anayeruka mipaka ya Allah basi amejidhulumu nafsi yake. Hujui (sababu ya kuamrisha haya). Labda Allah atatokezesha jambo jingine baada ya haya (yaani jambo la kupatana). (65:1)*

فَإِذَا بَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَأَمْسِكُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ أَوْ فَارِقُوهُنَّ بِمَعْرُوفٍ وَأَشْهِدُوا  
ذَوِي عَدْلٍ مِّنْكُمْ وَأَقِيمُوا الشَّهَادَةَ لِلَّهِ<sup>ع</sup> ذَلِكَمُ يُوعِظُ بِهِ<sup>ع</sup> مَنْ كَانَ  
يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ<sup>ع</sup> وَمَنْ يَتَّقِ اللَّهَ يَجْعَلْ لَهُ مَخْرَجًا ﴿٢﴾

*Basi wanapofikia muda wao, ima (warejeeni) muwaweke kwa wema, au farikianeni nao kwa wema; na mshuhudishe mashahidi wawili waadilifu miongoni mwenu. Na simamisheni ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Hivyo ndivyo anavyoagizwa yule anayemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Na anayemuogopa Mwenyezi Mungu, (Mwenyezi Mungu) humtengenezea njia ya kuokoka (katika kila balaa). (65:2)*

وَالَّتِي يَبْسُنَ مِنَ الْمَحِيضِ مِنْ نِسَائِكُمْ إِنْ أَرَبْتُمْ<sup>ع</sup> فَعِدَّتُهُنَّ ثَلَاثَةُ أَشْهُرٍ  
وَالَّتِي لَمْ تَحْضَنْ<sup>ع</sup> وَأَوْلَتْ الْأَحْمَالِ أَجَلُهُنَّ أَنْ يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ<sup>ع</sup> وَمَنْ يَتَّقِ  
اللَّهَ يَجْعَلْ لَهُ مَخْرَجًا مِنْ أَمْرِهِ يُسْرًا ﴿٣﴾

Na wale waliokoma na kutoka hedhi miongoni mwa wanawake wenu, ikiwa mnayo shaka (katika muda wao wa eda), basi muda wa eda yao ni miezi mitatu, na (pia ndiyo eda kwa wale) ambao hawajapata hedhi bado. Na wanawake wenye mimba eda yao ni mpaka watakapozaa. Na anayemwogopa Mwenyezi Mungu, (Mwenyezi Mungu) humfanyia mambo yake kuwa mepesi. (65:4)

أَسْكِنُوهُنَّ مِمَّنْ حَيْثُ سَكَنْتُمْ مِّنْ وَّجَدِكُمْ وَلَا تُضَارُوهُنَّ لِتُضَيِّقُوا  
عَلَيْهِنَّ ۚ وَإِنْ كُنَّ أُولَاتٍ حَمَلٍ فَأَنْفِقُوا عَلَيْهِنَّ حَتَّىٰ يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ ۚ فَإِنْ  
أَرْضَعْنَ لَكُمْ فَآتُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ ۗ وَأَتَمُّوا بَيْنَكُمْ بِمَعْرُوفٍ ۗ وَإِنْ تَعَاَسَرْتُم  
فَسْتَرْضِعْ لَهُنَّ أُخْرَىٰ ۗ ﴿٦٥﴾

Wawakeni humo humo mnamokaa nyinyi, kama mpatavyo (ijapokuwa mumewawacha; maadamu eda yao haijeshi). Wala msiwadhuru kwa kuwatia dhiki. Na kama wakiwa na mimba, wagherimieni mpaka wajifungue. Na kama wakikunyonyesheeni, basi wapeni ujira wao. Na shaurianeni kwa wema. Na kama mkiona udhia baina yenu, basi amnyonyeshe mwanawe (mwanamke) mwengine. (65:6)

وَالْمُطَلَّقَاتُ يَتَرَضَّعْنَ بِأَنْفُسِهِنَّ ثَلَاثَةَ قُرُوءٍ ۚ وَلَا سِحْلٌ لَّهُنَّ أَنْ يَكْتُمَنَّ  
مَا خَلَقَ اللَّهُ فِي أَرْحَامِهِنَّ إِنْ كُنَّ يُؤْمِنُنَّ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۚ وَبِعُولَتِهِنَّ  
أَحَقُّ بِرِدَّهِنَّ فِي ذَٰلِكَ إِنْ أَرَادُوا إِصْلَاحًا ۚ وَهُنَّ مِثْلُ الَّذِي عَلَيْهِنَّ  
بِالْمَعْرُوفِ ۚ وَلِلرِّجَالِ عَلَيْهِنَّ دَرَجَةٌ ۗ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٦٦﴾

Na wanawake walioachwa wangoje (wasiolewe) mpaka twahara tatu zishe. Wala haiwajuzii kuficha (mimba) aliyumba Mwenyezi Mungu katika matumbo yao, ikiwa wanamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho. Na waume wao wana haki ya kuwarejesha katika muda huo, kama wakitaka kufanya suluhu. Nao (wanawake) wanayo haki kwa Sharia (kufanyiwa na waume zao) kama ile haki iliyo juu yao kuwafanyia waume zao. Na wanaume wana daraja zaidi kuliko wao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu (na) Mwenye hikima. (2:228).

الطَّلُقُ مَرَّتَانٍ ۖ فإِمْسَاكٌ بِمَعْرُوفٍ أَوْ تَسْرِيحٌ بِإِحْسَنِ ۗ وَلَا سِحْلٌ لَكُمْ  
 أَنْ تَأْخُذُوا مِمَّا آتَيْتُمُوهُنَّ شَيْئًا إِلَّا أَنْ يَخَافَا أَلَّا يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ ۗ  
 فَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا فِيمَا افْتَدَتْ بِهِ ۗ  
 تِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ فَلَا تَعْتَدُوهَا ۗ وَمَنْ يَتَعَدَّ حُدُودَ اللَّهِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ

الظَّالِمُونَ ﴿٢٢٩﴾

*Talaka (unazoweza kumreja mwanamke) ni (zile zilizotolewa) mara mbili (za kwanza). Kisha ni kumweka kwa wema au kumwacha kwa ihsani. (Wala usiweze kumreja tena mpaka aolewe na mume mwingine). Wala si halali kwenu kuchukua cho chote mlichowapa (wake zenu), isipokuwa (wote wawili) wakiogopa ya kwamba hawataweza kusimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu. Basi mkiogopa kwamba hawataweza kusimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu, hapo itakuwa hapana dhambi kwao (mwanamume wala mwanamke katika) kupokea (au kutoa) ajikomboleacho mwanamke. Hii ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu; basi msiiruke. Na watakaoiruka mipaka ya Mwenyezi Mungu, hao ndio madhalimu (wa nafsi zao). (2:229).*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa utaratibu wa kutaliki Kiislamu ni kama ifuatavyo:

1. Talaka hutolewa kwa matamshi au maandishi kuwa “Nimekuacha” (au kwa maneno mengine yenye maana hiyo).
2. Utoaji wa talaka ushuhudiliwe na mashahidi wawili waadilifu.
3. Talaka itolewe wakati mke yuko katika kipindi cha twahara na wasiwe wamefanya tendo la ndoa katika kipindi hicho. Kama wamefanya tendo la ndoa katika kipindi hicho cha twahara talaka isitolewe kwani haitasihi.

Vile vile talaka haisihi kutolewa mwanamke anapokuwa katika hedhi.

4. Baada ya talaka kutolewa mke analazimika kukaa eda mle mle katika nyumba ya mumewe wakiishi pamoja kama kawaida isipokuwa tu watatengana kwenye malazi. Kila mmoja atawajibika kwa mwenzake kama kawaida katika kipindi chote cha eda.

Eda ya kuachwa ni kipindi maalumu anachokaa mwanamke aliyeachwa ambamo mume aliyemtaliki anaweza kumreja (kwa talaka rejea). Mwanamke huachika baada ya eda na kuwa huru kuolewa na mume mwingine. Kipindi




cha eda kwa wanawake kwa wale wanaopata hedhi ni twahara tatu na wale wasiopata hedhi ni miezi mitatu baada ya kutamkwa talaka. Eda ya mwanamke mwenye mimba huisha pale anapojifungua.

Hekima ya kuamrisha kukaa eda ni kama ifuatavyo:

- (a) Kuwapa wawili muda wa kufikiri zaidi juu ya kuachana kwao na ndio hekima ya amri ya Allah ya kukaa nyumba moja.  
Katika kipindi hiki mwanamke anashauriwa ajipambe na kujiringisha mbele ya mumewe. Kama mke ndiye aliyoomba talaka, mumewe anatakiwa ajirekebishe na kuonyesha mapenzi na upendo kwa mkewe na azidishe kumletea zawadi.
- (b) Kuthibitisha uhalali wa mtoto. Mtoto wa mume aliyetaliki asije akafanywa mtoto wa mume mwingine atakayemuoa mtalikiwa.
5. Kama wawili hawa wataamua kurejeana kabla ya eda kwisha watarejeana kwa wema kwa ahadi mbele ya Allah(s.w) kuwa wataishi kwa upendo.
6. Baada ya eda wawili hawa wanaamrisha na Mola wao kuachana kwa wema.
7. Si halali kwa mwanamume aliyetoa talaka kuchukua chochote katika vile alivyompa mkewe.
8. Mwanamume anayemwacha mkewe anawajibika kumliwaza kwa kumpa kitoka nyumba (kitu) kitakachomuwezesha kumuweka sawa kiuchumi na kisaikolojia kutokana na mabadiliko haya ya maisha (Qur-an 2:41)

Hakuna kiwango maalumu cha kitoka nyumba kilichowekwa, bali mume atatoa kiasi kinachokidhi haja kwa kadiri ya wasaa wake kama aya inavyotuelekeza:

..... وَمَتَّعُوهُنَّ عَلَى الْمَوْسِعِ قَدْرَهُ وَعَلَى الْمُقْتِرِ قَدْرَهُ ..... 

“.....Lakini wapeni cha kuwaliwaza (kitoka nyumba),mwenye wasaa kadiri awezavyo, na mwenye dhiki kadiri awezavyo.....” (2:236).

9. Mwanamke aliyeomba talaka anawajibika kujikomboa kwa kumrudishia mumewe mahari aliyompa. Mume akisamehe mahari hayo hapana lawama.

## Talaka Kabla ya Jimai:

Mwanamume au mwanamke anaweza kughairi na kuamua kuvunja ndoa mapema kabla ya kufanya tendo la ndoa. Mwanamume atatoa talaka na mkewe ataachika hapo hapo bila ya kukaa eda. Kama mwanamume ameshatoa mahari hatadai chochote kama yeye ndiye aliyeamua kumuacha mkewe bali atalazimika kumpa kiliwazo (kitoka nyumba). Ikiwa hajatoa mahari atalazimika kutoa nusu ya mahari. Kama mke ndiye aliyedai talaka atalazimika kumrudisha mumewe mahari aliyempa.

Hukumu ya talaka ya aina hii inabainika katika aya zifuatazo:

لَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ إِنْ طَلَقْتُمُ النِّسَاءَ مَا لَمْ تَمْسُوهُنَّ أَوْ تَفْرِضُوا لَهُنَّ  
فَرِيضَةً ۗ وَمَتَّعُوهُنَّ عَلَى الْمَوْسِعِ قَدْرَهُ وَعَلَى الْمُقْتَرِ قَدْرُهُ مَتَّعًا  
بِالْمَعْرُوفِ ۗ حَقًّا عَلَى الْمُحْسِنِينَ ﴿٣١﴾

Si dhambi kwenu kama mkiwapa wanawake talaka ambao hamjawagusa au kuwabainishia mahari (yao). Lakini wapeni cha kuwaliwaza (kitoka nyumba); mwenye wasaa kadiri awezavyo, na mwenye dhiki kadiri awezavyo. Matumizi hayo (wanayopewa) yawe kama inavyosema Sharia. Ndio wajibu kwa wafanyayo mema. (2:236)

وَإِنْ طَلَقْتُمُوهُنَّ مِنْ قَبْلِ أَنْ تَمْسُوهُنَّ وَقَدْ فَرَضْتُمْ لَهُنَّ فَرِيضَةً فَنِصْفُ  
مَا فَرَضْتُمْ إِلَّا أَنْ يَعْفُوبَ أَوْ يُعْفُوا الَّذِي بِيَدِهِ عُقْدَةُ النِّكَاحِ ۗ وَأَنْ  
تَعْفُوا أَقْرَبُ لِلتَّقْوَى ۗ وَلَا تَنْسُوا الْفَضْلَ بَيْنَكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ بِمَا  
تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٣٢﴾

Na kama mkiwapa talaka kabla ya kuwagusa na mmekwisha wawekeka hayo mahari (basi (wapeni) nusu ya hayo mahari mliyoagana, isipokuwa wanawake wenyewe waache (wasitake kitu), au yule (mume) ambaye kifungo cha ndoa ki mikononi mwake aache (haki yake kwa kumpa mahari kamili). Na kuachiana ndiyo kunakomkurubisha mtu sana na kumcha Mungu. Wala msisahau kufanyiana ihsani baina yenu; hakika Mwenyezi Mungu anayaona yote mnayoyafanya. (2:237)

## Talaka ya Aliyerukwa na Akili na Aliyetenywa Nguvu

Talaka si jambo la kulifanyia maskhara Muislamu anatakiwa awe hadhiri wakati wa kutoa talaka. Ahakikishe kuwa wakati anaamua kutoa talaka akili yake iko katika hali ya utulivu. Talaka ya aliyerukwa na akili haiswihi kama tunavyojifunza katika Hadith:

*Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: “Kila talaka ni halali isipokuwa talaka ya punguani na mwenye kurukwa na akili”. (Tirmidh).*

Pia mtu akilazimishwa kutoa talaka pasina sababu za kisheria au mume na mke wakitalakishwa kwa nguvu huku bado wanapendana katika mipaka ya Allah(s.w), talaka hiyo haitaswihi kama tunavyojifunza katika Hadithi:

*Aysha (r.a) ameeleza kuwa amemsikia Mtume wa Allahakisema: “Hakuna talaka wala hakuna kumwacha huru mtumwa kwa nguvu”. (Tirmidh).*

## Malezi ya Mtoto Mchanga baada ya Talaka

Mtoto mchanga hataachanishwa na mama yake mpaka awe na umri wa miaka miwili - umri wa kuacha kunyonya. Matumizi ya mama na mtoto katika kipindi hiki cha kunyonya mtoto yatakuwa juu ya mume japo mkewe aliyemtaliki atakuwa kwa wazazi wake au penginepo nje ya nyumbani kwake. Lakini mume na mke walioachana, wakiridhiana wanaweza kumwachisha kunyonya kabla ya miaka miwili au wanaweza kumkodisha mwanamke mwingine amnyonyeshe. Hukumu hii ya malezi ya mtoto baada ya mume na mke kuachana inabainishwa vyema katika Qur-an:

﴿ وَالْوَالِدَاتُ يُرْضِعْنَ أَوْلَدَهُنَّ حَوْلَيْنِ كَامِلَيْنِ لِمَنْ أَرَادَ أَنْ يُتِمَّ الرَّضَاعَةَ ۗ وَعَلَى الْمَوْلُودِ لَهُ رِزْقُهُنَّ وَكِسْوَتُهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ ۚ لَا تُكَلَّفُ نَفْسٌ إِلَّا وُسْعَهَا ۚ لَا تُضَارَّ وَالِدَةٌ بِوَلَدِهَا وَلَا مَوْلُودٌ لَهُ بِوَالِدِهِ ۗ وَعَلَى الْوَارِثِ مِثْلُ ذَلِكَ ۗ فَإِنْ أَرَادَا فِصَالًا عَنْ تَرَاضٍ مِّنْهُمَا وَتَشَاوُرٍ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا ۗ وَإِنْ أَرَدْتُمْ أَنْ تَسْتَرْضِعُوا أَوْلَادَكُمْ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ إِذَا سَلَّمْتُمْ مَا آتَيْتُم بِالْمَعْرُوفِ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ۝﴾

*Na wanawake waliozaa wawanyonyeshe watoto wao miaka miwili kamili; kwa anayetaka kukamilisha kunyonyesha; na ni juu ya baba (yake) chakula chao*

(hao watoto na mama) na nguo zao kwa sheria. Wala haikalifishwi nafsi yoyote ila kwa kadiri ya wasaa wake. Mama asitiwe taabuni kwa ajili ya mtoto wake, wala baba (asitiwe taabuni kwa ajili ya mtoto wake). Na kama wote wawili wakitaka kumwachisha ziwa (kabla ya miaka miwili), kwa kuridhiana na kushauriana, basi sio kosa juu yao. Na kama mkitaka kuwapatia watoto wenu mama wa kuwanyonyesha (wengine wasiokuwa mama zao) basi haitakuwa dhambi juu yenu kama mkitoa (kuwapa hao wanyonyeshaji) mlichowaahidi kwa sharia. Na mcheni Mwenyezi Mungu na jueni kwamba Mwenyezi Mungu anayaona yote mnayoyatenda. (2:233)

## Eda ya Kufiwa

Eda ni kipindi cha kungojelea mwanamke baada ya kupewa talaka au baada ya kufiwa na mumewe. Katika kipindi cha eda ni haramu mwanamke kuolewa na mume mwingine. Ambapo tumejifunza kuwa eda ya kuachwa inaisha baada ya twahara tatu au miezi mitatu (kwa wale wasiopata hedhi) au baada ya kujifungua (kwa mke aliyeachwa), eda ya kuachwa inachukua miezi minne na siku kumi au siku mia moja thelathini(130).

Hukumu ya Eda ya kufiwa inabainishwa katika Qur-an:

وَالَّذِينَ يُتَوَفَّوْنَ مِنْكُمْ وَيَذَرُونَ أَزْوَاجًا يَتَرَبَّصْنَ بِأَنْفُسِهِنَّ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ وَعَشْرًا ۖ فَإِذَا بَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِي مَا فَعَلْنَ فِي أَنْفُسِهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٢٣٤﴾ وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِي مَا عَرَضْتُمْ بِهِ مِنْ خِطْبَةِ النِّسَاءِ أَوْ أَكْنُتُمْ فِي أَنْفُسِكُمْ ۖ عَلِمَ اللَّهُ أَنَّكُمْ سَتَذْكُرُونَهُنَّ وَلَكِنْ لَا تُوَاعِدُوهُنَّ سِرًّا إِلَّا أَنْ تَقُولُوا قَوْلًا مَعْرُوفًا ۖ وَلَا تَعْرَبُوا ۚ عُقْدَةَ النِّكَاحِ حَتَّىٰ يَبْلُغَ الْكِتَابُ أَجَلَهُ ۚ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي أَنْفُسِكُمْ فَاحْذَرُوهُ ۚ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ غَفُورٌ حَلِيمٌ ﴿٢٣٥﴾

Na wale wanaofishwa (wanaokufa) miongoni mweni na kuacha wake; hawa (wake) wangoje (wasiolewe) miezi mine na siku kumi. Na wanapofikia muda wao (wa kumaliza eda yao hiyo), basi si dhambi juu yenu kwa yale wanayoyafanyia nafsi zao (hao wanawake) kwa yanayowafiki (kufuata) Sharia. Na Mwenyezi

*Mungu anazo habari za yote mnyoyatenda. Wala si dhambi kwenu katika kupeleka habari ya posa kwa ishara tu (si kwa maneno) kuwaoa wake (walio edani), wala (hapana dhambi pia) katika kutia katika nyoyo zenu azma (za kuwaoa;) Mwenyezi Mungu anajua kwamba nyinyi mtawakumbuka. Lakini msifunge nao ahadi kwa siri (ya kuwaoa maadam eda haijeshu); isipokuwa msemi maneno yaliyo mazuri. Wala msiazimie kufunga ndoa mpaka muda uliyoandikwa (katika eda) ufike mwisho wake. Na jueni ya kwamba Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo katika nafsi zenu, basi mwogopeni. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe, (na) Mpole sana. (2:234-235)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa kizuka (mwanamke aliyefiwa na mumewe) anapokuwa katika eda harusiwi kuolewa wala hata kuposwa wala hata kudhihirishiwa nia ya kuolewa baada ya eda. Bali ni ruhusa kuweka azma moyoni na kuongea naye kwa wema bila kuidhihirisha azma hiyo.

## Kuingizwa au Kutolewa Eda

Katika sheria ya Kiislamu hapana suala la kuingizwa au kutolewa eda na Sheikh. Kizuka huanza eda baada tu ya kufariki mumewe na eda yake huisha mara tu baada ya muda wa miezi mine na siku kumi kuisha. Wala hapana vazi maalum la kukalia eda. Si nguo nyeupe, wala nyeusi, wala kuvaa matambara kama baadhi ya watu wanavyoitakidi. Mwanamke mfiwa atabakia nyumbani kwa mumewe au kwa warithi wa mumewe katika sitara kama kawaida anavyotakiwa awe mwanamke yeyote wa Kiislamu na ataendelea kufanya shughuli zake za nyumbani na nje ya nyumbani zilizo katika mipaka ya sheria ya Kiislamu. Wala hapana sheria yoyote ya kukaa nyumbani kivivu-vivu kama wanavyoitakidi watu wengine.

Hekima kubwa ya kuamrisha kizuka kukaa eda, pamoja na haja ya kuangaliwa uwezekano wa kuachwa na mimba, kunampa kizuka nafasi ya kutulizana na kuliwazika baada ya kupatwa na msiba mkubwa kiasi hicho. Pamoja na kuwa mwanamke baada ya kipindi cha eda huwa huru kutoka nyumbani kwa mumewe marehemu na kuolewa na mume mwingine, akitaka kubakia katika nyumba ya mumewe pamoja na watoto wake, ana haki kisheria kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

وَالَّذِينَ يُتَوَفَّوْنَ مِنْكُمْ وَيَذَرُونَ أَزْوَاجًا وَصِيَّةً لِأَزْوَاجِهِمْ مَتَّعًا إِلَى  
 الْحَوْلِ غَيْرِ إِخْرَاجٍ فَإِنْ خَرَجْنَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِي مَا فَعَلْنَ فِي  
 أَنْفُسِهِنَّ مِنْ مَّعْرُوفٍ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٤٠﴾

*Na wale waliofishwa miongoni mwenu na wakawacha wake, wawausie (warithi wao) kwa ajili ya wake zao kupata matumizi ya mwaka mmoja bila ya kutolewa*

(katika nyumba za waume zao). Na kama wanawake wenyewe wakiondoka, basi si kosa juu yenu kwa yale waliyoyafanya kwa nafsi zao wenyewe yanayofuata sharia. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu, mwenye hikima. (2:240).

Katika baadhi ya jamii za kijahili pamekuwa na mtindo wa kuwarithi wanawake waliofiwa na waume zao kama mali inavyorithiwa na jamaa wa marehemu. Tabia hii ya kumdhaliisha mwanamke na kumnyima uhuru wake wa kuolewa na mwanamume ampendaye imepigwa marufuku katika sheria ya Kiislamu kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا لَا تَحِلُّ لَكُمْ اَنْ تَرِثُوْا النِّسَاءَ كَرِهًا <sup>ط</sup> وَلَا تَعْضُلُوْهُنَّ  
لِتَذَهَبُوْا بِبَعْضِ مَآءِ اٰتِيْتُمُوْهُنَّ .....

Enyi mlioamini! Si halali kwenu kurithi wanawake kwa jeuri. Wala msiwazulie (kuolewa na waume wengine) ili mpate kuwanyang'anya baadhi ya vile mlivyowapa (katika urithi wa waume zao.....) (4:19)

Ama mwanamke mjane wenyewe akiridhika kuolewa na ndugu au jamaa wa marehemu mumewe, ili aweze kubakia pale na watoto wake hapana ubaya ili mradi tu wafunge ndoa kama ilivyo katika sheria.

## Zoezi 2.2

1. Bainisha hatua zilizo muhimu wanandoa kuzifuata ili kuachana Kiislamu.
2. Kuna tafauti gani kati ya Talaka na Eda ?
3. Onesha tafauti zilizopo baina ya talaka zifuatazo:
  - (a) Talaka ya 'Ilaa na Talaka ya Li'aan
  - (b) Talaka ya Khul na Talaka Kabla ya Jimai
4. Eleza maana ya
  - (a) Talaka tatu
  - (b) Talaka rejea
5. Talaka, pamoja na kuwa ni halali inayochukiwa na Allah(s.w) kama inavyosema hadith, bado aya kadhaa za Qur'an zinaonesha umuhimu wake. Kwanini ?

## MIRATHI YA KIISLAMU

### Maana ya Mirathi

Mirathi katika Uislamu ni kanuni na taratibu alizoziweka Allah(s.w) katika kuwagawawia na kuwarithisha familia na jamaa, mali aliyoiacha marehemu. Qur'an inabainisha kuwa, mtu anapofariki dunia, mali yote aliyochuma hurithiwa na Allah(s.w), kisha Yeye huigawa na kuwarithisha watu wanaostahiki, katika uwiano wa haki na uadilifu.

..... اسْتَعِينُوا بِاللَّهِ وَاصْبِرُوا إِنَّ الْأَرْضَ لِلَّهِ يُورِثُهَا مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ ﴿١٢٨﴾

.....ombeni msaada kwa Mwenyezi Mungu na subirini. Ardhi ni ya Mwenyezi Mungu, anamrithisha amtakaye katika waja wake; na mwisho (mwema) ni kwa wamchao. (7:128)

..... وَاللَّهُ مِيرَاثُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ﴿١٠﴾

.....na urithi wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu.....(57:10)

Ukweli huu unajitokeza pia katika dua ya nabii Zakaria alipomuamba Allah(s.w) amjaalie mtoto. Nabii Zakaria alimwomba Mola wake akasema:

..... رَبِّ لَا تَذَرْنِي فَرْدًا وَأَنْتَ خَيْرُ الْوَارِثِينَ ﴿٨٩﴾

...Mola wangu! Usiniache peke yangu na Wewe ndiwe mbora wa wanaorithi (21:89)

### Mwanamke ana Haki ya Kurithi

Katika kugawanya na kuirithisha mali kwa wahusika, Allah(s.w)hakumnyima mwanamke haki ya kurithi akiwa mtoto, mke au mama. Wote wanawake na wanaume wanamafungu maalumu la kurithi katika mali aliyoiacha marehemu.

لِلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِّمَّا تَرَكَ الْوَالِدَانِ وَالْأَقْرَبُونَ وَلِلنِّسَاءِ نَصِيبٌ مِّمَّا تَرَكَ الْوَالِدَانِ وَالْأَقْرَبُونَ مِمَّا قَلَّ مِنْهُ أَوْ كَثُرَ نَصِيبًا مَّفْرُوضًا ﴿٧﴾

*“Wanaume wana sehemu katika mali wanayoyachumawazazi na jamaa walio karibu. Na wanawake (pia) wanayo sehemu katika yale waliyoyaacha wazazi na jamaa walio karibu. Yakiwa kidogo au mengi. (Hizi) ni sehemu zilizofaradhiwa (na Allah(s.w))” (4:7)*

## Mirathi katika Jamii za Kijahili

Katika jamii nyingi za kijahili kama vile jamii ya Waarabu kabla ya Mtume Muhammad(s.a.w), watoto wadogo ambao hawajafikia baleghe, walemavu na wazee ambao hawakuwa na uwezo wa kupigana vita katika kuihami heshima ya familia na kabila kwa ujumla, hawakupata chochote katika mirathi. Aghalabu katika jamii zote za kijahili mwanamke akiwa binti au mke, au mama au katika uhusiano wowote ule kwa marehemu, hakuwa na haki yoyote ile katika urithi.

Badala yake wanawake wenyewe walifanywa mali ya kurithiwa kwa nguvu na ndugu wa marehemu au mtoto mkubwa wa kiume wa marehemu ambaye hakuzaliwa na huyo mama anayerithiwa. Waliwarithi kama wake au vinginevyo waliwaoza kwa wanaume wengine kwa nguvu kinyume cha ridhaa ya wajane hao. Kwa namna hii wanawake walirithiwa kama sehemu ya mali ya marehemu na waliuzwa na kununuliwa kama bidhaa.

Uislamu umepiga marufuku tabia hii katika aya ifuautayo:

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَحِلُّ لَكُمْ أَنْ تَرْتُوا النِّسَاءَ كَرْهًا وَلَا تَعْضُلُوهُنَّ  
لِتَذْهَبُوا بِبَعْضِ مَا ءَاتَيْتُمُوهُنَّ إِلَّا أَنْ يَأْتِيَنَّ بِفَحِشَةٍ مُّبِينَةٍ  
وَعَاشِرُوهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ.....

*Enyi mlioamini! Si halali kwenu kurithi wanawake kwa jeuri. Wala msiwazuie (kuolewa na wanaume wengine) ili mpate kuwanyang'anya baadhi ya vile mlivyowapa (Hapana ruhusa haya) isipokuwa wawe wamefanya uovu ulio wazi nakaeni nao kwa wema.....” (4:19).*

وَلَا تَنْكِحُوا مَا نَكَحَ ءَابَاؤُكُمْ مِنَ النِّسَاءِ إِلَّا مَا قَدْ سَلَفَ إِنَّهُ  
كَانَ فَنَحِشَةً وَمَقْتًا وَسَاءَ سَبِيلًا

*Wala msiwaoe wake waliowaoa baba zenu, isipokuwa yale yaliyokwisha pita. Bila shaka jambo hili ni uovu na chukizo na ni njia mbaya. (4:22).*



## Mambo ya Kuzingatia Kabla ya Kugawanya Urithi

Kabla mali ya marehemu haijagawanywa kwa warihi wake, hapana budi kuzingatia yafuatayo:

### **(a)Haki zilizofungana na mali ya urithi:**

Mali ya marehemu haitakuwa halali kwa warithi wake mpaka zitolewe haki zifuatazo:

- (i) Madeni.
- (ii) Zakat.
- (iii) Gharama za makazi ya mkewe katika kipindi cha eda.
- (iv) Usia ambao hauzidi theluthi moja (1/3) ya mali yote iliyobakia.

### **(b)Sharti la kurithi:**

Kurithi kuna sharti tatu:

- (i) Kufa yule mwenye kurithiwa (si halali kurithi mali ya mtu aliyehai).
- (ii) Kuwepo hai mrithi wakati akifa mrithiwa. Kwa mfano, kama wawili wanaorithiana mathalani baba na mtoto wote wamekufa. Aliyekufa nyuma (au aliyeshuhudia kifo cha mwenzie) atakuwa mrithi wa yule aliyetangulia kufa.
- (iii)Kukosekana mambo yenye kumzuilia mtu kurithi.

### **(c) Mambo yanayomzuilia mtu kurithi**

Mrithi huzuilika kurithi itakapopatikana na moja kati ya sababu zifuatazo:

- (i) Kumuuu amrithiye: Yaani mtu hatamrithi aliyemuua ijapokuwa kwa bahati mbaya.

*Abu Hurairah(r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema Mwenye kuua hapati chochote katika mirathi. (Tirmidh, Ibn Majah).*

- (ii) Kuhitalifiana katika dini:

Muislamu hamrithi kafiri, mshirikina, mkristo au myahudi na wala kafiri, mshirikina, mkristo au myahudi hatamrithi Muislamu hata akiwa karibu naye kiasi gani katika nasaba.

*Usama bin Zaid(r.a)ameeleza kuwa mtume wa Allah amesema: Muislamu hamrithi mshirikina wala mshirikina hamrithi Muislamu. (Bukhaary na Muslim)*

*Pia Mtume(s.a.w) amesema katika Hadithi iliyosimuliwa na Abdullah bin Amri(r.a) kuwa: Watu wa dini mbili tofauti hawatarithiana. (Abu Dauwd, Ibn Majah, Tirmidh).*

(iii) Mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa hana haki ya kumrithi baba aliyemzaa na baba hana haki katika mirathi yake, kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Amri bin Shuab(r.a) ameeleza kutoka kwa baba yake naye kutoka kwa babu yake kuwa Mtume wa Allah amesema: "Atakayezini na mwanamke muungwana au na mjakazi, mtoto atakayepatikana humo hana haki naye. Hatomrithi na wala hatarithiwa naye". (Tirmidh)*

#### (d) Sababu za Kurithi:

Mtu hurithi kwa sababu moja katika hizi:

- (i) Kuwa na nasaba na marehemu (baba, mama, mtoto, ndugu, n.k.).
- (ii) Kuoana kwa ndoa halali (yaani mume humrithi mke na mke humrithi mumewe).
- (iii) Kuacha huru, yaani mwenye kumpa uhuru mtumwa humrithi huru wake.

### Qur'an Inavyogawa Mirathi

Mgawanyo wa mirathi umebainishwa katika Qur-an kama ifuatavyo:

يُوصِيكُمُ اللَّهُ فِي أَوْلَادِكُمْ لِلذَّكَرِ مِثْلُ حَظِّ الْأُنثِيَيْنِ ۚ فَإِن كُنَّ نِسَاءً فَوْقَ اثْنَتَيْنِ فَلَهُنَّ ثُلُثَا مَا تَرَكَ ۚ وَإِن كَانَتْ وَاحِدَةً فَلَهَا النِّصْفُ ۚ وَلِأَبَوَيْهِ لِكُلِّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا السُّدُسُ مِمَّا تَرَكَ إِن كَانَ لَهُ وَلَدٌ ۚ فَإِن لَّمْ يَكُن لَهُ وَلَدٌ وَوَرِثَتُهُ أَبَوَاهُ فَلِأُمِّهِ الثُّلُثُ ۚ فَإِن كَانَ لَهُ إِخْوَةٌ فَلِأُمِّهِ السُّدُسُ ۚ مِن بَعْدِ وَصِيَّةٍ يُوصِي بِهَا أَوْ دِينٍ ۚ ءِآبَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ لَا تَدْرُونَ أَيُّهُمْ أَقْرَبُ لَكُمْ نَفَعًا فَرِيضَةٌ مِّنَ اللَّهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿١١﴾

*Mwenyezi Mungu anakuusieni juu ya watoto wenu: Mwanamume apate sawa na sehemu ya wanawake wawili. Na ikiwa wanawake ni (wawili au) zaidi ya wawili, basi watapata thuluthi mbili (2/3) ya mali aliyoiacha (maiti). Lakini akiwa mtoto mwanamke ni mmoja, basi apewe nusu. Na wazazi wake wawili kila mmoja wao apate sudusi (1/6) ya mali aliyoiacha (maiti), akiwa maiti huyo*

(anaye mtoto au mjukuu). Lakini kama hana mtoto, na wazazi wake wawili wamekuwa ndio warithi wake basi mama yake atapata (1/3)(na baba) thuluthi mbili (2/3). Na kama (huyo maiti)anaye ndugu basi mama yake atapata sudusi moja (1/6). Na huku kurithi kunakuwa baada ya kutoa aliyoyausia au kulipa deni. Baba zenu na watoto wenu, nyinyi hamjui ni nani miongoni mwao aliye karibu zaidi kukunufaisheni. Hiyo ni sheria iliotoka kwa Mwenyezi Mungu. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni mjuzi mwenye hikima.(4:11)

﴿ وَلَكُمْ نَصْفُ مَا تَرَكَ أَزْوَاجُكُمْ إِنْ لَمْ يَكُنْ لَهُنَّ وَلَدٌ فَإِنْ كَانَ لَهُنَّ وَلَدٌ فَلَكُمْ الرُّبْعُ مِمَّا تَرَكَنَّ مِنْ بَعْدِ وَصِيَّةٍ يُوصِيَنَّ بِهَا أَوْ دَيْنٍ ۗ وَلَهُنَّ الرُّبْعُ مِمَّا تَرَكَتُمْ إِنْ لَمْ يَكُنْ لَكُمْ وَلَدٌ فَإِنْ كَانَ لَكُمْ وَلَدٌ فَلَهُنَّ الثُّمْنُ مِمَّا تَرَكَتُمْ ۗ مِنْ بَعْدِ وَصِيَّةٍ تُوصُونَ بِهَا أَوْ دَيْنٍ ۗ وَإِنْ كَانَ رَجُلٌ يُورَثُ كَلَلَةً أَوْ امْرَأَةً وَوَلَدًا أَخًا أَوْ أُخْتًا فَلِكُلِّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا الشُّدُسُ ۗ فَإِنْ كَانُوا أَكْثَرَ مِنْ ذَلِكَ فَهُمْ شُرَكَاءُ فِي الثُّلُثِ ۗ مِنْ بَعْدِ وَصِيَّةٍ يُوصَىٰ بِهَا أَوْ دَيْنٍ غَيْرِ مُضَارٍّ وَصِيَّةً مِّنَ اللَّهِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَلِيمٌ ﴿١٢﴾

Na nyinyi mtapata nusu (1/2) ya (mali) walizoacha wake zenu, kama wao hawana watoto (wala wajukuu). Na ikiwa wana mtoto (au mjukuu), nyinyi mtapata robo (1/4) yawalivyoviacha, baada ya kutoa walivyousia au kulipa deni. Nao (wake zenu watapata robo ya mlivyoviacha, ikiwa hamna mtoto (wala mjukuu) basi wao (hao wanawake) watapata thumni (1/8) ya vile mlivyoviacha, baada ya kutoa mlivyousia au kulipa deni. Na kama mwanamume au mwanamke ni mkiwa - hana mtoto (wala mjukuu) wala wazazi, lakini anaye kaka \*(wa kwa mama) au dada (wa kwa mama pia), basi kila mmoja katika hawa atapata sudusi (sehemu ya sita). Na wakiwa zaidi kuliko hivyo basi watashirikiana katika thuluthi baada ya kutoa vilivyousiwa au kulipa deni, pasipo kuleta dhara. (Huu) ndio wasia uliotoka kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye Upole. (4:12)

يَسْتَفْتُونَكَ قُلِ اللَّهُ يُفْتِيكُمْ فِي الْكَلَالَةِ ۚ إِنَّ أَمْثُلًا هَلَكَ لَيْسَ لَهُ وَاوَدٌ  
 وَلَهُرُ أُخْتٌ فَلَهَا نِصْفُ مَا تَرَكَ ۚ وَهُوَ يَرِثُهَا إِنْ لَمْ يَكُنْ لَهَا وَاوَدٌ ۚ وَإِنْ كَانَتْ  
 أَنْثَىٰ فَلَهَا مِثْلُ ثَلَاثِينَ ۚ مِمَّا تَرَكَ ۚ وَإِنْ كَانُوا إِخْوَةً رِجَالًا وَنِسَاءً فَلِلَّذَكَرِ مِثْلُ  
 حَظِّ الْأُنثَىٰ ۚ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ أَنْ تَضِلُّوا ۗ وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿١٧٦﴾

*Wanakuuliza sema: "Mwenyezi Mungu anakupeni hukumu juu ya mkiwa. Kama mtu amekufa, hali hana mtoto, lakini anaye dada; basi atapata (huyo dada) nusu ya yale aliyoyaacha (maiti). Na yeye (mtu huyu) atamrithi (dada yake) ikiwa hana mwana. Na kama wao ni (madada) wawili, basi watapata thuluthi mbili za yale aliyoyaacha. Na wakiwa ndugu wanaume na wanawake, basi (kila) mwanamume (mmoja) atapata sehemu iliyo sawa na ya wanawake wawili. Mwenyezi Mungu anakubainishieni ili msipotee; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu. (4:176)*

Kama ilivyosisitizwa mwishoni mwa aya hizi, huu ndio mgawanyo wa mirathi aliouweka Allah(s.w) na kugawanya mirathi kwa kufuata sheria ya kimila, sheria ya Bunge au sheria nyingine yoyote ya kitwaghuuti, ni kuchupa mipaka ya Mwenyezi Mungu. Allah(s.w) anasisitiza kufuatwa kwa sheria hii katika aya mbili zinazofuatia hizi:

تِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ ۚ وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ يُدْخِلْهُ جَنَّاتٍ تَجْرِي  
 مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ۚ وَذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١٣﴾  
 وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَتَعَدَّ حُدُودَهُ يُدْخِلْهُ نَارًا خَالِدًا فِيهَا  
 وَلَهُ عَذَابٌ مُهِينٌ ﴿١٤﴾

*Hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na anayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume, (Mwenyezi Mungu) atamwingiza katika Bustani zipitazo mito mbele yake, wakae humo milele. Na huko ndiko kufaulu kukubwa. Na anayemuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kuiruka mipaka yake, (Mwenyezi Mungu) atamwingiza motoni na humo atadumu na atapata adhabu zifedheheshazo. (4:13-14)*

Katika aya hizi zinazobainisha mgawanyo wa mirathi (4:11-12), (4:176) tunajifunza kuwa watoto wa kiume/wanaume wanapata mara mbili ya watoto wa kike/wanawake na baba anapata mara mbili zaidi kuliko mama. Je, sheria ya Allah(s.w) inapendelea wengine na kuwadhulumu wengine haki zao? Allah(s.w) ni Mkwasi, Mwenye kujitosheleza asiyehitajia chochote kutoka kwa viumbe vyake, bali viumbe ndio wanaomuhitajia. Pia Allah(s.w) ni Muadilifu na mpole mno kwa viumbe vyake. Hivyo, Allah(s.w) ametakasika na kila sifa mbaya na kila sifa za upungufu kama vile kupendelea au kudhulumu baadhi ya viumbe vyake. Kwa vyovyote vile, mgawanyo huu wa Allah(s.w) ni mgawanyo unaotoa haki kwa kila mrithi kwani ni mgawanyo wa mjuzi, mwenye hikima na mpole kwa viumbe vyake. Mwenyezi Allah(s.w) amemalizia aya hizi kwa msitizo:

..... إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿١١﴾

“...Bila shaka Mwenyezi Mungu ni mjuzi na mwenye hikima.” (4:11).

..... وَصِيَّةٌ يُوصَىٰ بِهَا أَوْ دَيْنٍ غَيْرَ مُضَارٍّ وَصِيَّةٌ مِّنَ اللَّهِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ

حَلِيمٌ ﴿١٢﴾

“..... Huu ndio usia uliotoka kwa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni mjuzi na mpole.”. (4:12).

..... يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ أَن تَضَلُّوا وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿١٧٦﴾

“... Mwenyezi Mungu anakubainishieni ili msipotee; na Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa kila kitu.” (4:176).

Kwa kuzingatia majukumu ya wanaume na wanawake katika familia, kuna hekima kubwa ya kumzidishia mwanamume mara mbili ya kile anachopata mwanamke katika mafungu ya mirathi. Mwanamke amepunguziwa fungu kwa kuwa hana matumizi ya kumlazimu kama alivyo mwanamume. Halazimiki kwa matumizi ya watoto wake, na kazi yake na hata matumizi yake binafsi.

Bali matumizi yote hayo huwa juu ya mwanamume. Kwa mfano, iwapo urithi ulioachwa na baba mzazi kwa mtoto wake wa kike na wa kiume ni shilingi 3,000,000/=, kulingana na mgawanyo wa Qur-an mtoto wa kiume atapata shilingi 2,000,000/= na mtoto wa kike atapata shilingi 1,000,000.

Utakuta zile za kijana mwanamume zitakwisha kwa matumizi mbali mbali yanayomlazimu ikiwa ni pamoja na matumizi ya huyo dada yake ambaye licha ya kutowajibika kutoa matumizi kwa yeyote yeye mwenyewe anabakia

kutunzwa na kulelewa na kaka yake na yuko huru kutumia urithi wake huo hata kwa kununulia mapambo ya dhahabu.

Mwanamume amezidishiwa fungu kwa sababu matumizi yake yanayomlazimu kisheria ni mengi. Ndiye mwenye jukumu la kugharamia gharama zote za maisha kwa mke wake/wake zake na watoto wake, wazazi wake na wale wote wanaomtegemea katika familia.

Bila shaka, wale wanaoishutumu sheria hii ya mirathi kuwa inawakandamiza wanawake, hawajaiona hekima hii au wamepata mwanya wa kuwaghilibu watu waone sheria zilizotungwa na mwanadamu ndizo bora kuliko sheria ya Allah(s.w). Allah(s.w) anatutanabahisha:

أَفْحُكْمَ الْجَاهِلِيَّةِ يَبْغُونَ وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ اللَّهِ حُكْمًا لِقَوْمٍ يُوقِنُونَ ﴿٥٠﴾

*Je, wao wanataka hukumu za kijahili? Na nani aliye mwema zaidi katika hukumu kuliko Mwenyezi Mungu, kwa watu wenye yakini? (5:50).*

Aya tulizozirejea (4:11-12) na (4:176) zimetaja kwa uwazi na kwa ukamilifu watu wenye kurithi na mafungu yanayorithiwa.

## **Wanaume Wenye Kurithi ni Kumi na Tano (15)**

- 1.Mtoto mwanamume.
- 2.Mtoto mwanamume wa mtoto mwanamume (mjukuu).
- 3.Baba.
- 4.Babu wa kwa baba.
- 5.Ndugu mwanamume wa kwa baba na mama.
- 6.Ndugu mwanamume wa kwa baba tu.
- 7.Ndugu mwanamume wa kwa mama tu.
- 8.Mtoto mwanamume wa kwa ndugu mwanamume wa kwa baba na mama.
- 9.Mtoto mwanamume wa ndugu mwanamume wa kwa baba tu.
- 10.Ami (baba mdogo) wa kwa baba na mama (ndugu yake baba na mama).
- 11.Ami wa kwa baba tu.
- 12.Mtoto mwanamume wa Ami wa kwa baba na mama.

- 13.Kijana mwanamume wa Ami wa kwa baba.
- 14.Mume.
- 15.Bwana mwenye kumwacha mtumwa huru.

### **Wanawake Wenye Kurithi ni Kumi (10)**

- 1.Binti (mtoto wa kike).
- 2.Binti wa mtoto mwanamume (mjukuu).
- 3.Mama.
- 4.Dada wa kwa baba na mama.
- 5.Dada wa kwa baba.
- 6.Dada wa kwa mama.
- 7.Bibi mzaa baba.
- 8.Bibi mzaa mama.
- 9.Mke.
- 10.Bibi mwenye kuacha mtumwa huru.

### **Kuzuiliana**

Tumeona kuwa wanaume wenye kurithi ni 15 na wanawake wanaorithi ni 10. Lakini wote hawa 25 wakikutana pamoja hawawezi kurithi wote bali baadhi yao huwazuilia wengine wasipate kitu au wasipate fungu kubwa. Katika kipengele hiki tunaonyesha wanaozuliwa na wasiozuliwa.

- 1.Mtoto mwanamume hazuiliwi na mtu.
- 2.Mjukuu huzuiliwa na mtoto mwanamume na kila mtoto wa kiume aliyeko mbali huzuiliwa na aliyoko karibu na marehemu.
- 3.Baba hazuiliwi na mtu.
4. Babu wa upande wowote huzuiliwa na baba au babu wa karibu zaidi (kama vile baba yake baba humzuilia babu yake baba).
5. Ndugu wa kwa baba huzuiliwa na ndugu wa kwa baba na mama; na kila amzuiliaye yeye (huyo ndugu wa kwa baba na mama) vile vile huzuiliwa na dada wa kwa baba na mama akiwa pamoja na binti au binti wa mtoto wa kiume (mjukuu) au wote wawili.

6. Ndugu wa kwa mama huzuiliwa na mtoto au mtoto wa mtoto mwanamume au baba au babu.
7. Mume hazuiliwi na mtu wala
8. Mke hazuiliwi na mtu.
9. Binti hazuiliwi.
10. Mama hazuiliwi.
11. Bibi huzuiliwa na mama.

Mafungu ya urithi yaliyotajwa katika Qur-an (4:11-12), (4:176) ni haya sita yafutayo:

1. Nusu (1/2)
2. Robo (1/4)
3. Thuluthi (1/3)
4. Thuluthi mbili (2/3)
5. Sudusi (1/6)
6. Thumuni (1/8)

## Wenye Kupewa Mafungu

Katika warithi kuna wenye kupata mafungu maalum katika hayo mafungu sita; na kuna wasiokuwa na mafungu maalum ambao hupata kilichobakia baada ya wenye mafungu kuchukua mafungu yao au kupata mali yote ikiwa hapana wenye mafungu. Wasio na mafungu huitwa asaba.

Wenye mafungu maalum katika urithi ni watu kumi na na mbili (12) wafuatao:

1. Baba.
2. Babu.
3. Binti.
4. Binti wa mtoto mwanamume (mjukuu).
5. Ndugu wa kwa mama.
6. Dada wa kwa baba na mama.
7. Dada wa kwa baba.



8.Dada wa kwa mama.

9.Mama.

10.Bibi.

11.Mume.

12.Mke.

## **Asaba - Warithi Wasio na Mafungu Maalum**

Asaba ni warithi wasiowekewa fungu maalum na hustahiki kupata mali yote ikiwa hapana wenye mafungu au kupata kilichobakia baada ya wenye mafungu kuchukua haki yao. Asaba wenyewe wako wa aina tatu:

(a)Asaba kwa nafsi yake.

(b)Asaba wa pamoja na mtu mwingine.

(c)Asaba kwa sababu ya mtu mwingine.

### ***(a)Asaba kwa nafsi yake***

Ni wale wanaume tu ambao uhusiano wao na huyu marehemu haukuingiliwa na mwanamke. Nao ni hawa wafuatao:

1.Mtoto mwanamume.

2.Mjukuu (mwanamume).

3.Baba.

4.Babu (baba yake baba).

5.Ndugu wa kwa baba na mama.

6.Ndugu wa kwa baba.

7.Mtoto mwanamume wa ndugu wa kwa baba na mama.

8.Mtoto mwanamume wa ndugu wa kwa baba.

9.Ami wa kwa baba na mama.

10.Ami wa kwa baba.

11.Mtoto mwanamume wa Ami wa kwa baba na mama.

- 12.Mtoto mwanamume wa Ami wa kwa baba.
- 13.Bwana na bibi mwenye kumuacha mtumwa huru.
- 14.Asaba wa mwenye kuacha huru mtumwa.

**(b) Asaba wa Pamoja na mtu mwingine:**

- 1.Binti akiwa pamoja na kijana mwanamume.
- 2.Binti wa mtoto wa kiume (mjukuu) akiwa pamoja na mtoto mwanamume wa mtoto mwanamume (mjukuu wa kiume).
- 3.Dada wa kwa baba na mama akiwa pamoja na ndugu wa kwa baba na mama.
- 4.Dada wa kwa baba akiwa pamoja na ndugu wa kwa baba.
- 5.Dada wa kwa baba na mama au wa kwa baba akiwa pamoja na babu.

**(c) Asaba kwa sababu ya mtu mwingine:**

Ni dada wa kwa baba na mama au wa kwa baba tu atakapokuwa pamoja na binti au binti wa mtoto wa kiume au wote wawili.

## **Musharakah - Kushirikiana Fungu:**

Ingawa asaba wote utaratibu wao wa kurithi ni mmoja lakini nani kati yao mwenye haki zaidi ya kurithi pindi wakitokea pamoja itategemea na uzawa wa karibu na uwiano wa uhusiano na maiti. Kwa mfano, uhusiano wa kwa baba na mama una nguvu zaidi kuliko uhusiano wa kwa baba tu, kwa hiyo, asaba wa kwa baba na mama ana haki ya kurithi kuliko asaba wa kwa baba tu.

Tumefahamu kwamba asaba hana fungu, bali huchukua urithi wote kama hakuna mwenye fungu, au huchukua kilicho bakia baada ya wenye mafungu kuchukua chao au hukosa kabisa kama hakuna kilicho bakia au wakati mwingine asaba wenye daraja sawa na mwenye fungu, watashirikiana fungu hilo. Kwa mfano: Amekufa mtu akaacha mume, mama, ndugu wa kwa mama zaidi ya mmoja na ndugu wa kwa baba na mama.

## **Ugawaji wa Mirathi**

- Mume ana nusu  $(1/2) = 1/2$
- Mama ana sudusi  $(1/6) = 1/6$
- Ndugu wengine wa kwa mama wana thuluthi  $(1/3) = 2/6$

Hapo utaona kuwa mafungu yote sita yamegawanywa yakaisha na ndugu wa kwa baba na mama hawakupata kitu. Hapa itabidi ile Thuluthi waliyoipata ndugu wa kwa mama wagawane sawa sawa na ndugu wa kwa baba na mama maana nao wanayo haki ya ndugu wa kwa mama kama wao na wala hakoseshwi kwa sababu ya unasaba wake.

## **Mifano ya Namna ya Kurithisha**

Wakikutana warithi na pakawa hapana amzuiliaye mwenziwe na ikawa wote ni **asaba**, wataigawanya mali iliyopo sawa sawa kwa kadri ya idadi yao. Kwa mfano: Akifa mtu, akawa ameacha vijana wanamume wanne, mali yote itagawanywa mafungu manne sawa sawa na kila mmoja apewe fungu lake.

Ama wakikutana **asaba** wanaume na wanawake, bali kila mwanamume atahesabiwa kuwa ni wanawake wawili na mali itapigwa mafungu kila mwanamume mmoja apewe mafungu mawili na kila mwanamuke apewe fungu moja. Kwa mfano: Amekufa mtu kaacha watoto **sita**, **wanne** wanaume na wawili wanawake. Wanaume **wane** watahesabiwa kuwa ni sawa na wanawake wanane. Kwa hiyo mali itagawanywa katika mafungu kumi yaliyo sawa sawa. Wanaume watapata mafungu mawili kila mmoja na wanawake watapata fungu moja moja.

Iwapo warithi ni mchanganyiko wa wenye mafungu maalum na **asaba**, itabidi kutafuta kigawe kidogo cha shirika (Kigawe kidogo cha shirika - KDS) ili kupata mafungu yatakayogawiwa kwa kila mrithi kwa kadiri ya haki yake anayoistahiki. Hebu tuangalie mifano kadhaa ya mgawanyo wa mirathi.

### **Mfano. 1**

Amekufa mke na kuacha

(i)Mume.

(ii)Mtoto mwanamume.

(iii)Baba.

Wenye mafungu maalum kati ya hawa ni:

(i) Mume - ana robo (1/4) madhali yupo mtoto.

(ii) Baba - ana sudusi(1/6) madhali yupo mtoto.

**Asaba:** Mtoto mwanamume na atachukua kitakachobakia.

**Ugawaji:** Mafungu yatakayotolewa ni:  $(1/4)$ ,  $(1/6)$ . Hesabu ndogo ambayo inaweza kutolewa mafungu ya urithi ni 12 yaani KDS ya 4 na 6. Kwa hiyo

mali ya urithi itagawanywa kwenye mafungu 12 yaliyo sawa sawa na ugawaji utakuwa kama ifuatavyo:

- (i) Mume atapata  $\frac{1}{4}$  ya 12 =  $\frac{1}{4} \times 12 = 3$  Yaani atachukua mafungu 3 katika mafungu 12
- (ii) Baba atapata  $(1/6)$  ya 12 =  $(1/6) \times 12 = 2$ . Yaani atachukua mafungu 2 kati ya mafungu 12.

### Mfano 2:

Amekufa mume na kuacha wafuatao:

- (i) Mke mmoja.
- (ii) Mama.
- (iii) Mjuku mmoja wa kike (binti wa mtoto mwanamume).
- (iv) Mtoto mwanamume.
- (v) Watoto watatu wanawake.

Kama mali iliyoachwa na marehemu ni shilingi 1,200,000/=, utarithisha wahusika kama ifuatavyo:

Wenye mafungu maalum kati ya hawa ni:

- (i) Mke ambaye atapata thumuni  $1/8$  kwa sababu wapo watoto.
- (ii) Mama atapata sudusi  $1/6$  ya mali kwa sababu wapo watoto.
- (iii) Mjuku hapati kitu kwa sababu wapo watoto ambao humzuilia.
- (iv) Mtoto mwanamume na watoto wanawakewatagawana mali iliyobakia, wakiwa hao asaba mwanamume achukue sawa na wanawake wawili(2:1)

Njia mbili zifuatazo zinaweza kutumika katika kurithisha wahusika:

### **(a) Hisabu ndogo inayoweza kutolewa mafungu ni 24. Yaani KDS ya 8 na 6.**

Kila fungu litakuwa na thamani ya shilingi 50,000 -  $(1,200,000/24)$  Mke atapata  $1/8$  ya 24 = 3 yaani atapata  $3 \times 50,000/=$

Mama atapata  $\frac{1}{6}$  ya 24 ( $1 \times 24$ ) = 4 yaani atapata  $4 \times 50,000 = 200,000/=$   
 Asaba watarithi mali iliyobakia ambayo ni  $1,200,000 - (150,000 + 200,000) = 850,000$ .

Mali hii itagawanywa katika mafungu 5 (kumbuka: Mwanamume atapata sawa na wanawake wawili). Hivyo, kila mtoto wa kike atapata:  
 Shs.  $\frac{1}{5} \times 850,000 = 170,000$

Mtoto wa kiume atapata shs.  $\frac{2}{5} \times 850,000$  (au  $2 \times 170,000$ ) = 340,000

(b)Njia ya pili ni kutafuta sehemu ya mali atakayopata kila mwenye fungu maalum. Kama mali inayorithiwa ni shs.  $1,200,000/=$

(i) Mke atapata  $\frac{1}{8}$  ya  $1,200,000 = 1 \times \frac{1,200,000}{8} = 150,000/=$

(ii) Mama atapata  $\frac{1}{6}$  ya  $1,200,000 = 1 \times \frac{1,200,000}{6} = 200,000/=$

(iii) Asaba watagawana mali iliyobakia ambayo ni  $1,200,000 - 350,000 = 850,000$ .

Kuna mabinti watatu na kijana mmoja ambaye ni sawa na mabinti wawili. Hivyo mali iliyobakia itagawanywa katika mafungu 5 ambapo kila binti atapata:  $1 \times \frac{850,000}{5} = 170,000/=$

Kijana atapata sawa na mabinti wawili sh.  $2 \times 170,000 = 340,000/=$

### **Kuongeza mafungu (Awl)**

Iwapo idadi ya mafungu yatakayogaiwa kwa warithi wenye mafungu maalum ni kubwa kuliko mafungu yaliyopatikana kwa njia ya (KDS), idadi ya mafungu itabidi iongezeke ili kila mmoja apate haki yake. Hebu tuangalie mifano ifuatayo:

#### **Mfano 1:**

Amefariki mke na kuacha warithi wafuatao:

(i) Mume.

(ii) Dada wawili wa kwa baba na mama.

Wote hawa wana mafungu maalum:

- (i) Mume atapata  $(1/2)$  kwa sababu hapana mtoto.
- (ii) Dada wawili watapata thuluthi mbili  $(2/3)$  kwa sababu wako zaidi ya mmoja.

KDS ya 2 na 3 ni 6, hivyo:

- (i) Mume atapata nusu  $(1/2)$  ya mafungu  $6 = 3$ .
- (ii) Dada wawili watapata thuluthi mbili  $(2/3)$  ya mafungu  $6 = 4$ .

Utakuta kuwa jumla ya mafungu yanayohitajika ni  $7(3 + 4)$  badala ya 6.

Hivyo mali ya marehemu itagawanywa katika mafungu yaliyo sawa sawa. Katika hayo mume atapata mafungu 3 na kila dada atapata mafungu 2.

### **Mfano 2:**

Amefariki mke na kuacha warithi wafuatao:

- (i) Mume.
- (ii) Mama.
- (iii) Dada mmoja wa kwa baba na mama.

Wote hawa wana mafungu maalum:

- (i) Mume atachukua  $(1/2)$  kwa sababu hapana mtoto.
- (ii) Mama atachukua  $(1/3)$  kwa sababu hapana mtoto na dada aliyopo ni mmoja tu.
- (iii) Dada atapata  $(1/2)$  yuko peke yake.

### **Mgawanyo:**

KDS ya 2 na 3 ni 6.

- (i) Mume atapata  $(1/2)$  ya mafungu  $6 =$  mafungu 3.
- (ii) Mama atapata  $(1/3)$  ya mafungu  $6 =$  mafungu 2.
- (iii) Dada atapata  $(1/2)$  ya mafungu  $6 =$  mafungu 3

Jumla ya mafungu yanayohitajika ni 8, badala ya 6. Hivyo itabidi mafungu mawili yaongezwe kwenye (KDS) ili kila mrithi apate haki yake.

## Sehemu ya Masikini na Jamaa wa Karibu katika Mirathi:

Waumini wana usiwa kuwa japo ni wazi kuwa mali ya urithi ni haki ya warithi kwa mujibu wa sheria, hawana budi kuwahurumia mayatima, masikini na jamaa wa karibu kwa kuwapa kitu kutokana na urithi japo kidogo na hasa watakapohudhuria wakati wa kugawanya.

Na wakati wa kugawanya wakihudhuria jamaa na mayatima na masikini, wapeni kitu katika hayo (mali ya urithi) na waambieni kauli njema(4:8).

### Zoezi 2:3

1. Ni haki zipi za awali zinazotakiwa kutolewa kabla ya kugawa mirathi kwa warithi.
2. Ni mambo yepi yanayotakiwa kusibu ili mali ya mtu iwe halali kurithiwa.
3. Taja sababu zinazompatia mtu haki ya kurithi.
4. Mwenye haki ya Kurithi hatorithi mali ya anayemuhusu ikiwa
  - (a) \_\_\_\_\_
  - (b) \_\_\_\_\_
5. Bainisha warithi waliotajwa katika Qur'an pamoja na fungu la kila mmoja wao.
6. Baada ya kuzikwa Hamza bin Abuu Taalib, ikabainika kuwa marehemu ameacha watoto wakiume watano na mabint sita, wajane watatu, pamoja na wazazi wake wawili. Ameacha pia wadogo zake wanne, wawili wakiwa wanawake.

Gawanya mirathi kwa wanaostahiki ikiwa, marehemu ameacha Nyumba Tatu za Kisasa zenye thamani ya milioni thelathini, duka lenye thamani ya milioni kumi na fedha tasilimu laki Tano.

## KUDHIBITI UZAZI

### Historia ya Kampeni ya Kudhibiti Uzazi

Upo ushahidi wa kutosha kuwa watu binafsi katika zama zote wamekuwa wakijitahidi kuzaa watoto wanaopishana miaka ili kuhifadhi afya ya mama na mtoto. Juhudi za serikali huko nyuma (yaani kabla ya karne ya 20) zilikuwa ni kuwashawishi raia kuoana na kuzaana. Lakini kuanzia karne ya 20 serikali zimejiingiza katika kampeni za kuwataka raia wadhibiti kizazi.

Neno kudhibiti uzazi (birth control) ambalo lilibuniwa na Margaret Sanger, mpiganiaji haki za wanawake wa huko Marekani, mwaka 1913 - 1915 lina maana ya njia za kuzuia mimba kwa kumtumia mwanamume au mwanamke, na hivi sasa zinajumuisha njia zote za kuzuia kizazi, ikiwa ni pamoja na kutoa mimba (abortion) au kuviza kizazi (sterilization). Hata hivyo jina la kampeni hii limekuwa likibadilika badilika. Katika miaka ya 1930 jina lilikuwa mpango wa familia (family planning) na katika miaka ya 1940 jina likawa mpango wa uzazi (planned parenthood). Baadaye yakazuka majina mengine mengi kama vile kuzuia mimba (contraceptive), uzazi wa hiari (voluntary parenthood), kupunguza familia (family limitation), vita dhidi ya mimba (anti conception) na kadhalika.

Kampeni hizo zilipokuja Afrika Mashariki zilipewa majina mbali mbali kama vile uzazi wa majira, mpango wa familia, uzazi na malezi bora, na sasa kampeni hii imepewa jina la Elimu ya ngono (sex education) na Tanzania Elimu ya ngono hufundishwa mashuleni kwa jina la Elimu ya Afya na Uzazi.

Kwa vile tumentaja Margaret Sanger kama mwanzilishi wa harakati za **“birth control”**, ni vyema tumzungumzie kwa ufupi ili tupate kuelewa vyema uzito wa neno alilolizua.

Margret Sanger alizaliwa 1879 na kuolewa na William Sanger akiwa na umri kati ya miaka 20 na 25. Alijenga na kuitekeleza kwa vitendo dhana ya “mtu kuwa huru” kutembea na mwanamume yeyote anayemtaka. Alizikuza tamaa zake juu ya ngono na hivyo akawa kahaba mkubwa wa zama zake japo alikuwa kaolewa.

Yaonesha kuwa bwana William, kinyume na tabia ya mkewe, alikuwa ni mtu na heshima zake. Katika hatma ya mambo hakuwa na la kufanya ila kumwacha Margaret. Kwani kila alipojaribu kumsema juu ya uzinifu wake, Margret alimshauri mumewe naye azini.

Ndoa yake ya pili iliangukia kwa mume ambaye naye aliikubali dhana angamizi ya mtu kufanya zinaa apendavyo hata akiwa ndani ya ndoa. Na bwana huyu ndiye aliyezipa nguvu harakati za Margret za kampeni za kudhibiti uzazi.



Kiu ya Margret isiyokatika, na ulafi uliopindukia wa ngono, ulimfanya azini na wanaume wanne tofauti wakati yupo katika fungate ya ndoa yake ya pili. Huyu ndiye mwanzilishi wa sera ya kudhibiti uzazi:

Kwa mujibu wa Encyclopedia Britannica (1985) mojawapo ya sababu zilizopelekea kuenea kwa kampeni hii ni manufaa ya faida ya kibiashara iliyotokana na kuuza madawa au vifaa vya kuzuia mimba.

Makampuni yanayotengeneza madawa hayo yalijikuta yanaingiza mamilioni ya dola. Hivyo, yakazidi kuitangaza biashara yao. Katika kuzivutia nchi changa, madawa hayo yamekuwa yakitolewa bure. Lakini sasa, baada ya kunogewa na sera hii, inabidi wasake madawa ya kuzuia mimba na magonjwa ya zinaa kwa bei mbaya.

## **Kustawi kwa Kampeni ya Kudhibiti Uzazi**

Miongoni mwa sababu zilizosaidia kustawi kwa kampeni hii ni matokeo ya mapinduzi ya viwanda (Industrial revolution) ya huko Ulaya.

**Kwanza** viwanda vilihitaji wafanyakazi kwa maelfu ambao japo walifanyishwa kazi sana, sehemu kubwa ilikwenda kwa wenye viwanda, hivyo wafanyakazi hawakuweza kuzikimu familia zao. Bidhaa za viwandani pia zikabadili mahitaji ya watu. Vitu ambavyo hapo awali havikuwepo sasa vikawa ni mahitaji ya lazima.

**Pili**, kwa kuwa pato la mfanyakazi halikumwezesha kuihudumia familia yake, mke na watoto walilazimika pia kufanya kazi viwandani ili kupata riziki zao. Matokeo ya utaratibu huu ni kuwa familia ziliparaganyika na yale malezi muhimu ambayo mtoto aliyapata kwa wazazi wake sasa yakakosekana. Kwa kuwa mke asingeweza kuishi bila kuajiriwa kiwandani na asingeweza kumudu zile kazi ngumu za kiwandani akiwa mjamzito au akiwa na mtoto mchanga, kuzaa kukaanza kuwa nuksi kubwa. Kwani kipindi chote ambacho mwanamke alishindwa kufanya kazi kwa sababu ya udhaifu wa afya hakulipwa kitu. Ndio maana kampeni hii ya kudhibiti uzazi ilianzishwa na kupiganiwa sana na wanawake. Kujiepusha na kuzaa kukaonekana kuwa ni ukombozi wa aina yake.

**Tatu**, mapinduzi hayo yaliambatana na utamaduni wake. Utamaduni ambao ulihimiza sana maendeleo na ustawi wa mtu binafsi. Ustawi kwa maana yakuwa na vitu vingi vya anasa na fahari. Matokeo yake yakawa watu walijiepusha sana na kila kitu ambacho walidhani kingeliweza kwa namna fulani kuathiri ustawi wao wa binafsi. Moyo wa ukarimu na kuhurumiana ukafa. Ikafikia hadi mtu akawaona wazazi wake kuwa ni mzigo mkubwa kuishi nao watampunguzia anasa zake. Kwa hoja hiyo kuzaa watoto kukawa balaa kubwa. Na aliyezaa akaishia mtoto mmoja au wawili.

**Nne**, kuparaganyika kwa familia kukapelekea kuondoka kwa uadilifu. Na hivyo uadilifu wa ndoa ukaonekana ni hekaya za watu wa kale. Badala yake falsafa za uhuru wa mtu binafsi zikapata nguvu. Kwa mujibu wa falsafa hiyo mtu anao uhuru wa kufanya analotaka na kazi ya serikali ni kuusimamia na kuudumisha uhuru huo. Hivyo kwa upande wa mahusiano ya ndoa falsafa hiyo iliona kuwa hilo ni suala la watu binafsi wanahiari ya kufanya lolote wapendalo. Na kampeni zote za kudhibiti uzazi katu hazijishughulishi kabisa na suala zima la uadilifu katika ndoa.

Bali hujishughulisha tu na kuwasaidia watu wasipate mimba. Na kama tutakavyoona baadaye hii ni dosari mojawapo kubwa ya kampeni hii.

## Hoja za Kudhibiti Uzazi Hivi Leo

Tumekwishaona kihistoria mambo yaliyopelekea kuibuka kwa kampeni hii. Lakini hoja kubwa inayofanya kampeni hii iendeshwe kote duniani hivi leo ni ya uwiano kati ya idadi ya watu na maendeleo ya kiuchumi. Na ni kwa sababu hiyo ndiyo maana serikali nyingi hivi sasa zimeamua kuipigia zumari kampeni hii. Hoja yenyewe siyo ngumu kuelewa: Watu kuongezeka kwa kasi zaidi kuliko ongezeko la pato la nchi kiuchumi. Matokeo yake ni kuwa taifa litashindwa kutoa huduma kuinua hali za wananchi. Hoja hii ni dhaifu sana. Lakini kabla hatujaonesha udhaifu wake tungependa kwanza kuelezea kwa ufasaha zaidi. Na tutanukuu hoja zilizotolewa na mtetezi mashuhuri sana wa udhibiti wa uzazi (birth control) Bwana Leonard Barnes.

Bwana Barnes katika kitabu chake (African Renaissance – sura ya 7) anatoa hoja ya kwanza kuwa nchi nyingi za Afrika ikiwemo Tanzania zina kundi kubwa la watu ambao hawana Elimu wala mafundisho yoyote.

Kundi ambalo halina manufaa yoyote kiuzalishaji mali na kwa hakika ni mzigo kwa taifa. Anasema kundi hili la watu kwa hakika halipaswi kuwepo. Kwa kufuata msingi wa aliyefika mwanzo, ahudumiwe kwanza, watu hawa wana haki ya kuitaka jamii iwape kipaumbele kabla ya kuwafikiria wale ambao hawajazaliwa.

Hoja ya pili ni kuwa kilicho muhimu kwa taifa, kama ilivyo katika kiwanda, siyo uwingi bali ubora wa watu. Kwa sababu hiyo ndiyo maana viwanda siku zote huweka ukomo katika idadi ya wafanyakazi wake kulingana na mahitaji ya kudumisha ufanisi wa kazi. Kama ambavyo hayo ni muhimu katika mpango wa kiwanda kimoja kimoja hayo ni muhimu pia kwa taifa kwa ujumla.

Katika kuisisitiza hoja hii Bwana Barnes anasema kama ambavyo serikali zote zimeweka idara za uhamiaji ili kudhibiti idadi ya wageni wanaoingia nchini, serikali za Kiafrika zimekawia mno kuzindukana kuwa ipo haja pia ya kudhibiti wageni wanaoingia nchini kwa njia ya kuzaana.

Anasema: *“Iwepo sheria ya uhamiaji wa mimba za binadamu”*. Leonard Barnes anaendelea kwa kusema:

Katika bara la Afrika mmomonyoko wa udongo unaosababishwa na mbinu duni za ukulima unaoana na mmomonyoko wa watu unaosabaishwa na mbinu duni za kuzaana. Ongezeko la watoto ni kubwa mno kiasi ambacho makazi, afya, shule na ajira haviwezi kudhibiti mtiririko wake, watu hao wanahitaji kuhifadhiwa kwa kuchukua hatua kama zile zinazochukuliwa katika kuhifadhi ardhi.

Akitoa mfano wa nchi ya Tanzania, bwana Barnes anasema baada ya kila miezi 18 idadi ya watoto wanaozaliwa huwa sawa na idadi ya watu wanaofanya kazi za ajira. Na kama uwiano uliopo sasa kati ya wafanyakazi na wakulima hautabadilika, basi watoto wapatao 10,000 kwa mwaka watazaliwa katika nyumba za watu wa mijini na watoto 190,000 watazaliwa vijijini.

Kwa kutumia takwimu zilizotolewa katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano, Bwana Barnes anasema, “watoto 66,000 (karibu theluthi moja ya watoto wote waliozaliwa) watakufa kabla yakufikia umri wa kuweza kulipa gharama ya malezi yao. Na wale wanaonusurika huishi katika tishio la maradhi na utapia mlo”.

Hoja ya tatu ya Bwana Barnes imejengwa juu ya hali hiyo duni inayowakabili watoto wa Kitanzania na wengine Afrika. Anasema nchi za Kiafrika zilipopigania uhuru zilifanya hivyo ili kujenga utu wa kurejesha heshima yao na kujiletea maendeleo ya baadaye. Kizazi hicho kitajihisi vipi juu ya utu na heshima yao kitakapogundua kuwa theluthi moja miongoni mwao wanatakiwa wafe kabla ya kufikia baleghe? Watahisi vipi juu ya uhuru wa kujiletea maendeleo yao ya baadaye iwapo nusu yao hawawezi hata kupata Elimu ya msingi katika shule duni? (Ikumbukwe kuwa, Bwana Barnes aliandika kitabu chake 1969). Kutokana na hayo Bwana Barnes anauliza:

Je, hatutakuwa tunawahurumia na kuwafanyia hisani ya kweli watoto hao iwapo tutawaomba waakhirishe kuja kwao duniani kwa muda, wakati kizazi cha sasa kikijitahidi kuondosha umasikini, maradhi na kujenga mfumo wa Elimu ambao angalau ni wa afadhali?

Kwa muhtasari hoja ya tatu ya Barnes ni kuwa ni kitendo cha ukatili kuwaleta watoto duniani halafu kuwatesa kwa njaa na maradhi. Si bora kuwazuia wasije? Bwana Barnes anasema kikwazo kikubwa kabisa cha maendeleo ya Afrika ni uongezekaji kiholela wa idadi ya watu. Hata kama matatizo yote mengine yatatatuliwa, lakini maadamu tatizo la uongezekaji wa watu halijapatiwa ufumbuzi, basi hakutakuwa na maendeleo Afrika.

Bwana Barnes anawalaumu sana wale wataalamu wa uchumi wanaosema kuwa ongezeko la watu katika Afrika kwa asilimia 3 kwa mwaka si tatizo maadamu ongezeko la uchumi litakuwa asilimia 5 kwa mwaka. Watu kama hao anasema wanapotosha hakika ya mambo yalivyo. Watu watakaoisaidia sana Afrika ni wale ambao watatambua umuhimu wa suala la idadi ya watu katika masuala yote ya maendeleo ya jamii na hasa kasi na namna ambayo kizazi kimoja huchukua nafasi ya kizazi kingine. Watu wanaojua umuhimu wa ubora na sio uwingi wa watu.

Sera kama hiyo Bwana Barnes anasema itawawezesha wapangaji wa mipango 'kuanza kwa kujiuliza kazi zipi ambazo jamii inataka zifanyike, na halafu izalishe na kuwafundisha watu wa kufanya kazi hizo. Bwana Barnes anamalizia kwa kusema kuwa ukatili wanaofanyiwa watoto wachanga ni matokeo ya huruma. Ni matokeo ya maendeleo ya sayansi ya tiba. Sayansi ya tiba (medical science) kwa kung'ang'ania kuokoa maisha ya watu bila kujali ubora wa maisha wanayoishi ndio imeleta matunda haya machungu. Na kwa hiyo sayansi ya tiba ifikiwiwe kuleta ufumbuzi wa ongezeko la watu.

Maandishi haya ya Bwana Leonard Barnes yanawakilisha hoja za wale wanaoiunga mkono kampeni hii ya kudhibiti ongezeko la watu. Sasa hebu tuangalie udhaifu wa hoja hizi.

## **Udhaifu wa Hoja za Kudhibiti Uzazi:**

Hoja nyingi zinazotolewa kuunga mkono udhibiti wa uzazi zimejengwa juu ya hali na mazingira ya maisha yaliyoletwa na utamaduni na maendeleo ya nchi za Ulaya na Marekani. Wale wanaoiunga mkono kampeni hii wanaamini kuwa, mila na mwenendo wa jamii za Ulaya ndio kiigizo cha watu wengine wote duniani. Historia ya maendeleo ya binadamu inatazamwa kana kwamba inafuata mstari ulionyooka. Watu wanatoka katika hali duni na kuelekea katika hali ya maendeleo. Na wanaoongoza maendeleo hayo ni watu wa Ulaya na Marekani. Kutokana na mwelekeo huo mtindo wa maisha wa huko Ulaya, mila za huko na taratibu za kiuchumi za huko zinaonekana kuwa hazitakiwi kubadilika. Kinachotakiwa kubadilika ni mila na desturi zilizo kinyume na zile za Ulaya. Matokeo ya mwelekeo huu ni kuwa watu hutafuta ufumbuzi wa matatizo yao kwa kutazama Ulaya hata kama mila za Ulaya ndizo zilizo yaleta matatizo hayo. Kama nchi za Afrika hazitaamua kuchukua mwelekeo tofauti kabisa katika kukabiliana na matatizo, zitaendelea kuwa wafungwa wa Ulaya kila uchao. Hilo linalodhaniwa kuwa ni tatizo la ongezeko la watu ni zao la mfumo wa kiuchumi na kijamii wa nchi za Ulaya. Ufumbuzi hauwezi kupatikana kwa kampeni za kudhibiti uzazi wakati uchumi wa nchi hizo unadhhibitiwa na watu wengine.

Watetezi wa kudhibiti uzazi (birth control) na kampeni za nyota ya kijani, hawataweza kuyaona makosa ya mwelekeo wao hadi watakapokuwa tayari

kuitazama upya misingi ya uhibitwa wa uzazi. Kinachohitajika siyo kukata matawi bali kung'oa mti mzima unaozalisha matunda haya machungu.

## **Hoja ya Uhaba wa Rasilimali za Kiuchumi**

Hoja yao maarufu kuliko zote kama tulivyoona ni juu ya uchumi. Hudaiwa kuwa sehemu ya kuishi katika ardhi ina ukomo na kwamba rasilimali za kiuchumi pia zina ukomo. Lakini hudaiwa kwamba uwezo wa mwanadamu wa kuzaliana ni mkubwa ambapo ardhi itajaa na chakula kitakosekana cha kuwatosheleza watu wote. Katika Encyclopaedia Britanica (1985) kwa mfano, inakadiriwa kuwa hadi mwisho wa karne hii ya ishirini idadi ya watu imekuwa ni zaidi ya bilioni sita (6,000,000,000). Hivyo, basi ili kujikinga na baa hilo watu hawana budi kudhibiti kizazi. Kwa mujibu wa Bwana Malthus na mwenzake Francis Place iwapo juhudi za kudhibiti uzazi (birth control) hazitatiliwa mkazo basi uwiano kati ya watu na mahitaji muhimu kama chakula utakuwa ni 4096:13 katika karne tatu na baada ya karne 20 uhusiano huo hautakuwapo kabisa. Yaani hakutakuwepo na uhai kabisa.

Hoja hii ya kwamba binadamu wanaongezeka sana, mara mbili kila baada ya robo karne, haina msingi kwa sababu si ya kweli. Lau madai hayo yangekuwa ya kweli basi leo kusingekuwa na binadamu ardhini. Kwa mujibu wa utafiti wa hivi karibuni uliochapishwa katika jarida liitwalo "National geographic" (Vol. 154 No.6) la huko Marekani, yamepatikana maandishi huko Syria yanayothibitisha kuwa miaka 3,000 kabla ya kuzaliwa kwa Nabii Issa (a.s) kulikuwa na dola nyingi sana zilizofikia kiwango kikubwa sana cha maendeleo. Dola hizo pia zilikuwa na watu wengi sana. Dola ya Ebla imetaja miji 5,000 waliyokuwa wakifanya nayo biashara. Mmoja kati ya miji hiyo ni Iram uliotajwa katika Qur-an 89:7. Na maandishi hayo yalikuwa katika makao ya Ikulu ya dola ya Ebla. Kama madai ya akina Malthus yangekuwa kweli basi hata Yesu asingezaliwa kwani zilikuwa zimekwishapita karne zaidi ya 30!

Wazo kwamba mahitaji muhimu hayatatosha ni dhaifu kwa sababu rasilimali zote ambazo mwanadamu anazihitaji zilikuwepo tokea dunia ilipoumbwa kwa ajili ya matumizi ya binadamu wa zama zote. Rasilimali hizi zinafahamika kwa binadamu kutokana na maendeleo ya kisayansi na teknolojia. Mfano watu wa zama za kale hawakuwa na habari kuhusu mafuta ya petroli yanavyoweza kuwa muhimu katika maendeleo ya binadamu japo yalikuwepo na japo Wasumeria walifahamu juu ya kuwepo kwa mafuta hayo. Mifano ya aina hii ni mingi sana. Hii ina maana kuwa kutokana na upeo wa sasa wa Elimu watu wanaweza kudhani kuwa vizazi vijavyo havitaweza kuishi kwa sababu ya uhaba wa mahitaji muhimu. Ni muhimu kutambua kuwa watu wakiongezeka upeo wa binadamu wa kuzalisha mali, vyakula n.k., nao pia huongezeka. Historia ya hivi karibuni imeonesha kuwa kuongezeka kwa binadamu hokusababishi uhaba wa mahitaji muhimu. Mwaka 1880 idadi ya Wajerumani ilikuwa milioni 45 hivi. Wakati huo

kulikuwa na uhaba wa chakula ukilinganisha na hivi sasa ambapo idadi yao ni zaidi ya milioni 68, na wanakula na kusaza. Uholanzi na Uingereza pia ni mifano mizuri katika kuelezea ukweli huu. Isitoshe zaidi ya binadamu kuna viumbe wengi sana juu ya ardhi hii yenye nafasi yenye ukomo. Na kila kiumbe kinao uwezo mkubwa sana wa kuzaliana kiasi ambacho kama pasingekuwepo na kanuni za kimaumbile (natural laws) za kudhibiti uwezo huo, basi aina moja tu ya viumbe ingeweza kuijaza ardhi yote katika kipindi kifupi mno. Kwa mfano, jamii ya aina fulani ya mti ijulikanayo kama *Symbrium Sophia*, ina uwezo wa kutoa mbegu kiasi cha robo tatu milioni. Inakadiriwa kuwa kama mbegu zote za mti mmoja tu zitaota, katika kipindi cha miaka mitatu tu mti huo utaijaza ardhi yote na pasiwe na nafasi ya kiumbe kingine chochote. Aina ya samaki ajulikanaye kama 'Star' fish hutaga mayai mia mbili milioni kwa mara moja. Kama yote yataaanguliwa basi baada ya vizazi vichache tu samaki huyo mmoja atazijaza bahari za dunia nzima na isiwepo hata nafasi ya tone moja la maji. Hali kadhalika ukimwangukia binadamu, manii anayotoa mara moja yanatosha kuwapa mimba wanawake milioni mia tatu hadi mia nne.

Hivyo kama uwezo wa mwanamume mmoja ungeruhusiwa kufanyakazi yake basi ingehitajia miaka michache tu kwa mwan aume huyo kuijaza dunia yote kwa watoto wake tu na kusiwe na nafasi ya watu wengine achilia mbali viumbe wengine. Ni nani anayedhibiti na kuweka uwiano kwa viumbe wote hawa?

Tatizo halijawahi kuwa uhaba wa rasilimali za kuwakimu watu, bali kasoro za kibiashara, ugawaji na usambazaji wa rasilimali hizo. Kwa mfano inafahamika kuwa asilimia 10 tu ya rasilimali zinazotumiwa kutengeneza silaha ulimwenguni zinatoshwa kufutilia mbali njaa na maradhi dunia nzima. Tukizingatia uwiano kati ya idadi ya watu na chakula duniani, tutaona wazi kuwa tatizo siyo uwingi wa watu. Mfano kwa upande mmoja mwaka 1982 Uingereza ilikuwa na watu 583 kwa kila maili mraba lakini ilikuwa haina tishio la njaa. Kadhalika Uholanzi ilikuwa na watu 1,117 katika maili mraba, lakini vile vile haikuwa na tishio la njaa.

Ambapo Brazil iliyokuwa na watu 38 na Bolivia watu 12 kwa kila maili mraba, zote zilikuwa na tishio la njaa. Tatizo hapa ni suala zima la uzalishaji mali na sio idadi ya watu katika mji. Ni mara ngapi tumeshuhudia mamilioni ya tani za vyakula yakiunguzwa moto au kumwagwa baharini katika nchi tajiri kama vile Marekani na hapo hapo mamilioni ya watu wanakufa njaa katika nchi masikini?

## **Tatizo la Vifo na Maradhi**

Watetezi wa kampeni ya kudhibiti uzazi (birth control) wanakiri kuwa maumbile (nature) hudhibiti kukua kwa idadi ya viumbe. Lakini wanasema maumbile hufanya kazi hii kwa njia ya vifo na maangamizi na hivyo kusababisha machungu na mateso ya kimwili na kisaikolojia. Kwa nini binadamu wasitafute njia nzuri zaidi ya kujipunguza wenyewe?

Yaani wajipunguze kwa njia ya kudhibiti uzazi (birth control) badala ya kungojea majanga kama njaa au mafuriko yaje kupunguza idadi ya watu.

Hoja hii pia inao udhaifu mkubwa. Ukweli ni kuwa uhai na kifo havipo katika milki ya binadamu. Hadhari yoyote utakayoichukua, kifo kinabakia kuwa ni tatizo lisilo na ufumbuzi. Swali ni je, ni hadhari gani ambayo binadamu anaweza kuichukua dhidi ya tetemeko la ardhi, kimbunga (au tufani), mafuriko, maradhi mabaya n.k.? Je, binadamu amefikia muafaka na Mwenyezi Mungu (au maumbile kama wanavyodai) kuwa njia nyingine zote za kuwafisha watu zitasimamishwa endapo taifa litazindua mpango wa kupunguza watu kwa njia ya kudhibiti uzazi? Je wametafakari juu ya msiba unaowasubiri endapo watasimamisha kuzaliana na wakati huo huo kifo kikaendelea kuchukua ushuru mkubwa wa roho za watu kwa kupitia mabalaa, kama mvua za elnino na mafuriko, tufani, matetemeko ya ardhi na volkeno, maradhi, vita, kuzama kwa meli, kupinduka kwa magari, treni, kuanguka kwa ndege n.k.? Na hii ni mbali na mwenendo wa kawaida wa kifo ambao hapana njia ya kuukwepa. Ni jambo la kushangaza kuwa wataalamu hao wanashindwa kufanya mahesabu rahisi kama haya! Kama kuna kupungua kwa watu daima pasipokuwa na njia mahsusi za kuleta ongezeko, ni athari gani zitafuata? Katika nchi zilizoendelea vifo vinavyosababishwa na maradhi ya zinaa ni vingi kuliko vifo vinavyosababishwa na vita. Usisahau vimbunga vya AIDS, Ebola, TB, Tauni n.k. Je, huku ndiko kushinda au kuepuka kifo? Kama sivyo, je watu hawatakuwa wanaunguza mshumaa kutoka pande mbili - kwa upande mmoja idadi ya watu itapungua kutokana na sababu tusizoweza kuzizuia (natural causes) na kwa upande mwingine kupunguza watu kwa kudhibiti uzazi? Ili mtu awe katika nafasi nzuri ya kudai udhibiti wa uzazi (birthcontrol) lazima awe na Elimu juu ya mambo kadhaa:

- Ajue idadi ya viumbe wote duniani waliotakiwa kuishi hapa duniani na kati ya hao ni wangapi wamekwishaishi na wangapi bado.
- Ajue idadi hasa ya chakula kiasi gani na chakula hicho huongezeka au hupungua vipi?
- Ajue pia ni kiasi gani cha viumbe watakaokufa kwa njaa, mafuriko, maradhi, vita na kadhalika na watakufa lini ili aweze kulinganisha na kiasi cha chakula kitakachokuwepo na mahitaji mengine.
- Ajue pia namna ambavyo sera yake ya kudhibiti uzazi itakavyohakikisha kuwa kila siku idadi ya watu wanaokufa na kuzaliwa haizidi wala kupungua kulinganisha na rasilimali zilizopo.

Kujiingiza katika kampeni za kudhibiti kizazi (birthcontrol) na nyota ya kijani bila ya kuwa na takwimu sahihi juu ya mambo yote hayo ni kujiingiza katika mchezo wa pata-potea.

## Hoja ya Ugumu wa Malezi

Hoja hutolewa kuwa wazazi walio na kipato kidogo watashindwa kulea watoto wengi. Watashindwa kuwapa Elimu nzuri, kuwalea katika hali nzuri ya kimaisha na kuwapa msingi wa kutosha wa kuanzia maisha. Isitoshe wanaweza kupata utapiamlo (malnutrition) na hata kufa wakati wa utoto wao.

Hoja hii yaweza kuwavutia watu wengi lakini nayo pia ni dhaifu. Kwanza, “Elimu bora”, “hali ya maisha” n.k. ni misemo tata (vague) isiyokuwa na tafsiri moja maalum. Kila mtu anayo namna yake ya kuyaangalia mambo. Lipo kosa linalofanyika la mtu kuacha kutazama hali yake na mazingira yake na kuangalia hali ya maisha ya mahali pengine na hivyo kuanza jitihada za kujaribu kuwakuta waliotangulia. Raia wa nchi za Kiafrika kwa mfano, wanahimizwa wakimbie kwa dhana kuwa wale waliombele wanatembea. Kinachosahauliwa ni kwamba utaratibu mbaya wa uchumi na biashara uliopo leo duniani ndio unaodumisha utajiri wakupindukia wa nchi zilizoendelea na ufakiri wa kupindukia kwa nchi masikini. Hivyo chini ya utaratibu huu jitihada za kuiga ‘maisha mazuri’ kwa kiigizo cha Ulaya na Marekani ni ndoto. Na watu wenye fikra hizo huepa kulea japo mtoto mmoja kwa kuhofia kuwa atakosa kupata maisha bora. Msimamo huu huwafanya watu wawanie kupata starehe za hali ya juu. Huishia kuleta ufisadi katika ardhi au kujinyonga wakishindwa kufikia lengo hilo.

Fikra kuwa watu wasizae watoto hadi wahakikishe kuwa watoto hao hawatapata matatizo yoyote kwakuwa kila kitu kitakuwa kimeandaliwa pia ni mwelekeo potofu. Ni hatari kwa ustawi wa taifa ikiwa kizazi chao kitalelewa katika starehe na anasa ya mali wasioichuma na iwapo hawatakabiliwa na matatizo na misukosuko ya maisha. Hali hiyo itawafanya wasione haja ya kujitahidi na kupambana na matatizo.

Matatizo ni tanuri linalomfunza na kumpevua mtu ajue namna ya kukabiliana na hali mbali mbali za maisha. Hivyo uvumilivu, subira, ukakamavu, na ujasiri ni mambo yatakayojenga tabia yake na kumfanya awe mtu mwenye manufaa katika jamii. Hakuna shule au chuo kinachoweza kutoa mafunzo haya, wala mtoto hawezi kupata mafunzo hayo kwa kuishi katika fahari na anasa tu. Misukosuko ni kiwanda kinachotenganisha nafaka na makapi. Mtu anakutana na misiba ili akabiliane nayo kiume, matatizo huja ili yamchochee kufanya jitihada zaidi ili ayatatue. Mambo magumu husafisha udhaifu wa binadamu na kuamsha vipawa vyake na kuvistawisha na hivyo kuleta maendeleo.

Wale wanaoweza kupita katika tanuri hilo kwa ujasiri ndio wanaoweza kutegemewa katika jamii. Katika historia ya binaadamu karibu asilimia 90 ya watu mashahuri waliozisaidia jamii zao walizaliwa katika familia masikini na mazingira magumu.



Hivyo fikra ya kutaka watoto wazaliwe chambilecho Waingereza wamesema na “vijiko vya fedha midomoni mwao”; wasome shule bora kabisa, walale katika majumba ya fahari wakati wanasoma na wanapoanza maisha wawe wameandaliwa kila kitu ni ya hatari. Itatuletea kizazi cha watu wapendao anasa na ambao wataona taabu kujitoa muhanga kwa lolote, na wataepuka kubeba dhamana nzito. Moto utakuwa umezaa jivu.

## Hoja ya Ubora na Siyo Uwingi wa Watu

Yasemekana kilicho muhimu siyo uwingi bali ubora wa watu. Hali hii imesimama juu ya dhana kuwa kama watazaliwa watoto wawili au mmoja basi watakuwa na akili nzuri, afya na uwezomkubwa wa kuzalisha. Lakini kama watazaliwa watoto wengi watakuwa dhaifu, wagonjwa, wajinga na wasiofaa kwa lolote. Hoja hii haina msingi wowote na haiwezi kuthibitishwa kwa uzoefu wala majaribio. Mtu aweza kuzaa mtoto mmoja tu na akawa juha au mwenye afya dhaifu sana. Tuchukuwe mfano wa mabwana wawili.

Mmoja amejaaliwa kuzaa watoto wawili tu, alijitahidi kuwalea watoto hawa kama yai. Aliwahangaikia kwa kila kitu mpaka wakawa watu Wazima. Matarajio ya bwana huyu kwa vijana wake ni kwamba kutokana na malezi ya starehe aliyowapa, watakapokuwa watu Wazima watatoa mchango wao kuwasaidia wazazi wao, familia zao na jamii kwa ujumla.

Kinyume na matarajio haya vijana hawa waliishi kwenye ulevi, ukahaba, na kila aina ya anasa yenye kumwangamiza mwanadamu! Bwana huyu akabakia katika hali ya ukiwa na kukata tamaa huku uzee unamuandama. Bwana wa pili amejaaliwa kuzaa watoto kumi. Hakuwa na kipato kikubwa kiuchumi hivyo alihangaika sana katika kuwalea watoto wake. Alimfanya kila mtoto atoe mchango wake kwa kadri ya umri wake kuongeza kipato cha familia yao. Vijana wawili kati ya vijana wake waliangukia kutokuwa na manufaa yoyote kwa wao wenyewe na kwa jamii kwa ujumla kama wale wa bwana wa mwanzo.

Vijana wake wanane waliobakia, walibakia kuwa watu wa maana kama walivyolelewa, wakawa ni wenye manufaa kwa wazazi wao na familia zao na wakawa ni wenye kutoa mchango mkubwa katika kuiendeleza jamii.

Kutokana na mfano huu, huoni hatari ya kudhibiti uzazi? Utahakikishaje kuwa hao wachache watakaozaliwa kuwa ndio watakaokuwa bora? Tusiufikirie ubora wa mwanadamu kama ule wa ng'ombe anayenenepeshwa kwa ajili ya nyama, au kutoa maziwa mengi!

Ubora wa binadamu uko katika utu wake. Kumlea mtoto katika starehe, hakuna uthibitisho wowote wa kuukuza utu wake, bali kuna uwezekano mkubwa wa kuudunisha. Hatuna budi kukumbuka kuwa msingi wa maendeleo ya jamii sio vitu bali ni utu.

## Hoja ya Nyongeza

Kama hoja ya nyongeza watetezi wa udhibiti wa uzazi wanasema kulea watoto wasiohitajika duniani na ambao hali zao za maisha zitakuwa duni na watakufa kabla ya kufikia ujana. Hoja hii ingekuwa na uzito kama binadamu angekuwa na njia za kujua kwa uhakika kabla mtoto hajazaliwa juu ya kuhitajika na manufaa ya mtoto huyo. Yaani, ajue tabia yake itakuwaje, ubora wa akili zake, vipawa vyake vingine, na kufaa au kutofaa kwake katika jamii. Maadamu ujuzi wa yote hayo upo nje ya uwezo wa binadamu hoja hii haina msingi wowote madhubuti.

Hoja nyingine ni kuwa kuzaa watoto wengi kunaharibu afya ya mama. Umbo na uzuri wake huathiriwa. Udhaifu wa hoja hii ni kuwa njia zinazotumiwa kuzuia mimba pia zina madhara kwa afya ya mama.

Wanawake wengi wameathiriwa na maradhi mbali mbali na hata kupoteza maisha yao kutokana na athari za madawa hayo. Kwa hoja za afya (medical reasons) mtu hawezi kuweka sheria mwanamke azae watoto wangapi. Jambo hili linategemea tofauti iliyopo kati ya mwanamke mmoja na mwingine. Ikiwa kutokana na afya ya mwanamke Fulani daktari anaona kuwa ni hatari kwake kuzaa basi hapo yafaa aruhusiwe kuzuia mimba au hata kuitoa iwapo imeshaingia. Lakini matatizo ya mwanamke mmoja hayawezi kuwa msingi wa kupitisha sera ya kuwazuia wanawake wengine kuendelea kuzaa.

## Matokeo ya Kufuata Sera ya Kudhibiti Uzazi

Tumekwishaona udhaifu wa hoja zinazotolewa kuunga mkono sera za kudhibiti uzazi (birth control). Sasa tuangalie matokeo ya kung'ang'ania sera hizo:

### *(i)Uhaba wa Wafanyakazi*

Serikali ikishajiingiza katika kampeni za kuwataka watu wadhhibiti uzazi basi mara nyingi matokeo yake huwa kinyume na makusudio ya sera. Lengo la awali huwa kuoanisha uwiano kati ya idadi ya watu na rasilimali za nchi. Kwa kuwa tatizo la sasa linadhaniwa ni kuwepo kwa watu wengi mno, kampeni za serikali zitaelekezwa katika kuwataka watu wasizae watoto wengi. Na njia pekee ya kuwafanya wakubaliane na sera hiyo ni kuendesha propaganda za kuwaonya kuwa wasipozaa watoto wengi hali zao zitakuwa nzuri. Raia wakishaitikia wito huo basi maslahi ya taifa huenda yasijaliwe tena. Kila mtu atataka kuishi maisha mazuri kwa kuepuka mzigo wa kuzaa na kulea watoto. Tatizo litakalotokea ni kwamba hata kama baadaye taifa lithitaji watu zaidi itakuwa vigumu sana kwa raia ambao wameshafundishwa kutukuza maslahi yao binafsi kuitikia wito wa kuzaa watoto wengi, kwa sababu watawapunguzia anasa zao.

Tatizo hili si la kubuni tu bali limekwishatokea na bado linazitatiza nchi zilizotutangulia katika kampeni hii. Kwa mujibu wa gazeti la Newsweek la Desemba 15, 1986 uk. 18-23, kuna upungufu mkubwa wa watoto huko Ulaya hivi sasa ambao haujawahi kutokea katika historia ya Ulaya. Vijana wengi wa kizungu wanakataa kuoana. Na wale wanaoana, huchelewa sana kuoana na kuzaa watoto wachache sana, na idadi kubwa ya watu ambao hufanya kazi za kuajiriwa huamua wasizae kabisa. Kutokana na hali hiyo idadi ya watu itadidimia zaidi Ulaya katika karne ijayo. Hali hiyo ilimpelekea Waziri Mkuu wa Ufaransa wa wakati huo Bwana Jacques Chirac kusema: “Kwa upunguzaji huu wa watu, Ulaya inatoweka”, na gazeti hilo lilimnukuu Bwana Gaston Thorm Waziri Mkuu wa zamani wa Luxembourg akisema: “Ulaya inajinyonga yenyewe” Serikali za Ulaya hivi sasa zinatahayari kuwataka raia zao wakubali tena jukumu la kuzaa na kulea watoto lakini wapi. Mafundisho yale ya mwanzo ya kuepa majukumu yamekwisha wakolea. Ufaransa inatoa zawadi kwa familia zitakazokubali kuzaa lakini kwa kuwa zawadi na heshima watakapopata hazilingani na dhamana ya kulea watoto bado watu wengi hawako tayari kuzaa watoto. Si hivyo tu lakini idadi ya wazee wa miaka 68-71 ndiyo inayoongezeka. Huko Ubelgiji serikali ililazimika kuwaachisha kazi Waalimu wa sekondari kwa sababu ya ukosefu wa wanafunzi. Huko Ufaransa serikali imekuwa ikichapisha mabango yenye picha ya mtoto mchanga halafu chini kuna maneno yasemayo: “Tafadhali zaa mtoto, tafadhali. Kuishi pamoja kwa ajili ya starehe ya ngono tu ni uchoyo na ubinafsi mbaya kabisa”. Lakini wapi, maji yamekwisha mwangika. Wakati wenzetu Ulaya wanawashawishi raia zao kwa mapesa wapate kuzaana Afrika ndio kwanza inaendesha kampeni za “nyota ya kijani” za kuwakataza raia kuzaana. Ilani ikiambazani. Afrika ina khiari ya kujinusurisha au kukimbilia kuingia katika jahazi linalozama.

### ***(ii) Tishio la kuanguka kwa nguvukazi ya Taifa***

Iwapo idadi ya watu katika taifa itaendelea kupungua kutokana na kudhibiti uzazi taifa litakuwa katika tishio la kupoteza nguvukazi yake iwapo litatokea janga lisilotazamiwa kama vita kwa mfano. Bomu lililopigwa huko Hiroshima liliua watu wapatao laki moja. Mauaji ya Rwanda yameteketeza malaki ya Watu. Vita kati ya Iraq na Iran imeteketeza watu milioni moja. Uvamizi wa Marekani na /rafiki zake umesababisha vifo na unaendelea kusababisha vifo vya mamia kwa maelfu ya watu wa Afghanistan Somalia na Iraq.

### ***(iii) Kuharibika kwa Maadili ya jamii***

Sera ya udhibiti wa uzazi huathiri sana mwelekeo wa maadili katika jamii. Kwanza, mwanaume na mwanamke wanakuwa na uhuru wa kufanya jimai na mtu yeyote. Hivyo hisia za uovu wa Zinaa huondoka, hufikia hadi Waziri

Mkuu wa nchi kuwataka wazazi wawagawie watoto wao mipira ya kufanyia zinaa (Kondomu)! Pili watu hupagawa na uzinzi kiasi ambacho kila siku hubuni mbinu mpya za kuchochea na kufanyia zinaa. Na hizi si dhana tu bali ufuska huko Ulaya na Marekani umefikia kilele ambacho hakijawahi kufikiwa katika historia ya binadamu. Kwa mujibu wa gazeti liitwalo, “The Illustrated Weekly of India” huko Sweden watu wamefikia hadi kufanyia zinaa katika jukwaa mbele ya watazamaji. Si yo tu kwamba ufisadi umeshtadi lakini wamefikia hadi wanaogopa kuyakemea maovu katika jamii zao. Magazeti na vyombo vingine vya habari vinaogopa kuwakemea mabaradhuli wanaolawitiana. Elimu ya ngono imezua kitendawili - “kipi kilianza, kuku au yai?”

Tatizo ni hili: Je, Elimu ya ngono kama inavyofundishwa na uzazi wa mpango imechangia katika kushuka kwa afya ya watu kutokana na kuongezeka kwa uasherati, magonjwa ya zinaa na utoaji mimba? Au je, kutolewa kwa Elimu hiyo kunatokana na ongezeko la shughuli za ngono miongoni mwa vijana (na wasichana) kama watetezi wake wanavyodai?

Njia ya hekima kukifumbua kitendawili hiki ni kuangalia kumbukumbu za Elimu ya ngono katika nchi za Sweden na Amerika ambazo zimepiga hatua katika suala hili kama zilivyoandikwa na Keith Bower and John F. Kippley.

### *(a)Sweden*

Elimu ya ngono ilifanywa lazima mwaka 1954 na baada ya muda mfupi tu ilizaa matunda. Kati ya mwaka 1959 na 1964 ugonjwa wa gonorea (gonorrhoea) uliongezeka kwa asilimia 75 na asilimia 52 ya waliokuwa na ugonjwa huo walikuwa vijana. Kati ya mwaka 1963 na 1974, talaka ziliongezeka kutoka 8,496 (1963) hadi 27,208 (1974). Na wakati huo huo idadi ya wanaoana ikipungua kwa asilimia 66 (kutoka watu 7.8 kwa kila watu 1000 hadi kufikia watu 4.8 kwa kila watu 1000). Kufikia mwaka 1976 kulikuwa na mtoto mmoja aliyezaliwa nje ya ndoa kwa kila watoto watatu. Hii ni mbali na ukweli kwamba nusu ya wasichana wanaoshika mimba huzitoa. Kwa kweli kilichovunwa Sweden kutokana na kufundisha Elimu ya ngono ni msukumo unaowalazimisha watoto wa shule wazini wakitaka wasitake.

### *(b)Amerika*

Toka Margaret aanze kueneza falsafa yake juu ya ngono na “birth control” talaka Marekani ziliongezeka kwa asilimia mia tano (500%) kati ya mwaka 1913 na 1977. Kati ya mwaka 1971 na 1978 gharama za kuendesha kampeni za (birth control) ziliongezeka kwa asilimia 198 (kutoka Dola 129 milioni hadi dola 384 milioni) na vijana wanaohudhuria vipindi vya Elimu ya ngono wakaongezeka toka laki 3 (300,000) hadi milioni moja na laki mbili (1,200,000). Nini matokeo yake? Idadi ya vijana wanaotumia madawa ya kuzuia mimba iliongezeka kwa asilimia 62 (62%). Kutoka 1971 hadi 1974 kulikuwa na ongezeko la asilimia

hamsini (50%) la watoto wa umri kati ya miaka 10 hadi 20 (teenagers) wanaozini na ongezeko la asilimia 80 (80%) la Malaya miongoni mwa wasichana (teenage girls). Mimba nje ya ndoa kwa “teenage girls” wote ziliongezeka kwa asilimia 90 (90%) wakati zile za “White teenage girls” peke yao ziliongezeka kwa asilimia 140 (140%).

Kinachoonekana kutokana na kumbukumbu hizi, ni kuwa Sweden na Marekani zimefanya majaribio, ya kutunga sera za taifa juu ya Elimu ya ngono na udhibiti wa uzazi, kwa kutumia vijana wa nchi hizo. Majaribio hayo yamezua ongezeko kubwa la shughuli za ngono, mimba nje ya ndoa, utoaji mimba na watoto wa nje ya ndoa. Mamilioni ya pesa za walipa kodi yamepotezwa, familia zimevunjika na uangalizi wa wazee masikini umeharibiwa.

#### *(iv)Hoja ya Kushindwa Kuitokomeza Zinaa*

Tumeona baadhi tu ya madhara na hasara ambazo huweza kutokea pindi sera ya kudhibiti uzazi (birth control) ikitekelezwa. Watu wengi hata miongoni mwa watetezi wa kampeni hii wanakiri kuwa mpango huu unastawisha ufuska na zinaa. Ndio maana kampeni hizi zilipoanzishwa huko Ulaya zilipingwa sana kwa hoja kuwa zinaangusha maadili ya jamii (na kweli hatimaye zimeangusha).

Hata hivyo hoja inayotolewa na watetezi wa kampeni hizi ni kuwa hata kama uasherati na zinaa zitaongezeka “watu wasishtuke kwa sababu kwa mujibu wa gazeti la serikali “Sunday News” la Novemba 30, 1986, mambo haya yamekuwepo tangu kuanza kwa jamii ya binadamu na hayataondoka hadi mwisho wake licha ya ukweli kwamba mambo hayo ni vienzi vikubwa vya maradhi yanayoua kama “Ukimwi”. Hoja hii si madhubuti kwa sababu katika jamii zote yapo maovu mengi ambayo yamekuwepo tangu zama, kama vile wizi, ujambazi, uuaji, kubaka, n.k.

Tena basi maovu hayo wakati mwingine yamekuwa yakiongezeka. Lakini haijatolewa rai katika magazeti ya kuwataka watu wasishtushwe na majambazi wenye silaha wanaowapora abiria mali zao na hata kuwaua kwa hoja kuwa mauaji yamekuwepo duniani tangu zama na zama.

Ukweli unaojitokeza ni kuwa kutokuwepo kwa kampeni za kukataza zinaa na uasherati siyo kwa sababu ya kushindwa kuyatokomeza maovu hayo bali kwa sababu tangu hapo zinaa haihesabiwi kuwa ni miongoni mwa mambo maovu katika jamii. Na ndio maana japo waendeshaji wa kampeni za udhibiti uzazi (birth control) na ufundishaji wa Elimu ya ngono(sex education) wana jua kuwa hatima ya kampeni hizo ni kushtadi kwa uzinzi, hilo haliwashtui, ni kelele za mlango tu.

Kama tulivyosema hapo awali, huu ni udhaifu mkubwa wa kampeni hii. Mawazo kuwa ikiwa raia wawili wameridhia kustareheshana kwa ngono jamii

haidhuriki kwa lolote ni ya hatari sana. Zinaa ni uhaini kwa jamii na ni mbegu ya maangamizi. Yafuatayo ni baadhi tu ya madhara ya zinaa.

**Kwanza**, mzinzi anajiweka katika hatari kubwa sana ya kuweza kupata na kueneza maradhi ya uasherati. Maradhi hayo yataidhoofisha sana afya yake na ya wengine na hivyo kumpunguzia sana uwezo wake wa uzalishaji mali. Watu wengine katika jamii hiyo watalazimika kuchangia gharama za kumtibu. Hivyo rasilimali za jamii itabidi zitumike kununulia dawa za kaswende, kisonono, badala ya mabasi au vitabu. Na zinaa ikienea idadi ya wenye maradhi hayo pia huongezeka na hali kadhalika mzigo wa gharama. Isitoshe maradhi ya kaswende hata baada ya kupona yanaweza kurithishwa kwa vizazi vijavyo. Hivyo starehe ya watu wawili hatima yake ni kuwaletea janga watu wengine chungu nzima.

**Pili**, japo yawezekana kuwa wazinzi wengine huenda wasipate maradhi ya uasherati lakini hakuna mzinzi anayeweza kunusurika na zile tabia mbaya zinazoandamana na uzinzi. Miongoni mwa sifa hizo ni kutokuwa na aibu, kukosa uaminifu, kutawaliwa na fikra za uasherati, utovu wa nidhamu, ulaghai, uwongo, ubinafsi na kupupia machafu. Mtu akishakuwa na sifa hizi chafu zinakuwa ni sehemu ya mwenendo wake na hivyo anaendelea kuwa nazo popote alipo. Hapana shaka kuwa jamii yenye watu wengi wenye zile tabia zinazoandamana na uzinzi katika jeshi lake, polisi, serikali, mahakama, benki, vyama vya ushirika, n.k. lazima itaathirika sana.

**Tatu**, zinaa ikiruhusiwa basi lazima pia jamii iruhusu kundi kubwa la wasichana ambao ni mabinti na dada za wanajamii wenyewe lifanye kazi ya ukahaba. Hivyo basi badala ya kuanzisha familia na kuishi kama binadamu wanaoheshimika, itabidi wavuliwe heshima yao na wafunzwe kuuza miili yao, mioyo yao, mapenzi yao na uzuri wao kwa kila fasiki na mpita njia. Wanawake hao watakuwa wameyafuja maisha yao bila ya manufaa yoyote kwao wala kwa jamii yao. Lakini kwa vyovyote vile jamii inayohusika itabidi ibebe matokeo yake kiuchumi na kijamii.

**Nne**, kuruhusu zinaa lazima kutaondosha umuhimu na heshima ya ndoa na hatimaye zinaa itachukua nafasi ya ndoa. Kwa sababu sifazinazomea pamoja na uzinzi ni kinyume na zile zihitajiwazo kwa nidhamu ya maisha ya ndoa. Tangu hapo jamii inayohakikisha kuwa yeyote anayetaka kustarehe kwa jimai bila ya kubeba dhamana yoyote anaipata starehe hiyo, basi idadi ya wanaume wataochagua kuoa lazima itapungua kila siku ipitayo.

**Tano**, zinaa lazima hatimaye iutokomezee umma wa binadamu wenyewe. Hii ni kwa sababu katika mazingira ambayo mwanamke anakwenda na mwanamume yoyote, hakuna mwanamume atakayekubali kubeba mzigo wa malezi ya mtoto atakayezaliwa. Bila shaka dhamana ya kumlea mtoto itabidi kubebwa na mwanamke peke yake. Hatimaye wanawake nao watalazimika

kujitahidi kila wawezavyo kujiepusha na mimba, na ikitokea wakapata, wataitoka na pindi isipotoka watahakikisha wanamtupa mtoto mara tu baada ya kuzaliwa. Ni dhahiri kuwa kama watu hawako tayari kuzaa na kulea watoto jamii hiyo baadaye itafutika duniani.

**Sita**, zinaa italetwa watoto wa nje ya ndoa. Na katika kuufunika funika uhaini huu mkubwa kwa jamii baadhi ya watu wanajidai kuwa tofauti ya mtoto wa zinaa na mtoto wa ndoa imo mawazoni mwa watu tu. Lakini kwa hakika hakuna tofauti ya mtoto wa zinaa na mtoto wa ndoa. Madai haya si ya kweli. Mtoto ambaye kuzaliwa kwake kumemchukiza sana baba yake na mama yake hawezi akalelewa katika malezi mema na upendo, hivyo itaathiri upeo na manufa yake kwa jamii. Ili kuliondoshwa tatizo hili baadhi ya watu wanapendekeza kuwa jamii ichukue dhamana ya kuwalea watoto hawa wakati wazinzi wanaendelea kutapakaza mbegu zao. Kioja hapa ni kuwa watu watakaokabidhiwa kazi hiyo ya malezi lazima wawe na nidhamu na uadilifu. Swali ni je, watatoka wapi watu wa aina hiyo kama jamii imeruhusu zinaa, na kama hata asili ya kuanzisha taasisi hizo za kulelea watoto ni kuwawezesha watu watosheleze hamu zao kirahisi na kwa uhuru? Ni nini kitakachowazuia hao watu wasitosheleze hamu zao kirahisi na kwa uhuru? Ni nini kitakachowazuia hao wafanyakazi wanaotakiwa kuwalea watoto hao wasitosheleze hamu zao kwa watoto hao kama wanavyofanya wazazi wao kwa watoto wa wengine?

**Saba**, mtu anayempa mimba mwanamke nje ya ndoa anayaharibu maisha ya mwanamke huyo, kiuchumi na kijamii. Hapa pia kuna watu wanaodai kuwa ni makosa kumshutumua mwanamke huyo kwani uzazi ni jambo jema la kuheshimiwa bila kujali kama mzazi ana mume au la! Fikra hizi zina kasoro kubwa. Ni kweli kuna mtazamo huo utamfurahisha yule mwanamke mzinifu lakini jamii itakula hasara kubwa. Jamii ikikilaani kitendo cha kuzaa nje ya ndoa; laana na uchukivu huo vitakuwa ni kizuizi kikubwa cha kujiepusha na zinaa. Pili laana na uchukivu huo ni dalili kuwa jamii haijafaa kimaadili; bado ni hai na hivyo inaweza kutofautisha kati ya jambo zuri na jambo ovu. Ukweli unabakia kuwa mwanamke mpumbavu aliyeridhia kuzini na mtu ambaye hayuko tayari kuchukua dhamana ya kumkimu yeye wala mtoto hawezi akawa sawa na yule mwanamke mwenye busara aliyejizuia hadi alipompata mtu atakaye chukua dhamana kama mume. Hata kama jamii itajidai kuwa wawili hao wana hadhi sawa, hilo halitatumia matatizo halisi yanayomkumba mama asiye na mume. Nani atampa mapenzi, hifadhi na matunzo anayopata mama aliyeelewa? Ni wapi atakomnunulia mwanawe mapenzi ya baba? Ataupata wapi mdomo wa kumkanya binti yake asiye na baba kujiepusha na zinaa?

Haya ni baadhi tu ya madhara yanayoonyesha kuwa zinaa ni kitu cha hatari sana katika uhai na ustawi wa jamii yoyote ile. Hivyo kampeni za kudhibiti uzazi (birth control) kwa kudhani kuwa zinaa ni jambo la watu binafsi na halina madhara yoyote kwa jamii zinatishia uhai wa jamii nzima. Jamii yoyote inayolidharau jambo hili inajikaribishia maangamizi yake yenyewe.

Ama wale wanaoayaona maendeleo ya uchumi huko Marekani, Uholanzi, Ufaransa, Sweden, Ujerumani n.k. yanakwenda sambamba na kushtadi kwa zinaa katika nchi hizo halafu wakadhani kama wanavyodhani wengine kuwa ufuska wa zinaa ndio uliowapelekea kupata ustawi na hivyo kushauri kuwa “wakati umefika kwa Waafrika kuivua aibu yetu na kukubaliana na hali halisi ilivyo, kwa sababu ni aibu ambayo inatuweka gizani, kutuambia kuwa “nchi zilizoendelea sana wake kwa waume hutembea uchi na haya ni maendeleo”. Wanatumia mantiki lemavu. Kama mfanyabiashara aliyefanikiwa sana katika biashara zake vile vile ni mlevi, muasherati na mcheza kamari ni makosa kudhani kuwa ni ulevi wake, uasherati wake na kucheza kamari kwake ndiko kulikomletea mafanikio yake katika biashara. Kinyume chake tabia hizi zinaweza kumfilisisha mara moja.

## **Msimamo wa Uislamu Juu ya Kudhibiti Uzazi**

Kama tulivyoona, msukumo wa kampeni ya kudhibiti kizazi, umetokana na mfumo mbaya wa kijamii na kiuchumi ulioundwa na wanadamu kutokana na matashi yao ya ubinafsi. Je, katika Uislamu ambapo kila kipengele cha maisha katika jamii kinaendeshwa kwa kufuata sheria za muumba, kuna haja ya kampeni ya kudhibiti kizazi?

Hebu tujibu swali kwa kuuangalia kwa muhtasari mfumo wa jami ya Kiislamu.

Mfumo wa uchumi wa Kiislamu unapingana na mfumo wa kibepari na uchumi wa ulimbikizaji mali pasi na kutoa jasho. Uislamu umeharamisha riba, kamari, kuhodhi bidhaa, udanganyifu na ujanja katika biashara, n.k. Badala yake Uislamu umeweka mfumo wa uchumi ambao unamlazimu kila mtu kutekeleza wajibu wake katika kuchuma na kujipatia chumo halali linalotokana na jasho lake. Pia Uislamu umeweka mfumo wa mgawanyo wa uchumi kwa njia ya Zakat, Sadaqa, urithi, mshahara unaolingana na kazi na kuhakikisha kuwa kila mtu anapata mahitaji muhimu ya maisha yake, ambapo humpelekea kuinua hali za watu mbali mbali za kiuchumi ili kuondoa matatizo yanayosababishwa na mgawanyo mbaya wa uchumi kama ule wa nchi za Ulaya na Marekani uliosababisha kuinukia kwa watu wachache kumiliki uchumi wote wa jamii na kuwanyonya sana watu wengine waliobakia katika jamii. Jamii ya Kiislamu pia imempa mwanamke haki zake zote za kisheria, kijamii na kiuchumi sawa na ilivyompa mwanaume. Mke ana haki ya kisheria katika kipato cha mumewe, ana haki zote za kumiliki kile alichokichuma mwenyewe, ana haki ya kuwa na hisa kwa jina lake katika taasisi yoyote ya kiuchumi. Bali Uislamu umeweka mipaka ya ufanyaji kazi baina ya wanaume na wanawake. Umeweka mgawanyo wa kazi za wanaume na kazi za wanawake kulingana na maumbile yao.

Mchanganyiko holela kati ya wanaume na wanawake umeharamishwa na wanawake wameamrisha kuvaa “hijabu” (vazi la Kiislami lenye kumstiri



mwanamke vizuri kama anavyoridhia Allah(s.w)) wakati wanapokuwa nje ya majumba yao au wakati wakiwa katika hadhara ya wanaume waasio maharimu zao.

Hivi ndivyo Uislamu ulivyotatua matatizo mengi ya kiuchumi na kijamii ambayo huwapelekea wanaume na wanawake kuchupa mipaka ya maumbile katika utendaji wao. Hifadhi na maendeleo ya maisha ya mwanadamu havikuachwa vibuniwe na mwanadamu, bali mfumo mzima wa maisha ya jamii umewekwa na Muumba kwa kiasi kwamba kwa upande mmoja mahitajio yote muhimu ya maisha ya mwanadamu (kama vile chakula, mavazi, makazi) yanakidhiwa na kwa upande mwingine jukumu la kuzaa na kulea kizazi kipya linaendelea kwa namna bora kabisa.

Kwa upande wa maadili, Uislamu unamtaka mwanadamu aishi maisha ya heshima na sitara yaliyoepukana na mambo ya aibu. Uislamu unaharamisha mambo yote yanayomvunjia mwanadamu hadhi yake na utu wake ikiwa ni pamoja na ulevi, uzinifu, uzururaji, uvivu na upotezaji muda katika mambo ya upuuzi. Uislamu unaalani uzembe na kutowajibika, ubadhilifu, anasa na mambo yote yanayompelekea mwanadamu kujisahau. Uislamu unamtaka mwanadamu aishi maisha ya kati na kati- afanye kazi kwa bidii na kupumzika, awe na vitu na utu, ayajali maisha yake ya binafsi na maisha ya jamii. Kwa mfano katika Quran tunahimizwa:

﴿ يَبْنَى ءآءَمَ ٱءُءُوا زَبْنَءَكُمُ عِنءَ كُلِّ مَسْءِءٍ وَكُلُوا وَآشْرَبُوا وَلَا

كُسْرَفُوا إِنَّهُءَ لَا يُءِبُّ الْمُسْرَفِينَ ﴿٧٣١﴾

“ Enyi wanadamu chukueni mapambo yenu wakati wa kila sala na kuleni (vizuri) na kunyweni (vizuri) lakini msipite kiasi (msifanye israfu). Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wapitao kiasi (wapindukiao mipaka). (7:31).

Mtizamo wa Uislamu juu ya matumizi, ni kwamba utajiri wote na kila alichu nacho mwanadamu ni amana ya Allah(s.w) ambayo hana budi kuitumia kwa kuzingatia maagizo Yake (s.w). Hana budi kuitumia katika mambo ya halali kwa kiasi kile kile kinachohitajika. Kwa hiyo, Uislamu haukubaliani kabisa na anasa na ubadhilifu wa mali, vitu ambavyo ndio vichochezi vikubwa vya kampeni hii ya kudhibiti uzazi.

Pia Uislamu unawahimiza watu kupendana, kusaidiana na kuhurumiana. Unasisitiza kila mtu kupewa haki yake katika jamii na unaweka utaratibu wa kushirikiana na kusaidiana. Uislamu umeweka mfumo unaoifanya jamii iwajibike katika kuwasaidia na kuwahifadhi mafukara, masikini na wale wote walioathirika kiuchumi kutokanana tatizo moja au jingine bila ya ubaguzi wa dini, rangi, kabila

wala taifa. Pia Uislamu umeweka utaratibu wenye kuzuia uchoyo, ubinafsi na unyonyaji, maovu ambayo yamekuwa ndio vichochezi vikubwa sana katika kuleta dhana ya kuwa na sera ya kudhibiti uzazi.

Pamoja na mfumo huu wa Kiislamu, Uislamu unamkumbusha mwanadamu mara kwa mara kuwa hapa ulimwenguni hayuko mwenyewe katika kuendesha maisha yake, bali yuko karibu sana na Mwenyezi Mungu ambaye ni Muumba wake, Mlezi wake na Bwana wake pekee.

Mwanadamu hana budi kujitahidi katika kuchuma lakini hana budi kukumbuka kuwa matunda yajitihada zake yatapatikana kutoka kwa Allah(s.w).Jitihada za mja hazishindi kudra ya Muumba. Kwa hiyo mwanadamu pamoja na kujitahidi katika kuchuma hana budi kumtegemea Muumba wake na awe na yakini kuwa Yeye pekee ndiye Mlishaji na Mlezi wake kama anavyovilisha na kuvilea viumbe vyote vilivyomzunguka. Utambuzi huu utamwondolea mwanadamu dhana na kiburi kuwa yeye mwenyewe ndiye anayejilisha na kujitosheleza kwa kila kitu. Dhana hii ya kuwa mwanadamu anajilisha na kujitegemea mwenyewe ni sababu nyingine iliyochochea sera hii ya kudhibiti uzazi.

Allah(s.w) anatuasa katika aya zifuatazo:

وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ حَشِيَّةَ إِمْلَاقٍ نَحْنُ نَرْزُقُهُمْ وَإِيَّاكُمْ إِن قَاتَلْتُمُ كَانَ  
خَطْبًا كَبِيرًا

*Wala msiwaue watoto wenu kwa kuogopa umasikini. Sisindio tunaowaruzuku wao na nyinyi (pia). Kwa yakini kuua ni hatia kubwa. (17:31).*

وَكَأَينَ مِّن دَابَّةٍ لَا تَحْمِلُ رِزْقَهَا اللَّهُ يَرْزُقُهَا وَإِيَّاكُمْ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ

*Na wanyama wangapi hawawezi kujimilikia rikizi zao; Mwenyezi Mungu huwaruzuku wao na nyinyi pia, naye ndiye asikiaye, ajuaye. (29: 60)*

Aya hizi na nyingine kama hizi (Rejea Qur-an 2:29, 67:15, 51:58,15:20-21) zinamkumbusha mwanadamu kuwa pamoja na jitihada zake za kujitafutia maslahi ya maisha yake na ya wale walio chini ya uangalizi wake, hana budi kufahamu kuwa riziki inatoka kwa Allah(s.w). Kwa mtazamo huu wa kumuelekea Allah(s.w) kuwa ndiye Rabbi (Bwana,Muumbaji, Mlishaji na Mlezi) wa viumbe vyote, jamii ya Kiislamu kamwe haiwezi hata kukaribisha mawazo ya kuwa na sera ya kudhibiti uzazi, eti kwa kuhofia njaa au upungufu wa mahitajio muhimu ya maisha.

Kwa muhtasari, tumeona kuwa mfumo wa Uislamu ukiwa ni pamoja na mfumo wake wa uchumi, utamaduni, maadili na mtazamo wake juu ya uendeshaji wa maisha na kufikia lengo lake, hauna nafasi ya kuruhusu msukumo uliopo lekea kutokea kwa kampeni hii ya kudhibiti uzazi na kuifanya sera ya jamii. Kwa hiyo usitazamie kamwe kwa jamii ya Kiislamu kufikiria kuwa na sera ya kudhibiti uzazi.

Kwa maelezo yote haya, ni dhahiri kuwa sera ya kudhibiti uzazi haina nafasi katika Uislamu - wala si jambo la kulikaribisha katika fikra za Muislamu kwa sababu:

- (a) Dhana kuwa wanadamu wakiwa wengi watakosa riziki ni potofu. Ni kukana uwezo wa Allah, na huo ni utwaghuuti (uchupaji mipaka).
- (b) Matatizo ya uchumi (mbali na mengine pia) yashawekewa ufumbuzi wake na mfumo wa maisha ya Kiislamu.
- (c) Sababu nyingine inayofanya sera ya kudhibiti uzazi kijamii isikubalike katika Uislamu ni kuwa huchochea uzinifu. Sera hii imejengwa juu ya dhana kuwa hakuna makosa mume na mke kuingiliana iwe ni nje ya ndoa, wawe ni watoto wa shule n.k. bali lililokosa ni kuzaa mtoto. Kwa hiyo ili mafasiki wautumie “uhuru wao kikamilifu” hapana budi uwepo utaratibu wa kuwahifadhi wasifanye kosa la kuzaa - au tuseme kuzaa kiholela. Huku ni kueneza uzinifu na ufuska katika jamii. Hapana haja ya kuyakariri tena madhara yake hapa, lakini jambo la kutilia mkazo hapa ni kuwa sera ya kudhibiti uzazi inachochea zinaa na zinaa ina madhara makubwa katika jamii. Ndio maana Uislamu umeiharamisha zinaa na kuikemea vikali:

وَلَا تَقْرُبُوا الزَّوْجَ إِتْرَ كَانَ فَنَحِشَةً وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿١٧﴾

*Wala msikaribie zinaa. Hakika hiyo ni uchafu (mkubwa) na ni njia mbaya (kabisa). (17:32)*

الرَّزَانِيَةُ وَالزَّانِي فَاجْلِدُوا كُلَّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا مِائَةَ جَلْدَةٍ وَلَا تَأْخُذْكُمْ بِهِمَا رَأْفَةٌ فِي دِينِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَلَيْشَهَدَ عَذَابَهُمَا

طَائِفَةٌ مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٤﴾

*Mzinifu mwanamke na mzinifu mwanamume, mpigeni kila mmoja katika wao mijeledi (bakora) mia. Wala isiwashike kwa ajili yao huruma katika (kupitisha) hukumu hii ya Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi mnamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Na lishuhudie adhabu (hii) kundi la waislamu. (24:2)*

Zaidi ya kuweka makemeo na adhabu kali kwa mzinfu, Uislamu umeweka kanuni za kudhibiti vishawishi vya zinaa kwa kuhimiza “Hijab”

(d)Tusisahau pia kuwa kuweka sera ya kudhibiti uzazi ni kuingilia mfumo na utaratibu wa Allah(s.w). Allah(s.w) ameweka utaratibu wa mahusiano ya mume na mke yawe kwa njia ya ndoa. Kuhusu malengo ya ndoa tunafahamishwa katika Qur-an:

..... هُنَّ لِبَاسٌ لَكُمْ وَأَنْتُمْ لِبَاسٌ لَهُنَّ ..... ﴿١٧٧﴾

“... Wao (wanawake) ni kama nguo kwenu na nyinyi (wanaume) ni kama nguo kwao...” (2:187).

نِسَاؤُكُمْ حَرْثٌ لَكُمْ فَأْتُوا حَرْثَكُمْ أَنْي شَيْئُمْ وَقَدِّمُوا لِأَنْفُسِكُمْ وَأَتَّقُوا  
اللَّهَ وَاعْلَمُوا أَنَّكُمْ مُلْقَوَةٌ ..... ﴿١٧٧﴾

“Wanawake ni kama konde zenu. Basi ziendeeni konde zenu mpendavyo. Na tangulizeni (wema) nafsi zenu; na mcheni Allah na jueni kwamba mtakutana naye.....” (2:223)

وَمِنْ ءَايَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا وَجَعَلَ  
بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً وَرَحْمَةً إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٣٠﴾

Na katika Ishara Zake nikuwa amekuumbieni wake zenu kama jinsi yenu ili mpate utulivu kwao. Naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Bila shaka katika haya ziko ishara kwa watu wanaofikiri. (30:21)

Kama aya zinazobainisha, malengo ya ndoa ni

- (i) Kupata watoto na kuendeleza kizazi.
- (ii) Kujenga maisha ya jamii. Mume na mke wanapoamua kuishi pamoja katika misingi ya ndoa, makutano yao kimwili hupalilia mapenzi na huruma kati yao ambayo huwa msingi imara wa kuunda jamii yenye kuishi kwa furaha na amani.


Je, kukutana mwanamke na mwanamume kwa lengo tu la kufurahia ngono, kunapelekea kufikiwa kwa moja ya malengo haya? Kama sivyo huku ni kutumia vipawa vya kimaumbile nje ya lengo lililokusudiwa na ni kuingilia mfumo wa maumbile aliouweka Allah(s.w). Qur-an imekuwa bayana mno kuwa kuingilia au kubatilisha mfumo wa maumbile aliouweka Allah ni kitendo kiovu mno na cha kitwaghuuti.

## Kupanga Uzazi katika Uislamu

Kama ilivyo haramishwa kwa jamii, Uislamu umeharamisha pia kudhibiti uzazi kwa mtu binafsi kwa khofu ya kushindwa kuwalisha au visingizio vingine. Hata hivyo Uislamu haujawataka watu wazae kiholela.

**Kwanza** umekataza watu kuzaana nje ya ndoa.

**Pili**, waliona wanatakiwa wazingatie umri baina ya mtoto na mtoto mwingine. Kwa anayetaka kukamilisha muda wa kunyonyesha, basi amnyonyeshe mtoto wake kwa miaka mwili:

❖ وَالْوَالِدَاتُ يُرْضِعْنَ أَوْلَادَهُنَّ حَوْلَيْنِ كَامِلَيْنِ ۗ لِمَنْ أَرَادَ أَنْ يُنْمِئَهُنَّ  
الرَّضَاعَةَ ..... 

*Na wanawake waliozaa wawanyonyeshe watoto wao miaka miwili kamili, kwa anayetaka kukamilisha kunyonyesha.....” (2:233)*

Kunyonyesha humsababisha mama mzazi kuchukua muda mkubwa kabla ya kuingia tena katika siku zake. Iwapo mwanamke atapata siku zake wakati mtoto yungali mchanga (hajafikia umri wa miaka miwili), anatakiwa ajizuie asipate mimba; kwani katika Hadith iliyosimuliwa na Imamu Muslim, Mtume(s.a.w) amesema kuwa mwanamke akipata mimba wakati yungali na mtoto mchanga, afya ya mtoto hudhurika. Njia za kuzuia mimba katika kipindi hiki cha kunyonyesha ni zile ambazo hazina madhara ya kiafya kwa baba wala mama. Katika Hadith iliyopokelewa na Bukhaary na Muslim, Jabir(r.a) amesema kuwa wakati wa Mtume(s.a.w) wao walikuwa wanatumia njia ya kuzuia mimba inayoitwa ‘azal” (with drawal au coitus interruptus), yaani njia ya kumwaga mbegu za uzazi nje lakini Mtume(s.a.w) hakuikataza.

Hapa ifahamike kwamba suala la kupanga juu ya muda wa kunyonya mtoto linamhusu baba na mama na si suala la kuwekewa sera na taifa; kwani hali za watu zinatafautiana.

Ama kwa mama atakayekuwa na matatizo ya kiafya, ikathibiti kuwa akibeba mimba atadhurika au kuhatarisha maisha yake, anaruhusiwa kufunga kizazi hata kutoa mimba ambayo imeshatunga.

## Hitimisho Juu ya Kudhibiti Uzazi

Tumeona kuwa kuongezeka kwa watu si tatizo kwani hakuna tatizo la riziki kama wale wasiomtegemea Allah(s.w) wanavyodai. Hivyo, kuwapangia watu wazae watoto idadi Fulani ni kinyume kabisa na mafundisho ya Uislamu. Wajibu

wa mwanadamu ni kufanya kazi kwa bidii na maarifa, na pia kuweka utaratibu mzuri wa mgao wa rasilimali katika jamii.

Uislamu umekemea vikali zinaa na kuweka adhabu kali kwa wazunifu. Sera ya kudhibiti uzazi na Elimu ya ngono (sex education) ni nyenzo “nzuri sana na madhubuti” za kupalilia zinaa katika jamii. Katu waislamu hawatazikaribisha. Huu ndio msimamo wa Uislamu juu ya suala la kudhibiti uzazi na waislamu wa kweli daima watakuwa katika msimamo huu kwani:

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَىٰ اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ  
الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلِيلًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾

*Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume, hakika amepotea upotofu ulio wazi kabisa. (33:36)*

## Zoezi 2:4

- (a) Unaelewa nini juu ya kudhibiti Uzazi?  
(b) Bainisha sababu za kuibuka kwa kampeni ya Kudhibiti Uzazi na makusudio yake.
- Kwanini hoja za kampeni za Kudhibiti Uzazi hazina mashiko wala tija yoyote kwa jamii.
- Bashiri (predict) matunda yatakayopatikana iwapo sera ya kudhibiti uzazi itafikia kilele cha mafanikio yake katika jamii yetu.
- Wala usiikaribie zinaa, kwa hakika huo (uzinifu) ni uchafu na ninjia mbaya kabisa (17:32).

Tumia mifano halisi katika jamii kuonesha kusibu kwa kauli hii ya Allah(s.w) inayopingwa na kukiukwa na wanadamu kila uchao.

- Eleza kwa kuzingatia dondoo muhimu namna Uislamu unavyodhibiti uholela wa kuongozeka kwa watu, na msimamo wake katika kupanga Uzazi.
- Katika Jamii ya watanzania, tatizo la kuongezeka kwa watu kiholela halisababishwi na ndoa, ila zinaa. Unasemaje?

## **HADHI NA HAKI ZA MWANAMKE KATIKA JAMII**

### *Utangulizi:*

Uislamu unamuelekeza mwanadamu namna nzuri ya kuendesha maisha yake katika kila kipengele cha maisha akiwa binafsi, katika familia na katika jamii. Mfumo huu wa Uislamu, kwa kuwa umeasisiwa na Allah(s.w), Aliye Mjuzi Mwenye Hekima, ndio pekee uanomuelekeza mwanadamu kujenga familia imara iliyosimamishwa juu ya msingi wa haki na uadilifu. Hivyo utaona katika jamii zote za Ulimwengu, ni jamii ya Kiislamu pekee inayompa mwanamke hadhi na haki zake zote anazostahiki. Kinyume chake jamii nyingine zote zilizobakia, za kale na za sasa, zimemnyanyasa na kumdumisha mwanamke kwa kiasi kikubwa.

Sura hii, ili kuonesha kwa uwazi ubora wa mfumo wa Kiislamu katika kumpa mwanamke hadhi na haki zake zote anazostahiki, ukilinganisha na mifumo ya maisha ya kijahili, tumeigawanya katika sehemu mbili:

- Hadhi na haki za mwanamke katika jamii za kijahili.
- Hadhi na haki za mwanamke katika jamii ya Kiislamu.

### **Hadhi na Haki za Mwanamke katika Jamii za Kijahili**

Hivi leo duniani kote, suala la hadhi na haki za mwanamke katika jamii linaongelewa katika kumbi mbali mbali za kitaifa na kimataifa.

Pametokea makundi ya harakati ya kitaifa na kimataifa ya kutetea hadhi na haki za wanawake ziliziporwa na wanaume. Swali la kujuliza ni; Je, jitihada hizi zimefanikiwa au zinaonyesha kuleta mafanikio yoyote hapo baadaye? Jibu la swali hili tutalipata baada ya kupitia mifano michache ya kihistoria inayoonesha jinsi mwanamke alivyo nyanyaswa na kudunishwa na jamii mbali mbali za kijahili na hatua zilizochukuliwa na jamii hizo ili kumkomboa. Katika sehemu hii tutazipitia jamii zifuatazo:

1. Jamii za Magharibi.
2. Jamii za Mashariki.
3. Jamii za Kiafrika.

## 1. Jami za Magharibi

### (a) Ugiriki

Tunajifunza katika historia ya Ulimwengu kuwa jamii ya Wagiriki ilikuwa miongoni mwa jamii zilizoanza kustarabika. Lakini utakuta kuwa hadhi ya mwanamke katika jamii hiyo ilikuwa chini sana. Bwana E.A. Allen katika kitabu chake “History of Civilization Vol. 3” anasema mwanamke wa Kigiriki alilazimishwa kuolewa pasina idhini yake.

Mumewe huyo alihesabiwa kuwa Bwana (Lord) wake. Mwanamke alihesabiwa kuwa ni kama mtoto na kwahiyo alitakiwa kumtii mumewe bila kuhoji. Wanawake huko Ugiriki waligawanyika katika makundi matatu:

- (i) Makahaba (Malaya) ambao kazi yao ilikuwa ni kuwastarehesha wanaume tu.
- (ii) Watumishi ambao kazi yao ilikuwa kuangalia na kutunza siha za mabwana zao.
- (iii) Wake ambao kazi yao ni kuzaa na kulea watoto.

Mke alitakiwa awe mwadilifu na achunge murua wake lakini haikuwa vibaya kwa mwanamume kujamii nje ya ndoa. Matokeo ya utaratibu huu ni kuwa wanawake makahaba wakawavutia watu wa ngazi zote – wanafalsafa, washairi, wanahistoria, wanafasihi na wasanii. Picha na sanamu za wanawake walio uchi zikazidi kuchochea zinaa na ufasiki.

Ndoa ikaja kuonekana kuwa kero na zinaa ikawa jambo takatifu. Kuzama katika uzinifu kuliwapeleka Wagiriki kuchonga na kuabudu **Aphrodite** – mungu wa kike wa urembo na mahaba. Kwa mujibu wa mafundisho ya Wagiriki ni kuwa huyo “Aphrodite” anasemekana kuwa alikuwa ni mungu wa kike aliyeolewa na mungu mwingine. Lakini hakutosheka na mume huyo mmoja. Akaanza kuzini na miungu wengine watatu na akawa pia anazini na binadamu mmoja. Mungu huyo alipofanya jimai na binadamu, wakazaa mungu wa kiume aliyeitwa **Cupid** yaani mungu wa mapenzi. Uzinifu wa “Aphrodite” na kuabudiwa kwake na Wagiriki ni kielelezo cha namna jamii hii iliwaatukuza makahaba na kuupa uzinzi hadhi kubwa.

Kutokana na haya tunajifunza kuwa mwanzoni mwanamke katika jamii ya Ugiriki alidunishwa sana. Baadaye jamii ilipopiga hatua mbele katika maendeleo ya kiuchumi, hadhi duni ya mwanamke ilibadilishwa sura. Mwanamke aligeuzwa kuwa chombo cha kuwastarehesha wanaume jambo ambalo lililizi kumdunisha na kumdhaliisha.



**(b) Warumi**

Jamii ya Warumi nayo ni miongoni mwa jamii zinazohesabika kuwa zilianza kustaarabika mapema katika historia ya ulimwengu. Je jamii hii ilimpa mwanamke heshima na hadhi anayostahiki? Katika historia ya Urumi tunajifunza kuwa Warumi walimwona mwanamke kama mtoto anayetakiwa kuangaliwa na kukemewa. Akiolewa yeye na mali yake ni mali ya mume. Akikosea, mume alikuwa na mamlaka ya kupitisha hukumu yoyote. aliyoweza hata ya kutoa adhabu ya kifo.

Mwanamke alikatazwa kushiriki katika jambo lolote. Hakuruhusiwa kutoa ushahidi wala kumuwekea mtu dhamana. Mumewe akifariki, Shemeji zake walikuwa na haki ya kumrithi.

Hapo awali katika historia ya Urumi, wanawake walibakia nyumbani na ukahaba (umalaya) haukujulikana. Mtu kufanya kitendo cha mapenzi na mkewe kama vile kumbusu mkewe hadharani ilionekana ni kitendo kiovu na utovu wa adabu na heshima. Kiongozi mmoja wa Kirumi alishutumiwa vibaya na raia wake kwa kitendo cha kumbusu mkewe mbele ya binti yake.

Warumi waliposongambele katika maendeleo ya kijamii, waliona wamkomboe mwanamke kwa kulegeza sharia ya ndoa kiasi cha kuifanya kama mkataba wa wawili wanaopendana. Wanawake walipewa haki ya kurithi na walikuwa huru na mamlaka ya baba au mume. Katika wakati huu sio tu kuwa wanawake wa Kirumi walijitegemea kiuchumi bali walikuwa wakiwakopesha waume zao kwa riba kubwa kwa kiasi kwamba wanaume ambao wake zao walikuwa matajiri walijikuta wamekuwa watumwa wao.

Kutaliki kulikuwa jambo jepesi na ndoa zilikatika bila ya sababu za msingi. Kwa mfano Seneca (4B.C – 65 A.D), Mwanfalsafa Mashuhuri wa Kirumi alitoka shutuma kwa watu wake kutokana na kiwango cha talaka kilicho kithini katika jamii yake kwa kusema:

*“Now divorce is not regarded as something shameful in Rome. Women calculate their age by the number of husbands they have taken.”*

**Tafsiri:**

*Talaka sasa hainonekani kuwa ni jambo la aibu hapa Urumi. Wanawake wanahesabu umri wao kwa idadi ya Wanaume waliofunga nao ndoa.*

Yaani, wanawake wa Kirumi katika wakati huo wa historia, kwa uhuru waliopewa na jamii waliweza kuolewa na wanaume wengi kwa muda mfupi. Kwa mfano Martial (43 A.D – 104 A.D) ameeleza juu ya mwanamke aliyolewa na wanaume kumi. Juvenal (60 A.D – 130 A.D) ameandika juu ya mwanamke aliyolewa na wanaume wanane, mmoja baada ya mwingine, katika kipindi cha miaka 8. St. Jerome (340 A.D – 420 A.D) ameeleza juu ya mwanamke wa ajabu

ambaye mume wake wa mwisho alikuwa wa 23, mmoja baada ya mwingine. Yeye mwenyewe kwa mumewe huyo wa mwisho alikuwa ni mke wake wa 21. ni katika wakati huu uzinifu ulianza kustawi na wazinifu hawakuhesabiwa kuwa ni wakosaji wanaostahiki kuadhibiwa.

Katika historia hii fupi, tunajifunza jinsi mwanamke alivyokandamizwa na jamii hapo awali na tumeona hali ya mwanamke ilivyokuwa baada ya kukombolewa. Je, ukombozi huu ulimpa mwanamke **hadhi** yake anayostahiki?

### *(c) Ulaya chini ya Kanisa*

Ukristo ulipoingia Ulaya uliisaidia jamii kuondoa mila chafu na kukomesha mwenendo mchafu wa wanawake kuuza miili na utu wao kwa wanaume. Pamoja na jitihada hizi bado, mafundisho ya Ukristo yalizidi kumnyanyasa mwanamke na kumuona yeye kuwa ndio chanzo cha matatizo yote katika jamii. Hapa tutajaribu kunukuu maandiko machache ya Watakatifu na viongozi wa Kanisa kuonesha ukristo ulivyomnyanyasa na kumnyanyapaa mwanamke.

Mawazo ya Paulo, ambaye ameandika vitabu 14 kati ya vitabu 27 vya Agano Jipya, yanaathari kubwa katika historia ya Ukristo. Paulo anawahesabu wanawake kuwa ni waovu kwa hiyo anawapiga marufuku kufundisha:

*Mwanamke na ajifunze katika utulivu, akitii kwa kila namna, simpji mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala mwanamume, bali awe katika utulivu. Kwa maana Adamu ndiye aliyeumbwa kwanza, na Hawa baadaye. Wala Adamu hakudanganywa, ila mwanamke alidanganywa kabisa akaingia katika hali ya kukosa. (Timotheo 2:11-14).*

Zaidi ya hivyo, Paulo anasema wanaume ni mfano wa utukufu lakini wanawake ni utukufu wa mwanamume:

*Lakini nataka mjue ya kuwa kichwa cha kila mwanamume ni Kristo, na kichwa cha mwanamke ni wanamume, na kichwa cha Kiristo ni Mungu... Kwa maana kweli haimpasi mwanamume kufunikwa kichwa, kwa sababu yeye ni mfano wa utukufu wa Mungu. Lakini mwanamke ni utukufu wa mwanamume... Kwa hiyo imempasa mwanamke awe na dalili ya kumilikiwa kichwani. (Wakorintho 11:3, 7, 10).*

Paulo ambaye hakupata kuoja katika maisha yake anarudia mitholojia ya nyoka kusisitiza jinsi mwanamke anavyodanganywa:

*“Lakini nachelea, kama yule nyoka alivyomdanganya Hawa kwa hila yake, asije akawaharibu fikra zenu mkaacha unyoofo na usafi kwa Kristo”. (Wakorintho 11:3).*

Pamoja na maandiko haya ya Paulo kuna maandishi mengi mengineyo ya viongozi wa kanisa ambayo yamewaelezea wanawake kama viumbe viovu kabisa. Akitoa muhtasari wa msimamo wa viongozi wa kanisa, mwanahistoria mashuhuri, Bwana Leakey ameandika hivi:

*This pious incentive, which formed so conspicuous and so grotisue a portion of the writing of the fathers... Woman was represented as the door of hell, as the mother of all human ills. She should be ashamed at the very thought that she is a woman. She should live and continue in penance on account of the curse she has brought upon the world. She should be ashamed of her dress for it is a memorial of her fall, she should be especially ashamed of her beauty for it is the most potent instrument of the devil.*

### **Tafsiri:**

*Kilichoko hiki kitakatifu kilichozusha maandishi ya kutisha ya Mapadre... mwanamke alitajwa kama mlango wa Jahannam na mama wa maovu yote ya binadamu. Fikra tu ya kuwa yu mwanamke yampasa aone aibu. Aishi na adumu katika matubio kwa sababu ya laana aliyoiteta duniani. Hana budi kulionea haya vazi lake kwani ni kumbukumbu ya kuanguka kwake (dhambini), na hasa hasa auonee aibu urembo wake kwani hiyo ni silaha kubwa ya shetani.*

Tertullian Quintus Septimius Florens (160 A.D – 220 A.D) naye ameandika juu ya Mwanamke. Miongoni mwa maandiko yake ni haya yafuatayo:

*You are the devils, getaway, you are the ... of the forbidden tree, you are the first deserters of the divine law. You are she who persuaded him whom the devil was not valiant enough to attack. You destroyed so easily God's image, man. On account for your deserving death even as the son of God had to die.*

### **Tafsiri:**

*Wewe (mwanamke) ni mlango wa shetani, wewe ndiye... wa mti uliokatazwa, wewe ndiye wa kwanza kuitelekeza sheria ya Mungu. Wewe ndiye (yule mwanamke) aliyemshawishi yule (mwanamume) ambaye shetani hakuweza kumshambulia. Wewe ulimharibu kirahisi sana yule ambaye ni mfano wa Mungu, (yaani) mwanamume. Kwa sababu ya dhambi zako mwana wa Mungu (yaani Yesu) ilibidi afe (msalabani).*

Maandiko haya yanaonesha Ukristo unavyomnyanyasa mwanake.

*Ni katika imani ya Kikristo kuwa mwanamke ni chanzo cha dhambi, kutokana na madai yao kwamba ni Hawa aliyemhadaa mumewe Adam wakala tunda katika mti waliokatazwa huko Peponi kabla ya kuletwa kwao hapa duniani. Wakristo wanaamini kuwa kama Hawa asingalimhadaa Adam wakala tunda pasingalikuwa na maisha haya machungu ya hapa duniani bali mwanadamu angali bakia na uzima wa milele huko peponi. Kutokana na imani ya Wakristo, dhambi hii ya asili aliyoisababisha mwanamke wa kwanza, haikusamehewa kwa mwanadamu mpaka alipokuja Yesu kumkomboa mwanadamu kutokana na dhambi hii kwa kujitoa muhanga huko msalabani.*

Pamoja na itikadi hii ya Dhambi ya Asili, itikadi nyingine ya Wakristo ni kwamba kitendo cha jimai ni kitendo kiovu na kichafu hata kama mume na mke wamefunga ndoa ya halali. Pia ni katika msingi huu kukaa bila kuoa au kuolewa, imedhaniwa na Wakristo Wakatoliki kuwa ni kitendo cha hali ya juu cha ucha-Mungu. Kwa mtazamo huu kuoa kumefanywa kuwa jambo ovu lisilo budi. Itikadi hii iliifanya jamii ya Kikristo ione kuwa ndoa ni mzigo mkubwa kwa mwanamume na mwanamke.

Tumejifunza katika sheria ya familia ya huko Ulaya chini ya kanisa kuwa:

- (1) Mwanamke alinyimwa haki za kiuchumi na alifanywa amtegemee mwanamume moja kwa moja. Alipewa sehemu ndogo tu ya urithi, alikuwa na haki finyu sana za kuchuma mali, hakuwa na mamlaka juu ya mali yake aliyoichuma kwani hii ilikuwa katika mamlaka ya mumewe ambaye alikuwa na haki zote juu yake.
- (2) Talaka iliharamishwa kabisa katika sheria hii. Mume na mke walilazimika kuishi pamoja mpaka wafe hata kama hawakuelewana. Katika kiwango kikubwa cha kutoelewana, mke na mume wanaruhusiwa kutengana lakini hapana ruhusa kuoa au kuolewa tena. Hatua hii iliwafanya wawili hawa kuwa watawa au kutumbukia katika ufuska.
- (3) Ilionekana ni jambo la kuchukiza au dhambi kwa mtu kuoa au kuolewa tena, baada ya mke au mume kufariki. Ndoa baada ya kufiwa na mume au mke ilihesabiwa kama “uzinifu wa aina yake – “Civilized Adultery”.

Mtu akizingatia kwa makini mafundisho ya Ukristo juu ya mwanamke na sheria ya ndoa ya Kikristo, anaweza kuelewa kwa nini wanawake katika nchi za Kikristo huko Ulaya na Marekani walikuja yakataa mafundisho haya na kupigania haki ya kuwa sawa na wanaume. Kosa ambalo watu wengi hulifanya ni kudhani kuwa maadam Ukristo unamdhalilisha mwanamke, na Uislamu vile vile unamdhalilisha mwanamke. Na baadhi ya Waislamu ambao hawajafanya juhudi za kujifunza Uislamu na Ukristo wamejikuta wanasaidia kukuza dhana hii.

#### ***(d) Ulaya Wakati wa Mapinduzi ya Viwanda***

Katika karne ya 18, wanafalsafa na waandishi wa Ulaya walipaza sauti za dhidi ya jamii iliyojengwa katika misingi ya Ukristo iliyochanganyika na ukabaila (feudalism), ambayo ilikuwa ikiwanyonya na kuwanyanyasa wanyonge. Ni katika wakati huo palitokea mapinduzi ya viwanda yaliyoipa Ulaya na Marekani sura mpya ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Hatua za mwanzo zilizochukuliwa na jamii hii ya mapinduzi ni pamoja na kumkomboa mwanamke na kuinua hadhi yake kutoka kwenye hali ya kudunishwa na kumfikisha kwenye hali ya kuwa na heshima na haki sawa na wanamume katika jamii. Sheria za Ndoa na talaka zilirekebishwa. Haki ya

kuchuma na kumiliki mali ilirejeshwa kwa mwanamke. Itikadi zote za kidini na mila zilizomdhalilisha mwanamke zilirekebisha. Wanawake walipata fursa sawa na wanaume katika elimu na mafunzo ya juu. Marekebisha haya yaliamsha ari na vipawa vya mwanake vilivyo kandamizwa hapo awali. Wanawake walizipamba nyumba na kuichangamsha jamii kwa kujiingiza katika shughuli mbali mbali za ustawi wa jamii. Matunda yaliyopatikana kutokana na kumpa mwanamke heshima yake na haki zake nyingine za msingi kupatikana kwa malezi na afya bora kwa jamii na ukuaji wa sayansi kimu ( Domestic Science).

Pamoja na matunda haya, kwa upande mwingine, jamii ya Ulaya iliporomoka sana kimaadili kutokana na mtazamo wake juu ya demokrasia kati ya wanaume na wanawake. Katika kumtetea mwanake Ulaya Magharibi ilizingatia vipengele vifuatavyo:

- (i) Usawa kati ya Mume na Mke bila kujali maumbile yao ya kijinsia.
- (ii) Kujitegemea kiuchumi kwa mwanamke.
- (iii) Uhuru wa kuchanganyika wanaume na wanawake.

Je, jamii ya Ulaya iliyoundwa juu ya misingi hii ya demokrasia kati ya mwanamume na mwanamke, ilistawi na kumbakisha mwanamke katika hadhi yake? Hebu tuangalie matokeo ya utekelezaji wa Demokrasia hii:

**Kwanza**, Uoni juu ya usawa kati ya mwanamke na mwanamume haukuishia kwenye kupata heshima na haki sawa kati yao, bali ilichukuliwa kuwa hata kimaumbile wako sawa. Hivyo mwanamke naye alidai kufanya shughuli zile zile anazofanya mwanamume. Wanawake walidai kuwa wawe huru katika kuchunga miiko ya maadili. Wawe huru kuvaa na kujistarehesha kama wanaume. Mtizamo huu wa usawa ulimfanya mwanamke aidharau nafasi yake kama mlezi wa familia na badala yake akajiweka katika mashindano na wanaume katika uchumi, siasa na harakait nyinginezo za kijamii. Alijiingiza katika kampeni za kugombea uongozi wa kisiasa, alikimbilia kazi za Ofisini na viwandani, alishindana na wanaume katika biashara na viwanda, katika michezo na mazoezi ya kimwili, katika kuendesha vilabu vya michezo na upigaji wa muziki. Katika hali hii, kuwalea watoto na kuiweka familia katika utulivu, upendo na ushirikiano, ilikatika kuwa jukumu lake la asili. Kwa mtazamo huu wa usawa, maisha ya ndoa yalidharaulika na uzinifu katika jamii ukawa ni jambo la kawaida na kuigharimu jamii kiasi kikubwa (zingatia madhara ya uzinifu katika jamii) na kuzidi kumdunisha mwanamke.

**Pili**, Kujitegemea kiuchumi kwa mwanamke kumemdanganya asiwe na haja ya kuwajibika kwa mumewe na kuvunja utaratibu wa asili wa “Man for the field and Woman for the hearth” yaani “Mwanamume ni wa shambani na mwanamke ni wa nyumbani”. Katika mtazamo huu wa maendeleo ya Ulaya, mwanamume na mwanamke wote wana jukumu sawa la kuchuma na malezi ya familia

yakakabidhiwa watumishi wa nyumbani (House girls/House boys), taasisi nyingine kama vile vituo vya watoto, shule n.k. Katika hali hii ya mwanamke kujitegemea kiuchumi, hapakuwa na kiungo chochote cha kumuunganisha mwanamume na mwanamke ila haja tu ya kutosheleza matamano ya ngono. Sasa, kama mwanamke anajitegemea mwenyewe kwa chakula, mavazi, makazi, na kwa mahitaji yake yote mengine, kwa nini abakie kuwa mwaminifu kwa mume mmoja ambaye hamuhitaji kwa lolote ila kwa jimai tu? Kwa nini ajiingize katika maisha ya ndoa ambayo yamefungamana na kanuni za kimaadili na sheria? Kama, kwa mtazamo wa usawa tuliouona, umeshamuondolea vizingiti na kumpa uhuru kamili wa kuzini kwa nini asifuate njia hii nyepesi na ya haraka ya kutosheleza matamano yake ya kimwili na badala yake achague njia ndefu ambayo si tu kuwa imeambatana na majukumu bali pia inataka kujitua muhanga? Kwa hali hii umalaya katika jamii ulikuzwa na kutetewa kama haki nyingine zilivyotetewa. Mwanzoni walipatikana watoto wengi waliozaliwa nje ya ndoa, lakini sasa idadi hii imepunguzwa baada ya kubuniwa njia mbali mbali za kuzuia (kudhibiti) kizazi. Pia ili kujiepusha na kupata watoto, wanaume kwa wanawake walifikia kiwango cha kufanya jimai na mbwa. Hiki ndicho chanzo kikubwa cha magonjwa ya ya zinaa – kaswende, kisonono, AIDS n.k. Hata hivyo, hapakuwa na ubaya wowote katika jamii hii mwanamke kupata mtoto nje ya ndoa.

Mamia kwa maelfu ya vijana wanawake katika nchi za Ulaya na Marekani wanapendelea kuishi maisha ya kutoolewa na wamefanya umalaya kuwa mtindo wa maisha. Wale wachache wanaoolewa, kwa kuwa kuna huo uhuru wa kujitegemea kiuchumi na kutomtegemea kabisa mume kwa mahitaji yoyote yale, ila kwa jimai tu, ndoa nyingi huwa ni zenye kuyumba. Panakosekana kiungo madhubuti cha unyumba wao. Mume na mke ambao kila mmoja anajitegemea kiuchumi, hujikuta hawana kitu madhubuti cha kuwaunganisha na kuwafanya wakubaliane na kuvumiliana katika mambo mbali mbali ya kiunyumba. Upendo wa kishabiki unaopatikana katika ule muda mfupi wa jimai hautoshi kuwafanya hawa wawili waishi maisha ya kuvumiliana. Kutoelewana katika jambo dogo tu hivi huwa ni sababu tosha ya kuvunja ndoa.

**Tatu,** Uhuru wa kuchanganyika wanaume na wanawake umechangia sehemu kubwa ya kukuza umalaya katika nchi za Ulaya. Matamano ya ngono hupata nguvu sana wanawake na wanaume wanapochanganyika pasi na mipaka. Katika kuukuza umalaya, wanawake katika nchi nyingi za Ulaya na Marekani hujitahidi sana kujipodoa kwa vipodozi vya aina mbali mbali, kuvaa mavazi mafupi, yanayobana yanayoonyesha mwili (transparent). Wakati mwingine hutembea uchi wa nyama. Picha za wanawake walio uchi katika vitabu vya mapenzi, magazeti, sinema, n.k. ni vitu vya kawaida katika nchi nyingi za Ulaya na Marekani. Mazingira haya yamechochea wanaume kupata na kiu isiyokatika ya kutaka kutosheleza matamano ya ngono. Kutokana na mazingira haya vijana wadogo huingizwa katika uzinzi hata kabla ya kufikia baleghe.

Mabinti wadogo kuwa na marafiki wa kiume (boy friends) ni jambo la kawaida linaloshangiliwa na wazazi. Hii ndio jamii inayohesabika kuwa imeendelea katika kutetea haki na heshima ya mwanamke.

## 2. Jamii za Mashariki

Kila jamii utakayoichunguza utakuta kunyanyaswa na kudhalilishwa kwa mwanamke kuko pale pale. Ukichunguza hata zile nchi zilizohesabika katika historia kuwa mbele katika maendeleo ya mwanadamu kama vile China, India, Iraq na Iran, utasikitishwa na vitimbwi alivyokuwa akifanyiwa mwanamke. Hebu tuanglie baadhi ya jamii chache za nchi za Mashariki.

### (a) Uchina

Mwanamke wa Uchina alikuwa hana haki yoyote katika jamii. Hata watoto wake aliowazaa mwenyewe hakuwa na haki nao. Mume wake aliweza kuuza mwili wake kwa mume mwingine. Baada ya mumewe kufariki alirithiwa kama mali na ndugu wa mumewe na haikuwezekana kwake kuolewa tena. Juu ya yote hayo, wanawake waliuzwa na kufanywa watumwa. Mpaka kufikia 1937, Uchina ilikuwa na wasichana watumwa milioni mbili.

Katika kitabu chao kiitwacho, Marriage East and West (New York, 1960) David na Mace wanasema hadhi ya mwanamke huko Uchina ilikuwa duni sana. Mshairi mashuhuri wa China aliyemitwa Xuan, (100B.C) aliandika katika shairi moja:

*Ni huzuni ilioje kuwa mwanamke Duniani hakuna kilicho duni Duniani hakuna kilicho duni kuliko mwanamke.*

Mwana falsafa wao mkubwa, Bwana Confusious ambaye alikuwa pia kiongozi wa kidini aliwafundisha watu kuwa wajibu mkuu wa mwanamke ni utii. Akiwa mtoto amtii baba yake, akiolewa amtii mumewe na akifiwa na mumewe basi amtii mwanawe wa kiume. Na atii kila kitu bila kuhoji. Wachina pia waliamini kuwa mtu akipata mtoto wa kiume amepata hidaya kutoka kwa Mwenyezi Mungu lakini akipata binti, basi ni nuksi.

### (b) India

Katika jamii ya India mwanamke hakuthaminiwa kabisa. Mwanamke alihesabiwa kama mashine ya uzazi. Iwapo mwanamke hakujaaliwa kupata mtoto wa kiume kwa mume aliyemuoa, alilazimishwa azini na mume asiyemjua ili apate mtoto wa kiume. Budha, kiongozi wa kidini huko India aliwafundisha wafuasi wake kuwa mwanamke ni kiumbe duni aliyejawa na dhambi. Hakuna kiumbe anayefaa kuhofiwa na kuepukwa kama mwanamke. Na kwa mujibu wa sheria ya Manu wa huko huko India, wanawake ni lazima wabanwe na kudhibitiwa vikali kwani wao ndio chanzo cha madhambi yote na ufidadi.

Mwanamke hakuna na haki ya urithi bali urithi ulikuwa ni haki ya watoto wa kiumbe tu. Mke alitakiwa amwite mume wake ama Bwana wangu au Mungu wangu kwani mume alihesabiwa kuwa ni mungu wake hapa duniani. Ilikuwa marufuku mke kula pamoja na mumewe. Jimai hata kati ya mtu na mkewe ilihesabika kuwa ni kitu kiovu na kichafu. Mke mwema alikuwa yule ambaye akili zake, kauli yake na mwili wake si huru.

Mke hakuruhusiwa kuolewa tena pindi mumewe akifariki. Ilibidi afanye moja katika mawili, ama ajichome moto ili afe na kumfuata mumewe au awe mtumishi wa shemeji zake hadi atakapo fariki. Mwenendo huu wa kujichoma moto au kuchomwa moto na mashemeji zake bado unaendelea hadi leo. Gazeti liitwalo "The Economist" 27 August – 2 September 1983 liliandika hivi:

*The grisly practice of wife burning in India shows no sign of succumbing on its own to modern ideas about the value of a woman's life. Many women are doused with kerosene and set aflame by in-laws greedy for more dowries... The official figures shows 610 burnings in 1982.*

#### **Tafsiri:**

*Mwenendo wa kutisha wa kuwachoma moto wanawake huko India hauonyeshi dalili za kukoma kutokana na fikra za kisasa juu ya thamani ya uhai wa mwanamke. Wanawake wengi humwagiwa mafuta ya taa na kuchomwa moto na mashemeji kwa uroho wa kutafuta mahari nyingine. Taarifa rasmi ya serikali yaonyesha kuwa wanawake 610 walichomwa moto mwaka 1982.*

Hali ilikuwa hivyo hivyo huko Japan.

#### **(c) Mashariki ya kati**

Urabuni kabla ya Ujumbe wa Mtume Muhammad(s.a.w) mwanamke alionekana kitu duni na nuksi kwa jamii. Baba akipewa habari ya kuzaliwa mtoto wa kike alijinyonga nyonga na kuhuzunika sana. Wanaume walikuwa wakitafuta kila njia ya kujiokoa na aibu hiyo ya kupata mtoto wa kike. Ilikuwa kuchagua moja katika njia mbili: Ama amzike binti huyo mzima akiwa hai au aendelee kuishi maisha ya aibu na fedheha kwa kumbakisha hai. Mara nyingine wanaume walikuwa wakiwalazimisha wake zao wanapoanza mwezi wa tisa wa ujauzito wa kuchimba shimo uvungni mwa kitanda. Shimo likiwa tayari mume anamuagiza mkewe: "Ukimzaa mtoto mwanake basi haraka sana mfukie mwenyewe katika shimo hii kabla sijaja." Qur'an inatufahamisha tabia ya Waarabu dhidi ya watoto wa kike katika aya zifuatazo:



وَإِذَا بُشِّرَ أَحَدُهُم بِالْأُنثَىٰ ظَلَّ وَجْهُهُ مُسْوَدًّا وَهُوَ كَظِيمٌ ﴿٥٨﴾ يَتَوَارَىٰ  
 مِنَ الْقَوْمِ مِنْ سُوءِ مَا بُشِّرَبِهِ ۚ أَيَسْكَبُ عَلَىٰ هُونٍ أَمْرًا يُدْسُهُ فِي  
 التُّرَابِ ۗ أَلَا سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ ﴿٥٩﴾

*Na mmoja wao anapopewa habari ya (kuzaliwa) mtoto wa kike, husawajika uso wake, akajaa sikitiko (akawa) anajificha na watu kwa sababu ya habar mbaya ile aliyoaambiwa (anafanya shauri) Je, akae naye juu ya fedheha hiyo au amfukie udongoni (akiwa hai). Sikilizeni! Ni mbaya mno hukumu yao hiyo. (16:58-59).*

Wanawake baada ya kufiwa na waume zao, walirithiwa na wanawe wa kambo au shemeji zao. Walikuwa hawaruhusiwi kuolewa tena. Qur'an inakataza tabia hii kama ifuatavyo:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَحِلُّ لَكُمْ أَنْ تَرِثُوا النِّسَاءَ كَرْهًا وَلَا تَعْضُلُوهُنَّ  
 لِتَذْهَبُوا بِبَعْضِ مَآءِ تَيْتُمُوهُنَّ ..... ﴿١٩﴾

*Enyi mlioamini! Si halali kwenu kurithi wanawake kwa jeuri. Wala msiwazuie (kuolewa na wanaume wengine) ili mpate kuwanyang'anya baadhi ya vile mlivyo wapa...(4:19).*

### 3. Jamii za Kiafrika

Katika bara la Afrika pamoja na kuwa na jamii nyingi zenye mila na desturi zinazotofautiana hatupati hata jamii moja ya kitwaghati iliyompa mwanamke sauti katika nyumba wala katika jamii. Matatizo au makosa yote yaliyofanyika nyumbani yalisukumizwa kwa mwanamke.

Mwanamke alifanyishwa kazi na kubebeshwa mizigo kama punda. Mwanamke hakuwa na haki ya kumiliki mali aliyochuma mwenyewe. Kutokana na mahari yaliyolipwa wakati wa kuolewa mwanamke alifanywa mali ya mumewe ambaye aliweza kumfanya lolote alitakalo kama anavyofanyiwa mtumwa. Pia katika jamii nyingi za Kiafrika, si tu kwamba mwanamke hakuwa na haki ya urithi bali yeye mwenyewe alirithiwa kwa nguvu na mmoja wa shemeji zake. Akili ya mwanamke katika jamii nyingi imelinganishwa na ile ya mtoto mdogo. Kwa sababu hii mwanamke hakutakiwa ushauri kwa jambo lolote lile katika familia. Mara nyingi ushauri wa mtoto wa kiume ulithaminiwa kuliko ule wa mama yake. Kwa ujumla katika jamii nyingi za Kiafrika mwanamke alidunishwa

kwa kiasi kikubwa. Pamoja na kazi kubwa ya uzazi na malezi ya watoto, mwanamke aliachiwa majukumu yote ya nyumbani na alikuwa mshiriki mkuu katika shughuli za uchumi ambapo mali aliyoichuma kwa jasho lake ilichukuliwa na mwanamume bila hata kushauriwa. Hivi ndivyo alivyo nyanyaswa na kudunishwa mwanamke katika jamii mbali mbali za ulimwengu katika nyakati mbali mbali za historia. Je hivi leo zimechukuliwa hatua gani ili kukomesha uonevu huu dhidi ya mwanamke?

Katika miaka hii pamekuwa na vuguvugu la kumkomboa mwanamke ili kumrudishia haki zake na hadhi yake iliyodhulumiwa na wanaume. Vyama vingi vya kisiasa vimelipa suala hili kipa umbele na vimeundwa vyama vya wanawake vya Kitaifa na Kimataifa vinavyojishughulisha tu na kumkomboa mwanamke. Je, vyama hivi vimeleta mafanikio yoyote? Ukichunguza mbinu zinazotumiwa na vyama hivi katika ukombozi huu wa mwanamke, utakuta hazina tofauti kabisa na zile zilizotumiwa na Ulaya na Marekani katika kipindi cha mapinduzi ya viwanda za kumtaka mwanamke.

- (a) Awe sawa na mwanamume kwa kila kitu bila ya kuzingatia tofauti za kimaumbile na nafasi ya mwanamke na mwanamume katika jamii.
- (b) Ashiriki sawa na mwanamume katika uchumi na siasa na kumfanya ajitegemee kiuchumi.
- (c) Awe huru kutoka nyumbani kwake na kuchanganyika na wanaume apendavyo.

Tuliona kuwa, matokeo ya kumtetea mwanamke kwa mtazamo huu haikuwa kumkomboa bali kumdhaliilisha zaidi na kumvua haya na utu wake. Pia ukombozi wa mwanamke kwa mtazamo huu haukuleta nafuu yoyote katika jamii bali umezidi kuidumaza na kuigharimu kiasi kikubwa. Kampeni hii ya ukombozi wa mwanamke imechangia sana katika kuvunja maisha ya familia na kueneza magonjwa ya zinaa na kuongeza idadi ya wavuta bangi, wazururaji na majambazi kaitika jamii. Ni nani hasa aliyekombozi wa mwanamke? Bila shaka ni yule aliyemuumba na kumleta hapaduniani kama mwenza wa mwanamume.

Hivyo haki na hadhi ya mwanamke itapatikana kwa kumuamini Allah(s.w) na kufuata muongozo wa maisha aliouweka katika kukiendea kila kipengele cha maisha ya binafsi, familia.

## **Hadhi na Haki za Mwanamke katika Jamii ya Kiislamu.**

Maadui wa Uislamu na watu wasio ufahamu Uislamu vizuri, wameuangalia Uislamu kama wanavyoziangalia jamii nyinginezo na kushutumu Sheria za Kiislamu kuwa nazo zinamkandamiza mwanamke. Kutokana na shutuma hizi imekuwa ni wajibu kwetu katika sehemu hii kuonesha kwa uwazi jinsi

Uislamu unavyompa mwanamke **hadhi** na **haki** zake. Tumeshona kuwa wale wote waliojipiga kifua kuwa wanamtetea mwanamke na kumpa hadhi yake anayostahiki, harakati zao ziliishia ukutani. Walivunja familia ambayo ndio msingi wa jamii na walizidi kumdhaliisha mwanamke mpaka kufikia uduni kuliko ule wa hayawani.

Bila shaka watetezi hawa wa haki na hadhi ya mwanamke hawakuwa na nia mbaya ya kuzidi kumdunisha na kumkandamiza bali kosa lao kubwa ni kule kujiingiza kwao kwenye kazi wasio na ujuzi nayo. Allah(s.w) ndiye aliyemuumba mwanadamu na vyote vilivyomzunguka. Hivyo ni Allah(s.w) pekee mwenye haki na uwezo wa kumuwekea mwanadamu muongozo wa maisha mwenye kumuelekeza namna ya kukiendea kila kipengele cha maisha yake ya binafsi, familia, uchumi, siasa, utamaduni na maisha yote ya kijamii kwa ujumla ili aweze kuishi kwa furaha na amani na hapo hapo afikie lengo la kuumbwa kwake. Ni dhahiri kwamba watu wanaokana au wasiotambua kuwepo kwa Allah(s.w) na mwongozo wake, ambao hujiundia sheria za kuiongoza na kuilinda jamii kutokana na msukumo wa matashi yao, kamwe hawawezi kuweka utaratibu utakao mhakikishia kila mtu katika jamii kupata haki zake zote na kuishi kwa furaha na amani. Hivyo wale wote wasiofuata mwongozo wa Allah(s.w),wasitegemee kamwe kupata haki zao na kuishi kwa furaha na amani katika jamii zao.

Tofauti na sheria za jamii zinazotungwa na binadamu baada ya haja kutokea, sheria za Kiislamu kwa kuwa zimewekwa na Allah(s.w), Mjuzi Mwenye Hekima, haziko pale kutosheleza haja ya dharura, bali zimekuwa pale hata kabla ya Adam(a.s) kuja hapa ulimwenguni. Hivyo ni vyema ifahamike tangu mwanzo kuwa katika mjadala wetu huu utaratibu au sheria ya Kiislamu ambayo inamhakikishia mwanamke kupata haki na hadhi yake, haikutungwa baada ya kuona kuwa mwanamke anakandamizwa na kupuuzwa, bali ilikuwepo sheria hiyo hata kabla ya kuumbwa Adam na Hawa. Allah(s.w) anamfahamu vyema mwanadamu kuwa endapo hatapewa mwongozo kutoka kwake na kuufuata ni muhali kuepokana na maisha hayo ya kudhulumiana na hasa wenye nguvu kuwadhulumu wanyonge.

Ili kutofautisha hatua za kumkomboa mwanamke zilizochukuliwa na jamii zilizojitahidi kufanya hivyo na hatua zinazochukuliwa na sheria ya Kiislamu, hapa tutajihusisha na vipengele vitatu:

## **Mtizamo wa Uislamu Juu ya Usawa kati ya Mwanamume na Mwanamke.**

- Haki za mwanamke katika Uislamu.
- Hifadhi ya mwanamke na maadili ya Jamii.
- Mtizamo wa Uislamu juu ya Usawa kati ya Mwanamke na Mwanamume.

Usawa kati ya mwanamume na mwanamke katika Uislamu umetokana na suala la lengo la maisha ya mwanadamu hapa duniani na namna ya kulifikia. Tumeona kuwa madai ya usawa kati ya mwanamume na mwanamke katika nchi za Ulaya, Marekani na katika nchi za Kikomunisti, yametokana na hali halisi ya mazingira yao. Katika nchi za Ulaya na marekani madai ya usawa kati ya wanawake na wanaume ni zao la hali ngumu ya maisha wakati wa maendeleo ya viwanda. Na katika nchi za Kikomunisti, hasa Urusi, madai ya usawa msingi wake ni kutoa “Bakshishi” kwa wanawake baada ya kushiriki kwao kwa kiasi kikubwa katika kufanikisha mapinduzi ya Urusi ya Oktoba, 1917 (The Great October Russian Revolution). Katika Uislamu sheria ya usawa kati ya mwanamume na mwanamke sio zao la hali yoyote ya mazingira bali imezingatia suala zima la lengo la kuumbwa mwanadamu na nafasi yake hapa duniani. Ni katika utaratibu wa Allah(s.w) ili kuyawezesha maisha ya viumbe yaendeleo na kufikia lengo lililokusudiwa ameumba vitu viwili viwili ambavyo kimoja hakijitoshelezi mpaka mwenziwe awepo kama vile usiku na mchana, utamu na uchungu, uhai na umauti, chanya na hasi, kike na kiume, n.k. Ni pale tu jozi hizi za vitu viwili zitakapo shikamana ndipo kitakapotokea kitu kamili. Allah(s.w) anatumfahamisha hili kaitika Qur’an:

وَمِنْ كُلِّ شَيْءٍ خَلَقْنَا زَوْجَيْنِ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٥١﴾

*Na hakika katika kila kitu tumekiumba dume na jike ili mpate kufahamu (51:49).*

Kwa hiyo mwanamke kuwa kama alivyo si ishara ya udhaifu wala mwanamume kuumbwa kama alivyo si ishara ya ukamilifu. mume na na mke hawababudi kuishi maisha ya kusaidiana ili kufanya kitu kimoja kizima ili maisha yawezekane na yafikie lengo lake. Kiasili wanaume na wanawake wako sawa katika maeneo yafuatayo:

### 1. Asili yao ni Moja

Tunafahamishwa katika Qur’an kuwa usawa kati ya mwanamume na mwanamke umekuwepo tangu mwanzo wa kuumbwa kwake:

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ آتِفُوا رَبُّكُمْ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَاءً ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي تَسَاءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيبًا ﴿٥١﴾

*Enyi watu! Mcheni Mola wenu ambaye amekuumbeni katika nafsi moja na akamuumba mkewe katika nafsi ileile. Na akaeneza wanaume wengi na*

wanawake kutoka katika wawili hao. Na Mcheni Mwenyezi Mungu ambaye kwaye mnaombana (mnategemeana). Na (muwatazame) jamaa. Hakika Mwenyezi Mungu ni mlinzi juu yenu (anayeyaona kila mnayoyafanya). (4:1).

Katika aya hii tunafahamishwa kwa uwazi kuwa mwanadamu asili yake ni moja na tunasisitizwa kufanyiana wema baina yetu, jambo ambalo iwapo hatutalifanya, Mwenyezi Mungu(s.w) atatuadhibu vikali.

Tofauti za kimaumbile, tofauti za kijinsia, tofauti za mazingira na wakati na tofauti nyingine kama hizi, sizo zinazomfanya mwanadamu mmoja awe bora kuliko mwingine, au kumfanya mwanamume awe bora kuliko mwanamke, bali aliye bora zaidi ya wengine ni yule amchaye Mwenyezi Mungu zaidi ya wengine. Tunajifunza hili katika aya ifuatayo:

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُمْ مِنْ ذَكَرٍ وَأُنْثَىٰ وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا وَقَبَائِلَ  
لِتَعَارَفُوا ۗ إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتْقَىٰكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿١٣﴾

Enyi watu! Kwa hakika tumekuumbeni (nyote) kwa (yule) mwanamume (mmoja, Adam) na (yule yule) mwanamke (mmoja Hawa). Na tumekufanyeni mataifa na makabila (mbali mbali) ili mjuane. Hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu ni yule amchaye Mwenyezi Mungu zaidi katika nyinyi. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mjuzi mwenye khabari (zote). (49:13).

## 2. Lengo la Kuumbwa Kwao ni Moja

Jambo lingine linalosisitiza usawa kati ya mwanamke na mwanamume ni usawa wa lengo la kuumbwa mwanadamu. Lengo la maisha ya mwanadamu hapa ulimwenguni linadhihirishwa katika Qur'an:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾

“Sikuwaumba majini na watu ila waniabudu”. (51:56)

Kumuabudu Allah(s.w) ni kuishi maisha yote kwa kufuata hukumu Zake(s.w) katika kuendesha maisha ya kila siku katika nyanja zote za maisha. Katika aya mbali mbali za Qur'an tunafahamishwa kuwa wanaume na wanawake watalipwa sawa sawa kulingana na amali zao bila ya kujali jinsi yao. Hebu turejee aya zifuatazo:

فَأَسْتَجَابَ لَهُمْ رَبُّهُمْ أَنِّي لَا أُضِيعُ عَمَلَ عَمَلٍ مِّنْكُمْ مِنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْثَىٰ  
بَعْضُكُمْ مِنْ بَعْضٍ ۗ

*Mola wao akawakubalia (maombi yao kwa kusema): “Hakika mimi sitapoteza juhudi ya mfanya juhudi miongoni mwenu akiwa mwanamume au mwanamke, kwani nyinyi ni nyinyi kwa nyinyi....” (3:195).*

وَمَنْ يَعْمَلْ مِنَ الصَّالِحَاتِ مِنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْثَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَأُولَٰئِكَ  
يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ وَلَا يُظْلَمُونَ نَقِيرًا ﴿١٩٥﴾

*Na watakaofanya vitendo vizuri, wakiwa wanaume au wanawake, hali wao ni wenye kuamini, basi hao wataingia peponi wala hawatadhulumuwa hata tundu ya kokwa ya tende. (4:124).*

وَعَدَّ اللَّهُ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ  
خَالِدِينَ فِيهَا وَمَسْكَنٌ طَيِّبٌ فِي جَنَّاتِ عَدْنٍ ۚ وَرِضْوَانٌ مِّنَ اللَّهِ  
أَكْبَرُ ۚ ذَٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١٩٦﴾

*Mwenyezi Mungu amewaahidi wanaoamini wanaume na wanaoamini wanawake (Amewaahidi) mabustani yapitayo mito mbele yake wakae humo daima na makazi mazuri kwenye mabustani hayo yenye kudumu. Na radhi za Mwenyezi Mungu ndizo kubwa zaidi. Huko ndiko kufuzu (kufaulu) kukubwa (9:72).*

### 3. Wote wamekusudiwa kuwa Makhalifa wa Allah(s.w) katika jamii

Jambo lingine linalodhihirisha usawa kati ya wanaume na wanawake katika Uislamu ni hadhi ya mwanadamu hapa ulimwenguni.

Mwanadamu ameletwa hapa ulimwenguni ili awe Khalifa wa Allah(s.w) katika ardhi hii kama tunavyojifunza katika Qur'an:

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلٰٓئِكَةِ اِنِّيْ جَاعِلٌ فِى الْاَرْضِ خَلِيْفَةً ۗ قَالُوْۤا اَتَجْعَلُ  
فِيْهَا مَن يُفْسِدُ فِيْهَا وَيَسْفِكُ الدِّمَآءَ وَنَحْنُ نُسَبِّحُ بِحَمْدِكَ وَنُقَدِّسُ لَكَ  
ۗ قَالَ اِنِّيْۤ اَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُوْنَ ﴿٢٠﴾

*Wakati Mola wako alipowaambia Malaika: “Mimi nitaleta katika ardhi Khalifa(wangu).” Wakasema: Utaweka humo watakaofanya uharibifu humo na kumwaga damu, hali sisi tunakutukuza kwa sifa na kukutaja kwa utukufu wako? Akasema (Mwenyezi Mungu): “hakika mimi najua msiyoyajua”. (2:30).*

Katika aya hii tunajifunza kuwa mwanadamu amekusudiwa kuwa Khalifa wa Allah(s.w) hapa ulimwenguni. Kuwa Khalifa wa Allah(s.w) ni kuwa kiongozi kwa niaba ya Allah(s.w) hapa ulimwenguni. Yaani kuutawala ulimwengu kwa kufuata mwongozo na sheria za Allah(s.w).

Pia tunajifunza kuwa cheo cha Ukhalifa ni cheo chenye hadhi kubwa sana kiasi kwamba malaika walimuonea wivu mwanadamu na kupendekeza kuwa wao ndio stahiki kupata cheo hicho.

Katika aya hii hatuoni ubaguzi wowote kati ya mwanamume na mwanamke bali tunafahamishwa kuwa watakapo chukua cheo hiki ni wanaume na wanawake watakapo muamini na kumtii Allah(s.w) ipasavyo:

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ  
 كَمَا أَسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ  
 وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا..... ﴿٥٥﴾

*Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mweni na kufanya vitendo vizuri, kuwa atawafanya makhalifa (watawala) katika ardhi kama alivyowafanya Makhhalifa wale waliokuweco kabla yao, na kwa yakini Atawasimamishia dini yao, Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wawe wananiabudu, hawanishirikishi na chochote .....” (24:55).*

Hivyo ukhalifa ni kwa wote wanawake na wanaume. Kila mmoja anao wajibu wa kusimamisha ufalme wa Allah(s.w) hapa ulimwenguni kwa kila mmoja kutekeleza jukumu lake alilopangiwa katika jamii kulingana na umbile, uwezo, vipawa, bahati na fursa alizotunukiwa.

#### **4. Hakuna Dhambi ya Asili**

Suala la dhambi ya asili anayonasibishiwa nayo mwanamke kama tulivyoona katika maandiko ya Wakristo, halipo kabisa katika Uislamu. Katika maandiko hayo, Hawa ndiye pekee aliyeonekana mkosaji katika kuvunja amri ya Mwenyezi Mungu ya kula tunda kutoka kwenye ule mti ulioharamishwa. Katika Qur'an tunajifunza kuwa wote walikuwa wakosaji mbele ya Allah(s.w) na wote walitubia na kusamehewa.

وَقُلْنَا يَا آدَامُ اسْكُنْ أَنْتَ وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ وَكُلَا مِنْهَا رَغَدًا حَيْثُ شِئْتُمَا  
وَلَا تَقْرَبَا هَذِهِ الشَّجَرَةَ فَتَكُونَا مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٢٥﴾ فَأَزَلَّهُمَا الشَّيْطَانُ  
عَنْهَا فَأَخْرَجَهُمَا مِمَّا كَانَا فِيهِ ..... ﴿٢٦﴾

*Na tukasema: Ewe adam! Kaa wewe na mkeo katika bustani hii na kuleni humo maridhawa popote mpendapo lakini msikurubie mti huu tu, msije kuwa miongoni mwa waliोधहulumu. (lakini) shetani (yule Iblis adui yao) aliwatelezesha wote wawili wakakhalifu amri ile, wakala katika mti huo walio katazwa na akawatoa katika ile (hali) waliyokuwa nayo... ” (2:35-36).*

وَيَعَادِمُ اسْكُنْ أَنْتَ وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ فَكُلَا مِنْ حَيْثُ شِئْتُمَا وَلَا تَقْرَبَا  
هَذِهِ الشَّجَرَةَ فَتَكُونَا مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٢٥﴾ فَوَسْوَسَ لَهُمَا الشَّيْطَانُ  
لِيُبْدِيَ لَهُمَا مَا وُورَىٰ عَنْهُمَا مِنْ سَوَاءٍ تَهُمَا وَقَالَ مَا نَهَاكُمَا رَبُّكُمَا  
عَنْ هَذِهِ الشَّجَرَةِ إِلَّا أَنْ تَكُونَا مَلَكَيْنِ أَوْ تَكُونَا مِنَ الْخَالِدِينَ ﴿٢٦﴾  
وَقَاسَمَهُمَا إِنِّي لَكُمَا لَمِنَ النَّصِيحِينَ ﴿٢٧﴾

*(Kisha Allah(s.w) akasema): Na wewe Adam kaa peponi pamoja na mkeo na kuleni mnapopenda lakini msikurubie mti huu msije kuwa miongoni mwa waliोधहulumu (nafsi zao). Basi shetani aliwatia wasi wasi ili kuwadhihirishia aibu zao walizofichiwa na akasema: “Mola wenu hakukukatazeni mti huu ila (kwa sababu hii): msije kuwa malaika au kuwa miongoni mwa wakaao milele (wasife). Naye akawaapia: Kwa yakini mimi ni mmoja wa watoa ushauri mwema kwenu. (7:19 -21)*

فَدَلَّيَهُمَا بِغُرُورٍ ۗ فَلَمَّا ذَاقَا الشَّجَرَةَ بَدَتَا لَهُمَا سَوَاءَهُمَا وَطَفِقَا  
مَخَصِفَانِ عَلَيْهِمَا مِنْ وَرَقِ الْجَنَّةِ ۗ وَنَادَاهُمَا رَبُّهُمَا أَلَمْ أَنْهَكُمَا عَنْ تِلْكَمَا  
الشَّجَرَةِ وَأَقُلْتُ لَكُمَا إِنَّ الشَّيْطَانَ لَكُمَا عَدُوٌّ مُبِينٌ ﴿٢٧﴾ قَالَا رَبَّنَا  
ظَلَمْنَا أَنْفُسَنَا وَإِن لَّمْ تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٢٨﴾



*Basi akawateka (wote wawili) kwa hadaa yake. Na walipouonja mti ule, aibu zao ziliwadhihirikia na wakaingia kujibambikiza majani ya peponi. Na Mola wao akawaita (na kuwauliza): Je, sikukukatazeni mti huu na kukwambieni ya kwamba shetani ni adui yenu aliye dhahiri? Wakasema:*

..... رَبَّنَا ظَلَمْنَا أَنفُسَنَا وَإِن لَّمْ تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ

الْخٰسِرِيْنَ ﴿٢٣﴾

*“Mola wetu! Tumedhulumu nafsi zetu, na kama hutatusamehe na kuturehemu, bila shaka tutakuwa miongoni mwa wenye khasara (7:23).*

Kutokana na aya hizi wote wawili, Adam na Hawa, walikosa na wote walitubia na kusamehewa. Hivyo hapana tena dhambi ya Asili. Hata kama Adam na Hawa wasingali samehewa haingelikuwa dhambi hii iendeleo kwa watoto wao na kizazi chote cha binadamu kwani Allah(s.w) si mwenye kuonea waja wake na ni katika utaratibu wake kuwa hambebeshi mtu mzigo usio muhusu.

..... وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ۗ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُم مَّرْجِعُكُمْ ..... ﴿١٦٤﴾

*“... Wala mbebaji (mizigo yake ya dhambi) hatabeba mizigo ya mwingine. Kisha marejeo yenu (nyote) ni kwa Mola wenu...” (6:164).*

Wala isichukuliwe kuwa Adam na Hawa kutolewa Peponi na kuletwa hapa ulimwenguni kuwa ni adhabu kwani ilibainishwa tangu mwanzo kabla ya kuumbwa kwao, kuwa wao ni Makhaliifa wa Allah(s.w) hapa ulimwenguni.

Pamoja na kuona msimamo wa Sharia ya Kiislamu juu ya usawa kati ya mwanamume na mwanamke, hatuna budi kutafakari “usawa” huu kwa undani zaidi. Hatuna budi kufahamu kuwa kuna “usawa” wa sheria na usawa wa maumbile. Uislamu unasimamisha usawa wa sheria.

Binadamu wanaweza kuwa sawa kisheria lakini ni jambo lisilowezekana kupata usawa wa maumbile, vipaji, uwezo, bahati, fursa, n.k. kati ya wanadamu. Ukweli ni kwamba hakuna watu wawili, hata kama ni mapacha (identical twins), walio sawa moja kwa moja. Wanadamu wanatofautiana sana katika wajihi, akili, uwezo, vipaji, majukumu, na kadhalika. Hizi ni tofauti za kimaumbile anazozaliwa nazo mwanadamu.

Tofauti hizi za kimaumbile sizo zinazoleta tofauti za hadhi na haki miongoni mwa watu bali kinachofanya watu watofautiane katika kupata hadhi na haki wanazostahiki ni sheria, mila na desturi za jamii. Ni wajibu wa jamii kuondoa sheria, mila na desturi zinazoondoa usawa miongoni mwa watu katika jamii na kubakisha tu zile sheria, mila na desturi ambazo humpa kila mtu hadhi na haki

zake na kumwezesha kutoa kwa ukamilifu mchango wake katika kuistawisha na kuiendeleza jamii. Uislamu unapinga vikali ule usawa unaopigiwa zumari na matwaghuti wa kumtoa mwanamke awe sawa na mwanamume kimaumbile kivipawa na kimajukumu na kumfanya mke asiwe mwenza wa mume bali kila mmoja ajitegemee kimaisha na kuwa mshindani wa mwenzake katika uchumi, siasa, n.k. hatima ya usawa wa aina hii, kama tulivyoona katika nchi ya Ulaya na Marekani, ni kuua taasisi ya familia, kuivuruga jamii na kumdhalilisha mwanamke kwa kiasi kikubwa. Uislamu unasisitiza sana usawa kati ya mke na mume na kati ya binadamu wote kwa ujumla lakini pamoja na kuzingatia tofauti za kimaumbile, kivipawa na kimajukumu zilizopo. Kutokana na tofauti hizi za kimaumbile utamkuta mwanamke ana uwezo zaidi wa kutekeleza majukumu fulani ambayo ni muhimu kwa maisha ya mwanadamu katika jamii. Hivyo hivyo, utamkuta mwanamume anafursa na uwezo wa kutekeleza majukumu mengine zaidi kuliko mwanamke. Kuna baadhi ya majukumu anayoweza mwanamke peke yake na mwanamume hana uwezo nayo. Kwa mfano, kubeba mimba, kuzaa mtoto na kumlea mpaka afikie umri wa miaka miwili, ni jukumu analolibeba mwanamke peke yake.

Je, katika kutekeleza jukumu hili, mwanamke huyu atakuwa na uwezo mkubwa tena wa kushiriki kwa ukamilifu katika uchumi, siasa, na katika shughuli nyinginezo muhimu za jamii? Ikumbukwe kuwa jukumu hili moja la kuzaa na kulea mtoto ni kubwa sana linalochukua muda mrefu, miezi 30 kama Allah(s.w) anavyotufahamisha katika aya ifuatayo:

وَوَصَّيْنَا الْإِنْسَانَ بِوَالِدَيْهِ إِحْسَانًا ط حَمَلَتْهُ أُمُّهُ كُرْهًا وَوَضَعَتْهُ كُرْهًا  
 وَحَمَلُهُ وَفَصَّلُهِ ثَلَاثُونَ شَهْرًا ..... ﴿١٥﴾

*Na tumemuusia mwanaadam afanye wema kwa wazazi wake. Mama yake amechukua mimba yake kwa taabu na akamzaa kwa taabu. Na kubeba mimba yake hata kumwachisha ziwa (kwa uchache) ni miezi thelathini ..... (46: 15).*

Katika muda huu wote sehemu kubwa ya akili na fikra ya mama huyu imeelekezwa katika jukumu hili kwa kiasi kwamba humfanya asiwe na umakini katika shughuli nyingine yoyote ile. Je, kama tutadharau ukweli huu tukaendelea kudai kuwa wanawake na wanaume wako sawa katika kutekeleza majukumu mengine yote ya msingi ya jamii, kama vile uchumi, uongozi n.k. huoni kuwa mwanamke anakandamizwa kwa kuvishwa majukumu mengi na mazito kuliko mwanamume?

Kumdanganya mwanamke kuwa kuacha kazi ya kulea watoto nyumbani na kwenda shambani, ofisini au kiwandani ndio kujikomboa kwake na kuwa sawa na wanaume ni:-

**Kwanza**, kumlaghai na kumnyonya. Chukua mfano wa mume na mke wanaofanya kazi ofisini. Mke asubuhi, wakati mumewe anaendelea kulala, ataamka mapema kuhakikisha kuwa ataondoka nyumbani akiwa ameiacha nyumba katika hali nzuri. Kisha baada ya mumewe kuamka atamhudumia ili wawe tayari kuondoka. Baada ya kazi wote hurudi nyumbani pamoja lakini wakati baba anapumzika, mke hujishughulisha na kufahamu watoto walivyolishwa, walivyofuliwa, walivyokogeshwa na husikiliza shida zao nyingine mbali mbali. Huhakikisha watoto na watu wote nyumbani wanakula na kulala. ndio naye alale. Je, huu si utumwa wa hiari kwa mwanamke huyu? Je, huoni wanamke wa namna hii hufanya kazi maradufu ya ile ya wanaume - kazi ya ofisini na kazi ya malezi? ,Je, kama mama naye, kwa kudai usawa, ataamua abakie na kazi ya ofisini tu, familia yenye mshikamano na utulivu itapatikana? Je, ni nani anayempa mwanamke haki zake na kutetea usawa, huyu anayemng'ang'aniza aende ofisini au Uislamu unaompunguzia mwanamke majukumu ya kuhemea na. kumbakishia majukumu ya kuzaa na kulea watoto, kutunza mali ya mumewe, kumliwaza na kumfariji arudipo kazini?

**Pili**, kumpachika mwanamke majukumu mengine zaidi ya lile la kuilea familia ni kumpunguzia ufanisi na kuidodesha jamii. Mwanamke mwenye mimba na watoto wa kulea nyumbani, akiwa mwanadamu wa kawaida, unadhani ataweza kufanya kazi yake ofisini kwa ufanisi?

Atafanyaje kazi vizuri na ili hali ni mgonjwa kwa kipindi chote cha ujauzito? Kama ataiweka familia yake vizuri ni wazi kuwa kazi za ofisini zitadorora. Na atakapo jifungua itambidi achukue likizo ya uzazi ya miezi mitatu. Hata baada ya miezi mitatu ya likizo, fikra zake zitakuwa kwa mtoto wake mpaka angalau miaka miwili itimie. Tuseme mathalan, wanawake 1000 walioshika nafasi muhimu katika uchumi na uongozi wa jamii wawe wamechukua likizo ya uzazi miezi mitatu, muda huu wote nani atakaye fanya kazi zao?

**Tatu**, kudharau kazi ya malezi ya familia. Malezi ya familia ni kazi muhimu sana kwa jamii inayotaka maendeleo ya vitu na maadili. Kuikuza na kuilea familia katika maadili ni kazi muhimu inayotaka ifanyike kwa uanga 1ifu na kwa upendo na huruma za mzazi. Hakuna mtaalam yoyote anayeweza kuifanya kazi hii vizuri isipokuwa mama watoto mwenyewe. Ni katika msingi huu Sheria ya Kiislam imemuondolea mwanamke majukumu yote ya nje ya nyumba yake na kumbakishia jukumu la uzazi, ulezi na utunzaji wa nyumba na mali ya mumewe. Allah(s.w)amesema:

*Mwanamke ni Malikia wa nyumba ya mume wake na atakuwa. masuuli juu ya wajibu wake huu (Bukhaary).*

Kwa ajili ya umuhimu wake kuwepo nyumbani saa zote, mwanamke amesamehewa lbada zote zinazofanywa nje ya nyumba. Kwa mfano si lazima kwake kuswali swala ya Ijmaa na amesamehewa kwenda msikitini kwa swala

za jamaa japo ameruhusiwa kwenda akitaka. Vile vile si faradhi kwa mwanamke kwenda Jihad japo hawakatazwi kwenda hasa pale msaada wao utakapo hitajika. Kwa ujumla Uislamu haumtaki mwanamke kutoka toka nyumbani kwake ila kwa haja maalumu. Amri ya wanawake kubakia katika majumba yao inadhihirika katika aya ifuatayo:

وَقَرْنَ فِي بُيُوتِكُنَّ وَلَا تَبَرَّجْنَ تَبَرُّجَ الْجَاهِلِيَّةِ الْأُولَىٰ ..... ﴿٣٣﴾

*Na kaeni majumbani mwenu, wala msionyeshe mapambo yenu kama walivyokuwa wakionyesha mapambo yao wanawake wa zama za ujahili ... (33:33).*

Pamoja na amri hii wanawake wameruhusiwa kwa haja maalumu kutoka nje ya nyumba zao. Kwa mfano mwanamke asiye na yeyote wa kumtegemea kiuchumi itabidi atoke kutafuta mahitaji ya maisha. Au wakati mwingine mwanamke analazimika kutoka kufanya kazi ili kuongeza kipato cha mumewe kutokana na umasikini, ugonjwa au jambo lingine lolote linalomzuia kukidhi mahitaji ya familia. Kwa hali hii Uislam uumetoa ruhusa ya mwanamke kufanya kazi nje ya nyumba yake Allah(s.w) amesema:

*Allah amewaruhusu(wanawake) kutoka nje ya majumba yenu kwa haja maalum (Bukhaary).*

Kumbakisha mwanamke nyumbani kwake si kumnyima uhuru bali ni kumpa uhuru na wasaa wa kutekeleza majukumu yake vizuri zaidi ili aweze kuilea familia kwa utulivu na kwa ufanisi. Kwa upande mwingine mwanamume kupewa jukumu la kuiongoza familia na kukidhi mahitaji yake muhimu, siyo sababu ya kujifanya bora zaidi kuliko mkewe, bali amepewa jukumu hilo kulingana na umbile lake, vipawa na nafasi aliyonayo ambayo humruhusu kutekeleza majukumu hayo. Vile vile hapana upendeleo wowote, uliofanyika katika kumpa mwanamke na mwanamume majukumu hayo. Wote wanatakiwa washirikiane kwa upendo na huruma katika kutekeleza majukumu ya familia na jamii kwa ujumla.

## Haki za Mwanamke katika Uislamu

Katika kuhakikisha kuwa mwanamke anapata haki zake Uislamu umesisitiza mambo ya msingi yafuatayo:

**Kwanza**, Uislamu umeweka wazi kuwa uongozi aliopewa mwanamume juu ya familia yake asije akautumia vibaya na akawageuza watu wa familia yake kuwa “Watumwa” naye akawa “Bwana”. Bali anatarajiwa kuiongoza familia na kufikia lengo tarajiwa.

**Pili**, Uislamu umesisitiza kuwa wanawake wapewe fursa zote zitakazo wawezesha kuendeleza vipawa vyao katika kiwango cha juu ili kuinua na kuiendeleza jamii, ila tu mipaka ya Uislamu ichungwe.

**Tatu**, Uislamu unasisitiza kumuendeleza mwanamke kiwango cha hali ya juu na kumbakisha katika hadhi ya mwanamke. Kuwa mwanamume au kumtayarisha kwa majukumu ya wanaume si katika haki zake wala si jambo litakalo mletea maendeleo yeye binafsi na jamii nzima kwa ujumla.

Kwa kuzingatia vipengele hivi vya msingi Uislamu unampa mwanamke haki katika nyanja zote za kijamii kama ifuatavyo:

## **Haki za Uchumi**

Kuwa imara kiuchumi ni sababu mojawapo kubwa ya kumpa mtu hadhi katika jamii. Kama tulivyoona jamii nyingi za kale, zilimnyima mwanamke haki ya kiuchumi na kumfanya kama mtumwa katika jamii.

Wanawake walifanya kazi sana lakini hawakuwa na haki ya kumiliki kile walichokichuma, chochote walichokuwa nacho kilikuwa ni mali ya waume zao, hawakuwa na haki ya urithi bali wenyewe walirithi wa mume zao walipofariki. Kama tulivyoona wakati wa maendeleo ya viwanda, nchi za Ulaya zilichukua jukumu la kumkomboa mwanamke kwa kumuingiza kazini ili naye ainuke kiuchumi. Ukombozi huu wa kumfanya mwanamke afanye kazi viwandani sawa na wanaume haukuwa ukombozi kitu kwani yalizuka matatizo mengine yaliyozidi kumdunisha mwanamke na kuidhoofisha jamii kimaadili.

## **Ni Uislamu Pekee Umemuinua Mwanamke Kiuchumi na Maadili.**

Katika Sheria ya Kiislamu, mwanamke anayo haki ya kupata mahitaji yake yote ya maisha chakula, nguo, makazi, n.k. kutoka kwa mumewe. Ni haki yake kupewa mahari na mumewe kabla ya kuolewa na ni haki yake pekee kumiliki mali hiyo inayotokana na mahari bila ya kuingiliwa na baba yake, mlezi wake, mum ewe au yeyote yule. Vile vile mwanamke amepewa na sheria ya Kiislamu haki ya kuwarithi wazazi wake, mume wake, watoto wake na jamaa zake wengine wa karibu. Pia mwanamke amepewa uhuru kamili wa kuchuma na kumiliki alichokichuma. Ana uhuru kamili wa kuwa na hisa katika biashara au kampuni kwa jina lake mwenyewe.

Pamoja na uhuru huu aliopewa mwanamke wa kuchuma na kumiliki mwenyewe alichokichuma kwa mikono yake alimuradi tu anazingatia mipaka ya Allah(s.w) bado mumewe anawajibika kukidhi mahitajio yake yote muhimu ya maisha kama vile chakula, mavazi na makazi. Kwa hiyo hali ya kiuchurni kwa mwanamke imehifadhiwa na Sheria ya Kiislamu kwa kiasi kwamba mwanamke mara nyingi anakuwa tajiri kuliko mumewe. Hata hivyo mwanamke anao uhuru kamili wa kumfanyia mumewe ihsani kwa kummegea kile alichokichuma au kumpunguzia majukumu kwa kujitosheleza yeye mwenyewe kwa mahitaji yake

muhimu. Na wanaume nao wakifanyiwa ihasani na wake zao wapokee kwa furaha kama tunavyojifunza katika Qur'an:

..... فَإِنْ طِبَّنَ لَكُمْ عَنْ شَيْءٍ مِّنْهُ نَفْسًا فَكُلُوهُ هَنِيئًا مَّرِيئًا ﴿٤﴾

*(Wake zenu) wakikupeni kwa radhi ya nafsi zao kitu katika hayo (mali yao) basi kuleni kwa furaha na kunufaika (4:4).*

leleweke kuwa si tu wanawake wanaruhusiwa kuchuma kwa kujajiri tu wenyewe bali pia wanaweza kuajiriwa katika kazi yoyote ile inayoheshimu hadhi yake na kuchunga mipaka aliyoiweka Allah(s.w).

Bali katika jamii ya Kiislamu baadhi ya wanawake wanalazimika waajiriwe kufanya kazi mahsus. Kwa mfano katika Sheria ya Kiislamu ni vizuri mgonjwa wa kike kuchunguzwa matatizo yake ya siri na daktari mwanamke. Vile vile mgonjwa mwanamke ni vyema auguzwe na muuguzi (Nurse) mwanamke. Ni vizuri zaidi pia watoto au wanafunzi wa kike kufundishwa na walimu wa kike. Hii ina maana kuwa linahitajika kundi kubwa la wanawake watakaofanya kazi hizi. Kwa mujibu wa Sheria ya Kiislamu wanawake pia wanayo haki ya kupata malipo sawa na wanaume kulingana na sifa.

Pamoja na mwanamke kupewa uhuru wa kushiriki katika harakati za uchumi, ikumbukwe kuwa jukumu kubwa na muhimu kwa mwanamke ni kuilea familia kiafya na kimaadili. Kuna baadhi ya watu ambao wanadai kuwa katika jamii ya leo maendeleo yatapatikana tu iwapo wanaume na wanawake watafanya kazi za kuajiriwa. Kwa hoja hii inadaiwa kuwa kuwataka wanawake kushughulikia malezi ya watoto wao ni kurudisha nyuma maendeleo ya kijamii. Madai haya hayana msingi. Kwanza hatulijui ni jukumu gani kubwa na bora zaidi kuliko lile la mama kuwa mlezi wa watoto wake. Swali la kujiuliza hapa ni je, tunayatafsiri vipi maendeleo ya jamii? Je, tunayatafsiri maendeleo kwa kiasi cha Dola (\$) na Shilingi kilichomo nchini? Au tunazungumzia pia maendeleo ya kiroho na kimaadili? Ni dhahiri kuwa kama tutapanua upeo wetu wa tafsiri ya maendeleo tutaona kuwa jamii itanufaika sana siyo tu kwa kuwa na barabara zenye lami na mabasi mengi bali pia iwapo raia katika jamii hiyo watakuwa wamelelewa katika kuthamini uadilifu kuliko hata mali. Vinginevyo mabasi hayo yatakuwa kama majeneza yanayoelekea kwenye maangamizi kutokana na kuvamiwa na majambazi vaporaji ambao hawasiti kuwaua binadamu wenzao kama kuku. Tukipanua upeo wetu tutaona kuwa malezi bora ya watoto yatolewayo kwa mapenzi na huruma na mama ni hazina kubwa kwa jamii yoyote ile. Na kwa nini hasa mwanamke akifanya kazi nje ya nyumba yake anahesabiwa anafanya kazi lakini akifanya kazi nyumbani mwake tangu alfajiri hadi usiku anahesabiwa hafanyi kazi? Tunaitafsiri vipi kazi? Je, kipimo ni kule kutoka nje ya nyumba au kufanya mbali na nyumbani? Na kwa nini katika jamii zetu za leo tunamhesabu mwanamke anayepika chakula hotelini kuwa

anafaya kazi lakini akiwapikia awapendao nyumbani mwake anahesabiwa hafanyi kazi? Kwa nini mwanamke akishona nguo au kufuma sweta katika kiwanda anahesabiwa anafanya kazi lakini akiwashonea wanawe nyumbani anahesabiwa anakaa bure hafanyi kazi? Kwa nini akilea watoto wa mwenzake katika vituo vya watoto anahesabiwa yuko kazini lakini akiwalea watoto wake hafanyi kazi? Kwa nini mwanamke akiwa Sekretari anayepanga na kuratibu kazi za boshi wake anahesabiwa kuwa anafanya kazi lakini akipanga na kuratibu shughuli nyumbani mwake anahesabiwa kuwa hafanyi kazi? Tatizo linalozikabili jamii nyingi hivi leo ni kudhani kuwa kuolewa na kulea watoto ni mambo ya kizamani, na kwa kuwa ni yakizamani basi ni mabaya na hayana faida yoyote. Lakini ukweli unabakia kuwa lau mume angalijaribu kuitathmini kazi anayoifanya mkewe katika mizani ya pesa na halafu akaamua kumlipa basi angalifilisika mara moja hata angalikuwa tajiri vipi. Mama kwa mfano, anaweza kujikuta halali usiku kucha kwa sababu ya kumuuguza mwanawe kwa huruma na mapenzi bila ya kusimamiwa na mtu na bila kutaraji malipo kwa mtu. Kazi hiyo yastahiki malipo kiasi gani?

Matokeo ya kupuuzia jukumu hili la mama kuwalea watoto wao wenyewe, ni kuwa baada ya muda fulani jamii itajikuta inakabiliwa na wimbi kubwa sana la wizi, ujambazi, uporaji na hata uuaji kama matunda ya kutowalea watoto ipasavyo au kwa kuwakabidhi watu ambao hawajali wala hawana habari juu ya makuzi ya kiroho na kimaadili ya mtoto.


## Haki za Kijamii

Pamoja na haki za kiuchumi, Uislamu unampa mwanamke haki za kijamii zifuatazo:

**Kwanza**, mwanamke amepewa uhuru kamili wa kuolewa na mwanamume ampendaye. Ndoa ya Kiislamu haisihi iwapo mwanamke atalazimishwa kuolewa kinyume na ridhaa yake. Vile vile hapana ruhusa ya kumkataza mwanamke asiolewe na mwanamume ampendaye ndani ya mipaka ya sheria ya Kiislamu.

**Pili**, mwanamke amepewa haki zote za kisheria za kumuacha mumewe ambaye amekosa nguvu za kiume (impotent), ambaye ni katili wake na ambaye anamchukia.

**Tatu**, mwanamume ameamrisha kutumia madaraka aliyopewa juu ya mkewe kwa huruma na upendo. Kama Qur'an inavyoagiza:

 ..... وَعَاشِرُهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ ٤

“ ... basi kaeni nao kwa wema ... ” (4: 19).

..... وَلَا تَسْأُوا الْفَضْلَ بَيْنَكُمْ ۗ ..... ﴿١٧٧﴾

« Wala msisahau kufanyiana Ihsani baina yenu ... » (2:237).

Na Allah(s.w) amesema: “Wabora wenu ni wale walio wema kwa wake zao na watu wao (katika familia)”. Kama mwanamume atatumia vibaya madaraka yake, mwanamke ana kila haki ya kukiendea chombo cha sheria na kumshitakia mumewe ambaye hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**Nne**, wanawake wajane na waliotengana na waume zao wanahaki na uhuru kamili wa kuolewa tena. Haki hii haijapatikana kwa jamii nyingi ulimwenguni.

**Tano**, kuna usawa kamili kati ya wanaume na wanawake kwa upande wa sheria za madai na jinai. Sheria ya Kiislamu haibagui wala haipendelei mwanamume au mwanamke katika kulinda haki za watu na haki zajamii kwa ujumla. Kwa mfano hukumu ya Kiislamu kwa mwizi ni kukatwa mkono, awe mwanamume au mwanamke kama inavyobainishwa katika Qur'an;

وَالسَّارِقُ وَالسَّارِقَةُ فَاقْطَعُوا أَيْدِيَهُمَا جَزَاءً بِمَا كَسَبَا نَكَالًا مِّنَ اللَّهِ ۗ  
وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٣٨﴾

Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, ikateni mikono yao, malipo ya yale waliyoyachuma. Ndiyo adhabu itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye Hekima (5:38).

Kuhusu adhabu ya wazinfu tunafahamishwa:

الزَّانِيَةُ وَالزَّانِي فَاجْلِدُوا كُلَّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا مِائَةَ جَلْدَةٍ وَلَا تَأْخُذْكُمْ بِهِمَا رَأْفَةٌ فِي دِينِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَلَيْشِهْدَ عَذَابَهُمَا طَآئِفَةٌ مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٤﴾

Mzinfu mwanamke na mzinfu mwanamume mpigeni kila mmoja katika wao mijeledi mia. Wala isiwashikeni kwa ajili yao huruma katika kupitisha hukumu hii ya Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi mnamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Na lishuhudie adhabu hiyo kundi la Waislamu. (24:2).



**Sita**, vile vile wanawake nao kama wanaume wanaruhusiwa kutoa ushahidi mahakamani au pale ushahidi wao unapohitajika. Bali katika kipengele hiki itatubidi tuwe wazi kwa kujibu maswali mbali mbali yanayoweza kuulizwa kama vile:

Kwa nini wanatakiwa mashahidi wawili wanawake badala ya shahidi mmoja mwanamume? Je, hii ina maana kuwa Uislamu unamhesabu mwanamke kuwa ni nusu ya mwanamume? La! Hasha. Kama katika suala la urithi, ukitazama kwa sura ya nje unaweza kudhani kuwa mwanamke amelewa na mwanamume kapendelewa kwa mwanamume kupewa mara mbili ya mwanamke. Hivyo hivyo katika suala la ushahidi, kwa kutakiwa wanawake wawili haina maana kuwa Uislamu unamuona mwanamke kuwa ni nusu ya mwanamume. Lau ingekuwa hivyo, Uislam ungeweza kuukataa ushahidi wake moja kwa moja. Na katika karne ya 7A.D iliposhuka Qur'an hata huko kuukubali ushahidi wa mwanamke kulionekana ni kioja na kuruka mipaka.

Aya ya Qur'an inayohusika inasema hivi:

..... وَأَسْتَشْهِدُوا شَهِيدَيْنِ مِنْ رِجَالِكُمْ ۖ فَإِنْ لَمْ يَكُونَا رَجُلَيْنِ  
فَرَجُلٌ وَامْرَأَتَانِ مِمَّن تَرْضَوْنَ مِنَ الشُّهَدَاءِ أَنْ تَضِلَّ إِحْدَاهُمَا  
فَتُذَكَّرَ إِحْدَاهُمَا الْأُخْرَى ۚ

« ..... Na mshuhudishe mashahidi wawili katika watu wenu wanaume. Lakini ikiwa hakuna wanaume wawili, basi mwanamume mmoja na wanawake wawili; katika wale mnaowakubali kuwa mashahidi. Ili kama mmoja wao akipotea, mmoja wao amkumbushe mwingine ..... » (2:282).

Ushahidi unaotajwa katika aya hii unahusiana na mikataba ya mambo ya fedha. Mashahidi wanatakiwa wawe ama wanaume wawili au mwanamume mmoja na wanawake wawili. Na sababu ya kuwaweka wanawake wawili imetajwa nayo ni kuwa akisahau mmoja mwenzake atamkumbusha. Swali la kujiuliza hapa ni kuwa kwa nini ihojiwe kuwa mwanamke ndiye atakayesahau na siyo mwanamume? Tatizo lililopo hapa kwa kiasi fulani linatokana na kasoro za kutafsiri neno "tadhila" kama kusahau. Neno "tadhila" halina maana ya kutokuwa na kumbukumbu (memory). Kwani mara nyingi wanawake hukumbuka zaidi kumbukumbu zao za kuzaliwa kuliko hata wanaume. Katika Uislam mwanamke ambaye kwa kawaida atakuwa anatimiza majukumu yake kama mke au mama aweza kujishughulisha na hayo kiasi cha kumfanya asiwe hadhiri sana wakati wa majadiliano yanayohusu kuandikiana mikataba ya masuala ya fedha, masuala ambayo hahusiki nayo mara kwa mara. Hii ni kwa kawaida, lakini haina maana kuwa kila mwanamke lazima atakuwa hivyo. Hata hivyo kwa sababu lengo la sheria ni kulinda haki za watu,

sheria imeweka hadhari hiyo ili kuhakikisha kuwa haki za watu zinahifadhiwa. Na lengo si kumdhaliisha mwanamke. Kwani lau ushahidi wa mwanamke ungekuwa unakataliwa tu kwa sababu mwanamke ni kiumbe dhilili basi Hadith zilizopokewa kutoka kwa wanawake zingekataliwa. Lakini Hadith zilizopokelewa kutoka kwa Bibi Aisha kwa mfano ni sehemu ya msingi wa sheria yenyewe. Ni upi ushahidi mzito zaidi, wa kupokea Hadith au wa kuandikishiana mikataba ya pesa? Yote hayo yanaonesha kuwa lengo ni kuhifadhi haki za watu zisipotee kwa sababu ya kughafilika na siyo kumdundisha mwanamke.

## Haki ya Kushiriki katika Siasa.

Siasa ni mambo yote yale yanayohusiana na jamii kwa ujumla. Hivi sasa neno siasa limefungamanishwa zaidi na uendeshaji wa Serikali na utawala. Tukumbuke kuwa Uislamu ni mfumo unaotawala uendeshaji wa maisha yote ya binadamu. Hakuna kipengele chochote cha maisha, si uchumi, siasa, utamaduni, n.k. ambacho kiko nje ya usimamizi wa Uislamu. Pia Qur'an imedhihirisha wazi kuwa jukumu la kuiendesha jamii katika misingi ya Kiislamu liko kwa wote, wanawake na wanaume. Qur'an inawataka Waislamu wote washirikiane katika kutenda na kuamrisha yaliyo mema na washirikiane katika kuyaepuka na kuyakataza yaliyo maovu na yanayovuruga amani. Hatuikuti Qur'an kuwabagua wanawake na wanaume katika jukumu hili bali inasisitiza:

وَالْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ يَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ  
وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَيُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَيُطِيعُونَ  
اللَّهَ وَرَسُولَهُ أُولَئِكَ سَيَرْحَمُهُمُ اللَّهُ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٧١﴾

*Na Wanaoamini wanaume na wanaoamini wanawake ni marafiki wao kwa wao huyaamrisha yaliyo mema na kuyakataza yaliyo mabaya na husimamisha swala na hutoa zaka na humtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu atawarehemu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu na Mwenye hikima. (9:71).*

Je, wanawake wanaruhusiwa kutoa maoni yao juu ya masuala ya kisiasa?

Katika Uislamu, wanawake wanayo haki sawa na wanaume katika kutoa maoni yao juu ya uongozi wa nchi. Ukirejea na kukiangalia kile kipindi bora katika historia ya Uislam, kipindi ambacho Waislamu walikuwa wakiyaendesha mambo yao kwa misingi ya Uislamu yaani wakati wa Mtume(s.a.w) na wakati wa Makhalfu wanne wa Mtume(s.a.w) tutaona kuwa wanawake walishiriki katika masuala ya jamii zao.

Sura ya 58 katika Qur'an inaitwa "Mujadila" kwani inataja habari za mwanamke aitwaye Khuwaylah binti Tha'labah, mke wa Aus bin Samit, ambaye alikwenda kulalamika kwa Mtume(s.a.w) juu ya mila ya kijahili iliyojulikana kwa jina la "Zihar". Allah(s.w) hakuwa na majibu kuhusiana na majadiliano aliyoyafanya na Khuwaylah, ndipo Allah(s.w) akateremsha aya za kisheria za kuharamisha "Zihar". *Mwenyezi Mungu ameshasikia usemi wa mwanamke yule anayejadiliana nawe sababu ya mumewe na anashtaki mbele ya Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu anayasikia majibizano yenu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kuona. Wale miongoni mwenu wawaitao wake zao mama zao) hao si mama zao. Hawakuwa mama zao ila wale walio wazaa. Wanasema neno baya na la uwongo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Msamaha na Mwenye Maghfira.*

الَّذِينَ يُظَاهِرُونَ مِنْكُمْ مِمَّن نَسَأَهُمْ مَا هُمْ بِأُمَّهَاتِهِمْ إِنَّمَا هُمُ الْمُحْرِمُونَ إِلَّا  
 الَّتِي وَلَدْتَهُمْ وَإِنَّهُمْ لَيَقُولُونَ مُنْكَرًا مِنَ الْقَوْلِ وَزُورًا وَإِنَّ اللَّهَ  
 لَعَفُوٌّ غَفُورٌ ﴿٥٨﴾ وَالَّذِينَ يُظَاهِرُونَ مِنْ نِسَائِهِمْ ثُمَّ يَعُودُونَ لِمَا قَالُوا  
 فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مِّن قَبْلِ أَنْ يَتَمَاسَّا ذَلِكُمْ تَوْعَظُونَ بِهِ وَاللَّهُ بِمَا  
 تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٥٩﴾ فَمَنْ لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامَ شَهْرَيْنِ مُتَتَابِعَيْنِ مِّن قَبْلِ أَنْ  
 يَتَمَاسَّا فَمَنْ لَّمْ يَسْتَطِعْ فإِطْعَامُ سِتِّينَ مِسْكِينًا ذَلِكَ لِتُؤْمِنُوا بِاللَّهِ  
 وَرَسُولِهِ وَتَلَّكَ حُذُودُ اللَّهِ وَلِلْكَافِرِينَ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٦٠﴾

*Na wale wawaitao wake zao mama zao kisha wakarudia katika yale waliyosema basi wampe mtumwa huru kabla ya kugusana. Mnapewa maonyo kwa haya. Na Mwenyezi Mungu anayajua yote mnayoyatenda. Na asiyepata (mtumwa) basi afunge saumu ya miezi miwili mfululizo kabla ya kugusana; na asiyeweza basi awalisha masikini sitini. (Mmeamrisha) haya ili mumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake; na hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu) na kwa makafiri iko adhabu iumizayo. (58:2-4).*

Khuwaylah alikwenda kujadiliana na Mtume(s.a.w) juu ya suala hili la kisheria na akatoa masikitiko yake. Qur'an katika aya hizi, iliondosha tatizo hili katika jamii na wala haikumlaumu mwanamke huyu kwa kutoa malalamiko yake. Wala Mtume(s.a.w) hakumkataza kutoa malalamiko hayo.

Wakati wa Ukhalifa wa Uthman, bibi Aisha mke wa Mtume wa Allah(s.w) hakuafikiana na maamuzi mengi ya Uthman. Pamoja na hayo Uthman

hakupata kumwambia hana haki ya kutoa maoni yake juu ya masuala ya dola kwa sababu yeye ni mwanamke. Bibi Aisha pia alipinga vikali sana uteuzi wa Ali kuwa Khalifa, na baadhi ya masahaba walimuunga mkono.

Hakuna aliyesema; Wewe ni mwanamke, huna haki ya kuingilia masuala haya. Hapana shaka yoyote kuwa baadaye Bibi Aisha alijutia sana msimamo wake huo wa kupinga uteuzi wa Ali. Hakujutia kwa sababu alijiingiza katika masuala ya kisasa, la. Bali alijutia kwa sababu rai yake juu ya Ali haikuwa sahihi.

Aidha siku moja Khalifa Uthman alikuwa amekaa na mshauri wak mkuu aitwaye Mar'wan bin Hassan. Mkewe Uthman alikuwepo wakati Mar'wan akimshauri Uthman. Akaupinga ushauri wa Mar'wan. Mar'wan akakasirika akasema: Nyamaza, tunazungumza mambo ambayo hayakuhusu. Khalifa Uthman akasema: Mwache kwa sababu yeye ni mkweli zaidi katika nasaha zake kwangu kuliko wewe. Tazama, Uthman hakusema, sawa wewe ni mke tu, nyamaza. Hii ni mifano tu. Hapana shaka kuwa katika Uislamu msisitizo ni kuwa jukumu la kwanza ni kuwa mke ni mjenzi na mlezi wa nyumba yake, ili nyumbani pawe ni kimbilio, kwa sababu ya utulivu, furaha na amani. Lakini hii haina maana kuwa kwa sababu hiyo mwanamke hatakiwi kutoa rai yake juu ya masuala ya kisiasa.

## Je, Wanawake Wanaye Haki ya Kupiga Kura?

Muundo wa upigaji kura siku hizi ni tofauti na ulivyokuwa zamani. Siku hizi kuna kujiandikisha, halafu vituo na masanduku maalum na mihuri ya kupigia kura. Katika zama za Mtume(s.a.w) ikiwa watu walitaka kumchagua mtu fulani kuwa kiongozi walitumia utaratibu uliojulikana kama "Bai'at" yaani kiapo cha utiifu (oath of allegiance). Utaratibu huu umetajwa katika Qur'an na Hadith. Allah(s.w) amesema katika Qur'an:

يَأْتِيهَا النَّبِيُّ إِذَا جَاءَكَ الْمُؤْمِنَاتُ يُبَايِعْنَكَ عَلَىٰ أَنْ لَا يُشْرِكْنَ بِاللَّهِ شَيْئًا وَلَا يَسْرِقْنَ وَلَا يَزْنِينَ وَلَا يَقْتُلْنَ أَوْلَادَهُنَّ وَلَا يَأْتِينَ بِبُهْتَانٍ يَفْتَرِينَهُ بَيْنَ أَيْدِيهِنَّ وَأَرْجُلِهِنَّ وَلَا يَعْصِيَنَّكَ فِي مَعْرُوفٍ فَبَايِعَهُنَّ  
وَاسْتَغْفِرَ لَهُنَّ اللَّهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ

*Ewe Nabii! Watakapokujia wanawake walioamini wanakuahidi ya kwamba hawatamshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote, wala hawataiba, wala hawatazini, wala hawatawaua watoto wao, wala hawataleta uzushi wanaozusha tu wenyewe baina ya mikono yao na miguu yao, wala hawakuasi katika jambo*

*jema, basi peana ahadi nao na uwatakie maghufira kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwingi wa rehema. (60: 12).*

Na katika mkataba wa Aqabah Mtume wa Allah(s.w) alichukua ahadi ya aina hiyo kwa wanaume na wanawake. Haki ya watu wote kupiga kura (universal suffrage) katika nchi za Ulaya magharibi imekuja miaka 1200 baada ya haki hiyo kutangazwa na Uislamu.

### **“Bai’at” Ilihusu Masuala ya Imani tu?**

Kutokana na aya hiyo hapo juu (60: 12) wako watu wanaotoa hoja kuwa “bai’at” yaani ahadi ya utii ilihusu masuala ya imani tu, hivyo haiwezi kuhusu viongozi wa serikali au dola. Hoja hii haina nguvu kwa sababu:

1. Mtume(s.a.w) alipewa ahadi ya utii siyo tu kama Mtume bali pia kama kiongozi wa dola (head of state).
2. Katika Uislamu hakuna mgawanyo wa vipengele vya kiimani na kidunia, mambo yote yamefungamana pamoja. Imani pia inahusiana na uadilifu, sheria n.k.
3. Aya (60: 12) pia imesema lwapo “hawakuasi katika jambo jema”. Msemo huu unaashiria kuwa ahadi hiyo pia inahusu maamuzi atakayoyafanya kama kiongozi wa dola, kama vile maamuzi ya kisiasa au kijeshi.

### **Je, Wanawake Wanayo Haki ya Kushiriki Katika Bunge?**

Muundo wa mabunge ya leo ni tofauti kabisa na hali ilivyokuwa wakati wa Mtume(s.a.w). Msingi wa kuwepo bunge hata hivyo ni kuwapa fursa wana jamii kujadiliana juu ya mambo yanayoihusu jamii yao. Katika Uislamu msingi mmojawapo wa uendeshaji wa serikali ya Kiislamu ni “Shuura”. Waislam lazima washauriane katika uendeshaji wa mambo yao. Khalifa (kiongozi) aliwaita watu wengi au wachache na kutaka ushauri wao juu ya jambo fulani. Hivyo utaratibu huu haukuwa rasmi.

Hata hivyo amri ya kushauriana ipo katika Qur’an hivyo muundo wa kupata ushauri huo waweza kubadilika kulingana na kubadilika kwa mazingira, maadam amri ile ya kushauriana inatekelezwa. Hata hivyo baada ya kutawafu Mtume(s.a.w) ilizuka dhana ya kuwa na “*Ahlul haal wal aql*” yaani watu wenye vipawa na uwezo maalum kuwa ndio watakaofanya kazi hii ya kumshauri kiongozi wa dola. Wanawake wenye uwezo huo waliendewa majumbani mwao na kutakiwa watoe ushauri wao. Hakuna mwanachuoni au Khalifa aliyesema: Kwa nini mnawataka ushauri wanawake au wanawake wasihusishwe na siasa. Sharti pekee la kuzingatia ni kuwa yote hayo yafanywe kwa kuzingatia misingi ya Uislamu, adabu za Kiislamu na maadili yake. Kisa kimoja kilichotokea wakati wa ukhalifa wa Umar(r.a) chaweza kusaidia kufafanua haki ya wanawake

kushiriki katika maamuzi. Umar (r.a)aliona na hakufurahishwa na tabia iliyoziuka ya wanawake kudai mahari kiasi kikubwa sana. Hivyo akaamua kuikomesha tabia hiyo, akasimama katika mimbar msikitini na kusema kuwa kuanzia wakati ule mahari isivuke dirham 400. Na mwanamke atakayedai mahari yatakayozidi dirham 400 basi ziada yote nitaichukua na kuitia katika *Baitul Maal* yaani hazina ya serikali ya Kiislamu. Papo hapo akasimama mwanamke mmoja akasema: “*Yaa Umar! Laisa Laka dhaalika*”, yaani “Ewe Umar! Huna mamlaka juu ya hilo”. Akamkumbusha aya ya Qur’an (4:20) inayowakataza wanaume kudai mahari wanapowaacha wake zao hata kama waliwapa “mrundi wa mali”. Neno lililotumika katika Qur’an ni “Qintara” yaani tani. Yaani hata kama mtu atakuwa ametoa tani za dhahabu kama mahari. Yule mwanamke akamwuliza Umar, kwa misingi gani wewe unataka kuwanyang’anya wanawake haki waliyopewa na Allah?

Lau ingekuwa ni makosa kwa mwanamke kusimama katika hadhara ya wanaume na kutoa rai yake basi watu wote wangemkemea na kumtaka akae chini. Hakuna aliyemkataza. Na baada ya kusema hivyo Umar akasema kwa unyenyekevu: “Mwanamke yu sahihi na Umar amekosea”. Na akaifuta kauli yake. Umar anajulikana kuwa alikuwa kiongozi madhubuti ambaye hachelei chochote katika kusimamia dini ya Allah. Lau kama ingekuwa ni makosa kwa mwanamke kusimama katika hadhara ya wanaume na kutoa fikra zake basi Umar asingesita hata kidogo kusema: Sawa mimi nimekosea, na wewe pia umekosea kusimama hadharani na kutoa rai yako. Huu ni mfano wa majadiliano ya wazi (open discussion) ya kujadili muswada wa sheria ambayo Umar alitaka kuipitisha. Lakini ilikwama kwa sababu ya hoja zilizotolewa na mwanamke yule. Kisa hiki kinaweza kulinganishwa na majadiliano ya bungeni katika vipengele vifuatavyo:

- (i) Umar, ambaye alikuwa ni kiongozi wa Waislamu alipoona kuwa wanawake walikuwa wakitaja mahari mengi na akaamua kuzuia tabia hiyo kwa kuweka kiwango cha juu kabisa kisizidi dirham 400. Leo,kitendo hicho kinaweza kulinganishwa na uamuzi wa serikali au mswada (bill) wa sheria unaowasilishwa bungeni.
- (ii) Mapendekezo hayo ya Umar yalitangazwa msikitini. Na kwa Waislamu msikitini si mahali pa kuendeshea swala tu bali pia katika zama zote msikiti umekuwa ukitumika pia kama mahali pa kujadiliana juu ya masuala mbali mbali ya kijamii, kisiasa na kijeshi. Misikiti pia ilikuwa ndiyo maktaba ya Waislam na mahali pa kuendeshea darsa. Hivyo, misikiti ni majlisi ya halali ya Waislamu kujadiliana mambo yao kama ilivyo bunge. Tofauti iliyopo ni kuwa bunge linaruhusu watu maalum tu lakini misikiti iwazi kwa kila Muislamu.
- (iii) Ukweli kuwa Umar aliutangaza uamuzi huo hadharani kabla ya kuutekeleza kunaonesha kuwa watu walikuwa wamepewa fursa ya kutoa rai zao au upinzani wao juu ya uamuzi huo kama ambavyo wabunge hutoa rai zao juu ya mswada wa sheria.

- (iv) Yule mwanamke aliupinga uamuzi wa Umar kwa sababu ulikwenda kinyume na Qur'an. Katika sheria za mabunge, katiba ya nchi ndiyo sheria kuu ya nchi (basic law of the land). Sheria yoyote itakayokiuka katiba hutanguka kwani katiba ndio msingi wa sheria zote. Na kwa Waislam Qur'an ndiyo Katiba yao, ndiyo msingi wa sheria zote. Uamuzi wowote unaokiuka Qur'an ni batili na hauwezi kuruhusiwa kupita. Hivyo yule mwanamke alimwonyesha Umar kuwa uamuzi wake ulikuwa unakiuka Qur'an, katiba ya Waislamu. Katiba ambayo haiwezi kufanyiwa marekebisha.
- (v) Umar alikiri kuwa yule mwanamke alikuwa sahihi na yeye alikuwa amekosea. Kitendo hicho cha Umar kinaweza kulinganishwa na uamuzi wa serikali kuuondosha mswada wake bungeni. Hivyo ni dhahiri kuwa kuna kufanana kati ya kisa hiki na majadiliano ya bunge. Zaidi ya kufanana huko yapo pia mambo mengine ya kuzingatia.

**Kwanza**, ni kuwa msimulizi wa Hadith amesema "Mwanamke alisimama nyuma" bila kulitaja jina la mwanamke huyo. Kwa kawaida wasimulizi wa Hadith husema fulani bin au binti fulani alisema kadha kadha. Kutomtaja jina hapa kunaonesha kuwa mwanamke aliyetoa hoja ya kumpinga Umar hakuwa mwanamke mashuhuri anayejulikana kwa watu wengi bali ni mwanamke wa kawaida tu. Na hili laonesha kuwa uhuru na haki ya kumsahihisha kiongozi hata kama ni mkuu wa nchi alikuwano kila mtu.

**Pili**, ni kuwa msikiti ulikuwa umefurika watu, ambao waliishi na kumfuata Mtume Muhammad(s.a.w) alipokuwa hai pamoja nao. Walikuwepo maswahaba ambao Mwenyezi Mungu amewasifu katika Qur'an (9: 100) kwa ucha Mungu wao. Lakini hakuna hata mmoja aliyemkemea mwanamke huyo kwa kusimama hadharani na kutoa hoja yake. Na Umar ambaye ujasiri na ukali wake unajulikana sana asingeliruhusu hilo kutokea machoni pake lau angejua kuwa linapingwa na Sheria ya Kiislamu.

Na mfano mwingine ni kuwa baada ya kuuliwa kwa Umar, na mashauriano yalipokuwa yakifanyika juu ya nani ashike uongozi wa dola ya Kiislamu, Bwana Abdulrahman bin Auf alipewa jukumu la kuwauliza watu yupi kati ya Uthman na Ali awe kiongozi. Na imeelezwa katika kitabu kitiwacho *Al-Bidaya Wan Nihaya* kilichoandikwa na mwanahistoria mashuhuri Ibn Kathiir kuwa miongoni mwa watu walioulizwa walikuwa wanawake.

## **Je, Uislamu Unawakataza Wanawake Kuwa Viongozi?**

Ili swali hili lijibiwe kwa ufasaha inabidi kwanza upatikane ufafanuzi juu ya nini maana ya uongozi. Katika tafsiri yenye upeo mpana uongozi ni nafasi ya madaraka ya kubeba dhamana (responsibility) na ya kutoa mwongozo au maelekezo. Tutaona katika kipengele kifuatacho "Haki ya Elimu" kuwa katika jamii bora ya Kiislamu (ideal Muslim society) ni vizuri baadhi ya wanawake

wawe madaktari, walimu, wauguzi n.k. Je, hizi si nafasi muhimu zenye dhamana nzito? Je, hizi si nafasi za kutoa mwongozo na maelekezo kwa wengine?

Na hata kama mwanamke hajaajiriwa, nani anaweza kusema kuwa nafasi ya mama nyumbani haibebi majukumu ya uongozi? Nani anaweza kusema kuwa malezi ya watoto si dhamana inayohitaji kutoa maelekezo na mwongozo? Na ni jukumu lipi hasa ambalo ni muhimu zaidi kuliko lile la kukiongoza kizazi kipya katika njia iliyonyooka? Kwa hakika ni kukosekana kwa uongozi huu muhimu ndiko kunakochangia kwa kiasi kikubwa sana kuparaganyika na kuanguka kwa jamii zetu leo. Kutokana na ukweli huu Allah(s.w) amesema katika Hadith:

*“Kila mmoja wenu ni mchungaji (yaani kiongozi), na kila mmoja wenu ataulizwa juu ya alivyovichunga. Mtawala ataulizwa juu ya raia zake, mume ataulizwa juu ya familia yake, mke ataulizwa juu ya wanakewe na nyumba yake, mtumishi ataulizwa juu ya amana alizokabidhiwa”.* (Bukhaary na Muslim)

Kutokana na Hadhith hii hata kama mwanamke hakuajiriwa bado ni kiongozi.

Hata hivyo kama kilichokusudiwa ni uongozi katika taasisi za umma, hakuna aya ya Qur’an inayokataza moja kwa moja wanawake kuwa viongozi bila kujali kiwango cha nafasi hiyo ya uongozi au umbile la nafasi hiyo. Iwapo kutakuwepo na ulazima, na iwapo uongozi wa mwanamke hautakiuka vipengele vingine vya Sheria ya Kiislamu, basi mwanamke anaweza kuwa kiongozi.

Ngazi pekee ya uongozi ambayo Uislamu haumruhusu mwanamke kuishika ni ile ya ukuu wa nchi. Hata hivyo kwa kutumia kanuni ya qiyas baadhi ya wanazuoni wanasema mwanamke pia asiwe Kamanda wa Majeshi.

## **Kwa nini Mwanamke Haruhusiwi Kuwa Mkuu wa Nchi?**

Katika Qur’an hakuna aya inayowakataza wanawake kuwa viongozi.

Lakini katika Hadith Sahihi iliyosimuliwa na Bukhaary, Muslim, At-Tirmidhy, An-Nasai na wengineo Mtume(s.a.w) alipoambiwa kuwa Waajemi walikuwa wakifanya mabinti za Wafalme wao waliofariki kuwa viongozi wao, alisema: “Watu hawataendelea, hawatafanikiwa katika mambo yao ikiwa watawachagua wanawake kuwa viongozi wao wa nchi.”

Hikma ya kuzuiliwa wanawake kuwa viongozi wa nchi ni kuwa katika Uislam mkuu wa nchi si nafasi ya hadhi tu (ceremonial or figure head) bali ni cheo chenye majukumu mengi mazito. Mkuu wa nchi ndiye imamu wa sala za jamaa misikitini. Anatakiwa pia aliongoze jeshi vitani. Kama tulivyoona huko nyuma mwanamke hawezi kuwa imamu wa swala zenye mchanganyiko wa wanaume na wanawake. Na kwa kawaida wanawake wasingependa kuwa makamanda wa majeshi hata wale wanawake wanaodai wafanye kila kazi inayofanywa na wanaume. Na kwa hakika ikifikia katika jamii wanawake wakapenda kuongoza



vita, kufanya mipango na kushiriki katika kumwanga damu za watu, basi wakati huo maisha yatapoteza uzuri wake, uzuri unaotokana na moyo wa huruma na mapenzi walionayo wanawake. Uwiano mzuri wa maisha utaondoka iwapo wanawake nao watakuwa na mioyo migumu isiyosita kumwaga damu.

Jambo jingine la kuzingatia ni kuwa katika Uislamu urais si cheo cha kukigombea bali ni jukumu zito la kukimbiwa. Hii ni kwa sababu kiongozi wa nchi anatakiwa asiishi maisha yaliyo bora kuliko ya raia yoyote wa nchi yake. Matokeo yake ni kuwa hata kama mtu alikuwa na maisha mazuri ya anasa kabla ya kuwa kiongozi akipata uongozi anakuwa na maisha duni zaidi. Mtume(s.a.w) kabla ya utume alikuwa na maisha bora zaidi kiuchumi kuliko alipokuwa Mtume. Ingawa angetaka angeweza hata kuwa milionea kutokana na nafasi yake. Katika Hadith zilizokusanywa na An-Nawawi, Bibi Aisha(r.a) amesema mwezi mmoja au miwili ilipita bila kuwasha moto nyumbani mwao kwa sababu hakukuwa na cha kupika.

Waliishi kwa tende na maji. Na hii ni pamoja na kuwa Mtume angeweza kuishi katika anasa. Hali ilikuwa ngumu hadi wakeze walianza kulalamika.

Wakakemewa na Mwenyezi Mungu (33:28-29). Na hali ilikuwa hivyo hivyo kwa Makhalifa waliofuatia. Hivyo uraisi si cheo ambacho mtu atakigombea kwa hila, rushwa na kampeni za usiku na mchana.

Vyovyote itakavyokuwa katika Uislam mtu hajipendekezi yeye mwenyewe jina lake bali wenzake ndio wampendekeze. Suala la wanawake kuziuliwa kuwa maraisi si la msingi kwa sababu tangu hapo katika idadi ya sasa watu wapatao elfu nne milioni(Bilioni 6) waliopo duniani ni wanaume wangapi ni maraisi au wanaweza kuwa marais?

## **Je, Wanawake Wanaweza kuwa Majaji?**

Juu ya sualala hili wanazuoni wa Kiislamu wamehitilafiana.

Tunachoweza kufanya hapa ni kuzibainisha tu rai zao bila upendeleo.

Rai ya **kwanza** ni ile inayosema kuwa mwanamke hawezi kuwa jaji.

Hoja zao ni mbili: Ya kwanza ni kuwa mwanamke hawezi kuwa mkuu wa nchi basi hawezi pia kuwa jaji kwa sababu ujaji unaweza kulinganishwa na utawala. Jaji anafanya kazi za kiutawala. Hoja ya pili ni kuwa katika Uislamu, mume ndiye mkuu wa familia. Hivyo kama sheria haijampa mwanamke ukuu wa familia ambayo ni taasisi ndogo basi hawezi kupewa ujaji ambayo ni taasisi kubwa zaidi. Rai hii ndiyo inayofuatwa na wanazuoni walio wengi.

Rai ya **pili** ni ile inayosema kuwa mwanamke anaweza kuwa jaji.

Hii ndiyo rai ya mwanazuoni mashuhuri aitwaye At-Tabari. Hoja yake ni kuwa kulinganisha ukuu wa nchi na ujaji si sahihi kwa sababu Hadith imebainisha wazi wazi kuwa walichozuiliwa ni ukuu wa nchi. Kulinganisha ukuu wa nchi na maeneo mengine si sahihi.

Rai ya **tatu** ni ile iliyotolewa na Imam Abu Hanifa. Yeye anasema ikiwa mwanamke anaweza kuwa shahidi katika masuala ya fedha basi anaweza pia kuwa jaji katika masuala ya fedha. Hivyo ni dhahiri kuwa ukiondoa ukuu wa nchi, wanazuoni hawajaafikiana wote kwa kauli moja kama katika maeneo mengine wanawake wanaweza kuwa viongozi au la.

## Haki ya Elimu

Katika Uislamu kujielimisha ni faradhi inayowahusu Waislamu wote, wanaume na wanawake:

أَقْرَأْ بِأَسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ ﴿١﴾

“Soma kwa jina la Mola wako aliyeyumba” (96: 1).

Aya hii na nyingi nyinginezo zinazosisitiza elimu katika Uislamu hazikumbagua mwanamke. Pia Allah(s.w) katika kusisitiza elimu amesema:

“Kutafuta elimu ni faradhi kwa kila Muislamu mwanamume na kila Muislamu mwanamke”.

Bali kutokana na tabia ya jamii nyingine ulimwenguni ya kuwanyanyasa wanawake na kuwaona kuwa ni nuksi, wasiostahiki kulelewa vizuri na kuelimishwa, Uislamu umetoa motisha mkubwa wa ahadi ya kupata malipo makubwa kutoka kwa Allah(s.w) kwa kuwalelea watoto wa kike vizuri na kuwaelimisha ipasavyo. Katika Hadith iliyosimuliwa na Imam Ahmad, Allah(s.w) amesema:

*Yeyote atakayewalea mabinti wawili hadi wakakua, yeye na mimi Siku ya Kiyama tutakuwa kama hivi. (Akaonesha vidole vyake viwili ili kupigia mfano watakavyokuwa karibu sana huko Peponi). (Ahmad)*

Lengo la mafundisho haya ya Allah(s.w) ni kuwaondosha watu katika zile fikra dhafu za kuwaona watoto wa kike kama kwamba si watu. Na katika Hadith nyingine iliyosimuliwa pia na Ahmad, Allah(s.w) amesema:

*Yeyote ambaye amemzaa binti, na hakumzika yungali hai, na hakumtukana au kumkashifu, na hakumpendelea mtoto wake wa kiume zaidi kuliko huyo wa kike, Allah atamuungiza Peponi. (Ahmad)*

Zaidi ya mafundisho haya Allah(s.w) alionesha mfano katika maisha yake mwenyewe, kwa kuwaheshimu na kuwatendea vizuri binti zake, kiasi ambacho

aliwahi kusema juu ya binti yake, Fatma; “Fatma ni sehemu yangu mimi, furaha yake ni yangu, na ghadhabu zake ni uchungu wangu”.

Umuhimu wa kuwaelimisha watoto wa kike uko wazi. Tumeona kuwa katika jamii ya Kiislamu hapana budi kuwepo wanawake madaktari, wauguzi, walimu n.k. Ni dhahiri kuwa itabidi waelimishwe kwanza ndio waweze kupata ujuzi wa kufanya kazi hizo. Wanawake wajifunze fani zipi za Elimu? Qur’an haijaweka mipaka yoyote inayowakataza wanawake fani fulani fulani za elimu. Kama kuna fani ya elimu ambayo ni haramu kwa wanawake basi fani hiyo itakuwa pia haramu kwa wanaume. Kwa mfano kujifundisha uchawi ni haramu kwa Waislamu wote (wanaume na wanawake), Qur’an (2: 102).

Ingawa kila mtu anayohaki ya kujipatia elimu, katika fani na kiwango chochote anachoweza, kipo kiwango fulani cha elimu ambacho ni lazima kila mtu awe nacho. Elimu ya lazima ni pamoja na kujua misingi ya Uislamu - Imani na Nguzo za Uislamu, namna ya kutekeleza Kwa ukamilifu Ibada maalum kama vile, kusimamisha swala, zakati, funga, hija, n.k., kujua wajibu katika familia na katika jamii, kujua katika maisha yetu ya kila siku lipi ni halali kulitenda na lipi ni haramu kwa mujibu wa Qur’an na Sunnah. Kwa ujumla elimu juu ya mambo haya ya msingi, tunaiita “ elimu ya mwongozo”. Elimu hii ni faradh ain kwa kila muislamu mwanamume na mwanamke.

Ingawa wanawake hawajazuliwa kusomea fani yoyote ya elimu, bado tunaweza kusema kuwa zipo baadhi ya fani za elimu ambazo ni vizuri sana wanawake wakizisomea kwani zitawafaa sana katika kutimiza jukumu la uzazi na malezi ya jamii, kama vile elimu ya tiba (medicine) uuguzi (nursing), ualimu, uendeshaji wa nyumba (home management), saikolojia, n.k. Fani nyingine za elimu zinabakia kuwa ni halali kwao kama zilivyo halali kwa wanaume. Kutokana na mifano hii michache katika maeneo haya ya haki tuliyojaribu kuyabainisha humu, Uislamu kama ulivyo Dini ya haki, humpa kila mtu haki yake bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

### ***(c) Hifadhi ya Mwanamke na Maadili ya Jamii***

Kimaumbile wanadamu kama walivyo wanyama, wamejaaliwa kuwa na mvuto wa kimapenzi kati ya mume na mke ili kuwawezesha kutekeleza wajibu mkubwa wa kuzaana na kuendeleza kizazi. Wanyama, matamania yao ya kukutana dume na jike yanakuwa juu kwa kipindi maalum, pale wanapokuwa tayari kuanzisha uzazi. Tofauti na wanyama, matamania ya mwanadamu ya kukutana kimwii kati ya mwanamume na mwanamke yako juu siku zote alimradi tu vipatikane vishawishi. Katika hali hii, endapo wanaume na wanawake watachiwa huru kuchanganyika na kuingiliana pasina kuwekewa mipaka, watakidhi matamania yao hadharani kama wanyama na pengine zaidi ya wanyama. Hali hii tumeiona katika jamii za Ulaya na Marekani baada ya kutolewa uhuru kwa wanawake kuchanganyika na kubusiana na wanaume wependavyo

na bila ya mipaka. Athari ya uhuru huu kwa jamii ya Ulaya na Marekani tumeiona katika kushamiri kwa umalaya, kuenea magonjwa ya zinaa, kuwa na watoto wa nje ya ndoa, kuvunjika kwa familia, n.k. Lakini aliyeathirika zaidi ni mwanamke ambaye uke wake umefanywa ni bidhaa ya kuuzwa na kununuliwa na urembo wake umefanywa ni chombo cha matangazo ya biashara.

Allah(s.w) hakujaalia mvuto wa mapenzi kati ya mwanamume na mwanamke, ili kumdhaliisha mwanamke na kuiangamiza jamii, bali amejaalia mvuto huu wa kimapenzi kati ya mume na mke ili wanadamu waweze kuendeleza kizazi na kuishi maisha ya kijamii yaliyojngwa juu ya misingi imara ya upendo na ushirikiano:

أَقْرَأْ بِاسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ

*Na katika ishara Zake ni kuwa amekuumbieni wake zenu katika jinsia yenu ili mpate utulivu kwao, naye amejaalia mapenzi 'na huruma baina yenu ..... (30:21).*

Ili tuweze kufikia lengo hili, Allah(s.w) ametuwekea utaratibu maalumu wa mahusiano kati ya wanaume na wanawake. Allah(s.w) ameturuhusu, wanaume na wanawake, tukidhi matashi ya kimaumbile kati ya mwanamke kwa njia ya ndoa na ametuharamishia mahusiano yoyote kati ya mume na mke nje ya mipaka ya ndoa. Ili kurahisisha maisha ya ndoa na kuyafanya mahusiano kati ya mume na mke nje ya ndoa yawe magumu, Uislamu umeweka vipengele kadhaa vya kuihifadhi jamii na zinaa:

- (i) Kujitakasa mtu binafsi (ucha-Mungu)
- (ii) Kutoa adhabu kali kwa wazunifu
- (iii) Kutokomezwa vishawishi vya zinaa

### **(i) Kujitakasa Mtu binafsi (Ucha-Mungu)**

Ucha-Mungu ni kuishi kwa kuchunga mipaka ya Allah(s.w) kwa unyenyekevu. Imani thabiti ndio nyenzo kubwa ya kumuwezesha mja kuchunga mipaka ya Allah(s.w). Muumini wa kweli ni yule anayefuata kwa ukamilifu sheria ya Kiislamu katika maisha yake yote kwa kuhakikisha kuwa anafuata maamrisha yote ya Allah(s.w) na kuacha makatazo yake yote. Kwa Muumini huyu anachohitajia ni kujua tu Allah(s.w) na Mtume wake wamearisha nini na wamekataza nini. Muislamu mcha-Mungu atakapojua kuwa jambo fulani limekatanzwa katika kitabu cha Allah(s.w) kama vile zinaa ilivyoharamishwa katika aya kadhaa(rejea Qur'an: 17:32), hatajipusha na kulitenda tu bali hata pia kuliwaza. Miongoni mwa nyenzo zilizowekwa na Uislamu ili kumuwezesha mtu binafsi kuepukana na tendo ovu la zinaa ni kuwasisitiza waumini kuwa na haya, kujiepusha na fikra mbaya juu ya wanawake/wanaume, kujiepusha na kutizama kwa matamano na wanawake kujiepusha na kushawishi kwa sauti kali, kudhihirisha mapambo na

kupaka manukato makali.

“**Haya**” ni msingi wa Imani na ngao ya kumkinga mtu na maovu. Iliyoye ni kwamba matendo maovu kama vile uzinifu, wizi, uwongo, n.k. ambavyo mwanaadam huyatenda kutokana na msukumo wa matashi ya unyama wake, yanampelekea kwenda kinyume na utu wake. Matendo yote maovu yameelezwa katika Qur’an kwa neno “Munkar” lenye maana “isiyojulikana” au “jambo geni”. Vitendo hivi vimeitwa “Munkar” kwa sababu ni vigeni katika utu wa mwanaadam. Mwanaadam ameumbwa na nguvu ya kupigana ndani kwa ndani na maovu. Nguvu hii ni “haya”. Nguvu hii ipo kwa kila mtu lakini inahitaji kuamshwa kwa kupewa mara kwa mara mafundisho ya maadili ya Uislamu. Katika kuonesha nafasi ya “haya” katika maadili ya Uislamu Mtume(s.a.w) amesema:

«Kila dini ina maadili yake na maadili ya Uislam ni «Haya”. “Haya” ndiyo inayomuwezesha mwanaadam kujiepusha na maovu bila ya nguvu za polisi. Kinyume chake mtu asiye na haya hufanya ovu lolote alitakalo. Mtume(s.a.w) kasema:

*«Unapokuwa huna haya unaweza kufanya ulitakalo”. Muislam katika kujiepusha na matendo maovu na machafu, hawaonei haya wanaadam wenziwe tu bali humuonea haya zaidi Mwenyezi Mungu ambaye yu karibu yake zaidi kuliko mshipa wake mkuu wa damu (Jugular vein). Allah(s.w) amesema: «Allah(s.w) anahaki zaidi ya kuonewa haya” (Tirmidh). Kama mtu anaona haya kutenda kitendo kiovu mbele ya watu, basi aone haya zaidi kutenda kitendo hicho mbele ya Allah(s.w).*

## **Kujiepusha na Vishawishi vya Zinaa**

Katika macho ya sheria kitendo cha zinaa kinahesabiwa pale wanapokutana kimwili mwanamume na mwanamke nje ya ndoa. Lakini katika maadili ya Kiislamu kitendo chochote kitakacho fanywa na mwanamume au mwanamke ambacho kitapelekea kuleta matamano ya jimai nje ya ndoa, kinahesabiwa kuwa ni kitendo cha uzinifu wa aina yake. Kwa mfano mtu kumwanguka kwa matamano mwanamke asiye kuwa mkewe, kufurahia tusi, uzuri wa sauti ya mwanamke asiyekuwa mkewe, kufurahia maongezi na mwanamke asiyekuwa mkewe au maharimu wake na kumtembelea mara kwa mara mwanamke asiyekuwa mkewe au maharimu wake atakuwa amefanya uzinifu kwa macho, masikio, ulimi na miguu yake. Hapana sheria yoyote itakayomkamata kwa uzinifu, lakini muumini wa kweli atajihukumu mwenyewe na kujihesabu kuwa ni mkosaji mbele ya Allah(s.w). Hivyo atatubia kwa Mola wake na kujiepusha mbali na vishawishi hivi vya zinaa. Kuhusu zinaa ya viungo mbali mbali vya mwili Allah(s.w) amesema:

*“Macho yanazini na uziniji wa macho ni mtazamo mbaya (kutizama kwa matamano (evil look), mikono inazini na zinaa ya mikono ni kuvuruga amani*

(kufanya mabaya); miguu inazini na zinaa ya miguu ni kuendea maovu; uziniji wa ulimi ni maongezi mabaya au yasiyo maana; na uzinifu wa moyo (nafsi) ni matamania mabaya. Hatimaye viungo vya siri vinathabitisha (kwa kuviunga mkono) au kuvikatalia.

Mtazamo muovu ni hatari zaidi katika kuwapelekea watu katika kitendo cha zinaa. Katika Qur'an tunaamrisha tujiepushe na mtazamo muovu katika aya zifuatazo:

قُلْ لِلْمُؤْمِنِينَ يَغُضُّوا مِنْ أَبْصَرِهِمْ وَيَحْفَظُوا فُرُوجَهُمْ ذَٰلِكَ أَزْكَىٰ لَهُمْ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا يَصْنَعُونَ ﴿٣٠﴾ وَقُلْ لِلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَرِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ ..... ﴿٣١﴾

Waambie Waislam wanaume wainamishe macho yao (wasitizame yaliyokatazwa), na wazilinde tupu zao, hili nitakaso kwao, bila shaka Mwenyezi Mungu anazo habari za yote wanayofanya Na waambie Waislam wanawake wainamishe macho yao, na walinde tupu zao ..... (24:30-31).

Utekelezaji wa amri hii umefafanuliwa katika Hadith mbali mbali za Mtume(s.a.w) amesema:

Mwana wa Adam! Mtazamo wako wa kwanza unasamehewa, lakini kuwa mwangalifu kuwa hutazami mara ya pili. (Al-Jassaas).

Mtume wa Allah(s.w) alimuusia Ali(r.a):

Ewe Ali, usirudie mtazamo wa pili baada ya ule wa kwanza. Mtazamo wa kwanza unasamehewa lakini sio ule wa pili. (Abu Daud).

Jabir(r. a) alimuuliza Mtume kuwa atafanya nini endapo macho yake yatamwangukia mwanamke bila kudhamiria? Mtume(s.a. w) alimuelekeza kuwa ageuze macho yake pale pale. (Abu- Daud).

Mwanamke kuonesha urembo wake na mapambo yake ni kitendo kiovu kinachoambatanishwa na mtazamo muovu. Hiki ni kishawishi kingine cha zinaa na wanawake wamekatazwa kufanya hivyo katika Qur'an:

..... وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا ..... ﴿٣١﴾

“...Wala wasidhihirishe viungo vyao isipokuwavinavyodhihirika ..... “(24:31).

..... وَلَا تَبْرَحْنَ تَبْرُجَ الْجَهْلِيَّةِ الْأُولَىٰ ..... ﴿٣٣﴾

“Wala msionyesheshe mapambo yenu kama walivyokua wakionyeshesha mapambo yao wanawake wa zama za ujahili (33:33).

Sauti ya mwanamke ni kishawishi kingine cha zinaa endapo ataongea kwa kuilegeza. Hivyo wanawake Wakiislamu wanaonywa wasifanye hivyo:

..... إِنَّ أَتَقِيْتَنَّ فَلَا تَخْضَعْنَ بِالْقَوْلِ فَيَطْمَعَ الَّذِي فِي قَلْبِهِ مَرَضٌ

﴿٣٢﴾ وَقَلْنَ قَوْلًا مَّعْرُوفًا

“... Kama mnamuogopa Mwenyezi Mungu, basi msilegeze sauti (zenu) mnaposema na wanaume) ili asitamani mtu mwenye ugonjwa moyoni mwake (kufanya mabaya na nyinyi) na semeni maneno mazuri’ (33:32).

Si sauti yake tu iliyokishawishi kitendo cha zinaa bali hata sauti ya mapambo ya mwanamke huwavutia wanaume na kuwapelekea kwenye fikra mbaya ya zinaa. Katika Qur’an wanawake wa Kiislamu wanakatazwa kudhihirisha sauti za mapambo yao:

..... وَلَا يَضْرِبْنَ بِأَرْجُلِهِنَّ لِيُعْلَمَ مَا يُخْفِينَ مِنْ زِينَتِهِنَّ ..... ﴿٣١﴾

.....Wala wasipige miguu yao (wasijitingishe) ili yajulikane wanayoyaficha katika mapambo yao .....(24:31).

Manukato yenye harufu kali kwa wanawake pia ni kichocheo kingine cha zinaa. Mtume(s.a.w) kasema:

Mwanamke anayetumia manukato na kupita mbele ya watu ni muovu. (At-Tirmidh).

Uislamu umeweka tahadhari hizi na nyinginezo ambazo mtu binafsi, akizingatia inakuwa ni ngao madhubuti ya kuikinga jamii na uovu wa Zinaa.

## (ii) Hatua za Kuzuia Uzinzi katika Jamii

Uislamu pamoja na kutoa mafunzo ya maadhi yanayomuwezesha mtu binafsi ajjepushe kwa hiari yake na kitendo kibaya cha zinaa, umechukua hatua mbali mbali ambazo huifanya zinaa isiwe kitendo chepesi katika jamii. Kwani Uislam haukatazi tu kufanya kitendo cha zinaa bali hata kufanya kitendo chochote kitakacho shawishi zinaa ni haramu. Tumeamrisha katika Qur’an:

وَلَا تَقْرُبُوا الزَّيْنَىٰ ۗ إِنَّهُ كَانَ فَحِشَةً وَسَاءَ سَبِيلًا ۝

*Wala msikaribie zinaa. Hakika hiyo zinaa ni uchafu (mkubwa) na njia mbaya kabisa. (17:32).*

Kuzuia ugonjwa ni bora na ni rahisi zaidi kuliko kutibu. Uislamu umeweka taratibu zifuatazo ili kuzuia ugonjwa mbaya wa zinaa usienee na kuiathiri jamii:

## (1) Mavazi na Stara ya Kiislamu

Uislamu umelichukulia kwa umakini mkubwa suala la kujisitiri uchi kwa namna ambayo hapana jamii nyingine ulimwenguni iliyofikia kiwango chake. Kabla ya Mtume wa Allah(s.w) kuuhiisha Uislamu, jamii ya Waarabu ilikuwa hajjali kabisa suala la kusitiri uchi. Watu katika jamii hiyo, walikuwa wakivua nguo hadharani wakati wa kuoga au kujisaidia bila ya kujali nani yuko mbele yao. Walizoea kukaa uchi kwa kiasi kwamba, wake kwa waume walitufu Ka'aba uchi wa mnyama. Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba, hata baada ya Mtume(s.a.w)kuhiisha Uislamu na kuyaeneza maadili ya Kiislamu ulimwenguni kote, bado leo kuna watu katika jamii mbali mbali wanaotembea uchi hadharani. Utakuta hata zile jamii ambazo zinatambua kuwa mwanadamu anastahiki kusitiri uchi wake, hazikuweka mipaka ya uchi wa mwanadamu kwa kiasi kwamba kwa wengi wao sitara imeishia kwenye kufunika sehemu za siri tu. Ni Uislamu pekee, kwa kuzingatia umbile la wanaume na wanawake, umetoa mipaka ya uchi kwa wanaume na wanawake na kuelekeza namna bora ya kujisitiri ili kuondoa vishawishi vyote vya zinaa vinavyotokana na mavazi. Mafundisho ya Uislamu juu ya mavazi yanaanza na aya ifuatayo:

يَبْنِي ۙءَادَمَ قَدْ أَنْزَلْنَا عَلَيْكُمْ لِبَاسًا يُورِي سَوَاءَ تَكُمُ وَرِيشًا ۙوَلِبَاسُ

التَّقْوَىٰ ذَٰلِكَ خَيْرٌ ذَٰلِكَ مِّنْ ءَايَاتِ اللَّهِ لَعَلَّهُمْ يَذَّكَّرُونَ ۝

*Enyi wanadamu Hakika Tumekuteremshieni nguo zifichazo tupu zenu na nguo za pambo; na nguo za ucha-Mungu ndizo bora. Hayo ni katika (alama za) Mwenyezi Mungu ili wapate kukumbuka. (7:26).*

Aya hii inatukumbusha kuwa pamoja na vazi kuwa pambo kwa mwanadamu lengo lake ni kusitiri uchi na vazi linalositiri uchi kwa namna alivyoelekeza Mwenyezi Mungu na mtume wake ndilo vazi la ucha-Mungu. Kinyume na vazi la ucha-Mungu ni vazi la shetani ambaye daima anatushawishi kwenda uchi. Allah(s.w) anatushadharisha na Shetani katika aya ifuatayo:



يَبْنِي ۚ أَدَمَ لَا يَفْتِنَنَّكُمْ الشَّيْطَانُ كَمَا أَخْرَجَ أَبَوَيْكُمْ مِنَ الْجَنَّةِ يَنْزِعُ عَنْهُمَا لِبَاسَهُمَا لِيُرِيَهُمَا سَوْءَ تَمِيمًا ۗ إِنَّهُ يَرِيكُمْ هُوَ وَقَبِيلُهُ مِنْ حَيْثُ لَا تَرَوْنَهُمْ ۗ إِنَّا جَعَلْنَا الشَّيْطَانَ أَوْلِيَاءَ لِلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٧﴾

*Enyi wanadamu!, Shetani asikutieni katika matata, kama alivyowatoa wazee wenu katika pepo; akawavua nguo zao ili kuwaonesha tupu zao. Hakika yeye pamoja na kabila yake wanakuoneni na hali ya kuwa hamuwaoni. Bila shaka Sisi tumejaalia mashetani kuwa marafiki wa wale wasioamini. (7:27).*

Mavazi ya stara na heshima yanawahusu wote wanawake na wanaume kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

قُلْ لِلْمُؤْمِنِينَ يَغُضُّوا مِنْ أَبْصَارِهِمْ وَيَحْفَظُوا فُرُوجَهُمْ ۗ ذَٰلِكَ أَزْكَىٰ لَهُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا يَصْنَعُونَ ﴿٣٠﴾ وَقُلْ لِلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَارِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ ۗ..... ﴿٣١﴾

*“Waambie Waislam wanaume wainamishe macho yao na wazilinde tupu zao Na waambie Waislam wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao hili nitakaso kwao; bilashaka Mwenyezi Mungu anazo habari za wanayoyafanya. Na waambie waislamu wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao..... (24:30-31).*

## Mipaka ya Stara (Awrah) ya Mwanamume

Sitara au “awrah” ni neno lenye maana pana zaidi ya uchi. Ambapo uchi ni ile sehemu tu ya siri ya mwanamume au mwanamke, Awrah au Sitara ni sehemu yenye mipaka mipana zaidi. Awrah ya mwanamume ni kati ya kitovu na magoti. Hivyo uchi wa mwanamume katika maadili ya Kiislamu ni sehemu yote iliyo kati ya kitovu na magoti. Hivyo ni haramu kwa mwanamume kuacha wazi sehemu yoyote ile kati ya kitovu na magoti mbele ya mtu yeyote isipokuwa mkewe na yule iliyomiliki mikono yake ya kuume (mjakazi) na ni haramu pia yeye kuangalia uchi wa mtu mwingine kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Sehemu yoyote ile iliyo juu ya magoti haina budi kufunikwa na sehemu yoyote iliyo chini ya kitovu ni lazima ifunikwe. (Darqutny)*

*Mwanamume hana budi kufunika sehemu ya mwili wake iliyo kati ya kitovu na magoti. (Al-Nabsut).*

*Ali bin Abi Taalib (r.a) ameeleza kuwa Allah(s.w)amesema: Usifunue mapaja yako mbele ya mwingine wala usiangalie paja la mwingine akiwa hai au maiti. (Tasfiri-Kabiir).*

## Mipaka ya Stara (Awrah) ya Mwanamke

Mipaka ya sitara ya mwanamke, kutokana na umbile lake mipana zaidi kuliko ile ya mwanamume. Ambapo mipaka ya satar ya mwanamume ni kati ya kitovu na magoti, satar ya mwanamke ni mwili mzima isipokuwa uso na vitanga vya mikono. Wanawake wameamrisha kujisitiri hivi katika aya zifuatazo:

وَقُلْ لِلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَرِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَلْيَضْرِبْنَ خُمُرَهُنَّ عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ ..... ﴿٦٧﴾

*Na waambie waislamu wanawake wainamishe macho yao na wazilinde tupu zao wala wasidhihirishe viungo uyao isipokuwa vinavyodhihirika (uso na viganja vya mikono) na waangushe shungi zao (mitandio yao) mpaka vifuani mwao ..... (24:31)*

يَأْتِيهَا النَّبِيُّ قُلْ لِأَزْوَاجِكَ وَبَنَاتِكَ وَنِسَاءِ الْمُؤْمِنِينَ يُدْنِينَ عَلَيْهِنَّ مِنْ جَلِيبِهِنَّ ۚ ذَلِكَ أَدْنَىٰ أَنْ يُعْرَفْنَ فَلَا يُؤْذَيْنَ ..... ﴿٥٩﴾

*Ewe Mtume! Waambie wake zako na binti zako na wanawake wa Kiislamu wajiteremshie uzuri nguo zao(majalabibi yao). Kufanya hivyo kutawapelekea upesi wajulikane (kuwa ni watu wa heshima) wasibughudhiwe ..... (33:59).*

Allah(s.w) amezisherehesha aya hizi katika Hadith zifuatazo:

*Mtume(s.a.w)amesema; Si halali kwa mwanamke yeyote anayemuamini Allah(s. w) na Siku ya Mwisho kuacha wazi mkono wake zaidi ya hapa - kisha akaonyesha mkono wake mwanzo wa kiganja (wrist joint) (Ibn Jaryr). Mwanamke anapofikia baleghe hataiacha wazi sehemu yoyote ya mwili wake isipokuwa uso na viganja. (Abu Daud).*

Katika Hadith nyingine, Aisha(r.a) ameeleza kuwa alitokea mbele ya mpwa wake Abdullah bin Al-Tufail, akiwa amejipamba. Mtume(s.a.w) hakupendezewa. Aisha akasema: “Ewe Mtume wa Allah ni mpwa wangu”. Mtume(s.a.w) akasema:

*Mwanamke anapofikia baleghe si halali kwake kuiacha wazi sehemu yoyote ya mwili wake ila uso wake na hapa – kisha akashika sehemu ya ungio la kiganja cha mkono (wrist joint) kiasi cha kuacha sehemu ndogo kati ya hapo aliposhika na mwanzo wa kiganja. (Ibn Majah).*

Vazi linaloonesha (transparent) hata kama linafunika mwili mpaka kwenye mipaka ya awrah iliyowekwa, pia limeharamishwa katika Uislamu kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Aisha(r.a) amesimulia kuwa: wanawake katika ukoo wa bani Tamiimu walikuja (kwake Aisha) wakiwa wamevalia nguo nyepesi, Aisha akawaambia kama ninyi ni wanawake mlioamini kweli kweli, hizi si nguo za wanawake walioamini” Pia akasema alikuja bint kigori akiwa amevalia shungi na gauni linaloangaza, Aisha akamuambia; yeyote katika wanawake atakayeava hivi haamini yaliyoteremshwa katika suratun Nuur(Abuu Dawud)*

Pia vazi la Kiislamu halitakiwi likawa lenye kubana kiasi cha kuonyesha mchoro wa mwili:

*Umar(r. a) amesema: Msiwavalishe wake zenu nguo zinazobana kiasi cha kuonyesha makunjo yote ya mwili. (A I-Mabsuut).*

## **Kwa nini Stara zaidi Yatakikana kwa Mwanamke?**

Kutokana na mipaka ya stara ya wanawake na wanaume tuliyojifunza hapa tumeona kuwa sitara yatakikana zaidi kwa mwanamke kuliko kwa mwanamume. Kuna watu wanaopenda kujua kwa nini mwanamke anatakiwa ajisitiri mwili mzima wakati mwanamume anatakiwa ajisitiri sehemu tu ya mwili? Kwani wanawake nao pia wanaweza kuvutiwa na hizo sehemu za wanaume kama wao wanavyovutiwa na wanawake kwa kuangalia sehemu zao za mwili na ndio maana kwenye Qur’an wameamrisha wote kuinamisha macho yao na kulinda tupu zao. Lakini pamoja na ukweli huu si kweli kabisa kudai kuwa mvuto wa umbile la mwanamke kwa mwanamume ni sawa na ule wa umbile la mwanamume kwa mwanamke. Ukiwalinganisha na wanaume, wanawake wamejaaliwa sura nzuri zaidi na umbile la kuwavutia wanaume. Kwa mfano, katika hali halisi mwanamume anaweza kutembea bila shati maadam amejisitiri kati ya kitovu na magoti, lakini kama hali halisi ni viroja kwa mwanamke kutembea kifua wazi. Iivyo ni kwamba wanaume wanavutiwa kwa urahisi na umbo la mwanamke na wanawake ni wepesi kuhadaishwa na mapenzi ya wanaume. Kwa kuzingatia ukweli huu ndio Uislamu ukaweka mipaka ya stara na mahusiano kati ya wanaume na wanawake ili kuiepusha jamii na Zinaa. Jambo la kuzingatia na wenye kuuliza swali hili ni kwamba aliyetoa mipaka hii ya stara ya wanawake na wanaume ni Allah(s.w), Mjuzi, Mwenye hekima, Mwenye kujitosheleza na aliyemkamilifu ambaye hana sababu ya kumpendelea au kumwonea yeyote kati ya wanawake na wanaume. Bali ameweka mipaka hii ya stara kulingana na umbile la mwanamke na umbile la mwanamume. Hivyo, mwanamke Muislamu anapotekeleza amri hii ya kujisitiri Kiislamu asifanye hivyo kwa kuchelea kulaaniwa na jamii bali atekeleze agizo hili kwa sababu tu ni amri ya Allah(s.w). Kwa msimamo huu mwanamke Muislamu ataendelea kulitekeleza agizo hili hata kama mawazo ya jamii yatabadilika na kuanza

kudhani kuwa mwanamke kutembea uchi kwa kuvaa kaboka, mini-skirt, n.k. ndio alama ya maendeleo. Muislamu wa kweli hana hiari katika kutekeleza amri ya Allah(s.w) kama tunavyokumbushwa katika Qur'an:

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ  
الْخَيْرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾

*Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliye amini, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapo kata shauri, wawe na hiari katika shauri lao. Na Mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hakika amepotea upotofu ulio wazi. (33:36).*

Masharti ya stara hulegezwa kwa mwanamke anapokuwa nyumbani kwake au katika hadhara ya wanawake au hadhara ya maharimu wake (wale walioharamishwa kumuoa) kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

وَقُلْ لِلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَرِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ وَلَا  
يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا ۗ وَلْيَضْرِبْنَ بخُمْرِهِنَّ عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ ۗ  
وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا لِبُعُولَتِهِنَّ أَوْ آبَائِهِنَّ أَوْ آبَاءِ  
بُعُولَتِهِنَّ أَوْ أَبْنَائِهِنَّ أَوْ أَبْنَاءِ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ إِخْوَانِهِنَّ أَوْ بَنِي  
إِخْوَانِهِنَّ أَوْ بَنِي أَخَوَاتِهِنَّ أَوْ نِسَائِهِنَّ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُنَّ أَوْ  
التَّابِعِينَ غَيْرِ أُولِي الْإِرْبَةِ مِنَ الرِّجَالِ أَوِ الطِّفْلِ الَّذِينَ لَمْ يَظْهَرُوا  
عَلَىٰ عَوْرَاتِ النِّسَاءِ ۗ..... ﴿٣٧﴾

*Na waambie Waislamu wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, wala wasidhihirishe viungo vyao isipokuwa vinavyodhihirika. Na waangushe shungi zao mpaka vifuani mwao na wasionyeshe mapambo yao ila kwa waume zao, au baba zao, au baba za waume zao au watoto wao, au watoto wa wanaume zao, au kaka zao, au wana wa kaka zao, au wana wa dada zao, au wanawake wenziwao, au wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume, au wafuasi wanaume wasio na matamanio (kwa wanawake kama vile wazee) au watoto*

ambao hawajui mambo yanayohusu uke ..... (24:31).

Pia masharti ya stara yamelegezwa kwa wanawake vikongwe ambao hawavutii tena wanaume kama tunavyojifunza katika Qur'an.

وَالْقَوَاعِدُ مِنَ النِّسَاءِ الَّتِي لَا يَرَجُونَ نِكَاحًا فَلَيْسَ عَلَيْهِنَّ جُنَاحٌ أَنْ  
يَضَعْنَ ثِيَابَهُنَّ غَيْرَ مُتَبَرِّجَاتٍ بِزِينَةٍ وَأَنْ يَسْتَعْفِفْنَ خَيْرٌ  
لَهُنَّ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٦٠﴾

Na wanawake wenye kujiweka ambao hawatumaini tena kuolewa si vibaya kwao kupunguza baadhi ya nguo zao lakini bila ya kuonyesha mapambo yao. Na kama wakijizuia (kupunguza hizo nguo) ndio bora kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua. (24:60).

Aya hii inazidi kutuonyesha kuwa hekima ya wanawake kuamrisha kujisitiri kwa kujifunika mwili mzima ni kuzuia zinaa.

## (2) Kubisha Hodi.

Katika kuzuia kitendo kibaya cha zinaa Uislamu umewakataza Waislamu wanaume kuingia kwenye nyumba bila ya kuwatahadharisha wanawake waliomo ndani ili wasije wakawakuta katika hali isiyo ya stara. Qur'an inaanrisha:

وَإِذَا بَلَغَ الْأَطْفَالُ مِنْكُمُ الْحُلُمَ فَلْيَسْتَعِذُوا كَمَا اسْتَعِذَ الَّذِينَ  
مِنْ قَبْلِهِمْ كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٥٩﴾

Na watoto miongoni mwenu, watakapo baleghe basi na wabishe hodi kama walivyobisha hodi wale wa kabla yao. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu anavyokubainishieni aya zake. (24:59).

Hapa tunaona amri ya kubisha hodi inakuwepo baada ya kufikia baleghe. Pamoja na amri hii, watu wengine wasiokuwa wenyeji wa nyumba wanaamrisha kubisha hodi kabla hawajaingia katika majumba ya watu kama ifuatavyo:

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَدْخُلُوا بُيُوتًا غَيْرَ بُيُوتِكُمْ حَتَّى تَسْتَأْذِنُوا  
وَتُسَلِّمُوا عَلَى أَهْلِهَا ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٦١﴾

*Enyi mlioamini! Msiingie nyumba ambazo si nyumba zenu mpaka muombe ruhusa, na muwatolee salam waliomo humo. Hayo ni bora kwenu, huenda mtakumbuka. (24:27).*

Lengo la amri hii ni kuchunga stara na uhuru wa wakazi wa nyumba. Amri hi iliposhuka, baadhi ya watu hawakujua maana yake, kwa hiyo wakawa mara kwa mara wanachungulia dirishani ili kuwaangalia watu waliomo ndani. Siku moja wakati Mtume(s.a.w) alipokuwemo chumbani mwake, mtu mmoja alimchungulia dirishani ndipo Allah(s.w) akamwambia:

*Kama ningalijua kwamba unachungulia ningalisukumiza kitu jichoni mwako. Amri ya kubisha hodi imetolewa ili kuwahifadhi watu na mtazamo mbaya (kutizama visivyo ruhuswa). (Al-Bukhaary).*

Kisha Mtume(s.a.w) alitangaza hadharani:

Kama mtu atachungulia ndani ya nyumba ya mtu mwingine bila ya ruhusa, watu wa nyumba hiyo hawatalaumiwa iwapo watalitoboa jicho lake. (Muslim).

Pia tunaamrisha kwamba tukiwa na haja ya kitu katika nyumba ya mtu mwingine tusingie ndani moja kwa moja kuomba kitu hicho bali tuombe tukiwa nje au nyuma ya pazia:

..... وَإِذَا سَأَلْتُمُوهُنَّ مَتَعًا فَسْأَلُوهُنَّ مِنْ وَرَاءِ حِجَابٍ ذَلِكُمْ  
أَطْهَرُ لِقُلُوبِكُمْ وَقُلُوبِهِنَّ ..... ﴿٥٣﴾

*“.....Nanyi mnapowauliza (wanawake) waulizeni nyuma ya pazia. Kufanya haya kutasafisha nyoyo zenu na nyoyo zao ....(33:53).*

Aya hii inaonyesha wazi kuwa amri hii imewekwa ili kuzuia vishawishi vya zinaa kutokana na msemo “ ... kufanya haya kutasafisha nyoyo zenu na nyoyo zao ..... “ Yaani huwazuia wanaume na wanawake kuwa na fikra mbaya zitakazo wapelekea kwenye zinaa.

### **(3) Makatazo ya Kuwashika Wanawake na Kukaa Faragha Nao.**

Kuwashika wanawake wasiomaharimu au kukaa faragha nao ni haram katika Uislamu kwani ni vishawishi vikubwa vya zinaa. Imepokelewa kwa Uqbah bin Amir kuwa Mtume(s.a.w) amesema:

*Tahadhari kumwita mwanamke faraghani. Ansvar mmoja akauliza: Ewe Mtume wa Allah, vipi kwa kaka au mdogo wa mume wangu (vipi kwa shemeji yangu)? Mtume wa Allah(s.w) akasema: “Amekufa!” (Bukhaary, Muslim na Tirmidh).*

Pia Mtume(s.a.w) ameonya:

*Msiwatembelee wanawake waume zao wakiwa hawapo kwa sababu Shetani anaweza kuzunguka ndani ya yoyote kati yenu kama damu inavyozunguka mwilini. (At-Tirmidh).*

*Kutoka kwa Amr bin As, Allah(s.w) amewakataza waume kuwaita au kuwatembelea wanawake bila ya ruhusa ya waume zao. (Tirmidh).*

Pia Mtume(s.a.w) kasema:

*Kuanzia leo, hapana mwanamume anayeruhusiwa kumtembelea mwanamke atakapokuwa hayupo mume wake mpaka atakapokuwa ameongozana na mtu mwingine, mmoja au wawili. (Muslim).*

Uharamu wa kumshika mwanamke asiye kuwa mke au maharimu, umedhihirika katika Hadith zifuatazo: Allah(s.w) amesema:

*Atakayeshika kiganja cha mwanamke asiye kuwa maharimu wake Siku ya Kiyama atawekewa kaa la moto juu ya kiganja chake (Tirmidh, Fat-h al-Qdr). Aysha(r.a) amesema kuwa Mtume(s.a.w) alipokea kiapo cha utii (Bai'ah) kutoka kwa wanawake bila ya kuwashika mikono. Hajawahi Mtume(s.a.w) kushika kiganja cha mwanamke ambaye si mke wake. (Bukhaary).*

*Umaimah bint Ruqaiyah) amesimulia kuwa alikwenda kwa Mtume wa Allah(s.w) akiwa ameongozana na wanawake wengine kutoa kiapo cha utii (Bai'ah). Mtume(s.a.w) aliwataka waahidi kuwa watajiepusha na ushirikina wizi uziniju, fitna na kumuasi Mtume. Walipochukua kiapo walimuomba awashike mkono iwe alama ya ahadi yao. Mtume(s.a. w) alisema: Sishiki mkono wa mwanamke. Makubaliano ya mdomo yanatosha. (Nasai Ibn Majah).*

### **(iii) Adhabu ya Uzinifu**

Katika Sheria ya Kiislamu mtu haadhibiwi mpaka atende kwa uwazi matendo yenye kuvuruga utaratibu na amani ya jamii. Mtu hataadhibiwa mpaka upatikane ushahidi wa wazi na wakutosha. Kwa upande mmoja, Sheria ya Kiislamu imeweka masharti magumu sana ya ushahidi wa makosa ya jinai, bali ushahidi wa kosa la zinaa ni mgumu zaidi. Ambapo mashahidi wa makosa yote ya jinai ni wawili, mashahidi wa zinaa ni wanne walioshuhudia kwa macho yao wakati kitendo kinafanyika. Ushahidi katika sheria ya Kiislamu umewekewa masharti magumu ili kuwaokoa watu na hatia ya kuadhibiwa kwa makosa. Imesimuliwa na Aysha (r.a) kuwa Mtume(s.a.w) amesema:

*Walindenii Waislamu kwa kila iwezekanavyo na matumizi ya Sheria dhidi yao. Mwachenii mkosaji atoke katika hatia kama atakuwa na haki ya kutoka. Kwa kiongozi kufanya kosa la kumsamehe mtu aliye na hatia ni bora kuliko kukosea kumuadhibu mtu asiye na hatia. (A t - Tirmidh).*

Kwa upande mwingine, mara tu ushahidi wa kutosha utakapopatikana dhidi ya mkosaji, Sheria ya Kiislamu itatoa adhabu kali sana ambayo haitamzuia tu muhalifu na kuendelea na kosa hilo, bali itawazuilia maelfu ya watu wengine ambao wangaliendea kosa hilo. Lengo la sheria ya adhabu katika Uislamu ni kuitakasa jamii na maovu na wala si kuwashawishi watu wafanye kosa na kuendelea kuwaadhibu tena na tena. Zinaa ni kitendo kiovu chenye kuathiri mno jamii. Mtu anayefanya kosa hili anauhakikishia ulimwengu kuwa unyama wake umemtawala kwa kiasi kwamba hastahiki kuishi katika jamii ya binadamu. Jamii ya wazunifu ni jamii duni kuliko jamii ya hayawani kimaadili. Kwa mtazamo huu, Sheria ya Kiislamu imetoa adhabu kali kwa wazunifu kama inavyobainishwa katika Qur'an:

الزَّانِيَةُ وَالزَّانِي فَاجْلِدُوا كُلَّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا مِائَةَ جَلْدَةٍ وَلَا تَأْخُذْكُم بِهِمَا رَأْفَةٌ فِي دِينِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَلَيْشَهَّدَ عَلَيْكُمَا طَائِفَةٌ مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٤﴾

Mzunifu mwanamke na mzunifu mwanamume mpigeni kila mmoja katika wao mijeledi (bakora) mia. Wala isiwashikeni kwa ajili y'ao huruma katika (kupitisha) hukumu hii ya Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi mnamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Na lishuhudie adhabu yao hii kundi la Waislam. (24:2).

Adhabu hii kulingana na Hadith ni kwa wale ambao hawajawahi kuoa au kuolewa. Baada ya kuchapwa viboko mia hutengwa na miji yao kwa muda wa mwaka mmoja kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

Ubadah bin Swamit ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Nisikilizeni, nisikilizeni. Hakika Allah ametoa adhabu kwa mzunifu mwanamke ambaye hajapata kuolewa na mzunifu mwanamume ambaye hajapata kuoa ni viboko 100 na kuhamishwa mjini kwa mwaka mmoja. Na adhabu ya mzunifu aliyeoa na aliyeolewa ni viboko 100 na kupigwa mawe mpaka kufa. (Muslim).

Hadith hii pia imetufahamisha kuwa adhabu ya mzunifu mwanamke aliyeolewa au aliyewahi kuolewa au mzunifu mwanamume aliyeoa au aliyewahi kuoa ni kifo kwa kupigwa mawe. Katika Hadith nyingine tunajifunza kuwa Mtume wa Allah(s.w) na Makhalifa wake walitoa adhabu hii kwa watu mbali mbali waliofanya kitendo hiki cha kinyama kidhalilishacho jamii. Miongoni mwa Hadith hizo ni hii ifuatayo:

Ibn Abbas ameeleza kuwa Ma'z bin Malik alikuja kwa Mtume wa Allah(s.w) akasema kuwa amezini. Allah(s.w) akamwambia: Labda umebusu, au umeshika au umeangalia tu. Akajibu (Ma'z): «Hapana, Ewe Mtume wa Allah».



*Akamuuliza tena Mtume: Umezini na yeye? Akajibu; 'Ndio'. Kisha Mtume alitoa amri apigwe mpaka afe. (Bukhaary)*

Sheria ya Kiislam ya adhabu ya mzinifu inatofautiana mno na sheria za jamii nyingine. Kwa mfano sheria ya Uingereza (British Law) ambayo ndiyo iliyorithiwa na nchi zote zilizotawaliwa na Uingereza na nchi yetu hii ikiwemo, haichukulii kitendo cha uzinifu chenyewe kama kilivyo kuwa ni kosa, bali kosa linapatikana pale kitendo hicho kitakapo fanywa kwa kumshika mwanamke kwa nguvu (ubakaji) au kitakapofanywa na mke wa mtu bila ya ridhaa yake au kwa hapa kwetu kitakaposababisha mimba kwa mtoto wa shule. Kwa maana nyingine katika sheria ya nchi uzinifu sio kitendo kiovu bali kina kuwa kiovu tu pale kitakapofanywa kwa nguvu au kitakapoathiri haki za wengine. Kutokana na mtazamo huu sheria ya adhabu ya uzinifu ya nchi . ni lazima itofautiane sana na sheria ya Kiislamu dhidi ya kosa hili katika sheria ya nchi, adhabu ya ubakaji ni kifungo cha miaka thelathini (30), adhabu ya kukamatwa ugoni ni kumlipa fidia yule mume aliyeziniwa mkewe na adhabu ya kumtia mtoto wa shule mimba ni kumuoa au kumlea mtoto mpaka aweze kujitegemea. Adhabu kama hizi haziwezi kamwe kukomesha uzinifu bali huzidi kuupalilia. Kwa mfano, ukimtaka mke wa mtu ni kiasi cha kumuendea na kuwa tayari kumlipa mumewe fidia. Ni katika mtizamo huu zinaa imekuwa ni mtindo wa maisha na kitendo cha maendeleo katika jamii zetu hizi. Sera za kudhibiti uzazi zimewekwa katika jamii mbali mbali ili zinaa iendelee pasina kutokea mimba zisizohitajika.

Kinyume na mtazamo wanchi juu ya zinaa, katika maadili ya Kiislamu zinaa ni kitendo kiovu mno kinachoidhalilisha jamii na kuivuruga. Ni katika mtizamo huu, sheria ya Kiislamu imetoa adhabu kali sana kwa wazinifu ili iwe onyo kali kwa wakosaji na kwa jamii nzima kwa ujumla. Ndio maana katika nchi zinazosimamisha sheria hii huoni uzinifu kuwa mtindo wa maisha na hupati watu wanaougua magonjwa ya zinaa kama huu ugonjwa wa UKIMWI (AIDS). Utakuta ugonjwa wa UKIMWI umejizatiti katika maeneo yale ambayo zinaa imefanywa mtindo wa maisha.

## **Adhabu kwa Wenye Kuwasingizia Wanawake Watahirifu kuwa Wamezini.**

Kitendo chakuwasingizia wanawake watwaharifu kuwa wamezini nacho ni kitendo kiovu mno chenye kuivuruga jamii, kwani kumsingizia mwanamke uzinifu hakuishii tu kwenye kumvunjia heshima na hadhi yake bali huwahusu wazazi, ndugu, jamaa na marafiki. Wote wanaomuhusu huvurugikiwa na mawazo na imani yao juu yake hupungua na unyumba huvunjika. Tunajifunza katika Qur'an na Hadith kuwa jamii ya Mtume wa Allah(s.w) ilivurugikiwa na kuyumba wakati mke wa Mtume, Aisha(r.a), aliposingiziwa kuwa amezini na swahaba mmoja. Maonyo makali na makemeo kwa jamii kutoka kwa Allah (s. w) juu ya kitendo hiki kiovu tunayapata katika Qur'an, sura ya 24 aya 10-20. Kutokana na ubaya

wa kitendo hiki cha kuwasingizia wanawake wataharifu kuwa wamezini, Sheria ya Kiislamu inatoa adhabu kali sana kwa wahalifu kama inavyobainishwa katika aya ifuatayo:

وَالَّذِينَ يَرْمُونَ الْمُحْصَنَاتِ ثُمَّ لَمْ يَأْتُوا بِأَرْبَعَةِ شُهَدَاءَ فَاجْلِدُوهُمْ  
 ثَمَّسِينَ جَلْدَةً وَلَا تَقْبَلُوا لَهُمْ شَهَادَةً أَبَدًا وَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٤٤﴾

*Na wale wanaowasingizia wanawake watwaharifu (kuwa wamezini) kisha hawaleti mashahidi wanne basi wapigeni mijeledi (bakora) thamanini na msiwakubalie ushahidi wao tena) na hao ndio mafasiki (24:4).*

## Zoezi 2:5

1. Linganisha na tofautisha hadhi ya mwanamke kwa msimamo wa Biblia na ule wa Qur'an.
2. Mwanamke si sawa na mwanaume, bali ni viumbe wenye hadhi sawa, wanaotegemeana. Jadili.
3. Tatizo la mwanamke kuonewa, kunyonywa, kudhalilishwa na kunyimwa haki zake halipo kabisa katika mfumo wa maisha wa Kiislamu. Thibitisha.
4. Mungu "Akamwambia mwanamke, Hakika nitakuzidishia uchungu wako, na kuzaa kwako; kwa utungu utazaa watoto; na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala (Mwanzo 3:16) Mwanamke na ajifunze katika utulivu, akitii kwa kila namna. Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala mwanamume, bali awe katika utulivu. (1 Timotheo 2:11-12)

Enyi wake, watiini waume zenu...wake nao wawatii waume zao katika kila jambo. (waefezo 5:22-24).

Wanawake...wakitaka kujifunza neno lolote, na wawaulize waume zao wenyewe nyumbani mwao; maana ni aibu mwanamke kunena katika kanisa. (1 wakorintho12:34-35) Mwanamke hufungwa maadamu mume yu hai, lakini ikiwa mumewe amefariki, yu huru kuolewa na mtu yeyote amtakaye; katika Bwana tu. (1wakorintho12:39) Kwa kuzingatia mafundisho ya maandiko haya ya Biblia; ni haki zipi alizopewa mwanamke au kunyimwa?

5. Mwanamke katika jamii zisizofuata mfumo wa maisha wa kiislamu, ni kitega uchumi, kiburudisho na nguvukazi ya bei poa kwa mwanaume. Unasemaje?

## MISINGI YA MAADILI KATIKA UISLAMU

### Binadamu si Mnyama

Mtu ni kiumbe tofauti na viumbe wengine, hata wale waliokaribiana kimaumbile katika kundi la mamalia (mammals). Pamoja na makafiri kudai kuwa asili ya mtu ni jamii ya masokwe kwa kuwa wanakaribia kufanana kimaumbile, wametafautiana mno. Tofauti hii inatokana na vipawa maalum alivyotunukiwa mtu ukilinganisha na vipawa vya wanyama. Vipawa hivi humfanya mwanadamu aunde au kufuata maadili fulani, jambo ambalo wanyama hawana. Vipawa hivi ni:

1. **Akili** yenye kumuwezesha kutafakari juu ya mambo mbali mbali.
2. **Kujitambua** (Self consciousness) kunakomuwezesha mtu kujua mahusiano yake na mazingira yake.
3. **Elimu** yenye kumuwezesha kuendesha maisha yake hapa ulimwenguni kwa wepesi na kwa ufanisi.
4. **Uhuru** wa kuchagua na kutenda alitakalo ndani ya kanuni za maumbile:

Vipawa hivi humfanya mtu mwenye akili timamu ajiulize maswali mengi ya msingi kama vile, nini chanzo cha ulimwengu na vyote vilivyomo, nini kusudio la kuwepo watu na maumbile yote yaliyowazunguka, ni ipi hatima ya ulimwengu na vyote vilivyomo, n.k. Mwenendo wa tabia ya mtu itategemeana na majibu atakayoyapata kutokana na maswali hayo ya msingi. Akipata majibu sahihi ataweza kuishi maisha mazuri yenye kulingana na lengo la kuumbwa kwake. Kwa hakika majibu sahihi atayapata kutoka kwa yule aliye Muumba yeye pamoja na maumbile yote yaliyomzunguka. Anapaswa kumtambua Muumba wake kwa kutumia vipawa hivi vya ziada alivyotunukiwa kama inavyosisitizwa katika Qur-an:

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَأَخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ لَآيَاتٍ لِّأُولِي

الْأَلْبَابِ ﴿١٩٠﴾

*Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na mfuatano wa usiku na mchana, ziko hoja (za kuonyesha kuwapo Mwenyezi Mungu mmoja), kwa wenye akili. (3:190)*

الَّذِينَ يَذْكُرُونَ اللَّهَ قِيَمًا وَقُعُودًا وَعَلَىٰ جُنُوبِهِمْ وَيَتَفَكَّرُونَ فِي خَلْقِ

السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ رَبَّنَا مَا خَلَقْتَ هَذَا بَطْلًا سُبْحَانَكَ فَقِنَا عَذَابَ

النَّارِ ﴿١٩١﴾

*Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa na wakilala. Na hufikiri umbo la mbingu na ardhi (kisha) wakasema “Mola wetu! Hukuviumba hivi bure. Utukufu ni wako. Basi tuelepe na adhabu ya Moto.” (3:191)*

Kwa mujibu wa aya hizi, kinachofuatia baada ya mtu kumtambua Muumba, ni kufuata mwongozo wake katika kila kipengele cha maisha.

Endapo binadamu atatumia vipawa vyake vya akili, utambuzi wa ubinafsi, elimu na uhuria kwa kufuata msukumo wa matashi yake atapotea njia na kuishi maisha yasiyo na muelekeo na atakuwa na mwenendo na tabia iliyochupa utu inayompelekea kufanya mambo maovu na duni kuliko yale yanayofanywa na wanyama. Juu ya hili Muumba wetu karimu anatutanabahisha:

وَلَقَدْ ذَرَأْنَا لِجَهَنَّمَ كَثِيرًا مِّنَ الْإِنسِ ۖ لَهُمْ قُلُوبٌ لَا يَفْقَهُونَ بِهَا ۖ وَهُمْ أَعْيُنٌ لَا يُبْصِرُونَ بِهَا ۖ وَهُمْ ءَاذَانٌ لَا يَسْمَعُونَ بِهَا ۚ أُولَٰئِكَ كَالْأَنْعَامِ بَلَّ هُمْ أَضَلُّ ۚ أُولَٰئِكَ هُمُ الْغَافِلُونَ ﴿١٧٦﴾

*“Na bila shaka tumewaumbia Moto wa Jahannamu wengi katika majini na watu (kwa sababu hii): Nyoyo (akili) wanazo, lakini hawafahamu kwazo, na macho wanayo lakini hawaoni kwayo, na masikio wanayo lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama wanyama, bali wao ni wapotofu zaidi. Hao ndio walioghafilika.”(7:179)*

Inadhihirika bayana kuwa pamoja na maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia, amani katika maisha ya hivi leo chini ya mfumo wa kitwaghutii (mfumo unaochupa mipaka ya utu aliyoiweka Muumba), imetoweka kabisa, na dhuluma imeshamiri. Kutoa na kupokea rushwa ndio mtindo wa maisha; ujambazi na uporaji umeongezeka kitaifa na kimataifa; familia zinavunjika na ufuska kustawi; vijana wengi wametumbukia katika unywaji pombe, uvutaji bangi, utumiaji wa madawa ya kulevya na kupoteza kabisa dira ya maisha yao; ukweli na uaminifu vimekuwa vitu adimu, ambapo fitina na propaganda za uwongo uliokithiri vimeshamiri katika vyombo vya habari kitaifa na kimataifa.

Ukatili wanaofanyiana binadamu hivi leo ni wa kutisha kiasi ambacho mwanafalsafa mmoja wa Kiingereza aitwaye *Bertrand Russell* alifikia kusema kuwa si haki kabisa kumnasibisha binadamu na mnyama kwa sababu mnyama anatabia nzuri sana kuliko binadamu! Mara nyingi mnyama akiua, hua kwa haja ya chakula cha wakati huo huo na si kuzusha vita isiyoyote na maana yoyote na kuu mamiloni ya watu wasio na hatia.

Mauwaji ya halaiki yaliyofanywa na Majeshi ya Marekani na Washirika wake dhidi ya wananchi na raia wa Afghanistan na Iraq, pamoja na unyama wa Serikali ya Israil dhidi ya Wapalestina, ni ushahidi wa alichokisema *Russell*.

Akijadili juu ya maadili ya binadamu yalivyo katika ulimwengu huu wa maendeleo ya sayansi na teknolojia, mwanafalsafa mwingine Harold H. Titus ameamdika:

*“Mlolongo wa matukio katika miaka ya hivi karibuni umedhihirisha wazi kuwa kuna jambo lililokwenda kombo katika maisha ya binadamu. Binadamu amejipatia uwezo mkubwa mpya katika nyanja za sayansi na teknolojia, lakini mara nyingi uwezo huo umetumika katika njia za uharibifu. Binadamu amepanua upeo na ubora wa ujuzi wake, lakini amepiga hatua ndogo sana, kama basi amepiga hatua yoyote, katika kujiletea furaha na amani”.*

Aidha, mwanasaikologia aitwaye F.S.C. Northrop, naye anaishangaa hali hii ya maadili na kuandika:

*“Ulimwengu wetu ni wa kitendawili. Mafanikio ambayo ndio fahari yake yanatishia kuuangamiza... yaelekea kila tunapopiga hatua ya maendeleo ndivyo tunavyoshindwa kudumisha ustaarabu”.*

Wanafalsafa hawa wangelikuwa Ulul-albaab (wenye akili) na kumtambua Muumba wao, wasingeliishangaa hali hii kwani imedhihirishwa na Muumba Karimu tangu karne ya sita (A.D.), pale Mtume Muhammad(s.a.w) aliposhushiwa wahyi wa Qur-an:

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ ﴿١﴾ ثُمَّ رَدَدْنَاهُ أَسْفَلَ سَافِلِينَ ﴿٢﴾  
إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَلَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ ﴿٣﴾

*Bila shaka TumeMuumba mwanadamu kwa umbo lililobora kabisa. Halafu tukamrudisha kuwa chini kuliko walio chini. Ila wale wenye kuamini na kutenda mema, watakuwa na ujira usiokwisha, (unaendelea maisha) (95:4-6)*

Aya hizi zinatukumbusha kuwa pamoja na binadamu kuumbwa katika umbo bora na kutunukiwa vipaji alivyo navyo hawezi kuwa na mwenendo na tabia njema mpaka awe amemtambua na kumuamini Mola wake Muumba na kufuata mwongozo wake pekee katika kuendesha maisha yake ya kila siku ya kibinafsi na kijamii huku akitarajia kupata radhi zake na malipo kutoka kwake katika maisha ya hapa duniani na ya kesho akhera.

## **Mtizamo wa Kikafiri juu ya Maadili**

Maadili ni mwenendo mwema unaombakisha binadamu katika hadhi yake na kumfikisha katika lengo la kuumbwa kwake. Katika jitihada za kumfanya binadamu awe na tabia ya kufanya mema na kuacha maovu ili kuleta furaha na amani katika jamii, baadhi ya wanafalsafa wa kikafiri wanauliza na kujaribu kutoa majibu ya maswali makuu manne yafuatayo:

1. Ni kitu gani ambacho ndicho lengo kuu la maisha?
2. Zipi chem chem, tunazozitegemea katika ujuzi wetu juu ya mema na maovu? Yaani tutajuaje kuwa jambo fulani ni baya au zuri? Tunapata kutoka wapi habari hizi za mema na maovu?
3. Ni nani msimamizi wa mwenendo wa tabia ya binadamu? Yaani ni mamlaka ipi yenye kuhakikisha kuwa watu wanakuwa waadilifu?
4. Ni kitu gani kinachowasukuma watu wafuate mwenendo fulani wa tabia? Wanahamasishwa na nini?

Hebu tupitie majibu wanayotoa wanafalsafa na udhaifu wa majibu hayo:

## **1. Lengo Kuu la Maisha kwa Mtazamo wa Makafiri**

Katika kujibu swali la kwanza “Ni lipi lengo kuu la maisha yetu”, wanafalsafa wa kikafiri wamegawanyika katika makundi mengi miongoni mwa hayo ni haya matatu.

Kundi la kwanza linasema lengo kuu la maisha yetu hapa duniani ni kuishi maisha yenye furaha. Hivyo basi jambo lolote linalotuongezea furaha yetu ni jema na lolote lile linalotuletea machungu, huzuni, na majonzi ni ovu.

Kundi la pili linasema lengo kuu la maisha yetu hapa duniani ni kufikia utimilifu (perfection). Hivyo kitendo chochote kinachopelekea katika kukuza na kukamilisha vipawa vyetu ni kitendo chema na jambo lolote linalokwaza na kuviza vipawa vyetu visifikie kilele cha ukamilifu wake ni jambo ovu.

Kundi la tatu linasema lengo kuu la maisha haya ni kuwa kila mtu atimize wajibu wake kwa madhumuni ya kutimiza wajibu tu basi (duty for the sake of duty). Hivyo jambo lolote linalomfanya mtu atimize wajibu wake bila ya kutarajia chochote ni jema na kila linalomzuia kutimiza wajibu wake kwa madhumuni tu ya kutimiza wajibu basi ni ovu.

### ***Udhaifu wa majibu hayo***

Tukichunguza majibu ya wanafalsafa wa kikafiri juu ya lengo la maisha, tunaona kuwa yanapwaya sana.

Tukianza na jibu la kwanza linalosema kuwa furaha ndio lengo kuu la maisha yetu hapa duniani, maswali kadhaa yanazuka. Ni furaha ya aina gani hiyo inayotafutwa? Ni furaha anayoihisi mtu baada ya kutosheleza matamano yake ya kimwili au ni furaha inayotokana na kujifaharisha? Ni furaha itokanayo na kutathmini kazi za sana au furaha ya kiroho? Ni furaha ya nani inayotafutwa, ya mtu binafsi au ya jamii ambamo anaishi? Au furaha ya watu wote au ni furaha ya kikundi cha watu tu?

Tukichukua jibu la pili lisemalo kuwa lengo kuu ni kufikia utimilifu, pia yanajitokeza maswali kadhaa. Nini maana ya utimilifu? Ni kipi kipimo cha utimilifu? Ni utimilifu wa nani unaotafutwa wa tabaka au kikundi alichu mtu au wa mtu binafsi au wa jamii?

Vivyo hivyo tukichukua jibu la tatu lisemalo lengo kuu ni kutimiza wajibu kwa lengo tu la kutimiza wajibu, hatuwezi kuepuka maswali haya: Lengo hili maana yake ni nini hasa? Nani aliyeliweka? Nini hekima ya kulifuata?

## 2. Utambuzi wa Mema na Maovu kwa Mtizamo wa Makafiri

Katika kujibu swali la pili, “zipi chem chem. (sources of knowledge) tunazozitegemea katika ujuzi wetu juu ya mema na maovu, wanafalsafa wamegawanyika makundi matatu vile vile.

Kundi la kwanza, linasema uzoefu wa binadamu (human experience) ndio chem chem pekee ya hakika inayomuwezesha mtu kujua lipi jema na lipi ovu. Rai hii hujulikana kama “*empiricism*” katika lugha ya Kiingereza. Kwa mujibu wa rai hii tunajua kuwa jambo fulani ni baya kwa sababu katika maisha yetu ya kila siku uzoefu wetu umetuonyesha kuwa jambo hilo lina madhara fulani kwetu.

Kundi la pili, linasema kinachotujulisha kuwa jambo fulani ni zuri au baya ni silka zetu (*intuition*). Na rai hii hujulikana kama “*intuitionism*” kwa lugha ya Kiingereza.

Kundi la tatu, linasema kuwa kinachotuwezesha kupambanua zuri na baya ni kipawa cha kufikiri na kuhoji au “*Rationalism*” kama rai hii inavyojulikana kwa Kiingereza.

### *Udhaifu wa Makafiri juu ya Chem chem ya Ujuzi wa Wema na Uovu*

Iwapo tutazifanya rai hizo za makafiri kuwa ndio chem chem ya ujuzi wa mema na maovu, tutajikuta katika hali ya kutatanisha sana. Jema la asubuhi laweza kuwa ovu la jioni na kinyume chake.

Kasoro za rai kuwa, “chem chem ya ujuzi juu ya wema na ovu ni uzoefu” ni hizi zifuatazo:

**Kwanza**, inabidi watu wasubiri mpaka kiyama ndio wang’amue kuwa jambo fulani lilikuwa baya au zuri ili upatikane uzoefu wa watu wote na halafu uzoefu huo uchambuliwe na kutafsiriwa kwa ufasaha bila upendeleo wowote. Hii ina maana kuwa watu itabidi wasubiri mpaka siku ya kiyama kabla ya kujua kuwa jambo fulani ni baya au zuri. Na zaidi hakuna mtu anayeweza kuatafsiri uzoefu wa watu wote kwa usahihi bila ya upendeleo.

**Pili**, uzoefu wowote alionao binadamu leo umegawanyika katika fani chungu nzima za Elimu na mabingwa wa kila fani wanautafsiri uzoefu wao kulingana na mwangaza wa taaluma zao. Tuchukue uzoefu wa nani katika kuamua lipi ni jema na lipi ovu? Na kama kila mtu afuate uzoefu wake basi hapatakuwa na jambo lolote ambalo tunaweza kusema ni jema au baya, kwa mfano, wizi ni jambo baya, mwizi atasema hapana, uzoefu wangu unanionesha kuwa nikiiba nakula na kustarehe bila ya kuhangaika huku na huko!

Halikadhalika kutegemea hoja, akili na silka kuna matatizo kama hayo. Hapana shaka yoyote kuwa kipaji cha akili ni hazina kubwa yenye manufaa mengi na kiongozi kikubwa katika maisha yetu na husaidia kuturekebisha katika namna mbali mbali. Lakini katika suala hili haitufikishi popote. Kwanza lina zuka swali lile lile: Je, tuitegemee akili ya nani? Akili yangu au yako au ya huyu au ya yule? Au tutegemee akili ya kikundi Fulani cha watu au ya watu wote au ya watu wa kizazi hiki au kilichopita au cha baadaye?

**Tatu**, swali zito zaidi ni kama akili ya binadamu peke yake haiwezi kufanya kazi hiyo, kwa sababu lipo suala la upendeleo na chuki ambalo huipotosha akili. Athari za hisia, harara za maono, dhana za awali na sababu za kimakuzi au za kimazingira juu ya akili haziwezi kupuuzwa. Kutokana na udhaifu huu si busara kuifanya akili na silka kuwa chem chem za ujuzi juu ya mema na maovu.

### 3.Msimamizi wa Maadili kwa Mtizamo wa Makafiri

Katika kujibu swali la tatu, “*Ni nani msimamizi wa tabia ya binadamu?*”, wanafalsafa wa kikafiri wametofautiana pia.

Kundi la **kwanza** linasema kuwa maadili ya jamii yatasimamiwa na lengo tarajiwa. Yaani kama lengo kuu ni “furaha” basi ni kule kupatikana kwa furaha ndiko kutakako simamia maadili ya jamii.

Kundi la **pili**, linasema msimamizi ni kitu wanachokiita “law of practical reason”, yaani “kanuni zinazooana na hoja”. Rai hii inafanana na ile ya “Rationalism” ya kutumia akili.

Kundi la **tatu**, linasema msimamizi ni serikali kwa kutumia askari polisi, mahakama na magereza.

Kundi la **nne**, linasema msimamizi ni maoni ya watu katika jamii hiyo hiyo yaani “Social pressure”.

### 4.Motisha wa Kufuata Maadili kwa Mtizamo wa Makafiri

Katika kujibu swali la nne, “Ni kitu gani kinachowasukuma wawe na maadili wafuate maadili ya jamii, baadhi ya wanafalsafa wanasema ni katika



maumbile ya binadamu kutii na kuheshimu sheria. Lakini tunaona siku hizi watu wanavyoshindana kuvunja sheria!

Kundi la pili la wanafalsafa linadai kuwa kinachomsukuma mtu kufuata maadili ya jamii ni kutaka malipo na kuepukana na adhabu (Reward and Punishment). Swali linakuja: “Ni nani anayetoa malipo au adhabu hiyo?” Wengine wanasema ni dola au serikali na wengine wanasema ni jamii anamoishi mtu.

Itadhihirika wazi kuwa majibu yanayotolewa na wanafalsafa wanaojaribu kusimamisha maadili ya jamii kwa misingi ya kikafiri yanapwaya na hutatanisha sana. Hata hivyo haina maana kuwa yote yaliyosemwa na wanafalsafa hawa ni upuuzi usiokuwa na ukweli wowote. Zipo chembe chembe za ukweli hapa na pale lakini bila kudhibitiwa na mfumo sahihi hoja zao zinaelea tu angani. Dosari kubwa kupita zote katika jitihada zao ni kule kumtaka binadamu awe muadilifu bila kwanza kumuamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho.

## Mtizamo wa Uislamu Juu ya Uadilifu

Kosa kubwa walilolifanya wanafalsafa wa kikafiri katika jitihada za kuchunguza mwenendo wa tabia ya binadamu ni kule kuanzia utafiti wao katikati badala ya kuanzia mwanzo. Kabla ya kuingia kwenye yale maswali manne, walitakiwa waulize na kuyatafutia majibu sahihi maswali mawili ya kwanza ya msingi yafuatayo:

1. Nini chanzo cha binadamu? Yaani binadamu ametokea wapi au “Nani aliyemfanya akawepo?”
2. Ni ipi hadhi na nafasi ya binadamu katika ulimwengu huu?

Katika kujibu swali la kwanza tunajifunza katika Qur-an kuwa binadamu ni kiumbe wa Mwenyezi Mungu aliyetukuzwa:

وَلَقَدْ خَلَقْنَاكُمْ ثُمَّ صَوَّرْنَاكُمْ ثُمَّ قُلْنَا لِلْمَلَكِئَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ  
فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ لَمْ يَكُنْ مِنَ السَّاجِدِينَ ﴿١٦﴾

“Na hakika tulikuumbeni, kisha tukakutieni sura, kisha tukawaambia malaika: “Msujudieni Adamu” Basi wakasujudu isipokuwa Ibilis hakuwa miongoni mwa waliosujudu.” (7:11)

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَكِئَةِ إِنِّي خَلَقْتُ بَشَرًا مِّنْ صَلْصَلٍ مِّنْ حَمَإٍ مَّسْنُونٍ  
فَإِذَا سَوَّيْتُهُ وَنَفَخْتُ فِيهِ مِنْ رُّوحِي فَقَعُوا لَهُ سَاجِدِينَ ﴿١٧﴾

“Na (kumbuka) Mola wako alipowaambia Malaika, hakika Mimi nitaMuumba mtu kwa udongo mkavu unaotoa sauti; wenye kutokana na matope meusi yaliyovunda. Basi nitakapomkamilisha na kumpulizia roho inayotokana na Mimi basi mumuangukie kwa sijida (kuonyesha utii wenu)” Basi Malaika wakamsujudia wote pamoja.” (15:28-30)

Kuhusu hadhi na nafasi ya binadamu hapa ulimwenguni tunajifunza katika Qur-an kuwa yeye ni Khalifa au balozi (mwakilishi) wa Mwenyezi Mungu hapa ulimwenguni anayepaswa kuuongoza kwa uadilifu kwa kufuata mwongozo wa yule aliyemteua kuwa balozi hapa. Kuhusu nafasi hii ya mwanadamu Qur-an inatukumbusha:

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلٰٓئِكَةِ اِنِّىْ جَاعِلٌ فِى الْاَرْضِ خَلِيْفَةً..... ﴿٢٠﴾

“(Wakumbushe) wakati Mola wako alipowaambia Malaika: ‘Mimi nitaleta Khalifa katika ardhi...’ (2:30)

Ili kumuwezesha binadamu kuchukua nafasi yake hapa ardhini, Allah(s.w) amemtunuku elimu ya mazingira yake pamoja na mwongozo utokao kwake kupitia kwa Mitume wake na vitabu vyake kama tulivyojifunza katika aya zifuatazo:

وَعَلَّمَ اٰدَمَ الْاَسْمَاءَ كُلَّهَا..... ﴿٣١﴾

“Na (Mwenyezi Mungu) akamfundisha Adamu majina ya vitu vyote...” (2:31)

قُلْنَا اهْبِطُوۤا مِنْهَا جَمِيْعًا ۗ فَاِۤمَّا يٰٓاَتِيۤنَكُم مِّنۡىْ هُدًى فَمَنْ تَبِعَ هُدٰى فَلَآ

خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُوۡنَ ﴿٣٨﴾

“Tukasema “Shukeni humo nyote, na kama ukikufikieni uongozi utokao kwangu, basi watakaofuata uongozi wangu huo haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika.(2:38)

وَالَّذِيۡنَ كَفَرُوۡا وَكَذَّبُوۡا بِآيٰتِنَاۗ اُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ النَّارِ ۗ هُمْ فِيۡهَا خٰلِدُوۡنَ ﴿٣٩﴾

Lakini wenye kukufuru na kuyakadhibisha maneno yetu, hao ndio watakao kuwa watu wa motoni, humo watakaa milele.” (2:39)

Pamoja na kutunukiwa elimu na kupewa mwongozo wa maisha, binadamu pia ametiishiwa viumbe vyote, ikiwa ni pamoja na Malaika. Qur-an inazidi kutukumbusha:

هُوَ الَّذِي خَلَقَ لَكُمْ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا ..... ﴿١٦﴾

“Yeye (Allah) ndiye aliyekuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi, ....” (2:29)

Binadamu kwa kupewa nafasi ya Ukhalifa na kutunukiwa elimu na vipawa vyote alivyonavyo, maisha yake hapa ulimwenguni yamekuwa mtihani.

تَبْرَكَ الَّذِي يَدِيَهِ الْمَلِكُ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٧﴾ الَّذِي خَلَقَ

الْمَوْتَ وَالْحَيَاةَ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْغَفُورُ ﴿١٨﴾

Ametukuka yule ambaye Mkononi mwake umo ufalme (wote); Naye ni mwenye uweza juu ya kila kitu. Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni (kukufanyieni mtihani); ni nani miongoni mweni mwenye amali nzuri. Naye ni Mwenye nguvu na Mwenye Msamaha. (67:1-2)

إِنَّا خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنْ نُطْفَةٍ أَمْشَاجٍ نَبْتَلِيهِ فَجَعَلْنَاهُ سَمِيعًا بَصِيرًا ﴿١٩﴾

إِنَّا هَدَيْنَاهُ السَّبِيلَ ۖ إِمَّا شَاكِرًا وَإِمَّا كَفُورًا ﴿٢٠﴾

Kwa hakika tumemuumba mtu kutokana na mbegu ya uhai iliyochanganyika: (ya mwanamke na mwanaume), ili tumfanyie mtihani (kwa amri na makatazo); kwa hivyo tukamfanya ni Mwenye kusikia Mwenye kuona. Hakika sisi tumemuongoa, (tumembainishia njia (zote mbili hizi kuwa hii ndio ya kheri na hii ndio ya shari) basi mwenyewe tena atakuwa mwenye shukrani au awe mwenye kukufuru (kukanusha) (76:2-3)

Binadamu atafaulu mtihani huu kama ataishi hapa ulimwenguni kama mja na khalifa wa Allah(s.w) kwa kufuata na kusimamisha sheria ya Allah(s.w) ambayo itapelekea kusimamisha uadilifu katika jamii.

Mtu, atafeli mtihani huu kama ataishi hapa ulimwenguni kwa kufuata na kusimamisha sheria zilizotungwa na watu zinazopelekea ulimwengu kuwa uwanja wa fujo na vurugu.

Matokeo ya mtihani huu hayatatangazwa katika maisha yetu ya hapa duniani bali yatatolewa baada ya watu wote kumaliza makazi yao hapa duniani na baada ya mema na maovu yao kujidhihirisha kikamilifu. Ni katika wakati huo ambapo Allah(s.w) atamhesabu kila mtu na kuamua ni yupi alitimiza wajibu wake kama Khalifa wake hapa ulimwenguni na yupi ambaye hakutimiza. Hisabu hiyo haitahusu jambo moja maalumu au kipengele fulani tu bali itahusu maisha yote ya binadamu ya kibinafsi na kijamii. Itahusu pia vipawa vyake vyote vya mwili na akili na amana yoyote aliyopewa juu ya watu au vitu.

Kwa mtizamo wa Uislamu, Ufalme ni wa Allah(s.w) peke yake na binadamu ni khalifa wake tu, hivyo njia pekee ya uadilifu inayompasa binadamu ni kutekeleza wajibu aliopewa na Allah(s.w). Hana uhuru wa kuamua apendavyo upi uwe mwenendo wake wa tabia, bali kipimo cha lipi jema na lipi ovu lazima kichukuliwe kutoka kwa Allah(s.w), wajibu wa binadamu ni kutekeleza kwa ukamilifu na uaminifu wajibu aliokabidhiwa na Muumba wake.

Maadili ya jamii hayatabuniwa na binadamu bali utachukuliwa kutoka kwa Allah(s.w) ambaye ndiye Muumba na mpangaji wa sheria. Binadamu hanabudi kuishi na kutenda kulingana na maamrisha na sheria ya Allah(s.w). Uhusiano huu uliopo kati ya Allah(s.w) na binadamu utakapo eleweka, yale maswali manne ya wanafalsafa wa kikafiri, kuhusiana na Maadili ya jamii, yatapata majibu yaliyowazi na yanayotua akilini.

## Majibu ya Maswali Manne Yanavyotolewa na Uislamu

Pindi mtu akiikubali nafasi ya **uja** na **ukhalifa** aliyopewa binadamu na Muumba wake, maswali makuu manne ya wanafalsafa wa kikafiri, juu ya mwenendo wa tabia ya binadamu, yanajibiwa na Uislamu kwa wepesi kama ifuatavyo:

### 1.Lengo Kuu la Maisha kwa Mtizamo wa Uislamu

Kufuzu mtihani wa Allah(s.w) na kupata radhi zake ndiyo lengo kuu la maisha ya binadamu hapa duniani. Atafuzu mtihani wa Mola wake, endapo binadamu atajitahidi kutii sheria za Allah(s.w) katika kila kipengele cha maisha yake binafsi na kujitahidi kusimamisha sheria hizo katika jamii. Yaani binadamu atafuzu kwa kufanya biashara na Allah(s.w) kama inavyobainishwa katika aya zifuatazo:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا هَلْ أَذَلَّكُمْ عَلَىٰ تِجَارَةٍ تُنْجِيكُمْ مِّنْ عَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٦١﴾  
 تَوَمَّنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَتُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنفُسِكُمْ  
 ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٦٢﴾

*Enyi mlioamini! Je! Nikujulisheni biashara itakayokuokoeni na adhabu iumizayo?(Biashara yenyewe ni hii):Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na piganieni dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na nafsi zenu, haya ni bora kwenu; ikiwa mnajua. (61:10-11)*

يَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَيُدْخِلْكُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ وَمَسْكِنٍ  
طَيِّبَةً فِي جَنَّاتٍ عَدْنٍ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١١﴾

(Mkifanya haya) atakusameheni dhambi zenu na atakuingizeni katika mabustani yapitayo mito mbele yake na (atakupeni) maskani mazuri mazuri katika Bustani za milele; Huku ndiko kufuzu kukubwa” (61:12)

﴿ إِنَّ اللَّهَ اشْتَرَى مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ بِأَبْلٍ لَهُمْ  
الْجَنَّةَ يُقْتَلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ وَعَدًّا عَلَيْهِ حَقًّا  
فِي التَّوْرَةِ وَالْإِنْجِيلِ وَالْقُرْآنِ وَمَنْ أَوْفَىٰ بِعَهْدِهِ مِنَ اللَّهِ  
فَأَسْتَبْشِرُوا بَبَيْعِكُمُ الَّذِي بَايَعْتُمْ بِهِ ۗ وَذَٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١١﴾

“Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waislamu nafsi zao na mali zao ili naye awape Pepo. Wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu; wanaua na wanauawa. Hii ndiyo ahadi aliyojilazimisha (Mwenyezi Mungu) katika Taurati, Injili na Qur-an. Na ni nani atakelezaye zaidi ahadi yake kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa biashara yenu mliyofanya naye. Na huko ndiko kufuzu kukubwa.” (9:111)

## 2. Chem chem ya Ujuzi wa Wema na Uovu kwa Mtizamo wa Uislamu

Chem chem za kweli anazoweza kuzitegemea binadamu katika kutambua mema na maovu ni Allah(s.w) kupitia kwa Mitume na vitabu vyake.

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيَقُومَ  
النَّاسُ بِالْقِسْطِ ..... ﴿٥٧﴾

“Kwa hakika tumewapeleka Mitume wetu kwa dalili wazi wazi na tukaviteremsha vitabu na uadilifu pamoja nao, ili watu wasimamie uadilifu.....” (57:25)

## 3. Msimamizi wa Maadili kwa Mtizamo wa Uislamu

Msimamizi wa mwenendo wa tabia njema inayompeleka binadamu kwenye kusimamisha uadilifu ni Imani thabiti juu ya Allah(s.w) na Siku ya mwisho (siku ya malipo) na juu ya vipengele vingine vya nguzo sita za imani ya Kiislamu.

Muumini wa kweli hana hiari ya kwenda kinyume na maamrisha na makatazo ya Allah(s.w) na Mitume wake.

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا لِمُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ  
الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾

“Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao.” (33:36)

#### 4. Motisha inayowapelekea Waislamu kusimamisha Uadilifu katika jamii

Kinachowachochea Waislamu kuwa na tabia ya kufanya mema na kuacha maovu, na kisha kuamrisha mema na kukataza maovu katika jamii ni matarajio ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu na kukhofia ghadhabu zake. Matokeo ya kupata radhi za Allah(s.w) na kuepuka ghadhabu zake ni kuepukana na maisha ya huzuni na hofu hapa duniani na kupata maisha ya furaha na amani ya milele huko akhera.

Majibu haya yanayotolewa na Uislamu yanatanzua utatanishi wote uliokuwepo katika majibu yaliyotolewa na wanafalsafa wa kikafiri juu ya maadili.

#### Zoezi 2:6

1. Taja vipawa alivyotunukiwa Mwanadamu vinavyomtofautisha na wanyama.
2. Bainisha makusudio ya Allah(s.w) yanayotarajiwa kufikiwa na mwanadamu aliyetunukiwa vipawa hivi.
3. Ng’amua na kubainisha sababu kubwa mbili zilizopelekea makafiri wasiafikiane, wala kufaulu kudhihirisha lengo halisi la maisha ya mwanadamu hapa duniani.
4. Eleza kwa kutoa mifano hai, upogo na udhaifu uliopo katika dhana za makafiri juu ya maadili na uadilifu katika mawanda manne.
5. Ukiondoa suala la Qadar, taja misingi mitano iliyobainishwa ndani ya Qur’an ambayo ndiyo mihimili mikuu ya maadili mema ya Kiislamu.
6. Tumia Qur’an kujibu kwa ufasaha wa kukinaisha , maswali manne ya makafiri juu ya misingi ya Maadili na uadilifu.
7. (a) Nini maana ya Maadili?  
(b) Wakati wanyama huongozwa na silka, wanadamu wana Maadili, kwanini?

8. Kwanini mtu asiyemuamini Allah na siku ya mwisho, hawezi kufanya wema muda wote au kuacha maovu kabisa?

## UTAMADUNI

Uislamu ni utaratibu kamili wa maisha uliofumwa na Allah(s.w) unaoelekeza namna Muumini anavyoweza kukiendea kila kipengele cha maisha yake ya kila siku ili kumuwezesha kuishi kwa furaha na amani na kufikia lengo la maisha yake hapa ulimwenguni. Miongoni mwa vipengele muhimu vya maisha ambavyo jamii ya mwanadamu haina budi kuviendea ni kipengele cha utamaduni au mila na desturi za jamii. Sio kila mila na desturi za jamii zinamfikisha mwanadamu katika lengo la maisha yake hapa duniani kwa furaha na amani.

Ukichunguza tamaduni za jamii mbali mbali utagundua kuwa tamaduni hizo hazimuinui mwanadamu na kumfikisha katika kilele cha hadhi yake, bali kinyume chake huiteremsha hadhi yake na kuifanya duni kuliko ile ya wanyama.Ni utamaduni wa Kiislamu pekee unaomuina mwanadamu na kumbakisha katika kilele cha hadhi yake tukufu ya Ukhalifa wa Allah(s.w), kwa vile utamaduni huu umefumwa na Mwenyewe Sub-haanahu Wata'aala, Mjuzi wa kila kitu, Mwenye hekima.

## Utamaduni wa Muislamu

Waislamu tumehimizwa katika Qur-an kuwa tusifuute utamaduni mwingine au mila nyingine isiyokuwa ile mila ya Nabii Ibrahim(a.s) kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

وَمَنْ يَرْغَبْ عَنِ مِلَّةِ إِبْرَاهِيمَ إِلَّا مِنْ سَفِهَةِ نَفْسِهِ ۗ وَلَقَدْ أَصْطَفَيْنَاهُ فِي  
الدُّنْيَا وَإِنَّهُ فِي الْآخِرَةِ لَمِنَ الصَّالِحِينَ ﴿١٢٤﴾

*Na nani atakayejitenga na mila ya Ibrahim isipokuwa anayeitia nafsi yake katika upumbavu. Na kwa yakini sisi tulimchagua (Ibrahimu) katika dunia, na kwa hakika yeye katika akhera atakuwa miongoni mwa watu wema kabisa. (2:130)*

وَمَنْ أَحْسَنُ دِينًا مِمَّنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُ لِلَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ وَاتَّبَعَ مِلَّةَ  
إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا ۗ وَاتَّخَذَ اللَّهُ إِبْرَاهِيمَ خَلِيلًا ﴿١٢٥﴾

*Na nani aliye bora kwa dini kuliko yule ambaye ameuzelekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu, naye ni mwema, na anafuata mila ya Ibrahim (kuwa Muislamu kweli kweli). Na Mwenyezi Mungu amemfanya Ibrahim kuwa kipenzi chake. (4:125)*

Mila ya Ibrahim (a.s) iliyosisitizwa katika aya hizi si nyingine zaidi ya ile ya kumpwekesha Allah(s.w) na kujitupa kwake kwa utii na unyenyekevu. Yaani mila ya Ibrahim(a.s) ni kuufuata Uislamu kwa ukamilifu kwa kutii kwa unyenyekevu maamrisha yote ya Allah(s.w) na kujitenga kwa utii na unyenyekevu na yale yote aliyoyakataza(s.w). Mwenendo huu wa Nabii Ibrahim ambao tunasisitizwa tuufanye utamaduni wetu uko bayana katika Qur-an:

إِذْ قَالَ لَهُ رَبُّهُ أَسْلِمَ قَالَ أَسْلَمْتُ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٣١﴾

*(Kumbukeni) Mola wake (Ibrahim) alipomwambia Silimu (jisalimisha kwa unyenyekevu), akanena: "Nimejisalimisha kwa Mola wa Ulimwengu wote".(2:131)*

وَوَصَّىٰ بِهَا إِبْرَاهِيمَ بَنِيهِ وَيَعْقُوبَ بَنِيَّ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَىٰ لَكُمْ الدِّينَ فَلَا

تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿١٣٢﴾

*Na Ibrahim akawausia haya wanawe na Yaaqubu (pia akawausia wanawe): Enyi wanangu! Hakika Mwenyezi Mungu amekuchaguliene dini hii, basi msife ila nanyi mmekuwa Waislamu (wanyenyekevu kwa Allah(s.w). (2:132).*

Tunajifunza katika aya hizi kuwa hatua ya kwanza ya kufuata mila ya Ibrahim ni sisi wenyewe kujisalimisha kikweli kweli kwa Allah(s.w) kwa kufuata maamrisha yake yote na kuacha makatazo yake yote. Hatua ya pili ya kufuata mila ya Ibrahim ni ile ya kuwahimiza ahali zetu kuwa Waislamu wa kweli wenye kufuata mwenendo wa maisha anaoridhia Allah(s.w) katika kuendea kila kipengele cha maisha yao ya kila siku.

Pia aya zifuatazo zinatubainishia kwa uwazi mwenendo wa Nabii Ibrahim (a.s) ambao tunahimizwa tuuige na tuufanye ndio mila yetu:

إِنَّ إِبْرَاهِيمَ كَانَ أُمَّةً قَانِتًا لِلَّهِ حَنِيفًا وَلَمْ يَكُ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٣٤﴾

شَاكِرًا لِأَنْعُمِهِ أَجْتَبَنَاهُ وَهَدَيْنَاهُ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿١٣٥﴾

*Hakika Ibrahimu alikuwa kiongozi (mfano mzuri wa kuigwa) mnyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu mtii kamili, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.*



(Alikuwa) mwenye kushukuru neema zake (Allah). (Mwenyezi Mungu) akamchagua na kumuongoza katika njia iliyonyooka. (16:120 - 121).

وَأَتَيْنَاهُ فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَإِنهٗ فِي الْآخِرَةِ لَمِنَ الصَّٰلِحِينَ ﴿١٢١﴾

Na tukampa wema katika dunia; na hakika yeye katika akhera atakuwa miongoni mwa watu wema (pia). (16:122).

Nabii Ibrahim(a.s) alikataa kata kata mila ya jamii yake na akawahakikishia kwa maneno na matendo kuwa yeye ni Muislamu na si miongoni mwa washirikina:

إِنِّي وَجَّهْتُ وَجْهِيَ لِلذِّى فَطَرَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ حَنِيفًا وَمَا اَنَا مِنَ الْمُشْرِكِيْنَ ﴿٦٧﴾

Mimi nimeuelekeza uso wangu kwa yule aliyeziumba mbingu na ardhi. Hali ya kuwa nimeacha dini ya upotofu. Mimi (ni Muislamu) si miongoni mwa washirikina. (6:79).

Vile vile Muislamu wa kweli anayefuata vilivyo mila ya Ibrahimu(a.s) hana budi kuwahakikishia ulimwengu kwa maneno na matendo kuwa yeye ni Muislamu katika hali zote na si miongoni mwa washirikina. Msimamo wa Muislamu wa kweli ni huu ufuatao:

قُلْ اِنِّى هَدٰنِى رَبِّىْ اِلَى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيْمٍ دِيْنًا قِيْمًا مِّلَّةَ اِبْرٰهِيْمَ حَنِيفًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِيْنَ ﴿٦٨﴾ قُلْ اِنَّ صَلَاتِىْ وَنُسُكِىْ وَمَحْيَاىْ وَمَمَاتِىْ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٦٩﴾ لَا شَرِيْكَ لَهٗ وَبِذٰلِكَ اُمِرْتُ وَاَنَا اَوَّلُ الْمُسْلِمِيْنَ ﴿٧٠﴾

Sema: Kwa hakika mimi Mola wangu ameniongoza katika njia iliyonyooka, katika dini iliyo sawa kabisa ambayo ndiyo mila ya Ibrahim aliyekuwa muongofu, wala (kabisa) hakuwa miongoni mwa washirikina.” Sema: “Hakika swala yangu na Ibada zangu (nyingine zote) na maisha yangu na kufa kwangu (vyote) ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Bwana (Rabii) wa walimwengu wote. Hana mshirika wake. Na haya ndiyo niliyoamrisha na mimi ni wakwanza wa waliojisalimisha”. (6:161 - 163).

Tumejifunza kutokana na aya hizi kuwa mila ya Muislamu ni Uislamu. Yaani Muislamu wa kweli hana mila nyingine isiyo kuwa ile ya kufuata vilivyo mwenendo wa kujisalimisha kwa Allah(s.w) kwa kila kipengele cha maisha.

## Vipengele vya Utamaduni wa Kiislamu

Tumejifunza kuwa utamaduni wa Kiislamu ni mwendo wa maisha unaofuata bara bara misingi ya Uislamu kwa kuchunga vilivyo mipaka ya Allah(s.w) katika kukiendea kila kipengele cha maisha. Hivyo kila kipengele cha maisha ya jamii ya Kiislamu ni kipengele cha utamaduni wa Kiislamu.

### Tabia Njema

Muislamu wa kweli ni yule anayejitahidi kwa kadri ya uwezo wake kujipamba na tabia njema. Tabia njema ndio mwenendo wa Mitume wa Allah(s.w) ambao tumeamrisha tuigize mwenendo wao hatua kwa hatua. Msisitizo wa kufuata mwenendo wa Nabii Ibrahim (a.s) tumeshauona na pia tuisahau msisitizo wa kuigiza mwenendo wa Mtume(s.a.w) unaobainishwa na aya ifuatayo:-

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ

الْآخِرِ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا ﴿٣١﴾

*Bila shaka mnao mfano mwema (kiigizo chema) kwa Mtume wa Allah, kwa mwenye kumuogopa Allah(s.w) na siku ya mwisho na mwenye kumkumbuka Allah(s.w) kwa wingi. (33:21).*

Mtume(s.a.w) ambaye tunatakiwa tumuigize alikuwa ni mwenye tabia nzuri kweli kweli kama Mola wake anavyomsifu katika Qur-an:

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٦٨﴾

*Na bila shaka unatabia njema kabisa (68:4).*

Mtume mwenyewe katika kuwasisitiza Waislamu kujivisha vazi zuri la tabia njema amesema:

*Aliye mbora kuliko wote miongoni mwenu ni yule aliye wazidi kwa tabia njema. (Bukhaary na Muslim).*

Pia Mtume(s.a.w) amebainisha ubaya wa mtu kuwa na tabia mbaya aliposema:

*Yule ambaye tabia yake ni mbaya na katili (harsh) hataingia Peponi.(Abu Daudi).*

Vipengele vya tabia njema ambavyo kila Muislamu anahimizwa ajivishe na kujipamba kwavyo vimebainishwa kwa uwazi katika Qur-an na Hadith (Rejea Juzuu ya 2 na 3) na kwa muhtasari Muislamu wa kweli anatakiwa afanye kila

jambo kwa ajili ya Allah(s.w) na awe mwenye kumkumbuka Allah(s.w) kila wakati awe mwema na mwenye kuwahurumia wanadamu wenziwe na viumbe wengine, awe mwepesi wa kutoa msaada wa hali na mali, awe mwenye kumuheshimu kila mtu, awe mwenye kuongea maneno mazuri na kwa upole awe ni mwenye kujizuia na hasira na kuwavumilia wengine, awe mwenye subira na mwepesi wa kusamehe wengine kwa ajili ya Allah(s.w), awe mwenye kutoa haki za wengine na awe jasiri na mwenye msimamo katika kutetea haki za wengine na katika kusimamisha haki katika jamii, awe tayari kutoa nafsi yake na mali yake kwa ajili ya kusimamisha Uislamu katika jamii, awe mwenye kukinai, awe mkarimu, awe mwenye kujitahidi kujipamba na tabia njema nyinginezo ambazo huzaa mahaba, furaha na amani katika jamii na awe mwenye kujiepusha na maneno na matendo yote maovu ambayo huzaa bugh-dha, chuki, uadui na vurugu katika jamii ya mwanadamu.

Wazazi wa Kiislamu na wahusika na taasisi zote za Kiislamu zinazohusika na malezi ya watoto, wanayodhima kubwa ya kuwalea vijana wa katika maadili haya mema. Ni vyema tukumbushane Waislamu wote kuwa suala la kuwalea vijana wetu katika maadili ya Kiislamu ni suala la msingi na la muhimu kuliko shughuli nyingine yoyote ile tutakayowafanyia vijana hawa. Amesema kweli Mtume wa Allah aliposisitiza:

*Hapana zawadi yoyote atakayoitoa baba kumpa kijana wake itakayozidi kumfunza tabia njema. (Tirmidh).*

Waislamu, tutakapoacha kuchukua dhima hii ya kuwalea vijana wetu katika mila ya Ibrahim na badala yake tukawaachia walelewe katika mila za kitwaaghuti tutakuwa tumewapoteza vijana wetu na tutakosa wa kuwarithisha katika uongozi wa kusimamisha Uislamu katika jamii. Tunawajibika kuwarithisha watoto wetu utamaduni wa Kiislamu kama alivyofanya Nabii Ibrahim(a.s).

وَوَصَّىٰ بِهَا إِبْرَاهِيمُ بَنِيهِ وَيَعْقُوبُ بَنِيَّ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَىٰ لَكُمْ الدِّينَ فَلَا

تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿١٣٢﴾

*Na Ibrahimu akawausia haya wanawe na Yaaqubu (mjukuu wake na kuwaambia) Enyi wanangu! Hakika Mwenyezi Mungu amekuchaguliene dini hii; basi msife ila nanyi mmekuwa Waislamu". (2:132)*

Waislamu kamwe tusitarajie kuwa Uislamu utasisimama katika jamii yetu bila ya kuwalea vijana wetu katika maadili ya Kiislamu pamoja na kuomba msaada wa Allah(s.w) atuwezeshe kufanya kazi hii kama alivyotufundisha kuomba katika Qur-an:

وَالَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا هَبْ لَنَا مِنْ أَزْوَاجِنَا وَذُرِّيَّاتِنَا قُرَّةَ أَعْيُنٍ  
وَأَجْعَلْنَا لِلْمُتَّقِينَ إِمَامًا ﴿٧٤﴾

*Mola wetu! Tupe katika wake zetu na watoto wetu yatuburudishayo macho (yetu – nyoyo zetu) na utujaalie tuwe viongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu. (25:74).*

## Vazi la Kiislamu

Vazi la Kiislamu ni sehemu ya utamaduni wa Kiislamu. Vazi la Kiislamu ni lile vazi linalositiri uchi kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu. Lengo la vazi kwa jamii ya mwanadamu linabainishwa katika Qur-an:

يَبْنَىٰ ءَادَمَ قَدْ أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ لِبَاسًا يُورِي سَوَءَاتِكُمْ وَرِيشًا وَ لِبَاسُ  
الَّتَقْوَىٰ ذَٰلِكَ خَيْرٌ ذَٰلِكَ مِّنْ ءَايَاتِ اللَّهِ لَعَلَّهُمْ يَذَّكَّرُونَ ﴿٧٦﴾

*Enyi wanadamu! Hakika tumekuteremshieni nguo zifichazo tupu zenu na nguo za pambo na nguo za ucha-Mungu ndizo bora. Hiyo ni katika ishara za Mwenyezi Mungu ili mpate kukumbuka. (7:26)*

Kama inavyobainishwa katika aya hii lengo kuu la vazi la Kiislamu ni kusitiri awrah (uchi). Vazi la Kiislamu ni lile linalotekeleza masharti yafuatayo:

### (a) Vazi lisitiri Awrah (uchi)

**Awrah ya mwanamke** ni mwili mzima isipokuwa uso na viganja vya mikono kwa mujibu wa kauli ya Mtume(s.a.w) aliposema:

*Mwanamke atakapofikia baleghe hataacha wazi sehemu yoyote ya mwili wake isipokuwa uso na viganja (Abu Daud).*

Amri ya kujisitiri kwa wanawake inabainishwa katika aya zifuatazo:

وَقُلْ لِلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَرِهِنَّ وَحَفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ وَلَا  
يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَلْيَضْرِبْنَ بِخُمُرِهِنَّ عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ  
وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا لِبُعُولَتِهِنَّ أَوْ آبَائِهِنَّ أَوْ آبَاءِ

بُعُولَتِهِمْ أَوْ أُبْنَائِهِمْ أَوْ أُبْنَاتِهِمْ أَوْ إِخْوَانِهِمْ أَوْ بَنِي إِخْوَانِهِمْ أَوْ بَنِي أَخَوَاتِهِمْ أَوْ نِسَائِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ أَوْ التَّسْبِيعِينَ غَيْرِ أُولِي الْإِرْزَةِ مِنَ الرِّجَالِ أَوْ الْوَالِدِينَ لَمْ يَطْهَرُوا عَلَى عَوْرَاتِ النِّسَاءِ وَلَا يَضْرِبْنَ بَأَرْجُلِهِنَّ لِيُعْلَمَ مَا يُخْفِينَ مِنْ زِينَتِهِنَّ ۗ وَتُوبُوا إِلَى اللَّهِ جَمِيعًا أَيُّهُ الْمُؤْمِنُونَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٣١﴾

Na waambie Waislamu wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, wala wasidhihirishe viungo vyao isipokuwa vinavyodhihirika (uso na viganja). Na waangushe shungi zao mpaka vifuani mwao na wasionyeshe mapambo yao ila kwa waume zao au baba zao, au baba za waume zao, au watoto wao, au watoto wa waume zao, au kaka zao, au wana wa kaka zao, au wana wa dada zao, au wanawake wenzi wao, au wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume, au wafuasi wanaume wasio na matamania au watoto ambao hawajajua mambo yaliyohusu uke. Wala wasipige miguu yao ili yajulikane wanayoyaficha katika mapambo yao. Na tubieni nyote kwa Mwenyezi Mungu, enyi Waislamu ili mpate kufaulu. (24:31).

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ قُلْ لَلزَّوْجِكَ وَبَنَاتِكَ وَنِسَاءِ الْمُؤْمِنِينَ يُدْنِينَ عَلَيْنَّ مِنْ جَلْبِيبِهِنَّ ذَلِكَ أَدْنَى أَنْ يُعْرَفْنَ فَلَا يُؤْذِينَ ۗ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٣٢﴾

Ewe Mtume! Waambie wake zako na binti zako, na wanawake wa Kiislamu wajiteremshie uzuri nguo zao. Kufanya hivyo kutapelekea upesi wajulikane (kuwa ni watu wa heshima ili) wasiudhiwe. Na Mwenyezi Mungu ni mwingi wa kusamehe (na) mwingi wa kurehemu. (33:59).

Pamoja na mwanamke kuamrisha kujifunika mwili mzima isipokuwa uso na viganja, pia katika aya hizi anaamrisha:

- Ateremshe shungi mpaka kifuani. Shungi ni kitambaa (mtandio) kinachofunika kichwa, shingo na kifua.
- Asidhihirishe mapambo yake na
- Asitingishe miguu yake na viungo vyake vingine kiasi cha kujulisha aliyoyaficha katika mapambo.

**Awrah ya mwanauume** ni sehemu yote iliyo kati ya kitovu na magoti kwa mujibu wa kauli ya Mtume(s.a.w) aliposema:

*Sehemu yoyote iliyo juu ya magoti haina budi kufunikwa na sehemu yoyote iliyo chini ya kitovu haina budi kufunikwa. (Darqutny).*

*Mwanamume hana budi kufunika ile sehemu ya mwili wake iliyo kati ya kitovu na magoti. (Al-Mabsuut).*

Ni haram kwa Muislamu mwanamume kuvaa bukta au kaptura nje ya chumbani kwake.

### **(b) Vazi lisibane**

Vazi la mwanamke au mwanamume lisibane kiasi cha kuonyesha mchoro wa sehemu za mwili zinazotakiwa zisitiriwe.

### **(c) Vazi lisiwe lenye Kuonyesha (transparent)**

Mwenye kuvaa vazi linaloonyesha rangi ya mwili anahesabika kuwa yuko uchi kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Hafsa bint Abdur-Rahman, alikuja kwa Aysha (r.a) akiwa amevaa shungi inayoonyesha kichwa chake na mabega. Aysha aliichana chana na kumfunika shungi nzito. (Imam Malik)*

Mtume(s.a.w) amesema: Allah amewalaani wanawake waliovaa nguo na huku bado wako uchi.

### **(d) Vazi Lisiwe Lenye Kuvutia**

Wanawake wameamrisha kufunika mwili mzima ili kuficha uzuri wao wa asili (natural beauty) na mapambo yao ili wasiyavute matamano ya wanaume. Ni katika msingi huu pia wanawake wa Kiislamu hawaruhusiwi kuvaa vazi linalovutia sana nje ya nyumbani kwake. Ni katika msingi huu pia wanawake wa Kiislamu hawaruhusiwi kutoka majumbani mwao ila kwa dharura kama inavyosisitizwa katika Qur-an:

Ni mwenendo wa kitwaghuti kwa wanawake kutokatoka majumbani mwao ovyo na kuonyesha ovyo mapambo yao ikiwa ni pamoja na mavazi yanayovutia.

### **(e) Vazi la mwanamke lisifanane na la mwanamume na kinyume chake**

Ni haramu kwa mwanamume kuvaa mavazi ya wanawake na pia ni haramu kwa wanawake kuvaa mavazi ya wanaume. Katika Hadith iliyosimuliwa na Ibn Abbas, Mtume(s.a.w) amewalaani wanaume wanaoigiza mavazi na tabia za kike na wanawake wanaoigiza mavazi na tabia za kiume.

**(f) Vazi lisiwe kiigizo cha vazi la wasiokuwa Waislamu**

Ni haramu kwa Muislamu kuigiza mavazi ya wasiokuwa Waislamu. Hii ni kwa sababu Waislamu wanao utamaduni wao ambao ni tofauti na wa watu wengine. Muislamu anatakiwa atambulikane, ili kwa mfano aweze kusalimiwa na Waislamu wenziwe kwa “Assalaam Alaykum” maamkizi ya Kiislamu waliyoyatumia mitume wote na wafuasi wao na ndiyo yatakayo kuwa maamkizi ya Peponi. Kuamkiana huko hakutawezekana kwa mfano iwapo Waislamu wanaona haya kuvaa vazi litakalawatambulisha kuwa ni Waislamu.

Matokeo yake ni kwamba utamaduni wao utapotea na wao kumezwa katika utamaduni wa kijahili. Muislam anatakiwa ajirekebishe haraka iwapo kwa mavazi yake watu wanashindwa kumtofautisha na kafiri au mtu wa utamaduni mwingine. Ni aibu ilioje kwa Muislamu kujikuta anaambiwa na mtu mwingine: “Mimi siku zote hizi sikujua kama wewe ni Muislamu”. Tunafahamishwa katika Hadithi iliyosimuliwa na Ibn Umar kuwa Mtume(s.a.w) amesema:

*Atakaye waigiza watu, atahusikana nao (atakurwa pamoja nao). (Ahmad, Abu-Daud).*

**(g) Vazi lisiwe la majivuno na kujifaharisha**

Vazi linalompelekea mtu kwenye majivuno na kujifaharisha ni vazi haramu, na limekemewa vikali na Mtume(s.a.w) kama tunavyojifunza katika Hadithi zifuatazo:

*Ibn Umar ameeleza kuwa atakaye ning'iniza suruali yake kwa kujifaharisha, Allah(s.w) hatamwangalia siku ya kiyama. (Bukhaary na Muslim).*

*Ibn Umar ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: “Avaaye vaa vazi la fahari katika ulimwengu huu, Allah(s.w) atamvisha vazi la huzuni (hizya) siku ya kufufuliwa”. (Tirmidh, Ahmed, Abu Daud, Ibn Majah).*

**(h) Vazi lisiwe chafu na la kujidhalilisha**

Kinyume cha kujifaharisha ni kujidhalilisha. Ni haramu kwa Muislamu kuvaa vazi linalo mdhalilisha. Muislamu anatakiwa ale vizuri na kuvaa vizuri ila tu asijifaharisha wala asifanye israfu. Allah(s.w) ametuamrisha kutangaza neema zake:

وَأَمَّا بِنِعْمَةِ رَبِّكَ فَحَدِّثْ

“Na neema za Mola wako zisimulie” (93:11).

Ni katika kushukuru na kutangaza neema za Allah(s.w) kwa mtu kuvaa vizuri na kula vizuri na kwa kadri ya uwezo wake. Pia tunajifunza hili katika Hadith ifuatayo:

*Amr bin Shuaib amesimulia kutoka kwa baba yake, kutoka kwa babu yake kuwa Mtume wa Allah amesema: “Hakika Allah anapenda kuona matokeo ya neema zake kwa mja wake”. (Tirmidh).*

Yaani Allah(s.w) hampendi mtu ambaye ingawa amemneemsha bado anaendelea kuishi katika hali ile ile duni kama kwamba hakuneemeshwa neema yoyote. Pia Waislamu wanahimizwa wajenge tabia ya usafi na umaridadi wa miili yao na nguo zao kama tunavyojifunza katika Qur-an:

وَيَا بَكَ فَطَهِّرْ

*Na nguo zako uzitakase. (74:4).*

..... وَاللَّهُ يُحِبُّ الْمُتَطَهِّرِينَ

*“.....Na Mwenyezi Mungu anawapenda wajitakasao”. (9:108)*

..... إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ التَّوَّابِينَ وَيُحِبُّ الْمُتَطَهِّرِينَ

*“Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaotubu na huwapenda wanojitakasa”. (2:222).*

Kujitakasa katika aya hizi, hakuishii kwenye kujitakasa nafsi tu bali ni pamoja na kujitakasa mwili, nguo na matendo.

*Jabir anasimulia: Mtume(s.a.w) alipokuja kutuona alimkuta mtu mwenye nywele nyingi zisizochanwa, kisha Mtume akasema: Huyu mtu hajapata kitu cha kuchania kichwa chake! Na alimuona mtu aliyevaa nguo chafu, kisha akasema: Huyu mtu hajapata kitu (maji) cha kufulia nguo zake! (Ahmad, Nisai)*

Unadhifu ni katika utamaduni wa Kiislamu. Mtume(s.a.w) amehimiza:

*“Uislamu ni nadhifu, basi jinadhifisheni”.*

Kwa ajili ya unadhifu Mtume(s.a.w) alipendelea sana vazi jeupe kama inavyobainika katika Hadith zifuatazo:

*Abu Dard'a amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Hakika vazi bora ambalo waweza kuwa nalo katika kukutana na Mola wako kaburini au msikitini ni vazi jeupe. (Ibn Majah).*

*Samurah ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Vaa vazi jeupe kwa sababu ni safi na linapendeza, na lifanyeni sanda kwa ajili ya maiti wenu. (Ahmad, Tirmidh, Nisai).*



**(i) Vazi la hariri limeharamishwa kwa wanaume**

Ni haramu kwa wanaume kuvaa nguo za hariri au mapambo ya dhahabu na fedha kwa mujibu wa Hadith zifuatazo:

*Ibn Umar amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: “Hakika anayevaa nguo za hariri katika ulimwengu huu hatakuwa na kitu katika siku ya Malipo”. (Bukhaary na Muslim).*

*Hudhaifa amesimulia “Mtume wa Allah ametukataza kutumia vyombo vya dhahabu na fedha na pia ametukataza vazi la hariri hata kukaa juu yake”. (Bukhaary na Muslim).*

Bali wanawake wameruhusiwa kuvaa nguo za hariri na kuvaa mapambo ya dhahabu na fedha ila tu wachunge mipaka iliyowekwa:

*Abu Mussa anaeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: “Dhahabu na hariri vimefanywa halali kwa wafuasi wangu wanawake na vimefanywa haramu kwa wafuasi wangu wanaume” (Tirmidh, Nisai)*

Pia vazi jekundu (sio lenye mistari au michirizi myekundu)limeharamishwa kwa wanaume. Tunafahamishwa katika Hadith kuwa:

*Abdullah bin Amr amesimulia: “Mwanamume mmoja aliyevalia vipande viwili vya nguo nyekundu alipita na akamsalimia Mtume, lakini Mtume hakuitikia salam hiyo” (Tirmidh, Abu Daud).*

**(j) Wanaume wamekokotzwa kuvaa kofia**

Wanaume wamehimizwa sana kuvaa kitu cha kufunika kichwa iwe kofia au kilemba. Katika Hadith iliyo nukuliwa na Baihaq na Tirmidh, Mtume(s.a.w) amesema kuwa kufunika kichwa kwa kilemba ni katika mwenendo wa Malaika. Ikumbukwe kuwa kwa wanawake kufunika kichwa si jambo la kupendeza tu bali ni wajibu. Mwanamke akiacha kichwa wazi hatakama amefunika sehemu nyingine yote ya mwili atahesabika kuwa yuko uchi na akitembea hivyo mbele ya wanaume wasio maharimu wake, laana ya Allah(s.w) itakuwa juu yake.

Huu ndio utamaduni wa Kiislamu ambao kila Muislamu wa kweli analazimika kujiambatanisha nao. Utamaduni mwingine wowote utakaompelekea Muislamu kuvaa kinyume na vazi la Kiislamu utakuwa ni utamaduni wa Kijahili au wa shetani. Allah(s.w) anatumadharisha na Shetani katika aya ifuatayo:

يَبْنَىءَ آدَمَ لَا يَفْتِنَنَّكُمْ الشَّيْطَانُ كَمَا أَخْرَجَ أَبَوَيْكُمْ مِنَ الْجَنَّةِ يَنْزِعُ

عَنْهُمَا لِبَاسَهُمَا لِيُرِيَهُمَا سَوْءَٰتِهِمَا ۗ إِنَّهُ يَرِنَكُمْ هُوَ وَقَبِيلُهُ مِّنْ حَيْثُ لَا

تَرَوْنَهُمْ ۗ إِنَّا جَعَلْنَا الشَّيْطَانَ أَوْلِيَاءَ لِلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٢٧﴾

*Enyi wanadamu! Shetani asikutieni katika matata, kama alivyowatoa wazee wenu katika pepo akawavua nguo zao ili kuwaonyesha tupu zao. Hakika yeye pamoja na kabila yake wanakuoneni, na hali ya kuwa nyinyi hamuwaoni. Bila shaka sisi tumejaalia mashetani kuwa marafiki wa wale wasioamini. (7:27).*

## Miiko katika Kula na Kunywa

Hata kula na kunywa katika Uislamu kuna miiko yake. Muislamu wa kweli hatakula na kunywa tu bila kuchunga miiko na kufuata utaratibu uliowekwa. Mwongozo wa kula na kunywa uko bayana katika Qur-an. Hebu turejee aya zifuatazo:

*Enyi watu! Kuleni vilivyomo katika ardhi, halali na vizuri wala msifuate nyayo za shetani, bila shaka yeye kwenu ni adui dhahiri. (2:168).*

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا كُلُوْا مِنْ طَيِّبٰتِ مَا رَزَقْنٰكُمْ وَاَشْكُرُوْا لِلّٰهِ اِنْ

كُنْتُمْ اِيَّاهُ تَعْبُدُوْنَ ﴿١٧٢﴾

*Enyi mlioamini! Kuleni vizuri tulivyokuruzukuni, na mumshukuru Mwenyezi Mungu, ikiwa mnamuabudu yeye peke yake. (2:172).*

..... وَكُلُوْا وَاَشْرَبُوْا وَلَا تُسْرِفُوْا اِنَّهٗ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِيْنَ ﴿١٧٣﴾

*“... Na kuleni (vizuri) na kunyweni (vizuri). Lakini msipite kiasi tu. Hakika yeye (Mwenyezi Mungu) hawapendi wapitao kiasi”. (7:31).*

Katika aya hizi Allah(s.w) anatuagiza kuwa:

- (i) Tule vilivyo halali na vilivyopatikana kwa chumo halali.
- (ii) Tule vizuri tuvipendavyo kwa kadiri ya uwezo wetu.
- (iii) Tusifanye ubadhirifu katika kula na kunywa.
- (iv) Tumshukuru Yeye kwa vile alivyotuneemesha, kwa kufuata maamrishi yake kwa utii na kuchunga mipaka yake kwa unyenyekevu katika maisha yetu ya kila siku.

Wanaokula na kunywa bila kufuata mazingatio haya wanakuwa hawatofautiani kabisa na wanyama. Qur-an inasema:

..... وَالَّذِينَ كَفَرُوا يَتَمَتَّعُونَ وَيَأْكُلُونَ كَمَا تَأْكُلُ الْأَنْعَامُ وَالنَّارُ

مَثْوَى لَهُمْ ﴿١٢﴾

Lakini waliokufuru hujifurahisha (hapa duniani) na kula kama walavyo wanyama, na moto ndio makazi yao. (47:12)

## Vyakula Vilivyo Haramishwa

Vyakula vyote visivyo haramishwa katika Qur-an na Hadith ni halali. Vyakula vilivyoharamishwa katika Qur-an:

حُرِّمَتْ عَلَيْكُمْ أَلْمَيْتَةُ وَالِدَمُ وَلَحْمُ الْحَنْزِيرِ وَمَا أَهَلَ لِغَيْرِ اللَّهِ بِهِ

وَالْمَنْخَنِقَةُ وَالْمَوْقُوذَةُ وَالْمُتَرَدِّيَةُ وَالنَّطِيحَةُ وَمَا أَكَلَ السَّبُعُ إِلَّا مَا

ذَكَّيْتُمْ وَمَا ذُبِحَ عَلَى النُّصُبِ ..... ﴿١٣﴾

Mnaharamishiwa nyamafu na damu na nyama ya nguruwe na mnyama aliyechinjwa si kwa ajili ya Allah, na kilichokufa kwa kusongeka koo, na kilichokufa kwa kupigwa, na kilichokufa kwa kuanguka, na kilichokufa kwa kupigwa pembe (na wanyama wengine), na alichokila mnyama ila mkiwahi kukichinja. Na (pia mmeharamishiwa) kilichochinjwa panapo fanyiwa Ibada isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu (kama mizimu)... (5:3).

Aya hizi za Qur-an pamoja na (6:145) zinatupatia mafunzo yafuatayo juu ya vyakula vilivyoharamishwa:

1. Mnyama aliye kufa bila ya kuchinjwa kwa sababu yoyote iwayo (mzoga).
2. Mnyama asiyechinjwa kwa jina la Allah – Tumeamrisha katika Qur-an:

فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَأَنْحَرْ ﴿١٤﴾

Basi swali kwa ajili ya Mola wako na uchinje (kwa ajili ya Mola wako). (108:2).

Kutokana na amri hii si halali kula nyama ya mnyama aliyechinjwa na Kafiri, Mshirikina au yeyote asiye Muamini Allah(s.w) na Upweke wake. Nyama itakuwa halali iwapo mchinjaji ni Muislamu atakaye chinja kwa jina la Allah – Bismillah Allahu Akbar na atakayezingatia masharti ya kuchinja ya kumkata mnyama koo (shingo) kwa kisu kikali au kitu chochote cha kukatia kilicho kikali.

Muislamu yeyote awe mtoto, mwanamume au mwanamke katika hali yoyote anaruhusiwa kuchinja. Wala hapana suala la kupewa kisu na Sheikh.

3. Mnyama aliyechinjwa kwa ajili ya matambiko, mashindano, n.k. mnyama huyo maadam kusudio la kuchinjwa kwake ni kumshirikisha Allah(s.w) nyama yake ni haramu kuila hata kama mwenye kuchinja anajiita Muislamu na ametaja jina la Allah wakati wa kuchinja.
4. Nyama ya nguruwe.
5. Damu inayomwagika – damu inayobakia kwenye nyama si haramu.

Vyakula vilivyoharamishwa katika Hadith

6. Wanyama na ndege wote wanaowinda wengine kwa makucha na meno au midomo yao ni haramu kula nyama yao kwa mnasaba wa Hadith zifuatazo:

*Abu Hurairah amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: “Kila mnyama awinda kwa meno ni haramu kuliwa” (Muslim).*

*Ibn Abbas ameeleza kuwa Mtume wa Allah aliharamisha kila mnyama awindaye kwa meno na kila ndege anayewinda wengine kwa kucha (Muslim).*

Wanyama wanaowinda kwa meno na kucha ni kama simba, chui, paka, fisi, vicheche, mbwa mwitu, n.k.

Ndege wanao winda kwa makucha ni kama tai, mwewe, kipanga, n.k.

7. Nyama ya punda wa nyumbani, farasi na nyumbu ni haramu kwa mnasaba wa Hadith ifuatayo

*Khalid bin Walid ameeleza kuwa Mtume wa Allah ameharamisha nyama ya farasi, nyumbu na punda wa nyumbani (Abu Daud, Nisai).*

Bali nyama ya punda milia ni halali kama tunavyofunzwa katika Hadithi ifuatayo:

*Abu Watadah ameeleza kuwa alimchinja pundamilia (punda wa porini). Mtume(s.a.w) akamuuliza: “Unachochote katika nyama yake?” Alijibu: Tuna miguu miwili ya nyuma. Kisha alichukua na kula. (Bukhaary na Muslim).*

8. Nyama ya wanyama wachafu wenye kuathiri mwili na utu kama nguruwe, mbwa, paka, n.k.

*Ibn Umar amesimulia kuwa Mtume wa Allah ameharamisha nyama na maziwa ya wanyama wachafu. (Tirmidh).*

9. Ni haramu kula nyama ya mjusi na jamii yote ya mijusi:

*Abdul-Rahman bin Shibl amesimulia kuwa Mtume(s.a.w) ameharamisha nyama ya mijusi. (Abu Daud).*

## 10. Nyama ya paka ni haramu:

Jabir amesimulia kuwa Mtume(s.a.w) ameharamisha nyama ya paka na kumpiga bei.

## 11. Nyama ya kiungo cha mnyama kilichokatwa mwenyewe akiwa yungali hai kama vile mkia wa kondoo, mguu wa mnyama uliokatika kwa ajali, n.k. ni haramu kwa mnasaba wa Hadith ifuatayo:

*Abu Waqidil Laysi ameeleza kuwa Mtume(s.a.w) alikuja Madina akawakuta wanapenda nundu za ngamia na kukata mikia ya kondoo. Mtume(s.a.w) akasema: "Kile kilichokatwa kwa wanyama walingali hai ni mzoga. Ni haramu kuliwa" (Tirmidh, Abu Daud).*

## 12. Ni haramu kula wadudu isipokuwa nzige kwa mujibu wa Hadith ifuatayo:

*Ibn Umar ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Mizoga ya aina mbili na damu za aina mbili, vimefanywa halali kwetu: Mizoga ya samaki na nzige na damu ya maini na wengu. (Ahmad, Ibn Majah, Darqutni).*

Hivi ndivyo vyakula vilivyo haramishwa katika Qur-an na Hadith lakini Muislamu atakaposongwa na njaa ya kufa na kupona na pakawa hapana njia yoyote ya kupata chakula, ameruhusiwa kula haramu kiasi kidogo cha kumuwezesha kuishi na wala asile kwa kufurahia kama tunavyojifunza katika Qur-an:

..... فَمَنْ أَضْطَرَّ غَيْرَ بَاغٍ وَلَا عَادٍ فَإِنَّ رَبَّكَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٤٥﴾

"... Lakini aliyelazimika (kula kwa ajili ya njaa, n.k.) pasipokupenda wala kwa kuvuka mipaka, basi, Mwenyezi Mungu ni mwingi wa kusamehe na mwingi wa kurehemu. (6:145)

## Vinywaji Vilivyoharamishwa

Vinywaji vyote vinavyolevya (intoxicants) vimeharamishwa hata kuonja.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَزْلَمُ رِجْسٌ مِّن

عَمَلِ الشَّيْطَانِ فَأَجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٩٠﴾

*Enyi mlioamini! Bila shaka ulevi na kamari na kuabudiwa (na kuombwa) asiye kuwa Mwenyezi Mungu, na kutazamia kwa mishale ya kupigia ramli (na kwa vinginevyo); (yote haya) ni uchafu (ni) katika kazi ya shetani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufaulu (kutengenekewa). (5:90)*

Ulevi, kamari, kumshirikisha Allah na kutazamia ni matendo yanayoivuruga jamii na kuifarikisha:

إِنَّمَا يُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُوقِعَ بَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةَ وَالْبَغْضَاءَ فِي الْخَمْرِ  
وَالْمَيْسِرِ وَيُصْذِكُمْ عَن ذِكْرِ اللَّهِ وَعَنِ الصَّلَاةِ فَهَلْ أَنْتُمْ مُنْتَهُونَ ﴿١١﴾

*Hakika shetani anataka kukutieni uadui na bughudha baina yenu kwa ajili ya ulevi na kamari na anataka kukuzuilieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na (kukuzuilieni) kuswali. Basi je, hamtaacha haya? (5:91).*

Vinywaji vyote vinavyolevya na vilivyo najsi kama vile damu, mkojo, n.k. vimeharamishwa kunywewa hata kwa dawa kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Waili al-Hadhrami ameeleza: Tariqa bin Suwaid alimuuliza Mtume(s.a.w) juu ya ulevi. Mtume(s.a.w) aliharamisha. (Tariqa) akasema hakika natengeneza ulevi kwa ajili ya dawa. Mtume(s.a.w) alijibu: Huo si dawa bali ni ugonjwa (Muslim).*

Ulevi ni haramu ukinywewa kwa wingi au kwa uchache kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Jabir ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: “Kinacholevya ni haramu kikiwa kingi au kidogo (Tirmidh, Abu Daud, Ibn Majah).*

## Vyakula na Vinywaji Halali

Vyakula na vinywaji vyote vilivyo patikana kwa njia ya halali au kutokana na chumo la halali na visivyo haramishwa katika Qur-an na Sunnah, ni halali kwa Waislamu. Ni haramu mtu kuharamisha alivyovihalalisha Allah(s.w).

Mtume(s.a.w) alipoapa kutokula “asali” kwa sababu tu ya kutaka kuwaridhisha wake zake, Mola wake alimuonya na kwa hiyo tunaonywa Waislamu wote:

يَأْتِيهَا النَّبِيُّ لِمَ تُحْرِمُ مَا أَحَلَّ اللَّهُ لَكَ تَبْتَغِي مَرْضَاتَ أَزْوَاجِكَ وَاللَّهُ  
غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١١﴾

*Ewe Mtume: Mbona unaharamisha alichokuhalalishia Mwenyezi Mungu? Unatafuta radhi za wake zako? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu. (66:1).*

Kama mtu chakula fulani kinamdhuru au hakipendi atakuwa na udhuru wa kutokila lakini asikiharamishe.

## Adabu za Kula

Kula kwa Muislamu ni Ibada, kwani wakati anapokula anatakiwa azikumbuke neema za Allah(s.w) na azishukuru kwa kumuabudu Mola wake ipasavyo. Mtu anayemkufuru Allah(s.w) na kuona kuwa lengo la kuwepo kwake hapa ulimwenguni ni kula na kustarehe, mbele ya Allah(s.w) anawekwa katika kundi la wanyama kama tunavyojifunza katika aya ifuatavyo:

إِنَّ اللَّهَ يُدْخِلُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا  
الْأَنْهَارُ وَالَّذِينَ كَفَرُوا يَتَمَتَّعُونَ وَيَأْكُلُونَ كَمَا تَأْكُلُ الْأَنْعَامُ وَالنَّارُ  
مَثْوًى لَهُمْ

*Kwa hakika Mwenyezi Mungu atawaingiza walioamini na kufanya mema katika mabustani yapitayo mito mbele yake. Lakini waliokufuru hujifurahisha (hapa duniani) na kula kama walavyo wanyama, na moto ndio makazi yao. (47:12)*

Muislamu hatarajiwi ale kama walavyo wanyama, bali anatarajiwa ale kwa heshima na adabu iliyobainishwa na Uislamu kama tunavyojifunza katika kipengele hiki. Adabu za kula hapa tutazigawanya katika mbeya nne zifuatazo:

- (a) Kabla ya kuanza kula.
- (b) Wakati wa kula.
- (c) Baada ya kula.
- (d) Kula katika kundi.

### (a) Kabla ya kuanza kula

- (i) Kuhakikisha kuwa chakula Muislamu anacho kwenda kula ni halali kwani tonge moja la chakula haramu linamfanya mtu asikubaliwe Ibada zake kwa siku 40. Pia tunafahamishwa kuwa mwili uliojengwa na chakula haramu umeharamishiwa pepo na mahali unapojuzu kuingia ni motoni.
- (ii) Kuosha mikono kabla ya kuanza kula ili kutoa uchafu kwa ajili ya afya. Pia kufanya hivyo kuna baraka ndani yake kama tunavyofahamishwa katika Hadith ifuatavyo:

*Salman ameeleza; Nimesoma katika Taurati kuwa baraka za chakula zinapatikana kwa kuosha mikono baada ya kula. Nilipolieleza hili kwa*

*Mtume(s.a.w) alisema: Baraka za chakula zinapatikana kwa kuosha mikono kabla ya kuanza kula na baada ya kumaliza kula. (Tirmidh).*

- (iii)Meza au mahali pa kulia patandikwe kitambaa safi, vyema kiwe cheupe ili chakula kitakachodondoka humo kiokotwe na kuliwa kama alivyosisitiza Mtume(s.a.w). Mtume(s.a.w) hakuwahi kulia kwenye meza kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Anas(r.a) amesimulia: Kwa kadri ni juavyo, Mtume(s.a.w) kamwe hakuwahi kula chakula kwenye trei kubwa, wala hakuwahi kula silesi za mkate zilizokaushwa, wala hakuwahi kula mezani. (Bukhaary).*

- (iv)Wakati wa kula mtu akae vizuri, asiwe amejiegemeza wala asile huku amelala. Akae mkao ambao utamuwezesha kula kwa starehe:

*Abdullah bin Amr amesimulia kuwa Mtume wa Allah hakuwahi kuonekana akila huku ameegemea mahali...” (Abu Daud)*

- (v) Kuweka nia ya kula ili kupata nguvu za kumtumikia (kumuabudu) Allah(s.w) inavyostahiki na kuzingatia aya ifuatayo:

ثُمَّ لَتُسْئَلُنَّ يَوْمَئِذٍ عَنِ النَّعِيمِ ﴿٨﴾

*Kisha kwa hakika mtaulizwa siku hiyo juu ya neema (mlizopewa mlizitumiaje). (102:8)*

- (vi)Mgeni atosheke na chakula kilichotayarishwa na wenyeji wake, badala ya kuwasumbua wenyeji wake wamtayarishie chakula kingine. Ila ikiwa chakula hicho ni kigeni kwake na hawezi kula, basi itakuwa hapana budi atafutiwe chakula kingine.

- (vii)Ni vyema kula chakula pamoja kuliko kula mmoja mmoja kwani chakula kinacholiwa kwa pamoja kina baraka kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Umar bin Khattab ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Kula pamoja na sio kwa kutengana kwani baraka ziko kwa walio pamoja na wengi. (ibn Majah).*

Pia kuwakaribisha chakula wageni, fukara, masikini, yatima na wote wenye kuhitajia ni jambo lililosisitizwa sana katika Uislamu.Tunafahamishwa katika Qur-an kuwa mtu asiyejihimiza kuwalisha masikini na kuwaangalia vyema yatima amekadhibisha siku ya malipo hata kama atajiita Muislamu:



أَرَأَيْتَ الَّذِي يُكَذِّبُ بِالْإِيمَانِ ﴿١﴾ فَذَلِكَ الَّذِي يَدْعُ الْيَتِيمَ ﴿٢﴾  
وَلَا يَحْضُ عَلَىٰ طَعَامِ الْمَسْكِينِ ﴿٣﴾

*Je, unemuona yule anayekadhibisha dini (asiyeamini akhera)? Huyu ni yule anayemsukuma yatima, wala hajihimizi kuwalisha masikini. (107:1-3).*

Katika Hadith iliyosimuliwa na Ibn Abbas, Mtume(s.a.w) amesema:

*Baraka zinashuka haraka haraka katika nyumba ambamo chakula hutolewa kuliko kisu kinavyopita katika nundu ya ngamia(Ibn Majah)*

### **(b) Wakati wa kula**

- (i) Kuanza kula kwa jina la Allah kwa kusema: “Bismillahir rahmanir Rahiim”. Muislamu kuanza kula bila ya kulitaja jina la Allah(s.w) ni kumkaribisha Shetani katika chakula chake. Katika Hadith iliyosimuliwa na Hudhaifah Mtume wa Allah amesema:

*Hakika Shetani anakifanya chakula kiwe halali kwake pale ambapo jina la Allah halikutajwa(Muslim).*

Kama Muislamu amesahau kuanza kwa jina la Allah wakati wa kula atakapokumbuka aseme:

*“Bismillahi awwalahu wa aakhirahu” yaani “Naanza kwa jina la Allah mwanzoni mwake na mwishoni mwake”. (Tirmidh, Abu Daudi).*

- (ii) Kula kwa mkono wa kulia. Mtume(s.a.w) amesema:

*“Mmoja wenu atakapokuwa ana kula, na ale kwa mkono wa kulia na atakapokuwa anakunywa, na anywe kwa mkono wa kulia”. (Muslim).*

- (iii)Kumega chakula sehemu iliyo mbele yako, ukianza chini na wala sio juu kama inavyosisitizwa katika Hadith ifuatayo:

*Ibn Abbas ameeleza kuwa Mtume(s.a.w) aliletewa chakula kisha akasema:Anza kumega pembeni mwake na wala isiwe katikati kwa sababu baraka zinamiminika kwenda chini kupitia katikati. (Tirmidh, Ibn Majah na Darimi).*

Katika riwaya ya Abu Daud, alisema: “Wakati mmoja wenu anakula, asile kutokea sehemu ya juu ya chakula bali amege kuanzia sehemu ya chini pembeni mwa sahani kwa sababu baraka zinashuka kutokea sehemu ya juu.

Pia tunakatazwa kuyumbayumba kwenye sahani wakati wa kula kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Amir bin Salamah amehadithia: Nilikuwa kijana mdogo chini ya malezi ya Mtume wa Allah na mkono wangu ulikuwa unayumba yumba katika sahani kwa hiyo aliniona: "Kula kwa mkono wako wa kulia na mega pale palipo karibu yako" (Bukhaary na Muslim)*

(iv) Muislamu akila anatakiwa amege tonge ndogo ndogo na atafune vizuri ili kurahisisha usagaji wa chakula tumboni.

(v) Ni vizuri kukata nyama kwa meno kuliko kutumia kisu kama Mtume(s.a.w) anavyotuhimiza katika Hadith ifuatayo:

*Aysha ameeleza kuwa Mtume wa Allah anasema: "Usikate nyama kwa kisu kwa sababu ni jambo la wageni, lakini ichane kwa meno kwani huleta utamu zaidi na ni wepesi zaidi kufanya hivyo." (Abu Daud, Darimi).*

(vi) Kama chakula ni cha moto ni vizuri kusubiri kipoe na sivizuri kupoozesha chakula kwa kupuliza.

(vii) Kula kwa kiasi. Si vizuri Muislamu kujaza sana tumbo. Hiyo ni israfu na ina madhara yake kiafya na kiroho:

*Miqdam bin Maadi amesimulia: "Nimemsikia Mtume wa Allah akisema: "Hapana mtu kujaza sana tumbo lake kiasi cha kuchukiza. Hapana budi pawe na kipimo cha kujaza tumbo kwa mwanadamu kiasi cha kuubakisha uti wake wa mgongo katika hali ya kunyooka. Kama hawezi kuweka kipimo hicho, basi theluthi (1/3) ya tumbo lake aijaze chakula, theluthi (1/3) iliyobakia kwa ajili ya hewa. (Tirmidh, Ibn Majah).*

(viii) Kuokota tonge la chakula lililoanguka kwa bahati mbaya na kula kama liliangukia kwenye kitambaa maalum kilichotayarishwa kwa ajili hiyo. Kama tonge hilo litakuwa limeanguka chini, utaondoa sehemu iliyoshika chini na kula sehemu safi iliyobakia. Jitihada zote hizi ni ili kuepukana na israfu ambayo ni njia ya Shetani. Tunajifunza hili katika Hadith ifuatayo:

*Jabir ameeleza kuwa alimsikia Mtume wa Allah akisema: Hakika Shetani anamuhudhuria kila mtu katika kila kitu anachokifanya hata wakati wa chakula. Tonge la chakula litakapomponyoka mmoja wenu na atupe sehemu iliyo shika vumbi na ale kilichobakia na asimwachie shetani. Na atakapo maliza chakula chake na alambe vidole vyake kwani hajui ni wapi katika chakula chake kuna baraka(muslim).*

(ix) Kulamba sahani na vidole ili kuhakikisha kuwa hakuna hata chembe ya chakula inayotupwa, ni miongoni mwa adabu za kula kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Kaab bin Malik ameeleza kuwa Mtume(s.a.w) alikuwa akila kwa vidole vitatu na alikuwa akilamba mkono wake kabla hajanawa. (Muslim).*

*Jabir amesimulia kuwa Mtume(s.a.w) alikuwa akilamba vidole vyake na sahani na akisema: Hujui ni wapi katika chakula kuna baraka. (Muslim)*

*Ibn Abbas ameeleza kuwa Mtume(s.a.w) amesema: Mmoja wenu anapokula chakula hatanawa bila ya kulamba mkono wake. (Bukhaary na Muslim).*

### **(c) Baada ya chakula**

- (i) Baada ya Kulamba vidole, na sahani tunanawa mikono kwa ajili ya unadhifu na kutunza afya zetu. Mtume(s.a.w) ametusisitiza kunawa baada ya kula kama inavyobainishwa katika Hadith:

*Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Atakayepitisha usiku na uchafu mkononi mwake kwa sababu ya kutonawa (baada ya kula) ikatokea kudhurika kutokana na uchafu huo, asimlaumu yeyote ila yeye mwenyewe. (Tirmidh, Abu Daud, Ibn Majah).*

- (ii) Kumshukuru Allah(s.w). Baada ya Muislamu kula au kunywa kitu chochote humshukuru Allah(s.w) kwa kusema:“Al-hamdulillaahi Rabbil-aalamiin” yaani shukrani zote anastahiki Bwana mlezi wa viumbe vyote”. Amesimulia Abu Sayyid Al-Kudriyyi kuwa Mtume(s.a.w) alipomaliza kula alizoea kushukuru hivi:

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِيْ اَطْعَمَنَا وَسَقَّنَا وَجَعَلَنَا مِنَ الْمُسْلِمِيْنَ

*Al-hamdulillaahil-ladhii atwa-amaana wasaqaanaa wajaalnaa minal muslimiina.*

Yaani:

*Sifa zote njema zinamstahiki Allah aliyetulisha, akatunywesha na akatufanya kuwa Waislamu. (Tirmidh, Abu Daud, Ibn Majah).*

Muislamu atatakiwa akiweke kila kitendo anachokifanya katika Ibada kwa kukianza kwa jina la Allah, kuchunga mipaka ya Allah wakati wa kukifanya na kumaliza kwa kumshukuru Allah(s.w).

Hivyo, kula kutakuwa Ibada endapo Muislamu atanza kula kwa jina la Allah, kisha akawa anamkumbuka Allah(s.w). Faida zaidi ya kumshukuru Allah(s.w) baada ya kula inabainishwa katika Hadith ifuatayo:

*Anas ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Hakika Allah anamfurahia mja anayekula chakula kisha akamshukuru baada yake au anayekunywa kisha akamshukuru baada yake. (Muslim).*

(iii) Kumshukuru mwenyeji au mtayarishaji wa chakula kwa kumwambia “*Ahsante*” au “*Shukran*” kwani asiye mshukuru mwanaadam aliyemtendea wema, hawezi kumshukuru Allah(s.w):

*Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Mlaji mwenye shukrani ni sawa na mfungaji mwenye subira. (Tirmidh, Ibn Majah).*

Kulinganishwa mlaji na mfungaji ni kielelezo kingine kuwa kula ni lbada kama ilivyo kufunga kama utaratibu wa kula utafuatwa kama unavyofuatwa katika kufunga.

Pamoja na kutoa shukrani kwa mtayarishaji wa chakula, ni vyema pia kumuomba dua kwa kusema: “*Jazakallahu khair*” akiwa mwanamume, na akiwa mwanamke utamuomba kheria kwa kusema: “*Jazakillahi khair*” yaani “*Allah akujazie kheri*”.

#### **(d) Adabu za kula katika Kundi**

- (i) Mtu asianze kula kabla ya wengine.
- (ii) Asifanye haraka, ale kwa kasi inayolingana na wengine na awafikirie wengine ili asiwapunje.
- (iii) Kama kila mmoja anajiwekea chakula katika sahani yake kutoka kwenye dish kubwa, hana budi kuchukua kiasi kidogo kwanza mpaka wote waenee, kisha akihitaji baadaye ataongeza lakini vile vile awafikirie wengine nao watakaotaka kuongeza.
- (iv) Asiwang’ang’anize wengine kula aina ya chakula asichokipenda, badala yake awapendeele wengine kile anachokipenda.
- (v) Asiwaangalie wengine wanavyokula wala sahani zao.
- (vi) Awapendeele wengine kupata kitu kama vile maji kabla ya yeye mwenyewe kupata.
- (vii) Vile vile awe tayari kuwahudumia wengine kabla yeye hajahudumiwa.
- (viii) Asiache kula na kunawa kabla ya wengine. Hata kama ameanza kushiba, itabidi aendeele kidogo kidogo mpaka wote washibe kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Ibn Umar ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Nguo ya chakula inapotandikwa, hapana mtu atakayesimama mpaka nguo hiyo iondolewe wala hapana mtu atakayetoa mkono wake kwenye chakula hata kama ameshiba mpaka watu wote wamemaliza kula. Ikibidi aache kula kabla ya wengine, na awatake radhi kwani bila ya kufanya hivyo atawavunja moyo (atawanyima raha) wenzake... (Ibn Majah).*

(ix) Asikosoe chakula au kinywaji mbele ya wengine.

*Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume(s.a.w) hakuwahi kubainisha ubaya wa chakula (au kukiadhiri chakula) chochote kama alikipenda chakula alikila na akama hakukipenda chakula aliacha kula(Bukhaary na Muslim).*

## **Michezo na Burudani**

Uislamu ni utaratibu wa maisha uliokamilika. Umebainisha namna ya kuliendea kila jambo linalohitajika katika kuendesha maisha ya mwanaadam ya kila siku katika kila uwanja ili kumuinua mwanadamu kimwili, kiutu na kijamii. Michezo ni miongoni mwa vipengele hivi. Uislamu unawataka watu wacheze na kufurahia lakini kwa kuchunga mipaka iliyowekwa na kuzingatia lengo la maisha ya mwanadamu hapa ulimwenguni.

## **Michezo Iliyohusiana katika Uislamu**

Michezo yote ambayo humfanya mchezaji kupata uwezo zaidi wa kiafya na kiakili wa kumuabudu Allah(s.w) inasisitizwa kufanywa na Uislamu. Mtume(s.a.w) amesema: “Afya kwa mtu anayemwogopa Allah(s.w) ni bora kuliko utajiri”. Mara kwa mara Mtume(s.a.w) katika kusisitiza afya njema ya mwili na akili amesema: “Waumini (wacha Mungu) wote mbele ya Allah ni sawa lakini aliyebora zaidi ni yule mwenye siha nzuri zaidi”. Hivyo, michezo yote isiyochupa mipaka ya Allah(s.w) itakayochezwa kwa lengo la kujenga afya ya mwili na akili haikukatazwa katika Uislamu.

Aidha, michezo yote ya mazoezi ya kivita kama vile kulenga shabaha, kutupa mkuki, kareti, mieleka, mbio za farasi, imesisitizwa na Uislamu. Ikumbukwe kuwa Waislamu ni askari wa Allah(s.w) ambao daima wanatakiwa wawe tayari kupigana na maadui wa Uislamu na Waislamu mara watakapoanza kuwachokoza. Kazi ya kupigania dini ya Allah(s.w) haikupachikwa kwa jeshi maalumu lililoandaliwa kwa kazi hiyo, bali hiyo ni Ibada inayomuhusu kila Muislamu.

Utbah bin Amir ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: “Kila mchezo atakaocheza mtu ni haramu ila kutupa mishale, kumfunza farasi wake na kucheza na mkewe. Hakika hii ndio michezo ya kweli (yenye faida).

Pamoja na kwamba michezo yote hii iliyotajwa katika Hadith hii inatoa mazoezi ya mwili na kuituliza akili bado kuna faida za ziada zinazopatikana. Ambapo michezo miwili ya kwanza inampa Muislamu mazoezi ya kijeshi, mchezo wa kucheza mtu na mkewe chumbani au katika mazingira ya nyumbani kwao, huimarisha furaha na upendo katika familia.

## Michezo Iliyoharamishwa katika Uislamu

Michezo iliyoharamishwa katika Uislamu tunaweza kuigawa katika mafungu mawili:

**Kwanza**, uharamu unaotokana na kuchupa mipaka ya Allah(s.w). Hata kama atacheza michezo iliyoruhusiwa kwa nia nzuri ya kuupa mwili mazoezi, kujipa mazoezi ya kijeshi n.k. itakuwa ni haramu michezo hiyo endapo atachupa mipaka ya Allah(s.w) katika uchezaji wake kama vile kucheza na bukta hadharani, kupita wakati wa swala, kutumia lugha chafu, n.k.

**Pili**, kucheza michezo yote iliyoharamishwa katika Qur-an na inayofanana na hiyo. Michezo yote ya kamari au ya kibahati nasibu (games of chance) na yenye mfano wa hiyo imekatazwa katika Qur-an:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَزْلَمُ رِجْسٌ مِّنْ  
عَمَلِ الشَّيْطَانِ فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٩٠﴾

*Enyi mlioamini! Bila shaka ulevi na kamari na kuabudiwa (au kuombwa) asiye kuwa Mwenyezi Mungu, na kutazamia (kupiga ramli, utabiri, n.k.) ni uchafu na ni kazi ya shetani. Basi jiepusheni navyo ili mpate kufaulu. (5:90).*

Michezo yote ya kibahati nasibu kama vile michezo yote ya pata-potea, karata, dama, bao, chess na michezo yote ya mashindano kama vile mpira riyadha, ndondi, n.k. imeharamishwa kwa sababu inaleta madhara makubwa katika jamii. Pamoja na faida inayotazamiwa katika michezo hiyo, madhara yake ni makubwa zaidi. Hili anatumia Allah(s.w) katika Qur-an:

﴿ يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ ۖ قُلْ فِيهِمَا إِثْمٌ كَبِيرٌ وَمَنْفَعَةٌ  
لِّلنَّاسِ وَإِثْمُهُمَا أَكْبَرُ مِنْ نَّفْعِهِمَا ۗ ..... ﴾

*Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari, Sema: Katika hivyo mna madhara makubwa na manufaa kwa (baadhi ya) watu. Lakini madhara yake ni makubwa zaidi kuliko manufaa yake.... (2:219).*

Pamoja na madhara mengine mengi madogo na makubwa yanayotokana na michezo ya kikamari (kibahati nasibu), madhara makuu yamebainishwa katika Qur-an kama ifuatayo:

Hakika Shetani anataka kukutilieni uadui na bughudha baina yenu kwa ajili ya ulevi na kamari na anataka kukuzuilieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na (kukuzuilieni) kuswali. Basi, je hamtaacha (mabaya hayo)?

Madhara makubwa ya michezo yote ya kikamari kama yalivyobainishwa katika aya hii ni:

- (a) Kusababisha uadui na bughudha.
- (b) Kuwazuilia waumini kumkumbuka Allah(s.w)
- (c) Kuwazuilia waumini kuswali (kwa wakati).

Hebu tuangalie madhara haya kwa kuzingatia hali halisi ya michezo ambayo imepewa nafasi kubwa na kuundiwa wizara katika jamii za kitwaghati.

***(a) Michezo ya Kikamari Husababisha Uadui na Bughudha***

Wale wote wanaojihusisha au waliowahi kujihusisha na michezo hii watakuwa mashahidi wa ukweli huu. Ilivyo kawaida ni kwamba anayepata ushindi katika michezo hiyo hufurahia na kujiona na yule anayeshindwa huchukia na huwa na hisia za kutaka kulipiza kisasi. Kwa ujumla katika michezo ni furaha na ufakhari kwa mshindi na ni huzuni na chuki kwa aliyeshindwa. Ukichanganya hali hizi mbili unachotarajia ni nini kama sio uadui na bughudha baina ya wachezaji wa pande mbili. Kuteta, kusengenya, matusi na utani ni lugha ya kawaida ya michezo. Uadui kati ya timu mbili za mpira na washabiki wake si jambo geni kwetu. Watu kuuana kutokana na kudhulumiana katika michezo ya kamari si jambo geni.

Utashangaa vipi dola za kitwaghati zinaipa michezo hii kipaumbele! Kisingizio chao kikubwa ni kwamba inaleta ushirikiano na kujenga udugu. Hii ni kauli ya uongo inayopingana na hali halisi. Tumeelezwa kuwa michezo ya kikamari na ya mashindano ni kazi ya Shetani. Ni muhali kutokea ushirikiano na upendo katika uwanja wa michezo ambapo Shetani ndiye mgeni rasmi.

***(b) Michezo ya Kikamari (Games of chance) huwazuilia Waumini kumkumbuka Allah(s.w)***

Kila mchezaji au aliyeshuhudia michezo ya karata, bao, chess, gudugudu, na michezo mingine yote ya kibahati nasibu (games of chance), pamoja na mchezo wa mpira, anafahamu vyema jinsi michezo hii inavyopoteza muda na kumsahaulisha mtu na majukumu muhimu ya maisha yake binafsi, familia na jamii kwa ujumla. Ni mara ngapi tunawaona watu wazima na akili zao na wenye majukumu mengi mbele yao, wakishinda kutwa wanacheza bao bila hata kula.

Ni mara ngapi tunaona wakati umetangazwa mchezo kati ya timu mbili maarufu za mpira, watazamaji wakihudhuria uwanjani saa mbili asubuhi na kungojea humo uwanjani mpaka saa kumi alasiri, mechi itakapoanza?

Ni jambo la kawaida vile vile kuwakuta watu wazima na nguvu zao na akili zao timamu wakitumia muda mrefu katika michezo ya karata na mingineyo kama hiyo. Michezo yote hii hupumbaza wachezaji na watazamaji wasiweze kufikiri mambo ya msingi ya maisha yao. Utashangaa kwa nini michezo ya aina hii inapewa kipaumbele katika jamii za kitwaghuti hasa kwa vijana wa mashuleni na mitaani. Bila shaka huu ni mpango wa kuwapumbaza vijana ili watawala madhalimu waendeleo kuiendesha jamii watakavyo kwa maslahi yao binafsi.

Katika Uislamu michezo yote inayompumbaza mtu asitekeleze majukumu yake na kuliendea lengo lake la kuwepo hapa ulimwenguni imeharamishwa na atakayejitumbukiza humo atakuwa miongoni mwa watu wa motoni kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ رَهِينَةٌ ﴿٧٨﴾ إِلَّا أَصْحَابَ آيْمِينٍ ﴿٧٩﴾ فِي جَنَّتٍ  
يَتَسَاءَلُونَ ﴿٤٤﴾ عَنِ الْمُجْرِمِينَ ﴿٤١﴾ مَا سَلَكَكُمْ فِي سَقَرٍ ﴿٤٢﴾ قَالُوا  
لَمْ نَكُ مِنَ الْمُصَلِّينَ ﴿٤٣﴾ وَلَمْ نَكُ نُطْعِمُ الْمَسْكِينِ ﴿٤٤﴾ وَكُنَّا  
نُحْوِضُ مَعَ الْخَائِضِينَ ﴿٤٥﴾

*Kila nafsi itafungika (motoni) kwa amali (mbovu) ilizozichuma. Isipokuwa watu wa kuliani, wanaulizana juu ya watu wabaya: Ni kipi kilichokupelekeni motoni? Waseme: Hatukuwa miongoni mwa waliokuwa wakisali, wala hatukuwa tunalisha masikini. Na tulikuwa tukizama (katika upuuzi) pamoja na waliokuwa wakizama. (74:38-45).*

Lengo la maisha ya mwanadamu ni kumtumikia Allah(s.w) kwa kusimamisha Ufalme wake katika jamii kwa kuhakikisha kwa hali na mali kuwa utaratibu wa maisha unaofuatwa na jamii ni ule aliouweka Yeye. Ili kufikia lengo hili kuu, kila wakati mwanadamu anatakiwa akumbuke uhusiano wake na Allah(s.w) na daima akumbuke kuwa yeye hapa ulimwenguni ni Khalifa wa Allah(s.w). Mtu aliyezama kwenye michezo ya upuuzi inayopoteza muda na kupumbaza ni muhali kuwa na kumbukumbu hizi hata kama atajiita Muislamu. Waislamu hasa waliofuzu mbele ya Allah(s.w) ni wale wanaojiepusha na michezo yote ya upuuzi (laghwi) kama tunavyojifunza katika Qur-an:

قَدْ أَفْلَحَ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ الَّذِينَ هُمْ فِي صَلَاتِهِمْ خَاشِعُونَ ﴿٢﴾ وَالَّذِينَ  
هُمْ عَنِ اللَّغْوِ مُعْرِضُونَ ﴿٣﴾

*Hakika wamefuzu Waislamu, ambao katika swala zao huwa ni wanyenyekevu. Na ambao hujiiepusha na mambo ya upuuzi. (23:1-3).*



Katika suratul Furqaan tunafahamishwa kuwa miongoni mwa sifa za waja wa Rahman ni pamoja na wale ambao hawajihusishi na mambo ya upuuzi, hata tu kuwa watazamaji:

وَالَّذِينَ لَا يَشْهَدُونَ الزُّورَ وَإِذَا مَرُّوا بِاللَّغْوِ مَرُّوا كِرَامًا

*Na wale ambao hawashuhudii shahada za uwongo, na wanapopita penye upuuzi, hupita kwa heshima (zao) (25:72)*

### **(c) Michezo ya Upuuzi huwazuilia Waumini kuswali**

Michezo ya upuuzi kama vile mpira, bao, karata, n.k huwapumbaza wachezaji na wasikilizaji kiasi cha kujenga tabia ya kupuuzi swala. Tumeyashuhudia haya katika magenge ya mabao. Ni jambo la kushangaza kuwakuta Waislamu wakiendelea na bao kuanzia asubuhi mpaka jioni na kupitwa na swala zote za kutwa kisha huziswali kadha wakati wa isha, jambo ambalo halimo kabisa katika utaratibu wa kusimamisha swala tano. Swala ni faradhi kuswali katika wakati wake maalumu.

..... إِنَّ الصَّلَاةَ كَانَتْ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ كِتَابًا مَوْقُوتًا

*“... Kwa hakika swala kwa Waislamu ni faradhi iliyowekewa nyakati makhususi”. (4:103).*

Swala ndio zana ya kumuwezesha Muislamu kumuabudu Mola wake ipasavyo na humuwezesha kuishi kwa nidhamu katika jamii kama Khalifa wa Allah(s.w). Nidhamu katika jamii haipatikani pale ambapo swala imepuuzwa.

Hivyo michezo yote inayomtoa mtu katika lengo la kuumbwa kwake ni michezo ya upuuzi na Muumini wa kweli hana budi kujiepushia mbali na michezo hiyo.

## **Sherehe na Burudani**

Maisha ya mwanadamu yamezungukwa na furaha na majonzi penye furaha watu hushereheka na penye msiba watu huomboleza. Katika kipengele hiki tutazingatia sherehe na burdani katika jamii ya Kiislamu ukilinganisha na jamii za kitwaghuti. Katika jamii ya kitwaghuti iliyozunguka tunawaona watu wakijiburudisha na kujitumbuiza katika sherehe zao kwa ngoma, disco, nyimbo, mashairi, ngonjera n.k. Je, Uislamu unamtazamo upi juu ya sherehe na burdani na kushereheka kwa Waislamu kunatofautianaje na kushereheka kwa majahili?

Majahili hawajui halali wala haramu katika sherehe zao na katika kushereheka kwao. Kwa maana nyingine majahili hawajali kuona nafasi ya sherehe iliyo mbele yao kuwa ni yenye kumridhisha Allah(s.w) au ni yenye

kumchukiza na katika kushereheka kwao hawana habari na mipaka ya Allah(s.w) aliyoiweka.

## Sherehe ya Kiislamu ni Tofauti sana na Hizi za Kitwaghuti.

Kwanza katika Uislamu, sherehe yoyote ile inayopingana na hukumu za Allah(s.w) ni haramu na hivyo si ruhusa Waislamu kushiriki. Kwa mfano ni haramu kwa Waislamu kuitika mwito wa harusi ya kumuoza binti wa Kiislamu kwa Mkristo au kwa yeyote asiyekuwa Muislamu. Halikadhalika ni haramu kwa Waislamu kujiunga na sherehe zozote zile za kidini minghairi ya Uislamu. Kwa mfano, kama ilivyo haramu kwa Waislamu kujitumbukiza katika sherehe za matambiko ya aina yote ndivyo ilivyo haramu kwa Waislamu kushereheka Krismas, Mwaka mpya na Pasaka.

Jambo la pili linalozingatiwa na Waislamu katika sherehe zao ni uchungaji wa mipaka ya Allah(s.w) katika kushereheka kwenyewe. Vyakula na vinywaji vitakavyotumika katika sherehe havina budi kuwa halali, vitolewe bila ya kufanya israfu na pasiwe na ubaguzi wowote katika kuvigawanya.

*Imesimuliwa na Abu Hurairah kuwa Mtume(s.a.w) amesema: “Karamu ya harusi iliyo mbaya kuliko zote ni ile ambayo wamealikwa matajiri wakaachwa masikini” (Bukhaary na Muslim).*

Kwa ujumla sherehe za Kiislamu zinatakiwa ziambatanishwe na kutoa sadaqa ili kuwafurahisha majirani na wenye matatizo. Maandalizi ya sherehe za Kiislamu kuanzia hatua ya mwanzo hadi ya mwisho hayanabudi kuzingatia mipaka yote ya Allah(s.w). Kilele cha sherehe za Kiislamu kinafikiwa kwa kumtaja Allah(s.w) na kumtaka maghfira. Qur-an inatuongoza kuwa:

إِذَا جَاءَ نَصْرُ اللَّهِ وَالْفَتْحُ ﴿١﴾ وَرَأَيْتَ النَّاسَ يَدْخُلُونَ فِي دِينِ اللَّهِ

أَفْوَاجًا ﴿٢﴾ فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَأَسْتَغْفِرْهُ إِنَّهُ كَانَ تَوَّابًا ﴿٣﴾

*Itakapofika nusra ya Mwenyezi Mungu na kushinda. Na ukawaona watu wakiingia katika dini ya Mwenyezi Mungu makundi makundi. Basi hapo mtakase Mola wako pamoja na kumsifu, umuombe maghufira (msamaha) hakika yeye ndiye apokeaye toba. (110:1-3).*

Katika aya hizi tunakumbushwa kuwa hatuna budi kukumbuka daima kuwa ushindi au furaha ya aina yoyote analeta Allah(s.w). Hivyo, katika hali hiyo ya furaha hatuna budi kumshukuru Allah na kumsifu kwa sifa zake na kumuomba msamaha kwa makosa yetu ili furaha hiyo tuliyoipata hapa duniani iwe yenye kuendelea katika maisha ya akhera, Muislamu kamwe hatathubutu kujihashirisha na kujitumbukiza katika huzuni ya milele katika maisha yake ya akhera kwa sababu ya furaha zidaganyazo za hapa duniani.

Furaha ya kweli kwa Muislamu ni ile iliyoambatana na Radhi za Allah(s.w). Na lolote lile linalomghadhibisha Allah(s.w) ni msiba na huzuni kubwa kwa Muislamu hata kama limesherehekewa na walimwengu wote.

Hebu sasa tuanglie mtazamo wa Uislamu juu ya matumizi ya ngoma, “disco”, nyimbo na mashairi kama burdani na kama sehemu ya sherehe.

### **Ngoma na “Disco”.**

Michezo yote ya ngoma, disco, dansi, n.k. kama tuionavyo katika utamaduni wa jamii hizi za kijahili, ni haramu kwa sababu zifuatazo:

**Kwanza**, ni laghwi yaani michezo ya upuuzi kwani huwafanya watu wapoteze muda mwingi nje ya lengo la kuumbwa kwao hapa ulimwenguni. Yaani michezo hii ya ngoma na “disco” huwasahaulisha wachezaji na watazamaji kumkumbuka na kumtukuza Allah(s.w). Kwa hiyo michezo hii ya ngoma ni miongoni mwa kazi ya shetani na Allah(s.w) ametukataza kushiriki katika shughuli zote za Shetani.

**Pili**, michezo mingi ya ngoma na “madisco” huchezwa katika mchanganyiko wa wanawake na wanaume na huwa ni vichocheo vikubwa sana vya zinaa. Katika Uislamu ni haramu kushiriki katika shughuli yoyote inayochochea zinaa.

وَلَا تَقْرُبُوا الزُّنَىٰ ۗ إِنَّهُ كَانَ فَحِشَةً وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿٣٢﴾

*Wala msikaribie zinaa. Hakika hiyo ni uchafu mkubwa) na njia mbaya (kabisa). (17:32)*

Katika sherehe za harusi wanawake wameruhusiwa kupiga dufu na kuimba nyimbo ambazo hazichupi mipaka ya Allah(s.w) kama tunavyojifunza katika sunnah. Hapana kamwe katika mafundisho ya Mtume(s.a.w) ambapo dufu limetiliwa mkazo kama Waislamu wanavyolitilia leo hii.

### **Nyimbo na Mashairi**

Nyimbo na mashairi huwa halali au haramu kutegemeana na madhumuni ya nyimbo au mashairi hayo. Ni wazi kuwa nyimbo au mashairi ya kimapenzi ambayo ni vichochezi vya zinaa ni haramu moja kwa moja. Pia mashairi au nyimbo ambazo ndani yake kuna lugha mbaya, au kuna kuitukana au kuipinga dini ya Allah(s.w), basi mashairi hayo au nyimbo hizo zitakuwa ni haramu. Hali kadhalika mashairi na nyimbo ambazo ziko pale kumpotezea mtu muda wake ni laghwi na ni haramu.

Nyimbo na mashairi ambayo ndani yake kuna hekima na mafunzo ya aina mbali mbali ambayo hayaambatani na sauti na midundo ya ngoma za miziki, yanakubalika katika Uislamu. Nyimbo na mashairi ya Kiislamu hayana budi

kumuelekeza Muislamu katika kumcha Mwenyezi Mungu zaidi na katika kumpa nguvu na hamasa ya kupigania dini ya Allah(s.w). Tunajifunza katika Hadith ya Bukhaary na Muslim iliyosimuliwa na Jundub kuwa Mtume wa Allah(s.w) alijipooza kishairi alipoumia vidole vyake katika vita vya Uhud.

Alijiliwaza katika shairi hilo kuwa kutokwa na damu kwake si kwa sababu nyingine ila ni kwa ajili ya Allah(s.w) na kwa ajili ya dini yake. Pia katika Hadith nyingine ya Bukhaary na Muslim iliyosimuliwa na Barasi, tunajifunza kuwa Mtume(s.a.w) aliimba wimbo wa kuwatia nguvu Waislamu walipokuwa katika kazi ngumu sana ya kuchimba handaki katika vita vya Handaki wakati Waislamu wapatao alfu mbili (2,000) tu walipovamiwa mjini mwao na jeshi la watu wapatao alfu ishirini na nne (24,000) mnamo 5 A.H. Wimbo huu umesheheni na maneno ya hekima na kuwapelekea Waislamu kuwa imara kwa kumtegemea Allah(s.w). Hakika Allah(s.w) aliwanusuru Waislamu katika vita hivyo.

## Misiba na Maombolezo

Misiba na maombolezo ni miongoni mwa vipengele vya utamaduni wa jamii. Kila jamii ina namna yake ya kupokea misiba na kuomboleza. Katika jamii za kijahili misiba yote imeambatanishwa na mkono wa mwanadamu au nguvu zinazotokana na maumbile asili yaliyomzingira mwanadamu.

Maombolezo ya misiba, kama vile maombolezo ya vifo, katika jamii za kijahili huambatana na malalamiko, lawama, masononeko. Wengine, katika kupunguza msononeko hulewa sana, huhezeshia ngoma na hufanya kila jambo lingine litakalowapumbaza ili wasahau kifo.

Mtazamo wa Uislamu juu ya misiba na maombolezo yake ni tofauti kabisa na mitazamo ya kijahili, Waislamu wanamini kuwa kila jambo hutokea kwa Qadar ya Allah(s.w) pamoja na kwamba kila jambo linalotokea limeambatanishwa na sababu za kimaumbile. Kwa mfano ni kawaida kuwa ukimkata mtu shingo kwa kisu kilichokikali atachinjika na atakufa lakini haitatokea hivyo iwapo kitendo hicho hakikulandana na Qadar ya Allah(s.w). Nabii Ismail(a.s) hakuchinjika pamoja na jitihada za baba yake – Ibrahimu (a.s) za kumchinja kwa kisu kikali sana. Mwenyewe Nabii Ibrahim(a.s) hakuungua moto alipotumbukizwa kwenye moto mkubwa na mkali kwa kuwa kitendo hicho cha kumuua kwa kumchoma moto hakikulandana na Qadar ya Allah(s.w). Kutokana na mifano hii miwili tunaona wazi kuwa hautokei msiba wowote ila uko mikononi mwa Allah(s.w):

مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي أَنْفُسِكُمْ إِلَّا فِي كِتَابٍ مِّن  
 قَبْلٍ أَنْ نَبْرَأَهَا إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٢٢﴾ لِكَيْلَا تَأْسَوْا عَلَىٰ مَا  
 فَاتَكُمْ وَلَا تَفْرَحُوا بِمَا آتَاكُمْ وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ ﴿٢٣﴾

*Haitokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwisha andikwa katika kitabu kabla hatujaumba; hakika jambo hilo ni jepesi kwa Allah. Ili msihuzunike sana juu ya kitu kilichokupoteeni wala msifurahi sana kwa alichokupeni. Na Mwenyezi Mungu hampendi kila ajivunaye, ajifaharishaye. (57:22-23).*

Kwa mtazamo wa Uislamu, furaha na huzuni ndio hali halisi ya mazingira ya ulimwengu na yote ni mitihani kwa mwanadamu. Mwanadamu mwenye akili atakayefaulu vizuri mtihani huu wa furaha ni yule anayefahamu fika kuwa furaha zote anazozipata katika ulimwengu huu zimetoka kwa Allah(s.w) ili kumjaribu kuwa atakuwa ni mwenye shukurani na kutumia furaha hizo kwa kumtukuza Allah(s.w) na kumuabudu inavyostahiki ikiwa ni pamoja na kumuomba msamaha kutokana na udhaifu wake wote uliompelekea kumkosea Bwana Mlezi (Rabb) wake.

Atakayefurahia maisha yake hapa ulimwenguni kama kwamba yeye mwenyewe binafsi au wengine katika wanadamu ndio chanzo cha furaha hizo na kwa hiyo akafurahia atakavyo bila ya kujali mipaka aliyoweka Allah(s.w), basi atakuwa ni mwenye kubunda katika mtihani wa furaha.

Na mwanadamu mwenye akili atakayestahiki kufaulu mtihani wa msiba ni yule anayefahamu vyema kuwa mtu hawezi kufikwa na msiba wowote ila Allah(s.w) apende; kuwa hapana mtu yeyote awezaye kumletea mtu msiba iwapo Allah(s.w) hakumwandikia msiba huo na wala hapana yeyote awezaye kumuondolea mtu msiba iwapo Allah(s.w) amemuandikia msiba huo.

Atafulu mbele ya Allah(s.w) yule ambaye anapofikwa na msiba hapapatiki, hanung'uniki na kulalama bali huupokea msiba huo kwa moyo mkunjufu na kuridhia kuwa huo ni utaratibu wa Allah(s.w) usio na makosa na kwamba kila alilolipanga Allah(s.w) ni lenye kumnufaisha mwanadamu. Namna Waislamu wanavyotakiwa waipokee misiba imebainishwa katika aya zifuatazo:

وَلَنْبَلُونَكُمْ بِشَيْءٍ مِّنَ الْخَوْفِ وَالْجُوعِ وَنَقْصٍ مِّنَ الْأَمْوَالِ وَالْأَنْفُسِ  
 وَالشَّمْرَاتِ ۗ وَبَشِّرِ الصَّابِرِينَ ﴿١٥٥﴾ الَّذِينَ إِذَا أَصَابَتْهُمُ مُصِيبَةٌ قَالُوا  
 إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ ﴿١٥٦﴾

*Na tutakutieni katika msukosuko wa (baadhi ya mambo haya); khofu na njaa na upungufu wa mali na wa watu na matunda. Na wapashe habari njema wanaosubiri. Ambao uwapatapo msiba husema: Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake yeye tutarejea (atatupa jaza yake)". Hao juu yao zitakuwa baraka zitokazo kwa Mola wao na Rehema, na ndio wenye kuongoka. (2:155-157).*

Waislamu wanapopatwa na msiba wanatakiwa wasubiri kama iliyobainishwa katika aya hizi na pia wanatakiwa wamuombe Allah(s.w) awawezeshe kuwa miongoni mwa wenye subira na awabariki na kuwarehemu kutokana na msiba hiyo. Katika Hadith iliyosimuliwa na Abu Hurairah, Mtume(s.a.w) amesema:

*Allah(s.w) atasema: "Hapana zawadi mbele yangu ila Pepo kwa mja wangu ambaye ninapomfisha kipenzi chake miongoni mwa watu katika dunia huomba ujira mwema kutokana na msiba huo." (Bukhaary).*

Waislamu wanawajibika kuwapa mkono wa pole na kuwaliwaza wale waliopatwa na msiba kwa maneno yafuatayo aliyotufunza Mtume(s.a.w): "Hakika kila alichokichukua Allah(s.w) ni chake na kile alichokitoa ni chake na kila kitu kitarejea kwake kwa muda maalum". Kwa hiyo kuwa mwenye subira na tarajia kupata malipo". (Bukhaary na Muslim). Tunajifunza vile vile katika Hadith kuwa, mwenye kumliwaza aliyepatwa na msiba amepata malipo sawa na yule aliyesubiri katika msiba:

*Abdullah bin Masud ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema "Anaye mliwaza yule aliyekuwa na msiba, kuna kwake malipo sawa na yule aliyefikwa na msiba". (Tirmidh, Ibn Majah)*

Iwapo kwa njia moja au nyingine Muislamu ataona kuwa msiba uliomtokea ni matokeo ya matendo yake maovu au kupuuza kwake mwongozo wa Allah(s.w), hana budi kujitupa kwa Allah(s.w) kwa toba ya kweli na kusubiri na sio kukata tamaa. Kwani pamoja na kukosea kwake, Allah(s.w) ameahidi kumsamehe kama tunavyojifunza katika Qur-an:

وَمَا أَصَابَكُمْ مِّنْ مُّصِيبَةٍ فَبِمَا كَسَبَتْ أَيْدِيكُمْ وَيَعْفُوا عَنْ كَثِيرٍ

*Na msiba inayokupateni ni kwa sababu ya vitendo vya mikono yenu, na (juu ya hivi Mwenyezi Mungu) anasamehe mengi. (42:30).*

## 7. Maombi na Dua

Ni katika utamaduni wa Kiislamu Muislamu kumtegemea Allah(s.w) kwa kila jambo. Muislamu wa kweli anafahamu vyema kuwa mafanikio yote hutokana na Allah(s.w). Hivyo anapopatwa na tatizo lolote hana budi kwanza kabisa kumuelekea Mola wake na kumuomba msaada kabla hajamuelekea mtu yeyote kwa msaada. Hii ndio ahadi tunayoitoa kila mara tusomapo suratul-Fatiha:

## إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٥﴾

*Wewe tu ndiye tunayekuabudu na wewe tu ndiye tunayekuomba msaada. (1:5).*

Hatuna budi kukumbuka kuwa matatizo na shida mbali mbali zinazotufika ni mtihani kwetu kuwa tutakuwa ni wenye kusubiri na kuomba msaada wa Allah(s.w) au tutapapatika na kutafuta misaada kwa wengine minghairi ya Allah(s.w). anaituita Allah(s.w) katika Qur-an:

## يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا اسْتَعِيْنُوْا بِالصَّبْرِ وَالصَّلٰوةِ ۗ اِنَّ اللّٰهَ مَعَ الصّٰبِرِيْنَ ﴿١٥٣﴾

*Enyi mlioamini! Jisaidieni (katika mambo yenu) kwa subira na swala bila ya shaka Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaosubiri. (2:153).*

Pia Waislamu hatuna budi kuwa na hakika, mia kwa mia, kuwa Allah(s.w) ni muweza wa kila kitu na halishindikani kwake jambo na kwamba ni mwenye kusikia maombi yetu na yukaribu zaidi kuliko tulivyo karibu na mshipa mkuu wa damu wa shingoni (jangular vain) mwetu:

## وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْاِنْسَانَ ۗ وَنَعَلْمُوْهُ مَا تُوَسْوِسُ بِهٖ نَفْسُهٗ ۗ وَنَحْنُ اَقْرَبُ اِلَيْهٖ

## مِّنْ حَبْلِ الْوَرِيْدِ ﴿١٦﴾

*Na bila shaka tumemuumba mtu nasi tunajua yanayopita katika nafsi yake, nasi tukokaribu naye zaidi kuliko mshipa wa shingo (yake). (50:16)*

Baada ya kuwa na uhakika wa namna hii hatuna budi kuyaelekeza maombi yetu moja kwa moja kwa Allah(s.w) kwa matumaini makubwa ya kupata kila tunachokiomba. Tunajifunza katika aya zifuatazo namna ya kumuomba Allah(s.w):

## وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيْبٌ ۗ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدّٰعِ إِذَا دَعَانِ ۗ

## فَلْيَسْتَجِيبُوْا لِيْ وَلْيُؤْمِنُوْا بِيْ لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُوْنَ ﴿١٨٦﴾


*Na waja wangu watakapokuuliza hakika yangu (waambie kuwa) mimi niko karibu nao. Naitikia maombi ya mwombaji anaponiomba. Basi na waniitikie na waniamini, ili wapate kuongoka. (2:186).*



 أَدْعُوا رَبَّكُمْ تَضَرُّعًا وَخُفْيَةً إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ

*Mwombeni Mola wenu kwa unyenyekevu na kwa siri (kwa suati ndogo bila ya kufanya kelele). Yeye (Mwenyezi Mungu) hawapendi wapitao mipaka(7:55).*

Katika aya hizi tunajifunza yafuatayo:

**Kwanza**, tunatakiwa tumuombe Allah(s.w) moja kwa moja bila ya kupitishia maombi yetu kwa yeyote yule na wala tusiombe kwa baraka za yoyote yule. Kumuomba Allah kwa baraka za yeyote au kupitia kwa yeyote ni kumdunisha Allah(s.w) na kukanusha Qur-an (2:186). Tunaamrisha tumuombe Allah(s.w) na kwa baraka zake na majina yake matukufu:


 وَلِلَّهِ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ فَادْعُوهُ بِهَا وَذَرُوا الَّذِينَ يُلْحِدُونَ فِي أَسْمَائِهِ


 سَيُجْزَوْنَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

*Na Mwenyezi Mungu ana majina (sifa) mazuri mazuri, muombeni kwayo, na waacheni wale wanaoharibu utukufu wa majina yake. Karibuni hivi watalipwa yale waliyokuwa wakitenda. (7:180).*

**Pili**, tunatakiwa pia tumuombe Allah(s.w) kwa unyenyekevu, na kwa siri sio kwa kupiga makelele. Ili tuwe wanyenyekevu kwa Allah(s.w) wakati wa kuomba hatuna budi kuomba kwa lugha tunayoifahamu vyema. Tukiwa ndani ya swala tutaomba kwa lugha ya Kiarabu lakini hatuna budi kufahamu tafsiri au maana ya yale tunayoyaomba.

**Tatu**, vile vile tunatakiwa wakati wa kumuomba Allah(s.w) tuwe na khofu kwa kuzingatia Hadhi yake na Utukufu wake na papo hapo tuwe na yakini kuwa ameyasikia maombi yetu na atatujibu kulingana na ahadi yake, kwani yeye ni muweza wa kutujibu na si mwenye kukhalifu miadi yake.

**Nne**, sharti kubwa tunalotakiwa tulitekeleze ili maombi yetu yajibiwe ni kumuitikia Allah(s.w). Kumuitikia Allah(s.w) ni kumuamini Allah(s.w) inavyostahiki na kumuabudu ipasavyo kwa kumtii kwa unyenyekevu katika kukiendea kila kipengele cha maisha yetu ya kila siku. Kuchunga mipaka yote ya Allah(s.w) kwa kutekeleza maamrisha yake yote na kujiepusha mbali na makatazo yake yote ni katika kumuitikia Allah(s.w). Hivyo ili yajibiwe maombi yetu mbalimbali tunayomuomba Allah(s.w), hatuna budi kujitahidi kwa kadri ya uwezo wetu kufuata utaratibu wa maisha aliotufunulia Allah(s.w) katika kuendesha maisha yetu ya kila siku.

Waislamu hatupaswi kumuomba Allah(s.w) tukiwa na shida au tunapohitajia msaada tu wa maisha ya dunia, bali tunatakiwa tumuombe Allah(s.w) nyakati



zote, tukiwa katika furaha au tukiwa katika matatizo. Tukiwa katika furaha tunatakiwa tumuombe Allah(s.w) aijaalie furaha hiyo iwe yenye kheri. Tukiwa katika matatizo tunamuomba Allah(s.w) atuondolee matatizo hayo na atulipe ujira mwema kutokana na kusubiri kwetu juu ya matatizo hayo na iwe ni sababu ya kutusamehe makosa yetu. Kwa mtazamo huu Muislamu katika nyakati zote na katika hali zote yuko katika lbada ya Allah(s.w) na hupata thawabu (ujira mwema mbele ya Allah(s.w)) akiwa katika dhiki au katika furaha. Kwa ujumla tunatakiwa katika maombi yetu, tumuombe Allah(s.w) atupe mema ya hapa duniani na huko akhera na atuondolee dhiki ya hapa duniani na adhabu kali ya huko akhera.

..... رَبَّنَا إِنَّا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةٌ وَفِي الآخِرَةِ حَسَنَةٌ وَقِنَا عَذَابَ



“...Mola wetu! Tupe mema duniani na (tupe) mema akhera, na utulinde na adhabu ya moto. (2:201)

Dua mashuhuri ambazo tunaweza kuzitumia katika kumuomba Allah(s.w) ni zile zilizoombwa na waja wake mbali mbali kama zilivyobainishwa katika Qur-an na zile alizozitumia Mtume Muhammad(s.a.w) katika kumuomba Mola wake katika hali na nyakati mbali mbali kama zinavyobainika katika Hadith mbali mbali. Hapa tumejaribu kubainisha aya za Qur-an mnamopatikana dua mbali mbali walizoomba waja wa Allah(s.w).

Dua ya Adam(a.s) na Hawa ya kuomba msamaha baada ya kumkosea Mola wao kwa kula tunda walilokatazwa: (7:23)

Dua alizoomba Nabii Nuhu (a.s):

(23:26), (26:117-118), (54:10), (71:26-28), (11:41), (11:45), (11:47), (23:29).

Dua ya Nabii Swaleh (a.s): (23:39)

Maombi ya Nabii Ibrahim (a.s)

(2:126-129), (14:35-41), (26:83-89), (37:99-100), (60:4-5).

Maombi ya Nabii Lut (a.s):

(26:169), (29:26), (29:30).

Maombi ya Nabii Ayyub (a.s)

(21:83), (38:41).

Maombi ya Nabii Yusuf (a.s)

(12:33), (12:101).

Dua ya Nabii Shuayb (a.s)

(7:89).

Maombi ya Nabii Mussa (a.s)

(28:16), (28:17), (28:21), (28:24), (7:148), (20:25-35), (7:151), (10:88),  
(7:155-156), (2:67), (5:25).

Maombi ya wafuasi wa Nabii Mussa(a.s):

(10:85-86), (7:126).

Dua ya Bi Asia, Mkewe Firaun: (66:11).

Maombi ya watu wa Talut wakati walipokuwa wakipambana na Jaluti (Mfalme wa Maadui): (2:250).

Dua ya Nabii Sulaiman (a.s): (27:19), (38:35).

Dua ya Malkia wa Sheba – Bibi Bilqis: (27:44).

Dua ya Nabii Yunus (a.s) - (21:87).

Maombi ya Nabii Zakaria (a.s) – Mlezi wa Bibi Mariam:

(3:38), (19:4-6), (21:89).

Maombi ya Hannah – Mama wa Bibi Maryam – (3:35-36).

Maombi ya wafuasi wa Nabii Issa (a.s): (3:53).

Dua ya Vijana wa pangoni: (18:10).

Dua ya mwenye Bustani: (68:29).

Dua ya Mume na mke kabla ya mtoto kuzaliwa – (7:189).

Dua za Malaika: (11:73), (40:7-9).

Dua ya watu wema: (7:47)

Dua za Mtume Muhammad(s.a.w) na wafuasi wake:

(1:1-7), (2:156), (2:201), (2:286), (3:8-9), (3:16), (3:26-27), (3:191-194),  
(4:45), (5:83), (6:161-163), (9:59), (17:24), (20:114), (21:112), (23:93-  
94), (23:97-98), (23:109), (23:118), (25:65-66), (25:74), (39:46), (46:15),  
(59:10), (66:8), (113:1-5), (114:1-6).

### ***(vii) Kumkumbuka Allah(s.w) Saa 24***

Kumkumbuka Allah(s.w) muda wote wa maisha ndio lengo lililombele ya kila Muislamu wa kweli. Lengo la kuletwa kwetu hapa ulimwenguni ni kumuabudu Allah(s.w), yaani kumtumikia Allah(s.w) kwa unyenyekevu kwa muda wote wa maisha yetu. Kumtumikia Allah(s.w) kwa muda wote wa maisha

yetu kunawezekana tu endapo tutaendesha maisha yetu yote ya saa 24 kwa kuchunga barabara mipaka ya Allah(s.w) aliyotuwekea katika kukiendea kila kipengele cha maisha yetu katika kila fani ya mtu binafsi, familia, uchumi, siasa, utamaduni, sheria na fani nyinginezo za maisha ya jamii. Kuchunga mipaka ya Allah(s.w) kwa muda wote wa saa 24 katika kila kipengele na kila fani ya maisha ni jambo linalowezekana pale Muislamu atakapoibakisha akilini mwake kumbukumbu ya Allah(s.w) kila wakati. Ni vipi Muislamu ataweza kumkumbuka Allah(s.w) kila wakati?

**Kwanza**, Muislamu ataweza kumbukumbuka Allah(s.w) na utukufu wake kila wakati, endapo kila mara atazichunguza neema zote zilizomzunguka alizotunukiwa na Mola wake kisha akawa ni mwenye shukurani kwake kwa kumtii na kumtukuza ipasavyo. Pia Muislamu atazidi kukuza yakini juu ya uwezo na utukufu wa Allah(s.w) endapo atatafakari kwa makini umbile la mbingu na ardhi na vyote vilivyomo. Allah(s.w) anatumia akili zao vilivyo katika kutafakari maumbile yaliyowazunguka ndio pekee wanaoweza kumkumbuka na kuuona utukufu wake kwa muda wote wa saa 24.

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ لَآيَاتٍ لِّأُولِي  
 الْأَلْبَابِ ﴿١٩٠﴾ الَّذِينَ يَذْكُرُونَ اللَّهَ قِيَمًا وَقُعُودًا وَعَلَىٰ جُنُوبِهِمْ  
 وَيَتَفَكَّرُونَ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ رَبَّنَا مَا خَلَقْتَ هَذَا بَطْلًا  
 سُبْحَانَكَ فَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ﴿١٩١﴾

*Katika kuumbwa kwa mbingu na ardhi na mfuatano wa usiku na mchana, ziko hoja (za kuonyesha kuwepo Allah(s.w) na utukufu wake) kwa wenye akili. Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima, na wakiwa wamekaa na wakiwa wamelala. Na hutafakari juu ya umbile la mbingu na ardhi (kisha husema): Mola wetu! Hukuviumba hivi bure. Utukufu ni wako. Basi tuelewe na adhabu ya moto. (3:190 - 191).*

**Pili**, Muislamu ataweza kubakia katika kumkumbuka Allah(s.w) endapo atajitahidi kwa kadri ya uwezo wake kusimamisha swala tano za faradhi kama ipasavyo na pia akajitahidi kwa kadri iwezekanavyo kufuatilizia swala za Sunnah na hasa zile zilizokokotewa. Kazi ya swala iliyosimamishwa vilivyo katika kumuwezesha Muislamu aweze kumkumbuka Mola wake kwa nyakati zote imebainishwa wazi katika aya ifuatayo:

أَتْلُ مَا أُوحِيَ إِلَيْكَ مِنَ الْكِتَابِ وَأَقِمِ الصَّلَاةَ ۖ إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَىٰ  
عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ ۗ وَلَذِكْرُ اللَّهِ أَكْبَرُ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ ﴿٤٥﴾

*Soma uliyoletewa wahyi katika kitabu (hiki ulicholetewa) na usimamisha swala. Bila shaka swala (ikiswaliwa vilivyo) humzuilia (huyo mwenye kuswali na) mambo machafu na maovu, na kwa yakini (ndani ya swala) kuna kumkumbuka Mwenyezi Mungu kukubwa. Na Mwenyezi Mungu anajua mnayotenda. (29:45).*

**Tatu**, Muislamu ataweza kubakia katika kumkumbuka Allah(s.w) nyakati zote iwapo atajitahidi kwa kadri ya uwezo wake kutekeleza nguzo ya Zakat na kuwa mwepesi wa kutoa mali yake na kujitolea nafsi yake kwa ajili ya Allah(s.w) katika kusaidia na kutoa huduma mbali mbali za kijamii.

Pia Muislamu atabakia katika kumkumbuka Allah s.w) na utukufu wake kila wakati endapo atakamilisha nguzo ya funga ya Ramadhani na kuiambatanisha na funga za Sunnah kwa kadri ya uwezo wake kisha akatekeleza nguzo ya Hija iwapo anauwezo. Tukumbuke kuwa, lengo la nguzo tano za Uislamu ni kumtayarisha mja aweze kumtumikia Mola wake ipasavyo katika kila kipengele cha maisha yake.

**Nne**, kumsafia nia Allah(s.w) na kumtanguiliza katika kila kitendo tunachokifanya. Kabla hatujafanya kitendo chochote kile hatuna budi kukichunguza kitendo hicho kuwa kitatupelekea kupata radhi za Allah(s.w) au ghadhabu zake. Endapo kitendo hicho ni chema na chenye kutupelekea kupata radhi za Allah(s.w) tukifanye. Endapo kitendo hicho chema kitawaudhi makafiri, washirikina, wanafiki na maadui wengine wa Allah(s.w) tuisite kukifanya maadam matarajio yetu ni radhi za Allah(s.w) tu. Endapo kitendo hicho ni kiovu na chenye kutupelekea kughadhibikiwa na Allah(s.w) tukiache na kujiepusha mbali nacho hata kama kufanya hivyo kutawakasirisha walimwengu wote. Hii ndiyo tabia ya Waislamu wa kweli kama inavyobainishwa katika aya zifuatazo:

مَنْ جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ عَشْرُ أَمْثَالِهَا ۖ وَمَنْ جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَلَا تَجْزِيهِ إِلَّا  
مِثْلُهَا وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿٦١﴾

*Afanyaye kitendo kizuri (kila kitendo kilichofanywa kwa ajili ya Allah ni kitendo kizuri) atalipwa (mbele ya Allah) mfano wake mara kumi. Na afanyaye kitendo kibaya hatalipwa ila sawa nacho tu. Nao (wote hao) hawata dhulumiwa. (6:160)*

قُلْ إِنِّي هَدَيْتَنِي رَبِّيَ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ دِينًا قَيْمًا مِثْلَ آبَائِهِمْ حَنِيفًا  
وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٦١﴾

Sema: Kwa hakika mimi Mola wangu ameniongoza katika njia iliyonyooka, (katika) dini iliyosawa sawa kabisa ambayo ndiyo dini ya Ibrahim aliyekuwa mwongofu, wala kabisa hakuwa miongoni mwa washirikina. (6:161)

قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٦٢﴾

Sema: Hakika swala yangu, matendo yangu yote mengine, na uzima wangu, na kufa kwangu (yote) ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Muumba Mlezi wa walimwengu wote.(6:162)

يَفْقَهُونَ بِهَا وَهُمْ أَعْيُنٌ لَا يُبْصِرُونَ بِهَا وَهُمْ ءَاذَانٌ لَا يَسْمَعُونَ بِهَا  
أُولَئِكَ كَالْأَنْعَامِ بَلَّ هُمْ أَضَلُّ أُولَئِكَ هُمُ الْغَافِلُونَ ﴿١٦٣﴾

وَمِنْ حَيْثُ خَرَجْتَ فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَحَيْثُ مَا  
كُنْتُمْ فَوَلُّوا وُجُوهَكُمْ ..... ﴿١٦٤﴾

Na haya ndiyo niliyoamrisha, na mimi ni wa kwanza wa waliojisalimisha kwa Mwenyezi Mungu (6:163).

Tunajifunza katika aya hizi kuwa jambo lolote atakalolifanya Muislamu kwa ajili ya Allah(s.w) ni jambo jema (amali swalihi), na kila jambo jema analolifanya mja hulipwa ujira mwema (thawabu) kutokana na kitendo hicho mara kumi. Tunahimizwa kuwa katika lbada ya Allah(s.w) katika kila kitendo chetu. Muda tutakao kuwa nje ya lbada ya Allah(s.w) tutakuwa katika lbada (utumishi wa) ya wengine minghairi ya Allah(s.w) na bila shaka wakati huo tutakuwa ni washirikina. Jambo lingine ambalo ni la msaada kwetu litakalotupelekea kuyafanya matendo yetu yote yawe lbada ni kuanza kila jambo kwa jina la Allah, yaani kuanza kila jambo kwa “Bismillahir Rahmaanir Rahiim – “Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema Mwenye kurehemu”. Muislamu anatakiwa ajenge tabia ya kuanza kila jambo jema kwa “Bismillah”. Miongoni mwa faida kubwa zinazopatikana kwa Muislamu kwa kuanza kila jambo lake kwa “Bismillahir Rahmaanir Rahiim” huku akiwa anazingatia maana yake ni hizi zifuatazo:

- (1) Mtu anapoanza na “*Bismillah*” anatanguliza maombi yake ya kutaka msaada wa Allah(s.w), ili alifanikishe jambo hilo analotaka kulifanya kwa ajili yake.
- (2) Kuanza kila jambo kwa “*Bismillah*” kutamkinga kufanya mambo machafu na maovu kwani kama ni Muislamu wa kweli atamuonea haya Allah(s.w) na hatathubutu kufanya jambo ovu kwa jina lake.
- (3) Kitendo cha kuanza kwa “*Bismillah*” ni kitendo kinachompelekea Muislamu kuwa hadhiri na kile anachoanza kukifanya na humkumbusha kutia nia yake ya kufanya kitendo hicho kwa ajili tu ya kutafuta radhi za Allah(s.w).

## Zoezi la 2:7

1. (a) Eleza maana ya utamaduni
  - (b) Msingi wa Utamaduni wa Kiislamu ni Mila ya nani?
2. Kwanini ni muhimu kwa jamii kufuata Mila ya nabii Ibrahiim (a.s)
3. Orodhesha masharti ya vazi la Kiislamu
4. Taja mambo manne muhimu ambayo Qur’an inamtaka kila Muislamu ayazingatie katika kula na kunywa.
5. Orodhesha
  - (a) Vyakula vilivyoharamishwa kwa Muislamu.
  - (b) Vinywaji vilivyoharamishwa kwa Muislamu.
6. Eleza kwa muhtasari adabu anazotakiwa kuzitekeleza Muislamu katika kula.
7. (a) Michezo ina umuhimu gani kwa Muislamu.
  - (b) Ni michezo ipi isiyoruhusiwa kwa Waislamu, na kwanini?
8. Taja mambo ya Msingi yanayohitajika kuyafanya na kuyasimamia ili sherehe na burdani za Waislamu zisikiuke Qur’an na Sunnah ya Mtume Muhammad(s.a.w), kama zilivyo sherehe na burdani za wasiokuwa Waislamu.
9. Muislamu anapofikwa na msiba, anatafautianaje na asiyekuwa Muislamu katika kuomboleza?
10. Soma kwa makini sura 3:190-192. Kisha oneshwa vipengele na mkakati wa namna ya kutekeleza maudhui yake, na ushikamane nayo kila siku.

## SHERIA KATIKA UISLAMU

### *Maana ya Sheria*

Katika lugha ya Kiarabu, neno Shariah lina maana ya njia ya kufuatwa. Kiistilahi neno sheria linakusanya katika maana yake, taratibu, sharti, kanuni (principles) na amri (rules) ambazo huwekwa ili kuongoza mahusiano ya watu katika jamii inayohusika.

Sheria ni fani muhimu mno katika maisha ya jamii. Haijatokea jamii yoyote ile katika kipindi cha historia ya mwanadamu isiyo na sheria. Kazi ya sheria ni kuiweka jamii katika nidhamu na kulinda haki za raia ili ipatikane furaha na amani katika jamii hiyo.

Sheria ni kanuni au amri ambazo si tu hupasa kutiwa, bali pia zinapovunjwa, mvunjaji hudhibitiwa baada ya kugundulika na kuadhibiwa na vyombo vinavyohusika na usimamiaji wa hiyo sheria. Kwahiyo, ili pawepo na sheria ni lazima pia pawepo na vyombo vyenye mamlaka na nguvu ya kusimamia ili kuhakikisha kuwa hiyo sheria inafuatwa na iwapo itavunjwa basi hatua zitachukuliwa dhidi ya mvunjaji.

### **Kazi ya Sheria katika Jamii**

**Kwanza** sheria humlinda binadamu binafsi dhidi ya madhara mbali mbali yanayoweza kusababishwa na mwenendo wake mbaya. Kwa mfano sheria ya kulazimishwa watu kufanya kazi ina lengo la kuwaepusha watu na umasikini wa kujitakia. Sheria ya kumkataza mtu kuvuta bangi na kutumia madawa ya kulevya ina lengo la kulinda afya yake. Sheria ya barabarani ina lengo la kumuepusha mtu na ajali. Uzoefu unaonesha kuwa sheria zinapokuwa madhubuti mwenendo na hulka ya watu hubadilika na hivyo hujiepusha na maovu.

**Pili**, sheria hulinda watu na mali zao. Kwa mfano sheria zinazokataza kuua (bila ya sababu inayokubalika kisheria), kumjeruhi mtu, kuiba, kunyang'anya, kulaghai, kupunja vipimo, n.k. ziko pale ili kulinda uhai na mali za watu. Bila ya kuwepo sheria kama hizi watu watadhulumiana na kuliana mali kwa batili.

**Tatu**, sheria ni muhimu ili kuhifadhi amani na usalama katika jamii, ili jamii iweze kuishi bila ya migongano na vurugu. Bila ya kuwepo amani na usalama jamii haiwezi kupiga hatua za kimaendeleo bali maisha hujaa hofu na vitisho.

**Nne**, sheria huhifadhi maadili ya jamii. Inafahamika kuwa maadili ni moja ya misingi mikuu ya mwenendo wa jamii. Hivyo moja ya malengo makuu ya sheria kwa kawaida huwa ni kulinda maadili ili kuhakikisha kuwa jamii inaendeshwa katika mwenendo mwema.

**Tano**, sheria inapanga utaratibu juu ya namna ya kuendesha shughuli mbali mbali zenye maingiliano ya kijamii. Mfano sheria ya ujenzi wa makazi mijini, matumizi ya barabara, taratibu za uendeshaji serikali na vyombo vyake, uendeshaji wa masoko, uendeshaji wa biashara, utunzaji wa mazingira, ulinzi na usalama wa raia na taifa, n.k.

Kwa ujumla, kazi kuu ya sheria ni kuiweka jamii katika nidhamu na kulinda haki za raia ili ipatikane amani na furaha katika maisha ya mtu binafsi na jamii kwa ujumla. Pamoja na ukweli huu, swali linakuja: “kama kazi ya sheria nikuiweka jamii katika nidhamu na kuleta furaha na amani, mbona hivi leo, pamoja na jamii za kitaifa na kimataifa kujiwekea sheria, hatuoni dalili ya furaha na amani isipokuwa vurugu, vita, mauaji ya halaiki, ukandamizaji na unyanyasaji wa kila aina?”

Hatuna budi kufahamu kuwa si kila sheria ya jamii inaleta furaha na amani kwa raia wote. Sheria nyingi zilizotungwa na wanadamu zina udhaifu mkubwa kama tutakavyoona. Kwa hiyo pamoja na nia njema inayokuwepo wakati wa kuzitunga, katika matumizi yake hazifikii kabisa lengo linalokusudiwa. Ni sheria za Allah(s.w) pekee zinazoweza kuiweka jamii ya mwanadamu katika nidhamu inayotakikana na kuiwezesha kuishi kwa furaha na amani. Sheria ya Kiislamu inaweza kuifikisha jamii kwenye lengo hilo kwa kuwa imewekwa na Muumba mwenyewe ambaye anamjua vyema mwanadamu, matashi yake, matatizo yake, ujanja wake na udhaifu wake kwa ujumla kama Qur-an inavyotutanabahisha:

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ وَنَعْلَمُ مَا تُوَسَّوَسُ بِهِ نَفْسُهُ وَنَحْنُ أَقْرَبُ إِلَيْهِ

مِنْ حَبْلِ الْوَرِيدِ ﴿٥٠﴾

*Bila shaka tumemuumba mtu, nasi tunajua yanayopita katika nafsi yake; nasi tu karibu naye zaidi; kuliko mshipa wa shingo (yake).” (50:16)*

## Chimbuko la Sheria za Kitwaghuti

Chimbuko la sheria zilizotungwa na wanadamu ni vipawa vya wanadamu vya kufikiri na kuhoji (reason) na mila na desturi zilizozoeleka. Hivyo sheria hizo ni zao la akili ya mwanadamu na mazingira yake. Hata hivyo, pamoja na kuwa vipawa hivyo vya kuhoji, miiko na desturi hizo ni nyenzo za muhimu, lakini zenyewe tu bila ya ufunuo (revelation) kutoka kwa Mwenyezi Mungu hutoa ujumbe wa kubahatisha na usio na uhakika wa kudumu. Hata hivyo wale wakanao ufunuo hushikilia kuwa ndizo chemchem za hakika katika utunzi wa sheria na kanuni mbali mbali. Kwa jitihada hizo za akili (bila ya ufunuo), jamii, nchi na mataifa yote ya kitwaghuti hujitungia sheria mbali mbali ambazo nazo hutokana na chimbuko kuu, ambalo ni Katiba. Katiba za nchi ndizo msingi wa sheria zote.



## Udhaifu wa Sheria Zilizotungwa na Binadamu

Ni wazi kuwa kutumia akili na kufikiri ni jambo muhimu sana kwa mwanadamu, lakini je akili ya mwanadamu au fikra zinaweza kutoa sheria ambazo ndio mwongozo wa maisha? Wanadamu hutofautiana sana katika kufikiri na huathiriwa sana na mazingira, wakati na matashi. Ni nani mwenye fikra za kutoa sheria sahihi zenye kuweza kuwaongoza wanadamu hapa ulimwenguni zisizoathiriwa na mazingira yake; wakati na matashi yake. Ukweli ni kwamba uamuzi unaotokana na fikra ya mwanadamu hutegemea mazingira yake ambayo yako katika upeo wa milango ya fahamu ambayo tayari ina udhaifu mkubwa. Kama taarifa iliyopatikana kutokana na milango ya fahamu itakuwa na kasoro, pia uamuzi utakaotegemea taarifa hiyo nao utakuwa na kasoro.

Hali kadhalika, ujuzi na uwezo wa kufahamu wa mwanadamu haumtoshi kuweza kuyazingatia mazingira yote yanayopasa kuzingatiwa katika kumpangia mwanadamu sheria, au utaratibu unaofaa wa maisha. Watafiti wa mambo ya uwezo wa akili ya mwanadamu wameonesha kuwa akili ya binadamu siku zote uwezo wake umefungika katika mazingira aliyomo na upeo wa maendeleo ya sayansi ambao jamii yake imeufikia. Ni ukweli unaokubaliwa na watu wote kuwa, mambo yote anayoyajua mwanadamu kuhusu nafsi na mwili wake yeye mwenyewe na kuhusu mazingira yake ni machache ikilinganishwa na yale yote anayohitajia kuyajua ili kujitosheleza katika ujuzi alionao.

Udhaifu huu umepelekea mwanadamu kutegemea zaidi dhana na ujuzi usiotosheleza katika kutoa maamuzi ya lipi baya na lipi zuri. Hii imepelekea mwanadamu kujipangia taratibu zisizomfaa kwa dhana ya kuwa hizo ndizo zifaazo. Hivyo, mara nyingi hata mwanadamu anapokusudia kujipangia taratibu nzuri zifaazo ameishia kutunga sheria zisizofaa, na pengine zenye madhara kwake mwenyewe. Hii ndio imekuwa moja ya sababu kubwa za kubadilishwa mara kwa mara kwa sheria za kutungwa na mwanadamu. Ukizichambua vyema sheria hizo utakuta kuwa mara nyingi badala ya kutimiza malengo ya kuwepo kwake katika jamii, zenyewe huenda kinyume chake. Matokeo yake, kwa mfano badala ya kumkinga mwanadamu na maovu na madhara yake, zenyewe huyachochea. Na badala ya kulinda maadili zenyewe husaidia kuyabomoa. Na huchochea dhulma badala ya kuzuia. Bali katika jamii nyingine, sheria huwa ndio chimbuko la ukandamizaji na uonevu wa kila hali.

Sheria kama zile zinazounga mkono mifumo ya utumwa katika jamii, ubaguzi wa rangi n.k. ni mifano ya udhaifu mwingi uliopo katika mifumo ya sheria zilizotungwa na binadamu.

Jambo lingine ni kuwa, moyo wa mwanadamu nao umetawaliwa na matashi ambayo mara nyingi huwapelekea watungaji wa sheria wasiofuata mwongozo wa Muumba kujipendelea katika sheria wanazozitunga. Hili linadhihiri katika kila kaumu ya watu wafuatao sheria zilizowekwa na wanadamu.

Mfano wakati wa Firauni yeye mwenyewe alijikweza na kujifanya Mungu. Sheria ziliwapendelea na kuwakweza jamaa na watu wa kabila lake (yaani Wamisri):

إِنَّ فِرْعَوْنَ عَلَا فِي الْأَرْضِ وَجَعَلَ أَهْلَهَا شِيَعًا يَسْتَضِعُّ طَائِفَةً مِنْهُمْ  
يُذَبِّحُ أَبْنَاءَهُمْ وَيَسْتَحْيِي نِسَاءَهُمْ إِنَّهُ كَانَ مِنَ الْمُفْسِدِينَ ﴿٤﴾

*“Hakika Firauni alitakabari (alijitukuzi) katika ardhi na akawafanya watu wa huko makundi mbali mbali. Akalidhoofisha kundi moja miongoni mwao, akiwachinja watoto wao wanaume na kuwawacha hai watoto wao wanawake. Hakika yeye alikuwa miongoni mwa waharibifu (kabisa).” (28:4).*

Mifano ya namna hii ni mingi. Wagiriki wa zamani pamoja na kusifiwa kwao kuwa chimbuko la dhana ya demokrasia na falsafa za kuigwa za kina Socrates, Plato, Aristotle n.k, walijitungia sheria zilizowagawa watu kati ya mabwana na watumwa. Katika jamii hiyo, watumwa, wanawake na wale ambao hawakuwa wazawa walikuwa hawana haki yoyote, na zaidi watumwa walikuwa ni sawa na bidhaa zinazoweza kuuzwa na kununuliwa, bali hata na kuuawa na mabwana zao kama njia ya kujifurahisha!

Katika wakati huu tulionao pia udhaifu huu wa matashi ya watu umetawala utunzi wa sheria. Katika sheria za kimataifa, mataifa makubwa ya Ulaya na Marekani yamelaumiwa kwa kujipendelea. Huko Marekani, watu weusi wanakandamizwa na kubanwa sana. Hivyo sheria zilizotungwa na mwanadamu mara nyingi haziafikiani na misingi ya haki na usawa.

Pia mara nyingi sheria hizo hushindwa kuyazingatia na kuyasimamia sawasawa maslahi ya kweli ya mwanadamu. Hii inatokana na zile sifa za udhaifu alizonazo huyo mwanadamu mwenye kuzitunga hizo sheria. Sifa zile tulizo zitaja juu pamoja na nyingine nyingi kama vile za uongo, wivu, husuda, hila na ulaghai, ubinafsi, uchoyo, hasira, kiburi, n.k., pamoja na ile sifa ya ufynyu na uwezo wa kujua mambo. Ni kwa msingi huu Allah(s.w) ametutanabahisha:

وَأَنْ تَطَّعَ أَكْثَرُ مَنْ فِي الْأَرْضِ يُضِلُّوكَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ إِنَّ يَتَّبِعُونَ  
إِلَّا الظَّنَّ وَإِنْ هُمْ إِلَّا يَخْرُصُونَ ﴿١١٦﴾

*“Na kama ukiwatii wengi katika (hawa) waliomo ulimwenguni watakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu hawafuati ila dhana tu na hawakuwa ila ni wenye kuzua (tu basi).” (6:116)*

Hivyo ni makosa makubwa akili ya mwanadamu kubeba dhima ya utunzi wa sheria. Matokeo yake, badala ya sheria hizo kutimiza malengo ya kuwepo kwake katika jamii, zinakiuka na kuchochea madhara. Haweki haki na uadilifu, ila dhuluma. Na kwahivyo sheria huwa ndio chimbuko la ukandamizaji na uonevu wa kila namna. Sheria kama zile zinazoruhusu ulevi, uzinifu, utumwa, ubaguzi wa rangi, ukoloni, riba, kamari (n.k.) ni mifano ya udhaifu mwingi uliopo katika mifumo ya sheria zilizotungwa na mwanadamu.

Matokeo ya sheria hizo kuyaruhusu mambo hayo imekuwa ni ya maafa na maangamizi makubwa kwa watu wa dunia nzima. Ulevi umekuwa ndio sababu inayoongoza kwa kusababisha maafa ya ajali barabarani na matatizo mengi ya kiafya. Zinaa imesababisha magonjwa mbali mbali kama vile Kaswende, Kisonono na Ukimwi. Riba na Kamari navyo vimekuwa ndio sababu kubwa ya umasikini katika nchi za ulimwengu wa tatu. Sehemu kubwa ya mzigo wa madeni ya mataifa masikini inatokana na riba. Na hali ya uchumi ilivyo kwa sasa ni kuwa nchi masikini kamwe hazitaweza kujivua mzigo wa madeni ambayo huongezeka siku zote kutokana na kukua kwa riba. Kwa ujumla sheria zilizotungwa na mwanadamu zimeshindwa kabisa kuiongoza jamii katika misingi ya haki na usawa.

## **Udhaifu katika Usimamizi wa Sheria za Kitwaghuti**

Pamoja na udhaifu katika utunzi wa sheria, upo pia udhaifu katika usimamiaji wa sheria hizo. Hii inatokana na ukweli kwamba kila anachoweza kukipanga mwanadamu, mwanadamu anaweza kukipangua. Sheria zilizotungwa na binadamu hazimjengei mja ile fikra muhimu sana ya utii kwa yule aliyemwekea sheria, mwenye uwezo wa kubaini pindi tu mja huyo atakapozikiuka. Vile vile watunzi wa sheria hujiweka juu ya sheria daraja ambayo mwanadamu hastahiki kuwa nayo.

Sheria za kibinadamu pamoja na kuwepo vyombo vya dola vya kusimamia kama vile polisi, vikosi vya kuzuia fujo, kamisheni za kuzuia rushwa, magereza, idara za usalama wa taifa, na kadhalika, bado inashindikana kuhakikisha kuwa zinatekelezwa. Sababu ni kuwa ni vigumu binadamu kumchunga binadamu mwenzake kama awezavyo kumchunga mbuzi au kondoo. Ni rahisi mwanadamu kujificha mwanadamu mwenzake asimuone, na hivyo kufanya maovu bila taabu. Pia wakiukaji sheria waweza kushirikiana na wasimamizi wake kwa kutumia rushwa, udugu, ukabila, urafiki na kadhalika.

## **Chimbuko la Sheria ya Kiislamu**

Msingi wa kwanza wa sheria ya Kiislamu ni Qur-an. Qur-an ni mwongozo utokao moja kwa moja kwa Allah(s.w) kupitia kwa Mtume Muhammad(s.a.w). Allah(s.w) ndiye Muumba wa binadamu na vyote vilivyomzunguka katika mbingu

na ardhi. Amekiumba kila kitu kwa lengo na Ndiye pekee Mwenye kustahiki kutoa mwongozo, kuweka taratibu, na kanuni zitakazokiwezesha kila kiumbe kuwa na nidhamu itakayokipelekea kufikia lengo lake. Hivyo, Allah(s.w) ndiye chimbuko la sheria zote zinazomiliki maumbile yake (natural laws) zinazoyawezesha maumbile hayo yabakie katika nidhamu inayoyawezesha kufikia lengo lake. Pia Allah(s.w) ndiye pekee anayestahiki kumuwekea binadamu sheria (social laws) itakayomuwezesha kuwa na nidhamu itakayompelekea kuishi kama mja na khalifa wa Allah(s.w) hapa ulimwenguni.

Msingi wa pili wa sheria ya Kiislamu ni Sunnah ya Mtume Muhammad(s.a.w) Mtume Muhammad(s.a.w) pamoja na Mitume wengine, wameteuliwa na Allah(s.w) ili kuwa Waalimu katika jamii zao wanaoupokea na kuufundisha ujumbe kutoka kwa Allah(s.w) kinadharia na kimatendo. Si ujumbe wote kutoka kwa Allah(s.w) kupitia kwa mitume ulioandikwa na kuhifadhiwa katika vitabu vyake bali sehemu kubwa ya ujumbe wa Allah(s.w) unadhiri katika maelekezo na utendaji wa Mitume kama Qur-an inavyotuthibitishia juu ya Mtume(s.a.w):

وَمَا يَنْطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ ۗ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ ۗ

*Wala hasemi kwa matamano (ya nafsi yake). Hayakuwa haya (anayosema) ila ni wahyi uliofunuliwa (kwake).(53:3-4)*

Hivyo ni wajibu kwa Waislamu kumtii Mtume(s.a.w) kwa kufuata vilivyo mafundisho yake na kumuigiza tabia yake.

## Vyanzo Vingine vya Sheria ya Kiislamu

Tumeona kuwa vyanzo vikuu vya sheria ya Kiislamu ni Qur-an na Sunnah. Vyanzo vya aina ya pili vya sheria ya Kiislamu ni vile vinavyopatikana kwa kutumia vigezo vya Qur-an na Sunnah. Vyanzo hivi ni Al-Ijmaa, Al-Qiyaas na Al-Ijtihad.

### *Al-Ijmaa'*

Al-Ijmaa ni makubaliano ya kongamano la wanazuoni (shura ya wataalamu) wa jamii, baada ya kufariki Mtume(s.a.w). Makubaliano hayo yanafikiwa kwa kuzingatia mipaka ya Qur-an na Sunnah na maslahi ya jamii. Ijmaa, haitakubalika pale itakapokwenda kinyume na Qur-an na Sunnah. Allah(s.w) mwenyewe anatumia kushauriana katika mambo mbali mbali ambayo hatuyapati moja kwa moja kutoka kwake katika aya zifuatazo:

فِيمَا رَحْمَةٍ مِّنَ اللَّهِ لِنْتَ لَهُمْ<sup>ط</sup> وَلَوْ كُنْتَ فَظًّا غَلِيظَ الْقَلْبِ لَأَنْفَضُوا  
 مِنْ حَوْلِكَ<sup>ط</sup> فَاعْفُ عَنْهُمْ<sup>ط</sup> وَاسْتَغْفِرْ لَهُمْ<sup>ط</sup> وَشَاوِرْهُمْ فِي الْأَمْرِ<sup>ط</sup> فَإِذَا عَزَمْتَ<sup>ط</sup>  
 فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ<sup>ع</sup> إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَوَكِّلِينَ ﴿٣٨﴾

Basi kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu umekuwa laini kwao (Ewe Muhammad). Na kama ungekuwa mkali na mwenye moyo mgumu bila shaka wangalikukimbia. Basi wasamehe wewe na uwaombe msamaha (kwa Mwenyezi Mungu) na ushauriane nao katika mambo. Na ufungapo nia mtegemee Mwenyezi Mungu (tu ufanye hili uliloazimia). Mwenyezi Mungu anawapenda wamtegemeao. (3:159)

وَالَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِرَبِّهِمْ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَأَمْرُهُمْ شُورَىٰ بَيْنَهُمْ وَمِمَّا  
 رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ ﴿٣٩﴾

Na wale waliomuitikia Mola wao (kwa kila amri Zake) na wakasimamisha Sala, na wanashauriana katika mambo yao na wanatoa katika yale tuliyowaruzuku. (42:38)

Pia Ijmaa inasisitizwa katika aya zifuatazo:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِيَ الْأَمْرِ مِنْكُمْ فَإِن  
 تَنَزَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ  
 الْآخِرِ<sup>ع</sup> ذَلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٤٠﴾

Enyi mlioamini! Mtiini Allah na mtiini mtume na wenye mamlaka juu yenu walio katika nyie. Na kama mkikhitalifiana juu ya jambo lolote basi lirudisheni kwa Allah na Mtume wake ikiwa mnamwamini Allah na siku ya mwisho. Hiyo ndiyo heri nayo ina matokeo bora kabisa. (4:59)

وَمَنْ يُشَاقِقِ الرَّسُولَ مِنْ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ الْهُدَىٰ وَيَتَّبِعْ غَيْرَ سَبِيلِ  
 الْمُؤْمِنِينَ نُوَلِّهِ مَا تَوَلَّىٰ وَنُصَلِّهِ<sup>ط</sup> جَهَنَّمَ وَسَاءَتْ مَصِيرًا ﴿٤١﴾

*Na atakayemuasi Mtume baada ya kumdhihirikia uwongofu na akafuata njia isiyokuwa ya Waislamu, tutamgeuza aliko geukia mwenyewe na tutamwingiza katika Jahannam; napo ni pahali pabaya kabisa pa mtu kurudia.” (4:115)*

Aya hizi zinasisitiza kuwa shura ya wataalamu na viongozi wa jamii ya Kiislamu itakapopitisha maamuzi ambayo hayapingani na Qur-an na Sunnah, Waislamu wanalazimika kutii vinginevyo watakuwa wamemuasi Allah(s.w) na Mtume wake.

Naye Mtume(s.a.w) katika kusisitiza Ijmaa, amesema katika Hadith:

*“Watu wangu (waumini wa kweli wa umma wake) hawatakubaliana na yeyote anayewapoteza na njia ya haki”*

Mifano mingi ya Ijmaa inapatikana katika kipindi cha Maswahaba, baada ya kufariki Mtume(s.a.w). Kwa mfano, katika Qur-an na katika Sunnah ya Mtume(s.a.w), adhabu ya mlevi haikubainishwa. Lakini shura ya maswahaba ilikaa na kuweka adhabu ya viboko thamanini kwa mlevi kutokana na ushauri ‘Ali bin Abu Taalib aliyesema: “Anayekunywa pombe analewa; mlevi huongea ovyo (kama kichaa); anayeongea ovyo huwazulia watu uovu; na anayewazulia watu uovu adhabu yake ni viboko thamanini kwa mujibu wa Qur-an:

وَالَّذِينَ يَرْمُونَ الْمُحْصَنَاتِ ثُمَّ لَمْ يَأْتُوا بِأَرْبَعَةِ شُهَدَاءَ فَاجْلِدُوهُمْ  
ثَمَنِينَ جَلْدَةً وَلَا تَقْبَلُوا لَهُمْ شَهَادَةً أَبَدًا وَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٨٤﴾

*“Na wale wanaowasingizia wanawake watahirifu (kuwa wamezini) kisha hawaleti mashahidi wane, basi wapigeni mijeledi thamanini, na msiwakubalie ushahidi wao tena, na hao ndio mafasiki”. (24:4)*

Al-Qiyaas (analogical Deduction)

Al-Qiyaas ni maamuzi(fat-wa)anatoa mwanachuoni (mjuzi wa Qur-an na Sunnah) kulingana na mazingira na kwa maslahi ya jamii, pale ambapo hapana fat’wa iliyotolewa na Qur-an au Hadith au Ijmaa. Suala la kutumia akili limesisitizwa mno katika Uislamu kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَأَخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ لَآيَاتٍ  
لِّأُولِي الْأَلْبَابِ ﴿١٠١﴾

*“Hakika kuumbwa mbingu na ardhi na mfuatano wa usiku na mchana ziko hoja (za kuonyesha kuwepo Allah(s.w) kwa wenye akili.” (3:190)*

وَلَقَدْ ذَرَأْنَا لِجَهَنَّمَ كَثِيرًا مِّنَ الْجِنِّ وَالإِنسِ ط لَهُمْ قُلُوبٌ لَّا  
يَفْقَهُونَ بِهَا وَهُمْ أَعْيُنٌ لَّا يُبْصِرُونَ بِهَا وَهُمْ ءَاذَانٌ لَّا يَسْمَعُونَ بِهَا  
أُولَئِكَ كَالْأَنْعَامِ بَلَّ هُمْ أَضَلُّ أُولَئِكَ هُمُ الْغَافِلُونَ ﴿٧٧﴾

“Na bila shaka tumewaambia Moto wa Jahannam wengi katika majini na watu (kwa sababu hii). Nyoyo (akili) wanazo lakini hawafahamu kwazo na macho wanayo lakini hawaoni kwayo na masikio wanayo lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama wanyama, bali wao ni wapotevu zaidi. Hao ndio walioghafilika.” (7:179)’

Suala la kutoa maamuzi kwa kutumia akili pale ambapo hapana fat-wa ya Qur-an na Sunnah ameliridhia Mtume(s.a.w) kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

“Mtume(s.a.w) alimtuma Mu’aadh bin Jabal Yemen kwenda kuwa Kadh (Jaji) na mkuu wa Jimbo (Governor). Kabla hajaondoka, Mtume(s.a.w) alimuuliza kuwa kama atafikwa na tatizo atalitua kwa kutumia kigezo gani. Mu’aadh alijibu kuwa atatoa maamuzi kutokana na Qur-an. Mtume(s.a.w) akamuuliza: Jaalia kuwa hukupata ufumbuzi wa tatizo hilo katika Qur-an, utafanyaje katika kutoa uamuzi?” Mu’aadh akajibu kuwa atatafuta ufumbuzi kutokana na Sunnah ya Mtume(s.a.w). Mtume(s.a.w) akaendelea kumuuliza: “Jaalia hukupata jibu kwenye Qur-an wala Sunnah utafanyaje?” Mu’aadh bin Jabal alijibu kuwa atatoa uamuzi kutokana na **akili** yake. Mtume(s.a.w) alifurahi kusikia jibu hili.”

Pia tunajifunza katika Hadith kuwa Mtume(s.a.w) alimtuma Abuu Musa al Ash-a’ri kwenda Yemen na kumuagiza kuwa ahukumu kwa mujibu wa Qur-an, na kama hakupata uamuzi kutoka kwenye Qur-an, atumie Hadith za Mtume(s.a.w) na akikosa kupata uamuzi kutokana na Hadith, basi atoe maamuzi kutokana na akili yake.

### ***Al-Ijtihad***

Ijtihad ni neno la Kiarabu lenye maana ya kufanya jitihada ili kufikia maamuzi binafsi. Katika masuala ya kisheria, **Ijtihad**, ni kutumia jitihada za kuchambua na kutoa ufafanuzi juu ya sheria.

Imamu Shafii, ameunga mkono suala la Ijtihad, kwa kurejea aya ya Qur-an ifuatayo:

وَمِنْ حَيْثُ خَرَجْتَ فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَحَيْثُ مَا

كُنْتُمْ فَأُولُوا وُجُوهَكُمْ ..... ﴿١٥٠﴾

*“Na po pote wendako geuza uso wako kwenye msikiti mtakatifu. Na popote mlipo geuzeni nyuso zenu upande uliko (msikiti huo) .....” (2:150).*

Imamu Shafii kutokana na agizo la aya hii, anasisitiza kuwa si rahisi mtu kujua upande ilipo Ka’abah bila kutumia jitihada binafsi, kwa kutumia jua, ramani, dira, n.k.

Ijtihad inakubalika kwa kuzingatia misingi ya Qur-an, Sunnah, Ijmaa na Qiyas. **Mujtahidi** hanabudi kuwa na ujuzi wa kina juu ya Qur-an, Sunnah, Ijmaa na Qiyas. Pamoja na ujuzi wa kutosha juu ya vyanzo hivi vinne vya sheria, Mujtahidi pia hanabudi kuwa na sifa zifuatazo:

- (a) Awe Muislamu mzuri wa vitendo.
- (b) Awe mcha-Mungu mwenye kushikamana na Qur-an na Sunnah.
- (c) Asiwe mwenye kuathiriwa na misimamo ya vikundi.
- (d) Awe muadilifu na muaminifu na awe ameepekana kabisa na matendo machafu.

## Halali na Haramu katika Sheria ya Kiislamu

Uislamu umepambanua na kuliweka wazi kila jambo. Uislamu pamoja na kuwataka watu wafanye mema na kuacha maovu umeainisha wazi wazi yepi mema (*Ma’arufaaf*).

Na yepi maovu (Munkaraat). Allah(s.w) peke yake ndiye mwenye mamlaka ya kuhalalisha na kuharamisha. Kuhalalisha alichu kiharamisha Allah(s.w) au kufanya kinyume chake ni kuchukua nafasi ya Allah(s.w) katika mamlaka yake na hiyo ni shirk kubwa.

Yale yote aliyohalalisha Allah(s.w) yana manufaa kwa binadamu kibinafsi na kijamii. Katika sheria ya Kiislamu mambo halali yamewekwa katika daraja tatu zifuatazo:

- (i) Faradh.
- (iii) Mustahabu.
- (iii) Mubaha.

(i) **Faradh** ni mambo ambayo ni halali lakini kutokana na umuhimu wake, Allah(s.w) amewaamrisha watu kuyatekeleza pasina hiari. Mwenye kuacha kufanya haya kwa makusudi atakuwa amevunja amri au sheria



ya Allah(s.w), na atastahiki **kughadhhibikiwa** na Mola wake na kustahiki adhabu yake iwapo hataleta **toba ya kweli**.

(ii)**Mustahabu** ni mambo ambayo sio tu kuwa ni halali kuyafanya, bali pia watu wanahimizwa sana wajitahidi kuyafanya kwa ajili ya manufaa binafsi na jamii kwa ujumla. Mambo hayo yanaweza kuwa yale yanayohusiana na lbada maalumu, siasa, uchumi, utamaduni, n.k.

(iii)**Mubaha**, katika sheria ya Kiislamu ni jambo lolote ambalo ni halali kulifanya lakini sio lazima kulifanya. Kwa mfano, iwapo mtu anapenda bustani ya maua anaruhusiwa na sheria kuwa nayo lakini sheria haimlazimishi mtu kuwa na bustani ya maua.

Yale yote aliyoyaharamisha Allah(s.w) yana madhara kwa binadamu kibinafsi na kijamii. Kufanya mambo yaliyoharamishwa ni kuvunja sheria ya Allah(s.w) na kustahiki **ghadhabu** zake na **adhabu** yake.

Kuna mambo ambayo japo sheria haijatumka waziwazi kuwa ni haramu lakini uzoefu unaonesha kuwa yana madhara kwa binadamu kibinafsi na kijamii. Mambo ya aina hii katika sheria ya Kiislamu huitwa **makruhu** Muislamu analazimika kujiepusha na mambo haya.

Ukichunguza makatazo yote katika sheria ya Kiislamu utaona kuwa yamewekwa kwa manufaa ya binadamu na yamegawanyika katika sehemu kuu tano zifuatazo:

- (i) Makatazo yenye lengo la kulinda na kuhifadhi **imani**.
- (ii) Makatazo yenye lengo la kulinda na kuhifadhi **maisha** na **uhai** wa binadamu.
- (iii) Makatazo yenye lengo la kulinda na kuhifadhi **akili** ya binadamu.
- (iv) Makatazo yenye lengo la kulinda na kuhifadhi **heshima** na **hadhi** ya binadamu.
- (v) Makatazo yenye lengo la kulinda na kuhifadhi **mali**.

## **Mahakama ya Kiislamu**

Uislamu huyaratibu maisha ya jamii na hivyo kuweka sheria zinazolinda maslahi ya mtu yasiharibiwe na mtu mwingine. Sheria pia inamhakikishia usalama wake raia anayetuhumiwa kuwa ametenda kosa fulani. Sheria ya Kiislamu husimamisha haki kwa kuzingatia; maslahi ya dola ya kuzuia uhalifu na kwa kuyalinda maslahi ya raia ili haki zake zidumishwe:

1. Kanuni ya uwajibikaji wa mhalifu.
2. Kanuni ya uwiano wa kosa na adhabu, na

### 3. Kanuni ya kutosogeza nyuma hukumu zinazotolewa kwa wahalifu.

#### 1. Kanuni ya uwajibikaji kwa mhalifu

Raia hawezi kuwa salama iwapo atalazimika kujibu mashtaka ya makosa ya mtu mwingine. Hivyo kanuni hii ni msingi wa usalama wa raia.

Kanuni hii ina maana kuwa ni yule mtendaji wa kosa tu ndiye ashitakiwe, na si mtu mwingine yeyote. Yaani ikiwa Juma ndiye aliyeteka nyara ndege basi yeye peke yake (kama alikuwa peke yake) ndiye ashitakiwe. Asichukuliwe baba yake mtu au mkewe n.k.

Kanuni hii pia maana yake ni kuwa ikiwa mtoto wa Rais ameiba pesa, basi asiachwe kwa sababu ni mtoto wa mtu mkubwa. Kanuni hii pia ina maana kuwa mtu aliyeshiriki katika kutenda kosa kama mtendaji mkuu au kama msaidizi hana budi kushitakiwa kwa mujibu wa kushiriki kwake. Qur-an imebainisha katika sehemu mbali mbali juu ya kanuni hii ya uwajibikaji wa mtu binafsi:

وَأَنْ لَّيْسَ لِلْإِنْسَانِ إِلَّا مَا سَعَىٰ ﴿٣٩﴾

*Na kwamba mtu hatapata ila yale aliyoyafanya. (53:39)*

مَنْ عَمِلْ صَالِحًا فَلِنَفْسِهِ ۖ وَمَنْ أَسَاءَ فَعَلَيْهَا ۗ وَمَا رَبُّكَ بِظَلَّامٍ لِّلْعَبِيدِ ﴿٤٦﴾

*Anayefanya mema anajifanyia (mwenyewe) nafsi yake, na mwenye kutenda ubaya ni juu (ya nafsi) yake (vile vile). Na Mola wako si dhalimu kwa waja wake (41:46)*

..... وَلَا تَكْسِبُ كُلُّ نَفْسٍ إِلَّا عَلَيْهَا ..... ﴿١٦﴾

*.....Wala nafsi yoyote haichumi (ubaya) ila ni juu yake. (6:164)*

وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ۗ ..... ﴿١٨﴾

*Wala hatabeba mzigo wa mwingine. (35:18)*

..... مَنْ يَعْمَلْ سُوءًا يُجْزَ بِهِ ۖ ..... ﴿١٢٢﴾

*.....Atakayefanya ubaya atalipwa kwa (ubaya) huo. (4:123)*

Hadith za Mtume(s.a.w) pia zinaithibitisha kanuni hii. Mtume(s.a.w) amesema:

*“Nafsi haitaulizwa kwa makosa ya baba, au ndugu yake.*

Huko Ulaya kanuni hii ilitambuliwa baada ya Mapinduzi ya Ufaransa. Kanuni hii ilipitishwa katika sheria ya Januari 21, 1790, na kuingizwa katika katiba 1791. Kabla ya hapo mtu aliwajibika siyo tu kwa makosa yake bali pia kwa makosa yaliyotendwa na wengine.

Kwa mfano sheria moja ya Kifaransa ya zama hizo ilikuwa inasema kuwa kusema maneno yasiyopendeza dhidi ya Mfalme ni kosa ambalo adhabu yake ni kifo kwa huyo msemaji na kufilisiwa mali ya familia ya mtu huyo.

## 2. Kanuni ya Uwiano wa Kosa na Adhabu

(a) Kanuni hii ina maana kuwa hakuna mtu anayeweza kushitakiwa au kuadhibiwa isipokuwa kama ilivyobainishwa na sheria. Kanuni hii ina maana kuwa makosa na adhabu zake lazima zitolewe na serikali.

Kanuni ya uhalali wa kosa na adhabu inalinda usalama wa raia kwa kuhakikisha kuwa mtu hanyanyaswi na dola. Kanuni hii pia inadhibiti mamlaka na uwezo wa hakimu kwani hawezi kutoa adhabu isipokuwa tu kama ilivyowekwa katika sheria, hata kama kosa hili limeudhi watu namna gani.

Hivyo basi sheria ndiyo inayogawa baina ya lipi halali na lipi haramu. Hakuna mtu atakayeadhibiwa au kushitakiwa kwa jambo ambalo halikubainishwa wazi kuwa ni kosa kabla ya kutendwa:

..... وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ نَبْعَثَ رَسُولًا ﴿١٧٥﴾

.....Na si wenye kuwaadhibisha (viumbe) mpaka tuwapelekee Mtume. (17:15)

رُسُلًا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ ۗ

وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿١٧٦﴾

(Hao ni) Mitume waliotoa khabari (kwa watu wema) wakawaonya (wabaya) ili watu wasiwe na hoja juu ya Allah baada ya (kuletwa hawa) Mitume. Allah ni Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima. (4:165).

وَمَا كَانَ رَبُّكَ مُهْلِكَ الْقُرَىٰ حَتَّىٰ يَبْعَثَ فِي أُمِّهَا رَسُولًا يَتْلُوا عَلَيْهِمْ

ءَايَاتِنَا ۗ ..... ﴿١٧٧﴾

*Na Mola wako haangamizi miji mpaka ampeleke Mtume katika mji wao mkuu, awasomee aya zetu. (28:59)*

..... وَأَوْحَىٰ إِلَيْنَا هَذَا الْقُرْآنَ لِأُنذِرْكُمْ بِهِ وَمَنْ بَلَغَ ..... ﴿١١﴾

*Na Qur-an hii imefunuliwa kwangu ili kwa hiyo nikuonyeni nyinyi na kila imfikiayo. (6:19).*

وَأَنْذِرْكُمْ بِهَا وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢٤﴾

*Na hakuna taifa lolote ila alipita humo muonyaji (Mtume). (35:24).*

Hivyo Qur-an ambayo ndio chimbuko kuu la sheria ya Kiislamu imeweka kanuni kuwa mshitakiwa hawezi kuadhibiwa mpaka kwanza awe ametaarifiwa juu ya kuwa jambo hili ni kosa. Haki ya kuarifiwa kosa na adhabu yake ndio lengo la kanuni hii ya uhalali wa kosa na adhabu.

### **3. Kanuni ya Kutosogeza nyuma hukumu zinazotolewa**

Raia hawawezi kuzitumia haki zao kwa usalama iwapo wanaweza kushitakiwa kwa makosa ambayo hayakuwa makosa wakati yalipotendwa. Kwa sababu hiyo Uislamu unatambua kanuni hii na kuitumia katika sheria zake. Kanuni hii ina maana kuwa sheria huanza kutumika baada ya kutangazwa na siyo kabla. Umuhimu wa kanuni hii ni kulinda usalama wa raia na pia inazuia matumizi mabaya ya madaraka.

Hii ni tofauti na mifumo ya sheria za kitwaghuti ambapo mtu anakamatwa kisha sheria inafuatia. Kama ilivyotokea hapa nchini miaka ya themanini watu walikamatwa kwa madai ya kuhujumu uchumi wa nchi wakati hakukuwa na sheria ya uhujumu uchumi. Baada ya watu kukamatwa ndipo ikatungwa sheria! Qur-an imetaja kanuni hii katika Aya mbali mbali. Allah alikataza riba lakini hakuwaadhibu wale waliotoa au kula riba kabla ya kushuka katazo hilo (*taz: Qur-an 2:275*). Allah pia anakataza kuwaoa ndugu wawili wakati mmoja, lakini hakuwaadhibu wale waliofanya hivyo kabla ya kulidhihirisha kuwa ni kosa. (*taz: Qur-an, 4:23*).

Hali kadhalika, makatazo ya zinaa, wizi, ulevi na makosa mengine hayakutolewa adhabu iwapo yalifanywa kabla ya kubainishwa wazi katika Qur-an.

Lengo la kanuni hii ni kutoa muda wa kutosha kwa watu juu ya makatazo ya Allah ili kuwapa fursa ya kujirekebisha.

## Taratibu za Mashtaka katika Sheria ya Kiislamu

Miongoni mwa mambo muhimu sana yanayohakikisha usalama wa raia ni taratibu zinazotawala mwenendo wa mashitaka. Taratibu hizi zina lengo la kuleta mizani ya haki kati ya haki ya dola ya kusimamia sheria na haki ya raia ya kuishi kwa amani bila usumbufu na kunyanyaswa kinyume cha sheria.

Katika sheria ya Kiislamu watu wote ni sawa mbele ya Sheria. Taratibu zake za mashitaka zaweza kugawanywa katika vipengele vikuu vinne:

1. Raia kudhaniwa kuwa hana hatia.
2. Upepelezi na kuhojiwa.
3. Haki za mshtakiwa wakati wa kusikiliza kesi.
4. Haki za mfungwa.

### 1. Raia kudhaniwa kuwa hana hatia

Kuhusu kanuni hii Mtume(s.a.w) amesema:

*“Kila mtoto huzaliwa bila doa; ni wazazi wake ndio wanaomfanya awe Myahudi, Mkristo au Mmajusi.” (Bukhaary)*

Mtume(s.a.w) pia amesema: *“Msitoe adhabu ikiwa mna shaka”.*

Hivyo chini ya sheria ya Kiislamu hadhi ya mshtakiwa ni ile ya mtu asiye na hatia. Hii ina maana kuwa jukumu la kuthibitisha kosa linakuwa mikononi mwa mtu anayeshtaki. Mshtakiwa hatakiwa kutoa ushahidi wa kukanusha kosa (negative evidence). Kumtaka mshtaki (mlalamikaji) atoe ushahidi wa kuthibitisha kutendeka kwa kosa (positive proof) kunatokana na Hadithi ya Mtume(s.a.w) aliposema:

*Lau watu wangeaminiwa kwa madai yao tu, baadhi ya watu wangedai damu na mali ya watu wengine, lakini mshtaki anawajibika kutoa uthibitisho wa madai yake. (Bukhaary, Muslim, Ahmad).*

Aidha matokeo mengine ya kanuni hii ni kuwa shaka (shubha) inamsaidia mshtakiwa. Katika sheria ya Kiislamu ili kumtia mtu hatiani (conviction) inategemea uhakika kuwa mshtakiwa alitenda kosa na siyo uwezekano kuwa alitenda kosa. Ikiwa kutokana na ushahidi uliotolewa hakim bado ana wasi wasi basi itambidi aamue kuwa mshtakiwa hana hatia.

Hii ni kutokana na Hadithi ya Mtume(s.a.w) aliposema:

*“Msitoe adhabu ikiwa mna shaka. Mwacheni huru mshitakiwa, kwani bora kufanya kosa la kumsamehe kuliko kosa la kumwadhibu.”*

## Haki za Mshitakiwa

## 2. Wakati wa Upelelezi

Kumvamia mtu nyumbani kwake na kumpekua ni kitendo kinachowaondoshea uhuru raia na cha kumdhalilisha mtuhumiwa, hivyo sheria ya Kiislamu imeweka taratibu za kulidhibiti hili. Ikumbukwe kuwa jamii itanufaika iwapo ukweli utajulikana kutokana na upelelezi utakaofanywa. Hivyo sheria ya Kiislamu imeweka kanuni ya kuyaweka katika mizani yote mawili.

Sheria ya Kiislamu inazuia upekuzi wa nyumba za watu pasi na sababu za kimsingi kisheria. Haki ya kila mtu kuwa faragha imebainishwa katika Qur-an aliposema Allah(s.w):

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَدْخُلُوا بُيُوتًا غَيْرَ بُيُوتِكُمْ حَتَّىٰ تَسْتَأْنِسُوا  
وَتُسَلِّمُوا عَلَىٰ أَهْلِهَا ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٢٧﴾

Enyi mlioamini! Msiingie nyumba ambazo si nyumba zenu mpaka muombe ruhusa na muwatolee Salaam waliomo humo. Hayo ni bora kwenu; huenda mtakumbuka. (24:27)

فَإِن لَّمْ تَجِدُوا فِيهَا أَحَدًا فَلَا تَدْخُلُوهَا حَتَّىٰ يُؤْذَنَ لَكُمْ وَإِن قِيلَ  
لَكُمْ أَرْجِعُوا فَأَرْجِعُوا ۗ هُوَ أَزْكَىٰ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ ﴿٢٨﴾

Na kama hamtamkuta humo yoyote, basi msiingie mpaka mruhusiwe. Na mkiambiwa “rudini”, basi rudini; hili ni takaso kwenu. Na Allah anajua mnyayoyatenda. (24:28).

Hivyo kwa mujibu wa aya hizi kuingia katika nyumba za watu kumekatazwa isipokuwa kwa idhini ya mwenye nyumba. Katazo hili halikomei katika nyumba tu, bali linahusu pia mali ya mwenye nyumba mwenyewe asipokuwapo. Mtume(s.a.w) amesema:

Mambo matatu hayaruhusiwi kwa mtu yeyote; mtu anayeongoza kundi katika swala asijiombee dua peke yake, kwani akifanya hivyo atakuwa amewasaliti. Mtu asiangalie ndani ya nyumba ya mtu ila akipewa ruhusa. Na mtu asiswali hali amebanwa na haja hadi ajisaidie kwanza. (Muslim).

Mtume(s.a.w) pia ametumia lugha ya ishara ili kusisitiza haki ya mtu kuwa huru kutokana na kubughudhiwa faragha katika Hadithi ifuatayo:

*“Ikiwa mtu anakutazama (anakukodoleo macho) bila ridhaa yako na ukampiga kwa jiwu hadi ukalipofua jicho lake huna hatia”.*


Haki hii pia inazihusu nguo zake mtu. Hakuna mtu mwenye haki ya kumfunua mwingine nguo ili kuangalia kitu alichokificha bila ya idhini na bila sababu ya msingi.

Aidha, kuilinda nyumba hakutakuwa na maana bila kumlinda mmilikaji pia. Barua zake mtu pia lazima zihifadhiwe. Hivyo ni haramu kuzisoma barua za mtu za kibinafsi baada ya kuzichukua kwa siri. Mtume(s.a.w) amesema: Mtu anayeisoma barua ya nduguye bila ruhusa yake, ataisoma barua hiyo motoni.

Hata hivyo, chini ya sheria ya Kiislamu haki ya kuwa na faragha na haki ya kutobughudhiwa yaweza kukiukwa ikibidi ili kudumisha amani na usalama wa jamii. Vyombo vya dola yaweza kumpekua mtu kwa maslahi ya jamii. Lakini haki hiyo ya kupekua inatawaliwa na masharti yanayohakikisha kuwa raia hanyanyaswi ovyo. Masharti hayo ni:

1. Mtoaji wa amri ya kupekuwa ni mkuu anayehusika na malalamiko (Wali-al-Muzahim). Kwa mujibu wa kanuni za mahakama za Kiislamu, hakimu hana haki ya kutoa amri ya upekuzi (search-warrant) wala si juu yake kutafuta ushahidi. Kazi yake ni kumwambia mlalamikaji kuleta ushahidi wa uthibitisho wa madai yake.
2. Hati ya kupekua haiwezi kutolewa hadi kwanza upatikane ushahidi wa kutosha unaoonesha kuwa upo uwezekano mkubwa kuwa kosa limetendwa na mshitakiwa. Kwa mfano ikiwa mtu mwadilifu anatoa taarifa kuwa amemwona mtu anaingia faraghani na mwanamke au kama mtu anapita nje ya nyumba na akasikia harufu ya pombe yatoka ndani na kelele za watu waliolewa.
3. Kosa ligunduliwe kihalali, kuwa ikiwa limegunduliwa kwa njia za haramu kama ujasusi (kwa mfano kwa kutoboa tundu ukutani na kuchungulia ndani aukusikliza kwa siri na kwa kuvizia. Ushahidi wa kijasusi hauwezi kutumika kumtia mtu hatiani.

Allah amesema:

..... وَلَا تَجَسَّسُوا ..... 

*“Wala msipeleleze.....” (49:12)*

## **Haki za Mtuhumiwa Wakati wa Kuhojiwa**

Katika sheria ya Kiislamu mahojiano siyo maana yake mtuhumiwa kujibu maswali tu la. Bali ni fursa ya kumwambia mtuhumiwa makosa yake na ushahidi uliopatikana dhidi yake, ili akiri au aukanushe ushahidi huo.

Vile vile katika sheria ya Kiislamu hakuna mtu atakayeadhibiwa mpaka kwanza mahakama ya wazi (yenye kushuhudiwa na watu) ithibitisha kosa lake. Kesi za faragha ni haramu kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu pia ni haramu kumkamata mtu kwa kumshuku tu na kumsukumiza jela bila ya kufuata utaratibu wa mahakama na bila ya kumpa fursa ya kujitetea. Aidha ni haramu kumtesa mtuhumiwa “ili aisaidie polisi” kuhusiana na uovu uliotendeka. Uadilifu katika kutoa hukumu, bila ya ubaguzi wa aina yoyote ni jambo lililositizwa katika misingi ya sheria ya Kiislamu:

..... وَإِذَا حَكَمْتُمْ بَيْنَ النَّاسِ أَنْ تَحْكُمُوا بِالْعَدْلِ ..... 

“.....Na mnapohukumu baina ya watu hukumuni kwa uadilifu”. (4:58)

Pia Mtume(s.a.w) amesisitiza:

“Nimeamrisha kuhukumu kwa uadilifu”.

Katika sheria ya Kiislamu hairuhusiwi mtu kuwekwa ndani mpaka ahukumiwe kwa uadilifu, wala hapana yoyote asiye na hatia kuadhibiwa au kutiwa ndani kwa makosa ya mwingine au kwa niaba ya mwingine.

Tofauti na sheria za kijahili ambazo humuona mtuhumiwa kuwa ana makosa kwanza mpaka aithibitishie mahakama kuwa hana makosa, sheria ya Kiislamu humuona mtuhumiwa hana makosa mpaka mahakama ithibitisha kuwa ana makosa.

Haki za mtuhumiwa zinavyohifadhiwa

1. Wanaohoji wawe wawili:
  - (i) Mkuu wa Malalamiko.
  - (ii) Mwendesha mashtaka (Muhtasib).
2. Mtuhumiwa katika makosa ya Hudud na Qisas ana haki ya kutoapa.
3. Katika uchunguzi wa makosa ya Hudud anayo haki ya kukataa kuhojiwa, na anayo haki ya kukaa kimya.
4. Kimya chake hakiwezi kuwa ushahidi dhidi yake.
5. Mtuhumiwa asiteswe (au kufanyiwa ukatili).

Mtume(s.a.w) amesema: Allah atawatesa siku ya malipo wale waliowatesa wenzao duniani. Bwana Audi ibn Artana alimwandikia Umar barua kumwomba ruhusa ya kuwatesa watu wanaokataa kutuo Zaka. Umar akamkatalia.



6. Mahojiano yawe ya kibinadamu, ili mtuhumiwa akiri kosa lake kwa hiari bila kulazimishwa. Mtume(s.a.w) alimwambia mtu aliyeketwa kwake kwa tuhuma za wizi: “*Sidhani kama uliiba; Je, uliiba? Au Bwana Maaz alipokiri kuwa kazini, Mtume(s.a.w) alimpa fursa ya kubatilisha ungamo lake, akamwambia, “Labda ulimbusu tu, au pengine ulimpapasa tu?” Aidha mwanamke mmoja alituhumiwa wizi, Mtume(s.a.w) akamwambia, “Je, uliiba? Sidhani kama uliiba. Sema hapana”* Hivyo kumpa fursa ya kufuta ungamo lake.
7. Chini ya sheria ya Kiislamu mtuhumiwa aweza kukana ungamo lake wakati wowote kabla ya kutolewa adhabu. Bwana Maaz, alikana ungamo lake baada ya kuanza kupigwa mawe, lakini wapigaji hawakumwacha. Alipoambiwa Mtume(s.a.w) akasema, “Kwa nini hamkumwacha atubie? Allah angepokea toba yake”.

### 3. *Haki za mshtakiwa wakati wa kusikilizwa kesi*

- (1) Afunguliwe mashtaka haraka na ahukumiwe.
- (2) Ushahidi katika makosa ya Hudud ni wa kisheria na si wa rai.
- (3) Anayohaki ya kulipwa fidia ikiwa atahukumiwa kimakosa.
- (4) Ashitakiwe katika mahakama yenye mahakimu wenye ujuzi na waadilifu.
- (5) Mtu yeyote pamoja na kiongozi wa nchi anaweza kujibu mashitaka mahakamani.
- (6) Mshitaki na mshtakiwa wote wana haki ya kumteua mtu wa kuwawakilisha mahakamani (wakili).

### 4. *Haki ya Kuhukumiwa kwa Uadilifu*

Sheria ya Kiislamu ipo pale kusimamia uadilifu na lengo lake si kuadhibu wala kukomoa bali kujenga jamii bora. Kila mtu bila ya kujali dini yake, rangi, taifa lake, uraia wake, (n.k.), anastahiki kuhukumiwa kwa uadilifu. Uadilifu katika kutoa hukumu umesisitizwa na ndio msingi mkuu wa sheria ya Kiislamu:

 ..... يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُونُوا قَوَّامِينَ لِلَّهِ شُهَدَاءَ بِالْقِسْطِ

*Enyi mlioamini! Kuweni wasimamizi (wa kupitisha haki) kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, muwe mkitoa ushahidi kwa uadilifu... (5:8).*

﴿ يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُونُوا قَوَّامِينَ بِالْقِسْطِ شُهَدَاءَ لِلَّهِ وَلَوْ عَلَىٰ  
 أَنفُسِكُمْ أَوِ الْوَالِدِينَ وَالْأَقْرَبِينَ ۚ إِن يَكُنْ غَنِيًّا أَوْ فَقِيرًا ۗ فَلَا  
 تُتَّبِعُوا أَهْوَىٰٓ أَن تَعْدِلُوا ۗ ..... ﴾

*Enyi mlioamini! Kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mtowao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu; ijapokuwa ni juu ya nafsi zenu au (juu ya) wazazi (wenu) na jamaa (zenu). Akiwa tajiri au masikini... basi msifuuate matamania mkaacha uadilifu... (4:135).*

## Mgawanyo wa Makosa

Sheria imeyagawanya makosa katika makundi makubwa matatu:

- (1) Makosa ya Hudud
- (2) Makosa ya Qisasi
- (3) Makosa ya Ta'azir

### (1) Makosa ya Hudud

Makosa ya Hudud ni yale ambayo yamekatazwa na Allah na hukumu zake kutajwa katika Qur-an au Sunnah. Makosa hayo ni haya yafuatayo:

#### (i) Kuritadi (Ridda)

Kuritadi ni Muislamu kuukanusha Uislamu kwa maneno aya yoyote ya Qur-an. Au kuukataa Uislamu kwa vitendo kama vile kwa kuzini au kuyawacha maamrisha ya Qur-an kama vile swala na zaka. Mtu anahesabiwa amekanusha Uislamu kwa makusudi na hali yakuwa anajua adhabu ya kufanya hivyo.

Mtu aliyeritadi anapewa muda wa kutubia kosa lake. Ukipita muda wa kutosha na hajatubia basi hukumu yake ni kuuliwa: Hukumu imetolewa katika Qur-an:

..... ﴿ فَأَقْتُلُوا الْمُشْرِكِينَ حَيْثُ وَجَدْتُمُوهُمْ وَخَذُوهُمْ وَأَحْصِرُوهُمْ  
 وَأَقْعُدُوا لَهُمْ كُلَّ مَرْصَدٍ ۚ فَإِن تَابُوا وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَءَاتَوْا الزَّكَاةَ  
 فَخَلُّوا سَبِيلَهُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴾

*Basi wauweni washirikina popote muwakutapo na wakamateni mateka, na wazungukeni na wakalieni katika kila njia. Lakini wakitubu na wakasimamisha swala na wakatoa zaka, basi iacheni njia yao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kurehemu. (9:5).*

### (ii) Uasi (Baghi)

Baghi ni uasi dhidi ya kiongozi halali wa Kiislamu. Uasi huo waweza kuwa hauna msingi wowote au waweza kuwa umetegemezwa katika kipengele fulani maalum ambacho hao wapiganaji Waislamu wamekitegemea katika uasi wao. Kiongozi wa Kiislamu anatakiwa awasihi waache uasi huo na ayajue madai yao ili ipatikane suluhu. Wakikataa ana haki ya kupigana nao. Hata hivyo iwapo madai yao ni ya haki na Imam ndiye aliyekwenda kinyume na Uislamu basi huyo kiongozi ndiye mwasi na wale wanaopigana naye hawataadhibiwa. Kuhusiana na Uasi Allah amesema katika Qur-an:

وَإِنْ طَآئِفَتَانِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ اقْتَتَلُوا فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا فَإِنْ بَغْتُمْ إِيَّاهُمْ  
عَلَى الْآخَرِي فَقْتَلُوا الَّتِي تَبَغَى حَتَّى تَفِيءَ إِلَى أَمْرِ اللَّهِ فَإِنْ فَاءَتْ  
فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا بِالْعَدْلِ وَأَقْسِطُوا إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ ﴿٩﴾

*Na ikiwa makundi mawili katika Waislamu wanapigana, basi fanyeni suluhu baina yao; na likiwa mojawapo linamdhulumu mwenziwe, basi lipigeni lile linaloonea mpaka lirudie katika amri ya Mwenyezi Mungu. Na kama likirudi basi yapatanisheni baina yao kwa uadilifu. Na hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaohukumu kwa haki. (49:9)*

### (iii) Wizi

Kuhusiana na wizi Allah anasema:

وَالسَّارِقُ وَالسَّارِقَةُ فَاقْطَعُوا أَيْدِيَهُمَا جَزَاءً بِمَا كَسَبَا نَكَالًا مِنَ اللَّهِ  
وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٥٨﴾

*Na mwizi mwanamume au mwizi mwanamke, ikateni mikono yao; malipo ya yale waliyoyachuma. Ndiyo adhabu, itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu na mwenye hikima. (5:38)*

Hukumu ya mwizi ni kukatwa mkono wake wa kulia iwapo yatatimia masharti yafuatayo:

- (a) Awe amekusudia kuchukua mali ya wizi pasi na idhini ya mwenye mali.
- (b) Awe ameiondoshia mali hiyo kutoka mahala inapowekwa.
- (c) Awe amevunja sefu au kasha au kibweta cha fedha.
- (d) Mali iliyoibiwa iwe ni halali katika Uislamu, isiwe mfano pombe, au nyama ya nguruwe au bangi n.k.
- (e) Mali iliyoibiwa iwe imefikia angalau thamani ya kima cha chini Nisab yaani angalau tu ifikie thamani iliyo sawa kifedha na mizani moja. Juu ya hili Mtume(s.a.w) analifahamisha: Mkono wa mwizi usikatwe ila kama thamani ya mali iliyoibiwa ni sawa na thamani ya mizani.
- Zipo kauli tofauti juu ya thamani ya Mizani, wengine wanasema ni robo ( $\frac{1}{4}$ ) ya dinar ya dhahabu au dinar tatu za fedha. Wengine wanasema ni dirham kumi za fedha.
- (f) Isiwepo “shubha”, yaani mazingira yatakayoruhusu kutendeka kosahilo.

### Tahadhari

Adhabu ya mtu ambaye imethibitika kwa haki ya sheria kuwa kaiba ni kukakwa mkono. Ndivyo Allah(s.w) alivyoamuru! Basi ole wao wale wanaochukuwa sheria mkononi kwa kuwapiga watu, kuwajeruhi, kuwachoma moto, na pengine kuwauwa kwa ajili ya kuwatuhumu uwizi. Ni vyema ikaeleweka kuwa mwenye haki ya kuhukumiwa kifo, ni mtu aliyuwa nafsi yenye haki ya kuwa hai kisheria. Vinginevyo Qur-an inakataza!

وَلَا تَقْتُلُوا أَنْفُسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ ..... ﴿١٧﴾

Wala usiuwe nafsi ambayo Mwenyezi Mungu amekataza (kuiuwa) isipokuwa kwa haki .....(17:33).

..... مَن قَتَلَ نَفْسًا بِغَيْرِ نَفْسٍ أَوْ فَسَادٍ فِي الْأَرْضِ فَكَأَنَّمَا قَتَلَ

الْنَّاسَ جَمِيعًا ..... ﴿٣٢﴾

“.....Atakayemuwa mtu bila ya yeye kuiwa mtu, au bila ya kufanya fisadi katika nchi, basi ni kama amewauwa watu wote.....” (5:32)

### (iv) Ujambazi (Haraba)

Adhabu ya ujambazi imefafanuliwa katika Qur-an kama ifuatavyo:

إِنَّمَا جَزَاءُ الَّذِينَ يُحَارِبُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَسْعَوْنَ فِي الْأَرْضِ فَسَادًا أَنْ يُقَتَّلُوا أَوْ يُصَلَّبُوا أَوْ تُقَطَّعَ أَيْدِيهِمْ وَأَرْجُلُهُمْ مِّنْ خَلْفٍ أَوْ يُنْفَوْا مِنَ الْأَرْضِ ۚ ذَٰلِكَ لَهُمْ خِزْيٌ فِي الدُّنْيَا وَلَهُمْ فِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٣٣﴾

*Basi malipo ya wale wanaopigana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kufanya uovu katika nchi ni kuuawa na kusulubiwa au kukatwa mikono yao na miguu yao kwa mabadilisho, au kuhamishwa katika nchi. Hii ndiyo fedheha yao katika dunia; na Akhera watapata adhabu kubwa. (5:33)*

Aya hii inawahusu wale wote wanaoifisidi jamii iwe kijeshi au kwa kuvuruga amani na usalama wa watu na mali zao, wanyama, mimea n.k. hivyo majambazi wanaotumia silaha wanaangukia chini ya sheria hii. Hukumu hii itatumika iwapo jambazi atakuwa amesababisha kifo au la Yaani katika hali zote nne:

- (a) Iwapo raia atavamiwa bila kuporwa mali yake.
- (b) Iwapo raia atanyang'anywa mali yake kwa nguvu lakini bila ya kuuliwa.
- (c) Iwapo raia atauliwa bila kuporwa mali.
- (d) Iwapo raia atauliwa na kuporwa mali.

#### (v) Uzinzi (zinaa)

Adhabu ya zinaa ni kupigwa fimbo 100 hadharani, Allah(s.w) anasema:

الزَّانِيَةُ وَالزَّانِي فَاجْلِدُوا كُلَّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا مِائَةَ جَلْدَةٍ وَلَا تَأْخُذْكُمْ بِهِمَا رَأْفَةٌ فِي دِينِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَلَيْشَهِدَ عَذَابَهُمَا طَآئِفَةٌ مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٤﴾

*Mzinifu mwanamke na mzinifu mwanamume, mpigeni kila mmoja katika wao mijeledi mia. Wala isiwashikeni kwa ajili yao huruma katika (kupitisha) hukumu hii ya Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi mnamuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Na lishuhudie adhabu yao (hii) kundi la Waislamu. (24:2).*

Sharti la kutolewa adhabu ya zinaa ni kupatikana kwa mashahidi wanne walioshuhudia kitendo hicho au kukiri kosa kwa mzinzi mwenyewe.

**(vi) Kashfa (Badhf)**

Kashfa (defamalion) yawezekana ikawa ni msemo (slander) vijembe (innuendo) au maandiko na machapisho (libel) yenye lengo la kutoa kejeli dhidi ya, kutusi au kushusha hadhi ya mtu. Kuhusiana na kosa hili Qur-an imetoa adhabu ifuatayo:

وَالَّذِينَ يَرْمُونَ الْمُحْصَنَاتِ ثُمَّ لَمْ يَأْتُوا بِأَرْبَعَةِ شُهَدَاءَ فَاجْلِدُوهُمْ  
ثَمَنِينَ جَلْدَةً وَلَا تَقْبَلُوا لَهُمْ شَهَادَةً أَبَدًا وَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٤٠﴾

*Wale wanaowasingizia wanawake wataharifu (kuwa wamezini) kisha hawaleti mashahidi wanne, basi wapigeni mijeledi thamanini na Msiwakubalie ushahidi wao tena, na hao ndio mafasiki. (24:4).*

Kashfa katika sheria ya Kiislamu ni kumzulua mtu kuwa kazini au kulawiti au kulawitiwa au kumkashifu mtu muadilifu, mwenye akili timamu na uwezo wa kimwili wa kutenda kosa alilozuliwa.

**(vii) Kunywa ulevi**

Qur-an imeharamisha ulevi pale aliposema Allah(s.w):

*Enyi mlioamini! Bila shaka ulevi na kamari na kuabudiwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu na kutazamia kwa mishale ya kupigia ramli ni uchafu (ni) katika kazi za shetani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufaulu. (5:90).*

Hivyo ilipotoremka aya hii ya 90 na 91 Waislamu waliitii amri ya Allah kwa kumwaga ulevi wote waliokuwa nao. Mtume(s.a.w) alitoa adhabu kwa mlevi kuwa ni kutandikwa viboko 40 kama alivyo amuru:

*“Yule anywaye ulevi mpigeni bakora”*

Imesimuliwa na Anas bin Malik(r.a) kuwa:

*Mtume(s.a.w) alimpiga mlevi kwa matawi (majani) ya mtende na kwa viatu. Na Abu Bakr alimwadhibu (mlevi) kwa fimbo arobaini. (Bukhaary).*

**Makosa ya Qisas**

Baada ya makosa ya Hudud, kundi la pili ni lile la makosa ya Qisas.

Neno qisasi lina maana ya “usawa” au “kufanana”. Lina maana kuwa mtu aliyetenda kosa fulani ataadhibiwa vile vile na kwa namna ile ile aliyotumia katika kumdhulumu mwenzake (kulipiziwa).

Haki ya Qisasi imewekwa na Allah(s.w) katika Qur-an:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِصَاصُ فِي الْقَتْلِ ۗ الْحَرْبُ بِالْحَرْبِ ۗ وَالْعَبْدُ  
 بِالْعَبْدِ ۗ وَالْأُنثَىٰ بِالْأُنثَىٰ ۗ فَمَنْ عُفِيَ لَهُ مِنْ أَخِيهِ شَيْءٌ فَاتَّبِعْهُ  
 بِالْمَعْرُوفِ وَأَدِّءْ إِلَيْهِ بِإِحْسَنٍ ۗ ذَلِكَ تَخْفِيفٌ مِّن رَّبِّكُمْ وَرَحْمَةٌ ۗ فَمَنْ  
 أَعْتَدَىٰ بَعْدَ ذَلِكَ فَلَهُ عَذَابٌ أَلِيمٌ

*Enyi mlioamini! Mmepewa ruhusa kulipa kisasi katika waliouawa – Muungwana kwa muungwana na mtumwa kwa mtumwa, na mwanamke kwa mwanamke. Na anayesamehewa na ndugu yake chochote basi ashikwe kulipa kwa wema; na yeye alipe kwa ihsani. Hiyo ni tahafifu itokayo kwa Mola wenu na ni rehema. Na atakayeruka mipaka baada ya haya, basi yeye atapata adhabu iumizayo. (2:178)*

Kimsingi makosa ya kisasi ni ya namna mbili: Makosa ya kuua na makosa ya kujeruhi. Makosa ya kisasi yanahesabiwa kuwa ni kukiuka haki ya mtu binafsi na hivyo sheria inampa fursa mtu au ndugu zake kulipa kisasi au kulipwa fidia. Kuhusu fidia tazama Qur-an 4:92. Haya ni maelezo ya jumla tu. Hata hivyo kabla ya kutekelezwa kwa kisasi au fidia yapo mambo kadhaa ya kuzingatia kuhusiana na ushahidi wa kosa, na adhabu.

## Makosa ya Ta'azir

Makosa ya Ta'azir ni yale yote ambayo Qur-an na Sunnah havijaweka adhabu fulani maalum. Adhabu za makosa ya aina hii hutolewa na Jaji kwa idhini ya kiongozi wa Kiislamu. Neno **Ta'azir** lina maana ya adhabu. Kisheria Ta'azir lina maana ya adhabu ambayo haijawekwa moja kwa moja katika Qur-an bali hutegemea maamuzi ya Jaji au hakimu kwa kulinganisha kosa, mazingira ya kosa na adhabu.

## Haki za wasiokuwa Waislamu (Dhimmi)

Sheria ya Kiislamu imewapa haki wasiokuwa Waislamu kama ifuatavyo:

### (i) Haki ya ulinzi wa maisha na mali

Damu ya Dhimmi ni haramu kumwagwa pasipo sababu kama ilivyo damu ya Muislamu. Muislamu akimua Dhimmi adhabu yake ni sawa na ile ya kumuua Muislamu. Mtume(s.a.w) amesema:

*“Ni jukumu langu kusimamia haki za wanyonge”.*

Vile vile mali ya Dhimmi katika sheria ya Kiislamu inathaminiwa kama ilivyo mali ya Muislamu. Muislamu akiiba mali ya Dhimmi kwa kiwango kile kilichotajwa na Mtume atahukumiwa kukatwa mkono kama kawaida.

Khalifa wa nne wa Mtume (s.a.w.) baada ya kumuhukumu Muislamu mmoja kuuawa na warithi wa Dhimmi aliyemuua, alisisitiza:

Yeyote aliye Dhimmi wetu damu yake ni takatifu kama damu yetu na mali yake ni takatifu kama mali yetu.

### ***(ii) Haki katika sheria ya jinai***

Katika sheria ya Kiislamu hukumu za makosa ya jinai (*penal laws*) zinawahusu wadhimmi sawa na zinavyowahusu Waislamu. Makosa ya jinai ni makosa yanayoathiri jamii nzima na mhalifu atakuwa anaidhulumu jamii nzima. Kwa hivyo Dhimmi akiiba atakatwa kiganja chake cha mkono wa kulia, akizini atatandikwa viboko 100.

Ila Dhimmi hataadhibiwa kwa kosa la ulevi kama atakavyoadhibiwa akilewa Muislamu kwa kutandikwa viboko 40,

### ***(iii) Haki katika sheria za Madai (Civil Laws)***

Katika sheria ya Kiislamu hukumu za madai ni sawa sawa kwa Waislamu na wasio kuwa Waislamu. Kila mwenye kudaiwa atahukumiwa na sheria kutoa haki ya mdai bila ya ubaguzi wa dini. Pia yale yaliyo haramishwa kwa Waislamu katika uchumi pia sheria inayakataza kwa madhimmi. Kwa mfano riba na kamari ni haramu kwa Waislamu na imekatazwa pia kwa wasiokuwa Waislamu kwani riba na kamari huiathiri jamii nzima.

### ***(iv) Haki ya heshima ya Dhimmi***

Kumvunjia heshima dhimmi kwa kumtukana, kumuita jina baya, kumdhuru, kumuadhiri, kumteta, n.k. ni makosa makubwa sana mbele ya Allah(s.w) kama ilivyo makosa makubwa kumfanyia Muislamu. Heshima ni haki inayomstahiki kila mwanadamu pasi na ubaguzi wa aina yoyote. Ni dhima ya serikali ya Kiislamu kulinda heshima ya kila mtu.

### ***(v) Sheria ya Mtu binafsi***

Katika sheria ya Kiislamu, mambo yote yanayohusu imani ya mtu binafsi huhukumiwa kulingana na imani ya dini yake. Kama jambo lililoharamishwa kwa Waislamu si haramu kulingana na imani ya Dhimmi, sheria itaendelea kumruhusu kulitenda jambo hilo.



## Zoezi 2:8

1. Eleza maana ya sheria kilugha na kisheria.
2. Taja na kufafanua kwa muhtasari kazi za sheria katika jamii na manufaa yake.
3. Sheria zilizotungwa na wanadamu hazizingatii umbile halisi la mwanadamu, hivyo huzidisha matatizo badala ya kutatua. Jadili kwa kutoa mifano hai toka katika jamii yako.
4. Bainisha udhaifu uliopo kwenye chimbuko la sheria zilizotungwa na wanadamu kwa msukumo wa matashi na mahitaji, uzoefu, sayansi, akili na fikra zao.
5. (a) Taja misingi mikubwa miwili ya sheria za Kiislamu.  
(b) Eleza maana ya **Al-Qiyaas** na **Al-Ijima'a**; na tafauti zake.
6. Eleza kwa muhtasari, kwanini sheria za Allah(s.w) ndizo zenye uwezo wa kuondoa dhulma na ukandamizaji, na kusimamisha haki na uadilifu katika jamii.
7. (a) Taja makundi mawili ya amali za waja kwa mujibu wa Qur'an.  
(b) Orodhesha daraja tatu za matendo mema.
8. Kazi ya Sheria za Kiislamu, ni kumnufaisha na kumhifadhi mwanadamu. Thibitisha kwa dondoo tano zenye maelezo mafupi.
9. Bainisha
  - (a) Kanuni tatu zenye kumtwika au kumvua mja dhima ya kuhukumu au kuhukumiwa katika sheria ya Kiislamu.
  - (b) Utaratibu wa mashitaka wa Kiislamu.
  - (c) Tanzu za makosa katika sheria ya Kiislamu.
10. Uislamu ni mfumo wa maisha wa kiadilifu, hivyo, haunyimi wala kukandamiza haki za wasiokuwa Waislamu. Dhihirisha ukweli huu kwa kurejea Qur'an na Sunnah.

## UCHUMI KATIKA UISLAMU

### *Maana ya Uchumi*

Mfumo wa maisha wa Kiislamu humuelekeza binadamu kujenga na kudumisha uhusiano wake na Allah(s.w), uhusiano wake na binadamu wenziwe na uhusiano wake na vinavyomzunguka katika ulimwengu huu. Aidha mfumo

wa Kiislamu una lengo la kuelekeza namna ya kukiendea kila kipengele muhimu cha maisha ya binadamu **uchumi** ukiwa miongoni.

Uchumi hujumuisha uzalishaji, usambazaji na utumiaji wa mali na huduma. Uislamu umelipa suala la uchumi nafasi muhimu kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

وَلَا تُؤْتُوا السُّفَهَاءَ أَمْوَالَكُمُ الَّتِي جَعَلَ اللَّهُ لَكُمْ قِيَمًا ..... ﴿٥﴾

*“Wala msiwape wapumbavu mali zenu ambazo Allah amezijaalia kuwa msingi wa maisha yenu...” (4:5)*

Uislamu umeweka utaratibu wa kiuchumi unaohakikisha kuwa haki inatendeka kwa wote ili kudumisha amani, utulivu na mshikamano wa kweli katika jamii. Katika sura hii tutaangalia uchumi katika Uislamu kwa kuzingatia maeneo yafuatayo:

1. Nadharia ya uchumi wa Kiislamu.
2. Umuhimu wa uchumi katika Uislamu.
3. Mazingatio muhimu katika uchumi wa Kiislamu.
4. Sera ya uchumi katika Uislamu.
5. Haki na Uhuru wa kuchuma katika Uislamu.
6. Mgawanyo wa mali katika Uislamu.
7. Umuhimu wa Benki katika Uchumi.
8. Tatizo la Riba.

## 1. Nadharia ya Uchumi wa Kiislamu

Mfumo wa uchumi katika Uislamu ni utaratibu utokanao na Qur-an na Sunnah juu ya uzalishaji, umilikaji, usambazaji, na utumiaji wa mali na huduma pamoja na miiko yake. Kwa msingi huo, uchumi huo umejengwa juu ya fikra ya ukati na kati (Iqtisaad), hivyo umetofautiana na mifumo mingine iliyobuniwa na watu. Dhana (concept) ya ukati (Iqtisaad) katika shughuli za kiuchumi ni kule kutoa uhuru kwa mtu binafsi (sekta binafsi) kuchuma na kumiliki mali ili iwe motisha kwake ya kuchapa kazi wakati huo huo serikali ikisimamia na kutoa miongozo katika uzalishaji na ugawaji, na vile vile kuwa na sekta zake (sekta za umma) ili kila mwana jamii apate haki za kimsingi. Mifumo iliyobuniwa na watu imeathiriwa na udhaifu wa kibinadamu wa kuelemea upande huu au ule.

Ipo mifumo ya kiuchumi kama vile ubepari ambao umeelemea mno katika ubinafsi kiasi ambacho umepuuza kabisa haki za kijamii. Katika mfumo huu (ubepari) umma hauna chake; mali, huduma na shughuli mbali mbali hubinafsishwa. Wachache chini ya mfumo huu ndio hunufaika na rasilimali za Taifa. Hujilimbikizia mali, na motisha yao ya uzalishaji ni ile faida waipatayo. Serikali kuu ya mfumo huu wa kibepari hushirikiana na wachache hao waliohodhi mali, kuwanyonya walio wengi.

Pia, kuna mfumo wa uchumi wa Kikomunist au Kijamaa ambao nadharia yake imeelemea mno katika **“usawa”** wa sare kiasi cha kudhoofisha mno motisha ya watu binafsi na hivyo kupelekea kukosekana kwa ufanisi katika uzalishaji. Katika mfumo huu mali na shughuli mbali mbali hutaifishwa (toka milki ya watu binafsi kuwa milki ya taifa). Ukweli ni kwamba huwa si mali ya taifa kama inavyotangazwa bali mbiu ya **“usawa”**, na **“mali ya umma”**, chini ya mfumo huu, ni mwavuli tu uliokinga kikundi cha watu kilichojipa mamlaka ya uendeshaji wa nchi kwa sura ya chama au serikali kwa maslahi ya kikundi hicho. Kikundi hicho ndicho humiliki na kutafuna mali huku wananchi wengi wakiendelea kudhulumwa kwa sababu mbali mbali. Hivyo hakuna usawa ulio chini ya mfumo huu bali ni ubinafsi ule ule ambao huhamishwa toka kwa mtu binafsi kwenda kwenye kikundi fulani.

## **Tofauti kati ya Mfumo wa Uchumi wa Kiislamu na Ile ya Kitwaghuti**

### *(i) Dhana ya mafanikio*

Katika mtazamo wa uchumi wa Kiislamu mafanikio yanatazamwa kwa kuzingatia hatima ya ama mtu kupata radhi za Mwenyezi Mungu au kubeba laana ya Mwenyezi Mungu. Mafanikio hayapimwi kwa mali. Katika uchumi wa Kitwaghuti mafanikio maana yake ni mafanikio ya kiuchumi. Ni kiasi gani cha mali mtu amefanikiwa kukipata. Jinsi atakavyojilimbikizia mali ndivyo itakavyoonesha **“mafanikio”** yake. Katika Uislamu kufuzu kwa kweli ni kupata radhi za Mwenyezi Mungu na kufeli kukubwa ni kule kukosa radhi hizo. Hivyo ili binadamu afanikiwe hana budi kuishi kwa uadilifu.

Mtazamo huu unaathiri pia mizani yake ya wakati. Muislamu anapozitumia rasilimali zilizomo katika ardhi hafikirii tu mahitaji yake ya binafsi ya sasa bali pia matokeo ya vitendo vyake kwa vizazi vijavyo.

Kwa mtazamo huu mtu anakuwa hana haki ya kufuja mali au rasilimali za ardhi, kwa vile anazingatia maslahi yake katika maisha haya, huko akhera na maslahi ya vizazi vijavyo. Mafanikio katika Uislamu ni kule kulijua lengo la maisha hapa ulimwenguni, kuwa na kumbukizi ya kisimamo mbele ya Mola siku ya hesabu, kukinai moyoni na kuona kila kitu cha ulimwengu huu kuwa ni

cha kawaida. Kujitahidi kuyaendea mambo mema bila ya kuchelea chochote na kujiepusha na yale yote yanayoweza kumtoa mtu au kumkhasirisha katika maisha yajayo hata kama yana “manufaa” kwa mtazamo wa wengi katika maisha haya. Kujali shida na matatizo ya wengine na kuweza kutoa kwa ajili ya kuwasaidia wengine kwa kadiri ya wasaa uliopo.

Kuwa na huruma, mapenzi na bashasha isiyobagua taifa, kabila, nasabu wala ukoo wa mtu. Kutokuwa na chuki, majivuno, kibri, utesi, usengenyi, ulimbukeni, kujiona, kujitukuza au kujidhalilisha na kujitweza kwa yeyote yule anayemulikwa na jua iwe kihali au kimali.

Aliyetajiri wa Nafsi ni yule ambaye fursa yoyote aliyonayo haiwi kero na huzuni kwa wengine bali huitumia mwisho wa uwezo wake kupambana na taratibu potofu na kandamizi zinazotawala jamii yake. Hii ndiyo Dhana ya mafanikio katika Uislamu.

### **(ii) Dhana ya umilikaji mali**

Katika Uislamu mmiliki wa hakika wa mali ni Mwenyezi Mungu, mwanadamu kama Khalifa wa Allah hapa duniani anamiliki mali kwa dhamana tu siyo kwa hakika na kwa sababu hiyo ataulizwa jinsi alivyotumia hiyo mali.

Pamoja na hivyo mali katika Uislamu si kitu kiovu bali kinachosisitizwa ni kuwa ichumwe na kutumiwa kwa kuzingatia maelekezo ya Mwenyezi Mungu.

Kuhusu kutafuta mali Qur-an inatueleza kama ifuatavyo:

وَأَبْتَغِ فِيمَا آتَاكَ اللَّهُ الدَّارَ الْآخِرَةَ وَلَا تَنْسَ نَصِيبَكَ مِنَ

الدُّنْيَا ..... 

“Na utafute – kwa yale aliyokupa Mwenyezi Mungu makazi mazuri ya akhera wala usisahau sehemu yako ya dunia”. (28:77)

### **(iii) Dhana ya bidhaa**

Katika uchumi wa kitwaghati kitu chochote chaweza kuwa ni bidhaa maadamu kinaweza kutumiwa na mtu. Kwa mfano pombe pamoja na madhara yake huitwa bidhaa kwa kuwa hutumiwa na baadhi ya watu.

Katika uchumi wa Kiislamu “bidhaa” huitwa ama “Atwayyibaati” au “Rizk”. Atwayyibaat ni kitu kizuri, safi, Twahara. Rizk ni neema, au hidaya itokayo kwa Allah(s.w). Hivyo katika uchumi wa Kiislamu bidhaa ni vile vitu halali tu kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu. Kisichokuwa halali si bidhaa. Kwa mfano pombe

ni haramu hivyo si bidhaa.

#### (iv) Dhana ya Matumizi

Kwa kuwa Allah ndiye Muumba wa watu na rasilimali zote katika ulimwengu, sera ya uchumi wa Kiislamu haimpi mtu fursa ya kufuja mali apendayo pamoja na uhalali atakaokuwa nao katika dhamana ya milki ya mali hiyo. Kinyume chake, katika uchumi wa Kitwaghuti mtu anayo fursa ya kufuja mali apendavyo maadamu ni mmiliki wa mali hiyo.

#### (v) Mizani ya wakati katika tabia ya mtumiaji

Mtu anapofanya maamuzi yoyote hujiuliza nini matokeo au matazamio ya kitendo hiki au uamuzi huu baada ya saa moja au wiki moja au mwezi mmoja au mwaka mmoja au miaka mitano au kumi n.k. Kipimo cha wakati katika uchumi wa Kitwaghuti na ule wa Kiislamu ni tofauti. Katika ujahili mtu hujiuliza mali kiasi gani awe amepata atakapofikia umri fulani, kinyume chake Muislamu anapofikiria jambo lolote, pamoja na masuala ya uchumi, kipimo chake cha wakati hukupa upeo mpana sana. Hujiuliza, je hiki kitendo ninachofanya kitakuwa na matokeo gani siyo tu kwa wiki hii au mwezi huu au mwaka huu au ujao bali kina matokeo gani siku ya kiyama. Muislamu anaamini kuwa ipo siku ya malipo na kwamba kuna pepo na moto. Watu watahesabiwa na kulipwa kwa mujibu wa matendo yao. Kila mtu binafsi atasimamishwa peke yake mbele ya Mwenyezi Mungu na kupewa hisabu yake. Imani hii ina athari kubwa kwa Muislamu na maamuzi yake anayochukuwa.

### Milki ya Rasilimali

Ili kujipatia maendeleo ya kiuchumi katika zama zote mwanadamu anahitaji rasilimali za kumwezesha kufikia azma hiyo. Miongoni mwa rasilimali kuu (natural resources) ni zile zinazohusiana na ardhi, maji na wanyama. Kwa mujibu wa Uislamu rasilimali hizo ni neema za Allah(s.w).

#### (a) Rasilimali za Ardhi

وَفِي الْأَرْضِ قِطْعٌ مُّتَجَوِّرَاتٌ ۖ وَجَنَّتٌ مِّنْ أَعْنَبٍ ۖ وَزَّرَعٌ ۖ وَنَخِيلٌ ۖ صِنَوَانٌ  
وَعَيْرٌ ۖ صِنَوَانٍ يُسْقَىٰ بِمَاءٍ وَاحِدٍ ۖ وَنُفُضِلٌ ۖ بَعْضُهَا عَلَىٰ بَعْضٍ فِي  
الْأَكْلِ ۚ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿١٠٠﴾

“Na katika ardhi mna vipande vinavyoangana (na kuzaa kwake namna mbali mbali) na mna mabustani ya mizabibu, na mimea mingine, na mitende ichipuyao katika shina moja na isiyochipua katika shina moja. Vyote vinavyonyweshelzwa

(vinamiminiwa) maji yale yale; na tunavifanya bora baadhi yake vyengine katika kula (katika utamu). Hakika katika haya zimo ishara kwa watu wanaotia mambo akilini”. (13:4)

### (b) Rasilimali za maji na mvua

..... وَتَرَى الْأَرْضَ هَامِدَةً فَإِذَا أَنْزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَاءَ اهْتَزَّتْ وَرَبَّتْ  
وَأُنبَتَتْ مِنْ كُلِّ زَوْجٍ بَهِيجٍ ﴿١٣﴾

“... Na unaiona ardhi imetulia kimya lakini anapoyateremsha maji juu yake, inataharaki na kukuwa na kuotesha kila namna ya mimea mizuri.” (22:5)

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَسَلَكَهُ يَنْبِيعَ فِي الْأَرْضِ ثُمَّ  
خُجِرَ بِهِ زُرْعًا مُخْتَلِفًا أَلْوَانُهُ ..... ﴿٣٩﴾

“Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu ameteremsha maji kutoka mawinguni. Kisha akayapitisha (chini kwa chini) yakawa chemchem katika ardhi, tena akaotesha kwayo mimea ya rangi mbali mbali (na sura mbali mbali)...” (39:21).

### (c) Rasilimali za bahari na samaki

﴿ اللَّهُ الَّذِي سَخَّرَ لَكُمْ الْبَحْرَ لِتَجْرِيَ الْفُلُكُ فِيهِ بِأَمْرِهِ ﴾ وَلِتَبْتَغُوا مِنْ  
فَضْلِهِ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٤٥﴾

“Mwenyezi Mungu ndiye aliyekutiishieni bahari ili humo zipite merikebu kwa amri yake, na ili mtafute fadhila yake na mpate kushukuru”. (45:12)

وَهُوَ الَّذِي سَخَّرَ الْبَحْرَ لِتَأْكُلُوا مِنْهُ لَحْمًا طَرِيًّا وَتَسْتَخْرِجُوا مِنْهُ  
حِلْيَةً تَلْبَسُونَهَا وَتَرَى الْفُلُكَ مَوَاحِرَ فِيهِ وَلِتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ  
وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿١٦﴾

“Na yeye ndiye aliyeitiisha bahari ili humo mule daima kitoweo kipya (samaki) na mtoe humo mapambo mnayoyavaa. Na utaona merikebu zikipasua humo, ili mtafute fadhila zake (kwa kufanya biashara) na ili mpate kushukuru.” (16:14)

**(d) Rasilimali za wanyama**

وَالَّذِينَ كَفَرُوا هُمْ أَكْثَرُ عَلَىٰ عُقُوبٍ ۗ وَأَلَّا تَعْمَرَ خَلْقَهَا ۗ لَكُمْ فِيهَا دِفْءٌ وَمَنْفَعٌ وَمِنْهَا تَأْكُلُونَ ﴿٥﴾  
 وَلَكُمْ فِيهَا جَمَالٌ حِينَ تُرْتَحُونَ وَحِينَ تَسْرَحُونَ ﴿٦﴾

“Na (pia) amewaumba wanyama. Katika hao mnapata (vifaa vitiavyo) joto na manufaa; na wengine mnawala. Na mnaona raha mnapowarudisha jioni na mnapowapeleka malishoni asubuhi. (16:5 - 6).

وَتَحْمِلُ أَثْقَالَكُمْ إِلَىٰ بَلَدٍ لَّمْ تَكُونُوا بَلِّغِيهِ إِلَّا بِشِقِّ الْأَنْفُسِ ۗ إِنَّ رَبَّكُمْ لَرءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿٧﴾ وَالْحَيْلَ وَالْبِغَالَ وَالْحَمِيرَ لِتَرْكَبُوهَا وَزِينَةً  
 وَيَخْلُقُ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٨﴾

Na (wanyama hao pia) hubeba mizigo yenu kupeleka katika miji msiyoweza kuifikia isipokuwa kwa mashaka na taabu. Hakika Mola wenu ni Mpole sana (na) Mwenye rehema nyingi. Na (amewaumba) farasi na nyumbu na punda ili muwapande na (wawe) mapambo. Na ataumba (vipando vyingine) msivyovijua”. (16:7 - 8).

**(e) Rasilimali za madini**

Muhutajari wa aya hizo juu ya rasilimali unapatikana katika aya ifuatayo:

هُوَ الَّذِي خَلَقَ لَكُمْ مَّا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا ..... ﴿٢٩﴾

“Yeye ndiye aliyekuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi.” (2:29).

**Wajibu wa Kufanyakazi**

Uislamu siyo tu unawahimiza watu kufanya kazi na kutokuwa wavivu bali kufanya kazi ni lbada. Kila jambo lenye manufaa kwa watu binafsi, familia, jamii (n.k) laweza kuhesabiwa kuwa ni lbada kwa Allah yakitimia masharti mawili; usafi wa nia (Ikhlas) na kutenda jambo kwa kuzingatia mipaka ya sheria ya Kiislamu. Hivyo kazi ni lbada. Kufanya kazi ni wajibu alionao mtu mbele ya Allah. Qur-an inawahimiza Waislamu kutenda kazi nzuri zenye manufaa katika eneo lolote lile.

وَقُلِ أَعْمَلُوا فَسَيَرَى اللَّهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ وَالْمُؤْمِنُونَ وَسَتُرَدُّونَ إِلَىٰ

عِلْمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَيُنبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٠٥﴾

*Na sema: Tendeni mambo (mazuri). Mwenyezi Mungu atayaona mambo yenu hayo na Mtume wake na Waislamu. Na mtarudishwa kwa mjuzi wa siri na dhahiri; naye atakwambieni (yote) mliyokuwa mkiyatenda.” (9:105)*

Katika aya hii Mwenyezi Mungu amefungua milango kwa watu kutenda mambo yote mema katika eneo lolote la uchumi au siasa na yeye atalionna na atalilipa.

## Uchaguzi wa Kazi

Uislamu umempa mtu uhuru wa kuchagua kazi yoyote aipendayo maadamu kazi hiyo ni ya halali kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu. Na ni wajibu wa serikali ya Kiislamu kuhakikisha kuwa watu wanapata fursa ya kufanya kazi wazipendazo. Watu watafanya kazi kwa mujibu wa vipaji vyao, kwani Mwenyezi Mungu amewajaalia watu vipawa mbali mbali:

..... وَرَفَعَ بَعْضَكُمْ فَوْقَ بَعْضٍ دَرَجَاتٍ لِّيُبْلُوَكُمْ فِي مَا آتَاكُمْ ..... ﴿١٦٥﴾

*“Na amewanyanyua baadhi yenu juu ya wengine daraja kubwa ili akufanyieni mtihani kwa hayo aliyokupeni.” (6:165).*

Kila mtu anafanyiwa mtihani kwa neema au kipawa alichopewa. Katika maisha yetu ya kila siku wanadamu ni viumbe wanaotegemeana kila mmoja ananufaika kwa kazi ya mwenzake. Daktari atamhitaji Muashi kumjengea nyumba yake na Muashi atamhitaji Daktari kumtibu maradhi yake n.k. Katika Uislamu kazi hutegemea uwezo tu hakuna kazi zilizotengwa kwa ajili ya watu wa ukoo au kabila au nasaba fulani.

## Tofauti ya Malipo

Tofauti ya mapato au malipo ipo kwa sababu ya utendaji, uwingi au ubora wa bidhaa zilizozalishwa. Ni halali kwa fundi aliyetengeneza mashati kumi, hasa amzidi kipato yule aliyetengeneza matano. Au yule aliyetengeneza kitu bora lazima amzidi yule aliyetengeneza kitu duni. Aidha tofauti ya mapato pia ni halali iwepo kutokana na muda mrefu wa mafunzo baadhi ya kazi zikilinganishwa na nyingine. Kwa mfano ikiwa mtu atajiriwa kufuta mavumbi katika madirisha ya ofisi atahitajia siku moja tu ya kuelekezwa namna ya kuifanya kazi hiyo. Lakini mtu akijiriwa kutengeneza madirisha hayo atahitajia



muda mrefu zaidi katika kujifunza useremala hawezi kuelekezwa kwa siku moja tu halafu akaweza kuunda dirisha. Hivyo malipo ya mfutaji na mtengenezaji wa madirisha hayawezi kuwa sawa. Malipo yao yakiwa sawa basi watu wanaweza kuzikwepa kazi zinazohitaji mafunzo ya muda mrefu kama udaktari, usanifu majengo uhandisi (n.k.) na kukimbilia zile zenye mafunzo ya muda mfupi kama utarishi, uhudumu, kufagia ofisi n.k.

Aidha malipo hayatakuwa halali iwapo shughuli anayoifanya Muislamu ni faradhi. Kwa mfano; si halali kwa Imamu kupokea mshahara kwa ajili ya kusalisha swala za faradhi, si halali kupokea malipo kutokana na kumhudumia masikini, n.k.

## Hifadhi ya Wafanyakazi

Uislamu pia umeweka taratibu za kuhifadhi haki na maslahi ya Wafanyakazi. Kwanza kila mfanyakazi lazima awe na mkataba na mwajiri wake. Mkataba huo uweke wazi malipo yake na kazi yake na makubaliano yao mengine. Mkataba huo ni bora uwe kwa maandishi lakini waweza pia kuwa kwa mdomo.

Mwenyezi Mungu ameagiza katika Qur-an kuwa watu watekeleze kikamilifu ahadi zao za halali.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا اَوْفُوْا بِالْعُقُوْدِ ..... ﴿٥﴾

“Enyi mlioamini tekelezeni wajibu ...” (5:1)

Katika Hadith iliyosimuliwa na Bukhaary, Mtume(s.a.w) amesema kuwa miongoni mwa watu watatu ambao Mtume(s.a.w) atawakataa siku ya Kiyama ni yule anayemwajiri mfanyakazi halafu asimpe haki zake. Katika Hadith nyingine amesema; Mlipeni mtu mliyemuajiri kabla ya jasho lake halijakauka. Mradi wa Hadith hii ni kuwa mtu asicheleweshewe malipo yake. Kama mapatano ni kila wiki au kila mwezi n.k. basi muda huo ukifika tu mtu alipwe. Vivyo hivyo kwa mfanyakazi malipo ya kazi yatakuwa ni halali iwapo atatimiza kipimo walichoafikiana na mwajiri kwa mshahara huo. Kutegea kazi humfanya mtu achukue sehemu ya malipo isiyohaki yake. Kwa hiyo, kipato kinachotokana na kazi iliyotegewa kimechanganyika na kipato cha haramu. Uislamu unamtaka kila muumini awe mwaminifu na muadilifu katika kazi baada ya kupatana na kukubaliana na muajiri.

## 2. Umuhimu wa Uchumi katika Uislamu

Mwanadamu ameumbwa na mahitajio mengi ambayo hana budi kuyapata ili aweze kuishi kwa furaha na amani hapa ulimwenguni. Kwa kuwa mwanadamu ni mchanganyiko wa mwili na roho, pia mahitajio yake yamegawanyika, ana mahitajio ya kiroho na kimwili. Mahitajio ya kiroho ambayo humuwezesha mwanadamu kuishi maisha ya utulivu yenye furaha na amani, hupatikana kwa

kufuata kwa utii na unyenyekevu mwongozo wa Allah(s.w).

Mahitajio ya kimwili kama vile chakula, mavazi, vipando na njia ya uchumi hupatikana kwa kuchapakazi chini ya mazingira yatokanayo na itikadi sahihi yenye kusimamiwa na viongozi wanaozingatia haki itokayo kwa Muumba. Katika Qur-an tunafahamishwa kuwa Allah(s.w) amejaalia mali anayoichuma mwanadamu iwe ndiyo inayoboresha maisha yake:

وَلَا تُؤْتُوا السُّفَهَاءَ أَمْوَالَكُمُ الَّتِي جَعَلَ اللَّهُ لَكُمْ قِيَمًا ..... ﴿٤﴾

“Wala msiwape wapumbavu mali zenu ambazo Mwenyezi Mungu amezijaalia kwa ajili ya maisha yenu ...” (4:5)

Kutokana na aya hii, kuchuma mali si jambo la hiari kwa mwanadamu kwani kwa namna Allah(s.w) alivyokadiria, maisha ya mwanadamu kwa hapa ulimwenguni hayawezekeani pasi na kuchuma.

Ni kweli kwamba vitu vyote vilivyomzunguka mwanadamu katika ulimwengu huu vimeumbwa kwa ajili yake kwa ushahidi wa Qur-an:

هُوَ الَّذِي خَلَقَ لَكُمْ مَّا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا ..... ﴿٢٩﴾

“Yeye ndiye aliyekuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi...” (2:29).

Lakini mara nyingi vitu hivi haviko katika hali ya kutumiwa na mwanadamu moja kwa moja. Bali mwanadamu analazimika kutumia elimu yake, Maarifa yake, juhudi zake na vipawa vyake vingine ili ayabadilishe mazingira yake yaweze kumtumikia na kukidhi haja zake.

Kwa mtazamo huu Uislamu unatuamrisha kuchuma kama unavyotuamrisha kusimamisha Swala, kutoa Zakat na kutekeleza lbada nyingine maalumu kama hizi:

فَإِذَا قُضِيَتِ الصَّلَاةُ فَانْتَشِرُوا فِي الْأَرْضِ وَابْتَغُوا مِن فَضْلِ اللَّهِ وَاذْكُرُوا

اللَّهُ كَثِيرًا لَّعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿١٠﴾

Na itakapokwisha swala, tawanyikeni katika ardhi mtafute fadhila za Mwenyezi Mungu na mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi, ili mpate kufaulu. (62:10)

Tunajifunza kutokana na aya hii kuwa, kuchuma ni wajibu unaompasa Muislamu mara tu baada ya kutekeleza lbada maalum. Hili linabainishwa katika Hadithi ifuatayo:

“Abdullah bin Mus’ud ameeleza kuwa Mtume(s.a.w) amesema: Kutafuta chumo la halali ni faradhi baada ya kutekeleza faradhi nyingine.” (Baihaqi).

Pia Mtume(s.a.w) amebainisha wazi ubora wa kujizatiti katika kutafuta chumo la halali kwenye Hadith ifuatayo:

“Miqdam bin Ma’ad Yakrab ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Hapana mmoja wenu aliyekula chakula kizuri kuliko kile alichokula kutokana na kazi ya mkono wake mwenyewe. Na Daud, Mtume wa Allah, alikuwa anakula kutokana na kazi ya mikono yake.” (Bukhaary)

Kwa upande mwingine Uislamu unalaani uvivu na kuwategemea wengine pasi na sababu au dharura maalum kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

“Jubair bin Awam ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Mmoja wenu kuchukua kamba na kisha akaja na mzigo wa kuni akiwa amebeba mgongoni mwake na akauuza, na kwakufanya hivyo Allah akailinda hadhi yake, ni bora kwake kuliko kuomba omba watu, wakimpa chochote au wasimpe (Bukhaary.)

Mpaka hapo tumejifunza kuwa kwa mtazamo wa Uislamu, uchumi ndio msingi wa maisha ya mwanadamu hapa ulimwenguni na Uislamu umewajibisha kuchuma kwa kila mwenye uwezo.

Ni makosa katika Uislamu mtu mwenye uwezo na afya kubweteka na kuwategemea wengine katika kukidhi mahitaji yake.

### 3.Mazingatio Muhimu katika Uchumi wa Kiislamu

Kanuni kuu za uchumi katika Uislamu ni:

- (i) Kumwamini Allah kuwa ndiye Muumba na mfalme wa ulimwengu huu yaani kumtii Allah katika mambo yote.
- (ii) Binadamu ni Khalifa wa Allah hapa duniani, hivyo wajibu wake ni kusimamisha amri ya Allah.
- (iii) Ili kumsaidia mwanadamu kutimiza wajibu wake kama Khalifa, Allah amemdhaliishia kila kitu katika ulimwengu huu:

﴿ اللَّهُ الَّذِي سَخَّرَ لَكُمُ الْبَحْرَ لِتَجْرِيَ الْفُلُكُ فِيهِ بِأَمْرِهِ وَلِتَبْتَغُوا مِنْ

فَضْلِهِ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿١٢﴾

“Mwenyezi Mungu ndiye aliyekutiishieni bahari ili humo zipite merikebu kwa amri yake ili tafute fadhila yake na mpate kushukuru”. (45:12).

﴿٦٥﴾ ..... أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ سَخَّرَ لَكُمْ مَّا فِي الْأَرْضِ

“Je, Hukuona kwamba Mwenyezi Mungu amevitiisha kwa ajili yenu vilivyomo ardhini...” (22:65)

أَلَمْ تَرَوْا أَنَّ اللَّهَ سَخَّرَ لَكُمْ مَّا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَأَسْبَغَ عَلَيْكُمْ نِعْمَهُ ظَهْرَةً وَبَاطِنَةً ﴿٦٦﴾ ..... ﴿٦٦﴾

“Je, Hukuona kwamba Mwenyezi Mungu amekutiishieni vilivyomo mbinguni na ardhini na anakukamilishieni neema zake zilizo dhahiri na za siri? ...” (31:20).

هُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ ذُلُولًا فَأَمْشُوا فِي مَنَاكِبِهَا وَكُلُوا مِن رِّزْقِهِ  
وَإِلَيْهِ النُّشُورُ ﴿٦٧﴾

“Yeye ndiye aliyefanya ardhi iweze kutumika kwa ajili yenu. Basi nendeni katika pande zake zote na kuleni katika rizki zake na kwake ndiyo marejeo.” (67:15).

Hivyo kuzitumia neema hizo za Allah si dhambi bali ni katika kushukuru.

(iv) Kutokana na wajibu wa Ukhalifa wa Allah, mwanadamu ataulizwa kwa neema alizompatia na atahesabiwa kwazo, ikiwa ni pamoja na namna alivyochuma na kutumia mali.

(v) Kuwa na mali au kutokuwa na mali nyingi au kidogo si dalili ya ubora au udhalili wa mtu. Hali zote mbili ni mtihani. Anachotazama Allah ni nyoyo za watu.

Misingi au kanuni hizo zikithibiti katika moyo wa mtu zinakuwa na athari kubwa sana katika shughuli za kiuchumi za Muislamu.

Kanuni ya **kwanza** kwa mfano humfanya mtu afuate maamrishi ya Allah na hivyo atafanya kila njia ajiepushe na makatazo yake.

**Pili**, kwa kujua kuwa yeye ni Khalifa tu atajua yeye si mmilikaji wa hakika, hivyo atafuata maagizo ya huyo aliyempa ukhalifa yaani Allah.

**Tatu**, atajua kuwa utajiri si kitu cha kukipigania, bali mtu apiganie maisha bora na afya katika kutafuta radhi za Allah(s.w).

**Nne**, kwa kujua kuwa atahesabiwa na Allah anayeshuhudia kila kitu ataendesha shughuli zake za kiuchumi kwa kumcha Allah.

## 4. Sera ya Uchumi katika Uislamu

**Kwanza**, katika Uislamu utekelezaji wa mambo yote hutegemea zaidi ucha-Mungu wa mtu binafsi na kuogopa kwake kusimamishwa mbele ya Allah na kuhisabiwa, kuliko usimamizi wa vyombo vya dola kama sheria, mahakama, na askari polisi. Hii ni kwa sababu hisabu siku ya kiyama itakuwa kwa kila mtu binafsi. Hapana shaka vyombo vya dola vipo katika Uislamu na vinafanya kazi lakini msisitizo wa utekelezaji wa mambo yote upo katika uadilifu na taqwa kuliko katika kuogopa polisi na mahakama.

**Pili**, uhuru wa watu binafsi kufanya wanalolitaka ndio sera inayofuatwa katika Uislamu. Yaani katika masuala ya uchumi Uislamu umempa uhuru kila mtu afanye lile analoliona linafaa. Na serikali ya Kiislamu haitaingilia uhuru wake huo isipokuwa tu pale ambapo haki haitatendeka iwapo uhuru huo hautaingiliwa. Mtume(s.a.w) amelielezea kwa ufasaha sana suala hili pale alipoyapigia mfano maisha ya watu katika jamii na wasafiri waliomo chomboni baharini:

*“Hebu tuchukue mfano wa meli inayosafiri baharini ikiwa imejaza abiria ambao wamekaa katika sehemu zote za chini na juu. Sasa iwapo abiria mmoja aliyekaa katika sakafu hiyo ataamua kujipatia maji kirahisi kwa kutoboa pale alipoketi na iwapo abiria wengine watamzuia kufanya hivyo (na ni wajibu wa abiria wote walio juu na chini kumzuia) watamnusuru yeye na wao wenyewe na kufa maji. Iwapo watamwacha atoboe basi watazama wote waliochini na juu ya meli.” (Bukhaary).*

Mfano huu unatuonesha kuwa japo Uislamu unampa kila mtu uhuru wa kufanya alitakalo lakini uhuru huo una mipaka. Iwapo mtu atafanya jambo lisilo la haki basi serikali ya Kiislamu lazima iingilie kati kwa maslahi ya jamii nzima.

**Tatu**, wajibu mkubwa wa serikali ya Kiislamu ni kusimamia haki na kuzuia dhulma katika maisha ya jamii.

## Haki ya Serikali kuzuia Dhulma

**Kwanza**, serikali ya Kiislamu inao wajibu wa kuandaa mazingira mazuri ya kihuduma na kimawasiliano kuwawezesha raia kujiletea maendeleo na inao wajibu wa kuingilia kati ili kusimamia haki na kuzuia dhulma. Ni wakati gani kwa mfano ambapo serikali inaweza kuingilia kati. Allah ndiye aliyeziumba rasilimali zilizopo duniani na hivyo ni wajibu wa binadamu kuzitumia rasilimali hizo kwa manufaa ya watu na kwa ufanisi. Hivyo serikali yaweza kuingilia kati iwapo rasilimali hizo zitatumiwa kuwadhulumu watu au hazitatumika kwa ufanisi.

**Pili**, baadhi ya kazi ni haramu katika Uislamu kwa sababu zimefungamana na mambo ya haramu, kama vile kamari, umalaya, uchawi, ulevi n.k. Ni wajibu wa serikali kuona kuwa mambo hayo hayapewi nafasi katika jamii.

**Tatu**, ni wajibu wa serikali pia kutoa fursa sawa kwa watu wote ya kuendeleza na kuvikua vipaji vyao kwa kuwapa fursa sawa za elimu na mafunzo. Ni wajibu wa serikali kugharamia elimu kwa ajili ya manufaa ya watu wote. Elimu ni haki ya msingi kwa wanadamu wote.

**Nne**, ni wajibu pia wa serikali kuhakikisha kuwa hata katika zile kazi za halali kisheria zinafanywa kwa uadilifu pasi na dhulma yoyote. Yaani Serikali ihakikishe mathalani kuwa bidhaa zinazotolewa zimefikia ubora kwa wanaoizalisha, kuona kuwa uadilifu wa kitaalamu unadumishwa, kuona kuwa Wafanyakazi wanalipwa mishahara kwa haki.

Hata hivyo, Uislamu hauelemei upande mmoja tu wa kumtetea mfanyakazi peke yake wala kumtetea mwajiri peke yake. Wafanyakazi pia wakileta madai yasiyo ya haki ni juu ya serikali kuingilia kati.

**Tano**, ni wajibu wa serikali pia kuzuia mambo yanayoweza kudhuru watu, kwa mfano kama mtu akijenga kiwanda cha hatari katika makazi wanamoishi watu. Au hata mambo yanayoweza kuwatesa wanyama, kama kuwabebecha mizigo mizito sana hadi wanaanguka na kuvunjika miguu au kufa, au kuwafanyisha kazi kwa mateso makubwa na kutowapa chakula cha kutosha. Hali kadhalika serikali inaweza kwa mfano kuzuia magari au meli iliyopakia abiria au mizigo kuliko uwezo wake.

**Sita**, katika suala la usambazaji wa bidhaa, serikali inaweza kuingilia kati iwapo watu watahodhi vyakula na bidhaa nyingine muhimu kwa lengo la kupandisha bei.

**Saba**, ni wajibu wa serikali kujenga miundo mbinu (infrastructures) na kuidhibiti, kwa mfano kujenga barabara, madaraja, reli, kusambaza maji ya bomba, kujenga mitambo ya umeme, simu n.k.

Wakati wa Ukhalifa wake, Ali (r.a) alimwambia Nahri, ambaye alikuwa mkuu wa jimbo la Misri; "Usifanye ukusanyaji wa kodi ya ardhi kuwa ndiyo kazi yako kubwa; kazi yako kubwa ni kuindeleza ardhi hiyo."

## **Nafasi ya Serikali katika Ugawaji**

Katika suala la ugawaji, wajibu wa serikali ya Kiislamu upo katika maeneo makuu yafuatayo:

- (i) Kusimamia utoaji na ukusanyaji wa zaka. Serikali ndiyo yenye wajibu wa kuhakikisha kuwa kila anayepaswa kutoa Zaka anatoa na serikali inasimamia ukusanyaji wake.
- (ii) Kutoza na kukusanya kodi iwapo zaka haikutosha.
- (iii) Kutoza na kukusanya Jizya (aina ya kodi) kutoka kwa wasiokuwa Waislamu (dhimmi) wanaoishi katika dola ya Kiislamu.

(iv)Serikali ya Kiislamu pia inao wajibu wa kuchukua hatua za kupunguza tafauti kati ya masikini na matajiri, kwa kugawa Zakat na kutoa huduma muhimu bure kwa masikini.

## 5. Haki na Uhuru wa kuchuma katika Uislamu

Kwa kuwa kuchuma kwa njia za halali ni wajibu kwa kila mwenye uwezo wa kufanya kazi, hapana budi kila mtu kupewa uhuru kamili wa kutumia juhudi yake na vipawa vyake katika kuchuma kwa njia za halali. Katika Uislamu ni kosa kubwa kwa serikali au Dola kuweka vikwazo vya kuwazuia watu wasitumie vipaji vyao na uwezo wao wote katika kuchuma kwa njia za halali. Kinyume chake, serikali au dola ya Kiislamu ina wajibu wa kuondoa vikwazo vyote vinavyowazuia watu kutumia vipawa vyao vyote katika kuchuma na inawajibu pia wa kutoa motisha na vishawishi vya kuwavutia watu binafsi au watu waliojiunga katika vikundi wajijiingize katika sekta mbali mbali za uchumi kwa juhudi kubwa na maarifa.

Pamoja na uhuru kamili uliotolewa na Uislamu wa kuchuma kwa njia za halali kwa kadri ya uwezo wa kila mtu, pia unampa kila mtu haki ya kumiliki kila alichokichuma kwa njia za halali kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

وَلَا تَتَمَنَّوْا مَا فَضَّلَ اللَّهُ بِهِ بَعْضَكُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ ۗ لِلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِّمَّا  
 أَكْتَسَبُوا وَلِلنِّسَاءِ نَصِيبٌ مِّمَّا أَكْتَسَبْنَ ۗ وَسَأَلُوا اللَّهَ مِنْ فَضْلِهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ  
 كَانَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا ﴿٣٢﴾

“Wala msitamani vile ambavyo Mwenyezi Mungu amewafadhilisha baadhi yenu kuliko wengine wanaume wanayo sehemu (kamili) ya vile walivyovichuma, na wanawake nao wanayo sehemu (kamili) ya vile walivyovichuma. Na mwombeni Mwenyezi Mungu fadhila zake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu. (4:32)

## Biashara

Biashara imepewa hadhi ya juu katika Qur-an na katika Hadith za Mtume(s.a.w) kwa sababu ya umuhimu wake katika kuwaunganisha wanadamu na kuharakisha maendeleo yao.

Kihistoria, maendeleo ya ulimwengu yalianza pale biashara ilipopanuka na kuufanya utajiri wa ulimwengu ufike katika kila kona ya dunia.

Tunafahamu kilimo na viwanda ni shughuli muhimu sana kwa maisha ya binadamu, lakini mazao ya shambani na bidhaa za viwandani bila ya kusambazwa kwa watu wanaozihitaji, binadamu bado watabakia katika hali duni. Inatokea hivyo kwa sababu binadamu hakuumbwa kujitegemea kwa kila kitu. Vipaji, bahati na fursa havikugawanywa sawa sawa kwa kila mtu au kwa kila nchi ya ulimwengu katika nyanja zote za maisha.

Kiungo kikubwa cha ushirikiano huu ni biashara kati ya watu wa jamii moja au nchi moja na nyingine. Hivyo biashara ina umuhimu wake katika maisha ya binadamu na maendeleo yake. Uhalali na msisitizo wa biashara uko bayana katika Qur-an:

..... ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ قَالُوا إِنَّمَا الْبَيْعُ مِثْلُ الرِّبَا وَأَحَلَّ اللَّهُ الْبَيْعَ وَحَرَّمَ

الرِّبَا ..... ﴿٢٧٥﴾

“... Haya ni kwa sababu wanasema: “biashara ni kama Riba” hali Mwenyezi Mungu amehalalisha biashara na kuiharamisha riba...” (2:275)

Katika aya hii tunafahamishwa wazi kuwa Allah amehalalisha biashara na kuiharamisha riba. Hivyo biashara yoyote itakayoambatana na riba. Kuuza kwa mkopo wa riba itakuwa ni biashara haramu. Katika kuonesha ubora wa biashara Mtume wa Allah amesema:

“Mfanya biashara mkweli na mwaminifu (mcha Mungu) atakuwa pamoja na Mitume, Masadiq na Mashahidi”. (( Tirmidh, Ibn Majah)

Malipo haya kwa mfanyabiashara yatapatikana tu iwapo atakuwa mkweli na mwaminifu katika biashara yake. Akiwa kinyume cha hivyo atakuwa pamoja na maasi katika siku ya Kiyama kama tunavyofahamishwa katika Hadith nyingine inayosema:

“Ubaid bin Rafa’a kutoka kwa baba yake ameeleza kuwa Mtume(s.a.w) amesema: “Wafanyabiashara watakusanywa pamoja na wakosaji ila wenye kumuogopa Allah, wacha Mungu na wakweli.” (Ibn Majah na Tirmidh).

Kwa hiyo ili biashara iweze kuleta mafanikio kwa mfanyabiashara na kwa jamii kwa ujumla, hapana budi kufuata miiko na taratibu zilizowekwa na Uislamu.

**Kwanza**, pasiwe na udanganyifu wowote katika uuzaji na ununuzi. Kila mmoja kati ya muuzaji na mnunuzi anatakiwa awe mkweli na mwaminifu kwa mwenzake. Hebu tuzingatie Hadith ifuatayo:

Jabir ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: “Allah amrehemu yule ambaye ana mahusiano mema wakati akiuza, akinunua na wakati wa kutoa uamuzi.” (Bukhaary).



Jambo muhimu la kuangalia, katika biashara ni uaminifu katika upimaji kwa vipimo vya uzito, urefu, na ujazo. Wafanyibiashara walio wengi huanguka kwenye mtihani huu wa vipimo na huishia katika laana ya Allah(s.w). Qur-an imesisitiza mno kuchunga haki katika vipimo:

وَأَوْفُوا الْكَيْلَ إِذَا كُلْتُمْ وَزِنُوا بِالْقِسْطَاسِ الْمُسْتَقِيمِ ذَلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿١٦﴾

“Na timizeni kipimo mpimapo, na pimeni kwa mizani zilizo sawa. Hayo ni wema kwenu na bora mwishoni.” (17:35)

• وَأَوْفُوا الْكَيْلَ وَلَا تَكُونُوا مِنَ الْمُخْسِرِينَ ﴿١٧﴾ وَزِنُوا بِالْقِسْطَاسِ الْمُسْتَقِيمِ ﴿١٨﴾ وَلَا تَبْخُسُوا النَّاسَ أَشْيَاءَهُمْ وَلَا تَعْتُوا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿١٩﴾

“Kijazeni kipimo cha pishi sawa sawa wakati mnapopima; (msidhulumiane) wala msiwe miongoni mwa wapunguzao. Na pimeni kwa mizani iliyo sawa (pia). Wala msiwapunguzie watu vitu vyao, wala msitembee katika ardhi mkifisidi.” (26:181-183).

Pamoja na msisitizo huu Allah(s.w) anatumfahamisha katika Qur-an kuwa aliangamiza kaumu ya Nabii Shuayb (a.s) kwa sababu ya kukithiri kwao katika kuwapunja watu katika vipimo katika biashara. Maangamizi hayakuishia kwenye kaumu ya Shuayb (a.s) tu bali Allah(s.w) ameahidi maangamizi kwa kila mwenye kupunja katika vipimo kama inavyodhihirishwa katika aya zifuatazo:

وَيْلٌ لِّلْمُطَفِّفِينَ ﴿٢٠﴾ الَّذِينَ إِذَا اكْتَالُوا عَلَى النَّاسِ يَسْتَوْفُونَ ﴿٢١﴾ وَإِذَا كَالُوهُمْ أَوْ وَزَنُوهُمْ يُخْسِرُونَ ﴿٢٢﴾ أَلَا يَظُنُّ أُولَئِكَ أَنَّهُمْ مَبْعُوثُونَ ﴿٢٣﴾

“Maangamizi yatawathibitikia wapunjao wenziwao. Ambao wanapojipimia kwa watu hupokea (kipimo) kamili. Lakini wanapowapimia kwa kipimo cha vibaba au mizani (au vinginevyo), wao hupunguza. Je! Wao hawafikiri ya kwamba watafufuliwa? (83:1-4)

Waislamu hatuna budi kuwa macho sana katika vipimo vya uzito, ujazo na urefu tunavyotumia katika biashara zetu. Kutokana na msisitizo uliopo katika

Qur-an mtu hata ajiite Muislamu mwenye kusali swala zote, akatoa zakat na sadaqa, akafunga, na akahiji, ataangamia na kuishia Jahannam iwapo katika biashara yake atakuwa anawapimia watu kwa ujanja ujanja.

Ugongaji wa vipimo vya ujazo na kuuza bei ya kipimo kizima, utegesheaji wa mizani, ugongaji wa mizani ili ishuke kabla ya kipimo kukamilika, uchanganyaji wa bidhaa mbovu na nzuri na kuiuza kwa bei nzuri (n.k.) ni miongoni mwa udanganyifu katika biashara. Mfanyabiashara wa namna hii ndiye yule Mtume(s.a.w) aliyesema atafufuliwa pamoja na waovu watakaoingia motoni. Pia tumefahamishwa katika Hadithi kuwa:

*Wasikh bin Asqa'a ameeleza: Nimesikia Mtume wa Allah akisema: Anayeua bidhaa mbovu bila kuonesha ubovu wake ataendelea kuwa katika laana ya Allah na malaika wataendelea kumlaani." (Ibn Majah).*

**Pili**, katika biashara pasiwe na viapo kwani hii ni miongoni mwa kuuza kwa ujanja-ujanja. Bidhaa iliyoapiwa sana na mwenye kuuza, inaweza imhadae mnunuzi aidhanie kuwa ni nzuri zaidi kuliko hali halisi. Mnunuzi atakapogundua baadaye ataona kuwa amedanganywa kwa viapo. Hivyo viapo vingi kwenye biashara, kwa muuzaji au mnunuzi vimekatazwa kwa sababu vina hila ndani yake. Mtume(s.a.w) ameonya katika Hadith ifuatayo:

*Abu Qatada ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema, "Kuwa muangalifu na viapo vingi katika uuzaji, kwa sababu japo kuwa kunarahisisha uuzaji, kuna punguza baraka. (Muslim).*

Kuapa sana katika biashara kuna hadaa, kwa sababu wanunuzi wanapogundua kuwa wamedanganywa kwa viapo, na kumbe bidhaa hiyo haikuwa nzuri kiasi walichotarajia, hawatapendelea tena kununua kwa mfanya biashara huyo.

**Tatu**, katika biashara pawe na uhuru kamili kwa mnunuzi wa kuikataa au kuikubali bidhaa baada ya kuiangalia. Uhuru wa kuikataa bidhaa unaendelea kwa mnunuzi hata baada ya kununua, iwapo atagundua dosari yoyote katika bidhaa hiyo kabla ya kuanza kuitumia bidhaa hiyo. Vile vile muuzaji anayohaki ya kukataa au kukubali kuuza bidhaa yake kwa bei anayoridhika nayo kabla ya mkataba wa kununua hauja kamilika. Muuzaji hana uhuru wa kuitaka bidhaa irudishwe baada ya mkataba wa kuuza na kununua kukamilika labda kwa mapatano yaliyofanywa katika mkataba wa kuuziana. Kuhusu jambo hili la uhuru wa uamuzi wa muuzaji na mnunuzi katika kuuza na kununua bidhaa, tunafahamishwa katika Hadith ifuatayo kuwa:

*Ibn Umar ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Mnunuzi na muuzaji kila mmoja katika wao ana uhuru wa mapatano na mwenzake ili mradi tu hawajaachana ila kwa uhuru wa uamuzi wa ununuzi (anaweza akakataa bidhaa hata baada ya kuelewana)." (Bukhaary na Muslim).*

Katika maelezo ya Muslim – wakati mnunuzi na muuzaji wanauziana kila mmoja katika wao ana uhuru wa uamuzi kutokana na mauzo au manunuzi yake, ili mradi tu wawe hawajaachana au wameuziana kwa mapatano. Kama kuuziana kwao ni kwa mapatano basi kila mmoja atafungika (kulingana na mapatano hayo).

Biashara yoyote itakayoendeshwa kwa kumnyima uhuru muuzaji au mnunuzi ni biashara haramu ambayo haimnufaishi mnunuzi wala muuzaji. Kutokana na uzoefu wetu tunayaona haya katika mazingira yetu. Ni mara ngapi tumeona watu wakilazimishwa kununua bidhaa wasizozipenda wala kuzihitaji? Kwa mfano utaona mtu akilazimishwa kununua kilo ya unga wa muhogo usiofaa kula kabisa, ili apatiwe kilo ya sukari anayohitajia. Huu ni uuzaji wa hila na ni uuzaji wa haramu. Kuna mifano mingi kama hii, Uislamu umetoa uhuru kwa muuzaji na mnunuzi.

Kwa ujumla utaona biashara itakayoendeshwa kwa misingi ya Kiislamu iliyoenezwa hapa kwa ufupi, ndio pekee biashara halali na ndio pekee yenye kutumainiwa kuleta ushirikiano, umoja, ustawi na amani ya kweli ulimwenguni. Kisiasa na kiuchumi inafahamika wazi kuwa matatizo mengi yanayokabili ulimwengu katika nyakati zote za historia yanasababishwa na kukiuka misingi ya haki ya biashara na ya uchumi, kwa ujumla aliyoiweka Allah(s.w).

Kwa hiyo Waislamu hatuna budi kujua kuwa utatuzi wa matatizo yanayokabili ulimwengu ni kusimamisha misingi ya Uislamu katika nyanja zote za maisha, hasa katika nyanja za uongozi na uchumi ambazo ndizo roho ya jamii.

## **Biashara Haramu**

Biashara inaweza kuwa haramu kwa namna mbili: kwanza kwa kutofuata misingi ya halali iliyowekwa na Allah(s.w). Pili, kuna biashara ambayo moja kwa moja imeharamishwa hata kama misingi ya halali itafuatwa. Kwa maana nyingine kuna biashara ambazo zimeharamishwa katika nafsi yake yenyewe. Katika kipengele hiki tutaorodhesha biashara ambazo zimeharamishwa moja kwa moja katika nafsi yake na Hadithi mbali mbali za Mtume(s.a.w).

### ***(i) Muzabanah***

Ni kunufaika kibiashara kutokana na matatizo ya watu wengine. Ni haramu kufaidi shida ya mwengine katika biashara. Uislamu unataka mwenye shida asaidiwe na wala asikandamizwe kutokana na shida yake. Biashara ya Muzabanah imeharamishwa kwa muuzaji na mnunuzi. Uislamu unasisitiza kuwa kinachouzwa na kinachobadilishwa nacho ni lazima kifahamike kwa mnunuzi na muuzaji.

**(ii) Mu'awamah**

Huu ni uuzaji wa matunda, nafaka, na mazao mengine ya shambani kabla ya kukomaa kiasi cha kufaa kuliwa; na ni haramu kama inavyosisitizwa katika Hadithi zifuatazo:

*Abdullah bin Umar ameeleza kuwa Mtume(s.a.w) ameharamisha kuuza matunda shambani mpaka yaive. Ameharamisha kwa muuzaji na mnunuzi (wamekubaliana Bukhaary na Muslim). Na katika maelezo ya Muslim: (Mtume) aliharamisha kuuza tende mpaka ziive na nafaka mpaka ziwe nyeupe na zisiwe zenye kudhuriwa tena na madhara mbali mbali.*

*Jabir ameeleza kuwa Mtume wa Allah ameharamisha kuuza (kwa matunda yangali mtini) kwa kipindi cha miaka, na ameamrisha kungojea kwanza yawe tayari (kiasi cha kutoweza kudhuriwa na chochote). (Muslim).*

**(iii) Hablul-Habalah**

Kuuza kilichotumboni kabla hakijazaliwa. Kwa mfano kuuza mimba ya ng'ombe, mbuzi, kondoo, ngamia, n.k ni haramu. Tunafahamishwa katika Hadithi ifuatayo:

*Ibn Umar ameeleza kuwa Mtume Mtukufu ameharamisha mauzo ya Habalul-Habalah; na ni uuzaji waliokuwa wakiufanya watu majahili. Mtu alikuwa akinunua ngamia mpaka ngamia jike lishike mimba na mpaka hicho nacho katika tumbo la uzazi kiwe na mimba. (Bukhaary na Muslim).*

Jambo linalosisitizwa katika Hadithi hii ni kwamba imeharamishwa kuuza mimba kwani ni jambo ambalo halina uhakika kabisa. Ajuaye na mwenye uhakika wa kuzaliwa au kutozaliwa kilichomo tumboni ni Allah(s.w) peke yake. Kwa hiyo uuzaji wa mimba ni uuzaji wa pata-potea (uuzaji hewa).

**(iv) Uuzaji wa bidhaa kabla hazijamfikia mnunuzi ni haram,**

Ununuzi au uuzaji hauhusiki mpaka mnunuzi ashuhudie bidhaa anazouziwa. Hivyo ndivyo tunavyofahamishwa katika Hadithi ifuatayo:

*Ibn Abbas ameeleza: "Katika mauzo aliyoyaharamisha Mtume(s.a.w) ni mauzo ya chakula mpaka yawe mikononi mwa mnunuzi..." (Bukhaary na Muslim).*

Msisitizo wa Hadithi hii ni kwamba mtu asiuze kitu ambacho hajakishuhudia machoni mwake au machoni mwa mwakilishi wake.

**(v) Uuzaji wa bidhaa njiani kabla ya wauzaji kufikisha bidhaa sokoni.**

Wakati mwingine wafanya biashara hufanya ujanja kwa kuteka nyara bidhaa njiani kabla hazijaingia sokoni ili kuwaghilibu na kuwapumbaza wauzaji ambao hawajajua bei halisi ya bidhaa ile sokoni.

Ununuzi wa namna hii ni ulanguzi na umeharamishwa katika Uislamu kama inavyosisitizwa katika Hadithi zifuatazo:

*Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: “Usimfuata mfanya biashara wa nafaka mkakutana naye njiani kabla (ya kuingia sokoni). Na endapo atanunua kutoka kwake-atakapoingia sokoni na kujua hali halisi ya soko ana haki ya kukataa mauziano ya awali. (Muslim, Bukhaary).*

*Ibn Umar (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: “Usikutane (usiteke nyara) bidhaa njiani mpaka zitakapofikishwa sokoni.” (Bukhaary na Muslim)*

Kununua bidhaa iliyonunuliwa na mwingine kwa kulipa bei kubwa zaidi au kwa sababu nyinginezo ni haramu kama inavyobainishwa katika Hadithi zifuatazo:

*Ibn Umar (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: “Hapana mapatano ya atakayenunua kitu yatayofanyika baada ya mwenzake kununua na hapana atakayemchumbia ambaye ameshachumbiwa na mwenzake (ndugu yake) mpaka apate ruhusa kutoka kwake (huyo) aliyeanza na kupatana bei au aliyeanza kuchumbia.” (Muslim).*

Kinachosisitizwa katika Hadithi hii ni kwamba, Muislamu haruhusiwi kununua bidhaa iliyonunuliwa na mwingine. Mara nyingine kwa sababu ya husuda au uroho matajiri huweza kuwashawishi watu wenye uroho kama wao wakaamua kuvunja mkataba wa mauzo uliofanyika hapo awali ili apate bei kubwa kwa huyu mteja aliyejitokeza baada ya mauzo kwa yule mteja wa kwanza.

**(vi) Kuuza maji au majani ambayo mtu hakuyagharamikia chochote imekatazwa katika Hadithi zifuatazo:**

*Jabir amesimulia kuwa Mtume wa Allah amekataza (ameharamisha) kuuza maji ya asili. (Muslim).*

*Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Majani ya asili hayatauzwa ili kununua malisho yaliyomo. (Bukhaary na Muslim).*

Hadithi hizi zinatufundisha kuwa mali asili kama maji, majani, miti ya porini (n.k.) ni haki ya kila mwanadamu kwa hiyo hapana mwenye haki ya kuzuia mali ya asili na kuifanya yake na kuwauzia watu wengine. Bali kama mali asili imeshughulikiwa ndio ifae kutumika, itajuzu mwenye kuishughulikia awe na haki ya kudai arudishiwe gharama alizozitoa katika shughuli hiyo. Kama gharama za bomba, na mashine ya kusukumia maji na kadhalika.

**(vii) Lakini kuyauza maji ya chemchem ya asili au mto ni haramu.**

Uuzaji wa samaki aliyeko majini, uuzaji wa ndege anayeruka angani (ambaye hafugwi), uuzaji wa maziwa ambayo hayajakamuliwa na uuzaji wa manyoya ya

mnyama yangali mwilini mwake ni uuzaji haramu. Ni wazi kuwa mauzo yote haya yameharamishwa kwa sababu bidhaa hizo hazina uhakika wa kuzipata. Ili pawe na haki kati ya muuzaji na mnunuzi bidhaa hizo hazina budi kupatikana kwanza mkononi ndio ziuze.

***(viii) Uuzaji wa damu na uuzaji wa mtu (utumwa)***

Uuzaji wa damu na uuzaji wa uhuru wa mtu (utumwa) uuzaji wa nywele na maziwa ya binadamu ni biashara haramu. Vitu vyote hivi si haki ya mwanadamu na havipatikani kutokana na jasho lake. Hivyo hana haki ya kuviuza na wala hana hata uwezo wa kukadiria thamani yake halisi. Kama hatuwezi kukadiria thamani ya mvuto mmoja wa hewa au thamani ya tone moja la maji, tunaweza kukadiria thamani ya damu, achilia mbali thamani ya maisha yetu?

***(ix) Mauzo ya mbwa, nguruwe, pombe***

Mauzo ya mbwa, nguruwe, pombe, damu na mzoga ni biashara haramu. Pia ni haramu kuuza picha na sanamu kama tunavyofahamishwa katika Hadithi zifuatazo:

*Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume wa Allah ameharamisha kipato kilichotokana na kuuza damu, mbwa, na kipato cha Malaya. Na amelaani mwenye kupokea na mwenye kutoa riba, na mwenye kuchora mwili kwa chale na mwenye kuchorwa mwili kwa chale na mchoraji wa picha (za wanyama) na watu. (Bukhaary).*

*Jabir ameeleza kuwa amemsikia Mtume wa Allah akisema katika mwaka wa ushindi (wa kuiteka Makka) wakati alipokuwa Makka. Hakika Allah na Mtume wake wameharamisha mauzo ya pombe; mizoga, nguruwe na masanamu. (Bukhaary na Muslim).*

***(x) Ulanguzi (Kuhodhi bidhaa)***

Hili ni neno pana linalotumiwa kwa maana mbali mbali; lakini katika kipengele hiki tutalitumia neno hili kuwakilisha kitendo cha kuteka nyara bidhaa muhimu sokoni kwa kuinunua kwa wingi labda kwa bei ya juu kidogo kwa madhumuni ya kuilundika (kuihodhi) na kuifanya iwe adimu ili hapo baadaye itakapokosekana sokoni iuzwe kwa bei ya juu sana na kutoa faida kubwa sana.

Biashara ya namna hii ni biashara haram kama tunavyofahamishwa katika Hadithi kadhaa zifuatazo:

*Umar amesimulia kutoka kwa Mtume wa Allah aliyesema: “Mwenye kuleta nafaka (mjini) anazidishiwa riziki na mkusanyaji na mfichaji wa bidhaa hizo amelaaniwa.” (Ibn Majah, Dirimi).*

*Umar amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: “Anayelundika na kuzuia bidhaa za chakula kwa siku 4 kwa nia ya kupata bei kubwa zaidi, anajitenga na Allah na Allah anajitenga naye.” (Razin).*

Hadithi zote hizi zimedhihirisha ubaya wa kuzuia bidhaa, hasa bidhaa muhimu kama vile chakula, na kuzifanya ziwe adimu ili kuuza kwa bei kubwa itakayotoa faida kubwa sana. Biashara ya namna hii ni biashara haramu na laana ya Allah iko juu ya walanguzi hawa:

*Mu’az amesimulia: Nimemsikia Mtume wa Allah akisema: “Mbaya ni yule anayelundika bidhaa na kuifanya iwe adimu. Kama Allah akifanya bidhaa kuwa rahisi, yeye anachukua na kama Allah akifanya kuwa ghali, anafurahi. (Razin, Baihaqi).*

Hadithi hii inatueleza sura hasa ya mlanguzi. Ama mtu kuweka bidhaa alizozilima na alizotengeneza mwenyewe au kuuza bidhaa alizozinunua kutoka masafa ya mbali si haramu. Lililoharamishwa ni kule kununua bidhaa katika soko la kawaida na kuzificha ili baadaye aziuze kwa bei kubwa baada ya bidhaa hiyo kuwa adimu katika soko.

Pamoja na Uislamu kulaani ulanguzi, hauruhusu kumkangandamiza mfanyabiashara kwa kumuwekea bei ya bidhaa yake. Bei inatakiwa ijiweke yenyewe kulingana na hali halisi ya soko. Bidhaa zikiwa nyingi bei itakuwa chini na bidhaa zikiwa chache itakuwa juu. Tunajifunza kutokana na Hadithi ifuatayo:

*Anas amesimulia kuwa wakati mmoja katika wakati wa Mtume wa Allah bei ya vitu ilikuwa ghali. Wakamuomba Mtume: Ewe Mtume wa Allah panga bei kwa nafuu yetu. Mtume wa Allah akajibu: Hakika Allah ndiye anayemiliki bidhaa, anapunguza, anatoa kwa wingi, anatoa riziki, na ananipendelea sana nikutane na Bwana wangu katika hali ambayo hapana yeyote kati yenu atakayenifanya niwe na dhima juu ya damu (iliyomwagika kwa sababu yangu) au mali (aliyopunjwa kwa sababu yangu)! (Tirmidh, Abu Daud, Ibn Majah).*

Uislamu kama usivyoruhusu kukandamizwa na kudhulumiwa mnunuzi ndivyo hivyo hivyo usivyoruhusu kukandamizwa kwa mchuuzi au muuzaji. Mtume(s.a.w) akiwa kiongozi mkuu wa serikali ya Kiislamu, hakuthubutu kutumia madaraka hayo kuingilia haki za wafanyabiashara walizopewa na Allah(s.w). Jibu lake kwa namna nyingine lilikuwa “anayepanga bei ni Allah(s.w).

Kutokana na Hadithi hii hapana yeyote aliyojitokeza mwenye haki ya kukaa chini na kumpangia mfanyabiashara bei iliyo kinyume na ile iliyojitokeza yenyewe sokoni. Kinachotakiwa kifanywe na nguvu za dola ni kutokomeza njama zote za ulanguzi na vikwazo vyote vya uchumi. Kisha kuwaacha huru wafanyabiashara wauze bidhaa zao kwa bei halisi inayokubaliwa katika soko huru.

(xi) Kupunguza kipimo cha ujazo au kilo kwa kuharibu mizani au kugonga vipimo vya ujazo ni haramu. Allah(s.w) anasema :

وَيْلٌ لِّلْمُطَفِّفِينَ ﴿١٦﴾ الَّذِينَ إِذَا اكْتَالُوا عَلَى النَّاسِ يَسْتَوْفُونَ ﴿١٧﴾ وَإِذَا كَالُوهُمْ أَوْ وَزَنُوهُمْ يُخْسِرُونَ ﴿١٨﴾

Maangamizo yatawathubutikia wapunjao (wenzao). Ambao wanapojipimia kwa watu hupokea (kipimo) kamili, lakini wanapowapimia kwa (kipimo cha) vibaba au mizani (au vinginevyo), wao hupunguza. (83:1-3)

وَأَوْفُوا الْكَيْلَ إِذَا كِلْتُمْ وَزِنُوا بِالْقِسْطَاسِ الْمُسْتَقِيمِ ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿١٩﴾

Na timizeni kipimo mpimapo; na pimeni kwa mizani zilizo sawa. Hayo ni wema kwenu na bora mwishoni (kwake). (17:35).

### (xii) Kuficha ila (dosari)

Kuficha ila (dosari) ya bidhaa inayouzwa ni haramu. Katika Hadithi iliyosimuliwa na Bukhaary, Baihaq na Al-Hakim, Mtume(s.a.w) amesema: Muuzaji na mnunuzi kila mmoja lazima atimize makubaliano. Na muuzaji akitoa habari zote juu ya bidhaa anayoiuza pamoja na mfano, kama unauza maharage makavu mwambie mnunuzi mathalan, uzuri wa maharage haya ni kuwa hayajatoboka lakini yana ila moja ya kuchelewa sana kuiva. Mwache mnunuzi apime hiari ya kununua au kuwacha.

Kutokana na maelezo yote haya; juu ya vipengele mbali mbali vilivyo haramishwa katika biashara, tunaona kuwa biashara japo ni kazi halali yenye hadhi kubwa mbele ya Allah, haitamnufaisha mwanadamu iwapo mipaka ya Allah(s.w) haitachungwa wakati wa kufanya shughuli hiyo.

## Haki ya Kumiliki Mali

Kumiliki mali ni suala la kimaumbile na limeshikamana na silka ya kujihami (self presevation).Katika historia ya binadamu suala la kumiliki mali limekuwa likiandamana na itikadi au falsafa inayotawala mahali.

Kwa mfano katika baadhi ya jamii za kitwaghati umilikaji wa mali uko chini ya familia au huwa chini ya “watu wote” (mali ya umma) au huwa chini ya mtu au



watu binafsi. Katika Uislamu kila kitu kipo chini ya miliki ya Mwenyezi Mungu:

قُلِ اللَّهُمَّ مَلَكَ الْمَلِكِ تُؤْتِي الْمَلِكِ مَنْ تَشَاءُ وَتَنْزِعُ الْمَلِكِ مِمَّنْ تَشَاءُ  
وَتُعْزِزُ مَنْ تَشَاءُ وَتُذِلُّ مَنْ تَشَاءُ بِيَدِكَ الْخَيْرُ إِنَّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٣٦﴾

“Sema Ee Mola uliyemiliki Ufalme wote! Humpa ufalme umtakaye na humuondolea ufalme umtakaye na humtukuzi umtakaye na humdhalilisha umtakaye, kheri imo mikononi mwako. Bila shaka wewe ni Mwenye Uwezo juu ya kila kitu”. (3:26).

Hivyo ni dhahiri kuwa Mwenyezi Mungu ndiye mmilikaji wa hakika wa vitu vyote. Binadamu anamiliki mali kwa dhamana tu siyo kwa hakika na kwa sababu hiyo ataulizwa jinsi alivyotumia. Katika Qur-an Allah(s.w) ameruhusu watu binafsi au kwa vikundi kumiliki mali pale aliposema:

خُذْ مِنْ أَمْوَالِهِمْ صَدَقَةً تُطَهِّرُهُمْ وَتُزَكِّيهِمْ بِهَا وَصَلِّ عَلَيْهِمْ إِنَّ صَلَاتَكَ  
سَكَنٌ لَهُمْ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١٠٣﴾

“Chukua sadaka katika mali zao, uwasafishe kwa ajili ya hizo (sadaka zao) na kuwataja kwa vizuri (mbele yangu) na uwaombe dua. Hakika kuwaombea kwako kutawapa utulivu (watengenekewe); na Mwenyezi Mungu ndiye asikiaye na ajuaye.” (9:103)

Hivyo Uislamu unakubali na kuheshimu haki ya mtu au watu binafsi kumiliki mali.

## Mipaka ya Umilikaji Mali

- (i) Mali hiyo iwe imechumwa kwa njia ya halali. Uislamu unaitambua haki ya kumiliki mali na haki ya kuilinda mali hiyo, lakini mali yenyewe iwe ya halali.
- (ii) Mtu anaweza kuiuza au kuitumia mali yake apendavyo maadamu ana akili timamu. Iwapo hana akili timamu, itabidi apatikane mdhamini wa kuingalia mali hiyo kwa niaba na manufaa yake na manufaa ya jamii.
- (iii) Maadamu mtu anayo mali basi anao pia wajibu wa kutekeleza majukumu yanayohusiana na mali aliyu nayo.
- (iv) Uislamu unakataza ubakhili na israfu (ubadhirifu) katika matumizi. Mwenyezi Mungu anasema:

وَلَا تَجْعَلْ يَدَكَ مَغْلُولَةً إِلَىٰ عُنُقِكَ وَلَا تَبْسُطْهَا كُلَّ الْبَسِطِ فَتَقْعُدَ

مَلُومًا مَّحْسُورًا ﴿١٧﴾

*Wala usifanye mkono wako (kama) uliofungwa shingoni mwako, wala usikunjue ovyo ovyo, utakuwa ni mwenye kulaumiwa na kufilisika. (17:29).*

﴿ يَبْنَئِي ۚ آدَمَ خُذُوا زِينَتَكُمْ عِنْدَ كُلِّ مَسْجِدٍ وَكُلُوا وَاشْرَبُوا وَلَا

تُسْرِفُوا ۚ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِينَ ﴿٣١﴾

*Enyi wanadamu! Chukueni mapambo yenu wakati wa kila sala; na kuleni (vizuri) na kunyweni (vizuri). Lakini msipite kiasi tu. Hakika Yeye hawapendi wapitao kiasi. (7:31).*

## Ubadhilifu ni Kufanya Mojawapo ya Mambo Matatu

**Kwanza**, kununua kitu usichokihitaji. Au kununua kitu unachokihitaji lakini kwa kiasi kingi kuliko unavyoweza kutumia. Kwa mfano kutengeneza chapati tano ilihali uwezo wako ni wa kula chapati mbili tu, halafu zile tatu ukazitupa jalalani. **Pili** ni ubadhilifu kununua kitu chochote kile cha haramu, hata ikiwa kwa thamani ndogo namna gani. Kwa mfano hata kama masanduku laki moja ya bia yanauzwa kwa shilingi hamsini ukiitoa shilingi hamsini hiyo kununua pombe hiyo unaandikiwa madhambi ya ubadhilifu. **Tatu** kutoa sadaka kwa ajili ya kujionesha kwa watu, badala ya kuandikiwa thawabu unaandikiwa madhambi ya israfu.

(v) Uislamu unakataza rasilimali zilizo katika jamii kuachwa bila kutumiwa Mtume(s.a.w) amesema mtu akiendeleza ardhi ana haki ya kuimiliki. Lakini akiiwacha kwa miaka mitatu bila kuitumia mtu mwingine ana haki ya kuiendeleza na kuimiliki.

## 6. Mgawanyo wa Mali katika Uislamu

Uislamu unasisitiza kuwa zaidi ya kuchuma, kumiliki na kusambaza mali, mgawanyo pia uwe wa haki katika jamii ili kujenga udugu, amani na utulivu wa kweli. Na katika kuhakikisha hilo mfumo wa uchumi wa Kiislamu (Iqtisad) unatumia njia zifuatazo:

### 1. Zakat

(i) Kilugha, neno zakat lina maana mbili: (a) Utakaso na (b) Ustawi. Hivyo zaka ni lbada inayochangia sana katika kuleta uadilifu na ustawi wa jamii kiuchumi na hata kisiasa.

- (ii) Zakat katika Uislamu ni taasisi maalumu na imesisitizwa katika Qur-an. Aya zipatazo 80 zimeitaja Zakat pamoja na Swala Zakat ina upeo mpana sana na ina husisha vipengele vingi kama vile:
- (a) Kijamii – Zakat ni kama bima ya jamii inayowahakikishia wakazi hifadhi ya kiuchumi endapo watapata matatizo kama ya umasikini au maafa. Zaka pia huondosha chuki na migogoro ya kitabaka na kujenga hisia za kuwa wamoja.
- (b) Kisaikolojia, Zakat inawalea watu katika moyo wa kuhurumiana na kusaidiana. Inawapa wanyonge na masikini moyo wa kujiamini na kujiona sawa na wengine.
- (c) Kiuchumi – Zakat ni njia mojawapo ya kupambana na tatizo la umasikini. Tatizo hili linazikabili nchi zote na Uislamu unalenga katika kuondoa umasikini pasi na jitihada za watu binafsi. Uislamu haupigani usawa bandia na kuwa kipato cha kila mtu kiwe sawa na mwingine wala Uislamu hauinyamazii hali ya wengine watumie na kusaza wakati wengine wanaendelea kutaabika kwa kushindwa kujipatia mahitaji muhimu. Tofauti za kimapato, vipaji na uwezo zitakuwepo katika jamii, lakini pengo la tofauti hiyo lisiwe kubwa sana.
- (d) Kwa maumbile yake, Zakat huwahimiza watu kuweka vitega uchumi na kuzalisha mali na kupiga vita tabia ya kuhodhi mali. Hii ni kwa sababu Zakat hutozwa kwa kipato kilichokaa mwaka mzima bila kutumika. Kila mtu hanabudi kupata mahitaji ya msingi.

## 2. *Sadakat*

Hisia za kuhurumiana na moyo wa kusaidiana kama ndugu zinazomsukuma mtu kutoa Zakat kwa kutaraji kupata radhi za Allah ndizo hizo hizo zinazomsukuma mtu kutoa sadaka. Hivyo tofauti kati ya Zakat na sadaka haipo katika lengo la kutoa bali katika wajibu wa kutoa. Zakat ni wajibu kutoa na sadaka ni amali iliyokokotezwa sana japo haikuwekewa kiwango na muda wa kutoa. Hutolewa kulingana na haja. Misingi ya kutoa sadaka ni ile ile ya kuhurumiana na kusaidiana kama Allah alivyoagiza katika Qur'an:

..... وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَىٰ ۖ وَلَا تَعَاوَنُوا عَلَى الْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ ۗ..... ﴿٥٢﴾

.....Na saidianeni katika wema na ucha-Mungu, wala msisaidiane katika dhambi na uadui” (5:2).

مَثَلُ الَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ كَمَثَلِ حَبَّةٍ أَنْبَتَتْ سَبْعَ سَنَابِلٍ فِي  
كُلِّ سُنْبَلَةٍ مِائَةٌ حَبَّةٌ وَاللَّهُ يُضْعِفُ لِمَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٦١﴾

*Mfano wa wale wanaotoa mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje moja iliyotoa mashuke saba; ikawa katika kila shuke pana punje mia., Na Mwenyezi Mungu humzidishia amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni mwenye wasaa mkubwa na Mwenye kujua.” (2:261).*

Aidha, Mtume(s.a.w.) amesisitiza katika Hadithi nyingi sana umuhimu wa kutoa sadaka. Katika Hadithi iliyosimuliwa na Bukhaary, Muslim, Ahmad na At-Tirmidh, Mtume (s.a.w.) amesema mtu asiyewahurumia watu hatahurumiwa na Allah. Na katika Hadithi iliyosimuliwa na Attabarani na Baihaqi, Mtume (s.a.w.) amesema: Naapa kwa Allah si muumini yule anayelala akiwa kashiba na ilhali jirani yake kalala na njaa.

Na katika Hadithi iliyosimuliwa na Al-Hakim, Mtume (s.a.w.) amesema ikiwa wakazi wa eneo fulani (kama vile mtaa) wakiamka asubuhi na ilhali mmoja wao ana njaa basi Allah hujitenga nao.

## Matukio Maalum ya Kutolewa kwa Sadaka

Baada ya kumaliza mfungo wa Ramadhani kutoa Zakatul Fitr ni lazima. Zakatul Fitr kiwango chake ni kilo 2½ za chakula kilichozeleka katika mji huo kama vile mchele au ngano.

Na mtu hutoa kiasi hicho kwa ajili yake mwenyewe na hutoa tena kiasi hicho hicho kwa kila mtu anayemtegemea katika familia yake. Hivyo atamtoto pia mkewe, na wanawe wote na wazazi wake iwapo anakaa nao na hawana uwezo.

**Tukio la pili** ni siku ya kuvuna mazao shambani, Mwenyezi Mungu ameagiza siku hiyo mtu atoe baadhi ya mazao yake na awape masikini, jamaa na majirani zake aliposema katika Qur'an:

﴿ وَهُوَ الَّذِي أَنْشَأَ جَنَّاتٍ مَعْرُوشَاتٍ وَغَيْرِ مَعْرُوشَاتٍ وَالنَّخْلَ وَالزَّرْعَ  
مُخْتَلِفًا أَكْلُهُمُ وَالزَّيْتُونَ وَالرُّمَانَ مُتَشَابِهًا وَغَيْرَ مُتَشَابِهٍ كُلُوا  
مِنْ ثَمَرِهِ إِذَا أَثْمَرَ وَآتُوا حَقَّهُ يَوْمَ حَصَادِهِ وَلَا تُسْرِفُوا إِنَّهُ لَا

يُحِبُّ الْمُسْرِفِينَ ﴿٢٦١﴾

*Naye (Allah) ndiye aliyeumba miti inayoegemezwa (katika chanja) katika kuota kwake na isiyoegemezwa na (akaumba) mitende na mimea ya matunda mbali mbali, na (akaumba) mizaituni na mikomamanga inayofanana na isiyofanana. Kuleni matunda yake inapotoa matunda; na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake (kwa kuwapa masikini na jamaa na majirani na wengineo) Wala msitumie kwa fujo, hakika Yeye (Allah hawapendi watumiao kwa fujo.” (6:141).*

**Tukio la tatu** ni wakati wa ndoa, Kuoana ni jambo lililohimizwa sana katika Uislamu. Hivyo Uislamu unasisitiza kuwa watu wasaidiane sana katika jambo hili. Wanazuoni wengi wanasema kuwa iwapo mtu anao uwezo wa kuoa lakini hapa mwanzo anakabiliwa na matatizo ya kifedha Hazina ya serikali ya Kiislamu (*Baitul Maal*) itumike kumsaidia. Wakati wa Ukhalifa wa Umar vijana kama hao walikuwa wakisaidiwa. Katika kuonesha ubora wa ndoa Allah amesema:

وَأَنْكِحُوا الْأَيْمَىٰ مِنْكُمْ وَالصَّالِحِينَ مِنْ عِبَادِكُمْ وَإِمَائِكُمْ ۚ إِنَّ  
يَكُونُوا فُقَرَاءَ يُغْنِهِمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ ۗ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٣٢﴾

*Na waozeni wajane miongoni mwenu (waungwana) na walio wema katika watumwa wenu (wanaume) na wajakazi wenu, kama watakuwa mafakiri Allah atawatajirisha katika fadhila zake; na Allah ni Mwenye wasaa” (24:32).*

**Tukio la nne** ni iwapo mtu atapata wageni. Uislamu unamtaka mtu awakirimu wageni wake. Katika Hadithi iliyosimuliwa na Bukhaary na Muslim, Mtume (s.a.w.) amesema: Yule anayemwamini Allah na siku ya mwisho awe mkarimu kwa wageni wake. Kwa mchana mmoja na usiku afanye takrima maalum. Kwa siku tatu zinazofuata afanye takrima ya kawaida na zaidi ya hapo ni sadaka ya hiari.

**Tukio la tano** ni wakati wa kugawa urithi, iwapo watakuwepo watu mafakiri wakati huo wa kugawa basi wapewe chochote, kwani Allah anasema:

وَإِذَا حَضَرَ الْقِسْمَةَ أُولُو الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينُ فَأَرْزُقُوهُمْ  
مِنْهُ وَقُولُوا لَهُمْ قَوْلًا مَعْرُوفًا ﴿٨﴾

*“Na wakati wa kugawanya wakihudhuria jamaa na mayatima na masikini, wapeni kitu katika hayo (mali ya urithi) na waambieni kauli njema.” (4:8).*

**Tukio la sita** ni agizo la Allah la kusaidiana kwa hali mbali mbali hasa majirani.

**Tukio la saba** ni wakati wa uzazi. Kama ambavyo Uislamu unahimiza ndoa ndivyo pia unavyothamini malezi ya watoto. Kihistoria Uislamu ndio ulioanzisha utaratibu wa kutoa malipo fulani maalum kwa familia zenye watoto wachanga.

Hivi leo ziko baadhi ya serikali duniani ambazo hutoa msaada wa pesa kwa familia zenye watoto wachanga. Huko Canada kwa mfano upo utaratibu wa kutoa msaada wa pesa kwa kila mtoto aliyezaliwa na kama watoto wakifikia umri wa miaka 18 na bado wanasoma kiwango cha pesa wanachopewa huongezwa.

Utaratibu huu ulianza katika karne ya 7 wakati wa ukhalifa wa Umar. Umar alianzisha mfumo wa kutoa dirham 100 kwa kila mtoto aliyezaliwa na kiwango hicho kiliongezwa kadiri mtoto alivyokua. Hivyo mfumo wa kutoa ruzuku kwa familia ni moja ya sadaqa zitolewazo katika mfumo wa uchumi wa Kiislamu.

## **Sadaka wakati wa Dharura**

Katika Hadithi iliyosimuliwa na Bukhaary na Muslim, Mtume (s.a.w.) aliwasifu sana Al-Afariyyin (watu wa ukoo wa Abu Musa). Akasema watu hao walipokuwa vitani au safarini na chakula kikapungua basi walikikusanya pamoja chakula chote kilichosalia na kukigawa tena sawa sawa miongoni mwao.

Au nchi ikiingia njaa - ilitokea njaa kubwa kwa mfano wakati wa Ukhalifa wa Umar. Alichokifanya ni kutoa taarifa kwa viongozi wa majimbo mbalimbali na kuwataka walete chakula cha ziada. Na kilipokuja alikigawa bila ya kujali cheo, madaraka au ukoo wa mtu bali kwa kujali mahitaji tu. Kwa bahati njema njaa hiyo ilikwisha mapema. Lakini miongoni mwa maneno aliyoyasema Umar ni kuwa lau njaa hiyo isingekwisha mapema, basi angewakusanya watu wote wenye njaa na angewagawa kwa familia zenye chakula. Akasema hii ni kwa sababu watu hawatakufa wakila chakula hata kama hawatashiba.

### **3. Kodi (Jizya)**

Ni njia nyingine itumiwayo na Uislamu katika kuigawanya mali katika jamii. Tafauti na Zakat na Sadaqa ambazo hupasa kutolewa na Waislamu, Jizya hutolewa na wasiokuwa Waislamu (Dhimmi), wanaoishi chini ya dola ya Kiislamu, kwa ajili ya kupata hifadhi na huduma mbalimbali.

### **4. Mikopo**

Mikopo kama njia mojawapo ya kugawa mali kwa watu wote, Uislamu unaruhusu watu kukopeshana. Mtu anaweza kumkopesha mwingine fedha ama kwa kutumia (matumizi ya kawaida katika maisha) au kwa kumsaidia mtaji kufanya biashara.

## Njia za Uchumi Zilizoharamishwa

Vipengele vya biashara haramu vilivyoorodheshwa nyuma ni miongoni mwa hizo. Njia nyingine za uchumi zilizoharamishwa ni hizi zifuatazo:

### (i) Wizi

Wizi wa aina yoyote ni kitendo cha dhulma ni haramu katika Uislamu.

### (ii) Ulevi

Ulevi wa aina yoyote kwa kiwango chochote ni haramu. Uharamu wa ulevi hauishii kwa mnywaji tu; bali pia ni haramu kushiriki katika hatua yoyote ile ya utengenezaji, uuzaji na uandazi.

*Anas ameeleza kuwa Mtume (s.a.w.) amewalaani (watu) kumi kuhusiana na pombe-yule anayeikamua, yule aliyehusishwa katika kuikamua, yule anayeinywa, yule anayeibeba, yule anayepelekewa, yule anayeandaa, yule anayeiuza, yule anayepanga bei yake, yule anayeinunua na yule anayemunulia. (Tirmidh, Ibn Majah).*

Kutokana na Hadithi hii, inatuwia wazi kuwa aina yoyote ile ya utengenezaji, uuzaji na unywaji imeharamishwa. Pato lolote mtu atakalolipata kama malipo ya kushiriki katika hatua yoyote ya matayarisho na unywaji wa ulevi, litakuwa ni pato la haramu. Hebu tuangalie hali halisi. Je, hatuwaoni Waislamu wakishiriki kwa ukamilifu katika viwanda vya pombe kama mameneja, makarani, wakemia, madereva, n.k.? Je, hawa wataridhika kuendelea kujijiita Waislamu na ili hali kila saa wako katika laana ya Allah na Mtume wake na ibada zao zote hazikubaliwi maadam miili yao imerutubishwa na kipato cha haramu; kivazi chao ni haramu na kila walicho nacho katika mazingira yao kimepatikana kwa pato la haramu?

### (iii) Kamari

Kamari imeharamishwa pamoja na pombe kama ilivyo katika aya ya (5:90) na (2:219).

Pia Hadithi ifuatayo inatubainishia kuharamishwa kwa kamari:

*Abdullah bin Amr ameeleza kuwa Mtume wa Allah ameharamisha ulevi, michezo ya bahati nasibu, kamari ya karata, na gobairah (aina ya pombe) na anasema: "Kila ulevi ni haram". (Abu Daud).*

Hadithi hii inatubainishia kuwa aina zote za kamari-gudugudu, pata-potea, karata, bahati nasibu, nakadhalika, ni haramu na kwa hiyo pato lolote litakalo tokana na kamari ni pato haramu.

Ni muhimu kufahamu kuwa uharamu wa kamari hauishii kwa watu wawili au kikundi cha watu wachache bali hata kama kamari hiyo itachezwa kitaifa, itabakia kuwa haramu tu.

Kwa hiyo bahati nasibu ya taifa, Bima ya Kimataifa, na michezo yote ya kamari iliyotolewa kibali na taifa, yote ni haramu mbele ya Allah na yeyote atakayeshiriki kwa namna yoyote katika michezo hiyo ya kamari atakuwa ameshiriki katika haramu na kipato chochote atakachokipata kutokana na ushiriki wake huo kitakuwa ni kipato cha haramu. Katika aya tulizozirejea hapo juu (5:90 -91) kamari imeharamishwa kwa sababu kuu tatu:

**Kwanza**, ni uchafu, kamari imeitwa “**rijsi**”. Kamari imeitwa uchafu kwa sababu pesa anazozipata mtu kwa kamari ni za dhulma na haramu. Kufumba na kufumbua mtu amepata maelfu ya pesa bila jasho lolote. Hivyo ni dhulma na ni haramu.

**Pili**, kamari inajenga chuki na uadui. Hii ni kwa sababu yule aliyeliwa pesa zake kwa maelfu kwa njia hii ya dhulma huwa ana mfundo mkubwa moyoni na anamchukia sana yule aliyechukua pesa zake hata kama ajidai kuwa hajali, ukweli ni kuwa pesa zake zitamuuma sana. Na mara kadhaa wacheza kamari wameishia kupigana na hata kuuana.

(iv) Kipato chochote kinachotokana na utengenezaji wa sanamu na picha za watu na wanyama ni kipato haramu. Rejea katika Hadithi zilizotolewa chini ya “Biashara haramu”.

(v) Kipato chochote kutokana na umalaya, ngoma na muziki wa aina yoyote ni kipato haramu. Kama inavyobainika katika Hadithi ifuatayo:

*Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume wa Allah ameharamisha kipato kutokana na mauzo ya mbwa, na kipato kutokana na kuimba kwa wasichana (singing girls) (Sharhi Sunnat).*

(vi) Kipato chochote kutokana na utabiri, ramli, na upigaji bao ni kipato haramu, na yote hayo ni kazi ya shetani katika Qur'an Allah(s.w.) ametuasa:

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْحَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَزْلَمُ رِجْسٌ مِّنْ

عَمَلِ الشَّيْطَانِ فَأَجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٩٠﴾

*Enyi mlioamini! Bila shaka ulevi na kamari na kuabudiwa (kuombwa) asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na kutazamia kwa mishale ya kupigia ramli (na kwa vinginevyo); (yote haya) ni uchafu (na ni) katika kazi ya shetani. Basi jiepusheni navyo ili mpate kufaulu” (5:90)*

Kutokana na aya hii upigaji ramli na utazamiaji wa aina yoyote ni haramu na kipato chake kitakachopatikana na kazi hiyo ni haramu pia. Utabiri wa aina yoyote ni haramu, hali kadhalika kipato kinachotokana na kazi hiyo ya utabiri ni haramu. Abu Bakar aliwahi kujitapisha baada ya kugundua kuwa amelishwa



kutokana na malipo ya utabiri. Pia kipato kutokana na uchawi ni kipato haramu.

### **(vii) Hongo (Rushwa)**

Utoaji na upokeaji wa rushwa ni haramu na pato lolote lililotokana na rushwa ni pato haramu. Mtoaji na mpokeaji wa rushwa wote wamelaaniwa na Allah na Mtume wake kama tunavyofahamishwa katika Hadithi ifuatayo:

*Abdullah bin Amr ameeleza kuwa Mtume wa Allah amemlaani mpokeaji rushwa na mtoaji rushwa katika kutoa hukumu. (Abu Daud, Ibn Majah).*

Hongo au rushwa ni kiasi chochote anachopokea muhudumu (mfanyakazi) zaidi kuliko malipo yake ya haki katika kutoa huduma alizoajiriwa kwazo. Kwa maana nyingine, mtu akipokea malipo yoyote, hata yawe madogo kiasi gani ambayo ni ziada ya mshahara wake katika kufanya kazi ile ile na katika kiwango kile kile cha kazi aliyojiriwa kwayo, atakuwa amepokea rushwa. Turejee kwa makini Hadithi ifuatayo:

*Abu Humaid as-Sayyid ameeleza Mtume (s.a.w.) alimteua mtu katika kabila la Azd aliyekuwa akiitwa Ibnul Luthiyyah kama, mkusanyaji wa zakat, Aliporudi Madina, alisema: “Hii ni kwa ajili yenu na hivi ni vyangu (nilivyopokea) kama zawadi Kisha Mtume (s.a.w.) alitoa hutuba baada ya kumhimidi na kumtukua Allah akasema: Jambo lingine ni kwamba nimewateua baadhi ya watu miongoni mwenu kufanya (kuongoza) shughuli ambazo Allah amenipa mamlaka kwazo. Mmoja wao anakuja na kusema: ‘Hii ni kwa ajili yenu na hii ni zawadi niliyopewa. Kwa nini basi asibakie katika nyumba ya baba yake au katika nyumba ya mama yake na kuona kuwa angalipewa zawadi au hangalipewa? Kwa yule ambaye mikononi mwake uko uhai wangu hapana yoyote atakayechukua kitu chochote kutokana na zakati awe siku ya Kiyama hakutokea huku amebeba kitu hicho mabegani mwake. Kama alichukua punda atakuwa analia humo begani; kama alichukua mbuzi atakuwa analia (mee mee) humo begani. Kisha Mtume (s.a.w.) aliinua mikono yake mpaka tukaona weupe wa makwapani na akasema: “Ee Allah! Nimefikisha ujumbe)? Ee Allah! Nimefikisha ujumbe)?” (Bukhaary na Muslim).*

Hadithi hii inatuonesha kuwa mkusanyaji hakuwa na haki ya kuchukua zawadi katika kukusanya mali ambayo ndiyo kazi aliyoteuliwa kwayo. Swali aliloulizwa ni: Je, angalikuwa nyumbani au asingalitoka kukusanya zakat, angaliletewa zawadi hizo? Jibu ni kwamba asingeletewa zawadi hizo nyumbani kwake. Kwa hiyo zawadi zinazopatikana kwa namna hiyo si zawadi bali ni rushwa au hongo. Hadithi hii inatupa fundisho kubwa juu ya upokeaji zawadi makazini. Mara nyingi watu hupokea rushwa kwa jina la “zawadi”. Hadithi hii imetuwekea mpaka unaotenganisha rushwa na zawadi. Kitu cha ziada ya malipo ya kazi au ziada ya mshahara kitabainika kuwa zawadi au hongo (rushwa) kutokana na jibu la swali lifuatalo:

*Je, kama afisa (mfanyakazi) asingelikuwa katika nafasi ya kazi aliyonayo au katika cheo alichonacho, angalipata zawadi hiyo au asingelipata? Kama jibu ni “asingalipata” basi afisa huyo au mfanyakazi huyo akipokea zawadi ajuwe amepokea hongo. Kama afisa au mfanyakazi huyo amepewa zawadi isiyohusiana na nafasi yake ya kazi; na angaliweza kupata zawadi hiyo hata kama angalikuwa hana kazi au angalikuwa mahali pengine, basi zawadi hiyo itakuwa ni zawadi kweli na itakuwa halali kwake.*

Madhara ya rushwa yako wazi. **Kwanza**, mwenye kupokea rushwa (hongo) anapokea chumo la haramu ambalo litamfanya asikubaliwe ibada zake zote. **Pili**, Mla rushwa hawezi kumsaidia mtu asiyejiweza. Kila mara watawahudumia wale wenye kitu cha kutoa hongo kwa namna nyingine mnyonge asiye na uwezo wa kutoa chochote hatapata huduma muhimu za maisha anazostahiki kupata. **Tatu**, mla rushwa hawezi kuheshimiwa au kuaminiwa katika jamii kwa shughuli yoyote ile.

## Suala la Omba-Omba

Tukiliangalia suala la omba-omba kwa upana kidogo, ambalo hivi sasa linaongelewa katika vikao mbalimbali vya kitaifa na kimataifa, tutaona kuwa ni Uislamu pekee unaotoa namna bora ya kulishughulikia suala hili. Omba omba ni kitendo kibaya sana kikiwa kimefanywa na mtu binafsi au taifa na kinashusha hadhi ya mtu binafsi na hadhi ya taifa kwa ujumla. Hivyo Uislamu ambao ndio njia sahihi pekee ya maisha, hauwezi kamwe ukapalilia omba omba na wala Zaka na sadaka kazi yake si kupalilia omba-omba, bali kinyume chake zaka na sadaka ni miongoni mwa silaha zinazotumiwa kutokomezwa omba omba. Uislamu unawashutumu vikali omba omba kama tunavyojifunza katika Hadithi ifuatayo:

*Hubshi bin Junadah ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Kuomba-omba si halali kwa mwenye uwezo wala kwa mwenye uzima wa afya na mwenye nguvu (za kufanya kazi) ila kwa mwenye kupigwa ufakiri na mwenye deni kubwa (asiloweza kulilipa). Na yule anayeomba watu ili ajiongezee mali yake atakuwa na mkwaruzo usoni mwake katika siku ya Kiyama na atayala kwa ulafi mkubwa mawe ya moto kutoka motoni. Kwa hiyo anayetaka, mwache aombe kidogo, na mwache aombe kingi. (Tirmidh)*

Wanaoruhusiwa kuomba kwa mujibu wa Hadith ni:

- (i) Mtu aliyesimama kumdamini mtu mwingine ili kuleta suluhu kati ya wgomvi wawili. huyu anaruhusiwa kuomba hata akiwa tajiri. Kwa mnasaba huu, waumini wa misikitini, madarasa, na shughuli mbali mbali za Kiislamu wanaruhusiwa kuomba michango ya Waislamu ili kufanikisha shughuli hizo.
- (ii) Mtu aliyepata ajali na kuharibikiwa kabisa na vitu vyake vyote kama vile ajali ya moto, mafuriko, nakadhalika.

- (iii) Mtu ambaye amepigwa na ufakiri na amekosa kabisa mahitaji muhimu ya maisha kama vile chakula, malazi na makazi, lakini mtu akiwa na angalau chakula cha siku moja na malazi mkononi mwake haruhusiwi kuomba kama tunavyofahamishwa katika Hadithi zifuatazo:

*Abdullah bin Mas'ud ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Anayeomba omba watu na ilhali ana mahitaji muhimu ya maisha atakuja siku ya Kiyama na mikwaruzo, vidonda au majeraha usoni mwake. Iliulizwa: Ee Mtume wa Allah! Ni kiasi gani kinachomtosha mtu? Akajibu: Dirham 50 au thamani yake. (Abu Daud, Tirmidh, Nisai, Ibn Majah).*

*Sahl bin Haohaliyya ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Yeyote yule anayeomba na ilihali anajitosheliza kwa mahitaji muhimu, anaomba moto (Jahannam). Nufaili ambaye ni miongoni mwa wasimulizi wa Hadithi hii katika sehemu nyingine aliuliza: Ni yupi mwenye uwezo ambaye kuomba ni haramu? Alijibu (Mtume s.a.w.): Yule mwenye uwezo wa kupata chakula cha asubuhi na usiku. Mahali pengine amesema: Yule mwenye chakula cha siku moja (usiku na mchana) (Abu Daud).*

Hivyo ikibidi mtu aombe, basi aombe kwa sababu hizo tatu zilizotajwa katika Hadithi hii. Kuomba omba bila ya sababu za msingi kumeharamishwa kwa sababu kuu tatu zifuatazo:

- (i) Kuomba omba kunamfanya mtu apoteze moyoni mwake ile hali ya kumtegemea Allah (s.w.) na atajenga moyoni mwake hali ya kulalamika juu ya neema za Allah zilizomzunguka kila mahali. Kwa msingi huu hatima ya kuomba omba ni kumfanya mja awategemee wengine kwa mahitajio yake badala ya kumtegemea Allah (s.w.) na kumfanya ashindwe kushukuru neema za Allah (s.w.).
- (ii) Kuomba omba humfanya mtu awe mnyonge na ajidhalilishe kwa wengine ambapo Muislamu anatakiwa ajidhalilishe kwa Allah (s.w.) peke yake.
- (iii) Vile vile kuomba omba kumekatazwa kwa sababu kunamuweka yule anayeombwa katika hali ngumu. Wakati mwingine anayeombwa hali yake si nzuri vile vile lakini kwa kuombwa hulazimika kutoa jambo ambalo linaweza kumuathiri yeye na wale anaowaangalia.

Uislamu haukuishia kwenye kukemea tu tabia ya omba omba bali umetoa njia za kutatua tatizo hili kama ifuatavyo:

- (i) Kuwasaidia wale wote wenye matatizo na dhiki mbali mbali kwa kuwapa Sadaqa na zakati kabla hawajaomba.
- (ii) Njia ya pili, ya kukomesha kuomba omba ni kujitegemea kwa kufanya kazi kwa kutumia juhudi na maarifa.

## 7. Mfumo wa Benki

Mabenki ni taasisi za fedha ambazo ni muhimu sana katika uchumi. Benki husaidia uchumi kwa kutoa huduma kuu zifuatazo:

**Kwanza**, Benki hutoa huduma ya kuhifadhi akiba za watu na kuhifadhi mali zenye thamani kubwa kama vile dhahabu, na mfano wake.

**Pili**, kutokana na akiba inazozikusanya, benki hujikuta kila wakati ina fedha nyingi zisizo na shughuli yoyote. Benki hukopesha fedha hizi kwa watu wanaozihitajia ili ziwe mtaji wa kuendeleza biashara, viwanda, kilimo na sekta nyingine mbali mbali za uchumi na utoaji huduma.

**Tatu**, benki hutoa huduma ya kurahisisha malipo kwa njia ya hundi (*cheque*) kuwalipa Wafanyakazi kupitia benki zao au kwa hundi, huwaepusha walipaji na hatari ya kuibiwa.

**Nne**, pia benki hutoa huduma ya kutoa malipo ya mbali popote pale penye matawi yake nchini au ulimwenguni. Huduma hii ni muhimu sana kwani huwapunguzia watu mzigo wa kusafiri na fedha nyingi mkononi.

Badala yake benki huidhinisha malipo kwa simu au kwa njia yoyote ya mawasiliano ya haraka katika tawi la Benki hiyo popote lilipo nchini au ulimwenguni kupitia kwenye *Account* ya huyo anayestahiki kulipwa.

Huduma hizi muhimu na nyinginezo nyingi ambazo hatukuzitaja hapa zinatudhirishia umuhimu wa kuwepo taasisi hii ya fedha katika jamii.

Hivyo ni dhahiri kwamba Uislamu ukiwa ni mfumo kamili wa maisha unaojitegemea kwa kila kitu, hautarajiwi ukapinga au ukaharamisha kuwepo kwa mabenki katika jamii. Bali Uislamu unaharamisha mabenki yanayoendeshwa kwa kipato cha riba.

## Mabenki ya Riba

Mabenki ya kitwaghuti (yasiyokuwa ya Kiislamu) sehemu kubwa ya kipato chake hutokana na riba.

Mabenki ya Riba hukopesha watu wenye miradi mbali mbali ya uchumi na kuwatoza riba kubwa katika mfumo wa malimbikizo (*compound interest*). Sehemu ndogo ya riba inayokusanywa na Benki za Riba, hutumiwa katika kuwalipa wateja walioweka akiba zao ambao ndio hasa matajiri walioifanya Benki iwepo.

Ni kutokana na unyonyaji wa namna hii utakuta, wakati wakulima na Wafanyakazi wa ngazi za chini ambao ndio wanaovuja jasho ili kuchangia riba,

hawajimudu katika kujipatia chakula, mavazi, na makazi bora, wenye mabenki wanagawa “*bonus*” kwa wafanya kazi wao na wao wenyewe wanaponda starehe na anasa zilizopindukia kutokana na riba ambayo hawakuitoleo jasho lolote.

## 8. Tatizo la Riba

Riba ni kupata chochote kile cha ziada kutoka katika mkopo au mtaji bila kushiriki katika faida au hasara. Mwenyezi Mungu anatufahamisha katika Qur’an:

الَّذِينَ يَأْكُلُونَ الرِّبَا لَا يَقُومُونَ إِلَّا كَمَا يَقُومُ الَّذِي يَتَخَبَّطُهُ  
الشَّيْطَانُ مِنَ الْمَسِّ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَالُوا إِنَّمَا الْبَيْعُ مِثْلُ الرِّبَا وَأَحَلَّ  
اللَّهُ الْبَيْعَ وَحَرَّمَ الرِّبَا.....

*Wale wanaokula riba hawasimami ila kama anavyosimama yule ambaye shetani kamzuga kwa kumsawaa; haya ni kwa sababu wamesema, Biashara ni kama riba, hali Mwenyezi Mungu amehalalisha biashara na kuiharamisha riba.....(2:275)*

يَمَحَقُ اللَّهُ الرِّبَا وَيُرِي الصَّدَقَتِ.....

*Mwenyezi Mungu huyafutia (baraka mali ya) riba; na kuyatia baraka (mali iliyotolewa) sadaka..... (2:276).*

## Madhara ya Riba katika Jamii

(i) Riba inachafua nafsi ya Tajiri na uchumi wake. Tajiri ambaye hayuko tayari kukukopesha mali yake pasi na riba, kamwe hawezi kutoa mali yake bure kuwasaidia wanyonge na wenye dhiki. Tajiri asiye tayari kutoa mali yake kuwasaidia wenziwe wenye dhiki na shida katika jamii huwa mchoyo, bahili, mpupiaji mali, asiyetosheka na utajiri alionao, mfujaji, muonevu na dhalimu. Tajiri mwenye moyo wa namna hii hata kama atajiita Muislamu hawezi kamwe kuchunga mipaka ya halali na haramu katika kuchuma!

(ii) Riba inamkandamiza Mnyonge mwenye dhiki. Wanyonge na wenye dhiki katika jamii inayoendesha uchumi wake katika misingi ya riba, hawapati msaada wowote wa bure kutoka kwa matajiri kwa kiasi ambacho wengi wa wale wasiojiweza kabisa kujitosheleza kwa mahitaji muhimu ya maisha yao kwa namna duni sana - wengi hujipatia chakula chao kutoka katika mapipa ya taka (watoto wa mtaani), wengi hujisitiri kwa masalio yaliyookotezwa hapa na pale na wengi makazi yao ni stesheni na sokoni. Hawa, kisaikolojia, hujiona ni watu

duni wasio na maana yoyote katika jamii na huwaona matajiri na watu wenye uwezo kuwa ndio wenye maana. Na hapa ndipo inapojengeka chuki baina ya wasionacho kuwachukia walio nacho.

(iii) Riba inaharibu uchumi wa jamii na maendeleo yake. Riba na msingi wake wa unyonyaji imma ikitozwa na tajiri mmoja au kikundi cha matajiri, imefanywa msingi wa uchumi wa taifa au wa kimataifa. Kwa bahati mbaya kutokana na mazoea tuliyonayo juu ya vyombo vya uchumi vya kitaifa na kimataifa vinavyoendeshwa katika misingi ya Riba kama vile mabenki ya taifa na shirika la Bima la Kimataifa, baadhi ya watu wamediriki kuhlalisha Riba ya mabenki na Bima. Kuhlalisha huku kwa riba ya mabenki na Bima aidha kumetokana na uzoefu wa uchumi haramu katika jamii zetu au umetokana na kushindwa kuona ubaya wa riba kitaifa au kimataifa.

Waislamu hatuna budi kukumbuka kuwa alichokiharamisha Allah(s.w) kinakuwa ni haramu katika wingi wake na katika uchache wake. Tukichukua mfano wa pombe Mtume(s.a.w.) amesema:

*Kinacholeweshwa kikiwa kingi ni haramu pia hata kikiwa kichache.*

*(Tirmidh, Abu Daud, Ibn Majah).*

Kwa hiyo kilicho haramishwa kwa mtu binafsi, pia ni haramu kwa taifa na ni haramu kwa mataifa yote ulimwenguni. Kwa upande mwingine jambo la haramu litakapotendwa kitaifa litakuwa na athari mbaya zaidi kwa jamii kuliko likitendwa katika kiwango cha mtu binafsi, hali kadhalika jambo baya likitendwa kimataifa huwa na athari kubwa na mbaya zaidi kwa jamii ya mwanadamu kuliko likitendwa katika kiwango cha kitaifa.

(iv) Riba ni mali ya dhulma inayonyakuliwa na matajiri kutoka kwa wanyonge kwa njia moja au nyingine kiuchumi, pia riba inaukandamiza na kuudidimiza uchumi wa kitaifa au kimataifa. Mali ya riba kwa kuwa ni mali inayopatikana bila jasho na bila hata ya kushiriki katika mashaka ya uchumi, huwafanya matajiri na wenye uwezo wa kuendesha miradi mbali mbali ya kiuchumi wakae tu bila kazi wakingojea fedha zao zizae katika mabenki ambazo wana kila uhakika wa kuzipata hata itokee gharka ya namna gani. Kwa hiyo kutokana na riba, jamii huwakosa watu wenye uwezo mkubwa wa kuzalisha mali ambao wangaliweza kuendesha miradi mbali mbali ya kiuchumi ambayo ingaliinua uchumi wa taifa na wa kimataifa kwa ujumla.

Wataalam wa uchumi wanakiri kuwa riba inaporomoshwa uchumi. Wamegundua kuwa kadiri kiwango cha riba kinavyokuwa kikubwa ndivyo uchumi unavyozidi kushuka kwa sababu matajiri huona kuwa wanapata faida kubwa zaidi na kwa njia nyepesi isiyotoa jasho lolote wakiweka fedha zao benki kuliko kuziingiza katika miradi ya kiuchumi. Hivyo utaona kuwa riba hupunguza uzalishaji na huongeza gharama za uzalishaji.

## Uharamu wa Riba katika Uislamu

**Kwanza**, Uislamu umeharamisha riba kwa sababu ni dhulma (unyonyaji). Ukichukua mkopo wa riba uliochukuliwa kwa madhumuni ya kukidhi haja ya matumizi ya lazima ya nyumbani, utozaji wa riba unakiuka lengo la Allah la kuumba (kuleta) mali kwa wanadamu. Utaratibu aliouweka Allah ni kwamba kwa kuwa mali ameileta kwa wanadamu wote:

هو الَّذِي خَلَقَ لَكُمْ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا..... ﴿٢٩﴾

*“Ye (Allah) Ndiye aliyekuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi...” (2:29).*

Ni lazima matajiri (wenye mali) wawapatie wanyonge na wenye dhiki mahitaji yao muhimu ya maisha.

**Pili**, riba imeharamishwa katika Uislamu kwa sababu inahamisha mali kutoka kwa masikini au wanyonge na kuipeleka kwa tajiri ambayo huzidi kuondoa usawa katika mgawanyo wa mali. Hii ni kinyume na mahitaji ya jamii. Uislamu unataka kila mtu apate mahitaji muhimu ya maisha. Hivyo wale walio na ziada ya mahitaji muhimu ya maisha wanatakiwa wawape wasionacho kabisa au wale waliopungukiwa kwa upendo na udugu. Riba inakanusha kabisa msimamo huu.

**Tatu**, riba imeharamishwa katika Uislamu kwa sababu hufanya kundi la watu katika jamii liishi kivivu bila ya kufanya shughuli yoyote ya uzalishaji, likitegemea kuishi kwa riba kutokana na mali zao walizozikusanya katika mabenki, bima, na vyombo vingine vya riba. Jamii inakosa mchango wa watu hawa katika uzalishaji na si hivyo tu, bali watu hawa wanakuwa mzigo na bughudha katika jamii. Ufasiki (uharibifu) wa aina zote katika ardhi hufanywa na kundi hili.

## Ufumbuzi wa Tatizo la Riba

Riba imeenea na kuzoeleka duniani kwa kiasi ambacho watu wengi wanadhani kuwa bila riba hakuna shughuli yoyote ya uchumi inayowezekana. Riba imechukuliwa kuwa kama motisha (faida) kwa mwenye kuruhusu fedha zake zitumiwe na mtu mwingine. Hivyo mikopo kutoka kwa watu, makampuni, mabenki, mashirika ya bima n.k. haipatikani bila riba. Hivi sasa mikopo karibu yote duniani haitolewi bila riba. Mikopo hii kwa kawaida imegawanywa katika makundi mawili:

- (a) Mikopo ya muda mfupi
- (b) Mikopo ya muda mrefu

Tatizo hasa la riba linaonekana katika aina ya pili ya mikopo (yaani mikopo ya muda mrefu) Hii ni kwa sababu kiasi cha riba huongezeka mwaka hadi

mwaka pengine kuzidi hata fedha zilizokopeshwa mwanzoni. Aidha katika mikopo hii, baya zaidi ni kuingizwa kwa rahani na hatari iliyopo ya mkopeshwaji kunyang'anywa mali aliyoweka rahani pindi atakaposhindwa kulipa deni kwa muda uliopangwa. Uislamu ukifuatwa vilivyo, tatizo hili haliwezi kujitokeza kwani mwenye fedha analazimishwa kufanya moja kati ya yafuatayo kwa mwenye kuhitaji fedha hizo:

- (a) Kumkopesha bila riba kwa muda watakaokubaliana. (Ama kwa kuweka au kutoweka rahani mali yake).
- (b) Kushirikiana katika mtaji na kugawana gharama za uendeshaji, faida na hasara.

### (a) Kukopesha bila riba

Uislamu ni mfumo kamili wa maisha alioufuma Allah (s.w.) na ni muhali kwa Allah (s.w.) kuwalazimisha wanadamu kufanya jambo wasiloliweza. Amekataza riba na kuruhusu biashara kwa sababu anafahamu kuwa riba inaweza kuepukika na biashara kufuatwa. Aidha uislamu unawaruhusu watu kukopeshana. Mtu anaweza kumkopesha mwingine fedha ama kwa kutumia (matumizi ya kawaida katika maisha), au kwa kumsaidia mtaji kufanyia biashara. Kwa hali yoyote itakavyokuwa mwenye kukopesha (mtoa fedha) analazimika kudai kiasi kile kile alichotoa kwa muda waliokubaliana bila ya kudai nyongeza yoyote. Sheria iliyopo katika Uislamu katika kukopeshana ni deni hilo kuandikwa (hata kama ni dogo) mbele ya mashahidi waadilifu. Allah (s.w.) hata hivyo ametoa ruhusa ya kukopeshana bila mwandishi kwa njia ya kuweka vitu rahani. Anayathibitisha haya Mwenyezi Mungu pale anaposema:

..... \* وَلَمْ تَجِدُوا كَاتِبًا فَرِهْنَ مَقْبُوضَةً فَإِنْ مِنْ بَعْضِكُمْ بَعْضًا

فَلْيُؤَدِّ الَّذِينَ الَّذِينَ أَوْتِنَ أَمْنَتَهُمْ وَلِيَتَّقِ اللَّهَ رَبَّهُمْ وَلَا تَكْتُمُوا الشَّهَادَةَ وَمَنْ

يَكْتُمْهَا فَإِنَّهُ آثِمٌ قَلْبُهُ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ ﴿٢٨٢﴾

“.....Na kama hamkupata mwandishi basi (mdai) apewe (astakabadhishwe) (kitu kiwe) rahani mikononi mwake. Na kama mmoja wenu amewekewa amana na mwenzake basi aliyeaminiwa airudishe amana ya mwenzake, na amche Mwenyezi Mungu Mola wake. Wala msifiche ushahidi (japo juu ya nafsi zenu) Na atakayeficha basi hakika moyo wake ni wenye kuingia dhambini. Na Mwenyezi Mungu huyajua mnayoyatenda.” (2:282).



**(b) Ushirika katika biashara**

Uislamu unaruhusu watu kufanya biashara kwa shirika maadamu wanachunga sheria zilizowekwa (za Uislamu). Ushirikiano katika biashara unaweza kuwa wa watu wawili au zaidi. Mara nyingi wanaoshirikiana huchangia katika mtaji wa biashara yao. Pindi watu wakikubaliana kufanya biashara kwa shirika Uislamu unawalazimisha kushirikiana vile vile katika gharama, faida au hasara itakayopatikana. Hii hutegemea kiasi gani kila mshirika amechangia katika biashara hiyo. Ushirikiano mwingine wowote usiokuwa katika mtaji utategemea makubaliano ya washirika. Hebu tutazame ni kwa jinsi gani ushirika katika mtaji wa biashara unavyoweza kutumika badala ya mikopo ya rahani yenye riba.

- (i) Mikopo inayopatikana kwa rahani (Mortgages). Kupata mkopo kwa kitu rahani si haramu katika Uislamu kama ilivyokwishabainishwa katika Qur'an. Hata Mtume Muhammad(s.a.w.) aliwahi kufanya hivyo kama tunavyofahamishwa katika Hadithi ifuatayo:

*Bi Aisha (r.a) amesimulia kuwa: Mtume (s.a.w.) alinunua vyakula kwa mkopo kwa muda maalum na aliweka rahani (armour) zake kwa ajili hiyo (Bukhaary).*

Wanyama wafugwao vile vile wanaweza kuwekwa rahani kwa ajili ya mkopo. Wanyama hawa wanaweza wakatumika hata kama bado wapo rahani. Hadithi ifuatayo inatuthibitishia hayo:

*Abu Hurairah(r.a) amesimulia: Mtume wa Allah amesema: "Mnyama aliyewekwa rahani anaweza kutumika kuendeshwa maadamu analishwa na maziwa ya mnyama atoaye maziwa yanaweza yakanyewa kulingana na kiasi mtu anagharimika juu yake. Yule anayemwendesha mnyama au kunywa maziwa yake hana budi kugharimia mahitaji ya mnyama huyo". (Bukhaary).*

Kinyume na utaratibu huo hivi sasa rahani hutumika katika kupata mikopo ya muda mrefu. Mikopo hii huweza kutolewa na makampuni ya bima au makampuni ya akiba. Kitu kinachowekwa rahani huhesabiwa kama dhamana ya mkopo uliotolewa. Kwa kawaida kitu kinachowekwa rahani ni kile ambacho kinaeleweka kuwa kina uwezo wa kuzalisha mathalani nyumba au mashine. Mkopo hulipwa na riba. Kama aliyekopeshwa atashindwa kutoa riba au malipo ya fedha za mkopo basi mkopeshaji huhesabiwa kuwa ana haki ya kuchukuwa mali ya dhulma iliyo bayana kwa aliyekopeshwa.

**(c) Ushirika katika mtaji badala ya mikopo ya rahani yenye riba**

Mtu anaweza kupata fedha kwa njia hii bila kutoa riba. Njia hii inawezekana tu kwa kuwafanya watu wengine wawe wanashirika katika mali/kitu ambacho kingewekwa rahani kwa kuchangia katika thamani ya kitu hicho kwa njia ya kununua hisa (*shared equity*). Watu hawa wataridhia iwapo watafahamu hisa walizonazo katika mali/kitu hicho. Iwapo kwa mfano kitu hicho ni nyumba kodi

itakayopatikana ni lazima igawanywe kwa wenye hisa wote (baada ya kutoa gharama za uendeshaji). Mwenye nyumba au mwenye nyumba mtarajiwa (*the owner to be*) atakubaliana na washiriki hao kununua hisa zao hatua kwa hatua mpaka hisa zote zitakapokuwa zake (yani nyumba itakapokuwa mali yake). Njia hii hutekelezwa kwa kufuata hatua zifuatazo:

(i) Makisio ya thamani ya kitu na idadi ya hisa. Kitu ambacho kilifikiriwa kuwekwa rahani ili kupata mikopo hufanyiwa utafiti wa bei ambayo ingeweza kuuzwa. Hii huchukuliwa kama thamani ya kuridhisha ya kitu hicho. Ni thamani hii ndiyo itakayogawanywa kwa watakaokuwa na hisa (akiwemo atakayekuwa mwenye nyumba) Thamani ya kila hisa huamuliwa na huyo mwenye kutafuta fedha kwa wengine.

Thamani ya kitu na thamani ya kila hisa ndivyo vitakavyoonesha idadi ya hisa. Iwapo thamani ya nyumba, mathalani ni shilingi 2,000,000 na thamani ya hisa moja ni shilingi 100,000 idadi ya hisa itakuwa.

(ii) Kutafuta mtaji wa mwanzo wa atakayekuwa mwenye mali. Atakayekuwa mwenye mali lazima afahamu kiasi cha mtaji au hisa atakazokuwa nazo mwanzoni kabla ya kutoza hisa nyingine kwa wengine.

(iii) Kufahamu idadi ya hisa za washirika wengine. Idadi ya hisa za washirika wengine katika mali inapatikana kwa kugawa thamani ya hisa zote kwa thamani ya hisa moja.

(iv) Kufahamu mapato (kabla ya kutoa gharama) na mapato halisi (baada ya kutoa gharama za uendeshaji). wa mali. Mapato ya mali ambayo ilikusudiwa kuwekwa rahani kwa ajili ya kupata mkopo lazima yafahamike. Mapato kwa ajili ya nyumba kwa kawaida huwa ni kodi ya nyumba (*rental charge*). Thamani ya mapato hayo (*gross rental value*) si yote yanayogawanywa kwa wenye hisa katika mali. Kuna umuhimu wa kutoa gharama zote za uendeshaji.

(v) Mapato yaliyobaki baada ya kutoa gharama za uendeshaji, hugawanywa kwa wenye hisa kulingana na idadi ya hisa mtu alizonazo katika mali ile.

Itaonekana wazi kuwa njia hii haihusu riba kwa namna yoyote ile. Tofauti zinazojitokeza kati ya njia hii na ile ya kukopa kwa kuweka vitu rahani ni:

1) Mali humilikiwa na wenye hisa wote mpaka hapo atakayekuwa mmilikaji atakapomaliza kununua hisa za wengine wote.

2) Wenye hisa wote wana haki ya kugawana (kulingana na hisa mtu alizo nazo) mapato yanayotokana na mali hiyo na pia wana wajibu wa kushiriki katika gharama zote za uendeshaji.

## Mali yenye Kuchangiwa Mtaji kwa Hisa

Mtu akishaamua kuuza hisa (*share*) kwa watu wengine kwa ajili ya mali fulani katika sheria ya Kiislamu anapoteza umilikaji wa mali wa mtu mmoja. Kuuza hisa kwa wengine kwa maana nyingine ni kukaribisha watu wengine kushiriki katika umilikaji wa mali ile. Nafasi ya mtu katika kumiliki mali hiyo itategemea idadi ya hisa alizonazo katika mali ile. Wenye hisa inabidi washirikiane katika faida na hasara pamoja na gharama za uendeshaji.

## Faida Anazopata Atakayekuwa Mwenye Kumiliki Mali

Zipo faida kadhaa ambazo atakayekuwa mwenye kumiliki mali huzipata kwa kufuata ushirika katika biashara, mtaji na faida (*Shared Equity and rental*) badala ya kupata mikopo ya biashara yenye riba. Faida kubwa atakayopata ni fadhila za Allah (s.w.) kwa kule kuepuka kwake kutoa riba kwa mkopo atakaopata. Tunajifunza katika Hadithi za Mtume (s.a.w.) kuwa laana ya Allah (s.w.) huwafikia wote wanaohusika na riba (mtoaji, mpokeaji, shahidi). Hata hivyo kuna faida nyingine ambazo anaweza kuzipata:

- (i) Atakayekuwa mwenye kumiliki mali kwa kutochukuwa mkopo wenye masharti ya riba hujiepusha kabisa na hatari ya kunyang'anywa mali yake (aliyoweka rahani) akishindwa kutimiza masharti yake.
- (ii) Fedha ambayo angeitoa kama riba kwa ajili ya mkopo atabaki nayo na kutumia kwa shughuli nyingine kuendeshea maisha yake.
- (iii) Atakuwa na uhakika wa kupata sehemu halali ya faida inayotokana na mali hiyo (kama ipo). Kadhalika kama ikitokea hasara haitamlazimu kubeba mzigo wote wa hasara kwani ushirika katika biashara huhusisha vile vile umuhimu wa kugawana hasara itokeapo.

## Faida kwa Wenye Kununua Hisa

Mwenye kununua hisa huchangia katika mtaji. Naye huepuka ghadhabu za Allah(s.w.) za utoaji mkopo kwa riba. Zaidi ya haya hupata faida zifuatazo:

- (i) Hupata sehemu ya faida itokanayo na mali hiyo kulingana na mchango wake kwenye biashara (idadi ya hisa alizonazo).
- (ii) Huwa na sauti kwenye mali kwani naye pia ni mwenye kumiliki mali ile mpaka atakapouza hisa zake. Isitoshe hutoa kiwango kidogo kujipatia haki ya kumiliki ukilinganisha na mtaji mzima.

Kwa ujumla jamii nzima itanufaika kwa kuacha mfumo wa mikopo kwa riba na kuhimiza watu kufanya ushirika katika biashara. Ilivyo waliokopeshana kwa riba hawawi katika uhusiano mzuri kiroho. Aliyekopeshwa ilimbidi kufanya hivyo kutokana na shida aliyokuwa nayo. Kutoa kwake riba anakufanya kwa kuwa anafahamu hatari za kutofanya hivyo (kupoteza mali yake) ingawa kitendo hicho

kinamuuma sana rohani. Hivyo urafiki kati ya mkopeshaji na mkopeshwaji huwa ni wa kinafiki. Jambo hili ni wazi sana katika jamii ya dunia ya sasa. Hebu fikirira athari za mikopo hii kwa nchi masikini duniani. Ni mara nyingi nchi masikini zimekuwa zikipiga kelele aidha kupunguziwa au kufutiwa kabisa baadhi ya madeni yao. Sehemu kubwa ya madeni hayo ni limbikizo la riba la miaka mingi.

Hivyo Uislamu unapiga vita riba kutokana na madhara yake kibinafsi, kitaifa na kimataifa. Aidha Uislamu unahimiza ushirikiano katika biashara kama ufumbuzi wa tatizo la riba.

## **Benki za Kiislamu**

Benki za Kiislamu ambazo hutoa huduma kama benki nyingine zinaendeshwa katika msingi wa biashara na sio ule wa riba. Benki za Kiislamu badala ya kukopesha kwa riba, hutumia rasilimali zake kwa zenyewe kujihusisha katika uzalishaji kwa kufuata misingi inayokubalika katika Uislamu. Miongoni mwa misingi inayokubalika kwa Muislamu au Benki ya Kiislamu kuingiza fedha zake katika miradi ya biashara au uzalishaji ni hii ifuatayo:

### ***(i) Mudharabah***

Mudharabah ni makubaliano kati ya watu wawili au zaidi ambapo mmoja au zaidi kati ya hao anatoa mtaji na mwingine hushiriki kwa ukamilifu katika kuendesha na kuongoza mradi wa uchumi. Faida itakayopatikana katika mradi huo itagawanywa kulingana na makubaliano yao. Hasara itakayotokana na mradi huo itakuwa ni ya mwenye kutoa mtaji. Wengine hawatoi chochote kusaidia hasara kwa sababu wameshatoa mchango wao wa hasara hiyo kwa jasho walilolitoa katika shughuli ambayo haikuzaa matunda bali hasara.

Benki za Kiislamu zinaingiza fedha zake katika miradi ya uchumi kwa njia hii ya Mudharabah ambapo benki hutoa mtaji kwa ajili ya miradi mbali mbali ya uchumi kwa mapatano ya kupata kiasi (asilimia) fulani cha faida itakayopatikana na kuwa tayari kulipa hasara itakayopatikana.

### ***(ii) Musharikah***

Musharikah ni ushiriki kati ya watu wawili ambapo, tofauti na *Mudharabah* wote wawili wanachangia mtaji na kushiriki katika uendeshaji wa shughuli ya kiuchumi, lakini si lazima watoe hisa sawa sawa, kwa makubaliano ya kugawana faida na hasara kulingana na kiasi cha hisa alichotoa kila mmoja wao. Kwa mtindo huu wa "Musharikah" Benki ya Kiislamu inaingia katika kuchangia mtaji, kuendesha na kusimamia mradi wa uchumi na watagawana (faida au hasara) kulingana na kiasi cha mtaji kila mmoja alichotoa.

### ***(iii) Ijara-Uara wa Iktina***

Huu ni utaratibu mwingine unaokubalika kisheria ambapo mtu au benki inatumia fedha zake katika kukodi vitu kama vile magari, majumba, ardhi, na kadhalika, ambavyo vikifanyiwa kazi huzalisha mali na kutoa faida. Benki za Kiislamu hujipatia faida kubwa kutokana na mtindo huu.

#### *(iv) Murabah*

Huu ni utaratibu unaotumiwa katika kununua bidhaa kwa wingi kwa ajili ya kuwauzia wafanya biashara ambao waliofikiana kuwa bidhaa hizo zinunuliwe kwa ajili yao. Benki kutokana na uwezo wake inapanga na wafanya biashara kuwa inunue bidhaa nyingi kutoka ndani na nje ya nchi kwa jina lake kisha iwauzie wafanyabiashara hao kwa bei itakayoipatia benki faida. Pia benki kwa mtindo huu inaweza kununua mazao ya wakulima na kuyauza kwa walaji kwa faida.

#### *(v) Muqaradha*

Mtindo huu wa Muqaradha humruhusu mtu au benki kununua “share” au “bonds” katika kampuni ya uzalishaji kwa mapatano ya kugawana faida au hasara kulingana na kiasi cha “share”.

Kwa kufuata mitindo hii katika kuingiza fedha zake katika miradi ya uchumi, Benki za Kiislamu hupata faida kubwa hata zaidi ya kipato cha riba kinachopatikana katika benki za riba. Benki za Kiislamu nazo hugawa faida inayopatikana kwa wateja wake walioweka fedha zao kwenye benki.

## **Uzuri wa Benki za Kiislamu**

Pamoja na benki za Kiislamu kutoa huduma zinazotolewa na kila benki kama tulivyoziorodhesha huko nyuma, kuna faida za ziada zinazopatikana kutokana na benki hizi kama ifuatavyo:

**Kwanza** benki za Kiislamu huiokoa jamii na uchumi wake na madhara yote yanayosababishwa na riba.

**Pili**, Benki za Kiislamu huwaingiza katika uchumi na kuwainua hata wale ambao hawana hata rasilimali yoyote kwa mtindo wa Mudharabah. Hivyo ni kwamba, benki zinazoendeshwa kwa mikopo ya riba, haziwezi kukopesha fedha zake kwa mtu yeyote asiye na rasilimali yenye thamani sawa au zaidi ya mkopo ili atakaposhindwa kulipa ifilisiwe rasilimali hiyo. Kwa mtindo huu wa mikopo ya riba, ni matajiri tu wanaopata mikopo ya benki na masikini wasio na rasilimali yoyote huachwa hivyo hivyo na umasikini wao bila ya msaada kutoka benki wa kuwainua kiuchumi.

**Tatu**, benki za Kiislamu huiuua uchumi wa jamii, kutokana na umakini na tahadhari kubwa zinazochukua katika kuchagua na kuendesha miradi mbali

mbali ya uchumi. Kwa kuwa benki zenyewe zinajiingiza katika uchumi, zinahakikisha kuwa miradi zitakazoichagua ni ile yenye uwezo mkubwa wa kuzalisha faida kubwa na yenye uwezekano mdogo wa kusababisha hasara.

## **Zoezi 2:9**

1. Uchumi ni nini?
2. Toa ufafanuzi mfupi namna Uislamu unavyoeleza dhana ya:
  - (a) Mafanikio
  - (b) Umiliki wa mali
  - (c) bidhaa
  - (d) Matumizi
3. Soma kwa makini Qur'an (9:105),(5:1) na (6:165), kisha toa mafunzo ya kiuchumi.
4. Nukuu aya za Qur'an zinazoonesha umuhimu wa uchumi, kisha bainisha mafunzo yake kwa muhtasari.
5. Katika uchumi wa Kiislamu, serikali ya Kiislamu inawajibu gani kwa wananchi na raia wake?
6. Taja mambo matatu yanayopaswa kuzingatiwa katika uuzaji na ununuzi wa bidhaa.
7. Bainisha biashara haramu zisizostahiki Muislamu kuzifanya kibidhaa na njia au kiutaratibu.
8. Mfumo wa Uchumi wa Kiislamu ni Rehema kwa walimwengu wote.  
Thibitisha neema hii kwa kuonesha namna Qur'an inavyoondoa dhiki na ukata wa kiuchumi katika jamii kupitia mgawanyo wake wa mali.
9. Soma kwa mazingatio Qur'an 89:19, 104:2, 90:6, 68:12, 89:17-18, 70:19-25. kwa mujibu wa Qur'an:
  - (a) Wajibu wa kusimamia Haki za masikini na mafukara kuwezesha kujikimu kiuchumi katika jamii, Allah(s.w) amewakabidhi akina nani?
  - (b) Ni akina nani wenye jukumu la kuondoa Omba-omba katika jamii ambao pia wanadhima ya kujibu mbele ya Allah(s.w) kwa kuwepo na kushamiri tatizo hilo katika jamii.
  - (c) Je, katika jamii ambayo waumini wamewaachia khatamu matwaghuti wenye mioyo ya uchoyo, unyimifu, ubakhili, kuhodhi, husda, na ubinafsi wa kutojali wengine; yafaa waumini kutowaangalia Omba-omba, ambao ni "madhuluman"?

10. (a) Onesha tafauti zilizopo baina ya biashara na riba.  
 (b) Riba ina madhara gani katika jamii?
11. Onesha kwa ufupi misingi ya uendeshaji benki ya Kiislamu pasina riba.

## **SIASA NA UENDASHAJI WA DOLA KATIKA UISLAMU**

### *Maana ya siasa*

Siasa ni sayansi ya uendeshaji mambo ya kijamii. Dhana kuu za siasa ni utawala (mamlaka), itikadi, matashi na maamuzi. Hivyo tunapoitizama siasa hatunabudi kuzingatia kuwa ni mfumo wa utawala, itiqadi, matashi na maamuzi ya mtu au kikundi cha watu au ufunuo kutoka kwa Allah(s.w).

Kumbukumbu za kihistoria zinatufahamisha kwamba siasa ilianza pale wanadamu walipoanza kuishi pamoja kama kijiji, mji, taifa hadi kufikia mataifa. Hivyo siasa ni jambo kongwe kama ilivyo historia ya mwanadamu mwenyewe.

Katika jamii ya mwanadamu kuna mfumo mikuu miwili ya siasa.

1. Mifumo ya siasa iliyobuniwa na wanadamu – siasa za kitwaghutii.
2. Mfumo wa siasa uliowekwa na Mwenyezi Mungu – siasa ya Kiislamu.

### **1. Mifumo ya Siasa za Kitwaghuti**

Kwa mtazamo wa Kiislamu, masuala ya kijamii yenye kufuata mitindo na mipangilio iliyobuniwa na watu ndiyo yanayofahamika kama siasa za kitwaghuti. Kihistoria siasa hizo zimepita katika vipindi mbali mbali hadi hivi leo. Vipindi hivyo ni pamoja na:

- (i) Ujima.
- (ii) Utumwa.
- (iii) Umwinyi.
- (iv) Ubepari.
- (v) Ujamaa na Ukomunisti.
- (vi) Demokrasia.

#### *(i) Ujima*

Nadharia za kitwaghutii zinamuangalia mwanadamu kama mnyama ambaye katika kipindi cha ujima (cha awali) hakutofautiana na wanyama wengine. Yeye pia aliishi mtini, akaenda kwa miguu na mikono kwa pamoja. Hakutofautiana

sana na nyani alipokuwa katika hali ya usokwe-mtu. Kutokana na mabadiliko ya kimazingira baadhi ya wanyama, miongoni mwao akiwemo sokwe-mtu, walitoka katika hali ya kuishi mitini, wakateremka chini. Hapo ndipo yalipotokea “mabadiliko” ya maumbile ya miili yao kulingana na mazingira mapya. Lakini kutokana na uhasama uliokuwepo katika mazingira hayo mapya, kwani misitu na wanyama wakali walienea kote, mtu wa mwanzo hakuweza kuishi peke yake kiubinafsi. Hali hizo za kimazingira zilimlazimisha mtu wa mwanzo aishi kwa ushirikiano na wenziwe ili aweze kupambana na mazingira hayo makali. Hapo ndipo ilipoanza siasa kwa mujibu wa nadharia hii.

### ***(ii) Mfumo wa siasa za utumwa***

Mfumo wa siasa za kitumwa unafuatia ujima katika siasa za kitwaghutii. Ni mfumo wa siasa za kitabaka ambapo watu huishi kwa jasho la watu wengine wanaomilikiwa kama bidhaa. Watu hao wenye fursa za mali au hadhi katika jamii huishi kwa kuwatumikisha wengine. Katika mfumo huu, utawala uko mikononi mwa matajiri ambao huendesha siasa za kuwatumikisha wengine na wao kuishi maisha ya raha. Chini ya mfumo huu wa siasa, uzalishaji mali umewekwa migongoni mwa watu wa tabaka la chini la watwana.

Mfumo huu wa kitumwa ulianza kuyumba kwa migongano mbalimbali. Watumwa walianza kujizatiti na kupinga vikali sana utumwa wao. Watu ambao hapo awali walinyang’anywa mali zao na mabwana wenye watumwa waliungana pamoja na watumwa katika mapambano ya kuufuta utumwa:

### ***(iii) Mfumo wa siasa za Ukabaila***

Siasa za Ukabaila ambazo zilifuatia baada ya siasa za kitumwa nazo vile vile zilikuwa na minyororo yake. Katika mfumo huu tabaka la Kikabaila hutawala njia zote za kijamii. Njia za kiuchumi hutawaliwa kwa kukodisha mashamba halafu kutoa fungu kubwa kwa mwenye shamba wakati wa mavuno. Wazalishaji kwenye mashamba hayo chini ya mfumo huu, tofauti na utumwa, hulipwa posho kidogo kama malipo ya kazi nzito walizotumikishwa. Kwa mtazamo wa Kitwaghuti juu ya historia ya mfumo huu, inadaiwa kuwa taasisi za dini pia zimetumika “kuhalalisha” ubwana na utwana! Mfumo wa siasa za Ukabaila ulisita kuendelea baada ya wanyonywaji kujiunga pamoja dhidi ya wanyonyaji.

### ***(iv) Mfumo wa siasa za kibepari***

Siasa za kibepari ni moja ya mifumo ya Kitwaghuti iliyokita mizizi katika jamii nyingi. Katika mfumo huu kila kitu kinachowezekana kufanywa ili “kuzalisha” pesa hufanywa. Wachache walio na fursa za mali na hadhi ndiyo huendesha masuala yote ya jamii na kundi kubwa la wanajamii huishi kwa kuuza nguvu, vipaji na taaluma zao kwa wachache hao, na wale wasio na chochote hulazimika kufanya vitendo vyovyote ili mradi wapate pesa.



**(v) Mfumo wa siasa za Kijamaa (Kikomunist)**

Katika mfumo huu uliodhaniwa na waasisi wake kuwa ungelimkomboa mwanadamu na kuleta “**usawa wa sare**”, chama ndicho hushika hatamu zote na “huwakilisha matakwa ya walio wengi” katika jamii. Aidha hudaiwa kuwa jamii chini ya mfumo huu wa siasa watu huwa huru kabisa na kuwa na “demokrasia” halisi. Hata hivyo historia inaonesha kuwa chini ya mfumo huu wa siasa, jamii hupumbazwa na kudumazwa kwa njia mbalimbali. Kwa kuwa chama hushika hatamu za maongozi, ni kamati ya watu wachache tu ndani ya chama hicho ndio inayoendesha masuala yote ya utawala Hudhibiti kila kitu kwa kuimarisha ulinzi wa siri ambao hupenyezwa kila eneo la jamii. Huendesha propaganda dhidi ya wale wote wenye fikra tofauti na zao. Njia zote za uchumi huwa chini ya kikundi hicho cha watu kwa sura ya “mali ya umma”. Katika Tasnifu (thesis) yake ya shahada ya udaktari wa falsafa mwaka 1946, Dk. Rafiuddiin, aliandika juu ya kuporomoka kwa siasa hii kama ifuatavyo:

*“Marxism (Communism), like every wrong ideal, contains the germs of its own dissolution and must break up sooner or later”<sup>1</sup>*

**Tafsiri**

*Umarx (ukomonist), kama ilivyo kwa itikadi yoyote ile ya urongo, umebeba sumu inayoumaliza, hivyo lazima uporomoke hivi karibuni au baadae”.*

Hali iliendelea kuwa ngumu katika nchi zilizokuwa viranja wa siasa hii na hadi kufikia mwaka 1989 miaka 70 ya mapinduzi hayo ya kikomonist, Urusi ilisambaratika na huo ukawa ndio mwisho wa siasa hii.

**(vi) Mfumo wa siasa za kidemokrasia**

Demokrasia ikiwa na maana ya maamuzi ya wengi katika kuweka mamlaka waitakayo ni mfumo wa maisha uliobuniwa Uyunani (Ugiriki). Wataalamu wa mambo ya siasa wanafahamisha kuwa neno *Democracy* ni muungano wa maneno mawili yenye kuleta maana moja; *Demos-nguvu* ya raia na *cracy* ni “utawala”, yaani utawala unaotokana na maamuzi ya wengi miongoni mwa raia.

Hivi leo Demokrasia hufahamika kama ni utawala wa watu uliowekwa na watu kwa ajili ya watu (*The government of the people by the people for the people*). Au ni uhuru wa kujiamulia mambo vile mtu apendavyo! Kutokana na tafsiri hiyo, kisiasa, kuna aina tofauti za miundo ya demokrasia; zipo demokrasia za chama kimoja, demokrasia za vyama viwili, demokrasia ya vyama vingi, demokrasia ya kiliberali ambayo ni demokrasia ya moja kwa moja (*direct democracy*) na demokrasia ya uwakilishi (*representative democracy*), nakadhalika.

## 2. Mfumo wa Siasa ya Kiislamu

Mfumo wa siasa ya Kiislamu ni utaratibu na muongozo wa masuala ya jamii ambao misingi yake ni vitabu vya Allah(s.w) na Sunnah za Mitume wake tangu Mtume wa kwanza, Adam (a.s) hadi Mtume wa Mwisho, Muhammad(s.a.w). Ni mfumo uliowekwa na Allah(s.w) kupitia kwa Mitume wake wote. Mitume wote walikuja kusimamisha mfumo wa maisha aliouridhia Allah (Dini ya Allah). Kuhusu Mtume Muhammad(s.a.w) tunafahamishwa katika Qur-an:

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ

كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٣٣﴾

“Yeye (Allah) ndiye aliyemleta Mtume wake (Nabii Muhammad) kwa uongofu na kwa dini ya haki ili aijaalie kushinda dini zote, ijapokuwa watachukia washirikina”. (9:33, 61:9)

Kwa ujumla, mitume wote waliwalingania watu wao kutambua kuwa mwenye haki ya kutoa mwongozo na kuweka utawala juu ya wanadamu ni Allah(s.w) pekee. Pia waliwalingania watu wao kuwa kufuata maongozi yoyote yale ya kijamii (siasa), kinyume na Allah(s.w) ni shirk. Hivyo, wale wote wanaoendesha masuala ya kijamii kwa kutumia taratibu na miongozo iliyoasisiwa na watu wanamshirikisha Allah(s.w) katika siasa na ni wazushi tu kama Mwenyewe Allah(s.w) anavyotutahadharisha:

وَإِنْ تَطَّعَ أَكْثَرُ مَنْ فِي الْأَرْضِ يُضِلُّوكَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ إِنْ يَتَّبِعُونَ

إِلَّا الظَّنَّ وَإِنْ هُمْ إِلَّا سَخِرُونَ ﴿١١٦﴾

Na kama ukiwatii wengi katika (hawa) waliomo ulimwenguni watakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu. Hawafuati ila dhana tu, na hawakuwa ila ni wenye kuzua (tu basi).” (6:116).

## Dhana ya Dola

Dola ni eneo la ardhi lenye mkusanyiko wa watu walio huru chini ya utawala mmoja wenye uwezo wa kujitosheleza kwa mahitaji muhimu na kulinda mipaka ya eneo lake. Eneo hili la ardhi huitwa nchi na wakazi wake ndio wazawa au wananchi wenye haki na eneo hili. Katika ulimwengu huu kuna aina kuu mbili za Dola. Dola za kitwaghati na Dola za Kiislamu.

Tutaangalia kwa muhtasari miundo na uendeshaji wa dola hizi ili tuweze kulinganisha na kutofautisha mifumo ya utawala iliyowekwa na wanadamu na ule uliowekwa na Muumba.

## Dola za Kitwaghuti

### 1. Muundo na Uendeshaji wake

Chombo kikuu cha **kwanza** katika dola za kitwaghuti ni **serikali**. Kazi kuu ya serikali ni kutawala kwa kutumia nguvu kuhakikisha kuwa jamii husika inafuata mwenendo unaotakiwa na serikali. Serikali inaundwa na sehemu tatu – Kiongozi Mkuu wa Dola au Rais. Baraza la Mawaziri na Majeshi. Kiongozi Mkuu wa Dola amekuwa ndiye mtendaji mkuu na muamrishaaji mkuu wa majeshi (Amir Jeshi Mkuu). Katika uhusiano na Dola nyingine, kiongozi mkuu ndiye msemaji mkuu kwa niaba ya Dola yake. Kiongozi huyu mkuu wa dola huwa juu ya sheria na hawezi kushitakiwa kwa kosa lolote analolitenda wakati wa utendaji kazi wake kama kiongozi mkuu wa dola

Majeshi ya serikali za kitwaghuti ndio nguvu ya dola. Majeshi hutumika kulinda, kutetea, na kuhakikisha matakwa na maslahi ya serikali yanapatikana. Majeshi vile vile hutumika katika kulinda mipaka na mamlaka ya dola. Wakati mwingine hutumika kuvamia nchi nyingine ili kupanua mipaka ya dola. Majeshi pia hutumiwa katika kusimamia utekelezaji wa sheria na amri zote zinazotakiwa na serikali. Majeshi yenyewe hugawanyika katika sehemu tofauti kiutendaji. Kuna jeshi la polisi lenye vikosi vya ulinzi wa kawaida kwa usalama wa raia, vikosi vya kutuliza fujo, vikosi vya usalama barabarani, na kadhalika, hivi vyote hushughulikia usalama wa raia tu. Kuna jeshi la ulinzi linaloshughulika na ulinzi wa mipaka ya dola kwa ujumla likiwa na vikosi vya nchi kavu, vikosi vya anga na vikosi vya majini. Kuna jeshi la magereza linaloshughulika na wahalifu wote wanaovunja sheria.

Pamoja na majeshi zipo idara au vitengo maalumu vya usalama vilivyo chini ya ofisi ya mkuu wa dola ambavyo hujishughulisha na utafiti wa habari muhimu kiutawala (Intelligence bureau) ambavyo ndani ya mipaka ya dola huchunguza kwa mbinu mbali mbali kutafuta hisia na minong'ono ya wananchi jinsi wanavyoitazama serikali na mipango yao dhidi yake.

Kwa ujumla Idara ya usalama hujishughulisha na maeneo yafuatayo:

- (1) Kupeleleza mambo mbali mbali kisha kuiarifu serikali sambamba na kupendekeza au kushauri hatua muafaka za kuchukuliwa.
- (2) Kukusanya habari na taarifa muhimu zinazohitajika na serikali kiusalama.
- (3) Kuingilia kati shughuli za idara au mashirika mengine ya upelelezi na ujasusi.
- (4) Kueneza na kushinikiza sera na matakwa ya serikali kwa njia mbali mbali za siri vikiwamo vitisho (intimidation), upotoshaji wa habari au kueneza habari zisizo zenyewe (disinformation), udhibiti wa habari, urubunifu, kuffitinisha na kufarakanisha wapinzani, kuendesha propaganda na

kuwadhibiti wapinzani wa kisiasa, kujipenyeza au kutumia watendaji (double agents) ndani ya makundi ya watu, taasisi au jumuiya ili kufahamu mipango yao ili waweze kuivuruga. Vile vile katika serikali kuna sehemu ya utawala (Administration) iliyoundwa kutokana na msururu mrefu wa urasimu. Warasimu hao waliogawanywa katika wizara, idara, na vitengo mbalimbali, husimamia shughuli za kila siku za serikali. Wanakuwa na mamlaka ya kutoa amri na maelekezo ya mara kwa mara. Mbali na kuwa na serikali kuu, Dola huwa pia na serikali za majimbo (mikoa), serikali za wilaya, miji, na za mitaa. Kila serikali inakuwa na kiongozi wake mkuu k.v. mkuu wa mkoa, mkuu wa wilaya.n.k.

Chombo kikuu cha **pili** cha dola ya kitwaghutii ni **Bunge**. Bunge nalo huwa na sehemu mbili. **Bunge** kwa maana ya wabunge tu na **Bunge Kuu** kwa maana ya wabunge na kiongozi mkuu wa dola (Rais). Kazi ya Bunge ni kutunga sheria na kudhibiti mwenendo wa serikali. Hata hivyo katika mfumo wa serikali iliyochini ya Rais (Presidential form of government) sheria zinazopitishwa na Bunge haziwi sheria mpaka akubali Rais na kuidhinisha kwa saine yake.

Vile vile bunge lina kazi ya kudhibiti mwenendo wa serikali kwa kujadili na kupitisha makisio ya mapato na matumizi ya serikali (Budget).

Chombo kikuu cha **tatu** cha Dola ni **Mahakama**. Kazi kuu ya mahakama katika mfumo wa kitwaghutii ni kueleza na kufafanua utekelezaji wa sheria. Kuonesha namna ya kuwajibika na kuadhibu pale inapolazimu. Kwa maana nyingine mahakama inayokazi ya kutoa au kusimamia utoaji wa haki. Mahakama zinaweza kuwa na mpangilio wa kuanzia ngazi ya chini hadi ya juu kama vile mahakama za mwanzo, mahakama ya wilaya, mahakama za mikoa, mahakama kuu na mahakama za Ruffaa.

Kwa ujumla vyombo vyote vilivyoorodheshwa husimamiwa moja kwa moja na Dola na huwajibika kwa dola. Vipo baadhi ya vyombo ambavyo sio mali ya Dola lakini hutumiwa na dola katika kutekeleza shughuli zake kama vile **vyombo vya Kijasusi na vyombo vya Itikadi**.

## **Vyombo vya Kijasusi**

Katika mataifa makubwa ya kisekula, mbali ya vitengo vya ndani vya upelelezi huwepo pia mashirika ya kijasusi yanayofanya ujasusi nchi nyingine kwa manufaa ya mataifa hayo. Mataifa hayo yana idara za usalama na mashirika ya ujasusi.

Nchi za Marekani na Israil ni maarufu katika shughuli hii ya ujasusi. Taifa la Marekani, kwa mfano, mbali ya shirika lake la ndani la upelelezi FBI (*Federal Bureau Investigation*) pia ina mashirika mengine kama CIA (*Central Intelligence Agency*), NSA (*National Security Agency*) na DIA (*Defence Intelligence*

Agency). Taifa la Israel lina mashirika mawili makubwa ya kijasusi, shirika la *Shin-Bet* likijishughulisha na upelelezi wa ndani ya Israel na shirika la *Mossad* linajishughulisha na “nje” ya Israel. Uingereza ina vitengo vikuu viwili. Kitengo cha usalama (M15) ambacho hushirikiana na idara maalum ya polisi iliyo chini ya ofisi ya waziri Mkuu vikiwajibika na usalama wa ndani. Pia kuna shirika la kijasusi la secret Intelligence Service (SIS) au M16, hili liko chini ya wizara ya mambo ya Nje. Secret Intelligence Service hufanya ujasusi nje ya Uingereza kulinda maslahi ya nchi hiyo. Ufaransa nayo ina shirika liitwalo Service Documentation Exterieur Contre Espionage (SDECE). Na Ujerumani ina kitengo kama hicho kitiwacho Bundes Nachristen Dienst (BND).

## Vyombo vya Itikadi

Katika dola za kisekula pamoja na kuwepo vyombo vya mabavu pia huwepo vyombo vya itikadi. Baadhi ya vyombo hivi huweza “kusimamiwa moja kwa moja na dola, wakati vingine huwa nje ya mamlaka hiyo.

Katika suala la itikadi chombo ambacho hupewa umuhimu wa “pekee” ni elimu. Elimu hutolewa ama na dola yenyewe au na taasisi zilizosajiliwa. Kazi moja ya dola ni kutoa au kusimamia utoaji na uendeshaji wa elimu na maarifa. Huunda, kutengeneza au kujenga itikadi na kuifanya iwe rasmi. Hulazimisha itikadi hiyo ikubalike na kufuatwa na watu wote. Japo itikadi hiyo hupingwa na jamii nzima, lakini ukweli ni kwamba itikadi inayotawala na kuongoza dola siku zote ni itikadi ya tabaka linalotawala Itikadi hii hutumika kutawala matabaka yanayotawaliwa katika kipindi cha “**amani na utulivu**”. Mara nyingi utii na unyenyekevu wa raia huwa ni wa woga kutokana na vitisho na mabavu ya watawala kwamba wote wanaokwenda, wanaoongea na wanaotenda kinyume cha itikadi rasmi hushughulikiwa na vyombo vya dola

Vyombo vya itikadi ni pamoja na shule na vyuo, dini, vyama vya siasa, miungano ya namna mbali mbali na vyombo vya habari. Pamoja na mengine vyombo vyote hivi huelimisha watu kuhusu itikadi, sera au dira ya tabaka linalotawala huwashawishi watu waikubali na kuifuata. Hujitahidi kuihalalisha kuwa ni sahihi na nzuri kuliko itikadi nyingine. Tabaka linalotawala huandaa mitaala ambayo katika ufundishaji hutumika kwenye Mashule; Vyuo, Vyuo Vikuu na Taasisi za elimu, mkazo mkubwa ukiwa kuifikisha itikadi ya watawala kwa wananchi, tangu wakiwa na umri mdogo kabisa hadi wanapokuwa watu wazima wenye uwezo wa kufahamu, kufikiri, kuchambua, kutathmini, kulinganisha, kuchanganua na kufikia, au kutoa “uamuzi huria”. Shule na vyuo huwalea watu wa umri mbali mbali na kutoa daraja mbali mbali za Wataalamu na wanafikara ambao hutazamiwa watende kulingana na matakwa ya Watawala.

Katika mfumo wa kisekula (hasa wa kijahilia) Dini na taasisi zake kama makanisa, misikiti, shule na vyuo mbali na kueneza “imani ya dini”, pia hutumika

kueneza itikadi ya tabaka linalotawala hufundisha waumini wao kutii dola, kufuata itikadi yake na kuwa waaminifu kwa kiongozi anayetawala

## Dosari za Dola za Kitwaghuti

Historia inatuonesha kuwa pamoja na umuhimu wa uongozi au serikali katika jamii, si kila serikali iliyoweza kuwashikamanisha wanadamu pamoja na kuwaelekeza katika lengo la maisha yao. Dola yoyote iliyowekwa na kuendeshwa kwa kufuata matashi ya binadamu imekuwa ikiwafarakanisha binadamu na kuwagawa katika matabaka mbali mbali.

Matabaka ya waungwana na watwana, matajiri na masikini, wenye nguvu na wanyonge, wageni na wazawa, watawala na watawaliwa, na kadhalika. Katika kipindi cha historia ya mwanadamu, watu wa matabaka ya juu daima wamekuwa wakiwanyonya na kuwakandamiza watu wa matabaka ya chini kwa kutumia hila mbali mbali.

### 2. Muundo wa Dola ya Kiislamu na Uendeshaji wake

Kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu, mwanadamu analazimika kuishi maisha ya kijamii ambayo humtaka ahusiane na kushirikiana na watu wengine ili aweze kufikia lengo la kuumbwa kwake la kuletwa hapa duniani. Ili wanadamu waweze kushirikiana na kuliendea lengo la maisha yao kwa pamoja hapana budi kuwa na serikali au uongozi madhubuti.

Adam(a.s) alipokuwa peponi (bustanini) pamoja na mkewe, alikuwa kiongozi. Aliposhushwa hapa duniani aliongoza familia yake (kizazi chake) kwa mwongozo utokao kwa Allah(s.w) kama tunavyofahamishwa katika Qur-an:

قُلْنَا أَهْبَطُوا مِنْهَا جَمِيعًا ۖ فَإِمَّا يَأْتِيَنَّكُمْ مِنِّي هُدًى فَمَنْ تَبِعَ هُدَايَ فَلَا

خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٣٨﴾

Tukasema: “Shukeni humo nyote; na kama ukikufikieni uwongozi utokao kwangu, basi watakaofuata uwongozi wangu huo haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika.(2:38)

وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۖ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٣٩﴾

Lakini wenye kukufuru na kuyakadhibisha maneno yetu, hao ndio watakaokuwa watu wa Motoni, humo watakaa milele.” (2:39)


Katika sehemu hii tutaangalia dhana ya utawala katika Uislamu na muundo

wa Dola ya Kiislamu na uendeshaji wake.

## Dhana ya Utawala katika Uislamu

Wataalamu wa siasa (Political scientists) wanautazama utawala kama “uwezo wa juu kabisa wa kuamuru, kuongoza na kudhibiti vyote vilivyo ndani ya mipaka ya Dola usio wajibika kwa yeyote yule ndani ya mipaka hiyo.” Kwa mtazamo huo mtu au kikundi cha watu (chama, taasisi, n.k.) kinaposhika utawala, basi neno au tamko la mtu huyo au kikundi hicho huwa ni amri au sheria ya kutiwa bila hiari.

Kwa hiyo, kwa namna dhana ya utawala ilivyo, hakuna mwanadamu mwenye sifa, uwezo na haki ya kushika nafasi ya utawala” Ni kwa msingi huu Qur’an imetoa msisitizo na maelezo yaliyo wazi kabisa kuwa utawala ni haki na milki ya Allah(s.w) pekee kwa sababu yeye:

 لَا يُسْأَلُ عَمَّا يَفْعَلُ وَهُمْ يُسْأَلُونَ

*Haulizwi (Mwenyezi Mungu) anayoyafanya (kwani yote ni ya haki) lakini wao (viumbe) wataulizwa. (21:23)*

قُلْ مَنْ مِنْ بَيْدِهِ مَلَكُوتُ كُلِّ شَيْءٍ وَهُوَ يُجِيرُ وَلَا يُجَارُ عَلَيْهِ إِنْ كُنْتُمْ

 تَعَامُونَ

*Sema: “Ni nani mkononi Mwake umo ufalme wa kila kitu, Naye, ndiye, alindaye, na hakilindwi (chochote) kinyume Naye, kama mnajua (jambo nambieni hili).” (23:88)*

Yeye, Allah(s.w), peke yake ndiye Muumba wa vyote na ndiye mtawala halisi wa ulimwengu na vyote vilivyomo. Si haki ya kiuumbe yeyote yule awezaye kuamrisha, kutiwa au kuongoza kinyume na Allah(s.w).

## Vyombo vya Dola ya Kiislamu

Serikali ndiyo taasisi kuu katika dola ya Kiislamu, nayo imegawanywa katika sehemu kuu tatu: Yaani Bunge (Shuura), Urasimu (mamlaka ya utendaji) na Mahakama.

### *Kazi za Bunge la Kiislamu*

Bunge la Kiislamu, tofauti na mabunge ya mifumo mingine, ni chombo cha **Mshawara** na ufafanuzi wa masuala mbali mbali ya dola. Bunge la Kiislamu si chombo cha kutunga sheria kinyume na zile zilizomo ndani ya Qur’an na Sunnah:

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ

الْحَيْرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾

“Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, hakika amepotea upotofu (upotevu) ulio wazi (kabisa) “. (33:36).

إِنَّا أَنْزَلْنَا التَّوْرَةَ فِيهَا هُدًى وَنُورٌ تَحْكُمُ بِهَا النَّبِيُّونَ الَّذِينَ أَسْلَمُوا

لِلَّذِينَ هَادُوا وَالرَّبَّانِيِّونَ وَالْأَحْبَابُ بِمَا آسْتَحْفِظُوا مِنْ كِتَابِ اللَّهِ

وَكَانُوا عَلَيْهِ شُهَدَاءَ ۚ فَلَا تَخْشَوُا النَّاسَ وَآخِشُونِ وَلَا تَشْتَرُوا بِعَآيَتِي

ثَمَنًا قَلِيلًا ۗ وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ ﴿٤٤﴾

“Hakika tuliteremsha Taurati yenye uwongozi na nuru; ambayo kwayo Manabii waliojisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu) waliwahukumu Mayahudi: na watawa na maulamaa pia (walihukumu kwa hiyo Taurati), kwa sababu walitakiwa kuhifadhi Kitabu (hicho) cha Mwenyezi Mungu; nao walikuwa mashahidi juu yake. Basi (nyinyi Waislamu) msiwaogope watu, bali niogopeni (mimi). Wala msibadilishe Aya zangu kwa thamani chache (ya duniani). Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri.” (5:44).

Pamoja na hivyo, Bunge la Kiislamu hufanya kazi zifuatazo:

- (i) Pale ambapo Qur'an na Sunnah zimeweka maelezo na hukumu wazi, bunge la Kiislamu halina uwezo wa kufanya vinginevyo bali kuyaweka maelezo hayo kulingana na mazingira, kutoa tafsiri na ufafanuzi wa kina na kuweka kanuni na maelekezo yatakayohimiza utekelezaji wa hukumu hizo.
- (ii) Pale ambapo Qur' an na Sunnah zina maelezo yenye tafsiri zaidi ya moja, wajibu wa bunge ndani ya dola ya Kiislamu ni kuchagua moja ya tafsiri hizo na kuiidhinisha kutumika kijamii kama rejea iliyokubalika.
- (iii) Pale ambapo hukumu (Qur'an na Sunna) haziko wazi, kazi ya bunge ni kujadili na kupitisha fat-wa ya kufuatwa na jamii. Msingi utakaozingatiwa katika majadiliano, ni ule usemao kuwa jambo lolote lile ambalo halikuharamishwa basi ni halali.



- (iv) Kutoa *Fat'wa* kuhusiana na hali za dharura zinazojitokeza kisiasa, kiuchumi n.k.

### ***Kazi za Warasimu (Ulul-Amri)***

Wenye mamlaka (*Ulul-Amri*) katika dola ya Kiislamu ni wasimamizi wa utekelezaji wa maamrishi na makatazo ya Allah (s.w.), kazi yao kubwa ni kuiandaa jamii kuyapokea, kuyakubali, kuyatii na kuyatekeleza maamrishi hayo katika maisha ya kila siku.

Utaratibu huu wa Urasimu wa dola ya Kiislamu unatofautiana na ule wa dola za kitwaghutii ambao huwafanya Warasimu kuwa waheshimiwa na watawala. Amri ya Allah juu utii kwa viongozi ni:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولَى الْأَمْرِ مِنْكُمْ فَإِن تَنَزَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ  
الْآخِرِ ذَٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٥٩﴾

*Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye mamlaka juu yenu, walio katika nyie (Waislamu wenzenu). Na kama mkikhitalifiana juu ya jambo lo lote basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Kufanya hivyo ni bora kwenu na kuna matokeo mazuri(4:59).*

Utii kwa wenye mamlaka ndani ya dola ya Kiislamu hutanguliza sharti la wao kwanza (*Ulul-Amri*) kuwa watiifu kwa Allah (s.w.) na Mtume wake. Kinyume na hivyo, Qur'an ina maelekezo yafuatayo:

وَلَا تُطِيعُوا أَمْرَ الْمُسْرِفِينَ ﴿١٥١﴾ الَّذِينَ يُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ وَلَا يُصْلِحُونَ ﴿١٥٢﴾

*“Wala msitii amri za wale maasi, (wenye kupindukia mipaka ya Mungu). “ Ambao wanafanya uharibifu tu katika ardhi wala hawaitengenzi. “ (26:151-152)*

### ***Kazi za Mahakama***

Wajibu wa Mahakama katika dola ya Kiislamu ni kufafanua, kusimamia na kuhakikisha hukumu na sheria za Allah zinatekelezwa ili kulinda haki; kuzuia maovu, ufisadi na dhulma katika jamii:

وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ الْكِتَابِ  
 وَمُهَيْمِنًا عَلَيْهِ ۗ فَاحْكُم بَيْنَهُم بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ عَمَّا  
 جَاءَكَ مِنَ الْحَقِّ ۗ لِكُلِّ جَعَلْنَا مِنْكُمْ شِرْعَةً وَمِنْهَاجًا ۗ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ  
 لَجَعَلَكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَلَٰكِن لِّيَبْلُوَكُمْ فِي مَا آتَاكُمْ ۗ فَاسْتَبِقُوا الْخَيْرَاتِ  
 إِلَى اللَّهِ مَرْجِعُكُمْ جَمِيعًا فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿٤٨﴾

*Na tumekuteremshia Kitabu kwa (ajili ya kubainisha) haki, kinachosadikisha vitabu vilivyokuwa kabla yake, na kuvihukumia (kama haya ndiyo yaliyoharibiwa au ndiyo yaliyoasalimika). Basi wahukumu baina yao kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuat matamano yao kwa kuacha haki iliyokufikia. Na kila (umma) katika nyinyi (binadamu) tumeujaalia sheria yake na njia yake. Na kama Mwenyezi Mungu angalitaka angekufanyeni kundi moja (la kufuata sheria moja), lakini anataka kukujaribuni kwa hayo aliyokupeni. Basi shindaneni kuyafikilia mambo ya kheri. Nyinyi nyote marudio yenu ni kwa Mwenyezi Mungu; naye atakwambieni (yote) yale mliyokuwa mkikhitilafiana. (5:48)*

وَأَنْ أَحْكُم بَيْنَهُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ ..... ﴿٤٩﴾

*Na wahukumu baina yao kwa yale aliyokuteremshia Mwenyezi Mungu, wala usifuat matamano yao... (5:49)*

أَفْحُكْمَ الْجَاهِلِيَّةِ يَبْغُونَ ۗ وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ اللَّهِ حُكْمًا لِقَوْمٍ يُوقِنُونَ ﴿٥٠﴾

*Je, wao wanataka hukumu za Kitwaghuti? Na nani aliye mwema zaidi katika hukumu kuliko Mwenyezi Mungu; (yanafahamika haya) kwa watu wenye yakini.” (5:50).*

Kuhukumu kinyume na hukumu za Allah (s.w.) ni kuleta dhulma katika jamii. Ni kwa msingi huu Allah (s.w.) anatuasa:

..... وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٥١﴾

*“... Na wasio hukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhalimu”. (5:45).*

## Uraia katika Dola ya Kiislamu

Dola ya Kiislamu ina raia wa aina mbili ndani ya mipaka yake:

(1) Waislamu (2) Dhimmi. Qur'an inafahamisha ifuatavyo:

*Hakika wale walioamini na wakahama na wakapigania dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na nafsi zao; (Nao ni wale Muhajiri -Waislamu wa Makka). Na wale waliowapa (Muhajiri) mahala pa kukaa (Nao ni Ansari) na wakainusuru (dini ya Mungu); hao ndio marafiki, wao kwa wao (katika kurithiana na mengineyo). Na wale walioamini, lakini hawakuhama, ninyi hamna haki ya kurithiana nao (wala ya mengineyo) hata kidogo mpaka wahame katika nchi ya kikafiri waje wakae nchi moja na nyinyi). Lakini wakiomba msaada kwenu katika dini, basi ni juu yenu kuwasaidia, isipokuwa juu ya watu ambao kuna mapatano baina yenu na wao, (hapo msiwasaidie wao mkapigana na waitifaki wenu. Lakini jitahidini kupatanisha). Na Mwenyezi Mungu anayaona (yote) mnayoyatenda. (8: 72).*

Kutokana na aya hii, sifa za kustahiki uraia ndani ya Dola ya Kiislamu ni Uislamu na asili au uzawa ndani ya mipaka ya Dola Kiislamu. Muislamu yoyote yule hata kama ni mhamiaji ni raia anaetambulika na kukubalika na Dola bila ya kujali rangi, taifa au lugha yake. Dola ya Kiislamu inawatambua Waislamu wote kama ni raia zake na wote hao ni ndugu:

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ فَأَصْلِحُوا بَيْنَ أَخَوَيْكُمْ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ

تُرْحَمُونَ

*Kwa hakika Waislamu wote ni ndugu; basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na Mcheni Mwenyezi Mungu (msipuuze jambo la kupatanisha) ili mrehemewe. “ (49:10).*

Kuhusiana na wale ambao si Waislamu lakini ni wazawa ndani ya mipaka ya Dola ya Kiislamu, uraia wao utatambuliwa iwapo watakubali kutii maamrisha ya Dola. Raia hawa watifu kwa Dola katika sheria ya Kiislamu huitwa dhimmi na hustahiki hupata haki zote kama raia.

## Msonge wa Uongozi katika Dola ya Kiislamu

Msonge wa uongozi katika Dola ya Kiislamu umebainishwa wazi katika Qur'an na kufasiriwa vyema na Mtume Muhammad(s.a.w) katika Dola ya Kiislamu aliyoiunda. Hebu turejee aya zifuatazo:

يٰٓأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُوْبِى الْأَمْرِ مِنْكُمْ فَإِن تَعَتَرْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ  
الْآخِرِ ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٥٩﴾

*Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtiini Mtume na wenye mamlaka juu yenu walio katika' nyie. Na kama mkikhitilafiana juu ya jambo lolote basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume; ikiwa mnamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Hiyo ndiyo kheri na ina matokeo bora kabisa. (4:59)*

Katika aya hii tunajifunza kuwa aliye juu na anayestahiki kupewa utii wa kwanza au anayestahiki kupwekeshwa kwa utii ni Allah (s.w.), kisha hufuatia Mtume wake ndipo hufuatia viongozi wa jamii (*Warasimu*) wa ngazi mbalimbali. Viongozi hawa wa jamii, kwa mujibu wa aya hii, watastahiki kutiwa tu pindi watakapokuwa ni Waislamu wanaoongoza kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah.

## Msonge wa Uongozi katika Uislamu

Msonge wa uongozi katika jamii yoyote ya Kiislamu.

Msonge wa Uongozi katika jamii yoyote ya Kiislamu	Msonge wa uongozi katika Dola ya Kiislamu wakati wa Mtume
1. Allah(s.w) Qur'an	1. Allah(s/w)
2. Mtume(s.a.w)(sunnah)	2. Mtume Muhammad(s.a.w)
3. Majlis Shura(Bunge)	3.Shura(sekretariati ya Mtume)
4. Viongozi wa Jamii wa ngazi zote(msonge wa uongozi utatiririka kuanzaia taifani hadi kwenye familia)	4. Viongozi was Mikoa na viongozi wengine katika ngazi na nyanja mbalimbali.
5. Raia (wenye mchanganyiko wa waislamu na wasiokuwa waislamu)	5. Raia (wenye mchanganyiko wa Mayahudi, Wakristo na Washirikiana)

## Kwa nini Utii Uelekezwe Kwanza kwa Allah (s.w.)?

Allah(s.w.) anastahiki kupewa nafasi ya kwanza na ya juu ya Utii wa mwanadamu kwa sababu yeye ndiye Muumba na Mmiliki pekee wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo - vidogo na vikubwa na vinavyoonekana na visivyooonekana. Yeye ndiye Mfalme wa kweli mwenye uwezo juu ya kila kitu asiyehitajia msaidizi au mshirika yeyote katika kuuendesha ufalme wake. Ufafanuzi wa ufalme wake tunaupata katika Qur'an. Hebu tuzingatie aya zifuatazo:

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ  
عَلَى الْعَرْشِ يُغْشِي اللَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ  
مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهِ ۗ أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ ۗ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٢٠١﴾

*Hakika Mola wenu ni Allah aliyeziumba mbingu na ardhi kwa nyakati sita. Kisha akatawalia juu ya arshi Yake. Huufunika usiku kwa mchana ufuatiao upesi upesi; (na huufunika mchana kwa usiku ufuatiao upesi upesi). Na ameliumba jua, mwezi na nyota (Na vyote) vimetiishwa kwa amri Yake. Fahamuni! Kuumba (ni kwa Allah) na amri zote ni zake. Ametukuka kweli kweli Allah, Mfalme (Rabbi) wa walimwengu wote. (7:54)*

الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَلَمْ يَكُن لَّهُ  
شَرِيكٌ فِي الْمُلْكِ وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ فَقَدَرَهُ تَقْدِيرًا ﴿٢٠٢﴾

*(Mwenyezi Mungu) ambaye ni wake (pekee) ufalme wa mbingu na ardhi, wala hakuzaa mtoto wala hana mshirika katika ufalme (wake) na ameumba kila kitu na akakikadiria kipimo (chake)(25:2).*

Allah(s.w.) amekiumba kila kitu kwa lengo na akakiwekea utaratibu (sheria madhubuti utakaokiwezesha kuwepo, kubakia na kufikia lengo lake. Hivyo ili kitu chochote kibakie hakina hiari ya kutii sheria za Allah (s.w.) alizokiwekea. Hizi ni sheria za maumbile(natural laws) ambazo hata miili yetu inazitii bila hiari. Allah(s.w.) anatutanabahisha:

أَفَغَيْرَ دِينِ اللَّهِ يَبْغُونَ وَلَهُ أَسْلَمَ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ طَوْعًا  
وَكَرْهًا وَإِلَيْهِ يُرْجَعُونَ ﴿٢٠٣﴾

*Je! wanataka dini isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu, na hali kila kilichomo mbinguni na ardhini kinamtii yeye kipende kisipende? Na kwake watarejeshwa wote. (3:83)*

Aya hii inamtanabahisha mwanadamu kuwa pamoja na kwamba amepewa uhuru na uwezo wa kujiamulia utaratibu wa maisha na kujiwekea sharia zitakazo muongoza katika kuendesha maisha yake ya kijamii, kwanini asitumie uhuru huo kwa busara kwa kuamua kufuata utaratibu au sheria za kuendesha maisha ya kijamii alizozitokea Allah(s.w.) ambazo zinalandana na sheria za maumbile zinazofuatwa na kila kilichomo mbinguni na ardhini pamoja na mwili wake

wenyewe Je, mwanadamu atakapo amua kutii utaratibu wa maisha kinyume na ule aliomuwekea Muumba wake; Maisha ya upinzani yatamfikisha wapi kama si katika matatizo ya kijamii ya kila namna na maangamivu? Mwanadamu mwenye akili na busara ni yule anayemtii Muumba wake ipasavyo kwa kuitikia wito wake ufuatao:

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا فِطْرَتَ اللَّهِ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا لَا  
تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّهِ ذَٰلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا

*Basi uelekeze uso wako katika dini iliyo sawa sawa - ndilo umbile Mwenyezi Mungu alilowaambia watu, (yaani dini hii ya Kiislamu inawafikiana bara bara na umbo la binadamu). Hakuna mabadiliko katika maumbile ya viumbe vya Mwenyezi Mungu. Hivyo ndiyo dini ilivyo haki, lakini watu wengi hawajui. (30:30)*

## Kwa nini Mtume(s.a.w) Achukue Nafasi ya Pili ya Utii?

Ilivyo ni kwamba, Allah (s.w.) katika utaratibu wake wenye hikima, hawasiliani na kila mwanadamu bali amewateua wajumbe wake miongoni mwa wanadamu kufikisha ujumbe wake kwa wanadamu wote na kuwafundisha kwa matendo namna ya kuutekeleza ujumbe huo katika kuendesha maisha yao ya kila siku kwa mtu binafsi na kwa jamii kwa ujumla.

Wajumbe hawa ni Mitume ambao walifunuliwa na Allah (s.w.) namna ya kuiongoza jamii katika njia anayoiridhia. Ambayo ndiyo pekee inayomfikisha mwanadamu katika lengo la kuumbwa kwake kwa furaha na amani. Mitume wa Allah (s.w.) wamethibitishwa kwa walimwengu na mwenyewe Allah(s.w) kwa kuwaambatanisha na dalili mbalimbali na pia amewateremshia vitabu kutoka kwake ambavyo ni mwongozo kamili wa maisha ya mwanadamu na ni vyenye kutoa hukumu baina ya watu kwa uadilifu.

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيَقُومَ  
النَّاسُ بِالْقِسْطِ ..... ﴿٢٥﴾

*Kwa hakika tuliwapeleka Mitume wetu kwa dalili wazi wazi na tukaviteremsha vitabu na uadilifu pamoja nao, ili watu wasimamie uadilifu(57:25)*

Mitume wa Allah(s.w.) ni tofauti na viongozi wa kawaida ambao huongoza kwa kutumia fikra na jitihada za kibinadamu ambazo mara zote huathiriwa na udhaifu mwingi alionao. Mwanadamu wa kawaida anaathiriwa sana na mazingira yake, matashi yake na ufinyu wa elimu yake. Kutokana na udhaifu

huu si lazima kila atakaloamua, liwe sahihi na lenye manufaa kwa jamii. Lakini Mitume hawaongozi kwa fikra na matashi yao, bali huongoza kwa ufunuo (Wahyi) kutoka kwa Allah (s.w.) ambaye ni mjuzi wa kila kitu mwenye habari ya mambo yote. Allah (s.w.) anatuthibitishia hili katika Qur'an:

وَالنَّجْمِ إِذَا هَوَىٰ ﴿١﴾ مَا ضَلَّ صَاحِبُكُمْ وَمَا غَوَىٰ ﴿٢﴾ وَمَا يَنْطِقُ  
عَنِ الْهَوَىٰ ﴿٣﴾ إِنَّ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ ﴿٤﴾ عَلَّمَهُ شَدِيدُ الْقُوَىٰ ﴿٥﴾

*Naapa kwa nyota zinapoanguka kwamba mtu wenu (huyu Nabii Muhammad) hakupotea wala hakukosa, wala hasemi kwa matamania (ya nafsi Yake). Hayakuwa haya anayosema ila ni Wahyi (ufunuo) uliofunuliwa (kwake). Amemfundisha (Malaika) mwenye nguvu sana. (53:1-5).*

Hivyo mwanadamu hawezi kufuata njia ya uongofu anayoiridhia Allah (s.w.) ambayo ndiyo pekee yenye kumuwezesha kupata furaha na amani katika maisha yake hapa ulimwenguni pasina na kumtii Mtume wa Allah (s.w.). Qur'an inatubainisha:

مَنْ يُطِيعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ اللَّهَ ..... ﴿٨٠﴾

*Mwenye kumtii Mtume amemtii Allah...". (4:80)*

قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ  
وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٨١﴾ قُلْ أَطِيعُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَإِنْ تَوَلَّوْا فَإِنَّ اللَّهَ  
لَا يُحِبُّ الْكٰفِرِينَ ﴿٨٢﴾

*Sema (ewe Muhammad): ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuatani (hapo) Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakughufirieni dhambi zenu. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye maghfira mwenye rehema. Sema: Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume (wake). Na kama mkikengeuka (Mwenyezi Mungu atakutieni adabu). Kwani Mwenyezi Mungu hawapendi Makafiri. (3:31-32)*

## Masharti ya Kuwatii Viongozi (Ulul-amri)

Viongozi au wenye mamlaka (*Ulul-amr*) waliokusudiwa katika Qur'an (4:59) ni viongozi wa aina zote na wa ngazi zote katika fani zote za jamii ambao huielekeza na kuiongoza jamii kwenye kuliendea lengo la maisha. Qur'an

haituamrishi kumtii kila kiongozi au kila mwenye mamlaka juu yetu kwa sababu si kila kiongozi anawaongoza vyema walio chini yake na kuwaelekeza kwenye kufikia lengo la maisha yao. Kuna viongozi wengine wanawatoa watu wao kwenye maisha ya furaha na amani na kuwatumbukiza kwenye maisha ya matatizo na huzuni. Viongozi tunaoamrisha na Allah (s.w.) kuwa tuwatii ni wale tu Waislamu ambao ni wacha Mungu wanaoongoza kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah. Viongozi hawa tulioamrisha kuwatii hawako juu ya sheria bali nao wako sawa na wale wanaoawaongoza. Wako tayari kukosolewa na kurejeshwa kwenye Qur'an na Sunnah endapo watateleza kidogo katika kufanyakazi yao. Viongozi wa namna hii ndio pekee tunaoamrisha tuwatii kwani ndio pekee wanaotuoongoza katika njia iliyonyooka:

اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ ءَامَنُوا يُخْرِجُهُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ ..... ﴿٢٥٧﴾

*Mwenyezi Mungu ni mlinzi (kiongozi) wa wale walioamini Huwatoa katika giza na kuwaingiza katika nuru..... (2:257)*

Kinyume chake, Waislamu tumeamrisha tusiwatii viongozi wanaoongoza kwa miongozo mingine kinyume na Qur'an na Sunnah. Inasisitizwa katika Qur'an:

وَلَا تُطِيعِ الْكٰفِرِيْنَ وَالْمُنٰفِقِيْنَ وَدَعِ اٰذْنَهُمْ وَتَوَكَّلْ عَلٰى اللّٰهِ وَكَفٰى  
بِاللّٰهِ وَكِيلًا ﴿٤٨﴾

*Na usiwatii makafiri na wanafiki wala usijali udhia wao, na mtegemee Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa mlinzi. (33:48)*

..... وَلَا تُطِيعِ مَنْ اَغْفَلْنَا قَلْبَهُ عَنْ ذِكْرِنَا وَاتَّبَعَ هَوٰىهُ وَكَانَ اٰمْرُهُ

﴿٢٨﴾ فُرطًا

*“...Wala usiwatii wale ambao tumezighafilisha nyoyo zao wakafuata matamania yao, na mambo yao yakawa yamepita mipaka (yaani makafiri). (18:28)*

Tukiwatii viongozi hawa kinyume na mwongozo wa Allah (s.w.) tutakuwa tumewafanya miungu yetu na kuangukia kwenye shirk. Tumekatazwa kuwatii hawa kwa sababu watatuelekeza kwenye maovu na kuacha maadili mema ili tu wakidhi matashi ya nafsi zao.



وَإِنْ جَاهَدَاكَ عَلَىٰ أَنْ تُشْرِكَ بِي مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ فَلَا تُطِعْهُمَا  
 وَصَاحِبُهُمَا فِي الدُّنْيَا مَعْرُوفًا ۗ وَاتَّبِعْ سَبِيلَ مَنْ أَنْابَ إِلَيَّ ۗ ثُمَّ إِلَيَّ  
 مَرْجِعُكُمْ فَأُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٥﴾

*Na (wazazi wako) wakikushurutisha kunishirikisha na (yale) ambayo huna elimu nayo, usiwatii lakini kaa nao kwa wema hapa duniani. Shika njia ya wale wanaoelekea kwangu kisha marejeo yenu ni kwangu, hapo nitakuambieni mliyokuwa mkiyatenda. (31: 15)*

Pia Mtume(s.a.w.) ametukataza kuwatii viongozi wanaotuelekeza kwenye uovu kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Ibn Umar (r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a. w.) amesema: Muislamu analazimika kumsikiliza na kumtii kiongozi kwa lolote lile atakalomuamrisha, likiwa linampendeza au linamchukiza alimradi hamuamrishi kufanya kitendo kiovu. Atakapo amrishwa kufanya kitendo kiovu, hakuna kumsikiliza wala kumtii” (Bukhaary na Muslim) Ali (r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a. w.) amesema:Hapana utii kwenye uovu (dhambi). Hakika utii ni wa matendo mazuri tu” (Bukhaary na Muslim)*

Tukiwatii viongozi hawa watatutoa kwenye maisha ya nuru, wema na uadilifu na kutuingiza kwenye maisha ya giza la uovu na utapeli ambayo daima huidumaza na kuihilikisha jamii. Allah (s.w.) anatumabahisha kwa kusema:

..... وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَوْلِيَاؤُهُمُ الطَّاغُوتُ يُخْرِجُونَهُمْ مِنَ النُّورِ  
 إِلَى الظُّلُمَاتِ ۗ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۗ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٥٧﴾

*“..... Na waliokufuru walinzi (viongozi) wao ni Matwaghuti (wachupaji mipaka ya Allah). Huwatoa katika nuru na kuwaingiza katika giza. Hao ndio watu wa motoni, humo watakaa milele. “ (2:257)*

Matwaghuti ni wachupaji mipaka ya Allah (s.w.). Wale wote wanaoiongoza jamii kwa miongozo inayochupa mipaka ya Allah (s.w.) au inayopingana na Qur'an na Sunnah. Pia Allah (s.w.) anawatanabahisha Waislamu juu ya viongozi hawa walio kataa mwongozo wake:

..... وَلَا يَزَالُونَ يُقَبِّلُونَكُمْ حَتَّىٰ يَرُدُّوكُمْ عَن دِينِكُمْ إِنِ اسْتَطَعُوا<sup>ط</sup>  
 وَمَنْ يَرْتَدِدْ مِنْكُمْ عَن دِينِهِ ۖ فَيْمُتْ وَهُوَ كَافِرٌ فَأُولَٰئِكَ حَبِطَتْ<sup>ع</sup>  
 أَعْمَالُهُمْ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ<sup>ط</sup> وَأُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۗ هُمْ فِيهَا<sup>ط</sup>  
 خَالِدُونَ ﴿٢١٧﴾

“Wala (Makafiri) hawataacha kupigana nanyi mpaka wakutoeni katika dini yenu kama wakiveza. Na watakaotoka katika dini yao katika nyinyi, kisha wakafa hali ya kuwa makafiri, basi hao ndio ambao amali zao zimeharibika katika dunia na Akhera. Na ndio watu wa Motoni; humo watakaa milele” (2:217)

Ni haramu kwa Waislamu wa kweli kweli kumtii yeyote kinyume na Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Kumtii yeyote kinyume na Allah (s.w.) ni kumfanya huyo unayemtii kuwa Mungu wako kama tunavyofahamishwa katika Qur'an:

أَتَّخَذُوا أَحْبَارَهُمْ وَرُهَبَانَهُمْ أَرْبَابًا مِّن دُونِ اللَّهِ ..... ﴿٩٣١﴾

Wamewafanya wanavyuoni wao na watawa wao kuwa ni Miungu badala ya Mwenyezi Mungu..... (9:31)

Katika aya hii Mayahudi na Wakristo wanashutumiwa kuwa waliwafanya viongozi wao Miungu badala ya Allah (s.w.). Mtume (s.a.w.) katika kufafanua aya hii anatufahamisha kuwa Mayahudi na Wakristo hawashutumiwi hivyo kwa kuwaita au kuitakidi kuwa viongozi wao ni Miungu, bali walishutumiwa hivyo kwa kuwa walikuwa wakiwatii kinyume na maamrishi na makatazo ya Allah (s.w.).

## Sifa za Anayestahiki Kuwa Kiongozi

Kiongozi wa Kiislamu hachaguliwi kwa kuomba kura na kuwahonga wapiga kura kama wachaguliwavyo viongozi wa Kitwaghuti. Mtume (s.a.w.) amekataza asichaguliwe kuwa kiongozi yule anayeomba uongozi:

Abdul-Rahman bin Samurah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: “Usiombe uongozi kwa sababu utakapopewa uongozi kwa kuomba utaachiwa peke yako jukumu la uongozi, na kama umepewa bila ya kuomba, utasaidiwa katika uongozi huo” (Bukhaary na Muslim)

Yeye mwenyewe Mtume (s.a.w.) alikataa kuwachagua wale walioomba uongozi miongoni mwa masahaba zake kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Abu Mussa ameeleza: “Tulikwenda kwa Mtume (s.a.w.), mimi pamoja na binamu zangu. Mmoja wao akasema: “Ee Mtume wa Mwenyezi Mungu! Nifanye niwe gavana wa nchi ambamo Allah (s.w.) amekupa mamlaka juu yake. Na yule mwingine naye akamuomba hivyo hivyo. Akasema Mtume wa Allah, “Hatumchagui kwenye uongozi huu yeyote anayeomba wala hachaguliwi yule aliye mroho wa uongozi. “ Katika riwaya nyingine alisema Mtume: “Hatuwachagui kwenye nafasi zetu za uongozi wale wanaotaka uongozi” (Bukhaary na Muslim)*

Muislamu wa kweli anafahamu vyema kuwa uongozi ni amana nzito na mtihani mkubwa. Hawezi kamwe kuomba uongozi, sembuse kuufanyia kampeni na kuununua kwa hongo! Mtume (s.a.w.) anahibitisha hivyo katika Hadith ifuatayo:

*Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: “Utawaona watu hawapendi kabisa kazi ya uongozi mpaka uchaguzi utakapo waangukia (kwa kubebeshwa)”. (Bukhaary na Muslim)*

Katika jamii ya Kiislamu atachaguliwa kuwa kiongozi mtu mwenye sifa zifuatazo:

**Kwanza**, awe Muislamu Mcha-Mungu. Hii ni tabia anayotakiwa asifike nayo kila Muislamu wa kweli. Mcha-Mungu ni yule anayeishi kwa kuchunga mipaka ya Allah (s.w.) kwa kujitahidi kwa jitihada zake zote kufuata maamrisha yote ya Allah (s.w.) na kuacha makatazo Yake yote. Anafanya hivyo kwa sababu anahofia adhabu kali ya Allah (s.w.) isiyo na kifani endapo atatenda kinyume na maamrisha Yake na pia ana matarajio ya kupata radhi ya Allah (s.w.) na malipo makubwa yasiyo na kifani endapo ataishi maisha ya kutii maamrisha Yake yote. Kiongozi Mcha-Mungu kwa vyovyote vile atakuwa muadilifu katika kazi yake.

**Pili**, awe mjuzi wa Qur’an na Sunnah na mwenye ujuzi na uzoefu wa kazi anayotakiwa aifanye katika eneo lake la uongozi. Ujuzi wa kutosha wa Qur’an na Hadith ni muhimu sana kwani ndio mwongozo anaotarajiwa kuutumia katika uongozi wake.

Ujuzi wa kazi ya uongozi ni muhimu pia kwani pamoja na ucha-Mungu wa mtu na ujuzi wa Qur’an na Hadith, hataweza kuongoza vizuri iwapo hana ujuzi na uzoefu wa uongozi. Umuhimu wa sifa ya elimu kuwa nayo kiongozi umebainishwa katika Qur’an, Taluti alipochaguliwa kuwa Mfalme wa Mayahudi:

وَقَالَ لَهُمْ نَبِيُّهُمْ إِنَّ اللَّهَ قَدْ بَعَثَ لَكُمْ طَالُوتَ مَلِكًا قَالُوا أَنَّى يَكُونُ لَهُ الْمَلِكُ عَلَيْنَا وَنَحْنُ أَحَقُّ بِالْمَلِكِ مِنْهُ وَلَمْ يُؤْتَ سَعَةً مِّنَ

أَلْمَالِ قَالَ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَاهُ عَلَيْكُمْ وَزَادَهُ بَسْطَةً فِي الْعِلْمِ وَالْجِسْمِ  
وَاللَّهُ يُؤْتِي مُلْكَهُ مَن يَشَاءُ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٤٧﴾

Na huyo Mtume wao akawaambia: “Mwenyezi Mungu amekuchagulieni Taluti kuwa Mfalme: Wakasema: “Vipi atakuwa na ufalme juu yetu, nahali sisi tumestahiki zaidi kupata ‘ufalme kuliko yeye, naye hakupewa wasaa wa mali?” Akasema: “Mwenyezi Mungu amemchagua juu yenu na amemzidishia wasaa wa elimu na kiwiliwili. Na Mwenyezi Mungu humpa ufalme wake amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye wasaa, Mjuzi”. (2:247)

Tunajifunza kuwa utajiri au nasaba ya mtu siyo vitu vya msingi vya kuangaliwa katika kumchagua kiongozi bali vitu vya msingi vinavyoangaliwa ni uchaji wa mtu na elimu Yake.

**Tatu**, ambayo pia imetajwa katika aya hii ni Siha nzuri na uwezo wa kimwili: Mtu mcha-Mungu, mwenye elimu mwenye siha nzuri na mwili wenye nguvu anastahiki zaidi kuchaguliwa kuwa kiongozi kuliko mtu dhaifu.

**Nne**, ya mtu anayestahiki kuchaguliwa kuwa kiongozi wa Waislamu ni tabia njema. Mtu mwenye tabia njema ni yule anayejitahidi kwa kadri ya uwezo wake kujipamba na vipengele vyote vya tabia njema. Kwa mtazamo mwingine mtu mwenye tabia njema ni yule anayejitahidi kuiga mwenendo wa Mtume (s.a.w.) kama inavyosisitizwa katika Qur’an:

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ  
الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا ﴿٣٣﴾

Bila shaka mnao mfano mwema (ruwaza nzuri) kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho na kumtaja Mwenyezi Mungu sana (33:21)

Na mwenendo wa Mtume ulikuwa ni kufuata Qur’an vilivyo. Allah (s.w.) anamsifu Mtume wake kwa tabia njema aliyokuwa nayo:

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٦٨﴾

Na bila shaka una Tabia njema kabisa (68:4)

Pia Mtume(s.a.w.) amesisitiza ubora wa mtu mwenye tabia njema kwa kusema:

“Mbora wenu ni yule aliyeba mbora kwenu kwa tabia njema”(Bukhaary na Muslim)

Hivyo, mwenye tabia njema kuliko wengine ndiye atakayestahiki kuchaguliwa kuwa kiongozi wa Waislamu.

Hizi ndizo sifa anazotakiwa awe nazo kiongozi wa Kiislamu. Yeyote katika jamii ya Kiislamu atakayekuwa na sifa hizi anastahiki kuwa kiongozi wa watu bila ya kujali nasaba yake, taifa lake, rangi yake, umaarufu wake au wasaa wake wa kimali. Aliowachagua Mtume (s.a.w.) kushika nyadhifa mbalimbali katika uongozi wa serikali ya Kiislamu walikuwa Waislamu wenye tabia njema kweli kweli. Katika uchaguzi wake hakujali nasaba, taifa au rangi. Kwa mfano, alimchagua Bilal (r.a) aliyekuwa Mhabeshi kuwa Muadhini bila ya kujali manung'uniko ya baadhi ya masahaba wake. Pia alichaguliwa Zaid bin Harith ambaye hakuwa na umaarufu wowote miongoni mwa Masahaba wake kuwa Kamanda wa jeshi pamoja na manung'uniko yaliyojitokeza mbele ya Mtume (s.a.w.).

Ikitokea watu wenye sifa hizi za uongozi ni wengi kuliko nafasi za uongozi, wale walio mstari wa mbele na uzoefu wa muda mrefu katika harakati za kuupigania Uislamu watachaguliwa kwanza. Endapo bado watakuwa wengi kuliko nafasi zilizo, watachaguliwa wale wenye umri mkubwa zaidi. Endapo bado watakuwa wengi kuliko mahitaji, itapigwa kura na Waislamu wote, wake kwa waume, na watakaopata kura nyingi zaidi ndio watakaostahiki kuwa viongozi wa jamii.

Mfano mzuri wa kuigwa ni ule wa kuchaguliwa kwa Abu Bakr (r.a.) kuwa Khalifa wa kwanza wa Mtume Muhammad (s.a.w.). Baada ya maafikiano kati ya Answar na Muhajirina kuwa kutokana na uzoefu wa kazi ya kusimamisha dini ya Allah (s.w.), Muhajiriina ndio wachukue nafasi ya Ukhalifa, Abu Bakr alimpendekeza Umar (r.a) au Abu-Ubaidah (r.a.) achaguliwe kuwa Khalifa. Lakini wote wawili walikataa pendekezo hilo na kusema “Hapana, hatuwezi kukutangulia mbele katika jambo hili. Bila shaka wewe ni mbora kuliko Muhajiriina wote (kwa kila kitu). Ulikuwa na Mtume katika pango, Mtume alikuchagua kuongoza swala kwa niaba yake alipokuwa mgonjwa, na swala ndiyo nguzo kubwa ya dini. Ni nani mwingine anayestahiki kuchukua nafasi hii ya Ukhalifa kuliko wewe? Nyoosha mkono wako tukupe “Bai’at”.

Baada ya kiongozi wa Kiislamu kuchaguliwa kwa kufuata utaratibu huu Waislamu hulazimika kutoa ahadi ya utii - Bai’at”. Ahadi hii inafungamana na kiongozi; bali pia ni ahadi kwa Allah (s.w.) kama inavyobainika katika Qur’an:

إِنَّ الَّذِينَ يُبَايِعُونَكَ إِنَّمَا يُبَايِعُونَ اللَّهَ يَدُ اللَّهِ فَوْقَ أَيْدِيهِمْ فَمَنْ نَكَثَ فَإِنَّمَا يَنْكُثُ عَلَىٰ نَفْسِهِ ۗ وَمَنْ أَوْفَىٰ بِمَا عَاهَدَ عَلَيْهِ اللَّهُ فَمَسِيئَتِهِ

أَجْرًا عَظِيمًا ﴿١٠١﴾

*Bila shaka wale waliofungamana nawe, kwa hakika wamefungamana na Mwenyezi Mungu. Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao. Bali avunjaye ahadi amevunja kwa kuidhuru nafsi yake, atekelezaye aliyomuahidi Mwenyezi Mungu; (Mwenyezi Mungu) atamlipa ujira mkubwa. (48:10).*

Amri ya kuwatii viongozi ipo wazi katika Qur'an (4:59). Pia msisitizo wa kuwatii viongozi unapatikana katika Hadithi ifuatayo:

*Abu Hurairah amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Atakayenitii amemtii Allah na atakayeniasi amemuasi Allah; na atakayemtii kiongozi amenitii na atakayemuasi kiongozi ameniasi" (Bukhaary na Muslim)*

Kumpinga kiongozi aliyechaguliwa na watu kwa halali ni katika uasi mkubwa. Yeyote yule anayempinga (anayempiga vita) kiongozi wa halali anayewaongoza watu katika njia ya usawa, anauchu wa madaraka na anataka kuvuruga amani, utulivu na mshikamano wa jamii. Mtu wa namna hii anastahiki kuuawa kwa mujibu wa Hadith zifautazo:

*Urfajah ameeleza kuwa amesikia Mtume (s.a. w.) akasema: "Hivi karibuni patakuwa na upinzani na uasi. Anayetaka kuwagawanya watu walioungana muueni popote pale alipo" (Muslim).*

*Abu Said (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a. w.) amesema: Ahadi ya utii itakapotolewa kwa Makhalfi wawili kwa wakati mmoja, muueni wa pili" (Muslim)*

Hadith zinaonesha uovu wa kupinga uongozi halali unaoendesha mambo kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah. Waislamu hawawajibiki kuwatii na wanaamrisha kutowatii viongozi wanao waongoza kwenye mambo maovu. Katika Khutuba yake ya kwanza baada ya kuchaguliwa kuwa Khalifa wa kwanza wa Mtume (s.a.w.) Abu Bakar (r.a) alisema: "Bila shaka nimechaguliwa kuwa Amir (kiongozi) wenu pamoja na kwamba mimi si mbora kuliko nyinyi. Nisaidieni nikiwa katika njia ya usawa na nikosoeni nikikosea" Waislamu walifanya hivyo. Hawakumchelea kiongozi yeyote aliyechupa mipaka ya uongozi wa Qur'an na Sunnah Waislamu wamekatazwa kuwachagua wanawake na watoto kuchukua nafasi ya uongozi wa juu katika jamii kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Abu Bakar (r.a) ameeleza: Mtume (s.a.w.) alipopata habari kuwa Waajemi wamemfanya binti Mfalme kuwa kiongozi wao alisema (Mtume): Hawatafanikiwa kamwe wanaomchagua mwanamke kuwa kiongozi wao "(Baihaq, Ahamad)*

Uongozi ni jukumu kubwa ambalo watoto na wanawake hawana uwezo wa kulibeba. Historia inashuhudia matatizo yaliyotokea katika jamii mbalimbali zilizotawaliwa na wanawake na watoto. Bila shaka hekima ya watoto kukataliwa kupewa uongozi wa jamii iko wazi kwamba akili zao hazijakomaa kiasi cha

kuweza kubeba dhima kubwa ya uongozi. Wanawake nao kulingana na umbile lao na dhima kubwa waliyo nayo ya uzazi na malezi ya familia, itakuwa ni kuwaonea kwa kuwapachika tena hii dhima ya uongozi wajamii. Hata hivyo wanawake wanawajibika kuwa viongozi wa jumuiya na idara za wanawake na katika kuongoza shughuli zote za huduma zitolewazo kwa wanawake tu.

## Wajibu wa Kiongozi katika Dola ya Kiislamu

Mtume (s.a.w.) ametukumbusha sote kuwa kila mtu ajue kuwa ni kiongozi anayewajibika juu ya wale anaowaongoza na hapana shaka ya kuwepo maulizo ya Allah (s.w.) juu ya uwajibikaji wake juu ya wale anaowaongoza kwa mujibu wa Hadith ifuatayo.

*Abdullah bin Umar (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Kila mmoja ni mchungu (kiongozi) na kila mmoja ataulizwa juu ya wale aliowaongoza. imam(kiongozi wa jamii) ni mchungu wa watu anaowaongoza na ataulizwa juu yao. Mwanamume ni kiongozi wa familia yake na ataulizwa juu ya watu wa familia yake. Mwanamke ni malkia wa nyumba ya mume wake na watoto na ataulizwa juu yao. Mtumishi ni mchungu wa vitu vya mwajiri wake na ataulizwa juu ya vitu hivyo. Sikilizeni! Hakika kila mmoja ni mchungu (kiongozi) na ataulizwa juu ya wale aliowachunga (aliowaongoza)" (Bukhaary na Muslim)*

Katika Hadith hii tunajifunza kuwa kila mtu ni kiongozi na kila kiongozi anao wajibu kwa wale anaowaongoza. Katika kipengele hiki tumejaribu kubainisha wajibu wa viongozi wa Kiislamu kama ifuatavyo:

### 1. Ucha-Mungu

Kiongozi ajitahidi kujikurubisha kwa Allah (s.w.) zaidi kwa kuzidisha swala za (Sunnah), fungua za Sunnah, kutoa sadaqa kwa wingi, kuomba dua na maghfira kwa wingi ili kupata msaada wa Allah (s.w.). Kwani kazi ya uongozi ni nzito mno inayohitajia sana msaada wa Allah (s.w.). Pia kiongozi wa jamii ya Kiislamu anawajibika kuzidisha kusoma Qur'an na Hadith ili aweze kufanya kazi yake kwa kuchunga mipaka ya Qur'an na Sunnah na pia aweze kujipamba na mwenendo mwema uliosisitizwa katika Qur'an na Hadith. Kiongozi wa Kiislamu hana budi kujitahidi kuwa kiigizo kwa ucha-Mungu kwa kutekeleza maamrisha yote ya Allah (s.w.) na kujiepusha na makatazo yake yote. Ucha-Mungu ni zana muhimu sana inayomwezesha kiongozi kutekeleza wajibu wake vilivyo.

### 2. Huruma

Kiongozi awe mnyenyekevu, mpole, mwenye huruma anaye wahurumia wale anaowaongoza na mwenye kuwapendelea lile analolipendelea katika nafsi yake. Kiongozi anatakiwa daima kuwa yeye ni mtumishi wa wale waliomuweka

katika uongozi, awaheshimu kama mtumishi anavyomuheshimu bwana wake. Wakati huo huo, kiongozi anatakiwa ajiweke katika nafasi ya ulezi ambayo hana budi kuwahurumia wale anaowalea. Kiongozi wa Kiislamu daima anatakiwa azingatie usia wa Allah(s.w.) ufuatao:

وَهُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ خَلِيفَةَ الْأَرْضِ وَرَفَعَ بَعْضَكُمْ فَوْقَ بَعْضٍ  
دَرَجَاتٍ لِّيُبْلُوَكُمْ فِي مَا آتَاكُمْ إِنَّ رَبَّكَ سَرِيعُ الْعِقَابِ وَإِنَّهُ لَغَفُورٌ

رَحِيمٌ

*Naye ndiye aliyekujaalieni kuwa Makhaliifa (viongozi) katika ardhi. Na amewanyanyua baadhi yenu juu ya wengine daraja kubwa kubwa ili akufanyieni mtihani kwa hayo aliyokupeni. Hakika Mola wako ni mwepesi wa kuhisabu na hakika yeye ni mwingi wa kusamehe, mwingi wa kurehemu. (6:165)*

Kutokana na aya hii tunajifunza kuwa kiongozi anatakiwa mara zote afahamu kuwa wadhifa wa uongozi alia nao ni mtihani kwake. Allah (s.w.) amemuinua daraja na kumfanya kiongozi juu ya wengine ili kumfanyia mtihani kuwa atashukuru neema hiyo aliyotunukiwa na Mola wake kwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo na kuchunga mipaka ya Allah (s.w.) katika kazi hiyo au atakufuru ajipe uungu kwa kuchupa mipaka ya Allah na kuwageuza watumwa wake wale waliomchagua na kumfanya kiongozi wao. Kiongozi anatakiwa awe msaada na rehema kwa wale anaowaongoza na wala asiwe mzigo na tatizo kwa raia zake hao. Mtume (s.a.w.) kila alipowachagua sahaba zake kuwa viongozi wa mahala mbalimbali daima alikuwa akiwausia kuwa watu wa msaada wenye huruma na upole kwa raia zao.

### 3. Uadilifu

Kiongozi wa Kiislamu anatakiwa awe muadilifu. Kipimo cha kiongozi mzuri ni uadilifu. Kiongozi wa Kiislamu akiwa muadilifu huwa Khalifa wa Allah (s. w.) na akiwa si muadilifu huwa Khalifa wa Shetani. Uadilifu unasisitizwa mno katika Qur' an kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُونُوا قَوَّامِينَ بِالْقِسْطِ شُهَدَاءَ لِلَّهِ وَلَوْ عَلَىٰ  
أَنْفُسِكُمْ أَوِ الْوَالِدِينَ وَالْأَقْرَبِينَ ۚ إِن يَكُنْ غَنِيًّا أَوْ فَقِيرًا ۖ ..... ﴾

*Enyi mlioamini! Kuweni wenye kusimamia uadilifu, mtoao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ijapokuwa ni juu ya nafsi zenu, au wazazi wenu, au jamaa. Akiwa tajiri au masikini..... (4: 135)*



Kiongozi muadilifu ni yule anayechunga haki za watu anaowaongoza. Yeye ni mchungu na mgawaji wa haki. Hana budi kuhakikisha kuwa yeye mwenyewe hachukui haki zake mpaka ahakikishe kuwa kila mtu amepata haki yake.

Mtume(s.a.w.) aliwaamuru wale aliowapa kazi kuwa wasivae kivazi kizuri zaidi kuliko wale wanaowaongoza na wasifunge milango yao wakati watu wanawahitajia haki zao, au wanataka kutoa madukuduku yao.’

Kiongozi wa Kiislamu anatakiwa awe muaminifu na mkweli na asijilimbikizie mali kwa kutumia madaraka yake ya uongozi. Amir au kiongozi wa juu wa Serikali ya Kiislamu anatakiwa achukue mshahara au posho kutoka kwenye mfuko wa serikali (*Baitul-mali*) kiasi kile tu kinachotosheleza mahitaji muhimu ya chakula, mavazi na makazi kwa yeye mwenyewe na familia yake. Kiongozi wa Kiislamu anatakiwa akumbuke daima kuwa uongozi katika Uislamu si kitega uchumi kama ulivyo uongozi wa Kitwaghuti. Mtume Muhammad (s.a.w.) ambaye ndiye kiongozi wa Ummah huu wa mwisho na kiigizo chetu kwa mwenendo na uongozi wake bora, aliishi maisha rahisi.

Abu Bakar(r.a) alichaguliwa kushika uongozi wa Umma wa Kiislamu mara baada ya kutawafu Mtume(s.a.w.), alifuata nyayo za Mtume(s.a.w.) kwa kila kitu. Maisha Yake yalikuwa rahisi mno. Umar(r.a) aliyechaguliwa kuwa kiongozi wa serikali ya Kiislamu baada ya Abu Bakar alifuata vyema nyayo za uongozi wa Mtume(s.a.w.) na ule wa Abu Bakar. Pamoja na kuwa Umar alikuwa kiongozi wa Dola kubwa ya Kiislamu iliyoenea mashariki ya kati yote na kupanuka hadi Spain, aliishi maisha rahisi sana.

Umar(r.a) alikuwa na kawaida ya kuzunguka usiku ili kujua matatizo ya watu wake. Siku moja katika mizunguko yake alimkuta mama mmoja porini na watoto wake wanalia. Umar (r.a) alipomuuliza kwanini wako pale alimjibu kuwa giza la usiku na baridi kali imewafanya walazimike kulala pale. Alipomuuliza kwanini watoto wanalia, alimjibu kuwa wananjaa. Umar(r.a) aliondoka mbio mpaka kwenye ghala ya Baitul-mali na kuchukua mgongoni mwake gunia la unga wa ngano na mafuta ya kupikia mpaka kwa yule mama. Umar(r.a) alisaidiana naye kupika na baada ya chakula kuiva aliwaamsha watoto na kuwalisha ndipo akarejea nyumbani kwake. Matukio ya aina hii yako mengi katika historia ya ukhalifa wa Umar bin Khattab(r.a)..

Kinyume chake viongozi wa Kitwaghuti, huchukua madaraka ya uongozi wanayopewa na jamii zao kama kitega uchumi chao kwa ajili ya kujinufaisha wao binafsi. Huifuja watakavyo na humpa yeyote wamtakaye kwa upendeleo mali ya jamii ambayo imepatikana kwa kukung’uta mifuko ya masikini. Muda mfupi baada ya kiongozi wa Kitwaghuti kukabidhiwa madaraka ya uongozi wa ngazi ya juu katika jamii, utamuona ana gari zuri jipya, ana nyumba nzuri mpya, na mabadiliko ya kila namna katika matumizi yake ya kimaisha pamoja na familia yake.

Kama mambo yenyewe ni haya, kwa nini watu wengine katika jamii ya Kitwaghutii wasiupupie uongozi kwa hali na mali au kwa kufa na kupona? Kwa nini mtu aliyeonja uongozi katika serikali ya Kitwaghuti asing'ang'anie kubakia humo kwa gharama yoyote ile?

Kwa nini mapinduzi ya mara kwa mara na mauaji yasitegemewe katika jamii za Kitwaghuti ambapo watu wanashindania uongozi kwa lengo la kujinufaisha wao binafsi? Haya yote ni matunda machungu yanayotarajiwa katika jamii kutokana na uongozi uliokosa uadilifu.

Kiongozi muadilifu hana budi kuhakikisha kuwa wanyonge katika jamii wanapata haki zao na wenye mali wanatoa haki za wanyonge. Abu Bakar, katika khutuba yake ya kwanza baada ya kuchaguliwa kuwa Khalifa wa kwanza wa Mtume (s.a.w.) alisisitiza:

*“Mnyonge miongoni mwenu ni mwenye nguvu katika uongozi wangu mpaka apate haki zake; na mwenye nguvu miongoni mwenu atakuwa dhaiifu katika uongozi wangu, mpaka akipenda Allah nichukue haki za watu anazodaiwa...”*

Vile vile ni katika uadilifu kwa kiongozi kuhakikisha kuwa kila mtu mkosaji anahukumiwa kwa mujibu wa sheria bila ya upendeleo au uonevu wowote. Kiongozi hatamchelea yeyote katika kupitisha hukumu. Katika Uislamu watu wote ni sawa mbele ya sheria na hakuna aliye juu ya sheria hata akiwa Amir (Rais) wa nchi.

#### **4. Subira**

Kiongozi katika dola ya Kiislamu anatakiwa awe mwenye subira, mvumilivu na mstahimilivu. Kiongozi atekeleze wajibu wake ipasavyo na asitarajiwe kupendwa na kufurahiwa na watu wote. Waumini wa kweli tu ndio watakaomfurahia na kumsaidia atakapowaongoza kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah. Lakini wanafiki, wenye husda, wapenda vyeo na sifa na maadui wote wa Uislamu hawawezi kamwe kumfurahia kiongozi wa Kiislamu.

Kiongozi wa Kiislamu hana budi kukumbuka kuwa anafanya kazi ile ile ya Mtume (s.a.w.). Arejee historia ajikumbushe maudhi na vitimbi vya kila namna alivyofanyiwa Mtume wa Allah na makafiri wa Makkah na Mayahudi na wanafiki wa Madina. Kisha katika uongozi wake anapokumbana na matatizo ya kutukanwa, kusingiziwa, kuupuzwa n.k. ajiulize: “Je haya yaliyonifikia yanaweza kulinganishwa na yale yaliyomfikia Mtume wa Allah”.

Pia kiongozi wa Kiislamu anayejitahidi kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah, hana budi kukumbuka kuwa malipo ya kazi yake yapo kwa Allah (s.w.) na ndiye pekee anayewajibika kumuogopa na kutaka radhi yake.

## Vyombo vya Dola katika Uislamu

Malengo ya vyombo vya dola (*State machineries*) katika dola ya Kiislamu yanatofautiana na yale ya serikali za Kitwaghutii. Vyombo kama usalama, polisi, mahakama, magereza n.k., vipo katika dola zote tofauti ni malengo ya kazi na majina. Katika dola ya Kiislamu, jeshi la polisi kwa mfano, kazi yake ni kuamrisha mema na kukataza maovu na vile vile kuwakamata wale wote wanaofanya uhalifu:

وَلْتَكُنْ مِنْكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى الْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ  
الْمُنْكَرِ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿١٠٤﴾

*Na wawepo katika nyinyi watu wanaolingania kheri na wanaoamrisha mema na wakataza maovu. Hao ndio watakaotengenekewa “ (3:104)*

Magereza hali kadhalika, kazi zake si kuwaadhibu tu wahalifu bali kurekebisha tabia na mienendo yao ili wanapotoka magerezani wawe raia wema na wajute kwa makosa yao ya awali.

Kinyume na Uislamu, vyombo vya dola za Kitwaghuti malengo yake ni kama tulivyokwishaona huko nyuma, ni mabavu na kulinda maslahi ya walio madarakani. Huwaonea raia badala ya kuwasaidia, aidha badala yake kurekebisha mienendo ya wakosefu huwafanya wazame zaidi katika uhalifu, bali vyombo hivyo hufanya ukandamizaji na dhulma kwa raia. Hivyo vyombo vya dola ya Kiislamu malengo yake ni tofauti kabisa na yale ya serikali za Kitwaghuuti.

## Demokrasia katika Dola ya Kiislamu

Pamoja na kuwepo uhuru kamili wa kuchagua viongozi kushiriki katika maamuzi ya kisiasa, kushiriki katika kuamrisha mema na kukataza maovu ili kuhakikisha kuwepo kwa amani na utulivu, dola ya Kiislamu si ya kidemokrasia kwa mtazamo wa kitwaghuti. Maana ya serikali ya kidemokrasia kwa mtazamo wa kitwaghutii ni “*Serikali ya watu inayoongozwa na watu kwa manufaa ya watu.*”

Hivyo, watu kwa mtazamo wa kitwaghuti, ndio wenye kauli au mamlaka ya mwisho. Katika Uislamu mamlaka yote ni ya Allah(s.w) pekee. Viongozi na watu wote wanatakiwa wajisalimishe chini ya sheria na amri za Allah(s.w). Katika dola ya Kiislamu hapana sera ya “wengi wape” hata kama ni kinyume na haki.

Katika Uislamu “*haki*” itabakia haki hata kama imefuatwa na mtu mmoja au watu wachache (minority) na “*dhuluma*” au “*batil*” itabakia kuwa hivyo hata kama imesimamiwa au imeungwa mkono na watu wengi (majority).

### Tafauti ya Serikali ya Kiislamu na ile ya kidemokrasia

Serikali ya Kiislamu	Serikali ya kidemokrasia
1. Watu wote wako chini ya Ufalme au utawala wa Allah (s.w.) na kila mtu ameku sudiwa awe Khalifa, wa Allah (s.w.) katika kusimamisha ufalme wake hapa ulimwenguni.	1. Ufalme au utawala uko chini ya watu walio wengi ( <i>popular sovereignty</i> ).
2. Itikadi na sheria zinatoka kwa Allah (s.w.) kupitia kwa Mitume wake. Kila Muislamu anawajibika kutii sheria za Allah na kutii maelekezo ya Mtume. Hakuna aliye juu ya sheria wote wanahukumiwa sawa.	2. Itikadi, sheria na sera hutungwa na Wananchi au wawakilishi wao katika bunge au kamati za vyama. Na kiongozi wa juu wa nchi (Rais) amepewa madaraka makubwa ya kuwa juu ya sheria.
3. Dola ya Kiislamu iko kwa madhumuni ya kusimamisha ufalme wa Allah na kutafuta radhi yake.	3. Madhumuni ya serikali ni kutosheleza mahitaji na matashi ya raia “walio wengi”.
4. Kwa ujumla Dola ya Kiislamu iko chini ya mamlaka ya Allah (s.w.) na Mtume wake, na huendesha mambo yake kwa kuchunga barabara mipaka ya Allah (s.w.) na Mtume wake.	4. Dola ya kidemokrasia ina mamlaka ya mwisho na uhuru wa kuendesha mambo bila ya kuwa na yeyote aliye juu yake.

### Serikali ya Kiislamu ni ya Ki-khalifa

Umma wote wa Kislamu unashika nafasi ya ukhalifa wa Allah(s.w). Yaani umma wote wa Kiislamu unamwakilisha Allah(s.w) katika kusimamisha ufalme wake hapa ulimwenguni kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي  
الْأَرْضِ كَمَا أَستَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي

أَرْضَىٰ هُمْ وَلِيَبَدِّلَهُمْ مِّنْ بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي  
شَيْئًا ۗ وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٥٥﴾

*Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa Atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale waliokuwako kabla yao, na kwa yakini Atawasimamishia dini yao aliyowapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu, hawanishirikishi na chochote. Na watakaokufuru baada ya hayo; basi hao ndio wavunjao amri zenu. (24:55)*

Hivyo, kila mmoja anayo haki na anayo mamlaka ya kuiongoza jamii chini ya ufalme wa Allah(s.w). Kiongozi wa nchi, japo amechaguliwa na watu hana mamlaka ya kujiamulia mwenyewe mambo ya jamii. Bali uamuzi wa mwisho utapitishwa na Majlis Shura (Bunge) yenye wajumbe waliochaguliwa na watu kutokana na watu wacha-Mungu, ili wawakilishe mawazo yao kwa niaba yao. Kushauriana katika kuiongoza jamii kunasisitizwa katika Qur-an kuwa ni miongoni mwa matendo mema ya jamii yatakayo iwezesha kufaulu:

وَالَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِرَبِّهِمْ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَأَمْرُهُمْ شُورَىٰ بَيْنَهُمْ وَمِمَّا  
رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ ﴿٣٨﴾

*Na wale waliomuitikia Mola wao (kwa kila amri zake) na wakasimamisha swala na wanashauriana katika mambo yao na wanatoa katika yale tuliyowaruzuku. (42:38).*

Pia Mtume(s.a.w) (na kwa hiyo viongozi wote) anaamrisha na Mola wake:

..... وَشَاوَرَهُمْ فِي الْأَمْرِ ۗ فَإِذَا عَزَمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ  
الْمُتَوَكِّلِينَ ﴿١٥٩﴾

*“... Na ushauriane nao katika mambo. Na ufungapo nia mtegemee Mwenyezi Mungu (kisha ufanye hilo ulilo azimia bila kurudia nyuma). Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wamtegemeao.” (3:159)*

Baada ya Waislamu kuamua jambo katika Shura yao, ambalo liko katika mipaka ya Allah(s.w) na Mtume wake, hawana budi kutegemeza mafanikio yake kwa Allah(s.w) na kuanza kulitekeleza kwa umoja pasi na kurudi nyuma. Kiongozi wa Dola na viongozi wengine walio chini yake, kazi yao itakuwa kusimamia utekelezaji, wao wenyewe wakiwa mfano bora, katika kutekeleza

yale yaliyoamuliwa na Majlis Shura. Endapo kiongozi atafanya kinyume na maamuzi ya Shura, Umma unayo haki ya kumkatalia. Tujikumbushe tena maneno ya Abu bakar (r.a) katika khutuba yake ya kwanza baada ya kuchaguliwa kuwa Amir wa Waislamu:

*“Bila shaka mmeshanichagua kuwa Amir wenu japokuwa mimi si mbora kuliko nyinyi. Nisaidieni nikiwa katika njia ya sawa na nikosoeni nitakapokuwa nina kwenda vibaya”.*

Katika Dola ya kikalifa viongozi na wanaoongozwa wote wana nafasi sawa ya ukhalifa. Hivyo wananchi pamoja na kuwa na uhuru wa kutoa mawazo yao pia wana uhuru kamili wa kuwakosoa viongozi wao na kudai haki zao kutoka hata kwa Amir mkuu (Rais) wa nchi. Mfano mzuri wa uhuru wa kukosoa viongozi tumeupata katika uongozi wa Umar bin Khattab (r.a). Umar hakufurahishwa na tabia ya wanawake iliyozuka ya kudai mahari kiasi kikubwa sana. Hivyo akaamua kuikomesha tabia hiyo. Akasimama katika mimbari msikitini na kuamuru kuwa kuanzia wakati ule mahari isivuke dirhamu 400. Na mwanamke atakaye dai mahari yaliyozidi kiasi hicho, ziada yote itachukuliwa na kutiwa katika Baitul Maali (hazina ya dola ya Kiislamu). Papo hapo akasimama mwanamke mmoja akasema:

*“Yaa Umar! Laisa laka ahalika”. Yaani “Ewe Umar! Huna mamlaka ya hilo”. Akamkumbusha aya ya Qur-an:*

وَإِنْ أَرَدْتُمْ أَنْ تَبْدِلَ زَوْجَ مَكَانِ زَوْجٍ وَأَنْتُمْ إِحْدَاهُنَّ قِطَارًا  
فَلَا تَأْخُذُوا مِنْهُ شَيْئًا أَتَأْخُذُونَهُ بِهْتِنًا وَإِنَّمَا مِيِّنًا

*Na kama mkitaka kubadilisha mke mahali pa mke, (yaani: kumwoa mke mwingine na kumwacha wa zamani) na hali mmoja wao (naye ndiye huyo atayeachwa) mmempa mrundi (tani) wa mali, basi msichukue chochote. Je, mtachukua kwa dhulma na kwa hatia iliyo wazi? (4:20)*

Aya hii inawakataza wanaume kudai mahari wanapowaacha wake zao hata kama waliwapa mali nyingi. Qintara Maana yake ni tani. Hivyo hata kama mtu ametoa mahari tani za dhahabu. Yule mwanamke akamuuliza Umar: “Kwa msingi gani wewe unataka kuwanyang’anya wanawake haki waliyopewa na Allah(s.w)? Kwa kumjibu, Umar alisema kwa unyenyekevu: “Mwanamke yu sahihi na Umar amekosea”. Na akaifuta kauli yake. Je, kuna uhuru wa kukosoa viongozi uliopita huu?

## Usimamishaji Haki katika Dola ya Kiislamu

Lengo la dola ya Kiislamu sio kutawala bali ni kuhuisha, kudumisha na kuendeleza maadili mema ambayo Allah(s.w) amemtaka mwanadamu ajipambe

kwayo; na kuzuia na kukomesha maovu ambayo Allah(s.w) amemuamrisha mwanadamu ajitenge nayo. Yaani lengo la Dola ya Kiislamu ni kuhuisha, kudumisha na kuendeleza maadili mema ambayo huwapelekea watu katika jamii kuishi kwa furaha na amani. Na papo hapo dola ya kiismau iko pale kuzuia na kukomesha maovu ambayo huleta vurugu, mashaka na huzuni katika jamii. Furaha na amani inapatikana katika jamii iwapo haki inasimamishwa na udhalimu unatokomezwa. Lengo hili linaelezwa vyema katika aya ifuatayo:

الَّذِينَ إِن مَّكَّنْتُمْ فِي الْأَرْضِ أَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ وَأَمْرُوهُمُ  
بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَوْا عَنِ الْمُنْكَرِ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالْأُمُورِ ﴿٤١﴾

*Wale ambao tukiwamakinisha (tukiwapa madaraka) katika ardhi husimamisha swala na wakatoa Zakat na wakaamrisha yaliyo mema na wakakataza yaliyo mabaya, na marejeo ya mambo ni kwa Mwenyezi Mungu. (22:41).*

Uislamu ni Dini ya Haki na Serikali yake iko pale kusimamisha haki kama tunavyojifunza katika Qur-an:

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِأَهْدَىٰ دِينٍ آخِرٍ لِّيُظَهِّرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ  
وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٦١﴾

*Eye (Allah(s.w) ndiye aliyemtuma Mtume wake kwa uongofu na kwa Dini ya Haki ili kufanya ishinde dini zote ijapokuwa washirikina watachukia. (61:9)*

Uislamu ni Dini ya Haki kwa kuwa ni utaratibu wa maisha uliowekwa na Mwenyezi Mungu kupitia kwa Mitume wake. Pia ni dini inayo simamia haki za binadamu. Hawi Muislamu wa kweli yule asiyechungu haki za wengine, kuwasia wengine kusimamisha haki na kuwasaidia wengine kwa hali na mali kupata haki zao. Katika Suratul Asr, Allah(s.w) anatumia haki kuwa wanadamu wako hasarani katika maisha ya duniani na akhera ila wale watakao muamini Allah na vipengele vyote vya nguzo za imani na kufanya matendo mema, na kusimamisha haki na kufanya subira ili kubakia katika haki. Kilicho iwezesha Dola ya Kiislamu wakati wa Mtume(s.a.w) na Makhalifa wane kuwa juu ya dola zote za ulimwenguni ni msimamo wake wa kusimamisha haki katika jamii kwa hali na mali.

Waislamu hawakupigana vita vyovyote ili kuwaingiza kwa nguvu watu katika Uislamu kama wanavyodai maadui wa Uislamu, bali walipigana na makabila na mataifa mbali mbali ili kutokomeza dhulma na unyonyaji wa kila aina ulioshamirishwa na watawala na kusimamisha haki kwa kuwaondoa

watawala wanyonyaji na kuwaweka viongozi wa Kiislamu waliokuwa watumwa wa Allah(s.w) pekee na watumishi halisi wa watu walio waongoza. Kiongozi wa watu kuwa na ulinzi mkali au “Body-Guard” ni jambo lisiloelekewa katika mtazamo wa uongozi wa Kiislamu.

Katika dola ya Kiislamu haki za mwanadamu zimezingatiwa kwa ukamilifu na hakuna mfano wake unaopatikana katika dola yoyote ya kitwaghutii. Dola ya Kiislamu imezigawanya haki za binadamu katika mbeaya tatu:

- (a) Haki zinazomstahiki kila mwanadamu.
- (b) Haki zinazowastahiki raia katika dola ya Kiislamu.
- (c) Haki zinazowastahiki wasio kuwa Waislamu katika dola ya Kiislamu.

## Haki Zinazomstahiki Kila Mwanadamu

Ni jukumu la dola ya Kiislamu kusimamia na kuhakikisha kuwa kila mwanadamu awe Muislamu au asiwe Muislamu, awe raia au mgeni katika dola ya Kiislamu, anapata haki zifuatazo:

### (i)Haki ya Kuishi

Kila mtu pasina ubaguzi wa aina yoyote ana haki ya kuishi na kulindiwa maisha yake. Kumuuua mtu yeyote awaye ni kosa la jinai na muuaji ni lazima ahukumiwe kwa sheria ya Kiislamu. Makemeo ya Qur-an kuhusu kosa hili yanadhahirisha kwa uwazi ubaya wa kuua mtu yoyote pasi na haki:

..... مَنْ قَتَلَ نَفْسًا بِغَيْرِ نَفْسٍ أَوْ فَسَادٍ فِي الْأَرْضِ فَكَأَنَّمَا قَتَلَ

النَّاسَ جَمِيعًا ..... ﴿١٧﴾

*Kwa sababu ya hayo tukawaandikia wana wa israil ya kwamba atakayemuua mtu bila ya yeye kuua mtu, au bila ya kufanya fisadi katika nchi, basi ni kama amewaua watu wote...” (5:32)*

..... وَلَا تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ ..... ﴿١٧﴾

*“... Wala msimuu mtu ambaye Mwenyezi Mungu ameharamisha (kuuwa) la ikiwa (imetokea) haki (ya kuuawa)...” (6:151)*



Hukumu ya muuaji ni kuuawa kama inavyobainishwa katika Qur-an:

وَلَا تَقْتُلُوا أَنْفُسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ ۗ وَمَنْ قُتِلَ مَظْلُومًا فَقَدْ جَعَلْنَا لَوْلِيَّهِ سُلْطٰنًا فَلَا يُسْرِفُ فِي الْقَتْلِ ۗ إِنَّهُ كَانَ مَنصُورًا ﴿٣١﴾

Wala msiue nafsi ambayo Mwenyezi Mungu ameiharamisha kuuawa isipokuwa kwa haki (Akahukumu hakimu wa Kiislamu kuwa mtu amestahiki kuuawa na akatoa amri ya kuuawa). Na mwenye kuuawa kwa kudhulumiwa, basi tumempa nguvu mrithi wake (juu ya muuaji huyo, akitaka ataomba kwa hakimu kuwa amuue au akitaka amtoze fidia au akitaka amsamehe). (17:33).

### (ii) Haki ya Usalama wa Maisha

Kila mtu katika dola ya Kiislamu anayo haki ya kuokolewa au upate ulinzi utakao muweka katika hali ya usalama bila ubaguzi wa aina yoyote. Tunafahamishwa katika Qur-an kuwa:

..... وَمَنْ أَحْيَاهَا فَكَأَنَّمَا أَحْيَا النَّاسَ جَمِيعًا ۗ ..... ﴿٣٢﴾

“... Na mwenye kumwacha mtu hai (kumsaidia kuishi) ni kama amewaacha hai watu wote...” (5:32).

Katika dola ya Kiislamu kila mtu awe mgeni au raia ana haki ya kupata mahitajio muhimu ya maisha yatakayomuwezesha kuishi na kila mtu anayo haki ya kupata hifadhi itakayomuhakikishia kuishi kwa usalama.

### (iii) Kuheshimu Utoharifu (Utakaso) wa Mwanamke

Dola ya Kiislamu inalojukumu la kuhakikisha kuwa kila mwanamke anapata hifadhi ya kutoguswa na mwanamume yoyote awaye nje ya utaratibu wa ndoa. Kitendo cha zinaa au kishawishi chochote cha zinaa kimekatazwa katika Uislamu bila ya kujali kuwa kimefanywa na Muislamu au na asiye kuwa Muislamu au kimefanywa na raia au mgeni wa Dola ya Kiislamu. Makemeo ya Qur-an juu ya kitendo hiki ni haya yafuatayo:

وَلَا تَقْرُبُوا الزُّنَىٰ ۗ إِنَّهُ كَانَ فَحِشَةً وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿٣٣﴾

Wala msikaribie zinaa. Hakika hiyo ni uchafu na ni njia mbaya kabisa. (17:32).

Uzinifu katika Uislamu ni kosa la jinai, na mzinifu yeyote anastahiki adhabu kali ya kupigwa viboko mia moja (Qur-an, 24:2) au kupondwa mawe mpaka kufa bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

**(iv) Haki ya Heshima**

Uislamu unatuamrisha kuwaheshimu wanadamu na kuwathamini pasi na ubaguzi wowote na unatukataza kufanya jambo lolote litakalotupelekea kuwavunjia heshima. Tunaamrisha katika Qur-an kuwa:

..... وَلَا تَلْمِزُوا أَنْفُسَكُمْ وَلَا تَنَابَزُوا بِالْأَلْقَابِ ..... ط

...Wala msitukanane kwa kabila, wala msiitane majina mabaya...(49:11)

Ni jukumu la dola ya Kiislamu kuhakikisha kuwa kila mtu anaheshimika bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

**(v) Haki ya Uhuru**

Ni jukumu la dola ya Kiislamu kuhakikisha kuwa mtu anakuwa huru na hawi mtumwa wa mwingine kimabavu au kifikra. Inasikitisha kuwa maadui wa Uislamu wanaunasibisha Uislamu na biashara ya watumwa. Wameunasibisha Uislamu na utumwa kwa kuwa eti walioonekana kuhusika na biashara hiyo hapa Afrika ya Mashariki ni waarabu. Wengi wa watu wasiokuwa Waislamu na hata baadhi ya Waislamu wasiojua vyema dini yao, wameuelewa Uislamu kuwa ni dini ya Waarabu. Hivyo kwa mtazamo wao huu, kila mwarabu ni Muislamu na kila alichokifanya Mwarabu kiwe kibaya au kizuri ni kitendo cha Kiislamu. Mtazamo huu ni mtazamo potofu. Uislamu ni Dini ya Allah(s.w) isiyo na ubaguzi wa aina yoyote. Uislamu ni dini ya walimwengu wote wa nyakati zote na wamataifa yote. Wote walioikubali dini hii ni ndugu (Qur-an 49:10) na Uislamu hautambui ubaguzi wowote katika mgawanyo wa haki za binadamu.

Uislamu umekomesha utumwa wa fikra na mawazo, kwa kuwahimiza waumini wake wawe watumwa wa Allah(s.w) peke yake kwa kujinyenyekesha kwake kwa utii na kufuata vilivyo mwongozo wa maisha alio mfunulia mwanadamu kupitia kwa Mitume wake.

Uislamu umekomesha utumwa uliokuwepo wakati wa ujahili kwa kuwahimiza Waislamu watumie mali zao kuwakomboa watumwa na katika Zakat limewekwa fungu maalumu la kuwagomboa watumwa. Katika historia ya Uislamu tunajifunza kuwa Mtume Muhammad(s.a.w) mwenyewe aliwagomboa watumwa 63 na kuwaachia huru. Mkewe Bi Aysha (r.a) aligomboa watumwa 67, Abbas (r.a) aligomboa watumwa watumwa 70, Abdullah bin Umar (r.a) aligomboa watumwa 1000, Abdur-Rahman (r.a) aliwagomboa watumwa 30,000 na maswhaba wengine wa Mtume(s.a.w) waliwagomboa watumwa mamia kwa mamia.

Mtume(s.a.w) amekemea vikali kitendo cha kumfanya mtu huru kuwa mtumwa wa mwingine kama tunayojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Kuna watu wa aina tatu ambao mimi mwenyewe nitasimama kuwashitaki katika siku ya hukumu; miongoni mwa hao ni yule anayemfanya mtu huru kuwa mtumwa na kumuza... (Bukhaary, Ibn Majah).*

### **(vi) Usalama na Uhuru wa Mtu binafsi**

Uislamu umeweka utaratibu kwamba, hakuna mtu atakayefungwa mpaka kwanza kosa lake lithibitishwe mbele ya mahakama ya wazi (yenye kushuhudiwa na watu). Kesi za faragha au “IN CAMERA” ni haramu katika Uislamu. Pia ni haramu kumkamata mtu kwa kumshuku tu na kumsukumiza jela bila ya kufuata utaratibu wa Mahakama na bila ya kumpa fursa ya kujitetea. Uadilifu katika kutoa hukumu, bila ubaguzi wa aina yoyote, ni jambo lililosisitizwa mno katika Qur-an:

..... وَإِذَا حَكَمْتُمْ بَيْنَ النَّاسِ أَنْ تَحْكُمُوا بِالْعَدْلِ ..... ﴿٥٨﴾

“... Na mnapohukumu baina ya watu hukumuni kwa uadilifu...” (4:58)

Katika Dola ya Kiislamu hakuna mtu atakayetiwa ndani mipaka ahukumiwe kwa uadilifu, wala hapana yeyote asiye na hatia atakaye adhibiwa au kutiwa ndani kwa makosa ya mwingine au kwa niaba ya mwingine.

### **(vii) Haki ya Kuhukumiwa kwa Uadilifu**

Jukumu kubwa la Dola ya Kiislamu ni kusimamia uadilifu. Kila mtu bila ya kujali dini yake, rangi yake, taifa lake, uraia wake, n.k. anastahiki kuhukumiwa kwa uadilifu. Uadilifu katika kutoa hukumu unasisitizwa mno katika Uislamu kama tunavyojifunza katika Qur-an:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُونُوا قَوْمِينَ لِلَّهِ شُهَدَاءَ بِالْقِسْطِ وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَاٰنُ قَوْمٍ عَلَىٰ ءَلَّا تَعْدِلُوْا ..... ﴿٥٨﴾

*Enyi mlioamini! Kuweni wasimamizi (wa haki) kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, muwe mkitoa shahada kwa uadilifu. Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutowafanyia uadilifu...” (5:8).*

﴿يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُوفُوا قَوْمِينَ بِأَلْقِسِطِ شُهَدَاءَ لِلَّهِ وَلَوْ عَلَىٰ  
 أَنفُسِكُمْ أَوِ الْوَالِدِينَ وَالْأَقْرَبِينَ ۚ إِن يَكُنْ غَنِيًّا أَوْ فَقِيرًا فَاللَّهُ أَوْلَىٰ  
 بِهِمَا ۗ فَلَا تَتَّبِعُوا أَهْوَىٰ أَن تَعْدِلُوا ۗ وَإِن تَلَوْتُمَا أَوْ تَعْرَضُوا ۗ فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ  
 بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ﴿١٣٥﴾

*Enyi mlioamini! Kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mtowao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, ijapokuwa ni juu ya nafsi zenu, au (juu ya) wazazi (wenu) na jamaa (zenu). Akiwa tajiri au masikini. Mwenyezi Mungu anawastahikia zaidi. Basi msifuuate matamania mkaacha kufanya uadilifu. Na kama mkipotoa (ushahidi) au mkijitenga (na kushuhudia, Mwenyezi Mungu atakuadhibuni), na Mwenyezi Mungu anazohabari za yale mnayoyatenda. (4:135).*

#### (viii) Haki ya Usawa wa Binadamu

Uislamu hauruhusu ubaguzi wa kabila, taifa, rangi, hadhi, kipato, ubaguzi wa aina yoyote ile. Tunafahamishwa katika Qur-an:

﴿يَأْتِيهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاهُمْ مِّن ذَكَرٍ وَأُنثَىٰ وَجَعَلْنَاهُمْ شُعُوبًا وَقَبَائِلَ  
 لِتَعَارَفُوا ۗ إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتَقَىٰكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿١٣٥﴾

*Enyi watu! Kwa hakika tumekuumbeni (nyote) kwa (yule) mwanamume (mmoja – Adam) na (yule yule) mwanamke (mmoja Hawa). Na tumekufanyeni mataifa na makabila (mbali mbali) ili mjuane (tu basi). Hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye Mungu zaidi katika nyinyi. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye habari zote. (49:13)*

Mtu hawi bora kwa kuwa ni tajiri, au kuwa na hadhi kubwa katika jamii, au kwa kuwa anatokana na taifa kubwa, bali aliye bora zaidi kuliko wote ni yule mcha-Mungu mwenye tabia njema na utu kwa wanadamu wenziwe. Mtume(s.a.w) katika kuisitiza kwake usawa wa binadamu amesema:

Hapana Mwarabu aliye bora zaidi kuliko asiye Mwarabu, wala asiye Mwarabu si bora zaidi kuliko Mwarabu. Pia mtu mweupe si bora kuliko mweusi, wala mtu

mweusi si bora kuliko mweupe. Wote ni watoto wa Adam na Adam ameumbwa kutokana na udongo (wa mfinyanzi). (Baihaqi na Bazzaaz).

### **(ix) Haki ya uhuru wa mahusiano**

Katika dola ya Kiislamu kila mtu anayo haki ya kujiunga na jumuiya, chama au kikundi chochote katika kuhuisha na kuendeleza mema kwa manufaa yake na manufaa ya jamii kwa ujumla. Pia kila mmoja anayo haki ya kutojiunga au kujitoa kwenye jumuiya au chama au kikundi chochote pindi atakapooona kuwa chama hicho au jumuiya hiyo haina manufaa na wala hainufaishi umma bali huleta fitina na uadui katika jamii. Mwongozo wa kushirikiana na kushikamana umewekwa wazi katika Qur-an:

..... وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَىٰ ۗ وَلَا تَعَاوَنُوا عَلَى الْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ ۗ

وَاتَّقُوا اللَّهَ ۗ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٥٢﴾

*Saidianeni katika wema na ucha-Mungu wala msisaidiane katika dhambi na uadui. Na Mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu. (5:2).*

## **Haki za Raia katika Dola ya Kiislamu**

Pamoja na haki za binadamu wote kwa ujumla zinazotolewa na kusimamiwa na dola ya Kiislamu, kuna zile haki zinazo wahuu raia tu wa Dola wakiwemo Waislamu na wasiokuwa Waislamu. Hapa tutarejea haki za Msingi zifuatazo:

### **(i) Haki ya Kuendesha maisha ya Binafsi**

Uislamu unatoa haki kwa kila raia kuwa asiingiliwe katika maisha yake binafsi maadam haendi kinyume na utaratibu wa kibinadamu. Tunaamrisha wa katika Qur-an kuwa:

..... وَلَا تَجَسَّسُوا ..... ﴿٤٩﴾

“... Wala msipeleleze (habari za watu)...” (49:12).

﴿ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُفُونًا قَوْمِينَ بِالْأَيْدِي شُهَدَاءَ لِلَّهِ وَلَوْ عَلَىٰ

أَنْفُسِكُمْ أَوِ الْوَالِدِينَ وَالْأَقْرَبِينَ ۗ إِنْ يَكُنْ غَنِيًّا أَوْ فَقِيرًا فَاللَّهُ أَوْلَىٰ

بِمَا تَتَّبِعُوا أَهْوَىٰٓ أَن تَعْدِلُوا ۖ وَإِن تَلُودُوا أَوْ تَعْرِضُوا فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ

بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ﴿٢٨﴾

*Enyi mlioamini! Msiingie nyumba ambazo si nyumba zenu mpaka muombe ruhusa (mpige hodi) na muwatolee Salaam waliomo humo. Hayo ni bora kwenu huenda mtakumbuka. Na kama hamtamkuta humo yoyote, basi msiingie mpaka mruhusiwe. Na mkimbiwa “Rudini” basi rudini, hili ni takaso kwenu. Na Mwenyezi Mungu anajua mnyotenda? (24:27 - 28).*

Mtume(s.a.w) amekemea vikali kuchungulia nyumba za watu kiasi cha kusema: Kama mtu atampofua macho au jicho mwenye kuchungulia nyumbani kwake, hatalaumiwa wala hatakuwa na hatia”. Mtume(s.a.w) pia amekataza kusoma barua za watu. Hii ndiyo hifadhi ya maisha ya mtu binafsi inayotolewa na Uislamu. Hifadhi hii haipo katika dola za Kitwaaghuti. Ni mara ngapi twaona barua zikisomwa na kuchukuliwa kopi (photocopy) kwa kisingizio cha usalama wa taifa? Vile vile katika dola za Kitwaaghuti, simu hutegwa katika nyumba za watu ili mazungumzo yao ya siri yajulikane. Kila dola ya kitwaghuti ina askari wa siri wengi ambao kazi zao ni kupeleleza habari za watu.

### **(ii) Haki ya Kupinga Udhalimu**

Dola ya Kiislamu inatoa haki kwa raia wake kupinga, kuonya au kukemea kitendo cha udhalimu kitakachofanywa na dola au viongozi wake. Kila raia katika dola ya Kiislamu anayo haki ya kukosoa serikali au kiongozi wa juu wa seriakli. Umar (r.a) akiwa Amir (Rais) wa dola kubwa ya Kiislamu alikosolewa hadharani na mwanamke alipotaka kuwadhulumu wanawake haki yao waliyopewa na Allah(s.w) ya kupanga kiasi cha mahari wanachokiridhia wao wenyewe. Pale pale mbele ya hadhara ya watu Umar (r.a) alikiri kuwa amekosa na akafuta amri yake.

### **(iii) Haki ya Uhuru wa Kutoa Maoni na Kuamrisha Mema**

Uislamu unatoa uhuru kamili kwa kila raia kutoa maoni yake yanayopelekea kwenye wema. Bali maoni ya kupelekea kwenye maovu, vurugu, fitina na uhasama katika jamii hayapewi nafasi katika Uislamu. Vile vile matumizi ya lugha mbaya ya matusi, dharau na kejeli katika kutoa maoni si jambo linalokubalika katika Uislamu.

Pamoja na kuwa kutoa maoni au mapendekezo katika serikali yanayopelekea kwenye wema ni haki ya kila raia, waumini wanawajibika kuamrisha mema na kukataza maovu katika jamii kama tunavojifunza katika aya zifuatazo:

وَلَتَكُنَّ مِّنكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى الْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿١٤﴾

Na wawepo katika nyinyi watu wanaolingania kheri na wanaoamrisha mema na kukataza maovu. Na hao ndio watakaotengenekeka. (3:104).

وَالْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ يَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ ..... ﴿١٦﴾

Na wanaoamini wanaume na wanaoamini wanawake ni marafiki wao kwa wao. Huyaamrisha yaliyo mema na huyakataza yaliyo mabaya.... (9:71).

Kwa kulinganisha tabia hii ya waumini na ile ya wanafiki Qur-an inatufahamisha:

الْمُنْفِقُونَ وَالْمُنْفِقَاتُ بَعْضُهُمْ مِّنْ بَعْضٍ يَأْمُرُونَ بِالْمُنْكَرِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمَعْرُوفِ ..... ﴿١٧﴾

Wanaume wanafiki na wanawake wanafiki, wote ni hali moja, huamrisha yaliyo mabaya na huyakataza yaliyo mazuri..... (9:67).

Katika kusesitiza wajibu wa Waislamu katika kuamrisha mema na kukataza maovu Mtume(s.a.w) amesema:

“Miongoni mwenu atakayeona ova hana budi kuliondoa kwa mkono wake (kutumia nguvu) iwapo anauwezo, kama hana uwezo wa) kuliondoa kwa mkono wake hana budi kuliondoa kwa ulimi wake (kulikemea); kama hana uwezo huo basi achukie na akilaani kitendo hicho kiovu moyoni mwake. Hali hii ya kuchukua ni kiwango cha chini kabisa cha imani.” (Sahihi Muslim)

#### (iv) Haki ya Uhuru wa Kufuata Dini Yoyote

Dola ya Kiislamu inatoa uhuru kamili kwa raia wake kutumia akili zao na vipaji vyao katika kuchagua dini wanayoiona kuwa ndiyo inayostahiki kufuatawa. Uislamu umekataza watu kushurutishwa kuingia katika dini kama tunavyojifunza katika Qur-an:

لَا إِكْرَاهَ فِي الدِّينِ ۗ قَدْ تَبَيَّنَ الرُّشْدُ مِنَ الْغَيِّ ۚ فَمَنْ يَكْفُرْ بِالطَّاغُوتِ  
 وَيُؤْمِرْ بِاللَّهِ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ لَا انفِصَامَ لَهَا ۗ..... ﴿٢٥٦﴾

*Hakuna kulazimishwa (mtu kuingia) katika dini. Uongofu umekwisha pambanuka na upotofu. Basi anayemkufuru twaghuti na kumwamini Mwenyezi Mungu, bila shaka yeye ameshika kishiko chenye nguvu kisichovunjika... (2:256).*

Waislamu hawaruhusiwi kutumia nguvu yoyote katika kuwaingiza watu katika dini bali wameariwa kuwalingania watu kwenye Dini ya Allah kwa mawaidha mazuri yanayofanana na vitendo vyao na kwa hekima kama tunavyojifunza katika Qur-an:

ادْعُ إِلَى سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحُكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ ۗ وَجِدِلْهُمْ بِالَّتِي هِيَ  
 أَحْسَنُ ۚ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنْ ضَلَّ عَنْ سَبِيلِهِ ۗ وَهُوَ أَعْلَمُ  
 بِالْمُهْتَدِينَ ﴿١٦٥﴾

*Wete (waite watu) katika njia ya Mola wako kwa hikima na mauidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora (siyo kwa kuwatukana wao au kutukana dini yao. Kwa njia hii huwezi kumvuta mtu) Hakika Mola wako ndiye anayemjua aliyepotea katika njia yake. Naye ndiye anayewajua walioongoka. (16:125)*

#### (v) Haki ya Kuabudu

Pamoja na haki ya kufuata dini mtu anayoitaka, Uislamu vile vile umetoa uhuru kamili kwa mtu kufanya lbada ya dini yake apendavyo. Dola ya Kiislamu inajukumu la kuhakikisha kuwa haki hii inapatikana kwa raia zake na inawajibu wa kuhakikisha kuwa lbada na mahali pa kuabudia panaheshimiwa. Tunaonywa katika Qur-an kuwa:

وَلَا تَسُبُّوا الَّذِينَ يَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ فَيَسُبُّوا اللَّهَ عَدْوًا بِغَيْرِ عِلْمٍ ۗ  
 كَذَلِكَ زَيْنًا لِكُلِّ أُمَّةٍ عَمَلُهُمْ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّهِمْ مَرْجِعُهُمْ فَيُنَبِّئُهُمْ بِمَا كَانُوا  
 يَعْمَلُونَ ﴿٣٨﴾



*Wala msiwatukane wale wanaowaabudu kinyume cha Mwenyezi Mungu, wasije wakamtukana Mwenyezi Mungu kwa jeuri zao bila kujua. Namna hivyo tumewapambia kila watu vitendo vyao. Kisha marejeo yatakuwa kwa Mola wao. Naye atawambia (yote) waliyokuwa wakiyatenda. (6:108).*

Ifahamike wazi kuwa Uislamu haumkatazi mtu kuwa na majadiliano juu ya mambo ya dini bali umesisitiza kuwa majadiliano hayo yaendeshwe kwa utaratibu mzuri bila ya kuwa na matukano, kuzozana na vurugu nyinginezo. Mabishano na mizozano imekatanzwa katika Uislamu kama tuavyokumbushwa katika aya ifuatayo:

❖ وَلَا تُجَادِلُوا أَهْلَ الْكِتَابِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ إِلَّا الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْهُمْ وَقُولُوا ءَأَمْنَا بِالَّذِي أَنْزَلَ إِلَيْنَا وَأَنْزَلَ إِلَيْكُمْ وَإِلَهُنَا وَإِلَهُكُمْ

وَاحِدٌ وَنَحْنُ لَهُ مُسْلِمُونَ

*Wala msibishane na watu waliopewa kitabu (kabla yenu) ila kwa yale (majadiliano) yaliyomazuri, isipokuwa wale waliodhulumu miongoni mwao. Na semeni: “Tunaamini yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoteremshwa kwenu, na Mu ngu wetu na Mungu wenu ni mmoja, nasi ni wenye kunyenyekea kwake.” (29:46).*

Amri hii haishii tu kwa watu wa Kitabu (wakristo na Mayahudi) bali ni pamoja na wanaofuata dini nyinginezo.

### **(vi) Haki ya Kuwashitaki Viongozi wa Juu wa Dola**

Katika Dola ya Kiislamu, Wafanyakazi wote wa serikali, akiwa kiongozi wa Dola au mfanyakazi wa kawaida, wote ni sawa mbele ya Sheria. Hakuna yeyote aliye juu ya sheria au asiyeguswa na sheria ya Dola. Raia yeyote katika dola ya Kiislamu anayo haki ya kutoa madai yake au mashitaka yake dhidi ya kiongozi yeyote, hata akiwa Rais wa nchi. Tunao mfano mzuri wa kuiga kwa Mtume wa Allah(s.w) kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Umar (r.a) amesema: Kwa macho yangu nilimuona Mtume(s.a.w) akijilipizia kisasi dhidi yake mwenyewe. Katika vita vya Badr wakati Mtume(s.a.w) alipokuwa akinyoosha mistari ya jeshi la Waislamu alilipiga tumbo la askari mmoja, kwa bahati mbaya, katika kujaribu kumrudisha nyuma katika mstari. Yule askari akalalamika: “Ewe Mtume! Umeniumiza na fimbo yako”. Mtume(s.a.w) pale pale alifunua wazi tumbo lake, akasema: “Samahani sana, unaweza kulipiza kisasi kwa kunifanyia kitendo hicho hicho nilichokufanyia’. Yule askari alitoka mbele na kulibusu tumbo la Mtume(s.a.w) na kusema: “Hicho ndicho nilichokitaka”,*

Mfano mwingine tunaupata katika uongozi wa Umar (la), khalifa wa pili wa Mtume(s.a.w). Wakati wa uongozi wa Umar, Muhammad mtoto wa Amr bin al-'As, Gavana wa Misri alimchapa (kwa maonevu) Mmisri mmoja. Yule Mmisri alifunga safari kwenda Madina kutoa malalamiko (mashtaka) yake kwa Khalifa Umar. Umar aliyapokea mashtaka na kumwita yule Gavana na mtoto wake waende Madina. Walipofika Madina, Khalifa alimpa mjeledi yule mlalamikaji wa Kimisri na akamwambia amtandike yule mtoto wa Gavana mbele yake. Baada ya kulipiza kisasi yule Mmisri alipotaka kurudisha ule mjeledi, Umar alimuamuru "Mtandike Gavana naye kiboko kimoja, kwani mtoto wake asingali kupiga kama si kiburi alichokuwa nacho kutokana na hadhi ya baba yake". Mlalamikaji alijibu: Mtu aliyenipiga nimelipiza kisasi changu kwake. Umar akasema: "Naapa kwa jina la Allah, kama ungalimtandika ('Gavana) nisingalikuzuia kufanya hivyo, umeacha kwa hiari yako mwenyewe". Kisha Khalifa wa Waumini kwa hasira alimgeukia Gavana, na kumkemea. "Ewe Amr, umeanza lini kuwafanya watu watumwa, japo wamezaliwa na mama zao wakiwa huru?"

### *(vii) Haki ya Kuiendesha Dola ya Kiislamu*

Wenye haki kushika hatamu ya uongozi wa dola ya Kiislamu si watu wa cheo Fulani, au wa kabila Fulani, au wa chama fulani, bali ni wale wote wanaomuamini Allah(s.w) ipasavyo na wanaoamini Ukhalifa wa mwanadamu hapa ulimwenguni. Uislamu unatufahamisha kuwa mwanadamu hapa ulimwenguni ni mwakilishi wa Allah(s.w), hivyo utawala wa Dola ya Kiislamu ni lazima ufuate kwa ukamilifu mwongozo wa Allah(s.w) na umshirikishe kila Muislamu kwa njia ya uwakilishi na kushauriana.

## **Haki za Wasiokuwa Waislamu katika Dola ya Kiislamu**

Pamoja na kuona haki zinazotolewa na dola ya Kislamu kwa binadamu wote na kwa raia zake – Waislamu na wasiokuwa Waislamu kama ilivyobainishwa katika vipengele (a) na (b) tunawajibika kubainisha kwa uwazi zaidi haki za wasiokuwa Waislamu katika Dola ya Kiislamu. Kuwajibika kwetu huku kunafuatiwa na kueleweka vibaya madhumuni na shabaha ya Dola ya Kiislamu kwa wasiokuwa Waislamu hasa wakristo, na hata kwa baadhi ya Waislamu wasioielewa dini yao vilivyoo. Kuna shutuma nyingi dhidi ya Dola za Kiislamu zinazotolewa na maadui wa Uislamu, hasa wakristo ambazo zinatoa picha kuwa Uislamu ni dini ya ukatili, inayoleta vurugu na fujo katika jamii. Hebu hapa tuangalie, kama mfano tu wa shutuma hizo, sehemu ya barua ndefu ya Rev. Christopher Mtikila aliyomwandikia Makamu Mwenyekiti, Halimashauri Kuu ya Chama, Dodoma (Tanzania) mnamo 1/2/1988. Katika kuonyesha ubaya wa Uislamu Rev. C. Mtikila amesema:

*“Ubaya sana na hatari kubwa ya siasa ya Islamu kwa wale wanaoifuata kwa kila herufi, ni kule kufika mahali wanapoamua kwamba watu wote ambao si Waislamu (na hasa Wakristo) ni OUTLAWS au “State Criminals”, yaani wahaini*

*au viumbe wasiotakiwa kabisa na Mungu wao na huwaita MAKAFIRI na kadiri wanavyoendelea, ndivyo hekima ya kuwawezesha kuishi na kuchukuliana na jamii zingine alizoziumba Mungu inavyozidi kuwatoka. Asiye kubaliana na Islamu ya jinsi hiyo huwa sasa ni adui, na Islamu hiyo imeletisha mauaji ambayo wahusika kwa kuharibikiwa akili zao eti kuyaita JIHAD pamoja na ukatili wa kinyama ulionao katika SHERIA. Hushindwa kutambua kuwa Mungu wao wa mashindano, chuki, wivu, ugomvi, uadui, mauaji, unyama, uzushi, usharati, husuda n.k. ni TOFAUTI KABISA na Mungu wetu wa ukweli, Upendo, furaha, Amani, Utu wema, Uvumilivu, Fadhili, Uaminifu, Upole na Kiasi! Inabidi ndugu zetu (viongozi Waislamu) mzinduke na kutambua kuwa mwapotea kwani: Islamu hiyo ni adui kabisa wa siasa yetu kwa vile humo kuna Ubwana na Utwana, na hata wewe, ndugu Makamu Mwenyekiti, unaitwa KAFIRI kwa vile u mweusi au wa asili ya Kiafrika na siyo ya Kiarabu!"*

Hizi ndizo fikra za Wakristo walio wengi juu ya dola ya Kiislamu. Pamoja na sababu nyingine, fikra hizi zimejitokeza kwa Wakristo na maadui wengi wa Uislamu kutokana na sababu kubwa mbili zifuatazo:

**Kwanza**, kutoufahamu Uislamu na matunda yanayoletwa na Uislamu katika jamii endapo misingi ya Uislamu itafuatwa vilivyo.

**Pili**, husda na chuki iliyopandikizwa kwa Wakristo na viongozi wao ili wauchukie Uislamu ambao endapo wataachwa huru kujifunza wataupenda na uwezekano wa wengi kusilimu. Pia viongozi wa Makanisa wanaogopa kuulizwa maswali na wafuasi wao ambayo wakiyajibu vilivyo watakuwa wanathibitisha kuwa Uislamu ni dini ya haki kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Ukristo ni dini iliyozuliwa tu na watu.

Hakuna muumini wa kweli wa Mungu wa haki atakayeufahamu Uislamu vilivyo aache kuwa Muislamu. Kila Wakristo walipopata mwanya wa kuufahamu vizuri Ukristo wao na Uislamu, wameamua kwa moyo mkunjufu kusilimu na kuwa Waislamu wa kweli.

Kuhusu sababu hii ya pili ya kuuchukia Uislamu kwa husda, kwa kuwa Uislamu ni dini ya kweli yenye hoja madhubuti zinazompelekea kuelewa upesi kila mwenye kuitaka, na kwa kuwa Qur-an inabainisha kwa uwazi ni wapi Wakristo na Mayahudi walipoacha njia ya uongofu na kupotea, hatuna msaada wowote wa kuwasaidia ndugu zetu hawa kwani huo ni uamuzi wao wenyewe. Pia, hatustushwi na chuki zao kama zilivyojionyesha katika barua ya Rev. C. Mtikila kwani hayo ndio mategemeo yetu kwao kama Allah(s.w) anavyotutahadharisha katika Qur-an:

يَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا بَطَانَةً مِّن دُونِكُمْ لَا يَأْلُونَكُمْ خَبَالًا  
وَدُّوا مَا عَنِتُّمْ قَد بَدَتِ الْبَغْضَاءُ مِن أَفْوَاهِهِمْ وَمَا تُخْفَىٰ صُدُورُهُمْ  
أَكْبَرُ قَدْ بَيَّنَّا لَكُمُ الْآيَاتِ إِن كُنْتُمْ تَعْقِلُونَ ﴿١١٨﴾

*Enyi mlioamini! Msiwafanye wasiri wenu watu wasiokuwa katika nyinyi: "hao hawataacha kukufanyieni ubaya. Wanayapenda yale yanayokudhuruni. Bughudha (yao juu yenu) inadhihirika katika midomo yao. Na yanayofichwa na vifua vyao ni makubwa zaidi. Tumekubainishieni dalili (zote) ikiwa nyinyi ni watu wa kufahamu.(3:118)*

Endapo fikra hizi mbaya dhidi ya Uislamu na dola ya Kiislamu zimetokea kutokana na kutoufahamu Uislamu vilivyo, tunachukua fursa hii kuwaelimisha Wakristo na wengineo wasio Waislamu na hata Waislamu ambao hawajapata fursa ya kuifahamu dini yao vizuri, kuwa Uislamu ni Dini ya Haki na dola ya Kiislamu lengo lake kuu ni kusimamisha Haki katika jamii kwa kuhakikisha kuwa kila mtu anapata haki yake bila ya kujali dini yake. Ili kuhakikisha hili linafanyika, Uislamu umetoa msisitizo maalumu kuhusu haki za wasio kuwa Waislamu katika dola ya Kiislamu kama ifuatavyo:

### **(i) Haki ya Ulinzi wa maisha na Mali**

Damu ya Dhimmi ni takatifu kama ilivyo damu ya Muislamu. Muislamu akimua dhimmi adhabu yake ni sawa na ile ya kumuua Muislamu. Muislamu mmoja alimua dhimmi wakati wa Mtume(s.a.w). Mtume(s.a.w) alimuhukumu kuuawa akasema:

*"Ni jukumu langu kusimamia haki za wanyonge".*

Wakati wa Ukhalifa wa Umar(r.a), Muislamu mmoja alimua dhimmi. Khalifa aliamuru muuaji akamatwe apeleke kwa jamaa wa marehemu. Hili lilifanyika na warithi wa marehemu walimua.

Vile vile mali ya dhimmi katika dola ya Kiislamu ni takatifu kama ilivyo takatifu mali ya Muislamu. Muislamu akiiba mali ya Dhimmi atahukumiwa kukatwa mkono kama kawaida.

Khalifa wa nne wa Mtume(s.a.w) baada ya kumuhukumu Muislamu mmoja kuuawa na warithi wa dhimmi aliyemua, alisisitiza:

Yeyote aliye Dhimmi wetu damu yake ni takatifu kama damu yetu na mali yake ni takatifu kama mali yetu.

***(ii) Dhimmi na sheria ya jinai***

Katika dola ya Kiislamu hukumu za makosa ya jinai (penal laws) zinawahusu madhimmi sawa na zinavyowahusu Waislamu. Makosa ya jinai ni makosa yanayoathiri jamii nzima na mhalifu atakuwa anaidhulumu jamii nzima. Kwa hiyo dhimmi akiiba atakatwa kiganja chake cha mkono wa kulia, akizini atatandikwa viboko 100 au kupigwa mawe mpaka kufa endapo amewahi kuoa au kuolewa.

Ila dhimmi hataadhibiwa kwa kosa la ulevi kama atakavyoadhibiwa akilewa Muislamu kwa kutandikwa viboko 40.

***(iii) Dhimmi na Sheria za Madai (Civil Laws)***

Katika dola ya Kiislamu hukumu za madai ni sawa kwa Waislamu na wasio kuwa Waislamu. Kila mwenye kudaiwa atahukumiwa na sheria kutoa haki ya mdai bila ya ubaguzi wa dini.

Pia yale yote yaliyoharamishwa kwa Waislamu katika uchumi, pia sheria inayakataza kwa madhimmi. Kwa mfano riba na Kamari ni haramu kwa Waislamu na imekatanzwa pia kwa wasiokuwa Waislamu kwani riba na kamari huiathiri jamii nzima.

Bali madhimmi wanaruhusiwa kulewa na kula nguruwe. Pia wana uhuru wa kutengeneza pombe na kufuga nguruwe katika maeneo yao ambamo hawaishi Waislamu. Hawaruhusiwi kufanya hivyo katika maeneo ya Waislamu wala hawaruhusiwi kutengeneza na kuuza pombe, kufuga na na kuuza nguruwe katika sehemu za umma zinazotumiwa na wote.

Muislamu akimuingilia dhimmi katika eneo lake ambapo anaruhusiwa na sheria kutengeneza pombe na kufuga nguruwe, kwa kuiharibu [pombe yake au kuwaua nguruwe wake atawajibika kulipa vitu hivyo mbele ya sheria ya Kiislamu.

***(iv) Haki ya Heshima***

Kumvunjia heshima dhimmi kwa kumtukana, kumuita jina baya, kumdharau, kumuadhiri, kumteta, n.k. ni makosa makubwa sana mbele ya Allah kama ilivyo makosa makubwa kumfanyia Muislamu.

Heshima ni haki inayomstahiki kila mwanadamu pasi na ubaguzi wa aina yoyote. Ni dhima ya Serikali ya Kiislamu kulinda heshima ya kila mtu.

***(v) Sheria ya Mtu Binafsi (Personal Law)***

Katika serikali ya Kiislamu, mambo yote yanayohusu imani ya mtu binafsi huhukumiwa kulingana na imani ya dini yake. Kama jambo lililoharamishwa kwa Waislamu si haramu kulingana na imani ya dhimmi, serikali itaendelea kumruhusu

kulitenda jambo hilo. Kwa mfano kuoa bila ya kutoa mahari au kufunga ndoa wakati wa kipindi cha eda ni haramu kwa Waislamu lakini kama katika imani ya dini ya dhimmi haya hayakukatazwa, basi mahakama ya Kiislamu haitamkataza dhimmi huyo kuoa pasi na kutoa mahari au kuoa wakati wa eda. Kwa ufupi, katika yale mambo yanayohusu imani za dini nyingine na ambayo hayaathiri jamii kwa ujumla, kama vile ndoa, talaka na mirathi, sheria ya Kiislamu imetoa haki ya madhimmi kuhukumiwa kulingana na imani za dini zao.

***(vi) Haki ya Kuabudu na Kupewa Heshima Mahali pa Kuabudia***

Katika dola ya Kiislamu, madhimmi wana uhuru kamili wa kuabudu kulingana na dini yao inavyowataka. Pia Waislamu wameamrisha kuheshimu dini za wengine – wasizitukane wala kuonyesha dharau ya aina yoyote – (Qur-an 6:108). Vile vile Waislamu wamekatazwa kujiingiza katika mabishano yasiyo na msingi na watu wa dini nyingine, (Qur-an 29:46).

***(vii)Haki ya Kusamehewa Kushiriki Jihad***

Dhimmi katika serikali ya Kiislamu wamesamehewa kupigana vita kwa sababu ulinzi wa serikali dhidi ya maadui zake ni jukumu la Waislamu tu. Inakuwa hivyo kwa sababu ni wale tu wanaokubaliana na itikadi ya dola ya Kiislamu, ndio tu watakaopigania dola kwa moyo mkunjufu wa kufa na kupona.

Pia ni waumini tu wa Kiislamu watakaoweza kuchunga kwa ukamilifu mipaka ya Uislamu iliyowekwa kuhusiana na vita vya jihadi. Dhimmi wanalazimika kutoa Jizya (kodi maalum) kama malipo ya ulinzi wanaopewa na Uislamu. Dola ya Kiislamu ikishindwa kutoa ulinzi kwa nchi ya Dhimmi iliyojisalimisha kwa dola ya Kiislamu, nchi hiyo ya Dhimmi haitalazimika kutoa Jizya.

***(viii)Nafasi ya Dhimmi Katika Kuendeleza Dola ya Kiislamu***

Kwa kuwa serikali ya Kiislamu inaendeshwa kwa misingi ya itiqadi ya Dini ya Kiislamu, wenye kustahiki kuongoza serikali ni wale tu wenye imani thabiti juu ya itikadi ya Kiislamu. Hawa pekee ndio watakaoweza kuongoza Dola kwa uadilifu mpaka kufikia lengo lake kuu la kusimamisha haki na kuiwezesha jamii kuishi kwa furaha na amani.

Watu wenye itikadi nyingine wanayo haki kamili ya kuchangia maendeleo ya serikali na wakipenda watashirikishwa katika sekta mbali mbali za kitaalamu na zisizokuwa za kitaalamu lakini hawatapewa kazi ya uongozi katika sekta yoyote au katika ngazi yoyote ya uongozi wa dola.

Uongozi ni dhimma ya Waislamu kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي  
الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ  
الَّذِي أَرْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۗ ﴿٥٥﴾

*Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mweni na kufanya vitendo vizuri, kuwa atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale waliokuwako kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya khofu yao... (24:55)*

Waislamu wa vitendo wamepewa haki hii kwa sababu ndio pekee, kutokana na imani yao thabiti juu ya Allah(s.w) na malipo ya Akhera, watakaoweza kusimama kidete kutetea haki za watu na kuhakikisha kuwa jamii inahuishia na kuendeleza mema na inaepukana na maovu. Waislamu hawapewi kazi hii ya uongozi kwa upendeleo, bali wamepewa kazi hii kwa kuwa wanao uwezo wa kuifanya kama Allah(s.w) anavyowatukuza katika Qur-an:

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ  
وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ ۗ وَلَوْ ءَامَنَ أَهْلُ الْكِتَابِ لَكَانَ خَيْرًا لَهُمْ ۗ ﴿١١٠﴾

*Nyinyi ndio umma bora kuliko umma zote zilizodhihirishwa watu (ulimwenguni) – mnaamrisha yaliyo mema na mnakataza yaliyo maovu, na mnamwamini Mwenyezi Mungu. Na kama wale waliopewa kitabu wangaliamini ingalikuwa bora kwao... (3:110)*

Waislamu wakiacha kuchukua dhima hii ya uongozi wa jamii na badala yake watu wengine wasiomwamini Allah ipasavyo na malipo ya akhera, wakaichukua kazi hii ya uongozi wa jamii na kuifanya kwa kufuata matashi yao kinyume na matashi ya Mwenyezi Mungu, jamii itatumbukia katika giza la huzuni na majuto kama ilivyo hivi sasa katika ulimwengu huu wa Kitwaghati kama tunavyojifunza katika Qur-an:

اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ ءَامَنُوا يُخْرِجُهُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ وَالَّذِينَ  
 كَفَرُوا أَوْلِيَاؤُهُمُ الطَّاغُوتُ يُخْرِجُونَهُم مِّنَ النُّورِ إِلَى الظُّلُمَاتِ  
 أُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٥٧﴾

“Mwenyezi Mungu ni mlinzi (kiongozi) wa wale waliomani. Huwatoa katika giza na kuwaingiza katika **nuru**. Lakini waliokufuru, walinzi (viongozi) wao ni **matwaghuti**. Huwatoa katika **nuru** na kuwaingiza katika **giza**. Hao ndio watu wa motoni humo watakaa milele”. (2:257).

## Zoezi 2:10

1. (a) Nini maana ya Siasa
  - (b) Taja tanzu za mfumo wa siasa za kitwaghuti
2. Linganisha na kutofautisha baina ya mfumo wa Siasa za Kidemocrasia na mfumo wa Siasa wa Kiislamu
3. (a) Eleza maana ya Dola.
  - (b) Onesha msonge wa utendaji katika dola ya kitwaghuti
4. Soma kwa makini Qur’an 27:48-49, 8:30,9:40.
  - (a) Ni chombo kipi kinachohusika na hila hizi katika dola la kitwaghuti?
  - (b) Ni mambo gani yanayofanya chombo hiki kufikia malengo yake?
5. Kuna tofauti gani kati ya kazi za bunge, mahamaka, na polisi katika dola ya kitwaghuti na kazi za vyombo hivyo katika dola ya Kiislamu.
6. Eleza, ni mfumo upi wa Dola, kati ya ule wa kitwaghuti na wa kiislamu ambao ni muhimu, na bora kwa jamii kuufuata.
7. Taja na kufafanua misingi ya utii katika maongozi ya dola ya Kiislamu na sababu zake.
8. Bainisha sifa na vigezo vya kumstahikisha mtu kuwakiongozi wa Kiislamu.
9. Taja, eleza na kuthibisha kwa Qur’an, njia za kumpata mtu atakaye kabidhiwa dhima ya kuwa kiongozi atakaye ongoza Waislamu na jamii katika kutekeleza wajibu na majukumu yao kulingana na lengo halisi la maisha.



9. Bainisha tofauti nne katika ya serikali ya Kiislamu na ile ya Kidemokrasia.
10. (a) Taja aina za raia katika Dola ya Kiislamu
  - (b) Onesha kwa ushahidi wa Qur'an na Sunnah, haki inazopasa kusimamia serikali ya kiislamu kwa raia zake.



*Sura ya Tatu***QUR'AN**

Somo la Qur'an katika sura hii linajihusisha na mada kuu zifuatazo:

- Madai ya Makafiri dhidi ya Qur'an na udhaifu wa madai hayo.
- Uthibitisho kuwa Qur'an ni neno la Allah(s.w).
- Mafunzo ya sura zilizochaguliwa.

**MADAI YA MAKAFIRI DHIDI YA QUR'AN NA UDHAIFU WA MADAI HAYO.****Madai ya Makafiri dhidi ya Qur'an**

Waislamu wanaamini pasi na tone la shaka kuwa Qur'an ni kitabu cha Allah(s.w) neno kwa neno kama mwenyewe anavyothibitisha:

ذَٰلِكَ الْكِتَابُ لَا رَيْبَ فِيهِ هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٢﴾

*“Hiki ni kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake, ni uongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu.” (2:2)*

Pamoja na uthibitisho huu, makafiri wa zama za kale na za sasa wameibuka na upinzani dhidi ya Qur'an na kudai kuwa kitabu hiki amekitunga mwenyewe Mtume Muhammad(s.a.w):

أَمْ يَقُولُونَ تَقْوَاهُ ۚ بَلْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٥٢﴾

*“Au ndio wanasema kuwa hii Qur'an amekitunga (Muhammad)? Bali wao hawaamini lolote.” (52:33)*

Dai hili la kumpa Mtume(s.a.w) utunzi wa Qur'an limewakilishwa katika sura mbali mbali na makafiri wa zama mbali mbali. Kwa ujumla makafiri wamedai kuwa Qur'an ni:

- (i) Mashairi aliyotunga Mtume Muhammad(s.a.w).
- (ii) Zao la njozi za Muhammad(s.a.w) zilizovurugika
- (iii) Zao la mwenye kujidhania kupata ufunuo

- (iv) Zao la mwenye kifafa na aliyepagawa na shetani.
- (v) Aya za shetani
- (vi) Uandishi wa Muhammad(s.a.w) kwa msaada wa Mayahudi na Wakristo.
- (vii) Utunzi wa Muhammad(s.a.w) ili kuleta umoja na ukombozi wa Waarabu.
- (viii) Utunzi wa Muhammad(s.a.w) ili kurekebisha tabia ya Waarabu.
- (ix) Utunzi wa Muhammad(s.a.w) ili ajinufaishe kiuchumi.
- (x) Utunzi wa Muhammad(s.a.w) ili kuwania madaraka na ukubwa.

Qur'an yenyewe inakanusha madai haya katika aya mbali mbali kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

فَلَا أَقْسِمُ بِمَا تُبْصِرُونَ ﴿٣٨﴾ وَمَا لَا تُبْصِرُونَ ﴿٣٩﴾ إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ﴿٤٠﴾  
 وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَاعِرٍ قَلِيلًا مَّا تُوْمِنُونَ ﴿٤١﴾ وَلَا بِقَوْلِ كَاهِنٍ قَلِيلًا مَّا تَذَكَّرُونَ ﴿٤٢﴾  
 تَنْزِيلٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٤٣﴾ وَلَوْ تَقَوَّلَ عَلَيْنَا بَعْضُ الْأَقَاوِيلِ ﴿٤٤﴾  
 لَأَخَذْنَا مِنْهُ بِالْيَمِينِ ﴿٤٥﴾ ثُمَّ لَقَطَعْنَا مِنْهُ الْوَتِينَ ﴿٤٦﴾

*Basi naapa kwa mnavyoviona. Na msivyoviona. Kwa hakika hii ni kauli iliyoletwa na Mjumbe (wa Mwenyezi Mungu) mwenye hishima (kubwa). Wala si kauli ya mtunga mashairi (kama mnavyosema). Ni machache sana mnavyoyaamini. Wala si kauli ya mchawi (kama mnavyodai). Ni kidogo kabisa kuwaidhika kwenu. Ni mteremsho utokao kwa Mola wa viumbe vyote. Na kama (Mtume) angelizua juu yetu baadhi ya maneno tu, bila shaka tungalimshika kwa mkono wa kuume, (wa kulia). Kisha kwa hakika tungalimkata mshipa mkubwa wa moyo (69:38-46).*

فَمَا مِنْكُمْ مِّنْ أَحَدٍ عَنْهُ حَاجِزِينَ ﴿٤٧﴾ وَإِنَّهُ لَتَذِكْرٌ لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٤٨﴾  
 وَإِنَّا لَنَعْلَمُ أَنَّ مِنْكُمْ مُّكَذِّبِينَ ﴿٤٩﴾ وَإِنَّهُ لَحَسْرَةٌ عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٥٠﴾  
 وَإِنَّهُ لَحَقُّ الْيَقِينِ ﴿٥١﴾ فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيمِ ﴿٥٢﴾

*Na hapana yeyote katika nyie angeweza kutuzuia naye. Kwa hakika hii (Qur'an) ni mawaidha kwa wanaomcha Mwenyezi Mungu. Na kwa yakini tunajua kuwa miongoni mwenu wamo wanaokadhibisha. Na itakuwa ni sikitiko, (majuto) juu ya wanaokanusha. Na hakika hii ni haki ya yakini. Basi litukuze jina la Mola wako aliye Mkuu. (69:47-52)*

Pamoja na aya hizi na nyingine nyingi zinazokanusha madai ya makafiri dhidi ya utunzi wa Qur'an bado Allah(s.w) ametoa changa moto kwa makafiri wa zama zote tangu ianze kushuka Qur'an hadi leo, kuwa:

وَإِنْ كُنْتُمْ فِي رَيْبٍ مِّمَّا نَزَّلْنَا عَلَىٰ عَبْدِنَا فَأْتُوا بِسُورَةٍ مِّمَّنْ مِثْلِهِ

وَادْعُوا شُهَدَاءَكُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٣﴾

*“Na ikiwa mna shaka kwa hayo tuliyomteremshia Mtumwa Wetu (kuwa hakuteremshiwa na Mwenyezi Mungu) basi leteni sura moja iliyofanywa na (mtu) aliye mfano wake, na muwaite waungu wenu bighairi ya Mwenyezi Mungu (wakusaidieni), ikiwa mnasema kweli.” (2:23)*

Pamoja na changamoto hii ya Qur'an, hebu tuangalie kwa undani kidogo udhaifu wa hizi hoja kumi za makafiri dhidi ya Qur'an:

#### **(i) Dai kuwa Qur'an ni Mashairi aliyotunga Muhammad(s.a.w):**

Dai hili lilitolewa na Makuraishi katika enzi hizo za kushuka kwa Qur'an pia linaendelea kutolewa na makafiri wa karne hizi. Kwa mfano Stober, baada ya kusoma tafsiri ya Qur'an alidai kuwa itakuwa imeandikwa na Mwarabu ambaye ni mweledi wa historia ya Mayahudi na mila za nchi yake ambaye pia ni mshairi mzuri.

#### **Udhaifu:**

Wasomaji wa mashairi ya Kiarabu wanafahamu kuwa mashairi hayo yana mizani, beti na vina na yanaimbika kwa kiasi kwamba wakati mwingine inabidi hata maana au sarufi viwekwe pembeni alimradi tu shairi liimbike. Hivi sivyo kabisa ulivyo mfumo wa Qur'an. Qur'an si mashairi bali ni ujumbe wenye maana kamili ulioandikwa katika fasihi ya hali ya juu kwa kuzingatia sarufi na miiko yote ya lugha hai.

Historia imeshuhudia kuwa Qur'an si mashairi. Ilikuwa kawaida ya washairi wakati ule wa Mtume(s.a.w) kubandika mashairi yao kwenye mlango wa Ka'aba kama changa-moto kwa washairi wengine. Ilitokea siku moja mshairi mashuhuri wa wakati huo, **Labbiib ibn Rabiah**, akabandika shairi lake kwenye mlango wa Ka'aba ili kutoa changamoto kwa washairi wengine. Shairi lake lilikuwa limetungwa kwa utaalumu mkubwa sana na lilikuwa zuri mno kiasi

cha kutohubutu mtu yeyote kupambanisha shairi lake na hilo. Lakini baada ya kubandikwa kipande cha Sura ya Qur'an karibu na shairi lake, Labbiid mwenyewe (ambaye alikuwa Mshirikina) baada ya kusoma mistari michache ya sura hiyo alinaswa na mvuto wake na kuiamini dini iliyofunuliwa kutoka kwa Allah(s.w) na kubandua shairi lake

**(ii) Dai kuwa Qur'an ni zao la njozi za Mtume(s.a.w) zilizovurugika:**

Katika miaka ya 1960 waandishi wawili, Anderson na Watt, walikuja na dai kuwa Qur'an ni zao la dhana (*Wishful Thinking*). Walidai kuwa maneno na maelezo ya habari mbalimbali yaliyomo katika Qur'an yametokana na mawazo ya Mtume(s.a.w) aliyoyatoa kwa dhana tu. Watt, kwa kutumia njia za kisasa za kuchunguza fasihi alihitimisha kuwa angelifanya makosa makubwa sana kama angeliamini kuwa Qur'an ni ujumbe wa Allah(s.w) kwani: "Kila kinachoonekana kinatoka nje ya fikra za mwanaadamu, kwa kweli hutokana na mawazo yake ya kinjozi ambayo hutokea bila ya kufikiri." Kwa hiyo alieleza Watt kuwa Qur'an ni zao la dhana (*Creative Imagination*)

**Udhaifu wa Dai hili:**

Nadharia ya Anderson na Watt haina nguvu yoyote kwa sababu katika historia nzima ya mwanaadamu hapajatokea mawazo ya kinjozi hata yawe yamebuniwa kwa uhodari kiasi gani yakaunda kitabu mithili ya Qur'an au hata angalau sura moja iliyo mithili na sura yoyote ya Qur'an. Hata hivyo, jambo la kukumbuka ni kwamba dai hili la Anderson na Watt na makafiri wengine wa kisasa wenye mawazo kama hayo, si geni bali ni dai kongwe lililotolewa na jamii ya Mtume(s.a.w) mwenyewe kama tunavyofahamishwa katika Qur'an:

بَلْ قَالُوا أَضْغَتْ أَحْلَمِ بَلِ افْتَرَاهُ بَلْ هُوَ شَاعِرٌ فَلْيَأْتِنَا بِآيَةٍ كَمَا

أُرْسِلَ الْأَوْلُونَ ﴿٥﴾

“Lakini (Makafiri) walisema: “(Hayo anayosimulia) ni ndoto zilizovurugika. Bali ameyabuni (mwenyewe). Bali huyu ni mtunga mashairi tu. Basi atuletee Muujiza kama walivyotumwa (Mitume) wa kwanza.” (21:5)

**(iii) Dai la Kujidhania Kupata Wahy (Self Revelation)**

Bwana E. Birmingham katika kitabu chake anadai kuwa, kwa sababu Muhammad(s.a.w) alikuwa mkweli na mwadilifu alichukia sana moyoni mwake kwa jinsi uovu na ufisadi ulivyoshamiri katika jamii yake. Kutokana na mwangaza aliokuwa nao yeye mwenyewe binafsi akaona kuwa ipo haja ya kuijenga upya jamii hiyo. Huenda pia alisikia juu ya kitabu cha Wayahudi na Wakristo lakini hakupendezwa na mafundisho ya Utatu Mtakatifu (Trinity). Na

yawezekana alisikia kuwa atakuja nabii kutoka katika eneo hilo. Mambo hayo yakawa yanazunguka ndani kabisa ya nafsi yake, hadi kufikia kuamini kuwa yeye ni mtume na ndipo akaanza kupata fikra za kimazezeta kuwa Malaika wanamsemesha.

### ***Udhaifu wa Dai hili:***

Endapo kama chimbuko la Qur'an ni hisia za ndani za nafsi ya Muhammad(s.a.w) (*subconsciousness*), basi Qur'an itakuwa inatokana na elimu na mazingira yake. Lakini ukiiangalia Qur'an kwa makini utaona kuwa imetoa taarifa nyingi sana ambazo vyovyote atakavyokuwa haziwezi kuwa zimetoka katika nafsi ya Muhammad(s.a.w).

Kwa mfano Qur'an inaeleza matukio ya kihistoria au matukio yatakayotokea baadaye ambayo Muhammad(s.a.w) hakuyajua na wala hakuwa na namna ya kuyajua. Kwa mfano:

Sura ya 18 ya Qur'an, Al-Kahf iliteremka baada ya Muhammad(s.a.w) kuulizwa maswali matatu na makafiri wa Makka ili kumjaribu. Maswali hayo waliyauliza baada ya kushauriana na watu wa Kitabu (Mayahudi). Maswali hayo yalikuwa:

- (i) Ni kipi kisa cha vijana wa pangoni?
- (ii) Ni kipi kisa cha Al-Khidhr?
- (iii) Unajua nini juu ya Dhul-qarnain?

Kwa kuwa maswali haya yalifungamana na historia ya Wakristo na Wayahudi, na habari zake hazikujulikana Hijaz, yalikusudiwa kumpima Mtume(s.a.w) kuwa kweli alikuwa Mtume wa Allah(s.w) aliyekuwa akipokea wahy kutoka kwake au ni mzushi tu.

Alipoulizwa maswali hayo Muhammad(s.a.w) alisema, "Nitakujibuni kesho" lakini hakusema, 'Inshaa-Allah'. Siku iliyofuata alikuwa bado hajapata wahy, hivyo walipokuja makafiri kusikiliza majibu, akawaambia waje siku iliyofuata. Walipokuja hakuwa na majibu. Hali ikaendelea hivyo kwa muda wa siku 15. Makafiri wakaanza kumkejeli na kumdhihaki. Muhammad(s.a.w) akahuzunika sana kwa kutopata wahy alioutazamia. Hatimaye Jibril (a.s) akamletea wahy akafahamishwa majibu ya maswali yote. Kule kuchelewa kuja kwa wahy kulikuwa ni fundisho kwake:

وَلَا تَقُولَنَّ لِشَيْءٍ إِنِّي فَاعِلٌ ذَٰلِكَ غَدًا ﴿١٦﴾ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ ۗ وَادْكُرْ

رَبِّكَ إِذَا نَسِيتَ وَقُلْ عَسَىٰ أَنْ يَهْدِيَنِّي رَبِّي لِأَقْرَبَ مِنْ هَٰذَا رَشْدًا ﴿١٧﴾

*Wala usiseme kamwe kwa lolote lile kuwa: "Nitalifanya kesho." Isipokuwa (uongeze) Isha-Allah. Na umkumbuke Mola wako unaposahau, na useme "Asaa Mola wangu ataniongoza njia iliyo karibu zaidi na uongofu kuliko hii" (18:23-24)*

Ingawa kuchelewa kwa kuja wahyi kulimsononesha sana Muhammad(s.a.w) ilikuwa ni ushahidi kuwa Qur'an haikutungwa na yeye. Laiti angelikuwa mtunzi wa Qur'an angeliyatoa majibu yale kesho yake ili kuepuka fedheha iliyompata.

Kuhusiana na hili la fikra za kimazezeta jambo la kuzingatia hapa ni kwamba Muhammad(s.a.w) aliulizwa maswali kuhusiana na matukio maalum,. Ni vigumu sana kuona jinsi ambavyo fikra za kimazezeta ya kidini zingeweza kumsaidia kujibu kwa usahihi maswali aliyoulizwa. Majibu ambayo yaliwatosheleza na kuwanyamazisha makafiri.

Na miongoni mwa mambo yanayojitokeza katika kisa hiki ni namna ulivyowasilishwa muda wa vijana waliokaa pangoni. Qur'an inasema:

وَلَبِثُوا فِي كَهْفِهِمْ ثَلَاثَ مِائَةٍ سِنِينَ وَازْدَادُوا تِسْعًا

*Na walikaa katika pango yao miaka mia tatu, na ongeza tisa. (18:25)*

Kwa nini aya haikusema moja kwa moja "miaka mia tatu na tisa" na badala yake ikasema "mia tatu na ongeza tisa?" Hii ni kwasababu vijana hao walikaa miaka 300 kwa kufuata kalenda ya jua (solar calendar) na ni miaka 309 kwa kufuata kalenda ya kuandama mwezi (lunar calendar). Sababu yake ni kuwa mwaka wa kuandama kwa miezi ni mfupi kwa siku 11 ukilinganishwa na ule wa jua. Hivyo  $11 \times 300/365 = 9$ . Yaani siku 11 mara 300 kugawanywa kwa 365 ni miaka 9. Hivyo basi madai kuwa mahesabu hayo sahihi yanatokana na kujidhania au mauzauza yaliyompanda Muhammad(s.a.w) hayana nguvu.

Mfano mwingine tunaukuta katika sura ya 89 ya Qur'an ambayo ina aya inayoutaja mji wa kale sana wa Iram:

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ ۖ إِرَمَ ذَاتِ الْعِمَادِ ۖ الَّتِي لَمْ تُلْخَقْ

مِثْلَهَا فِي الْبَلَدِ

*Je! Hukuona jinsi Mola wako alivyowafanya Adi, wa (mji wa) Iram, wenye majumba marefu marefu ambayo hawakuumbwa mfano wao katika mji (mingine). (89:6-8)*

Jina la mji huu lilikuwa halijulikani vizuri hata wakati wa uhai wa Mtume(s.a.w). Kwa sababu hiyo kulikuwa na utatanishi mkubwa juu ya ni ipi Jiografia ya mji

huo. Hata hivyo utafiti uliochapishwa katika jarida la chama cha Jiografia huko Marekani litwalo “*The National Geographic*” toleo la December 1978 umeonesha kuwa Iram ni jina la mji. Mwaka 1975 Dk. Paolo Mathiae wa chuo Kikuu cha Roma aligundua huko Syria maktaba ya kale sana iliyokuwa na vigae 15,000 vyenye maandishi. Miongoni mwa maelezo yaliyokuwamo katika vigae hivyo ilikuwa ni taarifa kuwa watu wa mji wa Ebla walikuwa wakifanya biashara na watu wa mji wa Iram.

Ni vigumu sana kuona ni kwa vipi fikra za kizezeta zingeweza kumwongoza Muhammad(s.a.w) kutoa taarifa sahihi juu ya majumba yaliyoharibiwa miaka 3,000 kabla yeye hajazaliwa!

Isitoshe Qur'an imetamka katika sehemu kadhaa kuwa Muhammad na watu wake hawakuvijua baadhi ya visa vilivyotajwa katika Qur'an:

تَلْكَ مِنْ أَنْبَاءِ الْغَيْبِ نُوحِيهَا إِلَيْكَ مَا كُنْتَ تَعْلَمُهَا أَنْتَ وَلَا قَوْمُكَ  
 مِنْ قَبْلِ هَذَا فَاصْبِرْ إِنَّ الْعَقِيبَةَ لِلْمُتَّقِينَ

*Hizi ni katika habari za ghaibu tunazokufunulia. Hukuwa ukizijua wewe, wala watu wako, kabla ya hii (Qur'an kuteremshwa). Hakika mwisho mwema ni wa wamchao Mwenyezi Mungu(11:49)*

Yafaa kuzingatia hapa kuwa hakuna hata mtu mmoja aliyejitokeza na kusema, “Ewe Muhammad, hayo uyasemayo si kweli. Mimi ni Mwarabu kama wewe na nilizijua habari hizi kabla ya huu wahy wako. Si hivyo tu, bali pia kama Muhammad(s.a.w) angekuwa ndiye mtunzi wa Qur'an asingethubutu kuitamka aya hii, au kama angeitamka basi angekuwa amejitia katika patapotea ya hatari kabisa kwa sababu zifuatazo:

**Kwanza**, hata kama tukisema mathalan kuwa Muhammad(s.a.w) kwa hakika alizijua habari hizo kabla lakini hapa anasingizia tu, basi hapana shaka yeye hatakuwa mtu pekee anayezijua. Hivyo asingeweza kusema kwa ujasiri kiasi hiki juu ya kutokujua kwa wengine. Atakuwa na uhakika gani kuwa watu wote wengine hawazijui?

**Pili**, hata kama ni kweli kuwa watu wengine hawakujua habari hizo, maadui na wapinzani wake wangeweza kusingizia kuwa wao kwa hakika walikuwa wanazijua habari hizo hasa hasa ilivyokuwa kauli hiyo imetamkwa katika Qur'an baada ya kumaliza kukisimulia kisa chenyewe. Lakini pamoja na yote hayo hakuna mtu aliyeitumia fursa hiyo. Muhammad(s.a.w) angewezaje kujua kuwa hakuna mtu atakayeitumia fursa hiyo?



*(iv) Dai kuwa Qur'an ni zao la Mwenye Kifafa na Aliyepagawa na Shetani:*

Waandishi kadhaa wa kikafiri katika maandishi yao wamedai bila kutoa ushahidi wowote unaotokana na historia kuwa Mtume Muhammad(s.a.w) alikuwa mwenye kifafa na mwenye kupagawa na Shetani na maneno yake alipokuwa katika hali ya ugonjwa ndiyo yaliyonukuliwa na kuunda Kitabu cha Qur'an!

*Udhaifu:*

Udhaifu wa dai hili tunaweza kuuona kwa kujiliza maswali yafuatayo: Je, kifafa, ugonjwa mbaya kama tunavyoufahamu, umewahi kumtokea mtu katika historia ya mwanaadamu na bado akawa mtu mwenye kutoa sheria za kufuatwa na umati wa watu wengi zaidi ya robo ya dunia? Je, historia ya mwanaadamu imewahi kumshuhudia mgonjwa wa kifafa au mwenye kupagawa na shetani kuwa na hadhi na uwezo mkubwa kuliko mtu yeyote ulimwenguni kama ilivyokuwa kwa Mtume Muhammad(s.a.w)? Kama mgonjwa wa kifafa ndiye aliyandika Qur'an, inakuwaje waandishi hodari wenye akili timamu na wanafalsafa wakubwa washindwe kuandika kitabu mithili ya angalau sura moja ya Qur'an na kukabili changa moto iliyotolewa na Qur'an karne nyingi zilizopita:

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَاهُ ۗ قُلْ فَأْتُوا بِسُورَةٍ مِّثْلِهِ ۚ وَادْعُوا مَنِ اسْتَعْظَمْتُمْ مِن

دُونِ اللَّهِ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٠٣٨﴾

*“Je! Ndiyo wanasema ameitunga? Sema: “Hebu (tungeni na nyie) mlete sura moja mfano wake na waiteni muwezao (kuwapata waje).- isipokuwa Mwenyezi Mungu - (wa kuwasaidieni) kama nyinyi mnasema kweli (kuwa haya ameyazua Muhammad).” (10:38)*

Kitaalam inafahamika kuwa ugonjwa wa kifafa baada ya muda humfanya mgonjwa kuwa taahira (punguani). Pia ugonjwa wa kifafa humdhoofisha mgonjwa na hutisha wauguzaji na wenye kumuangalia mgonjwa wakati ameshikwa na kifafa. Hapana ushahidi wowote katika historia ya Mtume(s.a.w) ambayo iko bayana mno kuliko historia ya mtu yeyote, kuwa alikuwa mwenye kifafa au mwenye kupagawa na shetani.

*(v) Dai kuwa Qur'an ni aya za Shetani*

Katika mwaka 1988 Salman Rushdie, Muingereza mwenye asili ya kihindi, aliandika kitabu chake alichokiita “Satanic Verses” (yaani aya za Shetani) ambamo amemtukana Mtume(s.a.w), Uislamu na Qur'an kwa kuiita “aya za Shetani.”

Katika kitabu chake hicho, Rushdie amedai kuwa hapakuwa na wahy wowote uliomshukia Muhammad(s.a.w) bali alikuwa akidai tu kuwa anashushiwa Wahy. Aidha Rushdie anadai kuwa Muhammad(s.a.w) alikuwa ni mtu aliyekuwa akifuata matashi yake mwenyewe akiongozwa na shetani na kwa hiyo yote yaliyomo ndani ya Qur'an ni maneno ya shetani.

Pia Rushdie katika kitabu chake hicho amedai kuwa Mtume(s.a.w) hakuwa na uwezo wa kutofautisha wahy kutoka kwa Malaika au wahy kutoka kwa shetani.

Vile vile Salman Rushdie amedai kuwa Mtume(s.a.w) hakuwa na kumbukumbu ya kile alichowasomea maandishi wake na wala hakuweza kutambua hata kile ambacho maandishi hao wamekiongeza kichini-chini. Amepiga mfano wa mwandishi mmoja wa Kifursi kuwa alisomewa na Mtume aandike "Mwenye kusikia, mwenye kujua kila kitu" lakini yeye akaandika "Mwenye kujua na Mwenye hikma" na Mtume hakung'amua mabadiliko hayo!

### *Udhaifu wa Madai ya Salman Rushdie*

**Kwanza**, ujumbe wa Qur'an umeteremshwa ili kumtoa binaadamu kutokana na hadaa zote za shetani. Shetani katika Qur'an ameelezwa wazi pamoja na vitimbi vyake na watu anaowatumia ili wanadamu wasiweze kupotezwa naye. Hebu turejee aya chache zifuatazo:

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا شَيْطِينَ الْإِنْسِ وَالْجِنَّ يُوحِي بَعْضُهُمْ  
إِلَى بَعْضٍ زُخْرُفَ الْقَوْلِ غُرُورًا ۗ وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ مَا فَعَلُوهُ ۗ فَذَرْهُمْ وَمَا  
يَفْتَرُونَ ﴿١١٢﴾

*"Na namna hii tumemfanyia kila Nabii maadui, (nao ni) mashetani katika watu na (mashetani) katika majini. Baadhi yao wanawafunulia wenzao maneno ya kupamba pamba ili kuwadanganya. Na Mola wako angelipenda wasingelifanya hayo. Basi waache na uongo wao." (6:112)*

يَبْنِيءَ آدَمَ لَا يَفْتِنَنَّكُمْ الشَّيْطَانُ كَمَا أَخْرَجَ أَبَوَيْكُمْ مِنَ الْجَنَّةِ يَنْزِعُ  
عَنْهُمَا لِبَاسَهُمَا لِيُرِيَهُمَا سَوْءَٰتِهِمَا ۗ إِنَّهُ يَرِنُّكُمْ هُوَ وَقَبِيلُهُ مِنْ حَيْثُ لَا  
تَرَوْنَهُمْ ۗ إِنَّا جَعَلْنَا الشَّيْطَانَ أَوْلِيَاءَ لِلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١١٣﴾

*“Enyi wanaadamu! Shetani (Iblisi) asikutieni katika matata, kama alivyowatoa wazee wenu katika Pepo akawavua nguo zao ili kuwaonesha tupu zao. Hakika yeye pamoja na kabila yake wanakuoneni na hali ya kuwa hamuwaoni.” Bila shaka sisi tumewajaalia mashetani kuwa marafiki wa wale wasioamini.” (7:27)*

إِنَّ الشَّيْطَانَ لَكُمْ عَدُوٌّ فَاتَّخِذُوهُ عَدُوًّا إِنَّمَا يَدْعُوا حِزْبَهُ لِيَكُونُوا مِنْ

أَصْحَابِ السَّعِيرِ ﴿٦١﴾

*“Kwa yakini Shetani ni adui yenu, basi mfanyeni adui (yenu; kwa hivyo msimtii) kwani anaita (analiita) kundi lake liwe katika watu wa Motoni.” (35:6)*

Kama Qur'an ni maneno ya Shetani, inakuwaje tena shetani mwenyewe ajidhihirishe kiasi hicho ili watu wamkimbie?

**Pili**, Allah(s.w) anasema kuwa laiti ingelikuwa hii Qur'an inatoka kwa mwingine asiye kuwa Yeye au kama ingekuwa ina maandishi wawili tofauti ambao wana malengo yanayopingana mmoja anavutia kwenye mema na mwingine kwenye uovu pangelikuwa na khitilafu nyingi (Qur'an 4:82). Je, uko mgongano wowote katika maneno ya Qur'an? Haupo, bali maneno yote ya Qur'an ni yenye kusadikishana. Hivyo haiwezekani Qur'an kuwa na mchanganyiko wa maneno ya shetani na ya Allah(s.w) kwa pamoja.

**Tatu**, Qur'an yenyewe imekataa kuwa Qur'an si maneno ya shetani.

وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَيْطَانٍ رَّجِيمٍ ﴿٦٥﴾

*“Wala hii si kauli ya shetani aliyefukuzwa (katika rehema za Mwenyezi Mungu.) (81:25)*

**Nne**, Sote tunamfahamu shetani kuwa ni kiumbe dhaifu pamoja na kuwa hatumuoni. Sasa ikiwa shetani ameleta maneno na ujumbe mzito uliomo ndani ya Qur'an, kwanini na mashetani wengine nao hawakai pamoja kujibu zile changamoto zilizotolewa? “Mahound” kama alivyomwita Rushdie ni shetani mmoja tu, je pamekuwa na uzito gani kwa wanaadamu pamoja na majini wakichanganyika kuleta mfano wa angalau sura moja ya Qur'an? Qur'an imetoa changamoto hiyo tangu kuanza kushuka kwake:

قُلْ لِّئِنِ اجْتَمَعَتِ الْإِنْسُ وَالْجِنُّ عَلَىٰ أَنْ يَأْتُوا بِمِثْلِ هَذَا الْقُرْآنِ لَا

يَأْتُونَ بِمِثْلِهِ وَلَوْ كَانَ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظَهِيرًا ﴿٨١﴾

*“Sema “Hata wakijikusanya watu (wote) na majini kuleta mfano wa hii Qur'an basi hawangaliweza kuleta mfano wake, hata kama watasaidiana (vipi) wao kwa wao.” (17:88)*

**(vi)Madai Kuwa Mtume(s.a.w) Aliandika Qur'an kwa Msaada wa Mayahudi na Wakristo:**

Tunakutana na madai mengine kuwa Mtume(s.a.w) aliandika Qur'an baada ya kusoma Biblia au wengine wanadai kuwa alifundishwa na Mayahudi na Wakristo ndio naye akaandika Qur'an kwa kuzingatia wakati na watu aliokuwa nao. Makafiri wa karne hii sio tu walioanzisha madai haya bali madai haya ni makongwe kama ilivyo kongwe Qur'an yenyewe.

Pametolewa madai mengi ya namna hii kuanzia karne hizo za kushushwa Qur'an kwa Mtume(s.a.w) mpaka hivi leo. Hebu tuangalie dai hili la baadhi ya makafiri wa karne hizi za usoni ambalo limegawanyika katika sehemu zifuatazo:

**(a)Dai la Kufundishwa na Padri Bahira:**

Baadhi ya makafiri wanadai kuwa Mtume Muhammad(s.a.w) alijifunza Uyahudi na Ukristo katika safari zake mbili za biashara alizofanya Sham (Syria), hasa katika safari yake ya kwanza alipokutana na Padri Bahirah, alipokuwa na umri wa miaka 12. Tunavyojifunza katika historia ni kuwa Bahirah alikutana na Mtume(s.a.w) njiani na kuashiria kwa Ami yake Abutwalib, kuwa anamkisia kijana wake (Muhammad) ana sifa za yule mtume aliyetabiriwa katika Injili (Rejea Qur'an 61:6). Je, inamkinika kuwa mazungumzo haya ya njiani ya muda mfupi yawe ndiyo yaliyompelekea Mtume(s.a.w) kuandika Qur'an miaka 28 baada ya makutano hayo? Ikumbukwe kuwa Mtume(s.a.w) alianza kushushiwa wahy wa Quran alipokuwa na umri wa miaka arobaini ambapo alikutana na Bahirah akiwa na umri wa miaka kumi na mbili.

Safari ya pili ya Mtume(s.a.w) kwenda Syria kwa biashara ni pale alipokodiwa na Bibi Khadijah alipokuwa na umri miaka ishirini na tano. Katika kumbukumbu za historia, Mtume(s.a.w) hakufanya mkutano wowote na Wakristo wala Mayahudi kabla ya Utume.

**(b)Dai la Kunakili Biblia**

Aidha wengine wanasema Muhammad alinakili mafundisho ya Biblia na halafu akadai kuwa yanatoka kwa Allah(s.w). Lakini inadaiwa kuwa hakunakili kila kitu bali alichagua sehemu fulani fulani alizoziona nzuri. Ushahidi wanaoutoa ni kuwa zipo sehemu katika Qur'an ambazo zinafanana na zile zilizomo katika Biblia. Hivyo, kwa kuwa ilitangulia Biblia kabla ya Qur'an ni wazi kuwa Qur'an ndiyo iliyochota kutoka katika Biblia. Madai haya ni dhaifu kwa sababu zifuatazo:

- (i) Muhammad(s.a.w) alisema na kuisitiza kuwa Qur'an imetokakwa Mwenyezi Mungu(s.w).
- (ii) Muhammad(s.a.w)hakujuua kusoma wala kuandika.
- (iii)Nakala ya kwanza ya Agano la Kale(Old Testament) kufasiriwa kwa lugha ya Kiarabu ilipatikana mwaka 900A.D.Wakati huo ilikuwa imekwishapita miaka 200 tangu Muhamad kutawafu. Ama Agano Jipya (New Testament) lilitolewa kwa mara ya kwanza mwaka 1616, miaka elfu baada ya Muhammad(s.a.w) kufariki dunia!
- (iv)Qur'an (4:82) imesema kuwa lau kama hii Qur'an ingetoka k w a a s i y e kuwa Allah ingekuwa na khitilafu nyingi. Hivyo mtu mwenye shaka na aitumie fursa hiyo kutafuta khitilafu katika Qur'an.
- (v)Isitoshe, ikiwa kuna tungo mbili au vitabu viwili vimefanana, kufanana huko peke yake si ushahidi wa kutosha kuwa kitabu kimoja kimenakili kutoka katika kitabu cha kwanza kuandikwa. Hii ni kwa sababu yawezekana pia kuwa vitabu vyote viwili vikawa vimetegemea au kunakili kutoka katika kitabu cha tatu ambacho sisi hatukijui. Ilivyo ni kuwa Taurati, Injili na Quran ni vitabu vya Mwenyezi Mungu. Hivyo ni wazi kuwa kama Biblia imenukuu aya halisi za Tourati na Injili lazima aya hizo zitafanana na aya za Qur'an,kwa vile zote zinatokana na Allah(s.w).
- (vi) Isitoshe utafiti uliofanywa na baadhi ya wanazuoni umeonesha kuwa amri kumi za Mungu zilizomo katika Agano la Kale kwa mfano, zimekuwemo katika vitabu vya Wahindu kabla ya kuja kwa Agano hilo la kale. Je, tuseme biblia ilinakili amri hizo kutoka kwa Wahindu? Si lazima iwe hivyo.

Pamoja na kufanana huko katika baadhi ya sehemu bado kimsingi Biblia na Qur'an zimetofautiana kiasi kikubwa.

## **Tofauti za Kimsingi kati ya Qur'an na Biblia**

**Kwanza**,Biblia si kitabu kimoja bali ni mkusanyiko wa vitabu 73 kwa mujibu wa madhehebu ya Wakatoliki au vitabu 66 kwa mujibu wa madhehebu ya Waprotestanti. Vitabu hivyo viliandikwa na waandishi wasiopungua 40. Qur'an ni kitabu kimoja kilichotoka kwa Mwenyezi Mungu na aya zake zote ziliandikwa mara tu baada ya kushuka.

**Pili**, Biblia ni kitabu chenye mchanganyiko wa maneno ya Mwenyezi Mungu, Mitume na maoni ya wanahistoria. Qur'an ni neno la Allah(s.w) tu peke yake. Hata maneno ya Muhammad(s.a.w) hayamo katika Qur'an.

**Tatu**, Katika Agano la Kale na Jipya yapo maelezo juu ya historia ya maisha ya Mitume. Kumbukumbu la Torati siyo tu ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa watu bali pia historia ya maisha ya nabii Mussa (a.s). Injili ya Mathayo, Luka, Marko na Yohana zinaelezea historia ya Yesu kama ilivyosimuliwa

na wanafunzi wake. Qur'an inataja habari za mitume waliopita ili kutoa mafundisho kwa watu lakini sio kama sira (biography) za mitume hao.

**Nne**, Biblia inavyo vitabu kadhaa ambavyo viliandikwa miaka mingi sana baada ya kutawafu mitume hao. Ndio maana wanazuoni Wakikristo hupata matatizo sana katika uchambuzi wa maandiko hayo kwani hushindwa kumjua nani mwandishi na aliandika lini. Kwa mfano katika Biblia iliyotolewa na Collins iitwayo: Revised Standad Version ya 1971 uk. 12-17 imeandikwa kuwa Mwandishi wa 1 Samweli hajulikani, pia hajulikani mwandishi wa kitabu cha 2 Samweli, 1 Wafalme, 1 Mambo ya Nyakati, Esta, Ayubu, Yona na Habakuki. Hali kadhalika mpaka leo kuna wasiwasi kama kitabu cha Waebraia kiliandikwa na Paulo au na mtu mwingine. Na Encyclopaedia Britannica inakiri kuwa mpaka hivi hatuna uhakika jinsi au wapi vitabu 4 vya Injili vilizuka. Kinyume chake Qur'an yote iliandikwa wakati wa uhai wa Muhammad(s.a.w) na ikahifadhiwa kitabuni na vifuani mwa mamia ya watu.

**Tano**, Injili 4 zilizomo katika Agano Jipya siyo Injili zote zilizoandikwa. Zilikuwapo Injili nyingine nyingi. Ilifanyika Sinodi (mkutano wa wawakilishi wa makanisa) mwaka 325 ili kuamua Injili zipi zichukuliwe na zipi zikataliwe. Injili ya Barnabas ilikataliwa. Na katika historia ya Kanisa viko vitabu vilivyokubaliwa na baadaye kukataliwa na kinyume chake. Ni binaadamu waliokuja baadaye ndio waliokuwa na uwezo wa kuamua lipi liwe neno la Mungu na lipi lisiwe. Katika Uislamu hakukuwa na Ijtimai yoyote iliyokaa kuamua sura ipi iwe Qur'an ama isiwe.

### *(c) Dai la Kufundishwa na Jabir na Yasir:*

Makafiri wengine wanadai kuwa Mtume(s.a.w) alifundishwa na Jabir na Yasir waliokuwa watumwa kutoka Ethiopia (Uhabeshi) na wakasilimu mbele ya Mtume(s.a.w). Wanadai hivyo kwa kuwa bwana wao aliyekuwa akiwatesa sana kwa sababu ya kusilimu kwao alikuwa akiwapiga sana na kuwaambia: *“Mnamfundisha Muhammad?”* na walikuwa wakijibu *“Kwa jina la Allah hatumfundishi bali ndiye anayetufundisha na kutuongoza”*.

Bila ya kuangalia majibu ya Jabir na Yasir, wameshikilia swali alilouliza bwana wao kuwa ndio ushahidi wao kuwa Mtume(s.a.w) alifundishwa Qur'an na watu hao.

Makafiri wengine wamedai kuwa Mtume(s.a.w) aliandika Qur'an kwa kusaidiwa na Salman aliyekuwa Mfursi (Persian). Salman alikuwa Mzoroastian kabla ya kuwa Mkristo huko Sham (Syria). Baadaye Salman alisafiri kwenda Madina ambapo alikutana na Mtume(s.a.w) na kusilimu.

Madai haya ni dhaifu kwa sababu mbili. Kwanza, karibu theluthi mbili ya Qur'an ilishuka Makka kabla Mtume(s.a.w) hajahamia Madina ambapo

alikutana na Salman. Pili, fasihi ya lugha iliyotumika katika Qur'an ni ya hali ya juu mno kiasi ambacho wanafasihi mashuhuri wa Kiarabu walijaribu kwa miaka mingi kuigiza Qur'an bila ya mafanikio yoyote, itakuwaje Mfursi awe ndiye aliyelandika?

Madai haya yamerejewa kwenye Qur'an kama tunavyosoma katika aya ifuatayo:

وَلَقَدْ نَعَلْنَا أَنَّهُمْ يَقُولُونَ إِنَّمَا يُعَلِّمُهُ بَشَرٌ لِّسَانُ الَّذِي

يُلْحِدُونَ إِلَيْهِ أَعْجَمِيٌّ وَهَذَا لِسَانٌ عَرَبِيٌّ مُبِينٌ ﴿١٠٣﴾

*“Na bila shaka tunajua kwamba wanasema:”Yuko mtu anayemfundisha,” (lakini) lugha ya yule wanayemuelekezea (kuwa anamfundisha Mtume) ni ya kigeni na hii (lugha iliyotumika katika Qur'an) ni lugha ya Kiarabu fasaha (bulbul).” (16:103)*

Madai yote haya pamoja na madai mengine mengi ambayo yamekuwa yakitolewa katika muda wote wa historia tangu ishuke Qur'an mpaka hivi leo, ni madai dhaifu mno ambayo hayana ushahidi wowote wa kiakili au wa kihistoria kuwa mwandishi (mtunzi) wa Qur'an ni mwingine asiye kuwa Allah(s.w).

Historia ya Mtume(s.a.w) imeandikwa na kuhifadhiwa vema kuliko historia ya mtu yeyote ulimwenguni, lakini hatuoni katika historia hiyo mahali popote tunapofahamishwa kuwa alikaa kitako kwa mtu yeyote kujifunza chochote. Kwani kama Muhammad(s.a.w) angelikuwa amesoma kwa Makasisi na Mapadri wa Kiyahudi na Kikristo au kwa mtu yeyote yafuatayo yangelijitokeza.

- (i) Muhammad(s.a.w) hangelificha kueleza hayo kwani alikuwa mashuhuri katika maisha yake yote kwa kuhubiri na kusema ukweli. Aliitwa As-swadiq - Mkweli. Ndani ya Qur'an yenyewe yamezungumzwa mambo yake ya ndani lakini bado hakuyaficha bali aliyadhahirisha kama yalivyo.
- (ii) Hangelifundisha imani iliyo tofautiana sana na Ukristo na Uyahudi hasa kuhusu misingi ya dini hizo. Lakini imani ya Kiislamu ni mbali na ni kinyume kabisa na imani ya Kikristo na Kiyahudi.
- (iii) Yeyote yule aliyemfundisha angeliweza kuandika kitabu mfano wa Qur'an angalau sura moja. Lakini hakutokea mtu yeyote mwenye uwezo huo.
- (iv) Mayahudi ambao katika Qur'an wameitwa “Ahlul-Kitaabi” au wana wa Israil (Bani Israil) wamekuwa katika muda wote wa utume wake wakimhoji-hoji Mtume Muhammad(s.a.w) na kumcheza shere na walikuwa wakimficha Mtume vitabu vyao. Kunawezekanaje watu hawa kama ndio waliomfundisha Mtume Qur'an wawe wanamhoji hoji tena juu ya Qur'an? Kama wanalikuwa wamemfundisha Mtume chochote, kwa

nini wasingelikuwa watu wa kwanza kutangaza kwa watu kuwa wao ndio waliomfundisha ili kuonesha uongo wa utume wake?

- (v) Mtume Muhammad(s.a.w) asingelikuwa mkweli katika utume wake na mwaminifu katika kutoa ujumbe aliotumwa autowe kwa watu, wafuasi wake wasingelikuwa wanyenyekevu kwake kiasi hicho na wasingelijizatiti katika kusimamisha mafundisho yake kiasi hicho katika mazingira magumu ya kufa na kupona. Historia inaonesha kuwa Waumini waliomfuata hawakumsaliti hata chembe.

## **Qur'an ni Furqan (inasadikisha Ukweli)**

Sifa ya Qur'an ni kuwa inasadikisha yaliyo ya kweli katika vitabu vilivyopita. Hivyo Muislamu anaweza kujua kwa urahisi kabisa lipi ni sahihi katika Biblia na lipi si sahihi. Lolote lililomo katika vitabu vilivyotangulia ambalo linawafikiana na Qur'an ni sahihi. Na lolote linalokwenda kinyume na Qur'an ni batili.

Jambo la kusesitiza hapa ni kuwa kuhusu vitabu vilivyotangulia Qur'an imevitaja kuwa ni Suhf, Zabur, Taurat na Injili. Muislamu anayevikana vitabu hivi katika asili yake anakoma kuwa Muislamu.

Kama tulivyokwishasema Biblia inavyo kwa uchache vitabu 66. Agano la Kale lina vitabu 39 na Jipya inavyo 27. Katika vile 39 vya Agano la Kale ni vitano tu ndivyo vinavyoitwa Taurati ya Musa.

Qur'an inapotaja Taurati haikusudii Biblia au vitabu 39 vya Agano la Kale wala hivyo vitano vinavyodaiwa kuwa viliandikwa na Musa. Qur'an imeitaja Taurati kama ni ufunuo kutoka kwa Allah. Lakini tunaona kitabu cha Mwanzo ambacho kina taarifa za zamani sana kabla ya yeye (Musa) kuzaliwa. Hatuna uhakika kama kitabu hicho cha Mwanzo ilikuwa ni sehemu ya ufunuo aliouputa kwenye mlima Sinai.

Isitoshe nusu ya kitabu cha "Kutoka" inazungumzia habari za kutoka kwa Wayahudi Misri. Hayo pia yalitokea kabla ya Musa kupata Taurati. Kitabu cha Kumbukumbu la Torati ambacho inadaiwa kiliandikwa na Musa kimeandikwa pia habari za kufariki kwa Musa:

*Basi Musa, mtumishi wa BWANA, akafa huko, katika nchi ya Moabu, kukabili Beth-peori; lakini hapana mtu ajuaye kaburi lake hata leo. Musa alikuwa mtu wa miaka mia na ishirini alipokufa; jicho lake halikupofuka, wala nguvu za mwili wake hazikupunguka. Wana wa Israeli wakamwombolezea Musa katika uwanda wa Moabu siku thelathini; basi siku za maombolezo ya matanga ya Musa zikaisha. (Kumbukumbu la Torati 34:4-12)*

Ni dhahiri kuwa upo wasiwasi kama Nabii Musa (a.s) ndiye mwandishi wa kitabu hiki kwa sababu asingeweza kusimulia habari ya kifo chake na matanga yake mwenyewe.



(vii) Dai kuwa Muhammad(s.a.w) alitunga Qur'an ili kuleta Umoja na Ukombozi wa Waarabu:

Wako baadhi ya watu wanaodai kuwa Muhammad(s.a.w) aliitunga Qur'an ili awaunganishe na kuwakomboa Waarabu. Dai hili pia halina nguvu kwa sababu zifuatazo:

**Kwanza**, lau dai hilo lingekuwa la kweli basi hapana shaka kuwa Qur'an ingetia msisitizo mkubwa sana katika mada ya umoja na ukombozi wa Waarabu. Kwa hakika hakuna aya hata moja katika Qur'an nzima inayolingania umoja na ukombozi wa taifa la Kiarabu. Itayumkinikaje basi Muhammad(s.a.w) atunge Kitabu kwa lengo la kujenga utaiwa wa Waarabu na kusiweko katika kitabu hicho hata aya moja juu ya suala hilo?

**Pili**, msingi wa umma (taifa) unaofundishwa na Qur'an umejengwa juu ya itikadi ya haki na Qur'an inapinga hisia zote za utaiwa kwa kufuata misingi ya rangi au kabila. Kila anayekubali itikadi ya Uislamu anakubalika katika umma wa Waislamu bila ya kujali rangi au kabila, au Taifa. Umoja uliodhihiri Arabia baada ya kushamiri kwa Uislamu ulikuwa umejengwa juu ya misingi ya Uislamu na siyo utaiwa wa Kiarabu.

**Tatu**, lau umoja wa Waarabu ungekuwa ndilo jambo lililomsukuma Muhammad(s.a.w) hapana shaka angekubali kuwa mfalme wa Waarabu ili atumie fursa hio kujenga umoja wa taifa la Waarabu.

Lakini tunaona alikataa ufalme pale wakuu wa Kikuraysh walipotaka kumrubuni ili aache kuutangaza Uislamu.

**Nne**, zipo aya katika Qur'an zinazolikanusha dai hilo. Aya mojawapo ya Qur'an yasema:

وَإِذْ قَالَتِ الْمَلَائِكَةُ يَا مَرْيَمُ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَاكِ وَطَهَّرَكِ وَأَصْطَفَاكِ

عَلَى نِسَاءِ الْعَالَمِينَ ﴿٤٢﴾

*“Na (kumbuka) Malaika waliposema: Ewe Maryamu! Kwa hakika Allah amekuchagua na kukutakasa na kukutukuza kuliko wanawake wa ulimwengu (wote).” (3:42)*

Aya hii inamzungumzia Maryamu, mama yake Nabii Isa(a.s). Maryamu alikuwa ni Myahudi. Na Wayahudi walikuwa wanadharau Waarabu kuwa ni taifa duni. Muhammad(s.a.w) alikuwa ni Mwarabu na Qur'an imeshuka kwa lugha ya Kiarabu na watu wa mwanzo kusomewa hii Qur'an walikuwa Waarabu.

Swali ni hili: Ikiwa Muhammad(s.a.w) alitaka kukuza hisia za utaiwa wa Waarabu vipi basi aweke katika Qur'an aya hii inayomsifu mwanamke wa Kiyahudi kuwa amechaguliwa, ametakaswa na kutukuzwa na Allah(s.w) kuliko wanawake wote? Kwa nini asimsifie mama yake au mwanamke mwingine yeyote wa Kiarabu?

Aya nyingine ni hii ifuatayo:

يَبْنَى إِسْرَائِيلَ أَذْكُرُوا نِعْمَتِي الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ وَأَنِّي فَضَّلْتُكُمْ عَلَى

الْعَالَمِينَ ﴿٤٧﴾

*Enyi kizazi cha Israili (Mayahudi)! Kumbukeni neema zangu nilizokuneemesheni, na nikakutukuzeni kuliko viumbe wengine. (2:47)*

Mifano hii yaonesha kuwa haiingii akilini kuwa Muhammad(s.a.w) awe ametunga Qur'an kwa lengo la kuleta umoja na utukufu wa taifa la Waarabu halafu ndani ya hiyo hiyo Qur'an akasifia kwa sifa za kipeo cha juu kabisa watu walio maadui wa Waarabu!

#### **(viii) Dai la Kurekebisha Tabia ya Waarabu:**

Miongoni mwa wale wanaosema kuwa Muhammad(s.a.w) ndiye aliyetunga Qur'an wapo wanaodai kuwa Muhammad(s.a.w) alifanya hivyo kwa nia nzuri ya kutaka kujenga tabia na mwenendo mzuri miongoni mwa ndugu zake Waarabu. Yaani, Muhammad(s.a.w) alichukizwa sana na tabia mbaya walizokuwa nazo Waarabu wa zama zake na hivyo akaona lazima ajitahidi kuziondoa. Na ili afanikishe lengo lake hilo akaona atunge Qur'an na asingizie kuwa inatoka kwa Allah(s.w). Dai hili pia halina nguvu kwa sababu zifuatazo:

**Kwanza**, kujenga mwenendo mzuri wa tabia za watu ni jambo jema ambalo laweza kutekelezwa pasi na kutumia udanganyifu na na uovu mwingine. Ni kipi kilichomfanya Muhammad(s.a.w) atumie uwongo na udanganyifu ili awafundishe watu kuwa wa kweli na waaminifu?

**Pili**, Qur'an imeitaja dhambi ya kuzua uwongo kuwa ni miongoni mwa madhambi makubwa:

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ قَالَ أُوحِيَ إِلَيَّ وَلَمْ يُوحَ إِلَيْهِ شَيْءٌ وَمَنْ قَالَ سَأُنزِلُ مِثْلَ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الظَّالِمُونَ فِي غَمْرَاتِ الْمَوْتِ وَالْمَلَائِكَةُ بَاسِطُو أَيْدِيهِمْ أَخْرِجُوا أَنفُسَكُمُ الْيَوْمَ

تَجَزَّوْنَ عَذَابَ الْهَوْنِ بِمَا كُنْتُمْ تَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ غَيْرَ الْحَقِّ وَكُنْتُمْ

عَنْ آيَاتِهِ تَسْتَكْبِرُونَ ﴿١٣﴾

*"Na nani dhalimu mkubwa kuliko yule amtungiaye uwongo Allah au mwenye kusema: "Nimeletewa wahyi," na hali hakufunuliwa chochote; na yule asemaye: "Nitateremsha (ufunuo) kama ule aliouteremsha Allah." Na kama ungewaona madhalimu watakapokuwa katika mahangaiko ya mauti, na Malaika wamewanyooshea mikono yao (na kuwaambia): "Zitoeni roho zenu! Leo mtalipwa adhabu ifedheheshayo kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyasema juu ya Allah pasipo haki na kwa vile mliyokuwa mkizifanyia kiburi Aya zake." (6:93)*

Aya hii inasema hakuna dhalimu mkubwa kuliko yule anayemzulia uwongo Allah au atakayesingizia kuwa amepata wahyi kutoka kwa Allah na ilhali hakupata. Halafu aya hii inataja jinsi watu wa aina hiyo watakvoyofedheheshwa na jinsi watakvoyopapatika wakati wa kutolewa roho zao.

Lau kama Muhammad(s.a.w) angekuwa ndiye aliyeitunga halafu akamsingizia Allah(s.w), asingeiweka aya kama hii katika Qur'an kwa sababu angehisi kuwa anajitukana mwenyewe na kujilaani mwenyewe. Pia kwa kuhofia kuwa yaweza kutokezea siku ambayo watu watamgundua angehakikisha kuwa anaiandika aya hii kwa namna ambayo haitamfedhehesha hapo atakapojulikana.

Angeweza kwa mfano kusema: *"Hapana lawama kwa wale ambao, ikiwa hapana budi kusema uwongo kwa ajili ya Allah."* St. Paulo kwa mfano ameandika hivi katika Biblia:

*Lakini ikiwa kweli ya Mungu imezidi kudhihirisha utukufu wake kwa sababu ya uongo wangu, mbona mimi ningali nahukumiwa kuwa ni mwenye dhambi."*  
(Warumi 3:7)

Aidha madai kuwa Muhammad(s.a.w) alitunga Qur'an ili aitumie katika kurekebisha mwenendo wa tabia za watu pia yanatenguliwa na ukweli kwamba Qur'an haikushuka yote mara moja bali ililetwa kidogo kidogo kwa muda wa miaka 23. Na katika kipindi hicho Qur'an ilitoa ahadi ya kujibu maswali yote yatakaoulizwa wakati Qur'an bado inashuka.

..... وَإِنْ تَسْأَلُوا عَنْهَا حِينَ يُنَزَّلُ الْقُرْآنُ تُبَدَّ لَكُمْ ..... ﴿١٤﴾

*...Na kama mtayauliza, maadam inateremshwa Qur'an mtabainishiwa....."*  
(5:101)

Watu waliutumia fursa hiyo iliyotolewa na Qur'an kuuliza maswali mbali mbali kama vile juu ya ulevi, kamari, hedhi, ngawira, roho na hata juu ya watu

kama Dhur-qarnain. Katika kuyajibu maswali hayo Qur'an imetumia msembo "Wanakuuliza juu ya jambo kadhaa. Sema: Lipo namna kadhaa." Kwa mifano halisi tazama Qur'an 2:189, 2:215, 2:217, 2:219, 2:220, 2:222, 5:4, 7:187, 8:1, 17:85, 18:83, 20:105 na 79:42.

Tatizo linalojitokeza hapa ni kwamba Muhammad(s.a.w) asingeweza kujua kuwa maswali aliyowaruhusu watu kuuliza yatakuwa yanahusu marekebisho ya mwenendo na tabia za watu. Kwani inadaiwa kuwa haitakuwa jambo la busara kwa rais anayetaka kuzungumzia hali ya chakula nchini mwake kuwaita waandishi wa habari na kuwaruhusu waulize maswali yoyote yanayowatatiza. Rais huyo atakuwa na hakika gani kuwa watauliza juu ya hali ya chakula na siyo juu ya wafungwa wa kisiasa?

### *(ix)Dai kuwa Muhammad Alitunga Qur'an ili Ajinufaishe Kiuchumi*

Baadhi ya watu wanasema kuwa Muhammad (saw) ndiye mtunzi wa Qur'an na alifanya ili ajinufaishe kiuchumi. Wanasema kuwa yawezekana kuwa Muhammad(s.a.w) aliitunga Qur'an lakini akasema imetoka kwa Allah ili ajipatie manufaa makubwa zaidi. Kama tunazungumzia uwezekano, ni kweli kuwa uwezekano kama huu unaweza kuwepo. Swali la kujiuliza ni hili:Ni manufaa gani hasa ambayo Muhammad(s.a.w) tuseme alikuwa akiyawania? Manufaa hayo yanaweza kuwa ni wasaa wa mali, mamlaka, au ufalme. Hebu tuyafuatilie zaidi madai haya.

## **Muhammad Hakuwa Tajiri Baada ya Utume**

Kusema kuwa Muhammad(s.a.w) aliitunga Qur'an ili ajinufaishe maana yake ni kuwa Muhammad(s.a.w) alikuwa mrongo aliposema Qur'an inatoka kwa Allah(s.w). Madai kuwa Muhammad(s.a.w) alikuwa mwongo yanakwenda kinyume na ushahidi wa historia ya maisha yake. Hata hivyo kwa sababu za kutaka kuendeleza mjadala na utafiti wetu, hebu na tuuweke kando ukweli na uaminifu wa Muhammad(s.a.w) na tuchunguze alijinufaishaje kwa kudai kuwa Qur'an ni neno la Allah(s.w).

Tukianza na hali yake ya kiuchumi tunaona kuwa alikuwa na hali nzuri kabla kuliko baada ya kupata utume. Kabla ya kupata utume, alipokuwa na umri wa miaka 25 alimwoa bibi Khadija ambaye alikuwa ni mfanyabiashara tajiri sana. Muhammad(s.a.w) aliishi naye kwa wasaa mkubwa na pasi na dhiki yoyote. Baada ya kupata utume hali yake kiuchumi ilikuwa ngumu kwa kuwa karibu mali yote ilitumika kuwasaidia Waislamu wachache waliokuwa wakiteswa na kubughudhiwa na makafiri wa Makka. Na hata baada ya kusimama dola ya Kiislamu hali ya kiuchumi ya Muhammad(s.a.w) ilikuwa ndio ngumu zaidi.

## Baadhi ya Mifano ya Hali yake Kiuchumi

Katika kitabu cha Hadith cha An-Nawawi, mmoja wa wakeze Mtume(s.a.w) Bibi Aisha (r.a) amesema kuwa wakati mwingine ulipita mwezi mzima au hata miezi miwili pasi na moto kukokwa katika nyumba ya Mtume(s.a.w) kwa sababu hakukuwa na cha kupika. Walikuwa wakiishi kwa kula tende na kunywa maji. Wakati mwingine walipata maziwa ya mbuzi kutoka kwa watu wa Madina.

Katika kitabu cha maisha ya Muhammad(s.a.w) kilichoandikwa na Martin Lingas<sup>1</sup> imeelezwa kuwa Mtume(s.a.w) na familia yake walikuwa wanaishi katika hali ngumu sana kiuchumi. Wakati mwingine hawakupata japo hizo tende za kutosha.

Hali hii haikuwa ni matatizo ya kupita tu bali ilikuwa ndio mwenendo wa kudumu wa maisha. Mtume(s.a.w) aliishi katika hali hiyo wakati ambao angeweza kuishi kama mfalme kama angetaka. Kwa hakika ni kutokana na kuamua kwa makusudi kuishi maisha hayo pamoja na kuwa angeweza kuishi maisha ya anasa ndipo wakeze Mtume(s.a.w) wakaja juu. Kwa nini waendeleo kuishi maisha ya dhiki na hali wanaweza kuishi kwa wasaa? Mtume alitazwa na manung'uniko hayo ya wakeze.

Allah(s.w) akamteremshia wahyi uliomwamuru awaambie wakeze ama wamchague Allah(s.w) na Mtume wake au starehe ya kupita ya ulimwengu huu:

يَتَأَيُّهَا النَّبِيُّ قُلْ لِأَزْوَاجِكَ إِن كُنْتُنَّ تُرِدْنَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا وَزِينَتَهَا  
فَتَعَالَيْنَ أُمَتِّعَنَّ وَأَسْرَحَنَّ بِسَرَاحٍ جَمِيلًا ۖ وَإِن كُنْتُنَّ  
تُرِدْنَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَالْآخِرَةَ فَإِنَّ اللَّهَ أَعَدَّ لِلْمُحْسِنَاتِ مِنكُنَّ  
أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٣٨﴾

*Ewe Mtume! Waambie wake zako. "Ikiwa mnapenda maisha ya (hii) dunia na uzuri wake, njooni, nitakupeni kitoka nyumba, na kukuacheni muwachano mzuri. Na kama mnamtaka Allah na Mtume wake na nyumba ya Akhera, basi Allah amewaandalia wafanyao mema hayo, miongoni mwenu, malipo makubwa." (33:28-29)*

Kuhusiana na jinsi chumba cha Mtume kilivyokuwa Umar (r.a) anasema:

*Niliona kuwa mali yote iliyokuwa chumbani mwake ilikuwa ni vipande vitatu vya ngozi na fungu dogo la shayiri lililokuwa katika koa. Nikaangaza huku na huko lakini sikuona kitu kingine chochote. Nikaanza kulia. Akaniuliza: Kwanini unalia? Nikajibu: 'Ewe Mjumbe wa Allah! Kwanini nisilie? Naona alama ya*

*mkeka katika mwili wako, na naangalia pia mali yote uliyo nayo katika chumba hiki. Ewe, Mjumbe wa Allah! Mwambie Allah atuzidishie riziki, Waajemi na Warumi ambao hawana imani ya kweli na ambao hawamwabudu Allah bali wafalme wao - akina Kaizari - wanaishi katika mabustani yanayopita mito kati yao, lakini Mjumbe mteule na mja wa Allah akaishi katika umasikini kama huu!’ Mtume alikuwa amejipumzisha hali ya kuwa amelalia mto, lakini aliponisikia nikisema hivyo, akaketi na kusema; ‘Ewe Umar! Je, bado una shaka juu ya jambo hili? Raha na starehe za akhera ni bora kuliko raha na starehe za ulimwengu huu. Makafiri wanafaidi starehe zao zote hapa duniani na sisi tutakuwa na starehe zetu zote huko akhera.’ Nikamwomba Mtume kwa kusema: ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Niombe msamaha kwa Allah. Kwa hakika nilikosea.’*

*Alipoulizwa juu ya kitanda cha Mtume(s.a.w) kilivyo, Bibi Aisha alijibu: ‘Ni ngozi iliyojazwa magome ya mitende.’*

Ikumbukwe kuwa Muhammad(s.a.w) aliishi maisha ya namna hiyo kwa hiari yake kwa sababu kila alipopata zawadi aliligawa yote kwa mafakiri pasi na yeye mwenyewe kuchukua chochote. Safari moja alipewa na Chifu wa Fidak zawadi zilizobebwa na ngamia wanne, lakini alizigawa zote.

Wakati wa kutawafu kwake Muhammad(s.a.w) hakuwa na hata senti moja mfukoni. Alikuwa na dinari saba karibu ya kufariki kwake lakini akazigawa kwa maskini kabla ya kufariki. Isitoshe alipofariki, pamoja na ushindi mkubwa alioupata katika vita na pamoja na kuwa alikuwa ndiye kiongozi wa dola ya Kiislamu, Muhammad (s.a.w) alikuwa akidaiwa na ngao yake ilikuwa mikononi mwa Myahudi mmoja wa Madina kama rehani ya deni hilo.

Ipo mifano mingine mingi inayoonesha kuwa katika kipindi chake chote cha utume, Muhammad(s.a.w) aliishi katika maisha ya kujinyima. Kutokana na ushahidi huu unaotokana na historia ya maisha yake, ni wazi kuwa madai kuwa Muhammad(s.a.w) aliitunga Qur'an ili apate kujinufaisha kiuchumi hayana msingi.

**(x) *Dai kuwa Muhammad(s.a.w) aliitunga Qur'an ili Kuwania Madaraka na Ukubwa:***

Aidha, fikra kuwa huenda Muhammad(s.a.w) aliitunga Qur'an kwa sababu aliwania ukubwa na madaraka pia ni vigumu sana kuithibitisha, kwa sababu zifuatazo:

**Kwanza**, Muhammad(s.a.w) alijulikana sana ulimwengu mzima kama kiongozi aliyefanikiwa sana katika historia ya binaadamu. Mtu mwenye sifa kama hizo angeweza kuchukua uongozi na madaraka bila hata kudai kwanza utume. Kwa hakika kufanya hivyo kungekuwa rahisi zaidi kwake kama alikuwa anataka madaraka kuliko kudai utume kwanza.

**Pili**, Qur'an imetamka wazi wazi kuwa hakuna mtu yeyote ikiwa ni pamoja na Muhammad (saw) mwenyewe awezaye kuleta mfano wake. Kama lengo lake lilikuwa kupata utukufu miongoni mwa watu angejitapa kuwa ndiye mtunzi wa kitabu hiki kinachovishinda vitabu vyote.

Hata hivyo tabia yake haikuonesha dalili zozote za mtu anayepigania madaraka au utukufu. Kupenda madaraka na utukufu kwa kawaida kunajionesha kwa mtu kutaka majumba ya fahari ya kifalme, nguo za kipekee, kutaka kusifiwa na kuabudiwa na watu, n.k. Muhammad(s.a.w) alionesha mfano wa ajabu kabisa wa unyenyekevu. Pamoja na amana kubwa ya unabii aliyokuwa nayo na dhamana kubwa sana ya kuongoza dola ya Kiislamu, Muhammad(s.a.w) alikuwa akisaidia kufanya kazi ndogo ndogo za nyumbani. Akishona nguo zake na kuripea viatu vyake na akimkama mbuzi wake. Alikuwa akimsikiliza kwa makini kila aliyemwendea, kiasi ambacho Qur'an imesema makafiri walikuwa wakilalamika kwanini anawasikiliza hata wanyonge (Qur'an 9:61).

Wakati fulani Waislamu walikuwa wanasimama walipotaka kumwamkia kama ishara ya heshima. Lakini aliwakataza na kuwaambia, "Msisimame kama Waajemi wanavyofanya, baadhi yao kuwatukuza wengine."

Mifano mingine ya unyenyekevu wake ni ile iliyotajwa na mwanachuoni maarufu Dk. Gamal Badawi:

*Siku moja Mtume Muhammad(s.a.w) alikuwa akisafiri pamoja na baadhi ya maswahaba wake ambao njiani walipiga kambi na kuanza kupika chakula kwa kugawanya kazi za kufanya. Muhammad(s.a.w) alichagua kazi ya kutafuta kuni. Maswahaba wake wakamwambia asifanye kazi yoyote kwani wao watamfanyia. Muhammad(s.a.w) akawajibu, "Najua kuwa mnaweza kunifanyia lakini nachukia kupewa nafuu kuliko nyinyi."*

Mfano mwingine ni huu:

*Mtu mmoja alimwendea Mtume(s.a.w) huku akitetema kwa kumheshimu. Muhammad(s.a.w) alimwomba mtu yule amsogelee na akamkumbatia na kumpigapiga mgongoni kwa huruma kubwa, halafu akamwambia, 'Tulia ndugu yangu, mimi ni mtoto wa mwanamke aliyekuwa anakula mkate mkavu.'*

Aidha imeripotiwa kuwa baadhi ya watu walimwendea Mtume(s.a.w) na wakamsifu kwa kusema: "Ewe Mjumbe wa Allah(sw), wewe u-mbora kuliko sote na wewe ni mtoto wa mbora wetu, wewe ni kiongozi wetu na ni mtoto wa kiongozi wetu". Jibu lake lilikuwa:

*Enyi watu, semeni lile mlilolisema mwanzo (yaani "Ewe Mjumbe wa Allah,") na msikubali shetani awapotezeni. Mimi ni Muhammad, mja wa Allah na Mjumbe wake. Sipendi nyinyi muinue daraja yangu kuliko ile daraja ambayo Allah(s.w) amenipa.*

Vile vile ilisadifu kwamba kifo cha mwana mpenzi wa Muhammad(s.a.w) aliyetitwa Ibrahim kilitokea na jua likapatwa. Watu wakasema huo ni mwujiza utokao kwa Allah unaoonesha kuwa mbingu na ardhi zina majonzi kuhusiana na kifo cha Ibrahim. Aliposikia maneno hayo, Muhammad(s.a.w) alikasirika sana akasema: “Jua na mwezi ni dalili mbili miogoni mwa dalili nyingi za Allah(s.w). Jua na mwezi havipatwi kwa sababu ya kufa au kuzaliwa mtu yeyote.”

Mifano yote hii inaonesha kuwa madai kwamba Muhammad(s.a.w) aliitunga Qur'an ili ajipatie madaraka na utukufu pia hayana nguvu.

Kwa nini kwa mfano, atunge kitabu kinachomwamuru yeye mwenyewe awatangazie watu wote kuwa yeye hana uwezo wowote wala hana elimu ya ghaibu na kwamba lau angekuwa nayo angejizidishia heri zote na shari isingemgusa(Qur'an 7:188)? Au kwanini aandike kitabu kinachomwamuru aseme kwamba hakuja na itikadi mpya na kwamba hata hakutazamia kuwa kitabu kama hiki kingefunuliwa kwake na hivyo awaambie watu kuwa yeye ni mtu kama watu wengine? (Qur'an 46:9, 28:86, 8:110 na 6:50).

**Tatu**, hisia za Muhammad(s.a.w) baada ya kupata wahy mwanzo zaonyesha kuwa hakuwa anawania ukubwa kisiri siri. Baada ya yaliyomtokea katika pango la Hira alirejea haraka kwa mkewe hali ya kuwa anatetemeka kwa hofu kana kwamba alikuwa na homa kali. Akamwomba mkewe amfunike nguo nzito. Baada ya hofu kumwondoka akamsimulia mkewe yote aliyoyaona kisha akasema: ‘Ewe Khadijah, ni lipi linalotaka kunisibu?’Ni dhahiri kuwa kama kusingizia kupata wahy ilikuwa ni mbinu tu ya kujipatia ukubwa Muhammad(s.a.w) asingehofia chochote. Ushahidi uliopo unaonesha kuwa hakupanga apate wahy wala hakutegemea kupata wahy. Alijitukia tu analetewa wahy. Na juu ya jambo hili Qur'an yasema:

وَمَا كُنْتَ تَرْجُو أَنْ يُلْقَىٰ إِلَيْكَ الْكِتَابُ إِلَّا رَحْمَةً مِّن رَّبِّكَ ..... ﴿٢٨﴾

*Nawe hukuwa unatumai ya kwamba utaletewa Kitabu, lakini ni rehema ya Mola wako. (28:86)*

**Nne**, Jambo jingine linalozidi kudhihirisha kuwa Muhammad(s.a.w) hakuwania ukubwa na utukufu ni kule kukataa kwake alipopewa pendekezo hilo na Maquraishi.

Wakati ambapo Waislamu walikuwa wakibughudhiwa na kuteswa, Machifu wa Maquraishi wa Makka walimtaka Muhammad(s.a.w) aache kuhubiri dini ya Uislamu na wao watampatia alitakalo miongoni mwa yafuatayo:

- (1) Kama anataka mali watampatia mali nyingi hadi awe tajiri kuliko watu wote.
- (2) Kama anataka utukufu, watamfanya bwana wao na hawataamua lolote bila ridhaa yake.



(3) Kama anataka ufalme, watamfanya awe mfalme wao, na

(4) Kama amepagawa na pepo na ameshindwa kumwondoa mwilini mwake wao watamtafuta mganga atakayemtibu kwa gharama yoyote.

Lakini Muhammad (saw) aliyakataa yote hayo na badala yake akamsomea mjumbe aliyetumwa kumletea mapendekezo hayo, Utbah ibn Rabia, Qur'an (41: 1 - 37).

## **UTHIBITISHO KUWA QUR'AN NI NENO LA ALLAH(S.W)**

Baada ya kuona madai mbali mbali yaliyotolewa kupinga kuwa Qur'an si kitabu cha Allah(s.w) na baada ya kuona udhaifu wa madai hayo, ni vyema sasa kuonesha hoja madhubuti zinazothibitisha kuwa Qur'an ni kitabu cha Allah(s.w). Katika kuthibitisha kuwa Qur'an ni kitabu cha Allah(s.w), tuna vigezo viwili (a) Qur'an yenyewe na (b) Historia ya kushuka kwake.

### *(a) Uthibitisho kutokana na Qur'an yenyewe:*

Vipengele vinavyothibitisha kuwa Qur'an ni Kitabu cha Allah(s.w) kutokana na Qur'an yenyewe ni hivi vifuatavyo:

(i) Kutojua kusoma na kuandika kwa Mtume Muhammad(s.a.w).

(ii) Qur'an yenyewe inajieleza kuwa ni Kitabu cha Allah(s.w).

(iii) Hali aliyokuwa nayo Mtume katika kupokea wahyi.

(iv) Qur'an kushushwa kidogo kidogo kwa kipindi cha miaka ishirini na tatu (23).

(v) Kukosolewa kwa Mtume katika Qur'an.

(vi) Kutokea kweli yale yaliyotabiriwa katika Qur'an.

(vii) Mpangilio wa Qur'an.

(viii) Maudhui ya Qur'an na mvuto wa ujumbe wake.

### *(ix) Wanaadamu kushindwa kuandika kitabu mithili ya Qur'an.*

Hebu tuangalie jinsi kila kipengele kinavyothibitisha kuwa Qur'an ni neno la Allah(s.w).

### *(i) Mtume Muhammad(s.a.w) Kutojua Kusoma na Kuandika:*

Iwazi mno katika historia yake kuwa Mtume(s.a.w) hakujua kusoma wala kuandika. Ukweli huu wa historia unathibitishwa na aya za Qur'an zifuatazo:

قُلْ يَتَأْتِيهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا الَّذِي لَهُ مُلْكُ  
السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ يُحْيِي وَيُمِيتُ ۗ فَآمِنُوا بِاللَّهِ  
وَرَسُولِهِ الَّذِي الْأُمِّيُّ الَّذِي يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَكَلِمَتِهِ وَأَنْبِئُوهُ  
لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ ﴿١٥٨﴾

*“Sema (Wewe Nabii Muhammad): Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume wa Allah kwenu nyinyi nyote, (Allah) ambaye ana ufalme wa mbingu na ardhi, hapana aabudiwaye (kwa haki) ila Yeye, Ndiye ahuishaye na ndiye afishaye. Basi mwaminini Allah na Mtume wake, aliye Nabii Ummi, (asiyejua kusoma wala kuandika), ambaye humwamini Allah na maneno yake na mfuateni yeye ili mpate kuongoka.” (7:158)*

وَمَا كُنْتُمْ تَتْلُوا مِنْ قَبْلِهِ مِنْ كِتَابٍ وَلَا تَخُطُّهُمْ بِيَمِينِكَ ۗ إِذَا لَأَزْتَابُ

الْمُبْطُلُونَ ﴿١٥٩﴾

*“Na hukuwa mwenye kusoma kitabu chochote kabla ya hiki, wala hukukiandika kwa mkono wako wa kuume, ingekuwa hivyo wangepanya shaka wale wanaotaka kubadilisha (haki).” (29:48)*

Sababu ya Mtume(s.a.w) kutojua kusoma wala kuandika imebainishwa wazi katika aya hii ya (29:48) kuwa angelijua kusoma na kuandika watu wakaidi wasio tayari kumwamini Mtume na kuamini Qu-ran kwa sababu si maneno ya Allah(s.w) bali ni maneno aliyoyatunga Mtume(s.a.w) au ni maneno aliyoyanakili kutoka kwenye vitabu vya kale au ni maneno aliyofundishwa na watunga mashairi mashuhuri na kuyanukuu kwenye kitabu. Mtume(s.a.w) angalijua kusoma na kuandika ingalikuwa vigumu sana kuonesha udhaifu wa madai haya. Lakini kutojua kusoma wala kuandika kwa Mtume(s.a.w) kumewafanya wapinzani wengi wakose hoja ya uwazi ya kukataa kuwa Qur'an si Kitabu cha Allah(s.w).Hata hivyo, pamoja na ukweli wa historia kuwa Mtume(s.a.w) hakuwa ni mwenye kujua kusoma wala kuandika, walitokea watu waliojitia upofu na kudai kuwa Qur'an ni maneno ya Muhammad(s.a.w). Ili kuwahuzunisha na kuwaonesha kuwa ni waongo katika madai yao hayo, Allah(s.w) aliwawekea watu hao na walimwengu kwa ujumla changa moto ambayo tutaiona katika kipengele cha (ix).

Kwa hiyo Mtume Muhammad(s.a.w) kutojua kwake kusoma wala kuandika na bado akawasilisha kwa watu ujumbe mzito wenye hekima kubwa na wenye

kumuongoza mwanaadamu kwa usahihi katika kila kipengele cha maisha yake, ujumbe ambao hapana yeyote anayeweza kuleta mfano wake ni ushahidi mkubwa kuwa Qur'an yote kama ilivyo ni maneno ya Allah(s.w).

**(ii) Qur'an Yenyewe Inajieleza kuwa ni Ufunuo Kutoka kwa Allah(s.w) :**

Ukiisoma Qur'an kwa makini utakuta kuna aya nyingi zinazojieleza kuwa Qur'an imeshushwa kutoka kwa Allah, kama inavyodhihirika katika aya chache zifuatazo:

لَكِنَّ اللَّهَ يَشْهَدُ بِمَا أَنْزَلَ إِلَيْكَ أَنْزَلَهُ بِعِلْمِهِ وَالْمَلَكُ يَشْهَدُونَ

وَكَفَى بِاللَّهِ شَهِدًا

Lakini Allah anayashuhudia kuwa aliyokuteremshia (kuwa ni haki) ameyateremsha kwa ilimu yake, na Malaika (pia) wana shuhudia. Na Allah anatosha kuwa shahidi. (4:166).

تَنْزِيلُ الْكِتَابِ لَا رَيْبَ فِيهِ مِنْ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٣٢﴾ أَمْ يَقُولُونَ

أَفْتَرَاهُ بَلْ هُوَ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ لِتُنذِرَ قَوْمًا مَأْتَتْهُمْ مِنْ نَذِيرٍ مِّن قَبْلِكَ

لَعَلَّهُمْ يَهْتَدُونَ ﴿٣٣﴾

“Uteremsho wa Kitabu hiki hauna shaka kuwa umetoka kwa Muumba wa ulimwengu. Je, wanasema: “Amekitunga mwenyewe”. (Sivyo hivyo). Bali hicho ni haki itokayo kwa Mola wako ili uwaonye watu wasiojiwa na muonyaji kabla yako. Huenda wakaongoka.” (32:2-3)

وَالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ مِنَ الْكِتَابِ هُوَ الْحَقُّ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ إِنَّ

اللَّهَ بِعِبَادِهِ لَخَبِيرٌ بَصِيرٌ ﴿٣٤﴾

Na Kitabu tulichokuletea kwa wahyi ndicho cha haki, kinasadikisha (vitabu) vilivyokuwa kabla yake. Bila shaka Allah kwa waja wake ni Mwenye kuwajua vyema na kuwaona vizuri.” (35:31)

تَبَارَكَ الَّذِي نَزَّلَ الْفُرْقَانَ عَلَى عَبْدِهِ لِيَكُونَ لِلْعَالَمِينَ نَذِيرًا ﴿٣٥﴾

Ni mwenye kuleta baraka (kweli kweli) yule aliyeteremsha Qur'an kwa mja wake, ili awe muonyaji kwa walimwengu wote. (25:1)

## تَنْزِيلُ الْكِتَابِ مِنَ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ ﴿٢﴾

*Uteremsho wa Kitabu hiki umetoka kwa Allah, mwenye nguvu, na mwenye hikima. (45:2)*

Aya zote hizi na nyingi nyinginezo kama hizi zilizomo ndani ya Qur'an hujieleza wazi wazi kuwa Qur'an ni Kitabu cha Allah(s.w) alichowashushia wanaadamu kupitia kwa Mtume Muhammad(s.a.w). Pangelikuwa na haja gani Mtume kuandika kitabu kisha adai kuwa kinatoka kwa Allah(s.w) tukikumbuka kuwa yeye amekuwa mwaminifu na mkweli katika historia yote ya maisha yake.

### **(iii) Jinsi Mtume Muhammad(s.a.w) alivyoipokea Qur'an:**

Tumejifunza kuwa Allah(s.w) huwasiliana na wanaadamu kwa njia ya Wahyi (ufunuo) kwa kutumia njia za mawasiliano zifuatazo:

- Il-hamu.
- Kutumwa Malaika.
- Kuongelehwa nyuma ya pazia.
- Maandishi (yaliyoandikwa tayari).
- Ndoto za kweli.

Qur'an ilishushwa kwa Mtume(s.a.w) kwa njia hii ya wahyi kupitia kwa Malaika Jibril.

Kuonesha kuwa Qur'an ni neno la Allah(s.w) na wala si tungo za Mtume Muhammad(s.a.w) ni ile hali aliyokuwa nayo wakati wa kupokea wahyi. Wakati wa mwanzo mwanzo wa kuanza kushushiwa wahyi Mtume(s.a.w) alikuwa akiyarudia haraka haraka yale aliyokuwa anasomewa na Malaika Jibril kwa wasi wasi kuwa atasahau. Ndipo Allah(s.w) akamtoa wasi wasi huo kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

لَا تُحْرِكُ بِهِ لِسَانَكَ لِتَعْجَلَ بِهِ ﴿١٦﴾ إِنَّ عَلَيْنَا جَمْعَهُ وَقُرْءَانَهُ ﴿١٧﴾

فَإِذَا قَرَأْتَهُ فَاتَّبِعْ قُرْءَانَهُ ﴿١٨﴾ ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا بَيَانَهُ ﴿١٩﴾

*Usitukise ulimi wako kwa (kuufanyia haraka) wahyi (unapoteremka. Wewe sikiliza tu. Usiseme kitu). Kwa hakika ni juu yetu kuukusanya na kuusomesha (kukukusanyia na kukusomesha). Wakati tunapokusomea, basi fuata kusomwa kwake. Kisha ni juu yetu kuubainisha (kukubainishia). (75:16-19)*

سَنُقْرَأُكَ فَلَا تَنْسَى ﴿٢٠﴾ إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ إِنَّهُ يَعْلَمُ الْجَهْرَ وَمَا يَخْفَى ﴿٢١﴾

*Tutakusomesha (tutakusomea) wala hutasahau. Ila Akipenda Mwenyezi Mungu; Yeye anajua yaliyodhahiri na yaliyofichikana. (87:6-7)*

Kwa hiyo kutokana na aya hizi Qur'an si maneno ya Mtume Muhammad(s.a.w) aliyoyotoa kichwani mwake. Kwani yangelitoka kichwani mwake asingelikuwa na wasi wasi wowote kuwa atakuja yasahau. Alikuwa na wasi wasi kwa sababu yeye akiwa ni Mtume wa Allah(s.w) alijua fika kuwa jukumu lake kubwa ni kuufikisha ujumbe wa Allah kwa watu kama ulivyo bila ya kupunguza au kuzidisha hata chembe.

**(iv) Qur'an Kushuka Kidogo Kidogo kwa Kipindi cha Miaka 23:**

Historia inatuthibitishia kuwa Mtume Muhammad(s.a.w) hakuanza kuufundisha Uislamu na kuutangaza ulimwengu mzima kwa kurejea Qur'an kama Kitabu tulicho nacho hivi sasa bali aya za Qur'an zilikuwa zikimshukia kidogo kidogo kulingana na haja na wakati kwa kipindi chote cha Utume wake cha miaka 23. Kwa maana nyingine Qur'an imeshuka kidogo kidogo katika kipindi chote cha utume kuanzia mwanzo wa Utume 610 A.D. mpaka siku chache kabla ya kutawafu Mtume(saw), 632 A.D. Kuhusu Qur'an kushuka kidogo kidogo tunafahamishwa katika aya zifuatazo:

﴿١٦﴾ وَقُرْءَانَا فَرَقْنَاهُ لِتَقْرَأَهُ عَلَى النَّاسِ عَلَى مُكْثٍ وَنَزَّلْنَاهُ تَنْزِيلًا

*Na Qur'an tumeigawanya sehemu mbali mbali ili uwasomee watu kwa kituo, na tumeiteremsha kidogo kidogo. (17:106)*

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْلَا نُزِّلَ عَلَيْهِ الْقُرْءَانُ جُمْلَةً وَّاحِدَةً كَذَلِكَ

لِنُثَبِّتَ بِهِمُ فُؤَادَكَ وَرَتَّلْنَاهُ تَرْتِيلًا ﴿١٧﴾

*Na wakasema wale waliokufuru; Mbona hakuteremshiwa Qur'an yote kwa mara moja? Kama hivi (mnavyoona, tumeiteremsha kidogo kidogo) ili tuuthibitishie, (tuutie nguvu), moyo wako (kwa hizo aya mpya mpya zinazoteremshwa wakati baada ya wakati) na tumeipanga kwa uzuri. (25:32)*

﴿١٧﴾ إِنَّا لَنَحْنُ نَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْقُرْءَانَ تَنْزِيلًا

*Hakika sisi tumekuteremshia Qur'an sehemu sehemu (kidogo kidogo). (76:23).*

Kama inavyoonekana katika aya hizi. Qur'an imeshushwa kidogo kidogo ili iwe wepesi kwa Mtume Muhammad(s.a.w) kuufikisha ujumbe uliotangulia kwa ukamilifu kinadharia na kimatendo kabla ya ujumbe mwingine uliofuata.

Kwa upande mwingine Qur'an imeshuka kidogo kidogo ili kuwawezesha waumini wa mwanzo kuihifadhi Qur'an kwa wepesi, kuyaelewa fika mafundisho

yake kinadharia na kuwawezesha kuitekeleza Qur'an katika kila kipengele cha maisha yao ili wawe jamii bora ya kuigwa na jamii zitakazofuatia.

Kushuka Qur'an kidogo kidogo kwa muda wa miaka 23 ni hoja nyingine kuwa Qur'an ni Kitabu cha Allah(s.w). Kwa yeyote yule anayeisoma Qur'an kwa makini na akajua mpangilio wake wa aya na sura kama vile sura moja kuwa na mchanganyiko wa aya za mwanzo na zilizoshushwa mwishoni lakini bado kunapatikana mtiririko mzuri wa maudhui na mpangilio wa sura usiofuata mtiririko wa kushuka, utaona kuwa haiyumkiniki kuwa Qur'an ni Kitabu kilichoandikwa na Mtume Muhammad(s.a.w) kama wanavyodai makafiri.

Pia Qur'an ingelikuwa imeandikwa na Mtume Muhammad(s.a.w) isingelichukua muda wote huo, bali ingelibidi aiandike yote kwa muda mfupi ili aweze kuitumia katika kazi yake ya kuwaongoza watu. Ni kawaida kuwa ili kufanikiwa katika utekelezaji wa jambo lolote ni lazima kwanza pawe na nadharia nzuri inayoelekeza namna ya utekelezaji. Halikadhalika, Mtume Muhammad(s.a.w) aliyekuwa kiongozi wa Dola ambaye mfano wake haujapatikana, asingeliweza kufanya kazi nzito na kubwa kiasi hicho bila ya kuwa na nadharia ya kumwongoza. Hivyo, kwa kutokuwa na Qur'an yote mkononi mwake ili kuitumia katika kila hatua ya kazi yake, inadhihirisha kuwa alikuwa akiletewa mwongozo kutoka kwa Allah(sw) katika kila hatua ya kazi yake mpaka alipoikamilisha.

***(v)Kukosolewa Mtume(s.a.w) katika Qur'an ni Ushahidi Mwingine kuwa Qur'an ni Kitabu cha Allah(s.w):***

Hoja nyingine inayotufanya tuamini pasi na tone la shaka kuwa Qur'an ni Kitabu cha Allah(s.w) ni kule kukosolewa Mtume(s.a.w) ndani ya Qur'an. Si jambo la kawaida kwa mwanaadamu yeyote mwenye akili timamu kutangaza aibu zake na kujikosoa kwa namna Mtume(s.a.w) alivyokosolewa katika Qur'an, katika Kitabu chake mwenyewe. Atakalolifanya mwandishi mkweli na muadilifu ni kuacha tabia mbaya au udhaifu aliokuwa nao na kuwapa wengine ujumbe kuwa waache udhaifu huo. Lakini katika Qur'an tunaona kuwa pale Mtume Muhammad(s.a.w) alipoonesha kidogo udhaifu wa kibinaadamu na akaenda kidogo nje ya utendaji anaouridhia Allah(s.w) pale pale Allah(s.w) alimkosoa na kumrejsha katika njia iliyo sawa. Kwa mfano Mtume Muhammad(s.a.w) alipohisi ugumu katika kutekeleza amri ya Allah(sw) ya kumuoa Zainabu bint Jahsh baada ya kuachwa na Zaidi bin Harith, aliyekuwa mtoto wake wa kulea kwa kuchelea Uislamu kutukanwa na kupakwa matope na makafiri na wanafiki, Allah(s.w) alimzindua katika aya zifuatazo:

وَإِذْ تَقُولُ لِلَّذِي أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَأَنْعَمْتَ عَلَيْهِ أَمْسِكْ عَلَيْكَ زَوْجَكَ

وَاتَّقِ اللَّهَ وَتَخَفِي فِي نَفْسِكَ مَا اللَّهُ مُبْدِيهِ وَتَخْتِى النَّاسَ وَاللَّهُ أَحَقُّ أَنْ

تَخَشَّهُ ط فَلَمَّا قَضَى زَيْدٌ مِّنْهَا وَطَرًا زَوَّجْنَاكَهَا لِكَيْ لَا يَكُونَ عَلَى  
الْمُؤْمِنِينَ حَرَجٌ فِي أَزْوَاجٍ أَدْعِيَآبِهِمْ إِذَا قَضَوْا مِنْهُنَّ وَطَرًا ۖ وَكَانَ أَمْرٌ

اللَّهُ مَفْعُولًا ﴿٧٧﴾

*Na(wakumbushe)ulipomwambia yule ambaye Mwenyezi Mungu amemneemsha (kwa kumuafikia Uislamu) na wewe ukamneemsha kwa kumpa uungwana. naye ni Bwana Zaid bin Haritha ulipomwambia): "Shikamana na mkeo na umche Mwenyezi Mungu(usimuache)" na ukaficha katika nafsi yako aliyotaka Mwenyezi Mungu kuyatoa(Nayo ni kuwa Mwenyezi Mungu amekuamrisha umuoe wewe huyo mkewe atakapomuacha ili iondoke ile itikadi iliyokuwa ikiitakiwa ya kuwa mtoto wa kulea ni kama mtoto wa kumzaa), na ukawachelea watu, hali Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye haki zaidi ya kumchelea. Basi alipokwisha Zaidi haja yake na mwanamke huyo, Tulikuoa wewe ili isive taabu kwa Waislamu kuwaoa wale watoto wao wa kupanga wanapokuwa hawana haja nao. Na amri ya Mwenyezi Mungu ni yenye kutekelezwa (33:37)*

Mfano mwingine ni pale Mtume(s.a.w) aliposusa kula asali ili kuwaridhisha wake zake ambapo Allah(s.w) alimwonya kama aya ifuatayo inavyotufahamisha:

يَأْتِيهَا النَّبِيُّ لِمَ تُحَرِّمُ مَا أَحَلَّ اللَّهُ لَكَ ۖ تَبَغَّيْ مَرَضَاتِ أَزْوَاجِكَ ۖ وَاللَّهُ

غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٦٦﴾

*Ewe Mtume! Mbona (kwa nini) unaharamisha alichokuhalalishia Allah? Unatafuta radhi za wake zako ndiyo maana ukafanya hivi! Na Allah ni mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu. (66:1)*

Mfano mwingine ni ule wa kukosolewa Mtume(s.a.w) katika Qur'an ni pale alipomkasirikia sahaba kipofu aliyetaka kupata mawaidha mapya na badala yake akawaelekea wakubwa wa makafiri kwa matumaini kuwa watasilimu na kuleta nafuu kubwa katika kazi ya kuusimamisha Uislamu. Kitendo hiki hakukiridhia Allah(s.w) na akamkosoa Mtume wake katika aya zifuatazo:

عَبَسَ وَتَوَلَّى ﴿٦٥﴾ أَنْ جَاءَهُ الْأَعْمَى ﴿٦٦﴾ وَمَا يُدْرِيكَ لَعَلَّهُ يَزْكَى ﴿٦٧﴾

أَوْ يَذَّكَّرُ فَتَنْفَعَهُ الذِّكْرَى ﴿٦٨﴾ أَمَّا مَنْ أَسْتَغْنَى ﴿٦٩﴾ فَأَنْتَ لَهُ تَصَدَّى ﴿٧٠﴾

﴿٧١﴾ وَمَا عَلَيْكَ أَلَّا يَزْكَى ﴿٧٢﴾ وَأَمَّا مَنْ جَاءَكَ يَسْعَى ﴿٧٣﴾ وَهُوَ يَخْشَى ﴿٧٤﴾

﴿ ١ ﴾ فَأَنْتَ عَنْهُ تَلَهَّى ﴿ ٢ ﴾ كَلَّا إِنَّهَا تَذْكِرَةٌ ﴿ ٣ ﴾ فَمَنْ شَاءَ ذَكَرْهُ ﴿ ٤ ﴾

*Alikunja (Mtume) paji akageuza uso, kwa sababu alimjia kipofu, na nini kilichokujulisha (kuwa huyo sahaba pofu hahitaji mawaidha mapya) labda atatakasika (akisikia mawaidha mapya), au atakumbuka (aliyoyasahau) ukumbusho huo upate kumfaa, ama ajionaye hana haja (ya dini), wewe ndiye unayemshughulikia! Na si juu yako kama hakutakasika, lakini anayekukimbilia - naye anaogopa, wewe unampuza (usifanye hivyo). Sivyo! Hakika hii (Qur'an) ni nasaha (mawaidha), basi kila apendaye atawaidhika (asiyetaka basi muachilie mbali). (80:1-12).*

Ni dhahiri kuwa kama Mtume(s.a.w) asingelikuwa Mtume wa Allah(s.w) na kama ndiye yeye aliyelandika Qur'an, kamwe asingelithubutu kudhihirisha aya hizo katika kitabu chake. Kwa aya hizi na nyingine kama hizi kubakia katika Qur'an na Mtume(s.a.w) kuzitangaza kwa watu kama zilivyo kwa muda wote wa maisha yake ya Utume, ni hoja nyingine kuwa Qur'an si maneno ya Mtume Muhammad(s.a.w) bali ni maneno matukufu ya Allah(s.w).

#### **(vi)Kutokea Kweli Matukio yaliyotabiriwa katika Qur'an:**

Ushahidi mwingine unaonesha kuwa Qur'an ni neno la Allah(s.w) ni kutokea mambo kama yalivyotabiriwa hapo awali na Qur'an. Katika mwanzo wa kushuka Qur'an kuna mambo mbali mbali ambayo Mtume(s.a.w) aliahidiwa pamoja na Waislamu kuwa yatatokea hapo baadaye. Pamoja na kuonekana kwa watu kutokuwa na uwezekano kutokea hayo yaliyotabiriwa kulingana na hali halisi iliyokuwapo wakati huo ukweli ni kwamba yalitokea. Kwa mfano, katika siku za mwanzo za Utume, Mtume(s.a.w) na Waislamu waliahidiwa na Allah(s.w) kuwa pamoja na ugumu uliokuwa ukiwakabili na pamoja na udhaifu wa mali na uwezo waliokuwa nao, hali yao itazidi kuwa nzuri siku hadi siku na baadaye watafarjika na kuwa juu ya maadui zao. Ahadi hizi tunazikuta katika aya zifuatazo:

﴿ ١ ﴾ وَلَلْآخِرَةُ خَيْرٌ لَّكَ مِنَ الْأُولَىٰ ﴿ ٢ ﴾ وَلَسَوْفَ يُعْطِيكَ رَبُّكَ فَتَرْضَىٰ ﴿ ٣ ﴾

*Na bila shaka wakati ujao utakuwa ni bora kwako kuliko uliotangulia, na Mola wako atakupata mpaka uridhike. (93:4-5)*

﴿ ١ ﴾ فَإِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ﴿ ٢ ﴾ إِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ﴿ ٣ ﴾

*Na kwa hakika baada ya dhiki (huja) faraja. Hakika baada ya dhiki (huja) faraja. (94:5-6)*

Tukiangalia maisha ya Mtume na maswahaba wake, ahadi zote hizi zilitimia. Waislamu waliongezeka siku hadi siku na Uislamu ulisimama na kuwa juu ya



Dini zote (njia zote za maisha) katika kipindi kifupi cha miaka 23 tu. Mfano wa pili wa utabiri wa Qur'an uliotokea kweli baada ya kipindi kifupi tu ni ule uliotolewa katika Surat-ur-Ruum katika aya zifuatazo:

غَلَبَتِ الرُّومُ ﴿٦﴾ فِي أَدْنَى الْأَرْضِ وَهُمْ مِنْ بَعْدِ عَلَيْهِمْ سَيَغْلِبُونَ ﴿٧﴾ فِي  
بُضْعِ سِنِينَ ۗ لِلَّهِ الْأَمْرُ مِنْ قَبْلُ وَمِنْ بَعْدُ ۗ وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ ﴿٨﴾  
بَنَصْرِ اللَّهِ ۗ يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿٩﴾ وَعَدَّ اللَّهُ لَا تُخْلِفُ اللَّهُ  
وَعْدَهُ ۗ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٠﴾

*Warumi wameshindwa katika nchi iliyo karibu (na nchi ya Bara Arabu, nayo ni Sham) nao baada ya kushindwa kwao watashinda, katika miaka michache: Amri hii ni ya Allah kabla (yake) na baada (yake) na siku hiyo Waislamu watafurahi kwa nusra ya Allah (Atakayowapa wao. Nayo ni kuwashinda Makuraishi siku hiyo) (Allah) Humnusuru amtakaye; naye ni Mwenye Nguvu; Mwenye Rehma. Hii ni ahadi ya Allah, Allah havunji ahadi yake lakini watu wengi hawajui. (30:2-6)*

Katika mwaka wa sita au saba wa Utume, palikuja habari Makka kuwa Warumi ambao ni watu wa Kitabu (Ahlal-Kitab) wameshindwa vita na Waajemi ambao walikuwa ni washirikina kama washirikina wa Makka. Tukio hili liliwafurahisha sana washirikina wa Makka na kuwaambia Waislamu: “Wakristo, watu wa Kitabu kama nyinyi, wameshindwa na washirikina wenzetu, na hii ni ishara kuwa na sisi hivi karibuni tutakushindeni.” Ndipo Qur'an ikatangaza katika aya hizi bishara mbili; bishara ya kwanza ni kuwa katika muda wa miaka tisa Waajemi watashindwa na Warumi na ya pili ni kuwa Waislamu siku hiyo nao watafurahi na kuwacheka Washirikina wa Makka, yaani makafiri wa Makka nao watashindwa vibaya sana na Waislamu. Hivi ndivyo ilivyotokea, kwani katika mwaka 624 A.D. Warumi waliwashinda Waajemi na mwaka huo huo Waislamu 313 walishinda jeshi la makafiri wa Makka lililokuwa na askari 1000 katika vita vya Badr, kwa hiyo ahadi ya Allah(s.w) aliyoitoa katika Qur'an ilitimia. Je hii haithibitishi kuwa Qur'an ni maneno ya Allah(s.w), Mjuzi wa yote yaliyopita na yajayo? Hebu tuangalia tena mfano mwingine unaoonesha kutokea kweli ahadi alizozitangaza Allah(s.w) katika Qur'an. Katika suratul-Fat-h tunafahamishwa:

إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُبِينًا ﴿١﴾

*Bila shaka Tumekwisha kupa kushinda kuliko dhahiri. (48:1)*

Katika mwaka wa 6 A.H. Mtume(s.a.w) na baadhi ya Maswahaba wake walitoka kwenda Makka kufanya Ujra (Hija ndogo) lakini walipokaribia kuingia Makka makafiri waliwakatalia kata kata wasiende kufanya ibada hiyo.

Waislamu walikasirika sana mpaka kukaribia kupigana ndipo Allah(s.w) akawateremshia utulivu na wakakubaliana kufanya mkataba wa (Hudaibiya), kisha Allah(s.w) akawaahidi kupata ushindi baada ya muda mfupi. Ndivyo ilivyotokea.

Baada ya miaka miwili tu, na baada ya makafiri wenyewe kuvunja ule mkataba wa amani, Waislamu waliuteka mji wa Makka na kuwa mwisho wa kuabudiwa miungu mingine pamoja na Allah(s.w) katika Nyumba Takatifu (Al-Ka'aba) na katika muda mfupi huo watu wengi walisilimu. Je, kutimia kwa bishara hii ambayo iko wazi mno katika historia, haioneshi kuwa haikutolewa na yeyote ila yule mwenye elimu ya hakika juu ya yote yaliyopita na yajayo?

### **(vii)Mpangilio wa Qur'an:**

Ukiuchunguza msahafu kwa kina utagundua kuwa si kitabu cha kawaida kama vile wanavyo vitunga wanaadamu. Qur'an pamoja na aya zake kufumwa na maneno ya Kiarabu, pametumika ujuzi usio na mfano katika uchaguzi na mpangilio wa maneno. Maneno yamechaguliwa na kupangiliwa kwa kiasi kwamba huwianisha habari zote zilizoenezwa ndani ya Kitabu na kuufikisha ujumbe kwa wepesi. Mifano michache ifuatayo itatupa picha ya mpangilio wa ajabu wa Qur'an:

**Kwanza**, kutokana na uchunguzi uliofanyika kwa kutumia kompyuta imedhihirika kuwa sura zile zilizoanza na herufi kama **Qaf** (ق) zina idadi kubwa zaidi ya herufi hiyo ukilinganisha na herufi nyingine katika sura hizo.

**Pili**, Kuna sura 114 katika msahafu na kila sura imeanza kwa "Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim" isipokuwa Suratut Tawba. Hi huifanya idadi ya "Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim" kuwa 113. Lakini katika Suratun-Naml kuna "Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim" iliyoletwa katikati ya sura.

إِنَّهُ مِنْ سُلَيْمَانَ وَإِنَّهُ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿٣٠﴾

*Imetoka kwa Suleimani, nayo ni: Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu." (27:30)*

Hivyo huifanya idadi ya "Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim" kuwa 114 sawa na idadi ya sura zote katika msahafu. Je, hii imetokea kwa bahati tu au ni mpangilio wa Mjuzi, Mwenye Hikma.

**Tatu**, kutokana na uchunguzi imedhihirika kuwa maneno mbali mbali katika Qur'an yamerudiwa kwa kuzingatia idadi maalum. Kwa mfano neno "**Sema**" (قَالَ) limerudiwa mara 332 katika msahafu na neno "**Alisema**" (سَمِعَ سَمَاوَاتٍ) limerudiwa mara hizo hizo 332. Pia katika Qur'an zimetajwa "**Mbingu Saba**" (سَبْعَ سَمَاوَاتٍ) na maneno haya yamerudiwa mara saba tu katika msahafu mzima.

Kuna miezi kumi na mbili katika mwaka mmoja na neno “**Shahr**” (شَهْرٌ) lenye maana ya mwezi limetajwa mara 12 katika Qur'an. Neno “**Yaum**” (يَوْمٌ) katika Qur'an limetajwa mara 365 sawa na idadi ya siku za mwaka mmoja katika mwendo wa jua!

**Nne**, Qur'an inapofananisha jambo fulani na lingine, idadi ya utajo wa mambo hayo kitabuni humo pia huwiana. Kwa mfano katika sura ya 3 aya 59 Qur'an inasema:

إِنَّ مَثَلَ عِيسَىٰ عِنْدَ اللَّهِ كَمَثَلِ آدَمَ ۖ خَلَقَهُ مِن تُرَابٍ ثُمَّ قَالَ لَهُ  
كُنْ فَيَكُونُ ﴿٥٩﴾

*Bila shaka hali ya Isa mbele ya Allah ni kama ile ya Adam. Alimuumba kwa udongo, kisha akamwambia kuwa na akawa. (3:59).*

Adam(a.s) ametajwa mara 25 katika Qur'an. Isa(a.s) vile vile ametajwa mara 25 katika Qur'an. Zaidi ya hivyo katika sura 3:59, Adam ametajwa kwa mara ya saba vivyo hivyo Isa nae ametajwa kwa mara ya saba katika aya hiyo.

Adam(a.s) ametajwa katika aya zifuatazo:

2:31, 2:33, 2:34, 2:35, 2:37, 3:33, 3:59 (mara ya saba), 5:27, 7:11, 7:26, 7:31, 7:35, 7:35, 7:172, .17:61, 17:70, 18:50, 19:58, 20:115, 20:116, 20:117, 20:120, 20:121, 36:60.

Isa(a.s) ametajwa katika aya zifuatazo:

2:87, 2:136, 2:253, 3:45, 3:52, 3:55, 3:59 (mara ya saba), 3:84, 4:157, 4:163, 4:171, 5:46, 5:78, 5:110, 5:112, 5:114, 5:116, 6:85, 19:34, 33:7, 42:13, 43:63, 57:27, 61:6 na 61:14.

Mfano mwingine ni ule wa sura ya 7 aya ya 176. Qur'an inawalinganisha watu wanaofuata matamano ya nafsi zao kinyume na aya za Mwenyezi Mungu, kuwa hao ni sawa na mbwa (Kalb).

“Hali yao ni sawa na ile ya mbwa:

Tamko:”Wale wanaokanusha aya zetu”(الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا) limerejewa mara 5 katika Qur'an, na neno “mbwa”(الْكَلْبُ) limetajwa mara 5:

Tamko: "*Wale wanaokadhibisha aya zetu*" limetajwa katika aya zifuatazo: 7:176 (mara ya kwanza), 7:177, 21:77, 25:36 na 62:5 (mara ya tano).

Neno mbwa (kalb) limetajwa katika aya zifuatazo:

7:176 (mara ya kwanza), 18:18, 18:22

Aidha Qur'an inaposema jambo au kitu hiki si kama kile idadi ya mambo au vitu hivyo haviwiani katika kutajwa kwake ndani ya Qur'an.

Kutokana na mifano hii michache ni muhali mwanaadamu kuweza kuandika kitabu chenye mfumo wa maneno, aya na sura mithili ya Qur'an.

### *(viii) Maudhui ya Qur'an na Mvuto wa Ujumbe Wake*

Ukiisoma Qur'an na kuizingatia kwa makini na ukawa unajua lugha yake vizuri utakiri kuwa Qur'an ni Kitabu cha Allah(s.w) kwani ujumbe wake hupenya katika moyo hata wa yule anayeipinga.

Tunafahamishwa katika historia kuwa Waarabu waliopinga Qur'an walikuwa wakipiga kelele na kuziba masikio ili wasipate ujumbe wake wakati ilipokuwa ikisomwa. Kwani kila mwenye kuelewa vizuri lugha ya Qur'an aliathiriwa na ujumbe wake.

Mfano wa athari ya kupenyeza kwa Qur'an katika nyoyo za wanaadamu ni ule wa Labbiid ibn Rabiah aliyesilimu kutokana na changa moto ya aya za Qur'an dhidi ya shairi lake. Kwa kuwa yeye alikuwa mwanafasihi mashuhuri na aliyejamini mno katika fani ya mashairi, baada ya kusoma aya chache za sura ya Qur'an alikiri kuwa Qur'an si mashairi na wala haiwezi kuwa zao la mwanaadamu. Ilibidi akiri kuwa Qur'an ni Kitabu cha Allah(s.w) na akasilimu mbele ya Mtume(s.a.w).

Mfano mwingine ni ule wa 'Umar bin al-Khattab. Akiwa bado mmoja wa viongozi wa Washirikina waliokuwa katika harakati za kumpiga vita Mtume Muhammad(s.a.w) na dini aliyokuwa akiitangaza. 'Umar alichukia sana aliposikia kuwa dada yake amesilimu. Baada tu ya kupata habari ya kusilimu kwa dada yake aliharakisha kwenda nyumbani kwa dada yake kwa hasira na upanga mkononi. Alikuta nyumbani kwa dada yake ikisomwa Qur'an iliyoandikwa katika kipande cha karatasi ambacho alidai apewe. Dada yake alikataa kumpa mpaka alipokubaliana na masharti yake. Baada ya kusoma na kurudia aya chache za Suratu-Twaha (sura ya 20) alipoa na kuondoka moja kwa moja kwenda kwa Mtume Muhammad(s.a.w) na kusilimu.

Baada ya kusilimu, 'Umar ibn al-Khattab alikuwa ngao ya kuutetea Uislamu kwa hali na mali kwa muda wote wa maisha yake na alikuwa Khalifa wa pili wa Mtume(s.a.w) na kiongozi wa Kiislamu aliye mashuhuri katika historia ya ulimwengu.

Hebu turejee aya chache za sura hii zilizokuwa ndio sababu ya kusilimu 'Umar kutokana na mvuto wake:

طه ﴿١﴾ مَا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْقُرْآنَ لِتَشْقَى ﴿٢﴾ إِلَّا تَذَكْرَةً لِّمَن يَخْشَى ﴿٣﴾  
 ﴿٤﴾ تَنْزِيلًا مِّمَّنْ خَلَقَ الْأَرْضَ وَالسَّمَوَاتِ الْعُلَى ﴿٥﴾ الرَّحْمَنُ عَلَى  
 الْعَرْشِ اسْتَوَى ﴿٦﴾ لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا  
 وَمَا تَحْتَ الثَّرَى ﴿٧﴾ وَإِن تَجَهَّرَ بِالْقَوْلِ فَإِنَّهُ يَعْلَمُ السِّرَّ وَأَخْفَى ﴿٨﴾

*Twaaha! Hatukukuteremshia Qur'an ili upate mashaka. Bali iwe mawaidha kwa wenye kunyenyekea. Kiteremsho kinacho toka kwa Yule aliyeyumba ardhi na mbingu zilizo inuka juu. Ndiye Mungu mwenye rehema. Aliyetawala juu ya kiti cha Enzi. Ni vyake (tu peke yake) vyote vilivyomo Mbinguni na vilivyomo ardhini na vilivyo baina yao na vilivyomo chini ya ardhi. Na ukinena kwa sauti kubwa (au ndogo ni sawa sawa) kwani hakika Yeye anajua yaliyosiri na yaliyofichikana zaidi. Mwenyezi Mungu hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye. (20:1-7)*

Je, unaonaje ujumbe wa aya hizi za mwanzo ambazo hasa ni utangulizi wa sura hii? Utaona kuwa namna Qur'an inavyowasilisha ujumbe wake kwa watu ni tofauti kabisa na uwasilishaji wa ujumbe katika uandishi wa mwanaadamu.

Si tu kuwa ujumbe wa Qur'an unanasa kwa kila mwenye kuijua lugha yake, bali hukuti udhaifu wowote katika uandishi wake kama vile kuwa na maneno yanayopingana pamoja na kwamba uandishi wake mpaka kufikia kwenye msahafu huu tulionao ulichukua miaka 23 na mpangilio wa aya na sura ni tofauti kabisa na utaratibu wa kushuka kwake. Qur'an yenyewe inathibitisha hili katika aya zifuatazo:

أَفَلَا يَتَذَكَّرُونَ الْقُرْآنَ ۗ وَلَوْ كَانَ مِنْ عِنْدِ غَيْرِ اللَّهِ لَوَجَدُوا فِيهِ اخْتِلَافًا  
 كَثِيرًا ﴿٨٢﴾

*Hawaizingatii nini hii Qur'an? Na kama ingelitoka kwa asiyekuwa Allah bila shaka wanalikuta ndani yake hitilafu nyingi. (4:82).*

اللَّهُ نَزَّلَ أَحْسَنَ الْكِتَابِ كِتَابًا مُّتَشَابِهًا مَّثَانِيَ تَقْشَعِرُّ مِنْهُ جُلُودُ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ ثُمَّ تَلِينُ جُلُودُهُمْ وَقُلُوبُهُمْ إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ ۗ ذَلِكَ هُدَىٰ

اللَّهُ يَهْدِي بِهِ مَن يَشَاءُ ۚ وَمَن يُضَلِّلِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِن هَادٍ ﴿٣٢﴾

*Mwenyezi Mungu ameteremsha hadithi nzuri kabisa; Kitabu chenye maneno yanayowafikiana na yanayokaririwa; (bila kuchosha) husisimka kwayo ngozi za wale wanaomuogopa Mola wao; kisha ngozi zao na nyoyo zao huwa laini kwa kumkumbuka Mola wao. Huo ndio uongofu wa Allah; kwa huo humuongoza Amtakaye, na anayeachiwa na Allah kupotea basi hakuna wa kumuongoa. (39:23)*

Pamoja na kuona kuwa Qur'an ni Kitabu cha Allah(s.w) kutokana na mvuto wake na ukamilifu wake, hebu tuangalie maudhui ya aya mbali mbali za Qur'an ambazo zinaonekana wazi kuwa haziwezekani zikawa zimetungwa na Mtume Muhammad(s.a.w) na wala hapana yeyote miongoni mwa wanaadamu aliyemfundisha:

حَلَقَ السَّمَوَاتِ بِغَيْرِ عَمَدٍ تَرَوْنَهَا ۗ وَأَلْقَى فِي الْأَرْضِ رَوْسِي أَن تَمِيدَ ..... ﴿٣١﴾

*"Ameziumba mbingu na pasipo nguzo, msizoziona na ameiweka milima katika ardhi ili(ardhi) isikusukesukeni (isikutetemeseni)....(31:10)*

Aya hii inatufahamisha kuwa maumbile mbali mbali katika anga ikiwa pamoja na dunia yameshikiliwa na nguvu ya uvutano (gravitational force) ambayo hatuioni kwa macho yetu. Kama aya hii ilitungwa na Muhammad(s.a.w) miaka mingi kabla ya ugunduzi wa kuwepo kwa nguvu ya uvutano kati ya dunia, jua na sayari nyingine na kabla ya maendeleo ya sayansi yaliyopo hivi leo juu ya ulimwengu (universe) kwa ujumla kwa nini akaongeza neno "mzionazo" badala ya kusema tu "ameziumba mbingu pasipo nguzo?" Yeye alijuaje kwamba kuna nguvu ya uvutano na haionekani? Zaidi ya hivyo Mtume(s.a.w) angelijuaje kabla ya ugunduzi wa sayansi wa karne ya 19/20 A.D kuwa kuwepo kwa milima katika sehemu zake ni muhimu sana katika kuithubutisha dunia na kuifanya isiyumbe yumbe wakati ikizunguka kwa kasi sana katika muhimili wake, na kuzuia tetemeko? Imegundulika hivi karibuni kuwa milima ina mizizi.

Ujumbe wa aya hii wenye maelezo ya kisayansi yaliyotolewa na wanasayansi wa karne hizi za usoni hauwezi kuwa umetolewa na Mtume(s.a.w) katika karne ya Saba wakati uvumbuzi huu haujafahamika kwa mtu yeyote. Kwa hiyo ujumbe wa aya hii ni hoja tosha kuwa Qur'an ni neno linalotoka kwa Mjuzi wa yote.

وَأَن لَّكُم فِي الْأَنْعَامِ لَعِبْرَةٌ ۗ لِيُبَيِّنَ لَكُمْ أَنَّكُمْ بِرُءُوسِهِمْ مِن بَيْنِ فَتْرِ وَدَمٍ

لَبَنًا خَالِصًا سَابِغًا لِلشَّرْبِ بَيْنَ ﴿٣١﴾

“Na bila shaka katika wanyama muna mazingatio makubwa kwa ajili yenu. Tunakunywesheni katika vile vilivyomo matumboni mwao baina ya choo na damu, (Tumekunywesheni) maziwa safi (na) mazuri kwa wanyawao.” (16:66)

Ukweli kwamba maziwa katika wanyama hutengenezwa katika “mammary glands” kutokana na chakula kilichochunjwa kutoka tumboni na kikasafirishwa katika mikondo ya damu ni ugunduzi wa kisayansi wa hivi karibuni katika karne ya ishirini (20). Sasa Muhammad(s.a.w) angelipata wapi utaalumu huu kama kweli yeye ndiye mwandishi wa Qur'an?

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنْ سُلَالَةٍ مِنْ طِينٍ ﴿١٦﴾ ثُمَّ جَعَلْنَاهُ نُطْفَةً فِي قَرَارٍ

مَكِينٍ ﴿١٧﴾ ثُمَّ خَلَقْنَا النُّطْفَةَ عَلَقَةً فَخَلَقْنَا الْعَلَقَةَ مُضْغَةً فَخَلَقْنَا

الْمُضْغَةَ عِظْمًا فَكَسَوْنَا الْعِظْمَ لَحْمًا ثُمَّ أَنْشَأْنَاهُ خَلْقًا آخَرَ فَتَبَارَكَ

اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ ﴿١٨﴾

“Na kwa yakini tulimuumba mwanaadamu kwa udongo uliosafi, kisha tukamuumba kwa tone la manii lililowekwa katika makao yaliyohifadhika. Kisha tukalifanya tone hilo kuwa pande lenye kuning'inia, kisha tukalifanya kuwa pande la nyama kisha tukalifanya kuwa mifupa na mifupa tukaivisha nyama, kisha tukamfanya kiumbe mwingine. Basi Ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa Waumbaji.” (23:12-14)

إِنَّا خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنْ نُطْفَةٍ أَمْشَاجٍ نَبْتَلِيهِ فَجَعَلْنَاهُ سَمِيعًا بَصِيرًا ﴿٢٣﴾

“Kwa hakika tumemuumba mtu kutokana na mbegu ya uhai (uzazi) iliyochanganyika (ya mwanamume na mwanamke) ili Tumfanyie mthani, kwa hiyo Tukamfanya ni mwenye kusikia (na) mwenye kuona.” (76:2)

Kama Mtume Muhammad(s.a.w) ndiye mwandishi wa aya hizi, angelijua je au ni nani angelimfundisha wakati ule uhakika huu wa kisayansi juu ya hatua za kukua mtoto katika mfuko wa uzazi tokea kwenye mbegu za uzazi hadi kuwa mwanaadamu kamili? Hebu tumalizie mifano kwa kuzingatia tena aya zifuatazo:

﴿ وَهُوَ الَّذِي مَرَجَ الْبَحْرَيْنِ هَذَا عَذْبٌ فُرَاتٌ وَهَذَا مِلْحٌ أُجَاجٌ

﴿ وَجَعَلَ بَيْنَهُمَا بَرْزَخًا وَحِجْرًا مَحْجُورًا ﴾

“Naye (Mwenyezi Mungu) Ndiye anayeziunganisha bahari mbili hii ni tamu inayoondosha kiu, na hii ni yenye chumvi kali; na akaweka kinga kati yao na kizuizi kizuiacho.” (25:53)

مَرَجَ الْبَحْرَيْنِ يَلْتَقِيَانِ ﴿١٩﴾ بَيْنَهُمَا بَرْزَخٌ لَا يَبْغِيَانِ ﴿٢٠﴾

“Amezikutanisha bahari mbili. Baina yao kuna kizuizi,haziingiliani (hazichanganyiki).” (55:19-20).

Aya hizi na aya nyinginezo za Qur'an zinatufanya tuzidi kuwashangaa wale wanaodai kuwa mtunzi wa Qur'an ni Muhammad(s.a.w). Ni hivi karibuni tu, 1983, mtaalamu mmoja wa Ufaransa, Captain Jecques Consteau, amegundua kuwa maji ya bahari mbili hayachanganyiki jambo lililoelezwa katika Qur'an karne 14 zilizopita. Mtaalamu huyu aliposoma aya hizi za Qur'an ilibidi akiri:

“Nimeshuhudia kuwa Qur'an ni maneno ya Allah(s.w). Sayansi yetu ya leo inathibitisha tu yale yale yaliyoelezwa na Qur'an karne 14 zilizopita.”

Aya hizi tulitozinukuu kama mifano na nyingine nyingi kama hizi zinatufahamisha juu ya utaalumu wa hali ya juu, juu ya maumbile ambao ndio tu umegunduliwa katika karne hizi za 19/20 kutokana na utafiti wa kisayansi. Yapo mambo mengi yaliyoelezwa katika Qur'an juu ya maumbile ambayo mpaka hivi sasa mwanaadamu hajaweza kuyatolea maelezo ya kisayansi.

Kwa hiyo ukiichunguza Qur'an kwa makini na kuifanyia utafiti kwa kiwango cha utaalumu kilichofikiwa hivi sasa utaona kuwa Qur'an ni kitabu kinachoweka bayana na kuelezea kila kitu kinachohitajika katika kuleta ufanisi wa maisha ya mwanaadamu hapa ulimwenguni na huko Akhera. Qur'an yenyewe inadhihirisha hili katika aya zifuatazo:

الرَّ تِلْكَ ءَايَاتُ الْكِتَابِ وَقُرْءَانٍ مُّبِينٍ ﴿١٥﴾

“Alif Lam Raa, Hizi ni aya za Kitabu kilichokusanya kila yanayohitajiwa na kikayadhihirisha kwa vizuri.” (15:1)

تِلْكَ ءَايَاتُ الْكِتَابِ الْمُبِينِ ﴿٢٦﴾

“Hizi ni aya za kitabu kielezacho (kila linalohitajiwa).” (26:2)

طس تِلْكَ ءَايَاتُ الْقُرْءَانِ وَكِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿٢٧﴾

“Twa Sin. Hizi ni aya za Qur'an, (Kitabu kilichojaa kila yenye faida) na kitabu kielezacho (kila linalohitajika).” (27:1)



وَمَا عَلَّمْنَاهُ الشِّعْرَ وَمَا يَنْبَغِي لَهُ إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ وَقُرْآنٌ مُّبِينٌ ﴿٦٦﴾

لَيُنذِرَ مَنْ كَانَ حَيًّا وَبِحَقِّ الْقَوْلِ عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٦٧﴾

“Wala hatukumfundisha (Muhammad) mashairi, wala haiwi kwake (kuwa mtunga mashairi). Haikuwa (Qur'an) ila ni ukumbusho na Kitabu kibainishacho (kila yanayohitajiwa). Ili amwonye aliye hai na ihakikike kauli (ya kuadhibiwa) juu ya makafiri.” (36:69-70)

حَمَّ وَالْكِتَابِ الْمُبِينِ ﴿٦٨﴾

Haa Miim. ”Naapa kwa Kitabu (hiki) kinachobainisha (kila linalohitajika).” (44:1-2)

Aya zote hizi zinatufahamisha kuwa Qur'an imetubainishia kwa uwazi na kwa lugha nyepesi kila linalohitajika katika kuendesha maisha yetu ya kila siku kwa ufanisi. Anashuhudia ukweli huu kila mwenye kuisoma Qur'an kwa mazingatio. Kwa hiyo, ni muhali kabisa Qur'an kuwa kitabu kilichotungwa na mwanaadamu bali ni lazima mwandishi wake awe ni yule aliye mjuzi wa mambo yote yaliyo nyuma na mbele ya maisha ya mwanadamu na mwenye ujuzi huo si mwingine ila Allah(s.w).

### (ix) Wanaadamu kushindwa Kuandika Kitabu Mithili ya Qur'an

Ushahidi mkubwa na wa uwazi zaidi ni hii changa moto iliyonadiwa kwa wanaadamu wote na Qur'an yenyewe. Ni kwamba, watu waliokufuru wa nyakati zote za historia ya Qur'an wanadai kuwa Qur'an si kitabu cha Allah(s.w) bali ni kitabu kinachotokana na kazi ya mwanaadamu, hususan Mtume Muhammad(s.a.w). Baadhi ya madai yao tumeshayaona katika kurasa za nyuma. Baada ya kutoa madai yao hayo yasiyo na ushahidi wowote au fununu yoyote ya ukweli, Allah(s.w), aliye Mjuzi na Mwingi wa hekima, Alitoa changamoto si kwa hawa wapinzani tu bali kwa wanaadamu wote ili baada ya hapo kila mwenye akili timamu ashuhudie kuwa Qur'an ni Kitabu cha Allah(s.w). Allah(s.w) alitoa wito kwa wapinzani wote wa Qur'an kuwa wakusanyike pamoja na washirikiane na wataalamu wote wa ulimwengu walio na uzoefu na uhodari katika sanaa ya uandishi kisha katika ushirikiano wao huo watoe kitabu mfono wa Qur'an. Historia nzima inatuonesha kuwa hakuna aliyefua dafu. Hebu turejee changa moto hii katika aya ifuatayo:

قُلْ لَئِنِ اجْتَمَعَتِ الْإِنْسُ وَالْجِنُّ عَلَىٰ أَنْ يَأْتُوا بِمِثْلِ هَذَا الْقُرْآنِ لَا

يَأْتُونَ بِمِثْلِهِ وَلَوْ كَانَ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظَهِيرًا ﴿٦٩﴾

*Sema: "Hata wakijikusanya watu (wote) na majini ili kuleta mfano wa hii Qur'an basi hawangaliweza kuleta mfano wake, hata kama watasaidiana (vipi) wao kwa wao." (17:88)*

Baada ya kushindwa kutoa kitabu mfano wa Qur'an, Allah(s.w) aliwapa makafiri tahfifu ili wazidi kutanabahi na kuhuzunika kwa kuwanadia kuwa waandike mfano wa sura kumi tu za Qur'an badala ya sura 114, kama tunavyofahamishwa katika aya ifuatayo:

أَمْ يَقُولُونَ أَفْتَرْتَهُ<sup>ط</sup> قُلْ فَأْتُوا بِعَشْرِ سُوْرٍ مِّثْلِهِ مُفْتَرِيْنَ وَأَدْعُوا مَن  
 اسْتَطَعْتُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ إِن كُنْتُمْ صَادِقِيْنَ ﴿١١٣﴾

*Ndiyo kweli wanasema kuwa: "Ameitunga mwenyewe (Muhammad hii Qur'an)?" Sema: "Basi leteni sura kumi za uwongo zilizotungwa mfano wa hii, na waiteni muwawezao (kuwaita) badala ya Allah (waje wakusaidieni kutunga hivyo) ikiwa mnasema kweli." (11:13)'*

Hakuna aliyethubutu kutoa sura hizo kumi mfano wa Sura za Qur'an kwa wakati wote wa historia ya Qur'an. Allah(s.w) Mwingi wa Rehema na Mwingi wa Ujuzi na Hekima, alitoa tena tahfifu nyingine kwa kuwataka wale wote wanaodai kuwa Qur'an ni kitabu cha Mtume Muhammad(s.a.w) nao waandike angalau sura moja tu mfano wa sura za Qur'an kwa ufasaha wa lugha, mantiki, mtiririko wa maudhui na ukamilifu wa ujumbe. Hebu turejee aya zifuatazo:

وَإِن كُنْتُمْ فِي رَيْبٍ مِّمَّا نَزَّلْنَا عَلَىٰ عَبْدِنَا فَأْتُوا بِسُوْرَةٍ مِّثْلِهِ  
 وَأَدْعُوا شُهَدَاءَكُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ إِن كُنْتُمْ صَادِقِيْنَ ﴿٢٣﴾

*"Na ikiwa mna shaka kwa hayo tuliyomteremshia mtumwa wetu, (kuwa hakuteremshiwa na Allah), basi leteni sura moja iliyofanywa na (mtu) aliy mfano wake, na muwaite miungu yenu bighairi ya Allah (wakusaidieni) ikiwa mnasema kweli." (2:23)*

أَمْ يَقُولُونَ أَفْتَرْتَهُ<sup>ط</sup> قُلْ فَأْتُوا بِسُوْرَةٍ مِّثْلِهِ وَأَدْعُوا مَن اسْتَطَعْتُمْ مِّنْ  
 دُونِ اللَّهِ إِن كُنْتُمْ صَادِقِيْنَ ﴿٣٨﴾

*Je, ndiyo wanasema ameitunga? Sema: "Hebu (tungeni na nyie) mlete sura moja mfano wake na waiteni muwezao (kuwapata waje) isipokuwa Allah (wa kuwasaidieni) kama nyinyi mnasema kweli (kuwa haya ameyazua Muhammad)" (10:38)*

Kama Muhammad(s.a.w) ndiye mwandishi wa Qur'an angelithubutu kweli kutoa changa moto hii kwa walimwengu wote wa nyakati zote? Mtume(s.a.w) angaliwezaje kutamka kwa uhakika kiasi hicho kuwa walimwengu wote hata wakishirikiana pamoja hawawezi kuandika kitabu mithili ya Qur'an uhakika ambao umebakia mpaka hivi leo? Kwa hiyo kushindwa kwa wanaadamu wa enzi zote za historia ya Qur'an kuleta mfano wa Qur'an angalau sura moja ni hoja tosha kuwa Qur'an ni Kitabu cha Allah(s.w).

Aidha Qur'an pia imewajibu wale watu wanaosema kuwa Muhammad(s.a.w) ndiye aliyeandika Qur'an kwa kuwataka watu hao wazingatie mawili: **Kwanza** Muhammad aliishi nao kwa muda wa miaka 40 na hakuonesha dalili zozote za kuwa mwandishi wala mshairi. Imekuwaje ghafla mtu huyo akaweza kuandika aya ambazo hakuna awezaye kuleta mfano wake? **Pili**, Muhammad angewezaje kuandika Qur'an na ilhali hakujua kusoma wala kuandika? Hoja hizo zinapatikana katika aya zifuatazo za Qur'an:

قُلْ لَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا تَلَوْتُهُ عَلَيْكُمْ وَلَا أَدْرَنْكُمْ بِهِ ۖ فَقَدْ لَبِثْتُ فِيكُمْ  
عُمُرًا مِّن قَبْلِهِ ۗ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿١٠﴾

“Sema: Kama Allah angelitaka nisingalikusomeeni hii (Qur'an), wala asingalikusomeeni (hiyo Qur'an). Nalika baina yenu umri (mwingi) kabla ya haya; (hamkunisia kusema kitu). Basi hamfahamu (kuwa haya si yangu mwenyewe kwa nafsi yangu)? (10:16)

وَمَا كُنْتُمْ تَتْلُونَ مِّن قَبْلِهِ ۗ مِن كِتَابٍ وَلَا مَخْطُوءٍ بِمِثْلِكِ ۚ إِذَا لَأَرْتَابَ  
الْمُتَبَلِّغِينَ ﴿٤٨﴾

“Na hukuwa mwenye kusoma chochote kabla ya hiki, wala hukukiandika kwa mkono wako wa kuume, (ingekuwa hivyo) wangepanya shaka wale wanaotaka kubadilisha (haki). (29:48)

### (b)Uthibitisho kutokana na Historia (Hadith)

Historia ya kushuka Qur'an na namna Mtume(s.a.w) alivyoipokea ni ushahidi mwingine unaotuthibitishia kuwa Qur'an si kitabu alichokitunga Muhammad(s.a.w). Kuna maelezo kadhaa ya kihistoria tunayojifunza katika Hadith juu ya namna Mtume(s.a.w) alivyoipokea Qur'an. Hebu turejee hadithi zifuatazo:

**Kwanza**, Hadithi ya bibi Aysha(r.a) iliyopokelewa na Imamu Bukhari inatufahamisha namna Mtume(s.a.w) alivyoipokea wahyi wa kwanza wa

Qur'an alipokuwa katika pango la Jabal Hira katika Jabal Nuur. Kama tulivyojifunza katika Hadithi hiyo Mtume(s.a.w) alistushwa sana na tukio lile la kujiwa na Malaika Jibril(a.s) na kumuamrisha kusoma kinyume na uwezo wake. Tukio lile lilimhofisha sana Mtume(s.a.w) na kumfanya arejee nyumbani kwake akiwa anatetemeka. Tukio la Jabal Hira ni ushahidi mwingine tosha kuwa Qur'an si maneno ya Muhammad(s.a.w) bali ni ujumbe kutoka kwa Allah(s.w) uliofikishwa kwake kwa njia ya wahyi kupitia kwa Malaika Jibril.

**Pili**,Mtume(s.a.w) alikuwa akibadilika haiba yake na kutokwa na jasho wakati wa kupokea wahyi kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Bibi aysha (r.a) amesimulia: Kwa hakika nimemuona Mtume akiteremshiwa wahyi siku ya baridi kali na baada ya kumaliza kile kipindi cha kuteremshiwa wahyi aliminikwa na jasho jingi kichwani mwake.” (Malik)*

*Amesimulia Aysha (r.a), “Al-Harith bin Hisham (r.a) alimuuliza Mtume wa Allah, ‘Ee mtume wa Allah! Ni vipi wahyi unakuja?’ Mtume wa Allah alijibu, “Wakati mwingine ulifunuliwa kwangu kwa sauti mithili ya mlio wa kengele, wahyi ulioletwa kwa namna hii ulikuwa mgumu sana kuliko aina nyingine zote (za wahyi), kisha hali hii ilikwisha baada ya kukidhibiti kile kilichofunuliwa. Wakati mwingine Malaika (Jibril) alikuja katika umbile la binaadamu na kuzungumza nami, ambapo nilikidhibiti (nilikichukua) chochote kile alichosema.” Aysha (r.a) aliendelea kusema: Hakika nilimuona Mtume(s.a.w) wakati anateremshiwa wahyi siku ya baridi kali na kuona jasho likitiririka usoni mwake.” (Bukhari)*

Hadithi hizi nazo zinatuthibitishia kuwa Qur'an si utunzi wa Muhammad(s.a.w) kabisa,bali ni ujumbe wa Allah(s.w) uliopitia kwake kwa njia ya wahy.

## Kuhifadhiwa kwa Qur'an

Tofauti na vitabu vingine vya Allah(s.w) vilivyotangulia, Qur'an ina ahadi ya Allah(s.w) ya kuhifadhiwa kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ ﴿٩٦﴾

*“Hakika sisi ndio tulioteremsha mawaidha haya (hii Qur'an) na hakika sisi ndio tutakaoyalinda”. (15:9)*

لَا يَأْتِيهِ الْبَطْلُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِ ۗ تَنْزِيلٌ مِّنْ حَكِيمٍ حَمِيدٍ ﴿٤٢﴾

*“Haitakifikia batili mbele yake wala nyuma yake, kimeteremshwa na Mwenye Hikima ahimidiwaye.” (41:42)*

Kutokana na aya hizi, Qur'an iko vile vile kama ilivyoteremshwa na hajjabadilika hata kidogo. Kila aya zilivyoshuka zilihifadhiwa kwa njia tatu zifuatazo:

**Kwanza**, alihifadhiwa Mtume(s.a.w) na kuahidiwa na Mola wake kuwa hatasahau kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

سُقْرُتُكَ فَلَا تَنْسَى ۝ إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ ۚ إِنَّهُ يُعَلِّمُ الْجَهْرَ وَمَا يَخْفَى ۝

*“Tutakusomesha wala hutasahau ila akipenda Mwenyezi Mungu. Yeye anajua yaliyodhahiri na yaliyofichikana.” (87:6-7)*

لَا تُحْرِكْ بِهِ لِسَانَكَ لِتَعْجَلَ بِهِ ۝ إِنَّ عَلَيْنَا جَمْعَهُ وَقُرْآنَهُ ۝

فَإِذَا قَرَأْنَهُ فَاتَّبِعْ قُرْآنَهُ ۝ ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا بَيَانَهُ ۝

*“Usitikise ulimi wako kwa (kuufanyia haraka) wahyi. Kwa hakika ni juu yetu kuukusanya na kuusomesha. Wakati tunapokusomea basi fuata kusomwa kwake. Kisha ni juu yetu kuubainisha.” (75:16-19)*

**Pili**, Waislamu walihifadhi Qur'an vifuani mwao baada ya kusomewa na Mtume(s.a.w).

**Tatu**, Qur'an ilihifadhiwa katika maandishi chini ya usimamizi wa Mtume(s.a.w) mwenyewe. Kila aya ya Qur'an iliposhuka iliandikwa wakati ule ule katika karatasi maalumu za ngozi (Qur'an 52:3) na maandishi wa Mtume(s.a.w) chini ya uangalizi na usimamizi wake kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Uthman bin Affan (r.a) amesimulia: “Wakati wowote Mtume wa Allah alipoteremshiwa wahyi humuita mmoja wa watu waliochaguliwa kuandika.” (Tirmidh)*

Naye Zaid bin Thabit mmoja wa maandishi wa Qur'an anasema:

*“Nilikuwa jirani na Mtume wa Allah, kwa hiyo kila alipoteremshiwa wahyi ilikuwa kawaida yake kuniita nami niliandika aliyoniamuru.” (Abu Daud)*

Idadi ya maandishi wa Qur'an aliowateua Mtume(s.a.w) ilifikia hadi 42. Miongoni mwa maandishi wa Mtume(s.a.w) ni pamoja na Makhalifa wake wanne - Abu bakr, Umar, 'Uthman na Ally(r.a). Waandishi wengine waliokuwa mashuhuri ni Zaid bin Thabit, Abdullah bin Mas-'ud, Ubayyi bin Ka'ab, na Khalid bin Walid.

Mtume(s.a.w) baada ya kuwaamuru maandishi wake wa Qur'an waandike kile alichowasomea, pia aliwaamuru wamsomee walichoandika na alifanya marekebisho pale walipokosea kama tunavyojifunza katika hadith ifuatayo:

*Zaidi bin Thabit amesema: "... Kila nilipomaliza kuandika (Wahyi) Mtume aliniamuru nisome nilichoandika na nilikuwa ninamsomea. Kama palikuwa na kosa alilisahihisha kisha aliwapa watu (kunakili na kuhifadhi vifuani).*

Pia Mtume(s.a.w) ndiye aliyewaelekeza waandishi wake wa Qur'an wazipange aya na sura kama zilivyo katika msahafu tulionao hivi leo kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*'Uthman bin Affan(r.a) ameeleza: "Ilikuwa kawaida ya Mtume wa Allah kila aliposhushiwa aya za sura mbali mbali (za Qur'an) au kila aya iliposhuka alimuita mmoja wapo wa waandishi wa Qur'an na kumwambia, "Andika aya hizi katika Sura kadhaa baada ya aya kadhaa."*

Pamoja na Hadithi hii kuna hoja kadhaa za kihistoria zinazothibitisha kuwa Qur'an iliandikwa na kukusanywa katika msahafu tulionao hivi leo chini ya usimamizi na uangalizi wa Mtume(s.a.w) mwenyewe. Baadhi ya hoja hizo ni hizi zifuatazo:

**Kwanza** Anas(r.a) aliyekuwa miongoni mwa masahaba wa Mtume(s.a.w) ameeleza kuwa Mtume Muhammad(s.a.w) aliwaamuru waigawanye Qur'an katika mafungu saba baada ya Suratul-Fatiha (sura ya ufunguzi). Fungu la kwanza katika haya lilikuwa na sura tatu, kisha likafuatiwa na fungu la sura tano, kisha la sura saba, kisha la sura tisa, kisha la sura kumi na moja, kisha la sura kumi na tatu na mwishowe sura zote zilizobakia ziliwekwa katika fungu moja. Fungu hili la mwisho limeanza na Suratul-Qaaf. Ukihesabu sura zote pamoja na sura ya ufunguzi (Suratul-Fatiha) utakuta Suratul-Qaaf inakuwa ni sura ya hamsini (50). Sura hii pia ni ya 50 katika Msahafu tulionao hivi leo kuthibitisha kuwa mpango wa sura katika msahafu ulioelekezwa na Mtume Muhammad(s.a.w) haujabadilika mpaka hivi leo.

**Pili** Katika Hadithi ya Abu Daud, Hudhaifa(r.a) anasimulia kuwa amemuona Mtume(s.a.w) akisoma sura ya Al-Baqara, Al-Imran, An-Nisaa, Al-Maida na Al-An-'am katika mfuatano huo. Mpango wa sura hizi kama zilivyotajwa katika Hadithi hii ni kama ziiwyo kwenye msahafu baada ya sura ya ufunguzi ambayo pia imebakia sura ya kwanza katika msahafu tangu alivyoiweka Mtume(s.a.w) katika nafasi ilipo. Hii inaonesha kuwa mpango wa sura lazima uwe umepangwa na Mtume(s.a.w) mwenyewe kama alivyoongozwa na Allah(s.w).

**Tatu** Imam Tirmidh katika kitabu chake cha Hadithi anatufahamisha hadithi ifuatayo:

*"Mtu mmoja aliuliza: "Ewe Mtume wa Allah! Tendo lipi ambalo Allah hulipenda kuliko yote?" Akajibu (Mtume) ("Tendo) la yule amalizaye safari na kisha akaendelea nayo". Pakaulizwa: "Nini maana ya kumaliza safari na kuanza nyingine?" Mtume alijibu: "Mwenye kuisoma Qur'an anaisoma tangu mwanzo hadi mwisho na amalizapo anarudia mwanzo na kusoma tena hadi mwisho na hufanya hivi kuwa kawaida yake; yaani kila amalizapo anaanza upya" (Darmi).*

Suala la kusoma Qur'an tangu mwanzo hadi mwisho ni hoja tosha ya kuwepo kwa mpango wa sura ya kwanza hadi mwisho.

## **Je Qur'an Ilikusanywa na Kuandikwa katika Msahafu Wakati wa Uongozi wa Abu-Bakr(r.a)**

Kwa muda mrefu imekuwepo nadharia kuwa Qur'an katika umbo lake la Msahafu au kitabu imeanza wakati wa Khalifa Abu Bakr baada ya kushauriwa na 'Umar ibn Khattab(r.a). Na inavyosemekana ni kwamba kwanza Abu Bakr (r.a) alikataa ushauri huo kwa kuwa jambo hilo Mtume(s.a.w)hakufanya. Baada ya kuona kuwa ni kweli Qur'an itaweza kupotea maadamu wale waliokuwa wamehifadhi wanakufa, Abubakar alikubali ushauri wa Umar.

Tunaambiwa kuwa Khalifa Abu Bakr(ra) alimchagua Zaid bin Thabit kuifanya kazi ya kuandika Msahafu. Kazi hii ilifanyika kwa kukusanya mifupa, mawe, makozi ya mitende pamoja na ngozi ambamo inasadikiwa kuwa ndimo Qur'an ilimokuwa imeandikwa wakati wote wa miaka 23 ya Utume. Hebu turejee Hadith iliyopokelewa na Imam Bukhari, na kusimuliwa na Zaid bin Thabit (ra) kuwa:

*“Abu Bakr alinitumia mtu kuja kuniita wakati watu wa Yamama walipouliwa (masahaba walipopigana na Musailama). (Nilikwenda) na nilimkuta 'Umar bin Khattab amekaa pamoja naye, Abu Bakr akaniambia: “'Umar amenijia na akaniambia kuwa siku ya Yamama, mauaji mengi yametokea kwa mahafidhi wa Qur'an na nahofia kuwa huenda mauaji yakatokea tena kwa mahafidhi katika vita vingine jambo ambalo linaweza kupelekea sehemu kubwa ya Qur'an kupotea. Hivyo nakushauri (wewe Abu Bakr) kuwa uamrishe kuwa Qur'an ikusanywe.” Nikamwambia 'Umar: “Vipi nitafanya jambo ambalo Mtume wa Allah hajalifanya?” 'Umar akaniambia kuwa: “Wallahi; kufanya hivyo ni jambo zuri”, na hakuacha kunitaka kufanya hivyo mpaka Allah akaondosha uzito kifuani mwangu na nikaanza kuona uzuri wa mawazo aliyoyaona Umar. Kisha Abu Bakr akaniambia (mimi Zaid): “Wewe ni mtu mwenye akili na hatuna wasi wasi nawe, na wewe ulikuwa ukimwandikia wahyi Mtume(s.a.w). Hivyo vitafute vipande vya Qur'an na uvikusanye'. Wallah! (anasema Zaidi kuwa) lau kama wangeniamrisha kuondoa mmojawapo wa milima, basi lisingelikuwa jambo gumu (zito) kuliko kuikusanya Qur'an. Kisha nikamuuliza Abu Bakr: “Vipi utafanya kitu ambacho Mtume wa Allah hakukifanya?” Abu Bakr alijibu: “Wallahi; kufanya hivyo ni jambo zuri”, na akaendelea kunitaka nifanye hivyo mpaka Allah akanipa wepesi kifuani mwangu kama alivyofanya kwa Abu Bakr na 'Umar. Hivyo nikaanza kuitafuta Qur'an (iliyokuwa imetapanyika vipande vipande) katika makozi ya mitende, mawe na mahafidhi na kuikusanya mpaka nikaipata aya ya mwisho ya Suratul-Tawbah kwa Abi Khuza'ymal Ansari; na sikuikuta aya hii kwa yoyote isipokuwa yeye 'Amekujieni Mtume aliye jinsi moja na nyinyi, yanamuhuzunisha yanayokutaabisheni...” mpaka mwisho wa*

aya (9:128-129). Kisha nakala ya Msahafu ikabakia kwa Abu Bakr mpaka alipofariki, kisha ikabaki kwa 'Umar mpaka mwisho wa maisha yake na hapo tena kwa binti yake Hafsa. (Bukhari).

Hadithi hii pamoja na kuwa imepokelewa na Imam Bukhari bado inatupa maswali mengi sana ya kujiuliza kwani kwanza inapingana na Qur'an yenyewe, pili inapingana na ushahidi wa kihistoria pamoja na hadithi nyingine na tatu haikubaliki hata kiakili (kimantiki).

### (a)Kupingana na Qur'an:

Hadithi hii inayosimulia kuwa Qur'an ilikusanywa na Zaid bin Thabit(r.a) kutoka kwenye makozi ya mitende na mawe na kutoka kwa mahafidhi inapingana na Qur'an kwa sababu zifuatazo:

- (i) Mwenyezi Mungu (s.w) ameikusudia Qur'an iwe kitabu hata kabla ya kuumbwa chochote katika maumbile yake aliyoyaumba.Kama inavyoashiriwa katika aya mbali mbali kwamba Qur'an ilikuwako kwenye Lawhil Mahfudh hata kabla ya kuteremshwa kwa Mtume(s.a.w) kulingana na matukio mbali mbali yalivyotokea:

إِنَّهُ لَقُرْءَانٌ كَرِيمٌ ﴿٧٧﴾ فِي كِتَابٍ مَّكْنُونٍ ﴿٧٨﴾

“Bila shaka hiki (mnachosomewa) ni kitabu kilichokusanya kila yanayohitajiwa na chenye heshima. Kimetolewa katika hicho kitabu kilichohifadhiwa kweli kweli.” (56:77-78).

بَلْ هُوَ قُرْءَانٌ مَّجِيدٌ ﴿٨١﴾ فِي لَوْحٍ مَّحْفُوظٍ ﴿٨٢﴾

“Bali hii ni Qur'an tukufu. (Iliyotolewa) katika huo ubao uliohifadhiwa (wa Allah).” (85:21-22).

Aidha Mwenyezi Mungu katika aya mbali mbali amekuwa akiashiria Qur'an na akiita kitabu:

ذَٰلِكَ الْكِتَابُ لَا رَيْبَ فِيهِ هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٢﴾

“Hiki ni kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake; ni uongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu.” (2:2).

Vile vile rejea 3:3, 7; 7:2; 10:1; 13:1; 14:1, n.k

Kutokana na marejeo hayo haiwezekani kuwa pawe hapana kitu cha aina hiyo lakini bado Mwenyezi Mungu arudie namna hiyo. Kweli, neno “kitab” linatumika kwa vitu mbali mbali vilivyoandikwa kama mikataba au hata barua lakini bado katika Qur'an neno hili limetumika kurudia kitabu katika maana halisi hasa ya kitabu. Chukua mfano, aya ya 7 ya Suratul Al-Imran:



هُوَ الَّذِي أَنْزَلَ عَلَيْكَ الْكِتَابَ مِنْهُ آيَاتٌ مُحْكَمَاتٌ هُنَّ أُمُّ الْكِتَابِ وَأُخْرُ

مُتَشَابِهَاتٌ..... ﴿٧﴾

“Yeye ndiye aliyekuteremshia Kitabu. Ndani yake zimo aya Muhkam (nyepesi kufahamika) ambazo ndizo msingi (asili ya Kitabu). Na ziko nyingine Mutashabihat...” (3:7)

Hivyo Allah(s.w) alipotaja neno Al-Kitab kwa kuirudia Qur'an alikuwa na maana hiyo na ndiyo maana Mtume(s.a.w) alipokuwa katika Hija yake ya kuaga alisema nimekuachieni vitu viwili - Kitabu cha Allah na Mwendu wangu. Mtume(s.a.w) asingelisema hivyo kama kitabu hicho hakikuwepo.

(ii)Hadith hiyo pamoja na kuwa imepokelewa na Imam Bukhari bado inakataa aya zifuatazo za Qur'an:

وَكِتَابٍ مَّسْطُورٍ ﴿٦﴾ فِي رَقٍّ مَّنْشُورٍ ﴿٧﴾

Na (Naapa) kwa Kitabu kilichoandikwa katika karatasi ya ngozi (iliyo safi na kikakunjuliwa (kisomwe).” (52:2-3).

Katika aya hii Allah(s.w) anatuambia wazi wazi kuwa Qur'an ni Kitabu kilichoandikwa katika karatasi za aina fulani ambazo zilikuwa zikitumika wakati wa zama hizo. Ni karatasi za aina hiyo hiyo, kama tutakavyoona baadaye, ambazo Mtume(s.a.w) alizitumia kuandikia barua zake na kuwatumia wafalme mbali mbali na kutumiwa na baadhi ya Masahaba kuandikia vitabu vyao.

Kabla hatujaendelea kufafanua zaidi hoja hii ni vyema kunukuu maneno ya mwanazuoni - Qutubi alivyofafanua aya hizo:

“... Na ameapa (Mwenyezi Mungu) kwa “Kitabu manshurin” (kitabu kilichoandikwa) yaani kilichoandikwa nacho ni Qur'an wanayoisoma Waislamu katika Masahafu na wanayoisoma Malaika katika Lawhul Mahfudh. Na pia inasemwa kuwa (Allah) ameviapia vitabu vingine vyote vilivyoteremshwa kwa Mitume kwani kila kitabu kilikuwa katika karatasi (ya ngozi) wakikunjuliwa watu wake wakisome. Ama “Arraqqu” ni ile iliyotengenezwa kwa ngozi ili iandikiwe”.

Lawhul Mahfudh ambao ni ubao uliohifadhiwa hautegemewi kuwa karatasi za ngozi kwani hii ni teknolojia ya mwanaadamu ambayo Mtume(s.a.w) alikutana nayo. Hivyo makusudio ya aya ni Qur'an au Msahafu.

Kutokana na ufafanuzi huo hatuwezi kusema Qur'an ilikuwa imeandikwa katika mifupa wala makozi ya mitende kwani itapingana na aya hii ambayo iko wazi. Haitakuwa na nafasi hata ikipokelewa na maimamu wote kwani kigezo kikuu cha Hadithi ni kutopingana na aya yeyote ya Qur'an. Na

kwa nini Zaid(r.a) aone uzito wa kukusanya Qur'an ambayo imeashiriwa na Allah(s.w) kuwa ni kitu kilichopo? Na uzito wenyewe uwe ni zaidi ya kuusogeza mlima!

Kusema hivyo ni kukana aya nyingine za Qur'an pale Allah(s.w) aliposema kuwa kazi ya kuikusanya Qur'an ni yake. Turejee aya zifuatazo:

لَا تُحْرِكْ بِهِ لِسَانَكَ لِتَعْجَلَ بِهِ ۚ إِنَّ عَلَيْنَا جَمْعَهُ وَقُرْآنَهُ ۚ

*"Usiutikise ulimi wako kwa (kuufanyia haraka) wahyi (unapoteremka).Kwa hakika ni juu yetu kuikusanya na kuusomesha." (75:16-17)*

Hapa aya inasema wazi kuwa kazi ya kuikusanya Qur'an siyo kifuani mwa Mtume(s.a.w) tu bali kuhakikisha kutoharibiwa kwake pamoja na kuteremka kwake kidogo kidogo ni ya Allah(s.w) kinyume chake Hadith inasema kazi hiyo aliifanya Zaid(r.a)!

### **(b)Kupingana na Ushahidi wa Kihistoria**

Hadith hii pia inapingana na ushahidi wa kihistoria kwa sababu:

- (i) Katika hadithi maarufu sana iliyopokelewa na Imam Muslim toka kwa Ibn Mas-'ud, Mtume amesema katika Hija yake ya kuaga kuwa:

*"Na nimewaachieni vitu wili ambavyo mkishikamana navyo hamtapotea kamwe baada yangu - Kitabu cha Allah na Sunnah yangu." (Muslim)*

Hadith hii kiakili haiashirii kitu ambacho hakijulikani kilipo na chenye ugumu kupatikana kama alivyoeleza Zaid(r.a) bali ni kitu ambacho kila mmoja anatarajiwa kukifikia pasipo na ugumu wowote. Wala Hadith hii haishirii kitu ambacho kimetawanyika katika mawe na mifupa ambayo pa kupatikana hapafahamiki bali ni kitu kilichokusanywa na kuhifadhiwa mahala maalumu.

- (ii) Ukiacha hadith hiyo, kuna hadith nyingine ambayo ameipokea mwenyewe Imamu Bukhari ambayo inasema wazi kabisa kuwa Mtume ameacha Msahafu:

*'Abdul'-Aziz bin Rufai(ra) ameeleza kuwa: "Mimi na Shaddad bin Ma'aqil tuliingia kwa Ibn 'Abbas. Shaddad akamuuliza: Je Mtume(s.a.w) ameacha chochote?" akajibu (Ibn 'Abbas) "Hakuacha chochote isipokuwa (hiki) kilichopo baina ya magamba mawili (ya Qur'an)." Baadaye tulimtembelea Muhammad bin Al-Hanafiyya na akamuuliza suala (lile lile). Akajibu (Al-Hanafiyya), Mtume hakuacha kitu isipokuwa (hiki) kilichopo baina ya magamba mawili (yaani Qur'an)."'*

Hadithi hii, **kwanza**, inaisadikisha Qur'an kuwa ni kitabu (mas-hafu) ambacho kimeandikwa katika kurasa na kuwekewa magamba (bindings or covers) ili kihifadhike.

**Pili**, Hadithi hii inaisadikisha Hadith tuliyoirejea juu miongoni mwa vitu ambavyo Mtume ameviacha. Hapa tunaambiwa alichocha ni kile kilicho baina ya magamba mawili - la mwanzo na mwisho - yaliyokuwa yamehifadhi Qur'an ambayo hapana shaka ilikuwa ndani ya karatasi za aina yake na siyo ndani ya mawe au mifupa.

**Tatu**, Hadith hii inathibitisha kuwa kweli Allah(s.w) alikusanya Mwenyewe Qur'an na akaihifadhi katika muundo wa kitabu kupitia kwa Mtume wake.

- (iii) Inapingana na Hadith iliyotolewa na Maimamu Tirmidhi na Darimi kuwa Mtume(s.a.w) amesema kwamba msafiri mzuri ni yule anayeianza Qur'an upya kila anapomaliza kuisoma na kwamba hili ndilo tendo analolipenda Allah. Wakati wa Mtume(s.a.w) tunaambiwa kuwa masahaba wengi walikuwa wamehifadhi Qur'an yote lakini bado walipatikana wengine ambao hawakufikia hatua hiyo. Na kwa namna tunavyowafahamu masahaba ambao walikuwa wakishindana katika kufanya mambo mazuri ni lazima wawe ambao huirudia tena na tena kama alivyoashiria Mtume(s.a.w). Sasa watu hawa walikuwa wakiipata wapi Qur'an ambayo ilikuwa imetawanyika kiasi cha aya nyingine kutojulikana zilipo na kugundulikana baadaye kama zilivyokuwa aya za Suratut-Tawbah?

Mitume wa Allah(s.w) siku zote waliwafundisha wafuasi wao vitu wanavyoweza kuvitekeleza na vipo katika mazingira yao, hivyo Mtume(s.a.w) naye alipoongea hivyo alishiria kitu cha aina hiyo. Tunasoma katika historia kwamba hata baadhi ya masahaba ambao walikuwa mahafidhi wa Qur'an walikuwa wakisoma ile iliyoandikwa. Khalifa 'Uthman bin 'Affan aliuawa wakati akisoma Mas-hafu yake. Hii inawezekana kabisa kuwa ilikuwa ni desturi ya masahaba wengi na ndivyo Mtume(s.a.w) alivyoashiria.

- (iv) Mpangilio wa sura zote zilizomo Msahafuni ukilinganishwa na kushuka kwake umeonekana ni tofauti. Mpangilio huu ni ule ambao Mtume (saw) mwenyewe aliuwelekeza kama alivyoelekezwa na Allah(s.w). Katika hayo mawe na mifupa ni vipi Mtume(s.a.w) angeweza kuashiria kwa maandishi wake kuwa aya hii iwekeni baada ya aya fulani na sura hii baada ya sura fulani?

Tukizingatia maneno ya Zaid(r.a) utakuta kuwa jambo hilo lisingeliwezekana kwani tangu kufariki Mtume(s.a.w) na alipoanza hiyo kazi haukuwa umepita hata mwaka mmoja na maandishi wa Mtume(s.a.w) wote walikuwepo bado. Lakini bado anasema aya moja hakuwa nayo yeyote yule zaidi ya Abu Khuzaymal Ansari ambaye hatuambiwi kuwa alikuwa ni mwandishi wa Mtume! Hadith hii inakataana na hali halisi kama tunavyoendelea kuiona.

- (v) Tumeona kuwa Mtume(s.a.w) alikuwa na pupa ya kuhifadhi wahyi ili asije akasahau kiasi Allah(s.w) akamwambia asifanye hivyo:

لَا تُحْرِكْ بِهِ لِسَانَكَ لِتَعْجَلَ بِهِ ۗ

“Usitikise ulimi wako kwa (kuufanyia haraka) wahyi (unapoteremka).” (75:16)

.... وَلَا تَعْجَلْ بِالْقُرْآنِ مِنْ قَبْلِ أَنْ يُقْضَىٰ إِلَيْكَ وَحْيُهُ ۗ

“.....Wala usiifanyie haraka (hii) Qur'an (kwa kusoma), kabla haujamalizika wahyi (ufunuo) wake.....” (20:114).

Sasa Mtume(s.a.w) ambaye alikuwa na pupa kiasi kama hicho cha kuhakikisha amehifadhi kila alicheletewa na Jibril(a.s) na kuhakikisha inaandikwa kila aya inayoteremka, iweje tena kuandika kwenyewe kuwe ndani ya mawe, makozi ya mitende na mifupa kiasi kwamba alipofariki haijulikani ameiweka wapi hiyo mifupa! Mtume(s.a.w) kulingana na khofu hiyo kabisa asigeliandika Qur'an mahala kama humo halafu asiweke mtu wa kuitunza bali iwe pata-potea. Hapana shaka huku ni kumsingizia Mtume(s.a.w) kuwa alikuwa haijali Qur'an:

(vi)Swali jingine la kujuliza, kwa nini Mtume atumie mawe, mifupa na makozi ya mitende kuandikia maneno matukufu ya Allah(s.w) na wakati karatasi zilikuwepo na zikitumika? Qur'an yenyewe inathibitisha kuwa wakati ule karatasi zilikuwepo:

وَلَوْ نَزَّلْنَا عَلَيْكَ كِتَابًا فِي قِرْطَاسٍ فَلَمَسُوهُ بِأَيْدِيهِمْ لَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا

إِنْ هَذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ

“Na lau tungelikuteremshia maandishi katika karatasi(kama wanavyotaka) na wakayagusa (wakakigusa hicho kitabu) kwa mikono yao, bila shaka wale waliokufuru wangelisema: “Haya si chochote ila ni uchawi dhahiri.” (6:7)

Historia inatuambia kuwa Mtume(s.a.w) ametumia karatasi kuandikia Katiba yake iliyoandikwa mara tu baada ya kuingia Madina. Sulhu ya Hudaybia, barua alizowatumia wafalme mbali mbali.

Je kusema kuwa Mtume(s.a.w) ametumia mawe na mifupa kuandikia Qur'an haionekani kuwa Mtume(s.a.w) amethamini zaidi maandishi mengine kuliko maneno ya Mwenyezi Mungu? Haiwezekani iwe hivyo bali ni visa vilivyobuniwa kuudhoofisha ukweli na Hadhi ya Qur'an.

Huenda pia ikadhaniwa kuwa, kwa sababu ya ugumu wa kupatikana karatasi ndiyo Mtume akawa anatumia mawe na mifupa. Dhana hii vile vile haina msingi kwani tunaambiwa kuwa masahaba mbali mbali walikuwa na vitabu vyao wakiandika mafunzo ya Uislamu. Hebu turejee Hadith zifuatazo:

*Abu Hurayrah(ra) amesema: “Hapana hata mmoja katika masahaba wa Mtume ambaye amesimulia Hadith nyingi zaidi kuliko mimi ukimtoa (isipokuwa) ‘Abdullah bin ‘Amr ambaye alikuwa anaandika wakati mimi sikufanya hivyo.” (Bukhari).*

*“Abu Hudhaifa(ra) amesema: Nilimuuliza Ali je muna kitabu chochote kile (zaidi ya Qur'an)? Ali alisema hapana isipokuwa kitabu cha Mwenyezi Mungu au uwezo wa ufahamu ambao amepewa Muislamu au hiki kilichomo katika upande huu wa karatasi (sahifa)...” (Bukhari).*

Hivyo suala la ugumu wa karatasi halipo kwani hapana hata sahaba mmoja ambaye angekataa kutoa karatasi ya kuandikia Qur'an kama angetakiwa kufanya hivyo.

(vii)Suala la karatasi kuwepo tena kwa wingi linaonekana hata kwa Mayahudi na Wakristo ambao walikuwa na vitabu vyao vinavyobebeka siyo vya mifupa wala mawe.Hebu turejee Hadith ifuatayo: ‘Abdallah bin ‘Umar amesema:

*“Mayahudi walikwenda kwa Mtume na kueleza kwamba mwanamke na mwanamume mmoja wao amezini Mtume akawauliza: ‘Je katika Tawrat hakuna sheria ya kupiga mawe mpaka kufa?’ Wakajibu: ‘Tunawafedhehesha kisha tunawapiga bakora! ‘Abdullah bin Salaam akasema: “Waongo kwa hakika ndani ya Tawrat imo habari ya kupiga mawe hadi kifo. “Wakaletе Tawrat isomwe na mmoja wao akaifunika ile aya ya kupiga mawe kwa mkono wake na badala yake akasoma aya ya juu na chini. ‘Abdallah bin Salaam akamwambia: “Ondoa mkono wako.” Akaondoa na mara ikaonekana aya ya kupiga mawe. Akasema “Muhammad amesema kweli kweli kwani imo aya ya kupiga mawe...” (Bukhari na Muslim).*

Huo ni ushahidi wa vitabu vilivyokuwepo. Na hata katika Qur'an tunaambiwa kuwa imeandikwa katika karatasi (52:2-3) jambo ambalo limejitokeza wakati aliposilimu Umar bin Khatib. Tunaambiwa kuwa kilichomsilimisha ni suhafa - ukurasa wa karatasi ya wakati ule ambao ulikuwa umeandikwa Surat Taha.

### **(c)Hoja za Kiakili (mantiki - logic)**

Kimantiki vile vile Hadith ya Zaid haina nguvu kwa sababu:


(i)Katika masahaba ambao Mtume(s.a.w) aliwachagua kama waandishi wake wa wahyi hatumkuti mtu anayeitwa Abu Khuzaymal Ansari. Ukiwatoa makhalifa wanne na baadhi ya Muhajiriin tunawapata Ansari wachache sana ambao walishughulikia uandishi wa wahyi wakati wa Mtume(s.a.w). Jambo la kushangaza na kutia wasi wasi katika simulizi hii ni kuwa wale waandishi wote wa Mtume(s.a.w) walioteuliwa maalum kuandika wahyi hawakuwa na aya hizo isipokuwa sahaba huyu ambaye hakuwemo! Hivyo ni kweli, Mtume(s.a.w) ambaye kila unapoteremka wahyi hata usiku

huwafuata waandishi wake ili wauandike leo hii waandishi hao ambao walikuwa majirani zake wa pua na mdomo wasiwe na aya hizo mbili bali awe nazo mtu wa mbali ambaye ni mmoja tu? Haiwezekani kabisa.

Tatizo jingine la simulizi hii ni kupingana na Hadithi nyingine au tukio lingine ambalo vile vile ni lenye kutia wasi wasi. Katika simulizi nyingine aliyoitoa Anas bin Malik na kupokelewa na Imam Bukhari tunaambiwa kuwa Khalifa 'Uthman baada ya kupata habari kuwa Qur'an inatamkwa kinyume kabisa alivyoitamka Mtume(s.a.w) aliamrisha kuandikwa nakala sanifu kwa ajili ya marudio ya watu wote. Kazi hii ya kuinakili Qur'an kutoka Msahafu unaodaiwa wa Hafsa ambao uliandikwa wakati wa Abu Bakr walikabidhiwa:

- Zaid bin Thabit. (r.a)
- Abdallah bin Zubery.(r.a)
- Sa'id bin Al'As.(r.a)
- Abdulrahman bin Harith bin Hisham.(r.a)

Katika kunakili huku Msahafu wa Hafsa kulionekana kuwa aya moja ilikosekana na mara hii ilikuwa ni:

 ..... مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ

*“Wapo watu miongoni mwa walioamini waliotimiza ahadi walioahidiana na Mwenyezi Mungu.....” (33:23)*

Aidha aya hii ilipatikana kwa Khuzaymah bin Thabit al-Ansari! Hivyo ni kweli kwa kipindi cha zaidi ya miaka kumi na mbili kitabu cha Allah(s.w) kiwe kimepungua aya na watu wote wasijue pamoja na kuwepo mahafidhi chungu nzima? Msahafu huo unaoambiwa kuwa umeandikwa wakati wa Abu Bakr(r.a) ulikuwa ndio rejea ya watu wote, je kama mtu atasema kuwa Qur'an haikuwa imetimia kwa kipindi kile atakuwa na makosa? Watu wote walirejea msahafu huo pungufu, je ahadi ya Allah(s.w) ya kuihifadhi Qur'an iko wapi wakati Msahafu pekee uliokuwapo ulikuwa na kasoro ya aya moja? Hivyo, ni visa vya kubuni tu.

- (ii) Inavyofahamika ni kuwa Zaid bin Thabit (r.a) ni mtu wa Madina (Ansar) sasa vipi ilikuwa hali ya Makka ambapo yeye alikuwa hayupo? Bila shaka palikuwa pana waandishi wengine ambao walimtangulia kwenye kazi hiyo na akashirikiana nao walipokuwa Madina. Mtume(s.a.w) alikuwa na kikundi chake cha waandishi wa wahyi na maandishi mengine kama vile mikataba. Je, ni jambo lenye kuingia akilini kuwa watu wote hao ambao inasadikiwa kufika 42 waikose aya hiyo na badala yake awe nayo mtu wa mbali? Je waandishi hao walikuwa na kazi gani ikiwa kuna aya ambazo hawakuziandika? Desturi ya masahaba ilikuwa ni ya kusubiri wahyi mpya

kama vile watu wanavyosubiri taarifa ya habari siyo wajue tu bali watekeleze. Masahaba walikuwa wanapangiana zamu za kwenda kukaa kwa Mtume ili kujua jambo lolote jipya linalowahusu wao binafsi au jamii. Simulizi hii inatuambia pamoja na kusikilizwa mahafidhi bado aya hii ilipatikana kwa mtu mmoja! Je tuseme kwa kipindi chote hicho tangu alipofariki Mtume hadi kuanza kuandikwa wakati wa 'Uthman watu walihifadhi msahafu wenye upungufu? Haiwezekani bali simulizi ni ya uzushi.

(iii) Simulizi hii vile vile inatupa wasi wasi zaidi kwani haiwezi kujibu maswali ya fuatayo: Kwa nini Zaid(r.a) aisake mifupa na mawe ambayo yametumika kuandikia Qur'an na siyo kwenda kuyachukua mahali fulani tu? Je ni sahaba gani aliyekuwa dhamana ya kulinda mifupa na mawe hayo? Wakati Mtume alipohama Makka, mawe yale na mifupa ilichukuliwa? Makozi ya mitende katika kipindi cha miaka 13 hayaozi tu?!, Usafiri gani walitumia kubebea mawe, mifupa na makozi yaliyokuwa na aya za Qur'an? Kwa kusaidia kujibu maswali hayo ni kwamba lazima mawe au mifupa hiyo ingelikuwa imekusanywa katika mojawapo ya nyumba za Waislamu hivyo pasingekuwa na haja ya kusakwa. Ilivyokuwa hizo ni aya za Allah (sw), Mtume(s.a.w) asingethubutu kuwaachia makafiri wazichezee, hivyo lazima ingesimuliwa ni vipi alizihamisha, lakini hatuna habari kama hiyo. Ukizingatia idadi ya aya za Qur'an kuwa ni 6,236 ni lazima mawe na mifupa hiyo mikubwa ingekuwa imeshindiliwa katika magunia jambo ambalo siyo kweli. Hivyo maswali hayo na majibu yanatuhitishia kuwa hiki ni kisa cha kubuni ambacho hakiingii akilini.

(iv) Al-Bukhariy ni binaadam, pamoja na udhibitifu mkubwa aliokuwa nao Al-Bukhariy katika ukusanyaji, uchambuzi na uandishi wa Hadith bado yeye ni binaadam na anayomadhaifu, hakuwa akipokea wahy wowote hivyo ubinaadamu wake yatosha yeye kukosea kunakili jambo kama hili katika sahihi yake, kwani pia zipo Hadith nyingi tu dhaifu zinazopatikana katika sahihi yake. Pia inamkinika maadui wa Uislamu wakapachika Hadith hii katika kitabu chake. Tukikumbuka kuwa vitabu vya Hadith havina hifadhi ya Allah kama ilivyo Qur'an(15:9)

## Lugha ya Qur'an:

Lugha iliyotumika katika Qur'an ni Kiarabu sanifu kama tunavyojifunza katika Qur'an yenyewe:

وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ قُرْآنًا عَرَبِيًّا لِتُنذِرَ أُمَّ الْقُرَىٰ وَمَنْ حَوْلَهَا وَتُنذِرَ

يَوْمَ الْجَمْعِ لَا رَيْبَ فِيهِ فَرِيقٌ فِي الْجَنَّةِ وَفَرِيقٌ فِي السَّعِيرِ ﴿٥٦﴾

*“Na namna hii tumekufunulia Qur'an kwa Kiarabu ili uwaonye watu wa Makka na walio pembezoni mwake. Na uwaonye siku ya mkutano, siku isiyo na shaka. Kundi moja litakuwa Peponi na kundi jingine Motoni.” (42:7)*

## **Kwa nini Qur'an Imeshushwa kwa Lugha ya Kiarabu?**

Walimwengu walio wengi wakiwemo baadhi ya Waislamu wanaitakidi kuwa lugha ya Kiislamu ni Kiarabu na Uislamu ni dini ya Waarabu. Bila shaka mawazo haya yamejitokeza kutokana na kutoujua Uislamu kwa upeo wake. Uislamu ni Dini ya Walimwengu wote wa nyakati zote na ni Dini iliyofundishwa na Mitume wote. Je, Mitume wote walikuwa Waarabu au watu wote waliolinganiwa na Mitume hao na kuwafuata walikuwa Waarabu? Bila shaka jibu litakuwa “hapana”. Bali tunajifunza katika Qur'an yenyewe kuwa Allah(s.w) amewajaalia walimwengu kuzungumza lugha mbali mbali na ni katika ishara ya Uungu wake na utukufu wake.

وَمِنْ آيَاتِهِ خَلْقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاخْتِلَافَ أَلْسِنَتِكُمْ وَاللُّوَانِكُمْ

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّلْعَالَمِينَ ﴿١٧﴾

*“Na katika Ishara zake (zinazoonyesha uwezo wake) ni kuumba mbingu na ardhi, na kuhitilafiana lugha zetu na rangi zenu. Kwa yakini katika haya zimo ishara kwa wenye ujuzi.” (30:22)*

Kwa nini Qur'an imeshushwa kwa lugha ya Kiarabu? Jibu lake linapatikana ndani ya Qur'an yenyewe:

وَمَا أَرْسَلْنَا مِن رَّسُولٍ إِلَّا بِلِسَانِ قَوْمِهِ لِيُبَيِّنَ لَهُم فَيُضِلُّ اللَّهُ مَن

يَشَاءُ وَيَهْدِي مَن يَشَاءُ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٤٤﴾

*“Na hatukumpeleka Mtume yeyote isipokuwa kwa lugha ya watu wake ili apate kuwabainishia. Kisha, Mwenyezi Mungu anamuacha kupotea amtakaye (kwa kuwa hataki kufuata ujumbe uliomfikia wazi wazi) na humuongoza amtakaye. Naye ni Mwenye nguvu na Mwenye Hekima.” (14:4)*

Aya hii inatufahamisha kuwa kila Mtume alishushiwa Wahyi kwa lugha ya watu wake ili yeye mwenyewe apate kuwabainishia vizuri na wao wapate kumuelewa vizuri. Kwa kuwa Mtume Muhammad(s.a.w) alikuwa Mwarabu wa kabila la Kiquraishi na kwa kuwa Maquraish na Waarabu kwa ujumla ndio watu wake wa mwanzo kuwalingania Uislamu ili wamsaidie kuufikisha kote ulimwenguni, Qur'an ilibidi ishushwe kwa lugha ya Kiarabu cha Kiquraish kilichokuwa fasaha kuliko vilugha vyote vya Kiarabu. Watu wake wasingemuelewa kabisa kama Mtume(s.a.w) angewalighania kwa lugha isiyokuwa ya Kiarabu:



وَلَوْ جَعَلْنَاهُ قُرْءَانًا أَعْجَمِيًّا لَقَالُوا لَوْلَا فُصِّلَتْ آيَاتُهُ ءَأَعْجَمِيٌّ وَعَرَبِيٌّ ..... ﴿٤٤﴾

“Na lau kama tungaliifanya Qur'an lugha isiyo ya Kiarabu wangelisema: Kwa nini ayazake hazikupambanuliwa? Lo! Lugha isiyokuwa ya Kiarabu na (Mtume) Mwarabu! (Mambo gani hayo)?.....” (41:44).

وَلَوْ نَزَّلْنَاهُ عَلَىٰ بَعْضِ الْأَعْجَمِينَ ﴿٤٥﴾ فَقَرَأَهُ عَلَيْهِمْ مَا كَانُوا بِهِ

مُؤْمِنِينَ ﴿٤٦﴾

“Na lau tungaliiteremsha juu ya mmoja wa wasiokuwa Waarabu, na akawasomea (kwa ufasaha) wasingalikuwa wenye kuamini.” (26:198-199)

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa:

- (i) Ni desturi ya Allah(s.w) kumtuma mjumbe wake kwa lugha ya watu wake anaowafikishia.
- (ii) Qur'an imeteremshwa kwa lugha ya Kiarabu kwa kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) alikuwa Mwarabu na wale aliowalingania mara ya kwanza walikuwa ni Waarabu.
- (iii) Waarabu wa mwanzo kulinganiwa Uislamu na Mtume(s.a.w) wasingeliukubali ujumbe kama Mtume asingelikuwa Mwarabu na kama angelingania kwa lugha nyingine isiyokuwa ya Kiarabu.
- (iv) Kama Mtume s.a.w) angelingania kwa lugha nyingine isiyokuwa Kiarabu, ujumbe wake usingelifahamika na watu wake wasingelazimika kuufuata kwa kuwa hawauielewi.

## Ujumbe wa Qur'an Utawafikiaje Wale wasio Waarabu au wale Wasiojua Kiarabu?

Si jambo zuri na si hekima mtu kufikisha ujumbe kwa Kiarabu wakati wasikilizaji wake hawafahamu lugha hiyo. Ni kweli kuwa Kiarabu ni lugha ya Qur'an na lugha aliyoitumia Mtume(s.a.w) kufundishia yale aliyoteremshiwa kutoka kwa Allah(s.w). Hivyo ni lugha ambayo inampasa kila Muislamu ajitahidi kujifunza. Pamoja na umuhimu wa kuifahamu lugha ya Kiarabu, haina maana kuwa anayekijua Kiarabu ndiye Muislamu na yule asiyekijua ni Muislamu mwenye kasoro.

La muhimu ni kuujua ujumbe wa Qur'an na kuendesha maisha ya kila siku kwa mujibu wa ujumbe huo. Ujumbe wa Qur'an unaweza kumfikia kila Muislamu pasina shaka yoyote kwa lugha yake kwa kusoma tafsiri na sherehe ya Qur'an ambayo kwa Rehema ya Allah(s.w) imetolewa katika lugha mbali

mbali na wanachuoni wacha Mungu ambao ni mashuhuri katika uliwengu wa Waislamu. Tukumbuke kuwa Qur'an imeshushwa kwa ajili ya walimwengu wote ambao Allah(s.w) amewajaalia kuzungumza lugha zinazotofautiana (rejea Qur'an (39:22). Naye Mtume(s.a.w) pia ameletwa kwa ajili ya walimwengu wote. Hivyo ili ujumbe wa Qur'an na Sunnah uwafikie walengwa wote, hauna budi kufasiriwa kwa lugha za walengwa wote. Kazi ambayo kwa Rehema ya Allah(s.w) imeshafanyika. Leo hii hapana udhuru kwa mtu yeyote ulimwenguni wa kutoufahamu ujumbe wa Qur'an kwa sababu si Mwarabu au hajui Kiarabu.

## **Haja ya Kujifunza Lugha ya Kiarabu kwa Waislamu:**

Ipo haja kubwa kwa Waislamu kujifunza lugha ya Kiarabu kuliko ile haja tunayoitambua ya kujifunza lugha za kigeni na za Kimataifa kama vile Kiingereza, Kifaransa, n.k. Kwa mfano hapa Tanzania tunajifunza lugha ya Kiingereza (English) ili tuweze kufaidika kitaaluma, kiuchumi, na kisiasa n.k. Tukijifunza lugha ya Kiarabu tunafaidika na hayo yote pamoja na ziada ifuatayo:

- (i) Tutaufahamu ujumbe wa Qur'an na mafundisho ya Mtume(s.a.w) kwa lugha yake ya asili. Daima tafsiri haikosi upungufu japo kidogo.
- (ii) Tutaweza kufahamu maana ya undani ya dua na dhikiri mbali mbali tunazoleta katika ibada maalum kama vile swala ambapo haturuhusiwi kutumia lugha nyingine isiyokuwa Kiarabu. Kufahamu maana ya yote tuyasemayo katika swala hutupelekea kuwa na khushui inayotakikana.
- (iii) Lugha ya Kiarabu ni chombo cha kuwaunga nisha waislamu wote ulimwenguni ili wadumishe udugu na umoja wao kama wanavyotakiwa wawe. Kama Waislamu wanavyoshikamana katika swala kwa kutumia lugha moja ndivyo wanavyotakiwa waelewane na kushikamanakatikaibadazotezinazofanywakimataifakamavilelbadayaHijja.

## **Namna ya Kuiendea Qur'an**

Pamoja na kujifundisha kuisoma Qur'an kwa kuzingatia hukumu zake na kuwafundisha watoto wetu hivyo, hatuna budi kuisoma Qur'an kwa mazingatio ili kufikia lengo la kushushwa kwake. Qur'an imeshushwa ili iwe mwongozo wa maisha yetu yote ya binafsi na ya jamii. Mtume(s.a.w) alipoamrisha katika mwanzo wa Utume wake "Warattilil-Qur'an tar-tiilaa" - "na soma Qur'an vilivyo" haikuwa na maana ya kumtaka Mtume(s.a.w) kuisoma Qur'an kwa tajwidi kama wasomaji wa tajwid wanavyoghani, bali ni amri ya Allah(s.w) iliyomtaka Mtume(s.a.w) na wafuasi wake wote wa ulimwengu mzima, waisome Qur'an kwa mazingatio ili waupate kwa uwazi ujumbe uliomo na waweze kuufuata vilivyo katika maisha yao ya kila siku. Wale wanaosoma aya za Qur'an bila ya kuzizingatia na kuziingiza katika utendaji Allah(s.w) amewalinganisha na punda', mbwa, viziwi na vipofu

مَثَلُ الَّذِينَ حُمِلُوا التَّوْرَةَ ثُمَّ لَمْ يَحْمِلُوهَا كَمَثَلِ الْحِمَارِ يَحْمِلُ  
 أَسْفَارًا ۗ بِئْسَ مَثَلُ الْقَوْمِ الَّذِينَ كَذَبُوا بِقَايَتِ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي  
 الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿٥﴾

*Mfano wa wale waliopewa Taurati kisha hawakuichukua, ni kama mfano wa punda aliyebeba vitabu. Ni mfano mbaya kabisa wa watu waliokadhibisha aya za Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu. (62:5).*

..... فَمَثَلُهُ كَمَثَلِ الْكَلْبِ إِنْ حَمَلَ عَلَيْهِ يَلْهَثُ أَوْ تَتْرَكُهُ يَلْهَثُ ۗ .... ﴿٧٦﴾

*.....Basi mfano wake ni kama mfano wa mbwa, ukimkimea anahema, ukimwacha anahema.....(7:176).*

صُمُّ بَكْمٌ عُمَىٰ فَهَمٌّ لَا يَرِجَعُونَ ﴿١٨﴾

*“Viziwi, mabubu, vipofu, kwa hivyo hawatarejea (katika uongofu).” (2:18)*

Kwa namna nyingine, Allah(s.w) anatufahamisha kuwa, waja wake anaowapenda atakaowaongoza katika njia iliyonyooka hapa ulimwenguni na kuwalipa ghorofa za Peponi na makazi mazuri kabisa, ni pamoja:

وَالَّذِينَ إِذَا ذُكِّرُوا بِقَايَتِ رَبِّهِمْ لَمْ يَسْمِعُوا عَلَيْهَا صُماً وَعُمِيَانًا ﴿٧٦﴾

*“Na wale ambao wanapokumbushwa aya za Mola wao hawaziangukii kwa uziwi na upofu.” (25:73)*

Kwa kuzingatia maelezo haya, ili tuweze kuongozwa na Qur'an hatuna budi kufanya yafuatayo:

- (i) Tupitie kwa makini maelezo ya kitabu hiki ili tuwe na yakini kuwa Qur'an ni kitabu cha Allah(s.w) kisicho na shaka hata kidogo.
- (ii) Kwa kuwa na yakini kuwa Qur'an ni ujumbe kutoka kwa Allah(s.w),hatuna budi kuisoma kwa mazingatio na kujitahidi kupata ujumbe unaotokana na kila aya.
- (iii)Ili kuupata kwa uwazi ujumbe wa kila aya au kila sura ya Qur'an hatunabudi kusoma tafsiri na sherehe za wanazuoni mbali mbali waliojitahidi kuitafsiri Qur'an katika lugha tunayoimudu. Qur'an imetafsiriwa katika lugha mbali mbali kikiwemo Kiswahili na Kiingereza.
- (iv)Baada ya kuupata kwa uwazi ujumbe wa Qur'an hatuna budi kuyaingiza maagizo ya Mola wetu katika utendaji huku tukimfanya Mtume(s.a.w) kiigizo chetu na huku tukizingatia msisitizo wa aya zifuatazo:

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ  
الْحَيْزَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَنْ يَعِصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُبِينًا ﴿١٦﴾

“Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hakika amepotea upotofu ulio wazi (kabisa).” (33:36)

..... وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ ﴿١٧﴾

“.....Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri.” (5:44)

..... وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿١٨﴾

Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhalimu (5:45)

..... وَمَنْ لَّمْ يَحْكَمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿١٩﴾

“Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio mafasiki(5: 47)

(v) Ili kuiingiza Qur'an yote katika maisha yetu ya kila siku na kujipamba na tabia ya Qur'an lazima kujenga tabia ya kuwa wasafiri wa Qur'an wa kudumu kwa kuipitia kwa mazingatio kuanzia sura ya mwanzo (Al-Faatiha) mpaka ya mwisho (An-Naas) na iwe ni ada yetu mpaka tutakapokufa. Kufanya hivyo Mtume(s.a.w) amefananisha na mtu kufanya safari ya kheri isiyokatika, ambayo ina malipo makubwa mbele ya Allah(s.w). Kuipitia Qur'an yote mara kwa mara kwa mazingatio humfanya muumini aweze kuishi katika mipaka ya Allah(s.w) katika kila kipengele cha maisha yake.

(vi)Tuwe na tabia ya kuirejea Qur'an kila tunapokwama au tunapokabiliwa na tatizo lolote la kibinafsi au la kijamii. Tusiridhike kujifanyia au kufuata mkumbo katika kuendea mambo ya kibinafsi au ya kijamii bila ya kuangalia kwanza Allah(s.w) kasema nini au kaagiza nini juu ya jambo hilo au Mtume wake(s.a.w) ambaye ndiye mfasiri wa Qur'an, ameliendeaje jambo hilo. Katika kusisitiza nukta hii tuzingatie agizo la Mtume(s.a.w) alilolitoa mwezi 9 Dhul-Hajj, 10 A.H. (633 A.D) katika uwanja wa Arafa katika Hija ya kuaga (Hijjatul-Wadaa) pale aliposema:

قال رسول الله صلى الله عليه والسلام: تركت فيكم ما إن تمسكتم به  
لن تضلوا أبدا كتاب الله و سنتي.

*Amesema mjumbe wa wa Mwenyezimungu “Nimekuachieni vitu viwili ambavyo mkikamatana navyo hamtapotea abadan, navyo ni kitabu cha Allah (Al-Qur’an) na Sunnah ya Mtume wake.”*

- (vii)Tufanye juhudi ya kusimamisha Uislamu katika jamii kwa mali zetu na nafsi zetu, ili tuweze kuufuata Uislamu wote katika kila kipengele cha maisha ya binafsi na ya jamii kama Qur’an yenyewe inavyo sisitiza:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَدْخُلُوا فِي السِّلْمِ كَآفَّةً وَلَا تَتَّبِعُوا خُطُوَاتِ  
الشَّيْطَانِ إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ

*“Enyi mlioamini! Ingieni katika hukumu zote za Uislamu, wala msifuate nyayo za shetani, kwa hakika yeye kwenu ni adui dhahiri.” (2:208)*

Ni dhahiri kwamba pale ambapo Uislamu haujashika hatamu za Uongozi wa jamii, Waislamu watakuwa hawana namna ya kutofuata nyayo za shetani katika siasa, uchumi, utamaduni na katika kila nyanja ya maisha ya jamii. Pale ambapo Uislamu haujasimama katika jamii, Waislamu watakuwa wanaswali huku chakula chao na kivazi chao kinatokana na uchumi haramu unaotokana na uzinzi, kamari, riba, ulevi, rushwa na mengineyo. Watakuwa wanafunga huku futari na daku yao inatokana na uchumi haramu, watakuwa wanatoa zakat na kuhiji kwa mali inayotokana na uchumi haramu; watakuwa wanamuabudu Mwenyezi Mungu wakiwa misikitini na wanapotoka misikitini hufuata sera na sharia za kitwaghuti zilizotungwa mabungeni. Hivyo, ni wazi kuwa pale ambapo Uislamu haujasimama katika jamii, Qur’an haitapewa nafasi ya kuwaongoza Waislamu katika kila kipengele cha maisha yao, jambo ambalo inabidi Waislamu waingie katika jihadi ili kupigania uhuru wao wa kuongozwa na Qur’an. Kama Waislamu watapuuza suala hili la jihadi na wakaridhika kuishi maisha ya mseto ya kutumikia miungu wawili - Allah(s.w) katika swala, zakat, saum, n.k na Twaghuti katika uchumi, siasa, sheria, n.k. wajue kuwa hawana ridhaa ya Allah(s.w) bali hali yao halisi ni ile inayoelezwa katika aya zifuatazo:

..... أَفْتَوْمُنُونَ بَعْضُ الْكِتَابِ وَتَكْفُرُونَ بِبَعْضٍ فَمَا جَزَاءُ مَنْ  
يَفْعَلُ ذَلِكَ مِنْكُمْ إِلَّا خِزْيٌ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ  
يُرَدُّونَ إِلَىٰ أَشَدِّ الْعَذَابِ .....

“... Je! Mnaamini baadhi ya kitabu na kukataa baadhi (yake)? Basi hakuna malipo kwa mwenye kufanya haya katika nyinyi ila ni fedheha katika maisha ya dunia, na siku ya Kiyama watapelekwa katika adhabu kali...” (2:85)

اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ ءَامَنُوا يُخْرِجُهُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَوْلِيَاؤُهُمُ الطَّاغُوتُ يُخْرِجُونَهُم مِّنَ النُّورِ إِلَى الظُّلُمَاتِ أُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٥٧﴾

“Mwenyezi Mungu ni mlinzi (kiongozi) wa wale walioamini. Huwatoa katika giza na kuwaingiza katika nuru. Lakini waliokufuru walinzi (viongozi) wao ni matwaaghuti. Huwatoa katika nuru na kuwaingiza katika giza. Hao ndio watu wa motoni, humo watakaa milele. (2:257)

### Zoezi 3.1

- (a) Orodhesha madai kumi (10) wanayotoa makafiri dhidi ya Qur'an:  
(b) Onesha udhaifu wa madai matano (5) dhidi ya Qur'an.
- Kwa kuirejea Qur'an yenyewe na Historia ya kushuka kwake, toa hoja kumi (10) kuthibitisha kuwa Qur'an ni ufunuo kutoka kwa Allah(s.w).
- “Hakika sisi ndio tulioteremsha mawaidha haya (hii Qur'an) na hakika sisi ndio tutakaoyalinda”.

Onesha namna Qur'an ilivyohifadhiwa wakati wa Mtume(s.a.w).

- Kwa mujibu wa Qur'an, hekima ya Qur'an kushushwa kwa lugha ya Kiarabu ni:  
(a) \_\_\_\_\_  
(b) \_\_\_\_\_  
(c) \_\_\_\_\_  
(d) \_\_\_\_\_
- Ili Qur'an ituongoze kwenye njia iliyonyooka hatunabudi kufanya mawili yafuatayo:  
(a) \_\_\_\_\_  
(b) \_\_\_\_\_

## MAFUNZO YA SURA ZILIZOCHAGULIWA

Sura zilizochaguliwa kwa kidato cha nne ni

1. Al - 'A'ala.
2. Adh - Dhuhaa.
3. Alam Nashrah.
4. At - tyn.

### 1. Suratul Al-A'ala.

***Kwa Jina la Allah Mwingi wa  
Rehema Mwenye Kurehemu.***

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Litukuze jina la Mola wako  
aliyemtukufu.

سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى ﴿١﴾

2. Aliyeumba (kila kitu) na  
akakitengeneza.

الَّذِي خَلَقَ فَسَوَّى ﴿٢﴾

3. Na akakikadiria (kila kimoja  
jambo lake) na akakiongoza.

وَالَّذِي قَدَّرَ فَهَدَى ﴿٣﴾

4. Na aliyeotesha ndisha (malisho).

وَالَّذِي أَخْرَجَ الْمَرْعَى ﴿٤﴾

5. Kisha akaifanya mikavu yenye  
kupiga weusi.

فَجَعَلَهُ غُثَاءً أَحْوَى ﴿٥﴾

6. Tutakusomesha wala hutasahau.

سُنُقِرْنَاكَ فَلَا تَنْسَى ﴿٦﴾

7. Ila akipenda Mwenyezi Mungu;  
Yeye anajua yaliyodhahiri na  
yaliyofichikana.

إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ إِنَّهُ  
يَعْلَمُ الْجَهْرَ وَمَا يَخْفَى ﴿٧﴾

8. Nasi tutakusahilishia (kuitangaza)  
dini iliyo nyepesi (Uislamu).

وَنُيَسِّرُكَ لِلْيُسْرَى ﴿٨﴾

9. Basi waidhisha ikiwa utafaa  
waadhi.

فَذَكِّرْ إِنْ نَفَعَتِ الذِّكْرَىٰ ﴿٩﴾

10. Bila shaka atakumbuka mwenye  
kumuogopa Allah(s.w).

سَيَذَكَّرُ مَنْ نَحَّشَىٰ ﴿١٠﴾

11. Na mwingi wa mateso atajitenga  
mbali nayo hayo (mawaidha).

وَيَتَجَنَّبُهَا الْأَشْقَىٰ ﴿١١﴾

12. Ambaye atauingia Moto mkubwa

الَّذِي يَصِلَى النَّارَ الْكُبْرَىٰ ﴿١٢﴾

13. Kisha humo hatakuwa wala  
hatakuwa hai.

ثُمَّ لَا يَمُوتُ فِيهَا وَلَا يَحْيَىٰ ﴿١٣﴾

14. Hakika amekwishafaulu  
aliyejitakasa na mabaya

قَدْ أَفْلَحَ مَنْ تَزَكَّىٰ ﴿١٤﴾

15. Atakumbuka jina la Mola wake  
anakasali

وَذَكَرَ اسْمَ رَبِّهِ فَصَلَّىٰ ﴿١٥﴾

16. Lakini nyinyi mnapenda zaidi  
maisha ya dunia

بَلْ تُؤْثِرُونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ﴿١٦﴾

17. Hali ya kuwa ya Akhera ni bora  
zaidi kabisa yenye dumu

وَالْآخِرَةُ خَيْرٌ وَأَبْقَىٰ ﴿١٧﴾

18. Hakika haya (mnayoambiwa humu  
katika Qur'ani) yamo katika vitabu  
vilivyo tangulia.

إِنَّ هَذَا لَفِي الصُّحُفِ الْأُولَىٰ ﴿١٨﴾

19. Vitabu vya Ibrahimu na Musa(na  
wengineo)

صُّحُفِ إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَىٰ ﴿١٩﴾

### Maelezo juu ya Sura

Sura hii inapata jina lake kutokana na neno Al-a'ala la lililomo katika aya ya kwanza. Sura hii ni ya 87 katika msahafu na katika historia ya kushuka ni ya 8. Hivyo sura hii ni katika sura za Makka iliyoshushwa katika kipindi cha mwanzo wa Utume pale Mtume(s.a.w) alipokuwa hajazoea kupokea wahyi na akikhofu kuwa atasahau kile alichosomewa na Jibril(a.s). Ndipo Allah(s.w) akamliwaza katika aya ya 6 na 7.



سُنْقَرْتُكَ فَلَا تَنْسَى ﴿٦﴾ إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ ..... ﴿٧﴾

“Tutakusomesha wala hutasahu, ila akipenda Mwenyezi Mungu.....(87: 6-7)”

Pamoja na maliwazo hayo, Mtume(s.a.w) kwa kujua uzito wa kutofikisha vilivyo kile alichogizwa na Mola wake afikishe kwa watu, alijisahau tena na kuufanyia haraka wahyi; ndipo katika Suratul-Qiyaamah, ambayo ni ya 31 kushuka, Allah(s.w) alimliwaza tena Mtume wake kwa kumuagiza:

لَا تُحْرِكْ بِهِ لِسَانَكَ لِتَعْجَلَ بِهِ ﴿٨﴾ إِنَّ عَلَيْنَا جَمْعَهُ وَقُرْءَانَهُ ﴿٩﴾  
فَإِذَا قَرَأْتَهُ فَاتَّبِعْ قُرْءَانَهُ ﴿١٠﴾ ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا بَيَانَهُ ﴿١١﴾

“Usiutikise ulimi wako kwa (kuufanyia haraka) wahyi. Kwa hakika ni juu yetu kuukusanya na kuusomesha. Wakati tunapokusomea, basi fuata kusomwa kwake. Kisha ni juu yetu kuubainisha” (75:16-19)

Pamoja na Mtume(s.a.w) kuhakikishiwa udhibiti wa ujumbe wa Qur'an na Mola wake, hakuacha kuwa na wasiwasi kutokana na unyeti wa dhima aliyopewa. Ndipo tena Allah(s.w) akamliwaza katika Suratu Twaahaa ambayo ni ya 45 kushuka kama ifuatavyo:

فَتَعَلَى اللَّهِ الْمَلِكُ الْحَقُّ ﴿١٢﴾ وَلَا تَعْجَلْ بِالْقُرْءَانِ مِنْ قَبْلِ أَنْ يُقْضَىٰ  
إِلَيْكَ وَحْيُهُ ﴿١٣﴾ وَقُلْ رَبِّ زِدْنِي عِلْمًا ﴿١٤﴾

“Ametukuka Mwenyezi Mungu. Mfalme wa haki, wala usiifanyie haraka (hii) Qur'an (kwa kusoma), kabla haujamalizika wahayi wake. Na (uombe) useme: “Mola wangu nizidishie ilimu” (20:114)

Baada ya hapo, haikumtokea tena Mtume(s.a.w) kuwa na wasiwasi katika kupokea wahayi.

### Mafunzo

Katika aya ya kwanza ya Sura hii tunaamrisha kulitukuza jina la Mola wetu mlezi aliyemtukufu na katika aya ya 2 hadi ya 5, zinatolewa hoja kwanini Allah(s.w) pekee ndiye anayestahiki kutukuzwa na si mwinginewe.

Katika aya hizi inabainisha wazi kuwa Allah(s.w) ndiye muumbaji na mtengenezaji sura ya kila kitu pamoja na kukiumba kila kitu na kukipa sura yake, Allah(s.w) amekikadiria kila kiumbe jambo lake, akakiwekea mustakbali wake na akakiongoza kwa silka au kwa wahyi kufikia lengo lake lililokusudiwa. Kuongoza kwa Allah(s.w) ni kwa namna mbili: kwa viumbe visivyo na hiari na kwa viumbe vyenye hiari (majini na watu).

Viumbe visivyo na hiari kama wanyama, mimea na kadhalika, huongozwa kwa silka (instincts) ambazo huwaelekeza namna ya kutafuta chakula, kujihifadhi na mazingira, kujilinda na maadui, kuzaliana na kadhalika. Viumbe vya kundi hili hufuata kanuni na sharia za maumbile alizoziweka Allah(s.w) bila ya kuzikiuka. Tunathibitishiwa hili katika Qur'an:

سَبَّحَ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٦١﴾

*“Vinamtukuza Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na ardhini, na yeye ni mwenye nguvu, mwenye hikima” (61:1).*

يُسَبِّحُ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ الْمَلِكِ الْقُدُّوسِ الْعَزِيزِ

*Vinamtukuza Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini (Mwenyezi Mungu) aliye Mfalme, Mtakatifu, Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima” (62:1)*

Majini na watu pamoja na kuongozwa kisilka (ndani kwa ndani) katika maumbile yao kama wanyama, wadudu na mimea, wametunukiwa akili na uwezo wa kufikiri, elimu na uwezo wa kujelimisha, utambuzi binafsi (self consciousness) na hiari ya kuchagua lipi la kufuata. Katika hali hiyo Allah(s.w) amewaletea majini na watu mwongozo unawabainishia njia ya kheri (uongofo) itakayowafikisha kwenye lengo la maisha yao na ile ya shari (upotofu) itakayowakwamisha kufikia lengo tarajiwa. Na hili linathibitishwa katika Qur'an:

إِنَّا هَدَيْنَاهُ السَّبِيلَ إِمَّا شَاكِرًا وَإِمَّا كَفُورًا ﴿٧٦﴾

*“Hakika sisi tumemuongoa (binadamu kwa kumbainishia) njia (zote mbili hizi kuwa hii ndiyo ya kheri na hii ndiyo ya shari). Basi (mwenyewe tena) atakuwa mwenye shukrani au awe mwenye kukufuru” (76:3).*

Uoteshaji wa malisho ya wanyama umetajwa kama mfano wa kuwakilisha sifa ya Allah(s.w) ya ulishaji au utoaji riziki kwa viumbe vyote.

Pia umetajwa uwezo wa Allah(s.w) wa kuyafanya malisho (majani na mimea mingine) kukauka kama mfano wa kuwakilisha sifa nyingine ya Allah(s.w) ya kufisha vile alivyoviumba baada ya muda aliovikadiria kuisha.

Katika aya ya 6 hadi ya 8, Allah(s.w) anamliwaza Mtume(s.a.w) na kwahiyo, Waislamu wote kuwa atamfanyia wepesi kuifahamu Qur'an vilivyo na kumrahishia kazi ya kuuhisha na kuusimamisha Uislamu katika jamii. Hii imekaririwa katika aya nyingi kuwa Allah(s.w) ameifanya Qur'an kuwa nyepesi:

وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْآنَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِنْ مُدَّكِرٍ ﴿٧٧﴾

“Kwa yakini tumeifanya Qur'an iwe nyepesi kufahamika lakini yuko anayekumbuka?” (54:17,22,32,40)

Pia Allah(s.w) ametuhakikishia katika Suratul Hajj kuwa ameufanya Uislamu kuwa mwepesi:

..... وَمَا جَعَلْ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ ..... ﴿٧٨﴾

“..... Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika dini. ....(22:78)

Baada ya kuufahamu Uislamu na kuufuata tunalazimika kuufikisha ujumbe wa Uislamu kwa wale ambao haujawafikia, pia tunalazimika kuwakumbusha wale ambao tayari ujumbe umeshawafikia, lakini wakawa wanasahau au kughafilika.

Waumini wa kweli wanapokumbushwa aya za Mwenyezi Mungu huzifuata kwa unyenyekevu, lakini wale waliokufuru, hawaonyeki kwa ukumbusho wa aya wala Hadithi, na Mwenyezi Mungu amewakamia adhabu kali ya motoni.

Katika aya ya 14 na 15 wametajwa wale waliofaulu kuwa ni wale wanaojitakasa na kujiepusha na mambo maovu na machafu na wakawa wanamkumbuka Mola wao kwa wingi, wakawa wanasimamisha swala na wakawa wanatii kanuni na sharia za Allah(s.w) katika kukiendea kila kipengele cha maisha yao.

Katika aya ya 16 na 17 yanalinganishwa maisha ya dunia na maisha ya akhera. Maisha ya akhera yametajwa ni bora kwa mara nyingi zaidi na ya kudumu milele ambapo maisha ya dunia ni duni na ya muda mfupi sana.

Kuhusiana na muda mfupi wa maisha ya dunia ukilinganisha na ule wa maisha ya akhera, tunafahamishwa katika Qur'an kuwa watu watakapoulizwa kuwa waliishi muda gani humu duniani, watajibu,kuwa waliishi siku moja au sehemu ya siku hata wale walioishi zaidi ya miaka elfu. Kuhusu ubora wa starehe za dunia na ule wa starehe za akhera, Allah(s.w) anatumfahamisha:

كُلُّ نَفْسٍ ذَائِقَةُ الْمَوْتِ وَإِنَّمَا تُوَفَّوْنَ أَجُورَكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَمَنْ زُحِرَ عَنِ النَّارِ وَأُدْخِلَ الْجَنَّةَ فَقَدْ فَازَ وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا مَتَاعُ الْغُرُورِ ﴿١٨٥﴾

“Kila nafsi itaonja mauti. Na bila shaka mtapewa ujira wenu kamili siku ya kiyama. Na aliyewekwa mbali na Moto na akaingizwa peponi, basi amefuzu. Na maisha ya dunia si kitu ila starehe idanganyayo” (3:185)

Kwa bahati mbaya binaadamu waliowengi pamoja na ujumbe huu ulio wazi, wamechagua kuchukua starehe za dunia na kukosa starehe za akhera. Ni ujinga na uzembe ulioje!

Aya ya 18 na 19 inahitimisha kuwa mafunzo yaliyomo ndani ya Qur'an kupitia kwa Mtume Muhammad(s.a.w) si mageni bali ni yale yale yaliyofundishwa na Mitume waliotangulia na kubainishwa katika vitabu vyao, akiwemo Mtume Ibrahim(a.s) na Musa(a.s). Kwa ujumla tunajifunza katika Qur'an kuwa Uislamu ni mfumo sahihi wa maisha kwa ajili ya walimwengu wote wa nyakati zote. Mitume wote kuanzia Adamu(a.s) hadi Muhammad(s.a.w) wameletwa kuufundisha Uislamu na kuusimamisha katika jamii.

✽ شَرَعَ لَكُمْ مِنَ الدِّينِ مَا وَصَّى بِهِ نُوحًا وَالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ وَمَا وَصَّيْنَا بِهِ إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَى وَعِيسَى أَنْ أَقِيمُوا الدِّينَ وَلَا تَتَفَرَّقُوا فِيهِ ۚ كَبُرَ عَلَى الْمُشْرِكِينَ مَا تَدْعُوهُمْ إِلَيْهِ ۗ..... ﴿١٣﴾

*“Amekupeni sharia ya dini ile ile aliyomuusia Nuhu na tuliyokufunulia wewe na tuliyowausia Ibrahim na Musa na Isa, kwamba simamisheni dini wala msifarikiane kwayo. Ni ngumu kwa wenye kushirikisha (dini hii) unayowaitia...” (42:13)*

### **Mafunzo kwa Muhtasari**

Kwa muhtasari kutokana na sura hii tunajifunza kuwa:

- (1) Mwenyezi Mungu pekee ndiye anayestahiki kutukuzwa na kusifiwa kwa sababu ndiye aliyeumba kila kitu na kukitengeneza katika sura maridhawa kwa lengo maalumu, kisha akakipa mahitaji yake na akakilea na kukiongoza mpaka kikafikia lengo la kuumbwa kwake, kisha ndiye pekee atakayekifisha baada kumaliza muda wake aliokikadiria.
- (2) Qur'an imehifadhiwa na Mwenyewe Mwenyezi Mungu na ameijaalia kuwa nyepesi kwa yule anayetaka kuongoka na akatia juhudi ya kuisoma na kuifuata.
- (3) Uislamu ni dini nyepesi kujua na kuifuata.
- (4) Kila muislamu anawajibu kuujua Uislamu vilivyo na kuutekeleza.
- (5) Kila muislamu anawajibika kuufundisha na kuufikisha ujumbe wa Uislamu kwa wale ambao haujawafikia na kuwaonya na kuwakumbusha wale uliowafikia wakapuzia au wakasahau.
- (6) Wale watakaoupokea ujumbe wa Uislamu wakajitakasa na maovu na

wakajizatiti kumtukuza Mola wao katika kila kipengele cha maisha yao, wakawa wanasimamisha swala na kutekeleza lbada nyingine mbalimbali walizopangiwa na Mola wao, watakuwa ni wenye kufuzu katika maisha ya dunia na akhera.

- (7) Wale watakaopuuzwa mafundisho ya Uislamu, wakatakabari na kuendelea kufanya maovu watastahiki adhabu ya Mwenyezi Mungu iumizayo katika maisha ya akhera, japo hapa duniani wanaweza kuonjeshwa starehe ndogo.
- (8) Maisha ya akhera ndiyo bora kwani ni yenye starehe ya kweli yenye kudumu milele. Kinyume chake starehe ya hapa duniani ni ya uwongo na ni ya muda mfupi sana.
- (9) Uislamu ni dini pekee ya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya walimwengu wote wa nyakati zote.

إِنَّ الدِّينَ عِنْدَ اللَّهِ الْإِسْلَامُ ..... ﴿٣١٩﴾

*Bila shaka dini (ya haki) mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu.....” (3:19)*

وَمَنْ يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِينًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ

الْخَاسِرِينَ ﴿٣٨٥﴾

*“Na anayetaka dini isiyokuwa Uislamu, haitakubaliwa kwake. Naye akhera atakuwa katika wenye khasara (kubwa kabisa)” (3:85)*

## Zoezi 3:2

1. Hifadhi kifuani Suratul-A'alaah na tafsiri yake.
2. Onesha kuwa aya ya 6 na 7 (87:6-7) ya Suratul-A'alaah ni kiashiria kuwa sura hii ni miongoni mwa sura za Makka iliyoshushwa katika kipindi cha mwanzo cha Utume wa Muhammad(s.a.w).
3. Toa mafunzo makuu mawili (2) yatokanayo na aya ya 1 hadi ya 5 ya Suratul-A'alaah (87:1-5).
4. “Nasi tutakusahilishia (kuitangaza) dini iliyo nyepesi” (87:8)  
Toa hoja tatu za msingi kuonesha kuwa Uislamu ni dini nyepesi kwa binaadamu.
5. Ainisha mafunzo makuu yatokanayo na aya ya 9 hadi ya 15 ya Suratul-A'alaah (87:9-19)

## 2. Suratu Dhuhaa (93)

*Kwa jina la Allah Mwingi wa  
Rehema, Mwenye kurehemu.*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Naapa kwa mchana.

وَالضُّحَىٰ ﴿١﴾

2. Na kwa usiku unapotanda.

وَاللَّيْلِ إِذَا سَجَىٰ ﴿٢﴾

3. Hakukuacha Mola wako wala  
hakukukasirikia (ewe Nabii Muhammad).

مَا وَدَّعَكَ رَبُّكَ وَمَا قَلَىٰ ﴿٣﴾

4. Na bila shaka (kila) wakati ujao  
(utakuwa) bora zaidi kuliko  
uliotangulia.

وَلَلْآخِرَةُ خَيْرٌ لَّكَ مِنَ الْأُولَىٰ ﴿٤﴾

5. Na Mola wako atakupu mpaka  
uridhike.

وَلَسَوْفَ يُعْطِيكَ رَبُّكَ فَتَرْضَىٰ ﴿٥﴾

6. Je, hakukukuta yatima akakupu  
makazi (mazuri ya kukaa)?

أَلَمْ يَجِدْكَ يَتِيمًا فَآوَىٰ ﴿٦﴾

7. Na akakukuta hujui kuongoza njia,  
akakuongoza?

وَوَجَدَكَ ضَالًّا فَهَدَىٰ ﴿٧﴾

8. Na akakukuta fakiri akakutajirisha?

وَوَجَدَكَ عَائِلًا فَأَغْنَىٰ ﴿٨﴾

9. Basi usimuonee Yatima.

فَأَمَّا الْيَتِيمَ فَلَا تَقْهَرْ ﴿٩﴾

10. Wala usimkaripie aulizaye.

وَأَمَّا السَّائِلَ فَلَا تَنْهَرْ ﴿١٠﴾

11. Na neema ya Mola wako usimulie (kwa  
kushukuru na kufanya amali njema).

وَأَمَّا بِنِعْمَةِ رَبِّكَ فَحَدِّثْ ﴿١١﴾

**Maelezo juu ya Sura**

Sura hii jina lake limetokana na neno “*Wadh-dhuhaa*”, ambalo ndilo neno na aya ya kwanza. Sura hii ni ya 93 katika Msahafu, ni sura ya Makka na ni sura ya 11 kushuka ikiashiria kuwa ni katika sura za mwanzo mwanzo kumshukia Mtume(s.a.w).

Tunafahamishwa katika Hadithi kuwa wahay ulisitishwa kwa muda mrefu kidogo, kuliko kawaida aliyozoea Mtume(s.a.w), ikafuatiwa na Makafiri wa Kiquraish kudai kusomewa wahayi kwa kejeli, huku wakimdhihakiki kuwa Mola wake atakuwa amemkasirikia. Kibinaadamu, Mtume(s.a.w) naye akakumbwa na wasiwasi kuwa, huenda Mola wake amemkasirikia. Kila akijiuliza amekosea nini hapati jibu. Ndipo Mola wake akamshushia wahay huu wa kumliwaza kuwa hakumkasirikia bali ni katika hekima yake kusitisha wahay ili kumpumzisha.

Tukio hili la kusitishwa wahay lilimtokea Mtume(s.a.w) katika kipindi cha mwanzo cha utume, pale alipokuwa bado hajazoea kuhimili mzigo mkubwa wa wahy. Kwa sababu hiyo kipindi cha mapumziko kilikuwa ni cha lazima kwake. Baadaye, Mtume(s.a.w) alipozoea kubeba mzigo wa wahy hakukuwa tena na ulazima wa kupewa vipindi virefu vya mapumziko.

**Mafunzo**

Maudhui makubwa ya sura hii ni kumliwaza Mtume ili kumuondolea dukuduku na huzuni iliyomsibu kutokana na kusitishwa wahay kwa kipindi kirefu kidogo.

Allah(s.w) amemliwaza Mtume, kwa kumhakikishia kwa kiapo kuwa Mola wake hakumuacha (hakumsusa) wala hakumkasirikia, kisha akampa bishara njema kuwa matatizo aliyokuwa akikabiliiana nayo katika hiyo hatua ya mwanzo ya ujumbe wake hayatadumu kwa muda mrefu; na kila kipindi kijacho kitakuwa bora kwake na kwa Waislamu na Uislamu kuliko kilichopita.

Pia akambashiria kuwa baada ya muda si mrefu atamneemesha vilivyo, kwa kumuwezesha kusimamisha Uislamu, mpaka aridhike. Biashara hii ilipotolewa hapakuwa na dalili kabisa kuwa Mtume(s.a.w) pamoja na Waislamu wachache na dhaifu alikuwa nao kuwa watapata ushindi na kuufanya Uislamu uwe juu ya dini zote za ulimwengu wa wakati ule kwa kipindi cha muda mfupi uliofuatia. Baada ya mkataba wa Hudaybiyya, Mtume(s.a.w) aliwashinda maadui zake wote na Uislamu ukawa juu ya dini zote kama Qur'an inavyothibitisha

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ

كُلِّهِ ۗ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا

“Yeye ndiye aliyemtuma Mtume wake kwa uongofu na Dini ya haki, ili aishindishe juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi” (48:28)

Pamoja na bishara hii Allah(s.w) anazidi kumliwaza Mtume wake kwa kumkumbusha kuwa haiwi Mola wake amkasirikie kwani alimteua kuwa Mtume wake kwa walimwengu wote na kumuandaa tangu utotoni mwake ili aweze kuchukua jukumu hili adhimu na kuweza kulitekeleza ipasavyo. Allah(s.w) amemhakikishia Mtume wake kuwa yuko radhi naye kwa kumkumbusha neema alizomtangulizia hata kabla ya neema hii kubwa ya utume:

*“Je, hatukukuta yatima tukakupa makazi mema ya kukaa? Na tukakukuta hujui kuongoza njia, tukakuongoza kwa kukupa Utume? Na hatukukuta fakiri tukakutajirisha kupitia kwa Bibi Khadija?” Iweze tena hivi leo, ambapo ndio hasa unahitaji msaada zaidi kutoka kwetu ili uweze kufikia lengo lililokusudiwa, ndio tena tukususe na kukukasirikia?”*

Baada ya maliwazo hayo, Allah(s.w) anamfunza Mtume wake namna ya kushukuru neema. Akamuagiza Mtume kuwa awahurumie mayatima kama Mola wake alivyomhurumia na kumpa makazi mazuri, Asiwakaripie wale wanaotaka kuujua Uislamu na kuongoka bali awaangushie bawa la rehema na kuwaongoza kama Mola wake alivyomuongoza. Mwisho, Mtume(s.a.w) anaagizwa na Mola wake kuwa atangaze neema zake alizompa. Kusimulia neema ni kushukuru neema hizo kwa kuzitumia kwa ajili ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu. Neema kubwa aliyopewa Mtume pamoja na Waislamu wote ni Uislamu.

..... الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتَمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ

الْإِسْلَامَ دِينًا ..... ﴿٣﴾

*“..... Leo nimekukamilishieni dini yenu na kukutumizieni neema yangu, na ninakupendeleeni Uislamu uwe Dini yenu.....” (5:3)*

Hivyo kuisimulia neema hii kubwa ni kuishi kiislamu, kufundisha Uislamu na kuusimamisha Uislamu katika jamii. Mtume(s.a.w) na maswahaba zake walitekeleza agizo hili na kuutawalisha Uislamu juu ya mifumo mingine yote ya maisha iliyokuwemo wakati wa zama zao, na Allah(s.w) akawa ni shahidi juu ya hili.

### **Mafunzo kwa Muhtasari**

Pamoja na kuwa sura hii imeelekezwa kwa mtume katika kumliwaza, mafunzo yake yanawahusu Waislamu wote wa zama zote mpaka siku ya mwisho. Kwa muhtasari kutokana na sura hii tunajifunza yafuatayo:

1. Mwenyezi Mungu huapia viumbe vyake, ili hivyo viumbe kwa namna vinavyojulikana viwe ni ushahidi au dalili ya wazi ili kuyakinisha jambo linaloelezwa baada ya kiapo hicho.



2. Hakuna kipindi chochote cha harakati za kuhuisha na kusimamisha Uislamu ambacho Mtume(s.a.w) hakuwa na msaada wa Allah(s.w). Hivyo Waislamu walioko katika harakati hizi za kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii wasikatishwe tamaa na vikwazo mbalimbali vitakavyo wafika, bali wawe na yakini kuwa Mwenyezi Mungu yuko pamoja nao na watashinda.
3. Pamoja na hali duni waliyonayo Waislamu hivi sasa, wakifanya jitihada za kuujua Uislamu, kuutekeleza na kuufundisha kama alivyofanya Mtume(s.a.w) na maswahaba zake katika kipindi kigumu cha Makka, Uislamu utapata nguvu kila muda unavyosogea na hatimaye utafikia kilele cha kutawala katika jamii kama Mtume(s.a.w) alivyoutawalisha.

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَىٰ الدِّينِ

كُلِّمَةً وَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا

*“Yeye ndiye aliyemtuma, (aliyemleta) Mtume wake kwa uwongofu na dini iliyo ya haki, ili aishindishe juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi” (48:28)*

4. Muislamu anatakiwa awe na tabia ya kuwaangalia walio chini yake kihali na mali na asiwaangalie walio juu yake, ili aweze kukinai juu ya neema alizoneemeshwa na Mola wake na kuwahurumia wale walio chini yake. Tabia hii pia itamuwezesha kushukuru neema alizoneemeshwa na Mola wake.
5. Mwenyezi Mungu pekee ndiye mdhibiti wa mafanikio au shida. Huibadili hali moja hadi nyingine wakati wowote apendavyo. Wajibu wetu Waislamu ni kufanya jitihada za kuboresha hali zetu huku tukimuomba Mwenyezi Mungu na kufanya jitihada za makusudi za kusimamisha Dini yake kwa mali zetu na nafasi zetu. Tukifanya hivyo tutafanikiwa kwa ahadi ya Allah(s.w) ifuatayo:

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي

الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي

ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي

*Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale waliokuwako kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia dini yao aliyowapendelea, na atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wawe*

wananiabudu, hawanishirikishi na chochote. Na watakaokufuru baada ya hayo; basi hao ndio wavunja amri zetu. (24:55)

6. Hatunabudi kumshukuru Allah(s.w) kwa kila neema tuipatayo na njia bora ya kushukuru neema ni kuitumia neema hiyo kwa mujibu wa maagizo ya Mwenyezi Mungu na kuzidisha dhikiri na Ibada za ziada kama vile kukithirisha swala za sunnah, visimamo vya usiku, funga za sunnah, kutoa sadaqa, n.k. Neema kubwa tuliyopewa ni kuwa Waislamu. Hivyo, ili tuwe waja wenye shukrani mbele ya Allah(s.w), hatunabudi kuujuu Uislamu vilivyo, kuishi kiislamu na kufanya jitihada za makusudi za kuusimamisha Uislamu katika jamii.

### 3. Suratu - Alam - Nashrah (94)

*Kwa jina la Allah Mwingi wa  
Rehema, Mwenye kurehemu.*

1. Je, hatukukupanulia kifua chako.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

أَلَمْ نَشْرَحْ لَكَ صَدْرَكَ

2. Na tukakuondolea mzigo wako(mzito).

وَوَضَعْنَا عَنْكَ وِزْرَكَ

3. Uliovunja mgongo wako?

الَّذِي أَنْقَضَ ظَهْرَكَ

4. Na tukatukuza utajo wako?

وَرَفَعْنَا لَكَ ذِكْرَكَ

5. Basi kwa hakika baada ya dhiki  
(huja faraja.

فَإِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا

6. Hakika baada ya dhidi huja faraja.

إِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا

7. Basi ukisha maliza (kulingania)  
shughulika kwa Ibada nyingine.

فَإِذَا فَرَغْتَ فَانصَبْ

8. Na jipendekeze kwa Mola wako.

وَإِلَىٰ رَبِّكَ فَأَرْغَبْ

**Maelezo juu ya Sura**

Sura hii imepata jina lake kutokana na neno la kwanza - Alam-Nashrah. Hii ni sura ya 94 katika msahafu na ni ya 12 katika utaratibu wa kushuka. Kwa mujibu wa maelezo ya Ibn Abbas (r.a), sura hii iliteremshwa mara baada ya kuteremshwa Surat Dh-Dhuhaa.


**Mafunzo:**

Lengo na madhumuni ya sura hii pia ni kuuliwaza Mtume(s.a.w). Pamoja na wasiwasi aliokuwa nao Mtume(s.a.w), kuwa labda Mola wake alimkasirikia na kumsusa, kutokana na tukio la kuchelewesha wahyi lililoambatana na kejeli na dhihaka ya maadui zake, Mtume(s.a.w) alikuwa akikabiliana na magumu mengi kuanzia pale alipoanza kulingania ujumbe wa Uislamu kwa watu wote. Mara tu alipoanza kulingania Uislamu, jamii ile ile iliyompa heshima ya pekee, iliyompa jina la Aswadiq Al-Amiin, ilianza kumtukana, kumkejeli, kumdhihaki na kumshutumumu na kumpiga yeye pamoja na wafuasi wake wachache waliomuamini. Hali hii kibinaadamu ilikuwa inakatisha tamaa ya kufikiwa lengo lililokusudiwa la kuifanya Dini ya Allah(s.w) kuwa juu ya dini zote.

Pamoja na kuuliwaza Mtume(s.a.w) katika suratudh-Dhuhaa, katika sura hii, Allah(s.w) ameliwaza mtume wake kwa kukumbusha neema kuu tatu alizomtukia

- (i) Kupanuliwa kifua chake
- (ii) Kuondolewa mzigo mzito uliovunja mgongo wake
- (iii) Kukuzwa utajo wake.

Kupanuliwa kifua hapa inaashiria Mtume(s.a.w) kupewa uoni wa utume wa kuangalia maslahi ya jamii, hata kabla ya kupewa utume rasmi. Kifua chake kilizidi kupanuka pale alipopewa utume na kufundishwa Uislamu na Mola wake.

 ..... فَمَنْ يُرِدِ اللَّهُ أَنْ يَهْدِيَهُ يَشْرَحْ صَدْرَهُ لِلْإِسْلَامِ

*“Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumuongoza humfungulia kifua chake Uislamu .....” (6:125)*

Mzigo mzito alioubeba Mtume(s.a.w) ni ile hali ya kuona watu wakifanya maovu na kudhulumu haki za wengine na akawa hana uwezo wa kuzuia uovu huo. Baada ya kushindwa kubeba mzigo huo aliamia pangoni Hira katika mlima Nuur, ndipo Allah(s.w) akamuondolea mzigo huo kwa kumfanya Mtume wa kulingania Uislamu na kuusimamisha katika jamii. Utatuzi wa matatizo yote ya jamii ni Uislamu.

Pamoja na kwamba, Muhammad(s.a.w) alitajwa kwa sifa nzuri na watu wa jamii yake kabla ya utume, walimuita Aswadiq Al-Amiin, utajo wake ulivuma kwa ulimwengu mzima wa wakati ule mpaka hivi sasa. Haikamiliki shahada mpaka atajwe Mtume na imekuwa ni amri ya Allah(s.w) kwa waumini kumtakia Mtume Rehema na Amani mara kwa mara (katika kila swala) na kila atajwapo.

إِنَّ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا  
عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴿٥٦﴾

*“Hakika Mwenyezi Mungu anamteremshia rehema Mtume; na Malaika Wake (wanaomuomba dua) Basi; enyi mlioamini msalieni (muombeeni rehema) na amani” (33:56)*

Pia Mtume(s.a.w) pamoja na Waislamu aliokuwa nao, waliliwazwa na Mola wao mlezi kuwa pamoja na dhiki waliokuwa nayo, faraja itafuatia si muda mrefu. Hivyo waendeleo kutekeleza wajibu wao na kusubiri. Baada ya bishara hii njema historia inashuhudia kukua kwa nguvu ya Uislamu wakati wa Mtume(s.a.w) na kuwa juu ya mifumo mingine yote ya maisha iliyokuwepo kwa kipindi kifupi cha miaka 23 tu.

Mwisho, baada ya kukumbushwa neema na kubashiriwa ushindi, Mtume(s.a.w) anaagizwa na kwa hiyo Waislamu wote, kuwa baada ya kutekeleza wajibu wake wa kulingania Uislamu, ajikurubishe kwa Mwenyezi Mungu kwa kuleta adhkari nyingi na kuzidisha Ibada za ziada (nafilah) na visimamo vya usiku.

وَمِنَ اللَّيْلِ فَتَهَجَّدْ بِهِ نَافِلَةً لَّكَ عَسَىٰ أَنْ يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُودًا ﴿٧٩﴾

*“Na katika usiku jiondoshee usingizi kwa (kusoma) hiyo (Qur'an ndani ya swala) Hiyo ni (Ibada) ya ziada kwako. Huendea mola wako akakuinua cheo kinachosifika” (17:79)*

Katika kutekeleza agizo hili, Mtume(s.a.w) katika maisha yake yote alikuwa akimkumbuka Allah(s.w) kila wakati katika kila jambo alilolifanya hata alipokuwa akiingia na kutoka chooni. Alikuwa akisimama usiku kwa swala, kwa kitambo kirefu mpaka miguu yake ikawa inavimba na alikuwa akisujudu kirefu katika swala ya usiku, mpaka siku moja mkewe Aysha (r.a) akamdhania kuwa amekufa.

### **Mafunzo kwa Muhtasari**

Pamoja na kuwa sura hii imemlenga Mtume(s.a.w) moja kwa moja, bado mafunzo yake ni kwa ajili ya Waislamu wote wa nyakati zote. Kwa muhtasari kutokana na sura hii tunajifunza yafuatayo:

1. Hatunabudi kushukuru neema mbalimbali alizoturuzuku Allah (s.w) kwa kujizatiti kuifundisha na kuisimamisha Dini yake katika jamii.
2. Yeyote yule atakayedhamiria kuujuu Uislamu kwa usahihi na kuingiza katika utendaji katika kuendesha maisha yake ya kila siku, uoni wake wa maisha na wa masuala ya jamii utakuwa ni wa juu kuliko ule wa watu wengine. Dhima kuu ya muumini ni kusimamisha Uislamu katika jamii na kupata radhi za Mwenyezi Mungu zitakazompelekea kuingizwa peponi katika maisha ya akhera.
3. Muumini wa kweli anawajibu wa kuondoa maovu na dhuluma katika jamii na kusimamisha wema, haki na uadilifu. Wajibu huu waumini wataweza kuutekeleza pale tu watakapoufahamu Uislamu vilivyo, kisha wakaufundisha na kuusimamisha katika jamii kama alivyofanya Mtume(s.a.w) baada ya kupewa mwongozo.
4. Kwa mtazamo wa Uislamu, mwenye kuheshimika mbele ya Allah(s.w) si yule mwenye hadhi kubwa katika jamii kicheo au kimali; bali yule aliyemstari wa mbele katika kuufuata Uislamu na kuusimamisha katika jamii.

..... إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتَقَنُّكُمْ ..... ﴿١٣﴾

“...Hakika ahishimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye Mwenyezi Mungu zaidi katika nyinyi (49:13)

5. Wakati wowote Waislamu watakapojitahidi kuufahamu Uislamu vilivyo, kuutekeleza na kuusimamisha katika jamii, na wakasubiri juu ya magumu yanayowafika, Allah(s.w) atawafanyia wepesi kwa kila hatua wanayopiga kusonga mbele na hatimaye atawawezesha kusimamisha Uislamu katika jamii kama alivyomuwezesha Mtume(s.a.w) na maswahaba zake. Ahadi hii iko wazi katika Qur'an.

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي  
 الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي  
 ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي  
 شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿١٤﴾

“Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa Atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale waliokuwako kabla yao, na kwa yakini Atawasimamishia dini yao aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wawe wananiabudu, hawanishirikishi na chochote. Na watakaokufuru baada ya

*hayo; basi hao ndio wavunjao amri zetu. (24:55)*

6. Hakuna wakati wa kupoteza kwa muislamu. Kama muislamu hana la maana la kufanya amkumbuke Mwenyezi Mungu kwa kuleta adhkari mbalimbali. Aidha Waislamu wanaoharaka kusimamisha Uislamu katika jamii, wanahimizwa kujipendekeza kwa Allah(s.w) kwa kuzidisha adhkari, lbada za nyongeza (nawaafil) kama vile kuzidisha swala na funga za sunnah na kuzidisha na kurefusha visimamo vya usiku. Hizi ni nyenzo muhimu mno za kumuimarisha muislamu katika kazi hii aziz ya kusimamisha Uislamu katika jamii.

### Zoezi 3:3

1. Hifadhi kifuani Suratudh-Dhuhaa na Alam Nashrah na tafsiri.
2. Suratudh-Dhuhaa na Alam Nashrah zimeshushwa kumliwaza Mtume(s.a.w) na wale walioamini pamoja naye.
  - (a) Nini kisa na mkasa uliopelekea Mtume(s.a.w)aliwazwe na Mola wake?
  - (b) Ainisha maliwazo yaliyotolewa na sura hizi.
  - (c) Baada ya maliwazo Mtume(s.a.w) (na kwa hiyo waumini wote) alipewa majukumu ya kutekekeza. Ainisha majukumu hayo.
3. Toa mafunzo makuu matano (5) yatokanayo na
  - (a) Suratudh-Dhuhaa
  - (b) Surat Alam Nashrah.

## 4. Suratut - Tyn (95)

*Kwa jina la Allah Mwingi wa  
Rehma, Mwenye kurehemu.*

1.Naapa kwa Tini na Zaituni

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَالْتَيْنِ وَالزَّيْتُونَ ﴿١﴾

2.Na kwa mlima Sinai.

وَطُورِ سَيْنِينَ ﴿٢﴾

3.Na kwa mji huu (wa Makka)  
wenye amani.

وَهَذَا الْبَلَدِ الْأَمِينِ ﴿٣﴾

4. Bila ya shaka tumemuumba mwanaadamu  
kwa umbo lililo bora kabisa.

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ  
فِي أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ ﴿١٩٦﴾

5. Kisha tukamrudisha kuwa chini kuliko  
walio chini.

ثُمَّ رَدَدْنَاهُ أَسْفَلَ سَافِلِينَ ﴿١٩٧﴾

6. Ila wale wenye kuamini na kutenda mema,  
watakuwa na ujira usiokwisha  
(unaoendelea maisha).

إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا  
الصَّالِحَاتِ فَلَهُمْ أَجْرٌ  
غَيْرٌ مَّمْنُونٍ ﴿١٩٨﴾

7. Basi ukishamaliza (kulingania)  
shughulika (kwa ibada).

فَمَا يُكَذِّبُكَ بَعْدُ بِالذِّينِ ﴿١٩٩﴾

8. Na jipendekeze kwa Mola wako.

أَلَيْسَ اللَّهُ بِأَحْكَمِ الْحَاكِمِينَ ﴿٢٠٠﴾

### Maelezo juu ya Sura

Sura hii imepata jina lake kutokana na neno Wat-tyan ambalo ndilo neno lake la kwanza. Sura hii imeteremshwa Makka katika siku za mwanzo mwanzo za utume wa Muhammad(s.a.w). Ni sura ya 27 kuteremshwa na ni ya 95 katika Msahafu.

### Mafunzo

Sura hii imeanza kwa viapo katika aya ya kwanza hadi ya tatu. Katika viapo hivi Allah(s.w) anaapia mazingira ambamo wametokea Mitume wa Allah(s.w). Anaapia mimea ya Mitini na Mizaytuni inayostawi katika eneo la mashariki ya kati, katika makazi ya Mitume wengi wa Allah(s.w). Pia ameapia Mlima wa Sinai, sehemu ambayo Nabii Mussa (a.s) alikuwa akizungumza na Allah(s.w) nyuma ya pazia wakati akipokea wahay. Kisha ameapia mji wa Makkah, kituo ambacho Mtume(s.a.w) alianza kuuhiisha Uislamu. Kama kawaida ya viapo vya Allah(s.w), viapo hivi vimeletwa ili kumvuta msomaji atafakari juu ya ukweli unaobainishwa katika aya tatu zinazofuatia.

Kuhusu umbile la binaadamu, ni kweli kuwa binaadamu wenyewe hawajawa na hoja ya kuonesha kuwa kuna kiumbe mwingine wanaye mfahamu kwa dhahiri yake, mwenye sura na umbo lililo bora kuliko la binaadamu. Pia Allah(s.w) anamtanabahisha binaadamu juu ya umbile lake katika aya zifuatazo:

يَتَأْتِيهَا الْإِنْسَانُ مَا عَمَرَكَ بِرَبِّكَ الْكَرِيمِ ﴿٦٨﴾ الَّذِي خَلَقَكَ فَسَوَّاكَ  
فَعَدَلَكَ ﴿٦٩﴾ فِي أَيِّ صُورَةٍ مَّا شَاءَ رَكَّبَكَ ﴿٧٠﴾

*“Ewe mwanaadamu! Nini kikudanganyacho na Mola wako mtukufu (hata ukamkanusha)? Aliyekuumba na akakutengeneza, kisha akakulinganisha sawa sawa, katika sura yoyote aliyoipenda amekutengeneza” (82:6-8)*

Binaadamu pamoja na kutengenezwa katika sura na umbo zuri ametunukiwa pia na Mola wake vipawa vikubwa vinayomuwezesha kuwa bora kuliko viumbe vyote. Vipawa hivi ni vinne vifuatavyo:

- (i)Akili na ufahamu wa hali ya juu unaomuwezesha kufikiri na kutafakari.
- (ii)Utambuzi binafsi (self consciousness) unaomuwezesha kuunganisha, kuchambua na kuhusisha kila kitu au kila jambo na kuliweka mahali pake.
- (iii)Elimu ambayo humuwezesha kutenda kwa ufanisi.
- (iv)Uhuria - anao uwezo wa kufanya mema akitaka na ana uwezo wa kufanya maovu akitaka.

Pamoja na vipawa hivi pia binaadamu ametukuzwa na kukirimiwa na Mola wake neema mbalimbali kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

﴿ وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ وَحَمَلْنَاهُمْ فِي الْوَجْرِ وَالْبَحْرِ وَرَزَقْنَاهُمْ مِنْ  
الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَى كَثِيرٍ مِّمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيلًا ﴾ ﴿٧١﴾

*“Na hakika tumewatukuzwa binaadamu na tumewapa vya kupanda barani na baharini na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri na tumewatukuzwa kuliko wengi katika wale tuliowaumba, kwa utukufu ulio mkubwa (kabisa)” (17:70)*

Binaadam akiwa na busara na kuamua kutumia uhuru wake vizuri kwa kutumia vipawa na neema mbalimbali alizotunukiwa na Mola wake kwa kumtambua vilivyo na kumuabudu ipasavyo, huzidi



ubora wake kwa kustahiki cheo cha Ukhalifa wa Allah(s.w) hapa ulimwenguni cheo kilicho kitukufu na bora kuliko kile cha malaika mbele ya Allah(s.w) - Rejea Qur'an (2:30-34). Kwa kusimamisha ukhalifa katika ardhi, haki na uadilifu vitasimama na kustawisha furaha na amani ya kweli katika jamii.

Binaadamu akiwa mjinga na kuamua kutumia uhuru wake vibaya kwa kuamua kutumia vipawa na neema alizotunukiwa na Mola wake kwa kumkufuru na kumuasi, atashuka cheo na kudhalilika kuliko wanyama kama tunavyokumbushwa katika aya zifuatazo:

وَلَقَدْ ذَرَأْنَا لِجَهَنَّمَ كَثِيرًا مِّنَ الْجِنِّ وَالْإِنسِ ۗ لَهُمْ قُلُوبٌ لَّا يَفْقَهُونَ بِهَا ۖ وَهُمْ أَعْيُنٌ لَّا يُبْصِرُونَ بِهَا ۖ وَهُمْ ءَاذَانٌ لَّا يَسْمَعُونَ بِهَا ۗ أُولَٰئِكَ كَالْأَنْعَامِ بَلَّٰهُمْ أَضْلُ ۗ أُولَٰئِكَ هُمُ الْغَافِلُونَ ﴿١٧٩﴾

“Na bila shaka tumewaumbia moto wa Jahannamu wengi katika majini na wanaadamu (kwa sababu hii): Nyoyo wanazo, lakini hawafahamu kwazo (Hawataki kufahamu kwazo), na macho wanayo, lakini hawaoni kwayo, na masikio wanayo, lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama wanyama; bali wao ni wapotofu (wapotevu) zaidi. Hao ndio walioghafilika (7:179).

﴿١٧٩﴾ إِنَّ شَرَّ الدَّوَابِّ عِنْدَ اللَّهِ الصُّمُّ الْبُكْمُ الَّذِينَ لَا يَعْقِلُونَ ﴿١٨٠﴾

“Hakika vinyama viovu mbele ya Mwenyezi Mungu ni hawa wanaojipa uziwi (wa kutosikia haki), wanaojipa ububu (wasikiri hiyo haki), ambao hawayatii akilini (wanayoambiwa, bali wanayakataa tu vivi hivi bila ya kuyapima kwanza)” (8:22)

Binaadamu anapoamua kumkufuru na kumuasi Mola wake, hufanya uharibu mkubwa katika ardhi kuliko ule unaofanywa na wanyama waharibifu. Kwa mfano matatizo makubwa na majanga makubwa yanayokabili ulimwengu hivi leo kama vile maradhi mabaya ya Ukimwi, mauaji ya halaiki, utapia mlo, umaskini na ujinga kwa nchi zinazoitwa za dunia ya tatu, na kadhalika ni matokeo ya ukafiri na uasi wa binaadamu dhidi ya Mola wake.

Maswali yaliyoulizwa kwenye aya ya saba na ya nane yanatutaka tutafakari juu ya ukweli huu kuwa: “Wanaweza kuwa sawa katika malipo wale waliosimamisha uadilifu katika jamii na kuwawezesha watu kuishi kwa furaha na amani na wale waliofanya fisadi katika jamii na

kuwadhaliisha watu kwa kuwakhofisha na kuwadhulumu? “Kwa kipimo cha kibinaadamu na kiuadilifu, mwema na muovu hawawezi kulipwa sawa. Mtu mwena anastahiki kupongezwa na kuzawadiwa na mtu muovu anastahiki kulaumiwa na kuadhibiwa. Pia rejea Qur'an (32:18,59:20)

Je, ikitokea muovu akawa mbabe asiyewezekana kuadhibiwa na yoyote, kama George W. Bush na serikali yake alivyoivamia Afghanistan na Iraq kwa dhuluma, au ikitokea mtu mwema muadilifu aliyejizatiti kuleta amani na furaha ya kweli katika jamii, akawa badala ya kupongezwa na kuzawadiwa akaitwa gaidi na kupigwa vita kama alivyoitwa Mohammed Mullah na serikali yake ya Talaban (Afghanistan), itakuwa ni uadilifu mambo yaishie hapo? Akili ya binaadamu haikubaliani na hili. Bali, kiuadilifu ni lazima pawe na maisha mengine baada ya haya (maisha ya akhera) ambapo kila mtu aliyefanya wema hapa duniani atapongezwa na kuzawadiwa ipasavyo na kila aliyefanya uovu hapa duniani ataadhibiwa ipasavyo. Atakayesimamia hukumu hii ni Allah(s.w) ambaye ni hakimu muadilifu kuliko mahakimu wote.

### *Mafunzo kwa Muhtasari*

1. Allah(s.w) ameapia mazingira walimotokea mitume wake mbalimbali, ili kwa kuzingatia ujumbe wa mitume hao, iwe ni chachu kwa msomaji kutafakari juu ya ujumbe unaofuatia.
2. Ubora wa binaadamu hupatikana kutokana na imani sahihi iliyoambatana na vitendo vizuri.
3. Mwanaadamu akiamua kufuata maisha ya kumkufuru na kumuasi Mola wake, huwa muharibifu katika jamii kuliko wanyama waharibifu.
4. Malipo ya kumuamini Allah(s.w) na kufuata mwongozo wake hapa duniani ni kuishi kwa furaha na amani (maisha ya nuru)
5. Malipo ya kumkufuru na kumuasi Allah(s.w) na kufuata miongozo iliyo dhidi na uongozi wake hapa duniani ni kuishi maisha ya khofu na dhuluma (maisha ya giza)
6. Lazima iwepo siku ya mwisho ili waumini waliotenda vitendo vizuri na makafiri waliofisidi katika ardhi walipwe kwa uadilifu jaza ya vitendo yao.

### **Zoezi 3:4**

1. Hifadhi kifuani Suratut-Tyn na tafsiri yake.
2. “Bila shaka tumemuumba binaadamu kwa umbo lililo bora kabisa. Kisha tumemrudisha kuwa chini kuliko walio chini” (95:4-5).

- (a) Onesha ubora wa binaadamu ukilinganisha na viumbe wote waliomzunguka.
  - (b) Kiutendaji onesha ni vipi binaadamu atabakia na ubora wake.
  - (c) Ni kwa vipi binaadamu pamoja na kuumbwa kwa umbo bora, hushuka na kuwa chini kuliko vyote vilivyo chini.
3. Ainisha mafunzo matano (5) yatokanayo na Suratut-Tyn.



*Sura ya Nne***SUNNAH NA HADITH****Hadith zilizochaguliwa**

Katika kitabu cha nne cha Elimu ya Dini ya Kiislamu shule za Sekondari zimechaguliwa Hadith 10 kutokana na maudhui yafuatayo:

- Kumtangliza mwenzio na kufarijiana
- Uharamu wa kibri na majivuno
- Tabia njema
- Upole, uangalifu na utulivu
- Kutoa salaam.

Zimechaguliwa Hadith mbili kwa kila maudhui.

**KUMTANGULIZA MWENZIO NA KUFARIJIANA**

Kuwapendelea watu katika kuwafanyia wema ni katika amali njema itakayompelekea mja kufuzu na kustahiki malipo mema peponi kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

*“Hakika watu wazuri watakunywa kinywaji kilichochanganyika na kafuri. (Hiyo kafuri) ni mto watakaounywa waja wa Mwenyezi Mungu; watautiririsha mtiririsho (mzuri namna watakavyo). (Watu hao ni hawa) wanaotimiza wajibu (wao) na wanaoiogopa siku ambayo shari yake inaenea (sana). Na huwalisha chakula maskini na mayatima na wafungwa, na hali ya kuwa wenyewe wanakipenda (chakula hicho). (Husema wenyewe katika nyoyo zao wanapowapa chakula hicho): “Tunakulisheni kwa ajili ya kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu (tu) hatutaki kwenu malipo wala shukrani. “Hakika sisi tunaogopa kwa Mola wetu iyo siku yenye shida na taabu.” Basi Mwenyezi Mungu atawalinda na shari ya siku hiyo na kuwakutanisha na neema na furaha. Na Atawajazi Mabustani (ya Peponi) na maguo ya Hariri, kwa sababu ya kusubiri (kwao). Humo wataegemea viti vya enzi, hawataona humo jua (kali) wala baridi (kali)” (76:5-13).*

Kuhusu ukarimu wa Ansvari kwa Muhajiriina Qur'an inatufahamisha:

“Na (pia wapewe) wale waliofanya maskani yao hapa (yaani Madina) na wakautakasa Uislamu (wao barabara) kabla ya (kuja) hao (Muhajiri huko Madina) na wakawapenda hao waliohamia kwao, wala hawapati, hawaoni dhiki nyoyoni mwao kwa hayo waliyopewa (hao Muhajiri), na wanawapendelea kuliko nafsi zao ingawa wenyewe wana hali ndogo. Na waepushwao na ubakhili wa nafsi zao hao ndio wenye kufaulu kweli kweli” (59:9).

### Hadith 1:

وَعَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ: ﴿طَعَامُ الْاِثْنَيْنِ كَافِي الْثَلَاثَةِ، وَطَعَامُ الثَّلَاثَةِ كَافِي الْارْبَعَةِ﴾. مَتَّفَقٌ عَلَيْهِ.

Abuu Hurairah (r.a) amesema: Mtume(s.a.w) amesema: “Chakula cha watu wawili huwatosheleza watatu na cha kula cha watatu huwatosheleza wane.” (Bukhaary na Muslim).

### Hadith 2:

وعن أبي سعيد الخدري رضي الله عنه قال: بَيْنَمَا نَحْنُ فِي سَفَرٍ مَعَ النَّبِيِّ ﷺ إِذْ جَاءَ رَجُلٌ عَلَى رَاحِلَةٍ لَهُ، فَجَعَلَ يَصْرِفُ بَصْرَهُ يَمِينًا وَشِمَالًا، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ: ﴿مَنْ كَانَ مَعَهُ فَضْلٌ ظَهَرَ فَلْيَعْتِدْ بِهِ عَلَى مَنْ لَا ظَهَرَ لَهُ، وَمَنْ كَانَ لَهُ فَضْلٌ مِنْ زَادٍ، فَلْيَعْتِدْ بِهِ عَلَى مَنْ لَا زَادَ لَهُ﴾. فَذَكَرَ مِنْ أَصْنَافِ الْمَالِ مَا ذَكَرَ حَتَّى رَأَيْنَا أَنَّهُ لَا حَقَّ لِأَحَدٍ مِنَّا فِي فَضْلٍ. رَوَاهُ مُسْلِمٌ.

Abuu Sa'iid Al-Khudry(r.a) amesimulia: “Tulipokuwa safarini pamoja na Mtume(s.a.), mara akaja mtu aliyepanda mnyama wake, akawa anatazama kulia na kushoto. Mtume(s.a.w) akasema: “Mwenye mnyama wa ziada ampe sadaqa asiye na mnyama, na mwenye akiba ya ziada, ampe asiye na akiba”. Akataja aina kadhaa za mali kiasi alichotaja mpaka tukadhani kuwa hakuna haki kwa yeyote miongoni mwetu kubaki na ziada ya kitu”. (Muslim).

### Mafunzo ya Hadith

Kwa ujumla Hadith hizi zinatupatia mafunzo yafuatayo:

1. Muislamu wa kweli ni yule aliyejiepusha na uchoyo na ubakhili. Allah(s.w) anasisitiza katika Qur'an:

“...Na waepushwao na ubakhili wa nafsi zao hao ndio wenye kufaulu kweli kweli” (59:9).

2. Ili kuepukana na ubakhili; muislamu hanabudi kumpendelea ndugu yake apate kile anacho ipendelea nafsi yake.
3. Muislamu anatakiwa atoe sadaqa kutokana na kile kilicho ziada ya matumizi yake ya kawaida. Kwa mujibu wa Hadith nyingine ya Mtume(s.a.w): “Si katika Waislamu yule ambaye anakula na kusaza hali jirani yake amelala njaa”.

## UHARAMU WA KIBRI NA MAJIVUNO

Allah(s.w) anakemea suala la kibri na majivuno katika chungu ya aya. Hebu turejee aya chake zifuatazo:

“Wala usitembee (usende) katika ardhi kwa maringo. Hakika wewe huwezi kuipasua ardhi wala huwezi kufikia urefu wa milima. (Basi unajivuna nini)? Haya yote ubaya wake ni wenye kuchukiza mbele ya Mola wako.” (17:37-38).

“Hakika Qaruni alikuwa katika watu wa Musa, lakini aliwafanyia dhulma. Na Tulimpa hazina ambazo funguo zake zinawatopeza watu wenye nguvu (kuzichukua). Walimwambia watu wake: “Usijione (usijigambe); hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wanaojiona” (28:76).

“Wala usiwatazame (usiwafanyie watu jeuri), kwa upande mmoja wa uso, wala usende katika nchi kwa maringo; hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila ajivunaye, ajifaharishaye” (31:18).

Pia waovu wa kibri na majivuno unadhihirika katika Hadith zifuatazo:

### Hadith 3:

وعن عبد الله بن مسعود رضي الله عنه عَنِ النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم قَالَ: ﴿لَا يَدْخُلُ الْجَنَّةَ مَنْ كَانَ فِي قَلْبِهِ مِثْقَالُ ذَرَّةٍ مِنْ كِبْرٍ﴾ فَقَالَ رَجُلٌ: إِنَّ الرَّجُلَ يُحِبُّ أَنْ يَكُونَ ثَوْبُهُ حَسَنًا، وَنَعْلُهُ حَسَنَةً؟ قَالَ: ﴿إِنَّ اللَّهَ جَمِيلٌ يُحِبُّ الْجَمَالَ، الْكِبْرُ: بَطْرُ الْحَقِّ وَعَمَطُ النَّاسِ﴾.  
رَوَاهُ مُسْلِمٌ.

'Abdullah bin Mas'ud(r.a) amesimulia: Mtume(s.a.w) amesema: "Hataingia Peponi ambaye moyoni mwake muna kiburi uzito wa mdudu chungu". Mtu mmoja akauliza; "Mtu hupenda nguo yake iwe nzuri na viatu vyake viwe vizuri (itakuwaje)?" Akasema: "Hakika Allah ni Mzuri Yuwapenda uzuri. Kiburi ni kukataa haki na kudharau watu". (Muslim).

## Hadith 4:

وَعَنْهُ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ ﷺ قَالَ: ﴿بَيْنَمَا رَجُلٌ يَمْشِي فِي حُلَّةٍ تُعْجِبُهُ نَفْسُهُ، مُرَجِّلٌ رَأْسَهُ، يَجْتَالُ فِي مَشِيَّتِهِ، إِذْ حَسَفَ اللَّهُ بِهِ، فَهُوَ يَتَجَلَّجَلُ فِي الْأَرْضِ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ﴾. متفق عليه.

Abuu Huraira(r.a) amesimulia: "Mtume(s.a.w) amesimulia: "Mtu mmoja alipokuwa anatembea akiwa amevaa mavazi yaliyomfanya ajivune moyoni mwake, akiwa amechana nywele zake, anafanya kibri katika mwenendo wake, kwa ghafla Allah(s.w) akamdidimiza. Mtu huyo (hivi sasa) anaendelea kuzama katika ardhi hadi siku ya Qiyama". (Bukhaary na Muslim).

### Mafunzo ya Hadith

Kutokana na Hadith hizi mbili tunajifunza yafuatayo:

1. Kiburi ni kukataa haki na kuwadharau watu.
2. Kujivuna ni mtu kujisikia kuwa yeye ni zaidi au bora kuliko wengine.
3. Kiburi na majivuno ni tabia inayopelekea kuwadhalilisha, kuwanyanyasa na kuwadhulumu watu haki zao.
4. Mwishio wa mtu mwenye kibri na majivuno ni mbaya katika maisha ya dunia na katika kahera kuna adhabu kali inayomngoja,

## TABIA NJEMA

Mfano wa kuigwa kwa tabia njema ni Mtume Muhammad(s.a.w):

"Na bila shaka (ewe Muhammad) Unatabia njema kabisa" (68:4).

Mwenyewe Mtume(s.a.w) katika kusisitiza waumini kujipamba na tabia njema anasikika akisema katika Hadith zifuatazo:

**Hadith 5:**

وعن عبد الله بن عمرو بن العاص رضي الله عنهما، قَالَ: لَمْ يَكُن  
 رَسُولُ اللَّهِ ﷺ فَاحِشًا وَلَا مُتَفَحِّشًا، وَكَانَ يَقُولُ: ﴿إِنَّ مِنْ خِيَارِكُمْ أَحْسَنَكُمْ  
 أَخْلَاقًا﴾. متفقٌ عَلَيْهِ.

'Abdullah bin 'Amri bin Al-'as(r.a) amesema: Mtume(s.a.w) hakuwa na tabia mbaya wala hakuna mwenye kufanya mambo machafu. Alikuwa akisema (Mtume(s.a.w)): "Hakika katika wabora wenu ni wenye tabia njema". (Bukhaary na Muslim).

**Hadith 6:**

وعن جابر رضي الله عنه أن رسول الله ﷺ قَالَ: ﴿إِنَّ مِنْ أَحَبِّكُمْ إِلَيَّ، وَأَقْرَبِكُمْ مِنِّي  
 بَجَلْسَاءِ يَوْمِ الْقِيَامَةِ، أَحْسَنَكُمْ أَخْلَاقًا، وَإِنْ أَبْغَضْتُكُمْ إِلَيَّ وَأَبْعَدْتُكُمْ مِنِّي يَوْمَ الْقِيَامَةِ،  
 النَّزَّارُونَ وَالْمُتَشَدِّقُونَ وَالْمُتَفَيِّهُونَ﴾ قالوا: يَا رَسُولَ اللَّهِ، قَدْ عَلِمْنَا ﴿النَّزَّارُونَ  
 وَالْمُتَشَدِّقُونَ﴾، فَمَا الْمُتَفَيِّهُونَ؟ قَالَ: ﴿الْمُتَكَبِّرُونَ﴾. رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ، وَقَالَ:  
 حَدِيثٌ حَسَنٌ.

Jabir(r.a) amesimulia: Mtume(s.a.w) amesema: "Hakika wanaopendeza mno kwangu na watakaokuwa karibu mno nami kwa maskani siku ya Qiyama, ni wale wenye tabia njema. Na hakika wanaochukiza mno kwangu na watakaokuwa mbali nami siku ya Qiyama ni wale wenye porojo, wanaojigamba na "mutafaihiqun" Swahaba wakauliza: Yaa Rasuulallah, tumewajua wenye porojo na wanaojigamba, mutafaihiqun ni watu gani?" Akajibu: ni wenye kiburi" (Tirmidh, na amesema Hadith hii ni Hasan).

**Mafunzo ya Hadith**

Kutokana na Hadith hizi mbili tunajifunza yafuatayo:

Tabia njema ni kutenda na kuwafanyia watu mambo mema yanayopendeza watu yaliyo katika vigezo vya Qur'an na Sunnah na kujiepusha na kufanya au kuwafanyia watu mambo maovu na machafu yanayowachukiza watu pia kwa kigezo cha Qur'an na Sunnah.



Mtume(s.a.w) ndiye kiigizo chetu kikuu cha tabia njema:

*“Anas(r.a) ameeleza: “Mtume(s.a.w) alikuwa mwenye tabia nzuri kuliko watu wote”. (Bukhaary na Muslim).*

Mtu mwenye tabia njema hupendeka kwa Allah(s.w), kwa Mtume(s.a.w) na kwa watu wenye utu.

## **UPOLE, UANGALIFU NA UTULIVU**

Upole, uangalifu na utulivu ni miongoni mwa vipengele vya tabia njema. Mtu mpole ni yule anayejizuia kughadhibika na aliye mwepesi kusamehe. Allah(s.w) anatuhimiza tujipambe na tabia ya upole kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

*“Na yaendeeni upesi upesi maghufira ya Mola wenu na Pepo (Yake) ambayo upana wake (tu) ni (sawa na) mbingu na ardhi. (Pepo) iliyowekewa wamchao Mungu”. “Ambao hutoa katika (hali ya) wasaa na katika (hali ya dhiki), na wazuiyao ghadhabu na wanaosamehe watu (na wawafanyiao ihsani); na Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao ihsani” (3:133-134).*

*“Shikamana na kusamehe na amrisha mema na jitenge na majahili” (7:199).*

*“Mambo mazuri na mabaya hayawi sawa. Ondosha (ubaya unaofanyiwa kwa mema); tahamaki yule ambaye baina yako na baina yake kuna uadui atakuwa kama ni jamaa (yako) mwenye kukufia chungu.” “Lakini (jambo hili) hawatapewa ila wale wanaosubiri, wala hawatapewa ila wenye hadhi kubwa (kwa Mwenyezi Mungu)” (41:34-35).*

*“Na anayesubiri na kusamehe (atalipwa wema wake). Bila shaka hilo ni katika mambo makubwa ya kuazimiwa kufanywa (na kila muislamu)” (42:43).*

Mtume(s.a.w) naye amehimiza upole kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

### **Hadith 7:**

وَعنها أَنَّ النَّبِيَّ ﷺ قَالَ: ﴿إِنَّ اللَّهَ رَفِيقٌ يُحِبُّ الرَّفْقَ، وَيُعْطِي عَلَى الرَّفْقِ، مَا لَا يُعْطِي عَلَى الْعَنْفِ، وَمَا لَا يُعْطِي عَلَى مَا سِوَاهُ﴾. رَوَاهُ مُسْلِمٌ.

*‘Aisha(r.a) ameeleza kuwa Mtume(s.a.w) amesema: “Hakika Allah ni Mpole, Anawapenda wapole na Hutoa ujira Asioutoa kwa jambo lingine lolote wala hatoi juu ya ukali”. (Muslim).*

**Hadith 8:**

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رضي الله عنه قَالَ: بَالَ أَغْرَابِيٌّ فِي الْمَسْجِدِ، فَقَامَ النَّاسُ إِلَيْهِ لِيَقْعُوا فِيهِ، فَقَالَ النَّبِيُّ ﷺ: «دَعُوهُ وَارْبِقُوا عَلَى بَوْلِهِ سَجْلًا مِنْ مَاءٍ، أَوْ ذَنْبِيًا مِنْ مَاءٍ، فَأَتَمَّا بَعِثْتُمْ مُبْسِرِينَ وَلَمْ تُبْعَثُوا مُعَسِّرِينَ». رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ.

*Abuu Huraira(r.a) amesimulia: “Mbedui mmoja alikojoa msikitini, waut wakataka kwenda kumkaripia. Mtume(s.a.w) akawaambia: “Mwacheni na mmimine ndoo ya maji juu ya mkojo wake. Hakika mmeletwa muwe ni wenye kusahilisha wala hamkuletwa kuweka mikazo”. (Bukhaary).*

**Mafunzo ya Hadith**

Kutokana na Hadith hizi mbili tunajifunza yafuatayo:

1. Upole ni kipengele cha tabia njema kinachopendeza sana mbele ya Allah(s.w) kama Hadith nyingine zifuatazo zinavyosisitiza:

*‘Abdullah bin Abbaas(r.a) amesema: “Mtume(s.a.w) alimwambia Ashajji bin ‘Abdilqais: Hakika wewe una mambo mawili Anayoyapenda Allah; **upole na uangalifu**” (Muslim).*

Pia:

*“Aisha(r.a) amesema: Mtume(s.a.w) amesema: Hakika Allah ni mpole (kwa waja wake, Anapenda upole katika mambo yote”. (Bukhaary na Muslim).*

2. Upole ni kinga ya adhabu ya moto kwa muumini kama tunavyojifunza katika Hadith nyingine:

*‘Abdullaah bin Mas’uud(r.a) amesema: Mtume(s.a.w) amesema: “Je, niwaeleze mtu ambaye ni haramu kuingia motoni? Ni haramu kuingia motoni kila aliye karibu zaidi na watu, mpole, mlaini na sahali”. (Tirmidhy).*

3. Mtu aliyeruzukiwa upole ameruzukiwa kheri kubwa kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*“Jabir bin ‘Abdullaah(r.a) amesema: “Nilimsikia Mtume(s.a.w) akisema: “Atakaye nyimwa upole, ameshanyimwa kheri yote”. (Muslim).*

4. Waislamu wanatakiwa wasahalisha mambo (wayafanye yawe mepesi) wala wasiyafanywe kuwa mazito (magumu kutekelezeka) kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Anas(r.a) amesimulia: Mtume(s.a.w) amesema: “Sahihilisheni wala msifanyee uzito, wapendekezeni watu kheri na muwabashirie wala msiwakimbize”. (Muttafaq – Bukhaary na Muslim).*

Pia:

*‘Aisha(r.a) ameeleza: Mtume(s.a.w) hakukhiyarishwa baina ya mambo mawili katu ila kuchagua lililo sahali madamu halijakuwa ni la dhambi....” (Muttafaq – Bukhaary na Muslim).*

## **KUTOA SALAMU**

Suala la kutoa salamu ni utamaduni wa muislamu uliokokotenzwa kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

*“Enyi mlioamini: Msiingie nyumba ambazo si nyumba zenu mpaka muombe ruhusa (mpige hodi) na muwatolee salamu waliomo humo. Hayo ni bora kwenu; huenda mtakumbuka (mkaona ni mazuri haya mnyoambiwa)” (24:27).*

*“...Na mnapoingia katika majumba toleaneni salamu (maamkio haya) ni zawadi itokayo kwa Mwenyezi Mungu, yenye Baraka na mema. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu anavyokubainishieni aya (zake) ili mpate kufahamu” (24:61).*

*“Na mnapoamkiwa kwa maamkio yoyote yale, basi itikieni kwa yaliyo bora kuliko hayo, au rejesheni hayo hayo. Hakika Mwenyezi Mungu anafanya hisabu ya kila kitu ” (4:86).*

Ubora wa Salamu na namna ya kutoa salamu unaelezwa katika Hadith zifuatazo:

### **Hadith 9:**

وعن عبد الله بن عمرو بن العاص رضي الله عنها: أَنَّ رَجُلًا سَأَلَ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: أَيُّ الْإِسْلَامِ خَيْرٌ؟ قَالَ: ﴿تَطْعِمُ الطَّعَامَ، وَتَقْرَأُ السَّلَامَ عَلَى مَنْ عَرَفْتَ وَمَنْ لَمْ تَعْرِفْ﴾. مَتَّفَقٌ عَلَيْهِ.

*‘Abdullaah bin Amri bin Al-‘Aas(r.a) amehadithia kuwa mtu mmoja alimuuliza Mtume(s.a.w): “Ni amali gani katika Uislamu iliyo bora?” Akamjibu: “Ni kuisha chakula na kumtolea salamu unayemjua na usiyemjua”. (Bukhaary na Muslim).*

**Hadith 10:**

عن عِمْرَانَ بْنِ الْحَصِينِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا، قَالَ: جَاءَ رَجُلٌ إِلَى النَّبِيِّ ﷺ فَقَالَ: السَّلَامُ عَلَيْكُمْ، فَرَدَّ عَلَيْهِ ثُمَّ جَلَسَ، فَقَالَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: ﴿عَشْرٌ﴾ ثُمَّ جَاءَ آخَرَ، فَقَالَ: السَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللَّهِ، فَرَدَّ عَلَيْهِ فَجَلَسَ، فَقَالَ: ﴿عِشْرُونَ﴾ ثُمَّ جَاءَ آخَرَ، فَقَالَ: السَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ، فَرَدَّ عَلَيْهِ فَجَلَسَ، فَقَالَ: ﴿ثَلَاثُونَ﴾.. رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ وَالتِّرْمِذِيُّ، وَقَالَ: حَدِيثٌ حَسَنٌ.

*'Imraan bin Al-husain (r.a) amesimulia: Mtu mmoja alikuja kwa Mtume(s.a.w) akamwambia: "Assalaam 'Alaikum" (Mtume) akamrudishia, kisha mtu yule akaketi. Mtume(s.a.w) akasema: "Kumi". Kisha akaja mtu mwingine, akasema: "Assalaamu 'Alaikum Warahmatullaahi". Naye akamrudishia, yule mtu akaketi. Mtume(s.a.w) akasema: "Ishirin" Kisha akaja mtu mwingine akasema: "Assalaamu 'Alaikum Warahmatullaahi Wabarakatuh". Naye akamrudishia, yule mtu akaketi. Mtume(s.a.w) akasema: "(amepata thawabu thalathini)". (Abuu Daawuud na Tirmidhy).*

**Mafunzo ya Hadith**

Kutokana na Hadith hizi mbili tunajifunza yafuatayo:

1. Kuwatolea watu salamu unaowajua na usiowajua ni amali njema yenye malipo makubwa mbele ya Allah(s.w).
2. Ufupi wa salamu ni kusema: "Assalaamu 'Alaikum" na Muislamu hupata thawabu kumi kwa kusalimia hivyo.
3. Urefu wa salamu ni kusema: Assalaamu 'Alaikum Warahmatullaahi Wabarakatuh" na Muislamu hupata ujira maradufu kila anaporefusha salamu.
4. Anayesalimiwa arejeshe salamu kama alivyosalimiwa au azidishe.
5. Salamu hii ya Kiislamu ni zawadi aliyotupa Allah(s.w) yenye baraka na inayojenga mazingira yanayoashiria amani.

**Zoezi 4**

1. Nunua kitabu cha Hadith cha "Tafsiri ya RIYAADHU SWAALIHIIN" ukisome kila siku angalau kwa kupitia hadith tano.
2. Jitahidi kwa uwezo wako kuipamba na vipengele vya tabia njema zilizoanishwa katika Hadith 10 ulizozisoma katika sura hii.



*Sura ya Tano***TAREKH**

Somo la tarekh katika kitabu hiki litazingatia mada kuu zifuatazo:

- Uongozi wa Dola ya Kiislamu wakati wa Makhalifa waongofu wa Mtume(s.a.w).
- Kuhuisha Uislamu Wakati Wa Tabiina
- Kuhuisha Uislamu katika karne ya 20 A.D.
- Historia ya kuhuisha Uislamu Tanzania.

**UONGOZI WA DOLA YA KIISLAMU WAKATI WA MAKHALIFA WA MTUME(S.A.W)***Utangulizi*

Kifo cha Mtume(s.a.w) kiliacha pengo la kiongozi wa Dola ya Kiislamu. Muhammad(s.a.w) ni Mtume wa mwisho na hakuwa na naibu wake kama Haruna(a.s) alivyokuwa naibu wa Musa(a.s). Isitoshe, Mtume(s.a.w)hakuacha usia wowote wa nani awe kiongozi baada yake, sio kwa kauli wala maandishi. Hivyo ilibidi waislamu wazibe pengo la uongozi kwa kufuata utaratibu wa kuchagua viongozi wa Dola kwa kuzingatia mwongozo wa Qur'an na Sunnah. Kiongozi aliyechaguliwa kuchukua nafasi ya Mtume(s.a.w) aliiitwa Khalifa wa Mtume yaani kiongozi anayeongoza kwa niaba ya Mtume(s.a.w). Katika Historia ya Uislamu makhalifa waongofu walioongoza Dola ya Kiislamu nyayo kwa nyayo kama alivyofanya Mtume(s.a.w) ni wanne wafuatao:

- (1) Abubakar bin Abi-Qahafu(r.a) - 11-13AH(632-634 A.D)
- (2) Umar bin Khattab(r.a) - 14 - 24A.H(634 - 644 A.D)
- (3) Uthman bin Affan(r.a) - 24 - 36 A.H (644 - 656 A.D)
- (4) Ali bin Abu Twalib(r.a) - 36 - 41 A.H (656 - 661 A.D)

**Uchaguzi wa Abubakar Kuwa Khalifa**

Mara tu habari za kutawafu kwa Mtume(s.a.w) zilipoenea maswahaba waliokuwa wajumbe wa shura wakati wa uhai wa Mtume(s.a.w) walisahau wajibu wao wa kudhibiti pengo la uongozi lililojitokeza. Hali hii iliwapana nafasi Answar

kukutana kwenye ukumbi wa “Thaqifah Bani Saidah” na kuanza kuzungumzia uongozi. ‘Umar na Abubakar walipopata taarifa hii nao walienda kujiunga katika ukumbi huo. Wakati huo huo bani Hashim nao walikuwa wanakutana nyumbani kwa Fatma bint Muhammad kuzungumzia ukhalifa. Pale “Thaqifa Bani Saidah” mjadala mrefu ulipita, wapo waliotaka khalifa atoke upande wa Answar, wapo waliotaka khalifa atoke upande wa Muhajirina na wapo waliopendekeza kuwe na khalifa na naibu khalifa. Hatimaye walikubaliana kuwa pawe na khalifa mmoja ndipo Abubakar akampendekeza ‘Umar bin Khattab upande wa Muhajirina na Saad bin Ubaidah upande wa Answar. Wote kwa pamoja (‘Umar na Saad) wakasema hawana kifua cha kusimama katika jambo la ukhalifa badala ya Abubakar. Baada ya kauli hii ‘Umar alimpendekeza Abubakar na akampa mkono wa ahadi ya utii (Ba’iyah). Ndipo wote waliokuwepo kwenye ukumbi ule wakampa Abubakar mkono wa ahadi ya utii.

Siku ya pili jambo hili lilipelekwa msikitini kupata ridhaa ya Waislamu wote. Takriban watu thelathini na tatu elfu (33,000) walimkubali Abubakar awe khalifa na kumpa mkono wa ahadi ya utii. Lakini Ali bin Abutalib aliendelea na kikao cha ukoo wa bani Hashim na hakuwepo msikitini wakati Abubakar amepewa Ba’iyah na Waislamu 33,000 waliokuwemo. Ali alichukua miezi kabla ya kumpa khalifa Abubakar ahadi ya utii.

Abubakar alipewa ofisi ya ukhalifa kwa kufuata misingi ya Uislamu ya watu kumchagua kiongozi kwa kuzingatia sifa stahiki. Abubakar alistahiki kuchukua nafasi ya ukhalifa kwa sifa zifuatazo:

**Kwanza**, alikuwa na sifa zote za kiongozi wa Dola ya Kiislamu. Sifa hizi ni: Ucha-Mungu, ujuzi wa Qur-an na Sunnah, siha nzuri na tabia njema. Sifa zote hizi alikuwa nazo Abubakar(r.a)

**Pili**, Abubakar alikuwa karibu na Mtume(s.a.w) pengine kuliko swahaba yoyote. Hili linadhihirika zaidi katika msimamo wake wa kufuata hatua kwa hatua kila ambalo Mtume(s.a.w) amelifanya au kuliruhusu katika uhai wake alipokuwa akiendesha Dola ya Kiislamu. Usahibu wa Mtume(s.a.w) na Abubakar umetajwa katika Qur-an kuhusiana na tukio la pangoni Thaur, wakati wa kuhajir Mtume:

إِلَّا تَنْصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ اللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ الَّذِينَ كَفَرُوا ثَانِيَ اثْنَيْنِ إِذْ هُمَا فِي الْغَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَاحِبِهِ لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَيْهِ وَأَيَّدَهُ بِجُنُودٍ لَمْ تَرَوْهَا وَجَعَلَ كَلِمَةَ الَّذِينَ كَفَرُوا السُّفْلَىٰ وَكَلِمَةُ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٥﴾

*Kama hamtamnusuru (Mtume), basi Mwenyezi Mungu alimnusuru walipomtoa wale waliokufuru; alipokuwa (mmoja tu na mwenziwe) wa pili wake, (peke yao); walipokuwa wote wawili katika pango; (Mtume) alipomwambia sahibu yake: “Usihuzunike, kwa yakini Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi.” Mwenyezi Mungu akamteremshia utulivu wake, na akamnusuru kwa majeshi msiyoyaona, na akafanya neno la wale waliokufuru kuwa chini; na neno la Mwenyezi Mungu ndilo la juu. Na Mwenyezi Mungu ndiye anayeshinda na ndiye Mwenye hikima. (9:40)*

**Tatu**, Abubakar ndiye aliyeteuliwa na Mtume(s.a.w) kuongoza swala kwa niaba yake alipokuwa anaumwa karibu na kutawafu kwake. Katika siku hizo ambazo Abubakar aliteuliwa kuwa Imamu kwa niaba ya Mtume(s.a.w) ilitokezea siku moja akachelewa akaswalisha Imamu mwingine (aliswalisha ‘Umar bin Khattab). Mtume(s.a.w) aliposikia sauti isiyo ya Abubakar aliuliza juu ya Imamu (Abubakar) ambaye hakuwepo. Mtume hakupendezwa na akasema: “asiswalishe mtu mwingine ila Abu Qahafu (Abubakar). Baada ya hapo akaitwa Abubakar lakini wakati huo Imamu (‘Umar) alikwisha maliza swala. Mtume(s.a.w) aliamuru swala ile irudiwe nyuma ya Imamu Abubakar(r.a)

**Nne**, Abubakar alikuwa mtu mashuhuri anayekubalika, mtaratibu, mwenye istiqama na Ikhlas, mpevu wa uoni na mwenye uamuzi na alikuwa mfuasi wa Mtume(s.a.w) wa nyayo kwa nyayo.

Sifa zote hizi ukichanganya na umri wake, kwa wale waliokuwa kwenye ukumbi wa Thaqifa Bani Saidah hapana aliyemzidi kiumri, utaona kuwa Abubakar alistahiki kuwa Khalifa na hakuwa na upinzani kisifa.

Pia hutuba ya Abubakar aliyoitoa katika kupokea Ukhalifa nayo inaumuhimu wake katika kuonyesha wajibu wa kiongozi wa Dola ya Kiislamu, pale aliposema:

*“Enyi watu mmenichagua niwe mhamini wenu ingawa mimi sio bora kuliko wengi miongoni mwenu. Nikiwa sahihi nitiini. Nikipotoka nirekebisheni kwani ukweli ni uaminifu na uwongo ni kutoaminika. Aliyedhaifu atakuwa na nguvu mbele yangu mpaka nishindwe kumpatia haki zake Insha-Allah na mwenye nguvu mbele yangu atakuwa dhaifu mpaka alipe haki za wengine Insha-Allah. Allah huteremsha Nakama kwa watu walioacha Jihad katika njia yake. Vile vile Allah huteremsha maafa kwa watu ambao hufanya maovu”.*

## **Mawazo Tofauti Kuhusiana na Uchaguzi wa Abubakar**

Zipo tofauti za kimawazo kuhusiana na uchaguzi wa Khalifa wa kwanza, Abubakar(r.a.) mara baada ya kutawafu Mtume (s.a.w.).

Wapo wasemao uchaguzi ule ulifanyika katika mazingira ya kuchanganyikiwa, kwani mkutano haukuwa rasmi. Maelezo ya kundi hili yameegemea kauli zisemazo kuwa Abubakar(r.a.) na Umar(r.a.) walistushwa na taarifa kuwa Ansar walikuwa wamekutana kwenye ukumbi wa mikutano wa Thaqifa Bani Saidah,

kumchagua kiongozi anayetokana na wao ambaye angeshika uongozi wa dola ya Kiislamu baada ya Mtume(s.a.w.). Kwa mujibu wa kauli hizo, Abubakar(r.a.) na Umar(r.a.) walilazimika kwenda kwenye mkutano huo wakiwa na dhamira ya kuzuia usiendeleo, hasa ikizingatiwa kuwa Mtume alikuwa bado hajazikwa na hilo ni suala zito lilohitajia muafaka wa Waislamu wote.

Kundi jingine lina mawazo kuwa, pamoja na kuwa mkutano wa Ansar haukuwa rasmi, lakini kuchaguliwa Abubakar(r.a.) kuliwafiki, kwa kuzingatia dokezo za Mtume(s.a.w.), ishara zitokanazo na Qur'an na aliyokuja kuyafanya Abubakar(r.a.) wakati wa uongozi wake, ambayo yalidhihirisha usahihi wa chaguo la mkutano wa Thaqifa Bani Saidah.

Wapo wanaosema kuwa kutokuwepo kwa watu wa nyumba ya Mtume (Ahlul-Bayt) katika mkutano ule, kunabatilisha zoezi zima la uchaguzi wa Khalifa wa kwanza. Maelezo ya kundi hili yanatiwa tashdid na usia, unaodaiwa kuachwa na Mtume(s.a.w.) kwa "Ahlul-Bayt" muda mfupi kabla ya kutawafu kwake; unaosema kwamba haki ya uongozi wa ummah huu baada yake ni ya "Ahlul-Bayt". Kwa hivyo Ali(r.a.) ndiye aliyestahiki nafasi hiyo, na warithi baada yake ni wanawe Hassan na Hussein kwa kuwa ni wajukuu wa Mtume(s.a.w.). Kundi hili linadai Ukhalifa wa Abubakar(r.a.), Umar(r.a.) na Uthman(r.a.) ni batili kwa kuwa hao si katika watu wa nyumba ya Mtume(s.a.w.) na walipewa uongozi katika mikutano isiyo rasmi. Aidha hatua ya kuwafanya Makhalfu ni kudhulumu haki ya Ali(r.a.) akiwa ndugu wa Mtume.

Na kuna wasemao kwamba, kwa kuwa Uislamu ni dini ya Mwenyezi Mungu si ya ukoo, kabila au Taifa fulani, na kwa kuwa hakuna aya katika Qur'an inayomwamrisha Mtume(s.a.w.) kurithisha dhima ya uongozi baada yake kwa watu wa nyumbani kwake (Ahlul-Bayt), basi jukumu la uongozi wa ummah limeachwa mikononi mwa waumini wenyewe. Kiongozi atachaguliwa kwa kuzingatia sifa mbali mbali zikiwemo uoni, ucha Mungu, siha n.k. Sifa zote hizo zimpelekee kuongoza kwa haki na uadilifu. Kwa hiyo Ukhalifa wa Abubakar, Umar na Uthman si suala la kubishaniwa.

## **Uchaguzi wa 'Umar bin Khattab kuwa Khalifa wa Pili.**

Mtume(s.a.w.) kumchagua Abubakar kuwa Imam wa msikiti na kutoruhusu mtu mwingine kuswalisha na aliposwalisha mtu mwingine swala ikarudiwa ni dhahiri, kwa maoni yetu, Mtume(s.a.w.) aliashiria kuwa kiongozi awe Abubakar na akawaachia Waislamu waamue kumkubali au kumkataa. Tunaamini kuwa Abubakar alimuelewa hivi Mtume(s.a.w.) ndio maana alipokuwa anakaribia kutawafu aliwaita wajumbe wa Shura na kushauri kuwa yeye anampendekeza Umar awe ndiye Khalifa baada ya kifo chake. Wajumbe wa Shura walipokubali ndipo akamwambia Ali aandike usia huo. Abubakar alifanya hivi kwa jitihadi yake ambayo inakubalika katika Uislamu na hasa akizingatia hali ilivyokuwa



mara Mtume alipofariki, Waislamu walipogawanyika makundi matatu yaani ukoo wa Mtume, Muhajirin na Ansvari.

Hivyo alitumia njia hii ambayo ni ya Kiislamu, hakuiburuza Shura na kulikuwa na mjadala kabla ya kukubalika rai hiyo. Wajumbe maarufu wa Shura walikuwa 'Umar, Uthman, Ali, Talha, Abdul Rahman bin Auf, Muadh bin Jabal, Ubay bin Kaab, Zaid bin Thabit na wajumbe wengine mashuhuri kutoka Muhajirin na Ansar. Abubakar alitoa pendekezo lake la kumteua Umar kuwa Khalifa wa pili, wote walikubali ila walieleza wasi wasi wao juu ya ukali wa Umar, hii ndio hoja pekee iliyotolewa na Ali na Talha. Abubakar alikataa hoja hii kwa kuwafahamisha kuwa Ukhalifa utamfanya asiwe mkali. Kwa kuwa hoja dhidi ya Umar ilikuwa hii tu basi pendekezo likakubalika.

Hatua iliyofuata ambayo imeimarisha uhuru wa kuchagua viongozi ni kuwahutubia waumini katika msikiti wa Mtume, akisaidiwa na jamaa zake, alisimama kwenye mimbari, kwanza alitaka ule usia usomwe mbele ya watu wote waliokuwa msikitini na yeye azungumze nao. Usia wenyewe ulikuwa kama ifuatavyo:

*“Bismillahir Rahmanir Rahiim. Hili ni tamko linalofanywa na Abubakar bin Abi Qahafu ambaye yuko karibu ya kwenda akhera. Wakati wa kuwa katika hali ya kufa hata kafiri humuamini Mwenyezi Mungu, na hata mfanya madhambi hutubia (hurudi kwenye imani yake) na kafiri humtegemea Mwenyezi Mungu. Nimefanya kila jema kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kwa kuboresha dini yake na kwa manufaa ya Waislamu na kwa mimi mwenyewe katika kumteua Umar kuwa Khalifa. Nategemea atakuwa muaminifu na mtekelezaji haki lakini akibadilika na kuwa dhalimu mimi sina lawama kwa kuwa sina elimu ya ghaibu. Kila mmoja anawajibika kwa afanyayo”<sup>1</sup>*

Baada ya usia huu kusomwa, Abubakar alipanda kwenye mimbari huku akisaidiwa na kuuhutubia umma kama ifuatavyo:-

*“Enyi ndugu zangu, sikumchagua kuwa Khalifa ukoo wangu au ndugu zangu. Nimemteua aliyebora miongoni mwenu, mnakubaliana na uteuzi wangu? Wote waliitikia kwa kukubali”<sup>2</sup>*

## **Uchaguzi wa Uthman bin Affan Kuwa Khalifa wa Tatu**

Uislamu sio dini iliyofungwa katika mabano bali ina sifa ya kwenda na wakati kwa maana kuwa maamuzi yake ilimradi yamo katika mfumo wa Uislamu yanakubalika. Hali ilivyokuwa wakati alipotawafu Mtume(s.a.w) imetofautiana na ile ya wakati alipotawafu Abubakar. Wakati wa kifo cha Abubakar, Umar alikuwa amejitokeza kuwa ndiye Khalifa bila upinzani lakini wakati wa kifo cha Umar hali ilikuwa tofauti. Walikuwepo watu wengi wenye sifa zinazolingana hivyo alichokifanya Umar ni kuteua jopo la wagombea sita wa ukhalifa ambao walikuwa ni: Uthman, Ali, Saad, Talha, Zubair na Abdur-Rahman bin Auf.<sup>3</sup> Agizo

lingine alilotoa ni kuwa katika muda wa siku tatu baada ya kifo chake wawe wameshaamua wao wenyewe nani miongoni mwao awe Khalifa.

Jopo hili lilikaa kwa muda mrefu bila kufikia uamuzi ndipo Abdur-Rahman bin Auf aliposhauri kuwa kati yao mmoja ajitoe ili aweze kutoa uamuzi. Alipokosa jibu alijitoe mwenyewe na akaanza kazi ya kutafuta maoni ili kukamilisha uteuzi. Talha hakuwepo hivyo wagombea walibaki wanne. Imetokea kuwa Ali alimpendekeza Uthman na Uthman alimpendekeza Ali. Zubair na Saad walimpendekeza Uthman. Baada ya kushauriana na Maswahaba wengine na kwa kuzingatia muda wa siku tatu Abdur-Rahman bin Auf alitoe uamuzi asubuhi ya siku ya nne na kumtangaza Uthman kuwa ndiye Khalifa. Abdur-Rahman bin Auf(r.a.) alianza kumpa bai'at (mkono wa ahadi ya utii) na kutambua Ukhalifa wake ndipo Waislamu waliokuwa msikitini wakafuatia na kwa namna hii Uthman akawa Khalifa wa tatu. Talha aliporudi Madinah, Uthman alimshauri achague moja kati ya mawili, achukue nafasi ya Ukhalifa au ampe mkono wa ahadi ya utii. Talha alikubali kumpa mkono wa ahadi ya utii.

Utaratibu huu pia umo katika mkondo wa Uislamu na ni aina ya tatu ya utaratibu unaokubalika wa kupata viongozi katika Uislamu.

## **Uchaguzi wa Ali bin Abu Twalib kuwa Khalifa wa nne**

Mkondo wa historia ya Kiislamu juu ya utaratibu wa kuingia kwenye mamlaka umechukua sura mpya, pale alipouliwa Khalifa wa tatu na wapinzani, na kundi hili la wapinzani likamtaka Ali awe ndiye Khalifa wa nne. Kwa hali ilivyokuwa naye akakubali kuchukua nafasi hiyo. Jambo hili lilipelekwa msikitini na wapo waliokubali Ukhalifa wa Ali bila masharti, wapo waliokubali kwa sharti kuwa wahalifu waadhibiwe na wapo waliokataa kumpa mkono wa ahadi ya utii miongoni mwao ni Muhammad bin Muslimah, Usamah bin Zaid, Hassan bin Thabit, Ka'ab bin Malik, Abu Said Khudri, Numan bin Bashir, Zaid bin Thabit, Mughirah bin Shubah na Abdullah bin Salama.<sup>4</sup> Wengine waliokataa ni ndugu na jamaa wa ukoo wa Uthman. Baadhi ya waliokataa Ukhalifa wa Ali waliamia Syria. Kwa ujumla uchaguzi wa Ali(r.a) uliwagawa waislamu kwenye makundi manne yafuatayo:

- (i) Wafuasi wa Uthman (Uthmanis), ambao walitaka dola iwaadhibu wauwaji Watu wengi wa msimamo huu walikuwa wakazi wa Syria na Basra. Wasiria walimtaka Muawiyah ndiye awe Khalifa na sio Ali. Lakini Wabasra walitaka awe Talha au Zubeir.
- (ii) Marafiki wa Ali (Shian-i-Ali). Watu hawa hawakumuona kuwa Uthman angefaa kuwa Khalifa. Hivyo wakajiita wenyewe Shia-i-Ali (marafiki wa Ali) watu wa mji wa Kufa (Wakufa/Kufans) na Wamisri ndio waliokuwa na msimamo huu. Inaaminika kuwa kundi hili ndilo lililomuua Uthman.

(iii) Mashibah: Watu hawa walikuwa kwenye Jihad wakati Uthman anauliwa. Hawakuwaunga mkono Uthmanis wala Shias.

(iv) Ahli-Sunnah wal Jamaah: Kundi hili lilikuwa lenye maswahaba wengi na lilienea Dola yote ya Kiislamu. Hawa wanasema tunawapenda wote Uthman na Ali. Wote ni Maswahaba waongofu. Kama kuna aliyefanya makosa ni kutokana na ijthada, yake. Tunafuata Sunnah za Mtume na Sunna za Jamaa waongofu yaani kundi la Maswahaba.<sup>5</sup>

Utaratibu huu, ingawa kuna baadhi ya wanachuoni wanaoukubali lakini hauhitaji mjadala wowote, ni wazi kuwa hauna nafasi katika Uislamu. Kwa hakika watu wa Madina walikuwa na khofu na kundi hili la wauwaji hivyo kukubali kwao ule Ukhalifa wa Ali kwa mfumo ule yawezekana ni matokeo ya woga tu na siyo hiyari yao. Majibu ya Zubeir na Talha walipoulizwa na mjumbe wa Gavana wa Basra katika msafara wa Bibi Aisha kwa nini wanavunja Ahadi ya utii kwa Khalifa walisema. “Ba’iyah ilifanywa mbele ya ncha ya upanga na ahadi ya kuwaadhibu wauwaji.”<sup>6</sup>

Inawezekana pia hata kule kukubali kwa Ali kuwa Khalifa kunatokana na woga kwa sababu walipomtaka mara ya kwanza awe Khalifa kabla ya hao wauwaji kumuua Khalifa Uthman alikataa.<sup>7</sup> Si hivyo tu lakini alipoona wanamsonga kutaka kumshirikisha katika mzozo wao alihama Madina na kwenda Ahjar sehemu maili chache kutoka Madina.<sup>8</sup> Ingawa pia tukio hili linaonekana kumuweka Ali mahali pabaya.

Utaratibu wa kuingia katika uongozi wa dola ulizidi kuharibika alipouwawa Ali na mwanae mkubwa, Hassan akateuliwa kuwa Khalifa wa tano. Lakini Muawiyah alipopata habari hizi aliivamia Iraq. Hassan nae kwa upande wake alimteua Qays kuongoza majeshi ya kupigana na Muawiyah. Kulitokea uvumi kuwa Qays ameuwawa na hali hii ilipelekea majeshi ya Khalifa kumgeukia mwenyewe. Hassan alielewa hali ilivyokuwa mbaya hivyo alisalimu amri kwa Muawiyah, akaacha Ukhalifa kwa makubaliano kuwa atapofariki amuachie nduguye, Hussein ukhalifa. Baada ya makubaliano haya na Muawiyah, Hassan alirudi Madinah lakini aliuliwa kwa sumu aliyolishwa na mmoja wa wake zake kutokana na ushawishi wa Yazid.<sup>9</sup> Huu ndio ulikuwa mwisho wa Hassan mjukuu wa Mtume.

Taratibu zote hizi ni za kupora madaraka kama alivyofanya Muawiyah ingawa alishinda kivita, kuwekeana makubaliano na watoto wa Ali, Hassan kuwa atamwaachia madaraka Hussein baada ya kufa kwake, na utaratibu wa kurithishwa, taratibu zote hizi, hazikubaliki katika Uislamu ingawa mfumo huu wa mwisho ndiyo uliyotumika katika utawala wa Banu Umayya, Banu Abbasi na Fatimiya.

## **Kuzuka Imani ya Kishia**

Baada ya kuuwawa Ali(r.a), kundi la marafiki wa Ali(Shi'a Ali) lilianzisha imani mpya ya ushia. Walifuata itikaqadi iliyo buniwa na 'Abdallah bin Sabaa kuwa Ali ni Mrithi wa Mtume(s.a.w) kama Haruna(a.s) alivyokuwa mrithi Musa(a.s). Hivyo kundi hili lilitaqidi kuwa Ali(r.a) ndiye aliyekuwa Khalifa halali pekee na kuwaona Abubakar, 'Umar na Uthmani kuwa walikuwa madhalimu waliopora nafasi hiyo. Siku zilivyosonga mbele mashia waliandika vitabu vyao vya sheria, Hadith, Historia ya Uislamu na ufafanuzi wa Qur'an unaolandana na imani yao mpya. Kwa mujibu wa Imani ya kishia, kiongozi wa jamii lazima awe Imam ambaye uteuzi wake unatokana na Mtume(s.a.w). Baada yakutawafu Mtume(s.a.w),kulingana na Imani ya kishia Uimamu ulimshukia Ali(r.a) kupitia kwa mkewe Fatma bint Muhammed(s.a.w). Baada ya kuuliwa Ali(r.a) Uimamu uliwashukia watoto wa kiume wa Fatma hadi akafikia Imam wa kumi na moja anayeitwa Hassan al-Askari ambaye alifariki 874 A.D./260 A.H. katika utawala wa Abasi, ambao Khalifa wake alikuwa Matamid. Alipofariki Imam Hassan al-Askari Uimamu ulimshukia mwanee Muhammad anayejulikana kwa jina la Mahdi, Imam wa mwisho. Tarekh ya maimamu wa nyumba ya Mtume (Ahlul-Bayt) inatatanisha. Inaaminika Baba yake Hassan alihamishwa kutoka Madinah na kupelekwa Summara na dikteta Mutawakkil aliyekuwa Khalifa wakati huo, aliwekwa kizuizini huko Summara hadi akafa. Hassan naye aliwekwa kizuizini na aliyechukua nafasi ya Mutawakkil, mtoto wa Hassan aliyekaribia umri wa miaka mitano alianza kumtafuta baba yake katika pango lililokuwa karibu ya nyumba yao. Mtoto huyu hakurudi kutoka pangoni. Tukio hili limewapelekea Mashia kujaa matumaini kuwa mtoto huyu atarudi kuja kuikoa dunia kutokana na mzigo wa madhambi na uonevu.

Mtindo huu haumo katika mfumo wa Uislamu ingawa wafuasi wake wanatumia jina la Uislamu. Kwa nini mtindo huu haumo katika Uislamu tumeshazitaja sababu zake kuwa utume haurithiwi ila hapa tunataka kuongezea kuwa Imani hii ambayo ilipandikizwa baadaye katika historia ya Uislamu ina mizizi ya dini ya Uzoroastrian na Ukristu, dini ambazo zote zinamshirikisha Mwenyezi Mungu.

### ***Tanbih***

Kwa Waislamu hivi leo, mfumo wa usia kama wanavyofanya wafuasi wanaojiita Mashia si katika utaratibu unaokubalika katika Uislamu. Mtume hakulifanya, na hata Ali alipokuwa katika kitanda cha mauti baada ya kujeruhiwa aliulizwa na mtu mmoja kuwa Waislamu wampe mkono wa ahadi ya utii mwanee mkubwa, Hassan, awe Khalifa? Ali alijibu, "Nawaachia Waislamu waamue". Au mfumo wa ufalme (Royal Family) kama ule wa Saudia Arabia, Moroko, Oman, Qatar au mfumo wa vyama vingi au kimoja kama Pakistan, Misri, Libya, Syria n.k. siyo mifumo ya Kiislamu na nchi zinazofuata mifumo hiyo si za Kiislamu.

Hivyo ni dhahiri wajumbe wa Shura katika dola ya Kiislamu wanalazimika kwa kushirikiana na kiongozi aliyepo madarakani kumteua anayefaa kuwa kiongozi

kisha jina liwasilishwe kwa waumini kwa ajili ya kupitishwa au kukataliwa. Hivyo ni kweli kuwa jina linalotolewa na utaratibu unaotumika sasa wa chama kuteua mgombea katika chaguzi za Marais duniani kote ni mawazo yaliyoazimwa kutoka katika mfumo huu wa Kiislamu.

## Uendeshaji wa Dola ya Kiislamu Wakati wa Makhalifa

### *Kazi na Wajibu wa Khalifa*

Khalifa katika Serikali ya Kiislamu ndiye mtendaji mkuu wa Serikali kama alivyokuwa Mtume(s.a.w). Akiwa mtendaji mkuu wa Serikali, kwa ujumla Khalifa atasimamia utekelezaji wa madhumuni ya kuwepo Dola ya Kiislamu ambayo ni

- (1) Kuhuisha, kuendeleza na kudumisha maadili mema ambayo hupelekea watu katika jamii kuishi kwa furaha na amani.
- (2) Kuzuia na kukomesha maovu ambayo huleta vurugu, mashaka na huzuni katika jamii.

الَّذِينَ إِن مَكَّنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ أَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ وَأَمَرُوا

بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَوْا عَنِ الْمُنْكَرِ ۗ وَاللَّهُ عَاقِبَةُ الْأُمُورِ ﴿٤١﴾

*Wale ambao tukiwamakinisha, (tukiwaweka uzuri) katika ardhi husimamisha Sala na wakatoa Zaka na wakaamrisha yaliyo mema na wakakataza yaliyo mabaya. Na marejeo ya mambo ni kwa Mwenyezi Mungu. (22:41)*

Katika kutekeleza madhumuni haya ya Dola ya Kiislamu, Khalifa aliwajibika kufanya yafuatayo:

- (i) Kujenga maisha ya binaadamu juu ya msingi wa ucha-Mungu na matendo mema. Kuyasafisha maisha ya binaadamu kutokana na maasi, kudumisha haki na usawa, kukomesha ukatili, ukandamizaji, utabaka, uonevu, unyonyaji, udhalimu n.k.

*“Kwa hakika tuliwapeleka Mitume wetu kwa dalili wazi wazi na kuteremsha vitabu na uadilifu pamoja nao, ili watu wasimamie uadilifu.....” (57:25)*

- (ii) Kutumia uchumi wa Taifa kwa kukuza na kuendeleza maadili mema kwa raia wake.
- (iii) Kuamrisha mema na kukataza mabaya. Hatua nne zilichukuliwa katika kufanikisha jukumu hil:
  - (a) Kuteua mahakimu wacha-Mungu wa kusimamia haki na sheria.
  - (b) Kuteua Madai'yah (Waalimu) wa kuwaelekeza watu yepi mema na namna ya kuyaendea na yepi maovu na namna ya kuyaepuka.

- (c) Hutuba za Ijuma, Idd na Hijja zilitumika kukazia wema na ucha-Mungu.
- (d) Kuteua tume ya kufuatilia tabia za watu na kuadhibu hapo hapo kwa makosa yasiyohitaji kwenda mahakamani.
- (iv)Kulinda mipaka ya dola kwa gharama yoyote. Mipaka ya Dola ililindwa ama kwa vita au kwa diplomasia.
- (v)Pamoja na kulinda na kutekeleza madhumuni ya dola ya Kiislamu, Khalifa akishirikiana na Shura yake, aliteua viongozi mbali mbali wa Serikali ikiwa ni pamoja na wakuu wa majimbo(Walii au Gavana),Mahakimu, (Makadhi) wakusanya kodi,(maamil) majemedari,makatibu, wakuu wa polisi, n.k.
- Kwa mfano Khalifa Abubakar aliteua magavana 17 kuongoza majimbo (mikoa) 17 ya Serikali yake. Naye ‘Umar aliteua Magavana 15 katika Serikali yake.
- (vi)Khalifa alikuwa ndiye mkuu wa majeshi. Aliamuru vita vipiganwe au visipiganwe, alisaini mikataba, aliteua maamiri jeshi na kupeleka maelekezo katika uwanja wa vita. Abubakar na Ali waliongoza mapigano kama Mtume(s.a.w) alivyofanya, lakini ‘Umar na ‘Uthuman hawakujaaliwa fursa hii lakini wamekufa mashahidi kwa kuuliwa na wapinzani.
- (vii)Khalifa alikuwa ndiye mwanasheria mkuu wa Serikali.

Alisikiliza kesi na kutoa hukumu na yeye ndiye aliyekuwa mahakama ya rufaa. Mikoani waliteuliwa makadhi walioendesha kesi na kutoa hukumu kwa niaba yake.

## **Malipo ya Khalifa**

Abubakar alipochaguliwa kuwa Khalifa aliendelea na kazi yake ya biashara. Siku moja alipokuwa anakwenda sokoni kuuza nguo alikutana na Umar na Abu Ubaida ambao walimkataza asifanye hivyo kwa kazi nzito ya uongozi inayomkabili. Ndipo shura ikakaa na kuamua kuwa apewe kiwango maalum cha posho kutoka katika Baitul-Mali cha kumuwezesha kuishi maisha ya kawaida. Zaidi ya kasma hii hakuruhusiwa kuchukua zaidi. Hata hivyo Khalifa Abubakar alirudisha kwenye Baitul Mali posho yote aliyopewa kutokana na maelekezo yake alipokuwa anafariki Dunia. Katika Ukhalifa wa Umar mishahara ilipangwa kwa wafanyakazi na viongozi wa Serikali. Hivyo Khalifa Umar na Ali walichukua posho zao ila Uthman alitumia pesa zake kwa vile alikuwa na uwezo wa kiuchumi.

## **Khalifa na Utungaji Sheria**

Khalifa kama ilivyokwishaoneshwa sio mtungaji wa sheria kama ilivyo kwa marais wa leo na mabunge yao. Khalifa ni mtekelezaji na msimamizi mkuu

wa sheria za Mwenyezi Mungu. Katika kipindi cha Ukhalifa vyanzo vya sheria vilibakia kuwa Qur'an, Sunnah na Ijmaa na baadaye Umar, Khalifa wa pili, aliongeza Qiyas. Kwa hali hii Ufalme katika Dola ya Kiislamu ulibaki kuwa ni wa Mwenyezi Mungu tu.

Siku za mwanzo za ukhalifa kuliundwa tume ya sheria (Ofisi ya Mufti) ilipotokea haja. tume hii iliitwa na kupitisha uamuzi. Tume ya sheria ya Khalifa ilifanya kazi kwa kutegemea vyanzo vya sheria vilivyotajwa katika masuala ya kawaida, maamuzi ya tume yalikiidhi haja. Lakini yalipotokea masuala yasiyo ya kawaida na yenye umuhimu wa kitaifa ilikaa majlis ya Ansar, Muhajirin, wawakilishi wa Aus na Khazraj na kupitisha maamuzi; kwa mfano baada ya kutekwa kwa Iraq na Syria wapo maswahaba waliotaka ardhi igawiwe kwa askari waliopigana. Majlis iliyojumuisha Ansar, Muhajirin na watu mashuhuri watano watano kutoka makabila ya Aus na Khazraj ilifanyika kuamua suala hili. Baada ya mjadala mrefu Khalifa Umar alifanikiwa kuwaelewesha wajumbe wa majlis kwa kunukuu aya nyingi kuthibitisha kuwa katika ardhi hata vizazi vijavyo vina hisa kwa hiyo ardhi isigawiwe kwa askari waliopigana lakini waachiwe wenyewe waliotekwa na kodi itakayotokana na ardhi hii wagawiwe askari katika mfumo wa kiinua mgongo cha kila mwaka.

Hivyo ni dhahiri mkono wa Khalifa haukuwa juu ya sheria bali chini ya sheria ya Mwenyezi Mungu, kwa namna hii haikuwezekana kupendelea kundi au mtu yeyote au kuipinda sheria kwa kumpendelea kundi fulani. Hivyo kulikuwa na usawa kamili mbele ya sheria. Hali kadhalika katika masuala ya kodi kulikuwepo usawa na haki za kiraia. Hali hii ilipelekea mshikamano miongoni mwa waumini, uhuru wa maoni, haki katika jamii na kubwa kabisa ni kuwavumilia wafuasi wa dini nyingine.

## **Khalifa na Mahakama**

Kabla ya kuangalia suala la mahakama katika Uislamu, tuanze na mtazamo wa Uislamu juu ya uhalifu, makosa au hatia. Makosa katika Uislamu yapo katika mafungu matatu:

- (i) Makosa yanayomuhusu Mwenyezi Mungu kama vile uzinzi, ambao adhabu yake ni bakora mia moja, kumsingizia mtu kuzini, ambako adhabu yake viboko themanini, vileo adhabu yake viboko themanini, wizi ambao adhabu yake ni kukatwa mkono na au ujambazi ambao adhabu yake ni kukatwa mkono na miguu. Makosa haya yanajumuishwa katika istilahi moja kuwa ni Al-Hudud. Khalifa hawezi kusamehe makosa haya. Kazi yake ni kutekeleza hadd (adhabu). Kwa wasio Waislamu makosa haya husameheka endapo atasilimu.
- (ii) Makosa dhidi ya mwanadamu yanayohitaji fidia, "*al-qisas*". Mengi ya makosa haya kama kuuwa, kuumiza, kumtukana mtu n.k yanaweza

kumalizwa kwa makubaliano kwa mujibu wa sheria lakini Khalifa hana mamlaka ya kusamehe ila aliyekosewa. Hali kadhalika makosa haya hayahesabiwi kuwa makosa dhidi ya Serikali.

(iii)Yapo baadhi ya makosa kama, uasi (Rebellion), kula mali ya umma yamehesabika kama makosa dhidi ya Serikali.

Kwa kuzingatia haya, kazi za Khalifa kimahakama ni za aina tatu.

**Kwanza** kuhakikisha kuna amani katika himaya yake, maendeleo kwa tabaka zote za watu na kuwalinda wanyonge mbele ya wenye kujiweza. **Pili** ni kutekeleza adhabu, kuratibu na kutekeleza haki za wanaodhulumiwa. Na **tatu** ni kuteua mahakimu wa kusimamia haki.

Mahakimu hawa walikuwa watu wazima, waadilifu, waliobobea katika sheria ambao kazi zao ni pamoja na kuhukumu kesi, kusuluhisha magomvi, kurudisha amana za watu, ulipaji wa zaka, utekelezaji wa usia, utekelezaji wa adhabu, kusimamia mipango ya ndoa, mirathi, talaka, na haki za wanyonge.

Katika kuhakikisha kuwa haki inatendeka kwa wote, tangu wakati wa Ukhalifa wa Abubakar ilianzishwa ofisi ya mufti au taasisi ya mufti au tume ya uchambuzi wa sheria. Ofisi hii ndio pekee iliyoruhusiwa kutoa uchambuzi wa kina wa Fatwa za mamlaka mbali mbali. Hakuruhusiwa mtu mwingine kutoa uchambuzi wa sheria. Walioteuliwa wakati wa Abu bakar kushika wadhifa huu ni Umar, Ali, Uthman, Abul Rahman bin Auf, Ali bin Kaab, Zaid bin Thabit na Abu Huraira - Mufti hawa walisaidia kuwafahamisha watu kuhusu sheria na kuwashauri bila malipo. Serikali ilifanya hivi ili kupunguza makosa kwani kwa kujua sheria watu walijizua kufanya makosa.

Waraka, Khalifa Umar, aliowatumia mahakimu ni kielelezo cha utaratibu wa mahakama ulivyokuwa wakati wa makhaliifa ambao leo hii unafuatwa duniani kote. waraka huo tunaupitisha kama ifuatavyo:

- (i) Utawala wa haki ni amri ya Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume wake, hivyo ni lazima kufuatwa.
- (ii)Mashtaka yanapowasilishwa ipitishwe hukumu kwa uangalifu.
- (iii)Mshitaki na mshitakiwa wote watendewe haki ili maskini asikate t a m a a ya kufanyiwa haki na wenye uwezo wasifikirie kupendelewa.
- (iv)Ushahidi ni juu ya mlalamikaji na anayelalamikiwa anaweza kukana anacholalamikiwa kwa kuapa.
- (v)Suluhu inaweza kufikiwa nje ya mahakama lakini mazingira ya suluhu yasichupe mipaka ya maamrisha na makatazo ya Mwenyezi Mungu.
- (vi)Hukumu inaweza kubadilishwa katika jambo lililodhahiri, kwani kubadilishwa hukumu ni bora kuliko kuendelea na uonevu.



(vii) Ikitokea kesi isiyo angukia kwenye sheria wala hukumu iliyoitangulia, ilinganishwe na kesi zinazofanana kisha “*deduction*” itumike kupitisha hukumu inayompendeza Mwenyezi Mungu na ya haki.

(viii) Mlalamikaji apewe muda wa kutolea ushahidi kesi yake ataposhindwa kesi inaweza kufutwa.

(ix) Hakimu asijione wala kuonyesha kuchukia inaposemwa kweli.

“Watu wote ni sawa mbele ya sheria” ndio mafunzo ya Qur’an. Uislamu hauruhusu ule msemu wa “Mfalme hakosei”. Hakuna mwanadamu aliyekamilika asiye kosea kabisa. Mtume (s.a.w.) aliweka mfano pale alipowataka watu wenye madai dhidi yake wajitokeze. Maswahaba wake nao walifuata nyayo zake kama mtu angewashitaki kama ilivyotokea kwa Umar au wao pia wangeshitaki kama ilivyotokea kwa Ali.

Khalifa Umar na Ubayy ibn Kaab, walikuwa na tofauti zao. Ubayy ibn Kaab alikwenda kumshtaki Khalifa kwenye mahakama ya Zayd bin Thabit. Hivyo Khalifa aliingia mahakamani kwa kujitetea. Alipokuwa anaingia mahakamani Zayd alisimama. Hapa Khalifa alisema hili ni tendo la kwanza la kuvunja haki. Kwa kufuata nafasi ya Khalifa kuwa alikuwa anajitetea alilazimika kuapa. Hakimu Zayd alimuomba Ubayy aondoe haki yake ya kumtaka Khalifa aape. Khalifa Umar aliingilia kati na kusema “kama Umar na watu wengine siyo sawa mbele yako, hufai kuwa Hakim.”<sup>10</sup>

## **Khalifa na Uendeshaji wa Dola kwa Ujumla**

Khalifa ndiye mtendaji mkuu wa Serikali. Kwa hiyo jukumu lake la kwanza lilikuwa kuhakikisha kuwa maelekezo na amri za mamlaka kuu ya uendeshaji zinatekelezwa. Katika kuendesha shughuli za kila siku za Serikali alisaidiwa na shura – ambayo mfano wake katika Serikali za leo ni Baraza la Mawaziri au Cabinet. Majlisi shura au Tume ya ushauri ilitumiwa na kila Khalifa katika makhalifa wanne wa Mtume (s.a.w). Hakukua na idadi maalumu ya wajumbe wa shura. Wajumbe hawa waliteuliwa na khalifa kwa misingi ya ucha Mungu na mchango wao katika Uislamu na kujitoa muhanga kwao. Miongoni mwao walikuwemo maswahaba maarufu wakiwemo Abubakar, Umar, Uthman, Ali Abdurahman bin Auf, Talha, Zubair, Saad Ibn Waqqas, Abu Ubaidah Ibn Jarrah na Said Ibn Zaid. Viongozi maarufu kutokana Muhajirin na Answar walijumuishwa kwenye shura.

## **Haki za Wasiokuwa Waislamu Chini ya Uongozi wa Khalifa.**

Uislamu una vumilia dini nyingine ingawa ni za kishirikina. Kwa hiyo wasio Waislamu, walitekeleza sheria zao kwa mujibu wa dini zao hasa katika masuala

ya urithi, ndoa, talaka, namna ya kupata viongozi wao, uendeshaji wa ibada zao n.k. Kwa kweli walikuwa na uhuru kamili. Vile vile kama wangependa walikuwa na uhuru wa kupeleka kesi zao kwa Kadhi(hakimu).Kesi inapopeleka kwa hakimu haikuruhusiwa kuiondoa mahakamani.

Sheria ya makosa ya jinai, sheria ya ushahidi na mikataba iliwahusu Waislamu na wasio Waislamu. Katika kuwaadhibu wahalifu dhidi ya ubinaadamu kama uzinzi, mauaji, wizi, kupora, n.k. sheria ya Kiislamu ilitumika kwa Waislamu na wasio Waislamu.

Kama mzozo ulizuka baina ya Muislamu na asiye Muislamu kesi ya namna hii ilipeleka mahakamani na utaratibu ulikuwa kama ifuatavyo: Katika masuala ya ubinaadamu asiye Muislamu alihukumiwa sawa na Muislamu. Kwa mfano kama asiye Muislamu amemuua Muislamu adhabu atayopewa ni sawa na ile, kama kosa lile lingefanywa na Muislamu.

Tukio la kihistoria lifuatalo linaonesha haki ilivyo katika Uislamu hata kama asiye Muislamu alimkosea Khalifa.

Wakati Khalifa Ali alipokuwa anaondoka kwenda katika vita vya Siffin - alipoteza zirah yake. Aliporudi toka vitani alimuona Myahudi mmoja na zirah yake. Khalifa alimuuliza yule Myahudi alipataje ile zirah wakati ni yake na hajampa mtu wala hajaiuza. Yule Myahudi alijibu kijeuri: “Kwa kuwa ninayo mimi basi kiasili ni mali yangu”. Khalifa pamoja na kuwa ndiye mkuu wa Serikali hakuwa na jinsi isipokuwa kulikepeleka suala hili mahakamani. Kadhi Shurayb alimuuliza Khalifa aliyekuwa pamoja naye sababu ya kuwepo kwake pale mahakamani. Ndipo Khalifa akaeleza: “zirah aliyonayo huyu Myahudi ni yangu kwa vile sijampa mtu yeyote na sijaiuza”. Yule Myahudi alipotakiwa kujieleza alieleza kuwa kwa kuwa zirah iko mkononi mwake basi ni mali yake. Hapo ndipo hakimu alipomtaka Khalifa atoe ushahidi, lakini alipotaka kuwaleta mwanee Hassan na mfanyakazi wake Qanbar kama mashahidi hakimu hakukubali ushahidi wao kutokana na uhusiano wao na Khalifa. Kwa hali hii Myahudi alishinda kesi na akaachiwa aende na ile zirah. Myahudi huyu alishangazwa na hali hii ya Khalifa kusimama mahakamani na raia wake tena wa dini nyingine na hata hivyo akashindwa kesi na akaridhika. Hali hii ilimfanya akiri kuwa ile zirah ni ya Khalifa akamrudishia na yeye akasilimu”.<sup>11</sup>

## **Kuanzishwa kwa Polisi.**

Kuanzishwa kwa Polisi Wakati wa ukhalifa wa Umar ilikuwa hatua nyingine ya kupunguza makosa na kusimamia haki katika jamii. idara hii ilitwa Ahdath na mkuu wake alitwa Sahib Al-Ahdath (mkuu wa Polisi) Maaafisa kadhaa waliteuliwa katika sehemu kadhaa ili kudhibiti makosa; kwa mfano kudhibiti vipimo na mizani, usalama wa barabara kama kutojenga nyumba barabarani,

kuzuia kuwabebesha mizigo mikubwa wanyama, kuzuia uuzaji wa pombe, nakadhalika. Wakati wa Makhaliifa wanne polisi hawakuendesha mashitaka mahakamani.

## **Kuanzishwa kwa Magereza**

Sambamba na kuwepo kwa polisi yalianzishwa magereza (jela) wakati wa Khalifa wa pili. Mwanzoni makosa ya jinai tu ndiyo yaliyowapeleka watu jela. Lakini siku zilivyosogea hata makosa kama kurudiarudia pombe yaliwapeleka walevi kufungwa badala ya kuchapwa bakora.

## **Khalifa na Kamati za Utendaji**

Masuala mengi kuhusiana na Dola kama vile kupanga mishahara ya wanajeshi, kuanzisha idara mbali mbali, kuwapa vibali wageni kufanya biashara katika Dola ya Kiislamu na kiwango cha kodi wanachotakiwa kulipa, n.k. yaliamuliwa na Khalifa baada ya kushauriwa na kamati yake ya utendaji. Kamati hii ilikuwa ikikutana kila siku katika msikiti wa Mtume(s.a.w). Taarifa za wilayani na mikoani zilizowasilishwa kwa Khalifa zilijadiliwa na kupitishwa maamuzi.

Baadhi ya wanakamati wa kamati hii ya utendaji walipewa nyadhifa mbali mbali; kwa mfano – Abubakar alimteua ‘Umar kuwa Jaji Mkuu na msimamizi wa kugawa zaka. Ali aliteuliwa kuwa mkuu wa mawasiliano; kusimamia wafungwa wa kivita, fidia yao na kadhalika.

Mbali ya shura teule, makhaliifa wote walitumia shura ya watu wote msikitini kama chombo cha kusaidia uendeshaji. Uteuzi wa majaji, wakuu wa mikoa, n.k. ulifanywa hadharani (msikitini) ili kama kuna upinzani wowote juu ya mteuliwa, raia walikuwa huru kupinga kwa hoja wazijuazo. Si hivyo tu hata kama kiongozi ameteuliwa bado raia walikuwa na fursa ya kuwasilisha malalamiko dhidi ya kiongozi muhusika.

Ili kujua ukweli wa malalamiko ya watu na kufanya uchunguzi, Tume ya kufuatilia malalamiko ya raia dhidi ya viongozi wao iliundwa. Malalamiko yalipomfikia Khalifa, alitwa kiongozi muhusika kwa kuhojiwa au tume ilimuendea.

Chombo kingine cha utawala kilikuwa mkutano wa watendaji wote wa Serikali waliokuwa wanakutana baada ya Hija. Wakati huu Khalifa alikuwa anamsikiliza kila mwenye malalamiko dhidi ya Serikali. Kwa namna hii kila mwananchi alihusika na uendeshaji. Si hivyo tu bali Khalifa Uthman alianza utaratibu wa kusikiliza malalamiko ya wananchi kila Ijumaa.

Jambo lingine muhimu katika uendeshaji ni kuwa Serikali ilitoa mishahara iliyokidhi mahitaji ya watendaji ili kuzuia rushwa na mambo yanayolingana.

## Uongozi wa Majimbo na Wilaya

Kama ilivyokuwa wakati wa Mtume(s.a.w) kuitawala Dola iligawanywa kwenye majimbo na wilaya. Idadi ya majimbo na wilaya ilitegemea kupanuka kwa mipaka ya Dola. Kila jimbo au wilaya ilikuwa na viongozi watatu. Gavana au Walii, mkusanyaji mapato ya Serikali (Amil) na mwanasheria (Kadhi). Gavana alifanya kazi zote za Khalifa mkoani kwake. Aliendesha swala za kila siku ya Ijumaa, Idi zote mbili, na kuongoza msafara wa Hija wa watu wa mkoa wake. Alisimamia amani na utulivu mkoani kwake, pale ambapo kamanda wa kijeshi wa mkoa hakuwepo mkuu wa mkoa ndiye aliyejaza nafasi hiyo na kuwa kamanda wa majeshi ya mkoa na mara nyingine kuongoza mapiganano dhidi ya maadui.

Pamoja na Gavana viongozi wengine waliokuwa mkoani ni Sheikh UI-Kharaj au msimamizi wa mapato ya Serikali. Sahib Ahdath (mkuu wa polisi), Kadhi na Kamanda wa majeshi. Wakati wa ukhalifa wa Umar kiongozi alipoteuliwa aliorodhesha mali zake na itapoonekana anaongezeko lisiloleweka aliulizwa na mali yake kutaifishwa.

## Pato la Serikali

Moja ya shughuli muhimu katika uendeshaji wa Serikali ni namna Serikali ilivyopata mapato yake na ilivyotumia. Wakati wa Mtume(s.a.w) vyanzo vya pato la Serikali vilikuwa zaka, jizya, kharaj, khums na fay. Katika kipindi cha makhalifa wanne vyanzo vya pato la Serikali viliongezeka kama ifuatavyo;

**Ushr;** Ushr ni kodi ya mazao kutoka katika ardhi ya Waislamu iliyotekwa kivita na kugawiwa askari waliopigana au ardhi ya Serikali iliyoandaliwa kwa kilimo au mifugo. Kwa ardhi inayotegemea mvua ya asili, mabwawa na mito ya asili kima chake ni 1/10 (10%) ya mazao na kwa mashamba yanayomwagiliwa kiwango cha ushuru ni 1/20 (5%) ya pato la mwaka.

**Kharaj** au kodi ya Ardhi: Kodi hii iliwahusu wasio waislamu ambao ardhi yao ilitekwa kivita lakini wenyewe wameruhusiwa kudelea kutumia ile ardhi iliyotekwa ambayo ni mali ya dola ya Kiislamu. Kodi hii iliwekewa kima maalum baada ya tathmini ya ardhi na ililipwa kwa mwaka.

**Jizya;** ilikuwa chanzo kingine cha pato la Taifa. Kodi hii iliwahusu wasio waislamu tu, waliojulikana kwa jina la "Dhimmi". Serikali ya Kiislamu inachukua dhamana ya kuwalinda wasio Waislamu, wao na mali zao. Wasio Waislamu wanalipa kodi hii ya jizya ikiwa ni malipo ya kazi ya ulinzi wanayofanyiwa na Serikali. Kodi hii pia iliwekewa kiwango maalum na haikuwahusu vikongwe, watoto, walemavu na wanawake.

**Zaka na Sadaqa** nazo zilibakia kuwa vyanzo vya msingi vya pato la Serikali.

**Ngawira** ni mali inayopatikana kwa kumshinda adui. Hii nayo ilitumika kama chanzo cha pato la Serikali. Wapiganaji walichukua asilimia 80 au (4/5) na pato la serikkali lilikuwa asilimi 20 au (1/5) ya ngawira.

**Fay** kilikuwa ni chanzo kingine cha pato la Serikali katika kipindi cha Makhhalifa. Fay ni mali iliyotolewa na adui hata bila ya kupigana.

**Zaraib** ni kodi za muda zilizotowza na serikali kwa maslahi ya nchi

Mapato mengine ya Serikali yalitokana na wakfu, kodi za madini, kodi ya mali inayoingia nchini au inayopitishwa, na kadhalika.

Kwa vyanzo hivi Serikali iliweza kukusanya mapato yaliyowezesha kuendesha Serikali bila matatizo. Palikuwa na Baitil-Mali(Hazina). Mali ya Serikali ilitumika kwa mujibu ya maelekezo ya mafungu yake, maendeleo ya nchi na wananchi kwa ujumla.

Maendeleo ya nchi yaliyopatikana wakati wa Makhhalifa ni pamoja na ujenzi wa mifereji(Canals). Katika Ukhalifa wa 'Umar(r.a) ulijengwa mfareji kutoka mto Euphrates hadi Basra kuliko kuwa na ukame wa maji. Mfareji huu uliitwa kwa jina la Gavana wa Basra, "Canal Abi Musa". Mifereji mingine iliyojengwa kutoka Mto Euphrates ni "Canal Maakal na Canal Saad" iliyopeleka maji sehemu mbali mbali zilizokuwa kame.

Mfareji mwingine maarufu ni ule uliunganisha mto Nile na Red See (Bahari ya Shem) ambao uliitwa kwa jina la "*Canal Amirul-Muuminina*".

Maendeleo mengine yaliyofanywa kutokana na pato la Serikali katika kipindi cha Makhhalifa ni ujenzi wa barabara na madaraja, majengo ya ofisi, nyumba za wafanyakazi, ngome na kambi za jeshi, nyumba za wageni, majengo madhubuti ya Baitul-Mali na magereza. Visima na vituo kadhaa baina ya Makkah na Madina vilijengwa. Miji nayo ilianzishwa na maarufu katika hiyo ni Basra, Kufa, Fustat na Mosul.

Kazi ya ujenzi wa misikiti na upanuzi wa misikiti ya Makkah na Madinah ilishamiri katika kipindi cha Makhhalifa. Misikiti elfu nne (4,000) inakadiriwa kujengwa katika Ukhalifa wa 'Umar(r.a). Misikiti ya Makkah na Madina ilipanuliwa kwa kununua nyumba za majirani katika kipindi cha 'Umar na 'Uthman(r.a).

## **Ulinzi na Usalama**

Wakati wa Ukhalifa wa Makhhalifa wanne waongofu ulinzi ulimarishwa kwa kiwango kikubwa. Wakati wa Mtume(s.a.w) hakukua na jeshi maalum. Kila mtu alikuwa askari na vita ilipofika Waislamu walijitokeza wakapewa mafunzo na kwenda vitani. Ni kweli pia kuwa katika Dola ya Kiislamu kila Muumin ni askari wa Allah(s.w) na wakati wowote anapotakiwa ni lazima awe tayari kupigania dini ya Mwenyezi Mungu.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا هَلْ أَذَلُّكُمْ عَلَىٰ تَجْرِقَةٍ تُنَجِّيْكُمْ مِّنْ عَذَابٍ أَلِيمٍ  
 تَوْمُنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَتُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِكُمْ  
 وَأَنْفُسِكُمْ..... ﴿١١﴾

*“Enyi mlioamini Je! Nikujulisheni biashara itayokuokoeni na adhabu iumizayo Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na piganieni dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na nafsi zenu.....” (61:10-11)*

﴿ إِنَّ اللَّهَ اشْتَرَىٰ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنْفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ بِأَبْلِهِمْ  
 الْجَنَّةَ يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيَقْتُلُونَ يُقْتَلُونَ ..... ﴾ ﴿٩﴾

*Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waislamu nafsi zao na mali zao ili nae awape Pepo. Wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu wanauwa na wanauwawa.....” (9:111)*

Ni dhahiri Waislamu ni askari wa Mwenyezi Mungu. Pamoja na hivi tangu wakati wa Khalifa wa pili Umar, liliundwa jeshi kama yalivyo majeshi ya kileo. Khalifa ndie aliyekuwa mkuu wa majeshi, aliteua kamanda wa jeshi na makamanda wa mikoa na wilaya.

Idara ya ulinzi ilianzishwa na askari wote waliorodheshwa na utaratibu wa mshahara na posho ulianza kutumika kwa askari wa kudumu, wakujitolea na wale waliopigana vita vya awali kama Badr, Uhud, n.k.

Nchi iligawanywa kwenye maeneo ya kiulinzi, makao makuu ya maeneo haya yakawa Madina, Kufa, Basra, Mosul, Fustat, Damaskas, Hems, Jordan na Palestine. Katika sehemu zote hizi kambi zilijengwa kwa ajili ya askari. Mashamba ya mifugo yalipanuliwa kwa matumizi ya farasi na ngamia wa vita.

Pamoja na askari wa farasi na wa miguu jeshi la maji lilianza katika Ukhaliifa wa Uthman. Vita vya kwanza vya majini vilipiganwa na Muawiya alipovamia Cyprus mnamo mwaka wa 28 A.H. Makao makuu ya Jeshi la maji yalikuwa Alexandria Misri.

## Usalama wa Taifa

Idara ya usalama ilikuzwa. Ilianza tangu wakati wa Mtume(s.a.w) na kuendelezwa wakati wa Makhalifa wanne. Walitumika wanajeshi na wasio wanajeshi katika kazi ya kupata habari ndani na nje ya Dola na hasa kujua

mwenendo wa adui. Wapo Machief, kwa mfano Syria, waliochaguliwa kuwa wanausalama, kuchunguza mwenendo wa Warumi. Palestine lilikuwepo kundi la Wayahudi lililojulikana kwa jina la Samara lilijizatiti katika upelelezi. Khalifa Umar(r.a) aliweka wapelelezi ndani ya jeshi (military intelligence) ili apate habari zote. Hivyo idara hii nayo ilisaidia sana katika ulinzi na usalama wa Dola ya Kiislamu.

Hivi ndivyo Serikali ya Kiislamu ilivyoendeshwa kwa muda wa miaka 40 kuanzia kwa Mtume(s.a.w) hadi Makhalifa wake wanne na imekuwa ndio msingi wa uendeshaji wa Serikali zote za leo Duniani.

## **Upinzani Dhidi ya Dola ya Kiislamu Wakati wa Makhalifa**

Katika kipindi cha Makhalifa wanne wa Mtume(s.a.w), maadui wa Dola ya Kiislamu ni wale wale waliokabiliiana na Mtume na kuainishwa katika Qur-an japo walitofautiana kimbinu kulingana na mazingira. Maadui wakubwa walioainishwa katika Qur-an ni:

- (i) Adui mkubwa – Sheitwaan (katika Majini na Watu) anayepambana kwa kuishawishi na kuipambia nafsi ya mtu imuasi Mola wake.
- (ii) Makafiri na Washirikina – Wanaotaka mifumo yao ya maisha iwe juu ya Uislamu.
- (iii) Wanafiki – wanaotaka kuishi maisha ya mseto baina ya Uislamu na ukafiri kwa ajili ya maslahi ya dunia.
- (iv) Mayahudi - husuda na chuki yao dhidi ya Uislamu ilibainika tangu wakati wa Mtume(s.a.w) - kwa ajili ya kuipenda dunia kuliko akhera.
- (v) Wakristo wanachuki na husuda dhidi ya Uislamu kama Mayahudi.

## **Uasi wa Dola (Riddah)**

Habari za kutawafu kwa Mtume(s.a.w) zilipelekea makabila mengi ya Kiarabu yaliyokuwa chini ya himaya ya Dola ya Kiislamu kuasi. Tukio hili katika vitabu vya tarekh huitwa Riddah kwa Kiarabu na apostasy kwa Kiingereza.

Kwa ujumla dola ya Kiislamu wakati wa ukhalifa iligawanyika katika makundi sita ya watu. kuna waliobakia na Uislamu wao bila kutetereka hasa watu wa Madina, Taif na Makka. Wanafiki ni kundi lililokuwepo na hila zao za mwisho ziligonga ukuta mwaka mmoja tu kabla ya kutawafu kwa Mtume(s.a.w). Hivyo walikuwa macho kuvizia fursa yoyote iliyopatikana waitumie. Kulizuka kundi la Waislamu waliobakia Waislamu lakini walikataa kupeleka Zaka Madina kwa hoja kuwa itumike kuwasaidia wasiojiweza katika eneo lao.

Wapo waliobaki Waislamu lakini walikataa kulipa Zaka kabisa. Kundi lingine ni lile lililoritadi na kurudia dini zao za asili. Kundi lingine ni wale mitume wa uwongo waliojitangazia utume tangu wakati wa Mtume na sasa wakaongezeka kufikia wanne. Ikumbukwe pia wakati wa majilio ya wajumbe mbali mbali kwa Mtume(s.a.w) yapo makabila ambayo hayakusilimu ila yaliitambua Dola ya Kiislamu wakawa wanalipa Jizya. Mfano ni kabila la Hanifa la sehemu ya Arabia ya kati. Wayahudi nao ambao siku zote walikuwa maadui wa Mtume(s.a.w) si kuwa tu wametolewa Madina lakini hata huko Khaibar walikohamia walishindwa na kulazimishwa kuutambua utawala wa Kiislamu na kulipa Jizya.

Sio Wayahudi tu bali Wakristu wa Najran na Urumi waliazimia kuiangamiza dola ya Kiislamu kwa vile wote walikuwa wanalipa Jizya. Hivyo ni dhahiri uasi katika dola ya Kiislamu ulikuwa mkubwa. Dola yote ya Kiislamu ilisambaratika, maadui walikuwa wengi na waliobakia na utii kwa Dola ni miji baina ya Madina, Makka na Taif. Kabla ya kutazama hatua alizochukua Abubakr Siddiqi ni vyema kwanza tuchambue sababu zilizopelekea uasi huu.

## Sababu Zilizopelekea Uasi

Kwa wale waliosilimu kisha baada ya kutawafu Mtume walikataa kulipa Zaka na wale waliokubali kulipa Zaka lakini wakajenga hoja kuwa hawatapeleka Madina lakini itumike kwa watu wao; makundi yote haya Sababu yao kubwa ya kufanya hivi ni udhaifu wa Imani kama isemavyo Qur'an:

﴿ قَالَتِ الْأَعْرَابُ ءَأَمْنَا قُل لَّمْ تُؤْمِنُوا وَلَكِن قُولُوا أَسْلَمْنَا وَلَمَّا

يَدْخُلِ الْإِيمَانُ فِي قُلُوبِكُمْ ..... ﴾

*Walisema wanaokaa jangwani (kumwambia Mtume) "Tumeamini" Sema uwaambie Hamjaamini, Lakini semeni Tumesilimu maana imani haijaingia nyoyoni mwenu bado..... (49:14).*

Ama kwa wale waliorudia dini zao za awali walikuwa na sababu mbili, moja ya kiuchumi ya kulinda biashara zao na mali zao kwa kuondokana na kulipa Jizya na pili kulinda hadhi zao na nafasi zao katika koo na mila. Sababu hizi pia ndizo zilizopelekea uasi kwa wale waliokuwa hawakusilimu lakini walikuwa wanalipa Jizya. Na kwa wale waliodai utume na walioungana nao pamoja na sababu zilizotajwa walikuwa na husda na uroho wa mamlaka. Bado ipo hoja inayowahusu Waarabu wote, wengi wao walizoea maisha yasio na mpangilio maalum, yasiyo na nidhamu na hawakuzoea kutoa utii wao nje ya koo zao au makabila yao. Mabadiliko yaliyoletwa na Mtume(s.a.w) yaliwaweka katika mfumo wa maisha wenye nidhamu wasioitaka. Waliukubali wakati wa Mtume(s.a.w.) kwa kuwa walikuwa hawana jinsi. Kutawafu kwa Mtume(s.a.w)



kulitoa nafasi siyo tu ya kujitenga na utawala wa Madina bali walikusudia kuuhilikisha kabisa. Kwa upande wa Wayahudi na Wakristu ni kweli waliasi kulinda tawala zao na utukufu wao lakini kulinda dini (itikadi) zao pia kulitoa msukumo mkubwa. Sababu hizi na nyinginezo ambazo huenda hatukuzitaja zaweza kuwa ndio chimbuko la “Riddah”.

## **Kukomeshwa kwa Riddah na Chokocho Nyingine**

Miongoni mwa makabila yaliyovamia Madina ni Bani Abbas na Zukian. Makabila haya yalipokuwa yanakimbilia Rabaza baada ya kushindwa kuivamia Madina waliwaua kikatili watu wa makabila yao ambao hawakuasi. Khalifa Abubakar aliongoza msafara wa kuwafukuza. Adui alishindwa, wengi waliuliwa na baadhi yao kuchukuliwa mateka. Khalifa Abubakar, kwa ujumla aliendesha vita dhidi ya makundi yote ya waasi na muda mfupi akaurudisha utulivu wa Dola ya kiislamu kama alivyoiacha Mtume(s.a.w). Si tu kuirudisha Dola katika hali ya utulivu, bali kuifanya Dola kuimarika zaidi kijeshi na kiusalama.

Mitume wa uongo nao ambao idadi yao ilikuwa wanne walinyamazishwa. Mitume bandia hawa ni **Aswad Ausi, Tulaiha, Sajah bint Alharith na Musailamah Al-kadh-dhab(mzandiki)**. Aswad alitangaza utume wake Yemen baada ya kukusanya jeshi kubwa. Mtume huyu wa uwongo aliyekuwa anajitanda uso wote hata akaitwa mtume anayejitanda aliuliwa na Qais ibn Makshuh aliyekuwa chifu wa Waarabu akishirikiana na Feroze Dailme na Darweih.

**Tulaiha** anatoka katika kabila la Bani Asad kaskazini mwa Arabia. Mara baada ya kifo cha Mtume, alijitangazia utume. Khalifa Abubakar alimtuma Khalid bin Walid kuzima uasi huu. Khalid alikuwa jemadari mwenye kipaji cha kupigana na amerikodiwa kuwa miongoni mwa majemadari wa dunia. Mtume(s.a.w.) kwa uhodari wake alimwita “Upanga wa Mwenyezi Mungu”. Khalid alishinda makabila yote yaliyokuwa yanamuunga mkono Tulaiha, wakiwemo Bani Tay, Bani Ghatfan na Bani Asad. Katika vita vilivyopiganiwa mahali paitwapo Bozakha, Jeshi la adui liliongozwa na Uyeina. Tulaiha alikimbilia Syria na mkewe, Uyeina alikamatwa mateka na kupelekwa Madina pamoja na watemi wengine wawili ambako baada ya kuomba msamaha walisamehewa.

**Sajah bint Al-Harith** anatoka katika kabila la Bani Tamim. Baada ya kifo cha Mtume(s.a.w.) watemi wengi wa kabila hili waliritadi ndipo Sajah akajitangazia utume. Sajah alikusanya watu elfu nne tayari kuelekea Madinah. Alipokuwa anakwenda Madina akapata habari za jeshi la Khalid bin Walid lililomuamgamiza Tulaiha. Aliingiwa na khofu kwenda Madinah. Kwa udhuru huu akamuandikia Musailamah Mzandiki washirikiane ambaye naye alikwisha tangaza utume wake. Sajah aliungana na Musailamah mzandiki na kutambua utume wake. Wakati huo huo, Khalid bin Walid alifika makao makuu ya kabila la Bani Tamim na kutuliza uasi. Baada ya kutuliza fujo za kabila la Bani Tamim Khalid alimgeukia Musailamah Al-kadh-dhab.

Katika siku za mwisho za Utume katika mwaka wa kumi Hijriya(10 A.H.) Musailimah aliyeishi katika kitongoji cha Yamen (kakatikati ya Bara Arab) katika kabila la Bani Hanifa alijitangazia utume na akamuandikia Mtume (s.a.w.) juu ya utume wake na kumtaka wagawane Dunia nusu kwa nusu katika kuiendesha. Mtume (s.a.w.) alimjibu:

*“Kutoka kwa Muhammad, Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenda kwa Musailimah alkadhab (mzandiki). Dunia iko chini ya ufalme wa Mwenyezi Mungu na humuachia kuitawala amtakaye. Na mwisho mwema ni wa wakweli.”<sup>12</sup>*

Musailimah alikuwa na wafuasi wengi. Hivyo alikusanya jeshi la watu arobaini elfu lililopigana na jeshi la Waislamu la watu elfu kumi na tatu liliongozwa na Khalid bin Walid. Ikrima na Shurahbil walitangulia lakini walishindwa. Kuwasili kwa Khalid kuliwapelekea kukusanya nguvu na kufikia askari kumi na tatu elfu dhidi ya adui aliyekuwa na jeshi la watu arubaini elfu. Pambano hili ambalo matokeo yake yalikuwa “Bustani ya Vifo”, lilikuwa kali sana na lenye matokeo ya kuelemeza kwa adui. Waislamu waliwaangamiza Bani Hanifa na wasaidizi wao, wakawauwa adui 21,000 (ishirini na moja elfu) akiwemo na *Musailimah* aliyeuuliwa na *Wahshiy* aliyemuua Hamza katika vita vya Uhud. Waislamu waliouawa ni mia nane (800) wakiwemo maswahaba 360 (mia tatu sitini) wengi wao wakiwa mahifadhi wa Qur’an. Vita hivi vilipiganwa mnamo mwaka 633 A.D. au 11 A.H. vilichukua miezi Saba. Vita vya Yamama vilimalizia uasi wa Riddah na Dola ikarudia utulivu.

Chokochocho nyingine dhidi ya uongozi wa Abubakar zilitoka kwa Waajemi (Persians) waliokuwa washirikina na Warumi au Dola ya Wakristo wa Kirumi. Abubakar, aliwahamasisha Waislamu kuingia katika Jihad ili kuihami Dola ya Allah(s.w). Moja ya barua aliyoandika katika kuhamasisha Waislamu ni hii:

*K”utoka kwa Khalifa wa Mtume(s.a.w) kwenda kwa Waislamu wote wanaume na wanawake wa Yemen. Nawasalimia wote wanaosomewa barua hii. Namshukuru Mwenyezi Mungu anayepaswa kuabudiwa. Mwenyezi Mungu ameifaradhisha Jihad na kuwaamuru (waumini) waitekeleze wakiwa katika halinzuri au hali ngumu, wanatakiwa wajitokeze kwenda katika Jihad kwa mali zao na nafsi zao. Jihad ni wajibu na malipo yake ni makubwa. Nawasihii Waislamu mjitokeze kwenda kwenye Jihad dhidi ya Warumi wa Syria. Enyi waja wa Mwenyezi Mungu, shirikini katika Jihad kwa ikhlaswi. Hamtakosa moja ya zawadi hizi, ama kufa Shahid au ushindi na ngawira .....”<sup>13</sup>*

Waislamu walihamasika na kujitokeza kwa wingi na kuwashinda maadui zao ushindi wa kishindo katika Ukhalifa wa Abubakar, ‘Umar na Ukhalifa wa ‘Uthman pale Waislamu walipokuwa hawajaanza kugombana wenyewe kwa wenyewe.

## **Kuporomoka kwa Dola ya Kiislamu Aliyoicha Mtume(s.a.w)**

Dola ya Kiislamu ilianza kuporomoka katikati ya Uongozi wa Khalifa 'Uthman palipotokea fitna iliyowapelekea Waislamu kugombana wenyewe kwa wenyewe kiasi cha kuwafikisha mama wa waumini, Aysha(r.a) mkewe Mtume(s.a.w)na Ali bin Abu Taalib(r.a) kupambana kijeshi. Fitina hii ilipelekea kuuliwa kwa Uthman (r.a) na Ali(r.a) na kusambaratika kwa Dola ya Kiislamu na kuanza uongozi wa Kifalme. Mzizi wa Fitna hii ni Myahudi '*Abdallah bin Sabaa*' wa Yemen aliyesilimu kinafiki. Ili kupata mafunzo ya kina Waislamu hatuna budi kuipitia kwa makini historia hii ya kusikitisha, iliyopelekea kusambaratika kwa dola ya Kiislamu, katika kipindi cha Khalifa 'Uthman na Ali.

### **Upinzani Kutoka Miongoni mwa Waislamu**

Ukhalifa wa Uthman ulichukua miaka 12. Katika miaka sita ya mwano Dola ya Kiislamu iliimarika na mipaka yake kupanuka . Katika miaka sita aliyomalizia ukhalifa wake kulikuwa hakuna utulivu: Miongoni mwa Waislamu walizusha malalamiko ya uongo dhidi ya Khalifa na Serikali yake. Kiongozi wa kundi hili la wapinzani ni 'Abdullah Ibn Sanda alijulikana sana kwa jina la Ibn Sanda au Ibn Sabaa. Ibn Sanda alikuwa Myahudi anayetoka Yemen, alisilimu kinafiki kama alivyosilimu 'Abdallah bin Ubay wa Madinah, lakini ibn Sabaa tangu aliposilimu alikuwa tayari na mpango wake wa kuudhuru Uislamu hatua kwa hatua. Kundi la wanafiki lililoongozwa na Ibn Sabaa lilitumia shutuma dhidi ya Khalifa na Serikali yake kuficha unafiki wao kwa sababu madai yao yalikuwa ni ya uwongo na pale walipopewa maelezo ya kweli waliyafumbia macho na hawakuyakubali.

### **Madai Dhidi ya Khalifa Uthman**

Upinzani mkubwa ulitokea Misri ambapo 'Abdallah bin Sa'ad aliteuliwa badala ya Amri bin al As. Abdallah hapana shaka ni ndugu wa Uthman lakini mchango wake katika Uislamu ulikuwa mkubwa sana. Ndiye aliyeanzisha jeshi la majini la Dola ya Kiislamu na ushindi wake Afrika ya kaskazini. Ushindi huu ulionesha kuwa Abdallah bin Sa'ad alikuwa na uwezo wa kuongoza hivyo Khalifa alikuwa sahihi kumpa ugavana na hapana upendeleo hapa. Hata hivyo wanafiki hawa alipovamia Madinah na kudai kuwa hawamtaki Gavana Sa'ad; Khalifa alimbadiilisha na kumuweka mtu wanayemtaka, Muhammad bin Abubakar.

Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kuwa Khalifa Uthman hakuwa na upendeleo kwa ndugu zake kwa kuwapa nafasi za ugavana. Kama angekuwa nao ni dhahiri asinge waachisha kazi na pale walipokosea kuwachapa. Isitoshe magavana hawa waliteuliwa mwanzoni mwa ukhalifa wake wakati akipendwa kama Khalifa Umar. Ni kweli Uthman aliwavua madaraka baadhi ya magavana kama alivyofanya Umar kwa manufaa ya uislamu.

Dai linge liliopikwa na wanafiki wa kundi la Sabaa ni matumizi mabaya ya pesa za Serikali (Baitul-mal). Khalifa alisingiziwa kuwa anatumia vibaya pesa za Serikali na kuwapa ndugu zake. Dai hili halikuwa la kweli kabisa kwa Sababu zifuatazo:

Uthman alikuwa tajiri mkubwa Arabia hata akaitwa “Ghanir” (mtu tajiri). Lakini hakuwa tajiri tu lakini anajulikana kwa mchango wake katika njia ya Uislamu wakati wa Mtume(s.a.w.) na baada ya Mtume(s.a.w.) wema wake uliendelea. Katika Ukhalifa wake alitumia mali yake mwenyewe kusaidia maskini na ndugu zake. Katika ukhalifa wake kwa muda wote wa miaka 12 hakuchukua posho kwa ajili ya ukhalifa wake kutoka kwenye Baitul-Mal. Kulikuwa na zogo kubwa wakati Khalifa alipotamka kumpa zawadi Abi Sarh 1/5 ya ngawira ya Afrika ya kaskazini kwa kazi nzito aliyofanya ya kuteka Afrika kaskazini kama motisha. Jambo hili lilipolalamikiwa na watu, Khalifa alimtaka Sarh arudishe ile ngawira na akafanya hivyo. Vile vile ikasemwa kuwa amemruhusu mpwae Marwan anunue kasma ya Serikali ya mateka. Jambo hili na mengine kuhusu tuhuma hii kama kweli au sikweli tusome hotuba ya Khalifa mwenyewe.

“Watu wa Madina wanasema, nina pembe laini kwa ajili ya ndugu zangu na ninawafanyia wema (ninawapendelea ndugu zangu). Lakini kuwapenda kwangu hakuathiri haki ya mtu yeyote. Ninawapa wanachostahiki kutokana na mali yangu. Sijafikiria kujihalalishia mali ya Serikali kwa ajili yangu au mtu mwingine yeyote. Wakati wa Mtume, Abubakr na Umar nilitoa mali nyingi ingawa nilikuwa naipenda na bakhili. Hivi sasa niko ukingoni mwa uhai wangu na nimewaachia watoto na ukoo wangu, makafiri wanaeneza madai ya uzushi dhidi yangu. Hakuna mji uliotozwa kodi kwa ajili ya kufuja mali, bali kwa manufaa ya wananchi, Nina hisa ya moja ya tano, lakini sichukui kitu chochote kwa ajili yangu, inatumiwa na Waislamu wanaostahiki. Katika mali ya Mwenyezi Mungu hakuna kinachoibwa wala sichukui kitu. Ninaishi kwa kutegemea kipato changu”.<sup>14</sup>

Shutuma nyingine aliyotupiwa Khalifa Uthman ni kuchoma moto Qur’an. Dai hili pia si la kweli. Ukweli ni kuwa Uthman alituma nakala za Qur’an inayotokana na ule msahafu asili na kuamuru nakala nyingine zote zichomwe moto. Alichukua hatua hii kwa sababu zilikuwepo naksi za Qur’an zisizokuwa na mpangilio wa Mtume kwa mujibu wa aya na sura kama Jibrili alivyomuelekeza Mtume. Baadhi ya nakala zilizokuwa nje ya Madina zilikuwa hazikukamilika. Hali kadhalika miandiko tofauti ilileta tofauti. Tofauti nyingine ilikuwa ile ya usomaji. Hivyo ni dhahiri misahafu haikuchomwa na dai hili kama mengine ni la uwongo kwani kwa kazi hii Uthman amepewa jina la Jami-ul-Quran (mkusanyaji wa Qur’an).

Hata kazi ya kupanua eneo la Kaaba, na msikiti wa Madina ililaumiwa. Kazi ya upanuzi wa eneo la Kaaba ilianzwa na ‘Umar na Uthman aliendeleza. Wenye nyumba za karibu zilizovunjwa walikataa kuchukua fidiya, na kuanza kulalamika. Baadhi ya maswahaba walipinga kutumia fedha za Serikali

kupanulia msikiti wa Madina na uwanja wa Kaaba. Hata hivyo mnamo mwaka 29 A.H. Uthman aliamua kupanua msikiti wa Madina kwa pesa zake. Magogo ya miti yaliondolewa na kuta zikajengwa kwa matofali. Hebu ona kama sio unafiki na ukafiri kazi ya kurekebisha msikiti na upanuzi wa uwanja wa Kaaba ni vya kulalamikiwa, tena kwa gharama ya Khalifa mwenyewe ?

Lawama nyingine ambayo ni kuhusu mjomba wa Uthman Hakam Ibn Al-Aas ambaye alikuwa akiwatendea vibaya jirani zake na kumcheza shere Mtume. Alihamishwa Madina. Baada ya miaka michache Uthman alimuomba kwa Mtume na baada ya kuombwa mara nyingi Mtume aliahidi kulitazama upya suala hilo. Mtume alipokufa jambo hili lilikuwa halijapatiwa ufumbuzi. Uthman aliwaomba Abubakr na Umar wamrejeshe kutoka uhamishoni katika ukhalifa wao, lakini hawakuruhusu. Katika ukhalifa wa Uthman alimrudisha mjomba wake baada ya miaka 17 ya kuishi uhamishoni. Hili nalo limemfanya Khalifa kulaumiwa.

Hadithi zikavumishwa kuwa Khalifa amewanyanyasa baadhi ya maswahaba mfano unaotolewa ni wa Abu Dhar Ghifari. Swahaba huyu alikuwa mchamungu kama maswahaba wengine ila yeye alichukua muelekeo wa kisufi. Kwa imani yake hii alilaumu waliokuwa wanaishi maisha ya kujiweza hasa baada ya watu kupata utajiri kutokana na ngawira. Hali kadhalika alitaka Baitul Mal, pasiwe na salio. Fedha au mali igawiwe na itumike kadiri inavyokuja. alianza kueneza imani yake hii Syria. Gavana wa jimbo la Syria, Amir Muawiya alimuandikia Khalifa kumfahamisha juu ya shughuli za Abu Dhar Ghifari. Khalifa Uthman alimwita Abu Dhar Madinah. ‘Abdallah bin Sabaa alijaribu kumuomba alipokuwa Syria lakini Gavana Muawiya alimwambia imani anayofundisha ni mpya katika Uislamu na nia yake nikuleta mtafaruku miongoni mwa Waislamu.

Abu Dhar alipofika Madinah alijadiliana na Khalifa. Khalifa alimuuliza Abu Dhar: “Watu wakishatekeleza wajibu wao mimi nina mamlaka gani ya kuwataka watoe zaidi?” Abu Dhar alipoona hakuweza kumbadili Khalifa alikwenda kuishi kijiji cha Rabdhah karibu na Madinah na alifika hapo. Wanafiki waligeuza maneno na kusema kuwa Abu Dhar alitakiwa aishi kijijini hapo kwa amri ya Serikali hivyo alinyanyaswa. Ni dhahiri Khalifa hata kama alifanya hivyo alikuwa sahihi kwa vile ni kweli imani ya Abu Dhar haikuwa ya Kiislamu. Inasemekana pia kuwa maswahaba aliowanyanyasa ni pamoja na Ammar bin Yasir na ‘Abdullah bin Masud. Dai hili ni la uongo kama tulivyoonesha. Lakini linathibitika zaidi wakati Abu Ammar alipoteuliwa kuwa miongoni mwa wajumbe wa kwenda mikoani kuchunguza matatizo ya magavana.

Khalifa Uthman anatoka ukoo wa Banu Umayyah wa makureish. Kabla ya kuzaliwa Mtume(s.a.w) kulikuwa na kutoelewana baina ya ukoo wa Banu Ummayah na ukoo wa Banu Hashim anaotoka Mtume ambao nao ni wa Kikureish. Wasabaai waliwashawishi ukoo wa Banu Hashim kuwa Khalifa anapendelea ukoo wa Banu Ummaya kwa kuwapa nafasi za juu na kuwaondoa madarakani ukoo wa Banu Hashim.

Dai lingine ambalo halina msingi kama mengine linahusu mashamba ya Serikali ya kuchungia wanyama. Mtume(s.a.w.) alianzisha mashamba ya Serikali ya kuchungia wanyama. Umar aliongeza mawili. Wakati wa Uthman Farasi na ngamia wa Serikali waliongezeka. Kwa sababu hii Khalifa aliongezea mashamba ya kuchungia wanyama wa Serikali. Uzushi ukawa Khalifa ameruhusu ukoo wake wa Banu Ummaya uchungie wanyama wao katika shamba la Serikali.

Wingi wa vita ulilazimisha matumizi makubwa ya fedha kwa kuimarisha jeshi kwa kununua zana na vifaa vya jeshi la majini. Pamoja na ngawira iliyokuwa inatumika kwa kuimarisha jeshi. Uthman alitumia Zaka na Sadaqa kuimarisha ulinzi. Wapinzani wake wakashutumu kuwa, Zaka na Sadaqa zina matumizi yaliyotajwa kwenye Qur'an hivyo haikuwa sahihi kutumia kwa kuimarisha jeshi. Hiki ni kichekesho kwani moja ya matumizi ya Zaka na Sadaqa ni kuimarisha dini ya Allah(s.w). Ulinzi nao huimarisha dini ya Allah(s.w). Hata hivyo Khalifa alieleza kuwa alitumia fungu kwa kuliazima na atalirudisha.

Malalamiko mengine yaliyotolewa na wanafiki wale ni kuswali swala kamili bila kupunguza katika Hija, kupiga mahema Minna na kutoza Zaka farasi - mambo ambayo wakati wa Mtume(s.a.w.) wala wa Abubakar na wa Umar hayakufanywa. Kuhusu kutopunguza swala Khalifa alipoulizwa alisema nimefanya hivyo ili wakazi wa maeneo hayo wasidhanie kuwa kupunguza swala ndio utaratibu. Ama kuhusu mahema ni suala la maendeleo na kwa watu wa leo ni jambo halina msingi kabisa. Kwa vile mahema na nyumba za kitalii zinatumika sio Minna tu bali hata Makka. Ama kuhusu farasi kutozwa au kutotozwa Zaka wakati wa Mtume na makhaliifa wawili wa mwanzo yaweza kuwa uchache wao na kushiriki kwao kwenye vita. Wakati wa Khalifa Uthman na baada ya mfululizo wa vita hali ya uchumi ya Waarabu ilibadilika na Khalifa aliona ni Busara Zaka pia itolewe kwa farasi kama ilivyo kwa ngamia.

Sababu hasa ya chanzo cha ghasia hatimaye kumuua Khalifa Uthman hazikuanza wakati wa Uthman bali zilianza wakati wa Mtume(s.a.w.). Maadui wa Uislamu wakati wa Mtume walikuwa Maqureysh, Waarabu, Wayahudi, Wapersia na Wakristu wa Kirumi. Baada ya kutekwa Makka koo na makabila mengi yalisilimu, lakini walisilimu kwa nia mbali mbali ambapo hapa hatutazitaja. Linalothibitisha hili ni kule kuukana Uislamu kulikotokea mara tu baada yakutawafu Mtume(s.a.w), uasi ambao uliikumba karibu Arabia yote. Wapinzani hawa walishindwa nguvu wakati wa Abubakar halikadhalika wakati wa Umar. Lakini haiyumkini kuwa walikuwa wameridhika na ustawi wa uislamu. Kwa hiyo hili ni kundi moja ambalo miongoni mwao walitokea wapinzani.

Kundi la pili la wapinzani linatoka kwa wanafiki ambao njama yao ya kumuua Mtume ilitajwa kwenye Qur'an na hila zao kubainishwa mwaka wa 9 Hijria na hiki kilikuwa kipigo kikubwa kwao. Kubadilika kwa sera ya kuwataja wanafiki bayana na Mtume kukatazwa kuwaombea na kuwazika na kutotambulika katika jamii ya Waislamu kulistawisha chuki dhidi ya viongozi wa Waislamu.

Kifo cha Mtume kiliwagawa Waislamu katika makundi matatu. Ukoo wa Mtume(Ahlul Bayt), Muhajirin na Ansaar. Pamoja na kuwekwa sawa hali hii wapo walioendeleza vikundi vyao nyoyoni na hasa pale upinzani ulipochukua umbo la kuonesha makosa Serikalini. Bado lilikuwepo tatizo la watu binafsi. Wapo Waislamu waliojiingiza katika upinzani kwa maslahi yao binafsi. Mfano mzuri ni Muhammad bin Abubakar na Muhammad bin Hudhaifa.

Wayahudi nao hawakusahau kutolewa kwao Madinah na hata huko Khaibar walikohamia bado walitezwa nguvu na kulazimika kulipa Jizya. Makundi yote haya yaliungana kwa kujuana na kutokujuana kwa kusimamisha upinzani dhidi ya Khalifa Uthman na Serikali yake na hatimaye kumuua.

## **Fitna za Abdullah bin Sabaa**

Pamoja na makundi mengi haya, kiongozi wa udhia wote huu ni Myahudi aliyekuwa mkazi wa Yemen aliyejulikana kwa jina la Abdullah bin Sabaa. Sabaa hakuwa anautaka Uislamu na alipanga mpango wa kuudhuru. Mbinu aliyotumia ni kuingia katika Uislamu na kuupiga vita kutoka ndani.

Kwa kutumia hali ya mazingira ya wakati ule alitunga na kuhubiri imani zisizokuwemo katika Uislamu ambazo ni kila Mtume aliacha “*Was*” (mrithi wake katika ujumbe wake) na *wasi* wake alikuwa ndugu yake, kwa mfano Mtume Musa(a.s) alimfanya Haruna kuwa “*Was*” na Mtume(s.a.w) *wasi* wake ni ndugu yake Ali. Na Ali alikuwa mtu pekee aliyestahiki kupewa Ukhalifa. Sabaa alifikia kiwango cha kusema kuwa makhalifa watatu waliotangulia Abubakar,Umar na Uthman sio halali. Namna pekee ya kurekebisha mambo ni kumuondoa Khalifa Uthman madarakani.

Ibn Sabaa pia alifundisha imani ya kurudi kwa Mtume(s.a.w). Alikuwa akishangaa kuwa ni ajabu kuamini kuwa Nabii Isa(a.s) atakuja kutoka mbinguni ili afuate Uislamu na kuupigania dhidi ya maadui na kuamini kuwa Mtume Muhammad(s.a.w) hatarudi. Ibn Sabaa aliamini na kufundisha kuwa kwa kuwa Mtume Muhammad(s.a.w) ni bora kuliko Isa(a.s) na kwa kuwa yeye Muhammad(s.a.w) ndiye Mtume wa mwisho, basi atarudi. Hali kadhalika Ibn Sabaa alitoa tafsiri potofu za aya za Qur'an ili kubatilisha itiqadi zake.

Madina hakupata wafuasi, hivyo alikwenda Basra na kuendesha shughuli zake za upinzani dhidi ya Serikali. Gavana wa Basra Abdallah bin Amir alimwita na kumhoji kwa sababu hii Ibn Sabaa aliogopa akaondoka Basra na kuwacha wafuasi wake chini ya uwongozi wa Hakim Hublah adui wa Gavana.

Kutoka Basra alikwenda Kufa ambako alipata wafuasi wengi. Gavana, wa Kufa, Sa'd bin al As alimwita Ibn Sabaa na kumuonya juu ya udhalimu anaoufanyia Uislamu. Hatua hii ilimfanya ahame Kufa aende Damascus ambako hakufanikiwa lakini alimteua Ashtar kuwa naibu wake na kuacha maelekezo

kuwa ujumbe wake uendelee chini chini na yeye akahamia Misri. Ambako kwa kuwa Gavana wa Misri Abdallah bin Sarah alikuwa katika vita vya Warumi, Ibn Sabaa alipata muda wa kupandikiza fikra zake potofu akapata wafuasi wengi na kuweza kuwasiliana na vituo vyake vya Kufa na Basra.

Wafuasi wa uasi huu, walitumia mikakati mingi ya kujiimarisha. Walijionesha kuwa ni wacha Mungu na kushawishi watu waunde malalamiko dhidi ya Maafisa wa Serikali, Magavana na Khalifa. Walitawanya barua za kuonesha udhalimu wa Serikali hali ni madai ya uzushi. Barua hizi zilitumwa kwa wafuasi wa Ibn Sabaa nao wakawa wanazisoma hadharani. Walionesha kuwa Ali, Talha na Zubair, Maswahaba maarufu kwa wakati ule, waliwaunga mkono ili kuunda taswira ya kuonesha kuwa kweli Serikali ina matatizo.

Pamoja na barua watu walijajiwa kuendeleza madai dhidi ya Serikali na Khalifa. Hapo awali tulieleza kuwa wapo watu waliojiunga na ghasia za Ibn Sabaa kwa sababu zao binafsi wakiwemo Ammar bin Yasir, Muhammad bin Abu Hudhaifah na Muhammad bin Abubakar. Muhammad bin abu Hudhaifa alilelewa na Uthman tangu udogo kwa kuwa alikuwa yatima. Alitegemea apate nafasi kubwa katika Serikali alipoona hapati akaenda Misri kujiunga na wahaini. Ni hivyo hivyo kwa mtoto wa Abubakar. Alikuwa na kesi ya kudaiwa. Khalifa Uthman alihukumu kwa haki dhidi ya Muhammad bin Abubakar. Muhammad akaona kaonewa akaenda Misri kujiunga na Ibn Sabaa. Ammar alikuwa miongoni mwa maswahaba wanne waliotumwa kusikiliza malalamiko mikoani. Alipofika Misri alishawishiwa na akakubali kujiunga na wanafiki wa kundi la Ibn Sabaa. Abu Sarah Gavana wa Misri alimfahamisha Khalifa kushiriki kwa Maswahaba hawa katika ghasia za Ibn Sabaa na kushauri wachukuliwe hatua. Lakini Khalifa alikataza kuwachukulia hatua yoyote.

Kutokana na harakati hizi za wapinzani, wasiwasi ulienea nchi nzima na serikali sasa ikalazimika kuchukua hatua, ili kudhibiti hali ya nchi.

## **Hatua ya Serikali Dhidi ya Waanzilishi wa Fitna na Farka**

Hatua ya kwanza ilikuwa kuwahamishia Syria viongozi 10 wa upinzani kutoka Kufa. Wakorofi hawa walipopelekwa Syria, Amir Muawiya alizungumza nao na kusikiliza mafundisho yao lakini alipowasihi waache kupoteza watu walijifanya hawamuelewi kwa sababu hii Gavana Muawiya alimuandikia Khalifa Uthman kumuomba awarudishe walikotoka ili wasiwaharibu watu wa Syria kwa vile wanazungumza lugha ya shetani na lengo lao ni kuwagawa watu na kuunda fitna. Watu hawa walirudishwa Kufa na walipoendelea na shughuli zao walihamishiwa Hirus ambako walidhibitiwa kwa muda na gavana Abdur-Rahman mtoto wa Khalid.

Hatua ya pili iliyochukuliwa na Khalifa pamoja na Shura yake ni kutuma wajumbe wanne(4)kutembelea Dola nzima na kusikiliza malalamiko ya



wananchi. Maswahaba waliotumwa ni Muhammad bin Muslimah, Usamah bin Zaid, Ammar bin Yasir na Abdullah bin Umar. Wajumbe hawa ambao walirudi watatu walitoa taarifa kuwa hakukua na malalamiko. Ammar bin Yasir alibakia Misr na kujiunga na wapinzani.

## **Kuwasilisha Malalamiko Kwenye Kikao cha Magavana**

Kama kawaida magavana walikutana kila mwaka baada ya Hija. Katika mwaka ule taarifa zilitolewa kuwa wenye malalamiko waende kuwasilisha malalamiko yao kwenye kikao hicho. Lakini hakuna aliyejitokeza. Si hivyo tu lakini Khalifa Uthman alitimiza dai la wapinzani hawa kwa kumuweka Gavana wanayemtaka Kufa. Walichokifanya wapinzani ni kuwa walikusanya kundi la watu wapatao elfu moja na kumzuia Gavana wa Kufa asirudi madarakani alipokwenda Madinah mkutanoni. Walimzuia mahali paitwapo Ajara, mtumishi wake aliuliwa na yeye akarudi Madinah. Khalifa akamthibitisha Abu Mussa kuwa gavana wa Kufa baada ya kutakiwa na wapinzani. Hapa Khalifa alionesha udhaifu, watu hawa walistahiki kuadhibiwa kinyume na kukubali dai lao baada ya uhaini uliowazi.

Katika kikao cha Magavana Khalifa alitaka ushauri wa kuzima uasi nchini. Saad alishauri wapinzani wakamatwe na kuadhibiwa. Abu Sarah alishauri wasipewe posho; Ibn Aamir alitaka wapinzani wauawe; Muawiya pia alitaka zichukuliwe hatua kali. Kutokana na maoni haya Khalifa alijibu:

*Ukatili sitoruhusu, kama mapinduzi yakija sitaki kulaumiwa. Ukianza hivi mwisho wake mbaya. Ingekuwa vyema pale mapema wakati uasi haujaenea. Sasa hakuna la kufanya ila kukaa kimya na kusubiri bila kumkosea mtu yeyote.*

Muawiya alipokuwa anaondoka Madina alimsihi Khalifa akubali kuhama Madina lakini alikataa, na kusema hata kama ni kuokoa maisha yangu sitaondoka katika ardhi ambayo Mtume aliishi na kuzikwa.

Kisha Muawiya akamuomba akubali kuletewa jeshi lilinde mji wa Madina. Hali kadhalika Khalifa alikataa na kusema; “*Sitawaweka askari wanaokaa karibu na nyumba ya Mtume*”. Kwa hali hiyo Muawiya akajibu “Sioni kinachokusubiri ila umauti; “*Mwenyezi Mungu ndie mlinzi wangu,*” alisema Khalifa Uthman.<sup>15</sup> ambaye alikuwa mzee wa miaka 82.

Uthman bin Affan, alijua hatari iliyokuwa inamkabili lakini hakutaka kutumia nguvu kuwaadhibu wapinzani wake kwa kuhofia kuzuka vita vya wenyewe kwa wenyewe, alihiyari afe yeye kuliko kuzusha vita ambavyo vingegharimu roho nyingi.

## Khalifa Uthman Kufa Shahidi

Ni dhahiri wahaini wa Serikali waliona wakati umefika wa kufanya lile walilokusudia tangu pale walipoweza kumtoa Gavana wa Kufa na kumuweka wanayemtaka bila kuadhibiwa. Wakaibua mbinu ya kutuma watu watatu kwenda Madinah kuwasilisha malalamiko yao. Watatu hao walitoka Misri, Basra na Kufa. Walipofika Madinah baadhi ya maswahaba walimshauri Khalifa kuwa wauwawe lakini kwa msimamo ule ule wa kutotaka kumwaga damu ya Waislamu, Khalifa alikataa na kusema nitawasikiza. Khalifa aliwasikiliza kisha akatoa hutuba ndefu ambayo ndani yake alijibu shutuma zote. Baadhi ya sehemu ya hutuba hiyo ya kihistoria ni kama ifuatavyo:

*Ninalaumiwa kwa kuwapenda ndugu zangu. Sio dhambi kwa mtu kumpenda ndugu yake. lakini sijamfanyia mtu udhalimu kwa sababu ya kupenda ndugu. Sijatumia chochote kwa ajili ya ndugu zangu kutoka kwenye mfuko wa Serikali...*

*Imesemwa kuwa nimewateua vijana wadogo maafisa. nimefanya hivyo kwa kuzingatia mchango wao katika uislamu. Hakuna anayekanusha uaminifu wao na mchango wao katika Uislamu, na Waislamu. Kuteuliwa kwa Usamah na Mtume (s.a.w.) kuwa kamanda wa jeshi ni ushahidi kuwa ujana sio kipingamizi cha kupewa uafisa.*

*Imedaiwa nimempa gavana wa Misri ngawira yote ya Afrika kaskazini kama zawadi. Ni kweli lakini niliposikia jamii haikupendezwa na jambo hili nimezichukuwa fedha zote kutoka kwa gavana na kuziweka kwenye mfuko wa Serikali (Baitul Mal).*

*Inadaiwa kuwa nimetenga mbuga za malisho ya Serikali kwa ajili ya wanyama wangu. Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, sitafanya hivyo. Katika mbuga hizo (mashamba hayo) ni wanyama wa Serikali tu (Baitul-Mal) ndio wanaolishwa humo, wote mnaafhamu kuwa nilipopewa ukhalifa nilikuwa na wanyama wengi kuliko yeyote Arabia nzima. Leo nina ngamia wawili niliowaacha ili wanisaidie wakati wa Hija. Ingekuwaje, nitenge malisho ya Serikali kwa ajili yangu wakati wanyama wenyewe sina.*

*Watu wanailaumu kwa kuchoma nakala za Qur'an. Qur'an tukufu ni kitabu cha Mwenyezi Mungu alichoteremshiwa Mtume (s.a.w.). Maswahaba waliokiandika chini ya usimamizi wa Mtume wako hai. Nimepeleka ile nakala ya Qur'an iliyokusanywa na maswahaba.*

*Inasemwa kuwa nimemrudisha Hakam Madina ambaye alipeleka uhamishoni na Mtume. ukweli ni kwamba Mtume alimhamisha Hakam kutoka Makka kwenda Taif. Baada ya kumwombea Mtume alimruhusu aishi Madina. Nimetekeleza ruhusa iliyotolewa na Mtume (s.a.w.)...."*

*(Mwisho wa Hotuba yake akasema). Niambieni kama kuna kitu kisichokuwa cha kweli kati ya niliyosema....<sup>16</sup>*

Ingawa Khalifa alijibu shutuma zote kwa ufasaha, ukweli na uwazi, wawakilishi wa wapinzani walirudi na kusema uwongo kuwa Khalifa amepuuza madai yao.

Ndipo wakaja makundi ya watu elfu, elfu kutoka Misr, Basra na Kufa na kupiga kambi karibu na Madina. Waliotoka Basra walipiga kambi Dhikhasha, waliotoka kufa walikaa 'Awas na waliotoka Misri walikaa Dhi-Murwah. Makundi ya wahaini hawa walishindwa kuingia Madina moja kwa moja kwa sababu walipokuwa wanakaribia Madina, Khalifa alikusanya wakazi wa Madina na kuwahutubia kuwa:

*Wanani kusudia mimi, karibuni hivi watakumbuka wakati wa ukhalifa wangu na kuujutia, wataona siku moja ni kama mwaka kwa sababu ya vurugu umwagaji damu na uasi utaoenea nchi nzima.*<sup>17</sup>

Wananchi walichukua silaha na kuzuia uvamizi wa mji wao. Hali hii ndiyo iliyoilazimisha wahaini kukaa nje ya Madina.

Wahaini hawa walikuwa na agenda moja tu, ya kumwondoa Khalifa madarakani kwa hiyari au kwa nguvu. ndiyo maana walipofika tu Madina kila kikundi kilimkabili waliyemtaka awe Khalifa kwani katika hili walitofautiana. Ibn Sabaa na Wamisri walimtaka Ali. Watu wa Kufa walimtaka Zubair na watu wa Basra walimtaka Talha. Maswahaba wote hawa walikataa na kuwaambia kuwa Mtume(s.a.w.) aliwaambia makundi ya Dhikhasha, 'Awas na Dhi-murwah jamelaaniwa.<sup>18</sup>

Khalifa aliwatuma maswahaba maarufu akiwemo Ali kusikiliza malalamiko yao. Waliwakilisha matakwa yao pamoja na kutaka Muhammad Ibn Abubakar awe gavana wa Misri badala ya Abu Mussa. Khalifa alikubali bila kuuliza kisha akawaahidi kuwa atatekeleza maombi yao. Ali naye akasisitiza hivyo hivyo. Pamoja na kuwakubalia matakwa yao walivamia msikiti na kumuua Khalifa Uthman akiwa anasoma Qur'an.

## **Vita vya Wenyewe kwa Wenyewe**

Kipindi cha Ukhalifa wa Ali hakikuwa na wapinzani kutoka nje ya Dola ya Kiislamu. Na inaweza kusemwa kuwa hakukuwa na upinzani kwa sababu hapakuwa na kiongozi aliyechaguliwa kwa utaratibu unaokubalika na kwa sababu hii inakuwa vigumu kusema kulikuwa na upinzani ila kulikuwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe. Ni vigumu kusema kuwa Ali alikuwa ameteuliwa kwa utaratibu wa Uislamu kuwa Khalifa. Wahaini wale baada ya kumuua Khalifa Uthman, mji wa Madinah na Serikali yake ilikuwa chini yao kwa muda wa siku sita na swala ya Ijmaa waliendesha wao.

Siku ya sita Ali alitangazwa kuwa Khalifa na wauwaji. Wauwaji hawa hawa ndio waliofundisha kuwa Ali ni "wasi" wa Mtume(s.a.w). Aisha, Talha na Zubeir

ni vigumu kusema kuwa waliupinga Uislamu walipopigana na Ali katika vita vya Ngamia. Vile vile ni vigumu na haiwezekani Muawiya alipokataa kumtii Ali alikuwa amekosea hivyo alipinga Uislamu alipopigana na Ali katika vita vya Siffin. Tunachoweza kusema wakati wa Ali kulikuwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe. Katika vita hivyo, nani alipigania Uislamu, nani alipigania kundi lake, au ukoo wake au udugu au kabila lake n.k. ni maoni ya kila mwana historia baada ya kujua mkondo wa matukio ya kihistoria.

Jambo la kusikitisha ni kuwa kipindi cha Khalifa Ali kilitawaliwa na mapigano baina ya wenyewe kwa wenyewe. Baina ya Khalifa na Aisha, Talha na Zubair, Khalifa na Khawarij na Khalifa na Muawiya Gavana wa Syria. Matukio yalichukua mkondo ufuatao.

Baada ya kuuawa kwa Khalifa Uthman na kutawazwa kwa Ali baadhi ya jamaa wa Khalifa walikwenda Makka kueleza tukio lilivyokuwa, mama wa waumini Bi Aisha alistushwa sana na tukio hili, lakini lililotisha zaidi ni hatua ya Khalifa ya kuahirisha adhabu ya waliomuua Khalifa Uthman kwa hoja kuwa kwanza arudishe amani nchini kisha ndipo awaadhibu wauwaji. Hoja hii ilikuwa ni ngumu kueleweka hasa ukizingatia mambo matatu. **Kwanza**, muanzilishi wa ghasia na hatimaye kufikia kifo cha Khalifa Uthman alifundisha imani ya “wasi” wa Ali. **Pili**, hilo ndilo lililomuweka Ali madarakani na **tatu**, wauwaji hawa pamoja na kuambiwa waondoke Madina siku ya tatu ya Ukhalifa wa Ali kundi la Ibn Sabaa lilikhalifu amri ya Khalifa na kuendelea kubaki Madina kwa kisingizio cha urafiki. Mama wa waumini ambaye alikuwa anarudi Madinah kutoka kwenye Hija, alirudi Makka na kuwaomba watu kwenda kulipiza kifo cha Khalifa. Maswahaba maarufu Talha na Zubeir walimuunga mkono na wakawa naye. Wapiganaji 2,000 walipatikana. Lakini walipokuwa wanakwenda Madinah wakapata wazo la kupitia Basra kupata watu wengi. Walipokuwa njiani kuelekea Basra watu wengi wakaungana naye na alipofika Basra alikuwa na watu 3,000 chini ya Bendera yake.

Gavana wa Basra, Uthman bin Hunif alituma watu ili kujua lengo la ziara ya Bibi Aisha Basra. Wajumbe wa Gavana walifahamishwa kuwa yeye mama Aisha na Waislamu wengine walitaka kuwakumbusha Waislamu juu ya wajibu wao kwa Khalifa aliyeuawa. Na dhima yao ni kuwaadhibu wauwaji. Kusikia hivi Gavana alizuia msafara usiingie Basra. Kwa hiyo akaita mkutano na kuwaamuru watu wake wawapige Mama Aisha na wenzake baada ya kupata maelekezo kutoka kwa Khalifa Ali. Watu wake waligawanyika, kuna waliomuunga mkono yeye na wapo waliomuunga mkono Aisha. Mama Aisha alitoa Hotuba ambayo iliwezesha kuwateka nusu ya watu ambao mwanzoni walimuunga mkono Khalifa. Kuona hivi mama Aisha alitaka suluhu, lakini upande wa gavana kulikuwa na watu wa Ibn Sabaa ambao suluhu hawakuitaka - Hakim bin Hublan akiwa kiranja wa kundi hili lililotaka suluhu alivamia jeshi la Mama Aisha(r.a) hata kabla ya ruhusa ya gavana wake na uchokozi huu vita vikaanza, gavana akatekwa,

Hublan na wenzake wengi wapatao 600 wakauawa na Basra ikatekwa na kuwa chini ya Bibi Aisha, Talha na Zubeir.

## **Vita Kati ya Bibi Aisha na Khalifa Ali**

Khabari za kutekwa Basra zilimchukua kwa mshangao mkubwa Khalifa Ali ambaye alikuwa aende Syria kumrudi Muawiya lakini alilazimika kwenda Basra kwanza kutuliza hali ya kule.

Alipofika Dhi-Qar'a mahali karibu na Basra-alituma ujumbe kwa Aisha, Talha na Zubeir wafanye mazungumzo ya amani. Nafasi ilipatikana mazungumzo yakafanywa na wakawa karibu kukubaliana baada ya Ali kuahidi kuwa atawaadhibu wauwaji wa Uthman Dola itakapokuwa na amani. Lakini mpango wa amani haukuwa na maslahi kwa lile kundi la Ibn Sabaa ambalo lilifanya sehemu ya jeshi la Ali. Walinong'onezana kuwa Ali anataka kufikia makubaliano ya amani na ameahidi kuwaadhibu waliomuua Uthman. Kundi hili lilikuwa ndilo lililomuua Khalifa Uthman halikupendezwa na mpango huu, wakaunda hila iliyochochea kutokea vita. Mbinu mbili walizitumia. Kwanza walipeleka umbea Basra kuwa Ali akiingia Basra atawafanya watumwa wakazi wote na atawau vijana wote. Kwa sababu hii watu wa Basra lazima wapigane. Ibn Sabaa na wachochezi wake usiku usiku walivamia jeshi la mama Aisha ambaye aliarifiwa na kwa namna hii vita vikaanza. Vita hivi vinajulikana kwa jina la Vita vya ngamia.

Vita vilikuwa vikali kwa vile ukubwa wa jeshi ulilingana. Baada ya mapigano makali na kuuawa Waislamu wapatao elfu kumi, Talha aliuwawa na , Zubair aliacha kupigana na akawa anaelekea Madina ndipo akauliwa njiani. Wakati wote wa vita mama Aisha alikuwa katika sehemu ya uwanja wa vita akiwa amepanda ngamia. Kuwepo kwake kulifanya mapigano yaendeleo kwa kasi kubwa, bila kukoma, ndipo Ali alipoamuru ngamia wake akatwe miguu ya nyuma. Ngamia aliangukia miguu yake ya mbele na kwa heshima zote akatolewa mama Aisha ndani ya kikalio cha ngamia na vita vikaisha. Mama Aisha akasindikizwa Madinah na kaka yake Muhammad bin Abubakar.

Baada ya vita, Ali alizungumza na Waislamu katika msikiti wa Basra na Waislamu wakampa mkono wa utii. Alipoondoka alimuacha 'Abdallah bin Abbas kuwa Gavana wa Basra.

## **Vita Kati ya Khalifa Ali na Gavana Muawiya**

Vita vya **tatu** vya wenyewe kwa wenyewe ni vile vilivyopiganwa baina ya Khalifa Ali na Gavana Amir Muawiya wa Syria - vita hivi vinaitwa Vita vya Siffin.

Sababu hasa ya vita hivi ni vigumu kuitamka kuwa ni hii au ni ile. Kwa vyovyote ilivyokuwa ni vita ambavyo vingeweza kuepukika katika kiwango kikubwa kama viongozi wawili hawa wangetanguliza Uislamu kuliko vinginevyo.

Khalifa Ali alipopewa ukhalifa na wale wauwaji na kukubali kuwa Khalifa wapo maswahaba waliokataa kumtambua mpaka awaadhibu wauwaji. Ali alidai kuwa atawashughulikia nchi itakapotulia. Kinyume na ushauri wa maswahaba wakongwe wengi Ali aliamua kubadilisha Magavana wote. Gavana wa Kufa na Syria walikubali kwa sharti kuwa endapo atawaadhibu waliomuua Khalifa Uthman wangempa mkono wa utii na kuacha ugavana. Ammarah bin Hassan alipokwenda Kufa kuchukua nafasi ya ugavana alilazimishwa kurudi kwa vile watu wa Kufa hawakutaka gavana wao Musa Ashari abadilishwe. Ama yule aliyepangiwa Syria alipofika Tabuk, majeshi ya Muawiya yalimuamuru arudie pale.

Ali alituma wajumbe maalum Kufa na Syria. Gavana wa Kufa, Abu Mussa Ashari, alituma jibu la kuridhisha na kumuarifu Khalifa kuwa watu wa Kufa wamekubali kumtii na hivyo Gavana alichukua kiapo cha utii kwa niaba yake. Jibu hili lilimpendeza Ali, alimuacha Abu Mussa aendeleo kuwa Gavana na yeye mwenyewe akahamisha makao makuu ya Serikali kutoka Madinah na kuyapeleka Kufa. Sababu inayotajwa katika vitabu vya historia ni kuepuka umwagaji damu katika msikiti na mji mtakatifu wa Mtume(s.a.w.) kama ilivyotokea kwa Khalifa Uthman.

Lakini maoni ya kutungwa mkono sana Madinah na kuwa Kufa ndiko kulikokuwa chimbuko la wauwaji na kuwa pia jeshi lake lilikuwa na wachochezi wa Ibn Sabaa ambao inadhaniwa walikuwa na hisa kubwa katika uamuzi huu, havitajwi wala kuongelewa. Hata hivyo umwagaji damu katika mji na msikiti mtakatifu wa Madinah pengine na hata wa Makka haupekiki kwa kuhama Madinah. Umwagaji damu unaepukika kwa kutekeleza haki. Vile vile ghasia hazina mahali na damu siyo ya Khalifa tu bali damu ya yeyote siyo ya kumwagwa bila sababu za Kiislamu ambazo ni kuua au uhaini. Halafu hakuna mahali ambapo kumwaga damu ni halali na pengine ni kharamu. Ni haramu kumwaga damu iwe Madinah, Maka, Taif, Kufa, Basra, n.k. Hivyo hoja inayotolewa katika vitabu vya historia kuwa imempelekea Khalifa Ali kuhamishia makao makuu ya Serikali kutoka Madinah kwenda Kufa uzito wake ni hafifu na inakanganya.

Pamoja na Gavana wa Kufa kutambua Ukhalifa wa Ali na Khalifa akapeleka makao makuu ya Serikali Kufa, mambo hayakuwa hivyo kwa Syria. Kabla ya kuuawa kwa Khalifa Uthman, Amir Muawiya, gavana wa Syria alimuomba Khalifa akubali kwenda Syria au amletee jeshi la kumlinda. Maombi yote haya yalipokataliwa Muawiya alimwambia nduguye Uthman sioni kitu kinachokutokea ila kifo. Isitoshe Muawiya aliwafukuza mkoani kwake wachochezi wa ghasia. Ndiyo kusema alikuwa anafuatilia wimbi la upinzani na hakuridhika na kuuawa kwa Khalifa. Pia alishangazwa na Khalifa aliposhindwa kuwarudi wauwaji kwa hoja ya kuleta amani. Kilichotokea ni kuwa watu waliokuwa wanaona Uthman kaonewa walikimbilia Syria.

Pamoja nao wakaenda na vidole vilivyokatwa, vya mke wa Khalifa, Nailah, pamoja na shati lenye misindosindo ya damu ya Khalifa Uthman. Vitu hivi vikatundikwa nje ya msikiti wa mji wa Damascus, Syria. Wasiria walishikwa na uchungu mkubwa wakalia kwa machozi na kwikwi kwa kishindo kikubwa kwa kifo hiki cha kikatili cha Khalifa Uthman na kudai kulipiza kisasi kwa wauwaji. Hii ndiyo hali waliyokuwa nayo watu wa Syria. Hivyo Khalifa Ali alipotuma mjumbe wake maalumu kwa Muawiya, alichokifanya Muawiya ni kumuweka kizuizini mjumbe yule na baada ya miezi mitatu alituma mjumbe wake na barua yenye anuani “*Kutoka kwa Muawiya kwenda kwa Ali.*”

Barua hii ilipofunguliwa haikuwa na kitu ila Bismillahir-Rahmanir Rahiim. Isitoshe mjumbe yule alimwambia Ali kuwa; watu 50,000 wanaomboleza kifo cha Uthman na wako tayari kupigana mpaka wauwaji wa Khalifa wapatikane. Tukio hili linafanya sababu ya vita vya Siffin isieleweke. Khalifa Ali kusema kama alikuwa anawaogopa wahaini kwa sababu yoyote ile iwe wamo kwenye jeshi lake, au ndio waliomuweka madarakani au nyingine yoyote lakini bado ni kweli wamefanya kosa lisilovumilika kuwa nao. Ni kweli pia wapo wanaoleta hoja kuwa kwa sababu ya kujenga amani unaweza kuakhirisha adhabu ya watu, lakini kwa kiwango chochote kiwacho haki haiwezi kuahirishwa. Khalifa Ali aliahirisha haki ya kuwaadhibu wahalifu. Isitoshe wahalifu hawa walikuwa ndani ya jeshi lake. Tunachokisema ni kuwa kama hali ilikuwa hivi angeweza kutumia Wasyria kuzima uasi huu watu ambao walikuwa tayari kuwarudi wauwaji. Badala ya kuchukua njia hii ambayo inaonekana ingekuwa nyepesi na fupi, Khalifa alitangaza vita dhidi ya Gavana Muawiya kwa kile kilichodaiwa utovu wa nidhamu wa kutomtii Khalifa. Lakini hoja hii pia hairuhusu kumwaga damu ya Waislamu. Khalifa akamhukumu gavana kuwa ni mkorofi na anatumia kifo cha Uthman kama kisingizio tu. Gavana naye ambae amekaa Syria kwa miaka ishirini akamuona Khalifa kakumbatia wauwaji. Ameshindwa kuwaadhibu, kwa vile ndiwo waliomuweka madarakani na wamo katika jeshi lake. Gavana hakuona sababu ya kumtii.

Misingi hii ya tofauti za misimamo ndizo zilizopelekea vita vya Siffin ambavyo kwa kweli vingeweza kuepukika. Jambo hili linadhihirika tena Ali alipomuandikia barua Muawiyah ya kumtaka amtii na Muawiyah akamtuma mjumbe wake kwa Khalifa kumtaka kwanza wapatikane wauwaji wa Uthman. Watu 10,000 waliokuwa na Khalifa walijibu kuwa wote ndio waliomuua Uthman.

Hali hii ikamfanya Khalifa aende kumrudi Muawiyah na Muawiyah naye kwa upande wake akajiandaa. Wote wakapiga kambi mahali paitwapo Siffin wakiwa na idadi ya askari inayolingana ya 50,000 Katika uwanja huu wa vita Ali alijaribu tena kumtaka Muawiyah ajiuzulu na amtii. Muawiyah naye kwa upande wake alimtaka Ali amkabidhi waliomuua nduguye Uthman. Na anataka hivyo akiwa Walii wa Uthman kabla ya makubaliano yoyote. Dai hili lilikataliwa na mapigano ya wenyewe kwa wenyewe yakaanza.

Mapigano haya yalianza Dhul-Hijah 36 A.H. Lakini katika mwezi wote huo, mapigano yalikuwa mepesi. Ulipofika Muharram wote wakakubaliana kuahirisha vita.

Vita vilianza tena mnamo mwezi wa Safar 37 A.H. Vilichukua muda wa zaidi ya juma moja Waislamu wakiuana bila huruma. Kutokana na wingi wa maiti waliozagaa katika uwanja wa vita, vita vilisitishwa kidogo kwa ajili ya kuzika na kuwaondoa waliojeruhiwa katika uwanja wa vita. katika kipindi hiki Muawiya alimuandikia Ali kama ifuatavyo:

*“Kama wewe au mimi tungefahamu kuwa vita hivi vingechukua muda mrefu hivi hakuna ambaye angevianzisha. Tuache vita hivi viharibifu. Wote sisi tunatokana na ukoo wa Manafi na hakuna mbora mbele ya mwenzie. Makubaliano yanayolinda heshima na nafasi zetu lazima yafikiwe”<sup>19</sup>.*

Ali alikataa kufanya makubaliano yoyote. Baadhi ya wanahistoria wanamshutumu Muawiya kuwa ni mjanja mjanja na hasa mshauri wake Amr bin al As kwa kubuni njia ya kumaliza vita kwa kufunga karatasi za Qur’an katika ncha ya majambia yao ikimaanisha kuwa vita viishe na suluhu ipatikane kwa kutumia Qur’an. Inadaiwa kuwa Muawiya alifanya hivi kwa kuona kuwa alikuwa anakaribia kushindwa. Lakini ama ushahidi wa vyanzo vya historia unapingana au vinginevyo kwa sababu watu wa Khalifa nao hawakutaka kupigana tena. Kwani yasemekana pia “Ali alikuwa anazungumza na watu wake kirafiki katika namna ya kuhoji tendo la Muawiya. Ni mbinu ya watu waovu, wanaogopa kushindwa, wamefunika uasi wao kwa neno la mwenyezi Mungu! Watu wake wakajibu; ‘Tunaitwa kwenye Qur’an na hatuwezi kuidharau’. Katika mkutano wa hadhara walimtishia Khalifa kuwa kama hatakubali watamtoroka, kumkamata na kumkabidhi kwa adui. Walimlazimisha Khalifa amwite Usstur aliyekuwa kwenye mapigano.

## **Suluhu**

Watu wawili waliteuliwa, Musa Ashari kutoka upande wa Khalifa Ali na Amr bin al As kutoka upande wa Gavana Muawiya wafanye suluhu kwa mujibu wa Qur’an.

Wasipokubaliana uamuzi utolewe kwa kupiga kura na mshindi awe yule ambaye atapata kura nyingi. Kila upande ungetoa watu mia nne (400)na kufanya jumla ya watu 800. Majaji hawa wawili pamoja na watu hawa 800 wakitane Damat-ul-Jandal mahali palipo kati kati ya Syria na Iraq katika mwezi wa Ramadhani kufanya suluhu hii na kikao hiki kitangazwe. Hivyo, Ali na Muawiya walifanya makubaliano ya Muda. Mapigano yakasitishwa na majeshi yakaondoka kwenye uwanja wa mapambano.



## Kuibuka kwa Khawarij

Baada ya makubaliano, Ali aliwatangazia makubaliano haya wapiganaji wake. Lakini ndugu wawili wa kabila la Azza walisimama kupinga suluhu kwa hoja kuwa wanazo hukumu za Mwenyezi Mungu katika Qur'an hivyo hawahitaji wasuluhishi. Watu wengi waliunga mkono rai hii na kufikia 12,000. Wao hawakurudi Kufa, walipiga kambi, mahali paitwapo Harorah. Walimteua Sheikh bin Rabi kuwa kamanda wao na Abdullah bin Kawa kuwa Imam wa kuongoza Swala. Walitangaza imani yao ambayo ilikuwa:

*“Ba’iyah iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu, yeye tu ndiye wa kutiwa. Kuhubiri mema na kukataza mabaya. Hakuna Khalifa au Amir. wote Ali na Muawiyah wana makosa, Muawiyah anamakosa kwa kutomtii Ali, na Ali anamakosa kwa kukubaliana na Muawiyah juu ya suluhu. tutaposhika mamlaka tutaanzisha mfumo wa maisha ya jamii uliojengwa juu ya Qur’an”<sup>20</sup>.*

Ali aliporudi Kufa alimtuma Abdullah bin Abbas, Harorah kuzungumza na Khawarij. Aliweza kuwavuta na wakakubaliana na Khalifa baada ya mazungumzo ya muda mrefu. Hata hivyo kukubali huku kulikuwa kwa muda tu.

## Tamko la Wapatanishi

Baada ya mazungumzo marefu wapatanishi walikubaliana kuwa wote wawili Ali na Muawiyah hawafai kugombea nafasi ya ukhalifa. Amr bin al- As alimtegea Abu Mussa aanze yeye kusema msikitini juu ya maazimio yao. Abu Muusa akasema; “Enyi watu tumelizingatia vyema suala linalotukabili. Hatukuona njia nyingine ya kuleta amani miongoni mwa watu ila kuwaondoa wote katika nafasi ya kugombea Ukhaliifa. Baada ya hivi mchague Khalifa anayefaa<sup>21</sup>. Hii ndio hukumu yangu.

Alipopanda jukwaani Amr bin al As alibadili maneno na kusema maneno wasiyokubaliana na mwenziwe kwa kusema; “Mmesikia hukumu ya Abu Mussa. Amemuondoa mtu wake nami pia ninamuondoa. Lakini kwa chifu wangu Muawiyah, yeye ninamthibitisha, ni mrithi wa Uthman, mlipiza wa damu yake, ni bora kuliko wote kwa kuchukua nafasi yake<sup>22</sup>.

Wajumbe wote walichanganyikiwa kwa kauli hii na kukawa hakuna maelewano. Nusra Amr bin al-As auliwe na askari wa Ali. Uamuzi huu haukufuata Qur'an hivyo haukukubalika. Khawarij walijikusanya na kuanza uasi. Walihama Harorah na kwenda Nahruwan. Katika eneo hili waliuwa watu na kufanya ukatili. Khalifa Ali alizungumza na Khawarij hawa ili waache vitendo vyao na imani yao potofu.

Lakini hawakukubali, kwa hali hii mapigano yakawa lazima, hata hivyo walishindwa vibaya. Baada ya hapa Khalifa Ali aliamuru jeshi lake liende Syria

kupambana na Amir Muawiya kwa sababu suluhu haikuwa katika Qur'an. Lakini kabla ya kwenda Syria Khalifa Ali alipiga kambi mahali paitwapo Nakhila karibu na mji wa Kufa. Askari wake waliomba kwenda makwao na akawaruhusu, wengi hawakurudi na safari ikavunjika. Alijaribu mara mbili kukusanya askari kwenda Syria bila mafanikio na kutokana na hali hii suala zima la kupigana tena na Muawiya akaliacha.

## **Muawiyah Ateka Jimbo la Misri**

Khalifa Ali alimteua Qais bin Sad awe gavana wa Misri. Qais alichukua ahadi ya utii kwa niaba ya watu wa Misri, lakini watu wa jimbo la Khartaban hawakutoa ahadi ya utii kwa Khalifa Ali na Qais aliwaacha kwa kuwa kulikuwa na amani.

Hali hii ya kuwaacha watu wa Khartaban iliwafanya baadhi ya watu wamuone Qais sio mtiifu kwa Khalifa. Khalifa alikusudia kumjaribu Qais kwa kumuamuru awapige vita watu wa Khartaban. Qais hakuona sababu ya kupigana na watu wa Kharaban hivyo akaondolewa kwenye ugavana na nafasi yake akateuliwa Muhammad bin Abubakar.

Muhammad alikuwa kijana hivyo aliwalazimisha watu wa Khartaban wakubali Ukhalifa wa Ali. Watu wa Khartaban hawakukubali na walisubiri hadi vita vya Siffin vilipomalizika waliamua kujilinda dhidi ya majeshi ya gavana Muhammad bin Abubakar na mapigano yakazuka. Majeshi ya gavana yakashindwa mara mbili. Khalifa aliamua kumbadilisha Muhammad na kumtuma Ushtar kuwa gavana wa Misri. Lakini Ushtar alikufa alipofika mpakani mwa Misr hivyo Khalifa alimtaka Muhammad aendelee kushikilia ugavana wa Misri akamtumia askari 2,000 ambao aliwapata kwa taabu. Lakini kabla askari wa Khalifa hawajafika Muawiya alimtuma Amri bin al As na jeshi la kutosha, likayashinda majeshi ya gavana na yeye mwenyewe kuuliwa. Kwa ushindi huu Misri ikawa chini ya Muawiyah na Amr bin al As akawa gavana wa Muawiyah Misri. Hii ilikuwa katika mwaka wa 38 A.H.

## **Ghasia Sehemu Mbali Mbali za Dola ya Kiislamu**

Misri kuwa mikononi mwa Muawiyah kulichochea upinzani dhahiri baina ya Ali na Muawiyah. Mnamo mwaka 38 A.H. gavana wa Basra Abdallah bin Abbas alikwenda Kufa kumzuru Khalifa. Wakati huu Basra ilikuwa na wafuasi wa Ali, hali kadhalika wafuasi wa Muawiyah. Kutokuwepo kwa Gavana kulipelekea Ubaidullah Ibn Hadrani mfuasi wa Muawiyah kushawishi watu na kuunda jeshi la kulipiza kisasi dhidi ya mauaji ya Uthman. Alipata jeshi na akavamia Basra. Ziyad ibn Abi Sufiyan aliyekuwa amemshikia ugavana akashindwa kuyamudu majeshi ya Hadrani na kukimbia. Hata hivyo Khalifa aliposikia uasi huo alimtuma Jariah ibn Gudumah na jeshi ambalo liliweza kuzima upinzani. Hadrani na watu wengine sabini walijificha ndani ya nyumba ambayo wafuasi wa Ali waliichoma moto.

Khawarij nao waliendesha upinzani dhidi ya Serikali ya Ali. Upinzani mkali uliendeshwa na Khirrt ambae alipigana na Ali katika vita vya ngamia na vita vya Siffin akiongoza kabila lake la Bani Najja. Jitihada za kumteka katika vita hivi zilishindikana na alikimbilia Ahwaz na Ran Hermuz. Aliwashawishi, Waajemi (Persians), Wakurd (Kurds) na Wakristo wasilipe kodi, akiwa na kundi la wafuasi wake aliendesha uasi Faris na Kirman. Khalifa alituma jeshi ambalo liliweza kuzima uasi huu, katika mapigano haya Khirrt aliuliwa. Kwa ushindi huu jimbo la kusini mwa Persia likarudia utulivu na Ziyad akateuliwa Gavana wa jimbo hili.

Muawiya bado aliendelea kutumia vikundi vya askari katika sehemu mbali mbali za Dola ya Kiislamu. Numan ibn Bashir alitumwa Ain al-Tamr lakini alishindwa na gavana wa Ali, Maliki bin Kab. Kundi lingine la watu elfu sita chini ya uongozi wa Sufiyan ibn Auf lilikwenda Ambar na Madain (Madian), walifanikiwa kumuua kiongozi wa Ambar. Khalifa Ali alituma Said Ibn Auf na jeshi ambalo lilimfanya adui akimbie. Askari wengine elfu tatu chini ya uongozi wa Dahak ibn Qais walikaribia Basra. Mapigano yalitokea baina ya majeshi ya Khalifa na Waasi. Waasi 19 waliuliwa na wengine wakakimbia.

Ghasia zote hizi zilitokea katika mwaka wa 39 A.H. Katika mwaka huo huo wa 39 A.H. Ali alipeleka mwakilishi wake Ibn Abbas awe kiongozi wa Hijja, na Muawiyah naye alimpeleka Yazid ibn Sanjar, awe muwakilishi wake. Ugomvi baina yao ulizuka na suluhu ikawa wote wawili wasiongoze Hijja na Shaiban ibn Uthman ibn Abi Talha aliteuliwa kuongoza Hijja. Hali hii ilidhoofisha nafasi ya Ali kama Khalifa.

## **Kutekwa kwa Makka, Madina na Yemen**

Katika mwaka wa 40 A.H. Amir Muawiya alituma Busr Ibn Abi Artat na watu elfu tatu kwenda Hijazi ambako aliiteka Madina, Makka na mji wa Sanaa, Yemen na kuwataka wamtii Muawiyah. Huko Yemen aliuwa watoto wadogo wawili wa Gavana wa jimbo hilo Ubaidullah ambaye alikimbilia Kufa. Vile vile aliwaua wafuasi wengi wa Ali. Jariah Ibn Qudamah akiwa na askari elfu mbili alitumwa kurudisha maeneo yaliyotekwa. Alifanikiwa kuirejesha Sanaa mikononi mwa Khalifa kwani wakati huu Busr alikwisharudi Syria. Lakini alipofika Makka alipata taarifa ya kuuwawa kwa Ali na huu ukawa ndio mwisho wa Ali.

## **Kuuwawa kwa Ali(r.a)**

Baada ya vita vya Nahrwan, Khawarij waliendesha mambo yao chini chini. Inadaiwa waliendelea kuisakama Serikali. Hawakumpenda Ali wala Muawiyah kwa sababu wao ndio chanzo cha kugawanyika kwa Waislamu, katika kundi la Muawiyah na kundi la Ali. Amr bin al As naye walimuona ana makosa kwa vile ndiye mshauri na afisa mipango wa Muawiya. Hivyo walipanga kuwaua wote watatu alfajiri ya mwezi 17 Ramadhan 40 A.H. wakati wa swala ya Alfajiri.

Ilipangwa Ali auliwe na Abdur-Rahman Muljam. Muawiya auliwe na Bark Ibn Abdullah na Amr bin al As auliwe na Amr ibn Bark. Wauwaji hawa walitia sumu kali katika majambia yao na wote wakafanya kazi yao kama walivyopanga Misri, Syria na Kufa. Lakini matokeo hayakuwa mia kwa mia. Ali alijeruhiwa vibaya na jeraha lilisababisha kifo chake kilichotokea jioni ya mwezi 20 Ramadhan 40 A.H. Muljam alikamatwa na kuhojiwa. Kabla hajafa Khalifa Ali aliwaita watoto wake na kuwauusia kumcha Mungu. Lakini alipoulizwa kama Hassan atawazwe Ukhalifa alisema, “Nawaachia Waislamu waamue”. Khalifa Ali alitawala kwa miaka mine na miezi tisa. Alikufa akiwa na miaka 63.

Baada ya Khalifa Ali kuuliwa, mtoto wake, Hassan, alichaguliwa kuchukua nafasi ya Ukhalifa lakini Muawiyah aliasi na kuandaa jeshi dhidi yake. Baada ya mapigano kidogo, Hassan alizidiwa nguvu na akaona amwachie Muawiyah Ukhaifa kwa makubaliano kuwa baada yake uongozi uchukuliwe na ndugu yake, Hussein bin Ali. Kinyume na makubaliano hayo, ambayo pia hayakuwa ya Kiislamu, Muawiyah kabla hajafa, alimteua mtoto wake, Yazid bin Muawiyah kushika uongozi wa Dola baada yake.

## **Kuanzishwa Ufalme.**

Muawiyah kwa kumrithisha mtoto wake, Yazid, uongozi wa Dola, bila kuzingatia utaratibu wa kuchangua viongozi kutokana na sifa stahiki, alivunja maongozi ya Kiislamu na kuasisi utawala wa kifalme au utawala wa kiukoo ambao mpaka leo unaendelezwa katika nchi nyingi za Arabia(Bara Arab), Saud Arabia ikiwa miongoni.

Dola ya kifalme aliyoiasisi Muawiya ilitafautiana na Dola ya Kiislamu aliyoiasisi Mtume(s.a.w) na kuendelezwa na Makhhalifa wanne waongofu, Abubakar, ‘Umar, Uthman na Ali, kwa sababu:

- (i) Taasisi ya shura ilivyunjwa na raia walipokonywa uhuru wao wa kutoa maoni na kukosoa viongozi.
- (ii) Hazina ya Dola – Baitul-Mali, ilifanywa mali ya nyumba ya mfalme ambapo mfalme alitumia atakavyo kwa maslahi yake binafsi na familia ya kifalme.
- (iii) Tabia za kijahili za majivuno ya kikabila na kinasaba ziliibuka na kustawishwa na ufalme.
- (iv) Watawala (viongozi mbali mbali wa dola) walianza kuishi kwenye mahekalu na nyumba za kifahari za Kifalme.
- (v) Suala la kutenganisha maongozi ya Serikali na Dini liliibuka. Masheikh wazuri waliokuwa waadilifu walitengwa na kundi la watawala. Wao wakawa wanajitahidi kuirekebisha jamii lakini wakiwa ndani ya kuta nne za msikiti na nje ya vyombo vya dola.

## Zoezi la 5.1

- 1.(a) Wabainishe Makhalifa wanne waongofu wa Mtume(s.a.w) na muda aliiodumu katika uongozi kila mmoja wao.  
 (b) Eleza kwa ufupi namna kila Khalifa wa Mtume(s.a.w) alivyochaguliwa na kuingizwa kwenye uongozi.
2. Uchaguzi wa Ali(r.a) kuwa Khalifa wa nne wa Mtume(s.a.w) ulikuwa na utata. Jadili.
3. (a) Ainisha madhumuni ya Dola ya Kiislamu.  
 (b) Katika kutakeleza madhumuni ya Dola ya Kiislamu Khalifa aliwajibika kufanya yafuatayo:  
 (i) \_\_\_\_\_ (ii) \_\_\_\_\_ (iii) \_\_\_\_\_ (iv) \_\_\_\_\_ (v) \_\_\_\_\_
4. Ainisha vyanzo saba vya pato la serikali katika kipindi cha makahalifa wa Mtume(s.a.w).
5. Onesha kuwa wakati wa makhalifa ulinzi na usalama uliimarishwa zaidi kuliko kipindi kile cha Mtume(s.a.w). Kwanini ?
6. (a) Eleza juu ya uasi wa Dola(Riddah) uliotokea mara tu ya kutawafu Mtume(s.a.w).  
 (b) Ni sababu zipi zilizopelekea kutokea kwa “riddah”  
 (c) Onesha namna Khalifa Abubakar Siddiq(r.a) alivyokomesha riddah.
7. Toa maelezo mafupi juu ya:  
 (a) Vita vya ngamia  
 (b) Vita vya Siffin
8. Nikipi kilichopelekea kutokea kwa mapigano ya waislamu kwa waislamu wakati wa uongozi wa Khalifa Ali bin Abu Talib(r.a)”
9. Ni sababu zipi zilizopeleka kuuliwa:  
 (a) Khalifa ‘Uthman bin Affani  
 (b) Khalifa Ali bin Abu Twalib.
- 10.(a) Eleza hatua kwa hatua namna Dola ya Kiislamu aliyoisasi Mtume(s.a.w) ilivyoporomoka na kuzuka Dola za kifalme.  
 (b) Toa mafunzo matano (5) yatokanayo na kuporomoka kwa Dola ya Kiislamu aliyoisasi Mtume(s.a.w).

**KUHUISHA UISLAMU WAKATI WA TABIINA***Utangulizi*

Pamoja na kuporomoka kwa dola ya Kiislamu, waumini wa kweli wamekuwepo na kujitahidi hapa na pale, kwa mmoja mmoja na katika vikundi, kwa kadiri ya uwezo wao kuurudisha Uislamu katika ile hali aliyoiacha Mtume(s.a.w). Kwa mfano, pamoja na kuporomoka kwa Dola ya Kiislamu na maadili yake katika utawala wa kifalme wa Banu Umayyah, ulioasisiwa na Mu'awiya, aliibuka 'Umar bin Abdul Aziz aliyekuwa Muislamu mcha Mungu, ambaye alipopata tu fursa ya kuteuliwa kuwa Kiongozi wa Dola, aliirejesha dola kwenye Uislamu. Pia walitokea maimamu mashuhuri wa fiqh ambao walifanya jitihada kubwa na kuyatoa muhanga maisha yao yote katika kuurudisha Uislamu katika nafasi yake ya kutawala kila kipengele cha maishayakibinafsi na kijamii. Maimamu hawa ni Abu Hanifa, Maliki, Shafii na Hambali. Tabiin ni wafuasi wa maswahaba.

**Khalifa 'Umar bin Abdul Aziz**

Wakati watu wakiendelea kukata tamaa na utawala mbaya wa Banu Umayya aliibuka Umar bin Abdul Aziz mwaka 99 A.H(717A.D). 'Umar alizaliwa mwaka 61 Hijriya. Wakati wa utawala wa Suleiman Ibn Abdul Malik, akawa gavana wa Madina. Alikuwa kijana mtanashati na mwenye tabia nzuri. Kwa vile uongozi ulikuwa ukienda kiukoo, 'Umar hakuwa miongoni mwa waliotarajiwa kushika Ukhalifa. Hata hivyo Suleiman hakuwa na mtoto mkubwa hivyo ikatokea Umar kupendekezwa kuchukua uongozi na akakubalika.

Baada ya kushika uongozi, 'Umar alibadili maisha yake yakawa rahisi zaidi na ya uadilifu. Aliwaondoa magavana wote waliokuwa katili. Akarejesha hadhi ya Baitul-Mal, ikawa fedha ya umma inakusanywa na kutumiwa kwa uadilifu. Pamoja na yeye mwenyewe kujichunga katika kutumia Baitul-Mal, alikuwa mkali pia kufuatilia maafisa waliofuja mali ya umma. 'Umar bin Abdul Aziz hakuishia hapo, alitoa amri na kusimamia marekebisho ya vipimo(mizani, ili raia wasipunjwe). Aidha ardhi ambayo ilitengwa kwa ajili ya wakubwa aliichukua na kuwagawia raia. 'Umar bin Abdul Aziz alikuwa kiongozi rahim, mpenda watu, asiye na makuu. Alikuwa karibu na watu akisikiliza maoni yao juu ya uendeshaji wa dola, akitatua shida na matatizo ya raia. Kabla yake, Serikali zilizotangulia hazikujali hali wala hisia za raia. Zilikusanya kodi na kuendesha dola kwa misingi ya kujali zaidi familia na koo za wakuu. Hazikuwa zikijishughulisha kubadili tabia na mienendo ya watu. Kadhalika hazikuwa zikiwajenga watu kimaadili. Kazi hiyo waliachiwa masheikh. Uongozi wa 'Umar ulibadili mtazamo huo potofu wa kutenganisha Dini na Serikali badala yake ukasimamia kikamilifu kazi ya kuamrisha mema na kukataza maovu huku ukiboresha hali na maisha

ya watu. Kauli ya kukumbukwa ya ‘Umar bin Abdul Aziz juu ya wajibu wa kiongozi wa kiislamu ilikuwa: “Muhammad alitumwa kama Mtume sio mkusanya kodi”. Akiwa na maana wajibu wa kiongozi wa dola ya kiislamu haukomei katika kukusanya kodi tu bali anawajibika pia kuangalia maadili ya jamii.

Katika kujenga udugu miongoni mwa raia wake, Serikali ya ‘Umar ilipiga marufuku mila zote za kijahili ikiwa ni pamoja na mishikamano ya kikabila na kiukoo. Baadhi ya waliokuwa machifu wa makabila wakati wa utawala wa Banu Umayya walipotaka kufufua mila zao, ‘Umar bin Abdul Aziz aliwakemea vikali kwa kuwaambia: “Mila hizo za ukabila zinavuruga maana ya udugu wa kiislamu na mshikamano wa kijamii uliojengwa miongoni mwa raia (Waislamu). Akisisitiza msimamo huo, ‘Umar alionya kuwa yeyote ambaye angekutwa na tabia hiyo angekabiliwa na adhabu. Katika waraka wake kwa Dhahaakah Ibn Abdul Rahaman, Amiril Muuminina ‘Umar bin Abdul Aziz aliandika:

*“Shukrani zote anastahiki Allah na rehema iwe kwa Mtume wake. Baada ya hayo, mnapaswa kujua kwamba Allah haikubali dini nyingine yoyote zaidi ya Uislamu ambayo amewachagulia waja wake wema. Mwenyezi Mungu ameitukuza dini hii ya Uislamu kwa kuiwekea mwongozo unaoitofautisha na dini nyingine. Mwenyezi Mungu mtukufu amempa utume Muhammad na amemfunulia kitabu. Nye Waarabu, kama mnavyojua, mliishi kwenye ujahili, ushirikina na kila aina ya uchafu, mambo ambayo yalikusamisheni kwenye ufukara, vurugu na machafuko ya mara kwa mara miongoni mwenu. Mlikuwa watu wa kudharauliwa mbele ya wengine, uhai wenu ukiwa chini ya ujahili na ushirikina ambapo umauti wenu usingekuwa na mafikio mengine ila motoni. Mwenyezi Mungu amewaokoeni kutoka lindi la maovu, kuabudu masanamu na umwinyi, kuchukiana na migongano miongoni mwenu. Ingawa wengi miongoni mwenu mlimkataa Mtume wa Mwenyezi Mungu lakini aliendelea kuwaita katika uongofu. Mtume wa Mwenyezi Mungu ameondoka katika ulimwengu akiwa amekamilisha ujumbe aliotumwa na Allah.....”*

*“Nimeelezwa kwamba baadhi ya watu wamekuwa wakijikusanya kimakabila wa kujisaidia wao kwa wao kama ilivyokuwa zama zilizopita. Wanafanya hivyo wakijuwa wazi kuwa Mtume (s.a.w) alipiga marufuku ushirikiano huo. Mtume amesema hakuna utaiifa au ukabila katika Uislamu. Hakuna mtu kutukuza eneo analotoka juu ya wengine. Zama za ujahili, watu walikuwa wakishirikiana hata katika mambo maovu bila ya kujali athari kwa wasio na mahusiano nao. Watu walikuwa wakikandamizana, kubaguana, kuchukiana na kufanyiana machafu kwa sababu ya tofauti hizo. “Namusa kila atakayesoma au kusikia waraka huu ajipambe na vazi la Uislamu na asiwe na ndugu ila na yule aliyeshikamana na Allah na Mtume wake. Narudia tena kuonya kwa kumshuhudisha Mwenyezi Mungu dhidi ya atakayekiuka maamrisha hayo ya Allah na Mtume wake, kwani Mwenyezi Mungu ni mwenye uwezo na yuko karibu na yeyote kuliko mshipa wake mkuu wa damu”.*

Kwa upande wa uchumi Amiril Muuminina ‘Umar bin Abdul Aziz alisimamia nguzo ya zaka na ukusanyaji wa kodi mbali mbali. Kutokana na uadilifu uliokuwepo katika ukusanyaji na utumiaji wa mapato ya umma, ilifikia mahali ndani ya dola ya Kiislamu kukawa hakuna maskini wa kupewa zaka.

UchaMungu wa Ibn Abdul Aziz ulijitokeza hata alipokuwa akiyaamuru majeshi yake kupambana na maadui. Hakuwa tayari kuona askari wa kiislamu akikiuka mipaka kwa kisingizio cha “vita haina macho”. Moja ya maelekezo yake kwa makamanda walioongoza misafara ya kijeshi, ‘Umar Abdul Aziz aliwataka wajiegemeze kwa Allah(s.w) katika kila wanapokabiliana na maadui. Aliwataka wasipindukie mipaka katika kushambulia. Sehemu ya Waraka wake mrefu kwa makamanda wa Jeshi hilo umenukuliwa kama ifuatavyo:

*“Haya ni maelekezo kutoka kwa mja wa Allah na kamanda wa Waumini kwenda kwa Mansur Ibn Ghalib kamanda wa jeshi la kiislamu. Kamanda wa Waumini(Umar bin Abdul Aziz) anamuamuru Mansur kumpiga vita yule anayesimama kupambana naye. Aidha Mansur anaamriwa kumcha Mwenyezi Mungu katika kutekeleza wajibu huo na hiyo ndiyo strategija na nguvu halisi ya kijeshi. Dhambi ni hatari zaidi kuliko silaha ya adui. Kamanda wa Waumini anamuamuru Mansur badala ya kumuhofo adui anapaswa kuhofu kukiuka mipaka ya Allah. Tumekuwa tukiwashinda maadui zetu vitani si kutokana na uhodari mkubwa wa kijeshi tulionao bali ni kutokana na dhambi na maovu yao, ingelikuwa si hivyo tusingekuwa na ujasiri wa kupambana nao. Hatuwezi kuwa na jeshi linalolingana na lao kiidadi na kisilaha. Kwa hiyo iwapo tutakuwa watenda maovu kama maadui zetu bila shaka watatashinda kwa mapambano ya silaha. Tambueni, iwapo hatutamcha Mwenyezi Mungu hatutaweza kuwashinda maadui zetu kivita. Tuwe waangalifu zaidi wa matendo yetu. Msijiweke kwenye aibu ya kukiuka mipaka ya Allah. Kuweni wakarimu na wenye huruma, mkizingatia kuwa mmewaacha wapenzi wenu na majumba yenu kwa ajili ya Allah. Msijifakharishe mbele ya maadui zenu.*

*Kamanda wa Waumini vile vile anamtaka Mansur Ibn Ghalib awaongoze wapiganaji kwa upole na kujali hisia zao. Asiwe mkali na katili kwao. Na iwapo Mansur hatajali ubinadamu itakuwa nafasi nzuri kwa maadui kupata ushindi dhidi yake. Kamanda wa waumini anawaelekezeni kuwa waangalifu katika maeneo ya maadui, wekeni wapelelezi miongoni mwa maadui baada ya kuwachunguza na kuwaona ni waaminifu kwenu ili mpate ripoti kutoka upande wa adui. Hata hivyo, ripoti zilizo na udanganyifu ni za hatari kwenu katika uchukuaaji wa hatua, lazima muhakiki ripoti zao. Watakaowapeni habari kutoka kambi ya adui lazima nao muwatazame kama wapelelezi dhidi yenu. Amani ya Mwenyezi Mungu iwe juu yenu”.*

Kwa uadilifu na utendaji wake mzuri katika kuendesha Serikali, ‘Umar alifananishwa na Abubakar na aliitwa Khalifa wa tano wa Dola ya Kiislamu. ‘Umar bin Abdul Aziz alifariki mwaka 101Hijriya baada ya kutawala kwa miaka miwili na miezi mitano. Baada ya kufariki ‘Umar Abdul Aziz, ulifuatia msururu wa utawala wa Kifalme.



## **Maimamu Wanne wa Fiq-hi**

Pamoja na kutokea mara kwa mara viongozi wema waliojitahidi kuirejesha jamii ya Kiislamu katika sura yake asilia, kama alivyojitahidi ‘Umar bin Abdul Aziz, viongozi wengi waliendelea kuutawala ulimwengu wa Waislamu kwa kuimarisha Ufalme na Udikteta zaidi kuliko Uislamu. Lakini, pamoja na kuwepo hawa watawala waovu, bado palikuwepo watu wema katika miji mbali mbali ya Dola hizo za Kifalme. Kwamfano, mji wa Baghdad ulijaa watu ambao walikamatana na Uislamu. Aidha walikuwepo viongozi wa dini ambao, pamoja na kutotambuliwa na watawala, walisimama imara kuwaongoza Waislamu. Pamoja na maguvu na vyombo vya Dola vya kutisha walivyokuwanavyo watawala bado, raia waliwaheshimu na kuwatii zaidi viongozi wao wa kiislamu.

Katika kupanuka dola ya Kiislamu, tangu wakati wa Makhaliifa wanne wa Mtume(s.a.w), matatizo kadhaa yaliibuka ambayo yalihitaji ufumbuzi. Dola ilipanuka toka mashariki ya kati hadi Asia yote, sehemu za Afrika ya kaskazini na Hispania (Spain) huko Ulaya. Yaliibuka matatizo ya kisheria, taratibu za kibiashara na uchumi kwa ujumla na mila na desturi za watu mbalimbali . Uislamu ulitakiwa utoe fa-twa. Vinginevyo zingeibuka sheria na kanuni tofauti na Uislamu. Juhudi za mwanzo zilizofanywa ilikuwa ni utungaji na utoaji wa Fat’wa juu ya masuala mbalimbali kulingana na Qur’an na Sunnah. Hiki ndicho kipindi cha “Tabiina” ambacho waliibuka Maimamu wanne waliotumia uhai wao wote katika kutoa ufafanuzi, rai na Fat’wa juu ya sheria za Kiislamu katika mas’ala mbalimbali ya maisha. Hawa ni mabwana: Nu’man Ibn Thabit Abu Hanifa, Malik Ibn Anas, Muhammad Ibn Idris al-Shafii na Abu Abdallah bin Muhammad Ahmad Ibn Hambal. Wote hawa walitoa mchango mkubwa sana katika sheria ya Kiislamu na walikubaliana katika mambo yote ya msingi (Usul). Hawakufarakana kwa tofauti za maoni zilizojitokeza katika mambo madogo madogo.

Imam Abu Hanifa (80-150 A.H) na Imam Malik Ibn Anas (93-179 A.H) walirithi elimu ya moja kwa moja toka kwa masahaba iliyoegemea Qur’an na Sunnah. Aidha wao wenyewe walifanya juhudi kuongeza ujuzi wao kulingana na mazingira mapya yaliyokuwa yakijitokeza.

Imam Shafii (150 - 204 A. H) aliendeleza juhudi za Abu Hanifah na Malik kwa kufanya utafiti zaidi wa ukusanyaji na uchujaji wa Hadith, na maoni ya wataalamu mbalimbali wa sheria.

Imam Ahmad bin Hambal (164-204 A.H) aliandika Musnad ambacho ndicho kitabu mashuhuri kabisa cha Sunnah.

Maimamu wote hawa ama wamesoma na kufundishana au kusoma kwa Waalimu sawa. Imam Malik na Abu Hanifa wote walisoma Hadith kutoka kwa Imam Muhammad Ibn Shihab al-Zuhr. Imam J’afar al-Sadiq aliwahi

kuwa mwalimu wa wote Imam Abu Hanifa na Imam Malik. Aidha, wote hawa walisomeshwa pia na “Tabii” mashuhuri Muhammad bin al-Mukadir al-Madani.

Imam Abu Hanifah pamoja na utu uzima wake, alikuwa akihudhuria darasa hasa la Hadith la Imam Malik. Imam Shafii pia alisoma kwa Imam Malik. Kwa ujumla Maimamu wote wanne walihusiana sana katika kusoma kwao na japo walitofautiana katika maoni juu ya mambo kadhaa, walikuwa wamoja katika Uislamu na wakiheshimiana.

Hivi leo wapo watu wanaojinasibisha na madhehebu ambao hudai yapo madhehebu manne ndani ya Sunni wal-Jamaa, kila madhehebu ikinasibishwa na mmoja wa Maimamu hao wanne. Na japo haisemwi wazi wazi, lakini zipo hisia kwa mfano wanaojiita Shafii kuwaona wale wa Hambal, Hanafi na Malik kuwa hawapo sawa. Pengine na kinyume chake. Lakini hakika ya mambo na ushahidi wa vitabu vya historia haioneshi popote mabwana hawa kuhusika na fikra hizi za kuwa na madhehebu yasiyochanganyika. Kazi yao kubwa waliyofanya ni kutoa ufafanuzi wa kifiqh juu ya mas’ala mbalimbali na sio kuwagawa Waislamu kwenye madhehebu. Katika Uislamu suala la madhehebu ni uzushi. Labda ni vyema tuangalie kwa ufupi maisha na mchango wa kila Imam katika kuhuisha Uislamu.

## **Imam Abu Hanifah**

Imam Abu Hanifah ndiye anayenasibishwa na madh’hab ya Hanafi. Jina lake kamili ni Nu’man bin Thabit Abu Hanifah. Imam Abu Hanifah alizaliwa Kufa, Iraq katika mwaka wa 80 baada ya Hijrah. Yeye ni katika watu wa kipindi cha Tabiin kwani aliwashuhudia maswahaba wa Mtume ikiwa ni pamoja na Khalifa bin Abu Taalib, Anas bin Malik na Sahl bin Sa’d. Alipata elimu katika miji ya Kufa na Basra kisha Makka na Madinah. Miongoni mwa waalimu wake alikuwa Abdallah bin Umar mtoto wa Khalifa Umar bin Khattaab. Pamoja na kujikusanyia elimu nyingi na umaarufu kutokana na elimu na ucha Mungu wake; Imam Abu Hanifah alibakia kuwa mnyenyekevu na mwenye msimamo usiotetereka.

Mwaka 146 A.H Khalifah Mansur alimteua Abu Hanifah awe Kadhi; lakini alikataa akitoa hoja kuwa nafasi hiyo ni nzito kuliko uwezo wake. Mansur alikasirika na kumwambia Imam Abu Hanifah kuwa ni mwongo. Imam Abu Hanifah alimjibu, “kama mimi ni mwongo basi kauli yangu kuwa safai ni sahihi kwani mwongo hawezi kuchaguliwa kuwa Kadhi”. Mansur alikasirika zaidi na kumtupa gerezani Imam Abu Hanifah.

Hata hivyo, kutokana na vilio vya watu ilibidi Mansur aruhusu Imam Abu Hanifah aendeshe darsa hapo hapo jela. Lakini alivyoona watu wanazidi kufurika jela kuhudhuria darsa, alimpa sumu Abu Hanifah akafa katika mwezi wa Rajab 150 A.H., miaka kumi na nane (18) tangu Abbasids kushika mamlaka.

Jeneza lake liliswaliwa mara sita na kila mara watu zaidi ya hamsini elfu walisimama kumswalia. Na hata baada ya kuzikwa watu toka sehemu mbalimbali duniani walifurika kuja kuswali swala ya jeneza.

## **Imam Malik bin Anas**

Kwa mujibu wa “Kitab al-Ansab na Dhahabi, Tadhkirah al-Huffaz” juzuu ya kwanza, Imam Malik alizaliwa mwaka 93 A.H. Baadhi ya vitabu vimetaja pia mwaka 94 na 95 A.H. Wazazi wa Imam Malik walitoka katika familia ya kifalme ya Kiarabu toka Yemen ambayo ilihamia Madinah. Wakati anazaliwa Imam Malik dola ya Kiislamu ilikuwa chini ya uongozi wa Khalifa Walid bin Abd- al-Malik na japo makao makuu ya dola yalikuwa yamehamishiwa Damascus, Syria, lakini mji wa Madinah ulibakia mashuhuri na kitovu cha elimu ya Uislamu. Familia ya Imam Malik ilizungukwa na ndugu na jamaa wa karibu waliokuwa na elimu ya kutosha. Hivyo alianza kupata elimu yake katika mazingira ya nyumbani. Zaidi ya hapo alisoma kwa waalimu wengine saba mashuhuri wa fani mbalimbali, miongoni mwao alikuwa Jafar al-Sadiq, kitukuu cha Imam Hussein. Pamoja na kujikusanyia elimu nyingi, umaarufu wa Imam Malik ulizidi kuvuma kutokana na unyenyekevu na ucha Mungu wake. Watu walitoka masafa ya mbali kuja Madina kuhudhuria darsa za Imam Malik.

Sehemu kubwa ya muda wake aliitoa kwa kufundisha na akiifurahia kazi hii. Japo Imam Malik alikuwa mtaalam mzuri wa Hadith, lakini alikuwa dhaifu kidogo katika mambo ya sheria na kutoa fa-twa za kifiqh. Hata hivyo alikuwa mtu madhubuti na mwenye msimamo. Hakukubali kutolewa katika haki kwa hali yoyote iwayo. Wakati fulani alitoa fa'twa ambayo ilikuwa kinyume na matakwa ya Gavana wa Madinah. Gavana alimuonya asitoe fa'twa hiyo hadharani, lakini kwa kuridhika kuwa ndio haki, Imam Malik alitoa maoni yake hadharani na akachapwa viboko hadharani kwa tendo hilo. Katika kazi muhimu alizoziacha Imam Malik ni kitabu chake al-Muwatta chenye mjumuiiko wa Hadith na mafundisho ya Mtume(s.a.w) ya ibada na mas'ala mbalimbali ya Kiislamu. Imam Malik alitawafu mwaka 179A.H.Madinah.

## **Imam Muhammad Idris al-Shafii**

Imam Shafii alizaliwa mwaka (150 A.D.) huko Gaza katika ukanda wa Pwani ya bahari ya Mediteranean. Yeye ni wa kabila la Quraysh. Akiwa bado kijana, Imam Shafii alihifadhi Qur'an na Kitabu cha Imam Malik, al-Muwata. Alisoma elimu ya sheria ya Kiislamu toka kwa mwanachuoni mashuhuri na Mufti wa Makka Muslim bin Khalid al-Zanji. Baada ya kifo cha Khalid, alikwenda Madinah ambapo alisoma kwa Imam Malik bin Anas. Wakati Imam Malik anafariki tayari Imam Shafii alikuwa ashavuma ndani ya Arabuni na kwingineko kwa ujuzi wake wa elimu ya sheria na Uislamu kwa ujumla.

Kutokana na elimu na uadilifu wake, Imam Shafii aliteuliwa kufanya kazi Serikalini. Hata hivyo hakudumu kwani kwa uadilifu na utendaji wake wa kazi kwa haki aligongana na wakuu wa Serikali wasiotaka haki. Alikamatwa na kuhamishiwa Iraq akiwa amefungwa minyororo kwa tuhuma kuwa anafanya uchochezi dhidi ya Serikali. Huo ulikuwa mwaka 187 A.H. (803 A.D.) wakati wa utawala wa Harun al-Rashid. Baadae aliachiwa huru kwa kuonekana hana hatia. Alibaki kwa muda Baghdad akisoma chini ya wanafunzi wa Imam Abu Hanifah. Alifanya kazi ya kudarasisha Makka na akapata wasikilizaji wengi akiwemo Imam Ahmad bin Hambal ambaye wakati huo alikuwa anasoma Makka. Pamoja na kuwa alikuwa na maoni ya kifiqh tofauti na yale ya Imam Malik na Abu Hanafi, aliwaheshimu na kuthamini juhudi na michango yao. Hakujenga kundi la Shafii dhidi ya Maimamu wengine kama ambavyo baadhi ya Masheikh hufanya hivi leo.

Maimamu ambao tunajinasibisha nao hivi leo wao walikuwa wamoja katika Uislamu. Pale walipokuwa na maoni tofauti katika ufahamu wa baadhi ya mambo walikubaliana kutofautiana, wakazikubali tofauti zao, lakini walibaki kuwa wamoja walioshikamana katika kamba (dini) ya Allah(s.w).

Kazi kubwa ya kufundisha na uandishi, Imam Shafii aliifanyia Misri katika mji wa Cairo ya leo. Huko alizungukwa na wanafunzi na wanachuoni toka sehemu mbalimbali. Walijifunza na kuandika kila alichosema. Imam Shafii alikuwa na kawaida ya kuwaamrisha wanafunzi wake kusoma kwa sauti kila walichoandika ili apate kusahihisha. Kazi kubwa muhimu za Imam Shafii ambazo zinaendelea kutoa mchango mkubwa katika elimu ya Fiqh na sheria ya Kiislamu mpaka hivi leo ni Kitab al-Umm na Kitab al-Risalah Fi-Usul-al Fiqh (al-Risalah). Imam Shafii alifariki na kuzikwa Cairo mwezi Rajabu mwaka 204 A.H/201/820 A.D.

## **Imam Ahmad bin Muhammad bin Hambal**

Imam Abu 'Abdallah Ahmad bin Muhammad bin Hambal alizaliwa huko Marwa mwezi 20 Rabi-al-Awwal 164 A.H. Baba yake Muhammad alikuwa mujahid aliyesifika wakati akiishi Basra, Iraq. Baba yake aliamia Baghdad ambapo alifariki muda mfupi baadae na kumuacha Ahmad bin Muhammad akiwa bado mchanga. Pamoja na uyatima wake, kijana Ahmad alikuwa mwenye akili na akautumia ujana wake wote katika kujielimisha. Alisoma zaidi Hadith na akawa mwanasheria na mtaalam wa fiqh katika zama zake. Kwa hiyo Imam Shafii na Imam Ahmad Hambal walikuwa karibu sana. Imam Hambal alimheshimu mwalimu wake Shafii, na Imam Shafii alimheshimu mwanafunzi wake mashuhuri Hambal.

Imam Ahmad Hambal alikuwa mwanachuoni Mcha Mungu sana aliyejitoa maisha yake yote kusoma na kufundisha Hadith na Fiqh. Kwa ucha Mungu wake alikataa kufanya kazi Serikalini, kwani aliona Serikali ilikuwa haiongozwi

kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah. Zaidi ya hivyo alivunja uhusiano wa karibu na wote wale waliokubali kuwa ndani ya Serikali ya kidhalimu. Alikataa hata kupokea fedha au chakula kutoka kwa mtoto wake ambaye alikuwa akifanya kazi katika Serikali ile ya kidhalimu. Hata wakati alipokabiliwa na hali ngumu ya uchumi hakukubali kupokea msaada wowote ila kwa kuufanya kazi.

Katika kipindi cha uhai wa Imam Ahmad waliibuka wanafalsafa waliokuja na falsafa iliyoitwa Mu'tazili. Falsafa hii iliwaita watu wawe huria katika fikra. Walichanganya imani na kufr hata kufikia kuleta hoja kuwa Qur'an imetengenezwa tu. Harakati hizi za kuleta kufr ndani ya Uislamu zilitokana na athari ya falsafa za Wagiriki zilizowalevy baadhi ya Waislamu wa zama hizo.

Bahati mbaya watawala wa zama hizo nao waliathiriwa na falsafa hizo za Kigiriki na wakataka kuifanya kuwa imani rasmi ya dola ya Kiislamu. Viongozi waliotaka kuisimika imani hiyo ni Khalifa Ma'mun al-Rashid; Mu'taslim Billah na Al-Wathiq. Imam Ahmad bin Hambal alikataa kuikubali imani hiyo mpya ya watawala na akaendesha harakati kuipinga. Mtawala Mu'taslim alitoa amri akamatwe afungwe minyororo na kuhamishiwa Tarsus toka Baghdad. Huko alitupwa gerezani na kuteswa sana mpaka viungo vyake vingi vikavunjika. Imam Ahmad aliachwa adumu amefungwa minyororo mizito ndani ya chumba chenye giza gerezani. Pamoja na kuteswa sana ikiwa ni pamoja na kuchapwa mpaka kutoka damu, Imam Ahmad hakutetereka katika msimamo wake. Msimamo huu wa Imam Ahmad ulimstua Khalifa Mu'taslim. Aliikumbuka Akhera akahofia khatima yake. Aliamuru Imam Ahmad atolewe gerezani mwezi 25 Ramadhan mwaka 221 A.H na akamuomba msamaha, Imam Ahmad akamsamehe.

Miongoni mwa kazi muhimu alizofanya Imam Ahmad ni kuandika vitabu vifuatavyo: Kitab al-Amal al-Tafsir; Kitab al-Nasikh wal-Mansukh na kadhalika. Lakini kazi muhimu zaidi aliyoiacha Imam Ahmad ni ukusanyaji wa Hadith elfu nyingi na kuandika kitabu cha Hadith cha *Musnad ya Ibn Hambali*. Ulipofika mwaka wa 241 A.H Imam Ahmad alifariki dunia. Maelfu ya watu wa Baghdad walifurika kumzika.

### ***Hitimisho***

Maimamu wote wanne walikuwa wanachuoni wacha Mungu na waadilifu katika zama zao. Walifanya juhudi kubwa kusoma na kufanya ijthada ya kutafsiri na kutoa maoni yao juu ya sheria na masuala mbalimbali ya Fiqh. Ni vizuri tunufaike na matunda ya juhudi zao, lakini tusigawike wala kubaguana kutokana na maoni tofauti ya Maimamu hao juu ya masuala mbalimbali. Wao wenyewe walisoma pamoja au kusomesha na wakaheshimiana na wakaafikiana kutofautiana katika mambo ya msingi bila ya kugombana.

Jambo jingine la msingi la kuzingatia ni kuwa Maimamu hawa walipata mateso makubwa kutokana na misimamo na juhudi

zao katika kuuhuisha na kuusimamisha Uislamu katika jamii. Walichapwa viboko, walifungwa gereza na kufungwa minyororo na watawala madhalimu. Zaidi ya hivyo hawakukubali kununuliwa na Serikali. Walikataa kabisa kuwa vibaraka wa Serikali. Je, wakati tunafuata Fiqh na Fat'wa zao tunao pia uadilifu kama wao? Misimamo yetu juu ya Serikali za kidhalimu ni kama wao? Je, hatununuliwi na Serikali na kuifanyia kazi kinyume na maslahi ya Uislamu? Je, tupo tayari kufungwa na kuchapwa viboko kwa ajili ya kusimamisha haki kama Imam Abu Hanifa, Malik, Shafii na Hambal?

## **Zoezi la 5.2**

1. 'Umar bin Abdul-Aziz ameitwa 'Umar wa pili au Khalifa wa Tano wa Mtume(s.a.w). Jadili.
2. Tunajifunza nini kutokana na Historia ya 'Umar ibn Abdul-Aziz?
3. Bainisha maimamu wanne wa Fiqh wa wakati wa Tabiin na mchango wa kila mmoja katika kuhuisha Uislamu katika jamii yake.
4. Kwa kuzingatia wasifu wa maimamu wanne wa fiqh na ushirikiano wao katika kusoma na kusomesha tunajifunza nini juu ya suala la madhahabi waliyonasibishwa nayo?
5. Kwa kurejea historia ya maimamu wanne wa fiqh una maoni gani juu ya madha-hab manne yanayofuatwa na baadhi ya waislamu ?

## **KUHUISHA UISLAMU KATIKA KARNE YA 20 A.D**

### *Utangulizi*

Katika sura hii tutapitia harakati za baadhi ya vikundi mashuhuri vilivyojitahidi kuhuisha Uislamu katika karne ya 20 A.D. ambapo nchi nyingi za Waislamu zilikuwa chini ya ukoloni wa Wakristo wa Ulaya Magharibi zikiongozwa na Magavana au vibaraka wao. Vikundi vinne (4) mashuhuri vya harakati za kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii vilivyojitokeza katika karne ya 20 A.D ni:

- 1) Kikundi cha Badee – U-Zaman Said Nursi wa Uturuki.
- 2) “Ikhwan Muslimiin” kilichoasisiwa na Hassan al-Banna wa Misri.
- 3) “Ikhwani Muslimiin” kilichoasisiwa na Hassan al-Turabi wa Sudan.
- 4) Jama’atil Islamy kilichoasisiwa na Abul A’la Maududi wa Pakistan.

### **Badee – U-Zaman Said Nursi**

Imekuwa ni ada ya historia kwamba kila baada ya kipindi fulani hutokea muhuishaji (Mujadid) wa harakati za Kiislamu. Kama hivyo ndivyo; basi hapana shaka Badee-U-Zaman Said Nursi wa Uturuki alikuwa Mujadid aliyekuwa kupambana na maovu ya utawala wa dhalimu wa Mustafa Kamal Atatürk. Pamoja na vipingamizi vingi bado wafuasi wa Badee-U-Zaman wanafanya juhudi kubwa kuhuisha Uislamu hivi leo kupitia program mbali mbali. Badee-U-Zaman ni Mkurd aliyezaliwa huko Hizan jimbo la Bitlis Uturuki mwaka 1873. Ujana wake aliutumia kikamilifu katika kutafuta elimu. Awali, alisoma Qur-an, Sheria, Falsafa, Historia na Geografia. Baadaye aliona umuhimu wa kusoma Sayansi asilia. Kwa hiyo akasoma Hisabati, Baolojia na Lugha kadhaa za kigeni. Maisha yake yalikuwa rahisi na ya uadilifu. Qur-an na Sunnah vilikuwa ndio dira ya kila jambo lake. Alikuwa tayari kubaki njaa kama alikuwa na wasi wasi juu ya uhalali wa chakula kilicho mbele yake. Ilikuwa kawaida yake kuwapa chakula sisimizi na alipoulizwa kwanini anafanya hivyo alijibu kuwa ile ilikuwa zawadi yake kwa moyo wa kidemokrasia na utaratibu mzuri wa kazi wa wadudu hao wadogo.

### **Mwanzo wa Harakati Zake**

Siku moja Badee-U-Zaman alishtushwa na kauli ya Muingereza aliyekuwa Waziri wa Makoloni aliposema: *“Muda wa kuwa Waislamu wanayo Qur-an basi watakuwa kikwazo kwetu. Kwa hiyo ni lazima tuiondoe kutoka maishani mwao.”* Kutoka hapo akaamua kupambana bila ya kujali hatari yoyote itakayo mkabili. Alihamia Istambul na kuandaa mipango ya kuanzisha chuo Kikuu cha Zuhra mfano wa al-Azhar.

Baada ya mapinduzi ya mwaka 1908 ambapo Sultan Abdul Hamid II alipinduliwa: Badee-U-Zaman, alipambana na chama cha kisiasa kilichojulikana kama Kamati ya Umoja na Maendeleo. Chama hiki kilikuwa kimedhibitiwa na majasusi wa Kizayuni (Freemasons).

Katika kupambana na Chama hicho, Badee-U-Zaman, alianzisha Chama cha upinzani alichokiita **Ittihadil-Muhammad** kikiwa na malengo ya kuleta Umoja, Uhuru na Kusimamisha Uislamu. Aliandika na kusambaza makala ambazo zilielezea malengo na program za chama chake. Aidha aliwaonya Waislamu kuwa endapo watatafuta mwongozo wa maisha zaidi ya Qur-an na Sunnah, basi wajue wanakaribisha maangamizi.

Viongozi wa Kamati ya Umoja na Maendeleo hawakuweza kumvumilia Badee-U-Zaman. Walimkamata mnamo Machi 1909. Kumi na tisa kati ya wafuasi wake wakauawa. Badee-U-Zaman alifikishwa mahakamani. Baada ya hakimu Khurshid Pasha kupitisha hukumu ya kifo kwa wafuasi kumi na tano wa Badee-U-Zaman; alimgeukia na kumuulizia:

*“Wataka pia kutekelezwa kwa sheria ya Kiislamu?” Badee-U-Zaman alijibu; “Endapo ningepewa uhai elfu, ningetoa muhanga uhai huo kwa furaha, mmoja baada ya mwingine kwa ajili ya Uislamu. Jambo lolote geni katika Uislamu halikubaliki kwangu. Kwa hakika nangojea katika Barzakh kipando kitakacho nipeleka Akhera. Nipo tayari kwa safari ya kuungana na wenzangu ambao wamekwisha epukana na ukatili wako kupitia kitanzi.”*

Badee-U-Zaman alimalizia kwa kusema: *“Utamaduni na mfumo wa maisha ya Ulaya hauwafai watu wa Istambuli. Sifa zote ni zake Allah na ushindi ni kwa Uislamu”*.<sup>23</sup>

Tunapozungumzia mwanaharakati, huyu ndiye mwanaharakati. Tunapozungumzia subra na uvumilivu, basi kipimio chake ni hiki. Huku ndiko kujitoa muhanga kwa ajili ya Allah(s.w). Mahakama ilimwachia huru Badee-U-zaman kutokana na malalamiko ya wafuasi wake.

Baada ya kukaa kidogo Istambul, alikwenda Damascus, ambapo alitoa nasaha katika misikiti kuelezea matatizo yanayo ukabili Ummah wa kiislamu. Aliyataja matatizo hayo kuwa ni mifarakano ya kijamii na siasa, ubinafsi na kukata tamaa. Tatizo lingine alilolitaja kuwa linatishia Ummah ni kukua kwa tawala za ukandamizaji na kidhalimu.

Aliwahimiza Waarabu na Waturuki wajenge Umoja madhubuti kwani kushinda katika mapambano baina ya Waislamu na makafiri kunategemea sana Umoja wa Waislamu.

Baada ya safari yake ya Damascus alitumia muda wake mwingi kuanzisha Chuo Kikuu ambacho Mitaala na Mihutasari yake ingeweka pamoja mafundisho



ya Uislamu na elimu ya sayansi asilia na sayansi ya jamii. Hata hivyo kabla lengo lake halijitimia vita kuu ya kwanza ya dunia ililipuka.

Badee-U-Zaman akaingia vitani akiungana na jeshi la Kituruki. Kutokana na ujasiri wake alipewa Uafisa. Katika kambi yake alijenga mazingira ya kufanya lbada na kusomesha Qur-an. Askari wengi wakawa wanafika kambini kwake kusoma.

Kwa bahati mbaya kikosi chake kilizidiwa sana nguvu na Warusi, ambapo karibu askari wenzake wote waliuawa na yeye mwenyewe kupelekwa mateka Urusi.

Siku moja Generali wa Kirusi; Generali Nicholas alitembelea kambi (jela) yao. Wafungwa wote walisimama na kumpigia saluti isipokuwa Badee-U-Zaman peke yake. Generali Nicholas akamshangaa na kumuuliza endapo anamfahamu yeye ni nani. Badee-U-Zaman alijibu:

*“Ndio nakujua u Generali Nicholas Nikolarch. Lakini hiyo si hoja kwangu. Mimi ni Muislamu. Kwangu Muislamu ni bora kuliko kafiri. Namuabudu Allah peke yake. Siwezi kukutukuza.”*

Maneno haya ya kijasiri na pengine yanayoweza kuitwa ya kijeuri yalimfikisha Badee-U-Zaman kwenye mahakama ya kijeshi ambapo alizawadiwa adhabu ya kifo. Aliomba apewe fursa apate rakaa mbili kisha wampige risasi. Baadhi ya marafiki zake wakawa wanamshauri aombe msamaha. Lakini yeye aliwajibu; *“Pengine hukumu hii yaweza kuwa hati (passport) ya kunipeleka peponi.”*

Hatimaye Afande Nicholas alikuja akamuomba msamaha Badee-U-Zaman na kumwambia: *“Kwa sababu ya ukweli, imani na ujasiri wako adhabu ya kifo imefutwa”*. Baada ya miaka miwili na nusu ya ufungwa na utumwa huko Siberia; Badee-U-Zaman alitoroka na kuingia Istambul kupitia Petersburg, Warsaw na Vienna. Alipoingia Ankara alipata mapokezi makubwa kutoka kwa maulamaa na watu wa kawaida.

Mwaka 1920 Mustafa Kamal Ataturk alimwalika ahudhurie sherehe za siku ya Uhuru huko Ankara. Bade-U-Zaman alikwenda Ankara. Lakini kwa mshangao hakuona alama yoyote ya Uislamu kwa Mustafa Kamal Ataturk. Akaamua aondoke Ankara bila kuhudhuria sherehe hizo huku akiacha ujumbe kwa bunge la Uturuki lililokuwa likiongozwa na Kamal Pasha. Ujumbe wenyewe ulisema:

*Enyi wabunge! Kumbukeni siku ambapo mtahudhuria mbele ya Allah(s.w), Mfalme wa siku ya malipo. Msiharibu mazuri yaliyopatikana kutokana na kuwashinda maadui toka nje kwa ubaya kutokea ndani. Kama mna hiari kuwaiga wazungu na mifumo isiyokuwa ya Kiislamu; Waislamu watatafuta msaada kutoka watu wengine.*

Ujumbe huu ulisomwa Bungeni na Kazim Pasha na kuleta athari ya ajabu.

Wabunge waliowengi walichukua ahadi ya kuanza maisha mapya ya Ucha-Mungu ambapo Swala tano zilipewa umuhimu wa kwanza.

Hali hii ilimumiza sana Mustafa Kamal. Alimwita Badee-U-Zaman na kumshutumua kwanini analeta vurugu kwa kusisitiza umuhimu wa swala. Badee-U-Zaman alimjibu kuwa swala ndio jambo nambari moja katika Uislamu. Kama unaipuuza swala, Umemuasi Mwenyezi Mungu na hivyo basi utawala wako hauwezi kukubaliwa na kutiwa.”

Mustafa Kamal alidhani njia nzuri ya kumnyamazisha ni kumpa wadhifa. Akamchagua kuwa Mhubiri Mkuu wa jimbo la Anatolia na Mjumbe wa Baraza la Utendaji la Chuo Kikuu cha Dar-ul-Hikmat. Pamoja na marupurupu mengine alipewa jumba la fahari la kuishi. Lakini Badee-U-Zaman alikataa fadhila hizo akakimbilia Ankara ambapo aliendelea na kazi yake ya kuwaelimisha watu.

Haukupita muda Serikali ikamkamata na wafuasi wake. Kwa miaka minane Badee-U-Zaman aliwekwa kizuizini katika jela yenye ulinzi mkali sana. Hata hivyo askari jela waligeuka kuwa wafuasi wake kutokana na ujumbe aliowafikishia.

Akiwa kifungoni huko Burla, Badee-U-Zaman alianza kuandika ujumbe aliouita Risalat-Nuur uliopenya kuta za gereza na ulinzi mkali wa askari magereza na kuwafikia watu mitaani. Kila aliyepata nakala; alinakili upya na kuisambaza kwa wengine. Kwa mtindo huo Risalat-Nuur iliawafikia maelfu ya wasomaji.

Baada ya kifungo chake Burla, alielekea Isparta ambapo haukupita muda alikamatwa tena na wafuasi wake 120 kwa tuhuma kuwa amekula njama za kutaka kuipindua Serikali na kwamba anafanya shughuli za kuhubiri na kufundisha Qur-an bila ya kibali cha Serikali wakati kuna idara ya kazi hizo.

Kwa shutuma hii ya kufanya kazi bila ya kibali cha Serikali Badee-U-Zaman aliwajibu kuwa hawezi kuomba kibali cha kumuabudu Mwenyezi Mungu. Kisha akawauliza; *“Hivi nyinyi mwaweza kuzuia kifo (watu wasiendeleo kufa) kwa kuyafunga maeneo yote ya makaburi?”* Maana yake ni kwamba kama hilo hamliwezi vile vile hamuwezi kuzuia dini ya Allah kwa kuwazuia watu wasihubiri ila kwa vibali vyenu.

Baada ya malumbano makali mahakamani, Badee-U-zama aliachwa huru. Hata hivyo miaka michache baadaye alikamatwa tena na kufikishwa katika mahakama kuu ya Afyon kwa shutuma na madai yale yale ya awali.

Badee-U-Zaman alitoa maelezo marefu katika mahakama kuu ya Afyon na akamalizia kwa kusema:

*“Endapo Qur-an haina wafuasi katika ardhi hii nitahisi mateso makubwa hata kama nitawekwa peponi; lakini kama nitaona imani (ya Kiislamu) ya Waturuki ipo katika salama; nitapata furaha kubwa hata kama kiwiliwili changu kitakuwa kinaunguzwa katika moto”.*

Mahakimu na majaji waliokuwa wanaiendesha kesi hii walisita. Wakamuona Badee-U-Zaman hana hatia na wakageuka kuwa wafuasi wake. Lakini hamu ya dikiteta Mustafa Kamal Atatürk ni kuona harakati za Kiislamu haziendelei. Kesi iliamishwa mahakama nyingine ambapo ikawa inapigwa tarehe huku Mujaddid Badee-U-Zaman akiozea rumande.

Miezi miwili kabla ya kifo chake alipata ruhusa maalum akatembelea Ankara kisha Istanbul ambapo alipata mapokezi makubwa sana. Maadui wakahisi taabu wakamkamata na kumweka ndani. Katikati ya mwezi wa Ramadhan alipata maradhi ya ghafla. Aliwaomba wafuasi wake wamtoroshe kwa siri hadi Urfa ambapo alifariki mnamo 27 Ramadhan, mwaka 1959 akiwa na umri wa miaka 86.

Baada ya harakati za Kiislamu zilizoandamana na vifungo na mateso mbali mbali kwa ajili ya Allah(s.w), maisha ya Badee-U-Zaman, yalifikia ukingoni akiwa ameteteleza wasia wa aya ifuatayo:

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا اتَّقُوا اللّٰهَ وَابْتَغُوْا اِلَيْهِ الْوَسِيْلَةَ وَجَهْدُوْا فِيْ  
سَبِيْلِهِ لَعَلَّكُمْ تَفْلِحُوْنَ

*Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na tafuteni njia ya kumfikilia (kufikilia Pepo yake). Na piganeni kwa ajili ya dini yake ili mpate kufaulu. (5:35).*

### **Mafunzo:**

Kupitia Maisha na harakati za Badee-U-Zaman tunapata mafunzo makuu yafuatayo:

- (1) **Ujasiri na uvumilivu.** Maisha ya Badee-U-Zaman ni kielelezo tosha cha kiwango cha ujasiri na uvumilivu anaotakiwa awe nao Muislamu. Mateso na vitimbi vya madhalimu havikumyumbisha wala kumtoa kwenye lengo.
- (2) **Subira na kukamatana na lengo.** Pamoja na ujasiri lipo suala la subira na kudumu katika lengo. Pamoja na mateso na wakati mwingine vishawishi vya kupewa maslahi, Badee-U-Zaman hakutoka katika lengo la kuifundisha na kuisimamisha Qur-an.
- (3) **Nafasi ya Elimu.** Pengine jambo lililosaidia sana kufanikiwa Badee-U-Zaman ni kuzingatia kwake umuhimu wa elimu. Yeye binafsi alijielimisha

na alipoanza harakati, mkazo mkubwa aliuweka katika kuanzisha taasisi za elimu. Kwa njia hiyo watu wengi walielimika na kulijua lengo.

- (4) **Mwenendo mzuri.** Badee-U-Zaman na wafuasi wake walikuwa ni watu wa maadili mazuri ya kuigwa katika jamii. Hakuna mmoja wao aliyekamatwa au kushutumiwa kwa makosa ya kipuuzi au uhalifu dhidi ya sheria za nchi. Muda wote Serikali ilikuwa inapata taabu kufikisha mahakamani tuhuma za kutunga ambapo mahakama nazo zilikuwa zikipata taabu kuzikubali. Mtu unapoiingia katika harakati za Kiislamu uangalifuzaidi unatakiwa. Usipatikane mwanya wowote wa mtu kushutumiwa kwa dosari zozote ambazo zaweza kutia doa msimamo na juhudi zake katika dini.

## **Ikhwani Muslimiin wa Misr.**

Ikhwani Muslimiin ni kikundi cha harakati za Kiislamu ambacho kimeenea takriban katika nchi zote za Kiarabu. Harakati za Ikhwani toka kuanzishwa kwake zimelenga katika kuusimamisha Uislamu, ambapo sheria za Allah zitatawala katika kila kipengele cha maisha ya Muislamu kijamii na kwa mtu binafsi. Njia inayotumiwa kufikia lengo hilo ni:

- (a) Kujenga imani madhubuti juu ya Uislamu.
- (b) Mafunzo maalum ya harakati.
- (c) Kazi au utendaji wa kudumu.

Historia ya Ikhwani Muslimiin huanzia mwaka 1906 alipozaliwa muasisi wake – Shahiid Hassan Al-Banna. Yeye alizaliwa katika kijiji cha Mahmudiya na kupata elimu yake mjini Cairo ambapo mwaka 1927 alihitimu na kupata stashahada ya ualimu na kupangiwa kusomesha huko Ismailiya.

Katika kipindi hiki cha historia, wimbi la kuingia na kusambaa kwa utamaduni wa kimagharibi liliathiri sana Misri. Nadharia za kutenganisha Dini na Serikali (secularism), wanawake kwenda nusu uchi, kuenea kwa vishawishi vya zinaa, sinema na maovu mengine vilikuwa vikikita mizizi Misri kwa kasi kubwa. Uislamu ulikuwa ni suala la mtu binafsi na hata kwa ngazi hiyo kwa wengi ulibaki wa kuswali na kufunga tu.

Hali hii ilimuathiri sana Hassan Al-Banna. Alijiona anajukumu la kuuelimisha Ummah na kuuhisha upya Uislamu. Jitihada zake zilianza kwa kuunda kikundi cha wenye kuamrisha mema na kukataza maovu. Walielimisha watu, wakachapisha mabango yenye maamrishi na makatazo na wakayabandika misikitini na mitaani.

Kadri Hassan Al-Banna aliyoichambua jamii yake aliona inakwenda kasi kuelekea maangamizi yake kwa kuutupa mfumo wa maisha wa Kiislamu. Katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili aligundua kuwa:

- (1) Mahubiri ya Masheikh misikitini pekee hayatoshi.
- (2) Masheikh walio wengi walishindwa kabisa kupambana na wanaojiita “Secularists”(wasiofuata dini katika mambo yao) na “Modernists (wasomi wa kisasa).”Moderatist” (wanao chukua nusu Uislamu na nusu umagharibi)
- (3) Masheikh walio wengi walinunuliwa kirahisi na Serikali.

Kwa kuzingatia haya na hali halisi ya jamii, Hassan Al-Banna alianzisha kundi la harakati za Kiislamu mwaka 1928. Kundi hilo aliliita Ikhwani Muslimiin na alianza na wafuasi sita.

Kwa muda kama wa miaka minane hivi jitihada zote zilielekezwa katika kuwaelimisha Waislamu juu ya Uislamu wao kwa njia za darasa, mihadhara, mawaidha misikitini na kwa njia ya maandishi ya vitabu, magazeti,vipeperushi, n.k.. Uangalifu mkubwa sana ulichukuliwa katika kupata wana harakati. Yaliwekwa mafunzo maalum ambayo ilikuwa ni lazima kila mwanaharakati ayapitie.

Harakati zilianza kuyavuta macho ya Serikali mwaka 1936 wakati Hassan Al-Banna alipomwandikia Mfalme na Mawaziri wake kuwa waache tamaduni za Ulaya Magharibi na wafuate Uislamu.

Baada ya kupita kipindi cha mafunzo, wanaharakati wa Ikhwani Muslimiin waliingia katika kipindi kigumu ambapo makucha yote ya Serikali yalielekezwa kwao.

Mwaka 1949 Serikali ilipiga marufuku chama cha Ikhwani Muslimiin, wanachama wakawekwa ndani na mali zao kutaifishwa. Tarehe 12/2/1949 Hassan Al-Banna aliuawa kwa kupigwa risasi.

Kuuawa kwa Hassan Al-Banna hakukusimamisha harakati. Hassan Ismail Hidaybi alishika hatamu za uongozi na mapambano dhidi ya viongozi wasiotaka Uislamu kusimama yakaendelea. Yafaa kusesitiza hapa kuwa wanaharakati wa Ikhwani Muslimiin hawakuwa wanaendesha harakati ili wao wachukuwe madaraka ya kuiongoza Serikali, bali lengo lao ni kuona uovu unaondoshwa katika jamii na Uislamu unasimamishwa na Serikali ya kitwaghuti. Maneno yafuatayo ya Rais Jamal Abdul Nasser yanathibitisha mahitajio yao:

*“I met the Supreme Guide of the Muslim Brothers who then made demand on me. The first thing he asked was that we should proclaim that women should wear the veil, He then made other demands such as the closing down of the cinemas and theatres – in other words to make life dark and gloomy. It was of course, impossible to do such a thing”.*<sup>24</sup>

**Tafsiri:**

*“Nimekutana na kiongozi wa ngazi ya juu wa Ikhwani Muslimiin ambaye alileta madai kwangu. Kitu cha kwanza alichokitaka ni kwamba tuwaamrishe wanawake kuvaa Hijabu. Pia ameleta madai mengine kama vile kufunga majumba ya senema na majumba mengine ya starehe, kwa maana nyingine kuyatia maisha gizani na kuyadodesha. Bila shaka haikuwezekana kufanya kitu kama hicho”.*

Jaribio la kutaka kumuua Jamal Abdul Nasser Desemba 1964 lilitoa mwanya kwa Serikali, ikasingizia kuwa ni Ikhwani waliohusika. Wengi wakafungwa na sita wakahukumiwa kifo.

Rais Nasser aliunda kikosi maalum cha kuwashughulikia Ikhwani. Kikosi hicho kilitoa mapendekezo yafuatayo:

- (1) Somo la Uislamu (Islamiat) liondolewe katika mitaala ya masomo mashuleni. Badala yake utengenezwe mtaala wenye kusisitiza maadili ya Ujamaa.
- (2)Ukomunisti upewe fursa uvunjilie mbali imani za dini na harakati za vikundi vyenye mwelekeo wa Kikomunisti ziruhusiwe na vingine vyote vya Kiislamu vipigwe vita.
- (3) Watu wa dini (Uislamu) hata wale wasiotambulika kama memba wa Ikhwani wapigwe vita.
- (4) Vifungo na adhabu kali ziwaandame Ikhwani na wasipewe muda wa kupumua.

Kutokana na mapendekezo haya mateso makali yaliwaandama Ikhwani. Hassan Ismail Hdaybi aliyeshika uongozi baada ya Hassan Al-Banna alichapwa kwa mnyororo mzito mpaka akafa. Tarehe 29 agosti 1966 viongozi watatu walihukumiwa kunyongwa miongoni mwao akiwemo Mwanachuoni na Mwandishi mashuhuri, Sayyid Qutb. Kaka yake, Muhammad Qutb na dada yake, Amina Qutb, nao walitiwa kifungoni miezi michache kabla ya kuuwawa kwake. Dada yao mwingine Hamida Qutb alihukumiwa kifungo cha miaka 10 na kazi ngumu. Bibi Zainabu Al-Ghazal aliyekuwa Amirat wa Umoja wa Wanawake wa Kiislamu chini ya Ikhwani alikamatwa na kuteswa sana – rejea Kitabu chake – *“Siku katika Maisha yangu”*.

“Hawa ni baadhi tu ya wanaharakati wa Ikhwani Muslimiin na mateso waliyoyapata. Hata hivyo mateso hayo hayakusaidia kitu zaidi ya kuwapa mafunzo na kuwanoa zaidi kiimani wana-Ikhwani kwani harakati mpaka hivi leo zinaendelea. Hii ndio kawaida kama anavyo tukumbusha Allah(s.w):

وَلَمَّا رَأَى الْمُؤْمِنُونَ الْأَحْزَابَ قَالُوا هَذَا مَا وَعَدَنَا اللَّهُ وَرَسُولُهُ

وَصَدَقَ اللَّهُ وَرَسُولُهُ ۗ وَمَا زَادَهُمْ إِلَّا إِيمَانًا وَتَسْلِيمًا ﴿٣٣﴾

*Na Waumini walipoyaona majeshi (ya makafiri yamewashambulia hivyo), walisema: “Haya ndiyo aliyotuahidi Mwenyezi Mungu na Mtume wake “(kuwa tutapata misuko suko kisha tutashinda). Mwenyezi Mungu na Mtume wake wamesema kweli.” Na (jambo hili) halikuwazidishia ila imani na utii”. (33:22)*

## Muundo

Wanaharakati waligawanywa katika daraja tatu kutokana na kiwango cha juhudi na ushupavu waliokuwa nao katika kuendesha harakati hizi za Kiislamu. Palikuwa na:

- Kundi la kwanza (1st class)
- Kundi la pili (2nd class)
- Kundi la tatu (3rd class)

Mwana harakati alipanda daraja baada ya kupitia mafunzo maalum na kula kiapo. Ili kuwadhibiti wanaharakati na kurahisisha ufuatiliaji wa majukumu, wanaharakati waligawanyika katika vitengo(idara) mbali mbali vyenye majukumu tofauti. Mfano: Idara ya kushughulikia harakati za wanafunzi, kundi la mambo ya siasa, Idara la mambo ya Usalama na ulinzi, Idara ya mambo ya utamaduni; Idara ya huduma za kijamii na misaada; Idara ya elimu na mafunzo; Idara ya uchumi, Idara ya habari na utafiti n.k. Kila mwanahaarakati alitakiwa aweke kumbukumbu za utekelezaji wa majukumu yake.

## Matatizo

- Kupambana na nguvu za Jahiliya.
- Watu wengi kuteswa na kuuawa.

## Mafanikio

Ikhwani Muslimiin walifanikiwa kuweka msingi madhubuti wa harakati za kuung’oa ujahili. Harakati nyingi ambazo leo hii zinaupigania Uislamu, zina athari ya Ikhwani Muslimiin. Mfano mkubwa ni Sudan.

## **Ikhwani Muslimiin wa Sudan.**

Harakati za Ikhwani Muslimiin ziliingia Sudan katika miaka ya 1950 hivi. Harakati zilianzia Chuo Kikuu cha Khartoum, kisha zilienea kwenye vyuo vingine, mashuleni na sehemu za kazi.

Kimuundo na kimbinu, harakati zilichukua sura ile ile ya Ikhwani Muslimiin wa Misr. Wakati harakati hizi zinaingia Sudan, hali ya jamii ilikuwa mbaya sana. Kwani Uislamu ulikuwa ni kitu kilichotupwa na badala yake maadili ya Ulaya Magharibi na “*Umaksists*” vikawa vinashindana kushikilia hatamu za uongozi katika jamii.

Kupiga adhana na kuswali katika Chuo Kikuu kulionekana kiroja, mitaani wanawake walishavua Hijab zao, ulevi, kamari na maovu mengine yalishamiri mno katika jamii.

Katika Chuo Kikuu pamoja na jitihada za kuufundisha Uislamu vilivyo, harakati ziliendesha kampeni dhidi ya ukomunisti. Wanafunzi wanaharakati walisoma historia na nadharia ya Ukomusti wakaelewa vyema. Kisha kwa kutumia hoja toka kwenye Qur-an wakaonyesha udhaifu na upotofu wa Ukomunisti.

Kutokanana jitihada kubwa waliyoifanya kidogo kidogo Uislamu ukawa unaibuka chuo Kikuu na ukomunisti hatimaye ukawa ni kitu cha mtu kuona aibu kunasibishwa nacho.

Mwaka 1963 Dr. Hassan Turabi alirudi toka masomoni Ufaransa na kushika hatamu za uongozi wa harakati za Kiislamu. Kuelekea miaka ya 1970 hadi 1973 wanaharakati walipambana na mateso makubwa. Wengi walifungwa na kazi ngumu, kufilisiwa mali, kuishi uhamishoni n.k. Kutokana na matatizo haya uongozi uliangalia upya mbinu za utendaji kazi na wakaamua kubadili mbinu. Badala ya kufanya kazi nje ya serikali wakaona waingie ndani ya Serikali,waibane na kushinikiza kusimamisha Dola ya Kiislamu.

Mbinu hii ilifanyiwa kazi na hadi kufikia mwaka 1980 ikawa wanaharakati wengi wameshaingia katika sehemu nyingi nyeti za serikali. Ikawa serikali haipangi jambo la kuwadhuru wanaharakati ila watapata habari.

Wakati harakati zinaendeshwa kuizingira serikali, wanachi kwa ujumla walielimishwa na kuhamasishwa juu ya umuhimu na ulazima wa kusimamisha Sheria za Kiislamu katika jamii.

Kutokana na mbinu hizi serikali ilijikuta imezingirwa katika vyombo vyake vyote muhimu na wakati huo huo ikawa imenyang'anywa imani ya wananchi. Ni katika hali hii aliye kuwa Rais wa nchi hiyo, Jaafar Nimeir, ilibidi atangaze Serikali ya Kiislamu. Wanaharakati walijua vyema kuwa tangazo la Nimeiri ni la kinafiki kwani limetoka wakati maji yamemfika shingoni. Lakini waliona ni



vyema waliunge mkono tangazo lake ili wapate kutumia fursa ile na kutumia vyombo vya dola kufanikisha harakati zao.

Baada ya Nimeir kupumua kidogo aliandaa mkakati wa kuwakamata wanaharakati, hasa viongozi na kuwaweka ndani. Hata hivyo baada ya kuwakamata haukupita muda mrefu naye akapinduliwa na wanaharakati wakazidi kupata nguvu.

## **Wanaharakati wa Sudan katika Uwanja wa Siasa**

Kutokana na mabadiliko ya kisiasa yaliyoruhusu kuwapo vyama vingi vya siasa, mwaka 1985 wanaharakati walianzisha chama chao cha siasa, **National Islamic Front (N.I.F)**. Chama hiki kimekuwa maarufu na chenye sauti kubwa katika maongozi ya nchi. Hivi leo Sudan hakiwezi kufanikiwa kuchukua uongozi chama chochote bila ya ridhaa ya NIF.

Serikali ya Saddik Al-Mahd ilijaribu kuwaweka lkhwan nje ya serikali lakini haikuweza kupiga hatua. Na alipowaingiza ndani ya serikali hakuweza kupitisha lake kama hakupata ridhaa ya NIF.

### **Matatizo:**

Kama ilivyo mahali popote ambapo pana harakati za Kiislamu, wanaharakati wa Sudan walipambana na makucha ya serikali. Kuna waliouawa, wengi wametumikia vifungo virefu, na wengi wameishi uhamishoni muda mrefu, n.k.

### **Mafanikio**

Kundi limefanikiwa kuweka msingi madhubuti wa harakati za Kiislamu Sudan. Wamefanikiwa kujiimarisha kiuchumi kwa kuanzisha makampuni makubwa ya biashara na uzalishaji mali ndani na nje ya Sudan. Wamefanikiwa kuendesha mabanki ya Kiislamu. Mabanki haya yana matawi mengi ndani na nje ya Sudan pia. Kwa hiyo utaona kuwa zaidi ya kuwa wanapanga mambo yao kulingana na uwezo wao bila kuomba misaada, wanatoa nafasi za ajira kwa wananchi. Yaani wanajajiri kutokana na makampuni yao ya uzalishaji mali.

## **Jama'atil Islamy ya Pakistan.**

Mwanzilishi wa Jumuiya ya Jama'atil-Islamy ni Maulana Sayyid Abul Ala Maudud aliyezaliwa tarehe 25 Septemba, 1903 huko Aurangabad, Pakistan wakati huo Pakistan ikiwa ni sehemu ya India.

Sehemu kubwa ya elimu ya Maudud aliipata nyumbani katika madrasa za Masheikh. Hii ni kwa sababu baba yake aliogopa kuwa mtoto wake ataharibika katika shule za kawaida zilizofuata mitaala ya kimagharibi.

Wakati akiwa na miaka kumi na sita, baba yake alifariki. Kwa hiyo, mwaka 1920 alianza kujitegemea kwa kufanya kazi ya uadishi wa habari. Aliyafanyia kazi magazeti ya “*Taj*” na “*al-Jamiat*”. Mwaka 1932 alikwenda Hyderabad ambapo alianzisha gazeti lake la kila mwezi lililoitwa “*Tarjuman ul-Qur-an*”.

Januari 1938 aliitwa na Allama Muhammad Iqbal kwenda Punjab kufanya kazi ya kuihuisha sheria ya Kiislamu. Iqbal alikufa mwaka huo huo mwezi April na Mauduud akahamia Lahore ambapo alichaguliwa kuwa Mkuu wa kitivo cha dini bila ya malipo. Mwaka mmoja baadaye, Serikali ilisisitiza apewe mshahara lakini Mauduud, alikataa kwa kuhofia kuwa wakimlipa watamdhiti katika harakati zake. Kwa hiyo aliacha kazi hiyo na mwaka 1941 akaanzisha rasmi kikundi cha harakati za Kiislamu alichokiita Jama’atil-Islamy.

Maulana Mauduud ulianza kutambulika umaarufu wake mwaka 1926 baada ya kufafanua kwa kina katika jarida lake nadharia ya Jihad na kuitofautisha na vita vya kawaida.

Mwaka 1932 Mauduud aliandika kitabu maarufu kiitwacho *Towards Understanding Islam* (Katika kuufahamu Uislamu). Lengo la kuandika kitabu hicho lilikuwa kuwasaidia wasomi kuelewa Uislamu katika usahihi wake. Mwaka huo huo wa 1932 alianza kuchapisha *Tarjuman ul-Qur-an*.

Maulana Mauduud alieleza kwamba mpango aliokuwa nao mwaka 1932 alipoanza kuandika *Tarjuman ul-Qur-an*, ulikuwa kuvunja fikra potofu za Kimagharibi ambazo zilishaingizwa katika bongo za wasomi wa Kislamu. Alitaka kuwaonyesha kuwa Uislamu ni mfumo kamili na sahihi wa maisha usiohitaji kukopa jambo lolote kutoka mfumo wa kikafiri.

Zilipoanza harakati za Pakistan kujitenga kutoka India ya leo, Mauduud aliziunga mkono. Hata hivyo alionyesha wasi wasi wake kuwa yaelekea harakati hizo hazina msingi madhubuti wa kusimamisha Dola ya Kiislamu Pakistan bali Utaifa tu. Ili kuhakikisha kuwa Paksitan inakuwa dola ya Kiislamu na Waislamu watakaobaki India bado wanabaki Waislamu; Maulana Mauduud aliona kuna ulazima wa kuanzishakundi la harakati, Jama’atil-Islamy. Kwa kujua majukumu na lengo la Jama’atil-Islamy Mauduud alikuwa makini katika kupata wanakundi. Hakutaka kuunda jumuiya ambayo itakuwa wazi kwa kila mtu. Alitaka kundi la watu wenye tabia njema wasiotetereka katika maadili. Alitaka watu walio tayari kujitoa muhanga kwa ajili ya Uislamu.

Baada ya Pakistan kujitenga tarehe 14 Agosti, 1947 Mauduud alizipeleka juhudi zake katika kusimamisha mfumo wa Kiislamu Pakistan. Kati ya Januari na Machi, 1948 alitoa mfululizo wa vipindi katika Redio ambapo aliuchambua mfumo wa Uislamu kwa kuangalia falsafa, maisha ya kiroho, maadili, mfumo wa elimu, uchumi na utamaduni. Kwa kuendesha harakati kuwa Pakistan iongozwe Kiislamu, alishutumiwa kuwa ni adui wa Serikali kwa hiyo akatupwa gerezani toka tarehe 4 Oktoba 1948 hadi 28 Mei, 1950.

Hata hivyo juhudi zake hazikupotea bure, kwani hoja na mapendekezo yake yalipitishwa na bunge mnamo 7 machi, 1949

Kati ya mwaka 1952 na 1953 Waislamu wa Pakistan waliitaka Serikali ipitishie sheria ambayo itatamka wazi kuwa Makadiani sio Waislamu. Serikali ilitangaza sheria ya kijeshi kuzima harakati hizo. Mauduud aliandika makala aliyoiita: *“Tatizo la Qadiani” (The Qadiani Problem)* kuishutumu Serikali kwa msimamo wake na kuwatumia Makadiani kwa lengo la kuuvuruga Uislamu. Kwakuandika makala hiyo iliyobainisha wazi kwa data kuwa ukadiani si dhehebu la waislamu bali ni dini iliyeundwa na waingereza ili kuwagawanya waislamu ipate kuwatawala vizuri, ilimgharimu Mauduud kufungwa gereza bila yakufikishwa Mahakamani na hatimaye kuhukumikiwa adhabu ya kifo. Hata hivyo Mauduud aliposikia hukumu hiyo alisema:

*“Kama Mungu amependa ninyongwe, nitaipokea hukumu hiyo kwa furaha; lakini kama si mapenzi ya Mungu nife sasa; kwa vyovyote watakvayofanya, hawatanidhuru hata chembe.”*

Alipotakiwa aombe msamaha ili asamehewe Maulana Mauduud alikataa. Hata hivyo ulimwengu wa Kiislamu ulipiga kelele kupinga hukumu hiyo ya kifo. Hali hiyo ilipelekea hukumu ya kifo kubatilishwa na kuwa kifungo cha miaka 14. Lakini alipofikia tarehe 25 Mei, 1955 aliachiwa huru kwa amri ya Mahakama Kuu.

Mwezi machi 1956 katiba ya Serikali ya Kiislamu ya Paksitan ilipitishwa ambapo mapendekezo mengi ya Jama’atil-Islamy yalikuwemo katika katiba hiyo. Hata hivyo ubaya wa bahati, tarehe 7 Oktoba, 1958 Rais Iskander Hirza alipitisha sheria ya kuivunja katiba hiyo na mwezi huo huo tarehe 27, *“Field marshal”* Muhammad Ayub Khan akapindua Serikali na kutangaza sheria za kijeshi ambapo vyama vyote vya kisiasa vilipigwa marufuku ikiwemo Jama’atul Islamy.

Pamoja na vikwazo hivyo Mauduud hakukata tamaa. Katika hali hiyo ngumu ya sheria za kijeshi, alikusanya nakala na hotuba zake za kati ya 1939 na 1958 akatoa kitabu alichokiita; *Sheria ya Kiislamu na Katiba (Islamic Law and Constitution)*. Ndani ya kitabu hicho alitoa hoja kuonesha usahihi na utekelezaji wa sharia na Katiba ya Kiislamu katika ulimwengu wa leo. Kutokana na hoja zake katika kikao cha Majaji cha mahakama Kuu ya Pakistan 17 Februari, 1967, Majaji walieleza matakwa yao, kuona sheria ya Kiislamu inatekelezwa.

Mwaka 1961 Serikali ilipitisha sheria ya familia (the Muslim Family Law Ordinance) ambayo iliweka vikwazo vingi katika kanuni na taratibu za Kiislamu za ndoa na talaka. Maulana mauduud akiongoza kundi la Maulamaa wapatao 209 alipinga sheria hiyo kwa nguvu zote. Serikali ilikuja juu na kuwaweka ndani baadhi ya Maulamaa.

Katika jumla ya kazi muhimu alizoacha Maulana Mauduud ni tafsiri yake ya Qur-an, *tafhimul ul-Qur-an* (*The meaning of the Qur-an*). Kazi hii alianza mwaka 1943 na kuikamilisha Juni 1972. Katika kufanya kazi hiyo ilimbidi kusafiri sehemu mbali mbali kuziona sehemu zote za kihistoria zilizotajwa katika Qur-an.

Zaidi ya kupigania haki ya Pakistan kutawaliwa Kiislamu, Mauduud alipigania pia haki ya jimbo la Kashmir kujitawala, haki ya Wapalestina na kupinga udhalimu wa Israel katika ardhi za Waarabu. Aidha katika vikao muhimu vya Jumuiya za Kimataifa za Kiislamu kama Rabita-al-Alam-al-Islamia, Maulana Mauduud alisisitiza haja ya nchi za Kiislamu kujitegemea kiuchumi na kijamii kuliko kuzitegemea nchi za Magharibi.

Harakati za Maulana Mauduud zimekuwa ni kigezo cha kuuhiisha Uislamu katika karne ya Ishirini. Pamoja na kupigania kusimama kwa Dola ya Kiislamu Pakistan; Mauduud alikuwa pia mpinzani mkali wa sera za kimataifa zilizokinyume na mafundisho ya Uislamu.

Mwaka 1962 aliandika kitabu juu ya Uislamu na Udhhibiti wa Uzazi (Birth Control) akipinga sera za kitaifa na kimataifa za kidhibiti idadi ya watu kwa kuhofia uhaba wa rasilimali. Kitabu hicho kilipigwa marufuku tarehe 9 Agosti, 1966.

## **Muundo na Kazi za Jama'atil-Islamy**

Jama'atil-Islamy huongozwa na Amir akiwa msimamizi mkuu wa katiba na program za Jumuiya. Lipo Baraza Kuu (Central council) ambalo humsaidia na kumchunga Amir katika utendaji wake. Baraza hili pia huweka taratibu za mafunzo, upataji wa wanachama wapya; mipango ya uchumi na kutunza fedha.

Katika kila mji mkubwa lipo tawi la jumuiya ambalo huchagua Amir na Baraza la tawi. Aidha huwa na kamati mbali mbali kushughulikia masuala muhimu.

Vipo pia vikundi vidogo vidogo vya Jumuiya katika kila eneo. Vikundi hivi chini ya Amir wao hukutana mara moja kwa wiki ambapo hufanya darsa maalum na kutoa taarifa za kazi kutoka kwa kila mwanachama. Kila mwanachama anawajibika kuwasilisha ripoti ya kazi zake kwa wiki nzima kwa Amir kabla ya kikao.

Kuhusu mafunzo huandaliwa semina, Itqaf na kambi ambapo zaidi ya kutolewa mafunzo ya Uislamu kwa ujumla; mafunzo maalum juu ya harakati hutolewa. Hii ni pamoja na mbinu, mipango (planning) na uongozi.

Jama'atil-Islamy imeanza kwa kuweka mkazo mkubwa sana katika elimu. Imejenga na kuendesha taasisi za elimu katika viwango mbali mbali. Kutokana na kukua na kuimarika kwa mipango yake ya kiuchumi Jam'at-Islamy

hujishughulisha pia na kutoa huduma za kijamii. Hii ni pamoja na huduma za afya, kusaidia wenye njaa na waliofikwa na maafa kama mafuriko, n.k.

## **Mafanikio**

Katika jumla ya mafanikio makubwa iliyopata Jama'atil-Islamy ni kuwa na utaratibu mzuri wa mafunzo, utendaji na ushirikishwaji wa wanajumuiya katika kazi. Hali hiyo iliwezesha harakati za Jama'atil-Islamy kudumu hata pale viongozi wakuu wanapowekwa ndani au hata kufariki. Kwa hiyo haikuwa ni jumuiya iliyomtegemea mtu moja. Kwa mfano Maulana Mauduud alijiuzulu uongozi 1972 kutokana na hali yake ya afya kulega lega; Mian Tufail Muhammad akawa Amir na harakati zikaendelea kwa nguvu kama kawaida. Maulana Mauduud alifariki mwaka 1979. Jama'atil-Islamy bado inaendelea na harakati zake ikiwa na tawi la wanafunzi Jama'at-Talaban-Islamy.

## **Matatizo:**

**Kwanza**, kuna migawanyiko mikubwa miongoni mwa Waislamu. Hii imepelekea kuwa na vyama vingi vya kisiasa vinavyodai kusimamia Uislamu. Vyama hivi vimekuwa maadui huku wafuasi wa vyama wakihasisimiana na kuitana makafiri.

**Pili**, zipo pia taasisi na Jumuiya nyingi sana za Kiislamu na zote hizo hazifahamiani na kusaidiana. Kila jumuiya huhodhi wafuasi bila kuzingatia umuhimu na ulazima wa kushirikiana na kushikamana kidugu.

**Tatu**, tatizo jingine ni kuwepo kwa madrasa nyingi za kizamani ambazo huzalisha Masheikh vilema wa roho na akili. Madrasa hizo huwadumaza wanafunzi kiasi kwamba wanashindwa kuwa na uoni mpana na kujiendeleza kielimu ili kupambana na hali halisi ya maisha ya ulimwengu wa utandawazi.

Kwa ujumla historia ya Pakistan toka ikiwa sehemu ya India imekumbwa na mgawanyiko mkubwa wa Waislamu katika Twarika za kisufi, madh'hab na jumuiya mbali mbali zenye utii na mshikamano na Masheikh wao kuliko hata Qur-an na maelekezo ya Mtume(s.a.w). Hali hiyo imefanya kazi za Jama'atul-Islamy kuwa ngumu. Hata hivyo harakati zinaendelea.

**Zoezi la 5:3**

1. Orodhesha mambo aliyofanya mwanaharakati Badee-u-Zaman katika jitihada zake za kutaka wanajamii wapate haki na amani ya kweli kupitia mfumo wa maisha ya kiislamu.
2. Bainisha changamoto aliyokutana nayo Badee-u-Zaman katika harakati za kuhuisha Uislamu.
3. Bainisha wasifu na sifa za waliokuwa waasisi na viongozi wa Ikhwanil Muslimina wa Misr na Sudan.
4. Onesha pingamizi na fursa walizokuwanazo katika Da'awah
  - (a) Ikhwanil -Muslimiina wa Misr
  - (b) Ikhwanil-Muslimiina wa Sudan
5. Eleza kwa muhtasari matunda ya harakati za Ikhwanil - Muslimiina wa Misr na Sudan
6. Toa maelezo mafupi juu ya
  - (a) Maulana Sayyid Abul Ala Mauduud
  - (b) Mafunzo tuyapatayo toka maisha ya Abul Ala Mauduud na Jama'atul Islamy.
7. Taja na kufafanua njia na mbinu za kuhuisha Uislamu, zinazojitokeza kwenye harakati za Badee-U-Zamman, Ikhwanil Muslimiina na Jama'atil Islamy.

## HISTORIA YA KUHUISHA UISLAMU TANZANIA

“*Historia ya Kuhuisha Uislamu Tanzania, 700 hadi 2009*”, maudhui yanayotarajiwa yamfikishe msomaji kwenye lengo la kusimamisha uadilifu katika jamii ya Tanzania yamewasilishwa kwenye Sura kumi na tatu zifuatazo:

- Historia ya Kuingia Uislamu Afrika Mashariki.
- Upinzani Dhidi ya Uislamu Afrika Mashariki.
- Mchango wa Waislamu katika kuleta Uhuru Tanganyika.
- Mkutano wa Kwanza wa Waislamu, 1962.
- Mkutano wa Pili wa Waislamu, 1963.
- “**Mgogoro**” wa EAMWS, 1968.
- Kuasisiwa BAKWATA, 1968.
- Kuibuka Vikundi Mbalimbali Badala ya BAKWATA.
- Kuanzishwa Seminari ya Masjid Qubah 1983.
- Kuanzishwa BARAZA KUU, 1992.
- Kadhia ya Mabucha ya Nguruwe, 1993.
- Mauaji ya Waislamu Mwembechai, 1998.
- Kuanzishwa Kamati za Kuendeleza Uislamu, 2003.

Ni tumaini letu kuwa Muislamu na mtu yeyote mwenye uoni huru unaolandana na ukweli wa maumbile na mazingira ya Ulimwengu uliomzunguka, baada ya kusoma historia hii kwa makini ataona kuwa jamii ya Tanzania na ulimwengu kwa ujumla haiwezi kuishi maisha ya furaha na amani yaliyokitwa juu ya misingi ya uadilifu bila ya kuwepo kundi la waumini watakao simika uongozi (Ukhalifa) wa Allah(s.w) katika jamii kama Allah(s.w) anavyoagiza:

وَلَتَكُنَّ مِنْكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى الْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْعُرْفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ

الْمُنْكَرِ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿١٠٤﴾

“*Na wawepo katika nyinyi kundi la watu (ummah) wanaolingania kheri (Uislamu) na wanaoamrisha mema na wakakataza maovu. Na hao ndio watakaotengenekewa*” (3:104)

## Historia ya Kuingia Uislamu Afrika ya Mashariki

Hapana namna ya kuelewa vizuri harakati za kuhuisha Uislamu Tanzania au kuweka mikakati mizuri ya kuhuisha Uislamu na kuusimamisha katika jamii ya Tanzania, bila kwanza kurejea historia ya kuingia Uislamu Pwani ya Afrika ya Mashariki kisha Tanzania na namna ulivyosoteshwa mpaka kufikia hali hii iliyopo. Pia huna namna ya kutenganisha kupatikana uhuru wa Tanganyika kisha Tanzania na harakati za kuhuisha Uislamu Tanzania.

Viko vielelezo vingi vya kistoria vinavyobainisha kuwa Uislamu uliingia mapema Afrika ya Mashariki katika karne ya 7A.D, baada ya Mtume(s.a.w) kuhuisha na kusimamisha Uislamu ulimwenguni. Moja wapo ya vielelezo hivyo ni eneo la Ndongoni Mkumbuu, kisiwani Pemba ambako kuna msikiti uliojengwa karne ya 7 A.D. Katika kitabu cha "*A short History of Tanganyika*" tunafahamishwa kuwa katika miaka ya 700 A.D, vikundi vya waislamu kutoka Bara Arab viliingia Afrika ya Mashariki na kuweka makazi yao huko Sanje Majoma, kusini mwa mji wa Kilwa.<sup>25</sup>

Kielelezo kingine cha kuonesha ukale wa Uislamu Afrika Mashariki ni Msikiti wa Kizimkazi Dimbani, Mkoa wa Kusini Unguja. Katika msikiti huo liko jiwe lililojengwa Mihirabuni lenye maandishi yanayoonesha kuwa msikiti huo ulijengwa mwaka 1107 A.D.(500A.H). Wakati huo katika kisiwa cha Unguja, Kizimkazi ilikuwa ni njia na bandari muhimu ya kuwasiliana na nchi za nje kama Uajemi(Persia), Saud Arabia na nchi nyingine za Ghuba. Hivyo, msikiti wa Kizimkazi ni uthibitisho usio na wasiwasi katika kipidi cha mwisho wa karne ya 11A.D. Zanzibar tayari ilikuwa na waislamu wengi.

Kwa karne nyingi yalikuwepo mahusiano baina ya Pwani ya Afrika ya Mashariki na Asia. Wafanya biashara toka Saudi Arabia, India na nchi za Ghuba, walizitumia pepo za misimu (monsoon winds) kutembelea Afrika ya Mashariki kwa shughuli za kibiashara. Kufikia karne ya 9 na 10 A.D. wahamiaji toka Saudi Arabia walifanya makazi ya mwanzo huko Benadir katika pwani ya Somalia. Kisha ikafuatia miji ya Marca, Moghadishu na Barawa. Katika karne ya 12 A.D. wafanya biashara wengi walihama toka pwani ya Somalia wakaelekea kusini hadi Kilwa, Tanzania. Ni katika kipindi hiki vile vile ambapo wageni wengi kutoka Uajemi (Persia) na Oman walifika Kilwa. Katika karne ya 13 A.D. wageni wengine wengi toka Hadharamaut na Yemen walifika Afrika ya Mashariki.

Ibn Batuta alipotembelea Afrika ya Mashariki kwa mara ya pili 1332, miji ya pwani hasa Kilwa, ilikaliwa zaidi na Waislamu. Kutokana na mchanganyiko wa wageni na wenyeji, liliibuka kabila la *Waswahili* na lugha ya *Kiswahili* ambayo ni mchanganyiko wa lugha ya Kiarabu na Lugha za wenyeji. Miji ya Tanga, Dar-es-Salaam, Mombasa, Lamu, Malindi na Mikindani ikaibuka na kuwa vituo muhimu vya kueneza Uislamu katika miji mbali mbali ya bara ya Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Zaire, Msumbiji, Malawi na Burundi.



Tokea Unguja na Miji ya Pwani misafara ya biashara ya Waarabu na Waswahili iliingia miji ya Bara. Na kila walipofanya makao walijenga misikiti na kusilimisha wenyeji. Kutokana na fursa walizopata Waislamu kufanya biashara na wageni, miji mingi ya Afrika ya Mashariki ilikuja kukaliwa zaidi na Waislamu wakimiliki biashara za maduka, mahoteli, usafirishaji, na kadhalika.

Ukizingatia maelezo haya, utagundua kuwa waliotuletea Uislamu Afrika ya Mashariki wengi wao hawakuwa walinganiaji(missionaries) waliokuja rasmi kwa lengo hilo. Bali wengi wao walikuwa wanafanya biashara zaidi na kusilimisha, kufundisha kusoma Qur'an na Fiqh ya utekelezaji wa Ibada maalumu yalikuwa mambo ya ziada kwao. Hali hii iliathiri sana hali ya Uislamu baadae. Tokea awali haikuwepo azma ya kusimamisha Uislamu Afrika Mashariki. Hapakuwa na program madhubuti za kutoa elimu na mafunzo kwa muelekeo wa kusimamisha Uislamu. Toka zama hizo Uislamu umebakia Afrika ya Mashariki kuwa ni jambo la kiroho la mtu binafsi bila kujali nafasi ya Uislamu katika maisha ya jamii.

Pamoja na upungufu huo; wageni kutoka Ulaya ambao pia ni Wakristo hawakuacha kuonyesha wasi wasi wao hata katika huo Uislamu dhaifu. Wajerumani na Waingereza waliweka mikakati ambayo ilihakikisha Uislamu haupati nguvu na Waislamu wanabaki watu dhalili. Kinyume chake walilipa Kanisa fursa mbali mbali za kuliwezesha kustawi na kushamiri Afrika Mashariki. Mikakati hiyo ilikuja kurithiwa na kuendelezwa na viongozi wa Serikali baada ya Uhuru.

## **Upinzani Dhidi ya Uislamu Afrika ya Mashariki**

Wamishionari na Wakoloni waliona kuwa Uislamu ni kikwazo kwa ukoloni na utamaduni wao. Waliuona Ukristo na utamaduni wa Ulaya Magharibi kuwa ni pande mbili za sarafu moja. Hivyo mkakati ukawekwa wa kuupiga vita Uislamu hapa Afrika na kuunza Ukristo kama kitangulizi cha kuja kwa wakoloni. Vyama vingi vya makanisa viliundwa Ulaya ili vije vifanye kazi hii Afrika. Chama cha *White Fathers* ambacho kimefanya kazi kubwa sana hapa Afrika ya Mashariki pia kilianzishwa na Kadinal Lavigire kwa lengo maalumu la kuupiga vita Uislamu na kuunza Ukristo<sup>26</sup> Pia kumbu kumbu za chama cha "*Church Missionary Society*" za mwaka 1880-81 (uk. 2-3) zinasema wazi kuwa lengo lake ni kuukomboza ulimwengu uepukane na Uislamu. Na H.M. Stanley ameandika kuwa alipotembelea Uganda lengo lake lilikuwa kumfanya Mutesa awache Uislamu na ampokee Yesu Mnazareti.<sup>27</sup>

Katika mkutano wa Berlin wa wakoloni katika kugawana Bara la Afrika mwaka 1884, Ukristo ulipewa upendeleo (hadhi) maalumu. Ibara ya 6 ya makubaliano yao iliagiza kuwa dola zote za kikoloni zitoe hifadhi maalumu kwa makanisa ya Kikristo.<sup>28</sup> Na Bwana Roland Oliver ameandika kuwa huko Ulaya

Wazungu walihofia kuwa Afrika ya Mashariki ya Kiislamu itakuwa ni Afrika ya Mashariki dhidi ya Wazungu.<sup>29</sup>

Kutokana na mtizamo huu wa wakoloni kufikia mwaka 1900 na kuendelea iliwekwa sera ya kuhakikisha kuwa Wakristo wanashika nafasi za juu katika Serikali na Waislamu wanashika nafasi za chini kabisa. Kamishina wa Uganda kati ya 1899 -1901, Sir Herry Johnston, alitamka sera hii alipomwandikia D.C. wa Busoga kuhusiana na wasi wasi aliouonesha askofu Tucker juu ya kuenea kwa Uislamu. Sir H. Johnston alisema:

*“Haitakuwa kwa maslahi ya Serikali ya Uingereza iwapo Uislamu utapata wafuasi wengi kwani kwa asili yao Waislamu niwagumu kuwatawala na katika nyoyo zao wanapinga utawala wa dola ya Kikristo.”<sup>30</sup>*

Na akawaonya Machifu wafanye kila njia kuupiga vita Uislamu. Kufikia mwaka 1917 Uislamu ulikuwa umedhoofishwa sana Afrika Mashariki. Lakini pamoja na hayo Wakoloni wakaona bado haitoshi. Wakaweka mkakati wa kuzuia Uislamu usienee kusini mwa Sudan ili Uganda isiathiriwe sana na Uislamu. Waislamu wabakie Pwani ya Kenya na Tanganyika tu. Na wakati huo huo kuzidisha kampeni za kueneza Ukristo. Mkakati huu upo katika nyaraka za Serikali zilizopo Entebbe No. A. 23 na katika Uganda Annual Report, 1900-1.

Hatua nyingine kubwa iliyochukuliwa na wakoloni ilikuwa ni kuzibana juhudi za Waislamu za kueneza Uislamu na kuwabana katika fursa za elimu. Serikali ya Kikoloni huko Uganda kwa mfano ilimzuia Mwalimu wa Kiislamu kutoka India aliyelitwa na Waislamu wa huko kuingia Uganda. Mwaka 1944 Waislamu wa Uganda walipewa Pauni 213 tu kwa ajili ya elimu yao. Wakristo walipewa Pauni 134,000!! Ama kubanwa kwa Waislamu wa Tanganyika kielimu tangu zama hizo hadi leo hakuna haja ya kutolewa maelezo zaidi. Itoshe tu kusema kuwa katika utafiti uliofanywa na Dr. Malekela wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1983 umeonyesha kuwa katika kila watoto 100 wanaosoma sekondari 78 ni Wakristo na 22 ni Wapagani na Waislamu.

## **Mbinu za Kuwaghilibu na Kuwaritadisha Waislamu Afrika Mashariki**

Tafsiri ya hatua zote hizo hapo juu ni kwamba Uislamu uliokuja Afrika Mashariki miaka elfu moja iliyopita ukawa unadumaa na Ukristo uliokuja Afrika Mashariki miaka mia moja tu iliyopita ukawa unazidi kustawi. Utafiti uliofanywa juu ya siri ya mafanikio ya Wakristo dhidi ya Waislamu umegundua mbinu zilizotumika zifuatazo:

Mbinu na siri ya kwanza ni kujenga mahusiano ya karibu na waislamu. Mwanzoni kulikuwa na uhasama wa dhahiri kati ya Waislamu na Wakristo

hivyo haikuwezekana kabisa kwa Muislamu kuwa Mkristo. Baadaye Wakristo wakabadili mbinu. Wakajifanya ni marafiki wakubwa wa Waislamu na kuishi pamoja nao kindugu. Waislamu wakaamini na hata kuwasaidia sana katika harakati zao. Sultani Seyyid Said wa Unguja aliwakaribisha Wamishionari Unguja na akawapa barua ya kuwatambulisha iliyosema: “Dk. Krapf, Mjerumani, ni mtu mwema anayetaka kuwalingania watu kwa Mungu. Mfanyieni ihsani na msaidieni kila aendako.”<sup>31</sup>

Hata wale watu waliokuwa na chuki sana dhidi ya Uislamu walipata msaada wa Waislamu. Hali hii yaendelea hadi leo. Utafiti uliofanywa na Wakristo juu ya Waislamu wa Tanzania na kuchapishwa katika kitabu kitiwacho *Development and Religion in Tanzania uk. 27* unasema kuwa Waislamu wa Tanzania wanajali zaidi utaifa wao kuliko dini yao. Utawajua kuwa ni Waislamu wakiwa msikitini tu na siyo katika maisha ya jamii ya kila siku. Waislamu wanajali sana kuwa na uhusiano mwema na watu wa dini nyingine. Matokeo ya msimamo huu wa Waislamu ni kuwa Wakristo walipata fursa nzuri ya kuwaritadisha. Takwimu za 1965/6 zilizokusanywa na James D. Holway kwa nchi za Afrika Mashariki ni kama ifuatavyo:

### ***Wakristo Waliosilimu***

Tanzania	3104
Uganda	5
Kenya	42
<b>Jumla</b>	<b>315</b>

### ***Waislamu walioritadi***

Tanzania	8741
Uganda	-
Kenya	430
<b>Jumla</b>	<b>9171</b>

Source: James D. Holway; Mimeo 1965.

Mtu anaweza kuhoji usahihi wa takwimu hizi. Hata hivyo lililo muhimu ni kuwa Wakristo walikuwa wakifanikiwa zaidi kuliko Waislamu katika kulingania dini yao. Na kutokana na mafanikio hayo ndipo Wakristo wakaamua kuanzisha mradi mkubwa sana wa kuwaritadisha Waislamu wa Afrika uitwao “*Islam in Africa Project*” wenye makao yake makuu huko Nairobi Kenya. Ulianzishwa na Rev. James Jitchie aliyekuwa mshauri wa Baraza la Kikristo la Kenya (The National

Christian Council of Kenya). Mwaka 1971 na Rev. Tom Beetham akawa ndiye Mkurugenzi wa Mradi huo. Miongoni mwa Programu zinazoratibiwa na “*Islam in Africa Project*” ni pamoja na ile semina iliyofanyika Nairobi, Kenya Septemba 23, 1989 juu ya kukabiliana na Uislamu, kuandaa November Crusades katika nchi mbali mbali za Afrika n.k. Hii ni mbinu yao kubwa ya mwanzo iliyowapa mafanikio dhidi ya Waislamu wa Afrika Mashariki.

*Mbinu na Siri ya pili ya mafanikio ya Wakristo* ni kuwa wamejitahidi sana kuingia vijijini na kujenga makanisa, mashule na hospitali. Waislamu wengi wameishia mijini. Matokeo yake Wakristo wametapaka Afrika Mashariki nzima hadi vijijini lakini Waislamu wengi wako mijini. Na huu ni udhaifu mkubwa.

“*Mbinu na Siri kubwa ya tatu*” ya mafanikio ya Wakristo ni Umoja na mipango madhubuti ya muda mfupi na muda mrefu ya kufikia lengo lao. Ikiwa mtu atazingatia programu zinazoendeshwa na Wakristo kwa upande wa elimu tu peke yake na akatazama matunda yake itamdhihirikia ni kwa kiasi gani Waislamu tulivyo nyuma. Waislamu wa Kenya, Uganda na Tanzania hatuonyeshi kuwa tuna mwelekeo wala mpango wowote wa maana wa kuipigania Dini yetu. Mtu akisoma historia ya Waislamu wa Uganda, jinsi walivyopigwa vita na wakoloni na walivyogombanishwa wao kwa wao na Serikali ya Obote, Idi Amin na ya hivi sasa ya Museveni na wanavyoshitakiana kwa Serikali hiyo hiyo na halafu akatazama historia ya Waislamu wa Tanzania na Kenya atastushwa sana na kufanana mno kwa matatizo yetu.<sup>32</sup>

Pengine swali la kujuliza hivi sasa ni: Je! Kwanini Waislamu wa Afrika Mashariki, pamoja na matatizo yote haya yanayotukabili, hatuoneshi kuwa na mpango wowote wa kukabiliana nayo?

## **Kupigwa Vita Uislamu Tanganyika**

Wafanya biashara wa Kiarabu waliwatangulia watawala wa Kijerumani kuingia Tanganyika. Waarabu hawakuingia Tanganyika kama nchi au Serikali inayokuja kutawala. Ilikuwa ni familia zilizokuja kutafuta biashara. Kwa hiyo Tanganyika haikuwahi kutawaliwa na Serikali au nchi ya Kiarabu. Wafanya biashara hawa wa Kiarabu kila mahali walipoweka makao yao walijenga shule za Qur-an (madrasa). Pia walifundisha ujuzi wa kusoma na kuandika kwa kutumia herufi na nambari za Kiarabu.

Wakoloni wa Kijerumani walipoingia Tanganyika walijimarisha kwanza katika miji ya Pwani. Waliwakuta wenyeji wa Pwani wengi wao wakijua kusoma na kuandika kwa kutumia herufi za Kiarabu. Hawa wakawatumia katika kazi zao za utawala.

Shule za mwanzo za Serikali ya kikoloni zilianza kujengwa Bagamoyo na Tanga. Kulingana na hali halisi ya maeneo hayo wanafunzi wengi

wakawa Waislamu. Wakristo wakaja juu kumshutumua Gavana Von Soden kuwa anaendesha sera za kupendelea Waislamu. (Taz: Hornsby, German Achievement” uk. 84) Kutokea hapo Serikali ya kikoloni kwa kushirikiana na mashirika ya Kikristo toka Ulaya yakawa yanaendesha kampeni na mikakati ya kuwabana Waislamu katika elimu. Kwa hiyo japo Watanganyika wote walilipa kodi ya kichwa lakini ni Wakristo pekee waliokatiwa donge nono la kodi hiyo kujiimarisha kielimu.<sup>33</sup>

Alipoingia Muingereza alifuata sera ile ile ya Mjerumani. Mashirika ya Kikristo toka Ulaya yakapewa fursa zaidi kuimarisha elimu kwa Wakristo. Na Serikali yenyewe ikawa inatoa mapesa ya kodi za Watanganyika kuimarisha Ukristo na Wakristo. Dhuluma hii hawakuikubali Waislamu. Bwana J.G. Liebenow katika kitabu chake *“The Colonial Rule and Political Development in Tanzania”. The case of the Makonde*”; anatufahamisha kuwa watu wa mikoa ya Kusini hasa Wayao na Wamakonde waliilalamikia Serikali kuwa kwanini wakati walipa kodi wa eneo hilo wengi ni Waislamu, lakini fedha hupewa Wakristo wajenge na kuendesha shule. Muandishi Muchy Makajenga katika makala yake “Serikali inapendelea Wakristo?” amewaeleza ‘watu wa’ Mikoa ya Kusini kwamba hawajui thamani ya elimu. (Taz: WAKATI NI HUU na 20, Juni 1-7, 1993).

Watu hawa wasingejua thamani ya elimu vipi wangemlalamikia mkoloni? Dosari yoyote itakayoelezwa leo hii juu yao katika suala la elimu ni matokeo ya kudhalilishwa kwao kwa muda mrefu.

Kutokana na malalamiko ya Waislamu Serikali ya kikoloni ilianza kuwapa Waislamu nao fedha kidogo kwa ajili ya elimu. Mwaka 1957 Serikali ilitoa paundi 1,338,925 kwa ajili ya mashirika yanayotoa elimu. Waislamu walipewa paundi 6,848 tu kati ya hizo. Kwa hiyo utaona katika kipindi hicho nyeti na muhimu sana kwa upanuzi wa elimu kupitia msaada wa Serikali (*Aided System of Education*), Waislamu walifunguwa milango.

Hali hiyo ndiyo iliyompelekea Sheikh K.S. Kiangi Msuya kutoa maneno yafuatayo kwa uchungu mkubwa sana juu ya udhalili wa elimu kwa Waislamu wa Tanganyika. Maneno yake hayo yalichapishwa katika gazeti la Kiongozi la tarehe 26 Oktoba, 1956 uk. 3 chini ya kichwa cha habari:

***“Udhalili wa elimu kwa Waislamu Tanganyika”***

*“Inasemekana kuwa hesabu ya watu wa Tanganyika ni zaidi ya 8,102,000 na katika hesabu hii Waislamu ni zaidi ya 4,500,000. Sasa nataja schools zote uonekane udhalili ulioko juu ya Waislamu.*

## **Hesabu ya Schools zote Tanganyika 1955**

1. (a) *Schools za Utawala (Government & Native Authority) Primary School 656.*  
       (b) *Schools za wakristo Primary 1692.*  
       (c) *Schools za Waislamu Primary 28.*
- 2.(a) *Schools za Utawala (Government) Rural Middle 104.*  
       (b) *Schools za Wakristo Rural Middle 223.*  
       (c) *Schools za Waislamu Rural Middle-Hawana.*
- 3.(a) *Schools za Utawala (Government) Secondary 10*  
       (b) *Schools za Wakristo Secondary 16.*  
       (c) *Schools za Waislamu Secondary – hawana.*
- 4.(a) *Schools za Utawala (Government) T.T.C 7.*  
       (b) *Schools za Wakristo T.T.C 23*  
       (c) *Schools za Waislamu T.T.C. – Hawana.*
- 5.(a) *Schools za Utawala (Government) Ufundi,Utibabu n.k. 7*  
       (b) *Schools za Wakristo Ufundi & Utibabu 5.*  
       (c) *Schools za Waislamu Ufundi, Utibabu – Hawana.*

Schools hizi hapa juu huendeshwa kwa fedha tulipayo kwa kodi na ushuru wa watu wote wa Tanganyika, na Muislamu akihitaji kuingia Secondary ama T.T.C. za Wakristo huambiwa abatizwe awe Mkristo (ndipo ataweza kutumia fedha yake aliyolipa) ndipo atakubaliwa kusoma hapo. Pia schools za Middle 104 za government ambazo Serikali inasema inapokea watu wote; sivyo kabisa, kwani ataingiaje Middle naye hana Primary? Nataja moja kwa mfano Kibohehe, Machame wilaya ya Moshi ni school ya Utawala ina wanafunzi 140 kati yao Waislamu ni 12 tu na 128 ni Wakristo. Je, kuingia Secondary na Teacher Training college(T.T.C) itakuwaje?

Wanafunzi wa Tanganyika walioingia Makerere college 1950-1955 ni 500 na Waislamu katika mia ni watano na 95 Wakristo hivyo Waislamu watapataje maendeleo?" (Sheikh K.S. Kiangi Msuya).

Mwaka 1958 Novemba 20, Waislamu waliitisha mkutano mjini Dar es Salam. Katika mkutano huo ambao uliitwa "Africa Muslim Education conference", Waislamu waliorodhesha malalamiko yao dhidi ya Serikali ya kikoloni kuhusiana na ubaguzi katika elimu.

Miongoni mwa mambo yaliyolalamikiwa ni kuwa:

1. Mara Waislamu walipoanza kufungua shule Serikali ya kikoloni iliweka mpango wa elimu wa miaka mitano (FYP)kuwa isifunguliwe shule ya msingi tena.
2. Pale ambapo Waislamu wamefungua shule hulazimishwa wafundishe Qur-an tu; vinginevyo wanashitakiwa.
3. Shule za Muslim ambazo zimekubaliwa na Serikali zinanyimwa misaada (Grant in Aid) wakati Waislamu wanalipa kodi Serikalini.

## **MCHANGO WA WAISLAMU KATIKA KULETA UHURU TANGANYIKA**

Kwa upande mmoja wakoloni walijenga mahusiano ya karibu sana na mashirika ya dini ya Kikristo na walisomesha kundi la Wakristo na kuwa karibu nalo ili wawatumie katika kutawala.

Kwa upande mwingine kama tulivyokwishaona Waislamu walitengwa, kubaguliwa na kukandamizwa. Hali ilikuwa ngumu kiasi cha kuwapelekea Waislamu kuwa mstari wa mbele katika kuanzisha harakati za kumng'oa mkoloni. Harakati za mwanzo za kupambana na Serikali ya kikoloni zilianzia katika maeneo ya Waislamu. Katika vita vya maji maji mwaka 1905 Waislamu walipigana huku wakiyachukulia mapambano yale kuwa ni Jihad. Kwa upande wa Wakristo, wao walisimama kuwaunga mkono Wajerumani kupambana na Watanganyika wenzao.

Kati ya mwaka 1939 na 1947 Wafanyakazi bandarini Tanga na Dar es Salaam ambao wengi wao walikuwa Waislamu waliongoza migomo mikubwa kupinga dhuluma za kikoloni na kujenga mazingira ambayo baadaye yaliwaruhusu kuanzisha vyama vya wafanyakazi. Kiongozi wa harakati hizo Kleist Sykes alichaguliwa kuwa Katibu wa kwanza wa Jumuiya ya kwanza ya wafanyakazi Tanganyika. Ama huko nyuma mwaka 1940 Kleist na Waislamu wengine mashuhuri pamoja na Shariff Salim Omari aliyekuwa Liwali wa Dar es Salaam, Maalim Popo Saleh, Ali Kiro na Idi Tosiri walianzisha Al Jamiatul Islamiyya fi Tanganyika. Shariff Salim alichaguliwa kuwa Rais na Kleist Sykes katibu. Shariff Salim alipotoka chamani mnamo mwaka 1936, Mzee bin Sudi alichaguliwa kuwa Rais. Uongozi wa juu wa African Association iliyoanzishwa mwaka 1929 ulikuwa ndiyo ule ule katika “*Al Jamiatul Islamiyya fi Tanganyika*”. Ushawishi wa uongozi huu wa Waislamu katika “*African Association*” unaweza kuonekana katika mwaka 1930 wakati chama na siyo *Al Jamiatul Islamiyya* kilipoiandikia Serikali ya kikoloni kikidai kuchaguliwa kwa Mwafrika kama kadhi ili kuongoza kwa “sharia”.

TANU(*Tangayika African National Union*) asili yake ni TAA(*Tanganyika African Association*). TAA kulikuwa na kamati ya siasa ambayo ilikuwa na wajumbe Waislamu: Sheikh Hassan bin Amir, Mzee Kleist Sykes, Abdulwaheed Sykes, Hamza Kibwana Mwapachu, Said Chaurembo. Sheikh Hassan bin Amir alikuwa mjumbe wa kamati ya Utendaji ya Da'awat Al-Islamiyy wakati Kleist Sykes alikuwa katibu mkuu wa *Jamiatul Islamiyya*. Nyerere alikaribishwa na kupewa uongozi katika harakati za kisiasa katika hatua za mwanzo za kuanzishwa kwa TANU. Kuingia kwa Nyerere na wasomi wa Kikristo wengine katika TANU kulibadili sura ya siasa Tanganyika. Japo chama kilikuwa kimepata wasomi lakini muungano baina ya Waislamu na Wakristo nao ulianza. Kwa vile Wakristo hawa ndio wengi waliokuwa wasomi wakawa wanashika nafasi nyeti katika chama. Mwelekeo huu uliwatisha baadhi ya Waislamu. Waliona kuwa kuna uwezekano mkubwa kwa Wakristo hao kutokutenda haki, kinyume chake wakatamia nafasi zao kuendeleza dhulma ile ile ya wakoloni. Sheikh Suleiman Takadiri akiwa mwenyekiti wa Baraza la Wazee la TANU alikuwa wa mwanzo kuonesha wasiwasi wake hadharani. Hata hivyo akapigwa vita kwa kuitwa mdini "anachanganya dini na siasa". Waislamu wengine walipoona TANU imesahau agenda ya Waislamu wakaanzisha chama cha AMNUT, "*All Muslim National Union of Tanganyika*" mwaka 1957. Lengo lilikuwa ni kupigania haki sawa kwa wote. Lakini nacho kikapigwa vita kikatoweka. Kwa hiyo Waislamu wakabakia kuwa mstari wa mbele katika kupigania uhuru lakini katika mtizamo ulioitwa wa kutochanganya dini na siasa (*Secularism*). Sio wa kusimamisha Haki au "Ukhalifa". Kwa mtizamo huo wakampamba Mwalimu Nyerere kuwa Mwalimu wao katika siasa na harakati za kuendesha nchi baada ya uhuru. Lakini wakati Waislamu wanaacha agenda yao ya kusimamisha Ukhalifa, kisirisiri Mwalimu Nyerere alikuwa akipewa maandalizi ili aje kusimika utawala wa Kikatoliki Tanganyika. Mashirika ya Kikristo yalimsomesha na kumuandaa ili aje kutawala kama mkristo mkatoliki. Kufuatia safari yake Umoja wa Mataifa mwaka 1956 ambayo kwa kiwango kikubwa alisaidiwa na shirika la Kikatoliki la Maryknoll Fathers, Serikali ya kikoloni iliilalamikia Vatican. Padri William Collins aliyekuwa Katibu Mkuu wa Shirika la Maryknoll 1957, alitakiwa na Vatican, makao makuu ya Kanisa Katoliki duniani kuandika ripoti maalum. Ripoti hiyo ilitoa majibu kuhusiana na malalamiko ya Serikali ya wakoloni Tanganyika. Sehemu ya ripoti hiyo inasema:

*"Mapadri wa Maryknoll wamekubali kulipia tiketi ya kwenda na kurudi kutoka England kwenda New York. Safari yake kutoka Tanganyika hadi England na kurudi ililipiwa na chama chake. Shirika la Maryknoll limekubali kumlipia kuja hapa kwa vile ni kiongozi Mkatoliki kutoka wilaya ya Musoma tumeonelea ni vizuri apate fursa kuona hali ya Ukatoliki huko Amerika na pengine kupata nafasi za masomo zaidi kwa Watanzania.*



*Alifika mjini New York Novemba 13, 1956 na kuondoka Januari 5, kiasi cha majuma saba hivi. Wakati ule huko New York aliishi katika jumba la “Leo House” ambalo lilisimamiwa na Masista wa Mt. Agnes. Kisha alisafiri mpaka Washington ambako aliishi na White Fathers, halafu Chicago na Boston ambako alikaa na Maryknoll Fathers. Huko Washington katika Chuo Kikuu cha John Hopkins alitoa mhadhara, nako Chicago alikutana na viongozi wa vyama vya wafanyakazi na huko Boston alikuwa na mazungumzo katika Chuo Kikuu cha Boston. Akiwa mjini New York alihudhuria mikutano kadhaa ya Umoja wa Mataifa.*

*Maryknoll Fathers wamekubali kulipa tiketi ya kwenda Amerika na kurudi England kwa vile huyu ni kiongozi wa Kikatoliki, mtu kutoka jimbo la Musoma ambaye anaheshimiwa na Mapadri wetu. Kwa vile ni nia ya Serikali ya Waingereza kuwaandaa wenyeji kwa madaraka, Shirika la Maryknoll limeona kuwa msaada wowote linaoweza kuwapatia viongozi wa Kikatoliki utakuwa ni kulisaidia kanisa. Huyu ni Mkatoliki mzuri, mtu mwenye msimamo na busara katika kutaka kuwaelekeza watu wake kwenye uhuru kamili. Hakosi kuwa na habari kwamba kuna wapinzani fulani wenye siasa kali zaidi katika chama chake lakini anajitahidi kukiongoza kwa njia inayokubalika. Chama hiki, kimeandikishwa rasmi Serikalini na wala siyo chama cha siri”.*

Haya yameandikwa na William Collins katika ripoti iliyoitwa; “Report on Julius Nyerere and his relations with the Maryknoll Fathers in Tanganyika; British East Africa”. Feb. 11, 1957. Iitumwa kwa Fr. Heinzmann Rome, Italy).

Pamoja na kuandaliwa Nyerere, Maryknoll Fathers na White Fathers walikuwa pia wakiwaandaa watu wengine ili kuja kushika nafasi muhimu Serikalini baada ya uhuru. Padri Paul Crane aliyetembelea Tanganyika mwaka 1959 alidhihirisha siri hii pale aliposema:

*“Lazima tujitahidi kadri ya uwezo wetu kupata wasomi Wakatoliki ambao watahika nafasi muhimu kwenye ngazi zote za kijamii. Wakatoliki wajitahidi kushika nafasi hizi. Tutaweza kuwaingiza kwenye nafasi za uongozi kwa njia ya kujenga vikundi vidogo vidogo vya wasomi Wakatoliki”.*

(Haya yanapatikana katika kitabu cha Paul Crane “Problems of the movement of the Young away from the Church; Rome: CIPA; 1960).

Kutokana na maandalizi hayo Wakristo walihodhi nafasi zote nyeti za uongozi katika Serikali baada ya uhuru. Hali hiyo anasema Dk. Sivalon kuwa “imefanya matendo, msimamo na uamuzi wa viongozi wa Serikali ufanane mara kwa mara na kwa namna moja au nyingine na mafundisho na mwelekeo wa Kanisa.”<sup>34</sup>

Kwa hiyo kutokana na Nyerere kuwa Mkatoliki na kuwa kiini cha kikundi cha watawala Wakristo alikuja kuwa kiungo muhimu kati ya kanisa na Serikali. Kiungo hiki kililipa kanisa nafasi nzuri ya kuupiga vita Uislamu.

Kwa hiyo wakati Waislamu walikuwa wakipigania uhuru huku wakiitupa agenda ya Uislamu, wenzao walikuwa wakijiandaa kuja kushika Serikali katika mazingira ambayo yatawezesha kupambana na Uislamu. Na kweli walipambana nao mara tu baada ya uhuru.

## **Mkutano wa Kwanza wa Waislamu, 1962.**

Baada ya uhuru kupatikana mwaka 1961 Waislamu waliamini kuwa hali yao ya baadae katika Serikali huru itakuwa nzuri. Mwaka 1962 ukaitishwa mkutano wa Waislamu wa nchi nzima kujadili nafasi ya Uislamu katika Tanganyika huru. Taasisi zifuatazo zilihudhuria mkutano huo: *East African Muslim Welfare Society* (EAMWS), *Da'awat Islamiyya*, *Jamiatul Islamiya fi Tanganyika*, na *Muslim Education Union*. Mkutano ule ulikubaliana pamoja na mambo mengine umuhimu. Kuanzisha idara ya elimu chini ya EAMWS. Waislamu hawakusubiri Serikali itimize ahadi yake ya kurekebisha upogo uliokuwepo wa elimu kati ya Waislamu na Wakristo. Waislamu walianzisha mipango yao wenyewe ili isaidiane na juhudi ya Serikali. Mipango ikatayarishwa ya kujenga shule Tanganyika nzima na mwishowe kujenga Chuo Kikuu cha kwanza kwa Waislamu katika Afrika ya Mashariki. Mkutano ukamchagua Tewa Said Tewa, waziri wa Serikali, mwanasiasa wa TAA na mmoja wa wale wazalendo kumi na saba walioanzisha TANU, kuwa mwenyekiti wa EAMWS kwa upande wa Tanganyika.

Huu ndiyo ukawa mwanzo wa uadui kati ya Waislamu na Serikali ambayo ilikuwa mikononi mwa Wakristo. Uelewano uliodumu wakati wa kudai uhuru ukaanza kutoweka na siasa zikachukua sura mpya ya uhasama, kutoaminiana na kutofautiana kati ya jamii hizi mbili. Kisa cha hali hii mpya ni Waislamu kutaka kuondoa hali ya kikoloni iliyowakandamiza kwa miaka mingi. Waislamu waliona kuwa hili lilikuwa ni jambo lililokuwa na pingamizi kufanyika. Uhuru ili uwe na maana ni lazima Waislamu wajitoe ndani ya unyonge waliogubikwa na wakoloni. Kwa upande wa Wakristo hali hii ilisababisha hofu kuu nyoyoni mwao.

## **Pingamizi katika Kuleta Mabadiliko ya Kuwanufaisha Waislamu, 1963.**

Uhuru ulipopatikana kulikuwa na makundi makubwa mawili yaliyokuwa yanatawala siasa Tanganyika. Kwanza kulikuwa na Waislamu ambao tegemeo lao kubwa lilikuwa kuona ile hali yao ya unyonge iliyodumu kipindi chote cha ukoloni ikitoweka. Nguvu ya pili ilikuwa vyama vya wafanyakazi. Makundi haya yote yalikuwa na mategemeo makubwa kwa Serikali ya TANU kuwa itawapa haki zao bila ya matatizo yoyote. Pamoja na makundi haya palikuwapo na vyama vya upinzani, AMNUT na Congress ambavyo kwa kweli havikuwa na nguvu yoyote ya kuweza kupambana na TANU. Miezi michache kabla ya uhuru, Nyerere alitoa onyo ambalo dhahiri lilikuwa limeelekezwa kwa makundi

haya. Mwezi Mei, 1961 Nyerere alionya kuwa hatosita kuwaweka kizuizini viongozi wa vyama vya wafanyakazi, viongozi wa dini na wengineo endapo watakuwa tishio kwa Serikali yake.<sup>35</sup> Hapa ieleweke wazi kuwa viongozi wa dini aliowakusudia Nyerere kuwaweka kizuizini hawakuwa viongozi wa kanisa, bali Masheikh. Hawakuwa viongozi wa kanisa kwa kuwa mpaka uhuru unapatikana makanisa yalikuwa yamejitenga na siasa kwa ukamilifu. Huenda Nyerere alitoa onyo hilo kutokana na shutuma alizotoa mpinzani wake Rais wa Congress, Zuberi Mtemvu. Akiwahutubia wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Karl Marx mjini Leipzig, Ujerumani ya Mashariki, Mtemvu alibashiri kuwa kutolewa kwa uhuru wa Tanganyika kwa uongozi wa TANU, hakutabadili chochote kwa kuwa wanaoingia madarakani wameamua kushirikiana na wale wale wanyonyaji wa zamani na hii itavunja nguvu za wazalendo na matumaini yao.<sup>36</sup>

Haiwezekani kuielewa ahadi ya Nyerere katika haki na usawa kwa raia wote kama alivyoahidi wakati wa kudai uhuru, hadi usome hotuba yake aliyoitoa tarehe 10 Desemba, 1962 katika Bunge wakati Tanganyika inakuwa jamuhuri. Hotuba ya Nyerere ilijikita kwenye matatizo ya upogo kati ya Waislamu na Wakristo. Nyerere alifanya hivi labda akijua kuwa ingawa yeye alikuwa Rais Mkatoliki lakini waliomuweka madarakani kuitawala Tanganyika walikuwa Waislamu. Katika hotuba yake Nyerere alisema yafuatayo:

*“Hakuna njia nyepesi ya kuondoa tofauti baina ya raia wetu Waafrika na wasio Waafrika; hakuna njia nyepesi ya kuondoa tofauti za elimu kati ya Wakristo na Waislamu, au baina ya wachache wenye elimu na wengi wa watu wetu wasio kuwa na elimu; hakuna njia nyepesi ambayo Wamasai na Wagogo wanaweza wakalingana na Wahaya, Wachagga na Wanyakyusa.”<sup>37</sup>*

Hii ilikuwa kauli ya Serikali ya kudhihirisha nia yake njema. Kauli hii ilikuwa ya kuwapa matumaini na kuwahakikishia Waislamu na wale wote walioathirika na dhulma ya wakoloni, kuwa Serikali ilikuwa inatambua shida zao na ingechukua hatua zifaazo kurekebisha hali hiyo. Wakati Nyerere anatoa kauli hii ya kutia moyo, Serikali iliyokuwa imejaa viongozi wa Kikristo na taasisi za Kikristo zilikuwa zimejaa hofu zikiogopa harakati za Waislamu za kujiletea maendeleo zilizokuwa zikitapakaa nchi nzima kwa kasi. Walifahamu nguvu na umoja wa Waislamu ukitumiwa vyema hapana shaka Waislamu wangekuja juu. Kwa viongozi wa Kikristo walioshikilia madaraka ya Serikali, kwao ilimaanisha kugawana madaraka sawa na Waislamu. Harakati hizi mpya za waislamu ziliashiria kuanguka kwa himaya yao katika madaraka kama viongozi. Hii ilionekana kama harakati za awamu ya pili za Waislamu, safari hii kuchukua Serikali kutoka kwa Wakristo. Harakati za awamu ya kwanza zilikuwa zile za kumng’oa Mwingereza katika ardhi ya Tanganyika. Bila ya kutegemea, Serikali ikajikuta inakabiliana ana kwa ana na jumuiya ya Kiislamu iliyokuwa na nguvu ambayo kwa dhahiri yake kila Muislamu alikuwa ni mwanachama, na ndani yake imejumuisha wana-TANU shupavu pamoja na wapinzani wa TANU.

Wakati huo huo Baraza la Wazee wa TANU katika nafasi yake ya ushauri likawa linaishinikiza Serikali ifanye mabadiliko haraka kutokomeza mabaki ya ukoloni. Serikali ikaona harakati hizi ni sawasawa na kuendesha nchi katika misingi ya Uislamu. Baraza la Wazee wa TANU lilikuwa sasa limejigeuza kutoka kundi dogo la wazalendo na kuwa kundi lililokuwa likishinikiza Serikali ndani ya TANU. Serikali ilikuwa ama ikubali matakwa ya Waislamu au ikatae na ipambane na upinzani kutoka kwao. Tarehe 11 Machi, 1963, Kamati Kuu ya TANU iliyokutana Dar es Salaam ilipiga kura kuvunja kamati ya wajumbe kumi na moja ya Baraza la Wazee wa TANU chini ya Mwenyekiti wake Idd Tulio. Wazee walikusanyika katika ukumbi wa Arnautoglo na wakasomewa uamuzi wa Kamati Kuu ya kulivunja Baraza la Wazee.

Taarifa ilisema wazee hao ni kero kwa sababu 'dini na siasa vilikuwa vitu viwili tofauti na hawa wazee walikuwa wanachanganya dini na siasa.<sup>38</sup> Hiki kilikuwa chombo cha ushauri ambacho wajumbe wake wote walikuwa Waislamu; chombo kilichokuwa ndani ya TANU ambacho kilimuunga mkono Nyerere na TANU tangu siku za mwanzo kabisa, kwanza chini ya uongozi wa Sheikh Suleiman Takadir na kisha chini ya Idd Tulio baada ya kufukuzwa kwa Sheikh Takadir kutoka TANU. Wakati haya yote yakitendeka Kanisa ambalo wakati wa kudai uhuru lilijiweka mbali na halikutoa msaada wowote sasa likawa linanyemelea kujiingiza katika siasa likiwa na agenda yake: kuwaweka viongozi Wakristo katika nafasi za uongozi na kuwatoa nje ya uongozi Waislamu ambao Kanisa liliwaona hawana elimu.<sup>39</sup>

Jumuiya za Kiislamu kama Al Jamiatul Islamiyya fi Tanganyika na EAMWS zilikuwa sasa zikipigwa vita na Serikali ya Nyerere kama vyombo ambavyo havikuwa na umuhimu wowote katika Tanganyika mpya. Katika kumuhakikishia utiifu wao juu yake, Waislamu walijitahidi mwisho wa uwezo wao kuziweka Taasisi zao kando na chuki za kidini dhidi ya Wakristo.<sup>40</sup> Juhudi hizi hazikuthaminiwa. Serikali ilifanya juhudi za siri kuhakikisha kuwa jumuiya zote za Waislamu zinapigwa marufuku.<sup>41</sup>

Huu ndio ukawa mwanzo wa kampeni za kufuta historia ya Uislamu katika TANU na mwisho wa Waislamu kuwa na sauti katika siasa baada ya uhuru kupatikana. Baada ya kupatikana kwa uhuru, ile nguvu ya Waislamu iliyotumika kupambana na Waingereza kuleta uhuru, ikaonekana haina maana yoyote na haifai kitu tena. Kuvunjwa kwa Baraza la Wazee ilikuwa kishiko cha mwisho cha Waislamu katika TANU. Baada ya hapo Kanisa lililokuwa pembeni wakati wa kudai uhuru sasa likajitokeza waziwazi kuwapiga vita Waislam katika TANU. Katika kitendo ambacho kanisa halikupata kufanya, Kanisa Katoliki Bukoba liliteua wagombea wake wenyewe wapambane na wagombea Waislamu walioteuliwa na TANU kugombea nafasi katika uchaguzi wa Serikali za mitaa. Kanisa lilisema limeweka wagombea wake binafsi kwa kuwa wana elimu kupita wagombea wa TANU Waislamu. Kampeni kama hii ilifanyika vilevile Kigoma.

Hakuna ushahidi wowote unaoonyesha kuwa Nyerere, Serikali au TANU yenyewe ilichukua hatua zozote dhidi ya Kanisa kwa kuchanganya “*dini na siasa*”.

## **Mkutano wa Pili wa Waislamu, 1963**

Ulipoitishwa Mkutano wa Pili wa Waislamu Dar es Salaam matatizo haya mazito yaliwekwa kwenye agenda ili yajadiliwe. Mkutano ule ulithibitisha bila wasiwasi wowote kuwa kulikuwapo na njama za sirisiri ndani ya TANU kuhujumu Waislamu na njama hizi zikienda sambamba na kampeni nchi nzima dhidi ya Waislamu na viongozi wa EAMWS.<sup>42</sup> Nyerere alialikwa kufunga mkutano ule na Waislamu wakamueleza masikitiko yao kwa hali ile iliyojitokeza. Nyerere alizungumza kwa kirefu matatizo ya Waislamu na kwa kiasi aliweza kutuliza mambo. Lakini kulikuwa hapana shaka katika fikra za viongozi wa EAMWS kuwa kulikuwa na njama zilizopangwa na Kanisa mahsusi kwa minajili ya kupiga vita Uislamu na Waislamu. Uongozi wa Wakristo katika TANU, Serikali na Nyerere binafsi alitumika kufanikisha azma hiyo. Uongozi wa Kikristo katika taasisi za umma sasa ukawa unatumia nguvu za dola kulipa Kanisa madaraka ili liweze kudhibiti Serikali na TANU.

Tarehe 20 Januari, 1964 kulitokea maasi katika jeshi la *Tanganyika Rifles*. Nyerere alirudishwa madarakani na jeshi la Waingereza lililoletwa kuzima maasi. Baada ya mambo kutulia Nyerere akachukua nafasi hiyo kuwaweka kizuizini viongozi wa vyama vya wafanyakazi na masheikh maarufu katika Tanganyika. Kesi ya uhaini ya wanajeshi ilipofikishwa Mahakama Kuu hapakuwa na ushahidi wowote ule kuwa Masheikh walihusika kwa njia moja au nyingine katika uasi wa *Tanganyika Rifles*. Uvumi uliokumba mji wa Dar es salaam ni kuwa masheikh hao walikuwa wanapanga njama za kupindua Serikali. Baada ya hapo, mwanazuoni maarufu, Sharif Hussein Badawiy na mdogo wake Mwinyibaba, walipewa notisi ya kuondoka nchini kama wahamiaji wasiotakiwa. Kilichofanya Shariff Badawiy afukuzwe nchini ni kauli aliyotoa Mwinyibaba katika maulid.

Akiwahutubia Waislamu katika maulid yale, Sheikh Abdallah Chaurembo alisema kuwa Waislamu wanapaswa kuishukuru Serikali kwa kutoa ruhusa kwa Waislamu kuondoka kazini mapema siku ya Ijumaa ili wapate fursa ya kuswali swala ya Ijumaa. Baadhi ya Waislamu waliokuwapo pale waliona kama kwamba Sheikh Chaurembo alikuwa akijikomba kwa Serikali ili apate umaarufu wa bure na kwa ajili hiyo afaidike kisiasa. Iliamuliwa kuwa Waislamu lazima wajibu hotuba ya Sheikh Chaurembo usiku ule ule bila ya kungoja. Mwinyibaba alipanda kwenye mimbari ile ile ambayo muda mfupi uliopita Sheikh Chaurembo alihutubu. Mwinyibaba aliwaeleza Waislamu kuwa wao hawahitaji kumshukuru yeyote kwa ajili ya kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu. Vyovyote iwavyo swala ya Ijumaa ni fardh inayomuwajibikia kila Muislamu na hana khiyari ila kuitekeleza, Serikali iwe imetoa ruhusa au vinginevyo.

Sheikh Abdallah Chaurembo alikuwa hapo mwanzoni mwanafunzi wa Sheikh Hassan bin Amir na alikuwa chini ya Sheikh Hassan hadi ilipotokea mtafaruku baina yake na mwalimu wake mwaka 1961. Chanzo cha mtafaruku ilikuwa ni kuhusu mambo ya akida katika siasa za TANU. Kwa ajili hii ikabidi Sheikh Chaurembo ajiondoe kwa sheikh na akajihusisha katika siasa hadi akachaguliwa kuwa mjumbe wa Kamati Kuu ya TANU.

Jibu kama lile alilotoa Mwinyibaba likaonekana kama ni kuonyesha fedhuli kwa Serikali na TANU. Siku ya pili yake Serikali ikatoa amri Shariff Hussein afukuzwe nchini pamoja na mdogo wake Mwinyibaba ingawa yeye Shariff Hussein hakuwepo hata kwenye hafla ile ya maulid kwa kuwa alikuwa nje ya Dar es Salaam. Shariff Hussein na Mwinyibaba ikabidi waondoke na kurudi kwao Kenya. Lakini ili ieleweke sababu ya kutiwa kizuizini hawa masheikh inabidi turudi nyuma katika mkutano wa mwaka wa EAMWS uliofanyika mwaka 1963.

Jaribio la mwanzo la Nyerere kutaka kuivunja EAMWS lilikuwa mwaka 1963. Lakini jaribio hilo halikufanikiwa kwa sababu ya mpango uliopangwa na Mufti Sheikh Hassan bin Amir na kutekelezwa na Bilali Rehani Waikela, katibu wa EAMWS Tabora. Mwaka huu wa 1963 EAMWS ilifanya mkutano wake katika ukumbi wa Shule ya wasichana ya Aga Khan (shule ya Jangwani ya leo). Wajumbe wa mkutano huo walipowasili mjini Dar es Salaam walikuta uvumi kuwa wajumbe wa mkutano wa EAMWS watakatwa na kuwekwa kizuizini. Chanzo cha uvumi huu hakikufahamika lakini haikuwa vigumu kukisia. Baada ya kuvunjwa kwa Baraza la Wazee wa TANU mwaka ule ilikuwa wazi kuwa Nyerere alikuwa amewatupa mkono washirika wake wa zamani na sasa alikuwa akitafuta wanya ili kujenga upya msingi wake wa siasa. Kutokana na mambo yalivyokuwa yakienda ilikuwa ni dhahiri washirika wake wanya hawatakuwa Waislamu. Katibu wa EAMWS Tabora, Waikela alipowasili Dar es Salaam kuhudhuria mkutano alitwa na Sheikh Hassan bin Amir. Mufti Sheikh Hassan bin Amir mbele ya Mzee Ali Comorian, alimfahamisha Waikela kuwa kulikuwa na njama zilizokuwa zikipikwa na Nyerere kumuangamiza yeye na Tewa Said Tewa ili kuvunja EAMWS ipatikane nafasi ya kuanzishwa jumuiya ya Kiislamu ya Watanganyika itakayokuwa chini ya wanafiki. Sheikh Hassan bin Amir alimwambia Waikela kuwa harakati za uhuru ziilikuwa zinatekwa nyara na Wakristo kwa manufaa ya makanisa yao. Sheikh Hassan alimfahamisha Waikela kuwa ni lazima yeye afanye kila linalowezekana ili njama za Nyerere zishindwe. Baada ya maneno hayo Sheikh Hassan bin Amir alinyanyua mikono yake juu na kumuomba dua Waikela. Nyerere alikuwa anamfahamu Waikela kwa kuwa alikuwa muasisi wa TANU na alikuwa ametoa mchango mkubwa katika kupigania uhuru.

Nchi nzima hasa sehemu za Waislamu kulikuwa na mpango wa Serikali wa kuwavunja Waislamu nguvu na kuwakatisha tamaa. Waikela, kama ilivyokuwa kwa viongozi wengine wa EAMWS, alikuwa anasugua na Mkuu wa Mkoa wa Jimbo la Magharibi, Richard Wambura. Kulikuwa na ujeuri kwa upande wa Serikali

walipokuwa wanashughulikia matatizo ya Waislamu, mbali na mategemeo ya Waislamu waliyokuwanayo kabla ya uhuru. Subira ya Waikela ilifikia kikomo pale Wambura alipowatukana Waislamu katika mkutano wa hadhara. Baada ya kuhutubia Wambura, Waikela alipanda jukwaani na akaikumbusha Serikali kuwa isiwe mwizi wa fadhila kwa kusahau jinsi Waislamu walivyojitolea muhanga katika kudai uhuru. Serikali ikachukulia hotuba ya Waikela kama usaliti na yenye kuwashawishi Waislamu wasiitii Serikali. Ilikuwa katika hali hii Waikela mwanachama shupavu wa TANU alijitoa kwenye chama na akaamua kutumia nguvu zake kuwatumikia Waislam kupitia EAMWS. Ilikuwa wazi kuwa Nyerere alikuwa na habari za msuguano kati ya Serikali na Waislamu kule Tabora na mtu aliyehusika na msuguano huo.

Siku kabla ya mkutano wa EAMWS, Nyerere aliwaalika wajumbe wa mkutano *Government House* kwa chakula cha usiku. Hao waalikwa walikuwa wajumbe waliochaguliwa mahsusi. Waikela hakuwa mmoja wa hao waalikwa. Nyerere alichukua nafasi ile kuwashauri wajumbe wale waanzishe jumuiya ya Waislamu wa Tanganyika ichukue nafasi ya EAMWS. Wajumbe hawa walipoleta katika mkutano hoja ya kuanzisha jumuiya ya Waislamu wa Tanganyika, Waikela alisimama na kuipinga hoja ile. Alizungumza vilevile kuhusu uadui wa Serikali kwa Waislamu na Uislamu. Waikela alimaliza hotuba yake kwa kutoa changamoto kwa wajumbe wamuite Nyerere kwenye ufunguzi wa mkutano ili awaeleze wajumbe msimamo wake kuhusu kadhia ile ya chinichini baina ya Serikali na Waislamu.

Baada ya kushindwa kwa hoja ya kuivunja EAMWS wajumbe wa mkutano ikaonekana kuwa ingekuwa vyema Nyerere aitwe kufunga mkutano ule na asomewe makubaliano yaliyofikiwa. Nyerere alifika kufunga ule mkutano na akakutana uso kwa uso na Waikela, ambae alimsomea maazimio ya mkutano. Waikela alimfahamisha Nyerere kuwa umoja kwa Waislamu ni *faradh* (wajibu wa lazima). Ni kwenda kinyume na maamrisha ya Allah(s.w) kuwagawa watu. Baada ya utangulizi huu Waikela huku akimnyooshea Nyerere kidole alieleza uadui uliooneshwa na Serikali dhidi ya Waislamu. Waikela alimaliza hotuba yake kwa kitisho. Alimwambia Nyerere ikiwa Waislamu watamgeuka kupambana naye hatakuwa na uwezo wa kuwashinda. Nyerere alitulia pembeni mwa Rais wa Baraza la Tanganyika la EAMWS Tewa Said Tewa, akimsikiliza Waikela. Aliposimama kujibu hotuba ya Waikela Nyerere alisisitiza msimamo wa Serikali wa kutoa haki na usawa kwa raia wake wote. Kwa kiasi fulani Nyerere alikuwa amefanikiwa kupunguza joto kati ya Waislamu na Serikali.

Hotuba ya Waikela na ya Nyerere zikapewa umuhimu mkubwa katika radio. Waislamu wengi wakajitokeza stesheni ya gari moshi Tabora kumpokea shujaa Waikela. Alipewa heshima ile kwa kuwa na ujasiri wa kuweza kusimama kidete dhidi ya wale waliodhani kuwa wanaweza kuwakalia Waislamu vichwani. Nyerere alihisi ameumbuka na hili lilimchoma moyo sana. Kuanzia

hapa Nyerere hakumtazama Sheikh Hassan bin Amir kwa jicho jema. Mwaka uliofuata, tarehe 20 Januari, 1964 jeshi liliasi. Nyerere alichukua fursa ile kuwatia kizuizini masheikh walioonekana wanapinga Serikali na viongozi wa vyama vya wafanyakazi. Waikela alikuwa mmoja wa wale waliokamatwa na kuwekwa kizuizini.<sup>43</sup> Nyerere kwa wakati ule hakuwa na nguvu ya kumgusa Mufti Sheikh Hassan bin Amir.

Wakati ule, mwaka wa 1963, shughuli za kuendesha mafundisho ya Uislamu EAMWS ilikuwa ikienda vizuri sana. Da'awah ilikuwa chini ya Sheikh Amir bin Juma kutoka Tanga na Wakristo wengi walikuwa wakirudi katika Uislamu. Tabligh ilikuwa ikiongozwa kutoka kwa masheikh wa mikoa na wilaya. Fedha za kufanyia shughuli hizi zilikuwa zikichangwa na Waislamu wenyewe. Mufti Sheikh Hassan Bin Amir yeye alikuwa akisomesha fikh, mantik, tauhiid, na tafsir ya Qur'an katika misikiti mbalimbali ya Dar es Salaam. Wakati ule Katibu Mkuu wa EAMWS kwa Afrika ya Mashariki alikuwa V.M. Nazarali.

## **Juhudi za kuanzisha Chuo Kikuu cha Kiislamu Chini ya EAMWS, 1964**

Mwezi Aprili 1964 ujumbe wa hali ya juu wa EAMWS ndani yake wakiwemo Sheikh Hassan bin Amir, Sheikh Said Omari Abdallah, Tewa Said Tewa, Katibu wa EAMWS Abdul-Aziz Khaki na mzee wa TANU, Mzee Mwinjuma Mwinyikambi; Makisi Mbwana, Issa Mtambo, Omari Muhaji na Saleh Masasi waliondoka kwenda ziara ya nchi za Kiislamu kutafuta msaada wa kujenga Chuo Kikuu cha Kiislamu na kuanzisha uhusiano na nchi za Waislamu. Gamal Abdul Nasser alikutana na ujumbe ule akaupatia ofisi, huduma za simu, na makatibu muhtasi ili waweze kutayarisha mipango yao kwa Serikali ya Misr. Halikadhalika alimuagiza makamu wake Sharbasy afanye makubaliano na EAMWS kwa niaba yake. Serikali ya Misr ilikubali kugharamia ujenzi wa chuo hicho. Mkataba wa makubaliano ukatiwa sahihi mjini Cairo kati ya Tewa Said Tewa kwa niaba ya EAMWS na Makamu wa Rais wa Misr, Sharbasy kwa niaba ya Serikali yake.

Serikali ya Misr iliahidi kujenga Chuo cha Kiislamu ambacho kingemilikiwa na kuendeshwa na EAMWS. Gharama ya mradi mzima ilikuwa pauni milioni hamsini na tano (£ 55,000,000) za Ki-Misri. Baada ya kukamilisha kazi ile ujumbe ule uliondoka Cairo kuelekea Makka kufanya ibada ya Hija. Baada ya kumaliza Hija wajumbe wanne walirudi nyumbani na Tewa, Aziz Khaki, Sayyid Omar Abdallah wakaendelea na safari kwenda Aman, Jordan ambako walifanya mazungumzo na Mufti na Waziri wa Aukaf. Kutokea hapo ujumbe ulikwenda Kuwait ambako walikutana na Sheikh wa Kuwait kisha wakaenda Baghdad, Iraq na kukutana na Rais wake, Abdisalama Arifek. Kutoka hapo ujumbe ulielekea Beirut, Lebanon ambako ulifanya mazungumzo na viongozi wa harakati za Kiislamu. Baada ya kutoka Beirut ujumbe ule ulirudi tena Cairo



kwa ajili ya kukamilisha makubaliano ya kujenga Chuo Kikuu. Tarehe 20 Mei, 1964 ujumbe ulirejea Dar es Salaam na kupokelewa na viongozi wa EAMWS na Waislamu kwa ujumla.

Mkutano wa Halmashauri Kuu ya EAMWS ukaitishwa na Tewa Said Tewa akatoa taarifa yake kuhusu ujenzi wa Chuo Cha Kiislamu. Siku ya pili Tewa akaitisha mkutano wa waandishi wa habari na kutoa habari za kujengwa kwa Chuo Cha Kiislamu kwa vyombo vya habari na kwa Waislamu kwa ujumla. Kwa mafanikio haya Tewa akawa amejichimbia kaburi. Matokeo haya yalijaza hofu kwa viongozi wa Kanisa. Kampeni za chinichini dhidi ya Tewa binafsi na uongozi mzima wa EAMWS zilianza. Mara baada ya ujumbe wa EAMWS kurudi kutoka ziara yake, Nyerere alifanya mabadiliko katika Baraza la Mawaziri na Tewa Said Tewa, Mwenyekiti wa EAMWS upande wa Tanzania akajikuta nje ya Serikali. Nyerere akamteua Tewa Balози wa Tanzania katika Jamuhuri ya Watu wa China. Mwezi Januari, 1965 Tewa alikwenda China kuanza kazi yake mpya. Inasemekana uteuzi wa Tewa kwenda China ulisababishwa na juhudi zake za kutaka kuwaunganisha Waislamu kuwa kitu kimoja chini ya jumuiya moja yenye nguvu. Wakati ule ile mipango iliyopitishwa na mkutano wa Waislamu mwaka 1962 ilikuwa ikitekelezwa vyema, shule zilikuwa zimejengwa Ilala, Kigogo na Kurasini, Dar es Salaam; Ruvu na Maneromango. Shule hii ya Maneromango ilikuwa na umuhimu wa pekee kwa sababu hii ndiyo ilikuwa shule ya kwanza ya Waislamu kujengwa Uzaramoni. Shule za sekondari zilikuwa zikijengwa Dar es Salaam, Kinondoni na Moshi, Kibohehe. EAMWS ilikuwa vilevile imetiliana mkataba wa makubaliano na Serikali ya Misr kuipa scholarship thelathini na tano kila mwaka kwa wanafunzi wa Kiislamu kusoma Misri. EAMWS ilikuwa imejenga shule, misikiti, shule za ufundi na hosteli kwa ajili ya wanafunzi katika sehemu nyingi za Afrika ya Mashariki.

	<b>Uganda</b>	<b>Tanzania</b>	<b>Kenya</b>
Shule	77	70	28
Misikiti	67	53	29
Shule za Ufundi	3	-	-
Hosteli	1	-	-

Chanzo: Utafiti

Baada ya Tewa kuondoka Bibi Titi Mohamed akachaguliwa kuwa makamu mwenyekiti wa tawi la EAMWS la Tanzania ili kuongeza nguvu makao makuu kwa kuwa mwenyekiti hakuwepo. Kutokuwepo kwa Tewa nchini kulileta pengo ambalo ilibidi lijazwe. Ghafla palizuka uvumi kuwa Sheikh Abdallah Chaurembo alikuwa achukue uongozi wa EAMWS. Inasemekana nia yake ilikuwa ni kupata Urais wa EAMWS na kisha achaguliwe kuwa Mufti wa Tanzania. Uvumi huu

ulidumu kwa karibu mwaka mzima hadi pale Tewa aliporudi kutoka Peking baada ya kujuzulu Ubalazi kuja kugombea Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1965. Aliporudi Tewa alihojiwa na waandishi wa habari kuhusu uvumi ule na yeye jibu lake lilikuwa: “Muislamu yeyote mwenye sifa ya maadili mema ana haki ya kugombea nafasi yoyote katika uongozi wa EAMWS”. Neno alilolitumia Tewa katika kumueleza mtu ambaye angeweza kuwaongoza Waislamu lilikuwa “taq-wa”, neno la Kiarabu lenye maana ya ucha-mungu.

Nikuanzia katika matukio haya ndipo tunaweza sasa kuanza kuchunguza jinsi Nyerere akiitumia Serikali alivyoanza kuuhujumu umoja wa Waislamu kwa kutumia njama na hujuma za dhahiri na za kificho, propaganda na kueneza uongo dhidi ya uongozi wa EAMWS, ambao ulionekana ni tishio kwa utawala wake. Wakati ule Serikali nzima ilikuwa mikononi mwa Wakristo. Ukiwatoa Wazanzibari waliokuwa katika Serikali ya muungano – A.M. Maalim, Waziri wa Biashara na Viwanda; Aboud Jumbe, Waziri wa Nchi; A.M. Babu, Waziri wa Ardhi, Makazi na Maji; Hasnu Makame, Waziri wa Habari na Utalii; Rashid Kawawa ambae alikuwa mtu wa karibu sana na Nyerere, waziri Muislam katika Baraza la Mawaziri kumi na tano kutoka bara alikuwa Said Ali Maswanya, Waziri wa Mambo ya Ndani.

## **“Mgogoro” wa EAMWS, 1968**

Kutokana na katiba ya mwaka 1957, lengo kuu la EAMWS lilikuwa ni “kuutangaza Uislamu katika Afrika ya Mashariki”. EAMWS yenyewe ilikuwa ikijigamba kuwa uti wake wa mgongo ilikuwa ni tabligh, yaani utangazaji wa dini. Jumuiya hii toka ilipoanzishwa 1933 ilikuwa ya Waislamu wa mataifa yote katika uanachama na katika uongozi wake. Katika uhai wake wa miaka thelathini na tano EAMWS ilijiweka mbali sana na siasa. Jumuiya hii ilishughulikia kuuetea na kueneza Uislamu katika Afrika ya Mashariki. Lakini baada ya kutokea maasi ya *Tanganyika Rifles* mwaka 1964 yaliyopelekea viongozi wengi wa Kiislamu kuwekwa kizuizini, EAMWS ikawa imepoteza mwelekeo wake na kudhoofika. Baadhi ya matawi yaliyokuwa katika majimbo yakafungwa kwa woga na kukosa viongozi thabiti. Matawi mengine yalifungwa kwa sababu viongozi wake walikuwa wakichimbwa chinichini na Serikali. Waislamu wengi walihisi vitisho vya Serikali kwa hiyo waliogopa kuchukua uongozi wa EAMWS. Wengi waliogopa kuitumikia EAMWS kwa kuwa walihisi ofisi za jumuiya hiyo zilikuwa zikichukuliwa na Serikali kama vituo vya upinzani dhidi yake. Kwa zaidi ya miaka mitatu toka ule mkutano wa mwaka 1963, EAMWS haikuweza kufanya mkutano wowote.

EAMWS ilipokuja kuitisha mkutano wake wa mwaka mjini Arusha mwaka 1966 kikajitokeza kikundi kutoka upande wa Tanzania kikidai EAMWS ijigawe, kila nchi iwe na mamlaka yake na ijitegemee yenyewe, yaani Tanzania, Kenya na Uganda zote ziwe mbalimbali. Kikundi hiki kilichokuwa kikidai utengano

vilevile kikadai kuwa katiba ya EAMWS nayo iwe ya 'kizalendo'.<sup>44</sup> Hii ilikuwa na maana kuwa uongozi uifanyie katiba marekebisho ili kuiwezesha Tanzania kuwa huru ndani ya EAMWS. Wajumbe waliokuwa wanaona mbali kutoka Tanzania na wengine kutoka Kenya na Uganda, na kwa hakika mkutano mzima kwa ujumla walipinga kitendo hicho, wakidai kuwa kwa kufanya hivyo Waislamu wa Tanzania watakuwa wamejitenga na wa Uganda na Kenya. Jambo hili likitokea, si tu lingekuwa limewadhoofisha Waislamu wa Tanzania peke yao, bali Waislamu wa Afrika ya Mashariki nzima. Wajumbe wa Kenya na Uganda walikuwa wanatambua kuwa kulikuwa na shinikizo kubwa kutoka Serikali ya Tanzania kwa Watanzania kujitoa kutoka EAMWS.

Halikadhalika ilikuwa inafahamika kuwa wajumbe wa Tanzania walikuwa wakifanya kazi chini ya shinikizo kali kutoka Serikali ya Nyerere. Haikuwa siri sana kuwa baadhi ya viongozi wa EAMWS walikuwa kisirisiri wakiandamwa na Serikali. Lakini mkutano ule haukuzungumzia matatizo haya kwa kuwa hayo yalichukuliwa kama matatizo ya ndani ya nchi. Hata hivyo kwa ule moyo wa Kiislamu wa kuhurumiana, wajumbe wa Kenya na Uganda kwa faragha walionyesha masikitiko yao kwa Tewa kuhusu ile hali iliyokuwa ikiwakabili Waislamu wa Tanzania. Wajumbe walipokuwa wakiondoka kurejea makwao, ilikuwa wazi kuwa Serikali ya Tanzania ilikuwa ikiingilia kati EAMWS kiasi cha kuifanya jumuiya hiyo ishindwe kufanya kazi yake vyema na kupitisha maamuzi yake. Hali hii ilijidhihirisha wazi pale kwa kipindi kizima cha mkutano, makachero wa Serikali walikuwa wamejitokeza kwa wingi mjini Arusha. Haukupita muda ikadhihirika kuwa Serikali ilikuwa imepania kuivunja EAMWS kwa kuwatumia Waislamu wachache walioteuliwa kwa kazi hiyo. Lengo likiwa ni kuanzisha taasisi mpya ambayo Serikali ingeweza kuiamuru. Ieleweke hapa kuwa kama tulivyokwisha eleza hapo nyuma, Serikali nzima ya Tanzania ilikuwa mikononi mwa Wakristo na watendaji hawa walikuwa wapo chini ya Kanisa. Hii ilikuwa na maana kuwa kilichotakiwa kuwepo ilikuwa taasisi ya Kiislamu ambayo Kanisa lingeweza kuiamuru.

Hili lilikuwa ni jambo la lazima kufanyika ili kuwadhibiti Waislamu kama nguvu inayoweza kuleta mabadiliko ya siasa. Baada ya kuelewa hali hii ndipo sasa tunaweza kuangalia kile kilichoitwa 'mgogoro' wa EAMWS ambao ulidumu kwa miezi mitatu ya mwisho wa mwaka wa 1968.

Ili tuweze kuelewa vyema kisa kizima cha 'mgogoro' ni muhimu kwanza kuelewa chanzo chake, hadhi za wahusika wakuu na nafasi zao katika 'mgogoro' ule. Mwisho, ni muhimu kuweka bayana na kuchambua nafasi ya Julius Nyerere, Serikali yake, chama cha TANU na vyombo vya dola katika 'mgogoro' ule. Hii itasaidia kuelewa kama kweli ulikuwepo 'mgogoro' katika EAMWS, au 'mgogoro' ulibambikizwa na watu katika TANU, Serikali na ndani ya Waislamu wenyewe ili kuwadhoofisha Waislamu kwa nia ya kuwa usije Uislamu ukawa na nguvu katika Tanzania hivyo kuwawezesha Waislamu kushika madaraka

ya nchi. Mwaka wa 1967 Mwalimu Julius Nyerere alitangaza Azimio la Arusha hatua ambayo iliingiza Tanzania katika siasa ya ujamaa.

Adam Nasibu, mwalimu wa shule ya msingi, aliyekuwa katibu wa EAMWS kule Bukoba alijitafutia umaarufu kwa kuongoza maandamano hadi ofisi ya TANU ya Mkoa kumuunga mkono Mwl. Nyerere na sera yake mpya ya Azimio la Arusha. Inesemekana Adamu Nasibu alisema kuwa ujamaa ni sawa na mafundisho ya Qur'an Tukatifu. Adam Nasibu hakuishia hapo alikwenda mbele zaidi na kutoa 'miongozo kwa viongozi wote wa Kiislamu wa Bukoba akifafanua Azimio la Arusha'.<sup>45</sup> Wasiokuwa Waislamu walimuona Adam Nasibu kama Muislamu mwenye mwamko mzuri wa kimaendeleo, na kwa kuwa yeye alikuwa ni kiongozi wa EAMWS, kuunga kwake mkono Azimio la Arusha kulionekana kama kitendo rasmi cha jumuiya hiyo kuunga mkono sera hiyo.

Katika hali ya kawaida, uongozi wa EAMWS pale makao makuu Dar es Salaam ulikasirishwa kidogo na kitendo cha Adam Nasibu cha ushabiki wa siasa. Lakini uongozi wa EAMWS haukumuonya kiongozi wake wa Bukoba kuhusu jambo lile ambalo dhahiri halikuwa la kupendeza katika jumuiya. Bila shaka uongozi wa EAMWS ulichelea kuwa kwa kufanya hivyo wangelionekana si wazalendo, hasa ukiichukulia jinsi wananchi walivyohamasika na Azimio la Arusha.

Tofauti na mwaka 1963 wakati Nyerere alipojaribu kufanya mapinduzi dhidi ya uongozi wa EAMWS, mwaka 1967 hali ya mambo ilikuwa imebadilika sana yakimwendea Nyerere vyema. Serikali ilikuwa imedhibiti vyombo vyote vya habari ukiondoa gazeti la *The Tanganyika Standard* ambalo bado lilikuwa chini ya Lonrho. Nyerere alikuwa amemuweka Martin Kiama kama mkurugenzi wa radio ya taifa, na Benjamin Mkapa<sup>46</sup> kama mhariri wa magazeti mawili ya TANU, **The Nationalist** na Uhuru. Adam Nasibu aliandikwa katika magazeti na habari zake kutangazwa katika radio kwa ajili ya kitendo chake, hasa kuhusu yale maneno aliyosema kuwa ujamaa ni sawa na mafundisho ya Qur'an.

Katika hali ya mambo kama yalivyokuwa wakati ule hasa jinsi ile hali ya uhasama ilivyokuwapo baina ya Serikali na Waislamu, baadhi ya Waislamu walimuona Adam Nasibu kama kibaraka anayetafuta umaarufu wa bure kwa kujipendekeza kwa TANU, Nyerere na Serikali yake. Kwa wengine Adam Nasibu alionekana kama mzalendo na Muislamu aliyekuwa na 'uoni wa mbali'. Kwa ajili hii basi Serikali ikamuona kama kiongozi wa baadaye ambaye ingeweza kumtegemea wakati wa shida. Uongozi wa EAMWS makao makuu ukaonekana haupo pamoja na wananchi, wala haujali shida zao na uko mbali sana na sera za Serikali. Lakini kwa hakika EAMWS kama taasisi ya dini isingeliweza kujitokeza na kuunga mkono Azimio la Arusha kwa kuwa hayo yalikuwa mambo ya siasa. Kwa kufanya hivyo ingelikuwa inakwenda kinyume na msimamo wake wa kutojiingiza katika siasa.

Hata hivyo kuwa nje ya Azimio la Arusha kukaonekana kama kitendo cha kukosa uzalendo na kutoa picha kuwa jumuiya hiyo ilikuwa haijali maendeleo na ustawi wa watu wa Tanzania. Mambo yakawa yamevurugika zaidi kwa kuwa Rais wa EAMWS, Tewa Said na makamo wake Bibi Titi Mohamed waliokuwa katika Baraza la Mawaziri la Nyerere walipoteza nyadhifa zao za ubunge katika uchaguzi mkuu wa mwaka 1965. Kwa ajili hii basi Serikali ikawa inaeneza propaganda kuwa kwa kuwa Tewa na Bibi Titi waliokuwa katika uongozi wa juu wa EAMWS, walikuwa wanatumia nafasi zao kujijengea himaya mpya kutoka kwa Waislamu dhidi ya Nyerere. Viongozi hawa ikawa lazima washughulikiwe na kuangamizwa. Mtu wa kufanya kazi hii hakuwa mwingine ila Adam Nasibu, katibu wa EAMWS Bukoba. Adam Nasibu alikuwa tayari keshafanikiwa kufanya mapinduzi dhidi ya Rais wa EAMWS, Tewa Said Tewa. Kutokana na vitendo vyake alikuwa ameidhihirishia Serikali kuwa yeye angeweza kuwa mtumishi bora kwa dola kuliko ule uongozi wa EAMWS uliokuwa pale makao makuu Dar es Salaam ambao ulikuwa ukionekana umechoka.

Wakazi wa Dar es Salaam kila mwaka walikuwa wakifanya maulidi katika viwanja vya Mnazi Mmoja kuadhimisha kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (s.a.w). Huu ndio toka asili ulikuwa uwanja ambao TANU ilifanya mikutano yake yote wakati wa kupigania uhuru. Mwezi Juni 1968 maulidi mbili katika usiku mmoja zilisomwa kuadhimisha kuzaliwa kwa Mtume(s.a.w). Maulidi moja ilisomwa Mnazi Mmoja na nyingine Ilala. Chanzo cha haya yote ni kuwepo kwa kutoelewana kati ya viongozi wa Waislamu waliokuwa wanajiona kuwa ni 'wazalendo' wafuasi wa TANU na wale viongozi wa EAMWS ambao kambi nyingine ilikuwa ikiwaona kama wapinzani wa TANU. Yale maulidi yaliyosomwa Ilala yalihudhuriwa na viongozi wa EAMWS na yalipata watu wengi na yakafana sana ukilinganisha na yale maulidi ya Mnazi Mmoja, ya wafuasi wa TANU. Uongozi wa TANU ulitishika na hali hii iliyokuwa ikijitokeza kwa maana ilikuwa inaonyesha kuwa chama kilikuwa kinapoteza wafuasi ambao walikuwa wakijiunga na kambi ya Tewa na Titi iliyokuwa ikisemekana ipo dhidi ya Nyerere.

Tarehe 17 Juni, 1968, Adam Nasibu akatokea tena katika magazeti akifahamika kama katibu wa EAMWS kutoka Bukoba mwenye hamasa za kisiasa ambaye aliunga mkono Azimio la Arusha na kutoa maelekezo kwa viongozi wengine wa Kiislamu akieleza vipengele vya azimio hilo. Adam Nasibu alitangaza kupitia radio ya Serikali na magazeti ya TANU kuwa mkoa wake, Bukoba unajitoa kutoka EAMWS.<sup>47</sup> Ghafila Adam Nasibu akawa mtu mashuhuri wa kufahamika nchi nzima, magazeti ya TANU na radio ya Serikali ikaanza kumjenga haiba yake pamoja na kutangaza kile kilichokuja kujulikana kama 'mgogoro' wa Waislamu. Magazeti ya TANU chini ya Wiliam Benjamin Mkapa yakawa yamepata habari ya kushabikia. Radio ya Serikali na magazeti ya TANU kwa pamoja yakawa yanatoa habari kwa uzito wa hali ya juu kuhusu kujitoa kwa Bukoba katika EAMWS. Magazeti ya TANU yakiwa yamesheheneza vichwa vya habari na maelezo ya mgogoro na picha za Adam Nasibu zikipamba kurasa zake za mbele.<sup>48</sup>

Ilikuwa baada ya magazeti na radio kutangaza na kuandika habari hizo ndipo Waislamu kwa mara ya kwanza wakaja kutanabahi kuwa walikuwa wanakabiliwa na 'mgogoro' mkubwa wa nchi nzima. Lakini matatizo yalikuwa yameanza hasa toka siku ile watu wa Dar es Salaam waliposoma maulidi mbili mwezi wa Juni, 1968. Siku tano baadae, yaani tarehe 22 Oktoba, 1968 Sheikh Juma Jambia mwanakamati wa halmashauri kuu ya EAMWS kutoka Tanga na yeye akatangaza kuwa Tanga inajitoa katika EAMWS.<sup>49</sup> Mwenyekiti wa EAMWS Tewa Said Tewa akamfahamisha Sheikh Jambia kuwa uamuzi wake ulikuwa ni uamuzi wa mtu mmoja. Jibu la Sheikh Jambia lilikuwa ni kutoa taarifa kwa vyombo vya habari kuvifahamisha uamuzi huo. Sheikh Jambia alitoa taarifa hiyo pamoja na mtu mmoja aliyefahamika kwa jina la Abdi Matunga. Haukupita muda mrefu, Iringa nayo ikatangaza kuwa inajitoa kutoka EAMWS. Uongozi wa EAMWS kwa haraka ukaitisha mkutano kujadili hali ile mpya iliyojitokeza. Vyombo vile vya habari, Uhuru na *The Nationalist* ambavyo vilikuwa vikiwatumikia wale waliodai kujitenga na EAMWS, sasa vikawa havitaki kutoa au kuandika habari za viongozi wa EAMWS ambao walikuwa wanapigania umoja wa Waislamu. Hapa ikawa ni wazi kuwa Serikali ilikuwa inatumia vyombo vya habari, yaani magazeti yaliyokuwa chini ya TANU na radio ya Serikali kuwahujumu Waislamu na EAMWS. Uongozi wa EAMWS ulipokuja kutanabahi ni nani walikuwa nyuma ya hujuma ile wakawa wamebaini hatari iliyokuwa ikiwakabili, kwa ajili hii basi waliwageukia Waislamu kutaka msaada wao.

Kile kikundi kilichokuwa kikidai kujitenga kilitoa sababu nyingi za uamuzi wao huo. Lakini katika sababu zao zote kubwa zaidi ilikuwa katiba ya jumuiya ile ilikuwa haipo sawa na uongozi wa nchi. Walidai kuwa katiba iwe ya Kitanzania na Aga Khan asiwe patroni. Vilevile wakadai kuwa Katibu Mkuu wa jumuiya awe Mwafrika Muislamu. Wakati ule katibu alikuwa Abdul Aziz Khaki, Muismailia na Mtanzania wa asili ya Kihindi. Kikundi kile vile vile kilitaka kujua vyanzo vya misaada kwa Waislamu na misaada hiyo ilikuwa ikitumikaje.<sup>50</sup> Dai lingine na hili likawa zito kwa uongozi wa EAMWS lilikuwa "viongozi wa EAMWS wawe wale wanaoamini malengo ya TANU, wale ambao wanapinga TANU hawafai kuwa viongozi wa Waislamu wa Tanzania".<sup>51</sup> Madai haya yalifikishwa makao makuu ya EAMWS na Adam Nasibu, Muhammad Zoharia na Hamisi Kayamba. Tewa Said Tewa akiongoza Kamati Kuu ya EAMWS alijaribu kuzungumza na viongozi wale lakini hawakutaka maelewano ya aina yoyote. Siku ya pili baada ya kutoa madai haya Adam Nasibu aliitisha mkutano wa waandishi wa magazeti na ndipo akaeleza kuwa Bukoba imejitoa EAMWS.

Uislamu una kanuni na sheria zake za msingi ambazo ndizo zingewaongoza Waislamu katika maisha yao ya kila siku. Madai yaliyotolewa na kile kikundi hayakuwa madai yenye uzito mkubwa kiasi cha kusababisha farka kubwa kiasi kile kwa sababu madai yale yote yangeliweza kujibiwa kwa urahisi kabisa. Kulikuwa na baadhi ya madai ambayo yalikuwa hayajadiliki kwa sababu ya mafunzo ya msingi ya Uislamu. Tatizo la katiba lingeliweza kujadiliwa na

kumalizwa katika vikao vya kawaida. Lakini kuhoji rangi ya Muislamu hilo halijadiliki kwa kuwa Uislamu haubagui rangi ya mja kwa kuwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume na mafunzo ya Qur'an Tukufu. Ilikuwa wazi kuwa wale waliokuwa wakidai utengano katika EAMWS hawakuwa watu wajinga kiasi cha kukosa kujua kuwa hayo waliyokuwa wakidai yalikuwa kinyume na Uislamu. Kwa kuwa walikuwa wanang'ang'ania kujitoa katika EAMWS, ilikuwa sasa kitu dhahiri kuwa hiki kikundi cha Waislamu waliojawa na 'hamasa za kizalendo' walikuwa na mpango maalum uliokuwa ukisaidiwa na Serikali wa kuvunja umoja wa umma wa Kiislamu ili Waislamu wadhoofike na wawe hawana nguvu tena katika siasa.

Hata hivyo, tarehe 14 Novemba, 1968, Baraza la EAMWS la Tanzania lilitisha mkutano wa wajumbe kutoka mikoa yote ya Tanzania kujadili 'mgogoro'. Mkutano huu ulifanyika katika shule ya kiislamu Kinondoni. Pamoja na waliohudhuria ni wajumbe kutoka mikoa ambayo tayari ilikuwa imekwishajitenga na EAMWS, napajatokea katika historia ya Uislamu Tanzania mkutano kama ule. Uongozi ulikuwa unaingia katika chumba cha mkutano tayari umeshajeruhiwa vibaya sana na propaganda za magazeti ya TANU na radio ya Serikali. Katika moja ya shutuma ambazo zilikuwa zikiuandama uongozi wa EAMWS ilikuwa ni matumizi mabaya ya fedha za jumuiya.

Akifungua mkutano ule Tewa aliwatahadharisha wajumbe kuwa makini katika lolote watakaloamua kwa kuwa endapo wajumbe watashindwa kuafikiana basi matokeo yake ni kuvunjika kwa EAMWS, umoja wa Waislamu na mwisho wa miradi yote ya elimu pamoja na ujenzi wa Chuo Kikuu.<sup>52</sup> Hisia kali zilitawala mkutano huu na baadhi ya wajumbe wanawake walikuwa wakilia hasa pale baadhi ya wajumbe walipokuwa wakitoa michango yao katika mjadala walipokuwa wakisoma aya za Qur'an Tukufu na kueleza fadhila za kupigana jihad dhidi ya madhalimu na wanafiki. Hisia hizi kali zilitokana na ukweli kuwa wajumbe walikuwa wanafahamu kuwa wale wenzao waliokuwa wakidai kujitenga walikuwa wakitumiwa na madhalimu wala hawakuwa wakiyafanya yale kwa ajili ya Allah(s.w) na Mtume wake(s.aw). Mwenyekiti wa mkutano Tewa Said Tewa, aliahirisha mkutano hadi siku ya pili ili wajumbe wapoe na watoe mchango wakiwa katika hali ya utulivu.

Katika wajumbe ambao walisimama kidete kutetea umoja wa Waislamu walikuwa Sheikh Issa Mchowera kutoka Mtwara, Bilali Rehani Waikela, Hassan Johari na Sheikh Abdallah Said kutoka Kigoma.

Mkutano uliamua kuunda Tume ya Uchunguzi ya watu saba, kuchunguza chanzo cha 'mgogoro' na kisha itoe taarifa. Tume ya Uchunguzi ya Waislamu ilikuwa na wajumbe wafuatao: Mussa Kwikima (Dar es Salaam), Rajab Ukwaju (Mara), Dr. Hussein Lweno (Dar es Salaam), Mussa Nabahani (Lindi), Bilali Rehani Waikela (Tabora), Abdul Karim (Tanga) na Khamis Khalfani (Dodoma).

Mussa Kwikima kijana mwanasheria alichaguliwa kuwa katibu wa tume hiyo ya uchunguzi. Wakati huo mikoa tisa ilikuwa tayari imeshajitenga na EAMWS na magazeti ya TANU yakawa tayari yamejenga 'mgogoro' ule kufikia hali ya kuonekana kuwa ni 'mgogoro' wa taifa zima ambao kila mtu anaweza kuuingilia na kusema atakalo. Magazeti ya TANU yakawa yanaandika na kuchapisha mambo ya EAMWS kama yanavyotaka, wakizidi kutia chumvi katika ugomvi ambao tayari ulikuwa umeshaleta hofu na farka kubwa katika jamii. Inasemekana viongozi wengine wa EAMWS walikuwa wakiambiwa wajitoe huku wameshikiwa bunduki.

## **Mvutano wa Nyerere, Tewa na Bibi Titi kuhusu EAMWS, 1968.**

Ili tume ya uchunguzi ya Waislamu iweze kufanya kazi yake vyema na bila upendeleo, ilikuwa lazima kwanza ile tume iombe Serikali izuie propaganda iliyokuwa ikiendeshwa na wale waliokuwa wamejitenga na EAMWS, wakitumia jukwaa la radio ya Serikali na magazeti ya TANU. Tume ya Waislamu ilikutana na Waziri wa Habari na Utangazaji, Hasnu Makame, ofisini kwake tarehe 20 Novemba, 1968, kujadili tatizo lile. Hii haikusaidia kitu. Propaganda dhidi ya uongozi wa EAMWS iliendelea kwa nguvu zote. Mashambulizi kutoka pande tatu yaliyopangwa vyema yalikuwa kazini. Benjamini Mkapa akitumia gazeteti la *Nationalist* ataandika habari yoyote ya Adam Nasibu, Martin Kiama alitumia Radio Tanzania kutoa habari ile kama habari muhimu na kuitangaza kutwa nzima huku ofisi ya Rais ikiwa kimya kwa fitna ile. Lile kundi la waliojitenga na umma wa Waislamu, Adam Nasibu akiwa kama msemaji wao mkuu wakati mwingine kwa mastaajabu makubwa wakawa wanakiuka hata misingi ya akida ya Tanzania, wakitoa madai ya ubaguzi wa rangi, wakikazania lazima EAMWS ivunjwe. Adam Nasibu alinukuliwa na *The Nationalist* akisema kuwa:

*“Waislamu lazima wafahamishwe kwa nini East African Muslim Welfare Society iwe na katiba isiyoendana na mwelekeo wa nchi. Hatujui nafasi ya Aga Khan katika nchi yetu na ndiyo maana tunamkataa”.*<sup>53</sup>

Lakini cha kushangaza zaidi ilikuwa ule ukimya wa Serikali kuhusu matakwa ya kundi la Adam Nasibu lililokuwa likidai kuwa Waislamu wachanganye dini na siasa katika suala hili, wakati ilikuwa ikijulikana wazi kuwa kufanya hivyo ni mwiko mkubwa katika siasa za Tanzania.

Haya yote mbali, lile la kushangaza hasa na kitu ambacho kilikuwa kigeni katika Tanzania ilikuwa yale madai ya kuingiza ubaguzi wa rangi katika siasa za Tanzania. Ilikuwa inastaajibisha kuona magazeti ya TANU yaliyokuwa na sifa ya kuheshimu haki za binadamu yakichapisha na kuzipa uzito wa hali ya juu habari za kundi dogo la Waislamu waliokuwa wanawalaumu Waislamu wenzao wa Kiismailia kwa kutozaliwa weusi. Miaka kumi iliyopita watu wa Tanganyika,



Waislamu wenyewe waliokuwa ndiyo walioanzisha na kuijenga TANU, walipambana vikali dhidi ya siasa za kibaguzi za Zuberi Mtemvu na chama chake cha *African National Congress*. Mtemvu alishindwa na matokeo yake ikawa Tanganyika kuwa na Serikali ya watu wote isiyobagua rangi na ikitawala raia wa rangi zote kwa misingi ya haki. Kwa ajili hii nchi ikawa haina msugvano kwa ajili ya ubaguzi wa rangi.

Haya matokeo mapya yalikuwa hayaendani na misingi ya TANU. Ilipofikia hali hii, Rais wa EAMWS, Tewa Said Tewa na makamo wake Bibi Titi Mohamed, waliamua kulipeleka suala hili kwa Julius Nyerere, Rais wa Tanzania na mwenyekiti wa TANU, chama tawala. Watu hawa walikuwa wakichekeana jino pembe. Lakini ili tuelewe chanzo cha uadui huu inatulazimu turudi nyuma hadi mwaka 1963, katika siku za mwanzo za uhuru, katika mkutano wa Halmashauri Kuu ya TANU uliofanyika Ukumbi wa Karimjee. Kama ilivyokwishaelezwa hapo mwanzoni kuwa mwaka 1963 ulikuwa mwaka wa mambo mazito. Ulikuwa ndiyo mwaka ambao Kanisa Katoliki liliteua wagombea wake wapambane na wagombea wa TANU waliokuwa Waislamu katika uchaguzi wa Serikali za mitaa kule Kigoma na Bukoba. Ulikuwa ndiyo mwaka ambao Rais wa TANU, Nyerere alipogombana na EAMWS kupitia Bilali Rehani Waikela. Mwaka, 1963 ndio ulikuwa mwaka ambao Halmashauri Kuu ya TANU ilivunja Baraza la Wazee wa TANU lililokuwa limetawaliwa na Waislamu kwa madai kuwa baraza hilo lilikuwa 'likichanganya dini na siasa'. Mwaka 1963 ulikuwa mwaka muhimu kwa Halmashauri Kuu ya TANU kwa sababu ulikuwa mwaka ambao ilifanya maamuzi nyeti ya kidini. Mwaka ule Bibi Titi na Nyerere walishambuliana kwa maneno ndani ya Halmashauri Kuu ya TANU kuhusu jambo jingine tena la dini lililokuwa likihusu EAMWS.

Wanakamati wawili wa Halmashauri Kuu ya TANU, Selemani Kitundu na Rajab Diwani, waliomba Halmashauri Kuu ya TANU imjadili Aga Khan na nafasi yake kama patroni wa EAMWS. Kitundu na Diwani walidai kuwa wana habari Aga Khan anataka kuitawala Tanganyika kupitia Waislamu na EAMWS. Kwa ajili hii basi wakapendekeza EAMWS ifungiwe. Nyerere aliwaunga mkono Selemani Kitundu na Rajab Diwani. Bibi Titi akasimama kishujaa dhidi ya Diwani, Kitundu na Nyerere, akasema hakuna kati yao aliyekuwa na haki ya kuifungia jumuiya yoyote ya Waislamu. Kama walikuwepo watu ndani ya EAMWS ambao walikuwa wanakwenda kinyume na sheria basi watu hao wapelekwe mahakamani na sheria ichukue mkondo wake. Bibi Titi akaendelea kusema kuwa EAMWS imekuwepo kabla ya TANU na siku zote imekuwa ikitoa huduma kwa Uislamu. Inasemekana hasira zilipanda na kukawa na kutoleana maneno kati ya Bibi Titi na Nyerere. Bibi Titi akamwambia Nyerere yeye hamuogopi yeyote ila Allah.

Tuhuma zile dhidi ya Aga Khan na EAMWS hazikuweza kuthibitishwa na Halmashauri Kuu ya TANU ikaliacha jambo lile kwa wakati ule. Lakini Nyerere

alikuwa amefedheheka. Kuanzia hapo akajenga chuki dhidi ya Bibi Titi na kumweka Rajab Diwani na Selemani Kitundu karibu yake. Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1965 Bibi Titi na Tewa wakapoteza viti vyao kwa watu ambao walikuwa hata hawafahamiki – A.M. Mtanga na Ramadhani Dollah. Iliaminika kuwa Nyerere alikuwa anahusika na kuanguka kwa Bibi Titi na Tewa. Kuanzia hapo mambo yakawa dhahiri. Nyerere alikuwa amewatangazia vita wote wawili, Bibi Titi na Tewa. Nyerere alikuwa sasa ana imani kuwa wale maadui zake wawili walikuwa wamekwisha kisiasa. Lakini kilichokuwa kikimuudhi Nyerere zaidi ilikuwa taarifa ambazo alikuwa akizipata kuwa Tewa alikuwa akipewa mapokezi makubwa sana na Waislamu katika ziara zake huko mikoani kama Rais wa EAMWS.<sup>54</sup> Sasa mwaka wa 1968, Bibi Titi na Tewa walipokwenda kumuona Nyerere kuhusu jambo lililokuwa likiwahusu Waislamu, Nyerere alikuwa amejitayarisha vyema.

Viongozi hawa wawili wa Waislamu walimueleza Mwalimu masikitiko yao jinsi radio ya Serikali na magazeti ya TANU yalivyokuwa yakiandika habari kuhusu matatizo yale ya Waislamu. Walidai kuwa TANU ilikuwa ikichanganya dini na siasa. Waliokuwa wakimtahadharisha kuhusu jambo hilo hawakuwa wengine ila marafiki zake wa zamani na wa kutumainiwa, Tewa na Bibi Titi. Marafiki wa kutumainiwa kwa sababu Titi ndiye aliyemuunga mkono Nyerere katika siku za mwanzo za TANU, pale Suleiman Takadir, mmoja wa wazee wa TANU, aliposema kuwa TANU ilikuwa na Ukristo kama Mwalimu na Rupia, Rais na makamo wake walivyokuwa Wakristo. Yeye mwenyewe aliupa uzalendo nafasi ya mbele na Uislamu uwakawa unafuatia nyuma. Nyerere alijibu kwa mkato. ‘Mmeamua kunipiga vita, jiandaeni.’<sup>55</sup>

Mwalimu Nyerere alikuwa anawaambia Tewa Said Tewa na Bibi Titi Mohamed uso kwa uso wajiandae kwa kile kilichokuwa dhahiri: vita ya msalaba dhidi ya umoja wa Waislamu. Sheikh Suleiman Takadir aliyaona haya na aliomba TANU toka mwaka wa 1958 pawepo na uhakika kuwa Wakristo ambao walikuwa wanapanda juu ya migongo ya Waislamu na kuchukua uongozi hawatakuja kuwafanyia uadui Waislamu pale Waislamu watakapokuwa sasa wanataka kugawana madaraka ya kuongoza nchi sawa na Wakristo baada ya uhuru. Tewa Said Tewa, muasisi wa TANU, waziri katika Serikali ya kwanza ya uhuru, Balozi katika Jamuhuri ya watu wa China na Rais wa Baraza la Tanzania la EAMWS, pamoja na Bibi Titi, mwanamke aliyewakusanya wanawake wote nyuma ya Mwalimu Nyerere na TANU, walikuwa wakisemwa na Nyerere kama vile watoto wadogo wa shule waliokuwa watukutu kwa sababu tu, walikuja kumfahamisha Rais kuhusu kukiukwa kwa maadili ambayo ilihitaji yeye ashughulikie mara moja na kutoa uamuzi.

Ulipofika mwezi Oktoba, ‘mgogoro’ ukachukua mwelekeo mpya pale Makamo wa Rais wa Tanzania, Abeid Amani Karume, alipoishambulia EAMWS kuwa ni chombo cha unyonyaji.<sup>56</sup> Kutokea hapo Karume akawa anafanya

mashambulizi na kutoa shutuma kwa EAMWS, wakati mwingine akijaribu kufafanisha uhusiano wa EAMWS na Waislamu katika mtazamo wa Ki-Marxist, akidai kuwa jumuiya ile ilikuwa '*chombo cha makabaila wakubwa na kilikuwa chini yao kikiwanyonya watu wa chini*'. Mgogoro ulipozidi kukua mashambulizi yakahama sasa kutoka EAMWS na kuhamia kwenye mafunzo ya msingi katika Qur'an Tukufu. Katika mkutano wa hadhara Zanzibar, Karume alitoa changamoto kwa Muislamu yeyote ajitokeze bila ya woga kupinga kauli zake mbili kuwa 'Hakuna tofauti kati ya Uislamu na Ukristo', na 'Kufunga siyo lazima'.

Lakini juu ya mashambulizi dhidi ya uongozi wa Waislamu kutoka Serikalini, Nyerere alikuwa hana uwezo wa kumgusa Mufti Sheikh Hassan bin Amir licha ya kuwa alishaonesha kukosana na Serikali mara tu baada ya uhuru pale Kanisa Katoliki lilipotoa vitu vya kukumbuka uhuru vilivyokuwa vimenakshiwa picha za Kikristo. Sheikh Hassan bin Amir alikereka na hili na hasa pale George Kahama, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, alipokwenda Italia kuweka uhusiano baina ya Tanganyika na Vatikano. Kuanzia hapo, Sheikh Hassan bin Amir, kupitia *Daawat Islamiyya* na kwa kupitia wanafunzi wake waliokuwa wameenea nchi nzima alianza kuandika khutba za Ijumaa na kuzisambaza katika misikiti ya nchi nzima na khutba hizo zikawa zinasomwa katika swala ya Ijumaa. Ujumbe wake kwa Waislamu ulikuwa Waislamu watumie fursa iliyoletwa na uhuru kwa kujelimisha ili wagawane madaraka sawa na Wakristo katika kuiendesha nchi. Sheikh Hassan bin Amir akaanzisha mfuko wa elimu ambao Waislamu walitakiwa kuchanga fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule. Kwa ajili ya kuingia kwake kati pale Nyerere alipotaka kuivunja EAMWS, Sheikh Hassan bin Amir akaonekana ni kikwazo kwa Ukristo kuukalia juu Uislam.<sup>57</sup>

Sheikh Hassan bin Amir alikuwa na nguvu sana kiasi cha kwamba si Nyerere au yeyote yule aliyeweza kumgusa kwa wakati ule. Sheikh Hassan alikuwa kwenye siasa kabla ya vijana waliokuwa katika TANU na nafasi yake katika umma wa Kiislamu na uzalendo wake ulikuwa hauna shaka. Sheikh Hassan bin Amir aliingizwa TAA kwa mara ya kwanza mwaka 1950 na Abdulwahid Sykes akiwa mwanakamati katika Kamati ndogo ya siasa ya TAA. Kwa ajili hii basi, akawa mmoja wa wale waliotia sahihi ile memorandum iliyotayarishwa na TAA kwenda kwa Gavana wa Tanganyika, Edward Twining, kuhusu mabadiliko ya katiba ya Tanganyika. TANU ilipoasisiwa, Sheikh Hassan bin Amir alikuwa akiwakatia watu kadi za TANU msikitini huku akidarsisha. Baadhi ya wanachama shupavu wa TANU ambao Sheikh Hassan bin Amir aliwaingiza katika TANU ni Sheikh Mussa Rehani ambaye alipewa kadi yake ndani ya msikiti Kigoma. Wakati Nyerere alipokuja Dar es Salaam mwaka 1953, alimkuta Sheikh Hassan bin Amir mwenyeji katika siasa. Baada ya uhuru Sheikh Hassan bin Amir alijiuzulu siasa, kutokana na kauli yake alisema kuwa, ili awatumikie Waislamu vyema.

Nyerere alifahamu fika kuwa haitakuwa rahisi kwake kumweka Sheikh

Hassan bin Amir kizuizini kama alivyofanya kwa Waislamu wengine. Sheikh Hassan bin Amir alikuwa ndiye Mufti wa Tanganyika na Zanzibar na kwa ajili hii alikuwa na hadhi kubwa katika umma wa Waislamu. Halikadhalika haikuwa rahisi kwa yoyote kumkiuka Sheikh Hassan bin Amir na kuchukua uongozi wa Waislamu.

## **Kuasisiwa BAKWATA, 1968**

Hadi kufikia juma la kwanza la mwezi wa Desemba, mikoja mitatu kati ya kumi na saba ilikuwa tayari imeshajitenga kutoka EAMWS. Kile kikundi cha Adam Nasibu kikaunda kamati kwa ushirikiano na Kamati ya Maulidi ya Dar es Salaam Adam Nasib akiwa katibu na Sheikh Abdallah Chaurembo mwenyekiti. Kamati hii ikaitisha mkutano Ukumbi wa Arnatouglo tarehe 3 Desemba, 1968 kujadili 'mgogoro'. Aliyetumiwa kutoa tangazo lile alikuwa katibu wa Kamati ya Maulidi na Swala ya Iddi, Y. Osman. Kundi la Adam Nasib lilikuwa na mchanganyiko wa watu waliokuwa wanaungwa mkono na Serikali, Adam Nasib akiwa kiongozi Halikadhalika kulikuwa na Waislamu waliokuwa na nafasi katika TANU kama Sheikh Abdallah Chaurembo na Juma Sued kiongozi wa TANU kutoka Bukoba. Ilikuwa wazi kuwa Serikali ilikuwa inamtayarisha Sheikh Abdallah Chaurembo kuchukua nafasi ya mwalimu wake na mtu aliyemfikisha pale alipo, Sheikh Hassan bin Amir. Ikawa sasa lazima Sheikh Hassan bin Amir aondolewe na kupelekwa Zanzibar ili lile kundi la Serikali chini ya Adam Nasibu liweze kuchukua uongozi wa Waislam bila ya kipingamizi chochote.

Wakati vurugu hizi zinaendelea, Kamati Kuu ya TANU ilikuwa ikifanya kikao chake Tanga. Adam Nasibu, Omari Muhaji, Sheikh Abdallah Chaurembo na Saleh Masasi walipanda ndege hadi Tanga kwenda kushauriana na Kamati Kuu ya TANU jinsi ya kumaliza 'mgogoro' wa Waislamu. Ujumbe huu ulikwenda Tanga kuonana na Nyerere huku ukiwa na orodha ya Waislamu ambao kile kikundi cha Adam Nasibu kilitaka Serikali iwakamate na kuwatia kizuizini ili msuguano upate kumalizika. Dossa Aziz aliona Nyerere akipewa karatasi wakati kikao kikiendelea lakini hakufahamu ujumbe uliokuwamo ndani ya karatasi ile hadi hapo baadae. Alikuwa kutambua habari za karatasi ile baada ya majuma mawili kupita wakati alipofuatwa na jamaa yake mmoja na kumuomba aingilie kati ili rafiki yake aliyetiwa kizuizini na Nyerere aachiwe kutoka Jela ya Ukonga. Nyerere alipofahamishwa habari zile na Dossa, alisema kuwa yeye hakufahamu kuwa rafiki yake Dossa alikuwa katika orodha ile ambayo kwa umuhimu wa jambo lile ilibidi aletewe Tanga wakati wa mkutano wa Kamati Kuu. Kwa kejeli Nyerere akamwambia Dossa kuwa yeye huwa hachukuwi tabu ya kusoma majina ya watu anaowaweka kizuizini kwa kuwa anawaamini wale wanaofanya kazi ya kumletea majina yale.

Inspekta Jenerali wa Polisi, Hamza Aziz, mdogo wake Dossa alipopokea amri kutoka kwa Rais kupitia Waziri wa Mambo ya Ndani kuwa amkamate

Sheikh Hassan bin Amir, hakuweza kuamini masikio yake. Alitaka afahamishwe sababu za kutaka kukamatwa Mufti, kiongozi wa juu kabisa katika safu ya uongozi wa Waislamu katika Tanzania. Alipoambiwa kuwa sababu ni kuwa anaihumu Serikali, Hamza Aziz alimwambia Waziri wa Mambo ya Ndani kuwa huenda kuna makosa katika amri ile. Alimfahamisha waziri kuwa yeye binafsi alikuwa anamfahamu mzee yule toka yeye Hamza alipokuwa mtoto mdogo. Akimfahamu Sheikh Hassan bin Amir kama mwalimu na mtu aliyeshiriki katika ukombozi wa Tanganyika. Msimamo wake, heshima na hadhi yake mbele ya Waislamu ipo juu kabisa. Inspekta Jenerali wa Polisi alimwambia waziri kuwa haitawezekana kwake yeye kutii amri ile kwa sababu yeye haamini kuwa tuhuma zile dhidi ya Mufti Sheikh Hassan bin Amir ni za kweli. Nyerere alifahamishwa na Waziri wa Mambo ya Ndani kuwa Inspekta Generali wa Polisi, Hamza Aziz amekataa kutii amri yake ya kumkamata Mufti. Nyerere alitoa amri kwa watu wa Usalama wa Taifa kumkamata Sheikh Hassan bin Amir. Hii ilikuwa ni kinyume na utaratibu kwa kuwa Usalama wa Taifa hawana mamlaka ya kukamata watu.

Usiku wa manane siku hiyo hiyo Sheikh Hassan bin Amir alikamatwa na makachero wa Usalama wa Taifa akapelekwa uwanja wa ndege na kurudishwa Zanzibar.<sup>58</sup> Inaelekea kulikuwa na mpango uliokuwa umetayarishwa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kumpokea Sheikh Hassan bin Amir. Inasemekana mara kadhaa Karume alipata kumueleza Sheikh Hassan bin Amir kuwa Nyerere alikuwa hamtaki nchini kwake na akawa anamshauri arudi nyumbani Zanzibar. Sheikh Hassan alikataa ushauri ule hadi alipokamatwa na kurudishwa kwa nguvu. Karume alimpa Sheikh Hassan bin Amir hadhi zote alizostahili kama ulamaa na akamruhusu kuendesha darasa zake. Lakini Zanzibar ilikuwa imebadilika. Mapinduzi ya mwaka 1964 yalikuwa yameingiza katika Zanzibar fikra potofu zilizokuwa zinapinga Uislamu. Karume mwenyewe alikuwa ametoa amri ya kuchoma vitabu vyote vya Uislamu. Nakala za Qur'an Tukufu zilichomwa moto pamoja na taka za mji. Muslim Academy chuo kilichokuwa kikisomesha masomo ya dini kilifungwa. Mashine za kuchapa kwa lugha ya Kiarabu zikatupwa kutoka Government Press.<sup>59</sup> Maulamaa wengi na wanafunzi wa Sheikh Hassan bin Amir walikuwa wamekimbia Zanzibar kwenda kuishi uhamishoni. Zanzibar haikuwa tena kitovu cha elimu na maarifa ya Uislamu. Sheikh Hassan bin Amir akawa sasa mfungwa katika nchi yake mwenyewe kwa kuwa hakuwa na ruhusa ya kuondoka visiwani hapo na kurejea Tanzania bara. Mara baada ya kukamatwa kwa Sheikh Hassan bin Amir, Adam Nasibu akatangaza kufanyika kwa mkutano ambao ulikuja kujulikana kama Mkutano wa Waislamu wa Taifa. Mkutano ambao ulitangazwa utafanyika Iringa kuanzia tarehe 12-15 Desemba, 1968. Agenda kuu ya mkutano ule ilikuwa kujadili katiba kwa ajili ya jumuiya mpya ya Waislamu.

Baada ya kukamatwa kwa Sheikh Hassan Bin Amir, gazeti moja la Kiingereza lilimfuata Tewa Said Tewa ili afanye mazungumzo nalo. Tewa alimfahamisha mwandishi kuwa kulikuwa na hofu juu ya maendeleo yanayofanywa na

Waislamu na mikutano mikubwa ya Waislamu iliyokuwa ikifanyika nchi nzima. Waislamu waliokuwa na vyeo katika Serikali walikataa kabisa kuisaidia Tume ya Kwikima kwa njia yeyote wakidai kuwa kufanya hivyo ni sawasawa na kuchanganya dini na siasa. Waislamu hawa walikaa pembeni kama watazamaji huku Nyerere kwa taratibu akivunja uongozi wa EAMWS na kutayarisha watu wake kuwaongoza Waislamu. Kundi la Adam Nasibu lilikataa kukutana na Tume ya Kwikima. Maulamaa hawakuweza kufanya lolote kwa kuwa walikuwa wanajua fika kuwa aliyekuwa akivunja EAMWS hakuwa Adam Nasibu, yeye na wenzake walikuwa wakitumiwa tu. Kundi la Adam Nasibu lilikuwa halitaki chochote ila EAMWS ivunjwe na badala yake iundwe jumuiya itakayokuwa chini ya kivuli cha Serikali. Vilevile kukawa na uvumi kuwa Muislamu yeyote atakayejihusisha na shughuli za EAMWS atawekwa kizuizini na Serikali. Tume ya Kwikima haikuweza kupuuza vitisho hivyo kwa sababu Serikali ilishawahi kuwaweka vizuizini Masheikh.

Tume ya Kwikima ilikuwa ikilifamu lile kundi la Adam Nasibu kuwa halikuwa na nguvu wala uwezo wa kuivunja EAMWS. Kufuatia kutangazwa kwa mkutano wa Iringa wa kundi la Adam Nasibu, Tume ya Kwikima ilitoa taarifa yake tarehe 11 Desemba—siku moja kabla ya mkutano wa Iringa kuanza.<sup>60</sup> Taarifa ambayo ilitolewa kwa Waislamu wote, iliitisha mkutano mkuu wa EAMWS ambao ulikuwa ufanyike mwezi Februari mwaka unaofuata kujadili na kutoa uamuzi wa mwisho kuhusu ‘mgogoro’.<sup>61</sup> Tarehe ya mkutano ilibadilishwa hapo baadae na kuwa Januari kutokana na umuhimu wa ‘mgogoro’ uliokuwa ukikabili EAMWS. Mhariri wa Gazeti la TANU baada ya kusoma taarifa ya Kwikima aliamua kutoa maoni yake kuhusu taarifa ile kwa kusema kuwa haikuwa sawa.<sup>62</sup> Huu ulikuwa mpango uliosukwa mapema kuonyesha kuwa uongozi wa EAMWS ulikuwa na ubadhirifu. Juma lile lile Aga Khan ambae ndiye aliyekuwa akishambuliwa na kundi la Adam Nasibu, baada ya kutambua kuwa EAMWS isingeweza kamwe kuokolewa, akiwa Paris, Ufaransa alijiuzulu nafasi yake kama mlezi (patron) wa EAMWS.<sup>63</sup>

Wakati Tume ya Waislamu inasubiri mawazo ya Waislamu sasa kundi la Adam Nasibu wakijionesha wazi kuwa Serikali na TANU ilikuwa nyuma yao, lilikutana kwa ajili ya kile walichokiita Mkutano wa Waislamu wa Taifa ulioanza tarehe 13 Desemba, 1968. Serikali ikifanya kazi nyuma ya pazia ilijitahidi sana kuhakikisha kuwa mkutano ule unafanikiwa. Serikali ikitumia idara ya usalama ndiyo iliyotoa fedha za kufanyia mkutano ule, ikatoa vyombo vyake vya habari kwa ajili ya kuutangaza vizuri na ukatoa ulinzi kwa wajumbe wote. Operesheni hiyo iliendeshwa na Rashid Kayugwa, Afisa wa Usalama Taifa, Dar es Salaam ambaye alipewa kazi ya kudumisha mawasiliano kati ya kundi la Adam Nasibu na Serikali. Kayugwa ndiye aliyekuwa akielekeza kundi la Adam Nasibu mbinu za propaganda na nini kifanyike na kwa wakati gani ili kuvunja umoja wa Waislamu. Kayugwa alikuwa amepata mafunzo yake ya ukachero

Israel, Checkoslovakia na Marekani. Katika kuhakikisha mafanikio ya mkutano wa Iringa, Kayugwa ambae ni mzaliwa wa Iringa alipendekeza mkutano wa Waislamu wa Taifa ufanyike Iringa kwa kuhofu vurugu na upinzani kutoka kwa Waislamu wa Dar es Salaam.

Bwana Rashid Kayugwa baada ya kusoma kitabu cha Padri John Sivalon kilichoeleza kuwa Kanisa baada ya uhuru liliendesha hujuma dhidi ya Uislamu na Waislamu kwa kupitia Serikali, ndipo ilipomdhihirikia ukweli; kuwa alipokuwa akitumiwa kuhujumu EAMWS hakuwa akitumikia Serikali kama alivyokuwa anadhani bali alikuwa akilitumikia Kanisa. Kama kuomba maghufira kwa Mwenyezi Mungu, aliamua kueleza mchango wake katika kuwahujumu Waislamu na Uislamu ili iwe fundisho na onyo kwa Waislamu watakaokuwa katika utumishi wa vyombo kama hivyo siku za usoni. Kabla ya kufa kwake alieleza masikitiko yake kwa kukandamizwa kwa Waislamu na akatoa mfono wake mwenyewe wa kutopandishwa cheo katika Usalama wa Taifa kwa sababu tu yeye alikuwa Muislamu. Wajumbe waliohudhuria mkutano wa Iringa walikuwa kama mia mbili. Mkutano huu ulihudhuriwa na Waislamu waliokuwa na vyeo katika Serikali na TANU, Waislamu waliokuwa wakuu wa wilaya na mikoa na Waislamu wenyeviti wa TANU. Waislamu wote wenye majina walialikwa, pamoja na Waislamu waliokuwa katika halmashauri kuu ya TANU na baadhi ya wajumbe wa mkutano walitoka Zanzibar. Ulikuwa mkutano wa wanasiasa Waislamu ambao ukitoa majina yao walikuwa hawana chochote katika Uislamu. Lakini uzito wa mkutano huu ulitokana hasa na kuwa ulikuwa mkutano ambao ulitawaliwa na Waislamu waliokuwa hawapendezi mbele ya macho ya umma wa Kiislamu. Ni ukweli usioweza kupingika kuwa kama mkutano ule ungelikuwa hasa umetayarishwa kwa ajili ya kumtumikia Allah(s.w) ni wazi ungehudhuriwa na Waislamu wa kweli na wenye historia ya unyenyekevu na mapenzi kwa dini yao. Waislamu wa sifa hizi hawakuwepo katika mkutano ule ukimtoa Sheikh Mohamed Ramia wa Bagamoyo na wengine wachache ambao kwa kutotambua mambo waliitika mwito. Mkutano ulifunguliwa na Makamu wa kwanza wa Rais Abed Aman Karume na kufungwa na Makamu wa pili wa Rais Rashid Mfaume Kawawa. Katika hotuba yake ya ufunguzi Karume alisema maneno haya:

*“Dini haiwezi kuwa nje ya siasa kwa sababu siasa ndiyo damu inayoipa jamii uhai wake. Wakati wa ukoloni wananchi na dini zao zilikuwa chini ya utawala wa wageni. Hivi sasa watu wamevua mabaki ya ukoloni pamoja na kutawaliwa kwa misingi ya dini. Kuanzia sasa uongozi wa dini lazima uwe chini ya wananchi wenyewe bila ya kuongozwa na kiongozi kutoka nje”.*<sup>64</sup>

Mkutano wa Iringa ulipitisha katiba ya jumuiya mpya ya Waislamu, katiba ambayo ilikuwa sawasawa na katiba ya TANU. Hivi ndivyo Baraza Kuu la Waislamu Tanzania, BAKWATA, lilivyoundwa. BAKWATA ikamchagua Saleh Masasi, Muislamu tajiri na ambae alikuwa kama mwenyekiti wa mkutano ule kuwa Mwenyekiti wa Taifa na Adam Nasibu akawa Katibu Msaidizi. Nafasi zote

za juu katika BAKWATA kama ilivyotegemewa zilichukuliwa na kundi la Adam Nasibu, kundi ambalo toka mwanzo lilikuwa likidai kuvunjwa kwa EAMWS. Uongozi wa BAKWATA uliomba Serikali itambue jumuiya hiyo mara moja na ipige marufuku EAMWS kama jumuiya isiyo halali na mali zake zizuiwe. BAKWATA ilitoa maazimio kadha lakini azimio namba nne ndilo hasa linafaa kuelezwa. Azimio hilo liliomba Serikali, TANU na ASP kuwatazama na kufanya uchunguzi wa kina kwa viongozi wote wa EAMWS, hasa Rais, Makamo wa Rais, Katibu wao na baadhi ya viongozi wa mikoa na wilaya ambao wana chuki na hii jumuiya mpya.<sup>65</sup> Uongozi wa BAKWATA katika ushindi wao hawakutaka salama na maelewano na Waislamu wenzao katika EAMWS wala kuwaonea huruma kama Uislamu unavyofundisha, bali ulitaka chama na Serikali ya kitwaghuti viwaandame, hasa wale waliokuwa viongozi.

Baada ya kuundwa BAKWATA, ili kuondoa wasiwasi na kuwarudishia imani Waislamu, Katibu wa Tume ya Waislamu, Mussa Kwikima alitoa taarifa iliyosema:

*“Hakuna anaeweza kutishia kuwepo kwa EAMWS isipokuwa wanachama wake, sheria na Serikali, lakini si watu binafsi hata ikiwa mikoa yote kumi na saba ikijitoe haitamaanisha kuwa jumuiya imekufa kwa kuwa kuwepo kwake hakutokani na kuwepo kwa mikoa hiyo kama wanachama isipokuwa kuwepo kwa wanachama wake, Waislamu”.*<sup>66</sup>

Wakati ilipotoka taarifa hii BAKWATA ilikuwa bado haijaandikishwa rasmi na Msajili wa Vyama. Kisheria ilikuwa haiwezekani kwa kundi la Adam Nasibu kuunda jumuiya mpya iliyokuwa na malengo sawa na jumuiya ambayo tayari ishaandikishwa. Kwa muda wa siku tatu BAKWATA na EAMWS zikawepo kwa wakati mmoja. Ilionekana kama kwamba EAMWS itashinda vitimbi vya Serikali na vya kundi la Adam Nasibu.

Tarehe 19 Desemba, 1968 Serikali kama vile imegutushwa na taarifa ya Kwikima, iliipa BAKWATA Certificate of Exemption na kuifungia EAMWS.<sup>67</sup> Waziri wa Mambo ya Ndani Said Ali Maswanya kwa niaba ya Serikali alitoa taarifa fupi:

*“Waziri wa Mambo ya Ndani kwa kuamriwa na Rais anatangaza kuwa tawi la Tanzania la East African Muslim Welfare Society na Baraza la Tanzania la East African Muslim Welfare Society ni jumuiya zisizotambulika kisheria chini ya kifungu 6 (i) cha Sheria ya Vyama”.*<sup>68</sup>

Kwa tangazo hilo la Rais wa Tanzania, Julius Nyerere, Waislamu walinyimwa nafasi ya kukutana na kuzungumza kuhusu tatizo ambalo kwa kweli liliwahusu Waislamu peke yao. Kwa ajili hii basi Waislamu walinyimwa nafasi ya kujadili na kulitolea uamuzi tatizo hilo.



Viongozi wa EAMWS waliitwa mbele ya Kabidhi Wasii ambaye ndiye alikuwa amekabidhiwa na Serikali jukumu la kusimamia shughuli za kufunga rasmi shughuli za EAMWS. Viongozi walifahamishwa kuwa chini ya sheria ya vyama, mali zote za EAMWS zitauzwa na madeni yatalipwa kutokana na fedha hizo na fedha zitakazobaki watapewa wanachama. Serikali ilikuwa haiwezi kufanya kama sheria ilivyokuwa imeelekeza. Ilikuwa jambo zito sana kwa Serikali ya Nyerere kuonekana inasimamia kuuzwa kwa mali za Waislamu. Viongozi wa EAMWS walipoitwa kwa Kabidhi Wasii mara ya pili walifahamishwa kuwa Serikali imebadilisha mawazo yake kutekeleza amri kama sheria inavyosema kwa ajili hiyo basi imefanya mabadiliko ya sheria ya vyama ambayo inaiwezesha sasa kutoa mali ya EAMWS na kuikabidhi BAKWATA. Hivi ndivyo mali za EAMWS zilivyochukuliwa na kupewa BAKWATA bila ya ridhaa ya Waislamu wenyewe. Hivi ndivyo shule zote zilizojengwa na EAMWS pamoja na mradi wa Chuo Kikuu cha Kiislamu, iliopoangukia katika mikono ya kundi la Adam Nasibu.

BAKWATA haikuwa na uwezo wa kuendesha mipango yoyote na taratibu za shule na miradi yote ya elimu ikafifia na mwishowe kufa kabisa. Hivi ndivyo halikadhalika moto wa Waislamu uliowashwa kwa kupatikana kwa uhuru walioupigania ulivyozimika. Huu ukawa ndio mwisho wa kile kilichokuwa kikijulikana kama “mgogoro” wa Waislamu. Mgogoro ambao ulianza pale Bwana Adamu Nasibu alipofanya maandamano katika mitaa ya Bukoba akimuunga mkono Julius Nyerere na Azimio lake la Arusha na ukaishia kwa mwalimu huyu akiwa na nafasi ya juu katika jumuiya ya Kiislamu ambayo ilikuwa ikichukiza machoni mwa Waislamu. Adamu Nasibu alianza kazi yake kwa kuwashutumu Waislamu. Katika mkutano na waandishi wa habari, Adam Nasibu aliomba TANU na ASP kujikinga na watu wanaohujumu umoja wa nchi kupitia dini. Akaendelea na kusema kuwa BAKWATA ni sawa na Baraza la Kikristo la Tanzania.<sup>69</sup>

Mjumbe mmoja wa Tume ya Waislamu Mussa Kwikima anastahili kueleza habari zake. Mussa Kwikima mwaka 1968 alikuwa ameteuliwa kuwa jaji na Rais Nyerere. Yeye ndiye hasa alikuwa nguvu kuu katika tume ya Waislamu. Wakati alipojitolea kuisaidia tume katika kupambana na kundi la Adam Nasibu, Waikela alimuonya kuhusu hatari ambayo ingemkabili yeye mwenyewe binafsi na kazi yake. Kwikima alijibu kuwa umoja wa Waislamu ni muhimu kuliko maslahi yake binafsi. Ilipoundwa BAKWATA na hapo kuwa ndiyo mwisho wa ‘mgogoro’, Kwikima alihamishwa kutoka Dar es Salaam na kupelekwa Mwanza kama Hakimu Mkazi na Rais Nyerere akamvua madaraka ya ujaji wake.<sup>70</sup>

Kilichobakia baada ya kuvunjika kwa EAMWS ilikuwa ni kujaribu kuiweka BAKWATA katika mikoa kama jumuiya inayowakilisha Waislamu wote wa Tanzania Bara. Mwaka mzima wa 1969 Adam Nasibu na kamati ya watu wanne walitembea katika mikoa wakiahidi msaada wa fedha kwa katibu yeyote wa zamani wa EAMWS ambae atashirikiana na BAKWATA makao makuu

kuisaidia kufungua ofisi katika mkoa wake. Waislamu waliipuuza BAKWATA. Tabora ambayo haikujitoka katika EAMWS, Serikali iliwaruhusu Adam Nasibu na kikundi chake kufanya mkutano wa hadhara. Kabla Adam Nasibu hajahutubia Waislamu, Maulid Kivuruga, mmoja wa wakongwe wa *African Association* na muasisi wa TANU Tabora, alipanda jukwaani kwa niaba ya Waislamu wa Tabora na kuweka sharti kuwa Waislamu wangekuwa tayari kumsikiliza Adam Nasibu endapo Waikela mjumbe wa Tume ya Waislamu iliyokuwa ikitafuta sulhu na yeye angeruhusiwa na Serikali kuwahutubia Waislamu ili aeleze upande wa pili wa kisa kile. Kivuruga alisema kuwa Waislamu wanaomba sharti hili likubaliwe kwa sababu katika Uislamu panapotokea mgogoro basi mpatanishi ni lazima asikilize pande zote mbili. Sharti hili lilikataliwa na BAKWATA na Serikali. Palepale mbele ya waheshimiwa wa Serikali na viongozi wa BAKWATA, Waislamu wakaanza kuzomea huku wakitawanyika wakipiga takbir na wengine wakiitikia “*Allahu Akbar*”.

Siku chache baada ya tukio hili Waikela alitwa na Mkurugenzi wa Upelelezi wa Jinai kusailiwa kwa nini anaipinga BAKWATA. Wakiwa ndani ya chumba cha Tabora Hotel, Geoffrey Sawaya, Mkurugenzi wa C.I.D, alimpiga maswali Waikela na kutaka kujua kwa nini yeye hayuko tayari kushirikiana na Serikali kuipa nguvu na kuieneza BAKWATA. Sawaya akatoa hongo ya shilingi elfu arobaini kwa Waikela ili asaidie kuimarisha BAKWATA. Waikela alikataa kupokea hongo ile. Sawaya akamtisha lakini Waikela hakutishika. Waikela aliwekwa ndani ya chumba kile akiulizwa maswali kwa kiasi cha saa nne na kisha akaamrisha kuweka sahihi yake katika makaratasi fulani. Hili alilifanya. Waikela hakufuatwa tena na Serikali. Ingawa kulikuwepo na juhudi za chinichini za kuipinga BAKWATA, juhudi hizi hazikushinda kwa kuwa BAKWATA iliweza kufungua matawi yake nchi nzima pamoja na Tabora. Wapo baadhi ya viongozi ambao hawakuweza kuhimili vishawishi vya kupokea ile hongo ya Serikali na kwa ajili hii walishirikiana na Serikali hivyo kuwezesha ofisi za BAKWATA kufunguliwa, hata kama zipo pale kwa jina tu. Kuangushwa kwa EAMWS kulisababishwa na watu watatu ambao wao ndiyo walikuwa mstari wa mbele kabisa Adam Nasibu, Sheikh Kassim Juma na Abdallah Chaurembo<sup>71</sup> na njama hii ikaungwa mkono na Rashid Kawawa na Abeid Amani Karume. Mkono wa Julius Nyerere na Kanisa Katoliki katika njama hii haukuonekana kabisa kama ilivyo kawaida katika njama zote za kupiga vita Uislamu na Waislamu Tanzania.

## **Athari ya BAKWATA kwa Waislamu na Uislamu**

Kama ilivyoielezwa EAMWS ilivunjwa 20/12/1968. Siku hiyo Rais wa Jamhuri ya Muugano wa Tanzania, wakati huo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alimwamuru Waziri wa mambo ya Ndani wa wakati huo, Bwana Said Ali Maswanya, kutoa amri ya kulipiga marufuku tawi la Tanzania la EAMWS chini ya kifungu cha 6(1) cha sheria ya kuandikisha vyama.

Kutokana na mazingira ya kuanza kwake BAKWATA imeshindwa kuwa ya manufaa kwa Waislamu katika kipindi chote cha uhai wake. Hii inatokana na sababu kuu zifuatazo:

**Kwanza**, waislamu waliitambua BAKWATA kama ni chombo cha Serikali cha kuwadhhibiti. Hivyo Waislamu walio wengi waliiogopa BAKWATA na viongozi wake na kuichukia pia.

**Pili**, hofu na chuki hiyo ilizidi kupata nguvu kutokana na vitendo vyenyewe vya BAKWATA. Kila Waislamu walipojitutumua kutaka kufanya jambo lolote la maana basi adui yao wa kwanza alikuwa BAKWATA.

**Tatu**, pale ambapo Waislamu wamedhulumiwa haki zao BAKWATA kwa kawaida imekuwa haizipiganii haki za Waislamu. Kwa mfano Waislamu walipodhalilishwa na sungusungu Mwanza 1984 na kutakiwa kuliabudu jua, kuchapwa viboko na kuchanwa kwa Qur'an, Waislamu nchi nzima walikilaani kitendo hicho. Lakini BAKWATA iliyakanusha madai ya watu wa Mwanza. Na katika kuishukuru BAKWATA gazeti la CCM, Uhuru 7/12/1984 liliandika hivi katika maoni yake:

*“Kufuatana na taarifa iliyotolewa na Sheikh Mkuu baada ya uchunguzi huo, ilidhihirika kwamba hakuna vitabu vya Qur'an vilivyochanwa na sungu sungu bali vilikuwepo vitabu vya aina nyingine. Ni vizuri kwamba BAKWATA ilifanya uchunguzi wa jambo hili na kupata uhakika kwa sababu bila ya hivyo, baadhi ya Waislamu wangeweza kuchochewa na maandishi yaliyotawanywa ambayo hayakuwa na ukweli wowote (uk.4)*

Sofia Kawawa alipoikashifu Qur'an wale waliondamana Zanzibar walilaani wa na BAKWATA! Wala BAKWATA haikutoa kauli yoyote ya kuilaani kauli ya Sofia Kawawa.

Serikali ya CCM imekuwa ikiendesha kampeni nyingi za kuangamiza maadili ya Uislamu na jamii kwa ujumla. Kampeni hizo ni kama sera ya idadi ya watu, elimu ya ngono kwa watoto wa skuli, ugawaji wa kondomu kwa watoto wa skuli, na kadhalika. BAKWATA haijatoa kauli yoyote ya kulaani kampeni hizo. Aidha lipo tatizo la ufugaji na ulaji wa maguruwe kiholela bila ya kujali imani na uhuru wa Waislamu. BAKWATA haijathubutu kulikemea jambo hilo bali kinyume chake imekuwa ikishirikiana na maadui wa Uislamu. Mfano ni jinsi BAKWATA ilivyoshirikiana na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani A. Mrema kuwashambulia Waislamu wakati wa sakata ya uvunjaji wa mabucha ya nguruwe 1993. Jambo jingine ni juu ya mihadhara. Wakristo wakiishinikiza Serikali iwapige marufuku Waislamu wasihubiri hadharani kwa kisingizio kuwa wanakashifu dini nyingine, Mufti wa BAKWATA amekuwa akiungana na Maaskofu kutoa kauli mbalimbali za kuwasakama na kuwashitaki Waislamu Serikalini.

BAKWATA imekuwa ikishiriki waziwazi kuzuia na kuvuruga maendeleo ya Uislamu. Mfano ni kuvunjwa kwa shule za Kiislamu za seminari Kinondoni na Jumua mwaka 1982. Mfano mwingine ilivamia shule ya sekondari ya Bondeni Arusha na kuwafukuza waalimu Waislamu na kuweka Wakatoliki.

BAKWATA ilipoundwa ilirithi shule, miradi kadhaa na Taasisi nyingi za EAMWS. Ilichofanya BAKWATA ni ama kuu au kudumaza maendeleo ya miradi ya Uislamu. Aidha, toka imeundwa BAKWATA, haikuwahi kusajiliwa shule ya Kiislamu mpaka Marehemu Prof. Ali Kigoma Malima alipopata fursa ya kuwa Waziri wa Elimu kwa muda mfupi. Ukitaka kuanzisha shule unaambiwa lazima uwe chini ya BAKWATA. Ni Waziri Malima aliyewafunua macho Waislamu kuwa hapakuwa na sheria kama hiyo. Kila Waislamu walipotaka kufanya jambo lolote la maendeleo waliambiwa walete kibali cha BAKWATA. Wakienda BAKWATA haiwapi kibali hicho. Kwa hiyo kwa mahusiano na mawasiliano kati ya BAKWATA na Serikali miradi ya maendeleo ya Waislamu imedumazwa na kukwamishwa kwa kiwango cha kutisha.

BAKWATA imejishughulisha sana na kusimamia usalama wa nchi, ilhali Serikali inavyo vyombo vyake.

Kutokana na udhaifu huu Waislamu wengi wamejitenga na baraza hilo pandikizi(BAKWATA) na badala yake kumechipuka jumuiya nyingi sana za Kiislamu zilizosajiliwa Serikalini na ambazo hazijasajiliwa. Katika kipindi cha uongozi wa awamu ya pili, baada ya kung'atuka Mwalimu Nyerere.

## **Kuibuka kwa Vikundi Mbalimbali Badala ya BAKWATA**

Kwa kipindi cha zaidi ya miaka kumi toka iundwe BAKWATA 15 Desemba, 1968 hakukuibuka kikundi chochote cha Kiislamu kufanya kazi za Da'awah. Serikali ilifunga milango ya kusajili jumuiya za Kiislamu na kuipa BAKWATA ukiritimba wa kuwa chombo pekee kinachotambulika kuyashughulikia masuala ya Kiislamu.

Lakini BAKWATA kwa upande wake nayo ikawa haifanyi lolote la kuwaletea maendeleo Waislamu. Na kila aliyethubutu kuikosoa BAKWATA na pengine kutaka kufanya jambo lolote la Kiislamu bila ya kibali cha BAKWATA alifanyiwa fitna Serikalini.

Kuelekea mwisho wa miaka ya 1980 kulianza kuibuka jumuiya za Kiislamu ambazo zilifanya kazi bila kujali kuwa zina kibali cha BAKWATA au kusajiliwa na Serikali. Jumuiya hizo zilielekeza nguvu zake katika kuwaelimisha Waislamu na wakati huo huo kuishambulia BAKWATA kila inapoonekana kuuhujumu Uislamu.

Jumuiya ambazo zilivuma sana ni Umoja wa Wanafunzi wa Kiislamu wa chuo Kikuu cha Dar es Salaam (MSAUD) na Warsha ya Waandishi wa Kiislamu (Warsha).

MSAUD japo ilikuwa ni jumuiya ya wanafunzi lakini ilifanya kazi kubwa ya kuwaelimisha na kuwaamsha Waislamu kupitia majarida; makala mbali mbali na kuandaa semina. Jumuiya ilikuwa macho kufuatilia matukio mbali mbali ya kisiasa na yale ya kijamii yanayougusa Uislamu. Aidha walikuwa wakifuatilia kauli mbali mbali za viongozi wa BAKWATA na kuzitolea maelezo pale wanapoonaa wamekwenda kombo.

Kundi la Warsha lilijishughulisha zaidi na uandishi wa vitabu na makala mbali mbali za Kiislamu. Kama ilivyokuwa MSAUD Warsha nao walifuatilia kwa karibu sana shughuli za BAKWATA na kuwakosoa hadharani pale walipokwenda kombo.

Warsha ilikuwa ni kundi la vijana waliokuwa na ujasiri wa pekee. Walikuwa wa mwanzo kumsema na kumkosoa Nyerere na siasa zake hadharani. Waliandika na kusambaza makaratasi na makabrasha yaliyokuwa yakimshutumua Nyerere jinsi alivyokuwa akiwadhalilisha na kuwakandamiza Waislamu. Aidha walionyesha jinsi nchi hii ilivyokuwa ikiongozwa Kikristo.

Zaidi ya hivyo vijana wa Warsha walifanya kazi kubwa kuuzeleza Uislamu kama mfumo sahihi wa maisha uliokamilika; kinyume na ilivyokuwa inafahamika kwa wengi kuwa Uislamu ni kuswali na kufanya lbada nyingine maalumu tu. Walijaribu kuisafisha sumu iliyoenezwa na Mwalimu Nyerere kuwa Dini haichanganywi na siasa au Serikali haina dini. Katika kulifafanua hilo walitoa tafisiri sahihi ya dini ambapo walisema kuwa hata ujamaa wa Nyerere ni dini pia.

Waliandika vitabu juu ya mtizamo wa Uislamu juu ya Elimu, Mtizamo wa Uislamu juu ya Dini; Uchumi katika Uislamu n.k.

Warsha walifanya kazi kubwa kwani walifanikiwa kuingia ndani ya BAKWATA ambapo walileta mafanikio makubwa. Wakisihirikiana na Uongozi wa BAKWATA walizigeuza shule za sekondari za Kinondoni na Jumuiya kuwa za Seminari. Aidha walianzisha gazeti la Muislamu ambalo lilikuwa likitoka kila mwezi.

Pamoja na kazi kubwa iliyokuwa inaonekana ikifanywa na kikundi hicho, hakikuwa na watendaji wengi wenye ujuzi. Utendaji ulikuwa wa hamasa bila ya kujali nguvu zake na zile za mpinzani. Aidha hapakuwa na utaratibu wa kuwafunza, kuwalea na kuwachuja wanachama wake. Watu wakawa wanaingia katika Warsha kiholela jambo ambalo baadaye lilisababisha migogoro ndani ya Warsha na kuathiri sana shughuli zake na hatimaye kuisambaratisha.

## **Sheikh Malik na Warsha**

Haiwezekani ikatajwa *warsha* bila ya kumtaja Sheikh Mohamad Hussein Malik. Sheikh Malik alifika Tanzania katika miaka ya 1970 akiwa Mwalimu wa shule ya Tambaza; kisha Kinondoni Muslimu. Pamoja na kusomesha shule za

Sekondari alikusanya vijana wa Sekondari na Vyuo na kuwasomesha Uislamu katika mtizamo wa kiutekelezaji na usimamishaji Uislamu katika jamii kama mfumo pekee sahihi wa Maisha.

Akiwa mwanafunzi wa Sheikh Abul Ala Mauduud; Sheikh Mohamed Hussein Malik alifundisha Uislamu kwa mtizamo wa Qur-an na Hadith kuwa Uislamu ni utaratibu kamili wa maisha. Aidha kutokana na ufundishaji wake aliwawutia vijana wengi ambao aliwahimiza waandike vitabu na makala mbali mbali juu ya yale anayofundisha.

Sheikh Malik binafsi alisimamia kuanzishwa kwa Warsha ya Waandishi wa Vitabu vya Kiislamu katika Ofisi za BAKWATA Kinondoni. Yeye binafsi aliandika kitabu cha “Islamiati”. Mwaka 1978 Warsha iliamishwa Magomeni na ikawa na malengo na muelekeo tofauti na ule wa awali. Kwanza jina jipya likawa Warsha ya Waandishi wa Kiislamu badala ya Warsha ya Wandishi wa vitabu vya Kiislamu. Kisha ikapewa sura ya kiharakati kuliko kubakia tu kwenye kuandika vitabu. Waanzilishi wa Warsha zote mbili ni wanafunzi wa Sheikh Malik wakiwemo Mtengwa Burhani Mtengwa, Musa Abdul-Rahmaani Mdidi; Mohamed Ramadhan Kassim, Suleiman Swalehe, Ali Kilima, Abubakari Mwarwiro, Mohamed Bakari, Ahmed Mbaraka na wengineo.

Katika ufundishaji wake, Sheikh Malik hakuwa na darasa moja maalum. Bali alikuwa akizunguka Vyuo na Misikitini kwa siku tofauti tofauti katika wiki. Kwa mtindo huu aliwafikia watu wengi. Wanafunzi wake wa kudumu walikuwa wakimfuata kila penye darasa.

Haukupita muda mrefu maneno “*Uislamu mfumo sahihi wa maisha*” Uchumi katika Uislamu, dini na ujamaa, kusimamisha Uislamu n.k. yakaanza kusikika na kuwekwa katika maandishi.

Kufikia hapo maadui wa Uislamu ambao siku zote walikuwa wakifuatilia kwa karibu sana darsa za Sheikh Malik hawakuweza kuvumilia tena. Alipewa wiki moja kuondoka nchini na hakuruhusiwa kubadili fedha zake.

Lakusikitisha ni kuwa waliotumiwa kumjengea fitna Sheikh Malik ni Masheikh. Na hili liliidhihirika pale Sheikh Mohammad Ali alipokwenda kwa aliyekuwa Rais wakati huo Mwalimu Nyerere kulalamika kuwa inakuwaje Sheikh Malik afukuzwe bila ya kosa lolote. Nyerere alijitetea kuwa si yeye bali Masheikh ndio hawamtaki. Akamtajia na Orodha ya Masheikh waliohusika na fitina hiyo.

Sheikh Mohammad Hussein Malik aliamia Nairobi ambapo aliendelea kufundisha Uislamu katika Vyuo Vikuu mbali mbali na kuwa Mlezi wa Vijana wa Kiislamu wa Vyuo hivyo. Sheikh Malik ni Sheikh pekee aliyetoa mchango mkubwa sana katika kufundisha na kupandikiza fikra sahihi za kuusimamisha Uislamu nchini Tanzania.

Mchango wake katika kufundisha na kuwalea wanafunzi katika Mashule na vyuo ni mfano bora wa kuigwa. Siku zote alikuwa akiwahimiza wanafunzi wake kuwa watakuwa wanafanya jambo la maana pale watakapo dumu kufundisha Elimu ya Dini ya Kiislamu katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu vya serikali na vya Binafsi. Sheikh Malik amefariki dunia April, 2009. Tunamuomba Allah Amghufirie na kumrehemu.

Pamoja na kuibuka na kusajiliwa Taasisi na Jumuiya nyingi za kiislamu katika uongozi wa Rais Al-Hajj Hassan Mwinyi, harakati za kiislamu hazikuonekana kuzaa matunda yaliyotegemewa. Maendeleo ya waislamu yalizidi kudumaa na uislamu uliendelea kufutika katika maisha ya watu na jamii kwa ujumla. Dosari kubwa zilizokabili jumuiya hizo ni pamoja na:

- (i) Kukosa malengo yaliyo wazi na mipango ya uteklezaji ya Taasisi na Jumuiya zilizotawaliwa na hamasa na jaziba.
- (ii) Nyingi ya Taasisi na Jumuiya za waislamu zilianzishwa kama vitega uchumi vya watu binafsi.
- (iii) Kukosa nguvu kazi. Hapakuwa na taratibu za kuwafunza, kuwaandaa na kuwalea wanaharakati.
- (iv) Kukosa mtizamo sahihi juu ya Uislamu na namna ya kuusimamisha
- (v) Kukosekana kwa ushirikiano na mshikamano wa Taasisi na Jumuiya za Kiislamu. Baadhi zilihasimiana na kupigana vita.

## **Juhudi za Kuirekebisha BAKWATA, 1979**

Mwaka 1979, kulitokea kutoelewana baina ya Mwenyekiti wa BAKWATA, Al-Haj Salehe Masasi na katibu wake Mkuu, Sheikh Mohamed Ali. Ilionekana Sheikh Mohamed Ali, hakuridhishwa na uendeshaji wa BAKWATA, ikabidi Salehe Masasi atumike kumuondoa kwa kisingizio kuwa haonekani ofisini na mahali pake kumuweka Juma Mrindoko. Kipindi hicho Sheikh Mohamed Ali alikuwa katika tume ya Rais ya kuchunguza nidhamu ya viongozi, ambayo ilimshughulisha sana.

Sheikh Mohamed Ali aliyekuwa Mcha-mungu na sheikh msomi mwenye shahada ya sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam, alikuwa nitumaini la vijana wasomi na wanaharakati wa kiislamu kuwa wakimuunga mkono ataweza kuleta mabadiliko ndani ya BAKWATA. Vijana wa warsha na waislamu wengine wenye uoni mzuri walimuendea Sheikh Mohamed Ali na kumshawishi kuwa asikubali kutoka BAKWATA, bali uitishwe mkutano wa Halimashauri kuu ya BAKAWATA ili uthibitishwe uhalali wa kufukuzwa kwake, kwani kikatiba Masasi hakuwa na mamlaka ya kumfukuza. Sheikh Mohamed Ali alikubali na vijana wa Warsha na waislamu wenye kuhitajia maendeleo ya Dini yao walishiriki kikamilifu kuuitisha

na kuufanikisha mkutano ule wa Halimashauri Kuu ya BAKWATA, uliofanyika katika ukumbi wa Elimu ya Watu Wazaima, mtaa wa Lumumba, Dar es salaam. Mkutano ule uliokuwa halali kwa mujibu wa katiba ya BAKWATA ulipitisha maamuzi yafuatayo:

- (1) Kumfukuza katika uongozi, Salehe Masasi kwa kosa la kukataa kuhudhuria mkutano ule halali.
- (2) Kuteua kamati ya muda, Sheikh Mohamed Ali akiwa mwenyekiti wa k e iliyokuwa na kazi ya kuendesha shughuli za kila siku za BAKWATA makao makuu na kuandaa rasimu ya katiba mpya ya BAKWATA yenye muelekeo wa kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii. Kazi ya kuanda katiba na kupata uongozi mpya wa BAKWATA ilitarajiwa ikamilike katika kipindi cha miaka miwili.

Katika hiki kipindi cha mpito pamoja na kazi ya kuandaa rasimu ya katiba mpya ya BAKWATA lilianzishwa mara moja gazeti la "Muislamu" la kila mwezi lililotoa mchango mkubwa sana katika kuwaelimisha na kuwazindua waislamu. Pia kwa mtindo wa "*phasing out*" Shule za Kinondoni, Dar es salaam na Jumuiya, Tanga, zilizokabidhiwa BAKWATA kutoka EAMWS, zilifanywa seminari na kuanza kidato cha kwanza 1981 baada ya kuidhinishwa na Halimashauri Kuu ya BAKWATA. Lengo la shule hizi lilikuwa kutoa elimu na malezi sahihi kwa vijana wa Kiislamu ili kuwaandaa kuwa viongozi wa kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii kama seminari za wakatoliki zipatazo ishirini na tatu (23) wakati huo, zilivyokuwa na lengo la kuandaa vijana wa kikatoliki watakaochukua nafasi za uongozi wa jamii katika sekta mbalimbali.

Juhudi hizi zilipokelewa kwa furaha na matumaini makubwa na waislamu. Lakini kwa maadui wa uislamu hii ilionekana ni tishio na hatari kwa serikali ya Tanzania iliyo chini ya kanisa Katoliki.

Ndani ya BAKWATA kwenyewe mawakala wa maadui wa Uislamu walianza kuwa na wasiwasi. Walichukulia juhudi hizo za kuleta maendeleo ya Uislamu na Waislamu kuwa ni kulisaliti Baraza la Serikali. Mawakala wa maadui wa Uislamu ndani ya serikali nao wakaindama BAKWATA na kuitaka iwafukuze vijana wa *warsha* walioingia ndani ya BAKWATA na kutaka kuleta maendeleo ya Waislamu.

Mwalimu Nyerere, aliyeahidi kulipa kanisa katoliki upendeleo pekee, alidhihirisha chuki zake binafsi dhidi ya maendeleo haya ya BAKWATA, na hasa kuanzishwa kwa Seminari ya Kionondoni. Katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Dar es salaam, Novemba, 1981, Mwalimu Nyerere alidhihirisha chuki yake hiyo alipo muagiza makamu wa kwanza wa Rais, Al-Hajj Aboud Jumbe na makamu wake wa pili, Rashidi Mfaume Kawawa, kuwa akirudi kutoka safarini aikute Kinondoni imesharudishwa kuwa shule ya kawaida yenye mchanganyiko wa waislamu na wakristo na sio seminari tena. Viongozi hawa



wa serikali walitii agizo la Rais kwa kuwaita viongozi wa BAKWATA ili kuweka mikakati ya utekelezaji wa amri ile. Sheikh Mohamed Ali alikataa kutii amri ile kwa hoja kuwa atawaambia nini waislamu waliopitisha uamuzi ule kwenye Halimshauri kuu, ikizingatiwa kuwa wakati huo wakitoliki walikuwa na Seminari 23 zilizotapakaa kote nchini.

Mwaka 1982 Serikali kupitia kwa mawakala wake ndani ya BAKWATA, iliitisha mkutano wa Halimshauri kuu ya BAKWATA uliofanyika Chuo cha Ardhi, Dar es salaam. Mkutano ulizingirwa na ulinzi mkali na kabla mkutano haujaanza wajumbe wawili, Mtengwa Burhani Mtengwa na Musa Abdul-Rahmani Mmidi, waliokuwa watendaji na wawakilishi wa vijana wanaharakati walitolewa kwenye ukumbi wa mkutano na polisi na kusindikizwa na ulinzi mkali mpaka majumbani mwao. Sheikh Mohamed Ali alishutumiwa kwa kosa la kuwaingiza vijana wanaharakati ndani ya BAKWATA waliokuwa na lengo la kusimamisha Uislamu katika jamii. Kwa kosa hili na makosa mengine mengi aliyobambikiziwa, Sheikh Mohamed Ali aliwajibika kujiuzulu ukatibu Mkuu wa BAKWATA.

Baada ya kujiuzulu Sheikh Mohamed Ali na kufukuzwa watendaji walionekana wakorofi, gazeti la “Muislamu” lilianza kuyumba, likabadilishwa jina likaitwa “Safina” na hatimaye likafa kabisa. Shule mbili pekee za seminari nazo zikauwawa mara moja.

Kutoka kwa Sheikh Mohamed Ali kulimpa fursa Bwana Adam Nasibu kuchukua nafasi ya Katibu Mkuu wa BAKWATA, makamu mwenyekiti akiwa Mustafa Songambe. Adam Nasibu alitembea nchi nzima kuonesha uhatari wa vijana wa “*Warsha* ya Waandishi wa Kiislamu” na makala na vitabu walivyoandika vyenye lengo la kuhuisha na kusimamisha Dola ya kiislamu nchini.

## **Kuanzishwa Seminari ya Masjid Qubah, 1983**

Vijana wa “*Warsha*” waliokuwa watendaji wakuu katika BAKWATA ya Sheikh Mohamed Ali wakishirikiana na wazazi waislamu waliokerwa na kuuliwa kwa seminari ya Kinondoni waliamua kuanzisha seminari nyingine chini ya usimamizi wa kamati teule ya watu wanane akiwemo Musa Abdulrahman Mmidi, Mtengwa Burhan Mtengwa, Mohamed Ramadhani Kassim, Ahmed Mbaraka, Abubakar Marwiro, Waziri Nyelo, Mzee Abdallah Amour, na Mzee Abbas Shaban Kilima.

Kistratija, Shule hii haikutakiwa iwe moja kwa moja chini ya “*Warsha ya waandishi wa Kiislamu*” kwa sababu mbili, kwanza “*Warsha*” ilikuwa ni kikundi cha uhamasishaji kisichokuwa na tasjila ya kisheria. Pili propaganda za uhatari wa “*Warsha*” zilizofanywa na Adam Nasibu ziliwafanya waislamu waogope kujihusisha au kushirikiana na “*Warsha*”.

Mwaka 1983, mwaka uliofuatia baada ya kuvunjwa seminari ya Kinondoni, Dar es salaam na Jumuiya, Tanga, ilianzishwa, Seminari ya Masjid Qubah

katika madarasa ya msikiti wa “*Masjid Al-Amin*” ulipo karibu na uwanja wa Taifa ilipo shule ya Kiislamu ya Temeke hivi leo. Palikuwa na madarasa matatu na ofisi yaliyo kodiwa kwa Sh.2,000 kwa mwezi kwa wakati ule. Mwaka 1984, Shule ilihamia Kijitonyama, ilipo Masjid Qubah ya leo, ikiwa na mikondo minne ya kidato cha kwanza na mikondo miwili ya kidato cha pili.

Wislamu nchi nzima walifarijika na kuhamasika kutoa michango yao ya hali na mali katika kujenga na kuendeleza shule hii pekee ya Sekondari ya Kiislamu iliyoendeshwa kwa lengo la kuandaa nguvu kazi ya kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii.

Nyerere na Serikali yake ya mfumo katoliki, hakuwa radhi kabisa na maendeleo haya ya waislamu. Pamoja na kutekeleza masharti yote ya usajili, Serikali ilikataa kuisajili shule hii kwa sharti kwamba lazima iandikishwe chini ya BAKWATA. Sharti hili lilikataliwa kwa hoja kuwa, iweje seminari ya Masjid Qubah isajiliwe chini ya BAKWATA ambayo iliua seminari za waislamu za Kinondoni na Jumuiya. Pamoja na kutosajiliwa waislamu walimiminika Masjid Qubah kuleta watoto wao wapate elimu na maadili ya kiislamu. Mwaka 1985, Serikali ilifanikiwa kupenyeza watu wake ndani ya “warsha” na kuzusha fitina iliyopelekea kutolewa kundini watendaji wakuu wa kituo na ikawa ndio mwisho wa “Warsha” na Masjid Qubah ile.

## **Kuibuka kwa Seminari Nyingi za Kiislamu**

Alipoingia madarakani Rais wa awamu ya pili, Al-Hajj Ali Hassan Mwinyi, na kumuweka Kigoma Ali Malima kuwa Waziri wake wa Wizara ya Elimu, iligundulika kuwa hapakuwa na sheria yeyote ya Wizara ya Elimu inayowalazimisha waislamu kusajili shule zao za Kiislamu (seminari) chini ya BAKWATA. Kumbe hayo yalikuwa matashi binafsi ya Mwalimu Nyerere, mkatoliki, ili kudhibiti maendeleo ya waislamu. Kinyume chake, Rais Mwinyi mwenyewe alikuwa akiwahimiza waislamu kuanzisha shule zao na ikawa sababu ya kuanzishwa Al-Haramain Islamic College 1986 chini ya BAKWATA.

Miaka miwili iliyofuatia, 1989 zilianzishwa shule za Ununio Boys Islamic High School na Kunduchi Girls Islamic High School chini ya “Munadhamat-Da’awah”. Mwaka 1992, ilianzishwa Ubungo Islamic High School chini ya Islamic Propagation Centre ikifuatiwa na Mudio Islamic Seminary, Kirinjiko Islamic Secondary School na nyingine nyingi zilizoibuka. Mpaka hivi leo, 2016 tuna shule za Kiislamu za Msingi na Sekondari zaidi ya hamsini (50). Shule hizi zinajengwa na kuendeshwa na waislamu wenyewe pamoja na uchumi duni na uhaba wa nguvu kazi waliyo nayo.

## **Kuanzishwa Vyuo vya Ualimu na Chuo Kikuu cha Waislamu**

Sambamba na ujenzi wa Shule za Kiislamu za Msingi na Sekondari pamekuwa na ujenzi wa Vyuo vya Ualimu vya Kiislamu vyenye lengo la kutoa walimu bora katika ngazi ya cheti na stashahada ambao pamoja na kufundisha elimu ya mazingira watafundisha pia Maarifa ya Uislamu na kuwa walezi bora wa vijana wa Kiislamu. “Al-Haramain Islamic Teacher College ndicho chuo cha kwanza kilichoanzishwa kwa msukumo wa Rais Mwinyi, 1987. Chuo kilichofuatia ni “*Ubungo Islamic Teachers’ College*”, 1998 kisha kikafuatia Kirinjiko Islamic Teachers’ College, 2004.

Chuo cha Ubungo na Kirinjiko pamoja na kutoa kozi za Cheti na Stashahada vinaendesha pia kozi za muda mfupi (miezi sita/saba) kwa lengo la kuandaa walimu wa kufundisha somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu katika shule za awali, msingi na sekondari.

Mwaka 2005, Waislamu walianzisha Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro katika majengo waliyopewa na Serikali ya Rais Benjamin Mkapa. Majengo haya yalikuwa ya Chuo cha TANESCO. Chuo hiki kinata rajiwa kutoa masomo katika fani mbalimbali za elimu ya mazingira na elimu ya mwongozo kwa lengo la kutoa wataalamu watakapo kuwa nguvu kazi tarajiwa ya kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii.

Chuo hiki kiko chini ya taasisi ya Muslim Development Foundation(MDF). Iliyozanzishwa na waislamu kwa lengo la kusajili na kusimamia uendeshaji wa chuo hiki.

Ili waislamu waweze kuhuisha Uislamu na kutwaa mikononi mwao Uongozi wa jamii hawana budi kuwa na wataalamu na nguvu kazi ya kutosha itakayoweza kuendesha kwa ufanisi kila sekta ya maisha ya binafsi na jamii. Kwa kujua hili, waislamu wanaharakati kote nchini wanafanya jitihada za kuanzisha na kuendesha vituo vya elimu kwa njia ya mshikamano.

## **Kuanzishwa BARAZA KUU ,1992**

Katika kipindi chote cha uongozi wa Mwalimu Nyerere na hasa baada ya kuvunjwa kwa E.A.M.W.S na jumuiya nyingine za waislamu, haikuruhusiwa kusajiliwa Jumuiya au Taasisi yoyote ya Kiislamu ila sharti ipate kibali cha BAKWATA, na iwe chini ya BAKWATA. Kwahiyo, BAKWATA, iliyofanya kazi ya kuuhujumu Uislamu zaidi kuliko kuuendeleza, ilikuwa ndiyo Jumuiya pekee ya waislamu kwa kipindi cha miaka kumi na sita(16) kuanzia 15 Desemba,1968 ilipoanzishwa BAKWATA hadi 1985 alipong’atuka Mwalimu Nyerere.

Rais Mwinyi alipoingia madarakani mwishoni mwa mwaka 1985, iligundulika kwa waislamu kuwa hapakuwa na sheria yeyote ya nchi iliyoipa BAKWATA ukiritimba bali ilikuwa ni sera binafsi ya Nyerere na kanisa lake. Baada ya waislamu kugundua hili, kwa hamasa na hamu kubwa walianzisha utitiri wa Jumuiya na Taasisi za kiislamu kwa kiasi kwamba hata misikiti ilisajiliwa kama taasisi ili kujitoa kwenye makucha ya BAKWATA.

BAKWATA iliyolewa ukiritimba uliodumu kwa miongo miwili haikuwa radhi kuona ule mfumuko wa Jumuiya na Taasisi za Kiislamu zilizosajiliwa kihalali na Seriali bila ya kibali chake. Katika Baraza la Idil-Haji mwaka 1991 ambalo mgeni rasmi alikuwa mheshimiwa Rais Ali Hassan Mwinyi; Bwana Suleiman Hegga aliyekuwa kaimu Makamu Mwenyekiti wa BAKWATA aliilaumu Serikali kwanini imeruhusu kuwepo kwa vikundi vingi vya Kiislamu. Aidha aliitaka Serikali ividhibiti vikundi hivyo. Wakati Bwana Hegga analilia kubakishwa kwa ukiritimba wa BAKWATA, tayari Serikali ilikwishaingia kwenye sera ya vyama vingi vya siasa.

Mheshimiwa Rais wakati wa kujibu risala hiyo, alikataa suala la kudhibitiwa Taasisi na Jumuiya za Waislamu, kwani mchango wake katika kuleta maendeleo ya waislamu ulikuwa mkubwa kuliko ule wa BAKWATA. Rais aliinasihi BAKWATA ikutanishe vikundi vyote vya waislamu ili tofauti zilizopo zijadiliwe ili hatimaye upatikane umoja na mshikamano wa waislamu unaohitajika na ulioamrisha wa katika Qur-an (3:103).

BAKWATA hawakutekeleza nasaha hizo. Lakini walitokea wanaharakti wa kiislamu waliotumia fursa ile na kuandaa mkutano ambapo walialikwa wawakilishi toka Jumuiya na Taasisi za Kiislamu nchini kote. Aidha viongozi wa BAKWATA toka ngazi za wilaya hadi makao makuu walialikwa. Lengo la mkutano huo lilikuwa kujadili namna ya kuifanya BAKWATA ifanye kazi kwa maslahi ya Uislamu na waislamu wa nchi hii.

Lakini wakati maandalizi ya mkutano huo yanaendelea BAKWATA ilikuwa ikiendesha kampeni kujaribu kuwazuia Waislamu wasihudurie mkutano huo. Hata hivyo, juhudi zao hizo hazikuzaa matunda kwani maelfu ya Waislamu walikutana Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika Ukumbi wa Nkrumah siku ya Jumapili tarehe 15 Sep, 1991.

Mkutano huo ambao ulifunguliwa na Waziri katika Ofisi ya Rais anayeshughulikia ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Abdurahman Kinana pamoja na mambo mengine ulipitisha maazimio yafuatayo:

- (1) Kuwaondoa madarakani Kaimu Makamu Mwenyekiti wa BAKWATA Bwana Suleiman Hegga na Kaimu Katibu Mkuu Bwana Rajab Kundyia.
- (2) Kuteua kamati ya muda ambayo itasimamia shughuli za kila siku za BAKWATA Makao Makuu na kuandaa Rasimu ya marekebisho ya Katiba ya BAKWATA.

Kiutekelezaji azimio la kuwaondoa Bwana Hegga na Kundyia lilikwama. Aidha, kwa vile mabwana hao hawakubali kuachia ofisi, kamati ya muda iliyoundwa kusimamia shughuli za kila siku za Baraza makao Makuu haikuweza kufanya kazi.

Hata hivyo kamati iliendelea kuandaa rasimu ya marekebisho ya katiba ya BAKWATA. Zoezi hilo lilipokamilika uliitishwa mkutano mkuu ambao ulifanyika katika ukumbi wa Diamond Jubilee mjini Dar es Salaam.

Pamoja na kupitishwa kwa rasimu ya katiba Waislamu waliamua kulitwaa BAKWATA kwa nguvu ambapo ofisi za BAKWATA makao makuu, ofisi ya mkoa Dar es Salaam na shule ya Alharamain ilizingirwa na kuzuia watendaji wa ofisi hizo kuingia.

Ofisi hizo zilizingirwa kwa muda wa wiki moja hadi Rais Ali Hassan Mwinyi alipoingilia kati na kuzikutanisha pande mbili, 11, Januari, 1992. Viongozi wa BAKWATA na viongozi wa kamati teule iliyowekwa na mkutano wa 15 Septemba, 1991, walikubaliana mbele ya Rais Mwinyi kuwa zichaguliwe kamati za kusimamia uchaguzi toka ngazi ya chini hadi Taifa ambapo BAKWATA watatoa watu watano na “kamati teule” watu watano. Lengo lilikuwa kwamba endapo uchaguzi utasimamiwa vyema watapatikana viongozi waadilifu wanaokubalika na watakapo simamia maendeleo ya Uislamu na Waislamu. BAKWATA walivunja makubaliano yale kwa madai kuwa, kwa kauli ya aliyekuwa Sheikh Mkuu wa BAKWATA Hemed bin Juma bin Hemed katika Baraza la Idd kule Shinyanga, kuwa Rais Mwinyi ameingilia kati kitu asichokijua asili yake na madhumuni yake. Akaeleza Sheikh Mkuu huyo kuwa BAKWATA iliundwa na Serikali ili kudhibiti na kuzuia uanzishwaji wa vikundi mbalimbali vya Kiislamu vitakavyoweza kufanya harakati za kuleta maendeleo ya Uislamu na Waislamu. Katika Baraza hilo, Sheikh Mkuu alimsikitikia ndugu yake, Sheikh Mohamed Ali, kuwa aliponzwa na vijana wa “Warsha” aliowaingiza ndani ya BAKWATA ambao walikuwa na azma ya kusimamisha Dola ya kiislamu hapa nchini, ikabidi alazimishwe kujiuzulu ukatibu Mkuu wa BAKWATA. Rais Mwinyi baada ya kugundua kuwa BAKWATA ni zimwi la watu alizira na kujitoa katika usimamizi wa suluhu ile.

Kufikia hapo wale waliokuwa katika harakati za kuirekebisha BAKWATA wakaona waiache BAKWATA kama ilivyo na waanzishe Baraza litakalo kuwa mbadala, Baraza Kuu la Jumuiya na Taasisi za Kiislamu, kwa ufupi BARAZA KUU. Baraza Kuu lilisajiliwa rasmi mwaka huo wa 1992. Pamoja na Baraza Kuu, kupata tasjila, bado palikuwa na utata katika mchakato wa usajili wake. Aliyekuwa akifuatilia usajili ni Bwana mmoja aliyenjeingiza katika ile kamati teule na kupora ukatibu katika hali ya kutatanisha na baadaye ikadhihirika kuwa alikuwa Swahiba yake Mwalimu Nyerere mwenye BAKWATA yake iliyotaka kuuliwa au kudhoofishwa. Utata huu ulizidi kudhihiri pale tasjila ya Baraza Kuu ilipoletwa nyumbani kwa aliyekuwa Mwenyekiti wa kamati, Mzee Salumu Khamis na waziri wa mambo ya ndani mwenyewe, mheshimiwa Augustine

Lyatonga Mrema. Halikuwa jambo la kawaida. Baadhi ya waislamu wenye kuona mbali walitilia mashaka tasjila ile na wakathubutu kusema Baraza Kuu lilikufa siku ile lilipopata tasjila yake. Ukweli huu ulidhihiri katika mkutano Mkuu wa kwanza wa Baraza Kuu pale walipozuiliwa kuhudhuria mkutano huo wajumbe halali miongoni mwa waasisi wa Baraza Kuu walioitisha ule mkutano wa 15 Septemba, 1991. Matokeo yake, ule ukawa ni mkutano mkuu wa kwanza na wa mwisho wa Baraza kuu kwa mujibu wa katiba yake.

Waislamu walifarijika sana kwa kusajiliwa Baraza Kuu. Walitegemea kuwa lingeliwaunganisha waislamu na kujenga nguvu ya pamoja itakayopokea kuhuika na kusimama kwa Uislamu katika jamii. Kinyume na matumaini hayo katika siku za mwanzoni. Baraza Kuu lilibakia kushindana na BAKWATA katika kuendesha mabaraza ya Idd na Maulid. Baadaye likabakia na kutoa vyeti ya ndoa na kusuluhisha migogoro baina ya wana ndoa.

Hivyo, mpaka hivi sasa (2016) waislamu hawajawa na umoja wala uongozi unaoheshimika kwa wote (central leadership bali wamebakia kuwa na jumuiya na taasisi nyingi zisizoelewana katika mipango na utekelezaji wake. Wakati mwingine inafikia hatua ya jumuiya na taasisi hizi kuhasimiana, kushutumiana na kupigana vita. Tatizo hili la waislamu kukosa uongozi wa pamoja linaambatana na matatizo mengine yafuatayo:

- (i) Hakuna mipango ya kazi kulingana na mahitajio ya umma wa waislamu.
- (ii) Hakuna utaratibu wa kuwafunza na kuwalea watu kuelekea kwenye kusimamisha Uislamu.
- (iii) Kusema na kulalamika kumekuwa kwingi kuliko kupanga na kutenda.
- (iv) Kutokana na kukosekana kwa mafunzo na uongozi wa pamoja, waislamu wamekuwa wakifanya mambo kwa jazba. Hali hii imekuwa ikiwa sababishia waislamu madhara makubwa ikiwa ni pamoja na kadhia ya “mabucha ya nguruwe, 1993” na mauaji ya mwembe chai, 1998”.
- (v) Kutokana na kukosekana kwa malengo na mipango ya pamoja waislamu wa nchi hii wamekuwa hawapigi hatua yoyote ya maendeleo ya pamoja inayolandana na kasi ya adui.
- (vi) Kwa kukosa malengo na mipango ya pamoja waislamu wamekuwa wakiingizwa kwenye agenda za watu wengine na wakamalizia muda na guvu zao humo. Agenda za “O.I.C” na “Kadhi” zimewashughulisha sana waislamu.

## **Kadhia ya Mabucha ya Nyama ya Nguruwe, 1993**

Katika kuwachokoza na kuwadhalilisha waislamu ilifikia mahali wakristo kuachia huru mifugo yao ya nguruwe kuchafua mazingira ya waislamu hadi kuingia Misikitini Ubungo Darajani na Mabibo karibu na Mabibo Hostel ya Vyuo

Vikuu. Pia wakristo walifikia hatua ya kufungua mabucha ya nyama ya nguruwe sambamba na mabucha ya nyama halali kiasi kwamba mtoto akitumwa nyama hawezi kutofautisha nyama ya nguruwe na ya ngombe au mbuzi. Kwa namna hiyo ilitokea mara kadhaa watoto wa kiislamu kununua nyama ya nguruwe kwenye bucha la “Mbokomu Centre” Manzese/Tandale.

Hili suala la ufugaji na uuzaji wa nyama ya nguruwe katikati ya makazi ya waislamu si suala geni hapa Tanzania bali ni sera ya Serikali za mfumo kristo tangu wakati wa mkoloni. Katika kuupiga vita Uislamu ufugaji wa nguruwe ulitumika kama miongoni mwa zana za kudhibiti Uislamu usienee kama tunavyojifunza kutokana na waraka uliotolewa Dar-es-Salaam na Gavana wa Kijeruman, Schnee, 13 Oktoba 1913 kwenda kwa wakuu wa wilaya zote za Tanganyika na wakuu wote wa vituo vya jeshi. Waraka huo uliagiza:

Mnaombwa mlete taarifa katika kipindi cha miezi mitatu tokea kupokea waraka huu. Taarifa hiyo ieleze mambo gani wanaweza kufanyiwa watumishi wa Serikali na walimu wa serikali ili kuzuia kuenea kwa mafunzo ya Uislamu. Je, mnadhani inawezekana kutunga sheria ya kupiga marufuku Uislamu? Bila shaka inawezekana kutunga sheria ambayo itawazuia walimu waislamu wasitahiriwe, kuwazuia kuhubiri misikitini, n.k. Watumishi wengine wa serikali itabidi wahusike na sheria hiyo. Wataalamu wameshauri kuwa wenyeji (natives) washauriwe na watiwe hima kufuga nguruwe kwani kwa kufanya hivyo ueneaji wa uislamu utasimamishwa. Wazo hili lifikiwiwe pia.<sup>72</sup>

Waislamu wa Dar es salaam hawakuridhika na uchokozi huu wa ufugaji holela wa nguruwe na ufungaji holela wa mabucha ya nyama ya nguruwe. Waislamu wa Ubungo Kisiwani walioathiriwa na ufungaji holela wa nguruwe hadi nguruwe kukutwa amefia msikitini mwao, tarehe 2 Juni, 1987 walipeleka malalamiko yao kwa Rais Mwinyi kwa niaba ya wakazi wote wa Ubungo Kisiwani kama ifuatavyo:

## **Yah: Ufugaji mbaya wa nguruwe katika eneo hili la Ubungo kisiwani**

*Mtukufu Rais,*

*Kichwa cha habari hapo juu cha husika. Tunayo heshima kubwa kutuma barua yetu ya malalamiko ya wanyama hao mbele yako ili utusaidie kutupatia ufumbuzi wa swala hili.*

*Mtukufu Rais, wanyama hao wanafugwa katika sehemu za kuishi. Wafugaji wa wanyama hawa kwa hakika wanatunyanyasa sana tusiowatumia wanyama hao, hususan sisi waislamu.*

*Wanatembea ovyo majumbani mwetu, wanalamba vyombo makaroni mwetu,*

*wanaingia Misikitini na wanafia Misikitini jambo ambalo kwa sisi waislamu ni baya sana tena sana.*

*Mtukufu Rais, tumeshapeleka malalamiko yetu haya kwa Katibu Kata tarehe 22/4/1985 hatimaye tumepeleka barua ya malalamiko kwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni tarehe 10/2/1986 hata hivyo hakuna hatua zozote zilizochukuliwa.*

*Mtukufu Rais, sisi wenye majina hapa chini tunatuma malalamiko haya ya kuomba waondolewe nguruwe hawa wapelekwe sehemu ambazo hazitaleta maudhi kwa niaba ya wakazi wote wa eneo hili.*

*Mtukufu Rais, tunakuomba utusaidie kututatulia matatizo yetu kikamilifu Waislamu tulio mashakani.*

*Pamoja na bura hii hapa tunaambatanisha nakala za barua za malalamiko yetu kama uthibitisho wa madai haya.*

Hata baada ya kuandika barua hii bado ufumbuzi wa ufugaji holela wa nguruwe haukupatikana. Tumenukuu barua hii hapa ili kuonesha ni kiasi gani waislamu wa nchi hii wamekuwa wakiwavamilia wananchi wenzao wakristo ili tu upatiane ueleweno wa kijamii.

Mashuleni, Vyuoni na Jeshini ufugaji wa nguruwe umefanywa mradi mkubwa. Mara nyingi vijana wakiislamu hulazimishwa kushiriki katika mradi huu. Hata wale wanao samehewa kushiriki kwenye mradi huu baada ya kuvutana sana na uongozi baadhi ya shule au vyo, bado hawajaweza kuepukana na nguruwe, kwani shule nyingi huamua kuwalisha wanafunzi nyama ya nguruwe, na kutumia vyombo vilevile vinavyotumiwa na wanafunzi wote na waislamu wakiwemo. Pia pato linalotokana na mradi wa nguruwe huchanganywa katika mfuko wa shule au Chuo ambao hutumika kwa wanafunzi wote.

Kuna kesi nyingi sana za wanafunzi wa Kiislamu kulazimishwa kushiriki katika mradi wa nguruwe na upikwaji wa nyama ya nguruwe shuleni au vyuoni kwa kutumia vyombo vile vile vya wanafunzi wote. Kesi ya shule ya sekondari ya Rungwe ni miongoni mwa kesi hizo kama mwalimu Muislamu wa shule hiyo alivyolalamika katika gazeti la "Daily News" la tarehe 27/7/1988, uk.5:

*Rungwe Secondary School is among the best schools in the United Republic due to its best performance in both academic and development projects. But what has spoilt the school's good image is the Headmaster's dictatorial decision to include pork on the students menu disregarding the fact that the school is composed of both Christians and Moslems. How can pork be cooked in the same utensils used to cook food eaten by non-Christians, namely Muslim students? Doesn't the Headmaster know this is against the teaching of the Holy Qur'an?*



**Tafsiri**

*Shule ya Sekondari Rungwe ni miongoni mwa shule bora katika Jamhuri ya Muungano kutokana na kufanya kwake vizuri katika masomo na katika miradi ya maendeleo. Lakini kinacho haribu jina zuri la shule ni maamuzi ya kibinafsi (ya kidikteta) ya Mwalimu Mkuu ya kuingiza nyama ya nguruwe katika chakula cha wanafunzi bila ya kujali kuwa shule ina mchanganyiko wa wanafunzi Wakristo na Waislamu. Nyama ya nguruwe itapikwaje kwa kutumia vyombo vile vile vinavyotumika kupikia chakula kinacholiwa na wanafunzi wote, Waislamu na Wakristo? Je, Mkuu wa Shule hafahamu kuwa hili ni kinyume na mafundisho ya Qur'an?*

Dhidi ya shutuma hizi, Mkuu wa Shule alitoa jibu lifuatalo:

*The decision to allow Christian students to eat pork was made by the teaching staff in a staff meeting held on 14/4/87.*

*The decision was communicated to the students through the school Baraza on the 21/4/87. The Muslim students were involved and they allowed some of the school utensils to be used.*

**Tafsiri:**

*Uamuzi wa kuwaruhusu wanafunzi wakristo kula nyama ya nguruwe ulitolewa na walimu katika mkutano wao uliofanyika tarehe 14/4/87. Uamuzi huu ulifikishwa kwa wanafunzi kwenye Baraza la Shule lililofanyika 21/4/87. Wanafunzi waislamu walihusishwa na waliruhusu baadhi ya vyombo vya shule vitumiwe.*

Jibu hili la Mkuu wa Shule laonyesha jinsi wanafunzi Waislamu wanavyokandamizwa mashuleni katika suala zima la kufuata dini yao vilivyo. Kuna maswali mengi ya kujiuliza juu ya ufugaji na ulaji nguruwe mashuleni na vyuoni ambapo kuna mchanganyiko wa wanafunzi Waislamu na wasiokuwa waislamu. Kwa nini usichaguliwe mradi usioleta ubaguzi na ukandamizaji wa kundi la Waislamu? Kuna ulazima gani wa kupika nyama ya nguruwe shuleni au chuoni ambako kuna mchanganyiko wa wanafunzi waislamu na wasiokuwa waislamu? Je, uchache wa wanafunzi waislamu humo shuleni na vyuoni ndio unawafanya wastahiki kukosa haki na uhuru wao wa kuabudu? Na kwa nini waislamu wawe wachache humo shuleni na vyuoni na ili hali kundi la waislamu ndilo kubwa katika nchi? Je, tunaweza kusema shuleni hapana ubuguzi wa Dini? Ni nani aliyelea ubaguzi huu: Wanafunzi waislamu wanaokataa kulishwa nguruwe na kushirikishwa kwenye mradi wa nguruwe katika kutetea imani yao, au viongozi wa shule, vyo na Wizara zinazohusika kwa ujumla, unaowalazimisha wanafunzi Waislamu kushiriki katika mradi wa nguruwe au kula nguruwe kinyume na imani yao? Je, "udugu wetu" na "umoja wetu" vinapatikana tu wakati waislamu wanapoidharau na kuibezwa Dini yao na

kuziunga mkono na kuziendeleza dini za wengine kwa njia moja au nyingine, lakini waislamu hao hao wanapotanabahi na kuamua kuifuata dini yao vilivyo, wanashutumiwa kufanya fujo na kuleta ubaguzi wa kidini na Serikali kuchukua hatua kali dhidi yao?

Kuhusu kulishwa nyama ya nguruwe pale “Mbokomu Centre” Manzese Tandale. Waislamu wa mtaa ule walipeleka malalamiko yao kwa uongozi wa serikali ya mtaa hadi kwa Mkuu wa Wilaya ambapo pote walipuuza. Baada ya malalamiko yao kupuuzwa na serikali, vijana wanaharakati wa kiislamu wa Mkoa wa Dar es salaam waliamua kuchukua sheria mkononi na kuvunja bucha la nyama ya nguruwe la “Mbokomu Centre” la pale Manzese Tandale na lingine la Magomeni karibu na kituo cha polisi.

Serikali iliyopuuza malalamiko ya waislamu haikuvumilia hatua ile waliyoichukua waislamu, bali kesho yake vyombo vyote vya habari vililaani waislamu kwa kitendo kile. Rais Mwinyi aliyekuwa ziarani Zanzibar, baada ya kupelekewa habari za kadhia ile na viongozi wake wa juu wa chama na serikali akiwemo Waziri Mkuu, Waziri wa Mambo ya Ndani na Katibu Mkuu wa C.C.M. alitoa kauli huko huko kuwa “Rungu la Dola liwaangukie kwa nguvu zote” wote waliohusika na kitendo hicho.

Kilichofuatia sio serikali kuwakamata wale vijana waliohusika na uvunjaji wa mabucha yale ambao walivunja mchana mweupe (saa 11 alasiri), askari polisi na askari kanzu wakiwa wanawashuhudia, bali kuwa kamata na kuwasweka ndani wanaharakati wote wa nchi nzima akiwemo wahadhiri waislamu waliokuwa wakitumia Biblia, viongozi wa Taasisi za Kiislamu, n.k.

Wanaharakati na viongozi hawa wa waislamu walipofikishwa mahakamani, pamoja na shitaka la kuvunja bucha la nguruwe la “Mbokomu centre” Manzese na lile la Magomeni, walisomewa mashitaka mengine ya kutengeneza mabomu kwa lengo la kulipulia mabaa na kiwanda cha pombe cha Tanzania Bruweries”, Ilala, Dar es salaam. Watuhumiwa walinyimwa dhamana na kubakishwa rumande takriban kwa kipindi cha miezi sita. Katika jambo la kushangaza ni kuwa mlalamikaji wa uvunjaji wa mabucha ya nguruwe alikuwa serikali badala ya wenye mabucha yale.

Watuhumiwa wakitengeneza mabomu waliachiwa huru kwakukosekana ushahidi lakini wale walioshutumiwa kuvunja mabucha ya nyama ya nguruwe pale manzese na magomeni Dar es salaam, ambao kihalisia hawakuhusika kabisa hata kwenye mchakato wa maandalizi walihukumikiwa kifungo cha mwaka mmoja. Baada ya kutumikia kifungo kwa miezi kadhaa waliachiwa huru kwa msamaha wa Rais.

## **Mauaji ya Waislamu Mwembechai, 1998**

Rais William Benjamin Mkapa, Mkatoliki, alipoingia madarakani wakristo wakatoliki walitumia serikali yake vizuri kuwadhibiti na kuwakandamiza waislamu. Viongozi wa kanisa katokiki waliichochea na kuishinikiza serikali ya Mkapa idhibiti mihadhara ya Waislamu inayotumia Biblia iliyokuwa kero yao katika kipindi chote cha Rais Mwinyi.

January, 29, 1998 waislamu wa Dar es salaam walifanya Baraza la Iddil-Fitr katika Msikiti wa Mwembechai na maudhui makubwa ya Baraza hilo yalikuwa kuitanabahisha serikali juu ya kukiuka kwake katiba ya nchi kwa kuingilia uhuru wa dini. Aliyekuwa makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Omar Juma alitangaza kuwa itakuwa ni marufuku waislamu kuswali Iddil-Fitr kinyume na siku itakayotangazwa na Muft wa BAKWATA, Sheikh Hemed bin Jumaa bin Hemed. Wanaharakati wa kiislamu walipinga amri hiyo ya serikali na wakaswali swala ya Iddil-Fitr kama kawaida kabla ya siku iliyotangazwa na Muft Hemed. Katika Baraza la Idd waislamu walionyesha hisia zao na msimamo wao kuwa wamechoka kukandamizwa na serikali ya mfumo kristo (katoliki).

Februari 8, 1998, wiki moja baada ya Baraza la Idd la mwembechai, Padre Camillius Lwambano wa Parokia ya Mburahati, Dar es salaam, alidai kuwa siku ya Idd alipita msikiti wa Mtambani, Kinondoni na Mwembechai, Magomeni na kusikia Yesu akikashifiwa katika mihadhara ya Waislamu. Madai yake haya aliyoyatoa kwa jazba yalirushwa hewani na Radio Tumaini inayomilikwa na kuendeshwa na Kanisa Katoliki. Madai yake yalikuwa ni ya uwongo uliodhahiri kwani siku ile ya Idd hapakufanyika mihadhara ya Biblia katika misikiti aliyoitaja bali lilifanyika Baraza la Idd tu katika Msikiti wa Mwembachai.

Padre Lwambano aliilaumu Serikali ya Mkapa kwa kutotekeleza kwake ahadi ya kuwachukulia hatua wahadhiri waislamu wanaotumia Biblia na aliichagiza serikali ichague kati ya mawili: Kupiga marufuku mihadhara ya waislamu inayotumia Biblia na kuwachukulia hatua kali wahadhiri au itangaze kuwa imeshindwa kuzuia kashfa dhidi ya dini ya kikristo katika nchi.

Chagizo hilo lilitolewa Jamapili, 8 Februari, 1998. Jumatatu, 9 Februari, 1998, Serikali ilichukua hatua mbili:

**Kwanza**, Wakristo wote nchini walitakwa radhi kwa jinsi walivyoathiriwa na kashfa za waislamu dhidi ya dini yao siku ya Iddil-Fitr na **Pili**, iliahidi kuchukua hatua kali dhidi ya wahadhiri wa kiislamu walioendesha mihadhara ile siku ya Idd. Kauli hii ya Serikali ilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam, Yusufu Makamba.

Siku iliyofuatia, Jumanne, 10 Februari, 1998, Mkuu wa Polisi wa Mkoa wa Dar es salaam, Bw. Alfred Gewe, alitoa tamko lingine lililosisitiza lile la Mkuu wa

Mkoa kuwa Serikali itachukuwa hatua kali sana dhidi ya wahadhiri waislamu wanaolingania dini kwa kutumia Biblia. Usiku uliofuatia walianza kukamatwa Maimamu wa Misikiti ya Mtambani, Kibo na Mwenge kwa kuviziwa majumbani mwao usiku usiku karibu na alfajiri. Tarehe 11, Februari 1998 kikosi cha askari Polisi wenye silaha waliizingira shule ya Kiislamu ya Ubungo, wakidai kuwa wanamtafuta Shaabani Magezi, aliyekuwa miongoni mwa wahadhiri wa ulinganisho wa dini kwa kutumia Biblia na Qur-an. Walijibiwa kuwa Magezi hakuwa mwajiriwa wala mwanafunzi wa Ubungo Islamic High School.

Mnamo Saa 9 mchana siku ya Al-hamis, 12 Februari, 1998 kundi la askari Polisi kumi na mbili wenye silaha walivamia msikiti wa mwembechai na kumteka nyara Bw. Shabani Magezi na kuondoka naye. Hapakuwa na muhadhara siku hiyo. Saa moja hivi baada ya kutekwa nyara Magezi, Msikiti wa Mwembechai ulivamiwa na kuzingira na askari Polisi na Jeshi la kutuliza Fujo (F.F.U). Waislamu waliokutwa msikitini waliamua kutulizana mle ili wasije singiziwa kuwafanyia fujo askari. Ikawa kosa kufanya vile na ilipofika saa 2 usiku askari wengi zaidi wenye silaha waliongezwa na kuzingira eneo lote la Mwembechai na kuwakamata wapata njia.

Ilipofika saa 7 usiku serikali iliagiza shirika la umeme (TANESCO) kukata umeme wa pale msikitini na eneo linalozunguka. Baada ya eneo lote kuwa giza, askari walitupa mabomu ya machozi ndani ya msikiti kisha waliingia ndani na kuwapiga, kuwajeruhi, kuwakamata na kuwasukumiza kwenye makarandinga watu wapatao mia tatu. Walioathirika sana katika uvamizi ule wa polisi walikuwa wazee na wanawake na ndio wengi waliokamatwa. Swali la msingi la kujjuliza likawa, “kwanini serikali iliwaamuru polisi kuvamia msikiti na kuwafanyia waislamu waliokuwa wakiswali fujo zile? Nini hasa lilikuwa kosa la waislamu wale? Ili kuitakasa serikali na ovu hili, asubuhi yake aliyekuwa Waziri wa mambo ya ndani, Bw. Ali Ameir na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Dar es Salaam, Bw. Alfred Gewe walitoa kauli kuwa ilibidi polisi wavamie msikiti ule kwa sababu ulikuwa unatuhumiwa kuficha wahalifu.

Siku ya Ijumaa, 13 Februari, 1998 eneo lote lilizungukwa na askari polisi. Pamoja na hivyo, waislamu wengi walimiminika pale kwa ajili ya swala ya Ijumaa na kupata taarifa juu ya yale yaliyojiri katika usiku uliopita. Baada ya swala ya Ijumaa waislamu walifahamishwa yaliyotokea na ikaamuliwa kuwa waislamu wote wakitoka pale waende kituo cha Polisi kuwatolea dhamana ndugu zao. Waislamu walipotoka nje ili waanze safari ya kwenda kituo cha polisi Magomeni, walivamiwa na askari polisi na wengine zaidi wakakamatwa na kutupiwa kwenye makarandinga. Kitendo hiki kiliwakasirisha sana waislamu na wasiokuwa waislamu ikabidi waanze kupambana na askari polisi kwa mawe. Kikosi cha kutuliza fujo (F.F.U) kiliongezwa na mapambano yakazidi kuwa makali. Hali hi ilifanywa makusudi ili ipatikane fursa ya kuwauwa waislamu. Mwanya huu ulipopatikana makamanda wa polisi waliwaamrisha askari kuwalenga shabaha

watu walio wakusidia kwa kauli ya “piga yule”, “piga shaba,” yule piga shaba”, ..... (rejea mkanda wa mauaji ya mwembechai na I.T.V). Waliuliwa waislamu wanne(4) pale pale na maiti zao kuburuzwa na kutupiwa ndani ya gari la polisi kama mzoga. Waislamu na wananchi kwa ujumla walizidi kukasirika na kuamua kuzuia magari ya serikali, mashirika ya uma na yale ya chama tawala(C.C.M) na kuyachoma moto.

Baada tu ya mauaji ya mwembechai, mkutano mkuu wa chama tawala, C.C.M., mwenyekiti wake akiwa mheshimiwa Benjamin Mkuu ambaye pia alikuwa Rais wa nchi, uliipongeza Serikali kwa hatua iliyochukua Mwembechai. Pia kiongozi Mkuu wa kanisa Katoliki, muadhama Plycarp Cardinal Pengo, aliunga mkono mauaji yale ya waislamu akidai kuwa askari wale walikuwa na haki ya kuwapiga risasi za moto kwa kuwa na wao walikuwa wakiwatupia mawe. Akajaribu kuonesha kwa kurejea kisa cha Nabii Daud kuwa jiwe nalo linaua kama Daud(a.s) alivyomuua mfalme Jalut kwa jiwe. Swali aliloulizwa Muadhama Pengo na An-nuur ya wiki ile ni kuwa, “katika tukio la Mwembechai nani alikuwa Daud na nani Jalut?

Tukio la Mwembechai liliwakasirisha sana waislamu. Waislamu waliomba serikali ifuate mkondo wa sheria kwa kuunda tume huru ya kuchunguza mauaji ya waislamu Mwembechai. Serikali ilikataa. Mwanasheria mmoja, kwa jina maarufu, Abu Aziz alimwandikia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kumwomba aishauri serikali juu ya kuundwa kwa tume huru ya uchunguzi juu ya mauaji ya mwembe chai. Ombi lake pia lilipuuza. Baadhi ya Wabunge waliliomba Bunge liunde Tume ya Uchunguzi. Ombi hilo lilikataliwa kwa hoja kuwa hakukuwa na pesa.

Waziri wa Mambo ya Ndani akatoa taarifa za uwongo Bungeni juu ya sababu zilizopelekea polisi kumpiga risasi mwanafunzi Chuki Athumani pale mwembe chai. Bunge liliambiwa kuwa mwanafunzi huyo alikuwa na karatasi za uchochezi. Lakini serikali haikuweza kufafanua iwapo Chuki Athumani alipigwa risasi kabla au baada ya kukutwa na karatasi za uchochezi. Na karatasi hizo hazijaoneshwa mpaka leo hii. Hatimaye Halmashauri Kuu ya Waislamu walimwandikia Mheshimiwa Rais kumwomba, pamoja na mambo mengine, serikali iunde tume huru ya uchunguzi. Katika majibu yake alisema:

*Kuhusu suala la Mwembechai mimi nilifikiri tulishaelewana haitasaidia sana kuunda Tume ya Uchunguzi, maana tunajua kilichotokea. Na tunajua kuwa zile fujo, ambazo hatimaye zilihitaji nguvu kubwa ya dola kuzizima, hazikuwa na uhusiano na mambo ya dini kabisa. Ndio maana miongoni mwa waliokamatwa walikuwapo watu ambao wala si Waislamu. Bado haja na hoja ya kuunda Tume sijaiona (Mkapa, 1999).*

Tukio jingine muhimu katika kipindi cha kati ya Februari na Aprili, 1998 hapa nchini lilihusu ile kesi maarufu ya mbwa aliyeitwa “Imigresheni”. Bwana Anatory

Kachele Chizu wa huko Sumbawanga hakupendezwa na utendaji wa kazi wa maafisa wa Uhamiaji wa huko Sumbawanga. Kwa hasira akampa mbwa wake jina la “Imigresheni” na akajenga ada ya kwenda naye kwenye ofisi hizo. Na huko akawa kila mara anamwita mbwa wake kwa sauti ya juu. Mfanyakazi mmoja wa Uhamiaji, Bwana Stanley Anyitike, alikerwa na kitendo hicho na akamfikisha Bwana Chizu na mbwa wake mahakamani. Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, Bwana Onesmo Zunda alimtia hatiani Bwana Chizu na akamhukumu kwenda jela miezi sita na mbwa wake kuuliwa. Papo hapo maafisa wa Uhamiaji wakamwua mbwa huyo kwa rungu. Kesi na hukumu hii vilizua mjadala mkubwa ndani na nje ya nchi yetu. Tarehe 28 Aprili, 1998 Jaji Mkuu (wa wakati huo), Mheshimiwa Francis Nyalali alisema kwamba hukumu hiyo ni kiroja, kinyume na sheria na ni kinyume na haki. Pasi na kuombwa, Idara ya Mahakama iliona umuhimu wa kuchunguza kuuliwa kwa mbwa. Lakini pamoja na kuombwa rasmi Idara hiyo hiyo haikuona umuhimu wa kuchunguza kuuliwa kwa Waislamu Mwembechai. Na serikali pia ilikataa kufanya uchunguzi wa Muislamu Mohamed Omari (50) aliyefia mikononi mwa polisi tarehe 18 Mei, 1998.

Mauaji ya waislamu ni miongoni mwa vielelezo vya kuonesha udhalilishwaji wa waislamu hapa nchini. Hali hii ya waislamu itaendelea mpaka lini? Kisasi cha Mwembechai ni haki ya waislamu wa nchi hii lakini si kuua watu wanne kama wale wa Mwembechai au kumpiga risasi kijana wa shule kama alivyofanywa Chuki Athumani bali ni waislamu kujitahidi kuujua Uislamu sahihi na kufanya jitihada za makusudi za kuutawalisha Uislamu katika jamii kwa mali na nafsi zao.

## **Kuanzishwa Kamati za Kuendeleza Uislamu, 2002**

Katika kujaribu kutatua matatizo yalioanishwa hapo juu, pamoja na kutekeleza amri ya Allah(s.w) ya kuunda kundi la Harakati, Qur’an (3:104), Mwaka 2002, waislamu wanaharakati kutoka kote nchini walikutana Kirinjiko, Same na kuasisi kundi la Harakati kwa jina la “Kamati ya Kuendeleza Uislamu Tanzania”, kwa ufupi KKUT itakayokuwa na uongozi kuanzia ngazi ya mtaa hadi Taifa. KKUT katika kila ngazi inawajumuisha waislamu wote wanaofanya jitihada za makusudi za kuhuisha na kusimamisha Uislamu katika jamii. Kamati za kuendeleza Uislamu hazina ubaguzi wa kitaasisi au wa aina yoyote. Muislamu yeyote aliyetayari kushiriki kwa mali yake na nafsi yake katika harakati za kuuendeleza Uislamu kwa lengo la kuudhihirisha na kuutawalisha katika jamii anakuwa ni mwanakamati. Ili kupata wanakamati wenye sifa stahiki zinafanyika semina za uamsho kuanzia ngazi ya Taifa hadi Mtaa na kumewekwa mikakati ya kuwa na darasa duara kila mtaa. Kazi kubwa ya kwanza na ya msingi ya kamati za kuendeleza Uislamu ni kutoa elimu sahihi ya Uislamu na kusimamia utekelezaji wake katika kuyaendea maisha ya kila siku ya kibinafsi na kijamii. Ili hili lifanikiwe kamati za kuendeleza Uislamu katika kila ngazi zimeazimia kufanya yafuatayo:

- (i) Kuanzisha na kuendesha vituo vya elimu kuanzia shule za awali hadi vyuo vya ualimu.
- (ii) Kuanzisha na kuendesha Chuo Kikuu cha Kiislamu kitakachotoa elimu ya fani zote za elimu ya mazingira na mwongozo.
- (iii) Kusimamia ufundishaji wa Elimu ya Dini ya Kiislamu katika shule zote za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kote nchini.
- (iv) Kuwahamasisha (na kuwaandaa walimu wote waislamu kufundisha somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu katika shule zao za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu.
- (v) Kufanya jitihada za makusudi za kuandaa nguvu kazi ya kuendesha harakakati za kiislamu kutokana na wanafunzi wa sekondari, vyuo vya ualimu na vyuo vikuu nchini na nje ya nchi.
- (vi) Kujiimarisha kiuchumi kwa kuanzisha na kuendesha mifuko na miradi ya kiuchumi.
- (vii) Kuweka mipango ya muda mfupi na mrefu katika kutekeleza majukuu sita yaliyoainisha hapo juu na kufanya tathmini kitaifa kila baada ya miezi sita.



## **Rejea za Sura ya Tano.**

1. Athan Husain, The Glorius Caliphate, uk 54
2. Ibid, uk. 61
3. Ibid, uk. 57
4. Ibid, uk. 58
5. Dr. Majid Ali Khan, The Pions Capliphs, uk 153
6. Athan Husain, The Glorious Caliphate, uk. 32
7. Dr. Majid Ali Khan, The Pious Caliphs, uk. 50
8. S.A. The Husein, The Glorous Caliphate, uk. 32
9. Dr. Majid Ali Khan, The Pions Caliphas. uk. 131
10. A.H. Siddiq, Historical Survey of Islamic State
11. Ibid
12. Athan Husain, The Glorious Caliphate, uk. 23
13. M.M. Qureish, Land Mark of Jihad, uk. 50
14. Ather Husein, the Grorous Caliphate, uk. 112.
15. Ather Husein, the Grorous Caliphate, uk. 119.
16. Ather Husein, the Grorous Caliphate, uk. 120.
17. Ather Husein, the Grorous Caliphate, uk. 112.
18. Dr. M.A.Khan, The Pions Caliphs, uk. 153
19. Dr. M.A.Khan, The Pions Caliphs, uk. 153
20. Dr. Majid Ali Khan, The Pions Caliphs, uk. 205.
21. Ather Husein, the Grorous Caliphate, uk. 148.
22. Ather Husein, the Grorous Caliphate, uk. 112.
23. Marym Jameelah, Islam in Theory and Practice.
24. Muslim News International, Karachi, February 1966, uk. 25
25. P.H.C. Clarke, A Short History of Tanganyika, uk. 14 – 15.
26. G.D. Kitter, The White Fathers, London 1957 uk. 23-33.
27. Roland Oliver, The Missionary Factor in East Afrca, London 1962, uk. 206.
28. Hansen H.B. Mission, Church and State in Colonial Setting Uganda 1890 – 1925, London, 1984 uk. 26.



- 29.H.M. Stenley, Through the Dark continent, London 1978 Vol.II Uk. 194.
- 30.Tazama: Barua ya H. Johnston ya 3/12/1900.
- 31.Roland Oliver na Gervase Mathews, History of East Africa Vol.I Oup, London 1963 uk. 242.
- 32.Abdu B. Kasozi, The spread of Islam in Uganda, Nairobi, OUP, 1986.
- 33.M. Singleto, Muslims, Missionaries and the Millennium in Up Country Tanzania.
- 34.Dr. John Sivalon, Kanisa Katoliki na Siasa Tanzania 1953 – 1985.
- 35.Gazeti la Tanganyika Standard, 2 May, 1961.
- 36.Gazeti la Tanganyika Standard, 15 April, 1961. Kwa hoja kama hiyo angalia vile vile John Hatch, Two African Statesmen, London 1976, uk. 128.
- 37.Press Release B/1629/62 10th December, 1962.
- 38.Tanganyika Standard, 12th March, 1963.
- 39.K. Mayanja Kiwanuka, Op Cit uk. 57 – 58.
- 40.Report ya East Africa Muslim welfare Society, January/February, 1961.
- 41.Angalia Kwikima Report, The Standard 12th December, 1968 na The Nationalist, 24th October, 1968.
- 42.Mwaka 1963, waliokuwa viongozi wa EAMWS ni: Tewa Said Tewa, Aziz Khaki, Bibi Titi Mohamed, Salehe Masasi, Abdallah Jambia, Khamis Kyeyamba na Bilali Rehani Waikela.
- 43.Tewa Said Tewa Probe.
- 44.Kiwanuka, Op. Cit uk. 75.
- 45.Ibid.
46. Benjamin Mkapa alikuja kuwa Rais wa Tanzania wa Awamu ya tatu.
47. Taarifa ya kamati ya utendaji EAMWS Mkoa wa Tanga 23 Oktoba, 1968, Ripoti ya Sheik A.J. Jambia.
- 48.Kiwanuka Op. cit. uk.2.
49. Ripoti ya Kwikima katika the Tanganyika Standard 12 December, 1968.
- 50.Ripoti ya Kwikima.
- 51.Tewa, 'A Pobe.
- 52.Ujenzi wa Chuo Kikuu ulikuwa umeanza na jiwe la msingi lililowekwa na Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

- 53.The Nationalis, Nukuu kutoka kwa Kiwanuka, uk. 81.
- 54.November, 1967, Tewa Said Tewa alifanya ziara Mwanza na Bukoba iliyokuwa na mafanikio makubwa sana. Alifanya majadiliano na Sheikh Amin Abdallah wa Mwanza na Sheikh Sued Kagasheki wa Bukoba.
- 55.Kiwanuka, uk. 2 – 3.
- 56.Ibid.
- 57.The Standard, 9 November 1968 kutoka kwa Kiwanuka uk. 81. Vile vile angalia, The Standard, 20 November 1968. Hassan bin Amir alifariki 1993.
- 58.Miaka mingi baadae Rashid Kawawa alisema kuwa anajuta kuunga mkono kukamatwa kwa Mufti wa Tanganyika na Zanzibar, Sheikh Hassan bin Amir, akaelekeza lawama kwa wale waliomshauri kufanya vile.
- 59.Ali Muhsin, Op. Cit. uk. 87.
- 60.Pamoja na mambo mengine taarifa ya Tume ya Kwikima ilipendekeza mabadiliko katika katiba ya EAMWS, kuondolewa kwa nafasi ya Patron,kuasisiwa kwa jumuiya isiochanganya Dini na siasa.
- 61.Ibid.
- 62.The Nationalist, 15 December, 1968.
- 63.Baraza (Nairobi), 12 December, 1968.
- 64.Tewa, 'A brobe.
- 65.Kiwanuka, uk. 85. Vile vile proceeding of the Iringa conference 12 – 15 December, 1968.
- 66.The Standard, 18 December, 1968.
- 67.The Standard, 20 December, 1968.
- 68.Ibid.
- 69.Tewa, Ibid. Vile vile angalia The Standard, 20 December, 1968.
- 70.Kiwanuka, uk. 86.
- 71.Pamoja na watu hawa watu wengine waliokuwa katika mpango ule ni:Omar Muhaji, Juma Jambia na Juma Swedi.
- 72.Gazeti la Serikali, taarifa ya Serikali Na. 40 ya 15 Mei, 1916.